RohoYaUnabii.Org

INJILISTI

KIMETAFSIRIWA KUTOKA DONDOO ZA KITABU CHA

EVANGELISM

RohoYaUnabii

RohoYaUnabii.Org

Pen of Inspiration

2026 Edition, New Jersey, Marekani

By Samaritan Laymen Ministries

1946

MAARIFAMTANDAONI.COM

SALAAM!

Pokea Habari njema kupitia kitabu hiki cha UINJILISTI ambacho kimeandikwa kwa Huduma ya Roho ya Unabii kwa kuongozwa na MUNGU ili Dunia ipate nuru ya injili, inayoongoza kwenda uzimani.

Sambaza Machapisho Kwenye Kila Ardhi, Naam Nchini Kote au Mtandaoni (4T 472)

‘Maelfu ya watu wataoongoka kwenye ile Kweli, katika saa ya kumi na moja, AMBAO wataupata na kuukubali Ukweli wa injili na Neno la Mungu na KUHUISHWA KWA harakati za Roho wa Mungu.—EGW’88 755 (1890). – {LDE 212.2}.’ Unabii huu unatimia, Maelfu ya watu duniani kote wanamwamini Mwenyezi Mungu na kubatizwa kwa siku moja, kwa wazi au kwa faragha. Tafsiri zetu ni kama Wikipedia, ukitaka kuongeza ladha bila kupoteza maana, wewe boresha tu, ila usipoteze kabisa ujumbe na maana iliyokusudiwa. Kila Shuhuda imeharirіwa mara tano, binafsi nimepitia mara tatu. Tumeweka Pointers **{EVsw 88.4}** na kadhalika ili ujihakikishie mwenyewe na kutafsiri kwa ubora zaidi unapotaka. Sw inawakilisha, Kiswahili ambacho kinazidi kupanuka na kuwa moja za lugha za Wakristo wengi duniani. Niliona Machapisho ya Nuru kwa Kanisa ambayo sasa tukiyaona tunashangaa, ila enzi hizo yalikuwa yenyewe kabisa kwa uzuri, japo yalichuja kurasa 4738 na kuwa 80 tu!

Enendeni Mtandaoni Kote Ministry

Asante kwa Wasomaji, Watafsiri, Wahariri, Washauri, Wahakiki, Waombezi, Wanaufundi na wote ambao wanasaidia hii kazi ya Machapisho duniani kote. Tuna idadi ya vitabu 130 sasa. Kama umeshiriki hii kazi na jina lako halikuweka, tafadhali tujulishe, Asante

1.Grace Momadi Masaka-New Jersey, Marekani

2.Nhandi Emmanuel Masunga-Kigali, Rwanda

3.Musa Budodi -Shinyanga-Tanzania

4. Sandra Barron-North Carolina, Marekani

5. Judi Mmari Mugane-Boston, Marekani

6. John Murathi Mugane-Nakuru, Kenya

7. Daudi Jabez Masaka-North Carolina, Marekani

8. Denis Paul Masaka-New Jersey, Marekani

9. Mbusi Mpagalushu-Kampala, Uganda

10. Cindy Tusch-Washington, Marekani

11.Daniel Nyangaresi Masaka-Kisii, Kenya

Sambaza Machapisho Kwenye Kila Ardhi, Naam Nchini Kote au Mtandaoni (4T 472)

FANYA MAMBO HAYA 7 KILA SIKU:

1. Mkiri Yesu na kutubu.
2. Dumu Kusali Daima.
3. Soma Neno La Mungu kila Siku.
4. Ishi mtindo wa maisha kulingana na Neno.
5. Waambie wengine habari Njema.
6. Hudhuria ushirika unaofuata Maandiko
7. Gusa maisha ya watu katika jamii.

Jifunze zaidi:

https://rohoyaunabii.org.

https://MaarifaMtandaoni.com

MWITO KWA MPENDWA MSOMAJI…

Hitaji letu kuu katika huduma hii ya Machapisho Uhamishoni ni ROHO MTAKATIFU, ushauri, na Maombi yako msomaji. Wako watu wanaoishi nje ya Afrika Mashariki wanaohitaji pia kusoma Maandishi ya kalamu iliyovuviwa, kwa Lugha ya asili. Toka mtambo wa kuchapa ubuniwe kule Ujerumani mwaka 1456 na Johannes Gutenberg, Neno la MUNGU limefikia mabilioni, ila bado kuna makundi karibu 7000 kati ya 14,000, ambayo bado kufikiwa, angalia Joshuaproject.org na habari za '1040 window'

'Sambaza Biblia kote,' ndiyo kauli mbiu ya muumini; sambaza Neno la MUNGU kote.

Jiunge nasi katika kuandika vitabu, kutafsiri, kuhakiki, na kuhariri. Ikiwa kuna kosa lolote la kiuandishi au kiutafsiri, tafadhali wasiliana nasi na endapo ukiamua kuchapa, usibadilishe chochote labda typos tu.

Sasa umefika wakati wa kuandika vitabu ambavyo vinaendana na muktadha wa mazingira na utamaduni wetu, kwani ulimwengu wa Kikristo sasa umehamia Afrika na Amerika ya Kusini. Kwa hapa Kwetu Afrika Mashariki, tumekuwa wazito kuandika kuhusiana na Mada mbalimbali ambazo zinaendana na mazingira yetu; mada za afya, lishe, mahusiano kama ndoa, kilimo na mazao yake, kulea na kukuza watoto, aina za biashara zinazoendelea, hali ya kisiasa na muumini, utendaji wa kufikia watu na kujenga ufalme wa Mungu, nyimbo zetu na noti zake; haya yote tunayasoma na kuyaiga kwenye vitabu na mitandao ya magharibi na ni mema tu, lakini kama ulimwengu wa Kikristo umehamia kwetu Afrika, basi tunabidishwa pia kuwa waandishi, Watunzi wa nyimbo, na watu wa kuhifadhi kumbukumbu zetu kwa miaka mingi, kwa sababu tunajua hali yetu katika kufikia wengine au kuboresha afya Ya jamii kuliko mtu mwingine.

Kwa nini nyimbo zetu nzuri zenye ujumbe mzito zisichaguliwe kwa umakini, nyimbo zilizoimbwa miaka kama 50 hivi na kuwekwa kwenye vitabu vya tenzi na kisha watu waimbe? Tenzi tunazoimba za magharibi ni nzuri, ila hata wao wanaendelea kuziongeza vitabuni, nasi hapa tuna nyimbo nzuri, ambazo zinaendana na utamaduni wetu na mtindo wetu wa kuchukua mafungu ya Biblia takatifu, na kuelezea kisa fulani. Kwa nini basi tusijiongeze nasi, ili tuongeze kwenye maktaba yetu vitu vizuri, ikiwemo nyimbo za watoto? Tuna wataalamu wengi wa nyimbo. Pia umefika wakati wa 'Reverse Mission'-misheni iliyogeuka na kuwa kinyume cha kawaida. Watu wa Amerika ya Kusini sasa ni wainjilisti kila mahali duniani, ikiwemo magharibi kama vile Ulaya, Marekani na hata Asia, Australia, Mashariki ya kati na Afrika! Sisi Afrika tuna Waumini wengi kuliko Amerika ya kusini, na tunajua lugha nyingi

kubwa kama Kifaransa, Kireno, Kihispania na Kingereza, ila bado tunaona kwamba tupate waandishi kutoka nchi zenye Wakristo wachache kuliko sisi ambao hawaandiki kwa muktadha wa mazingira yetu. Watoto wetu na sisi mara zingine tunaona pengine tuwe na vile vitu walivyo navyo nchi zingine au tuwe na mwenendo kama ule.

Mfano mdogo sana ni ule waandishi wengi wa nje huandika vitu vingine visivyoendana na muktadha wetu, mfano vyakula kama Pizza, Tambi, Kimchi, Taco, Panzit, Empanada, Manicotti, Tortellini, Sushi, au Falafel. Je, viwanda vyetu hutengeneza vitu hivi? Kila chakula duniani kinacholimwa hufanana tu, ila maandalizi hupishana. Mwafrika atatumia ngano kupika ugali, Mhindi chapati, Mchina Noodle, Mzungu mkate au makaroni, nk.

Ni kweli Kiswahili ilikuwa lugha ya kuzungumzwa na siyo ya Maandishi, ila wakati umefika maandishi kuongezwa kwenye mambo mazuri! tunaelewa kwamba sio utamaduni wetu kuandika, ila sio utamaduni wetu kufanya mambo mengi ambayo sasa tunayafanya!

Sio kila kitabu tunachoandika ni lazima kiuzwe, vingine ni vya kusaidia jamii; wewe hautaweza kuuza kila kitu katika dunia hii, kama unataka kufanya uinjilisti au kubariki watu. Kitabu cha Jando na Unyago kwa muktadha wa Maandiko kwa Waamini ni vizuri tupatie watu wa kutusaidia kuandika, kwani jamii inaishi sehemu tofauti na asili ya kabila la mtu, na hii inafanya kusiwe na Mafundisho au kujifunza kwa mambo fulani muhimu toka kwa Kabila la mtu kama ilivyokuwa, na wakati huo huo pengine serikali haiwezi kukidhi hitaji hili kwa urahisi.

Watu husema utamaduni wa mtu mweusi ni kusaidia jamaa na ndugu zake wa damu tu na wala sio umma. Yawezekana ni kweli ila tuna la kujifunza kutoka kwa kila mwanadamu. Wenzetu wa Nigeria wameanza kuweka vitabu vyao mtandaoni ili watu wasome na kufaidika katika nyanja mbalimbali kama vile uchumba, maombi ya kuondoa laana kwenye familia nk. Joel Nanauka ni mfano mzuri katika Ulimwengu wa Kiswahili, kwenye kuandika na kugawia watu ujuzi wake. Tumevisoma vitabu vyake vizuri ambavyo ametubariki kwenye ujasiliamali, nk. Ukiwa na chochote, hata ikiwa ni kama senti mbili za Mjane, ujuzi, uwezeshaji wa aina fulani, tafadhali usisite kuutoa na pia kama una ujuzi wa kuandika vitabu au kufundisha wengine kuandika vitabu, fundisha wengine, maana ulimwengu wa Kiswahili una umasikini wa Maandishi yaliyoandikwa kwa muktadha wa utamaduni, nyenzo, na maisha yetu ya kila siku.

UTANGULIZI

Wapendwa vitabu hivi ni vyetu sote! Maana kila mtu anahitaji Mashauri. Shuhuda ni vitabu vya mashauri na maonyo. Kwenye wingi wa Ushauri hapaanguki jambo, na kuna usalama. Masihi Yu karibu kuja kuchukua bibi harusi asiye na waa wala kunyanzi. Maneno haya na yatuchome sana, na kutuvutia tusiwe waongofu tu bali wanafunzi na watu wanaoishi kwa uamsho na matengenezo kila siku, tukiendelea kuwezeshwa na ROHO MTAKATIFU kubadilisha mitindo yetu ya maisha ili tumpende na kumpendeza Mwenyezi MUNGU, na kuwapenda watu. Hivi ndivyo vitu pekee ambavyo tutaenda navyo mbinguni.

Shuhuda zimejaa mashauri, Makaripio na maonyo ya maisha ya kila siku kwa undani zaidi. Tumeambiwa kwenye maagizo kwamba shuhuda zina kila namna ya kukamilisha tabia zetu. Tulisikia kuhusu kuwepo kwa Shuhuda kwa Kanisa ila hatukujua sana kwamba zinahusiana na nini! Ila baada ya kuanza kusoma kila siku katika mpango wa kusoma Shuhuda Revivalplan.com kwa lugha ya Kiingereza tuliona kuna haja kubwa ya kuzitafsiri katika lugha ya Kiswahili maana waamini wengu wanaishi chini ya Sahara, ambao kuna wengi wanaozungumza Kiswahili. Kwa sasa, takwimu zinaonesha kuwa Afrika ina asilimia 50% ya waamini wanaotarajia marejeo ya YESU (Waadventista). Miaka kama 10 iliyopita, ni asilimia 3% tu ya Maandishi ya Roho ya Unabii ilikuwa imetafsiriwa Kiswahili.

Wana Marejeo wanaozungumza Kiswahili duniani sasa ni 11%. Kutokana na Google wale wanaozungumza Kingereza ‘fluently’ katika nchi za Kiswahilii ni asilimia ndogo sana kuliko tunavyofikiria! Tumepewa ulimwengu wa Kiswahili tuufikie. Hivyo Kutafsiri mambo haya ni jambo la dharura. Katika kutafsiri, Mambo manne ndiyo yalikuwa kwenye mawazo yetu kuliko mengine

1. Yesu Anarudi Upesi, inabidi shuhuda hizi ziwafikie watu mapema na kutayarisha tabia zetu na siku moja tusikie "Vyema mtumishi mwema, ulikuwa mwaminifu...."

2. Kubeba ujumbe kama ulivyo ili watu wapate kilichonuiwa, bila kupotosha Neno la MUNGU

3. Lugha rahisi itakayoweza kusomeka Kenya, Congo, Burundi, Rwanda, Uganda na Tanzania

4. Sarufi ya lugha ya Kiswahili sanifu iwe imezingatiwa.

Maombi yetu makuu yawe matatu. Nayo ni ROHO MTAKATIFU, kujisalimisha kwa MUNGU na kuwa ndani Yake Naye ndani yetu. Haya manne yatakuja na baraka zote tunazozihitaji tunaposoma Hizi shuhuda. Haya ni mausia ambayo yanatubidisha sote wenye mwili kuzisoma hizi shuhuda. Mambo mengine kwa kuelewa zaidi unaweza kupakua 'Google App' ya Roho ya Unabii kwa Kingereza.

Google imesaidia mambo kadhaa mfano Kujua zama hizo kulikuwa na mambo gani, mfano mitindo na mavazi ya sketi za hoops miaka ya 1800BK zilizozungumziwa; zitakupa maoni waliyokuwa nayo wakati ule utakapoingia katika tovuti. Japo hekima haiongezeki kwa urahisi, maarifa yameongezeka, hivyo angalia mambo haya kwa kichujio cha Biblia zaidi ya teknolojia. Usiogope kurejelea kamusi, ndio kujifunza. Muumini daima ni mwanafunzi na anasaidiwa zaidi kukumbuka mambo mengi anapotumia machapisho zaidi ya njia zingine. Mengine ya Kingereza imebidi tuweke maana tunayatumia na hivyo utapata utambuzi wa jambo haraka, mfano mara nyingi hatusemi Jimbo, ila Konferensi/conference, majina ya magonjwa au mitindo nk.

UTANGULIZI-JE, UINJILISTI NI NNI?

Uinjilisti ni kushiriki habari njema na wanadamu. Kuzaliwa Kwake Masihi, kuishi Kwake hapa duniani, kifo Chake na Kafara Yake ili tupate ukombozi Kufufuka Kwake, kupaa Kwake mbinguni, Maombezi anayoyafanya kwa ajili yetu sasa, na kurudi Kwake mara ya pili duniani, kufufua wafu na kutupeleka mbinguni tukae Naye milele. Dunia yetu iliumbwa kwa uzuri sana, na hata Bwana Mwenyewe alisema ni nzuri sana. Mungu alimweka mwanadamu katika bustani nzuri iitwayo raha au starehe, yaani Edeni (Pleasure). Katika hii bustani hapakuwa na machozi, kifo, jasho, uchungu au chochote kibaya. Adamu na Hawa walikuwa na afya tele. Ila mwanadamu alianguka dhambini, akitaka kuwa kama Mungu wakati yeye alikuwa ndiye kiumbe pekee aliyeumbwa kwa sura ya Mungu. Shetani alikuwa ameasi serikali ya Mungu huko mbinguni kama inavyosema Ufunuo 12 na Isaya 14, Ayubu 1 na Ezekieli 28. Huyu ndiye adui aliyewadanganya babu na bibi yetu Adamu na Hawa, kufanya dhambi na kumkosea. Mwenyezi Mungu alikuwa na suluhisho la kumrudisha mwanadamu katika Edeni ya milele tena, ila alipaswa atoke kwenye bustani, ili asije akala tunda la uzima wa milele na kisha akaishi milele, ila kwa huzuni tele.

Ndipo akafanya mpango wa kumtuma Mwanawe, tunayemjua kama Masihi ili kutukomboa, kwa vile mshahara wa dhambi ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele, na sote wanadamu tumefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. Mungu Ndiye Mwinjilisti na Mmishenari wa kwanza. Alituepusha kifo cha milele. Mungu aliwatuma manabii katika mpango wa wokovu ili kusaidia watu, na mwishowe akamtuma Mwanawe kuja hapa duniani na kufa kwaajili yetu ili tuweze kuokolewa. Mpango wa wokovu umefanikiwa kabisa, kupitia kifo cha Masihi.
Nasi sasa tunapaswa kuwaambia watu wengine habari njema. Mungu alimtoa Mwanawe ili kila mtu amwaminiaye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Na huo ndiyo muhtasari wa Biblia, yaani Uumbaji wa dunia, Kuanguka dhambini, na Wokovu. Sisi ambao tumejua mpango huu tunapaswa kuwaambia wengine, ili siku ya hukumu, wakutwe wako tayari kuurithi ufalme wa mbinguni, na kukaa na Mwenyezi Mungu milele. Tunapaswa kutayarisha watu kumwona Masihi siku ya hukumu.
Bwana atusaidie tufanane Naye, ili tuweze kuwa na upendo kama Wake. Kuwaambia watu kisa cha wokovu, kisa cha injili, au kisa cha upendo wa Mungu na Historia, yetu ndiyo Uinjilisti! Huu unaweza kufanyika kwa njia mbalimbali kama vile, kuzungumza na mtu mmoja mmoja ajaye karibu nasi, au kuwatembelea nyumba kwa nyumba, kutoa machapisho ya Injili, uinjilisti wa Kidijitali, kufanya mkutano wa hadhara au Efoti, kuhudumu kwa matendo ya huruma kwa jamii, jamii, kupanda makanisa, urafiki, apolojia, mtindo wa maisha yanayomtukuza Mungu, mihadhara,

Kila mwanafunzi wa kweli huzaliwa katika ufalme wa Mungu kama mmishenari. Yeye anywaye maji yaliyo hai anakuwa chemchemi ya uzima. Mpokeaji anakuwa mtoaji. Neema ya Kristo katika nafsi ni kama chemchemi jangwani, ikibubujika ili kuburudisha wote, na kuwafan ya wale walio tayari kuangamia wawe na hamu ya kunywa maji ya uzima. Tumaini la Vizazi vyote Uk 195. Muhtasari wa Neno la Mwenyezi Mungu ni Maneno matatu tu-Uumbaji-Mwanzo 1 na 2, Maanguko-Mwanzo 3, Kisha Ukombozi-Mwanzo 4 Mpaka Ufunuo 22. Mungu ameshugulika na ukombozi wa Mwanadamu kwa takribani ya miaka 6000 sasa!

Tunapaswa kujitahidi kuwa na moyo mkuu na upendo wa kuona kila mtu akiokolewa kutoka kwenye dunia hii yenye shida na huzuni. Bwana aweze kutusaidia kuishi maisha ya mmishenari wa tiba. Tuombeane katika huduma hii. Mambo saba muhimu ya kujitayarisha ili tuwe tayari Masihi akija ni:

1. Mwamini Mungu na ungama dhambi zote, usifiche dhambi!

2. 2. Soma Neno la Mungu kila siku kwa mpango, na kudai ahadi 8100+

3. Omba kila siku, na kupata hekima ya Bwana ya mambo ya kuombea.

4. Waambie watu kuhusu Injili, na kwamba wawe tayari.

5. Shiriki huduma za jamii -saidia wahitaji, yatima, wajane, wagonjwa nk.

6. Hudhuria Ushirika unaofuata Maandiko Matakatifu zaidi ya mara moja kwa wiki! Vikundi vya kusoma Neno na maombi.

7. Ishi Maandiko, usisome tu, ila omba Mungu akusaidie uwe barua Yake!

Roho Mtakatifu na bibi arusi wanasema, "Njoo!" Kila asikiaye hili aseme pia, "Njoo!" Wote wenye kiu waje wanywe maji ya uzima bure ikiwa wanataka. Yesu Ndiye anayeshuhudia kwamba haya yote ni Kweli. Sasa anasema, "Ndiyo, naja upesi."

Amina! Njoo, Bwana Yesu!

Neema ya Bwana Yesu iwe pamoja na watu wote.

Maranatha

Grace Momadi-Masaka

ENENDENI MTANDAONI KOTE!

Uinjilisti, moyo halisi wa Ukristo, ndio mada muhimu kwa wale walioitwa kutangaza onyo la mwisho la Mungu kwa ulimwengu uliohukumiwa. Tuko katika saa za mwisho za wakati, na ujumbe wa Majilio, uliotangazwa ili kuwaandaa watu walioandaliwa kwa ajili ya kurudi kwa Bwana wetu, lazima tuinuke hadi kilio kikuu hadi sehemu za mwisho za dunia.

Tangu siku za mwanzo za kazi ya Waadventista Wasabato, mafundisho ya Roho ya unabii yanayoweka msisitizo maalum juu ya kanuni na mazoezi ya uvuvio wa Roho yametolewa ili kuongoza katika kazi inayoendelea kupanuka. Baadhi ya awamu za uinjilisti zimefafanuliwa katika karibu vitabu vyote vya Roho ya Unabii. Kwa miaka mingi, katika Review and Herald, Signs of the Times, na majarida mengine, makala kutoka kwa mjumbe wa Bwana yametoa msukumo kwa huduma inayokua ya uinjilisti. Wainjilisti binafsi pia, mara kwa mara, walipendelewa kupokea mafundisho na onyo kuhusu mbinu zinazopaswa kuainisha kazi yao. Mara kwa mara vikundi vya wainjilisti na wasimamizi wa madhehebu vilihutubiwa na Bi. White, na hotuba hizi mara nyingi zilijumuisha ushauri mwingi wa manufaa.

Lakini makala hizi za majarida, ushuhuda maalum, mashauri ya kibinafsi, na hotuba hazipatikani kwa ujumla leo. Ni kwa ajili ya kufanya mkusanyiko huu kamili wa mafundisho ya wakati unaofaa upatikane kwa nguvu yetu ya sasa ya uinjilisti ya Watu wanaomngojea Yesu Kurudi, iliyopanuliwa sana kwamba sasa kuna mkusanyiko huu kamili, uliopangwa kwa mada. Kazi hii imejitolea kwa namna ya kipekee kwa mada muhimu ya uinjilisti.

Juzuu hili haitoi tu kanuni zinazoongoza na zilizopangwa vizuri ambazo zinapaswa kuunda kazi ya mwinjilisti na mwalimu wa Biblia lakini pia linatoa ushauri mwingi na wa kina kuhusu matumizi ya kanuni hizo. Kama mkusanyiko wa mafundisho ya thamani ambayo Bwana ametoa kwa miaka yote, ni kitabu cha mwongozo halisi cha uinjilisti kwa harakati ya watu wanaomngojea Kristo, arudi hivi karibuni.

Katika kukusanya na kupanga kwa mpangilio wa kimantiki kauli nyingi kutoka vyanzo mbalimbali, iligundulika kuwa mistari fulani ya jumla ya mafundisho ilijumuishwa mara kwa mara. Katika juhudi za kumpa msomaji yote yaliyochangia mada hiyo, bila kuwasilisha marudio yasiyofaa, zilichaguliwa aya fulani au makundi ya za kipekee. Katika baadhi ya matukio sentensi zinazorudiwa ziliondolewa hata kutoka kwenye dondoo fupi zilizotumika, na katika kila kesi kufutwa kwake kunaonyeshwa. Hata hivyo, uangalifu mkubwa umefanywa katika kuwasilisha kauli zenye urefu wa kutosha ili kutoa mpangilio sahihi wa shauri.

Jitihada imefanywa ili kufanya kila sehemu iwe kamili kwa mada inayowasilishwa. Kwa kufanya hivyo kuna kiwango fulani cha kurudia mawazo kisichoepukika ambacho kinasisitiza maagizo. Kama msaada katika kufanya marejeleo yawe tayari kwa kauli muhimu katika kitabu hiki. Vichwa vya habari vya pembeni vinavyoonekana kwa herufi nzito vimetolewa na wakusanyaji. Sifa ya chanzo inaonekana mwishoni mwa kila dondoo, na kama msaada zaidi kwa msomaji, kuna tarehe iliyoandikwa, ikiwa ni nukuu za muswada, au tarehe ya kuchapishwa kwa mara ya kwanza ikiwa ni marejeleo mengine.

Ujuzi wa wakati wa usemi wakati mwingine hutumika kama mwongozo muhimu wa matumizi ya shauri bainishi, kwani kazi yetu lazima ifanyike chini ya hali zinazobadilika. Na ingawa katika baadhi ya matukio inaweza isiwezekane kutumia mbinu za kina zilizopendekezwa katika miaka ya awali, lakini kanuni za msingi zilizotajwa au kuonyeshwa katika mashauri haya ya awali leo zitakuwa mwongozo wa mbinu salama na zenye matunda. Kanuni haibadiliki, ingawa matumizi yake yanaweza kuhitaji marekebisho na uratibu ili kukidhi hali za sasa. Tunatoa mfano halisi wa jambo hili.

Msomaji atakuta mkutano wa kambi ukitajwa mara kwa mara, na kutoa ushauri kuhusu mwenendo wake. Katika miaka ya sabini mikutano ya kambi ya Waadventista Wasabato ilivutia watu na mahudhurio yalikuwa makubwa sana hata kwa watu wasio Waadventista mwishoni mwa wiki,-nusu kwa nusu, kwa kuanza mpaka, watu kumi na watano wasio washiriki, kwa mshiriki mmoja wa kanisa. Katika miaka ya tisini mikutano ya kambi ya uinjilisti iliyofanikiwa sana iliyofanyika katika vitongoji vya miji mikubwa

ilidumu kutoka wiki mbili hadi mwezi. Mikutano kama hiyo ilikuwa na uwezo mkubwa wa kuongoa roho. Kauli nyingi zinazopongeza mikutano kama hiyo na kutoa maelekezo kuhusu mwenendo wao uliofanikiwa ziliandikwa katika miaka hiyo.

Lakini nyakati zimebadilika; mkutano wa kambi sasa umekuwa mara nyingi, mkusanyiko mara nyingi ni wa kundi kubwa la kanisa linalokua. Umati wa wasio Waadventista waliovutiwa katika miaka ya awali na mkutano wa kambi sasa unafikiwa kwa ufanisi zaidi kupitia mkutano wa hema au ukumbi-efoti. Hata hivyo, kanuni zinazoongoza kwa njia zilizofanikiwa katika mikutano ya kambi ya uinjilisti hutumika kwa usalama na vyema katika kuongoza kwa njia zenye matunda katika uinjilisti wa leo.

Maagizo katika kitabu hiki yamekita kabisa kwa kazi ya uinjilisti wa mchungaji na mwalimu wa Biblia. Ushauri mwingi kuhusu uinjilisti wa walei, uliowekwa kikamilifu katika maeneo mengine upo katika vitabu vingine vingi vya Roho ya Unabii. Na kisha mwongozo kuhusu uinjilisti wa vitabu ambao ni muhimu sana katika kazi yetu, hautarejelewa sana hapa kwa sababu ya upungufu wa nafasi. Vivyo hivyo, uinjilisti wa tiba (Medical Missionary Work), unaoshughulikiwa kikamilifu na vizuri katika Huduma ya Uponyaji, Huduma ya Tiba, na Ushauri wa Afya, hauzungumziwi hapa isipokuwa kama unahusiana na uwasilishaji wa hadharani wa ujumbe. Mengi zaidi yanaweza kujumuishwa kwenye sifa za mwinjilisti, lakini nukuu kuhusu mada hizi hapa zimepunguzwa kwa mambo ambayo yana uhusiano wa moja kwa moja na kazi yake maalum, iliyonuiwa hapa.
Juzuu hii sasa imetumwa katika uwanja huu kwa imani ili kwamba kuonekana kwake kutaashiria maendeleo dhahiri katika njia za uinjilisti kwa wote wanaopenda kushiriki habari njema na kuharakisha kurudi kwa Mwokozi. Tunashukuru kwa ushauri wa kalamu iliyovuviwa, wenye kujenga, wa kisasa, na maonyo yake ya wakati unaofaa, maoni yake kuhusu ushindi wa ujumbe, tunaamini, yatakuwa "mpango," unaoongoza uinjilisti utakaofikia kilele chake kitukufu chini ya kilio kikuu cha malaika wa tatu.

Sisi tunaamini Yesu anarudi hivi karibuni

Wadhamini wa

Kalamu Iliyovuviwa

SEHEMU YA 1—CHANGAMOTO ZA UINJILISTI

Kutangaza Ujumbe

Agizo la Kristo la Kufundisha — Maneno ya mwisho ya Kristo kwa wanafunzi Wake yalikuwa:

Tazama Mimi Nipo pamoja nanyi daima

"Mathayo 28:19-20

Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari." Enendeni hadi mipaka ya mbali ya dunia inayokaliwa na watu, nanyi fahamuni kwamba popote mnapoenda, uwepo Wangu utakuwa pamoja nanyi daima....**[EVsw 15.1]**

Agizo hili limetolewa pia kwetu. Tumeagizwa kuenenda, kama wajumbe wa **Kristo**, kufundisha, kuelekeza, na kushawishi wanaume na wanawake, kuwahimiza wazingatie **Neno** la uzima. Nasi pia tumepewa hakikisho la uwepo wa kudumu wa **Kristo**. Licha ya changamoto zozote tutakazokutana nazo, au majaribu yoyote tutakayopitia, ahadi ya neema ipo siku zote kwetu: "***na tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari***. —**Manuscript 24, 1903.[EVsw 15.2]**

Ujumbe Ni Nguvu Iliyo hai— Katika agizo Alilowapa wanafunzi Wake, Kristo hakubainisha tu kazi yao bali pia Aliwapa ujumbe wao. "Muwa***fundishe kuyashika yote niliyowaamuru ninyi;***" Alisema. Wanafunzi walipaswa kufundisha yale ambayo Kristo Mwenyewe alifundisha. Yote Aliyoyasema, si tu kwa kinywa Chake, bali pia kupitia manabii wote na walimu wa Agano la Kale, yamejumuishwa hapa. Mafundisho ya mwanadamu yameondolewa kabisa. Hakuna nafasi kwa ajili ya mapokeo, nadharia na mawazo ya wanadamu, wala maagizo ya kanisa (kanuni za utawala wa kanisa). Hakuna sheria zozote zilizowekwa na mamlaka za kiibada zilizoingizwa katika agizo hili. Hakuna hata moja kati ya hivi ambavyo watumishi wa **Kristo** wameamriwa kufundisha. "Torati na manabii," pamoja na kumbukumbu za maneno na matendo Yake mwenyewe, ndivyo hazina waliyopewa wanafunzi ili waitoe kwa dunia.... **[EVsw 15.3]**

Injili inapaswa kuwasilishwa, si kama nadharia isiyo na uhai, bali kama nguvu iliyo hai, yenye uwezo wa kubadili maisha. **Mungu** anatamani wale wanaopokea neema Yake wawe mashahidi wa nguvu Yake. **—The Desire of Ages, 826 (1898).[EVsw 16.1]**

Kanisa Lililokabidhiwa Ujumbe

Sasa tunaishi katika matukio ya mwisho ya historia ya ulimwengu huu. Hebu watu waogope na watetemeke kwa kuwa watatoa hesabu kwa kuijua Kweli. Miisho ya dunia imefika. Kutilia maanani ipasavyo kwa mambo haya kutawaongoza wote kuweka wakfu vyote walivyonavyo kwa **Mungu** wao.... **[EVsw 16.2]**

Wajibu mzito unaohusu kuuonya ulimwengu juu ya adhabu inayoujia, uko juu yetu. Kutoka kila upande, sehemu zilizo mbali na zilizopo karibu, miito inatujia ikituhitaji tutoe msaada. Kanisa, lililowekwa wakfu kwa ajili ya kazi hiyo, linapaswa kupeleka ujumbe kwa ulimwengu: likiuambia "Njooni kwenye karamu ya Injili; Chakula kimeandaliwa, njooni.... Taji, taji zisizoweza kuharibika, zinangoja kuvaliwa. Ufalme wa mbinguni unangoja kuurithi. Ulimwengu, unaoangamia katika dhambi, unapaswa kuangazwa. Lulu iliyopotea inapaswa itafutwe na kupatikana. Kondoo aliyepotea anapaswa arudishwe mahali salama kwenye zizi. Ni nani atakayejiunga ili kumtafuta? Ni nani atakayeibeba nuru kwa wale wanaotanga-tanga katika giza la upotovu? **—The Review and Herald, July 23, 1895. [EVsw 16.3]**

Mgogoro Uliopo -

Inatupasa sasa kuhisi wajibu wa kufanya kazi kwa bidii kubwa kuwagawia wengine **Kweli** ambazo **Mungu** ametoa kwaajili ya wakati huu. Hatuwezi kuwa dhati na bidii inayotosha au kupitiliza.....**[EVsw 16.4]**

Sasa ni wakati wa onyo la mwisho kutolewa. Kuna nguvu maalum katika uwasilishaji wa **Ukweli** kwa wakati huu; lakini hali itaendelea hivi mpaka lini? Muda kitambo tu. Ikiwa kumekuwa na dhahama kuu basi, ni sasa. **[EVsw 16.5]**

Wote sasa wanaamua hatima yao ya milele. Wanaume wanahitaji kuamshwa ili kutambua uzito wa wakati huo, ukaribu wa siku ambayo rehema ya kibinadamu itakomeshwa. Juhudi zilizoamuliwa zapaswa kufanywa ili kuleta ujumbe wa wakati huu kwa uwazi mbele ya watu. Malaika wa tatu atatoka kwa nguvu nyingi. **—Testimonies For The Church 6:16 (1900).** [EVsw 17.1]

Uinjilisti Kazi Yetu Halisi—

Kazi ya uinjilisti, kufungua Maandiko kwa wengine, kuwaonya wanaume na wanawake juu ya kile kinachokuja juu ya ulimwengu, inapaswa kuchukua muda zaidi maishani mwetu, haswa kwa watumishi wa **Mungu**. —**The Review and Herald, August 2, 1906.**[EVsw 17.2]

Kuuharakisha Ujumbe -

Kama watu tunahitaji sana kunyenyekeza mioyo yetu mbele za **Mungu**, tukiomba msamaha wake kwa ajili yetu kwa kupuuza kulitimiza agizo la Injili. Tumeweka vituo vikubwa katika maeneo machache, na kuacha bila kazi kufanyika katika miji mingi muhimu. Hebu sasa na tuichukue kazi tuliyoitiwa na kuutangaza ujumbe ambao utawaamsha wanaume na wanawake kuhisi hatari yao. Ikiwa kila Mwaadventista Msabato angefanya kazi iliyowekwa juu yake, idadi ya waumini ingekuwa kubwa zaidi kuliko ilivyo sasa. **—Testimonies For The Church 9:25 (1909).**[EVsw 17.3]

Wito wa Kazi ya Bidii -

Laiti kama wachungaji/wahudumu wetu wangetambua jinsi wakazi wa ulimwengu watakavyofikishwa upesi mbele ya kiti cha hukumu cha **Mungu**, kutoa hesabu kwa matendo yaliyofanywa katika mwili, ndipo wangejua ni kwa jinsi gani wangeliweza kufanya kazi pamoja na **Mungu** kwa dhati nabidii ili kuwasilisha Ukweli! Wangejua ni kwa jinsi gani wangejitahidi kwa bidii kuwaongoza wanadamu kuukubali Ukweli. Ni kwa jinsi gani wangejitahidi kuendeleza kazi ya **Mungu** duniani, kutangaza kwa maneno na matendo kwamba "Mwisho wa mambo yote umekaribia."—**Letter 43, 1902.** [EVsw 17.4]

Mkanganyiko Wakati Wa Siku Za Mwisho—

Maneno ya Yesu Kristo yanatamkwa kwetu tunaoishi hapa chini mwishoni mwa historia ya dunia hii. **"Luke 21:28** ***Basi mambo hayo yaanzapo kutokea, changamkeni, mkaviinue vichwa vyenu, kwa kuwa ukombozi wenu umekaribia."*** Mataifa yako kwenye machafuko. Nyakati za kuchanganyikiwa ziko juu yetu. Mawimbi ya bahari yananguruma; Mioyo ya watu ina hofu kwa yale yanayoijia dunia; Lakini wale wanaomwamini Mwana wa Mungu watasikia sauti Yake katikati ya dhoruba, Akiwaambia, ni Mimi, msiogope..... Tunaona ulimwengu umegeuka kwa mapatano katika uovu na ukengeufu. Uasi wa amri za **Mungu** unaonekana kuwa karibu ulimwenguni pote. Katikati ya msukosuko wa msisimko wa kuchanganyikiwa kila mahali, kuna kazi ya kufanywa ulimwenguni. —**Manuscript 44, 1900.** [EVsw 18:1]

Kupanda Kanuni Katika Maeneo Ya Giza-

Majeshi ya Shetani ni mengi, na watu wa **Mungu** lazima waenee juu ya ulimwengu wote, wakipanda/kukuza kanuni za Kweli katika mahali penye giza la dunia na kufanya kila wawezalo kuuharibu ufalme wa Shetani. **—Letter 91, 1900.** [EVsw 18:2]

Kazi ya Juu Zaidi, Kubwa Zaidi -

Bwana anapanga kwamba uwasilishaji wa ujumbe huu utakuwa kazi ya juu zaidi, na kubwa zaidi inayofanywa ulimwenguni kwa wakati huu. **—Testimonies For The Church 6:11 (1900).** [EVsw 18:3]

Maendeleo ya Haraka Zaidi -

Katika nchi hii na katika nchi za kigeni sababu pekee ya Ukweli wa leo, ni kufanya maendeleo ya haraka zaidi kuliko ilivyofanywa kabla. Ikiwa watu wetu watatoka kwa imani, wakifanya kila wawezalo ili kuanza, na kufanya kazi kwa kufuata njia za Kristo, njia itafunguliwa mbele yao. Ikiwa wataonyesha jitihada ambayo inayohitajika ili kupata mafanikio, na imani inayosonga mbele bila shaka katika utii wa amri ya **Mungu**, watapata mafanikio makubwa. Ni lazima waende sehemu za mbali na kwa haraka iwezekanavyo, wakiwa na dhamira ya kufanya mambo yale yale ambayo Bwana amesema yanapaswa kufanywa. Ni lazima wawe na imani inayowasukuma na ya dhati, isiyoyumba.... Ulimwengu lazima usikie ujumbe wa onyo. — **Manuscript 162, 1905.** [EVsw 18:4]

Ushawishi wa Injili Unaozidi Kuongezeka

Kuifikia Dunia Kwa Haraka (Kuifunga Dunia) -

Kila mahali nuru ya **Kweli** inapaswa kuangaza, ili mioyo iliyo katika usingizi wa ujinga iweze kuamshwa na kuongolewa. Katika nchi na miji yote Injili inapaswa kutangazwa....**[EVsw 19:1]**

Makanisa yanapaswa kupangwa na mikakati kuwekwa kwa ajili ya kazi inayotakiwa kufanywa na washiriki wa makanisa mapya yaliyopangwa. Kazi hii ya umishenari ya Injili inapaswa kuendelea ili kufikia na kuongeza eneo jipya, kupanua sehemu zilizolimwa za shamba la mizabibu. Mduara unapaswa kupanuka mpaka uufunge ulimwengu. **— Letter 86, 1902.** **[EVsw 19:2]**

Kaskazini, Kusini, Mashariki na Magharibi

Kutoka mji hadi mji, kutoka jiji hadi jiji, kutoka nchi hadi nchi, ujumbe wa onyo unapaswa kutangazwa, si kwa maonyesho ya nje, lakini kwa nguvu ya Roho, na watu wa imani. **[EVsw 19:3]**

Na ni muhimu kwamba aina bora ya kazi ifanywe. Wakati umefika, wakati muhimu, ambapo, kupitia wajumbe wa **Mungu**, gombo linafunuliwa kwa ulimwengu. Ukweli unaojumuishwa katika jumbe za malaika wa kwanza, wa pili, na wa tatu lazima uende kwa kila taifa, jamaa, lugha, na watu; unapaswa uangaze kwenye giza la kila bara na kuenea hadi visiwa vya bahari ....**[EVsw 19:4]**

Hebu kuwe na mipango ya busara zaidi ya mafanikio ya kazi. Juhudi zilizoamuliwa zinapaswa kufanywa ili kufungua maeneo mapya kaskazini, kusini, mashariki, na magharibi.... Ukweli kwamba uwasilishaji wa Kweli uliopuuzwa kwa muda mrefu unapaswa kuwapa matamanio wahudumu na watendakazi wetu kuingia katika maeneo haya na wasiiache kazi hiyo hadi pale watakapokuwa wametoa ujumbe huo waziwazi. —**Manuscript 11, 1908.** **[EVsw 19:5]**

Bila Kuzuiwa na Vizuizi au Vikwazo -

Kweli, ikiwapita wale wanaoidharau na kuikataa, itashinda. Ingawa wakati fulani huonekana kama imecheleweshwa, maendeleo yake hayajawahi kuzuiliwa. Ujumbe wa **Mungu** unapokutana na upinzani, Yeye huupa nguvu ya ziada ili uathiri mioyo kwa ufanisi mkubwa zaidi. Ukiwa umejazwa na nguvu za Kiungu, utapenya kupitia vizuizi vigumu zaidi na kushinda kila kikwazo. —The Acts of the Apostles, 601 (1911).**[EVsw 20:1]**

Kazi Kubwa -

Kazi ambayo Injili inaidhihirisha kama kazi ya umishenari ni kazi iliyonyooka, na kubwa ambayo itang'aa zaidi na kung'aa zaidi hadi utimilifu wa siku. **—Letter 215b, 1899.** **[EVsw 20:2]**

Ushawishi Unaozidi na Kupanuka—

Ushawishi wa jumbe hizi umekuwa ukiongezeka na kupanuka, ukianzisha chemchemi za utendaji katika maelfu ya mioyo, na kuleta uwepo wa taasisi za elimu, nyumba za uchapishaji, na taasisi za afya; Hivi vyote ni vyombo (vitendea kazi) vya **Mungu** vinavyoshirikiana katika kazi kuu inayowakilishwa na Malaika wa kwanza, wa pili, na wa tatu wanaoruka katikati ya mbingu ili kuwaonya wakaaji wa ulimwengu kwamba **Kristo** anakuja tena kwa nguvu na utukufu mkuu. —**The Review and Herald, December 6, 1892.** **[EVsw 20:3]**

Tangaza Ujumbe Katika Sehemu Mpya-

Tuna ujumbe mzito zaidi kuwahi kutolewa ulimwenguni. Lakini muda mwingi sana umetolewa kwa wale ambao tayari wanaijua ile Kweli. Nafasi inayohitaji kutumia muda kwa wale ambao wamepewa fursa nyingi za kujifunza ile **Kweli**, ni kwenda kwa watu ambao hawajawahi kusikia ujumbe wenu. Fanyeni mikutano yenu ya makambi [Zingatia. —Mikutano ya makambi ya Waadventista wa Sabato ya miaka ya awali ilikuwa mawakala wakubwa wa uinjilisti waliovuta hadhira (wasikilizaji) kubwa, makini, ya watu wasio Waadventista. Katika kutajwa mara kwa mara kwa mikutano ya makambi katika juzuu hii muktadha unaonyesha wazi kwamba ni mkutano wa hema wenye uwezo mkubwa wa uinjilisti ambao kwa kawaida hurejelewa. Tazama ukurasa wa 82, 83 kwa taarifa zinazoelezea mikutano hiyo. Katika miji ambayo **Ukweli** haujatangazwa. Wengine watahudhuria mikutano na kupokea ujumbe. —**Letter 87, 1896.** **[EVsw 20:4]**

Maeneo Mapya Maeneo Bora -

Maeneo ambayo **Ukweli** haujawahi kutangazwa ni mahali pazuri pa kufanyia kazi. Ukweli unapaswa kushika usikivu wa wale ambao hawajawahi kuusikia. Wataona hali ya matokeo ya uovu uletwao na dhambi, na toba yao itakuwa kamili na ya dhati. Bwana atafanya kazi juu ya mioyo ambayo katika siku za nyuma mara kwa mara haikuwahi kupewa wito, mioyo ambayo hapo awali haikuona ubaya wa dhambi. **—Letter 106, 1903.** [EVsw 21:1]

Ikiwa Ukweli Ungetangazwa kwa Nguvu-

Kulionekana mbele yangu mji baada ya mji uliohitaji jitihada za uinjilisti. Ikiwa jitihada za bidii zingetolewa kwa kazi ya kuutangaza **Ukweli** kwa wakati huu katika miji ambayo haijaonywa, watu wasingebaki bila toba kama walivyo sasa. Kutokana na nuru ambayo nimepewa najua kwamba huenda leo tungekuwa na maelfu ya watu zaidi wanaofurahia Ukweli kama kazi hiyo ingeendelezwa kama hali inavyodai, katika nyanja nyingi ya juhudi. **—Letter 94a, 1909.** [EVsw 21:2]

Hitaji la Watendakazi wa Uinjilisti

Mavuno Ni Mengi— Ujumbe wa onyo ulio mzito, na mtakatifu lazima utangazwe katika maeneo magumu zaidi na katika miji iliyojaa dhambi, kila mahali ambapo nuru ya ujumbe mkuu wa Injili wa Malaika watatu bado haijawahi kuchomoza. Kila mmoja lazima asikie mwito wa mwisho wa kuingia kwenye karamu ya arusi ya Mwana-Kondoo....[EVsw 21:3]

Nchi ambazo hadi sasa zilikuwa zimefungwa kwa Injili sasa zinafungua milango yake, na zinaomba **Neno** la **Mungu** lielezwe kwao. Wafalme na wakuu wanafungua milango yao iliyokuwa imefungwa kwa muda mrefu, wakiwalika watangazaji (wajumbe) wa Habari njema ya msalaba waingie. Hakika mavuno ni mengi. Ni umilele peke yake utakaoonyesha matokeo ya jitihada zilizopangwa vyema na zinazofanywa sasa. **—Gospel Workers, 27 (1915).**[EVsw 22:1]

Mabalozi wa Kristo—

Wahudumu wa **Mungu**, wenye mioyo inayowaka kwa upendo kwa **Kristo** na kwa wanadamu wenzenu, jitahidini kuwaamsha wale waliokufa kwa makosa na dhambi. Hebu maombi yenu ya dhati na maonyo yenu ya nguvu yapenye katika dhamiri zao. Sala zenu za bidii na za moto ziyeyushe mioyo yao na kuwaongoza katika toba kumwelekea Mwokozi. Ninyi ni mabalozi wa **Kristo**, mmeitwa kutangaza ujumbe Wake wa wokovu. — **Gospel Workers, 35 (1915).**[EVsw 22:1]

Watendakazi Mia Moja Ambapo Sasa ni Mmoja-

Muda ni mfupi. Watendakazi wa **Kristo** wanahitajika kila mahali. Kunapaswa kuwa na vibarua mia moja wenye bidii, waaminifu nyumbani na nje ya nchi ambapo sasa kuna mmoja tu. Barabara kuu na njia za kupita bado hazijafanyiwa kazi. Motisha za haraka zinapaswa kutolewa kwa wale ambao sasa wanapaswa kujishughulisha na kazi ya umishenari kwa ajili ya Bwana. **—Fundamentals of Christian Education, 488 (1903).** [EVsw 22:2]

Mgawanyo wa Busara wa Watu -

Kwa utimilifu wa yote ambayo **Mungu** anataka katika kuionya miji, watumishi Wake lazima wapange mgawanyo wa busara na wa nguvu za kufanya kazi. Mara nyingi vibarua ambao wangeweza kuwa na uwezo wa kufanya kazi katika mikutano ya hadhara, wanajishughulisha na kazi nyingine ambayo haiwapi muda wa kufanya huduma kamili miongoni mwa watu. Kwa ajili ya uendeshaji wa mambo katika vituo mbalimbali vya kazi yetu, wale walio katika wajibu lazima wajitahidi, iwezekanavyo, kupata watu waliowekwa wakfu ambao wamefunzwa katika nyanja za kazi. Kuna ulazima wa mara kwa mara wa kujilinda dhidi ya mwelekeo wa kushikilia katika vituo hivi vya mvuto watu ambao wangeweza kufanya kazi kubwa na muhimu zaidi kwenye jukwaa la umma, katika kuwasilisha mbele ya wasioamini zile Kweli za **Neno** la **Mungu**. -**The Review and Herald, April 7, 1910.**[EVsw 22:3]

Wito mkuu- Huduma ya Uchungaji

Haipaswi kuwa na upuziaji wa huduma ya Injili-huduma ya kichungaji. Hakuna kazi au mradi wowote unaopaswa kuendeshwa kwa namna itakayofanya huduma ya **Neno** kuonekana kama jambo la hadhi ya chini. Sivyo ilivyo. Wale wanaopuuza huduma ya Injili, naam huduma ya uchungaji, wanampuuza **Kristo**. Kazi iliyo

ya juu kuliko zote ni huduma katika nyanja zake mbalimbali, na ni lazima jambo hili liwekwe mbele ya vijana kwamba hakuna kazi iliyo na baraka kubwa zaidi kutoka kwa **Mungu** kuliko ile ya mhudumu wa injili. **[EVsw 23:1]**

Vijana wetu wasizuiliwe kuingia katika huduma ya Injili. Kuna hatari kwamba kupitia maelezo yanayopendeza mno, baadhi watavutwa mbali na njia ambayo **Mungu** anawaamuru waitembee. Baadhi wamehimizwa kuchukua kozi za masomo ya kitabibu wakati walipaswa kujitayarisha kuingia katika huduma ya Injili. —Testimonies For The Church 6:411 (1900).**[EVsw 23:2]**

Vijana Kuchukua Nafasi ya Wabeba Bendera (Kanuni)-

Wabeba-bendera wanaanguka kwa kifo, na vijana wanapaswa kuandaliwa kuchukua nafasi zilizobaki wazi, ili ujumbe uendelee kutangazwa. Vita vya mashambulizi lazima viongezwe. Wale wenye ujana na nguvu wanapaswa kwenda katika sehemu za giza za dunia, kuziita roho zinazopotea kwenye toba. —Gospel Workers, 104 (1915).**[EVsw 23:3]**

Kujiandaa Haraka Kwa Ajili ya Huduma -

Shule zetu zimeanzishwa na Bwana, na ikiwa zitaendeshwa kwa kupatana na kusudi Lake, vijana waliopelekwa katika hizo shule wataandaliwa kwa haraka kushiriki katika safu mbalimbali za kazi ya umishenari. Wengine watafunzwa kuingia shambani wakiwa wauguzi wamishenari, wengine wakiwa wauza vitabu vya injili, wengine wainjilisti, wengine wakiwa walimu, na wengine kama wachungaji na wahudumu wa injili. **—Letter 113, 1903. [EVsw 23:4]**

Wafundishe Vijana Kufanya Kazi ya Uinjilisti—

Bwana anatoa wito kwa wale waliojiunga na vituo vyetu vya afya, nyumba za uchapishaji, na shule kuwafundisha vijana kufanya kazi za uinjilisti. Wakati na nguvu zetu hazipaswi kutumika kwa kiasi kikubwa katika kuanzisha vituo vya afya, maduka ya chakula, na mikahawa kiasi kwamba kwamba kazi zingine zikapuuzwa. Vijana wa kiume na wa kike wanaopaswa kujishughulisha na huduma, katika kazi ya Biblia, na katika kazi ya kuuza vitabu hawapaswi kuwa chini ya kifungo (kuajiriwa katika) cha kazi ya ufundi/mitambo. **—The Review and Herald, May 16, 1912. [EVsw 24:1]**

Wito Kwa Vijana Wenye Nguvu -Wako wapi watu ambao wataenda kazini, wakimtumaini **Mungu** kikamilifu, walio tayari kutenda na kuthubutu? **Mungu** anatoa wito, "Mwanangu, nenda ukafanye kazi leo katika shamba Langu la mizabibu." **Mungu** atawafanya vijana wa leo kuwa hazina za mbingu zilizochaguliwa, ili kuwasilisha mbele ya watu **Ukweli** tofauti (kinyume na) na makosa na ushirikina, ikiwa watajitoa Kwake. Acha **Mungu** awape jukumu vijana wenye nguvu, ambao **Neno** Lake linadumu ndani yao na ambao watawapa wengine **Ukweli**. —**Manuscript 134, 1898.[EVsw 24:2]**

Watu Ambao Hawatarudi Nyuma -Mungu anawaita watendakazi waliowekwa wakfu ambao watakuwa waaminifu Kwake—watu wanyenyekevu wanaoona uhitaji wa kazi ya uinjilisti na hawarudi nyuma bali wanafanya kazi ya kila siku kwa uaminifu, wakimtegemea **Mungu** kwa msaada na nguvu katika kila dharura. Ujumbe huo unapaswa kuchukuliwa na wale wanaompenda na kumcha **Mungu**. Usiweke jukumu lako kuwa chini ya konferensi yoyote. Songeni mbele, na, kama wanjilisti, na kwa njia ya unyenyekevu mkiwasilisha "Ndivyo yasemavyo Maandiko." **—Letter 43, 1905.[EVsw 24:3]**

SEHEMU YA 2—MIKUSANYIKO YA MIJI MIKUU (Metropolitan Masses)

Katika Kivuli cha Adhabu Inayokaribia

Mamilioni ya watu mijini wanapaswa kufanya maamuzi hivi karibuni—Giza la kiroho linaloifunika dunia nzima leo, linazidishwa katika vituo vya watu wengi. Ni katika miji ya mataifa ambapo mtendakazi wa Injili hukutana na hali ya kutotubu na hitaji kuu zaidi.... **{EVsw 25:1}**

Rekodi ya uhalifu na uovu katika miji mikubwa ya nchi ni ya kutisha. Uovu wa waovu unazidi fahamu za mwanadamu. Miji mingi inazidi kuwa Sodoma mbele (machoni pa) za mbingu. Uovu unaoongezeka umekuwa kiasi kwamba umati wa watu unakaribia kwa kasi hatua inayozidi uzoefu wao binafsi ambayo itakuwa vigumu sana kuwafikishia ujuzi unaookoa wa ujumbe wa malaika wa tatu. Adui wa nafsi anafanya kazi kwa ustadi ili kupata udhibiti kamili wa akili ya mwanadamu; Na kile ambacho watumishi wa **Mungu** hufanya ili kuwaonya na kuwatayarisha wanadamu kwa ajili ya siku ya hukumu, lazima kifanyike haraka. {EVsw 25:2}

Masharti ambayo yanawakabili watendakazi wa Kikristo katika miji mikuu, yanahusisha wito mzito (makini) wa juhudi zisizochoka kwa niaba ya mamilioni wanaoishi ndani ya kivuli cha adhabu inayokuja. Hivi karibuni watu watalazimika kufanya maamuzi makubwa, na wanapaswa wapate nafasi ya kusikia na kuelewa **Ukweli** wa Biblia, ili waweze kuchukua msimamo wao kwa akili mahiri katika upande sahihi. **Mungu** anawaita sasa wajumbe Wake bila ya shaka, kuionya miji wakati rehema ingali ikiendelea, na huku umati wa watu ukiwa bado unahusika kwenye ushawishi wa kuongoka wa **Kweli** ya Biblia. **—The Review and Herald, April 7, 1910.** {EVsw 25:3}

Kwenye "Mwelekeo Wa Kifo-Gwaride linaolekea kifo" -

Shetani yuko kazini akishughulika sana katika miji yetu iliyo na msongamano wa watu. Kazi yake inaonekana kwa njia ya mkanganyiko, ugomvi na mifarakano kati ya kazi na mtaji, na unafiki ambao umeingia makanisani. Ili watu wasichukue muda wa kutafakari, Shetani anawaongoza katika mzunguko wa burudani na kutafuta raha, kula na kunywa. Anawajaza kwa tamaa ya kufanya maonyesho ambayo yataitukuza nafsi-kujipenda mwenyewe. Hatua kwa hatua, ulimwengu unafikia hali zilizokuwepo katika siku za Nuhu. Kila uhalifu unaowezekana unafanywa.Tamaa ya mwili, kiburi cha macho, maonyesho ya ubinafsi, matumizi mabaya ya mamlaka, ukatili, na nguvu iliyotumika kuwafanya watu waungane na mashirikisho na miungano—wakijifunga wenyewe kwenye mafungu ya kuwashia moto mkuu wa siku za mwisho. —Haya yote ni kazi ya mawakala wa kishetani. Mzunguko huu wa uhalifu na upumbavu watu huuita "maisha."... {EVsw 26:1}

Ulimwengu, ambao hutenda kana kwamba hakuna **Mungu**, uliozama katika shughuli za ubinafsi, hivi karibuni utapata uharibifu wa ghafla, na hautakwepa. Wengi wanaendelea katika kujiridhisha kizembe hadi wanachukizwa sana na maisha hadi wanajiua. Wakicheza dansi, wakipiga makelele mengi, na kunywa na kuvuta sigara, wakifurahia tamaa zao za wanyama, wanaenda kama ng'ombe kwenye mauaji. Shetani anafanya kazi kwa ustadi wake wote na uchawi ili kuwafanya watu wasonge mbele kwa upofu hadi Bwana atakapotoka mahali Pake ili kuwaadhibu wakaaji wa dunia kwa ajili ya maovu yao, wakati dunia itakapofichua damu yake na kutomfunika tena aliyeuawa. Ulimwengu wote unaonekana kuwa katika gwaride/maandamano ya kufa. **—Manuscript 139, 1903.** {EVsw 26:2}

Tamaa ya Makuu

Wanaume na wanawake waishio katika miji hii wanazidi kufungwa kwa haraka na mahusiano yao ya kibiashara. Kwa bidii isiyo na kiasi wanajenga majengo yenye minara inayoinuka juu hadi mbinguni. Akili zao zimejawa na mashauri ya kibinadamu na mipango ya tamaa ya makuu. **-Manuscript 154, 1902.** {EVsw 27:1}

Ikiwa Maonyo ya Mbinguni Hayatiliwi Maanani—

Nimeamriwa nitangaze ujumbe huu: Kwamba miji iliyojaa maasi, na dhambi kupita kiasi, itaangamizwa kwa matetemeko ya ardhi, kwa moto, na kwa gharika. Dunia yote itaonywa kwamba kuna **Mungu** atakayeonyesha mamlaka Yake kama **Mungu**. Mawakala Wake wasioonekana wataleta maangamizi, uharibifu, na mauti. Mali zote zilizokusanywa zitakuwa kama si kitu kabisa……..{EVsw 27:2}

Majanga yatakuja—majanga ya kutisha mno, yasiyotarajiwa kabisa; na maangamizi haya yatafuatana kwa mfululizo, moja baada ya jingine. Iwapo watu watasikiliza maonyo ambayo **Mungu** ameweka mbele yao, na iwapo makanisa yatatubu, yakiurudia uaminifu wao wa awali, basi miji mingine inaweza kuachwa salama kwa muda. Lakini kama watu waliodanganyika wataendelea kutembea katika njia ile ile—wakidharau sheria ya **Mungu** na kueneza udanganyifu mbele ya watu—**Mungu** ataruhusu wapate msiba-majanga, ili fahamu zao ziamshwe…….{EVsw 27:3}

Bwana hatawatupa mbali waasi wote ghafla, wala hataharibu mataifa yote kwa jumla; lakini ataiadhibu miji na maeneo ambamo watu wamejitoa kabisa wawe chini ya utawala wa mawakala wa Shetani. Kwa uangalifu mkubwa miji ya mataifa itakabiliwa na hukumu, lakini haitatembelewa kwa ukali wote wa ghadhabu ya **Mungu**, kwa kuwa bado zipo baadhi ya roho ambazo zitajikwamua kutoka katika udanganyifu

wa adui, na watatubu na kuongoka; ilhali wengi wataendelea kujikusanyia ghadhabu kwa ajili ya siku ya ghadhabu. —**Manuscript 35, 1906.** {EVsw 27:4}

"Kuwaamsha Watu"

Wakati nilipokuwa Loma Linda, California, Aprili 16, 1906, nilipewa maono ya ajabu sana. Katika maono ya usiku, nilijikuta nimesimama juu ya mahali pa juu, ambapo ningeweza kutazama chini na kuona nyumba zikitingishwa kama mwanzi upeponi. Majengo makubwa na madogo yalianguka chini. Maeneo ya anasa, kumbi za starehe, kumbi za drama, hoteli, na makao ya matajiri yalitikiswa na kuvunjika vipande vipande. Maisha wa watu wengi yalikatiliwa mbali, na anga lilijaa mayowe vya majeruhi na waliokuwa wamejaa hofu kuu.{EVsw 28:1}

Wale malaika wa uharibifu wa **Mungu** walikuwa kazini. Kwa mguso mmoja tu, majengo yaliyokuwa yamejengwa kwa ustadi mkubwa kiasi kwamba wanadamu waliamini kuwa yako salama dhidi ya hatari yoyote, yaligeuka haraka kuwa marundo ya kifusi. Hakukuwa na mahali pa usalama wa kweli. Sikuona kama nipo katika hatari yoyote ya moja kwa moja, lakini wingi na uzito wa yale niliyoyaona siwezi kuyaeleza kwa maneno. Ilionekana kana kwamba uvumilivu wa **Mungu** ulikuwa umefikia kikomo, na siku ya hukumu ilikuwa imewasili.{EVsw 28:2}

Malaika aliyesimama kando yangu alinieleza kwamba ni wachache mno wanaofahamu uovu uliokithiri katika dunia yetu leo hii, na hasa katika miji mikubwa. Alitangaza kuwa Bwana ameweka wakati ambao atawatembelea waasi kwa ghadhabu kwa sababu ya kudharau kwao kwa ukaidi sheria Yake takatifu. {EVsw 28:3}

Ingawa yale maono niliyoyaona yalikuwa ya kutisha, lile lililogusa moyo wangu zaidi ni mafundisho niliyopokea pamoja na maono hayo. Malaika aliyesimama nami alitangaza kuwa utawala mkuu wa **Mungu**, na utakatifu wa sheria Yake, lazima vifunuliwe kwa wale wanaokataa kwa ukaidi kumtii Mfalme wa wafalme. Wale wanaochagua kubaki katika hali ya kutokuwa waaminifu, ni lazima watembelewe kwa rehema kupitia hukumu, ili kwamba, ikiwezekana, waamshwe na kutambua uovu wa njia yao. **Testimonies For The Church 9:92 (1909).** {EVsw 28:4}

Maono ya Maangamizi Makubwa

Ijumaa iliyopita asubuhi, kabla sijaamka kabisa kutoka usingizini, nilionyeshwa tukio la kutisha sana. Nilionekana kana kwamba nimeamka kutoka usingizini, lakini sikuwa nyumbani kwangu. Kutoka kwenye madirisha, niliweza kuona moto mkubwa ukiwaka kwa nguvu. Mipira mikubwa ya moto ilikuwa ikianguka juu ya nyumba, na kutoka kwenye mipira hiyo, mishale ya moto ilikuwa ikiruka kwenda kila upande. Haikuwezekana kuzima moto uliokuwa umeanzishwa, na maeneo mengi yalikuwa yakiteketezwa. Hofu ya watu haingeweza kuelezwa kwa maneno. Baada ya muda fulani, niliamka na kujikuta niko nyumbani kwangu. —**Letter 278, 1906.** {EVsw 29:1}

Kwa Sababu Miji Mikubwa Itafagiliwa—

Kila mahali, wapo watu ambao wanapaswa kuwa katika huduma hai, wakitoa ujumbe wa mwisho wa onyo kwa ulimwengu uliopotoka. Kazi ambayo kwa muda mrefu ilipaswa kuwa ikiendelea kwa bidii kwa ajili ya kuwaleta watu kwa Kristo haijafanywa. Wakazi wa miji isiyomcha **Mungu**, ambayo muda si mrefu itatembelewa na maangamizi, wameachwa bila ya huruma. Wakati umekaribia ambapo miji mikubwa itafagiliwa, na kila mtu anapaswa kuonywa juu ya hukumu hizi zijazo. Lakini ni nani anayejitoa kwa moyo wote kwa kazi hii kama vile **Mungu** anavyotaka? …..{EVsw 29:2}

Kwa sasa, hata sehemu ya elfu moja ya kazi inayopaswa kufanyika katika miji haijafanyika; na kazi hiyo ingewekwa katika matendo iwapo wanaume kwa wanawake wangetimiza wajibu wao kikamilifu. —**Manuscript 53, 1910.** {EVsw 29:3}

Maangamizi ya Maelfu ya Miji—Laiti watu wa **Mungu** wangekuwa na ufahamu wa maangamizi yaliyo karibu kuyapata maelfu ya miji, ambayo sasa karibu yote imekabidhiwa kwa ibada ya sanamu. —**The Review and Herald, September 10, 1903.** {EVsw 29:4}

Harakisheni Kazi —

Ninapozitafakari hali za miji, ambazo kwa wazi zimo chini ya nguvu za Shetani, najiuliza swali hili: Je, mwisho wa mambo haya utakuwa upi? Uovu katika miji mingi unazidi kuongezeka. Uhalifu na maasi vinaendelea kushamiri kila upande. Aina mpya za sanamu na ibada za uongo zinaendelea kuingizwa katika jamii. Katika kila taifa, akili za wanadamu zimeelekezwa kwenye kuvumbua jambo jipya. Ujasiri wa kipumbavu na mkanganyiko wa mawazo vinaongezeka kila mahali. Hakika, miji ya dunia hii inafanana sana na Sodoma na Gomora. {EVsw 29:5}

Kama watu wa **Mungu**, twapaswa kuharakisha kazi katika miji, kazi ambayo imekwamishwa kwa sababu ya ukosefu wa watendakazi, ukosefu wa rasilimali, na kukosekana kwa roho ya kujitoa kikamilifu kwa **Mungu**. Wakati huu, watu wa **Mungu** wanahitaji kuielekeza mioyo yao kikamilifu kwa Bwana; maana mwisho wa mambo yote umekaribia. Wanahitaji kunyenyekeza mioyo yao, na kuwa makini kwa mapenzi ya Bwana, wakitenda kwa bidii kubwa ili kutimiza kile ambacho **Mungu** ameonyesha lazima kifanyike kwa ajili ya kuionya miji kuhusu maangamizi yanayoikabili. —**The Review and Herald, January 25, 1912.**{EVsw 30:1}

Magumu Yanavyozidi Kuongezeka

Songeni Mbele kwa Bidii Inayoongezeka

Tunakaribia pambano kuu la mwisho. Kila hatua tunayopiga sasa ni lazima ipigwe kwa bidii inayoongezeka; kwa kuwa Shetani anafanya kazi kwa nguvu zote ili kuongeza vizingiti mbele yetu. Adui anatumia hila zote za udanganyifu wa uovu ili kunasa roho za wanadamu. Nimepewa agizo la kuwaambia wahudumu wa Injili pamoja na madaktari wetu wa kimishenari: Songeni mbele. Kazi inayopaswa kufanywa inahitaji kujikana nafsi katika kila hatua; lakini songeni mbele. **—Letter 38, 1908.** {EVsw 30:2}

Hakuna Wakati wa Kupoteza — Hatuna wakati wa kupoteza. Mwisho umekaribia. Safari kutoka sehemu moja hadi nyingine ili kueneza Kweli hivi karibuni itazuiliwa kwa hatari upande wa kuume na wa kushoto. Kila kitu kitawekwa ili kuzuia njia ya wajumbe wa Bwana, hata wasiweze kutenda yale ambayo kwa sasa bado yawezekana kutendwa. Tunapaswa kuikabili kazi yetu kwa ujasiri, na kusonga mbele kwa haraka katika vita vya kiroho vyenye mashambulizi makali.{EVsw 30:3}

Kutokana na nuru niliyopewa na **Mungu**, najua ya kwamba nguvu za giza zinatenda kazi kwa bidii kuu kutoka chini, na kwa mwendo wa kujificha, Shetani anasonga mbele ili kuwateka wale waliolala usingizi, kama vile mbwa mwitu atekavyo mawindo yake. Tunayo maonyo sasa ambayo twaweza kutoa; tunayo kazi sasa ambayo twaweza kutenda; lakini muda si mrefu kazi hii itakuwa ngumu zaidi kuliko tuwezavyo kufikiri. **Mungu** atusaidie tubaki katika njia ya nuru, tukifanya kazi tukiwa tumemwelekezea macho Yesu, Kiongozi wetu, na kwa uvumilivu na kudumu tusonge mbele mpaka tupate ushindi. —**Testimonies For The Church 6:22 (1900).**{EVsw 31:1}

Uinjilisti wa Mijini Unazidi Kuwa Mgumu—

Hatufahamu kwa ukamilifu kiwango ambacho mawakala wa Shetani wanafanya kazi katika miji hii mikubwa. Kazi ya kupeleka ujumbe wa Kweli ya wakati huu mbele ya watu inazidi kuwa ngumu siku baada ya siku. Ni muhimu vipaji vipya na tofauti viungane katika kazi ya akili na hekima kwa ajili ya watu. — **Medical Ministry, 300 (1909).** {EVsw 31:2}

Wakati Unaofaa kwa Miji Umepita — Kazi kuu inapaswa kufanywa. Ninasukumwa na Roho wa **Mungu** kusema kwa wale wanaojishughulisha na kazi ya Bwana, kwamba wakati ufaao wa ujumbe wetu kufikishwa mijini umeshapita, na kazi hii haijafanyika. Nimelemewa sana na mzigo moyoni kwamba sasa ni lazima tuukomboe wakati uliopotea. —**Manuscript 62, 1903.** {EVsw 31:3}

Kazi ambayo kanisa limeshindwa kuifanya wakati wa amani na ustawi, litalazimika kuifanya wakati wa dhiki kuu, chini ya hali za kukatisha tamaa na za kutisha kabisa. —**Testimonies For The Church 5:463 (1885).** {EVsw 31:4}

Roho wa Mungu Anaondolewa taratibu —

Siku tunazoishi ni za huzuni na umuhimu mkubwa. Roho wa **Mungu** anajiondoa polepole lakini kwa hakika kutoka duniani. Mapigo na hukumu tayari yanawashukia wale wanaoidharau neema ya **Mungu**. Majanga ya nchi kavu na baharini, hali ya sintofahamu katika jamii, na makelele ya vita ni dalili za kutisha. Haya ni matukio yanayotangaza kuwa mambo makuu ya ajabu yapo karibu kutokea. {EVsw 31:5}

Mawakala wa uovu wanaunganisha nguvu zao na kuimarisha ushirikiano wao. Wanajitayarisha kwa ajili ya lile jaribio kuu la mwisho. Mabadiliko makubwa yako karibu kutokea katika dunia yetu, na hatua za mwisho zitakuwa za haraka mno. **—Testimonies, vol. 9, p 11. (1909).**{EVsw 32:1}

Roho ya Vita Yachochea Mataifa—Majaribu ya kutisha na mitihani mikubwa inawasubiri watu wa **Mungu**. Roho ya vita inachochea mataifa kutoka mwisho mmoja wa dunia hadi mwingine. —**Testimonies For The Church 9:17 (1909).**{EVsw 32:2}

Kabla ya Milango Iliyofunguliwa Kufungwa Tena

Mara kwa mara nimepewa maelekezo ya kuwasilisha kwa makanisa yetu kazi inayopaswa kufanywa katika miji mikubwa. Kazi kuu ipo ya kufanywa, siyo tu katika maeneo tuliyokuwa na makanisa tayari, bali pia mahali ambapo ile Kweli haijawasilishwa kwa ukamilifu. Hata katikati yetu kuna watu wasioifahamu Kweli, kama walivyo katika nchi za mbali. Njia lazima ifunguliwe ili kuwafikia hawa kwa Kweli ya wakati huu; na milango hii inapaswa kufunguliwa mara moja....{EVsw 32:3}

Mara nyingi tumeambiwa kuwa miji yetu itasikia ujumbe huu, lakini kwa polepole sana tunazingatia maagizo haya. Niliona Mtu mmoja amesimama kwenye jukwaa refu, mikono yake imeenea. Akageuka na kuonyesha kila mwelekeo, akisema, "Dunia inaangamizwa kwa kutojua sheria takatifu za **Mungu**, na Waadventista wa Sabato wamelala." Bwana anasihi kwa ajili ya watendakazi, kwa sababu kazi kuu ipo ya kufanywa. Kuna waongofu wa kweli wanaopaswa kuletwa (kufanywa) ambao wataongeza kanisa, wale ambao watakuwa wameokolewa. Wanaume na wanawake walioko katika njia kuu na katika mitaa midogo wanapaswa kufikiwa…..{EVsw 32:4}

Tuko nyuma sana katika kufuata nuru ambayo **Mungu** ametupatia kuhusu kazi katika miji mikubwa yetu. Wakati unakaribia ambapo sheria zitazingatiwa zitakazofunga milango ambayo sasa iko wazi kwa ujumbe huu. Tunahitaji kuamka sasa kwa bidii ya dhati na halisi, wakati malaika wa **Mungu** wanangojea kutoa msaada wao wa ajabu kwa wote watakaofanya kazi kuamsha dhamiri za wanaume na wanawake kuhusu haki, kiasi, uadilifu, udhibiti wa tamaa, na hukumu inayokuja. **—Manuscript 7, 1908.** {EVsw 33:1}

Fanya Kazi ungali Unaweza — Ndugu zangu, ingieni mijini kadiri mnanavyoweza. Katika miji ambayo tayari imefikiwa, bado wapo wengi ambao hawajawahi kusikia ujumbe wa Kweli. Wengine waliousikia wamegeuka, na wengine wamekufa katika imani. Bado kuna wengine wengi, wakipata nafasi, wataweza kusikia na kukubali ujumbe wa wokovu.... Hizi, jitihada zetu za mwisho kwa ajili ya kazi ya **Mungu** duniani, lazima ziwe na alama wazi za ushawishi wa **Mungu**. **—Manuscript 7, 1908.** {EVsw 33:2}

"Wito wa Kazi ya Haraka"

Muda Ni Mfupi

Ujumbe ambao nimeamriwa kuufikisha kwa watu wetu wakati huu ni huu: Fanyeni kazi mijini bila kuchelewa, kwa kuwa muda ni mfupi. Bwana ameweka kazi hii mbele yetu kwa miaka ishirini iliyopita au zaidi. Kidogo kimefanyika katika maeneo machache, lakini mengi zaidi yangaliweza kufanyika. **—Letter 168, 1909.** {EVsw 33:3}

Imani Yenu Iko Wapi? — Ninapofikiri juu ya miji mingi ambayo bado haijaonywa, siwezi kupata pumziko. Inasikitisha sana kutafakari kuwa miji hii imetelekezwa kwa muda mrefu namna hii. Kwa miaka mingi sana, miji ya Marekani, ikiwemo miji ya Kusini, imekuwa ikionyeshwa kwa watu wetu kama maeneo yanayohitaji uangalizi wa pekee. Wachache wamebeba mzigo wa kufanya kazi katika miji hii; lakini, tukilinganisha na mahitaji makubwa pamoja na fursa nyingi zilizopo, ni mambo machache mno yaliyofanyika. Imani yenu iko wapi, ndugu zangu? Wako wapi watenda kazi?….. {EVsw 33:4}

Je, hatutapanga kuwatuma wajumbe katika maeneo haya yote, na kuwategemeza kwa ukarimu? Je, watumishi wa **Mungu** hawatakwenda katika vituo hivi vilivyojaa watu, na kuinua sauti zao humo kwa ajili ya kutoa onyo kwa makutano? Katika wakati kama huu, kila mkono unapaswa kushika kazi. **—The Review and Herald, November 25, 1909.** {EVsw 34:1}

Wengi Hawajaonywa — Katika jiji la New York, [Tazama pia uk. 384-406, “Kazi Katika Miji Mikubwa ya Amerika”], na katika miji mingine mingi, kuna maelfu ya watu ambao hawajaonywa bado..... Tunapaswa kuanza kazi hii kwa bidii na moyo wa dhati, na kuifanya. Tukiacha kando maoni yetu ya kibinafsi na tofauti

zetu, tunapaswa kuhubiri **Ukweli** wa Biblia. Watu waliowekwa wakfu, wenye vipawa, wanapaswa kutumwa katika miji hii na kuanza kazi mara moja. —**Manuscript 25, 1910.**{EVsw 34:2}

Wakati wa Kuwamsha Walinzi

Miji yetu inahitaji kufikishiwa ujumbe wa kazi hii... Fedha zinahitajika ili kazi hii iweze kuendelea katika miji ya New York, Boston, Portland, Philadelphia, Buffalo, Chicago, St. Louis, New Orleans, pamoja na miji mingine mingi. Katika baadhi ya miji hii, watu waliamshwa kwa nguvu na ujumbe uliohubiriwa kati ya mwaka 1842 hadi 1844, lakini katika miaka ya hivi karibuni, kazi iliyofanyika haifanani hata kidogo na ile kazi kubwa ambayo inapaswa kuwa ikiendelea kwa sasa. Na inaonekana kana kwamba ni vigumu kuwafanya watu wetu kuhisi mzigo maalum kwa ajili ya kazi katika miji mikubwa.{EVsw 34:3}

Ninaelekeza wito huu kwa ndugu zangu ambao wamesikia ujumbe huu kwa miaka mingi. Wakati umefika wa kuwaamsha walinzi. Nimetumia nguvu zangu kutoa ujumbe ambao Bwana amenipa. Mzigo wa mahitaji ya miji yetu umekuwa mzito juu yangu kiasi kwamba wakati mwingine nimehisi kana kwamba nitakufa. Bwana na awape ndugu zetu hekima, ili wajue jinsi ya kuendeleza kazi hii kwa kupatana na mapenzi ya Bwana. —**Manuscript 13, 1910.**{EVsw 34:4}

Mamilioni Wasikie Ujumbe—Miji inapaswa ifanyiwe kazi.

Mamilioni wanaoishi katika vituo hivi vyenye msongamano mkubwa ni lazima wasikie ujumbe wa malaika wa tatu. Kazi hii ilipaswa kuwa imeendelea kwa haraka katika miaka michache iliyopita. **—The Review and Herald, July 5, 1906.** {EVsw 35:1}

Fursa Maalum za Uinjilisti”

Katika Mikutano Mikubwa Kama Maonyesho ya St. Louis

Nilipatiwa maagizo kwamba tunapokaribia mwisho wa wakati, kutakuwepo mikutano mikubwa mijini mwetu, kama ilivyokuwa karibuni katika maonyesho ya St. Louis, na kwamba maandalizi yafanywe ili kuwasilisha Ukweli katika mikusanyiko hiyo. Kristo alipokuwa duniani, alitumia fursa kama hizo kwa hekima. Popote palipokuwa na mkusanyiko mkubwa wa watu kwa sababu yoyote ile, sauti Yake ilisikika kwa uwazi na mamlaka, akiwaletea ujumbe wa uzima. Na matokeo yake yalikuwa kwamba, baada ya kusulubiwa na kupaa mbinguni, maelfu waliongozwa kutubu na kuamini kwa siku moja tu. Mbegu alizopanda **Kristo** zilipenya kwa kina mioyoni, zikamea, na wakati wanafunzi walipopokea karama ya Roho Mtakatifu, mavuno yalivunwa kwa wingi.{EVsw 35:2}

Wanafunzi walitoka na kuhubiri **Neno** kila mahali kwa nguvu ya ajabu, kiasi kwamba hofu ikawaangukia wapinzani wao, ambao hawakuthubutu kutenda maovu waliyokuwa wamekusudia, kwa sababu ya ushahidi wa wazi kwamba **Mungu** alikuwa akifanya kazi.{EVsw 35:3}

Katika kila mkusanyiko mkubwa, baadhi ya wachungaji/wahudumuwetu wanapaswa kuwepo. Wanapaswa kufanya kazi kwa busara ili kupata nafasi ya kusikilizwa, na kuleta nuru ya **Ukweli** mbele ya wengi iwezekanavyo…...{EVsw 35:4}

Tunapaswa kutumia kila fursa kama ile iliyowasilishwa katika maonyesho ya St. Louis. Katika mikusanyiko kama hiyo, kunapaswa kuwepo watu ambao **Mungu** anaweza kuwatumia. Vipeperushi vyenye nuru ya Kweli ya sasa vinapaswa kusambazwa miongoni mwa watu kama vile majani ya msimu wa kupukutisha majani, yanavyopeperushwa na upepo. Kwa wengi wanaohudhuria mikutano hiyo, vipeperushi hivyo vitakuwa kama majani ya mti wa uzima, ambayo ni kwa ajili ya kuponya mataifa.{EVsw 36:1}

Nawatumia ujumbe huu, ndugu zangu, ili mweze kuwashirikisha wengine. Wale wanaotoka kwenda kuhubiri **Ukweli** watabarikiwa na Yeye aliyewapa jukumu la kutangaza Kweli hii…….{EVsw 36:2}

Wakati umefika ambapo, kamwe hapajawahi kutokea kabla, Waadventista wa **Sabato** wanapaswa kuinuka na kuangaza, kwa sababu nuru yao imekuja, na utukufu wa Bwana umewazukia. **—Letter 296, 1904.**{EVsw 36:3}

"Kuchunguza Mahitaji ya Miji Mikuu"

Kazi ya Miji Ni Ngumu — Tunahisi kwa kina kuhusu kazi katika miji yetu. Ni wachache tu walio tayari kujihusisha na kazi ambayo inasubiri kufanywa. Kuna watu wa tabaka zote za maisha ambao tunapaswa kukutana nao; na kazi hii ni ngumu. Lakini tutahamasisha wote walio na hekima na uwezo wa kuelewa hali halisi wajitolee kwa kazi ya kupeleka sauti ya mwisho ya onyo kwa dunia. **—Letter 82, 1910.**{EVsw 36:4}

Hali ya Kutojali na Njia za Kufanikisha—Watendakazi wachache waaminifu wamekuwa wakijaribu kufanya kitu katika mji huu mkubwa na wenye maovu [New York]. [Angalia pia kurasa 384-389, "New York."] Lakini kazi yao imekuwa ngumu, kwa sababu walikuwa na vifaa vichache sana. Mzee ----- na mkewe wamefanya kazi kwa bidii na uaminifu. Lakini ni nani aliyehisi mzigo wa kuwaimarisha au kuwategemeza katika kazi zao? Ni nani kati ya viongozi wetu waliowatembelea, ili kujua mahitaji ya kazi hii? **—The General Conference Bulletin, April 7, 1903.** {EVsw 36:5}

Hali ngumu na Hofu Sababu ya Kusahau Kazi—Muda unapita kwa haraka kuelekea umilele, na miji hii bado haijaguswa vya kutosha. Kuna nguvu ambayo Roho wa **Mungu** anaweza kuipa **Kweli**. Kadri nuru inavyong'aa akilini, basi dhamiri itakamata mioyo kwa nguvu ambayo haitaweza kupingika……..{EVsw 37:1}

Wajibu wangu ni kusema kwamba **Mungu** anaita kwa nguvu kazi kubwa ifanyike katika miji hii. Maeneo mapya yanapaswa kufunguliwa. Wanaume wanaojua ujumbe na wanapaswa kuhisi wajibu wa kazi hii wameonyesha imani kidogo sana kiasi kwamba kwa sababu ya matatizo au hofu, kazi imeachwa kwa muda mrefu. **—Letter 150, 1909.** {EVsw 37:2}

Agizo la Kujifunza Mahitaji Maalum—Watu saba wangepaswa kuchaguliwa kuungana na mwenyekiti, ili kuanzisha kazi katika miji mikubwa kwa ajili ya wale wanaopotea bila Kweli, wakati juhudi za dhati hazitolewi kuwahifadhi. Watu hawa saba wanapaswa kuwa wale waliokuwa macho (mwamko mkubwa), wenye unyenyekevu, wanyenyekevu na wapole wa moyo. Kamwe miji haipaswi kusahaulika kama ilivyo sasa; maana ujumbe wa wazi umekuja, ujumbe baada ya ujumbe umewasili, ukibidisha kazi ya dhati na bidii ifanywe. {EVsw 37:3}

Watu wasiopungua saba wanapaswa kuchaguliwa kubeba majukumu makubwa ya kazi ya **Mungu** katika miji mikubwa. Watu hawa wanapaswa kujinyenyekeza mioyo yao kila siku na kumtafuta Bwana kwa moyo wote kwa hekima iliyohifadhiwa kwa ajili ya utakatifu. Wanafaa kujiweka mbele za **Mungu** kama watu wenye hamu kubwa ya kufundishwa. Lazima wawe watu wa maombi, wakitambua hatari inayowakumba kwa nafsi zao wenyewe. Je, kazi ya watu hawa saba itakuwa nini? Wanapaswa kuchunguza mahitaji ya miji na kutoa juhudi madhubuti, thabiti za kusukuma mbele kazi hii. **—Letter 58, 1910.** {EVsw 37:4}

Kuona Mahitaji Kama Mungu Anavyoyaona

Bwana anatamani tuutangaze kwa nguvu ujumbe wa malaika wa tatu katika miji hii mikubwa…... Tunapofanya kazi kwa nguvu zote ambazo **Mungu** anatupa, na kwa unyenyekevu wa moyo, tukimweka **Mungu** kuwa tumaini letu kuu, kazi zetu hazitaenda bure. Juhudi zetu thabiti na zilizoamuliwa kuleta roho katika ufahamu wa Kweli kwa wakati huu zitaungwa mkono na malaika watakatifu, na roho nyingi zitaokolewa. Bwana hatachoka wala kuwatelekeza wajumbe Wake waaminifu. Yeye hutoa msaada wa mawakala wa kimbingu, na huambatana na kazi zao kwa nguvu ya Roho Mtakatifu ili kuwashawishi na kuwaongoa watu. Mbingu zote zitaidhinisha maombi yenu. {EVsw 38:1}

Ah, kama tungeweza kuona mahitaji ya miji hii mikubwa kama **Mungu** anavyoyaona! Lazima tupange kuweka katika miji hii watu wenye uwezo, ambao wataweza kuwasilisha ujumbe wa malaika wa tatu kwa njia yenye nguvu kubwa, itakayogusa mioyo kwa undani. Watu wanaoweza kufanya kazi hii, hawawezi kukusanywa mahali pamoja kwa ajili ya kazi ambayo wengine wanaweza kuifanya... **Manuscript 53, 1909.**{EVsw 38:2}

Hali na Changamoto Maalum katika kufanya Uinjilisti Mijini

Kumbi Kubwa na Bora — Imekuwa tatizo gumu kufahamu jinsi ya kuwafikia watu katika miji mikubwa yenye watu wengi. Haturuhusiwi kuingia katika makanisa. Katika miji, kumbi kubwa ni ghali, na kwa kawaida watu wachache ndio hujitokeza katika kumbi bora. Tumekuwa tukisemwa vibaya na wale ambao hawakutujua vyema. Sababu za imani yetu hazieleweki kwa watu, na tumekuwa tukionekana kama wenye misimamo mikali, tuliopitiliza, wale watunzao Jumamosi kwa ujinga, yaani kutojua, badala ya Jumapili. Katika kazi yetu, tumefadhaishwa na jinsi ya kupata ufumbuzi wa changamoto ya kuta na vikwazo vya udunia na chuki, na namna ya kuleta mbele ya watu Ukweli wa thamani ambao unamaanisha mengi kwao. —**Testimonies for the Church 6:31, 32 (1900).**{EVsw 38:3}

Uhalisia wa changamoto ya Kupata Ukumbi wa Mikutano na Ufumbuzi wa Kivitendo

Magumu yaliyotajwa ndio yale tunayopaswa kuyakabili karibu kila mahali, lakini si kwa namna iliyo dhahiri kama ilivyo huko _____. Tunaamini kuwa Shetani ameweka kiti chake mahali hapo, ili kutekeleza kazi zake hapo na kupata kuwavunja moyo watenda kazi na kuwalazimisha waache kazi hiyo…..{EVsw 39:1}

Lazima tumwombe **Mungu** atupe hekima, kwa maana kwa imani naona kanisa imara likiimarishwa katika mji huo. Kazi yetu ni kukesha na kuomba, kutafuta ushauri kutoka kwa Yule ambaye ni **Mshauri** wa ajabu, Mwenye nguvu kuu. Yeye aliye na uwezo kuliko majeshi yote ya kuzimu anaweza kulinyang'anya taifa Lake kutoka mikononi mwa Shetani, na chini ya uongozi Wake, malaika wa mbinguni wataendeleza vita dhidi ya majeshi yote ya giza, na kusimika bendera ya Kweli na haki katika mji huo…..{EVsw 39:2}

Ndugu zetu wamekuwa wakitafuta mahali pa kufanyia mikutano. Kumbi na majumba ya sinema yanawasilisha changamoto nyingi zisizofaa, hivyo tunaona ni vyema kutumia uwanja wa michezo ya kuteleza kwenye barafu (skating), ambao hivi karibuni umetumika kwa mikutano ya kidini na ya uhamasishaji wa kiasi (temperance)..... Tukipata mahali pa kutangaza Neno la uzima, hakika itagharimu fedha. Lakini Mungu atatengeneza njia ili **Ukweli** Wake uwafikie watu, kwa maana hivyo ndivyo Alivyojitwalia ushindi mara kwa mara. **—Letter 79, 1893.**{EVsw 39:3}

Kuwapata na kuwatunza Wainjilisti wa Mijini—

Sasa, wakati Bwana anapotuita tena kutangaza ujumbe kwa nguvu katika upande wa Mashariki, anapotutuma kuingia katika miji ya Mashariki, na ya Kusini, na ya Kaskazini, na ya Magharibi, je, hatutaitika kwa moyo mmoja kutekeleza agizo Lake? Je, hatutapanga kwa bidii kuwatuma wajumbe katika maeneo haya yote na kuwategemeza kwa ukarimu? Miji yetu yote inapaswa kufikiwa. Bwana Yu karibu kuja. Mwisho umekaribia; naam, unakaribia sana! Kwa muda mfupi tu kutoka sasa, hatutaweza kufanya kazi kwa uhuru tunaofurahia sasa. Matukio ya kutisha yanatukabili, na lolote tutendalo ni lazima tulifanye kwa haraka. Ni lazima tujenge kazi ya **Mungu** katika kila mahali tunapoweza sasa. Na ili kazi hii itekelezwe ipasavyo, tunahitaji sana msaada wa wahudumu wenye uzoefu, waliokomaa katika imani, ambao wanaweza kuvuta usikivu wa makutano makubwa. {EVsw 39:4}

Bwana anatamani tutangaze ujumbe wa malaika wa tatu kwa nguvu katika miji hii. Hatuna uwezo ndani yetu wenyewe wa kuonyesha nguvu hii. Tunachoweza kufanya ni kuchagua watu wenye uwezo, na kuwasihi waingie katika njia hizi za fursa, na huko watangaze ujumbe katika nguvu ya Roho Mtakatifu. Wanapoinena **Kweli**, na kuiishi **Kweli**, na kuomba kwa ajili ya **Kweli**, **Mungu** atagusa mioyo ya watu. — **Manuscript 53, 1909.** {EVsw 40:1}

Wainjilisti wa "Njia Kuu"—Uwezo wa Ndugu ----- kama mhubiri unahitajika sana katika kuwasilisha Kweli katika njia kuu. Wakati Kweli inapotangazwa katika njia kuu, vizuizi vya mipakani huko vitafunguliwa, injili itafika mpaka uchochoroni na kazi iliyopanuliwa itafanyika. —**Letter 168, 1909.**{EVsw 40:2}

Juhudi Zisizo za Kawaida Zahitajika — Katika miji ya leo, ambako kuna mambo mengi ya kuvutia na kufurahisha, watu hawawezi kuvutiwa kwa juhudi za kawaida. Wahudumu waliowekwa na **Mungu** watalazimika kutumia juhudi zisizo za kawaida ili kuwavuta makutano. Na wanapofaulu kuwakusanya watu kwa idadi kubwa, ni lazima wapeleke ujumbe wa namna ya kipekee, usio wa kawaida, ambao utawaamsha na kuwaonya. Ni lazima watumie kila njia iwezekanayo ili Ukweli uonekane wazi na kwa utambuzi wa wazi. Ujumbe wa majaribio kwa wakati huu ni lazima uwasilishwe kwa uwazi, kwa kuamuliwa na kwa msisitizo mkubwa kiasi cha kuwatikisa wasikilizaji na kuwapelekea kutamani kujifunza Maandiko. **—Testimonies For The Church 9:109 (1909).**{EVsw 40:3}

Upinzani, Gharama, na Watazamaji Wanaobadilika—

Niliota ndoto kuwa ndugu zetu kadhaa walikuwa katika baraza, wakitafakari mipango ya kazi kwa majira haya [1874]. Waliona kuwa ingekuwa vyema kutolenga miji mikubwa, bali waanzie kazi katika maeneo madogo, yaliyo mbali na miji; huko wangekutana na upinzani mdogo kutoka kwa makasisi, na pia wangeepuka gharama kubwa. Walieleza kuwa wachungaji wetu, kwa kuwa ni wachache kwa idadi, wasingeweza kutolewa ili kuwafundisha na kuwalea wale ambao wangekubali Kweli mijini, na ambao, kwa sababu ya upinzani mkubwa zaidi watakaokutana nao huko, wangehitaji msaada wa karibu zaidi kuliko makanisa ya vijijini. Hivyo, matunda ya kutoa mfululizo wa hotuba mijini yangepotea kwa kiwango kikubwa. Tena, walihimiza kuwa, kwa sababu ya ukosefu wa rasilimali za kutosha, na kwa sababu ya hali ya kubadilika-badilika kwa washiriki wa kanisa katika miji mikubwa, ingekuwa vigumu kujenga kanisa

litakalokuwa ngome imara kwa ajili ya kazi ya **Mungu**. Mume wangu alikuwa akiwahimiza ndugu kuandaa mipango mipana bila kuchelewa, na kuanzisha juhudi pana na ya kina katika miji mikubwa, ambayo ingelingana vyema zaidi na tabia ya ujumbe wetu. Mtendakazi mmoja alisimulia matukio ya uzoefu wake katika miji, akionyesha kuwa kazi huko ilikuwa mbioni kushindwa, lakini alitoa ushuhuda wa mafanikio bora katika maeneo madogo.{EVsw 41:1}

Mmoja mwenye heshima na mamlaka—Yule ambaye Yupo katika mikutano yetu yote ya baraza—alikuwa akisikiliza kwa makini kila neno. Alizungumza kwa utulivu na kwa uhakikisho kamili:{EVsw 41:2}

"Ulimwengu wote," Alisema, "ni shamba kuu la mizabibu la **Mungu**. Miji na vijiji ni sehemu ya shamba hilo. Hivi viunga vyote ni lazima vifanyiwe kazi."—**Testimonies For The Church 7:34, 35 (1902).** {EVsw 42:1}

Kazi ya Gharama Kubwa — Yaonekana kana kwamba ni vigumu sana kwa mtu yeyote kuthubutu kuwaomba watenda kazi waende mijini, kwa sababu ya gharama kubwa inayohitajika ili kuendesha kazi iliyo imara na yenye misingi thabiti. Ni kweli kwamba kiasi kikubwa cha fedha kitahitajika ili kutimiza wajibu wetu kwa wale ambao bado hawajaonywa katika maeneo haya; na **Mungu** anatamani kuinuliwa kwa sauti zetu pamoja na mvuto wetu kwa ajili ya kuhimiza matumizi ya busara ya mali katika jitihada hii maalum. —**Manuscript 45, 1910.**{EVsw 42:1}

Ushirikiano wa Moyo Wote Ni wa Lazima—Katika miji yetu mikubwa, juhudi ya dhati, na iliyoamuliwa inapaswa kufanyika ili kufanya kazi kwa umoja. Katika roho na kwa kumcha **Mungu**, watendakazi wanapaswa kuungana kama mtu mmoja, wakifanya kazi kwa nguvu na bidii ya kweli. Kusiwepo na juhudi za kuchochea hisia, wala mashindano. Bali na ionekane toba ya kweli, huruma ya dhati, ushirikiano wa moyo wote, na kushindana kwa nia njema katika juhudi kuu na ya bidii ya kujifunza masomo ya kujinyima, kujikana nafsi na kujitoa mhanga kwa ajili ya kuwaokoa watu wanaoangamia kutoka mautini. **—Manuscript 128, 1901.** {EVsw 42:2}

Tumshukuru Bwana kwamba wapo wachache wanaojitahidi kwa kila njia kuinua alama za kumbukumbu kwa ajili ya **Mungu** katika miji yetu iliyopuuzwa. Tuwe na kumbukumbu daima kuwa ni wajibu wetu kuwatia moyo watenda kazi hawa. **Mungu** hafurahishwi na ukosefu wa kuthaminiwa na msaada unaoonyeshwa kwa watendakazi wetu waaminifu katika miji mikuu. —**Manuscript 154, 1902.** {EVsw 42:3}

Kushikilia Kazi Hadi Hitimisho Lililokomaa — Katika juhudi zinazofanywa katika miji mikubwa, nusu ya kazi hupotea kwa sababu watenda kazi hufunga kazi mapema mno na kuhamia eneo jipya. Paulo alifanya kazi kwa muda mrefu katika maeneo aliyohudumu, akiendelea na kazi yake kwa mwaka mzima mahali pamoja, na mwaka mmoja na nusu mahali pengine. Haraka ya kufunga mkutano wa 'efoti' au uinjilisti wa hadhara, mara nyingi imesababisha hasara kubwa. **—Letter 48, 1886.** {EVsw 42:4}

"Ahadi ya Mavuno Tele"

Tukio Lenye Kushangaza—Katika maono ya usiku, niliona tukio la kushangaza sana likitokea mbele yangu. Niliona mduara mkubwa wa moto ukidondoka katikati ya nyumba nzuri sana, na kusababisha uharibifu wake wa papo hapo. Nilisikia mtu akisema, "Tulijua hukumu za **Mungu** zinakuja duniani, lakini hatukujua zitakuja haraka hivi." Wengine, kwa sauti za maumivu, walijibu, "Hivi ninyi mlijua! Basi kwa nini hamkutufahamisha? Sisi hatukujua." Kila upande nilisikia maneno kama hayo ya lawama yakisemwa. {EVsw 43:1}

Niliamka nikiwa na huzuni kuu. Nikalala tena, na nikaona kuwa nipo kwenye mkutano mkubwa. Mmoja mwenye mamlaka alikuwa akizungumza mbele ya watu, mbele yake kulikuwa na ramani ya dunia iliyoenea. Alisema ramani hiyo ilikuwa picha ya shamba la **Mungu** ambalo lilihitaji kulimwa. Wakati nuru kutoka mbinguni inapoangaza mtu mmoja, mtu huyo alitakiwa kuakisi nuru hiyo kwa wanadamu wengine. Nuru ilipaswa kuwashwa (kuangazwa) sehemu nyingi, na kutoka katika sehemu hizo mianga mingine ilipaswa kuwashwa…….{EVsw 43:2}

Niliona miale ya mwanga ikitoka mijini na vijijini, kutoka sehemu za juu na sehemu za chini za dunia. Neno la **Mungu** lilikuwa likipewa utii (kuheshimiwa), na matokeo yake, kulikuwa na kumbukumbu Zake katika kila mji na kijiji. Ukweli Wake ulitangazwa kote duniani. **—Testimonies For The Church 9:28, 29 (1909).**{EVsw 43:3}

Maonyo Makini na Mazito Huamsha/Huchochea Maelfu

Watu wa imani na maombi watalazimika kusonga mbele na shauku takatifu, wakitangaza Maneno ambayo **Mungu** atawapa. Dhambi za Babeli zitafunuliwa waziwazi. Matokeo ya kutisha ya kutekeleza mamlaka ya serikali kwa kanisa, kujipenyeza kwa umizimu, maendeleo ya siri lakini ya haraka ya mamlaka ya Kipapa—yote yatafichuliwa. Kwa maonyo haya makini na mazito, watu watachochewa. Maelfu na maelfu watasikiliza, wale ambao kamwe hawajawahi kusikia maneno kama haya. Kwa mshangao wanasikia ushuhuda kwamba Babeli ni kanisa, lililoanguka kwa makosa na dhambi zake, kwa sababu ya kukataa **Ukweli** uliotumwa kutoka mbinguni**. —The Great Controversy, 606, 607 (1888).**{EVsw 43:4}

Wengi Watakuja kwenye Nuru—Kupitia neema ya Kristo, watumishi wa **Mungu** wanatumwa kuwa wajumbe wa nuru na baraka. Kwa maombi ya dhati na bidii na uvumilivu wanapata kipawa cha Roho Mtakatifu, na kusonga mbele wakiwa na jukumu zito la kuokoa nafsi, mioyo yao ikiwa imejazwa na ari ya kueneza ushindi wa msalaba, wataona matunda ya jitihada zao. Wakikataa kwa dhati kuonyesha hekima za kibinadamu au kujitukuza wenyewe, watatimiza kazi ambayo itaweza kuhimili mashambulizi ya Shetani. Roho nyingi zitageuzwa kutoka kwenye giza kwenda kwenye nuru, na makanisa mengi yataanzishwa. Watu wataongolewa, si kwa uwezo wa kibinadamu, bali kwa **Kristo**. **—The Acts of the Apostles, 278 (1911).**{EVsw 44:1}

SEHEMU YA 3 — JAMII NDOGO NA MAENEO YA VIJIJINI

Njia Kuu na Njia Ndogo

Nafasi Zilizopotea—Katika mipango yetu ya kueneza kazi hii, si miji peke yake tu inapaswa kuzingatiwa, bali pia sehemu mbali mbali zisizo za kawaida. Katika maeneo haya yaliyopotea, kuna familia nyingi sana zinazohitaji kuangaliwa, ili tujue kama wanaelewa kazi ambayo Yesu anafanya kwa ajili ya watu Wake.{EVsw 45:1}

Wale walioko katika barabara kuu hawapaswi kupuuzwa; wala wale walioko katika maeneo ya nje ya miji na mashambani. Tunaposafiri kutoka mahali hadi mahali tukipita nyumba baada ya nyumba, tunapaswa mara kwa mara kujiuliza, “Je, watu wanaoishi katika maeneo haya wamesikia ujumbe? Je, **Ukweli** wa **Neno** la **Mungu** umewafikia masikioni mwao? Je, wanaelewa kuwa mwisho wa kila kitu uko karibu, na hukumu za **Mungu** zinakaribia kutimia? Je, wanaelewa kuwa kila roho imenunuliwa kwa bei isiyo na kikomo?” Ninapotafakari nafsini mwangu kuhusu mambo haya, moyo wangu hujaa hamu ya kina kuona Ukweli ukisambazwa kwa njia rahisi kabisa hadi katika nyumba za watu hawa walioko kando ya barabara na maeneo yaliyo mbali na vituo vikuu vya watu wengi....{EVsw 45:2}

Ni fursa yetu kuwatembelea na kuwafahamisha juu ya upendo wa **Mungu** kwao na juu ya mpango Wake wa ajabu wa wokovu wa roho zao.{EVsw 45:3}

Katika kazi hii kwa barabara kuu na maeneo ya miti, kuna changamoto kubwa zinazotakiwa kukabiliana nazo na kuzitatua. Mtendakazi, anapotafuta roho, hapaswi kuogopa wala kukata tamaa, kwa maana **Mungu** ni msaidizi wake, na Ataendelea kuwa msaidizi wake; Naye Atafungua njia mbele ya watumishi Wake. —**Manuscript 15, 1909.**{EVsw 45:4}

Wito wa Mipango Mikubwa Zaidi — Tumekuwa wa mawazo finyu mno katika mipango yetu. Tunahitaji kuwa na fikira pana zaidi. **Mungu** anatamani tuendeleze katika kazi yetu kwa ajili Yake kanuni za Kweli na haki. Kazi Yake yapaswa kuendelea mbele katika miji mikuu, miji midogo na vijiji vyote…...{EVsw 46:1}

Lazima tuondokane na fikra zetu finyu na kuweka mipango mikubwa zaidi. Ni lazima kuwe na uoni mpana zaidi wa kuwafikia wale walio karibu na wale walio mbali. —**Manuscript 87, 1907.**{EVsw 46:2}

Maeneo Yasiyoonekana Kuwa na Matumaini

Eneo la kazi linapaswa kupanuliwa. Ujumbe wa Injili ni lazima ufike katika kila kona ya dunia. Hata maeneo yanayoonekana kuwa hayana tumaini kabisa yanapaswa kupokea kazi ya dhati bidii, iliyojdhamiriwa na kujitoa kwa kweli. Wana wa **Mungu**, waaminifu, wa kweli, wasio na ubinafsi, ni lazima watumie maarifa yote waliyo nayo katika kusimamia kazi hii ya muhimu sana. —**Manuscript 141, 1899.**{EVsw 46:3}

Watu wa Vijijini Hufikiwa kwa Urahisi Zaidi — Watu wanaoishi katika maeneo ya vijijini mara nyingi wanaweza kufikiwa kwa urahisi zaidi kuliko wale wanaoishi mijini kwenye makazi yaliyojaa msongamano mkubwa wa watu. Hapa, katikati ya mandhari ya asili, tabia ya Kikristo hujengeka kwa urahisi zaidi kuliko ilivyo katika maisha yaliyojaa uovu ya mijini. **Ukweli** unapogusa watu wenye mioyo sahili, na Roho wa **Mungu** akifanya kazi juu ya akili zao, akiwaongoza kuitikia tangazo la Neno la **Mungu**, kutakuwa na baadhi yao watakaoinuliwa ili kusaidia kazi ya **Mungu**, kwa mali zao na kwa kazi zao pia. **—Manuscript 65, 1908.**{EVsw 46:4}

Kwa Watu wa Tabaka Zote

Wanaume kwa wanawake walioko njiani na vichochoroni wafikiwe. Tunasoma kuhusu kazi za Kristo: "Yesu alikuwa akizunguka katika miji yote na vijiji, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri Injili ya Ufalme, na kuponya kila ugonjwa na kila maradhi miongoni mwa watu." Kazi ya namna hii hasa ndiyo yapaswa kufanywa katika miji yetu na vijijini, katika njia kuu na vichochoroni. Injili ya ujumbe wa malaika wa tatu lazima ifikishwe kwa watu wa tabaka zote. **—Manuscript 7, 1908.**{EVsw 46:5}

Kutoa Wito Katika Maeneo Mapya —

Kazi ya Mwokozi wetu ilikuwa ni kuonya miji, na kuweka wakazi waende kutoka mijini kwenda maeneo ambayo nuru haijawahi kutolewa hapo kabla, na kuinua bendera ya Kweli katika maeneo mapya……. Nuru niliyopewa ni kwamba hatupaswi kuwa na wasiwasi sana wa kukusanya mambo mengi sana katika eneo moja tu, bali tunapaswa kutafuta maeneo ya pembezoni, yasiyojulikana sana, na kufanya kazi huko, katika maeneo mapya. Kwa njia hii, watu wanaoweza kufikiwa na kuongolewa, watu wasiojua chochote kuhusu Kweli za thamani na za kujaribu za wakati huu, wanaweza kuokolewa. Wito wa mwisho unapaswa kutolewa kwa uzito uleule katika maeneo mapya humu nchini kama ulivyo katika nchi za mbali. Neno hili lilisemwa kuhusu maeneo ambayo ujumbe haujawahi kufikishwa huko. Mbegu za Kweli zinapaswa kupandwa katika vituo visivyolimwa au visivyofanyiwa kazi……. Kufanya kazi katika maeneo mapya kutakuza roho ya kimishenari. Ubinafsi wa kutaka watu wengi wabaki pamoja si mpango wa Bwana. Ingieni kila mahali penye uwezo wa kuingilika, na anzeni kazi ya kufundisha katika maeneo ambayo hawajasikia Kweli.{EVsw 47:1}

Kwa nini Mwokozi wetu alijitaabisha kupanda mbegu katika maeneo ya pembezoni? Kwa nini alisafiri polepole, akitoka katika vijijini ambavyo vilikuwa ni vituo Vyake vya kutoa nuru kwa kufungua Maandiko? Ni kwa sababu dunia nzima ilikuwa inahitaji kusikia, na baadhi ya roho zingekubali Kweli ambazo bado hawajawahi kuzisikia. Kristo alisafiri kwa utulivu na akafungua Maandiko kwa unyofu, kwa akili zilizokuwa tayari kupokea Kweli. **—Letter 318, 1908.**{EVsw 47:2}

Juhudi Efoti za Mkupuo au kwa Wakati Mmoja katika Miji Midogo—

Wakati wa kipindi ambacho mikutano ya makambi inaweza kufanyika katika konferensi hii, mikutano miwili au mitatu inapaswa kuendelea kwa wakati mmoja katika maeneo tofauti. Kuna kipindi ambapo mikutano hii haiwezi kufanyika; lakini katika miezi ile ambayo tunaweza kutumia makambi kwa manufaa, hatupaswi kuelekeza juhudi zetu katika miji mikubwa tu. Lazima tuwapelekee watu ujumbe wa onyo mahali pote. **—Manuscript 104, 1902.**{EVsw 47:3}

Watendakazi wa Vijijini

[Kumbuka.—Ingawa utambuzi kamili unatolewa kwa msaada muhimu wa walei katika shughuli zote za uinjilisti (tazama uk. 110-115), ni wazi kwamba wakazi wa maeneo ya vijijini watasikia ujumbe wa onyo tu pale watendakazi walioajiriwa katika kazi ya injili na walei wanapoungana katika kutangaza injili. Hivyo kitabu hiki kimetolewa kama ushauri tu kwa mtendakazi anayefanya uinjilisti, na katika kuwasilisha picha ya uinjilisti katika maeneo ya vijijini, kauli zilizotolewa hapa zinaonekana zikiwaita walei kufanya kazi katika maeneo yasiyo na watu wengi sana.—Wakusanyaji wa Nukuu.]

Watendakazi Wanaoanza Kazi kwa Mara ya Kwanza- Kuyafikia Maeneo Mapya-Tunakaribia mwisho wa historia ya dunia hii. Tunayo kazi kubwa mbele yetu, kazi ya kufunga kutoa ujumbe wa mwisho wa onyo kwa ulimwengu wenye dhambi. Kuna watu ambao watachukuliwa kutoka katika kilimo, kutoka katika shamba la mizabibu, kutoka katika matawi mengine ya kazi, na kutumwa na Bwana kutoa ujumbe huu kwa ulimwengu.{EVsw 48:1}

Ulimwengu hauko katika umoja. Tunapotazama picha, mwonekano wa nje unaonekana wa kukatisha tamaa. Lakini Kristo anawakaribisha kwa kuwatambua kwa tumaini lenye uhakikisho, wanaume na wanawake wote wanaosababisha tukate tamaa. Yeye anaona ndani yao sifa ambazo zitawawezesha kuchukua nafasi katika shamba Lake la mizabibu. Ikiwa watakuwa wanafunzi wanaoendelea kujifunza, kupitia uongozi Wake, Yeye atawafanya kuwa wanaume na wanawake wanaofaa kufanya kazi ambayo haiko nje ya uwezo wao; kupitia mwangaza wa Roho Mtakatifu, atawapa nguvu ya kutamka-nguvu ya usemi au kuhubiri.{EVsw 48:2}

Sehemu nyingi kame, ambazo hazijafanyiwa kazi lazima zifanyiwe kazi na watu wapya ambao hawajazoea kazi. Mwangaza wa mtazamo wa Mwokozi juu ya ulimwengu utachochea ujasiri kwa watendakazi wengi, ambao, ikiwa wataanza kwa unyenyekevu, na kuweka mioyo yao katika kazi hiyo, watakuwa watu sahihi kwa wakati na mahali sahihi. Kristo anaona taabu zote na kukata tamaa kwa ulimwengu, hali ambayo inaweza kuwalemea watendakazi wetu wenye uwezo mkubwa na uzito wa kukatisha tamaa kukubwa sana hata wasijue jinsi ya kuanza kazi ya kuongoza wanaume na wanawake katika mzunguko wa kwanza wa ngazi. Njia zao sahihi zina thamani ndogo. Wangeweza kusimama juu ya mzunguko wa chini wa ngazi, wakisema: "Njooni mahali tulipo." Lakini roho maskini hazijui wapi pa kuweka miguu yao.{EVsw 48:3}

Moyo wa Kristo unafurahishwa kwa kuwaona wale ambao ni masikini katika kila hali; huwatia moyo kwa mtazamo Wake wa wale wanaotendewa vibaya walio wapole; hutia moyo na wale wanaoonekana kuwa na njaa kwa ajili ya haki na kwa wengi kushindwa kuanza. Huwakaribisha, kama ilivyokuwa, hali halisi ya mambo ambayo yangeweza kuwavunja moyo wachungaji wengi. Yeye husahihisha uchaji Mungu wetu ulio na makosa, akiwapa mzigo wa kazi kwa ajili ya masikini na wahitaji katika maeneo magumu kwa wanaume na wanawake walio na mioyo inayoweza kuhisi kwa ajili ya wajinga na kwa ajili ya wale walio nje ya njia. Bwana anawafundisha watendakazi hawa jinsi ya kukutana na wale anaowataka wasaidiwe. Watatiwa moyo waonapo milango inafunguliwa kwa ajili ya wao kuingia mahali ambapo wanaweza kufanya kazi ya umishenari wa tiba/kitabibu. Wanampa **Mungu** utukufu wote kwa kutojitumainia nafsi zao……. {EVsw 49:1}

{Mikono yao inaweza kuwa inakwaruza na isiyo na ujuzi, lakini mioyo yao ni miepesi kuona huruma; wamejazwa na hamu ya dhati ya kufanya kitu ili kupunguza huzuni nyingi sana; na Kristo Yupo kwa ajili ya kuwasaidia. Yeye hufanya kazi kupitia wale wanaotambua rehema katika taabu, inayopatikana kwenye upotevu wa vitu vyote. Wakati Nuru ya ulimwengu inapopita, fadhili huonekana katika magumu yote, utaratibu katika machafuko, mafanikio na hekima ya **Mungu** katika yale ambayo huonekana kutowezekana. Ndugu na dada zangu, katika huduma yenu muwakaribie watu. Wainueni wale waliotupwa chini. Chukulia misiba kama baraka zilizojificha, na taabu kama rehema. Fanya kazi kwa namna ambayo italeta matumaini mahali pa kukata tamaa. }

Watu wa kawaida wanapaswa kuchukua nafasi zao kama watendakazi. Kwa kushiriki huzuni za wanadamu wenzao kama Mwokozi alivyoshiriki huzuni za wanadamu, kwa imani watamuona Mwokozi akifanya kazi nao. **—Testimonies For The Church 7:270-272 (1902).**{EVsw 49:2}

Vijana Wanaojitoa Kwa Ajili ya Maeneo Magumu — Vijana wa kiume na wa kike wanaojitoa kwa kazi ya kufundisha ile Kweli na kutafuta kuongoa roho kwa ajili ya Kristo, hawana budi kwanza kufanywa hai na Roho Mtakatifu; kisha na waende nje ya kambi, waingie katika maeneo yaliyoonekana kuwa yasiyo na matumaini. Bwana hajawapa wale wasio na uzoefu wa kutosha kazi ya kuyahubiria makanisa. Ujumbe unapaswa kutangazwa katika barabara kuu na kwenye njia za vichochoroni. —**Manuscript 3, 1901.** {EVsw 49:3}

Wanaume na Wanawake Walioko Ndani ya Ndoa Katika Maeneo Yaliyopuuzwa

Wanaume na wanawake walio katika ndoa na wanaojua **Kweli**, na waende katika maeneo yaliyopuuzwa ili kuwapatia wengine nuru. Na wafuate mfano wa wale waliotangulia kufanya kazi ya utangulizi katika maeneo mapya (pioneer work). Na wafanye kazi kwa hekima katika maeneo ambayo wanaweza kuhudumu kwa ufanisi zaidi. Na wajifunze kanuni za matengenezo ya afya, ili waweze kuwafundisha wengine. Kwa kusoma na kutafakari vitabu na majarida mbalimbali yahusuyo afya, na wajifunze namna ya kuwahudumia wagonjwa, ili kwa njia hiyo waweze kufanya kazi bora zaidi kwa ajili ya Bwana. —**Letter 136, 1902.**{EVsw 50:1}

Ujumbe Kupelekwa na Wale Walio Kwenye Miji Mikuu — Wale watu wetu wanaoishi katika miji mikuu wangepata uzoefu na wa kipekee, iwapo, wakiwa na Biblia mikononi mwao, na mioyo yao ikiwa wazi kupokea mvuto wa Roho Mtakatifu, wangeenda katika njia kuu na ng'ambo ya dunia hii, wakiwasilisha ujumbe walioupokea. **— Review and Herald, Agosti 2, 1906.**{EVsw 50:2}

Milimani na Mabondeni — Wakati nilipokuwa Lakeport [Kaskazini mwa California], niliguswa sana moyoni na ukweli kwamba hapa ni mahali ambapo kazi ya uaminifu inapaswa kufanyika ya kuwapelekea watu ujumbe wa Kweli. Katika eneo hili la milima kuna roho nyingi zinazohitaji Kweli za ujumbe wa malaika wa tatu. Chini ya ushawishi wa Roho Mtakatifu tunapaswa kuutangaza Ukweli wa wakati huu miongoni mwa makazi haya yaliyoko milimani na mabondeni. Maonyo yake adhimu yanapaswa kurudiwa na kurudiwa tena kama mwangwi. Na ujumbe huu lazima uwafikie watu haraka; lazima utolewe mstari juu ya mstari, amri juu ya amri, hapa kidogo na pale kidogo. Bila kuchelewa, wanaume na wanawake wenye hekima na akili wanapaswa kujitosa katika kazi ya kupanda mbegu ya Injili…….**{EVsw 50:3}**

Bwana atafanya kazi kupitia wale watakaowafungulia watu Maandiko, hasa wale waliotengeneza maskani yao katika maeneo haya ya faragha ya mashambani. Nawaomba ndugu zangu waungane katika kufanya kazi hii njema, na kuiendeleza hadi itakapokamilika…….**{EVsw 51:1}**

Sababu ya kuwasihi kuelekeza usikivu wenu Lakeport na makazi yanayouzunguka ni kwamba maeneo haya bado hayajapokea mtazamo sahihi kuhusu **Kweli** wa wakati huu. Huenda miongoni mwa watu wetu wapo ambao watakubali kutumia mali zao kwa ajili ya kufungua maeneo ya umishenari. Kwa watu kama hao ningesema, kwa ajili ya Bwana, fanyeni kila muwezalo ili kusaidia. Bado hatujachunguza kikamilifu ukubwa wa eneo la kazi lililopo hapa, lakini Lakeport ni miongoni mwa maeneo yaliyoonyeshwa kwangu kuwa yanahitaji uangalizi wetu.**{EVsw 51:2}**

Nina mengi ya kusema kuhusu makazi haya ya milimani. Haya ni kama makazi yaliyo karibu na Washington, ambapo kazi kama hiyo inapaswa kufanyika. Je, watu wetu hawatakuwa waaminifu zaidi katika kufanya kazi njia kuu na pembezoni? Shughuli za kibiashara zimewavutia sana na kuwateka uwezo na nia ya Waadventista wa **Sabato** wengi kiasi kwamba wengi wao hawana stahiki kabisa kufanya kazi ya kuwaletea nuru ya Kweli ya sasa wale wasioijua. Hatupaswi kuridhika na kuruhusu hali kama hiyo kuendelea.**{EVsw 51:3}**

Kuna wengi miongoni mwa watu wetu ambao, kama wangeondoka mijini na kuanza kufanya kazi katika sehemu hizi na pia pembezoni, wangerudisha afya zao za kimwili. Nawasihi ndugu zetu waende kama wamishenari, wawili kwa wawili, katika maeneo haya ya mashambani. Nendeni kwa unyenyekevu. Kristo ametupa mfano, na hakika Bwana atabariki juhudi za wale watakaotoka kwa kumcha **Mungu**, wakibeba ujumbe ambao Mwokozi aliwapa wanafunzi wa kwanza, “Ufalme wa **Mungu** umekaribia.”— **Manuscript 65, 1908.****{EVsw 51:4}**

Familia za Kimishenari kwa Ajili ya Miji na Vijiji — Ndugu wanaotamani kubadilisha makazi yao, ambao wana lengo la kulitukuza Jina la **Mungu**, na wanahisi kuwa wana wajibu binafsi wa kuwafanyia mema wengine, kuwasaidia wanadamu na kuokoa roho ambazo Kristo hakusita kutoa maisha Yake ya thamani kwa ajili yao, wanapaswa kuhamia kwenye miji na vijiji ambako kuna nuru ndogo au hakuna kabisa, ili waweze kuwa msaada wa kweli na baraka kwa katika huduma kwa wengine kupitia kazi yao na uzoefu wao. Wamishenari wanahitajika kwenda kwenye miji na vijiji, na kuinua kiwango cha Kweli, ili **Mungu** awe na mashahidi Wake waliotawanyika kote nchini, ili nuru ya Kweli iweze kupenya katika maeneo ambayo haijafika bado, na kiwango cha Kweli kikiinuliwa mahali ambako hakijulikani bado....**{EVsw 52:1}**

Yesu hakuvipuuzia vijiji. Maandiko yanasema kwamba “Alizunguka kila mji na kijiji, akihubiri na kutangaza habari njema za Ufalme wa **Mungu**” .....**{EVsw 52:2}**

Sasa je, si ni wajibu wa baadhi ya wale wanaosimama bila kazi hapa (Battle Creek), kwenda mahali ambapo wanaweza kumwakilisha Kristo na Kweli Yake ya thamani? **{EVsw 52:3}**

— The General Conference Daily Bulletin, Machi 20, 1891.

SEHEMU YA 4—MIPANGO YA KAMPENI ZA HADHARA (Efoti nk)

"Kufuata Mfano wa Mwinjilisti Mkuu"

Jifunze Mbinu za Kristo — Ikiwa kuna wakati wowote ambapo imekuwa muhimu sana kuelewa na kufuata mbinu sahihi za kufundisha na kuiga mfano wa Kristo, basi ni sasa. — **Letter 322, 1908.****{EVsw 53:1}**

Jinsi Alivyowafikia Watu

Ikiwa unataka kufikia watu kwa njia inayokubalika, nyenyekeza moyo wako mbele za **Mungu**, na ujifunze njia Zake. Tutanufaika sana katika kazi yetu kwa kujifunza mbinu za Kristo za kuhubiri na namna Alivyowakabili watu. Katika simulizi la Injili tunapata kumbukumbu/rekodi ya jinsi Alivyowafanyia kazi watu wa kila tabaka, na jinsi Alivyohubiri mijini na vijijini, maelfu walivutwa Kwake ili kusikia mafundisho Yake. Maneno ya Mwalimu yalikuwa wazi na dhahiri, na yalitamkwa kwa huruma nyororo na upole. Yalileta Uhakikisho kuwa hapo palikuwa na **Kweli**. Unyenyekevu, udhati na bidii ya Kristo katika kuhubiri ndizo zilizovutia umati wa watu. {EVsw 53:2}

Mwalimu Mkuu aliweka mipango ya kazi Yake. Jifunze mipango hiyo. Tunamwona akisafiri kutoka mahali hadi mahali, akifuatwa na umati wa wasikilizaji wenye shauku. Alipoweza, aliwapeleka mbali na miji yenye misongamano, akawapeleka katika utulivu wa mashambani. Huko alisali pamoja nao, na kuzungumza nao kuhusu Kweli za milele. **— Review and Herald, Januari 18, 1912.**{EVsw 53:3}

Katika Masinagogi—Kando ya Bahari

Kristo “alizunguka Galilaya yote, akifundisha katika masinagogi yao, akihubiri Injili ya Ufalme na kuponya kila namna ya maradhi.” Alihubiri katika masinagogi kwa kuwa alitaka kuwafikia wengi waliokusanyika huko. Kisha alitoka nje na kufundisha kando ya bahari na katika njia kuu za wasafiri. Hazina za Kweli Alizokuwa nazo hazikupaswa kufungwa ndani ya masinagogi tu…….{EVsw 54:1}

Kristo angeweza kushika nafasi ya juu kabisa miongoni mwa walimu wa taifa la Kiyahudi. Lakini alichagua kupeleka Injili kwa maskini. Alizunguka huku na huko, ili wale waliokuwa katika njia kuu na pembezoni wapate kusikia maneno ya Injili ya kweli. Alifanya kazi kwa njia ileile anayotaka watumishi Wake wafanye leo. Kando ya bahari, milimani, mitaani katika miji, sauti Yake ilisikika ikifafanua Maandiko ya Agano la Kale. Mafundisho Yake yalikuwa tofauti sana na ya waandishi na mafarisayo kiasi kwamba umakini wa watu ulivutwa. Alifundisha kama mtu mwenye mamlaka, na si kama waandishi. Kwa uwazi na nguvu Alitangaza ujumbe wa Injili. **— Letter 129, 1903.**{EVsw 54:2}

Mbinu Zake za Kipekee

Alihudhuria sikukuu kubwa za kila mwaka za taifa, na kwa umati uliokuwa umejawa na taratibu za kidini za nje, Aliwaelekeza kwenye mambo ya mbinguni, Akileta wazo la umilele mbele ya macho yao. Aliwaletea wote hazina kutoka ghala la hekima. Aliwaambia mambo kwa lugha rahisi sana kiasi kwamba wasingeweza kushindwa kuyaelewa. Kwa mbinu Zake za kipekee, Aliwasaidia wote waliokuwa katika huzuni na mateso. Kwa neema ya huruma nyororo na uungwana/kujali, Aliwahudumia wale walioumizwa na dhambi, Akileta uponyaji na nguvu.{EVsw 54:3}

Yeye akiwa Mkuu wa walimu, alitafuta kuwafikia watu kupitia njia ya mahusiano yao ya kawaida. Aliwasilisha Kweli kwa namna ambayo daima ingeunganisha kumbukumbu zao tukufu na huruma zao. Alifundisha kwa njia iliyowafanya watu wahisi kwamba inahusiana kabisa na mambo ya maisha yao na furaha yao. Mafundisho na Maagizo Yake yalikuwa ya moja kwa moja, vielelezo Vyake vilikuwa vya kufaa, maneno Yake yalijaa huruma na furaha, kiasi kwamba wasikilizaji Wake walivutiwa, na kuchangamka sana. Usahili, udhati na bidii aliyotumia kuwasiliana na wenye mahitaji vilitakasa kila Neno Alilolisema. **— The Ministry of Healing, uk. 22-24 (1905).**{EVsw 55:1}

Yesu Alisoma Nyuso

Hata ule umati uliokuwa ukimfuata kwa wingi haukuwa Kwake kama kundi la wanadamu asiowaelewa binafsi,- alitumia hekima ya kushugulika nao kiupekee/binafsi. Alizungumza moja kwa moja na kila akili na kugusa kila moyo. Aliziangalia nyuso za wasikilizaji Wake, akitambua kung'aa kwa uso wao, na mwanga wa macho uliothibitisha kuwa Kweli imeingia moyoni; na katika moyo Wake kulivuma furaha ya huruma inayojibu. — **Education, uk. 231 (1903).**{EVsw 55:1}

Mwito kwa Binadamu Aliyeanguka

Katika kila mwanadamu, haijalishi ameanguka kwa kina cha chini kiasi gani, **Kristo** aliona mtoto/mwana wa **Mungu**, mtu ambaye angeweza kurejeshwa katika hadhi ya kuwa na uhusiano wa Kiungu. **— Education, uk. 79 (1903).**{EVsw 55:2}

Usahili, Uwazi, na Kurudia-rudia

Mafundisho ya **Kristo** yalikuwa rahisi kabisa. Alifundisha kama mtu mwenye mamlaka. Wayahudi walitarajia na walidai kuwa ujio wa kwanza wa Kristo ungetukia kwa utukufu wote ambao utaandamana na ujio Wake wa pili. Lakini Mwalimu Mkuu alihubiri Kweli kwa wanadamu wengi ambao hawakuweza kupata elimu katika shule za marabi, wala falsafa za Kigiriki. Yesu aliisema **Kweli** kwa namna ya moja kwa moja, akitoa nguvu ya kipekee na mvuto kwa kila tamko Lake. Kama Angepaza sauti kwa namna isiyo ya kawaida, kama ambavyo wahubiri wengi hufanya leo, vile vipengele vya hisia za huruma, kujali, huzuni na muziki wa sauti ya mwanadamu vingepotea, na nguvu ya Kweli ingeharibika…..{EVsw 55:4}

Katika mafundisho Yake, Kristo hakuleta mambo mengi kwa wakati mmoja, ili asiwachanganye. Alifafanua kila hoja kwa uwazi. Hakudharau kurudia Kweli za zamani na zilizozoeleka katika unabii, kama zingesaidia kufundisha mawazo aliyokusudia kupandikiza. **— Manuscript 25, 1890.**{EVsw 56:1}

Aliwavutia Wenye Akili Kubwa/Wasomi

Ijapokuwa zile Kweli kuu zilizotamkwa na Bwana wetu zilikuwa kwa lugha rahisi, zilivalishwa na uzuri wa namna ya pekee kiasi kwamba ziliwavutia hata wenye akili mahiri zaidi…..{EVsw 56.2}

Ili kuonyesha kwa usahihi upendo wa huruma na uangalizi wa Baba Yake, Yesu alitoa mfano wa mwana mpotevu. Ingawa watoto Wake hukosea na kuondoka kutoka Kwake, wakitubu na kurudi, Atawapokea kwa furaha sawa na ile ya baba wa duniani anayempokea mwana wake aliyepotea kwa muda mrefu, anaporudi kwa toba. **— Manuscript 132, 1902.**{EVsw 56.3}

Watoto Walielewa

Mbinu ya Kristo ya kuwasilisha Kweli haiwezi kuboreshwa……. Maneno ya uzima yaliwasilishwa kwa urahisi kiasi kwamba mtoto aliweza kuyaelewa. Wanaume, wanawake, na watoto waliguswa sana na namna Alivyofafanua Maandiko kiasi kwamba waliiga hata lafudhi ya sauti Yake, wakasisitiza maneno yao kwa namna aliyofanya Yeye, na kuiga ishara Zake. Vijana waliikumbatia roho Yake ya huduma, na wakatamani kuiga njia Zake zenye neema kwa kuwasaidia wale waliokuwa katika uhitaji. **— Counsels on Health, uk. 498-499 (1914).**{EVsw 56.4}

Aliirejesha Kweli Kwenye Msingi Wake Halisi

Katika mafundisho Yake, Kristo hakutoa mahubiri marefu kama wahubiri wa leo. Kazi Yake ilikuwa ni kujenga juu ya msingi wa ile Kweli. Alikusanya vito vya thamani vya Kweli ambavyo vilikuwa vimechukuliwa na adui na kuwekwa katika mfumo wa uongo, na kuvirejesha katika mfumo wa Kweli, ili wote waliopokea Neno waweze kutajirika na kuboreshwa kwa njia hiyo. **— Manuscript 104, 1898.**{EVsw 57.1}

Aliimarisha Ujumbe

Kristo siku zote alikuwa tayari kumjibu mtafutaji wa Kweli kwa unyenyekevu. Wanafunzi Wake walipomjia wakitaka ufafanuzi wa Maneno Aliyokuwa amesema kwa umati, Aliyarudia mafundisho Yake kwa furaha. — **Letter 164, 1902.**{EVsw 57.2}

Alivuta kwa Upendo

Kristo alivuta mioyo ya wasikilizaji Wake Kwake kwa kudhihirisha upendo Wake; kisha, taratibu, na hatua kwa hatua, kwa kadiri walivyoweza kuvumilia, Aliwafunulia kweli kuu za Ufalme wa **Mungu**. Sisi pia tunapaswa kujifunza kulinganisha kazi yetu na hali ya watu—kuwafikia wanadamu pale walipo. Ingawa madai ya sheria ya **Mungu** yanapaswa kuwasilishwa kwa dunia, hatupaswi kusahau kwamba upendo—upendo wa Kristo—ndio nguvu pekee ya kuihuisha mioyo na kuiongoza kwa utii. **— The Review and Herald, Novemba 25, 1890.**{EVsw 57.3}

Alizuia Baadhi ya Kweli

Mwalimu Mkuu alikuwa na ramani kamili ya **Kweli** mkononi Mwake, lakini Hakuwafunulia wanafunzi Wake yote. Aliwafunulia tu yale ambayo yalikuwa ya lazima kwa maendeleo yao katika njia ya kuelekea mbinguni. Kulikuwa na mambo mengi ambayo hekima Yake ilimfanya akae kimya.{EVsw 57.4}

Kama vile **Kristo** alivyoacha kufunua mambo mengi kwa wanafunzi Wake kwa sababu Alijua kuwa wasingeweza kuyaelewa wakati huo, vivyo hivyo leo hata leo Anaacha kufunua mengi kwetu kwa sababu ya upeo mdogo wa uelewa wetu.{EVsw 57.5}

— Manuscript 118, mwaka 1902.

Katika Mahojiano ya Kipekee

Kazi ya Kristo kwa sehemu kubwa ilijumuisha mahojiano ya ana kwa ana. Alithamini sana hadhira ya nafsi moja (one soul audience); na nafsi hiyo moja iliweza kuwapelekea maelfu wengine ujumbe ilioupokea. **— The Review and Herald, Mei 9, 1899.** {EVsw 58.1}

Katika Sherehe

Kristo alipokuwa akiitwa kwenye sherehe au karamu, Alikubali mwaliko huo ili atakapokuwa ameketi mezani, aweze kupanda mbegu za Kweli katika mioyo ya wale waliokuwepo. Alijua kuwa mbegu hizo zingemea na kuzaa matunda. Alijua kuwa baadhi ya wale waliokula pamoja Naye wangekuja baadaye kuitikia mwito Wake wa, "Nifuateni." Ni fursa yetu kusoma namna **Kristo** alivyofundisha alipokuwa akitembea kutoka sehemu moja hadi nyingine, kila mahali akipanda mbegu za Kweli. **— Manuscript 113, 1902.**{EVsw 58.2}

Mpango wa Kristo wa Kufuatilia Kazi

Kristo aliwatuma wanafunzi Wake wawili wawili [Tazama pia ukurasa wa 72-74, "Wawili kwa Wawili"], waende mahali ambapo Yeye Mwenyewe angekuja baadaye.{EVsw 58.3}

— Manuscript 19, mwaka 1910.

Je, Njia ya Kristo Ilikuwa Sahihi?

Mfalme wa Enzi wa mbinguni alitembea kwa miguu kutoka mahali hadi mahali, akifundisha nje, kando ya bahari, na katika milima. Kwa njia hii aliwavuta watu Kwake. Je, sisi ni wakuu zaidi kuliko Bwana wetu? Je, njia Yake ilikuwa njia sahihi? Je, tumekuwa tukifanya kazi kwa busara au kwa upuuzi katika kudumisha unyenyekevu na kumcha **Mungu**? Bado hatujajifunza somo letu kama inavyotakiwa. Kristo anasema, **Mathayo 11:29** *"Jitieni nira Yangu, mjifunze Kwangu; kwa kuwa Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu;*" —**Letter 140, 1898.** {EVsw 58.4}

Kuunda na Kurekebisha Katika Huduma ya Kristo

Kazi ya wanafunzi ilihitaji kuundwa/kufinyangwa na kurekebishwa kwa nidhamu ya upole, na kwa kuwafungulia wengine maarifa ya Neno walilolipokea wenyewe; na Kristo aliwapa maelekezo maalum kuhusu njia yao ya kutenda na kazi yao. Katika maisha Yake Mwenyewe, Aliwapa mfano wa kufuata kwa ukamilifu sheria ambazo Aliwawekea. Hawakupaswa kuingia katika mabishano au migogoro; hiyo siyo kazi yao. Walipaswa kuonyesha na kutetea Ukweli kupitia tabia zao binafsi, kwa maombi ya dhati na tafakari, wakionyesha uzoefu wa kweli katika UKristo halisi. Hii ingetofautiana kabisa na dini ya Mafarisayo na Masadukayo. Walipaswa kuangazia wasikilizaji wao Ukweli mkubwa ambao bado ungefunuliwa. Walipaswa kurusha mshale, na Roho wa **Mungu** angeongoza mshale huo hadi moyoni. **—The Review and Herald, February 1, 1898.**{EVsw 58.5}

Kupanga Kueneza Habari za Injili kwa Upana

Wakati wa Kazi Yenye Nguvu — Kwa watu wote, mataifa, makabila na lugha zote, Ukweli unapaswa kutangazwa. Wakati umefika wa kufanya kazi zaidi yenye nguvu katika miji, na katika maeneo yote yaliyopuuzwa na ambayo hayajafanyiwa kazi. —**The Review and Herald, June 23, 1904.** {EVsw 59.1}

Mipango ya Busara — Kazi ya bidii inahitajika sasa katika wakati huu wa dharura, juhudi za sehemu tu hazitafaulu. Katika kazi zetu zote za mijini, tunapaswa kutafuta roho. Mipango ya busara inapaswa kutengenezwa ili kazi hiyo ifanyike kwa faida kubwa zaidi. —**The Review and Herald, Septemba 27, 1906.**{EVsw 59.2}

Kutweka Mpaka Kilindini — Kuna watu wanaodhani ni wajibu wao kuhubiri **Ukweli**, lakini hawataki kuondoka kando ya ufukwe, na hivyo hawapati samaki. Wanapendelea kuzunguka makanisani, na kurudia ardhi ile ile. Wanatoa ripoti kwamba wamekuwa na wakati mzuri, ziara na ugeni mwema, lakini hatuoni roho zinazoongolewa kupitia huduma yao. Wachungaji wa namna hii wanaikumbatia fukwe/pwani kwa

ukaribu sana. Hebu na watweke mpaka kilindini, na kisha watupe nyavu mahali walipo samaki. Hakuna ukosefu wa kazi za kufanya. Mamia wangeweza kuajiriwa katika shamba la Bwana mahali ambapo sasa kuna mchungaji mmoja tu. **—The True Missionary, February, 1874.**{EVsw 59.3}

Changamoto kwa Viongozi — Nawauliza wale walioko katika zamu ya kuongoza kwenye kazi zetu za injili: Kwa nini maeneo mengi yanapita bila kufanyiwa kazi? Angalia miji na miji mikubwa ambayo bado haijafanyiwa kazi. Kuna miji mingi mikubwa Amerika, si tu Kusini bali Kaskazini pia, bado inahitaji kufanyiwa kazi. Kila mji Marekani unapaswa kuwa na alama ya **Mungu**. Lakini naweza kutaja maeneo mengi ambayo nuru ya Kweli bado haijawaangazia. Malaika wa mbinguni wanangojea watendakazi wa kianadamu wawe mashahidi mahali ambapo **Ukweli** wa sasa bado haujaelezwa. —**The Review and Herald, Desember 30, 1902.**{EVsw 60.1}

Kushughulikia Eneo Jipya — Kuanzisha Vituo Vipya-Tayarisha watendakazi wa kilimo watakaoenda katika njia kuu na mipaka ya miji. Tunahitaji walezi wenye hekima watakaotoa miche ya miti kutoka katika kitalu, na kuipanda mbalimbali, katika maeneo tofauti na hivyo kuipa hali nzuri ili ikue. Ni wajibu wa dhati kwa watu wa **Mungu** kwenda katika maeneo mapya, hadi mwisho wa dunia yote. Ngazi zifunguliwe za kufanikisha kazi, kuanzisha vituo vipya vya mvuto popote panapopatikana nafasi. —**Manuscript 11, 1908.**{EVsw 60.2}

Kuvifikia Zaidi Vituo Vigumu vya Injili- Tukumbuke kuwa sisi kama watu tulioaminiwa kwa Ukweli mtakatifu, tumekuwa wavivu na hatari zaidi, hatuwezi kuwa waaminifu. Kazi imebaki katika vituo vichache tu, hadi watu walioko humo wamekuwa na moyo mgumu wa kupokea Injili. Ni vigumu kufikisha ujumbe na kutoa mguso kwa mioyo ya wale waliokwisha kusikia Ukweli mwingi lakini wameukataa. Katika maeneo machache, muda mwingi umetumika, wakati miji mingi haijawahi kupewa onyo na kufanyiwa kazi. Hii yote inatuumiza na kuwa dhidi yetu. Kama tungekuwa na juhudi za dhati kufikia wale ambao wangebadilika na kuwa wawakilishi wa kweli wa kile Ukweli wa sasa unachoweza kufanya kwa binadamu, kazi yetu ingeendelea zaidi sana sasa. Si sawa maeneo machache yapewe upendeleo wote, wakati mengine yakiwa yanatelekezwa. —**Letter 132, 1902.**{EVsw 61.1}

Kupanga Mikakati Kwa Ajili ya Maeneo Mapya- Ninasikia sauti usiku na usiku, “Endeleeni mbele; ongezeni maeneo mapya; ingieni katika maeneo mapya na kibanda, na mlete ujumbe wa mwisho wa onyo kwa dunia. Hakuna muda wa kupoteza. Wekeni kumbukumbu Yangu kila mahali mnapoenda. Roho Yangu itaenda mbele yenu, na utukufu wa Bwana utakuwa nyuma yenu.” {EVsw 61.2}

Kuna miji mingine si mbali sana na hapa, ambayo inapaswa kuwa na mkutano wa kambi mwaka ujao. Huu ndio mpango wa **Mungu** jinsi kazi inavyopaswa kufanyika. Wale waliokuwa na nuru kwa miaka mingi ya kuingia kwenye maeneo mapya na hema na kuweka mikutano ya kambi katika ardhi ile ile kwa miaka mingi, wanahitaji kuongoka wao wenyewe, kwa sababu hawajatii **Neno** la Bwana. —**Letter 174, 1900.**{EVsw 61.3}

Kusonga Mbele kwa Imani

Endelea kwa Imani—Msaada Utakuja

Je,kweli tunaweza kutegemea wakazi wa miji hii waje kwetu na kusema, "Ikiwa mtakuja kwetu kuhubiri, tutawasaidia kufanya hivi na vile"? Hawajui kitu kuhusu ujumbe wetu. Bwana anatamani turuhusu nuru yetu iangaze mbele ya watu, ili Roho Mtakatifu Wake awaelezee **Ukweli** wale wenye mioyo ya kweli inayotafuta **ile Kweli**. Tunapofanya kazi hii, tutagundua kuwa fedha za msaada zitajitokeza kwenye hazina zetu, na tutapata msaada wa kuendesha kazi kubwa zaidi na yenye ushawishi mpana. {EVsw 61.4}

Je, hatutasonga mbele kwa imani, kana kwamba tuna maelfu ya dola? Hatuna hata nusu ya imani. Hebu tutekeleze wajibu wetu wa kuonya miji hii. Ujumbe wa onyo lazima ufikie watu walioko katika hatari ya kuangamia, wasioonywa, wasiookolewa. Tunawezaje kuchelewa? Tunaposonga mbele, msaada utafuata. Lakini lazima tusonge mbele kwa imani, tukimwamini **Mungu** wa Israeli.{EVsw 62.1}

Usiku baada ya usiku sikuweza kulala kwa mzigo huu ulioko moyoni mwangu kwa niaba ya miji ambayo haijaonywa. Usiku baada ya usiku ninaomba na kujaribu kupanga mbinu za kuingia miji hii na kutoa onyo. Kwa nini? Kuna dunia nzima inayohitaji onyo na wokovu, na sisi tunapaswa kwenda Mashariki, Magharibi, Kaskazini na Kusini, tukifanya kazi kwa akili kwa watu waliotuzunguka. Tukianza kazi hii, tutaona wokovu wa **Mungu**. Faraja, na tumaini litakuja. **— Manuscript 53, 1909.**{EVsw 62.2}

Fuata Uongozi wa Mungu

Ikiwa tungefuata uongozi wa **Mungu**, tungekuwa waangalifu kugundua kila fursa, na kutumia kila nafasi tuliyonayo kwa ufanisi.... Kuna hofu ya kuingia katika kazi hii kuu, kwa hofu kwamba matumizi ya fedha yasiyoleta faida yatakuwa ndiyo matokeo. Je, vipi ikiwa tutatumia fedha na tusione roho zinaokolewa? Je, vipi ikiwa tutapoteza sehemu ya fedha zetu? Ni bora tuendelee kufanya kazi kuliko kutofanya lolote. Hujui ni ipi itafanikiwa—hii au ile.{EVsw 62.3}

Watu huwekeza katika haki za uvumbuzi na kupoteza sana, na hilo linachukuliwa kuwa jambo la kawaida. Lakini katika kazi na sababu ya **Mungu**, watu huwa na hofu ya kujitosa au kuthubutu. Fedha za kuwekeza kwa injili zinaonekana kuwa hasara tupu, bila hata faida, yaani malipo yasiyopatikana haraka, wanapowekeza katika kazi ya kuokoa roho. Fedha ambazo sasa zinahifadhiwa kwa ubinafsi, zitatupwa hivi karibuni pamoja na sanamu zote mbele ya wadudu, kuvu/fangasi na popo. Thamani ya pesa itashuka ghafla wakati ukweli wa uhalisia wa mambo ya umilele vitakapofunguliwa katika fahamu za mwanadamu.{EVsw 62.4}

Mungu atakuwa na watu wenye uthubutu kila katika kitu kwa ajili ya kuokoa roho. Wale wasiodiriki kusonga mbele hadi waone kila hatua imewekwa wazi mbele yao, hawatakuwa na umuhimu kwa sasa kwa ajili ya kuendeleza Ukweli wa **Mungu**. Lazima kuwe na watendakazi watakaosonga mbele gizani na kwenye nuru, na kusimama imara chini ya huzuni na matumaini yaliyokatika, lakini wakaendeleza kazi kwa imani, kwa machozi na matumaini ya uvumilivu, wakipanda kando ya chemichemi zote za maji, wakimuamini Bwana kuwa ataleta mavuno. **Mungu** anataka watu wenye ujasiri, matumaini, imani na uvumilivu kufikia lengo. —**The True Missionary, January, 1874.**{EVsw 63.1}

Kufaa kwa Kutumika

Katika nyakati hizi za hatari, hatupaswi kuacha mbinu yoyote ya kuonya watu bila kuijaribu. Tunapaswa kuwa na nia thabiti kuzuia maovu. Endelea kufanya kazi mtumishi! Kuwa na imani kwa **Mungu**. **— Letter 49, 1902.**{EVsw 63.2}

Sio Kwa Nguvu Zetu

Nawaalika, ndugu zangu wachungaji, kujiunga zaidi na kazi ya **Mungu**. Roho nyingi zinazoweza kuokolewa zitapotea, isipokuwa mtajitahidi kwa bidii kufanya kazi zenu ziwe bora zaidi. Kazi kubwa inasubiri kufanywa katika -----. Inaweza kuonekana kuwa inasogea polepole na ngumu mwanzoni; lakini **Mungu** atafanya kazi kuu kupitia ninyi ikiwa mtajitoa Kwake kikamilifu kabisa. Muda mwingi mtahitaji kutembea kwa imani, si kwa hisia/mihemko....{EVsw 63.4}

Popote mnapokuwa, haijalishi ni hali ngumu kiasi gani mnapitia, msizungumze kwa kuchoka moyo. Biblia imejaa ahadi nyingi nzuri. Je, wewe huwezi kuziamini? Tunapokwenda kufanya kazi ya kuokoa roho, **Mungu** hataki tuwe wapiganaji wenye nguvu zetu wenyewe. Hii inamaanisha nini? Inamaanisha hatupaswi kwenda kwa nguvu zetu, kwa sababu **Mungu** ameahidi katika Neno Lake kwamba Atakwenda pamoja nasi. — **Historical Sketches, uk. 128, 129. (1886).**{EVsw 64.1}

Katika Nyakati za Awali — Kwa amri ya **Mungu**, "Songeni mbele," tulisonga mbele hata pale changamoto zilipokuwa kubwa kiasi cha kuonekana haiwezekani kuendelea. Tunajua gharama kubwa iliyotolewa kutekeleza mipango ya **Mungu** zamani, ambayo imetufanya sisi kama watu, tuwe vile tulivyo leo. Kwa hiyo, kila mtu aepuke kwa uangalifu kuleta mashaka au kuchanganya mioyo kuhusu mambo ambayo **Mungu** ameweka kwa ajili ya ustawi na mafanikio yetu katika kuendeleza kusudi Lake. — **Letter 32, 1892.**{EVsw 64.2}

Acha Matokeo kwa Mungu — Mbegu nzuri inapopandwa, wakati mwingine inaweza kuangukia katika moyo usio na huruma, wenye ubaridi, wa kidunia na wenye ubinafsi, hivyo isiweze kuota mizizi; lakini mara zote Roho wa **Mungu** hufanya kazi katika moyo huo, na kuimwagilia mbegu hiyo kwa matone ya umande wa mbinguni, kisha mbegu hii iliyofichwa kwa muda mrefu huchipuka na hatimaye huzaa matunda bora kwa utukufu wa **Mungu**. Hatujui katika uzoefu wetu wa kufanya kazi kuwa ni mbegu ipi itafanikiwa, hii au ile. Haya sio maswali tunayopaswa kuyajibu sisi, kama wanadamu dhaifu. Tunapaswa tu kufanya kazi yetu, tukimwachia **Mungu** suala la matokeo. — **Testimonies for the Church 3:248 (1872).**{EVsw 64.3}

Kusaidia Makanisa Yanayofanya Kazi — Kila konferensi, iwe kubwa au mdogo, ina jukumu la kufanya kazi adhimu na ya dhati katika kuwaandaa watu kwa ajili ya kuja kwa Kristo. Makanisa yote katika konferensi yanayokubali kufanya kazi, na yanayohitaji msaada ili kujifunza jinsi ya kufanya kazi yenye ufanisi, yanapaswa kupatiwa msaada unaohitajika. Kila mtendakakazi wa konferensi ajitahidi, kuzinduka, kukodoa

macho kwa bidii, katika kuifanya konferensi yake kuwa chombo chenye nguvu kinachojenga kazi ya **Mungu**. Kila mshiriki wa kanisa awe mshiriki hai wa kazi za kiroho, kujenga maslahi ya kiroho. Kwa upendo mtakatifu, kwa maombi ya unyenyekevu na kazi ya dhati na bidii, wachungaji wafanye sehemu yao. — **Manuscript 7, 1908.**{EVsw 64.4}

Mikono ya Mungu Juu ya Gurudumu — Hatari kubwa zipo mbele ya wale wanaobeba jukumu la kazi ya **Mungu** — hatari ambazo ninapozifikiria tu ninatetemeka. Lakini Neno la uvuvio linakuja, "Mikono Yangu iko juu ya gurudumu, na sitaruhusu watu kudhibiti kazi Yangu wakati wa siku hizi za mwisho. Mikono Yangu inasukuma na kuliendesha gurudumu, na majaliwa Yangu yataendelea kufanya kazi hii- (mipango ya **Mungu)**, bila kujali ubunifu wa mwanadamu." …..{EVsw 65.1}

Katika kazi kubwa ya mwisho tutakutana na changamoto na mifadhaiko ambayo hatujui jinsi ya kutatua, lakini tusisahau kwamba mamlaka kuu tatu za mbinguni zinafanya kazi, kwamba mkono wa **Mungu** uko juu ya gurudumu, na **Mungu** atatekeleza kusudi Lake. — **Manuscript 118, 1902.**{EVsw 65.2}

Neema na Upendeleo/Favor, Hadi Kazi Itakapokamilika — Dunia yote inapaswa kuonywa. Tukeshe, kwa subira, tuombe, tufanye kazi, na tusiruhusu jambo lolote kufanyika kwa ubinafsi au kujigamba. Tusifanye jambo lolote linaloongeza chuki, bali tufanye kila linalowezekana ili kupunguza chuki kwa kuruhusu nuru, miale angavu ya Jua la Haki katikati ya giza la kimaadili. Kazi kubwa bado inasubiri kufanyika, na jitihada zote zinazowezekana zifanyike za kumfunua Kristo kama Mwokozi anayesamehe dhambi, Kristo kama Mbeba dhambi, Kristo kama Nyota ya asubuhi, na Bwana atatupa neema mbele ya dunia hadi kazi yetu itakapokamilika. — **Letter 35, 1895.**{EVsw 65.3}

Uinjilisti wa Aina ya Juu

Kwa hadhi na Neema, Uungwana, Usahili na Unyenyekevu

Wale wafanyao kazi ya Bwana katika miji lazima waweke juhudi za utulivu, thabiti, za kujitolea kwa ajili ya elimu za watu. Ingawa wanapaswa kufanya kazi kwa bidii ili kuvutia wasikilizaji na kuushikilia usikivu huu, bado wakati huo huo lazima wajilinde kwa uangalifu dhidi ya kitu chochote kinachopatana na mihemko/hisia. Katika kizazi hiki cha ubadhirifu na maonyesho ya nje, wakati watu wanafikiri ni muhimu kufanya maonyesho ili kupata kufanikiwa, wajumbe walioteuliwa, wa **Mungu** wanapaswa kuonesha uongo wa njia za matumizi ya mali bila ulazima. Kadri wanavyofanya kazi kwa usahili, unyenyekevu, na uungwana, staha na neema, wakiepuka kila kitu chenye asili ya maburudusho yenye maonyesho, kazi yao itakuwa na matokeo yenye mvuto wa kudumu kwa mema.{EVsw 66.1}

Hakika kuna ulazima wa kutumia pesa kwa busara katika kutangaza mikutano na katika kuendeleza kazi kwa uthabiti. Hata hivyo nguvu za kila mfanyakazi zitaonekana kusema uongo, si katika hawa mawakala wa nje, bali kwa kumtegemea **Mungu** kwa uaminifu, katika maombi ya dhati Kwake kwa ajili ya msaada, katika utii kwa **Neno** Lake. Maombi mengi zaidi, kufanana zaidi na Kristo, kupatana zaidi na mapenzi ya **Mungu**, kunapaswa kuletwa katika kazi ya Bwana. Maonyesho ya nje na matumizi mabaya ya mali hayatafanikisha kazi inayopaswa kufanywa.{EVsw 66.2}

Kazi ya **Mungu** inapaswa kuendelezwa kwa nguvu. Tunahitaji ubatizo wa Roho Mtakatifu. Tunahitaji kuelewa kwamba **Mungu** ataongeza kwenye safu za Jeshi la watu Wake, watu wenye uwezo na ushawishi ambao wanapaswa kufanya sehemu yao katika kuuonya ulimwengu. Watu wote ulimwenguni sio waasi na wenye dhambi. **Mungu** ana maelfu wengi ambao hawajapiga goti kwa Baali. Kuna wanaume na wanawake wanaomcha **Mungu** katika makanisa yaliyoanguka. Ikiwa isingelikuwa hivyo, hatungelipewa ujumbe wa kubeba: "Umeanguka, umeanguka Babeli ule mkuu.... tokeni kati yake, enyi watu Wangu." Ufunuo 18:2-4. Wengi wenye moyo wa uadilifu wanahema kwani wanashindwa kupumua vizuri, kwa kukosa pumzi ya uzima kutoka mbinguni. Watatambua injili inapoletwa kwao katika uzuri na usahili unaoonyeshwa kwa njia ya **Neno** la **Mungu**. —**Testimonies For The Church 9:109-111 (1909).** {EVsw 66.3}

Watendakazi Wenye Uzoefu kwa Maeneo Mapya Mijini-Watendakazi wenye uzoefu wanapaswa kupewa kazi ya kuingia katika maeneo mapya. Njia itumike kudumisha hadhi/heshima ya kazi hii takatifu. Kila wakati tukumbuke kuwa malaika waovu hutafuta nafasi ili kuzuia juhudi zetu.{EVsw 67.1}

Miji lazima ifanyiwe kazi. Kipindi cha jaribu kubwa kipo mbele yetu. Hivyo asiwepo atakayeipeleka nafsi yake kwa vitu visivyokuwa na maana au vya ubatili tu. Wale wanaotafuta taji ya uzima wawe na juhudi halali. Uwezo na vipawa vyetu vyote vitumike kwa kazi ya kuokoa roho zinazopotea na kuwavuta wengine

wawe watendakazi wenza wa Kristo. Maarifa na nguvu alizowapa **Mungu** wanaume na wanawake vitazidi kuongezeka wanapojenga ufalme Wake. **—Manuscript 19, 1910.**{EVsw 67.2}

Hali ya Ubora na iliyoinuliwa Juu, Usafi, dhamiri nyeti na Umakini

Katika vizazi vyote, **Mungu** amekuwa makini kuhusu kusudi na utekelezaji wa kazi Yake. Katika zama hizi, Yeye Ametoa nuru na mafundisho mengi kuhusu jinsi kazi Yake inavyopaswa kufanywa — kwa ubora, kuinuliwa na dhamiri nyeti, usafi, na umakini; na Anafurahishwa na wale wanaotekeleza kusudi Lake kwa uaminifu. **—The Review and Herald, September 14, 1905.** {EVsw 67.3}

Katika Ngazi ya Juu— Katika miaka ya huduma ya **Kristo** hapa duniani, wanawake wacha **Mungu** walishiriki katika kazi ambayo Mwokozi na wanafunzi Wake waliendelea kuifanya. Kama wale waliopinga kazi hii wangeweza kupata dosari yoyote nje ya mpangilio wa kawaida katika mwenendo wa wanawake hawa, kazi hiyo ingekuwa imefungwa mara moja. Lakini wakati wanawake walipokuwa wakishirikiana na **Kristo** na mitume, kazi yote ilifanywa katika kiwango cha juu sana kiasi kwamba haikuacha kivuli chochote cha tuhuma au kushukiwa. Hakukuwa na nafasi yoyote ya mashitaka. Mawazo ya wote yalielekezwa kwenye Maandiko, badala ya kwa watu binafsi. Ukweli ulitangazwa kwa uelewa mahiri, na kwa uwazi kiasi kwamba kila mtu angeweza kuuelewa....{EVsw 67.4}

Katika ujumbe huu kuna ulinganifu wa kupendeza unaogusa akili ya hukumu. Hatuwezi kuruhusu vipengele vya misisimko ya kihisia kuonyeshwa miongoni mwetu kwa namna ambayo ingeharibu ushawishi wetu kwa wale tunaotamani kuwafikia kwa njia ya Ukweli. **—Manuscript 115, 1908.**{EVsw 68.1}

Epuka Njia Zisizo na Heshima au Zinazoonyesha Kukosa Uungwana au Adabu/staha — Ingawa ni vyema kutumia mali kwa hekima na uchumi, kazi ya **Mungu** lazima isimame daima katika hadhi yake ya juu na yenye heshima kuu…….. Usiiweke kazi ya **Mungu** katika hali ya kudharauliwa. Kazi daima iachwe katika mkao wa kuonekana kwamba yatoka kwa **Mungu**; isiwe na alama ya kibinadamu, bali iwe na alama ya Kiungu. Nafsi ya mtu ichukuliwe kuwa si kitu mbele za Yesu…...{EVsw 68.2}

Kumekuwa na hasara kubwa kutokana na kufuata mawazo ya makosa ya ndugu zetu wema, ambao mipango yao ilikuwa finyu, wakaidunisha kazi ya **Mungu** kwa kuielekeza katika mitazamo na mawazo yao binafsi, kiasi kwamba watu wa tabaka za juu hawakufikiwa. Muonekano wa kazi hiyo uliwafanya wasioamini waihisi kuwa haina thamani yoyote—kama matawi yaliyopotea ya nadharia fulani za kidini (offshoot), yasiyostahili kupewa makini. Hasara kubwa imepatikana kwa sababu ya kukosa mbinu za hekima za kufanya kazi. {EVsw 68.3}

Kila jitihada inapaswa kufanywa ili kuipa kazi hii heshima na haiba. Jitihada maalum zinapaswa kufanywa ili kupata nia njema ya watu walio katika nafasi za uwajibikaji, bila kusalimisha hata kwa kanuni moja ya kweli au haki, bali kwa kujinyima njia zetu wenyewe na namna yetu ya kuufikia umma. Mambo mengi zaidi yangetendeka kama tungelitumia busara na werevu zaidi katika kuwasilisha Kweli. **—Letter 12, 1887.** {EVsw 68.4}

Mafundisho makuu ya Imani (Doctrines) Yapaswa Kupitia Uchunguzi wa Watu Wakubwa—

"Yohana 5:39 *Mwayachunguza Maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake*." Kila msimamo wa Kweli unaoshikiliwa na watu wetu utaweza kustahimili uchunguzi wa akili kubwa kabisa; watu wakuu wa dunia hii wataletwa uso kwa uso na **Kweli**, na kwa hiyo kila msimamo tunaouchukua unapaswa kuchunguzwa kwa kina na kujaribiwa kwa Maandiko. Kwa sasa twaonekana kama hatujulikani sana, lakini hali hiyo haitadumu milele. Harakati zinafanyika zitakazotuleta mbele ya umma, na kama mafundisho yetu ya **Kweli** yanaweza kubomolewa na wanahistoria au watu mashuhuri wa dunia, basi jambo hilo litafanyika. {EVsw 69.1}

Ni lazima kila mmoja wetu ajue binafsi **Ukweli** ni nini, na awe tayari kutoa sababu ya tumaini alilonalo kwa unyenyekevu na kwa hofu ya **Mungu**—si kwa majivuno wala kujitosheleza na kwa ujeuri, bali kwa roho ya Kristo. Tunakaribia wakati ambapo kila mmoja atasimama peke yake kujibu kwa ajili ya imani yake. Makosa ya kidini yanazidi kuongezeka na kujipenyeza miongoni mwa watu kwa nguvu za kishetani. Hakuna karibu fundisho lolote la Biblia ambalo halijapingwa. **—Letter 6, 1886.**{EVsw 69.2}

Mwinjilisti na Timu Yake

Uinjilisti na Wainjilisti — Ninapofikiria kuhusu miji ambayo kazi ndogo sana imefanyika, miji ambayo kuna maelfu ya watu wanaopaswa kuonywa kuhusu ujio wa karibu wa Mwokozi, nahisi shauku kubwa ya kuona wanaume na wanawake wakitoka kwenda kufanya kazi hii kwa nguvu ya Roho, wakiwa wamejawa na upendo wa Kristo kwa roho zinazopotea…..{EVsw 69.3}

Akili yangu inasisimuka kwa kina. Katika kila mji kuna kazi inayopaswa kufanywa. Watendakazi wanapaswa kwenda katika miji yetu mikubwa na kuandaa mikutano ya makambi. Katika mikutano hii, vipawa bora kabisa vinapaswa kutumika, ili **Ukweli** uweze kutangazwa kwa nguvu. Watu wenye vipawa mbalimbali wanapaswa kuletwa na kuhusishwa…..{EVsw 69.4}

Mbinu mpya zinapaswa kuanzishwa. Watu wa **Mungu** lazima waamke kwa mahitaji ya wakati wanaoishi. **Mungu** anao watu ambao atawaita katika huduma Yake—watu ambao hawataendeleza kazi kwa namna isiyo na uhai kama ilivyokuwa zamani…..{EVsw 70.1}

Katika miji yetu mikubwa ujumbe unapaswa kutolewa kama taa iwakayo. **Mungu** atainua watendakazi kwa kazi hii, na malaika Wake watatangulia mbele yao. Asiwepo mtu yeyote wa kuwazuia hawa watu waliowekwa na **Mungu**. Msiwazuie. **Mungu** amewapa kazi yao. Hebu ujumbe huo na utolewe kwa nguvu kiasi kwamba wasikilizaji washawishike. **—Review and Herald, September 30, 1902.**{EVsw 70.2}

Watu Wenye Nguvu Wanahitajika — Nawaomba ndugu zetu wahubiri kulifikiria jambo hili. Hebu watu wenye nguvu wawekwe rasmi kufanya kazi katika vituo vikuu. —**Manuscript 25, 1908.**{EVsw 70.3}

Vipawa Tofauti — Katika mikutano yetu ya makambi tunapaswa kuwa na wasemaji wanaoweza kuacha taswira nzuri kwa watu. Uwezo wa mtu mmoja, hata kama ni mwenye akili kiasi gani, hautoshi kutimiza mahitaji. Vipawa tofauti vinapaswa kushirikishwa katika mikutano hii. —**Manuscript 104, 1902.**{EVsw 70.4}

Mtu wa Pili Ni Uwekezaji Mzuri — Bwana anakusudia kazi Yake ifanyike kwa uthabiti. Kuingia kwenye eneo jipya kunahitaji gharama kubwa. Lakini gharama ya ziada ya mtu wa pili kusaidia Ndugu _____ itakuwa ni uwekezaji utakaorejesha faida. Nahisi kushinikizwa kulihimiza jambo hili kwa sababu kuna mengi yaliyoko hatarini. Naomba Bwana awatie mioyo yenu kutekeleza mapenzi Yake. **—Letter 261, 1905.**{EVsw 70.5}

Kushikilia Hadhira Kubwa — Bwana amewapa baadhi ya wahubiri uwezo wa kukusanya na kushikilia makutano makubwa. Wanapofanya kazi kwa hofu ya **Mungu**, juhudi zao zitaandamana na msukumo mkubwa wa Roho Mtakatifu juu ya mioyo ya wanadamu…..{EVsw 71.1}

Nimepewa agizo la kuwaamsha walinzi. Mwisho wa mambo yote umekaribia. Sasa ndiyo wakati unaokubalika. Wahubiri wetu na wenyeviti wetu wa makoferensi waonyeshe busara na ustadi katika kuwasilisha Ukweli mbele ya makundi makubwa ya watu mijini. Mnapofanya kazi kwa unyenyekevu, na usahili, mioyo itayeyuka. Kumbukeni kwamba mnapowasilisha ujumbe wa kujaribu kwa wakati huu, mioyo yenu wenyewe italainishwa na kuongozwa kwa wepesi kwa mvuto wa kunyenyekeza wa Roho Mtakatifu, na mtavuna roho kwa ajili ya Bwana. Mnaposimama mbele ya makutano mijini, kumbukeni kuwa **Mungu** Ndiye msaidizi wenu, na kwa baraka Yake mnaweza kuwasilisha ujumbe wa kugusa mioyo ya wasikilizaji. **—Manuscript 53, 1910.** {EVsw 71.2}

Wanaume na Wanawake Kufundisha Ukweli — Walimu wenye hekima—wanaume na wanawake waliobobea katika kufundisha Kweli za Neno—wanahitajika mijini. Hebu na wawasilishe **Ukweli** kwa hadhi yote ya Kiungu, na kwa usahili na unyenyekevu uliotakaswa. —**Review and Herald, January 25, 1912.**{EVsw 71.3}

Paulo Alikuwa Mwinjilisti Anayesafiri — Maisha ya Paulo yalikuwa ya shughuli nyingi na za aina mbalimbali. Kutoka mji hadi mji, kutoka nchi hadi nchi, alisafiri akisimulia kisa cha msalaba, akiwavuta watu waiamini Injili, na kuanzisha makanisa. **—Gospel Workers, uk. 58, 59 (1915).**{EVsw 71.4}

Watendakazi Hodari, Wenye Ujasiri — Watu walio dhaifu au wazee hawapaswi kutumwa kufanya kazi katika miji yenye msongamano na isiyo na afya. Hebu na wafanye kazi mahali ambapo maisha yao hayatawekwa hatarini na kutolewa dhabihu bila sababu. Ndugu zetu wanaoleta **Ukweli** mijini hawapaswi kulazimika kuhatarisha afya zao katika kelele, msongamano, na machafuko, ikiwa maeneo ya faragha yanaweza kupatikana.{EVsw 71.5}

Wale wanaohusika katika kazi ngumu na ya kujaribu mijini wanapaswa kupata kila aina ya kutiwa moyo iwezekanayo. Wasilalamikiwe kwa maneno yasiyo ya fadhili kutoka kwa ndugu zao-acheni kuwakosoa-

kosoa. Lazima tuonyeshe kujali kwa watendakazi wa Bwana wanaofungua nuru ya Kweli kwa wale walio katika giza la upotovu. **—Letter 168, 1909.** {EVsw 72.1}

Faida za Kufanya Kazi Wawili Wawili

Yesu Aliwatuma Ndugu Wawili Wawili

Alipowakusanya wale Thenashara karibu Naye, Yesu aliwaamuru waende wawili wawili kupitia miji na vijiji. Hakuna aliyekwenda peke yake; bali ndugu aliunganishwa na ndugu, rafiki na rafiki. Kwa njia hii wangeweza kusaidiana na kutiana moyo, wakishauriana na kuomba pamoja—nguvu ya mmoja ikikamilisha udhaifu wa mwingine. Vivyo hivyo baadaye Aliwatuma wale sabini. Ilikuwa ni kusudi la Mwokozi kwamba wajumbe wa Injili wafanye kazi kwa ushirikiano wa namna hii. Katika siku zetu, kazi ya uinjilisti ingezaa matunda mengi zaidi kama mfano huu ungefuatwa kwa ukaribu zaidi. **— The Desire of Ages, uk. 350 (1898)**{EVsw 72.2}

Mpango wa Mungu kwa Kazi Leo

Yesu alipowatuma wanafunzi Wake kwenda kufanya kazi,..... hawakuhisi kama wengine wanavyohisi leo kuwa wangependelea kufanya kazi peke yao kuliko kuwa na mtu ambaye hafanyi kazi kwa mtindo wao. Mwokozi wetu alielewa ni nani wa kumshirikisha na nani. Hakumwunganisha Yohana mpole na mpendwa na mtu wa tabia kama yake; bali alimuunganisha na Petro mwenye ari na msukumo wa haraka. Wanaume hawa wawili hawakuwa na tabia wala mitindo ya kazi inayofanana. Petro alikuwa mwepesi na mwenye bidii/ari, jasiri na asiyetetereka, na mara nyingi alijeruhi (kwa maneno au matendo); Yohana alikuwa mtulivu daima, na mwenye kuzingatia hisia za wengine, na angekuja baadaye kutuliza na kutia moyo. Kwa hivyo, mapungufu ya mmoja yalifunikwa kwa kiasi fulani na sifa za mwenzake. [Tazama pia uk. 103–107, “Kuruhusu Mbinu Zaidi ya Mmoja.”] {EVsw 72.3}

Mungu hakukusudia kwamba, kama kanuni, watumishi Wake waende kufanya kazi wakiwa peke yao. Kwa mfano: Hapa kuna ndugu wawili. Hawana hulka au tabia zinazofanana; mawazo yao hayafuati mkondo mmoja. Mmoja yuko katika hatari ya kufanya kazi kupita kiasi; mwingine anashindwa kubeba mizigo anayopaswa kubeba. Wakishirikiana, wanaweza kuwa na mvuto wa kufinyanga tabia ya kila mmoja, ili kwamba misimamo mikali ya tabia zao isiwe wazi sana katika kazi yao. Huenda isiwe lazima wawe pamoja katika kila mkutano, lakini wanaweza kufanya kazi katika maeneo yaliyotengana kwa maili kumi, kumi na tano au hata thelathini—lakini bado wakiwa karibu vya kutosha kiasi kwamba mmoja anapokumbwa na hali ngumu katika kazi yake, anaweza kumwita mwenzake amsaidie. Wapaswa pia kukutana mara kwa mara kwa ajili ya sala na mashauriano.{EVsw 73.1}

Mtu anapofanya kazi peke yake daima, huwa na mwelekeo wa kufikiri kwamba njia yake haiwezi kukosolewa, na hapati shauku yoyote ya kuwa na mwingine anayefanya kazi pamoja naye. Lakini ni mpango wa Kristo kwamba awepo mtu pembeni mwake, ili kazi isifinyangwe kabisa kwa mtazamo wa mtu mmoja, na ili mapungufu yake ya tabia yasionekane kama fadhila kwake mwenyewe au kwa wale wanaomsikiliza. {EVsw 73.2}

Mhubiri asipokuwa na mtu pembeni mwake wa kushiriki naye kazi, mara nyingi atajikuta katika hali ya kulazimika kuvunja sheria za uhai na afya. Kisha tena, mambo muhimu huweza kutokea yanayomlazimu kuondoka katikati ya kipindi chenye umuhimu mkubwa. Ikiwa wawili wanafanya kazi pamoja, kazi katika nyakati kama hizo haihitaji kuachwa bila uangalizi. **— Historical Sketches, uk. 126-127 (1886)** {EVsw 73.3}

Faida za Kazi ya Ushirikiano

Kuna haja ya wawili kufanya kazi pamoja; kwa kuwa mmoja anaweza kumtia moyo mwenzake, na wanaweza kushauriana, kuomba, na kuchunguza Biblia pamoja. Kwa njia hii wanaweza kupata mwanga mpana zaidi juu ya **Ukweli**; kwa kuwa mmoja ataona upande mmoja, na mwingine upande mwingine wa Kweli. Ikiwa wanakosea, wanaweza kusahihishana kwa maneno na mwenendo, ili kwamba **Ukweli** usidharauliwe kwa sababu ya mapungufu ya watangazaji wake. Watenda kazi wanapotumwa peke yao, hakuna wa kuona wala kusahihisha makosa yao; lakini wawili wanapokwenda pamoja, kazi ya kuwafundisha inaweza kufanyika, na kila mtenda kazi akawa vile anavyopaswa kuwa—mshindi wa roho aliye na mafanikio.{EVsw 74.1}

— The Review and Herald, July 4, 1893

Kwa Nini Sio Leo?

Kwa nini tumetoka katika njia ya huduma iliyowekwa na Mwalimu Mkuu? Kwa nini watenda kazi katika kazi Yake leo hawatumwi wawili wawili? “Ah,” mnasema, “hatuna watenda kazi wa kutosha kuifanyia kazi nchi yote.” Basi shikeni eneo dogo zaidi. Watumeni watenda kazi katika maeneo ambayo njia imefunguliwa, na fundisheni Ukweli wa thamani kwa wakati huu. Je, hatuoni hekima ya kuwafanya wainjilisti wawili kwenda pamoja kuhubiri Injili? **— The Review and Herald, April 19, 1892.** {EVsw 74.2}

Sehemu ya Kazi ya Uinjilisti

“Jifunze Mahali au Sehemu Uliyopo” - Ingia katika miji mikubwa, na uamshe hamu ya kujifunza kwa watu wa hali ya juu na ya chini. Ifanye kazi yako kuwa ni kuhubiri Injili kwa maskini, lakini usiishie hapo. Tafuta pia kuwafikia watu wa tabaka la juu. Jifunze mahali ulipo kwa nia ya kuangaza nuru yako kwa wengine. Kazi hii ilipaswa kuwa imefanyika tangu zamani sana. **— Testimonies to Ministers and Gospel Workers, uk. 400 (1896)** {EVsw 74.3}

Kazi Katika Kumbi - Hebu kumbi zikodishwe, na ujumbe utolewe kwa nguvu kiasi kwamba wasikilizaji washawishike. **Mungu** atawainua watenda kazi watakaokuwa na maeneo ya kipekee ya ushawishi, watenda kazi watakaobeba Ukweli hata kwa maeneo yanayoonekana kutokuwa na matumaini. **— Manuscript 127, 1901.** {EVsw 75.1}

Kumbi Kubwa Katika Miji Yetu - Kumbi kubwa katika miji yetu zinapaswa kupatikana ili ujumbe wa malaika wa tatu utangazwe kwa vinywa vya wanadamu. Maelfu watauthamini ujumbe huu. **— Letter 35, 1895.** {EVsw 75.2}

Kumbi Maarufu Zaidi - Inahitaji fedha ili kupeleka ujumbe wa onyo mijini. Wakati mwingine ni lazima kukodisha kwa gharama kubwa kumbi maarufu zaidi, ili tuweze kuwaita watu. Hapo ndipo tunapoweza kuwapa ushahidi wa kibiblia wa Ukweli. **— Manuscript 114, 1905.** {EVsw 75.3}

Anzeni kwa Kuchukua Tahadhari - Nimekuwa nikielekezwa, na bado ninaelekezwa, kuhusu mahitaji muhimu kwa kazi ya mijini. Tunapaswa kutafuta majengo kimya-kimya, bila kufafanua kila tunachokusudia kufanya. Tunahitaji busara kubwa katika maneno yetu, tusije tukazuiwa njia yetu. Lusifa ni mfanyakazi mwenye akili mahiri katika kazi yake (genius), akichota maarifa yote kutoka kwa watu wetu ili, ikiwa itawezekana, avuruge mipango iliyowekwa kwa ajili ya kuiamsha miji yetu. Kwa baadhi ya mambo, ukimya unanena kwa ubora zaidi. **— Letter 84, 1910.** {EVsw 75.4}

Kodisheni Kumbi Nzuri - Katika maeneo mengine kazi lazima ianze kwa njia ndogo, na isonge polepole. Hili ndilo ambalo tu watendakazi wanaweza kufanya. Lakini katika hali nyingi, juhudi pana na za wazi zaidi zingefanyika tangu mwanzo, na matokeo yangekuwa bora. Kazi katika _____ ingekuwa imeendelea zaidi sasa kama ndugu zetu, hapo mwanzoni mwa kazi pale, wasingefanya kwa njia ya gharama ndogo mno. Kama wangekodisha kumbi nzuri, na kuendeleza kazi kana kwamba tunazo Kweli kuu ambazo hakika zitashinda, wangepata mafanikio makubwa zaidi. **Mungu** angependa kazi ianzishwe kwa namna ambayo taswira ya kwanza itakayotolewa iwe bora kabisa iwezekanavyo. — **Gospel Workers, uk. 462 (1915).** {EVsw 75.5}

Mahema Yapigwe Katika Maeneo Yenye Faida Zaidi - Tunapaswa kuipeleka Kweli mijini. Mahema yapigwe katika maeneo yenye faida zaidi au penye kufaa zaidi, na mikutano ifanyike. **— The Review and Herald, Mei 25, 1905.** {EVsw 76.1}

Utunzaji wa Eneo la Hema - Mzee _____ amepiga hema kubwa la mikutano ya makambi huko Oakland (efoti). Wakati wa maandalizi alikuwa karibu ili kuongoza, na alifanya kazi kwa bidii kuhakikisha kuwa mazingira yanayozunguka hema yanaonekana vyema iwezekanavyo. — **Letter 352, 1906.** {EVsw 76.2}

Faida za Jumba la Mikutano Linalobebeka (mahema nk) - Natamani mngekuwa na jumba la mikutano linalobebeka. Hili lingekuwa bora zaidi kwa kazi yenu kuliko hema, hasa wakati wa msimu wa mvua. — **Letter 376, 1906.** {EVsw 76.3}

Vituo vya Mvuto nje ya Miji (Outpost Centers)

Kutoka Vituo vya Nje ya Miji—Ni kusudi la **Mungu** kwamba watu wetu waishi nje ya miji, na kutoka vituo hivi vya Nje ya Miji, waipe miji onyo, na kuinua ndani yake kumbukumbu kwa ajili ya **Mungu**. Lazima kuwe na nguvu ya ushawishi katika miji, ili ujumbe wa onyo usikike (Wainjilisti wakae vijijini, na wafanye kazi mijini). **—The Review and Herald, April 14, 1903.**{EVsw 76.4}

Kama Kizuizi Dhidi ya Ushawishi Mbaya—Lazima tufanye mipango ya hekima ili kuionya miji, na wakati huo huo tukae mahali ambapo tunaweza kuwalinda watoto wetu na sisi wenyewe dhidi ya ushawishi unaochafua na kudhoofisha maadili ambao umeenea sana katika maeneo haya yenye msongamano wa watu. **—Life Sketches, uk. 410 (1915).**{EVsw 76.5}

Nyumba za Bei Nafuu Vijijini—Tunapaswa kuwa na hekima kama nyoka na wapole kama hua katika jitihada zetu za kupata ardhi vijijini kwa bei ya chini, na kutoka vituo hivi vya nje ya miji (outpost centers) tuifanyie kazi miji. **—Special Testimonies, Series B, Na. 14, uk. 7 (1902).**{EVsw 77.1}

Sehemu Hizo ziwe Karibu na Ambazo zitaifikia Miji Kirahisi—Wateuliwe watu wa busara, si kwa kutangaza nia yao hadharani, bali kwa kutafuta ardhi na majengo kama hayo katika maeneo ya vijijini yaliyo karibu na miji, zinazofaa kwa shule ndogo za mafunzo ya watendakazi, na ambapo pia zitakuwa na miundombinu kwa ajili ya kutibu wagonjwa na roho zenye kuchoka ambazo hazijui Kweli. {EVsw 77.2}

Tafuteni maeneo kama hayo karibu na miji mikubwa, ambapo majengo yanayofaa yanaweza kupatikana, ama kwa zawadi kutoka kwa wamiliki wake, au kununuliwa kwa bei nzuri kwa msaada wa zawadi za watu wetu. Msijenge majengo katika miji yenye kelele. —**Medical Ministry, uk. 308, 309 (1909).**{EVsw 77.3}

Kufanya Kazi Ndani ya Miji, Lakini Sio Kuishi Ndani Yake—Ukweli lazima usemwe, iwe watu watapenda kusikia au wasipende kusikia. Miji imejaa vishawishi/majaribu. Tunapaswa kupanga kazi yetu kwa namna ya kuwaweka vijana wetu mbali kadiri iwezekanavyo na maambukizo ya uchafu huu wa maadili. Miji inapaswa kufanyiwa kazi kutoka vituo vya nje ya miji. Malaika wa **Mungu** alisema, "Je! miji haitakiwi kuonywa? Ndiyo, lakini si kwa watu wa **Mungu** kuishi ndani yake, bali kwa kuitembelea, na kuwaonya kuhusu yale yatakayokuja juu ya dunia."—**Letter 182, 1902.**{EVsw 77.4}

Kama Alivyofanya Henoko—Kama watu wa **Mungu** wanaoshika amri Zake, lazima tuiache miji. Kama alivyofanya Henoko, lazima tufanye kazi ndani ya miji lakini tusikae humo ndani. **—Manuscript 85, 1899.** {EVsw 77.5}

Masomo Kutoka kwa Lutu na Henoko—Wakati uovu unapozidi kusheheni katika taifa, daima kunapaswa kuwa na sauti inayotoa onyo na maagizo, kama vile sauti ya Lutu ilivyosikika kule Sodoma. Lakini Lutu angeweza kuilinda familia yake dhidi ya maovu mengi kama asingefanya makazi katika jiji hilo ovu na lililochafuka kimaadili. Kila jambo ambalo Lutu na familia yake walifanya kule Sodoma lingeweza kufanywa hata kama wangekuwa wanaishi umbali fulani kutoka jiji hilo. Henoko alitembea na **Mungu**, na bado hakuishi katikati ya jiji lililojaa vurugu na uovu wa kila namna, kama alivyofanya Lutu kule Sodoma. **—Manuscript 94, 1903.**{EVsw 78.1}

Mipango ya Mikutano ya Kanda na Vitongoji

Miji Mikubwa—Mikutano ya Uinjilisti Katika Maeneo Tofauti—

Sasa ndio wakati muafaka wa kufanya kazi mijini; kwa maana ni lazima tuwafikie watu walioko huko. Kama watu wa **Mungu**, tumekuwa katika hatari ya kuwekeza maslahi nyingi ya muhimu sehemu moja. Haya siyo maamuzi mema wala busara. Sasa ni wakati wa kuanzisha maslahi katika miji mikuu. Vituo vingi vidogo vinapaswa kuanzishwa badala ya kuwa na vituo vikubwa vichache…..{EVsw 78.2}

Wamishenari wafanye kazi wawili wawili katika maeneo tofauti ya miji yetu mikubwa yote. Watendakazi katika kila mji wanapaswa kukutana mara kwa mara kwa ajili ya mashauriano na maombi, ili wapate hekima na neema ya kufanya kazi kwa ufanisi na kwa umoja. Hebu wote wawe macho ili kutumia kila fursa ipasavyo. Watu wetu ni lazima wajifunge silaha na kuanzisha vituo vya kazi katika kila jiji kubwa. — **Medical Ministry, p. 300 (1909).**{EVsw 78.3}

Kuyafikia Maeneo ya Miji Yetu Ambayo Hayajapewa Onyo—

Ni lazima kuwe na ongezeko la nguvu kazi katika kila sehemu ya maeneo ya kazi. Hebu watendakazi waende wawili wawili, ili wafanye kazi pamoja katika maeneo mengi ya miji yetu ambayo yameachwa bila kupewa onyo kwa muda mrefu. —**Letter 8, 1910.**{EVsw 79.1}

Kila Sehemu Ifanyiwe Kazi—Kundi la watendakazi na waende kwenye mji na wafanye kazi kwa bidii kutangaza Ukweli katika kila sehemu ya mji huo. Washauriane juu ya njia bora ya kuendeleza kazi hiyo kwa gharama nafuu kadri iwezekanavyo. Wanafaa kufanya kazi kwa ukamilifu, huku wakidumisha mtazamo wa kiroho katika juhudi zao. — Manuscript 42, 1905.{EVsw 79.2}

Mahema Kusimamishwa Tena ili Kufikia Sehemu Tofauti za Mji—

Busara ya hali ya juu zaidi inapaswa kuonyeshwa katika kuchagua mahali pa kufanya mikutano ya makambi; haipaswi kufanyika katika maeneo ya mbali yasiyofikika, kwa maana mijini kuna watu wanaohitaji **Ukweli**. Mikutano ya makambi inapaswa kufanyika katika maeneo ambayo watu wa miji yetu mikubwa wanaweza kufikiwa…….**{EVsw 79.3}**

Mikutano ya makambi ni lazima ifanyike ndani au karibu na miji, ambapo watendakazi kwa wakati mmoja watasimamisha hema katika sehemu moja ya mji, na wakati mwingine sehemu nyingine. Hapo mlangoni mwetu pana watu wa mataifa wanaohitaji kusikia ujumbe wa onyo. Katika miji mikubwa ya Amerika, kumbukumbu kwa ajili ya **Mungu** ni lazima zianzishwe. —**Letter 164, 1901.{EVsw 79.4}**

Kupanga kwa ajili ya Kazi ya Kudumu

[Tazama pia ukurasa 321-326, “Kufunga Kazi Kikamilifu.”]

Kulima Juu-Juu—Mavuno Kidogo

Tuko katika hatari ya kupanua kazi katika maeneo mengi sana na kuanzisha miradi mingi zaidi ya uwezo wetu wa kuisimamia ipasavyo, na hiyo itageuka kuwa mzigo unaochosha kwani utanyonya rasilimali zetu nyingi. Kuna hatari ya kupitiliza katika baadhi ya matawi ya kazi, huku sehemu zingine muhimu za shamba la Bwana zikiachwa bila kutunzwa. Kujitwika kazi nyingi sana bila kuifanya kikamilifu si mpango mzuri. Tunapaswa kusonga mbele, lakini kwa shauri la **Mungu** pekee. Tusifike hatua ya kupoteza unyenyekevu, na usahili wa kazi kiasi cha kupoteza mtazamo wa kiroho, na ikawa vigumu kutunza kazi zote tulizoanzisha bila kuwapoteza wasaidizi wetu bora kwa ajili ya kudumisha mpangilio. Maisha na afya vinapaswa kuthaminiwa. **{EVsw 79.5}**

Ingawa tunapaswa kuwa tayari kila wakati kufuata majaliwa/uongozi wa **Mungu**, hatupaswi kuweka mipango mikubwa katika maeneo ambako kazi yetu tayari imeanzishwa, wala hatupaswi kuchukua maeneo zaidi ya yale tunayoweza kuyakamilisha vizuri. Kulima juu-juu huleta mavuno machache yaliyotawanyika. Endeleeni kuimarisha kazi iliyoanza tayari hadi wingu la uongozi wa **Mungu** lisonge, ndipo mlifuate. Ingawa kuna maeneo mapya yanayofunguka kwa ajili ya watenda kazi, mitazamo yetu nayo inapaswa kupanuka kuhusu watendakazi wanaopaswa kwenda katika maeneo mapya ya Bwana kuwaleta watu kwenye **Kweli**. —**Letter 14, 1886. {EVsw 80.1}**

Kusambaa Kupita Kiasi Lakini Kazi inakuwa Chache sana!

Msitawanye rasilimali zenu katika maeneo mengi kiasi kwamba hakuna jambo linalofanyika kwa kuridhisha mahali popote (kupika kwenye vyungu vingi). Inawezekana kwa watenda kazi kusambaza juhudi zao katika maeneo mengi sana hadi hakuna kinachofanyika ipasavyo hata pale ambapo kwa mwongozo wa Bwana kazi inapaswa kuimarishwa na kukamilishwa. —**Letter 87, 1902, {EVsw 80.2}**

Kazi inayokamilika Katika Mradi wa Uinjilisti (kinagaubaga)

Iwapo hali yetu ya kuwa na bidii hutufanya tusiwe na kiasi, na hivyo tunakusanya kazi nyingi kuliko uwezo wetu wa kimwili na wa neema ya Kristo kuifanya, bila uelewa, mpangilio, na usahihi, basi kila kitu tunachojaribu kufanya kitaonyesha mapungufu/ulema, na kazi itaharibika kila wakati. **Mungu** hatukuzwi hata kama nia ilikuwa njema. Kunakuwa na ukosefu wa hekima unaodhihirika wazi. Mtenda kazi hulalamika kuwa ana mizigo mizito kupita kiasi, ilhali **Mungu** hapendezwi na yeye kujitwika mizigo hiyo; anajisababishia maisha ya fadhaa, wasiwasi, hofu, na kuchoka kwa sababu hajifunzi somo alilopewa na Kristo: kuvaa nira Yake na kubeba mizigo Yake badala ya mizigo aliyojiundia mwenyewe…..**{EVsw 80.3}**

Mungu anataka watenda kazi wenye akili mahiri, wanaofanya kazi yao si kwa pupa bali kwa umakini na ukamilifu, huku wakidumisha unyenyekevu wa Yesu daima. Wale wanaotia mawazo na bidii katika kazi kubwa wanapaswa pia kuweka umakini katika kazi ndogo, wakionyesha usahihi, uadilifu na bidii. Oh, ni kazi ngapi zimefanyika kwa uzembe, na kuachwa tu, ni vitu vingapi vinaachwa hovyo ovyo tu bila kukamilika kwa sababu ya tamaa ya kuchukua kazi kubwa zaidi. Kazi ya **Mungu** inapitiwa juu juu kwa sababu tu kuna kazi nyingi mbele yao kiasi kwamba hakuna kinachofanyika kwa ukamilifu. Lakini kazi yote lazima ipite mbele ya uchunguzi wa Jaji wa dunia yote. Hata zile Kazi ndogo zilizo katika huduma ya Bwana zina umuhimu mkubwa, kwa sababu tu ni huduma ya Kristo. **—Letter 48, 1886. {EVsw 81.1}**

Hakuna Miradi Mipya Kabla Ya Kukamilisha Iliyopo

Hatupaswi kupanga kuanzisha kazi kubwa wakati bado hatuna uwezo wa kukamilisha ile ambayo tayari tumeianza. Hebu mradi mipya isije ikaanzishwa kabla ya wakati wake, nayo ikatumia rasilimali ambazo zinapaswa kujenga kazi katika _____. Maslahi ya mahali hapo lazima yaimarishwe kikamilifu kabla ya kuingia kwenye maeneo mengine. —**Letter 87, 1902.** {EVsw 81.2}

Kudumisha Shauku kwa Ujumbe

Uzoefu wa mikutano hii, pamoja na kile nilichoonyeshwa mara kwa mara kuhusu kufanya mikutano ya makambi katika miji mikubwa, hunifanya nishauri kuwa mikutano ya makambi ifanyike kwa wingi kila mwaka, hata kama baadhi yao ni midogo; kwa maana mikutano hii itakuwa njia yenye nguvu ya kuvuta usikivu wa umati. Kupitia mikutano ya makambi mijini, maelfu wataalikwa kwenye karamu: “Njoni; kwa maana vitu vyote viko tayari.” {EVsw 82.1}

Baada ya kuvuta usikivu wa watu, tusiikate mikutano hiyo kwa haraka, kuvunja mahema na kuwaacha watu wafikiri kuwa mkutano umeisha, wakati ambapo mamia ndiyo wanaanza kuonyesha hamu. Hapo ndipo kazi kubwa zaidi inaweza kufanyika kwa bidii na uaminifu. Mikutano lazima ipangwe kwa namna ambayo shauku ya umma itadumishwa.{EVsw 82.2}

Huenda ikawa vigumu mara nyingine kuwategemeza wahubiri wakuu kwa muda wa wiki chache ili kuendeleza shauku iliyoanza kwenye mkutano; huenda ikagharimu kuendeleza mahali pa mkutano, na kuweka mahema ya familia chache yaliyojitosheleza ili kudumisha mwonekano wa kambi; huenda familia chache zikabaki kwa kujitolea kusaidia wachungaji na Walimu wa Biblia (Bible Workers) ili kufuatilia watu majumbani, kujua kuhusu baraka walizopokea, na kuwaalika kuja tena; lakini matunda ya kazi hiyo, hakika yanastahili juhudi hiyo. Kwa kazi kama hiyo ya bidii na nia ya kweli, baadhi ya mikutano ya makambi yetu imewahi kuanzisha makanisa imara, yenye nguvu; na ni kwa kazi ya dhati na bidii kama hiyo, ndiyo ujumbe wa malaika wa tatu unapaswa kupelekwa kwa watu wa miji yetu. —**The Review and Herald, April 4, 1899.** {EVsw 82.3}

Juhudi Zilizopangwa kwa Muda Mrefu, na

Wakati mwingine idadi kubwa ya wahubiri huhudhuria mkutano wa kambi kwa siku chache; na wakati mvuto wa watu unaanza kuchipuka kikamilifu, karibu wote huondoka kwa haraka ili kwenda mkutano mwingine, na kuwaacha wanenaji wawili au watatu tu kuendelea kupambana na hali ya huzuni ya kupangua mahema ya mkutano na kutoa mahema ya familia zote. {EVsw 83.1}

Ingependeza zaidi, katika hali nyingi, kama mikutano ingeendelea kwa muda mrefu zaidi; kama watu wangekuja kutoka kila kanisa, wakiwa tayari kukaa mwezi mmoja au zaidi, kusaidia katika mikutano na kujifunza jinsi ya kufanya kazi inayokubalika. Kisha wangerudi makanisani mwao wakiwa na uzoefu wenye thamani. Ingekuwa bora kiasi gani, kama baadhi ya wahubiri wale wale waliowavutia watu wakati wa mahudhurio makubwa wangebaki ili kuendeleza kazi kwa juhudi za muda mrefu zilizoandaliwa vizuri. **—The Review and Herald, April 4, 1899.** {EVsw 83.2}

Kuacha Mavuno Bila Kukusanywa

Ingekuwa bora, na mengi yangetimizwa zaidi, ikiwa kungekuwa na mikutano michache ya hema, na nguvu kubwa, au kundi, na karama tofauti za kufanya kazi. Halafu kunapaswa kuwepo na kukawia mahali ambapo watu wanavutiwa. Kumekuwa na haraka sana katika kupangua hema. Wengine huanza kuvutiwa, na kuna haja ya juhudi za kudumu kuendelea kutolewa hadi akili zao zitulie na wajisalimishe katika Ukweli. Katika maeneo mengi ambapo hema limepigwa, watendakazi hukaa mpaka chuki ianze kutoweka, na watu waanze kusikiliza wakiwa na akili isiyo na chuki; hapo ndipo hema hiyo hushushwa na kuanza kusafikiri njiani, kuelekea mahali pengine. Mizunguko inapoisha, muda na mali zimetumiwa, na watumishi wa **Mungu** wanaweza kuona kuwa ni mafanikio kidogo tu yamepatikana kupitia msimu wa hema. Lakini ni wachache tu walioletwa kuukiri **Ukweli na kuongoka**, na watumishi wa **Mungu**, wakiwa wanakuwa wameona machache tu ya kuwachangamsha na kuwatia moyo, na kuinua karama iliyo ndani yao, basi hupoteza hali ya kiroho, na nguvu badala ya kuimarika. —**Testimonies for the Church 1:148 (1857).** {EVsw 83.3}

Watendakazi wa Kufuatilia

Nimekuwa nikikumbuka jinsi hali ilivyokuwa wakati kilio kikuu cha ujumbe wa malaika wa kwanza kilipotangazwa huko Portland na mjini Boston. Jitihada hizi ziliendelea kwa kazi ya kudumu kama ile

mnayofanya ninyi, Mzee _____ na Dada _____ pamoja na wasaidizi wenu. Kazi hii kwa kweli ni kazi ya Bwana. —**Letter 182, 1906.** {EVsw 84.1}

Kuweka Familia Ya Kuendeleza Mvuto

Pia kuna Mji wa Toronto [Australia], mahali pa mapumziko. Maeneo haya yote yapo ndani ya maili kumi hadi ishirini kutoka Cooranbong, na ni lazima yafikiwe mara tu tutakapopata familia zilizojitoa ambazo tunaweza kuwapeleka huko kuendeleza shauku iliyoamshwa. Maeneo haya yote yamekomaa kwa mavuno, lakini hatuwezi kufanya lolote bila watenda kazi waliotoa maisha yao, ambao wanaweza kuingia, kuamsha, na kudumisha hamu ya watu ya injili huko. —**Letter 76, 1899.** {EVsw 84.2}

Uongozi wa Busara Unahitajika

Uongozi wenye busara unahitajika katika kuchagua maeneo ya kazi. Mipango ifanyike kabla ya kuingia katika eneo, kuhusu namna ambavyo roho hizi zitatunzwa. Je, ni nani atawahudumia wale watakaopokea Kweli? Wamekubali Kweli usiopendwa na wengi au usio mashuhuri. Nani atawafundisha baada ya kujifunza “Utangulizi wa mafundisho ya Imani (ABC’s)”? Nani atatia chapa ya kiroho katika uzoefu wao? {EVsw 84.3}

Kufanya kazi kwa gharama kubwa kwa kuwaleta watu kwa ile Kweli, halafu kuwaacha wajifunze na kuunda uzoefu wao kulingana na mawazo potofu waliyopokea na kuyachanganya na dini yao au maisha yao ya kiroho, kungeacha kazi hiyo katika hali mbaya zaidi kuliko ule wakati ambapo ile **Kweli** ilikuwa haijawafikia. Kuacha kazi ikiwa haijakamilika na baadaye kuja kuondoa mafundo-fundo mabaya yatakayoingia, ni mbaya zaidi kuliko kungoja hadi kuwe na mipango ya kutosha ya kuwatunza wale ambao hawakuja katika imani au kukata shauri kwa ujumbe wa injili. —**Letter 60, 1886.** {EVsw 84.4}

Fedha na Bajeti

Kuketi Chini na Kuhesabu Gharama — Watu wa **Mungu** hawapaswi kusonga mbele kwa upofu kwa kuwekeza fedha ambazo hawana, na wala hawajui watakapozipata. Tunapaswa kuonyesha hekima katika hatua tunazochukua. Kristo ametuwekea mpango ambao kazi Yake inapaswa kuendeshwa. Wale wanaotamani kujenga, ni lazima waketi kwanza na kuhesabu gharama, kuona kama wana uwezo wa kukamilisha ujenzi huo. Kabla ya kutekeleza mipango yao, wanapaswa kushauriana na washauri wenye hekima. Ikiwa mtendakazi mmoja anakosa kuoanisha sababu na matokeo na yuko katika hatari ya kufanya maamuzi yasiyo ya busara, watendakazi wenzake wanapaswa kusema naye kwa busara, wakimwonyesha makosa yake. — **Letter 182, 1902.** {EVsw 85.1}

Kuzingatia hali ya Uchumi Kinagaubaga (strict) — Wote wanaojihusisha na kazi katika miji mikubwa wawe waangalifu katika jambo hili—pasifanyike matumizi ya pesa yasiyo ya lazima mahali popote. Sio kwa maonyesho ya nje kwamba watu watajifunza maana ya Kweli ya ujumbe wa sasa. Watenda kazi wetu wanapaswa kuishi kwa kuzingatia kwa umakini hali ya uchumi. **Mungu** anakataza ubadhirifu wa aina yoyote. Kila dola tuliyonayo inapaswa kutumiwa kwa busara. Pasiwepo na maonyesho makubwa yanayopaswa kufanywa. Fedha ya **Mungu** inapaswa kutumika kuendeleza kazi kwa njia Yake Mwenyewe, kazi ambayo Yeye Ameamuru ifanywe duniani. —**Letter 107, 1905.** {EVsw 85.2}

Anza Bila Maonyesho — Kwa nini tuchelewa kuanza kazi katika miji yetu? Hatupaswi kusubiri jambo la ajabu kufanyika au vifaa vya gharama kubwa kuandaliwa ili kufanya maonyesho makubwa. Je, kuna tofauti gani kati ya makapi na ngano ni ipi? Tukitembea na kufanya kazi kwa unyenyekevu mbele za **Mungu**, Yeye Atatuandalia njia. **—Letter 335, 1904.** {EVsw 85.3}

Uinjilisti Ulio na Uwiano-Balansi — **Mungu** apishilie mbali matumizi makubwa ya fedha katika sehemu chache bila kuzingatia uhitaji wa maeneo mengi yasiyo na msaada wowote. Kujinyima, kujikana nafsi kwa ndugu walioko katika maeneo yenye neema ili kuwasaidia walio katika uhitaji, kutasaidia kufanikisha kazi itakayomletea **Mungu** utukufu. Hakuna anayeweza kujenga mnara wa ushawishi sehemu moja na kuziacha sehemu nyingine bila kufikiwa. Bwana na atutakase akili zetu, ili tujifunze kupima mawazo yetu kwa kazi na Mafundisho ya Kristo. —**Letter 320, 1908.**{EVsw 86.2}

Kuchangia Gharama ya Mtendakazi — Katika miji mikuu kuna haja ya kuanzishwa huduma nyingi. Wale ambao hawawezi kushiriki moja kwa moja kwa kazi ya mikono yao, wanaweza kujihusisha kwa kuchangia gharama za mtendakazi anayeweza kwenda. Ndugu na dada zetu wasitoe visingizio vya kutoshiriki katika

kazi ya dhati na bidii. MKristo wa kweli, anayeishi kiulalisia, haishi kwa ajili yake mwenyewe. —**Manuscript 128, 1901.**{EVsw 86.3}

Makanisa Kufadhili Kazi Mpya — Wanaoijua **Kweli** wanapaswa kutiana moyo wakiwaambia wahudumu, "Songeni mbele kwenye eneo la mavuno kwa Jina la Bwana, na sala zetu zitakuwa pamoja nanyi kama miundu mikali." Hivyo, makanisa yetu yanapaswa kutoa ushuhuda dhahiri kwa **Mungu**, na pia wamtolee karama na sadaka zao, ili wale wanaoenda shambani mwa Bwana, wakafanye kazi kwa ajili ya roho. — **Manuscript 73a, 1900.**{EVsw 86.4}

Mpango wa Mungu kwa Kazi ya Mjini

Nimepokea ujumbe kutoka kwa Bwana, ambao nimewasilisha mara kwa mara kwa watu wetu, kwamba kuna watu wengi wenye mali ambao ni wepesi kuguswa mioyo na kushawishiwa na ujumbe wa Injili. Bwana ana watu ambao bado hawajawahi kusikia ileKweli. Endeleeni na kazi yenu, na mali itakayochangwa kwa ajili ya kuendeleza Kweli itumike kuanzisha kituo katika _____. Chagueni watu wanaofaa, ambao hawajawahi kuonyesha roho ya ubinafsi na tamaa ya fedha, inayozuia kutumia mali kwa kazi katika miji mikubwa, ili wengine waendelee na kazi hiyo, kwa kuwa **Mungu** anawatambua kama wateule Wake…….{EVsw 87.1}

Mungu atagusa mioyo ya watu wenye mali, wakati Biblia, na Biblia peke yake, itakapowasilishwa kama nuru ya dunia. Katika miji hii Kweli inapaswa kutangazwa kama taa iwakayo. {EVsw 87.2}

Swali limeulizwa: Kwa nini mwanalenga sana kuwafikia wale watu wa hali ya chini, waliodharauliwa, na kuwaacha watu wenye uwezo wa kutambua mambo na vipawa? Kuna eneo lililo tayari kwa mavuno, na Bwana ana fedha na njia za kufanikisha kulifanyia kazi. Wapo watu wenye uwezo mkubwa wa kibiashara ambao watakubali Kweli, watu wanaoamini Maandiko, ambao kutoka katika hazina ya mioyo yao wataweza kutoa mambo mapya na ya zamani. Wakitawaliwa na Roho Mtakatifu, watu hawa watatenda kwa namna ambayo itaondoa vizuizi, ili watu waweze kuonywa kuhusu kuja kwa haraka kwa Bwana…..{EVsw 87.3}

Katika Shuhuda nyingi, nimeeleza kwamba watu matajiri, ambao wanashikilia mali ya Bwana, watahamasishwa na Roho wa **Mungu** kufungua milango kwa ajili ya kusonga mbele kwa Kweli katika miji mikubwa. Watatumia mali waliyoaminiwa na Bwana kuwa nayo kama mawakili, nakuandaa njia ya Bwana, kuandaa njia ya kufika nyikani kwa **Mungu** wetu. {EVsw 87.4}

Wale wanaofanya kazi katika miji mikubwa wanapaswa, kwa kadiri itakavyowezekana, kuwafikia hata wale wa cheo cha juu duniani, hata mamlaka za utawala. Imani yetu iko wapi? Mungu amenionyesha mfano wa Nebukadneza. Bwana alitenda kwa nguvu kumleta mfalme mwenye mamlaka makubwa zaidi duniani kutambua na kukiri kuwa Yeye ni Mfalme juu ya wafalme wote. Aliugusa moyo wa mfalme mwenye kiburi, hadi Nebukadneza alipomkiri kuwa "**Mungu** Aliyetukuka juu Sana," ambaye "ufalme Wake ni wa milele, na mamlaka Yake hudumu kizazi baada ya kizazi."."—**Letter 132, 1901.** {EVsw 88.1}

Waombe Wenye Mali

Hebu wale wanaofanya kazi kwa ajili ya kazi ya **Mungu** waweke mahitaji ya kazi katika _____ mbele ya watu matajiri wa dunia hii. Fanyeni hivi kwa busara. Waambieni kile mnachojaribu kufanya. Waombeni michango yao. Ni mali ya **Mungu** waliyo nayo, mali ambayo inapaswa kutumika katika kuangazia dunia.{EVsw 88.2}

Kuna hazina nyingi za dhahabu na fedha zilizohifadhiwa duniani. Utajiri wa watu umeongezeka. Nendeni kwa watu hawa mkiwa na mioyo iliyojawa na upendo wa Kristo na kwa ajili ya wanadamu wanaoteseka, waombeni kuwasaidia katika kazi mnayojaribu kufanya kwa ajili ya Bwana. Watakapoona kwamba mnadhihirisha moyo wa ukarimu wa **Mungu**, wataguswa na hisia za huruma mioyoni mwao. Wataelewa kuwa wanaweza kuwa mkono wa kusaidia wa Kristo kwa kufanya kazi ya umishenari wa tiba. Watahamasika kushirikiana na **Mungu**, kutoa vifaa na kupanga mikakati inayohitajika ili kufanya kazi inayopaswa kufanyika, nayo iweze kutekelezwa. —**Manuscript 40, 1901.**{EVsw 88.3}

Wengine pia Wanapaswa Kupata Vifaa

Mzee _____ anatumia kwa ubadhirifu pesa ambazo zinapaswa kusaidia watenda kazi katika sehemu mbalimbali za huduma. Anatakiwa akumbuke kwamba kuna wengine pia kando naye ewanaopaswa kupata fursa ya kutumia vipawa vyao katika kazi ya Bwana. Na wanapaswa kupewa miundombinu na vifaa vya kazi, ili waweze kufanya kazi bila kuhatarisha afya au hata maisha yao. Mtendakazi mmoja hapaswi kutumia kiasi

kikubwa cha pesa ili tu kutekeleza kazi kwa mpango wake mwenyewe, huku mwenzake akiachwa bila rasilimali anazohitaji kutimiza kazi aliyopewa. Hata kama pesa hizo zinatoka kwa watu wa nje, bado ni pesa ya Bwana. **Mungu** hajapanga kwamba mtendakazi mmoja awe na ziada ya kila kitu, huku mwenzake akikosa hata kile cha kutosheleza kazi yake. —**Letter 49, 1902.**{EVsw 88.4}

Roho Zilizoongolewa Zitaleta Rasilimali

Wanaume na wanawake wanapoletwa kwenye Kweli katika miji, rasilimali-fedha zitaanza kuingia. Kwa hakika watu waaminifu watakapoongoka, mali yao itawekwa wakfu kwa ajili ya kazi ya Bwana, na tutaona ongezeko la fedha-rasilimali zetu. —**Manuscript 53, 1909.**{EVsw 89.1}

Jengeni Hazina ya Akiba

Kazi ya uinjilisti haipaswi kuendeshwa kwa njia ya ubinafsi na ya kujitukuza kama alivyoifanya Mzee _____. Rasilimali zinazokuja mikononi mwa watenda kazi katika kazi ya Bwana ni za **Mungu** na zinapaswa kutumiwa kwa matumizi sahihi, na kwa kujali uchumi (si kwa njia ya ovyo ovyo). Fedha nyingi zinapotolewa kwa kazi hiyo, sehemu ya fedha hizo iwekwe akiba; kwa kuwa kutakuwepo na dharura katika shamba kubwa la Bwana. —**Letter 149, 1901.**{EVsw 89.2}

Usimamizi wa Hekima katika Maeneo Mapya

Kuna umuhimu mkubwa wa kuanza kwa njia sahihi mwanzoni mwa kazi yetu. Nimeonyeshwa kwamba kazi katika _____ imekwamishwa bila kupata maendeleo makubwa ambayo yangeweza kupatikana kama kazi hiyo ingeanza kwa njia bora. Mambo mengi zaidi yangeweza kufanyika kwa njia tofauti ya usimamizi, na pesa kidogo zingetumika kutoka kwenye hazina. Tuna amana kubwa na takatifu katika zile Kweli zilizoinuliwa na Bwana na zilizotolewa kwetu. —**Letter 14, 1887.** {EVsw 89.3}

Kujali uchumi kusipitilize Kiasi, na kuwa Ubahili au Kuleta hali hatarishi

Ingawa tunapaswa kuwa kujali uchumi, hatupaswi kupitiliza katika kubana matumizi sana. Ni jambo la kusikitisha na la ajabu maishani kwamba makosa makubwa wakati mwingine hufanywa kwa kujitoa mhanga kwa kiwango cha kupita kiasi. Inawezekana kwa watenda kazi wa Bwana kuwa na kuwa na dhana isiyofaa (ujuvi/presumptious), na kujinyima kupita kiasi hadi kufikia kukosa chakula cha kutosha na mavazi ya kutosha, ili tu kufanya kila senti iwe na matumizi ya juu zaidi. Baadhi ya watenda kazi wanafanya kazi kupita kiasi na kuishi bila mahitaji ya msingi kwa sababu hakuna pesa ya kutosha kwenye hazina kusaidia idadi ya watenda kazi wanaopaswa kuwa kwenye shamba la Bwana. Kungekuwa na pesa zaidi au ya kutosha katika hazina kama kila mtu angefanya kazi kwa kuzingatia maagizo ya Kristo: *"Mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, na anifuate Mathayo 16:24."*—**Letter 49, 1902.**{EVsw 90.1}

Epukeni Ubahili wa Kijinga (Uchoyo wa senti chache-chache wakati unaharibu kazi)

Lengo kuu linalopaswa kuwekwa mbele ya akili ni kwamba ninyi ni wanamatengenezo na, sio watu mliopitiliza katika maoni yetu- au mashupavu wenye ujinga (bigots). Katika kushughulika na wasioamini, msionyeshe roho ya kudharau na uchoyo, au ubahili wa kijinga, kwa kuwa mkibishania kiasi kidogo cha fedha, mwishowe mtapoteza kiasi kikubwa zaidi. Watasema, "Mtu huyu ni mjanja mno; atakuibia haki zako ikiwa ataweza, kwa hiyo kuwa makini unapofanya naye biashara." Lakini ikiwa katika makubaliano kidogo jambo linawekwa kwa faida ya mwingine, mtu huyo atafanya kazi nanyi kwa moyo huohuo wa ukarimu. Uchoyo huzaa uchoyo -ufinyu na ubahili, huzaa ufinyu na ubahili, na roho ya ufukara huzaa hali hiyo hiyo. Wale wanaofanya hivi hawaoni jinsi inavyodhalilisha mbele za wengine, hasa wale wasio wa imani yetu; na kazi ya thamani ya kweli huonekana kuwa na kasoro hii (usiwe mtu wa kufanya dili za kupunguza bei za vitu dukani, mpaka unawapunja watu ambao unajaribu kuwafikia, watakuona wewe ni mwenye tamaa na bahili tu, wala huna ujumbe wa uzima wa milele kwao!) —**Letter 14, 1887**. {EVsw 90.2}

Usimamizi wa Kibiashara wa Kampeni

Wahudumu Wasilemewe na Mambo ya Kibiashara — Kila mtu amepewa kazi yake. Wale wanaoingia katika huduma ya Injili wanashiriki katika kazi maalum, nao wanapaswa kujitoa kwa maombi na kwa kulihubiri Neno. Akili zao hazipaswi kulemewa na masuala ya kibiashara. Kwa miaka mingi Bwana ameniongoza kuwaonya ndugu zetu wahudumu wasiruhusu akili zao kuhenyeshwa mno na masuala ya biashara kiasi kwamba hawapati muda wa kuzungumza na **Mungu** na kuwa na ushirika na Roho. Mchungaji hawezi kudumisha hali bora ya kiroho iwapo anahitajika kila mara kutatua matatizo madogo madogo katika

makanisa mbalimbali. Hii si kazi aliyoitiwa Mchungaji. **Mungu** anataka kutumia kila kipawa cha wajumbe Wake aliowachugua. Akili zao hazipaswi kuchoshwa na mikutano mirefu ya kamati usiku, kwa kuwa **Mungu** anataka nguvu zao zote za kiakili zitumike katika kutangaza Injili kwa uwazi na kwa nguvu/msukumo, kama ilivyo katika Kristo Yesu.{EVsw 91.1}

Akiwa amelemewa, mhudumu mara nyingi huwa na haraka kiasi kwamba hawezi kupata muda wa kujichunguza mwenyewe kama yu katika imani. Anapata muda mchache sana wa kutafakari (Maandiko) na kuomba. Kristo katika huduma Yake alichanganya maombi na kazi. Aliutumia usiku baada ya 'usiku wote' katika maombi. Wahudumu ni lazima wamtafute **Mungu** ili wapate Roho Mtakatifu, ili waweze kuwasilisha ile Kweli kwa usahihi. — **Manuscript 127, 1902.** {EVsw 91.2}

Masuala ya Kibiashara Yabebwe na Watu Wenye Uwezo wa Kibiashara — Ni kosa kubwa kumweka mchungaji ambaye ana kipawa cha kuhubiri Injili katika shughuli za biashara kila wakati (business meeting-bajeti ya kanisa nk). Yeye anayehubiri Neno la uzima, hapaswi kuruhusu mizigo mingi kuwekwa juu yake…...{EVsw 91.3}

Fedha za kazi hii ya **Mungu** zinapaswa kusimamiwa vizuri na watu walio na uwezo wa kibiashara (wahasibu, watunza hazina nk); lakini wahubiri na wainjilisti wamewekwa wakfu kwa ajili ya kazi tofauti. Usimamizi wa masuala ya kifedha uachwe kwa watu wengine, si wale waliowekwa kwa kazi ya kuhubiri Injili. Wachungaji wetu hawapaswi kulemewa na masuala ya kibiashara/business yanayohusiana na kazi ya kiInjilisti katika miji mikubwa. Wale wanaosimamia mikutano ya mashauri yetu wanapaswa kuwatafuta watu wa biashara/business waangalie masuala ya kifedha ya kazi ya mijini. Ikiwa watu wa aina hiyo hawapatikani, basi kuwe na mpango wa kuwaandaa watu watakaobeba mizigo hiyo. — **Review and Herald, Oktoba 5, 1905.**{EVsw 92.1}

SEHEMU YA 5—KUANDAA MIKUTANO YA KIINJILISTI

Mbinu na Mpangilio wa Kazi

Kazi Kubwa Kwa Mbinu Rahisi

Sifa kuu ya kazi za **Mungu** ni kufanikisha kazi kubwa zaidi inayoweza kufanywa duniani kwa mbinu rahisi mno. Huu ni mpango wa **Mungu** kwamba kila sehemu ya utawala (serikali) Yake iungane na kila sehemu nyingine, kama gurudumu ndani ya gurudumu, ikifanya kazi kwa maelewemo/umoja kamili. **Mungu** hugusa moyo nguvu za watu, na Roho Yake hugusa nyuzi zisizoonekana, na mdundo wake hupitishwa hadi mwisho wa sayari zote. **—Manuscript 22, 1897.**{EVsw 93.1}

Mafanikio Ni Matokeo ya Mpangilio na Ushirikiano wa Amani

Mungu ni **Mungu** wa mpangilio. Kila jambo linalohusiana na mbingu lina utaratibu mkamilifu; utii na nidhamu ya kina vinatawala mienendo ya jeshi la malaika. Mafanikio hayawezi kupatikana ila kwa utaratibu na ushirikiano wenye maelewano. **Mungu** anahitaji utaratibu na mpango katika kazi Yake sasa kama alivyohitaji katika siku za Israeli. Wote wanaomfanyia kazi Yeye wanapaswa kufanya hivyo kwa akili mahiri, na sio kwa uzembe au kwa namna isiyo na mpangilio. Yeye hutaka kazi Yake ifanywe kwa imani na kwa usahihi, ili aweze kuiwekea muhuri wa idhini Yake hiyo kazi. **—Patriarchs and Prophets, 376 (1890).** {EVsw 93.2}

Kufuata Mpango Uliopangwa [Angalizo: —Haja na faida za kuwa na mpangilio wa kina zimeelezwa hapa kupitia kauli mbalimbali, baadhi zikiwa zimeelekezwa kwa wasimamizi wa taasisi. Hata hivyo, kanuni hizi zinahusu kila aina ya kazi, na kwa sababu hiyo, zina uhalali wa kujumuishwa hapa. —Wachapishaji].{EVsw 94.1}

Ni muhimu kufanya kazi kwa mpangilio, ukifuata mpango uliopangwa na lengo dhahiri. Hakuna mtu anayeweza kumfundisha mwenzake ipasavyo isipokuwa ameona kwamba kazi itafanywa kwa mfumo na kwa mpangilio, ili ifanyike kwa wakati unaostahili…...{EVsw 94.1}

Wakati mipango iliyo wazi inapaswa kuwasilishwa kwa wale wote wanaohusika, na kuhakikisha kwamba wote wameielewa, watu wote walioko juu ya idara mbalimbali wanapaswa kushirikiana kutekeleza mipango hii. Ikiwa njia hii thabiti itafuatwa kwa moyo na nia njema, itazuia kazi nyingi kufanywa bila lengo dhahiri na migongano isiyo na maana. —**Manuscript 24, 1887.**{EVsw 94.2}

Mipango Iliyofahamika Vizuri

Kazi unayojishughulisha nayo haiwezi kufanyika isipokuwa kwa nguvu zinazotokana na mipango iliyofahamika vizuri. **—Letter 14, 1887.**{EVsw 94.3}

Kutafakari na maono ya Mbele, Mpangilio na Maombi

Ni dhambi kuwa mzembe, mtu usiyejali, asiye na lengo au mgeni katika kazi yoyote tunayojihusisha nayo, hasa katika kazi ya **Mungu**. Kila juhudi inayohusiana na kazi Yake inapaswa kuendeshwa kwa mpangilio, maono, na maombi ya dhati. —**The Review and Herald, Machi 18, 1884.** {EVsw 94.4}

Ukamilifu na Haraka

Itakuwa rahisi kufanya makosa makubwa ikiwa kazi haitafuatiliwa kwa umakini na kwa tahadhari. Ingawa mtendakazi mgeni anayeanza kujifunza kazi au mwajiriwa aliye mafunzoni, kama hakuna mtu wa kuzisimamia idara mbalimbali, mtu aliyehitimu kwa kazi yake, kutakuwa na kushindwa kwa kazi nyingi tofauti-tofauti. Kazi inapoendelea, haitakuwa rahisi hata mara moja kucheleweshe kazi kutoka tarehe moja hadi nyingine. Kile ambacho hakifanyiki kwa wakati, iwe katika mambo ya kiroho au ya kidunia, kina hatari kubwa ya kutofanyika kabisa; kwa hali yoyote, kazi hiyo haiwezi kufanyika vizuri kama ilivyopaswa kwa wakati unaostahili. **—Manuscript 24, 1887.**{EVsw 94.5}

Kila Mtu Katika Sehemu Yake Sahihi

Kwa kila mtu **Mungu** amempatia kazi yake, kulingana na uwezo na vipaji vyake. Mipango ya busara inahitajika kumweka kila mmoja sehemu yake sahihi katika kazi, ili apate uzoefu utakaomtayarisha kubeba majukumu makubwa zaidi. —**Letter 45, 1889.**{EVsw 95.1}

Fanya Kazi Kama Jeshi lililo na Nidhamu

Tukumbuke kwamba sisi ni watendakazi pamoja na **Mungu**. Sisi hatuna hekima ya kufanya kazi peke yetu. **Mungu** ametufanya sisi kuwa wasimamizi (mawakili) Wake, kutujaribu kama alivyoijaribu Israeli ya zamani. Yeye Hataki jeshi Lake liwe na askari wasiokuwa na nidhamu, wasiosafishwa, wa hovyo, ambao hawatawakilisha vyema mpangilio na usafi Wake. —**The Review and Herald, Oktoba 8, 1901.** {EVsw 95.2}

Uwezo wa Kupanga na Kufanya Kazi

Uwezo wa ubunifu wa hali ya juu, na akili mahiri katika kupanga na kufanya kazi kwa mshikamano unahitajika (genius!) Tunataka wale watakaojitahidi si kwa faida zao tu, wakichukua kila walichoweza kwa kazi zao, bali watekeleze kazi kwa nia moja, kwa ajili ya utukufu wa **Mungu**, kwa ajili ya kuendeleza kazi kwa kasi katika nyanja mbalimbali. Hii ni nafasi adhimu ya kuonyesha kujitolea kwao katika kazi ya Bwana na uwezo wao kwa kazi hiyo. Kila mtu amepewa kazi yake, si kwa ajili ya kujitukuza mwenyewe, bali kwa utukufu wa **Mungu**. **—Manuscript 25, 1895.**{EVsw 95.3}

Mipango Busara Huokoa Kuhenyeka katika Kazi kwa Kupindukia

Nahitaji kuwahimiza watendakazi ni lazima wapangilie kazi zao ili wasichoke kwa kazi nyingi mno. — **Letter 17, 1902.** {EVsw 95.4}

Kikundi cha Uinjilisti

Uundaji wa Makundi unahitajika — **Mungu** anasema, "Ingieni mijini. Wape wakazi wa miji huo wito wa kujiandaa kwa ajili ya kuja kwa Bwana."…..{EVsw 96.1}

Wengi katika miji bado hawajapokea nuru ya ujumbe wa Injili. Wale wanaokiuka wajibu wa kueneza ujumbe wa mwisho wa onyo watajuta sana siku za usoni. Ujumbe wangu ni huu, "Waandae makundi ya watu ili waingie mijini. Tafuteni maeneo sahihi ya kufanyia mikutano. Sambaza maandiko yetu. Fanya jitihada za dhati kuwafikia watu." —**Letter 106, 1910.**{EVsw 96.2}

Jeshi la Watendakazi Kila Mji Mkubwa — Kila mji mkubwa kunapaswa kuwa na jeshi la watendakazi waliopangwa vizuri, wenye nidhamu; sio mtu mmoja au wawili tu, bali makundi mengi ya watu wafanye kazi....{EVsw 96.3}

Kila kundi la watendakazi liwe chini ya uongozi wa kiongozi mwenye uwezo, na wawe daima wakiwajibika kuwa watumishi wa **Mungu** kwa maana halisi ya neno hilo. Kazi hii inayopangwa kwa hekima italeta matunda mema. —**Medical Ministry, 300, 301 (1892).**{EVsw 96.4}

Vipaji Mbalimbali Vinahitajika — Bwana anataka miji ifanyiwe kazi kwa juhudi za pamoja za watendakazi wenye uwezo tofauti-tofauti. Wote wanapaswa kumwangalia Yesu ili awaongoze, wala wasitegemee hekima ya kibinadamu, ili wasipotezwe. —**Testimonies for the Church 9:109 (1909).**{EVsw 96.5}

Makundi Yaliyoandaliwa Vizuri — Makundi ya watu yanapaswa kuundwa na kufunzwa kwa kina ili wafanye kazi kama wauguzi, wainjilisti, wachungaji, (wahudumu wa Injili), wainjilisti wa kuuza vitabu, na wanafunzi wa Neno la **Mungu**, ili kukamilisha tabia kwa mfano wa **Mungu**. **—Testimonies For The Church 9:171, 172 (1909).**{EVsw 96.6}

Uongozi Huweka Mkao/Tuni ya Watu Kufanya Kazi — Hebu kila mtu afanye kazi ambaye anaweza kufanya kazi. Kiongozi mkuu mzuri si yule anayeweza kufanya kazi nyingi mwenyewe, bali ni yule anayeruhusu utendaji mkubwa zaidi kutoka kwa wengine, anagawa kazi-delegation. —**Letter 1, 1883.**{EVsw 96.7}

Umuhimu wa Ushauri wa Maombi

Kukabiliana na Changamoto kwa Ushauri na Maombi —Lazima kuwe na tahadhari fulani ya kuchukuliwa na uthubutu fulani kwa wale waliopo katika uwanja wa mapambano. Hawapaswi kila wakati kuhisi wanahitaji kupata maagizo kutoka makao makuu. Wanapaswa kufanya kwa juhudi zao zote chini ya hali yoyote, wakisaidiana kwa ushauri pamoja na maombi mengi ya dhati kwa **Mungu** kwa ajili ya kupokea hekima Yake. Lazima kuwe, maelewano na mshikamano katika jitihada. —**Letter 14, 1887.**{EVsw 97.4}

Mikutano ya Mara kwa Mara ya Ushauri — Katika kueneza ujumbe katika miji mikubwa, kuna aina nyingi za kazi zinazofanywa na watendakazi wenye vipaji mbalimbali. Wengine wanapaswa kufanya kazi kwa njia moja, wengine kwa njia nyingine... Kama watendakazi pamoja na **Mungu**, wanapaswa kutafuta kuungana kwa moyo mmoja. Inafaa kuwa na mikutano ya mara kwa mara ya ushauri, na ushirikiano wa dhati na wa moyo wote. Hata hivyo, wote wanapaswa kumtazama Yesu kwa ajili ya hekima, bila kutegemea wanadamu pekee kwa maelekezo. **— Testimonies For The Church 9:109 (1909).**{EVsw 97.2}

Ndugu Waombe Ushauri kwa Ndugu — Kama watendakazi tunahitaji kushauriana pamoja kuhusu masuala magumu. Ni sahihi kwa ndugu kumshauri ndugu mwenzake. Na ni heshima yetu baada ya kufanya hivyo, kuungana kwa pamoja kwa sala na kuomba hekima na ushauri wa Kiungu. Lakini sauti moja ya binadamu kuwa ndio mamlaka/nguvu ya kuongoza ni kosa la kusikitisha. —**Letter 186, 1907.**{EVsw 97.3}

Mapungufu Yanayoonekana — Katika kazi ya watendakazi kunapaswa kuwepo ushauri wa pamoja. Hakuna mtu anayepaswa kuchukua maamuzi kwa akili yake pekee na kufanya kazi kwa mujibu wa mawazo yake binafsi, isipokuwa awe na hazina ya kuchota maarifa. Nimeonyeshwa kwamba usimamizi wa kazi haupaswi kuaminiwa mikononi mwa watu wasio na uzoefu. Wale ambao hawajapata uzoefu mpana hawapaswi kubeba majukumu makubwa, hata kama wao wanaweza kujiona wenye uwezo wa kufanya hivyo. Ndugu zao wanaweza kuona kasoro pale wao wenyewe wanapojiona wamekamilika. —**The Review and Herald, Desemba 8, 1885.**{EVsw 97.4}

Wachungaji Kuwa na Muda wa Kuomba — Nimehamasika kuita watu wetu kufanya juhudi zote kuokoa roho. Tunahitaji imani inayoongezeka. Mioyo ya washiriki wa kanisa letu inapaswa kuelekezwa kwenye maombi kwa ajili ya wale wanaohubiri Injili. Na wachungaji wanapaswa kuwa na muda wa maombi kwa ajili yao wenyewe na kwa ajili ya watu wa **Mungu** walioteuliwa kuhudumu. —**Letter 49, 1903.**{EVsw 98.1}

Muda wa Maombi Unaleta Faraja — Kama watendakazi, hebu tumtafute Bwana kwa pamoja. Kwa nguvu zetu wenyewe hatuwezi kufanya lolote; lakini kupitia Kristo tunaweza kufanya mambo yote. **Mungu** anakusudia tuwe msaada na baraka kwa kila mmoja, na tuwe na nguvu katika Bwana na katika uwezo wa nguvu Zake…... **Mungu** anaishi na kutawala; Naye Atatupa msaada wote tunao hitaji. Ni neema na heshima kubwa kila wakati kupata nguvu na faraja kutoka kwa ahadi Yake takatifu, “Neema Yangu inatosha kwako.”— **Historical Sketches, p. 129. (1886).** {EVsw 98.2}

Umoja Katika Utofauti

Mpango wa Mungu Katika Tofauti ya Karama — Katika mipango yote ya Bwana, hakuna kitu kizuri zaidi kuliko mpango Wake wa kuwapa wanaume na wanawake karama mbalimbali. Kanisa ni bustani Yake, iliyopambwa na aina mbalimbali za miti, mimea, na maua. Yeye Hatarajii kwamba mti wa hisopou iwe kama

mwerezi mkubwa, wala mzeituni kufikia kimo cha mtende mrefu. Wengi wamepokea mafunzo machache ya kiroho na kielimu, lakini **Mungu** anao mpango-kazi kwa ajili ya kundi hili iwapo watatenda kazi kwa unyenyekevu, wakimtegemea Yeye. —**Letter 122, 1902.**{EVsw 98.3}

Tabia zipo Tofauti Kama Maua — Kutokana na wingi wa aina za mimea na maua, tunaweza kujifunza somo muhimu. Sio maua yote yana umbo au rangi sawa. Baadhi yana nguvu ya kuponya. Baadhi yanatoa harufu nzuri daima. Kuna Wakristo wa jina tu wanaofikiri ni wajibu wao kumfanya kila Mkristo awe kama wao. Huu ni mpango wa mwanadamu, si wa **Mungu**. Katika kanisa la **Mungu** kuna nafasi kwa ajili ya tabia mbalimbali kama ilivyo kwa maua katika bustani. Katika bustani Yake ya kiroho kuna aina nyingi za maua. —**Letter 95, 1902.**{EVsw 99.1}

Tofauti za Mawazo na Nia/Akili — Ingawa tuna mawazo na nia/akili tofauti, kuna somo moja linalopaswa kutuunganisha mioyo—kuwaongoa watu waifuate ileKweli, jambo ambalo linawavuta wote msalabani. — **Letter 31, 1892.** {EVsw 99.2}

Karama Maalum kwa Kazi Maalum — Mtendakazi mmoja anaweza kuwa mzungumzaji hodari; mwingine mwandishi mzuri; mwingine anaweza kuwa na kipawa cha maombi ya dhati, na bidii; mwingine anaweza kuwa na kipawa cha uimbaji; mwingine anaweza kuwa na uwezo wa pekee wa kufafanua Neno la **Mungu** kwa uwazi. Na kila karama inapaswa kuwa nguvu kwa ajili ya **Mungu**, kwa sababu Yeye anafanya kazi pamoja na mtendakazi. **Mungu** humpa mmoja Neno la hekima, mwingine maarifa, mwingine imani; lakini wote wanapaswa kufanya kazi chini ya Kiongozi mmoja. Tofauti ya karama hupelekea tofauti ya huduma; lakini "ni **Mungu** YuleYule atendaye yote katika wote." — **1 Wakorintho 12:6.** {EVsw 99.3}

Bwana anataka watumishi Wake walioteuliwa wajifunze kushirikiana kwa juhudi za pamoja na kwa maelewano. Huenda kwa baadhi, tofauti ya karama kati yao na wenzao ikaonekana kuwa kubwa mno kiasi cha kutoweza kushirikiana kwa maelewano; lakini wakikumbuka kwamba kuna akili tofauti-tofauti zinazopaswa kufikiwa, na kwamba baadhi watakataa Kweli ikiwakilishwa na mmoja, lakini wataifungua mioyo yao kwa ile Kweli ya **Mungu** ikiwakilishwa kwa namna tofauti na mtendakazi mwingine, basi watatamani kwa matumaini kufanya kazi kwa umoja. Karama zao, ingawa tofauti, zinaweza kuwa chini ya udhibiti wa Roho Mmoja. Katika kila neno na tendo, wema na upendo vitaonekana; na kila mtendakazi anapojaza nafasi yake kwa uaminifu, ombi la Kristo kwa ajili ya umoja wa wafuasi Wake litajibiwa, na dunia itajua kuwa hawa ni wanafunzi Wake…..{EVsw 99.4}

Watendakazi katika miji mikubwa lazima watimize majukumu yao mbalimbali, wakifanya kila jitihada kupata matokeo bora. Wanapaswa kuzungumza kwa imani na kutenda kwa njia itakayogusa watu. Wasiifinyange kazi kulingana na maoni yao finyu na binafsi. Huko nyuma, tumefanya hivyo sana kama watu, na hilo limekuwa kikwazo kwa mafanikio ya kazi. Tukumbuke kuwa Bwana ana njia tofauti za kufanya kazi, na ana watendakazi tofauti anaowawezesha kwa karama tofauti. **—Testimonies for the Church 9:144-146 (1909).** {EVsw 100:1}

Juhudi za Shetani za Kuwagawanya Watendakazi — Tunapoanza kazi hai ya moja kwa moja kwa ajili ya makundi makubwa katika miji, adui atafanya kazi kwa nguvu kuleta mkanganyiko, akitumaini kuharibu vikosi vya kazi. Baadhi ambao hawajabadilishwa kikamilifu, wako katika hatari ya kuchukua maoni ya adui kuwa ndiyo uongozi wa Roho wa **Mungu**. Kwa kuwa Bwana ametupa nuru, hebu na tutembee katika nuru hiyo. — **Manuscript 13, 1910.** {EVsw 100:2}

Jihadharini na Mipango ya Shetani — Sio wote wanaoshiriki kazi watakuwa na hulka na haiba sawa. Hawatakuwa watu wa elimu au mafunzo sawa, na kwa hakika watatenda kwa njia zinazokinzana kwa kadri wanavyotofautiana kwa tabia, isipokuwa tu wawe watu waliobadilishwa (wanaoongoka) kila siku.{EVsw 100:3}

Kila siku Shetani ana mipango yake ya kuitekeleza—mipango fulani ambayo itaziba njia ya wale wanaoshuhudia kwa niaba ya Yesu Kristo. Iwapo mawakala wa **Mungu** walio hai hawatakuwa wanyenyekevu, wapole, na wenye moyo mnyofu kwa kujifunza kutoka kwa Yesu, wataanguka kwenye majaribu kwa hakika; kwa maana Shetani ni mwerevu na mwenye ujanja, na ikiwa watendakazi hawatakuwa watu wa maombi, watanaswa bila kujua. Adui anajitokeza kama mwizi usiku na kuwafanya mateka. Kisha hufanya kazi juu ya akili za watu binafsi kupotosha mawazo yao na kupanga mipango yao; na ndugu wakiona hatari na kuitaja, wanahisi kuwa wamekosewa binafsi, kana kwamba mtu anajaribu kudhoofisha ushawishi wao. Mmoja huvutwa upande huu, na mwingine upande mwingine kabisa.{EVsw 101:1}

Kazi imefungwa, hatua potofu zimechukuliwa, na Shetani amefurahi. Kama nafsi isingelindwa mno na kutunzwa kwa hofu ya kupoteza hadhi yake ya asili, Bwana angeweza kutumia tabia hizo tofauti kufanya kazi nzuri na kubwa zaidi; kwa maana katika tofauti zao za karama, lakini umoja ndani ya Kristo, ndimo kulikuwapo nguvu ya matumizi yao. Kama matawi mbalimbali ya mzabibu yanavyounganishwa katika shina, yote yangetoa matunda matamu na ya thamani. Kungekuwa na maelewano kamili katika utofauti wao, kwa kuwa wanashiriki lishe na nguvu ya mzabibu.**{EVsw 101:2}**

Bwana hafurahii ukosefu wa maelewano ambao umekuwepo kati ya watendakazi. Yeye Hawezi kuwapa Roho Wake Mtakatifu, kwa kuwa wamejikita katika kutaka njia zao wenyewe, ilhali Bwana anawaonyesha njia Yake. Shetani na washirika wake wataleta hali ya kukatisha tamaa, lakini "nyote ni ndugu," na ni kosa mbele za **Mungu** mnaporuhusu tabia zenu binafsi ambazo hazijatakaswa kutumika kama chombo cha kuvunja moyo kwa mwingine. —**Letter 31, 1892. {EVsw 101:3}**

Shikamaneni, Shikamaneni — Kujipenda nafsi, kiburi, na kutegemea nafsi ndicho chanzo cha majaribu makubwa na migawanyiko mikubwa zaidi iliyowahi kuwepo katika ulimwengu wa dini. Mara kwa mara malaika ameniambia, "Shikamaneni, shikamaneni, muwe na nia moja, hukumu moja." (press together, Press together). Kristo Ndiye kiongozi, nanyi ni ndugu; mfuateni Yeye. —**Letter 4, 1890. {EVsw 102:1}**

Kugombania Ukuu — Tukifungamana kwa kuaminiana, katika vifungo vya upendo mtakatifu, ndugu anaweza kusaidiana na ndugu mwingine kwa kadiri ya uwezo wa kibinadamu…..**{EVsw 102:2}**

Kugombania ukuu kunaonyesha roho ambayo, ikiwa itahifadhiwa, mwishowe itawafungia nje wale waishikao roho hiyo wasiwe katika Ufalme wa **Mungu**. Amani ya Kristo haiwezi kukaa katika akili na moyo wa mtendakazi anayemkosoa na kumlaumu mtendakazi mwenzake kwa sababu tu mwingine hatumii njia ambazo yeye anaona ni bora, au kwa sababu anahisi hakuthaminiwa. Bwana hambariki kamwe mtu anayewakosoa na kuwashtaki ndugu zake, kwa kuwa hiyo ni kazi ya Shetani. —**Manuscript 21, 1894. {EVsw 102:3}**

Kuthamini Karama za Wengine — Ndugu zangu, jaribuni kuvaa nira ya Kristo. Shukeni kutoka kwenye vimo vyenu vya kiroho vya kujidai na mfundishe neema ya unyenyekevu. Wekeni mbali kila dhana mbaya, kushukiana, kusengenyana na muwe tayari kutambua thamani ya karama ambazo **Mungu** amewapa ndugu zenu. **—Letter 125, 1903. {EVsw 102:4}**

Hulka na Haiba Tofauti, Lakini Wamoja Katika Roho — Katika nyumba yetu hakuna mfarakano, wala maneno ya kutopatana na kukosa subira. Watendakazi wangu wako na tofauti kwa tabia, na njia zao na mienendo yao ni tofauti, lakini tunashirikiana kwa vitendo na kusimama tukiwa wamoja katika roho, tukitafuta kusaidiana na kuimarishana. Tunajua kuwa hatuwezi kumudu kuwa na mfarakano kwa sababu tu ya tofauti za hulka au haiba. Sisi ni watoto wadogo wa **Mungu**, nasi humwomba Atusaidie kuishi, si kwa ajili ya kujiridhisha wenyewe au kutimiza njia zetu binafsi, bali kumpendeza na kumtukuza Yeye. —**Letter 252, 1903**.**{EVsw 102:5}**

Kuruhusu Mbinu Zaidi ya Moja

(Tazama pia ukurasa wa 72–74: "Faida za Kufanya Kazi kwa Wawili.")

Vipawa Tofauti Vikijumuishwa

Katika ushirikiano wetu sisi kwa sisi, tukumbuke ya kuwa wote hatuna vipawa sawa wala tabia zinazofanana. Watenda kazi wanatofautiana kwa mipango na mitazamo yao. Kwa hiyo, mchanganyiko wa vipawa mbalimbali ni wa lazima ili kazi ifanikishwe. Tukumbuke kuwa kuna wengine wanaoweza kutekeleza majukumu fulani kwa ufanisi zaidi kuliko wenzao. Mtendakazi aliyepewa busara, stadi na uwezo kwa kazi maalum asiwalaumu wengine kwa kushindwa kufanya yale ambayo kwake ni rahisi. Je, si kweli kwamba kuna mambo ambayo wenzake wanaweza kuyatekeleza kwa mafanikio zaidi kuliko yeye? **{EVsw 103:1}**

Vipawa vyote ambavyo Bwana amevikabidhi kwa watumishi Wake ni vya thamani katika kazi Yake. Sehemu mbalimbali za kazi lazima ziunganishwe kwa utaratibu, kipande na kipande, hadi kuunda kazi kamilifu. Sehemu za jengo haziwezi kuwa sawa, wala hazitengenezwi kwa namna moja. Vivyo hivyo, mistari ya kazi ya **Mungu** haifanani yote, wala haipaswi kufuatwa kwa mtindo mmoja. — **Letter 116, 1903.{EVsw 103:2}**

Upungufu wa Kipawa cha Mtu Mmoja

Asiwepo mtu yeyote wa kudhani kwamba kipawa chake pekee kinatosha kwa kazi ya **Mungu**; kwamba anaweza peke yake kuendesha mfululizo wa mikutano na kuikamilisha kazi kwa ukamilifu. Njia zake huenda zikawa nzuri, lakini vipawa mbalimbali ni vya lazima. Mawazo ya mtu mmoja hayatakiwi kuwa kigezo cha sura ya kazi yote. Ili kazi ijengwe imara na kwa uwiano kamili, kuna haja ya vipawa mbalimbali na vitendea kazi tofauti, vyote vikiongozwa na Bwana. Yeye huwapa watenda kazi maagizo kulingana na uwezo wao. Ushirikiano na umoja ni vipengele vya lazima ili kazi iendelee kwa amani na mafanikio, kila mmoja akitimiza sehemu aliyokabidhiwa na **Mungu**, akijaza mapungufu ya mwingine. Mtendakazi mmoja akiachwa peke yake, huwa katika hatari ya kudhani kwamba kipawa chake kinatosha kwa kila jambo, na kufanya mambo yawe kamili.{EVsw 104:1}

Popote pale ambapo watendakazi wanaungana kwa kazi, wana nafasi ya kushauriana, kuomba pamoja, na kushirikiana kwa moyo mmoja. Hakuna anayepaswa kufikiri ni lazima ajitenge kwa sababu wenzake hawafuati njia ile ile kama yake. — **Special Testimonies, Series A, No. 7, pp. 14, 15. (1874).**{EVsw 104:2}

Pale Ambapo Mmoja ni Dhoofu, Mwingine Imara

Bwana huwainua wachungaji wa aina mbalimbali, ili walilishe kundi Lake kwa chakula kiwafaacho. Watatufunulia ile Kweli katika maeneo ambayo wenzao hawakuyaona kuwa ni ya msingi. Kama kazi ya kuwahudumia watu ingeachiwa kwa mtu mmoja tu, kungekuwepo na mapungufu makubwa. Kwa hekima Yake, Bwana huwatuma watenda kazi wa namna mbalimbali. Mmoja akiwa hodari katika jambo fulani la msingi, mwingine anaweza kuwa dhaifu katika hilo. — **Manuscript 21, 1894.**{EVsw 104:3}

Msizuie Mwendo wa Kazi-Usishike gurudumu na kulifanya lisiende!

Kuna watu ambao hawakui pamoja na kazi, bali huiacha ikiwapita kwa mbali. Wale wasiotambua wala kuendana na mahitaji yanayoongezeka ya kazi ya **Mungu** hawapaswi kusimama kama kikwazo katika gurudumu la kazi, wakizuia maendeleo ya wengine. — **Letter 45, 1889.** {EVsw 104:4}

Mbinu Ziboreshwe

Hakuna mbinu za kazi zisizobadilika zinazopaswa kukaa hapo tu; kazi yetu ni endelevu, na ni lazima pawe na nafasi ya kuboresha mbinu mbalimbali. Lakini chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu, umoja lazima utunzwe. — **Review and Herald, Julai 23, 1895.**{EVsw 105:1}

Mbinu Tofauti na za Zamani

Njia mbalimbali zitabuniwa ili kufikia mioyo ya watu. Baadhi ya mbinu zitakazotumika zitakuwa tofauti na zile zilizotumika zamani, lakini tusiruhusu hali hiyo iwe sababu ya kuzuia kazi kwa njia ya lawama na ukosoaji. **— Review and Herald, September 30, 1902.**{EVsw 105:2}

Uhai Mpya Katika Mbinu za Kale

Watu wanaohitajiwa ni wale wanaomwomba **Mungu** kwa ajili ya hekima, na ambao, chini ya uongozi wa **Mungu**, wanaweza kuingiza uhai mpya katika mbinu zilizokuwepo, na kuvumbua njia mpya za kuwafanya washiriki wa kanisa na watu wa ulimwengu wazinduke, na wafikiwe. — **Manuscript 117, 1907.**{EVsw 105:3}

Kumwekea Mungu Mipaka Kupitia Mpango wa Kazi Moja

Mpango wowote unaomweka mtu mmoja kama kitovu na mfano wa kuigwa hauwezi kutekelezwa na yeye au mwingine yeyote. Hii siyo njia ya **Mungu**. Mtu anapodhani kuwa ni akili yake tu inayostahili kupanga hatua kubwa za kazi ya **Mungu**, na kuwa uwezo wake tu ndiyo unaweza kufanikisha yote, huwa anaweka mipaka kwa nguvu ya **Mungu** kutimiza makusudi Yake duniani. {EVsw 105:4}

Mungu anahitaji wanaume na wanawake watakaofanya kazi kwa usahili na unyenyekevu wa Kristo, ili kuifikisha Kweli kwa wale wanaohitaji nguvu yake ya kukomboa. Lakini pale inapobainishwa njia moja tu mahsusi ya namna fulani, ndiyo itumike na watendakazi katika kutoa ujumbe wa injili, basi mpaka huwekwa, unaofanya watenda kazi wengi wasiweze kunufaisha wanadamu au kazi ya Mungu. — **Letter 404, 1907.**{EVsw 105:4}

Epuka Kuingia katika Mfumo Uleule au shimo lile lile (avoid a rut)

Watumishi wa **Mungu** wanapaswa kuwa watu wa vipawa mbalimbali, wenye upeo mpana wa tabia. Wasizame katika mfumo mmoja wa kufikiri au kufanya kazi, wasiingie kwenye shimo na kujificha humo (rut), bali wawe tayari kubadilika kulingana na aina ya watu wanaohudumiwa na hali waliyomo-wasiwe na unyanyapaa. — **Letter 12, 1887.**{EVsw 106:1}

Mbinu Iamuliwe Kulingana na Aina ya Watu

Tusisahau kwamba mbinu tofauti zinapaswa kutumika ili kuwakomboa watu wa aina mbalimbali. — **Review and Herald, April 14, 1903.**{EVsw 106:2}

Umepewa eneo gumu la kazi, lakini Injili ni nguvu ya **Mungu**. Aina ya watu unaokutana nao ndio wataamua njia unayopaswa kuitumia katika kazi hiyo. — **Letter 97a, 1901.**{EVsw 106:3}

Msiharibu Kazi ya Wengine-Msiisambaratishe

Kumbukeni kuwa sisi ni watenda kazi pamoja na **Mungu**. Yeye Ndiye mtekelezaji mkuu. Watumishi Wake ni vyombo Vyake. Wasivurugane kila mmoja akijiongoza kwa maoni yake binafsi, bali washirikiane kwa upole, maelewano kimkakati, kwa heshima na upendo wa kindugu. Asiwepo mwenye maneno ya ukali, ukosoaji au anayevuruga kazi ya mwingine. Wote wafanye kazi kwa pamoja, wakiwa na lengo moja. — **Review and Herald, Desemba 11, 1900.**{EVsw 106:4}

Onyo kwa Watumishi Wenye Uzoefu

Nimeamriwa kuwaambia ndugu zangu wazee-mliozeeka: tembeeni kwa unyenyekevu pamoja na **Mungu**. Msiwe washtaki wa ndugu zenu. Fanyeni kazi mliyopewa chini ya uongozi wa **Mungu** wa Israeli. Jaribu la kukosoa wengine ni mtego mkubwa kwa wengi. Ndugu wale mnaowatamani kuwalaumu wamekabidhiwa majukumu ambayo ninyi hamwezi kuyabeba. Lakini mnaweza kuwasaidia. Mnaweza kufanya huduma kubwa kwa ajili ya kazi ya **Mungu** kwa kuwasilisha uzoefu wenu wa kale katika kazi pamoja na wengine. Bwana hajamkabidhi yeyote kazi ya kusahihisha na kulaumu ndugu zake…...{EVsw 106:5}

Tembeeni pamoja na ndugu zenu katika kumjua Bwana. Wahurumieni wale wanaobeba mizigo mizito, na watieni moyo kila mnapopata nafasi. Sauti zenu zisikike katika umoja, si katika migawanyiko. — **Letter 204, 1907.** {EVsw 107:1}

Shule ya Mafunzo ya Kazi ya Injili Katika Miji

Kuweka Msingi wa Huduma

Kabla ya mtu kujiandaa kuwa mwalimu wa Kweli kwa wale walio gizani, ni lazima kwanza awe mwanafunzi.... Kila mara panapopangwa jitihada maalum (efoti) katika eneo muhimu, ni lazima kuwe na mpango ulioandaliwa vizuri wa kazi, ili wale wanaotamani kuwa wauzaji (wainjilisti) wa vitabu (colporteurs) na wale walio na kipawa cha kutoa mafundisho ya Biblia majumbani, waweze kupatiwa mafunzo stahiki…...{EVsw 107:2}

Ni vyema wahusiane na shule za mafunzo kwa ajili ya utume wetu, kwa ajili ya wale wanaojitayarisha kuyafikia maeneo kama watenda kazi. Wajisikie kuwa wao ni wanafunzi wanaojifunza kazi ya kuwavuta watu kwa Kristo. Shughuli katika shule hizi zinapaswa kuwa za aina mbalimbali. Kujifunza Biblia kunapaswa kupewa kipaumbele cha kwanza, na wakati huo huo kuwe na mafunzo ya mpangilio kwa ajili ya akili na tabia, ili wajifunze namna bora ya kuwafikia watu. Wote wanapaswa kujifunza namna ya kufanya kazi kwa werevu, kwa adabu, uungwana, staha na kwa Roho wa Kristo. — **Review and Herald, June 14, 1887.** {EVsw 107:3}

Kuwafundisha Watenda Kazi Wakati wa Mikutano ya Injili

Kazi iliyo na uwiano mzuri inaweza kufanyika kwa mafanikio zaidi mijini wakati shule ya Biblia kwa ajili ya mafunzo ya watenda kazi inaendelea sambamba na mikutano ya hadhara. Shule hii ya mafunzo au utume wa mjini inapaswa kuhusisha watenda kazi waliobobea, waliokomaa kiroho kwa kina, ambao wanaweza kutoa mafundisho ya kila siku kwa wale wanaofanya kazi ya Biblia, na pia kushiriki kikamilifu

katika jitihada za umma (efoti-uinjilisti wa hadhara). Wakati wanaume na wanawake wanapobadilishwa na kuukubali Ukweli, viongozi wa kazi hiyo ya utume, kwa maombi mengi, wanapaswa kuwaongoza waongofu hao wapya kuuruhusu uweza wa Kweli ndani ya mioyo yao. Kazi ya utume wa namna hiyo, ikiongozwa kwa hekima, itakuwa kama taa ing'aayo gizani. — **Gospel Workers, uk. 364-365.** {EVsw 108:1}

Shule ya Mafunzo Kwa Matendo

Ndugu na Dada Haskell wamepanga nyumba katika eneo bora la jiji, na wamekusanya watu wa kuwasaidia waliojiweka wakfu, ambao kila siku hutoka kwenda kutoa mafundisho ya Biblia, kuuza magazeti yetu, na kufanya kazi ya umishenari wa tiba. Wakati wa ibada, watendakazi hushirikiana kutoa ushuhuda wa matukio ya huduma yao. Mafundisho ya Biblia hufanyika kwa ratiba nyumbani, na vijana wanaoshiriki katika kazi hiyo ya utume hupatiwa mafunzo ya vitendo na ya kina kuhusu jinsi ya kuongoza masomo ya Biblia na jinsi ya kuuza machapisho yetu. Bwana amebariki kazi yao—wengine wameukubali Ukweli, na wengi wameonyesha kuvutiwa sana.....{EVsw 108:2}

Kazi ya aina hii inapaswa kufanyika katika miji mingi. Vijana wanaotumwa kufanya kazi mijini wanapaswa kuwa chini ya uongozi wa viongozi wenye uzoefu na waliotawaliwa na roho ya kujitoa. Hebu watendakazi wanapaswa kuwekewa makazi bora, ambapo wanaweza kupatiwa mafunzo kamili.{EVsw 108:3}

— Review and Herald, September 7, 1905

Kufanya Kazi na Mtu Mwenye Uzoefu

Mungu anawaita wahubiri, watendakazi wa Biblia, na wauzaji wa vitabu vya injili. Vijana wetu, wanaume kwa wanawake, waende wakifanya kazi ya Injili na ya Biblia, wakiandamana na mtumishi mwenye uzoefu ambaye anaweza kuwaonyesha njia ya kufanikisha huduma. — **Manuscript 71, 1903.** {EVsw 109:1}

Mbinu ya Kristo ya Kutoa Mafunzo

Katika ushirika wao na Mwalimu, wanafunzi walipokea mafunzo ya vitendo kwa ajili ya kazi ya umishenari. Waliona jinsi Alivyowasilisha Ukweli, na jinsi Alivyoshughulikia maswali magumu yaliyotokea katika huduma Yake. Waliona huduma Yake ya kuwaponya wagonjwa kila mahali Alipokwenda; walisikia Injili ikihubiriwa kwa maskini. Katika siku zetu, kutokana na kumbukumbu ya maisha Yake, wote tunapaswa kujifunza mbinu Zake za kufanya kazi. — **Letter 208a, 1902.** {EVsw 109:2}

Mafunzo Sahihi Huongeza Ufanisi

Mtumishi mmoja aliyefunzwa na kuelimishwa ipasavyo, na ambaye anatawaliwa na Roho wa Kristo, atafanya kazi yenye matokeo zaidi kuliko watumishi kumi waliokwenda bila maarifa ya kutosha, na dhaifu katika imani. Yule anayefanya kazi kwa mshikamano na ushauri wa **Mungu**, na kwa umoja na ndugu wengine, atakuwa na uwezo mkubwa na ufanisi wa kufanya mema kuliko watu kumi wasiotambua haja ya kumtegemea **Mungu** na kutenda kwa mpangilio wa kazi ya pamoja. **— Review and Herald, May 29, 1888.** {EVsw 109:3}

Kituo cha Mafunzo na Kazi ya Ufuatiliaji

Baada ya jamii kuguswa kwa njia ya mkutano mkubwa wa kambi ulioandaliwa kwa mpangilio mzuri, je, watenda kazi waondoke tu hivyo na kwenda mkutano mwingine na kuacha kazi hiyo ipotee? La! hasha. Hebu na wagawanye watenda kazi, na wengine waendelee sehemu hiyo kwa kutoa mafundisho ya Biblia, kufanya kazi ya kuuza vitabu vya injili, kuuza majarida, n.k. Hebu pawepo na nyumba ya misheni ya kuwaandaa watenda kazi kwa mafunzo ya kila aina ya kazi ya Injili. Hili litazuia kazi isiwe ya kupotea. Matokeo mazuri ambayo wajumbe wa **Mungu** wameacha mioyoni mwa watu hayatapotea.{EVsw 109:4}

Huduma hii ya nyumba kwa nyumba, ya kutafuta roho, kuwafuata kondoo waliopotea, ndiyo kazi muhimu sana inayoweza kufanywa. Watu sabini na tano wamepangwa na kuwa kanisa katika (organized church) -----. Tunamshukuru **Mungu** kwa hili. Hamsini kati yao wameukubali **Ukweli** tangu mkutano wa kambi. — **Letter 137, 1898.** {EVsw 110:1}

Kuamsha na Kuandaa Kanisa kwa Ajili ya Huduma

Kuhuisha Washiriki wa Kanisa — Bwana hafanyi kazi sasa ya kuzileta roho nyingi katika Kweli kwa sababu ya washiriki wa kanisa ambao hawajawahi kuongoka, na wale waliowahi kuongoka lakini sasa wamerudi nyuma. —**Testimonies For The Church 6:371 (1900).**{EVsw 110:2}

Roho Ishirini Badala ya Moja — Kuna takataka nyingi sana zinazoletwa mbele na wanaodai kumwamini Kristo, ambazo huzuia njia ya kuelekea msalabani. Licha ya haya yote, wako baadhi ambao wameshawishika kwa kina kiasi kwamba watapita katika kila hali ya kukatishwa tamaa na kushinda kila kizuizi ili waipate ile Kweli. Lakini kama wale waaminio Kweli wangalisafisha akili zao kwa kuitii, kama wangalitambua umuhimu wa maarifa na ustaarabu wa tabia katika kazi ya Kristo, mahali ambapo roho moja imeokolewa, roho ishirini zingeweza kuokolewa. —**Testimonies For The Church 4:68 (1876).**{EVsw 110:3}

Kuwafundisha Kwanza Washiriki wa Kanisa — Kuhusu kufanya kazi mahali ambapo tayari kuna waumini, mchungaji asilenge sana kuwaongoa wasioamini kwanza, bali afanye juhudi kuwaandaa washiriki wa kanisa kwa ushirikiano wa kukubalika. Hebu na awahudumie watu binafsi, akijitahidi kuwachochea watafute uzoefu wa kina zaidi wao wenyewe, na pia wafanye kazi kwa ajili ya wengine. Watakapokuwa tayari kumtegemeza mchungaji kwa maombi na kazi zao, mafanikio makubwa zaidi yataambatana na jitihada zake. — **Gospel Workers, 196 (1915).**{EVsw 110:4}

Kusafisha Njia ya Mfalme — Wakati juhudi maalum za kuokoa roho zinafanywa na watenda kazi wenye uzoefu katika jamii ambako watu wetu wanaishi, kuna wajibu mzito juu ya kila muumini katika eneo hilo kuhakikisha kwamba anaondoa kila dhambi inayoweza kumzuia kushirikiana na **Mungu** na ndugu zake katika kazi hiyo-kuweka njia kwenda ka mfalme wazi, kuondoa vikwazo vya kiroho- Isaya 40:3. **— The Review and Herald, Desember 6, 1906.**{EVsw 111:1}

Ushauri kwa Makanisa Ambapo mahubiri ya hadhara au Efoti zinafanyika — Takribani miaka minne iliyopita, wakati Mzee Haskell na wengine walikuwa wakifanya shule ya mafunzo ya Biblia na mikutano ya jioni katika jiji la New York, neno la Bwana kwa watendakazi lilikuwa: “Acha Waumini wanaoishi karibu na mahali ambapo mikutano inafanyika, washiriki mzigo wa kazi. Wajisikie kuwa ni wajibu, upendeleo na heshima kusaidia kufanikisha mikutano hiyo. **Mungu** hupendezwa na juhudi za kuwaweka kazini. Anataka kila mshiriki wa kanisa afanye kazi kama mkono Wake wa kusaidia, akitafuta kwa huduma ya upendo kuwaleta watu kwa Kristo.”…...{EVsw 111:2}

Na kwa kanisa la Los Angeles, zaidi ya mwaka mmoja uliopita, wakati Bwana alipokuwa akiwagusa watu sana kupitia mikutano ya kambi iliyokuwa ikiendelea, neno lilitumwa:

“Hebu kanisa la Los Angeles na liwe na vipindi maalum vya maombi kila siku kwa ajili ya kazi inayofanyika. Baraka ya Bwana itawajia washiriki wa kanisa wanaoshiriki hivyo, wakikusanyika kwa vikundi vidogo kila siku kuombea mafanikio ya kazi. Kwa njia hii, waumini watapata neema kwa ajili yao wenyewe, na kazi ya Bwana itasonga mbele.{EVsw 111:3}

“Hivi ndivyo tulivyokuwa tukifanya zamani. Tuliombea roho zetu wenyewe na wale waliokuwa wakifanya kazi. Bwana Yesu anatangaza kwamba wawili au watatu wakikusanyika kwa Jina Lake, Yeye Yuko katikati yao kuwatunuku baraka. Na kuwe na mazungumzo machache, na maombi ya kweli yenye bidii zaidi.{EVsw 112:1}

“Nina hofu kwamba juhudi zinazofanyika kutangaza Kweli huko Los Angeles hazitathaminiwa. Kila mmoja ajitokeze kumsaidia Bwana dhidi ya adui mkuu-Waamuzi 5:23-26. Mahali ambapo kazi maalum inafanyika, kama ilivyoonekana katika kazi ya kiinjilisti huko Los Angeles, kila mshiriki wa kanisa na amkaribie **Mungu**. Kila mmoja ajichunguze moyoni mwake kwa mwanga wa Neno. Ikiwa dhambi itagunduliwa, na ifanyiwe toba na ungamo. Hebu kila msaidizi awe katika hali nzuri ya kufanya kazi ya Mungu. Bwana atasikia na kujibu maombi. Wasidhani washiriki wa kanisa kwamba juhudi za kiinjilisti ni kwa ajili yao tu, bali wajiunge na kazi ya kuwaleta wale waliopuuzwa, wale ambao juhudi maalum hazijawahi kufanywa kwa ajili yao.{EVsw 112:2}

“Pale ambapo kazi kama hiyo imefanyika kama ilivyofanyika Los Angeles, washiriki wa kanisa na wasafishe njia ya Mfalme, na wasaidie kwa mali zao kazi inayoendelea-Isaya 40:3. Hebu waonyeshe kuwa wako katika umoja kamili. Wafike mikutanoni wakiwa wamejiandaa kwa huduma, tayari kuzungumza na yeyote anayevutiwa. Waombe na wafanye kazi kwa ajili ya kondoo waliopotea.” **— The Review and Herald, Desember 20, 1906.**{EVsw 112:3}

Mfano kwa Waongofu Wapya — Hebu washiriki wa zamani wa kanisa wawe mfano kwa wale waliokuja hivi karibuni katika Kweli. Naomba wale waliodumu katika Kweli kwa muda mrefu wasiwaumize waongofu wapya kwa maisha yasiyo ya kidini. Acheni kulalamika na fanyeni kazi ndani ya mioyo yenu. Lainisheni udongo mgumu wa mioyo yenu, kwa kuukatua vizuri na mtafute kujua mnachoweza kufanya ili kuendeleza kazi…….. (Hosea 10:12, Yeremia 4:3)**{EVsw 112:4}**

Amkeni, amkeni, na mtoe ushuhuda kwa wale wasioongoka kwamba mnaamini Kweli ya asili ya mbinguni. Msipoamka, dunia haitasadiki kuwa mnaishi kwa ile Kweli mnayodai kuiamini. — **Letter 75, 1905. {EVsw 113:1}**

Washiriki wa Kanisa Wasaidie — Bwana anataka juhudi binafsi kwa kiwango kikubwa zaidi zifanywe na washiriki wa makanisa yetu. Roho zimepuuzwa, miji na vijiji havijasikia ile Kweli ya wakati huu kwa sababu juhudi za utume zenye hekima hazijafanywa... Wachungaji wetu waliowekwa wakfu wafanye kilicho ndani ya uwezo wao, lakini si vema kutarajia mtu mmoja afanye kazi yote. Bwana amempa kila mtu kazi yake. Kuna kutembelea, kuna kuomba, kuna kutoa faraja; na uchaji—moyo na mkono—wa kanisa zima vinatakiwa kuwa kazini. Mnaweza kuketi na rafiki zenu, na kwa njia ya mazungumzo ya kirafiki, na kuzungumza kuhusu imani ya thamani ya Biblia. — **The Review and Herald, August 13, 1889.{EVsw 113:2}**

Wachungaji Walete Makanisa Katika Uinjilisti — Wakati mwingine wachungaji hufanya kazi nyingi kupita kiasi; wanajaribu kubeba kazi yote mikoni mwao wenyewe. Inawameza na kuwazuia kukua, wanakuwa mbilikimo; lakini wanaendelea kung'ang'ania kufanya kila kitu. Wanaonekana kufikiri kuwa wao peke yao ndio wanapaswa kufanya kazi ya **Mungu**, huku washiriki wa kanisa wakiwa hawafanyi chochote. Huu sio mpango wa **Mungu** hata kidogo. — **The Review and Herald, November 18, 1884. {EVsw 113:3}**

Nguvu ya Kazi, Inayojumisha Walei — Je, ndugu na dada zetu wanawezaje kuendelea kuishi karibu na watu wengi ambao hawajawahi kuonywa, bila hata kupanga mbinu za kuweka kazini kila chombo ambacho Bwana anaweza kukitumia kwa utukufu wa Jina Lake? Viongozi wetu walio na uzoefu mrefu wataelewa umuhimu wa mambo haya, na wanaweza kufanya mengi kuongeza nguvu ya kazi. Wanaweza kupanga kuwafikia wengi walioko njia kuu na pembezoni. Wanapoweka juhudi thabiti na za kujitoa kuwaelimisha washiriki wa kanisa kufanya kazi binafsi kwa ajili ya roho mahali popote ambapo kuna nafasi nzuri, mafanikio yataandamana na kazi yao. — **Manuscript 53, 1910. {EVsw 114:1}**

Mashamba Yaliyo Karibu Nanyi Yameiva — Kweli itashinda kwa ushindi mkuu na utukufu. Makanisa yaanze kazi ambayo Bwana amewapa—ya kufungua Maandiko kwa wale walio gizani. Ndugu na dada zangu, kuna roho katika jirani zenu ambao, kama wangetendewa kazi kwa busara, wangeongoka. Juhudi lazima zifanywe kwa ajili ya wale wasioelewa Neno. Hebu wale wanaodai kuamini Kweli na washiriki asili ya Kiungu, ndipo wataona kuwa mashamba yameiva kwa ajili ya kazi ambayo kila mmoja anaweza kufanya ikiwa roho zimeandaliwa kwa kuliishi Neno. **— Union Conference Record (Australasia), March 11, 1907. {EVsw 114:1}**

Kusambaza Machapisho ya Uinjilisti Nyumba kwa Nyumba — Ndugu na dada, je, mtaivaa silaha ya Kikristo? "Miguu yenu ikiwa imevishwa na utayari wa Injili ya amani," mtakuwa tayari kutembea nyumba kwa nyumba, mkiipeleka Kweli kwa watu. Wakati mwingine mtakutana na changamoto katika aina hii ya kazi; lakini mkisonga mbele kwa imani, Bwana atawatangulia, Naye ataangaza nuru Yake juu ya njia yenu. Mkitembelea majumbani mwa jirani zenu kwa kuuza au kugawa vitabu vyetu, na kwa unyenyekevu kuwafundisha ile Kweli, mtaandamana na nuru ya mbinguni, ambayo itakaa katika nyumba hizo. — **The Review and Herald, May 24, 1906.{EVsw 114:2}**

Kuandaliwa kwa Mipango kwa Kuweka Vikundi vya Kazi — Katika makanisa yetu, hebu na vianzishwe vikundi kwa ajili ya huduma. Katika kazi ya Bwana, hapapaswi kuwa na wavivu au watu wanaomangamanga bila kazi. Watu tofauti na waungane katika kazi kama wavuvi wa watu. Watafute kukusanya roho kutoka katika hali ya ufisadi wa dunia na kuwaingiza katika usafi wa upendo wa Kristo.**{EVsw 115:1}**

Kuundwa kwa vikundi vidogo kama msingi wa juhudi za Kikristo ni mpango ambao nimeonyeshwa na Yule asiyeweza kukosea. Ikiwa kuna idadi kubwa ya watukatika kanisa, basi washiriki waandaliwe kwa makundi madogo, kwa ajili ya kufanya kazi si tu kwa ajili ya washiriki wa kanisa bali pia kwa wasioamini. **— (Australasian) Union Conference Record, March 11, 1907.{EVsw 115:2}**

Kama Kikosi cha Askari Waliozoeshwa Vizuri — Wahudumu wanapaswa kupenda utaratibu, wajidhibiti wenyewe, ndipo wataweza kuwafundisha washiriki wa kanisa kufanya kazi kwa mshikamano, kama kikosi cha

askari kilichozoeshwa vizuri-nidhamu na kupigana. Kama nidhamu na utaratibu ni muhimu kwa mafanikio vitani, basi ni muhimu zaidi katika vita vya kiroho ambavyo tunashiriki, kwa sababu lengo lake ni la thamani kubwa na tukufu zaidi. Katika mapambano tunayopitia, masuala ya milele yako hatarini.{EVsw 115:3}

Malaika hufanya kazi kwa mshikamano-maelewano. Kila hatua yao inaongozwa na utaratibu mkamilifu. Kadiri tunavyowafuata kwa karibu katika mshikamano na utaratibu, ndivyo jitihada zao kwa ajili yetu zitakavyofaulu zaidi. **— Letter 32, 1892.** {EVsw 115:4}

Uhusiano wa Mwinjilisti na Mchungaji

Wainjilisti na Wachungaji Wanahitajika-Mungu anawaita wainjilisti. Mwinjilisti wa kweli ni mpenda roho za watu. Hutafuta na kuvua watu kwa ajili ya Kristo. Wachungaji pia wanahitajika —[Tazama pia uk. 345-351, "Uinjilisti wa Kichungaji."]—wachungaji waaminifu—ambao hawatapendelea watu wa **Mungu** kwa maneno matamu wala kuwatendea kwa ukatili, bali watawalisha kwa mkate wa uzima.{EVsw 116:1}

Kazi ya kila mtendakazi mwaminifu iko karibu sana na moyo wa Yeye aliyejitoa kwa ajili ya ukombozi wa jamii ya wanadamu. —**Letter 21, 1903.**{EVsw 116:1}

Mwinjilisti- Ambaye ni Mchungaji

Kwa kawaida mtu mmoja huhudumu katika kazi ambayo inapaswa kufanywa na watu wawili; kwani kazi ya mwinjilisti shurti iambatane na kazi ya mchungaji, na hivyo kuweka mzigo maradufu juu ya mtendakazi wa Injili. **—Testimonies For The Church 4:260 (1876).**{EVsw 116:3}

Imani kwa Mtendakazi Mpya

hebu Mtendakazi asihofu kwamba kwa sababu mtendakazi mpya ameletwa miongoni mwa watu, basi kazi aliyokuwa akiifanya itavurugika au kupoteza mvuto.{EVsw 116:4}

Acha kazi ya **Mungu** iwe mikononi mwa **Mungu-Ondoa mikono yako kwenye Sanduku la Agano**; Yeye Mwenyewe ataifanya kazi Yake na kuiendeleza. Nuru ya ziada itang'aa kupitia watu wanaotumwa na **Mungu**, ambao ni washiriki pamoja Naye. Watendakazi wa mwanzo wanapaswa kuwapokea kwa moyo safi wajumbe wa **Mungu**, kuwatendea kwa heshima, na kuwaalika washirikiane nao na kuongea na watu. **— Manuscript 21, 1894.** {EVsw 116:5}

Kujihadhari na Uratibu uliopitiliza, Uramsi au Mipango Iliyopitiliza

Kujongea, au harakati nyingi, sio lazima iwe uhai

Sio mafundisho sahihi ya kidhehebu, wala kuwa mshiriki wa kanisa, wala kutimiza kwa bidii majukumu ya kila siku, kunakothibitisha kuwa na uhai wa kiroho. Katika mnara wa kale huko Uswisi, niliona sanamu ya mtu iliyokuwa ikionekana kana kwamba ilikuwa hai. Ilionekana kama mtu aliye hai, na nilipokaribia nilinong'ona, ili kujua kama ingeweza kunisikia. Lakini ingawa ilionekana kuwa hai, haikuwa na uhai wa kweli. Ilikuwa inaendeshwa na mashine. {EVsw 116:6}

Harakati au kujongea kwa mwili si uhai. Tunaweza kupitia taratibu na ibada zote za kidini; lakini kama hatuishi ndani ya Kristo, kazi yetu haina thamani. Bwana anawaita WaKristo hai—wanaoamini, wanaotenda, na walio hai katika Kristo. —**Review and Herald, April 21, 1903.**{EVsw 117:1}

Kazi Inakuwa Ngumu kwa Ubunifu Usiokuwa wa Lazima

Watu hufanya kazi ya kusambaza Ukweli kuwa ngumu mara kumi kuliko ilivyo, kwa kujaribu kuingilia kazi ya **Mungu** na kuifanya kwa akili zao finyu. Hudhani kwamba lazima wabuni mbinu mpya kila mara za kuwalazimisha watu kufanya mambo wanayodhani wanapaswa kuyafanya. Wakati unaotumika hivyo huifanya kazi kuwa ngumu zaidi; kwa maana Mtendakazi Mkuu, yaani Kristo, amewekwa pembeni katika malezi ya urithi Wake. Watu hujitwika wajibu wa kurekebisha tabia za wengine, lakini huishia kuziharibu zaidi. Wangekuwa na busara zaidi kama wangeiachia kazi hiyo mikononi mwa **Mungu**, kwa maana Yeye hawaoni kuwa wao wana uwezo wa kuumba tabia mpya.…..{EVsw 117:2}

Badala ya kupoteza muda kwa kutengeneza sheria na kanuni, ni afadhali mngeomba na kusalimisha mapenzi yenu na njia zenu kwa Kristo. Hajafurahishwa pale mnapofanya kuwa ngumu kile ambacho Yeye amekifanya kuwa rahisi. {EVsw 117:3}

Yeye Anasema: "*Jitieni nira yangu, mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu*; **Mathayo 11:29**."

Bwana Yesu anapenda urithi Wake. Kama watu hawatajiona kuwa wao ni wasimamizi wa kipekee wa kuweka sheria kwa ajili ya wenzao, bali wataishi kwa kuiga maisha ya Kristo na kuleta sheria Zake maishani mwao, basi kila mmoja atakuwa mfano wa kuigwa, siyo hakimu. —**Manuscript 44, 1894.**{EVsw 117:3}

Kinyume na Mipango ya Kibinadamu

Ikiwa wale wanaoweza kusaidia katika kazi ya Bwana hawataamshwa wajue wajibu wao, hawatatambua kazi ya **Mungu** wakati sauti kuu ya malaika wa tatu itakaposikika. Wakati nuru itakapomulika ulimwengu mzima, badala ya kujiunga kusaidia kazi ya Bwana, baadhi yao watataka kuizuia ili iendane na mitazamo yao finyu. Nakuambia kwamba Bwana atafanya kazi hii ya mwisho kwa namna isiyo ya kawaida, na kwa njia zitakazokinzana na mipango ya kibinadamu. Kutakuwa na watu miongoni mwetu ambao siku zote watataka kuongoza kazi ya **Mungu**, hata kuamua hatua zipi zichukuliwe wakati kazi inasonga mbele chini ya uongozi wa malaika anayeungana na malaika wa tatu katika ujumbe unaotakiwa kutolewa kwa dunia. **Mungu** atatumia njia na vyombo vitakavyoonyesha wazi kuwa Yeye mwenyewe ndiye ameshika hatamu za kazi hii mikononi Mwake. Watendakazi watashangazwa na urahisi wa njia Atakazotumia kumalizia na kukamilisha kazi ya haki. —**Testimonies to Ministers and Gospel Workers, 300 (1885).**{EVsw 118:1}

SEHEMU YA 6—HUDUMA YA UINJILISTI WA HADHARA (EFOTI)

Ujumbe Wetu wa Ukweli wa Sasa

Kuyafikia Makundi Makubwa ya Watu

Tunapaswa kufanya juhudi za kuita makundi makubwa ya watu ili wasikie maneno ya mhubiri wa Injili. Nao wanaohubiri Neno la Bwana wanapaswa kusema Ukweli. Wanapaswa kuwaelekeza wasikilizaji wao, kana kwamba wapo miguuni pa Sinai, kusikia maneno yaliyosemwa na **Mungu** katikati ya mandhari ya adhama kuu ya kutisha. —**Letter 187, 1903.** {EVsw 119:1}

Mpiga Tarumbeta na Atoe Sauti Iliyo ya Hakika

Wale wanaowasilisha Ukweli hawapaswi kuingia katika mabishano au migogoro. Wanapaswa kuhubiri Injili kwa imani na bidii kubwa kiasi kwamba mvuto wa Kweli uamshwe. Kupitia maneno wanayosema, sala wanazotoa, na ushawishi wao, wanapaswa kupanda mbegu zitakazozaa matunda kwa utukufu wa **Mungu**. Asiwepo atakayekuwa na wasiwasi au kuyumba. Tarumbeta lazima itoe sauti iliyo ya hakika. Umakini wa watu unapaswa kuelekezwa kwa ujumbe wa malaika wa tatu. Watumishi wa **Mungu** wasiwe kama watu watembeao huku wamelala, bali kama wanaojiandaa kwa ajili ya kuja kwa Kristo. —**The Review and Herald, March 2, 1905.**{EVsw 119:2}

Kutangaza Ukweli Ndiyo Kazi Yetu

Kwa namna ya pekee, Waadventista wa Sabato wamewekwa ulimwenguni kama walinzi na wabeba nuru. Wamekabidhiwa onyo la mwisho kwa dunia inayopotea. Wanapaswa kuiangaza nuru ya ajabu kutoka katika Neno la **Mungu**. Wamepewa kazi iliyo adhimu, muhimu na nzito kupita zote—kutangaza ujumbe wa malaika wa kwanza, wa pili na wa tatu. Hakuna kazi nyingine iliyo ya muhimu zaidi ya hii. Hawapaswi kuruhusu jambo lolote lingine kutumia bongo zao au kuwanyang'anya usikivu wao.{EVsw 119:3}

.

Ukweli ulio wa adhimu na mzito zaidi kuwahi kukabidhiwa wanadamu umetolewa kwetu ili tuutangaze kwa dunia. Kutangaza Kweli hizi ndiyo kazi yetu. Dunia inapaswa kuonywa, na watu wa **Mungu** wanapaswa kuwa waaminifu, na wakweli kwa agizo walilopewa…..{EVsw 120:1}

Je, tutaingoja hukumu ya **Mungu** iwapate wavunjaji wa sheria kabla hatujawaambia jinsi ya kuiepuka? Je, imani yetu katika Neno la **Mungu** iko wapi? Je, ni lazima tuone mambo yaliyotabiriwa yakitimia kabla ya kuamini Alichosema? Katika miale ya wazi na ya dhahiri, nuru imetufikia, ikionyesha kuwa

siku kuu ya Bwana iko karibu sana, “naam imefika hata mlangoni.”—**Testimonies for the Church 9:19, 20 (1909).**{EVsw 120:2}

Tusiikose Alama/Dalili au Ishara hii-Hapana muda wa kupotezwa bure katika kazi hii kuu. Hatupaswi kukosa alama na hivyo kutenda dhambi. Muda ni mfupi sana kwa sisi kujaribu kufichua kila jambo ambalo lingeweza kufunguliwa na kuonekana machoni petu wenyewe. Umilele utahitajika ili tufahamu upana wote, urefu, kimo na kina cha Maandiko…..{EVsw 120:3}

Kwa mtume Yohana, akiwa katika kisiwa cha Patmo, yalifunuliwa mambo ambayo **Mungu** alitaka awape watu. Jifunzeni Mafunuo haya. Hapa kuna mada zinazostahili kutafakariwa, masomo mapana na ya kina ambayo majeshi yote ya malaika sasa wanatafuta kuyawasilisha. Angalieni maisha na tabia ya Kristo, na jifunzeni kazi Yake ya upatanisho. Hapa kuna hekima isiyo na mipaka, upendo usio na kifani, haki isiyo na mwisho, na rehema ya milele. Hapa kuna kina na kimo, urefu na upana kwa ajili ya tafakari yetu. Kalamu zisizo na idadi zimekuwa zikitumika kuwasilisha kwa dunia maisha, tabia, na kazi ya upatanisho ya Kristo; lakini kila akili ambayo Roho Mtakatifu amefanya kazi nayo imewasilisha mada hizi kwa nuru mpya na hai, kulingana na akili na roho ya mhusika wa kibinadamu…..{EVsw 120:4}

Tunahitaji Ukweli kama ulivyo katika Yesu; kwa maana tunatamani kuwasaidia watu waelewe Kristo ni nani kwao, na majukumu wanayoitwa kuyakubali ndani Yake. Kama wawakilishi na mashahidi Wake, tunahitaji kufikia uelewa kamili wa Kweli ya wokovu kwa njia ya maarifa yenye uzoefu. —**The Review and Herald, April 4, 1899.** {EVsw 121:1}

Kutilia Mkazo Kweli Maalum

Tunalo jukumu la kutangaza kwa uaminifu shauri lote la **Mungu**. Hatupaswi kupunguza umuhimu wa Kweli maalum zilizotutenga na dunia, na kutufanya tuwe jinsi tulivyo; kwa kuwa Kweli hizi zina uzito wa milele. **Mungu** ametupa nuru kuhusu mambo yanayotokea sasa katika kipindi cha mwisho wa wakati uliosalia, na kwa kalamu na kwa sauti tunapaswa kuutangazia ulimwengu Ukweli huo, sio kwa kuwa waoga, tuanonyata na kunyamaza kimya (tame) bila ujasiri au uchangamfu, bali kwa maelekezo ya Roho na uwezo wa **Mungu**. —**Testimonies to Ministers and Gospel Workers, uk. 470 (1890).** {EVsw 121:2}

Ujumbe wa Kiadventista

Katika wakati huu, ambapo mwisho uko karibu sana, je, tutafanana sana na dunia katika mwenendo wetu kiasi kwamba watu wasiweze tena kuwaona watu wa **Mungu** walioitwa kwa jina Lake? Je, kuna mtu yeyote atakayekuwa tayari kuuza sifa zetu za kipekee kama watu walioteuliwa na **Mungu** kwa ajili ya faida zozote za kidunia? Je, kibali cha wale wavunjao sheria ya **Mungu** kinaweza kuonekana kuwa na thamani kuu? Je, watu ambao Bwana amewaita Wake wataweza kufikiri kuwa kuna mamlaka yoyote iliyo kuu kuliko “MIMI NIKO”? Je, tutajaribu kufuta vipengele vya imani vinavyotutambulisha sisi kama Waadventista wa Sabato? {EVsw 121:3}

Usalama wetu pekee ni kusimama daima katika nuru ya uso wa **Mungu**. —**Manuscript 84, 1905.**{EVsw 121:4}

Ujumbe wa Ukweli wa Sasa uliochangamka

Sasa, hivi sasa, tunapaswa kutangaza Ukweli wa sasa kwa hakika na kwa nguvu. Msitoe sauti ya huzuni; msiiimbe nyimbo za mazishi. —**Letter 311, 1905.**{EVsw 122:1}

Kusadikishwa kwa Uzito wa Ushahidi

Mungu anawasilisha katika akili za watu vito vya thamani vya Ukweli vilivyowekwa kwa wakati huu maalum. **Mungu** ameziokoa Kweli hizi kutoka kwa ushirika wa uongo, na kuziweka katika fremu/nafasi yake inayostahili. Wakati kweli hizi zinapowekwa katika nafasi yake sahihi katika mpango mkuu wa **Mungu**, na zikawasilishwa kwa dhati, akili inayotumia hekima, kwa bidii, na kwa hofu ya **Mungu** na watumishi wa Bwana, wengi wataamini kwa dhamiri kwa sababu ya uzito wa ushahidi, bila kungoja kila pingamizi linaloweza kujitokeza katika akili zao kuondolewa kwanza. —**Manuscript 8a, 1888.** {EVsw 122:2}

Kuvuta Usikivu wa Watu Wengi

Kwa Mbinu za Ajabu— Katika miji ya siku hizi, ambako kuna mambo mengi ya kuwavutia na kuwafurahisha watu, hakuna juhudi za kawaida zitakazoweza kuamsha ari ya watu. Wahudumu waliowekwa

na **Mungu** watahitaji kutumia mbinu zisizo za kawaida ili kuvuta usikivu wa makundi ya watu. Na wanapofanikiwa kuwakusanya watu wengi, ni lazima wawaletee ujumbe wa kipekee, wa aina isiyo ya kawaida, ili kuwaamsha na kuwaonya. Wanapaswa kutumia kila njia inayowezekana ili kuifanya Kweli iwe wazi na kwa upekee. **— Testimonies For The Church 9:109 (1909).** {EVsw 122:3}

Kubuni Mipango ya Kipekee— Hebu kila mtendakazi katika shamba la Bwana na asome, apange, na kubuni mbinu za kuwafikia watu mahali walipo. Hatupaswi kufanya mambo kwa mazoea tu. Tunapaswa kuvuta usikivu wao. Lazima tuwe na bidii ya dhati. Tuko karibu mno na nyakati za taabu na mshangao ambazo hata hatujaweza kuziota katika ndoto zetu. —**Letter 20, 1893.**{EVsw 122:4}

Kristo Alitumia Mbinu Mbalimbali— Kutokana na mbinu za kazi za Kristo tunaweza kujifunza masomo mengi ya thamani. Yeye Hakufuata mbinu moja tu; kwa njia mbalimbali Alitafuta kuvuta usikivu wa makutano; kisha akawafundisha Kweli za Injili. —**Review and Herald, January 17, 1907.** {EVsw 123:1}

Urahisi, Udhati na Uaminifu Vilivutia Wengi— Ujumbe Wake wa rehema ulitofautiana kulingana na hadhira Yake. Alijua "jinsi ya kunena Neno kwa wakati kwa yule aliyechoka"; maana neema ilimiminwa midomoni Mwake, ili Aweze kuwafikishia watu hazina ya Kweli kwa njia ya kuvutia. Alikuwa na hekima ya kuwafikia wale waliokuwa na nia ya chuki, na kuwashangaza kwa mifano iliyowavuta. Kupitia fikra, Aligusa mioyo yao. Mifano Yake ilitokana na maisha ya kila siku, na ingawa ilikuwa rahisi, ilikuwa na maana ya kina ya ajabu. Ndege wa angani, maua ya porini, mbegu, mchungaji na kondoo, —kwa vitu hivi Kristo alifundisha Kweli za milele; na kila walipoona vitu hivi baadaye, walikumbuka mafundisho Yake. Mifano aliyoitumia Kristo ilikuwa ni njia ya kurejelea masomo Yake mara kwa mara. {EVsw 123:2}

Kristo hakuwahi kuwasifu watu kwa kuwahadaa ili awafurahishe, au ajikombe kwao (hakuwapaka watu mafuta kwa mgongo wa chupa). Hakusema maneno ya kuhamasisha mawazo ya kufikirika kwao na kuwapumbaza (fancies/fantasies), au kuwapongeza kwa ubunifu-janja wao; lakini wale waliokuwa na fikra za kina na zisizo na upendeleo/chuki walipokea mafundisho Yake, na waliona jinsi yalivyojaribu hekima yao. Walishangazwa na zile Kweli za kiroho zilizowasilishwa kwa lugha rahisi kabisa. Hata wasomi walivutiwa na Maneno Yake, na wasiosoma walifaidika sana. Alikuwa na ujumbe kwa wasio na elimu; na Aliwafanya hata wapagani kufahamu kuwa Alikuwa na ujumbe kwao.{EVsw 123:3}

Huruma Yake iliwagusa wale waliokuwa na majonzi na uchovu kwa njia ya uponyaji. Hata katikati ya maadui wenye hasira, aliambatana na hali ya amani. Uzuri wa uso Wake, upole wa tabia Yake, na zaidi ya yote, upendo uliodhihirika katika macho na sauti Yake, vilimvuta kila mtu ambaye moyo wake haukuwa mgumu kwa kutokuamini. Isingekuwa kupitia roho Yake nzuri ya huruma iliyodhihirika kwa kila neno na mtazamo, Asingevutia makutano makubwa kama Alivyofanya. Wale waliokuja Kwake wakiwa na maumivu walihisi kuwa Alikuwa rafiki wa karibu na mwaminifu, na walitamani kujua zaidi kuhusu kweli Alizofundisha. Mbingu ilionekana kuwa karibu. Walitamani kukaa katika uwepo Wake, ili faraja ya upendo Wake iwafuate daima. —**The Desire of Ages, uk. 254 (1898).** {EVsw 124:1}

Kuvutia na Kudumisha Makutano Makubwa— Wale ambao watajifunza namna ya mafundisho ya Kristo, na kujielimisha wenyewe kufuata njia Yake, watavutia na kushikilia idadi kubwa sasa, kama Kristo alivyowashikilia watu katika siku Yake.... Lakini Ukweli katika tabia yake ya vitendo unaposisitizwa juu ya watu kwa sababu unawapenda, roho zitahukumiwa, kwa sababu Roho Mtakatifu wa **Mungu** atavutia mioyo yao. {EVsw 124:2}

"Jivikeni unyenyekevu; ombeni ili malaika wa **Mungu** waje karibu nanyi ili kuvutia akili zenu; kwa maana si ninyi mnaomtumia Roho Mtakatifu, bali ni lazima Roho Mtakatifu awatumie ninyi. Ni Roho Mtakatifu anayeifanya kweli kuwa na mvuto. Daima wekeni kweli ya kiutendaji mbele ya watu. — **Testimonies For The Church 6:57 (1900).**{EVsw 124:3}

Faida ya Kufanya Kwa Kushtukiza Katika Maeneo Fulani— Nilipewa nuru na Bwana kwamba si jambo la busara kutangaza hadharani kile tunachokusudia kufanya; kwa sababu mara tu nia zetu zinapojulikana, adui zetu huamka na kuzuia njia. Wahubiri huita wenzao kuja kupinga ujumbe wa kweli. Onyo hutolewa kutoka madhabahuni kwa makusanyiko, wakieleza kile Wasabato (Waaventista) wanapanga kufanya.{EVsw 125:1}

Kutoka katika nuru niliyopewa na Bwana, nina onyo kwa ndugu zetu. Je, majemedari wenye hekima hawafichi mipango yao ili adui asifahamu na kuipinga? Ikiwa adui hana habari kuhusu mipango yao, basi wanakuwa na faida kubwa.{EVsw 125:2}

Tunapaswa kuchunguza eneo kwa makini na tusidhani kwamba ni lazima kutumia njia zilezile kila mahali. Tukitenda kwa hekima, bila kujisifu, bila kuwachokoza maadui, tukisonga mbele kwa mstari baada ya mwingine wa kweli, tukiwasilisha kweli muhimu na zenye kujaribu nafsi, Bwana atashughulikia matokeo…...{EVsw 125:3}

Subirini; simamisheni mahema wakati wa mikutano ya makambi unapowadia. Yafanyeni kwa haraka, kisha toa taarifa za mikutano. Haijalishi mlivyofanya zamani, si lazima kurudia njia hiyo kila mara. **Mungu** anataka mbinu mpya na ambazo hazijajaribiwa. Vunjeni ukawaida—watu washangae. —**Manuscript 121, 1897.**{EVsw 125:4}

Mbinu za Hekima, Sio Udanganyifu— Huna sababu ya kujisikia kuwa ni lazima kusema kweli yote kwa wasioamini kila wakati. Unapaswa kupanga kwa uangalifu nini cha kusema na nini cha kuacha. Kufanya hivi si kudanganya; ni kufanya kazi kama Paulo alivyofanya. Anasema, "2 Wakorintho 12:16 *Lakini na iwe hivyo, mimi sikuwalemea; bali kwa kuwa mwerevu naliwapata kwa hila."* Unapaswa kubadilisha namna ya kazi, usiwe na njia moja tu unayoamini kuwa inafaa kutumiwa kila wakati na kila mahali. Njia zako zinaweza kuonekana kuwa za mafanikio kwako, lakini kama ungetumia hekima zaidi, na werevu kama wa nyoka, ungetazama matokeo halisi zaidi ya kazi yako. —**Letter 12, 1887.** {EVsw 125:5}

Ukumbi Duni Hutangaza Kushindwa— Ninaamini kwamba tungeweza kupata wasikilizaji wengi iwapo ndugu zetu wangechukua ukumbi unaofaa wa kuwapokea watu. Lakini hawakutarajia makubwa, na hivyo hawakupokea makubwa. Hatuwezi kutarajia watu kuja kusikiliza kweli isiyopendwa ikiwa mikutano itafanyika kwenye eneo au ukumbi mdogo wa watu mia moja tu... Kwa ukosefu wa imani, watenda kazi wetu wakati mwingine hujiletea ugumu wao wenyewe. —**Historical Sketches, uk. 200 (1886).** {EVsw 126:1}

Kwa Njia ya Mungu Mwenyewe

Sio kwa maonyesho ya nje ndipo wanaume na wanawake watajifunza maana ya kweli ya sasa. Watendakazi wetu wanapaswa kuishi maisha ya uchumi wa hali ya juu. **Mungu** amekataza aina zote za matumizi ya anasa. Kila dola tuliyonayo inapaswa kutumiwa kwa hekima na kwa uangalifu mkubwa. Tusifanye maonyesho makubwa. Fedha ya **Mungu** ni kwa ajili ya kuendeleza kazi Yake kwa njia ile ile Aliyoamuru ifanyike ulimwenguni mwetu. —**Letter 107, 1905.**{EVsw 126:2}

Maonyesho si Njia Bora ya Kutangaza

Miji mikubwa inapaswa kuonywa, lakini ndugu yangu, si kila mbinu unayotumia katika kazi hii ni sahihi. Unadhani kuwa uko huru kutumia fedha nyingi kadri upendavyo ili kuvuta hisia za watu. Lakini kumbuka kwamba katika shamba la Bwana kuna maeneo mengi sana yanayohitaji kufikiwa, na kila dola ni muhimu. {EVsw 126:3}

Mungu hapendezwi na matumizi yako makubwa ya fedha katika kutangaza mikutano yako, wala na maonyesho yanayofanywa katika vipengele vingine vya kazi yako. Maonyesho hayo hayalingani na kanuni za Neno la **Mungu**. Anatiwa aibu na maandalizi yako ya gharama kubwa. Mara nyingine unafanya jambo ambalo limeonyeshwa kwangu kuwa ni kama kukatakata matikiti mwitu na kuyatia ndani ya sufuria. Maonyesho hayo hufanya Kweli ionekane kama imechanganywa na ladha nyingine. Mwanadamu hutukuzwa, lakini Kweli haisongi mbele bali huzuiliwa. Watu wenye akili na busara wanaweza kuona kwamba maigizo ya kisanaa hayaendani na ujumbe mzito unaoubeba. —**Letter 190, 1902.**{EVsw 127:1}

Matokeo ya Kukatisha Tamaa Kutokana na Mbinu za Gharama Kubwa

Punguza gharama za kutangaza mikutano yako, na kama kiasi kikubwa cha fedha kitakusanywa wakati wa mikutano, tumia fedha hiyo kuendeleza kazi katika maeneo mapya.{EVsw 127:2}

Usiwaajiri wanamuziki wa kidunia kama jambo hilo linaweza kuepukika. Kusanya waimbaji watakaoiimba kwa roho na kwa ufahamu pia. Maonyesho ya ziada unayoyafanya mara nyingine huongeza gharama zisizo za lazima, ambazo ndugu hawapaswi kubebeshwa. Na utagundua kuwa baada ya muda wale wasio waumini hawatakuwa tayari tena kutoa pesa kufanikisha matumizi hayo…..{EVsw 127:3}

Nakuomba kwa dhati uache kufuata mbinu hizi za gharama kubwa katika utumishi. Lazima nikwambie kwamba Bwana hazibariki mbinu hizi. Wala haziletei matokeo unayodhani. —**Letter 51, 1902.**{EVsw 127:4}

Lazima Kumtegemea Mungu

Kuna kazi kubwa sana inayofanywa na ulimwengu wa Mbinguni kuliko tunavyoweza kuelewa, katika kuandaa njia ili roho zipate kuongoka. Tunapaswa kufanya kazi kwa kushirikiana na wajumbe wa Mbinguni. Tunahitaji kuwa na **Mungu** zaidi; hatupaswi kuhisi kuwa ni kwa mazungumzo yetu au mahubiri yetu ndipo kazi itafanyika; bali tunapaswa kuelewa kwamba kama watu hawataguswa na **Mungu**, hawataguswa kamwe. —**Manuscript 19b, 1890.** {EVsw 127:5}

Jifunze Mbinu za Kuwaendea Watu

Kazi ya kuleta roho kwa Kristo inahitaji maandalizi makini. Mwanadamu hawezi kuingia katika huduma ya Bwana bila mafunzo yanayohitajika na kutarajia kufanikiwa kwa kiwango cha juu…….Mbunifu wa majengo atakuambia ni muda gani ilimchukua kuelewa jinsi ya kupanga jengo la kuvutia na lenye nafasi nzuri. Vivyo hivyo ndivyo ilivyo katika kazi zote ambazo watu hufuata. Je, watumishi wa Kristo waonyeshe bidii ndogo katika kujiandaa kwa kazi iliyo ya umuhimu usio na kifani? Je, wafanikiwe bila kuelewa njia na mbinu za kufikia roho? Inahitaji maarifa ya asili ya mwanadamu, kujifunza kwa karibu, fikra makini, na maombi ya bidii ili kuelewa jinsi ya kuwakabili wanaume na wanawake kuhusu masuala makubwa yanayohusu wokovu wao wa milele. —**Gospel Workers, ukurasa wa 92 (1915).** {EVsw 128:1}

Njia Zenye Mafanikio na Zenye Kuvutia za Matangazo

Kazi Yetu Inavyohukumiwa kwa Mbinu Zetu za Kutangaza

Tabia na umuhimu wa kazi yetu vinahukumiwa kwa jitihada tunazofanya kuileta mbele ya jamii. Jitihada hizi zinapokuwa za kiwango cha chini, hutolewa taswira kuwa ujumbe tunaowasilisha hauna uzito wa kuzingatiwa. — **Historical Sketches, uk. 200 (1886).**{EVsw 128:2}

Matumizi ya Hekima katika Matangazo

Ni kweli kwamba kuna haja ya kutumia fedha kwa busara katika kutangaza mikutano na kuendeleza kazi kwa msingi imara. Hata hivyo, nguvu ya kila mtendakazi haitatokana na njia hizi za nje, bali kutokana na kutegemea kwa imani msaada wa **Mungu**, na kwa maombi ya bidii kwa ajili ya msaada Wake, pamoja na utii kwa **Neno** Lake. — **Testimonies for the Church 9:110 (1909).**{EVsw 128:3}

Kubuni Mbinu za Kuwafikia Watu

Wahudumu wenye akili angavu wanahitajika ili wabuni mbinu za kuwafikia watu. Sharti kitu kifanyike ili kuvunja chuki iliyoenea ulimwenguni dhidi ya Kweli. — **Letter 152, 1901.** {EVsw 129:1}

Makala katika Magazeti ya Kidunia

Watu watapotosha mafundisho tunayoyaamini na kuyafundisha kama kweli ya Biblia, na ni lazima mipango ya hekima iwekwe ili kupata fursa ya kuchapisha makala katika magazeti ya kawaida; kwa maana hii itakuwa njia ya kuziamsha roho kuona Kweli. **Mungu** atawainua watu watakaostahili kupanda mbegu karibu na maji yote. **Mungu** ametupa nuru kuu juu ya kweli muhimu, na nuru hiyo lazima iwafikie watu wa dunia. — **Letter 1, 1875.**{EVsw 129:2}

Matangazo ya Maalum kwa Wafanyabiashara

Kwa shauku kuu, **Mungu** anatazama dunia hii. Ameona uwezo wa wanadamu katika huduma. Akiangalia kupitia vizazi, Amewahesabu watendakazi Wake, waume kwa wake, na Amewaandalia njia, akisema, “Nitawatuma wajumbe Wangu kwao, nao wataona nuru kuu iking’aa katikati ya giza. Wakivutwa kwa huduma ya Kristo, watatumia vipaji vyao kwa utukufu wa Jina Langu. Wataenda kufanya kazi kwa bidii na uaminifu kwa ajili Yangu. Kupitia juhudi zao, kweli itazungumza kwa maelfu kwa njia yenye nguvu, na waliopofushwa kiroho watafumbuliwa macho, nao wataona wokovu Wangu.{EVsw 129:3}

Kweli itawekwa wazi kiasi kwamba kila anayeikimbia ataweza kuisoma. Mbinu zitabuniwa kufikia mioyo ya watu. Baadhi ya mbinu zitakazotumika katika kazi hii zitakuwa tofauti na zile zilizotumiwa zamani; lakini mtu yeyote asizuie mbinu kwa lawama kwa sababu ya hilo.” **— Review and Herald, September 30, 1902.** {EVsw 129:4}

Kutumia Vyombo vya Habari kama Mtambo wa kuchapisha nk kwa Ufanisi

Lazima tutumie kila njia za haki kuwasilisha nuru mbele ya watu. Vyombo vya habari viweze kutumika, na kila shirika la matangazo litumiwe kwa njia yoyote itakayosaidia kuelekeza fikra za watu kwa kazi hii. Hili halipaswi kuonekana kuwa jambo lisilo la lazima. Kwenye kila kona ya mtaa utaona matangazo na mabango yanayotoa habari juu ya mambo mbalimbali yanayoendelea, baadhi yake yakiwa ya maadili ya kutiliwa shaka; je, wale waliokuwa na nuru ya uzima waridhike na jitihada dhaifu katika kuielekeza jamii kwenye Kweli? {EVsw 130:1}

Wale wanaovutiwa watalazimika kukabiliana na hoja za upotoshaji kutoka kwa wahubiri wa madhehebu, na hawatajua jinsi ya kuyajibu. Kweli inayowasilishwa na mhubiri hai iandikwe kwa muhtasari na isambazwe kwa wingi. Ikiwezekana, mahubiri muhimu yanayotolewa kwenye mikutano yetu ya kambi yaandikwe katika magazeti. Kwa njia hiyo, kweli iliyowasilishwa kwa kundi dogo itaweza kuwafikia wengi. Na pale kweli ilipopotoshwa, watu watakuwa na nafasi ya kujua kile hasa ambacho mhubiri alisema.{EVsw 130:2}

Weka nuru yako juu ya kinara ili iangaze kwa wote waliomo nyumbani. Ikiwa kweli imetolewa kwetu, basi tuifanye iwe wazi kwa wengine kiasi kwamba wale waaminifu kwa mioyo yao waione na kushangilia mwangaza wake. — **Testimonies for the Church 6:36-37 (1900).**{EVsw 130:3}

Kuepuka Matangazo Yenye Kushtua na Kuleta Hofu

Sikuridhishwa na matangazo ya kushangaza ya mikutano yenu. Yanabeba harufu ya ushabiki... Msitoe matangazo yaliyoandikwa kwa namna ya kuleta hofu. Wakati Bwana atakapokuwa tayari kwa tangazo la wazi dhidi ya miji yenye uovu, Atawaambia watu Wake. Lakini hilo litakuwa baada ya miji hiyo kuwa imepewa nafasi ya kusikia na kupokea Neno lile lenye uzima wa milele. {EVsw 130:4}

Kazi yetu sasa ni kuangazia na kufundisha akili kuhusu yale yasemwayo na Maandiko. Milango imefunguliwa kwa ajili ya kupeleka Kweli. Tumia fursa hii kuwafikia wale ambao hawajawahi kuisikia Kweli. Elezeni kweli kama Kristo alivyofanya—kwa njia nyingi, kwa mifano na mafumbo. Na ule uwasilishaji wa kuvutia wa Ukweli kwa kutumia michoro, kama afanyavyo Mzee _____, unaweza kuigwa kwa mafanikio. Mambo haya na yaweze kuzungumza na hisia za watu. Msihimize kitu chochote kinachofanana na harakati za ushabiki. Shetani hufanya kazi katika eneo hilo, akijaribu kuwavuta wafuasi kwa njia ya picha ambazo, kama ingewezekana, zingewadanganya hata wateule. — **Letter 17, 1902.**{EVsw 131:1}

Matangazo Yenye Kushangaza

Matangazo ya kushtua ni ya kuharibu kazi. — **Review and Herald, July 5, 1906.**{EVsw 131:2}

Ninawahakikishia kwamba tunawaombea ninyi pamoja na kazi huko Jiji la New York. Lakini tafadhali ondoeni matangazo yale ya kushtua kuhusu mikutano yenu. Ikiwa wimbi la ushabiki lingetokea New York wakati huu, Shetani angewachochea watu, akianzisha kazi ambayo hamjajiandaa kuimudu. Siyo msisimko tunaohitaji wakati huu, bali juhudi tulivu, thabiti, na za kujitolea kwa ajili ya kuwaelimisha watu. **— Letter 17, 1902.** {EVsw 131:3}

Mwinjilisti na Umaarufu

Kujisifu Hakufai

Kujisifu juu ya sifa tulizonazo wenyewe hakufai kabisa... Siri ya mafanikio haipatikani katika elimu yetu, nafasi zetu, idadi yetu au vipawa tulivyopewa, wala si katika mapenzi ya mwanadamu. —**Christ's Object Lessons, 401, 404 (1900).**{EVsw 131:4}

Si kwa Njia za Dunia

Hatupaswi kufuata namna ya dunia katika kutenda. Tunapaswa kuonyesha mfano bora zaidi kwa dunia, tukidhihirisha kwamba imani yetu ni ya hali ya juu na tukufu... Hivyo basi, mitazamo ya ajabu ajabu, tabia binafsi zisizo za kawaida na mipango finyu ambayo huweza kutoa taswira potofu ya ukuu wa kazi, yapaswa kuepukwa. —**Letter 14, 1887.**{EVsw 132:1}

Hakuna Kupotosha Ili Kupata Kibali

Hatupaswi kupotosha yale tunayodai kuyamini ili kupata kibali. **Mungu** huchukia unafiki na udanganyifu. Hatavumilia mtu anayesema lakini hatendi. Kazi bora na tukufu zaidi hufanyika kwa njia ya uaminifu na haki. —**Letter 232, 1899.** {EVsw 132:2}

Kristo Hakujiita "Professa au Rabbi au Mwalimu"

Sio kutafuta ukuu ndiko kutakakokufanya uwe mkuu machoni pa **Mungu**, bali ni maisha ya unyenyekevu, wema, upole, uaminifu na usafi, yatakayokufanya uwe chini ya ulinzi maalum wa malaika wa mbinguni. Mfano wetu Mkuu, Ambaye hakuona kuwa kule kuwa sawa na **Mungu**, kuwa ni kitu cha kushikamana nacho, Alichukua asili yetu na akaishi karibu miaka thelathini katika mji usiojulikana huko Galilaya, uliojificha milimani. Maelfu ya malaika walikuwa chini ya amri Yake; lakini Hakudai kuwa mtu mkuu au aliyeinuliwa. Hakujiita "Mwalimu" ili kujiridhisha. Alikuwa seremala, akifanya kazi ya mikono, akifanya kazi kwa ajili ya mshahara, akihudumu kwa wale Aliowafanyia kazi. —**Letter 1, 1880.** {EVsw 132:3}

Kristo Aliwakemea kwa Ubatili wao-Kujiweka juu...Aliwakemea kwa kutamani vyeo kama "rabi" au "mwalimu." Alisema vyeo hivyo havifai kwa wanadamu, bali ni vya Kristo pekee. Makuhani, waandishi, watawala, viongozi na watekelezaji wa sheria walikuwa ndugu, watoto wa Baba mmoja. Yesu aliwafundisha watu wasimpe mtu yeyote cheo cha heshima kinachoashiria mamlaka juu ya dhamiri au imani yao. {EVsw 132:4}

Kama Kristo angekuwa duniani leo, akiwa katikati ya wale wanaojiita "Mtukufu" au "Mheshimiwa Mtukufu," je, asingerudia maneno haya: Mathew 23:10 "*Wala msitwe viongozi, maana kiongozi wenu ni mmoja, naye ndiye Kristo*"? Maandiko yanasema juu ya **Mungu**, "*Jina Lake ni takatifu na la kuogopwa.*" *(Zaburi 111:9)*. Ni mwanadamu yupi anayestahili kuitwa kwa jina hilo? —**The Desire of Ages, 613 (1898).**{EVsw 133:1}

Hakuna Haki ya Kutumia Cheo cha "Mtukufu"

Kiwango cha elimu ya kweli hakipaswi kupunguzwa. Kinapaswa kuinuliwa juu zaidi ya kilipo sasa. Hatupaswi kuinua wala kuabudu wanadamu; ni **Mungu** pekee, aliye wa kweli na aishiye, ndiye Anayestahili ibada yetu na heshima yetu.{EVsw 133:2}

Kwa mujibu wa maandiko, ni kinyume cha heshima kwa **Mungu** kuwaita wahubiri "Mtukufu." Hakuna mwanadamu aliye na haki ya kujiita au kumwita mwingine kwa jina hilo. Ni jina la **Mungu** pekee, linalomtenganisha na viumbe wote. Wale wanaolitumia jina hilo hujivika utukufu wa **Mungu** kinyume cha haki. "*Jina lake ni takatifu na la kuogopwa.*" Tunamdharau **Mungu** tunapolitumia neno hilo pasipo haki. —**The Youth's Instructor, July 7, 1898.**{EVsw 133:3}

Watu Wadogo Wakishughulikia Masomo Makuu

Wahubiri wa Injili wanapaswa kuwasilisha Ukweli kwa unyofu, kwa baraka za **Mungu**, wakifanya Maandiko kuwa yafaa kwa mafundisho, kwa kuwaonya watu makosa yao, kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadabisha katika haki. "Wakiligawanya sawasawa **Neno** la Kweli"—hili ndilo linalopaswa kusemwa juu ya wahubiri wetu wote.{EVsw 133:4}

Lakini wengi wamepotoka mbali na mipango ya Kristo. Wanatamani sifa za wanadamu, na hutumia nguvu nyingi kutafuta mambo ya ajabu ya kusema. Bwana amenituma kuwashauri watembee kwa unyenyekevu na kwa maombi pamoja Naye... Wajitayarishe kuwa watu wadogo wanaoshughulikia mambo makuu. —**Manuscript 62, 1905.**{EVsw 134:1}

Hakuna Watu Mashuhuri

Hatuna watu mashuhuri miongoni mwetu, wala hakuna kwa mtu yeyote kujaribu kujionyesha kuwa kile ambacho si kweli-yaani, mtu wa ajabu au wa pekee. Si busara kwa mtu yeyote kujaribu kujionyesha kana kwamba ana uwezo wa kipekee, kana kwamba yeye ni Moody (mhubiri maarufu karne ya 19) au Sankey (mwimbaji maarufu wa Injili karne ya 19) kwa kipindi chetu. *[1. Moody-Hii inarejelea Dwight L. Moody (1837–1899), ambaye alikuwa mhubiri wa Kiprotestanti mashuhuri kutoka Marekani. Alijulikana kwa mahubiri yenye nguvu, uvumbuzi wa kazi ya uinjilisti wa mijini, na kuanzisha taasisi ya mafunzo ya Biblia (Moody Bible Institute). Kwahiyo Moody ni Mhubiri mashuhuri wa kiinjilisti wa karne ya 19 kutoka Marekani. 2. Sankey-Hii inarejelea Ira D.* ***Sankey*** *(1840–1908), mwimbaji na mtunzi wa nyimbo za Kikristo ambaye alishirikiana na Moody katika huduma ya uinjilisti. Sankey alitambulika kwa kuimba kwa sauti ya kugusa mioyo, na aliandaa vitabu vya nyimbo vilivyosaidia sana kazi ya uinjilisti. Kwahiyo Sankey ni Mwimbaji wa*

nyimbo za injili na mshirika wa huduma ya uinjilisti wa Moody]. —**The Review and Herald, December 8, 1885.** {EVsw 134:2}

Ujumbe, Siyo Mjumbe

Mhubiri aliyejifunza kwa Kristo daima atatambua kuwa yeye ni mjumbe wa **Mungu**, aliyeagizwa kutenda kazi kwa ajili ya wakati huu na kwa ajili ya umilele. Haipaswi kuwa lengo lake kujionyesha au kuonyesha elimu yake au uwezo wake. Lengo lake lote linapaswa kuwa kuwaongoza wakosefu kutubu, akiwaelekeza kwa mfano na mafundisho kwa Mwana-Kondoo wa **Mungu** aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Nafsi yake inapaswa kujificha ndani ya Yesu. Watu wa namna hiyo watanena kama wenye mamlaka kutoka kwa **Mungu**, wakiwa wasemaji Wake. Mahubiri yao yatakuwa na nguvu ya ushawishi itakayowaongoza wakosefu kuona hali yao ya kupotea na kutafuta kimbilio kwa Kristo. —**The Review and Herald, August 8, 1878.** {EVsw 134:3}

Yohana Alikuwa Sauti Tu

Akiangalia kwa imani kwa Mkombozi, Yohana alifikia kilele cha kujikana nafsi. Hakutaka kuwavuta watu kwake, bali alitaka kuwaelekeza juu na juu zaidi, hadi fikra zao zipumzike kwa Mwana-Kondoo wa **Mungu**. Yeye Mwenyewe alikuwa sauti tu, mwito nyikani. —**Gospel Workers, 56 (1915).**{EVsw 134:4}

Wanaochaguliwa Leo ni Kama Yohana

Ili kutimiza nafasi ya juu mbele ya watu, mbingu humchagua yule anayechukua nafasi ya chini mbele za **Mungu**, kama Yohana Mbatizaji. Mwanafunzi mwenye unyenyekevu zaidi ndiye mwenye ufanisi zaidi katika kazi ya **Mungu**. Viumbe wa mbinguni wanaweza kushirikiana na mtu anayejitahidi si kwa ajili ya kujitukuza, bali kwa ajili ya kuokoa roho. —**The Desire of Ages, 436 (1898).** {EVsw 135:1}

Kazi Inapoharibiwa kwa Kujitukuza

Hakuna dini inayotokana na kujikweza. Yule anayejitafutia utukufu, atakosa neema inayoweza kumfanya afae katika huduma ya Kristo. Kila mara kiburi na kuridhika na nafsi vinapopewa nafasi, kazi huharibika. **—Christ's Object Lessons, 402 (1900).**{EVsw 135:2}

Kipimo Halisi cha Mwanadamu

Thamani ya Kikristo haitegemei vipawa vya ajabu, nasaba ya kifalme, au uwezo wa kipekee, bali moyo safi—moyo uliosafishwa na kutakaswa, usiojivuna, bali unaoakisi taswira ya Kiungu kwa kumtazama Kristo. —**Letter 16, 1902.**{EVsw 135:3}

Yesu Peke Yake

Wasipoonesha hekima ya kibinadamu na kukataa kujitukuza, [wahubiri wa **Mungu**] watafanya kazi itakayodumu dhidi ya mashambulizi ya Shetani. Roho nyingi zitaongoka kutoka gizani hadi kwenye nuru, na makanisa mengi yataanzishwa. Watu wataongoka, si kwa ajili ya binadamu, bali kwa ajili ya Kristo. Nafsi ya mwanadamu itabaki nyuma; Yesu peke Yake, Mtu wa Kalvari, ataonekana. —**The Acts of the Apostles, 278 (1911).** {EVsw 135:4}

Kuepuka Maonyesho na Mambo ya Kusisimua

Mafanikio Hayategemei Maonyesho ya Nje — Wahubiri wengine hufikiri kimakosa kuwa mafanikio yanategemea kuvutia umati mkubwa wa watu kwa kutumia maonyesho ya kuvutia, kisha kutoa ujumbe wa kweli kwa mtindo wa kisanii wa maigizo. Lakini kitendo hiki ni kutumia moto wa kigeni badala ya ule moto mtakatifu uliowashwa na **Mungu**. Bwana hatukuzwi kwa namna hii ya kufanya kazi. Kazi Yake haitakamilishwa kwa matangazo ya kushtua na maonyesho ya gharama kubwa, bali kwa kufuata mbinu za Kristo. "Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali kwa Roho yangu, asema Bwana wa majeshi." Ni ukweli uliowazi, ambao kama upanga ukatao kuwili, hukata pande zote mbili, ukiwaamsha walio wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zao. Watu watatambua Injili iwapo italetwa kwao kwa njia inayopatana na makusudi ya **Mungu**. — **Gospel Workers, uk. 383 (1915).**{EVsw 136:1}

Mbinu Zenye Akili ya Kawaida — Wapo watu ambao huwa tayari kushikilia jambo la ajabu, ambalo wanalileta kama mshangao kwa watu ili kuwaamsha kwa hofu na kuanzisha kazi ya ajabu ambayo huharibu kazi nzuri iliyoanzishwa kwa njia sahihi.…{EVsw 136:2}

Wale wanaoshughulikia Kweli kuu, tukufu na inayoinua ya **Neno** la **Mungu** lazima waonyeshe roho ya kina, bidii, ari, lakini ya utulivu na iliyojaa akili ya kawaida, ili vinywa vya wapinzani vinyamazishwe. Msihimize wimbi la uzushi litakaloharibu kazi iliyoanzishwa kwa usahihi, na kuendelezwa kwa Neno la **Mungu** mikononi mwenu……{EVsw 136:3}

Wale wanaofanya kazi huko New York wasifikiri kuwa lazima walete jambo la ajabu na kulichanganya na kazi yao kama ushahidi kuwa kazi hiyo ni ya **Mungu**. Kazi yao ni kusema na watu kwa unyenyekevu, kwa imani ya kuamini, wakiomba shauri kwa **Mungu**, si kufuata mawazo yao wenyewe, wala si kutegemea kuleta mambo ya kuvutia hisia za walio wafu kwa sababu ya dhambi. Mfumo wa kweli uliomo katika Neno la **Mungu** unao uwezo wa kuacha matokeo yale yale ambayo Mwalimu Mkuu anatamani yawepo katika akili za watu. — **Letter 17, 1902.** {EVsw 136:4}

Usishushe Kiwango cha Kweli— Kamwe usishushe kiwango cha Kweli ili kupata waongofu, bali wainue wenye dhambi na walioharibika hadi kwenye kiwango cha juu cha sheria ya **Mungu**. — **Manuscript 7, 1900.**{EVsw 137:1}

Epuka Maonyesho ya Kimaigizo — Nina ujumbe kwa wale wanaosimamia kazi yetu. Msihimize watu wanaopaswa kushiriki kazi hii kufikiri kuwa lazima watangaze ujumbe huu mtakatifu kwa mtindo wa maigizo. Hakuna sehemu hata ndogo ya maigizo inapaswa kuletwa katika kazi yetu. Kazi ya **Mungu** inapaswa kuwa na chapa ya mbinguni, iliyo takatifu. Kila kitu kinachohusiana na utoaji wa ujumbe wa wakati huu lazima kiwe na muhuri wa Kiungu. Hakuna jambo la kisanii au la maigizo linapaswa kuruhusiwa, kwa kuwa litapunguza utakatifu wa kazi hii.{EVsw 137:2}

Nimefundishwa kuwa tutakutana na kila aina ya uzoefu, na kuwa watu watataka kuleta mambo ya ajabu katika kazi ya **Mungu**. Tumekutana na hali hizi katika sehemu nyingi. Tangu mwanzo wa huduma yangu, ujumbe uliotolewa ulikuwa kwamba maonyesho ya kimaigizo katika mahubiri ya Kweli ya sasa ni lazima yakataliwe na kupingwa. Watu waliodhani wana kazi kubwa ya kufanya walijaribu kuleta mienendo ya ajabu na maonyesho ya mwili yasiyo ya kawaida. Nuru niliyopewa ilikuwa, “Usitoe idhini yoyote.” Maonyesho haya, yaliyokuwa na harufu ya maigizo, hayapaswi kuwa sehemu ya utangazaji wa ujumbe mzito ulioaminiwa kwetu. Adui atatambua kwa karibu kila nafasi ya kushusha hadhi ya Kweli kwa kuingiza maonyesho yasiyo ya heshima. Hakuna kati ya haya yanayopaswa kuhimizwa. Kweli ya thamani tuliyopewa inapaswa kutangazwa kwa uzito wote na kwa hofu takatifu. — **Manuscript 19, 1910.**{EVsw 138:1}

Hatari ya Mafundisho ya Kusisimua — Unaweza kuwa na uhakika kuwa dini safi na isiyo na mawaa si dini ya kusisimua. **Mungu** hajampa yeyote jukumu la kuhamasisha tamaa ya mafundisho ya kubahatisha na nadharia. Ndugu zangu, epukeni mambo haya katika mafundisho yenu. **—(Australasian) Union Conference Record, March 15, 1904.** {EVsw 138:2}

Epukeni Uzushi — Hatupaswi kuhimizwa kuwa na roho ya ushabiki inayowasha ari kwa muda, lakini baadaye huisha, ikiacha huzuni na kukata tamaa. Tunahitaji mkate wa uzima utokao mbinguni kuipa nafsi uzima. Jifunzeni Neno la **Mungu**. Msiongozwe na hisia. Wote wanaofanya kazi katika shamba la Bwana lazima wajifunze kuwa hisia si imani. Haitakiwi tuwe katika hali ya juu ya kihisia muda wote, lakini inatakiwa tuwe na imani thabiti katika **Neno** la **Mungu** kama mwili na damu ya Kristo.{EVsw 138:3}

Wanaofanya kazi ya Bwana mijini mwao lazima wafunge na kufunga kwa nguvu milango dhidi ya msisimko na uzushi. Neno la **Mungu** ndilo utakaso wetu na haki yetu, kwa sababu ni chakula cha kiroho. Kulisoma ni kula majani ya mti wa uzima. Hakuna jambo linalowainua zaidi watumishi wa **Mungu** kuliko kufundisha Maandiko kama Kristo alivyofundisha. **Neno** la **Mungu** lina chakula cha Kiungu kinachotosheleza tamaa ya chakula cha kiroho. — **Letter 17, 1902.** {EVsw 138:4}

Mbinu za Gharama na za Pekee — Umechagua kufanya kazi kwa namna inayokuchosha sana na kutumia rasilimali nyingi. {EVsw 139:1}

Matumizi haya ya gharama kubwa yameonyeshwa mbele yako katika uzito wake halisi, na umeambiwa kuwa njia hiyo ya kazi haipatani na mapenzi ya **Mungu**. Mbinu zako za kipekee na za gharama kubwa zinaweza kuonekana mwanzoni kuwa zinawavutia watu, lakini muda si mrefu watu hutambua kuwa maonyesho hayo yamefanyika ili kuvutia watu kwa wewe mwenyewe, mke wako na watoto wako. Matumizi hayo makubwa

hayapatani na kweli zenye uzito zinazowasilishwa. Nafsi imewekwa mbele. — **Letter 205, 1904.**{EVsw 139:2}

Msiige Mfano wa Dunia — Tunashughulikia masuala yanayohusu hatima ya milele, na hatupaswi kuigiiza dunia kwa namna yoyote ile ya ujinga kama vile sokwe mtu wanavyoigiza watu wafanyao matendo fulani (to ape methods!).{EVsw 139:3}

Tunapaswa kufuata kwa ukaribu hatua za Kristo. Yeye ni sehemu tosha ya roho, na anaweza kutimiza mahitaji yetu yote. — **Manuscript 96, 1898.**{EVsw 139:4}

Kulinda Njia Sahihi za Kuwafikia Watu

Yesu Alijifunza Mtiririko wa Mawazo wa Kawaida

Matendo ya rehema au ya wema ya asili hayatendeki kwa njia za ghafla na za kushangaza; wanadamu hawaruhusiwi kuichukua kazi ya wema ya asili mikononi mwao (hawachukui sifa zake kwamba wao wamehusika nk). **Mungu** hufanya kazi kupitia utaratibu wa utendaji wa sheria Zake alizoweka. Vivyo hivyo katika mambo ya kiroho. Shetani huchochea matokeo kwa njia za nguvu, ujeuri na hata ukatili; lakini Yesu alipata njia ya kuingia katika mawazo ya wanadamu kupitia njia ya uhusiano wao wa kawaida. Aliepuka kuvuruga mtiririko wao wa kawaida wa fikra kwa matendo ya ghafla au sheria kali. Aliwaheshimu wanadamu kwa kuwaamini, hivyo kuwaweka katika heshima yao binafsi. Alizitambulisha Kweli za kale kwa nuru mpya na yenye thamani. Ndipo Alipokuwa na umri wa miaka kumi na miwili tu, aliwashangaza walimu wa sheria kwa maswali Yake hekaluni.{EVsw 139:5}

Yesu alichukua ubinadamu ili akutane na ubinadamu. Yeye Huleta wanadamu chini ya nguvu ya kugeuza ya Kweli kwa kuwafikia pale walipo. Aligusa mioyo yao kwa kuwahurumia, Akiwafanya wote wahisi kuwa ameungana kabisa na asili na maslahi yao. Kweli kutoka kinywani Mwake ilikuwa nzuri kwa unyenyekevu Wake, lakini ikiwa na heshima na nguvu. Bwana wetu Yesu Kristo alikuwa Mwalimu wa ajabu kiasi gani! Kwa upole Alivyowatendea kila mtafutaji mwaminifu wa kweli, ili apate kuwahurumia, na kupata makazi moyoni mwao. —**Manuscript 44, 1894.**{EVsw 140:1}

Matokeo Yanayotegemea Njia ya Kuwafikia Watu

Tunapaswa kusimama ulimwenguni kana kwamba wale waliotuzunguka wote ni watu waliokombolewa kwa damu ya Kristo, na kana kwamba maneno yetu, mwenendo wetu, na namna tunavyofanya kazi vina mchango mkubwa kwamba nafsi hizo zitakombolewa au la.... Inategemea sana jinsi tunavyoanza na kuendelea na kazi yetuna na iwapo tutazaa matunda ya roho zilizookolewa kutokana na juhudi zetu. —**Manuscript 14, 1887.**{EVsw 140:2}

Njia Sahihi za Kukabiliana na Chuki

Ndugu zangu, ninyi mnaoenda kufanya kazi kwa ajili ya waliokamatwa katika minyororo ya chuki na ujinga, mnahitaji kutumia hekima ileile ya Kiungu ambayo Paulo alionyesha. Mnapofanya kazi mahali ambapo watu ndio kwanza wanaanza kuona kwa namna ya awali (kama kuona watu kama miti inayotembea), jihadharini sana msiwasilishe Kweli kwa namna itakayochochea upinzani na chuki, na kufunga mlango wa mioyo yao dhidi ya Ukweli. Kubalianeni nao katika kila kipengele mnachoweza kwa usahihi au kwa kuendana na ile Kweli. Waonyesheni kwamba mnawapenda na mnatakia roho zao mema, na kwamba mnatamani kuwa katika uhusiano mwema nao kwa kadiri iwezekanavyo. Ikiwa upendo wa Kristo utaonekana katika juhudi zenu zote, mtaweza kupanda mbegu ya Kweli mioyoni mwao; **Mungu** atainyeshea mvua mbegu, na **Kweli** itamea na kuzaa matunda kwa utukufu Wake.{EVsw 140:3}

Wachungaji (wahudumu) wetu wanahitaji hekima zaidi kama ile ya Paulo. Alipofanya kazi kwa ajili ya Wayahudi, hakuanza mara moja kuzungumzia Ukweli kuhusu kuzaliwa, kusalitiwa, kusulubiwa na kufufuka kwa Kristo, ingawa hayo ndiyo yalikuwa Kweli kuu za wakati huo. Kwanza aliwapeleka hatua kwa hatua kupitia ahadi zilizotolewa kuhusu Mwokozi, na unabii uliomwelezea. Baada ya kushughulikia mambo hayo mpaka wakayaelewa kwa dhahiri, ndipo alipowaambia kuwa Mwokozi Huyo Alikuwa amekwisha kuja, na kwamba Yesu Kristo alitimiza kila Neno la unabii. Hii ndiyo “hila takatifu” aliyotumia Paulo kuvuta roho. Aliwasilisha Kweli kwa namna ambayo chuki yao isingeweza kuwazuia au kupotosha hukumu yao. **—Historical Sketches, uk. 121-122 (1886).** {EVsw 141:1}

Tahadhari Katika Kuwasilisha Mafundisho ya Awali

Tunahitajika kuwa waangalifu sana tunaposhughulikia na roho hizi. Daima uwe macho. Usianze kwa kuweka mbele mambo ya imani yetu ambayo ni ya kuudhi sana kwa wengine, la sivyo unaweza kuwafunga masikio kabla hawajapata nafasi ya kusikia Kweli.{EVsw 141:2}

Wape sehemu za Kweli ambazo wanaweza kuelewa na kuthamini; hata ikiwa zitawashangaza au kuonekana ni mpya, wengi watazitambua kwa furaha kama nuru mpya inayong'aa kuhusu Neno la **Mungu**. Lakini kama Kweli itawasilishwa kwa namna isiyovumilika, wengine wataondoka na kisha wasirudi tena. Zaidi ya hayo, watapotosha Kweli hiyo na kupindua Maandiko kwa njia ya kuwapotosha wengine. Tunapaswa kutumia mazingira yaliyopo kwa hekima ili kunufaisha kazi ya injili. Wasilisha ile **Kweli** kama ilivyo katika Yesu. Isiwepo roho ya mabishano wala vita katika kuiwasilisha Kweli. —**Manuscript 44, 1894.** {EVsw 142:1}

Soma Mahitaji ya Jamii Kabla ya Kuchagua Mada

Wajue watu katika makazi yao. Pima hali ya kiroho ya jamii, kisha peleka vita katika kambi ya adui. Wafanye wawe na shauku au wafanye watamani injili. Omba na uamini, nawe utapata uzoefu wa thamani. Usichukue mada nzito zinazohitaji mawazo ya kina kueleweka. Omba na uamini unavyofanya kazi. Amsha watu wachukue hatua. Fanya kazi kwa bidii kwa Jina la Bwana. —**Letter 189, 1899.** {EVsw 142:2}

Andaa Udongo kwa Ajili ya Mbegu Nzuri

Kumbuka kwamba ni lazima kuwa waangalifu sana katika namna unavyowasilisha Kweli. Peleka fikra za watu hatua kwa hatua kwa tahadhari. Zungumzia utauwa wa vitendo, ukiunganisha na mafundisho ya kiimani. Mafundisho na upendo wa Kristo vitautayarisha na kuutuliza moyo kwa ajili ya mbegu njema ya Kweli. —**Letter 14, 1887.** {EVsw 142:3}

Epuka Kuchochea Mabishano na Upinzani

Jifunze kuwakuta watu mahali walipo. Usilete mada zitakazoamsha mabishano. Hebu mafundisho yako yasiwe ya kufadhaisha watu au kuyachanganya mawazo. —**Testimonies for the Church 6:58 (1900).** {EVsw 142:4}

Usichochee upinzani kabla watu hawajapata nafasi ya kusikia ile Kweli na kujua wanachokipinga. —**Testimonies for the Church 6:36 (1900).** {EVsw 143:1}

Usiwakimbize Watu Kutoka Kwenye Kweli

Sisis tumepewa wajibu mkuu wa kuiwasilisha Kweli kwa watu wasioamini kwa njia yenye nguvu. Jinsi tunavyopaswa kuwa waangalifu tusiiwasilishe Kweli kwa namna itakayowakimbiza watu! Walimu wa dini wamesimama mahali ambapo wanaweza kufanya mema makubwa au maovu makubwa…..{EVsw 143:2}

Bwana anatuita sisi kuja kwenye karamu ya Kweli, kisha kutoka kwenda njia kuu na pembezoni, na kuita/kukusanya roho kuja kwa njia ya kuiwasilisha dhabihu kuu na ya ajabu ambayo Kristo ameitoa kwa dunia. Tuwasilishe Kweli kwa namna ile ile Kristo aliyowaambia wanafunzi Wake—kwa unyenyekevu, usahili na upendo. —**Letter 177, 1903.** {EVsw 143:3}

Hebu na Muwajali Wachungaji wa Madhehebu Mengine

Daima ionekane wazi kwamba sisi ni wanamatengenezo, lakini siyo watu wenye misimamo mikali, au watu waliopitiliza kwa kukosa hekima. Wahubiri wetu wanapoingia katika eneo jipya la kazi, wanapaswa kujitahidi kufahamiana na wachungaji wa makanisa mbalimbali katika eneo hilo. Mengi yamepotezwa kwa kutochukua hatua hii. Ikiwa wahubiri wetu wataonyesha kuwa ni watu wenye moyo wa kirafiki na wanaochangamana na jamii, na pia watu wasiokuwa na aibu kuhusu ujumbe wao, hili litakuwa na matokeo mazuri, na huenda likawapa wachungaji hao na makusanyiko yao mtazamo mzuri juu ya ile Kweli. Angalau, ni sahihi kwa ajili ya kuwapa nafasi ya kuwa wema na wa msaada kama watataka.{EVsw 143:4}

Wahubiri wetu wawe waangalifu sana wasitoe taswira kwamba wao ni mbwa-mwitu wanaoiba kondoo, bali wawafahamishe wachungaji hao msimamo wao na lengo la huduma yao—kuelekeza watu kwenye Kweli za Neno la **Mungu**. Kuna Kweli nyingi ambazo zinapendwa na kugusa moyo wa Wakristo wote

(Asilimia 95% ya Biblia inapendwa na kila Mkristo!) Hapa ndipo kuna msingi wa pamoja kwamba sote tunafanana katika vipengele hivyo na kisha tunaweza kukutana na watu hawa wa madhehebu mengine; na tunapowafahamu, hebu tuzungumzie mambo ambayo yanagusa maslahi ya Wakristo wote, na ambayo hayatatupeleka moja kwa moja kwenye tofauti zetu za Mafundisho mauu ya imani (Doctrines). —**Review and Herald, June 13, 1912.** {EVsw 143:5}

Epuka Vizuizi Visivyo vya Lazima

Tunapoingia katika eneo jipya, hatupaswi kusimika vizuizi visivyo vya lazima kati yetu na madhehebu mengine, hasa Wakatoliki, kiasi cha kuwafanya wahisi kuwa sisi ni maadui wao wa dhahiri. Tusichochee chuki yao bila sababu kwa kufanya mashambulizi dhidi yao. Wapo wengi miongoni mwa Wakatoliki wanaoishi kulingana na nuru waliyo nayo kwa uaminifu zaidi kuliko wengi wanaodai kuamini Kweli ya sasa, na **Mungu** atawajaribu na kuwathibitisha kama anavyotujaribu na kututhibitisha sisi. —**Manuscript 14, 1887.** {EVsw 144:1}

Hitaji la Kuona kwa Macho ya Kiroho

Wakati, wakati wa thamani, umepotezwa. Fursa za dhahabu zimepita bila kutumiwa kwa sababu ya ukosefu wa uoni wa kiroho usio na uwazi na ukosefu wa busara ya kupanga na kutekeleza njia za kufadhaisha na kushinda adui na kuutwaa uwanja wa kazi....{EVsw 144:2}

Walinzi waliolala, je, hamjui ni wakati gani wa usiku? Je, hamhisi mzigo kwa ajili kupaza sauti ya tahadhari na kutoa onyo la wakati huu? Kama hamna, shukeni kutoka kwenye minara ya Sayuni, kwa kuwa **Mungu** hatakukabidhi nuru atakayotoa. Nuru hutolewa kwa wale tu watakaoitoa kwa wengine. —**Manuscript 107, 1898.**{EVsw 144:3}

Nidhamu/Staha Madhabahuni, Matangazo, na Mambo ya Awali

Heshima ya Mjumbe — Nidhamu ni ya lazima madhabahuni. Mhudumu wa Injili hapaswi kuwa mzembe katika mwonekano wake. Ikiwa yeye ni mwakilishi wa Kristo, mwenendo wake, mtazamo wake, na ishara zake vinapaswa kuwa vya namna ambayo havitawachukiza watazamaji. Wahudumu wanapaswa kuwa na adabu na uungwana/ustaarabu. Wanapaswa kuachana kabisa na mienendo isiyopendeza, mitazamo isiyofaa, na ishara zisizo na heshima, bali wajitahidi kuwa na unyenyekevu wenye heshima katika namna yao ya kujieleza. Wanapaswa pia kuvalia kwa namna inayolingana na heshima ya wadhifa wao. Maneno yao yafaa kuwa yenye uzito, yaliyochaguliwa kwa busara na yenye hekima katika kila hali. — **Testimonies for the Church 1:648, 649 (1868).**{EVsw 145:1}

Mwenendo Madhabahuni — Lakini mara nyingi mambo yasiyofaa hutendeka madhabahuni. Mhudumu mmoja akizungumza na mwingine mbele ya kusanyiko, wakicheka kana kwamba hawana mzigo wa kazi yao, au kuonekana kana kwamba hawana utambuzi wa uzito wa wito wao mtakatifu, jambo hili hudhalilisha Kweli na huleta mambo matakatifu katika kiwango cha kawaida kisicho na tofauti. — **Testimonies for the Church 2:612, 613 (1871).**{EVsw 145:2}

Kumchukiza Mungu — Wakati mwingine mikusanyiko ya watu wa **Mungu** imechukuliwa kama kitu cha kawaida kwa namna iliyomkera **Mungu** na kuondoa utakatifu na usafi katika kazi Yake takatifu. — **Letter 155, 1900.**{EVsw 145:3}

Epuka Kupoteza Muda kwa Kuomba Radhi — Wahubiri wengi hupoteza muda na nguvu kwa kuanza na maelezo marefu ya awali kwa kuomba radhi, au utambulisho mrefu. Wengine hutumia karibu nusu saa kwa kuomba msamaha; hivyo muda hupotea, na wanapofika kwenye ujumbe wao na kujaribu kuunganisha mawazo ya Ukweli katika akili za wasikilizaji, watu huwa wamechoka na hawawezi kuona uzito wa yale yanayosemwa.{EVsw 145:4}

Badala ya kuomba msamaha kwa sababu anaenda kuzungumza mbele ya watu, mhubiri anapaswa kuanza kana kwamba anajua anatoa ujumbe kutoka kwa **Mungu**. — **Gospel Workers, 168 (1915).**{EVsw 146:1}

Maombi ya Hadhara — Maombi yanayotolewa hadharani yanapaswa kuwa mafupi, yenye kueleweka na ya moja kwa moja. **Mungu** hahitaji tuufanye muda wa ibada kuwa wa kuchosha kwa maombi marefu yasiyoisha……. Dakika chache zinatosha kwa maombi ya kawaida ya hadhara. — **Gospel Workers, 175 (1915).** {EVsw 146:2}

Ombeni kwa Unyofu wa Moyo (dhati) — Hatuhitaji kutoa maombi marefu mbele ya watu. Kwa unyofu wa moyo na usahili, tunapaswa kueleza mahitaji yetu kwa Bwana, na kudai ahadi Zake kwa imani na ujasiri kiasi kwamba kusanyiko litajua kuwa tumejifunza jinsi ya kumlilia **Mungu** kwa mafanikio. Watu watatiwa moyo kwa kuamini kuwa uwepo wa Bwana umo mkutanoni, na watafungua mioyo yao kupokea baraka Zake tele. Imani yao juu ya uaminifu wako itaongezeka, nao watakuwa tayari kusikiliza kwa hamu mafundisho yatolewayo na mzungumzaji. — **Manuscript 127, 1902.**{EVsw 146:3}

Kuepuka Haraka-Haraka Isiyo ya Kawaida — Bwana alikupa kazi yako, sio ili ifanywe kwa kukurupuka, bali kwa namna ya utulivu, na busara. Bwana kamwe *hashurutishi* mijongeo ya haraka, yenye utata. — **Testimonies for the Church 8:189 (1904).**{EVsw 146:4}

Epuka Mienendo ya Ajabu — Hatuwezi kuwa wachungaji wa kundi la Bwana kama hatujaachana na tabia zetu binafsi, mazoea, na desturi, ili kufanana na Kristo (no peculiar habits). Tunapokula mwili Wake na kunywa damu Yake, basi vipengele vya uzima wa milele vitaonekana katika huduma. Hapatakuwa na maelezo yale yale ya zamani yanayorudiwa kila wakati. Kutakuwepo na uelewa mpya wa Ukweli.{EVsw 146:1}

Baadhi ya wanaosimama mimbarini huwafanya hata wajumbe wa mbinguni waliopo kati ya kusanyiko kuona aibu kwa niaba yao. Injili ya thamani, ambayo imeigharimu sana dunia kuipokea, hudhalilishwa. Kuna mazungumzo ya kawaida yasiyo na heshima; mienendo ya ajabu ya sura na mwili. Kwa baadhi, maneno hutamkwa kwa kasi kupita kiasi, kwa wengine hutamkwa kwa ugumu na kwa namna isiyoeleweka. Kila mmoja anayehudumu mbele ya watu anapaswa kuhisi kuwa ni wajibu wake mtakatifu kujithibiti binafsi. Anapaswa kwanza kujitoa mwenyewe kwa Bwana kwa kujikana kabisa, akiwa na azimio kwamba hatakuwa na lolote la binafsi, bali yote yatokane na Yesu. — **Testimonies to Ministers and Gospel Workers, 339 (1896).**{EVsw 147:1}

Ondoa Ishara Zisizofaa na Maneno Yasiyo ya Adabu au hata matusi — Mtendakazi wa **Mungu** anapaswa kufanya jitihada za dhati kuwa mwakilishi wa Kristo, kwa kuachana na ishara zote zisizofaa na maneno yasiyo na staha. Anapaswa kujitahidi kutumia lugha sahihi. Kuna kundi kubwa la watu wanaozembea katika namna yao ya kusema; lakini kwa juhudi za makusudi na umakini, wanaweza kuwa wawakilishi wa kweli wa Ukweli. Kila siku wanapaswa kupiga hatua na kusonga mbele. Hawapaswi kupunguza ufanisi na mvuto wao kwa kushikilia mapungufu ya mwenendo, sauti, toni au lugha. — **Counsels to Parents, Teachers, and Students, 238 (1913).** {EVsw 147:2}

Haiba au Hulka ya Mwinjilisti — Nafasi ya wachungaji wetu wa Injili inahitaji afya ya mwili na nidhamu ya akili. Akili yenye busara, mishipa imara, na tabia ya furaha vitamfanya mhudumu wa Injili afae kila mahali na kuwa utambulisho mzuri. Haya yanapaswa kutafutwa na kufanyiwa kazi kwa bidii kila wakati. — **Testimonies for the Church 3:466 (1875).**{EVsw 147:2}

Sifa Zinazovutia za Mafundisho ya Kweli

Kweli Inapaswa Kuvutia

Msijitahidi kufuata njia za ulimwengu, bali fuateni njia ya **Mungu**. Maonyesho ya nje hayawezi kutekeleza kazi ambayo Bwana anatamani ifanyike ili kuwaamsha watu wa tabaka la juu watambue kuwa wamesikia **Ukweli**. Msiitoe heshima ya **Ukweli** na uzito wake kwa mambo yanayofanana zaidi na ya kidunia kuliko ya mbinguni. Waelezeni wasikilizaji wenu waziwazi kuwa mikutano ya jioni ya Jumapili haikusudiwi kuwavutia kwa muziki au burudani nyinginezo, bali ni kwa ajili ya kuhubiri Ukweli kwa adhima/uzito wake wote, ili uwafikie kama onyo, ukiwaamsha kutoka usingizi wa mauti wa kujipenda nafsi. Ni Ukweli usiofunikwa, unaokatakata kama upanga mkali ndio wenye makali yakatayo kuwili…..{EVsw 148:1}

Wale wanaotegemea mipango ya kidunia ili kufanikisha kazi yao kwa ajili ya **Mungu** watashindwa. Bwana anataka mabadiliko ya namna ya kufanya kazi yenu. Yeye Anatamani mfanye mazoezi ya masomo aliyofundisha Kristo katika maisha Yake. Hapo ndipo sura ya **Kristo** itaonekana katika kila mkutano mnaoufanya. **— Letter 48, 1902.** {EVsw 148:2}

Ufundishaji wa Ubunifu

Mkuu wa walimu alitafuta kuwafikia watu kupitia njia zilizokuwa za kawaida katika maisha yao ya kila siku. Aliwasilisha mbele ya wasikilizaji wake Ukweli kwa namna ambayo uliunganishwa na kumbukumbu

na hisia zao takatifu. Mafundisho Yake yalionyesha mshikamano kamili na maslahi na furaha yao. Mafundisho Yake yalikuwa rahisi, vielelezo Vyake vilifaa, na maneno Yake yalijaa huruma na furaha kiasi cha kuwavutia sana wasikilizaji Wake.{EVsw 148:3}

Kristo alichota vielelezo na mafundisho Yake kutoka kwenye Jumba kuu la hazina ya asili. Alitwaa ua la lili (yangeyange nk) na kuwaelekeza wasikilizaji Wake katika urahisi na uzuri wake wa ajabu. Alionyesha majani ya kondeni akisema, **Mathayo 6:30** *"Ikiwa* ***Mungu*** *huyavika hivi majani ya kondeni, yaliyopo leo, na kesho hutupwa kalibuni, je, Hatazidi sana kuwavika ninyi, enyi wa imani Haba?"* Yeye Anataka tuelewe kuwa vitu vya asili ni taswira ya upendo wa **Mungu**, na kwamba, ingawa vimeharibiwa na dhambi, bado vinatukumbusha makazi ya Edeni ambamo Adamu na Hawa waliwekwa. Yeye Anataka vitu hivyo vitukumbushe wakati ambapo nyumba hiyo itarejeshwa, na dunia itajaa sifa za Bwana. — **Letter 213, 1902.**{EVsw 148:4}



Alivuta Shauku

Watu walilisikiliza Neno la rehema lililotiririka kwa wingi kutoka mdomoni mwa Mwana wa **Mungu**. Waliyasikia Maneno ya neema, rahisi na wazi kiasi kwamba yalikuwa kama dawa ya Gileadi kwa roho zao (Yeremia 8:22). Mguso wa mkono Wake wa Kiungu unaoponya, ulileta furaha na uhai kwa waliokuwa wanachungulia kaburi, na faraja na afya kwa walioteseka na magonjwa. Siku hiyo iliwatokea wanadamu kama mbingu duniani, kiasi kwamba hawakujua hata muda umepita kiasi gani, tangu walipokula mara ya mwisho…,,{EVsw 149:1}

Yeye aliyewafundisha watu njia ya kupata amani na furaha alikuwa na wazo pia juu ya mahitaji yao ya muda na ya kawaida kama Alivyojali yale ya kiroho. Watu walikuwa wamechoka na dhaifu. Kulikuwa na akina mama waliobeba watoto, na watoto wadogo waliokuwa wameshikilia mavazi ya wazazi wao. Wengi walikuwa wamesimama kwa saa nyingi. Walikuwa wamevutiwa sana na Maneno ya Kristo kiasi kwamba hawakuwahi kufikiria hata kuketi chini, na umati ulikuwa mkubwa kiasi cha kuwa na hatari ya watu kukanyagwa. Yesu aliwaambia waketi chini ili wapumzike. Mahali pale palikuwa na majani mengi, hivyo wote waliweza kupumzika kwa starehe au faraja. — **The Desire of Ages, uk. 365-366 (1898).** {EVsw 149:2}

Mpango Wa Kuvutia na Wenye Ufanisi

Nilionyeshwa maono mengine. Mahema yalihamishiwa maeneo tofauti wakati wa mikutano ya makambi. Mikutano hiyo ya kambi ilifanyika maeneo mbalimbali na kuongozwa na watu hodari, wacha **Mungu**, waliokuwa na wasaidizi wanaofaa. Kulikuwa na mikutano ya watoto, mikutano ya uamsho, na jitihada za dhati za kuwaongoza watu kufanya maamuzi. Paulo alipanda, Apolo akatia maji, bali Mwenye kukuza ni **Mungu** …. **1 Wakorintho 3:6.** {EVsw 150:1}

Hebu talanta ya uimbaji iletwe katika kazi hii. Matumizi ya vyombo vya muziki si tatizo kabisa. Vyombo hivyo vilitumika hata katika ibada za zamani. Waabudu walimsifu **Mungu** kwa vinubi na matoazi, na muziki unapaswa kuwa na nafasi katika ibada zetu. Muziki utaongeza mvuto na kupendeza.{EVsw 150:2}

Lakini zingatieni usikivu wa watu kwa kuwasilisha mbele yao Ukweli ulivyo ndani ya Yesu. Daima waonyesheni msalaba wa Kalvari. Ni nini kilichomfanya Kristo afe? Ni uvunjaji wa sheria. Kristo alikufa ili kuwapa wanadamu nafasi ya kuwa raia waaminifu wa ufalme Wake.{EVsw 150:3}

Hebu kuwepo na hotuba fupi, maombi yawe mafupi, ya bidii na yenye joto la kiroho. Fundisheni, fundisheni kuhusu huduma ya moyo wote. Kujitoa kikamilifu, maombi mengi, na bidii ya dhati, vitaleta matokeo; kwa kuwa malaika wa **Mungu** watakuwa hapo ili kugusa mioyo ya watu. — **Letter 132, 1898.**{EVsw 150:4}

Aina Tofauti za Mvuto wa Kiinjilisti

Katika mikutano hii, wanakusanyika matajiri na maskini, watu wa cheo na wa hali ya kawaida, wenye dhambi wa viwango vyote, na wote wakisikia ujumbe wa rehema kutoka kwa watumishi walioteuliwa na Bwana. Kuna mada mbalimbali za Biblia zinazowasilishwa, na shughuli mbalimbali za kiroho.{EVsw 150:5}

Wazee kwa vijana wanaitwa, na Bwana anagusa mioyo ya wasikilizaji. Kupitia njia hii, mwaliko wa karamu, kama ulivyo katika mfano, unafikishwa kwa wote. Wengine, kwa kauli zao wenyewe, walikiri kuwa hawajaingia kanisani kwa miaka kumi na mbili, kumi na nne, hata kumi na sita, lakini wanashawishika na kuongoka. Washiriki wa kanisa wanaamshwa kwa kina, wakisikiliza kwa mshangao mahubiri na masomo ya Biblia yanayofafanua Maandiko; na katika mikutano ya kijamii, kila mtu anapata jambo linalomfaa. — **Manuscript 7, 1900.**{EVsw 150:6}

Mada Kuu—Ujumbe Unaolingana na Wakati

Wale wanaosimama mbele ya watu kama walimu wa Kweli wanapaswa kushughulika na mada kuu. Hawapasi kupoteza muda wa thamani kwa kujadili mambo madogo. Hebu na wajifunze Neno, na walihubiri Neno. Na Neno liwe mikononi mwao kama upanga mkali wenye makali kuwili. Na lishuhudie Ukweli wa zamani na kuonyesha mambo yajayo. {EVsw 151:1}

Kristo alikuja kutoka mbinguni kumletea Yohana Kweli kubwa na za ajabu zinazopaswa kujenga maisha yetu, na ambayo sisi tunapaswa kuitangaza kwa ulimwengu. Tunapaswa kutunza wakati huu, tukitoa ushuhuda ulio wazi, na wenye akili, tukiwa tumeongozwa na upako wa Roho Mtakatifu. **— Review and Herald, April 19, 1906.**{EVsw 151:2}

Mikutano ya Maswali na Majadiliano

Waiteni Wanaovutiwa Baada ya Mkutano

Ukweli wa kujaribu wa wakati huu unapaswa kufahamika na maelezo kutolewa. Tabaka zote—watu wa tabaka za juu na wale wa hali ya chini kabisa—hushiriki katika mikutano hii, na tunapaswa kuwahudumia wote. Baada ya ujumbe wa onyo kutolewa, waiteni wale waliovutiwa kwa namna ya pekee waende kwenye hema pekee yao, kisha fanyeni kazi ya kuongoa mioyo yao. Kazi hii ni ya kimishenari ya kiwango cha juu kabisa. —**Letter 86, 1900.**{EVsw 151:3}

Fundisheni Watu Jinsi ya Kuwa WaKristo

Napenda muelewe jambo hili kwa wazi: nafsi nyingi hukosa kutii Kweli kwa sababu ya kuchanganyikiwa kwa mawazo, na pia kwa sababu hawajui namna ya kujisalimisha kwa Yesu—nia zao na mapenzi yao. Wanahitaji mafundisho ya pekee kuhusu jinsi ya kuwa WaKristo. Kazi inayofanywa kwa ajili ya Kristo ulimwenguni si matendo makubwa au ya ajabu. Hayo huja panapohitajika. Lakini kazi yenye mafanikio zaidi ni ile inayoiwezesha nafsi kujifikiria yenyewe kwa udogo kwa kadri iwezekanavyo (kuondoa umimi). Ni kazi ya kuwapa watu mafundisho mstari kwa mstari, amri juu ya amri—hapa kidogo, pale kidogo—kwa kugusa mioyo ya watu kwa njia ya huruma. Hii ndiyo huduma inayofanywa kwa Yesu Kristo ambayo itatambuliwa katika siku ya mwisho. —**Letter 48, 1886.**{EVsw 152:1}

Kuwa Karibu na Watu Baada ya Hotuba

Kuna hatari ya kupita kwa haraka kutoka hoja moja hadi nyingine. Toeni mafundisho mafupi, lakini mara kwa mara. Baada ya kufungua hazina za Kweli kwa watu, bado kuna kazi kubwa ya kuwahudumia wale waliovutiwa na yale yaliyowasilishwa.{EVsw 152:2}

Baada ya mahubiri mafupi, badilisheni utaratibu wa ibada, na toeni nafasi kwa wale wote wanaotaka kubaki kwa ajili ya mazungumzo ya baada ya ibada au darasa la Biblia, ili waweze kuuliza maswali kuhusu mambo yanayowatatiza. Mtapata mafanikio makubwa kwa kukaa kwa karibu katika Mafundisho haya ya Biblia. Watenda kazi wanaoshirikiana na mchungaji/mhubiri wanapaswa kujitahidi kwa subira na upole kuwaongoza wanaouliza kuelewa Ukweli.{EVsw 152:3}

Hata kama unaye mmoja tu wa kumfundisha, mtu huyo akishaamini kikamilifu, atawashirikisha wengine nuru aliyoipokea. Hizi Kweli za kujaribu ni za muhimu mno kiasi kwamba zinapaswa kuwasilishwa tena na tena, na kupandikizwa katika akili za wasikilizaji. —**Special [153] Testimonies, Series A, No. 7, p. 7. (1874).**{EVsw 152:4}

Nafasi ya Kuuliza Maswali

Pale inapowezekana, kila hotuba muhimu inapaswa kufuatiwa na somo la Biblia. Hapa hoja zilizowasilishwa zinaweza kutumika moja kwa moja, maswali yanaweza kuulizwa, na mawazo sahihi yanapaswa kufundishwa. Muda mwingi unapaswa utolewe kwa ajili ya kuwafundisha watu na kuwapa nafasi ya kujieleza. Watu wanahitaji mafundisho haya, mstari kwa mstari, amri juu ya amri.{EVsw 153:1}

Mikutano maalum pia inapaswa kufanywa kwa ajili ya wale wanaoanza kuvutiwa na Ukweli na wanahitaji mafundisho zaidi. Waalike watu kwenye mikutano hii—waumini na wasioamini—na wote wapewe nafasi ya kuuliza maswali kuhusu mambo wasiyoyaelewa vizuri. Wapeni nafasi watu wote kueleza mashaka yao, kwa kuwa hakika watakuwa nayo. Katika kila mahubiri na kila somo la Biblia, watu waonyeshwe kuwa kila hoja ina msingi wake katika Maneno ya wazi ya **Mungu**: “Asema Bwana.”{EVsw 153:2}

Hii ndiyo njia ambayo Kristo alitumia kufundisha. Alipoongea na watu, waliuliza maana ya maneno Yake. Kwa wale waliokuwa wakitafuta nuru kwa unyenyekevu, Alikuwa tayari kuwafafanulia. Lakini Kristo hakuhimiza malalamiko wala ubishi—wala nasi hatupaswi kufanya hivyo. Wakati watu wanapojaribu kuleta mabishano kuhusu hoja tata za mafundisho, waambieni kuwa mkutano haukuwekwa kwa ajili ya madhumuni hayo.{EVsw 153:3}

Unapojibu swali, hakikisha wasikilizaji wanaona na kukiri kuwa limejibiwa. Usiruhusu swali kuachwa bila jibu ukisema litaulizwa tena. Endelea hatua kwa hatua, ukifahamu ni kiasi gani umefanikiwa.{EVsw 153:4}

Katika mikutano hii, wale wanaofahamu ujumbe wanaweza kuuliza maswali yatakayofunua mwanga watu juu ya hoja za Kweli. Lakini wengine huenda wasiwe na hekima ya kufanya hivyo. Wakati maswali yanayopandikiza mashaka na kuchanganya akili yanapoulizwa, waonyeni waache kufanya hivyo. Tunapaswa kujifunza wakati gani wa kusema, na wakati gani wa kukaa kimya; kujifunza kupanda mbegu za imani na kueneza nuru—si giza. —**Testimonies for the Church, 6:68, 69 (1900).**{EVsw 153:5}

Wavutieni Watu kwa Maswali

Baada ya hotuba fupi, bakia ukiwa mchangamfu (fresh), ili uweze kufanya somo la Biblia kuhusu hoja ulizozizungumza, ukiwavutia watu kwa maswali. Nenda moja kwa moja kwenye mioyo ya wasikilizaji wako, ukiwahimiza waeleze shida zao kwako, ili uweze kuwaeleza Maandiko wasiyoyafahamu. —**Letter 8, 1895.**{EVsw 154:1}

Jambo la Kulilinda kwa Umakini

Kila mara Bwana anapokuwa na kazi maalum ya kufanya miongoni mwa watu Wake, na Anapotaka kuwachochea kufikiri kuhusu Kweli za uzima, Shetani hufanya kazi ya kugeuza fikra kwa kuanzisha mijadala ya hoja ndogo-ndogo zisizo za msingi. Lengo lake ni kuleta mgawanyiko na kuwatoa watu kwenye usikivu kwa hoja ya muhimu.{EVsw 154:2}

Mara nyingi wakati huu ambapo Bwana anaweka ujumbe Wake mioyoni mwa watu kwa ajili ya wokovu wao, Shetani huvuta mawazo yao kwenda kwenye jambo lisilo la maana, na kuwagawa kwa jambo hilo dogo, hadi mioyo yao ifungike dhidi ya nuru na kweli. Hapo ndipo Shetani hufurahi kwa ushindi wa kijinga. —**The Review and Herald, Oktober 18, 1892.**{EVsw 154:3}

Roho ya Mabishano, Malumbano, au Ugomvi Huua Ushahidi

Shetani hufanya kazi kwa bidii ili kuwavuta watu kwenye mambo ya dunia, ili Kweli ipoteze nguvu yake moyoni; na hapo hakutakuwa na maendeleo yoyote kutoka kwenye nuru na maarifa hadi kwenye nuru kuu zaidi. Pasipo wafuasi wa Kristo kuamshwa kila mara kuishi katika Kweli, hawatatakaswa kupitia kwayo. Maswali, hoja, nadharia zisizo na mashiko, mashaka, na mambo yasiyo ya msingi yanachota akili, na kuwa maudhui ya mazungumzo; kutakuwa na ubishi juu ya maneno, na mawazo tofauti-tofauti kuhusu vipengele visivyo muhimu.....{EVsw 154:3}

Mtenda kazi wa **Mungu** lazima awe na hekima ya kuona hila ya adui, na akatae kupotoshwa au kuhamishwa fikra na kupindishwa akili. Kazi yake kuu inapaswa kuwa uongofu wa mioyo ya wasikilizaji wake. Hebu na aepuke mabishano na ahubiri Neno la **Mungu**.{EVsw 155:1}

Kazi ya pekee ya udanganyifu ya Shetani imekuwa ni kuanzisha mabishano, ili kuwe na mabishano juu ya maneno yasiyofaa na yasiyo na tija. Anajua kuwa haya yatahusisha akili na wakati, yatainua roho ya malumbano, na kuua roho ya ushuhuda wa kweli. Hii husababisha mitazamo tofauti, mashutumu, na chuki ambayo hufunga milango dhidi ya Kweli. —**The Review and Herald, September 11, 1888.**{EVsw 155:1}

Kuomba na Walio Chini ya Usadikisho

Wachungaji na wahubiri waendelee kuwa na nyakati za maombi ya dhati pamoja na wale wanaoguswa na ile Kweli. Kumbukeni kuwa Kristo Yuko pamoja nanyi kila wakati. Bwana amekwishaandaa maonyesho ya thamani ya neema Yake ili kuwatia nguvu na kuwahimiza wale wanaofanya kazi kwa unyenyekevu na kwa moyo mnyofu. —**Manuscript 78, 1900.**{EVsw 155:2}

Wasaidieni Wenye Fadhaa

Wengi wanaokuja kwenye mikutano hubeba mizigo mizito ya dhambi. Hawaoni usalama katika imani yao ya kidini. Hebu fursa itolewe kwa wale wenye shida na wanaotamani kupata pumziko la roho wapate msaada. Baada ya hotuba, waalikeni wale wanaotamani kumfuata Kristo kuonyesha shauku yao. Waambieni wote ambao hawana hakika kuwa wako tayari kwa kurudi kwa Kristo, na wale wote wanaojihisi kubeba mizigo mizito, wakutane mahali pa faragha. Wale walio wa kiroho wazungumze nao, waombe pamoja nao na kwa ajili yao. Tengeni muda mwingi kwa maombi na kuchunguza kwa undani Neno la **Mungu**. Kila mmoja apate uhalisia wa imani katika nafsi yake kwa kuamini kuwa Roho Mtakatifu atamiminwa kwao kwa sababu wana njaa na kiu ya haki. Wafundisheni jinsi ya kujisalimisha kwa **Mungu**, jinsi ya kuamini, jinsi ya kudai ahadi Zake. Na upendo wa **Mungu** wa kina uonyeshwe kwao kupitia maneno ya faraja na maombezi. — **Testimonies for the Church 6:65 (1900).**{EVsw 155:4}

Kujitambulisha kwa Watu na Kufahamiana

Kukutana na Watu Wanapokuja na Kuondoka — Katika kuendesha kazi muhimu ya mikutano karibu na jiji kubwa, ushirikiano wa watendakazi wote ni wa lazima. Wanapaswa kuwa katika mazingira ya mikutano, wakijitambulisha kwa watu wanapokuja na kuondoka, wakionesha uungwana wa hali ya juu, upole na huruma nyororo kwa ajili ya roho zao. Wanapaswa kuwa tayari kuzungumza nao wakati ufaao na usiofaa, wakikesha kwa ajili ya kuongoa roho. Laiti watendakazi wa Kristo wangekuwa na nusu ya uangalifu ambao Shetani anao, ambaye siku zote yuko macho, akiwavizia wanadamu, na kutafuta mtego wa kuwaangamiza. — **Testimonies For The Church 6:46 (1900).** {EVsw 156:1}

Wajibu wa Mwinjilisti kwa Wale Waliovutiwa — Ni jambo muhimu kwa wale wote wanaokusudia kufanya kazi katika shamba la **Mungu** kujifunza njia bora kabisa ya kutekeleza kazi yao... Nimeonyeshwa kuwa juhudi nyingi zilizogharimu fedha nyingi kwa ajili ya kuwasilisha Ukweli, hazikufanikiwa kwa kiwango kikubwa kwa sababu kazi mahsusi iliyohitajika haikufanyika. Tumekuwa tukijaribu kwa miaka mingi kuwaeleza watu wetu juu ya umuhimu wa kufanya kazi kwa maarifa zaidi.....{EVsw 156:2}

Hotuba inapowasilishwa mimbari, hapo ndipo kazi inaingia tu katika hatua ya awali. Kisha, mchungaji anapaswa, kwa jitihada-binafsi ikiwezekana, kujitambulisha kwa kila msikilizaji wake. Ikiwa wameonyesha nia ya kuja na kusikiliza unalosema, basi ni wajibu wako pia kuonyesha nia ya dhati kwa kujua hali yao binafsi.....{EVsw 157:1}

Shetani na mawakala wake ni werevu kuliko watendakazi wetu. Wakati yeye anapanga kwa makini mitego ya kuwanasa watu bila kujua, ndugu zetu mara nyingi wanachukua mambo kwa urahisi mno, hivyo Shetani anawazidi mbinu karibu kila wakati. Sasa, kama wanataka uwanja wa kazi ujazwe na **Mungu** na

malaika wa mbinguni, ni lazima waweke nafsi zao zote — roho, mwili, na akili — katika kazi ya **Mungu**, na si kufanya kazi kwa jina tu, wakati kazi yenyewe haijakamilika hata nusu.....{EVsw 157:2}

Hotuba ya mimbari haipaswi kuwa ndefu, kwa kuwa huwachosha watu, na pia humchukua muda na nguvu mhubiri kiasi kwamba hawezi tena kujihusisha na kazi yake binafsi inayopaswa kufuatilia. Anapaswa kutembelea nyumba kwa nyumba, na kufanya kazi na familia, akielekeza mawazo yao kwenye Kweli za milele zilizomo katika Neno la **Mungu**. Akiifanya kazi hii kwa unyenyekevu wa Kristo, hakika atakuwa na malaika wa **Mungu** wakishirikiana naye. Lakini sisi tumekuwa na imani kiasi kidogo mno, imani na mawazo yetu ni finyu mno, pamoja na mipango yetu. — **Manuscript 14, 1887.**{EVsw 157:3}

Mhubiri atafahamiana na wazazi na watoto katika kusanyiko lake, na atasema nao maneno ya fadhili na ya dhati. — **Review and Herald, January 21, 1902.** {EVsw 158:1}

Ingia Ndani ya Familia — Kuwa karibu na watu; ingia katika familia zao kila inapowezekana; usisubiri watu wakutafute kama mchungaji. Kuwa na ujasiri na hakikisho la imani inayoonyesha wazi kwamba hautegemei hekaya zisizo na msingi bali unasimama juu ya, "Ndivyo Asemavyo Bwana." — **Letter 8, 1895.**{EVsw 158:2}

Mawasiliano (contacts) Katika Mikutano ya Umma na walengwa kwa mtupo wa jicho — Kristo alipokuwa akifundisha duniani, Alikuwa akitazama nyuso za wasikilizaji Wake, na kwa macho angavu, uso wenye shauku, vilimwambia mara moja mtu alipokubaliana na Ukweli. Vivyo hivyo, walimu wa watu leo wanapaswa kusoma nyuso za wasikilizaji wao.{EVsw 158:3}

Wanapoona mtu katika hadhira anayeonekana kuvutiwa, wanapaswa kufanya bidii kumfahamu kabla ya kuondoka mahali pa mkutano, na, ikiwezekana, wajue anakaa wapi, na wamtembelee. Ni kazi hii binafsi inayosaidia kumfanya mhudumu kuwa mhudumu asiyetahayari. Humpa nafasi ya kuonyesha ushahidi wa huduma yake. Hii pia ndiyo njia yenye mafanikio zaidi ya kuwafikia watu; kwa kuwa kwa njia hii ndipo umakini wao hutwaliwa na kushikwa kwa urahisi. — **Historical Sketches, uk. 147-148 (1886).** {EVsw 158:4}

Kupata Ujasiri Kupitia Mikutano ya Nyumbani — Kuna familia nyingi ambazo haziwezi kufikiwa na Ukweli wa Neno la **Mungu** isipokuwa kwa njia ya mawakili wa neema mbalimbali za Kristo kuingia nyumbani mwao, na kwa huduma ya dhati, iliyotiwa muhuri wa baraka na Roho Mtakatifu, kubomoa vizuizi na kuingia katika mioyo ya watu. Watu wanapoona kwamba watenda kazi hawa ni wajumbe wa rehema, wahudumu wa neema, huwa tayari kusikiliza maneno yao.

Lakini mioyo ya wale wanaofanya kazi hii lazima idunde sambamba, na moyo wa Kristo. Wanapaswa kujitoa kikamilifu, kujiweka wakfu, kwa huduma ya **Mungu**, tayari kutekeleza mapenzi Yake, kwenda popote Atakapowaongoza kwa mkono wa uongozi Wake, na kusema Maneno atakayowapa. Na ikiwa watakuwa jinsi **Mungu** anavyotaka wawe, ikiwa wamejazwa na Roho Wake Mtakatifu, basi hushirikiana na majeshi ya mbinguni na hakika huwa "wafanya kazi pamoja na **Mungu**." — **Letter 95, 1896.** {EVsw 158:5}

Mahubiri Yaliyochapwa Kwenye Machapisho

Matumizi Muhimu ya Machapisho—

Ukweli unapaswa kutangazwa kwa wingi zaidi na kusambaa kuliko ilivyo kwa sasa. Unapaswa kufafanuliwa kwa mistari ya wazi, thabiti mbele ya watu. Unapaswa kuwasilishwa kwa hoja fupi lakini za kuthibitisha, na mipango iwekwe ili kila mkutano ambapo Ukweli umetangazwa kwa watu, uweze kufuatwa na usambazaji wa majarida na vipeperushi vidogo vidogo. Kwa sasa inaweza kuwa lazima kuvisambaza vitu hivi bila malipo, lakini vitakuwa nguvu ya wokovu, na hakuna kitakachopotea. {EVsw 159:1}Hotuba zinazotolewa mbele ya umati kwenye mimbari, zitakuwa na nguvu zaidi endapo vitabu na machapisho yatagawanywa kwa kusambaza, kuwafunza wasikilizaji kuhusu Mafundisho ya Biblia. **Mungu** atafanya wengi wa kuwa na hamu ya kusoma, lakini pia kutakuwa na wengi watakaokataa kuona au kusikia chochote kuhusu Ukweli wa sasa. Lakini hatupaswi hata kufikiri hali hizi kuwa hazina tumaini, kwa kuwa Kristo anawavuta wengi Kwake.... Unapaswa kutoka ukiwa mkononi mwako, ukiwa umejaa machapisho yanayofaa ya kusoma, na moyo wako ukiwa umejaa upendo wa **Mungu**. —**Letter 1, 1875.**{EVsw 159:2}

Kuzuia Athari za Upinzani

Wakati hotuba inapotolewa, watu wanaweza kusikiliza kwa hamu, lakini yote ni mapya na ya ajabu kwao, na Shetani yuko tayari kupendekeza mawazo mengi yasiyo ya kweli kichwani mwao. Adui atajaribu kubadilisha na kukanusha maneno ya mzungumzaji. Basi sisi tufanye nini? {EVsw 159:3}

Hotuba zinazotoa sababu za uwepo wa imani yetu zinapaswa kuchapishwa katika vipeperushi vidogo, na kusambazwa kwa wingi kadri iwezekanavyo. [Kumbuka.—Kuhusu uchapishaji au kutumia muswada wa mahubiri kwa njia ya mitambo (mimeograph), kila mtendakazi anapaswa kushirikiana kwa makubaliano na ushauri wa Kamati ya Konferensi Kuu kama ilivyoainishwa katika azimio lililochukuliwa December 15, 1941, linalohusu usalama wa maneno yetu mbele ya umma:{EVsw 160:1}

"Kabla ya kuchapishwa, hotuba zote za mitambo na zilizochapishwa ziidhinishwe kwanza na viongozi wa koferensi mahalia sehemu ambayo unahudumu, kama hatua ya kuwalinda."]. Hivyo uongo na udanganyifu unaojaribu kusambazwa na adui wa Kweli utafunuliwa kwa asili yake halisi, na watu watapata nafasi ya kujua hasa alichosema mchungaji. —**The Review and Herald, Oktoba 14, 1902.**

Hotuba Fupi Zilizochapishwa

Hebu muhtasari wa hotuba uchapishwe na kusambazwa kwa upana. —**Manuscript 42, 1905.** {EVsw 160:2}

Vipeperushi au hata Matangazo ya Kuwakaribisha Watu Kwenye Mkutano

Iwapo mashine ya kuchapisha itapatikana, itakayofanya kazi wakati wa mkutano, kuchapisha vipeperushi, matangazo na karatasi za kusambaza, itakuwa na ushawishi mkubwa. —**Testimonies For The Church 6:36 (1900).**{EVsw 160:3}

Baadhi ya Watu Hufikika Kupitia Machapisho Pekee

Mafanikio makubwa zaidi yanaweza kupatikana kupitia mchungaji hai kwa kusambaza karatasi na vipeperushi kuliko kwa kuhubiri Neno peke yake bila machapisho……. Akili nyingi hufikika hivi na sio kwa njia nyingine. Hii ni kazi ya kweli ya utume ambayo kazi na fedha zinaweza kuwekezwa kwa matokeo bora zaidi. —**Life Sketches, uk. 217 (1915).**{EVsw 160:4}

Nguvu ya Vyombo vya Habari au Media, na Mitambo ya uchapishaji

Vyombo vya habari ni njia yenye nguvu ya kuhamasisha akili na mioyo ya watu. Watu wa dunia hii huchukua vyombo vya habari, media, mtandao na machapisho na kutumia kila nafasi kueneza machapisho yenye sumu kwa watu. Ikiwa watu, chini ya roho ya ulimwengu na Shetani, wana hamu kubwa ya kusambaza vitabu, vipeperushi, na machapisho yenye kuharibu roho, ni lazima wewe uwe na hamu kubwa zaidi ya kupata machapisho yenye kuelimisha na kuokoa watu.{EVsw 160:5}

Mungu ameweka chini ya usimamizi wa watu Wake faida katika vyombo vya habari, vinapounganishwa na taasisi nyingine, vitakafanikisha kusambaza maarifa ya Kweli. Vipeperushi, karatasi, na vitabu, kama inavyohitajika, vinapaswa kusambazwa katika miji na vijiji vyote nchini. —**Life Sketches, uk. 216, 217 (1915).** {EVsw 161:1}

Ukweli Unapewa Mabawa

Kuna haja kubwa ya kuwa na watu wanaoweza kutumia vyombo vya habari, mtandao, machapisho nk vyema ili Ukweli upate mabawa ya kuruka na kufikia kila taifa, kila lugha, na kila jamaa. —**Gospel Workers, 25 (1915).**{EVsw 161:2}

Ukurasa Uliochapishwa

Ingawa mchungaji anaweza kuwasilisha ujumbe kwa uaminifu, watu hawawezi kukumbuka yote. Kwa hiyo, ukurasa uliochapishwa ni muhimu si tu kuwahamasisha juu ya umuhimu wa Ukweli kwa wakati huu, bali pia kuimarisha na kusimika mizizi ya Ukweli, na kuuweka imara dhidi ya makosa ya udanganyifu. Machapisho ni njia ya Bwana ya kuweka ujumbe wa wakati huu mbele ya watu kila wakati. Katika kuangaza na kuimarisha roho katika Ukweli, machapisho yatafanya kazi kubwa zaidi kuliko huduma ya Neno peke yake. Wajumbe wa kimya wanaoachwa katika nyumba za watu kupitia kazi ya wainjilisti wa vitabu (wauzaji) wa vitabu watasaidia kuimarisha huduma ya Injili kwa kila njia; maana Roho Mtakatifu atavuta akili za wasomaji wanaposoma vitabu, kama anavyoleta hisia za watu wanaosikiliza hubiri la Neno. Huduma hiyo hiyo ya malaika huambatana na vitabu vinavyobeba Ukweli kama inavyofanyika kwa njia ya huduma ya Neno. —**Testimonies For The Church 6:315, 316 (1900).**{EVsw 161:3}

Mjadala

[Tazama pia kurasa 301-306, "Kukabiliana na Chuki na Upinzani."]

Mungu Hutukuzwa Kidogo — Katika baadhi ya nyakati, inaweza kuwa muhimu kukabiliana na mtu mwenye kiburi anayeipinga Kweli ya **Mungu** kwa mjadala wa wazi; lakini kwa kawaida, mijadala hii, iwe ya maneno au maandishi, husababisha madhara zaidi kuliko manufaa. —**Testimonies For The Church 3:213 (1872).** {EVsw 162:1}

Mijadala haiepukiki mara zote.... Watu wanaopenda kuona wapinzani wakilumbana, hutaka mijadala. Wengine, wana shauku ya kusikia ushahidi kutoka pande zote mbili, wanaweza kuchochea mjadala wakiwa na makusudi yote ya uaminifu; lakini pale mijadala inapoweza kuepukwa, inapaswa kuepukwa.... **Mungu** hutukuzwa kwa udogo au Ukweli hauendelei katika malumbano haya. —**Testimonies For The Church 3:424 (1875).** {EVsw 162:2}

Wapinzani Wakati Mwingine Lazima Wakabiliwe— Kuna nyakati ambapo uongo wao wa wazi lazima ukabiliane nao. Hata hivyo, inapaswa kufanyika haraka na kwa ufupi, halafu tuendelee na kazi yetu. — **Testimonies For The Church 3:37 (1872).**{EVsw 162:3}

Kukabiliana na Upinzani Bila Kupinga — Katika kuwasilisha Ukweli usiopendwa, ambao unahusisha mzigo mzito, wachungaji (wahudumu) wanapaswa kuwa waangalifu kwamba kila Neno liwe kama **Mungu** anavyotaka. Maneno yao hayapaswi kuwa ya kuumiza na kukatakata. Wanapaswa kuwasilisha **Ukweli** kwa unyenyekevu, kwa upendo mkubwa kwa ajili ya roho, na shauku ya dhati ya wokovu wao, na waruhusu Ukweli ufanye kazi ya kukata. Hawapaswi kuwapinga wachungaji/wahudumu wa madhehebu mengine, wala kujaribu kusababisha mjadala. Hawapaswi kusimama kama Goliathi alipolikabili jeshi la Israeli. Israeli haikumpinga au kumlaani Goliathi, bali Goliathi ndiye aliyetamka kwa kiburi dhidi ya **Mungu** na watu Wake. Upinzani, kiburi, laana na kejeli vinapaswa kutokea kwa wapinzani wa Ukweli, ambao ni kama Goliathi. Lakini roho hii haipaswi kuonekana kwa wale waliotumwa na **Mungu** kuhubiri ujumbe wa mwisho wa onyo kwa dunia usio na matumaini ya wakati ujao.{EVsw 162:4}

Kama kwa Daudi, watu wakipata nafasi ambapo kazi ya Mungu inawataka wakabiliane na mpinga Israeli, na wakatoka kwa nguvu za **Mungu**, wakimwamini Yeye peke yake, basi Yeye Atawasaidia na kuifanya Kweli Yake ishinde kwa utukufu. Kristo ametupa mfano. “Lakini Mikaeli Malaika Mkuu, alipokuwa anashindana na Ibilisi kuhusu mwili wa Musa, hakutaka kumshambulia kwa maneno ya kejeli, bali alisema, Bwana akukemee.”—**Testimonies For The Church 3:218-220 (1872).**{EVsw 163:1}

Roho ya Migogoro Huweka Msingi Dhaifu — Roho ya kutaka mjadala, ya ugomvi, ni mbinu ya Shetani kuchochea hasira na magomvi na hivyo kuficha Ukweli ulioko katika Yesu. Wengi wamekatishwa tamaa, na kuchukizwa badala ya kuvutwa kwa Kristo.....{EVsw 163:2}

Roho ya mjadala inahamasishwa. Wengi huonekana wanazingatia mada za Mafundisho ya imani kwa karibu, lakini uchaji **Mungu** halisi, kumjua **Mungu** kwa uzoefu, havipati kipaumbele (vinapata usikivu mdogo). Yesu, upendo Wake na neema, kujikana Kwake nafsi na kujitoa kwa ajili yetu, unyenyekevu Wake na uvumilivu, havidhihirishwi mbele ya watu kama inavyostahili. Makosa yanayoonekana kila mahali, kama vimelea, yamefunga sumu yao ya mauti kwenye matumbo (hatari) juu ya matawi ya Ukweli, na mioyo mingi inajitambulisha na roho hii; wengi wanaokubali Ukweli huufundisha kwa roho yenye ukali. Hivyo, watu hupokea dhana yake ya uongo , na Ukweli hauwezi kufanya kazi kwa wale ambao mioyo yao haijalainishwa wala haiko chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu....,,{EVsw 163:3}

Ni muhimu kwa wote kutambua na kuthamini Ukweli; kwa hiyo ni muhimu sana mbegu ya Neno iangukie katika udongo ulio tayari kuipokea. Swali kwetu binafsi linapaswa kuwa, Tutapandaje mbegu ya Kweli kwa namna gani ili isipotee, bali iote na kuzaa mavuno, ili miganda iletwe kwa Bwana? —**The Review and Herald, February 9, 1892.**{EVsw 164:1}

Hatari ya Hisia (Msisimko) Kali na Maamuzi ya Haraka — Ikiwa shauku inaongezeka kwa kasi, na watu wanasonga kwa uelewa, na wala haitokani na msukumo, lakini ni kutokana na kanuni, maslahi ni ya afya zaidi na ya kudumu kuliko pale ambapo kuna msisimko mkubwa na shauku hulipuka kwa ghafla, na hisia husisimuka kwa kusikiliza mjadala, mchuano mkali kwa pande zote mbili za swali, ama kwa kuunga mkono Ukweli au kwa kuwa kinyume cha Ukweli. Kwa hivyo upinzani mkali unaundwa, misimamo inachukuliwa, na maamuzi ya haraka hufanywa. Na matokeo yake ni hali ya homa ya mambo. Kuzingatia kwa utulivu na kufanya maamuzi kunahitajika/hakupo. Wacha msisimko huu utulie, au acha mwitikio ufanyike kwa

usimamizi usio na busara, na shauku haiwezi kuoneshwa tena. Hisia na huruma za watu zilichochewa; lakini dhamiri zao hazikusadikishwa, na mioyo yao haikuvunjika na kunyenyekezwa mbele za **Mungu**. —**Testimonies For The Church 3:218 (1872).**{EVsw 164:2}

Kuwasilisha Ukweli kwa Mioyo Yenye chuki au Ubaguzi — Watumishi wa **Mungu** wasihesabu fursa za kujishughulisha na mijadala kama upendeleo mkubwa. Vipengele/Pointi zote za imani yetu zisibebwe na kuwasilishwa mbele ya umati wa watu wenye ubaguzi. Yesu alizungumza mbele ya mafarisayo na masadukayo kwa mafumbo, akificha uwazi wa Ukweli chini ya ishara takwimu kwa sababu wangeutumia vibaya Ukweli uliowasilishwa mbele yao; lakini kwa wanafunzi Wake alizungumza waziwazi. Tunapaswa kujifunza kutoka kwa njia za Kristo na kuwa makini ili tusikate masikio ya watu katika kuwasilisha Ukweli, ambao bado haujafafanuliwa vya kutosha, na watu hawako tayari kuupokea. Kweli ambazo tunazishikilia kwa pamoja zinapaswa kuzingatiwa kwanza na ujasiri wa wasikilizaji upatikane. —**Testimonies For The Church 3:426 (1875).**{EVsw 164:2}

Katika Mjadala Tunakutana na Shetani — Wahudumu wanaoshindana na wapinzani wa Kweli ya **Mungu** sio lazima wakutane na wanadamu tu, bali Shetani na jeshi lake la malaika waovu. Shetani hutafuta nafasi ya kupata faida ya wachungaji wanaotetea **Ukweli**, na wanapoacha kuweka imani yao yote kwa **Mungu**, na maneno yao hayako katika roho na upendo wa Kristo, malaika wa **Mungu** hawawezi kuwaimarisha na kuwaangazia. Wanawaacha kwa nguvu zao wenyewe, na malaika waovu wanashinikiza giza lao; kwa sababu hii wapinzani wa Ukweli nyakati fulani wanaonekana kuwa na faida, na majadiliano yana madhara zaidi kuliko manufaa halisi. —**Testimonies For The Church 3:220, 221 (1872).**{EVsw 165:1}

Ikiwa Mjadala Hauepukiki — Na wakati wowote inapohitajika kwa maendeleo ya kusudi la Ukweli na utukufu wa **Mungu** kwamba mpinzani afikiwe, basi wanapaswa kuingia kwenye pambano hilo kwa uangalifu na unyenyekevu kiasi gani. Kwa kujichunguza moyo, kuungama dhambi, na kuomba kwa bidii, na mara nyingi kufunga kwa muda, wanapaswa kuomba kwamba **Mungu** awasaidie na kuwapa Ukweli Wake unaookoa, wa thamani, ushindi mtukufu, ili makosa yaonekane katika uharibifu wake wa kweli na watetezi wake waaibike kabisa…….{EVsw 165:2}

Kamwe haupaswi kuingia kwenye mijadala inayoweka mambo mengi hatarini, ukitegemea uwezo wako wa kushughulikia hoja zenye nguvu. Ikiwa haiwezi kuepukwa vema, basi ingia katika hilo pambano, lakini ingia ukiwa na imani thabiti kwa **Mungu** na kwa roho yaunyenyekevu, kwa roho ya Yesu, ambaye amekuambia ujifunze Kwake Yeye, ambaye ni mpole na mnyenyekevu wa moyo. **—Testimonies For The Church 1:624, 626 (1867).**{EVsw 165:1}

Wasilisha Ukweli — Njia bora ya kukabiliana na makosa ni kuwasilisha Kweli, na kuachana na mawazo ya hovyo ili yafe kwa kukosa kutiliwa maanani/mbolea. Ukifananisha na Ukweli, udhaifu wa makosa unaonekana kwa akili zote zenye busara. Kadri madai potofu ya wapinzani na wale wanaojaribu kutapeli roho za watu, yanavyorudiwa, ndivyo hivyo suala la upotoshaji linavyosonga mbele. Kadri mipango ya Shetani inavyotangazwa zaidi, ndivyo utawala wa kishetani unavyofurahia. —**Testimonies to Ministers and Gospel Workers, 165 (1892).**{EVsw 166:1}

Tumia Hoja Imara Pekee — Ni muhimu kwamba katika kutetea Mafundisho ambayo tunazingatia kama vipengele vya msingi wa imani, tusijiruhusu kamwe kutumia hoja ambazo si sahihi kabisa. Haya yanaweza kusaidia kumnyamazisha mpinzani, lakini hayaheshimu Ukweli. Tunapaswa kuwasilisha hoja zenye mashiko, ambazo sio tu zitawanyamazisha wapinzani wetu, bali zitakuwa zimefanyiwa uchunguzi wa kina na wa karibu zaidi. Kwa wale ambao wamejielimisha kuwa wabishi (debate/mihadhara) kuna hatari kubwa ya kutolishughulikia Neno la **Mungu** kwa uadilifu. Katika kukutana na mpinzani inapaswa kuwa jitihada yetu ya dhati kuwasilisha masomo kwa namna ya kuamsha usadikisho katika akili yake, badala ya kutafuta tu kumpa muumini uhakika. —**Testimonies For The Church 5:708 (1889).**{EVsw 166:2}

Achana na Silaha za Kupigana (Masumbwi) — Wale wanaobeba ujumbe makini zaidi duniani wote wanapaswa kuachana na silaha za masumbwi, na kuvaa silaha za haki ya Kristo. Hatuhitaji kufanya kazi kwa nguvu zetu binafsi, maana malaika wa **Mungu** watakaa nyuma na kutuacha peke yetu kwenye vita. Lini wachungaji wetu watajifunza kutoka kwa Yesu? Maandalizi yetu ya kukabiliana na wapinzani au kuhudumia watu yanapaswa kupatikana kwa **Mungu** katika kiti cha neema ya mbinguni. Hapa, tukipokea neema ya **Mungu**, udhaifu wetu unaonekana na kukiriwa. Utukufu na heshima ya Kristo ndio nguvu yetu. Uongozi wa Roho Mtakatifu hutuelekeza katika kila **Ukweli**. Roho Mtakatifu huchukua mambo ya **Mungu** na hutuonyesha sisi, akiyaleta kama nguvu hai ndani ya moyo wenye utii. Ndipo tunapopata imani inayofanya kazi kwa upendo na kusafisha roho, ambayo hupata alama kamili ya Mwandishi wake. —**Letter 21a, 1895.**{EVsw 166:4}

SEHEMU YA 7 UJUMBE NA UWASILISHAJI WAKE

Roho na Mtindo wa Kuwasilisha Ujumbe

Umuhimu wa Mtindo wa Kuwasilisha Ukweli

Mtindo ambao Ukweli wa Biblia unawasilishwa mara nyingi una athari kubwa katika kuamua kama utakubalika au utakataliwa. —**Testimonies For The Church 4:404, 405 (1880).**{EVsw 168:1}

Ni jambo la kusikitisha kwamba wengi hawatambui kuwa namna ya kuwasilisha Ukweli wa Biblia ina mchango mkubwa katika mvuto unaowekwa akilini mwa watu, na katika tabia ya Kikristo inayokuja kuundwa kwa wale wanaoupokea. Badala ya kuiga mfano wa Kristo katika namna Yake ya kufanya kazi, wengi huwa wakali, wakosoaji, na wenye mamlaka kupita kiasi (madikteta). Badala ya kuvuta roho kwa Kristo, wao huzifukuza. Watu wa namna hii hawatajua kamwe ni roho ngapi dhaifu ambazo maneno yao makali yamejeruhi na kuongeza moyo wa kukata tamaa. —**Historical Sketches, uk. 121 (1886).**{EVsw 168:2}

Ujumbe wa Kushtua

Jumbe nyingi za kushangaza zitabebwa na watu walioteuliwa na **Mungu**, jumbe za tabia za kuwaonya watu, ili kuwaamsha. Na wakati wengine watachukizwa na onyo na kuongozwa kuipinga nuru na ushahidi, tunapaswa kuona kutokana na hili kwamba tunatoa ujumbe upimao kwa wakati huu..... Wakati utume wa miji unapaswa kuanzishwa mahali ambapo wainjilisti wa vitabu, watendakazi wa Biblia, na wamishenari wa kitabibu wanaweza kufundishwa kuyafikia matabaka fulani, lazima pia, katika miji yetu, tuwe na wainjilisti waliowekwa wakfu ambao kupitia kwao ujumbe unapaswa kutolewa kwa uthabiti ili kuwazindua na kuwashtua wasikilizaji. —**Testimonies For The Church 9:137 (1909).**{EVsw 168:3}

Kwa Uhakika na Maamuzi

Kuna nguvu hai katika Ukweli, na Roho Mtakatifu Ndiye wakala wa kufungua akili za watu kuuelewa. Lakini wahubiri na watenda kazi wanaowasilisha Ukweli ni lazima waonyeshe uhakika na maamuzi. Waende kwa imani, na wawasilishe Neno kana kwamba wanaliamini. Wajitahidi kuwafanya wale wanaowahudumia waelewe kuwa huu ni Ukweli wa **Mungu**. Mhubiri Yesu Kristo na Yeye aliyesulibiwa. Hili litakabiliana na uongo wa Shetani. —**Letter 34, 1896.**{EVsw 169:1}

Neno la Mungu Aliye Hai

Iwapo njia yako ya kuwasilisha Ukweli ni njia ya Mungu, hadhira yako itaguswa kwa kina na Ukweli unaouwasilisha. Watahisi kuwa ni **Neno** la **Mungu** Aliye hai, lililowasadikisha na utatimiza mapenzi ya Mungu kwa nguvu. —**Letter 48, 1902.** {EVsw 169:2}

Maono Makuu ya Ukweli wa Maandiko

Usijitangaze mwenyewe, bali uwasilishe Ukweli kwa namna ambayo utukufu wake wa ndani utaonekana wazi. Ukweli ni mpana, wa kina, na unaoenea sana kiasi kwamba mtu hujisahau mwenyewe.... Hubiri kwa namna ambayo watu wanaweza kushika maono makuu na kuchimba hazina ya thamani iliyofichwa katika Maandiko. —**Manuscript 7, 1894.**{EVsw 169:3}

Mikutano Ishuhudie Uwepo wa Roho Mtakatifu

Katika mikutano yetu mijini na kwenye mikutano ya kambi, hatuhitaji maonyesho makubwa, bali tunahitaji watu wanaosimama mbele ya watu kuwasilisha Ukweli, wawe dhati na bidii ya kweli, wakionyesha kuwa **Mungu** Yuko pamoja nao. Lazima pawepo na kutafuta uso wa **Mungu** kwa bidii, ili kazi ya mkutano ifanyike chini ya mvuto wa kina wa Roho Mtakatifu. Hakuna kuchanganya kilicho sahihi na makosa. —**The Review and Herald, Julai 23, 1908.**{EVsw 169:4}

Bidii na Ari Zaidi

Tunahitaji kuvunja mwendelezo wa hali ya kawaida katika kazi yetu ya dini. Tunafanya kazi duniani, lakini hatuonyeshi bidii ya kutosha wala ari ya kweli. Kama tungekuwa dhati na bidii zaidi, watu wangethibitishwa kuhusu Ukweli wa ujumbe wetu. Hali ya uvuguvugu na kawaida katika huduma yetu kwa

Mungu inawakatisha tamaa wengi wanaotazamia kuona ari ya kina, ya dhati, ya kweli, iliyo takatifu. Dini ya sheria peke yake haitoshi kwa wakati huu. Tunaweza kutimiza ibada zote za nje, lakini bado tukakosa mvuto wa kufufua wa Roho Mtakatifu, kama vile vilima vya Gilboa vinavyokosa umande na mvua. Tunahitaji chemichemi ya kiroho; na pia tunahitaji mwangaza mkali wa Jua la Haki kulainisha na kutakasa moyo. —**The Review and Herald, May 26, 1903.**{EVsw 169:5}

Mantiki ya Utulivu, iliyo dhati, Yenye Ari na busara

Siyo msisimko tunaotamani kuanzisha, bali tafakari ya kina na ya dhati, ili wale wanaosikia wafanye kazi imara, ya kweli, yenye mizizi, ambayo itadumu milele. Hatuhitaji msisimko wala vitu vya kuvutia kwa nje; kadri tunavyoepuka haya, ndivyo ilivyo bora. Mantiki ya utulivu, yenye ari, inayotoka kwenye Maandiko ni ya thamani na yenye matunda. Hapo ndipo ilipo siri ya mafanikio—kuhubiri Mwokozi hai, binafsi, kwa namna rahisi na ya dhati, ili watu waweze kushika kwa imani nguvu ya Neno la uzima. —**Letter 102, 1894.**{EVsw 170:1}

Kuwasilisha Ushahidi wa Ukweli

Watu hawawezi kutarajiwa kuona mara moja ubora wa Ukweli juu ya makosa waliyozoea. Njia bora ya kufichua udanganyifu wa kosa ni kuwasilisha ushahidi wa Ukweli. Hii ndiyo lawama kubwa zaidi inayoweza kutolewa dhidi ya kosa. Ondoa wingu la giza linalowazuia watu ili kuangaza mwanga wa Jua la Haki. —**Pacific Union Recorder, Oktober 23, 1902.**{EVsw 170:2}

Kuwavuta Watu Waamini

Wale wanaofanya kazi kwa ajili ya Kristo wanapaswa kuwa watu wa busara kubwa, ili wale wasioelewa mafundisho yao waweze kuwaheshimu na kuwaona kuwa ni watu wasio na itikadi kali wala hasira za haraka. Mahubiri yao, mwenendo na mazungumzo yao yawe ya namna itakayowafanya watu waone kuwa wahubiri hawa ni watu wa fikra za kina, wenye tabia thabiti, wanaomcha na kumpenda Baba yao wa mbinguni. Wawavute watu ili waamini, ili wale wanaosikiliza mahubiri wajue kuwa wahubiri hawajaja na hadithi zilizotungwa kwa werevu, bali kwamba maneno yao ni maneno ya thamani, ushuhuda unaohitaji tafakari na umakini. Hebu watu wasikuone wewe bali waone kuwa unamtukuza Yesu. —**The Review and Herald, April 26, 1892.**{EVsw 170:2}

Kuepuka Hoja Ndefu na za Kutatanisha

Kristo mara chache alijaribu kuthibitisha kuwa Ukweli ni Ukweli. Aliuweka Ukweli kwa mfano katika nyanja mbalimbali, kisha Aliwaacha wasikilizaji huru, kuukubali au kuukataa kulingana na uchaguzi wao. Hakumlazimisha mtu yeyote aamini. Katika mahubiri ya mlimani, Aliwafundisha watu utauwa wa vitendo, akiweka wazi wajibu wao. Alizungumza kwa namna iliyoelekeza Ukweli kwenye dhamiri. Nguvu ya wanafunzi wa Kristo ilidhihirika katika uwazi na ari waliyoonyesha walipowasilisha Ukweli.{EVsw 171:1}

Katika mafundisho ya Kristo hakuna hoja ndefu, zilizochukuliwa kutoka mbali au zinazochanganya. Alienda moja kwa moja kwenye pointi/kipengele. Katika huduma Yake aliweza kusoma mioyo ya watu kama kitabu kilicho wazi, na kutoka katika hazina isiyokauka ya hekima Yake, alitoa mambo mapya na ya kale ili kufafanua na kuimarisha mafundisho Yake. Aligusa moyo, na kuamsha huruma. **—Manuscript 24, 1891.**{EVsw 171:2}

Mafundisho Rahisi na Yenye Nguvu ya Mafundisho ya Imani

Kauli chache zenye uzito juu ya jambo fulani la mafundisho zitakuwa na nguvu ya kudumu zaidi katika akili ya mtu asiyejua imani yetu kuliko kama tungewapa wingi wa habari ambazo hazionekani wazi wala kueleweka kiurahisi. Mafundisho ya Yesu yanapaswa kuchanganywa na masomo ya vitendo ya unabii. —**Letter 48, 1886.**{EVsw 171:3}

Mungu Atatoa Maneno Ya Kufaa

Ni heshima iliyoje kuhudumu kwa ajili ya wokovu wa roho! Wito wetu ni wa juu mno... Ili kutuwezesha kufanya kazi hii, **Mungu** ataimarisha uwezo wetu wa kiakili kama vile alivyofanya kwa Danieli. Tunapowafundisha watu walioko gizani kuelewa Kweli zilizotupatia nuru sisi, **Mungu** atatufundisha kuelewa zaidi Kweli hizo sisi wenyewe. Atatupatia Maneno yanayofaa kusema, akitufunulia kupitia malaika anayesimama kando yetu. —**Manuscript 126, 1902.**{EVsw 172:1}

Mabishano Machache – Kumtangaza Kristo Zaidi

Tunahitaji kubishana kidogo sana, na kumtangaza sana Kristo. Mkombozi wetu Ndiye kiini cha imani na tumaini letu lote. Wale wanaoweza kuonyesha upendo Wake usio na kifani, na kuhamasisha mioyo kumpenda kwa moyo wao wote na maisha yao yote, wanafanya kazi kuu na takatifu. —**The Colporteur Evangelist, uk. 60-61 (1902).**{EVsw 172:2}

Mahubiri mengi ya mabishano yanayohubiriwa, mara chache sana huyalainisha na kuiisha mioyo. —**Letter 15, 1892.** {EVsw 172:3}

Usitukane

Wale wanaotetea Ukweli wanaweza kumudu kuonyeshahaki na kuwa watu wanaopendeka na kuchangamka. Ukweli hauna haja ya kuchanganywa na hisia za kibinadamu. Siyo jukumu lako kumtumia Roho Mtakatifu, bali Roho Mtakatifu Ndiye anayepaswa kukutumia wewe…..{EVsw 172:4}

Jihadhari usitukane hata mara moja. Tunahitaji Roho wa **Mungu** awe uhai na sauti yetu. Ulimi wetu unapaswa kuwa kama kalamu ya mwandishi mwenye utayari, kwa sababu Roho wa **Mungu** anasema nasi kupitia wakala wa kibinadamu. Unapoweka maneno ya dhihaka au kejeli, au machafu, unakuwa umejichochea ndani yako mwenyewe, na hatuhitaji kitu chochote cha mchanganyiko huo. **—Manuscript 7, 1894.**{EVsw 172:5}

Usishambulie Mamlaka

Kazi yetu sio kufanya mashambulizi dhidi ya Serikali, bali ni kuandaa watu kusimama katika siku kuu ya Bwana, siku ya hukumu. Kadiri tunavyopunguza mashambulizi dhidi ya viongozi na mamlaka, ndivyo tutakavyoweza kufanya kazi zaidi kwa ajili ya **Mungu** …..{EVsw 173:1}

Ingawa Ukweli lazima ulindwe, kazi hii ifanyike kwa roho ya Yesu. Kama watu wa **Mungu** wakifanya kazi bila amani na upendo, wanapoteza mengi, hasara isiyoweza kurekebishwa. Watu huondolewa kwa Kristo hata baada ya kuwa wameunganika na kazi Yake.{EVsw 173:2}

Hatupaswi kuwahukumu wale ambao hawajapata fursa na upendeleo tuliopewa sisi. Baadhi yao watawatangulia wengine kuingia mbinguni, kabla ya wale waliokuwa na nuru kuu lakini hawakuiishi nuru hiyo.{EVsw 173:3}

Kama tunataka kuwashawishi watu wasioamini kwamba tunayo Kweli inayotakasa roho na kugeuza tabia, hatupaswi kuwalaumu kwa jazba kuhusu makosa yao. Tukifanya hivyo, tutawafanya waamini, kwamba Kweli haijatufanya kuwa wapole na waungwana, bali wakali, jeuri na rafu.{EVsw 173:4}

Wengine, ambao huchochewa kwa urahisi, huwa tayari mara zote kuchukua silaha za mashambulizi. Wakati wa majaribu, wataonyesha kwamba hawakujenga imani yao juu ya mwamba thabiti……..{EVsw 173:5}

Hebu Waadventista Wasabato waepuke kufanya lolote litakalowaweka katika mwonekano wa kuwa waasi na wasiotii. Hebu na waondoe kila aina ya kutokuwiana katika maisha yao. Kazi yetu ni kutangaza Ukweli, na kumwachia Bwana suala la matokeo.{EVsw 173:6}

Fanya kila uwezalo kuangaza nuru, lakini usiseme maneno yatakayochochea hasira au kukera. —**Hati ya Maandishi 117a, 1901.**{EVsw 173:7}

Kuwasilisha Ukweli kwa Njia Kali

Hapo awali umeuwasilisha Ukweli kwa njia kali, kama fimbo ya kuadhibu. Hili halikumtukuza Bwana. Ingawa uliwapa watu hazina nyingi za **Neno** la Mungu, njia yako ya kulaumu na kuhukumu sana iliwafanya waukatae. Hukuwafundisha Ukweli kwa namna Kristo alivyofundisha. Umeuwasilisha kwa namna inayoharibu ushawishi wake…... Moyo wako unahitaji kujazwa neema ibadilishayo ya Kristo. —**Letter 164, 1902.**{EVsw 173:8}

Wasilisha Ukweli kwa Upole

Kila mhubiri ajifunze kuvaa viatu vya Injili. Yeye aliyevaa maandalizi ya Injili ya amani atatembea kama Kristo alivyotembea. Ataweza kusema maneno sahihi, na kuyasema kwa upendo. Hatajaribu

kulazimisha ujumbe wa **Mungu**. Atashughulikia kila moyo kwa upole, akitambua kuwa Roho Ndiye atakayeutia **Ukweli** katika mioyo ya wale walioko tayari kupokea msukumo wa Kiungu. Kamwe hatakuwa mkali katika mtindo wake. Kila neno litakalotamkwa litakuwa na mvuto wa kulainisha, kutiisha na wa kutakasa…..**{EVsw 174:1}**

Tunaposema maneno ya kukemea, tuweke upole wote wa Kristo na upendo iwezekanavyo ndani ya sauti. Kadri nafasi ya mhubiri ilivyo ya juu, ndivyo awe mwangalifu zaidi katika Neno na tendo. —**Manuscript 127, 1902.{EVsw 174:2}**

Kurejesha Badala ya Kuhukumu

Wote ambao mioyo yao iko sambamba na moyo wa upendo usio na Kifani watatafuta kurejesha, na siyo kuhukumu. Kristo akaaye moyoni ni chemchemi isiyokauka. Mahali anapoishi, kutakuwa na chemichemi ya fadhili isiyoisha. —**Thoughts from the Mount of Blessing, 39 (1896). {EVsw 174:3}**

Hubiri la Kiinjilisti

Hotuba Rahisi; Ufafanuzi Wazi — Bwana anataka ujifunze kutumia wavu wa Injili. Wengi wanahitaji kujifunza stadi-sanaa hii. Ili uweze kufanikiwa katika kazi yako, mashimo ya nyavu zako za kuvuvia — yaani matumizi ya Maandiko — lazima yawe karibu karibu, na maana yake iwe rahisi kueleweka. Kisha tumia fursa hii kikamilifu kuvuta nyavu ikiwa na samaki wengi zaidi. Nenda moja kwa moja kwenye hoja. Mfano wako uwe wazi na wa kueleweka moja kwa moja. Haijalishi mtu ana maarifa kiasi gani, haya hayana faida kama hawezi kuwasilisha kwa wengine. Sauti yako na hisia zake za ndani zilete tafakari katika mioyo. Wahimize wanafunzi wako kujitoa kwa **Mungu** .....**{EVsw 174:4}**

Fafanua kwa uwazi maneno yako, kwa kuwa najua kuna wengi wasioweza kuelewa mambo mengi wanayoambiwa. Ruhusu Roho Mtakatifu aitengeneze na kuifanya ivutie hotuba (kauli) yako, akiutoa uchafu wote. Zungumza kana kwamba unazungumza na watoto wadogo, ukikumbuka kuwa kuna watu wengi walio wakubwa kwa miaka lakini bado ni watoto katika kuelewa.**{EVsw 175:1}**

Kupitia maombi ya dhati, bidii na jitihada za dhati tunapaswa kupata sifa za kufaa kwa ajili ya kuhubiri. Sifa hizi ni pamoja na kutamka kila silabi kwa uwazi, na kuweka nguvu na mkazo mahali panapostahili. Zungumza polepole. Wengi huzungumza kwa kasi, wakiharakisha maneno kiasi kwamba matokeo ya ujumbe hupotea. Katika kile unachosema, weka msisitizo wa roho na maisha ya Kristo….. Kwa wasikilizaji, Injili huwa ni nguvu ya **Mungu** iletayo wokovu. Wasilisha mbele ya watu Injili kwa urahisi wake. —**Counsels to Parents, Teachers, and Students, 253-255 (1913).{EVsw 175:2}**

Umakini Wakati wa Kuandaa Hubiri — Hotuba zinazotolewa juu ya Kweli za sasa zimejaa mambo muhimu. Iwapo hotuba hizi zitafikiriwa kwa makini kabla ya kuwasilishwa kwa watu, zikipunguzwa na kutojaribu kugusa kila eneo, na kama roho ya Bwana itaambatana na maneno hayo, hakuna atakayebaki gizani, wala mtu yeyote hatalalamika kwamba hakupata chakula cha kiroho. Maandalizi ya mhubiri na ya msikilizaji yana mchango mkubwa katika matokeo ya kazi hiyo.**{EVsw 175:3}**

Ninakunukulia maneno machache niliyokutana nayo hivi karibuni: “Ninajua urefu wa mahubiri ya Cannon, kama amekuwepo sana nyumbani wiki yote au amesafiri,” alisema mmoja wa waumini wake. “Akiwa amejiandaa vizuri, hotuba zake huwa fupi, lakini ni vigumu kwa wasikilizaji kusahau alichofundisha. Asipopata muda wa kujiandaa, hotuba huwa ndefu bila kuwa na busara, na hakuna kinachobaki akilini baada ya kusikia.”**{EVsw 176:1}**

Mhubiri mwingine mwenye uwezo alipoulizwa huhubiri kwa muda gani alisema: “Nikijiandaa vizuri, nusu saa; nikijiandaa kwa juu juu, saa moja; lakini nisipojiandaa kabisa, ninahubiri na kuendelea kwa muda wote unaopenda wewe, bila kujua ni muda gani nitamalize.”**{EVsw 176:2}**

Kauli nyingine iliyosikika kwa nguvu ilisema: “Mchungaji mwema,” anasema mwandishi, “daima anapaswa kuwa na mkate tele katika mkoba wake, na mbwa wake awe chini ya amri yake. [*Mkate tele huwakilisha chakula cha kiroho (Neno la **Mungu**), maarifa, au hazina ya mafundisho ya kulisha kundi. Mbwa chini ya amri yake humaanisha nidhamu ya bidii au ari ya kufanya kazi kwa utii na usahihi. Mbwa wake ni bidii yake (Hapa mbwa ni mfano wa bidii, ari, au juhudi ya mchungaji katika kazi ya kiroho)].* Mbwa ndio bidii yake (anayopaswa kuiongoza, kuipa maagizo na kuitawala. Mfuko/mkoba wa mkate ni akili yake iliyojaa maarifa ya maana, na hebu awe tayari kila wakati kulisha kundi lake.”—**Letter 47, 1886.{EVsw 176:3}**

Kulinda Umeng'enyaji wa Kiroho wa Neno— "Sipendi kuzidisha sana zaidi ya nusu saa," alisema mchungaji mwaminifu na mwenye bidii, ambaye hakuwahi kuwapa wasikilizaji wake chochote ambacho yeye mwenyewe hakukiandaa. "Nafahamu umeng'enyaji wa Neno la Mungu au wa kiroho wa baadhi ya watu huwa ni dhaifu, na ningewakosea wasikilizaji wangu kutumia nusu ya pili ya saa huku wakisahau niliyosema mwanzoni, kwani ningetamani wakati wa kumaliza niwape wasikilizaji kiasi cha chakula ambacho wangeweza kubeba."—**Letter 47, 1886.**{EVsw 176:4}

Punguza au Kata Hotuba Zako Ndefu—Baadhi ya hotuba zako ndefu zingekuwa na matokeo makubwa zaidi kwa watu ikiwa zingegawanywa mara tatu. Watu hawawezi kumeng'enya mambo mengi kiasi hicho; akili zao hata wala hazielewi au kuzingatia, na wanachoka na kuchanganyikiwa kwa kuwa na mambo mengi katika hotuba moja. Theluthi mbili ya hotuba hizo ndefu hupotea, na mchungaji anachoka na kuchakaa. Wengi wa viongozi wetu wanakosea hapa. Matokeo yake si mazuri; wanahisi ubongo kuchoka na kuogopa kwamba wanabeba mizigo mizito kwa Bwana na kuugua kwa wakati mgumu.....{EVsw 176:5}

Ukweli ni tofauti kabisa na makosa yanayohubiriwa kutoka kwenye mimbari, hivyo unapoletwa kwa watu kwa mara ya kwanza, hukaribia kuwazidi uwezo. Ni chakula kizito na kinapaswa kutolewa kwa busara. Wakati baadhi ya akili ni nyepesi kunasa wazo, wengine huelewa kwa polepole (taratibu) Kkweli mpya na wa kushangaza unaoleta mabadiliko makubwa na utofauti kila hatua. Waachie muda wa kutafakari kumeng'enya Ukweli wa ajabu wa ujumbe unaowapelekea.{EVsw 177:1}

Mchungaji anapaswa kujua ufahamu na huruma waliyo nayo, pamoja na watu. Usiruke juu sana, ambako hawawezi kukufuata, bali toa Ukweli kidogo kidogo, polepole na kwa uwazi, ukibainisha hoja chache muhimu, kisha itakuwa kama msumari uliopigiliwa mahali salama na Bwana wa makutano. Ukimaliza wakati unaofaa, ukawapa tu kiasi wanachoweza kuelewa na kufaidika nacho, watakuwa na hamu ya kusikia zaidi, hivyo kuendeleza hamasa. —**Letter 39, 1887.**{EVsw 177:2}

Sifa ya Kuwa Mzungumzaji Mzuri, Unayevutia—Weka shauku yote unayoweza katika kazi yako. Zifanye hotuba zako ziwe fupi. Kuna sababu mbili za kufanya hivyo: Moja ni kupata sifa ya kuwa mzungumzaji mzuri anayevutia. Mbali na hilo, ni kutunza afya yako mwenyewe. —**Letter 112, 1902.**{EVsw 177:3}

Mahubiri Yenye Mawazo Mapya—Usiwachoshe wasikilizaji kwa hotuba ndefu. Hiyo si busara. Kwa miaka mingi nimekuwa nikiwaza hili, nikijaribu kuwahamasisha ndugu zetu wahubiri kidogo, na kutumia nguvu zao kuelezea hoja muhimu za Ukweli ulio wazi, kwa sababu kila hoja itapingwa na wapinzani wetu. Kila mtu anayehusiana na kazi hii anapaswa kuendelea kuwa na mawazo mapya; ….. na kwa hekima kubwa na utabiri lengo na kuvutia wasikilizaji wako kwa kadri uwezavyo kufanya. —**Letter 48, 1886.**{EVsw 178:1}

Tumia Ukweli Kufikia Moyo—Kwa kila wasilisho, kuwe na sehemu ya matumizi ya huo Ukweli ndani ya moyo, ili kila anayesikia afahamu, na kwamba wanaume, wanawake, na vijana wapate kuwa hai kwa **Mungu**. — **Testimonies to Ministers and Gospel Workers, 258 (1896).**{EVsw 178:2}

Rahisi Kueleweka—Hubiri Neno kwa njia rahisi yenye kueleweka. Wape watu njia ya kumfikia Yesu Kristo, ambaye ndilo tumaini lao la uzima wa milele..... Unapowasilisha Neno la **Mungu** kwa mtindo rahisi, mbegu itakua, na baada ya muda utavuna. Kupanda mbegu ni kazi yako; kuikuza mbegu ni kazi ya Kiungu ya Bwana. —**Letter 34, 1896.**{EVsw 178:3}

Utauwa wa Vitendo Katika Kila Hotuba—Ni vigumu kufikia mioyo ya watu leo kuliko miaka ishirini iliyopita. Huenda hoja za kushawishi sana zikatolewa, lakini wenye dhambi bado wanaonekana mbali na wokovu. Wachungaji wasihubiri mada za kidini pekee. Utauwa wa kivitendo wenye uhalisia, unapaswa kuonekana katika kila hotuba. —**The Review and Herald, April 23, 1908.**{EVsw 178:4}

Hubiri Ukweli wa Ujumbe—Katika tukio fulani, Betterton, mchekeshaji mashuhuri, alipokuwa akila na Dkt. Sheldon, Askofu Mkuu wa Canterbury, Askofu alisema, "Mzee Betterton, niambie kwa nini ninyi wachekeshaji mnawavutia wasikilizaji wenu kwa nguvu kwa kuzungumza mambo ya kufikirika." Betterton akajibu, "Mheshimiwa, kwa heshima kubwa, niruhusu niseme sababu, hakika ni rahisi; yote ni kwa sababu ya nguvu ya shauku. Sisi jukwaani tunazungumza mambo ya kufikirika kana kwamba ni halisi-ya kweli; nanyi kwenye mimbari mnazungumza mambo halisi kana kwamba ni ya kufikirika."— **Counsels to Parents, Teachers, and Students, 255 (1913).**{EVsw 179:1}

Hakuna Maridhiano—Hatuwezi kusinyaa wala kuomba msamaha kwa ulimwengu kwa kusema Ukweli; tunapaswa kutopendelea kujificha (we must scorn concealement). Yaweke wazi mawazo yako kuhusiana kusudi watu na malaika wapate faida-(weka rangi zako halisi wazi kushuhudia kwa malaika na wanadamu).

Hebu ieleweke kuwa Waadventista wa Sabato hawawezi kukubali maridhiano. Katika imani na maoni yako, usioneshe hata kidogo kushindwa au kumangamanga; ulimwengu una haki ya kujua, wanategemea nini kutoka kwetu. —**Manuscript 16, 1890.**{EVsw 179:2}

Ujumbe Wetu wa Ulimwengu—Tuko wamoja katika imani juu ya Kweli za msingi za Neno la **Mungu** .... Tuna ujumbe wa ulimwengu mzima. Amri za **Mungu** na ushuhuda wa Yesu Kristo ndilo mzigo na jukumu la kazi yetu. —**Letter 37, 1887.**{EVsw 179:3}

Hubiri kwa Ajili ya Uamsho—Tubuni, tubuni, ndiyo ujumbe alioupazia sauti Yohana Mbatizaji jangwani. Ujumbe wa Kristo kwa watu ulikuwa, "***…lakini msipotubu, ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo***. **Luka 13:5**. Na mitume waliagizwa kuhubiri kila mahali watu watubu. {EVsw 179:4}

Bwana anataka watumishi Wake leo wahubiri mafundisho ya zamani ya Injili, kuhuzunishwa na dhambi, toba, na maungamo. Tunataka mahubiri ya zamani (old fashion sermons), desturi za zamani, baba na mama wa zamani wa Israeli. Mdhambi anapaswa kuhubiriwa (kutendewa) kwa dhati, bidii, kwa uvumilivu, kwa busara, hadi aone kuwa ametenda dhambi dhidi ya sheria ya **Mungu**, afanye toba kwa **Mungu** na kumwamini Bwana Yesu Kristo. —**Undated Manuscript 111.**{EVsw 179:5}

Mahubiri Yenye Faraja na Nguvu—Unapaswa kuwa na ufahamu mzuri wa Injili. Maisha ya kidini si ya huzuni wala majonzi bali ni ya amani na furaha ikifuatana na heshima ya mfano wa Kristo na utulivu mtakatifu. Hatuhimizwi na Mwokozi wetu kuwa na mashaka, hofu, au mashaka yanayosababisha wasiwasi; haya hayaleti faraja kwa roho na yanapaswa kukosolewa badala ya kupongezwa. Tunaweza kuwa na furaha isiyoelezeka na yenye utukufu. Hebu tuachane na uvivu, ugoigoi na tusome Neno la **Mungu** mara kwa mara. Ikiwa tumewahi kuwa na uhitaji wa Roho Mtakatifu awe pamoja nasi, au uhitaji wa kuhubiri kwa nguvu ya Roho, ni wakati huu sasa. —**Manuscript 6, 1888.**{EVsw 180:1}

Ujumbe wa Furaha wa Ukweli wa Sasa—Sasa hivi, tunapaswa kutangaza Ukweli wa sasa kwa uhakika na kwa nguvu. Usitoea hata noti moja ya huzuni; usiimbe nyimbo za mazishi. —**Letter 311, 1905.** {EVsw 180:2}

Jinsi ya Kuhubiri kuhusu Majanga—Wainueni wale waliotupwa chini kwa majanga au huzuni. Chukulia misiba kama baraka zilizojificha, na taabu kama rehema. Fanya kazi kwa namna ambayo italeta matumaini mahali pa kukata tamaa. —**Testimonies For The Church 7:272 (1902).**{EVsw 180:3}

Haraka-haraka Hutoa Hotuba Zinazokauka—Unapofanya haraka kutoka katika jambo moja hadi lingine, wakati una mengi ya kufanya ambayo huwezi kuchukua muda wa kuzungumza na **Mungu**, unawezaje kutarajia nguvu katika kazi yako? Sababu ya wachungaji wetu wengi kuhubiri mazungumzo yasiyo na nguvu ya woga (tame), yasiyo na uhai ni kwamba wanaruhusu mambo mbalimbali ya ulimwengu kuchukua muda wao na umakini wao. —**Testimonies For The Church 7:251 (1902).**{EVsw 180:4}

Epuka Hotuba Dhaifu—Hoja fupi, zinazowasilishwa kwa uwazi zitakuwa na faida kubwa, epuka uzungumzaji unaoendelea muda mrefu kwa toni za chini na kuboa watu (rumblings). **Mungu** hataki uchoke kabla ya kuingia kwenye mkutano, kwa kuandika au kazi nyingine yoyote, kwa kuwa ukija na akili iliyochoka, unatoa hotuba isiyokamilika, na mbovu kwa watu. Wekeza nguvu zako mpya na bora zaidi kwenye kazi na usiruhusu hata dalili ndogo ya upungufu kuonekana katika jitihada zako.{EVsw 181:1}

Ikiwa kwa sababu yoyote umekuwa mchovu na umelemewa, kwa ajili ya Kristo usijaribu kutoa hotuba. Hebu yule ambaye hajachoka achukue nafasi ya kuongea, kwa ufupi, akilenga kwenye hoja, au tafakari ya kusoma Biblia; chochote isipokuwa hotuba dhaifu/gonjwa. Haya hayataleta madhara makubwa ikiwa wote ni waumini, lakini wakati Ukweli unapotakiwa kutangazwa mbele ya watu wasio wa imani, mhubiri lazima ajiandae kwa kazi hiyo. Asizungumze bila kukoma kama sauti ya treni inayotembea katika Biblia yote (rumbling) kwa mahubiri yasiyo na uwiano, bali atoe hotuba iliyo wazi, inayohusiana, ikionyesha anafahamu hoja anazotaka kufikisha. —**Letter 48, 1886.**{EVsw 181:2}

Mapambo Bandia — **Mungu** anawaita waumini wa Injili wasijaribu kujikuza kwa kuleta mapambo ya bandia, wakijaribu kupata sifa na makofi ya watu, wakiwa na matamanio ya ukuu na kuonyesha maarifa, akili mahiri na uhodari wa semi zisizo na maana na umbuji usiohitajika. Hivyo basi, shauku ya muumini na mchungaji iwe ni kusoma kwa makini Biblia, ili wajifunze kwa undani kuhusu **Mungu** na Yesu Kristo aliyemtuma. Kadri waumini wanavyomwona Kristo kwa uwazi zaidi na kupata Roho Mtakatifu, ndivyo wanavyotangaza kwa nguvu zaidi Ukweli rahisi ambao Kristo Ndiye kiini chake. —**The Review and Herald, March 24, 1896.**{EVsw 181:3}

Mahubiri Yenye Usemi Mzuri — Mchungaji anaweza kuruka juu angani kwa kutumia maelezo ya kifalme, kimashairi na maonyesho ya kufikirika ambayo hufurahisha hisia na kuimarisha mawazo ya kufikirika, lakini hayagusi uzoefu wa kawaida wa maisha, wala mahitaji ya kila siku; hayaupatii moyo Ukweli wa msingi ambao ni wa maslahi ya dhati. Mahitaji ya sasa, majaribu ya sasa, yanahitaji msaada na nguvu ya sasa—imani inayofanya kazi kwa upendo na kusafisha nafsi, si maneno yasiyo na matokeo halisi katika maisha ya kila siku ya Ukristo wa vitendo.{EVsw 182:1}

Mwinjilisti anaweza kufikiri kwamba kwa uhodari wake wa kufikirika ndiyo maana amefanikisha mambo makubwa kwa kuwalea kondoo wa **Mungu**; wasikilizaji wanaweza kudhani kwamba hawajawahi kusikia mada nzuri kama hizo, wala hawajawahi kuona Ukweli ukiwasilishwa kwa lugha nzuri kama hizo, na wakihisi msisimko wa hisia wakimwona **Mungu** katika ukuu Wake. Lakini fuatilia sababu na matokeo ya furaha hiyo yote inayosababishwa na maonyesho hayo ya kufikirika. Kunaweza kuwa na Ukweli, lakini mara nyingi sio chakula kitakachowaimarisha kwa mapigano ya kila siku ya maisha. —**Manuscript 59, 1900.**{EVsw 182:2}

Kutambulisha Mambo Yanayozungumziwa Pembeni — Ndugu hawawezi kuhisi kuwa ni fadhila kusimama pembeni kwa sababu hawana mtazamo sawa kuhusu masuala madogo-madogo. Ikiwa wanakubaliana katika zile Kweli za msingi, basi wasitofautiane wala kujadili mambo yasiyo na umuhimu mkubwa. Kukaa katika maswali magumu ambayo hatimaye hayana umuhimu mkubwa au matokeo, hupelekea akili kutengwa na Ukweli muhimu wa wokovu wa nafsi. Ndugu wanapaswa wawe na staha, uungwana, na unyenyekevu katika kusisitiza masuala haya ya pembeni ambayo mara nyingi wao wenyewe hawaelewi, au sio kweli kamili wala si muhimu kwa wokovu....{EVsw 182:3}

Nimeonyeshwa kuwa ni mbinu ya adui kugeuza mawazo ya watu kuelekea kwenye suala lisilo wazi au lisilo muhimu, jambo ambalo halijafunuliwa kikamilifu au halihitajiki kwa ajili ya wokovu. Hili hufanywa kuwa mada kuu inayonyonya akili yetu, "Ukweli wa sasa," wakati uchunguzi na dhana zote hufanya mambo kuwa magumu zaidi na kuchanganya akili za wengine ambao wanapaswa kutafuta umoja kupitia usafi wa ile Kweli. —**Undated Manuscript 111.**{EVsw 182:4}

Kutangazia Ukweli Unaothibitishwa — Ikiwa tutaruhusu akili iende kwa njia yake, kutakuwa na tofauti nyingi zinazoweza kujadiliwa na watu wanaomwamini Kristo, na kumfanya tumaini lao, na wanaopenda Ukweli kwa dhati, lakini wakiwa na maoni tofauti kuhusu masuala yasiyo ya umuhimu wa kweli. Maswali haya yasiyo na suluhisho hayapaswi kuletwa kwenye kipaumbele wala kusisitizwa kwa umma, bali, kama mtu yeyote anayo, basi yashugulikiwe kwa utulivu na bila ugomvi.....{EVsw 183:1}

Mtendakazi mwema, bora, mwungwana, aliyejiweka wakfu, anayejali na wa kiroho, ataona katika Ukweli mkubwa unaothibitishwa, ambao ni ujumbe mtakatifu wa kutolewa kwa dunia, sababu tosha ya kutunza tofauti ndogo zote kwa siri badala ya kuzitoa hadharani kuwa sababu za mabishano.Hebu akili izingatie kazi kuu ya ukombozi, kurudi haraka kwa Kristo, na amri za **Mungu**; na itagundua kuwa kuna chakula cha kutosha cha mawazo katika masuala haya yote na kuchukua umakini wote. —**The Review and Herald, September 11, 1888.**{EVsw 183:2}

Sauti Katika Uwasilishaji wa Mahubiri — Hubiri kwa kifupi, simamia sauti yako, [Angalia pia kurasa 665-670, "Sauti ya Mtendakazi wa Injili."] weka hisia zote na muziki ndani yake kadri uwezavyo, na kuepuka uchovu mkali unaoweza kuja kutokana na mahubiri marefu na kujitaabisha bure.....{EVsw 183:3}

Matokeo mengi ya mahubiri hupotea kwa sababu ya namna yanavyoelezwa. Mzungumzaji mara nyingi husahau kuwa yeye ni mjumbe wa **Mungu**, na kuwa Kristo na malaika wako kwenye hadhira kama wasikilizaji. Sauti yake haipaswi kuinuliwa kwa kiwango cha juu, akipaza sauti kwa toni ya juu kutangaza **Ukweli** kama tarumbeta; kwani kufanya hivi huwa anatumia nguvu za mihemko ya neva kuliko roho tulivu na nguvu za Roho Mtakatifu. Yesu, Mwalimu mkuu aliyewahi kujulikana duniani, Alikuwa mtulivu, makini, dhati na mwenye mvuto katika mahubiri Yake. Yeye ni Mfano wetu katika kila jambo. —**Letter 47, 1886.**{EVsw 183:4}

Ishara za kulazimisha — Bwana anakuita wewe uboreshe sana namna yako ya kuwasilisha Ukweli. Huna haja ya kuwa mtu wa kusisimka-mihemko au misukumo fulani. Hubiri Neno, kama Kristo, Mwana wa **Mungu**, Alivyohubiri Neno. Ishara za kulazimisha sauti hupunguza kwa kiasi kikubwa matokeo ya Ukweli katika mioyo ya watu na kupunguza nguvu za maelekezo ya Roho wa **Mungu**. Zinapunguza hisia za heshima kuhusu Neno la **Mungu** ambazo malaika wa watakatifu wanataka zichukuliwe akilini.....{EVsw 184:1}

Ndugu yangu, Bwana amenipa ujumbe kwako. Mhudumu wa Injili anahusika na kazi makini na iliyo mtakatifu. Katika kila mkutano ambapo Neno la **Mungu** hufundishwa, malaika wapo, na wale wanaoendesha mikutano hiyo wanapaswa kufanya kazi kwa kicho na uzito kama aliyoonyesha Kristo katika mafundisho Yake. Mtindo sahihi lazima uwepo katika kila uwasilishaji wa Ukweli wa Biblia. —**Letter 366, 1906.**{EVsw 184:2}

Kristo Ndiyo Kiini cha Ujumbe

Yesu Kristo, Kituo Kikuu cha Mvuto — Ujumbe wa malaika wa tatu unatoa wito wa kuwasilishwa kwa Sabato ya amri ya nne, na Kweli hii ni lazima iletwe mbele ya dunia; lakini kiini Kikuu cha mvuto, Yesu Kristo, kamwe hakipaswi kuachwa nje ya ujumbe wa malaika wa tatu.....{EVsw 184:3}

Mwenye dhambi ni lazima atazame Kalvari daima; na kwa imani rahisi kama ya mtoto mdogo, lazima abaki katika sifa na stahiki za Kristo, akiikubali haki Yake na kuamini rehema Yake. Watenda kazi katika kazi ya Ukweli wanapaswa kuwasilisha haki ya Kristo. — **Review and Herald, Machi 20, 1894.**{EVsw 185:1}

Mwinue Kristo — Kristo aliyesulubiwa, Kristo aliyefufuka, Kristo aliyepaa mbinguni, Kristo anayekuja tena, ndio ujumbe unaopaswa kuchukua nafasi kubwa akilini mwa mhubiri kiasi kwamba atawasilisha Kweli hizi kwa watu kwa upendo na bidii kuu na mioyo italainishwa. Hivyo mhubiri hatatazamwa tena, bali Yesu ataonekana wazi.{EVsw 185:2}

Mwinueni Yesu, ninyi mnaowafundisha watu; mwinueni katika mahubiri, katika nyimbo, na katika sala. Tumieni nguvu zenu zote kuelekeza roho zilizopotea na kuchanganyikiwa kwa "Mwana-Kondoo wa **Mungu**." Mwinueni Mwokozi aliyefufuka, na semeni kwa wote wasikiao, Njooni Kwake Yeye "Aliyetupenda, Akajitoa nafsi Yake kwa ajili yetu." Hebu Sayansi ya wokovu ndio iwe wajibu wa kila hubiri, mada ya kila wimbo. Ifurikie kwa kila dua. Msiongeze chochote kwenye mahubiri yenu kama kiambatisho kwa Kristo, hekima na nguvu ya **Mungu**. Shikeni Neno la uzima, mkimwasilisha Yesu kama tumaini kwa kila atubuye na ngome ya kila aaminiye. Waonyesheni waliotaabika njia ya amani, na ifunueni neema na ukamilifu wa Mwokozi. — **Gospel Workers, uk. 159-160 (1915).**{EVsw 185:3}

Katika Kila Hotuba — Watu wengi kuliko tunavyodhani wanatamani kumpata Kristo. Wale wanaohubiri ujumbe wa mwisho wa rehema wanapaswa kukumbuka kwamba Kristo Ndiye kimbilio la mwenye dhambi na anapaswa kuinuliwa. Wahubiri wengine hudhani kwamba si lazima kuhubiri toba na imani; hudhani kwamba wasikilizaji wao wanaelewa Injili, na kwamba ni lazima wawape mada tofauti ili kuwavutia. Lakini watu wengi hawana uelewa wa mpango wa wokovu; wanahitaji mafundisho zaidi kuhusu somo hili muhimu kuliko lingine lolote (Ni wajinga wa somo la wokovu).{EVsw 185:4}

Hotuba za kinadharia ni muhimu ili watu waone mnyororo wa Ukweli, kiungo baada ya kiungo, vikijumuika kuwa jambo kamili; lakini hakuna hotuba ambayo inapaswa kuhubiriwa bila kumwasilisha Kristo na Yeye aliyesulubiwa kama msingi wa Injili. Wahubiri wangeifikia mioyo ya watu zaidi kama wangesisitiza zaidi utauwa wa vitendo. — **Gospel Workers, uk. 158-159 (1915).** {EVsw 186:1}

Kumhubiri Kristo Kutokana na Uzoefu — Kila mjumbe anapaswa kubeba mzigo wa kuwasilisha ukamilifu wa Kristo. Wakati kipawa cha bure cha haki ya Kristo hakionyeshwi, hotuba huwa kavu na hazina ari-tija; kondoo na wana-kondoo hawalishwi. Paulo alisema katika, "1 Wakorintho 2:4. *Na neno langu na kuhubiri kwangu hakukuwa kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu, bali kwa dalili za Roho na za nguvu."* Kuna mafuta na unono katika Injili. Yesu Ndiye kiini hai cha kila kitu. Muwekeni Kristo katika kila hotuba. Tuzungumze juu ya wema, rehema, na utukufu wa Yesu Kristo mpaka Kristo aumbike ndani yetu, tumaini la utukufu…..{EVsw 186:2}

Hebu na tukusanye yale ambayo uzoefu wetu umetufunulia kuhusu thamani ya Kristo, na tuyawasilishe kwa wengine kama kito cha thamani kinachomeremeta. Hivyo mwenye dhambi atavutwa kwake Yeye anayeitwa Mashuhuri miongoni mwa elfu kumi, na Aliye mzuri kuliko wote. Msalaba wa Kalvari ni dhamana kwetu ya uzima wa milele. Imani katika Kristo ni kila kitu kwa aaminiye Kweli. Sifa za Yesu hufuta makosa, na hutuvika vazi la haki lililofumwa katika handaki la mbinguni. Taji ya uzima imewekwa mbele yetu kama utukufu/heshima itakayopokelewa mwisho wa mapambano haya. Ukweli huu wa thamani unapaswa kuwasilishwa kwa sura hai. — **Review and Herald, Machi 19, 1895.**{EVsw 186:3}

Mada za Mahubiri Yetu — Hizi ndizo mada zetu—Kristo aliyesulubiwa kwa ajili ya dhambi zetu, Kristo aliyefufuka kutoka katika wafu, Kristo Mwombezi wetu mbele za **Mungu**; na kwa karibu sana na haya ni kazi ya Roho Mtakatifu, Mwakilishi wa Kristo, aliyetumwa kwa nguvu za Kiungu na vipawa kwa ajili ya wanadamu. **— Letter 86, 1895.**{EVsw 187:1}

Kuwepo Kwake kabla-milele, kuja Kwake mara ya pili kwa utukufu na nguvu, heshima ya utu Wake binafsi, na sheria Yake takatifu iliyoinuliwa, ni mada zilizowasilishwa kwa unyenyekevu na nguvu. — **Letter 83, 1895.**{EVsw 187:2}

Ujumbe wenye uhakika — Toeni ujumbe wa kusadikisha kwa sauti ya hakika. Mwinueni, Mtu wa Kalvari, juu na zaidi. Kuna nguvu katika kuinua msalaba wa Kristo…..{EVsw 187:3}

Kristo anapaswa kuhubiriwa, si kwa mabishano, bali kwa kukiri kwa uthabiti. Simameni bila mabishano. Msiruhusu maneno yenu yawe ya mashaka. Neno la **Mungu** aliye hai liwe msingi wa imani yetu. Kusanyeni mada zote zenye nguvu za kukiri kuhusu upatanisho uliofanywa na Kristo kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Onyesheni hitaji la upatanisho huu na waambieni wanaume na wanaume kwamba wanaweza kuokolewa iwapo watatubu na kurudi kwenye uaminifu kwa sheria ya **Mungu**. Kusanyeni maelezo yanayosadikisha na kuleta uthibitisho unaoifanya Injili kuwa habari njema ya wokovu kwa wote wanaompokea na kumwamini Kristo kama Mwokozi wao binafsi. — **Letter 65, 1905.**{EVsw 187:4}

Mahubiri Kama Sadaka ya Kaini — Wahubiri wetu wengi wamekuwa wakitoa mahubiri tu, wakiwasilisha mada kwa mtazamo wa mabishano, na kwa nadra sana hutaja nguvu ya wokovu wa Mkombozi. Ushuhuda wao ulikosa damu ya wokovu ya Kristo. Sadaka yao imekuwa kama ya Kaini. Alimletea Bwana matunda ya shamba, ambayo yenyewe yalikuwa mazuri machoni pa **Mungu**. Matunda yalikuwa mazuri sana; lakini sifa kuu ya sadaka—damu ya Mwana-Kondoo aliyechinjwa, iliyowakilisha damu ya Kristo—ilikuwa haipo. Ndivyo ilivyo kwa mahubiri yasiyo na Kristo. Hayawagusi watu mioyoni; hayawafanyi watu wajiulize, Nifanye nini ili nipate kuokolewa? Miongoni mwa WaKristo wote, Waadventista wa Sabato wanapaswa kuwa wa kwanza kumwinua Kristo mbele ya dunia. — **Gospel Workers, uk. 156 (1915).**{EVsw 187:5}

Kwa Njia ya Wazi, Rahisi — Wahubiri wanahitaji kuwa na njia iliyo wazi na rahisi zaidi katika kuwasilisha Ukweli kama ulivyo katika Yesu. Akili zao wenyewe zinapaswa kuelewa mpango mkuu wa wokovu kwa undani zaidi. Ndipo wanaweza kuelekeza fikra za wasikilizaji kutoka mambo ya dunia hadi yale ya kiroho na ya milele. Wapo wengi wanaotamani kujua ni nini wafanye ili waokolewe. Wanahitaji maelezo ya wazi na rahisi kuhusu hatua zinazohitajika katika kuongoka, na hakuna hotuba yoyote inayopaswa kutolewa bila sehemu ya hotuba hiyo kueleza kwa uwazi njia ya wenye dhambi kumwendea Kristo na kuokolewa. Wanapaswa kuwaelekeza watu kwa Kristo, kama alivyofanya Yohana, na kwa unyenyekevu unaogusa moyo, mioyo yao ikiwaka kwa upendo wa Kristo, waseme: "*Tazama Mwana-Kondoo wa **Mungu**, aichukuaye dhambi ya ulimwengu.*" Miito ya shauku kubwa na yenye nguvu inapaswa kutolewa kwa wenye dhambi watubu na kuongoka. — **Review and Herald, Februari 22, 1887.**{EVsw 188:1}

Kweli Kama Ilivyo Katika Yesu

Fundisheni masomo rahisi aliyoyatoa Kristo. Simulieni habari za maisha Yake ya kujikana na kujitoa dhabihu, ya unyenyekevu na kifo Chake, ufufuo na kupaa Kwake mbinguni, na kazi Yake ya maombezi kwa ajili ya wenye dhambi huko mbinguni. Katika kila kusanyiko kuna roho ambazo Roho wa Bwana Yuko juu yao. Wasaidieni kuelewa Ukweli; walisheni mkate wa uzima; waelekezeni kwenye masuala ya msingi ya maisha.{EVsw 188:2}

Sauti nyingi zinatetea makosa; lakini sauti yako na itetee Kweli. Toa mafundisho yatakayokuwa kama malisho mabichi kwa kondoo wa zizi la **Mungu**. Usivute wasikilizaji wako kuingia katika nyika kavu, ambapo hawatakuwa karibu na chemchemi ya maji ya uzima kuliko walivyokuwa kabla ya kukusikiliza wewe. Toa Kweli kama ilivyo katika Yesu, ukifafanua kwa uwazi masharti ya sheria na Injili. Mwonyeshe Kristo kuwa ni —Njia, Kweli, na Uzima—na tangaza uwezo Wake wa kuwaokoa wote wamwendeao Yeye. Nahodha wa wokovu wetu anaombea watu Wake, si kama mwombaji anayejaribu kumsihi Baba ahurumie wanadamu, bali kama mshindi anayedai zawadi ya ushindi Wake. Yeye Anaweza kuwaokoa kikamilifu wote wamwendeao **Mungu** kwa njia Yake. Weka jambo hili wazi kabisa.{EVsw 189:1}

Kama wahudumu hawatajilinda, watauficha Ukweli chini ya mapambo ya kibinadamu. Mhudumu asidhanie kuwa yeye anaweza kugeuza mioyo kwa mahubiri ya ufasaha. Wale wanaofundisha wengine na wamwombe **Mungu** awajaze kwa Roho Wake, na kuwapa uwezo wa kumwinua Kristo kama tumaini la pekee la wenye dhambi. Hotuba za mashairi na mapambo au maua, hekaya, za kufurahisha, au zenye vichekesho visivyo na maana haviwezi kumshawishi mwenye dhambi. Watu husikiliza maneno kama hayo kama ambavyo wangesikiliza wimbo wa kupendeza. Ujumbe ambao mwenye dhambi anapaswa kuusikia ni huu: "*Kwa maana jinsi hii **Mungu** aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele: **Yohana 3:16**.*" — **Gospel Workers, uk. 154-155 (1915).**{EVsw 189:2}

Upendo wa Kristo Uinuliwe

Ili kubomoa vizuizi vya chuki na kutotubu, upendo wa Kristo lazima uwe sehemu ya kila hotuba. Wafundisheni watu kujua jinsi Yesu anavyowapenda, na ushahidi Aliowapa wa upendo huo. Ni upendo upi unaweza kulinganishwa na ule ambao **Mungu** ameuonyesha kwa mwanadamu kwa kifo cha Kristo msalabani? Moyo unapojazwa na upendo wa Yesu, huo unaweza kuwasilishwa kwa watu, nao utagusa na kuathiri mioyo. — **Letter 48, 1886.**{EVsw 189:3}

Msingi wa Kila Hotuba: Msalaba

Dhabihu ya Kristo kama upatanisho kwa ajili ya dhambi ni **Ukweli** mkuu ambao kila ukweli mwingine unajengwa na kuunganishwa juu yake. Ili kueleweka vizuri, kila Kweli ya Neno la **Mungu**, kuanzia Mwanzo hadi Ufunuo, lazima ichunguzwe kwa mwanga utokao msalabani. Nawasilisha mbele yenu kumbukumbu kuu ya rehema na kufanywa upya, wokovu na ukombozi—Mwana wa **Mungu** aliyenuliwa msalabani. Huu ndio msingi wa kila hotuba inayotolewa na wahudumu wetu. — **Gospel Workers, uk. 315 (1915).**{EVsw 190:1}

Kristo na Haki Yake

Kristo na haki Yake—na iwe ndiyo jukwaa letu, uhai halisi wa imani yetu. — **Review and Herald, August 31, 1905.**{EVsw 190:1}

Ujumbe wa Malaika wa Tatu kwa Ukamilifu Wake

Wengi wameandika kuniuliza ikiwa ujumbe wa kuhesabiwa haki kwa imani ndio ujumbe wa malaika wa tatu, nami nimejibu: “Ndiyo, ni ujumbe wa malaika wa tatu katika ukamilifu wake (Kweli).” — **Review and Herald, April 1, 1890.** {EVsw 190:3}

Unamwakilisha Mwokozi Aliyeinuliwa

Ujumbe huu ulikuwa na kusudi la kumweka Mwokozi aliyeinuliwa mbele ya dunia kwa namna iliyo wazi zaidi—Yule aliyejitoa kuwa dhabihu kwa ajili ya dhambi za ulimwengu mzima. Uliwasilisha haki kwa imani kwa kupitia Kwake Yeye aliye Mdhamini wetu; uliwaalika watu wapokee haki ya Kristo, inayodhihirika kwa utii wa amri zote za **Mungu**. Wengi walikuwa wamepoteza mtazamo wa Yesu. Walihitaji kuelekezwa tena kwa nafsi Yake ya Kiungu, fadhili Zake, na upendo Wake usiobadilika kwa wanadamu. Mamlaka yote yako mikononi Mwake, ili aweze kuwapa wanadamu vipawa vya thamani, akiwapa wanadamu kipawa cha thamani kubwa cha haki Yake kwa wale wote walio dhaifu. Huu ndio ujumbe ambao **Mungu** aliamuru utolewe kwa ulimwengu. Ni ujumbe wa malaika wa tatu, unaopaswa kutangazwa kwa sauti kuu, na kwa kuandamana na kumwagwa kwa Roho Wake kwa kipimo kikubwa.{EVsw 190:4}

Mwokozi aliyeinuliwa anapaswa kuonekana katika kazi Yake yenye nguvu kama Mwana-Kondoo aliyechinjwa, akikaa juu ya kiti cha enzi, ili kuwagawia wanadamu baraka za agano la thamani—fadhili ambazo alikufa kuzinunua kwa ajili ya kila nafsi imwaminiyo. Yohana hakuweza kueleza upendo huo kwa maneno; ulikuwa wa kina sana, mpana sana; anawaita wanadamu kuuangalia. Kristo anaendelea kuliombea kanisa katika huko mbinguni, akiwaombea wale aliolipa bei ili kuleta ukombozi kwa damu Yake Mwenyewe. Karne, vizazi na zama haviwezi kupunguza thamani ya dhabihu hii ya upatanisho. Ujumbe wa Injili ya neema Yake ulipaswa kutolewa kwa kanisa kwa njia ya wazi na thabiti, ili dunia isiseme tena kwamba Waadventista wa Sabato wanafundisha sheria tu, sheria tu, bila kumfundisha wala kumwamini Kristo. (efficacy). {EVsw 191:1}

Thamani wa damu ya Kristo ilipaswa kuwasilishwa kwa watu kwa upya na kwa nguvu, ili imani yao itegemee fadhili Zake. Stahiki Zake, Sifa Zake.....{EVsw 191:2}

Kwa miaka mingi, kanisa limekuwa likimwangalia mwanadamu, likitarajia mengi kutoka kwa mwanadamu, bila kumwangalia Yesu, ambaye ndani Yake ndimo tumaini letu la uzima wa milele linapopatikana. Kwa hiyo, **Mungu** aliwapa watumishi Wake ushuhuda ulioonyesha Kweli kama ilivyo katika Yesu, ambayo ndiyo ujumbe wa malaika wa tatu, kwa mistari iliyo wazi na dhahiri. —**Testimonies to Ministers and Gospel Workers, uk. 91-93 (1896).** {EVsw 191:3}

Kristo Dhidi ya Matendo ya Toba ya Kianadamu

Wakati ujumbe wa malaika wa tatu unahubiriwa jinsi inavyopaswa, nguvu ya **Mungu** huandamana nao, na unakuwa na athari ya kudumu. Lazima uambatane na nguvu ya Kiungu, la sivyo hautaweza kufanikisha chochote.....**{EVsw 191:4}**

Matendo ya kutubu/toba, kuutesa mwili, kuungama dhambi kila wakati bila toba ya kweli; kufunga, sherehe, na ibada za nje zisizo na ibada ya Kweli—vyote hivi havina thamani yoyote. Dhabihu ya Kristo inatosha; Yeye Alitoa dhabihu kamilifu, yenye thamani kwa **Mungu**; na jitihada za kibinadamu bila thamani ya Kristo ni bure kabisa.....**{EVsw 192:1}**

Mpango wa wokovu haupaswi kueleweka kuwa ni njia ya kuleta nguvu ya Kiungu kwa mwanadamu ili jitihada zake za kibinadamu zifanikiwe kikamilifu.....**{EVsw 192:2}**

Bila mchakato wa mabadiliko ambao unaweza kuja tu kwa njia ya nguvu ya Kiungu, asili ya dhambi hubaki ndani ya moyo katika nguvu yake yote, na kutengeneza minyororo mipya ya utumwa, utumwa ambao hauwezi kuvunjwa kwa uwezo wa kibinadamu. — **Review and Herald, August 19, 1890.{EVsw 192:3}**

Ujumbe wa Kweli wa Sasa

Tunamshukuru Bwana kwa moyo wote kwa kuwa tuna nuru ya thamani ya kuwasilisha mbele ya watu, na tunafurahi kwamba tunao ujumbe wa wakati huu ambao ni Ukweli wa sasa. Habari kwamba Kristo ni haki yetu imeleta faraja kwa wengi, nafsi nyingi sana, na **Mungu** anawaambia watu Wake, “Songeni mbele.” — **Review and Herald, July 23, 1889.{EVsw 192:4}**

Ujumbe kwa Kanisa na Kwa Maeneo Mapya

Wachungaji wanapaswa kumwasilisha Kristo katika utimilifu Wake, katika makanisa na pia katika maeneo mapya, ili wasikilizaji waweze kuwa na imani yenye ufahamu. Watu lazima wafundishwe kwamba Kristo ni wokovu na haki yao. Ni kusudi lililopangwa la Shetani kuzuia nafsi kuamini katika Kristo kama tumaini lao la pekee; kwa maana damu ya Kristo, isafishayo dhambi zote, ni inatenda kazi tu kwa wale wanaoamini katika thamani yake. — **Gospel Workers, uk. 162 (1915).{EVsw 192:5}**

Wengine Wanaosikiliza Mahubiri ya Mwisho

Mungu anataka kuvuta akili kutoka kwa msukumo wa mantiki kuelekea msukumo wa kina zaidi, safi, na wenye utukufu zaidi. Mara nyingi, mantiki ya kibinadamu imezima kabisa nuru ambayo **Mungu** alitaka iangaze kwa miale ya wazi ili kuwathibithishia watu kwamba Bwana wa maumbile (asili) anastahili sifa na utukufu wote, kwa sababu Yeye ni Muumba wa vyote.**{EVsw 193:1}**

Baadhi ya wahudumu hukosea kwa kufanya mahubiri yao kuwa hoja tupu au mabishano. Wako ambao husikiliza mafundisho ya Kweli, na kuguswa na ushahidi unaotolewa; kisha, Kristo anapowasilishwa kama Mwokozi wa ulimwengu, mbegu iliyopandwa huweza kuchipuka na kuzaa matunda kwa utukufu wa **Mungu**. Lakini mara nyingi msalaba wa Kalvari hauwasilishwi mbele ya watu. Wengine huenda wakawa wanasikiliza mahubiri ya mwisho kabisa watakayowahi kuyasikia, na nafasi ya thamani inayopotea basi inapotea milele. Kama pamoja na mafundisho ya Kweli, Kristo na upendo Wake wa ukombozi vingalitangazwa, hawa watu wangaliweza kuvutwa na kuwa upande Wake (Kristo). — **Gospel Workers, uk. 157-158 (1915). {EVsw 193:2}**

Mahubiri ya Kinabii Yanayovuta Umakini

Elekezeni Ulimwengu Kwenye Unabii

Wafuasi wa Kristo wanapaswa kushirikiana kwa bidii kuu kuwaelekeza watu wa ulimwengu kwenye unabii wa Neno la **Mungu** unaotimia kwa kasi. —**Manuscript 38, 1905.{EVsw 193:3}**

Unabii Pekee, Ndio una Jibu kwa Maswali ya Watu Wanaotafakari

Unabii ambao “MIMI NIKO” ameutoa katika Neno Lake, unaounganisha kiungo baada ya kingine katika mnyororo wa matukio, kutoka milele ya zamani hadi milele ya baadaye, unatufunulia mahali tulipo sasa katika mfululizo wa zama/vizazi, na kile kinachotarajiwa kutokea mbeleni. Yote ambayo unabii umetabiri kwamba yatatokea hadi sasa, tayari yameandikwa katika kurasa za historia. Na tunaweza kuwa na hakika kwamba yote yaliyosalia yatatimia kwa mpangilio wake.**{EVsw 193:4}**

Leo, dalili za nyakati zinathibitisha kuwa tuko kwenye kizingiti cha matukio makubwa na ya adhimu. Ulimwengu mzima uko katika hali ya msisimko. Mbele ya macho yetu unabii wa Mwokozi kuhusu matukio yatakayotokea kabla ya kurudi Kwake unatimia: "Nanyi mtasikia habari za vita na matetesi ya vita... Taifa litaondoka kupigana na taifa, na ufalme juu ya ufalme; na kutakuwa na njaa, tauni, na matetemeko ya ardhi katika sehemu mbalimbali." MATHAYO 24:6-10). {EVsw 194:1}

Wakati wa sasa ni wenye kustajaabisha na unaovutia shauku ya kila kiumbe hai. Watawala na viongozi wa kisiasa, watu waliokabidhiwa madaraka na mamlaka, wanaume na wanawake wa fikra kutoka tabaka mbalimbali, wameelekeza macho yao kwenye matukio yanayoendelea. Wanafuatilia kwa makini mahusiano kati ya mataifa. Wanatazama kwa shauku inayotawala kila hali ya kidunia, na wanatambua kuwa jambo kubwa na la lililoazimiwa liko karibu kutokea—kwamba dunia iko ukingoni mwa mgogoro mkubwa.{EVsw 194:2}

Biblia, na Biblia peke yake, ndiyo inayotoa mtazamo sahihi wa mambo haya. Ndani yake yamefunuliwa matukio ya mwisho ya historia ya dunia hii—matukio ambayo tayari yanatupa vivuli vyake mbele, sauti ya ujio wake ikitetemesha dunia na kuwatia watu hofu mioyoni mwao. —**Prophets and Kings, uk. 536-537 (1916).**{EVsw 194:3}

Paza Sauti ya Tarumbeta kwa Uhakika

Kuna wengi wasioelewa unabii unaohusu siku hizi, na ni lazima waangaziwe. Ni wajibu wa walinzi na waumini wa kawaida kupasa sauti ya tarumbeta kwa uhakika. Iwendi dhati na kuwa na bidii, "Piga kelele, usiache, paza sauti yako kama tarumbeta, uwahubiri watu wangu makosa yao, na nyumba ya Yakobo dhambi zao."—**Letter 1, 1875.** {EVsw 194:1}

Toa Ukweli wa Kinabii Ulio Wazi, na uliosheheni (*Crowd in Clear-cut Prophetic Truths*)

Hatari za siku za mwisho zimekuja juu yetu, na katika kazi yetu tunapaswa kuwaonya watu juu ya hatari waliomo. Tusiruhusu matukio ya kusisimua na mazito ambayo unabii umefunua yaaachwe bila kugusiwa (kwa hekima unabii tele ufundishwe, wakati tunazungumza, hasa kwa kuhusianisha na matukio). Kama watu wetu wangekuwa macho angalau nusu, kama wangetambua ukaribu wa matukio yaliyoonyeshwa katika kitabu cha Ufunuo, basi matengenezo yangetokea katika makanisa yetu, na watu wengi zaidi wangekubali ujumbe huu.{EVsw 195:1}

Hatuna muda wa kupoteza; **Mungu** anatuita tuwe walinzi wa roho kama wale ambao watatoa hesabu. Endelezeni kanuni mpya, na leteni Ukweli ulio wazi na unaokata. Itakuwa kama upanga ukatao pande zote mbili. Lakini msikimbilie mijadala ya mabishano. Kutakuwepo nyakati ambazo itatupasa kusimama kimya na kuuona wokovu wa Bwana. Mwacheni Danieli aseme, acheni Ufunuo useme, na uonyeshe kilicho kKweli. Lakini bila kujali ni upande gani wa somo unaowasilishwa, mtukuzeni Yesu kama kitovu cha tumaini lote, Mwinueni Yeye "Shina na uzao wa Daudi, na ile nyota ing'aayo ya asubuhi."—**Testimonies to Ministers and Gospel Workers, uk. 118 (1896).**{EVsw 195:2}

Kwa Njia Mpya na Yenye Mvuto

Usifundishe kwa namna kavu na ya kinadharia tu, kama ilivyofanyika mara nyingi, bali wasilisha Kweli za Neno la **Mungu** kwa njia mpya na yenye mvuto…….{EVsw 195:3}

Kitabu cha Ufunuo lazima kifunguliwe kwa watu. Wengi wamefundishwa kwamba ni kitabu kilichotiwa muhuri na kufungwa; lakini kimetiwa muhuri tu kwa wale wanaokataa nuru na Kweli. Ukweli kilicho nacho lazima kitangazwe ili watu wapate nafasi ya kujiandaa kwa matukio yatakayojiri karibuni. Ujumbe wa malaika wa tatu lazima uwasilishwe kama tumaini la pekee la wokovu kwa dunia inayopotea. —**Letter 87, 1896.** {EVsw 195:4}

Ujumbe wa Malaika Watatu Ni wa Umuhimu Mkubwa

Mada ya umuhimu mkuu ni ujumbe wa malaika wa tatu, unaojumuisha ujumbe wa malaika wa kwanza na wa pili. Kila mmoja anapaswa kuelewa kweli zilizomo katika ujumbe huu na kuzionyesha katika maisha ya kila siku, kwa kuwa hili ni muhimu kwa ajili ya wokovu. Tutalazimika kujifunza kwa bidii na kwa maombi ili kuelewa Kweli hizi kuu; na uwezo wetu wa kujifunza na kuelewa utawekwa chini ya jaribio la juu kabisa. —**Letter 97, 1902.**{EVsw 196:1}

Unabii—Msingi wa Imani Yetu

Wahubiri wanapaswa kuwasilisha Neno la unabii lililo hakika kama msingi wa imani ya Waadventista wa Sabato. Unabii wa Danieli na wa Ufunuo unapaswa kusomwa kwa makini, na sambamba na haya Maneno haya: "Tazama Mwana-Kondoo wa **Mungu**, aichukuaye dhambi ya ulimwengu." **Yohana 1:29.** {EVsw 196:2}

Sura ya ishirini na nne ya Mathayo imekuwa ikiletwa tena na tena mbele yangu kuwa jambo la kuangaziwa kwa wote. Tunaishi katika wakati ambapo unabii wa sura hiyo unatimia. Hebu wahubiri na walimu wetu waeleze unabii huu kwa wale wanaowafundisha. Waache mambo madogo yasiyo na uzito, na wawasilishe Kweli zitakazoamua hatima ya roho. —**Gospel Workers, uk. 148 (1915).**{EVsw 196:3}

Kweli Zinazowahusu Wote Wanaoishi Leo

Tunapaswa kuutangazia ulimwengu Kweli kuu, nzito na adhimu za Ufunuo. Ndani ya kusudi na kanuni za kanisa la **Mungu** kweli hizi zinapaswa kupenya. Baraka imetangazwa kwa wale wanaozipa heshima habari hizi (wanaoheshimu mawasiliano haya). Baraka hii imeahidiwa ili kuwahamasisha watu kukichunguza kitabu hiki.{EVsw 196:4}

Hatupaswi kwa vyovyote kuchoka kukitafakari kitabu hiki kwa sababu ya alama zake za kinabii zinazoonyesha kuchanganya. Kristo anaweza kutupa ufahamu…….azima kuwe na uchunguzi wa karibu na wa bidii zaidi wa Ufunuo, na uwasilishaji wa Kweli zake kwa juhudi kubwa—Kweli zinazomhusu kila mwanadamu anayeishi katika siku hizi za mwisho. **—Manuscript 105, 1902.**{EVsw 197:1}

Ujumbe kwa Ulimwengu Mzima

Maono ambayo Kristo alimpa Yohana, yaliyowasilisha amri za **Mungu** na imani ya Yesu, hakika yanapaswa kutangazwa kwa wazi kwa mataifa yote, watu, na lugha. Makanisa, yanayowakilishwa na Babeli, yameonyeshwa kuwa yameanguka kutoka hali ya kiroho hadi kuwa nguvu ya utesaji dhidi ya wale wanaoshika amri za **Mungu** na kuwa na ushuhuda wa Yesu Kristo. Kwa Yohana, nguvu hii ya kutesa imeonyeshwa kuwa na pembe kama za mwana-kondoo, lakini inanena kama joka. —**Testimonies to Ministers and Gospel Workers, uk. 117 (1896).**{EVsw 197:2}

Kupokea Majibu ya Kawaida ya Wajumbe wa Mkutano

Mikutano ya Ndugu ----- ilihudhuriwa na watu kwa wingi, nao walimsikiliza kwa hamu kubwa; shauku iliendelea hadi mwisho. Akiwa na Biblia mkononi, na aliweka hoja zake zote juu ya Neno la **Mungu**, Ndugu ------ aliwaonyesha unabii wa Danieli na Ufunuo. Maneno yake mwenyewe yalikuwa machache; aliyaacha Maandiko yenyewe kuelezea Ukweli kwa watu. Baada ya kuwafunulia Ukweli, Mzee ----- aliomba maoni kutoka kwa hadhira yake: "Sasa," alisema, "wale wanaoona Ukweli wa kile ninachosema, na wainue mikono yao"; na kwa kuitikia, mikono mingi ilinyoshwa juu. Siwezi kueleza vya kutosha ni kwa kiasi gani kazi yake ilivutia watu. —**Letter 400, 1906.**{EVsw 197:1}

Mtazamo wa Kisasa Kuhusu Ukweli wa Unabii

Kama ilivyokuwa zamani, ushuhuda wa wazi wa Neno la **Mungu** ulikumbana na swali hili: "Je, kuna mtawala au Farisayo yeyote aliyesadiki?" Na walipoona ugumu wa kupinga hoja zinazotolewa kutoka kwa vipindi vya unabii, wengi waliwachanganya wengine kwa kufundisha kwamba vitabu vya unabii vimefungwa na haviwezi kueleweka. Umati, walioweka tumaini lao kwa wachungaji wao, walikataa kusikiliza onyo; na wengine, ingawa walihakikishiwa **Ukweli**, waliogopa kuungama kwa hofu ya "kutengwa na sinagogi." Ujumbe ambao **Mungu** alikuwa ametuma kwa ajili ya kujaribu na kutakasa kanisa, ulionyesha wazi jinsi idadi kubwa ya watu walivyokuwa wameweka mapenzi na mioyo yao kwenye dunia kuliko kwa Kristo. Mifungo ya kidunia ilikuwa na nguvu zaidi kuliko kifungo cha mbinguni. Waliamua kusikiliza sauti ya hekima ya kidunia na kugeuka kutoka kwa ujumbe wa Ukweli unaochunguza mioyo. —**The Great Controversy, uk. 380 (1888).**{EVsw 198:1}

Kujua Vizuri Historia ya Unabii

Vijana wanaotamani kujitoa kwa huduma ya Injili, au ambao tayari wako katika huduma hiyo, wanapaswa kufahamu vizuri kila mstari wa historia ya unabii. —**Gospel Workers, uk. 98 (1915).**{EVsw 198:2}

Mwanga Zaidi Katika Unabii

Mwanga unaongezeka zaidi, utaangaza juu ya Ukweli mkuu wa unabii, na utaonekana kwa upya na kwa mwangaza mkuu, kwa sababu miale angavu ya Jua la Haki itaangazia kila kitu.{EVsw 198:3}

Je, tunaamini kwamba tunakaribia wakati wa mwisho, kwamba tunaishi katika matukio ya mwisho ya historia ya dunia? Je, tutaamka sasa na kufanya kazi ambayo inahitajika kwa wakati huu, au tutasubiri hadi mambo haya yatutokee? —**Manuscript 18, 1888.**{EVsw 198:4}

Unabii Umewekwa Wazi Tayari

Bwana anataka watu wote waelewe jinsi anavyoshughulika sasa, wakati huu tunaoishi. Hakuna haja ya majadiliano marefu kuhusu nadharia mpya juu ya unabii ambao tayari **Mungu** ameuweka wazi. Sasa kazi kubwa inayopaswa kuwa katika akili zetu ni kujitathmini wenyewe mbele za **Mungu**. Je, miguu yetu ipo juu ya Mwamba wa milele? Je, tunajificha katika kimbilio letu pekee? Dhoruba inakuja, kali isiyo na huruma. Je, tumejiandaa kuivumilia? Je, tumo ndani ya Kristo kama Yeye alivyo ndani ya Baba? Je, sisi ni warithi wa **Mungu** na warithi pamoja na Kristo? Je, tunashirikiana na Kristo? —**Manuscript 32a, 1896.**{EVsw 199:1}

Fundisha Mafundisho ya Kristo

Mtume anatoa agizo zito kwa kila mhubiri wa Injili. Anawaweka wakfu mbele za **Mungu** na Bwana Yesu Kristo, atakayewahukumu walio hai na waliokufa, kuhubiri Neno, na wasiweke msisitizo tu kwa unabii au sehemu za mabishano katika Maandiko, bali mafundisho makuu na ya muhimu zaidi ni yale yaliyotolewa na Yesu Kristo Mwenyewe.—**Manuscript 13, 1888.**{EVsw 199:2}

Kuzuia Bila Kuficha Ukweli

Chakula Kigumu Sio kwa Ajili ya Watoto Wachanga

Hebu wasilisha Ukweli kama ulivyo katika Yesu, mstari juu ya mstari, amri juu ya amri, hapa kidogo na pale kidogo. Zungumzia kuhusu upendo wa **Mungu** kwa maneno rahisi kueleweka. **Ukweli** wa Biblia, unapowasilishwa kwa unyenyekevu na upendo wa Yesu, utakuwa na matokeo makubwa, yanayozungumza katika akili za wengi.{EVsw 199:3}

Nafsi nyingi zinahisi njaa ya mkate wa uzima. Kilio chao ni: “Nipe mkate; usinipatie jiwe. Ninahitaji mkate.” Lisha roho hizi zinazokaribia kuangamia kwa njaa. Wahudumu wetu wakumbuke kwamba chakula kigumu si kwa ajili ya watoto wachanga wasiojua kanuni za kwanza za Ukweli tunaoamini. Katika kila kizazi, Bwana amekuwa na ujumbe maalum kwa watu wa wakati huo; vivyo hivyo, tuna ujumbe kwa watu wa kizazi hiki. Lakini ingawa tuna mengi ya kusema, tunaweza kulazimika kuzuia baadhi yake kwa muda, kwa sababu watu bado hawajawa tayari kuyapokea. —**Review and Herald, Oktoba 14, 1902.**{EVsw 200:1}

Andaa Udongo Kabla ya Kupanda Mbegu

Unapofanya kazi katika eneo jipya, usifikiri kuwa ni wajibu wako kusema mara moja kwa watu: Sisi ni Waadventista wa Sabato; tunaamini kuwa siku ya saba ni Sabato; tunaamini katika roho hufa mtu anapokufa, na wala haiendi mbinguni mpaka wakati wa ufufuo. Hili mara nyingi litajenga kizuizi kikubwa kati yako na wale unaotaka kuwafikia.{EVsw 200:2}

Zungumza nao, kadiri unavyopata fursa, kuhusu mafundisho ambayo mnaweza kukubaliana. Sisitiza umuhimu wa utauwa wa vitendo. Wape ushahidi kwamba wewe ni Mkristo, unayetaka amani, na kwamba unapenda roho zao. Waonyeshe kuwa wewe ni mtu wa dhamiri safi. Kwa njia hii utawafanya waamini; na kutakuwa na wakati wa kuzungumzia mafundisho. Wafanye waumini kwanza, andaa udongo, ndipo upande mbegu, ukiwasilisha kwa upendo Ukweli kama ulivyo katika Yesu. —**Gospel Workers, uk. 119-120 (1915).**{EVsw 200:3}

Jihadhari Usiyafunge Masikio ya Wasikilizaji

Usiku uliopita nikiwa usingizini nilionekana kuwa katika mkutano na ndugu zangu, nikimsikiliza Mmoja aliyesema kwa mamlaka. Alisema: “Nafsi nyingi zitahudhuria mkutano huu ambazo kwa uaminifu hawajui Ukweli utakaoletwa mbele yao. Watasikiliza na kuvutiwa, kwa sababu Kristo anawavuta. Dhamiri yao itawaambia kuwa wanachosikia ni Kweli, kwa kuwa msingi wake ni Biblia. Hivyo, unahitajika uangalifu mkubwa katika kushughulika na roho hizi.{EVsw 200:3}

Usianze kwa kuwapelekea watu vipengele vya mafundisho yetu vinavyowachukiza zaidi, kwa kuwa unaweza kuwafungia masikio yao, kwa kuwa mambo haya ni kama ufunuo mpya kwao. Toa sehemu za Ukweli ambazo wanaweza kuelewa na kuthamini; ingawa zinaweza kuonekana za ajabu au zenye kushtua, wengi watazitambua kwa furaha kama nuru mpya juu ya Neno la **Mungu**. Lakini ikiwa Ukweli utawasilishwa kwa kipimo kikubwa kiasi kwamba hawawezi kuukubali, baadhi watatoka na hawatarudi tena. Zaidi ya hayo, watapotosha Ukweli huo."—**General Conference Bulletin, February 25, 1895.**{EVsw 201:1}

Hapa Kidogo, Pale Kidogo

Wale waliopata mafundisho ya Ukweli kwa maelekezo na mfano wanapaswa kuwa wavumilivu kwa wale ambao hawajawahi kufundishwa Maandiko isipokuwa kupitia tafsiri zilizotolewa na wachungaji na washiriki wa kanisa, na waliopokea mapokeo na hekay kama Ukweli wa Biblia. Wanaposhuhudia Ukweli ukifundishwa, wanashangaa; ni kama ufunuo mpya kwao, na hawawezi kustahimili kupewa Ukweli wote kwa namna yake ya ajabu mara moja. Yote yanakuwa mapya, ya kushangaza, na tofauti kabisa na kile walichowahi kusikia kutoka kwa wachungaji wao, na hivyo wanashawishika kuamini kile walichoambiwa, kwamba Waadventista wa Sabato ni waasi wa imani na hawaamini Biblia. Wasilisha Ukweli kama ulivyo katika Yesu, mstari juu ya mstari, amri juu ya amri, hapa kidogo, na pale kidogo. — **Manuscript 95, 1894.**{EVsw 201:2}

Chukua Hoja au Pointi Moja Kwa Wakati, Kwa wakati mmoja

Walimu wa Neno la **Mungu** hawatakiwi kuacha sehemu yoyote ya shauri la **Mungu**, ili watu wasibaki katika ujinga wa wajibu wao na kutofahamu mapenzi ya **Mungu** juu yao, wakaanguka kwenye upotevu. Lakini, ingawa mwalimu wa Ukweli anapaswa kuwa mwaminifu katika kuwasilisha Injili, hebu asiwape watu mambo mengi ambayo hawawezi kuelewa kwa sababu ni mapya na magumu.{EVsw 201:3}

Chukua hoja moja kwa wakati, na ifanye hiyo hoja kuwa wazi, ukizungumza polepole na kwa sauti ya kueleweka. Zungumza kwa namna ambayo watu wataona uhusiano wa hoja hiyo na ukweli mwingine wa umuhimu wa kiroho. Itakuwa vigumu kuamsha chuki katika mioyo ya wale wanaotafuta Ukweli kama hazina iliyofichika, ikiwa mhubiri atajificha ndani ya Kristo; kwa maana hapo atamdhihirisha Kristo, na siyo nafsi yake. —**Manuscript 39, 1895.**{EVsw 201:3}

Kazia Ukweli wa Msingi

Usijikite sana katika hoja za kupinga au upinzani, bali jikusanyie Ukweli wa msingi wa imani, na uupandikize ndani yako kwa kujifunza kwa bidii, maombi ya dhati, na kujitoa moyo wako kwa **Mungu**. Hakikisha taa zako zimewashwa na zikiwa na mafuta; na acha miale yake iangaze, ili watu waone matendo yako mema, nao wamtukuze Baba yako aliye mbinguni.{EVsw 202:1}

Mwalimu Mkuu (Yesu Kristo) alishikilia ramani yote ya Ukweli mikononi Mwake, lakini hakuifungua yote kwa wanafunzi Wake. Aliwafunulia tu yale yaliyokuwa muhimu kwa maendeleo yao katika njia ya kuelekea mbinguni. Kulikuwa na mambo mengi ambayo hekima Yake ilimfanya anyamaze. Kama vile Kristo alivyowaficha wanafunzi Wake mambo mengi kwa kujua kuwa wakati huo hawangeweza kuyaelewa, vivyo hivyo leo anabakiza mambo mengine sababu ya uwezo wetu wa kuelewa ni mdogo. —**Review and Herald, Aprily 23, 1908.**{EVsw 202:2}

Dhana za Kufundishia ile Kweli

Mifano na Ishara za Kristo

Tunapaswa kujitahidi kufuata kwa karibu zaidi mfano wa Kristo, Mchungaji Mkuu, jinsi alivyofanya kazi na kundi Lake dogo la wanafunzi, Akijifunza pamoja nao na pamoja na watu Maandiko ya Agano la Kale. Huduma Yake haiwezi kufupishwa tu kwa mahubiri, bali ilikuwa ni kazi ya kuwaelimisha watu. Alipopitia vijiji mbalimbali, Alikutana na watu moja kwa moja katika nyumba zao, Akiwafundisha na kuwahudumia mahitaji yao. Alipokuwa akifuatwa na makundi makubwa ya watu, Alipofika mahali panapofaa, Aliwahutubia kwa kutumia mifano na alama ili kurahisisha mahubiri-mafundisho Yake. —**Letter 192, 1906.** {EVsw 203:1}

Matumizi ya Michoro-chati

Umejitahidi sana kutafakari jinsi ya kuifanya Kweli kuwa ya kuvutia, na chati/michoro uliyoitengeneza inakubaliana kabisa na kazi inayopaswa kufanyika. Michoro hii ni masomo ya mfano kwa watu. Umeweka fikra zako kwa bidii sana katika kutengeneza vielelezo hivi vya kuvutia. Michoro hii ina

matokeo makubwa sana inapowasilishwa kwa watu kwa ajili ya kutetea Kweli. Bwana huitumia kugusa mioyo. Nimepewa maagizo ya wazi na ya dhahiri kwamba michoro inapaswa kutumiwa katika kuwasilisha Kweli. Vielelezo hivi vinapaswa kuambatana na maneno yanayoonyesha umuhimu wa utii. —**Letter 51, 1902.** {EVsw 203:2}

Unabii Kufundishwa kwa Chati/Michoro Rahisi na Isiyo ya Gharama Kubwa

Matumizi ya chati/michoro ni yenye mafanikio makubwa katika kufafanua unabii unaohusu wakati uliopita, uliopo, na ujayo. Lakini tunapaswa kufanya kazi yetu kwa usahili na unyenyekevu na kwa njia isiyo ya gharama kubwa. Kweli inapaswa kufafanuliwa kwa unyofu. Kamwe tusifuate mfano wa maonyesho ya nje kama wafanyavyo watu wa dunia. —**Manuscript 42, 1905.** {EVsw 203:3}

Matumizi Yenye Ufanisi ya Vifaa Vinavyofaa

Ndugu S kwa sasa anafanya kazi huko Oakland….. Amepiga hema lake katika sehemu ya kati na amepata wasikilizaji wazuri, hata kuliko tulivyotarajia. {EVsw 204:1}

Ndugu S ni mhubiri mwenye akili mahiri. Huhubiri kwa unyenyekevu kama mtoto. Kamwe haingizi kejeli katika mahubiri yake. Huhubiri moja kwa moja kutoka katika Neno, akiliacha Neno linene kwa watu wa kila tabaka. Hoja zake kuu ni maneno ya Agano la Kale na Jipya. Hatafuti maneno ya kupendeza tu watu ili kuwaonyesha watu elimu yake, bali hujaribu kuacha Neno la **Mungu** lizungumze moja kwa moja kwao kwa uwazi na ya kipekee. Wale wanaokataa ujumbe, basi wanakataa Neno la **Mungu**.{EVsw 204:2}

Ndugu S anahubiri hasa juu ya unabii wa vitabu vya Danieli na Ufunuo. Ana vielelezo vikubwa vya wanyama waliotajwa katika vitabu hivyo. Vielelezo hivi vimetengenezwa kwa sanaa ya karatasi za gundi (papiermache), na kwa uvumbuzi wa kisanii, huletwa mbele ya kusanyiko kwa wakati unaofaa. Kwa njia hii huwavutia wasikilizaji wake huku akiwahubiria Kweli. Kupitia juhudi hizi, mamia wataelewa Biblia kwa undani zaidi kuliko hapo awali, na tunatumaini kutakuwa na wongofu wengi. —**Letter 326, 1906.** {EVsw 204:3}

Kanuni Sahihi ya Elimu ya Kiroho

Huduma ya Ndugu S inanifanya nikumbuke kazi iliyofanyika kati ya mwaka 1842 na 1844. Hutumia Biblia, na Biblia peke yake, kuthibitisha hoja zake. Huwasilisha wazi “Ndivyo Asemavyo Bwana.” Na kama mtu yeyote atapingana na maneno yake, huweka wazi kwamba wanabishana na **Mungu**, si yeye. Ana vielelezo vikubwa vya wanyama na alama zilizotajwa katika vitabu vya Danieli na Ufunuo, ambavyo huonyeshwa wakati ufaao ili kuonyesha hoja zake. Hakuna neno la mzaha au lisilo la lazima litokalo kinywani mwake. Husema kwa nguvu na kwa uzito. Wengi wa wasikilizaji wake hawajawahi kusikia mahubiri ya aina hiyo ya uzito. Hakuna mzaha unaoonyeshwa, bali hali ya hofu takatifu hutanda azungumzapo. —**Letter 350, 1906.** {EVsw 205:1}

Wakatoliki Huvutiwa na Alama

Ndugu S anaamsha shauku kubwa kwa watu wengi katika mikutano yake. Watu wa tabaka mbalimbali hujitokeza kusikiliza na kuona vielelezo vya wanyama wa Ufunuo vilivyotengenezwa kwa ukubwa wa maisha halisi. Wakatoliki wengi huja kumsikiliza. —**Letter 352, 1906.** {EVsw 205:2}

Mbinu za Kutumia Katika Kazi ya Mwisho

Nimefurahia jinsi ndugu yetu [Ndugu S] alivyoonyesha ubunifu na hekima katika kuandaa vielelezo vinavyofaa kwa mada anazowasilisha—mawakilishi wenye nguvu ya kushawishi. Mbinu kama hizi zitatumika zaidi na zaidi katika kazi ya mwisho. —**Manusripti 105, 1906.** {EVsw 205:3}

Vijana Kujifunza Jinsi ya Kuwasilisha Kweli ya Kielelezo

Bwana amekuwa akifanya kazi na Ndugu S, akimfundisha jinsi ya kuwapelekea watu ujumbe huu wa mwisho wa onyo. Njia yake ya kuacha Naneno ya Biblia yenyewe yahubiri Kweli ya wakati huu, na matumizi yake ya alama katika Ufunuo na Danieli, ni yenye mafanikio. Hebu vijana na wajifunze kile Kweli inachomaanisha kwa ajili ya maisha yao na jinsi inavyopaswa kuwasilishwa. Tunaishi katika siku za mwisho za mapambano makuu; ni ile Kweli tu ndiyo itakayoweza kutulinda salama katika wakati wa taabu. Njia ipasavyo iandaliwe kwa Ndugu S ili awasilishe ujumbe, na vijana wetu wahudhurie mikutano yake ya jioni. —**Letter 349, 1906.**{EVsw 205:4}

Watenda Kazi Kuwaza na Kubuni Vifaa (devices)

Watenda kazi wa **Mungu** na waonyeshe werevu na vipaji, na wabuni njia (vifaa) za kuwapelekea nuru wale walio karibu na walio mbali……. Muda wa thamani umepotea, nafasi za thamani hazijatumiwa, kwa sababu watu walikosa maono ya kiroho na hekima ya kupanga na kubuni njia (vifaa) za kutangulia kabla adui hajachukua nafasi. —**Review and Herald, March 24, 1896.**{EVsw 206:1}

Vifaa kwa Ajili ya Kufundisha, Siyo kutumbuiza watu

Kupitia michoro/chati, alama, na vielelezo mbalimbali, mhubiri anaweza kuifanya Kweli ionekane kwa uwazi na dhahiri. Hili ni jambo linalosaidia na linapatana na Neno la **Mungu**. Lakini mhudumu anapofanya kazi yake iwe ya gharama kubwa kiasi kwamba wengine hushindwa kupata msaada kutoka hazina ya kanisa kuwasaidia kuendelea katika huduma, basi hafanyi kazi kwa mpango wa **Mungu**.{EVsw 206:2}

Kazi katika miji mikubwa inapaswa kufanywa kwa namna ya Kristo, si kwa namna ya onesho la jukwaani. Siyo onesho la maigizo ndilo linalomtukuza **Mungu**, bali ni kuwasilisha Kweli kwa upendo wa Kristo. —**Testimonies for the Church, 9:142 (1909).** {EVsw 206:3}

Hadithi, Visa/anectodes, Mizaha, na Utani

Balozi wa Kristo

Mhubiri wa Injili ambaye ni mtendakazi pamoja na **Mungu**, hujifunza kila siku katika shule ya Kristo….. Hakutakuwa na maneno mepesi au ya mizaha yanayotoka midomoni mwake; kwani si balozi wa Kristo, mwenye ujumbe wa Kiungu kwa roho zinazopotea? Mizaha na utani wa kila namna, upuzi na mzaha, ni maumivu kwa mwanafunzi wa Kristo anayebeba msalaba. Moyo wake hubeba mzigo kwa ajili ya roho, na huendelea kumwomba **Mungu** kwa neema ili awe msimamizi na wakili mwaminifu. Huomba atakaswe na ahifadhiwe, na kupinga kuingia kwa kutokujali katika majaribu.{EVsw 206:4}

Husikiliza amri hii: “bali kama Yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote; kwa maana imeandikwa, Mtakuwa watakatifu kwa kuwa Mimi ni mtakatifu1 **Peter 1:15-16**.”……. Akikaa karibu na Mwalimu wake, hupokea Maneno kutoka Kwake ya kuongea na watu. Akiinua kama Kristo, akipenda kama Kristo, akifanya kazi kama Kristo, huzunguka akitenda mema. Hujitahidi kwa bidii kuboresha nafsi yake ili kwa mafundisho na mfano, awaongoze wengine kwenye maisha safi, ya juu, bora na yenye heshima. —**The Review and Herald, January 21, 1902.**{EVsw 207:1}

Kuishi Matokeo Makubwa ya Kiungu

Wachungaji/wahudumu hawapaswi kuhubiri maoni ya wanadamu, wala kusimulia visa, wala kuandaa maigizo au kujionyesha; bali wakiwa kama mbele za **Mungu** na Bwana Yesu Kristo, wahubiri Neno. Wasilete utani katika kazi ya huduma, bali wahubiri Neno kwa namna itakayowaachia wasikilizaji matokeo ya kiroho yenye uzito-utakatifu. —**The Review and Herald, September 28, 1897.**{EVsw 207:2}

Waonyeshe Wageni Ukuu wa Ukweli

Ni mapenzi ya **Mungu** kwamba huduma zote ziendeshwe kwa mpangilio unaofaa na wa heshima, ili hata wageni wanaohudhuria pamoja na waumini wa kawaida, waone ukubwa wa ile Kweli na uwezo wake wa kusafisha moyo.{EVsw 207:3}

Katika majaliwa/mpango wa **Mungu**, watu huongozwa kuhudhuria mikutano ya hema na ibada za kanisa. Baadhi huja ili kudadisi, wengine kwa kukosoa au kucheka. Mara nyingi hushawishiwa juu ya dhambi. Neno linalonenwa kwa roho ya upendo huwaacha na matokeo ya kudumu. Kwa hiyo, mikutano hii inapaswa kuendeshwa kwa umakini mkubwa. Maneno yahubiriwe kwa mamlaka, ili Roho Mtakatifu aweze kuyaingiza moyoni na kumgusa mtu. Mhubiri anayelekezwa na Roho wa **Mungu** ana heshima takatifu, na maneno yake huwa harufu ya uzima wa milele. Visa visivyofaa visiletwe kwenye mahubiri. Hebu maneno yahubiriwe kwa ajili ya kuujenga mwili wa Kristo. —**Letter 19, 1901.**{EVsw 207:4}

Mfano wa Yesu Katika- Mifano (vielelezo/illustration)

Ujumbe wa rehema wa Kristo ulionekana tofauti-tofauti, ili kuendana na hadhira Yake. Alijua jinsi ya kunena Neno kwa wakati unaofaa kwa yule aliyechoka; maana neema ilimwagwa kinywani Mwake, ili

awasilishe hazina za Kweli kwa njia ya kuvutia. Alikuwa na hekima ya kukutana na akili zenye chuki au ubaguzi na kuwavuta kwa mifano iliyowashangaza.{EVsw 208:1}

Kupitia fikra, aliufikia moyo. Mifano Yake ilitokana na maisha ya kila siku—ndege wa angani, maua ya kondeni, mbegu, mchungaji na kondoo—na ingawa ilikuwa rahisi, ilikuwa na maana ya kina cha ajabu. Kila mara walipoona vitu hivyo katika uumbaji, walikumbuka mafundisho Yake. —**The Desire of Ages, uk. 254 (1898).**{EVsw 208:2}

Kuuhafifisha Ujumbe Mtakatifu

Tusiwahi kusahau uzito wa kazi hii takatifu ya kufundisha watu kwa Neno na mafundisho. Ni kazi ya mhubiri kusema Ile Kweli takatifu, yenye uzito na adhimu. Wengine wamejenga tabia ya kusimulia visa katika mahubiri yao, jambo ambalo huwachangamsha wasikilizaji na kuondoa hali ya utakatifu ya Neno wanalopeleka. Hawa wapaswa kutafakari kuwa hawatoi Neno la Bwana. Mifano mingi isiyo na maana sahihi hudhalilisha heshima ya kazi ya Neno la **Mungu katika uwasilishaji**. —**The Review and Herald, February 22, 1887.** {EVsw 208:3}

Chakula Hafifu Sana

Wapo watu wanaosimama mimbarini kama wachungaji, wakidai kuwalisha kondoo, lakini kondoo wanaendelea kuona njaa ya mkate wa uzima. Mahubiri marefu yaliyosheheni visa visivyo na matokeo ndani ya moyo. Wengine huamshwa kihisia, wakilia machozi, lakini mioyo yao haijavunjika. Yesu amekuwa mgeni katika mahubiri haya, lakini maneno yao hayana umande wala mvua ya mbinguni. Wale waliotiwa mafuta kama ilivyoelezwa na nabii Zekaria (sura ya 4), hawajawahi kuwahudumia na kuwapatia wengine (Neno na huduma). Wale waliotiwa mafuta watakapoayaachia mafuta kupitia mirija ya dhahabu, mafuta yatatiririkka hadi kwenye bakuli la dhahabu, kisha yataenda kwenye taa, ambayo ni makanisa. Hii ni kazi ya kila mtumishi wa kweli na aliyejitoa wa **Mungu** aliye hai. Bwana **Mungu** wa mbinguni hawezi kuidhinisha mengi ambayo yanaletwa kwenye mimbari na wale wanaodai kusema Neno la Bwana. Hawafanyi Mawazo ambayo yatakuwa baraka kwa wale wanaosikiliza. Yale yanayopatikana katika baadhi ya mahubiri ni chakula hafifu (cheap/pumba tu), kisicho na faida kwa watu wa **Mungu**. —**Testimonies to Ministers and Gospel Workers, uk. 336, 337 (1896).**{EVsw 209:1}

Moto wa Kigeni

Lengo la kazi ya huduma si kuburudisha na kuchekesha watu. Sio kutoa maarifa pekee, wala kushawishi akili tu. Kuhubiri kunapaswa kuwagusa wasikilizaji kwa akili na moyo na kutoa maarifa ila ni zaidi ya hivyo. Baadhi wamekuwa na mtindo wa mahubiri ambao hauna mvuto sahihi…….. {EVsw 209:2}

Mchungaji anapotumia hekaya au hadithi za kufurahisha katika mahubiri yake, anatumia moto mgeni. Unakutana na watu wa kila aina ya mawazo. Katika kushughulika na Neno Takatifu, onyesha uzito, adhima, heshima na ibada. Usitoe taswira ya kuwa wewe ni mhubiri hafifu na juu juu tu (cheap surface speaker). Ondoa usimuliaji wa visa katika mahubiri yako. Hubiri Neno. Ungekuwa na mavuno mengi kwa ajili ya Bwana kama ungekuwa ukilihubiri Neno kila mara. Unafahamu kidogo sana juu ya haja kuu ya moyo/nafsi na tamanio lake. Wengine wanapambana na mashaka, giza, wakiwa karibu kukata tamaa…..{EVsw 210:1}

Mungu hukasirika wajumbe Wake wanapotumia maneno mepesi ya mzaha/futuhi. Sababu ile Kweli, hudharauliwa. Watu huchukulia kanisa lote kwa mfano wa mhubiri mmoja-wanahukumu kazi kwaajili ya mhubiri mmoja. Adui wa Kweli hutumia makosa hayo kudhalilisha kazi ya **Mungu**. —**Letter 61, 1896.** {EVsw 210:2}

Njaa ya Mkate wa Uzima

Weka hekaya/hadithi zako moyoni mwako mwenyewe. Watu hawana njaa ya hekaya hizo, bali wanahitaji mkate wa uzima—Neno liishilo na kudumu milele. Je, makapi au pumba ni ya nini kwenye ngano? —**Letter 61, 1896.**{EVsw 210:3}

Usadikisho Kupotezwa Kwa Mizaha na Ujinga mtupu

Baada ya kazi njema kufanywa, wale walioguswa moyo juu ya dhambi wanapaswa kufundishwa jinsi ya kushikilia mkono wa Bwana. Lakini kama hisia hizo njema hazitafuatiliwa na juhudi za kweli na za bidii, hakuna matokeo ya kudumu yatakayopatana. Matokeo yangekuwa tofauti kabisa kama tamaa ya burudani haingewatoa watu kwenye mawazo ya kiroho.....{EVsw 210:4}

Matumbuizo au burudani havipaswi kuchanganywa na mafundisho ya Maandiko. Iwapo hii itafanyika, wasikilizaji watakaoburudishwa na ucheshi wa usio na maana wa ujinga tu (nosense), watapoteza mzigo wa usadikisho. Fursa hupita, na hakuna anayeongozwa kwa kamba za upendo kwa Mwokozi. **—Manuscript 83, 1901.**{EVsw 211:1}

Uwe Huru Dhidi ya Maneno Mepesi na Kawaida (cheap and nosense words)

Ujumbe wa ile Kweli unapaswa kuwa huru kabisa dhidi ya maneno ya kawaida, duni na rahisi yaliyobuniwa na wanadamu. Kwa njia hiyo, athari zenye nguvu hutengenezwa mioyoni. Wachungaji wetu wasidhanie kwamba ni lazima walete vitu vipya na vya ajabu, au kwamba maneno ya kawaida yatawapa ushawishi. Wahubiri ni vinywa vya **Mungu**, na wanapaswa kuondoa kabisa kutoka katika usemi wao kila maneno ya kawaida au mepesi, duni au yenye ladha mbaya. Wawe waangalifu kwamba, kwa kujaribu kuleta kicheko, wasimvunjie **Mungu** heshima.{EVsw 211:2}

Ujumbe wetu ni mzito, adhimu na wa utakatifu, na ni lazima tuwe waangalifu katika maombi. Maneno yanayonenwa ni lazima yawe ya namna ambayo **Mungu** anaweza kuyatumia kugusa mioyo na akili. Hebu wahubiri wa Injili watakaswe kwa ile Kweli. —**Letter 356, 1906.**{EVsw 211:3}

Majaribio ya Uongo na Viwango Vilivyowekwa na Wanadamu

Fundisha Ukweli wa Msingi — Wale wanaotaka kufanya kazi ya kufundisha Neno na mafundisho wanapaswa kwanza kuwa imara katika Kweli kabla ya kupewa idhini ya kwenda kuifundisha kwa wengine. Ukweli safi, usiotiwa doa wala kuchanganywa, lazima uwasilishwe kwa watu. Ni ujumbe wa malaika wa tatu unaoleta kipimo halisi kwa watu. Shetani atawaongoza watu kutengeneza majaribio ya uongo ili kuuficha umuhimu wa ujumbe huu wa Kweli na kuufanya usiwe na athari yoyote.{EVsw 211:4}

Amri ya **Mungu** ambayo imekaribia kufutwa/kukanushwa karibu kwenye ulimwengu wote, ndiyo Kweli inayojaribu mioyo ya watu kwa wakati huu…... Wakati unakuja ambapo wanadamu wote wanaomwabudu **Mungu** watatambuliwa kwa alama hii. Watatambulika kama watumishi wa **Mungu** kwa alama hii ya uaminifu wao kwa Mbingu. Lakini majaribio yote yaliyowekwa na wanadamu yatapotosha mawazo dhidi ya Mafundisho Makuu na muhimu ambayo ndiyo Kweli ya sasa.{EVsw 212:1}

Ni mpango na shauku ya Shetani kuingiza miongoni mwetu watu wa msimamo mkali—watu wenye fikra finyu, wenye kukosoa sana, wakali na wanaoshikilia kwa nguvu maoni yao binafsi juu ya maana ya kweli. Watu hawa watakuwa wagumu, wakali na watajaribu kulazimisha majukumu mazito, wakizidisha mambo yasiyo ya maana huku wakisahau mambo yenye uzito zaidi ya sheria—hukumu, rehema, na upendo wa **Mungu**. Kwa kazi ya watu wachache wa namna hii, kundi lote la washika **Sabato** litachukuliwa kuwa ni wenye misimamo mikali, watu waliopitiliza, wanafiki, Mafarisayo, na wendawazimu. Kazi ya ile Kweli, kwa sababu ya watendakazi hawa, itachukuliwa kuwa haina umuhimu wowote, na haipaswi kupewa umakini. {EVsw 212:1}

Mungu anayo kazi maalum kwa ajili ya watu wenye uzoefu. Wao wameitwa kuilinda kazi ya **Mungu**. Ni jukumu lao kuhakikisha kuwa kazi ya **Mungu** haiwekwi mikononi mwa watu wanaojiona kuwa na haki ya kujiamulia mambo kwa maoni yao binafsi, kuhubiri wapendavyo, na wasiwajibike kwa mtu yeyote kuhusu mafundisho au kazi yao. Hebu roho hii ya kujitegemea, au kujitosheleza mwenyewe ikikubalika miongoni mwetu, hakutakuwa na maelewano, mshikamano katika utendaji, wala umoja wa kiroho, hakutakuwa na usalama kwa kazi hii takatifu, wala hakutakuwa na ukuaji wenye afya katika lile jambo la **Mungu**. Walimu wa uongo watajitokeza, watendaji wa uovu ambao kwa ujanja na udanganyifu watapenyeza makosa na kuwavuta watu mbali na **Kweli**. **Kristo** aliomba kwamba wafuasi Wake wawe na umoja kama Yeye alivyo na Baba. Wale wote wanaotamani kuona sala hii ya Mwokozi ikitimizwa, wanapaswa kujitahidi kukata mizizi ya kila dalili ya mgawanyiko, na kufanya bidii kudumisha roho ya umoja na upendo kati ya ndugu (udugu). — **The Review and Herald, May 29, 1888.**{EVsw 212:2}

Hekaya ndogo-ndogo—Hazina Thamani Yoyote ni kama pumba au vijiti visivyo na faida — Hatupaswi kutoa wito kwa wale ambao tayari wameupokea Ukweli na wameuelewa, ambao wameusikia tena na tena mpaka mtu fulani anahisi anapaswa kuleta kitu cha kipekee (original). Hapo ndipo huleta hekaya ndogo-ndogo zisizo na thamani hata kidogo kama pumba tu (straws), na kuzifanya kuwa majaribio aliyoweka **Mungu**, ilhali ni Shetani ndiye aliyeleta mambo hayo ili kugeuza mawazo kutoka kwa majaribio ya Kweli aliyoweka **Mungu**.{EVsw 213:1}

—The General Conference Bulletin, April 16, 1901.

Majaribio Mapya na Mageni na ya Kushangaza Kutoka kwa Wanadamu — Hakuna mtu anayepaswa kuilazimisha Kweli na kuitesa kwa kuipatia maana ngeni, za kushangaza au za mafumbo ambayo yanaonekana kama ushirikina fulani (mystical). Hivyo, wengine wapo katika hatari kwa kuigeuza Kweli ya **Mungu** kuwa uongo. Wapo wanaohitaji kuguswa na Roho wa **Mungu** mioyoni mwao. Kisha ujumbe wa wakati huu utakuwa mzigo wao. Hawatatafuta majaribio ya kibinadamu, mambo mapya na ya ajabu. Sabato ya amri ya nne ndiyo jaribio kwa wakati huu, na kila kilichoambatanishwa na ukumbusho huu mkuu kinapaswa kuwekwa mbele ya watu. **—Undated Manuscript 111.**{EVsw 213:2}

Kuwa Huru dhidi ya Mawazo au dhana ya Kibinadamu — Kazi ya **Mungu** ni kazi kuu. Watu wenye hekima wanahitajika ili kudumisha kanuni za Biblia zisichanganywe hata kidogo na sera au mbinu za kidunia. Kila mtendakazi anaendelea kujaribiwa. Paulo anazungumzia wale wanaojenga msingi kwa kutumia miti, mbao, majani makavu, na mabua. Hawa ni wale ambao wanawakilisha watu waletao mambo yasiyo kweli kwamba ndiyo Kweli, na hata dhana zao ambazo hazina uhakika na mambo wanayojitungia wenyewe vichwani mwao. Kama roho hizi zitaokolewa, itakuwa ni kama kwa moto, kwa sababu katika dhamiri zao walijua kwamba walikuwa wakifanya kazi kwa sambamba na Neno la Mungu. Hawa watakuwa kama vijinga vilivyonyakuliwa kutoka kwenye moto.{EVsw 213:3}

Kazi ambayo ingeweza kuwa safi, ya kiwango cha juu, iliyotakaswa, bora na tukufu, imekorogwa-korogwa na makosa, na imani zisizokuwa na hekima zilizoingizwa na wanadamu. Hivyo uzuri wa Kweli umeharibiwa. Hakuna kitu kinachong'aa bila doa la ubinafsi. Mchanganyiko huu wa makosa na kazi ya **Mungu** umeifanya kazi ambayo ilipaswa kuonekana wazi mbele ya dunia kuwa mkorogo wa vitu vingi ulio na misingi inayopingana. **—Letter 3, 1901.**{EVsw 214:1}

Hubiri Neno — Nina maneno ya kusema kwa vijana waliokuwa wakifundisha Kweli. Hubirini Neno. Huenda mkawa na akili za ubunifu. Huenda mkawa mahiri kama walimu Wayahudi katika kuunda nadharia mpya; lakini Kristo alisema juu yao, "*Nao waniabudu bure, Wakifundisha mafundisho Yaliyo maagizo ya wanadamu*." (Mathayo 15:9). Walikuwa wakileta mbele ya watu mapokeo, mawazo, dhana na hekaya za kila aina (Kama Talmud, Tobiti, Makabayo nk). Sheria na ibada walizoingiza zilifanya kuwa vigumu kwa watu kujua kama walikuwa wakitii Neno la **Mungu** au mapokeo ya wanadamu.{EVsw 214:2}

Shetani hufurahi anapoweza kuikanganya akili kwa njia hii. Wahubiri wasifundishe mawazo yao binafsi. Hebu watafute Maandiko kwa bidii, wakitambua kwa uzito kwamba wakifundisha kama mafundisho yale yasiyoandikwa katika Neno la **Mungu**, watakuwa kama wale wanaotajwa katika sura ya mwisho ya Ufunuo-Ufunuo 22.{EVsw 214:3}

Hebu wale wanaojaribiwa kufuata mafundisho ya kufikirika, wajichimbie sana ndani ya hazina ya kweli ya mbinguni, wakitafuta hazina ya thamani ambayo huleta uzima wa milele kwa wanaoipokea. Hazina ya thamani itapatikana na wale wanaolisoma Neno la **Mungu** kwa dhati na bidii, kwa kuwa malaika wa mbinguni watawaongoza katika utafutaji na uchungazaji wao. - **Manuscript 82, 1894.**{EVsw 214:1}

Wakati Watu Wanaposuka Ubunifu wa Kibinadamu — Wakati watu wanapofuma mawazo yao katika mkeka wakazi ya **Mungu**, Bwana huwa Hana haraka. Yeye husubiri mpaka watu waache uvumbuzi wao binafsi na kuukubali mpango na mapenzi ya Bwana. —**Letter 181, 1901.**{EVsw 215:1}

Kufanya Dunia Kutokana na Chembe/atomi moja — Loo, ni watu wangapi wangeweza kufanya kazi kuu ya kujikana na kujitoa wakfu, lakini wamejishughulisha mno na mambo madogo-madogo ya maisha! Wamepofuka na hawaoni mbali. Wanageuza jambo dogo kama atomi kuwa kubwa kama dunia nzima, na jambo kubwa kuwa dogo kama chembe ya atomi. Wamekuwa kama vijito vya maji visivyo na kina, kwa sababu hawawapi wengine maji ya uzima. **—Manuscript 173, 1898.** {EVsw 215:2}

Ujumbe Umeharibiwa na Mtu wa Wazo Moja — Kulikuwa na vipaji vya thamani katika kanisa la -----, lakini **Mungu** hakuweza kuwatumia ndugu hawa hadi watakapoongoka. Baadhi walikuwa na uwezo wa kusaidia kanisa, lakini walihitaji kwanza kuisafisha mioyo yao na kuiweka katika mpango, na hivyo kuwa sawa. Wengine walikuwa wakiingiza majaribio ya uongo, wakifanya mawazo na mitazamo yao kuwa kipimo, wakikuza mambo madogo na kuyafanya kuwa vipimo vya ushirika wa Kikristo, na kuwawekea wengine mizigo mizito. Kwa njia hii, roho ya kukosoa wengine, kulaumiana na migawanyiko iliingia, ambayo ilikuwa na madhara makubwa kwa kanisa. Ilitengeneza taswira fulani kwa watu wasioamini kuwa Watunza Sabato ni watu wa msimamo mkali, na imani yao ya kipekee, iliwafanya kuwa watu waliopitiliza, wasio na huruma, wasio wema, wasio na adabu, wasio waungwana, na kwa kweli si Wakristo. Kwa hiyo, mwenendo wa wachache wenye msimamo mkali uliizuia Kweli kuwafikia watu.{EVsw 215:3}

Wengine walikuwa wakifanya mavazi kuwa jambo la kwanza, wakikosoa mavazi ya wengine, au vazi hili au lile na kuwa tayari kuwalaumu wote wasiokubaliana na mitazamo yao. Wengine walikemea picha, wakidai kuwa zimekatazwa na amri ya pili, na kwamba kila kitu cha namna hiyo kinapaswa kuharibiwa.{EVsw 215:4}

Watu hawa wa 'wazo moja- one idea man' hawaoni kitu kingine ila jambo moja tu linalowajia akilini mwao. Miaka mingi iliyopita tulikumbana na roho na kazi kama hiyo. Watu walijitokeza wakidai kutumwa na ujumbe wa kulaani picha, wakisisitiza kuwa kila mfano wa kitu chochote unapaswa kuharibiwa. Walikwenda mbali hadi kuhukumu saa zilizo na picha, maumbo au alama. {EVsw 216:1}

Baadhi ya watu wachache huko ----- walifika hatua ya kuchoma picha zote walizokuwa nazo, hata zile za wapendwa wao. Ingawa hatukuwa na huruma na harakati hizi za msimamo mkali, tulishauri kuwa wale walioteketeza picha zao hawapaswi kutumia pesa kuzirudisha tena. Kama walifanya hivyo kwa dhamiri, wangeridhika na kuacha jambo hilo hapo-hapo. Lakini hawakupaswa kuwalazimisha wengine wafanye kama wao. Hawakupaswa kuwa dhamiri ya ndugu na dada zao. **—Historical Sketches, kurasa 211-212 (1886).**{EVsw 216:2}

SEHEMU YA 8—KUHUBIRI KWELI ZA KIPEKEE

Kutangaza Kurudi Kwa Kristo Mara Ya Pili

Kuamsha Watu kwa Maandalizi — Tunaishi katika mwisho wa historia ya dunia hii..... Unabii unatimia. Hivi karibuni Kristo atakuja kwa nguvu na utukufu mkuu. Hatuna muda wa kupoteza. Hebu ujumbe huu upeperushwe kwa maneno ya onyo yaliyojaa bidii.{EVsw 217:1}

Lazima tushawishi watu kila mahali kutubu na kuikimbia ghadhabu inayokuja. Wana roho za kuokolewa au kupotea. Tusiruhusu kutojali kuingia katika jambo hili. Bwana anawaita watendakazi waliojaa kusudi thabiti na ari ya kweli. Wawaambie watu wawe tayari wakati wote, unaofaa na usiofaa—. Ukiwa na maneno ya uzima kinywani mwako, ondoka na uwaambie wanaume na wanawake kwamba mwisho wa mambo yote umekaribia.{EVsw 217:2}

hebu tuweke roho zetu ndani ya upendo wa **Mungu**. Sauti ya onyo lazima isikike. Kweli isibaki midomoni mwetu bila ya ari/juhudi. Lazima tuwaamshe watu kwa maandalizi ya haraka, kwa maana hatujui kikamilifu kilicho mbele yetu. Imani yangu bado ni thabiti kwamba tunaishi katika masalio ya mwisho wa wakati. hebu kila mwalimu afungue mlango wa wokovu kwa wote watakaomjia Yesu kwa kutubu dhambi zao. —**Letter 105, 1903.** {EVsw 217:3}

Utangazwe Katika Kila Nchi — Nimeagizwa kuandika maneno ya onyo kwa ndugu zetu walio hatarini kupoteza mtazamo wa kazi maalum ya wakati huu... Katika kila nchi tumeagizwa kutangaza kurudi kwa Kristo mara ya pili, kwa lugha ya mwandishi wa Ufunuo ikitangaza: "*Tazama, Yuaja na mawingu; na kila jicho litamwona Yeye*, ***UFUNUO 1:7***."— —**Testimonies For The Church 8:116 (1904).** {EVsw 217:4}

Wakati umefika ambapo ujumbe wa kurudi kwa Kristo kwa haraka unapaswa kusikika duniani kote. — **Testimonies For The Church 9:24 (1909).**{EVsw 217:1}

Ujumbe: "Bwana Anakuja" — Bwana anakuja. Inueni vichwa vyenu na shangilieni. Lo! Ingetarajiwa kwamba wale wanaosikia habari hizi za furaha, wanaodai kumpenda Yesu, wangekuwa wamejaa furaha isiyosemeka na yenye utukufu. Huu ni ujumbe mzuri, wa furaha kuu, unaopaswa kuamsha kila roho, urudiwe katika familia zetu, na kusimuliwa kwa wale tunaokutana nao mitaani. Kuna habari gani ya furaha iliyo kuu kuliko hii! {EVsw 218:2}

Sauti ya mlinzi wa Kweli inapaswa kusikika kote, "Mchana unakuja, na usiku pia **Isaya 21:12**." Tarumbeta lazima itoe sauti bainishi, sauti inayojulikana, kwa maana tuko katika siku kuu ya maandalizi ya Bwana. —**Letter 55, 1886.**{EVsw 218:3}

Hakuna Muda wa Kupoteza — Pigeni kengele ya onyo katika nchi yote. Waambieni watu kwamba siku ya Bwana iko karibu, tena inakaribia sana. hebu asiwepo mtu yoyote bila onyo. Sisi wenyewe tungeweza kuwa mahali pa wale maskini walio katika makosa. Kwa kweli yale tuliyokabidhiwa kuliko wengine, tunawiwa kuwashirikisha.{EVsw 218:4}

Hatuna muda wa kupoteza. Nguvu za giza zinafanya kazi kwa bidii na nguvu kubwa, na kwa ujanja Shetani anasonga mbele kuwanasa wale waliolala, kama mbwa mwitu anavyonasa mawindo yake. Tunalo onyo la sasa la kuwapa wanadamu, kazi ya sasa ya kufanya, lakini hivi karibuni kazi hii itakuwa ngumu kuliko tunavyofikiria.....**{EVsw 218:5}**

Kurudi kwa Bwana ni karibu kuliko tulivyoaanza kuamini. Pambano kuu linakaribia mwisho wake. Kila habari ya janga baharini au nchi kavu ni ushuhuda kwamba mwisho wa mambo yote umekaribia. Vita na uvumi wa vita vinathibitisha hilo. Je, kuna MKristo ambaye moyo wake haudundi kwa kasi anapotarajia matukio haya makuu yanayofunguka mbele yetu? **{EVsw 219:1}**

Bwana anakuja. Tunasikia hatua za **Mungu** anayekaribia kuingia, anapokuja kuiadhibu dunia kwa uovu wake. Tunapaswa kutengeneza njia kwa ajili Yake kwa kutekeleza sehemu yetu katika kuwaandaa watu kwa ajili ya siku hiyo kuu. **—Review and Herald, November 12, 1914. {EVsw 219:2}**

Nguvu Hai Inapaswa Kupeleka Ujumbe — Ujumbe wa kuja kwa Kristo mara ya pili lazima uandamane na nguvu hai. Hatupaswi kupumzika hadi tuone watu wengi wakigeuka na kuamini tumaini la kurudi kwa Bwana. Katika siku za mitume, ujumbe wao ulifanya kazi halisi, ukiwageuza watu kutoka kwa sanamu na kuwaelekeza kwa **Mungu** aliye hai. Kazi ya leo ni halisi vilevile, na Kweli ni ile ile; ila sisi tunapaswa kuitangaza kwa dhati na bidii zaidi kwa kuwa kurudi kwa Bwana kunakaribia. Ujumbe wa wakati huu ni wa hakika, rahisi, na wa umuhimu mkuu sana. Lazima tutende kama watu wanaouamini. Kusubiri, kuangalia, kufanya kazi, kuomba, na kuonya dunia—hii ndiyo kazi yetu.....**{EVsw 219:4}**

Mbingu yote imechangamkia jambo hili, wakati ikijiandaa kwa siku ya kisasi cha **Mungu**, siku ya ukombozi wa Sayuni. Muda wa kungoja unakaribia mwisho wake. Wahamiaji na wageni, na wasafiri waliokuwa wakitafuta nchi iliyo bora kwa muda mrefu karibu wamefika nyumbani. Najisikia kana kwamba lazima nilie kilio cha furaha kwa sauti ya juu: "Tuko njiani kuelekea nyumbani!" Kwa kasi tunakaribia wakati ambapo Kristo atakuja kuwakusanya watu Wake waliokombolewa waende Kwake. —**Review and Herald, November 13, 1913. {EVsw 219:4}**

Hotuba Zote Ziegemee Katika Nuru ya Kurudi kwa Kristo — Kweli za unabii zimefungamana pamoja, na tunapozisoma, zinaunda mkusanyiko mzuri wa kweli za Kikristo za kiutendaji. Hotuba zote tunazotoa zinapaswa kuonyesha wazi kuwa tunasubiri, tunafanya kazi, na tunaomba kwa ajili ya kurudi kwa Mwana wa **Mungu**. Kurudi Kwake ndilo tumaini letu. Tumaini hili linapaswa kuambatana na maneno na matendo yetu yote, pamoja na mahusiano na ushirika wetu wote. —**Letter 150, 1902. {EVsw 220:1}**

Ufunguo wa Historia — Ufahamu wa tumaini la kurudi kwa Kristo mara ya pili ni ufunguo unaofungua historia yote inayofuata, na kueleza mafundisho yote yajayo. —**Letter 218, 1906. {EVsw 220:2}**

Matokeo ya Kutangaza Kurudi kwa Kristo — Kurudi kwa Mwana wa Adamu ni somo kuu linalopaswa kuwekwa mbele ya watu. Hili ni jambo lisilopaswa kuachwa katika hotuba zetu. Ukweli wa milele lazima uwe mbele ya macho ya akili, na uzuri wa mambo ya dunia utaonekana jinsi ulivyo—bure tu, kama ubatili. Tunapaswa kufanya nini na ubatili wa dunia, sifa zake, mali zake, heshima zake au anasa zake? **{EVsw 220:3}**

Sisi ni wapitaji na wasafiri wanaosubiri, wanaotumaini, na wanaoomba kwa ajili ya tumaini lenye baraka—kuonekana kwa utukufu kwa Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo. Tukiamini hili na kulileta katika maisha yetu ya kila siku, ni matendo ya ajabu na yenye nguvu kiasi gani, na imani na tumaini kubwa kiasi gani hili lingeleta; ni upendo wa joto-joto kiasi gani tungekuwa nao kwa mtu mwingine; ni maisha ya utakatifu kiasi gani kwa ajili ya utukufu wa **Mungu tutaishi**; na kwa heshima ya thawabu, ni tofauti gani ya wazi ingeonekana kati yetu na dunia. **— Manuscript 39, 1893.{EVsw 220:4}**

Uwekwe Mbele ya Watu Kila Wakati — Ukweli kwamba Kristo anakuja unapaswa kuwekwa mbele ya akili ya kila mmoja. —**Letter 131, 1900. {EVsw 220:5}**

Onyo Dhidi ya Kuweka Majira Mahsusi — Majira na nyakati **Mungu** ameyaweka katika mamlaka Yake Mwenyewe. Kwa nini **Mungu** hakutupa maarifa haya? — Kwa sababu hatungeyatumia kwa njia sahihi hata kama tungepewa. Hali fulani ingejitokeza miongoni mwa watu wetu ambayo ingekwamisha kazi ya **Mungu** katika kuwaandaa watu kusimama siku ile kuu inayokuja. Hatupaswi kujihenyesha na dhana au uvumi kuhusu majira ambayo **Mungu** hajayafunua. Yesu aliwaambia wanafunzi Wake "kukesha," lakini si kwa ajili ya wakati maalum. Wafuasi Wake wanapaswa kuwa katika hali ya kusikiliza maagizo ya Kamanda wao; wanapaswa kukesha, kungoja, kuomba na kufanya kazi wanapokaribia wakati wa kurudi kwa Bwana; lakini hakuna mtu atakayekuwa na uwezo wa kusema ni lini hasa wakati huo utafika; kwa kuwa "hakuna mtu

ajuaye siku wala saa." Huwezi kusema atakuja baada ya mwaka mmoja, miwili, au mitano, wala hupaswi kusema kwamba hatakuja hadi baada ya miaka kumi au ishirini..... Hatupaswi kujua wakati maalum wa kumiminwa kwa Roho Mtakatifu wala kurudi kwa Kristo. —**Review and Herald, March 22, 1892.** {EVsw 221:1}

Kweli ya Patakatifu

Msingi wa Imani Yetu

Ufahamu sahihi wa huduma katika Patakatifu pa mbinguni ndio msingi wa imani yetu. — **Letter 208, 1906.**{EVsw 221:2}

Kitovu cha Kazi ya Upatanisho wa Kristo

Somo la Patakatifu na hukumu ya upelelezi linapaswa kueleweka kwa uwazi na watu wa **Mungu**. Kila mtu anahitaji kuwa na maarifa binafsi kuhusu nafasi na kazi ya Kuhani wetu Mkuu. La sivyo, haitakuwa rahisi kwao kuwa na imani inayohitajika wakati huu, wala kuchukua nafasi ambayo **Mungu** amewakusudia kuwa nayo. Kila mtu ana nafsi ya kuokolewa au kupotea. Kila mmoja ana kesi inayosubiriwa mbele ya kiti cha hukumu cha **Mungu**. Kila mtu atalazimika kukutana na Hakimu Mkuu uso kwa uso. hivyo jambo hili ni la muhimu sana kiasi gani,kwamba kila mtu anapaswa kulifikiri mara kwa mara, naam, tukio hilo la hukumu, wakati vitabu vitakapofunguliwa, na, kama kitabu cha Danieli kinavyosema, kila mmoja atasimama mahali pake mwishoni mwa siku.{EVsw 221:3}

Wote waliopokea nuru kuhusu mambo haya wanapaswa kutoa ushuhuda juu ya Kweli kuu ambazo **Mungu** amewapa. Patakatifu pa mbinguni ndilo kitovu hasa cha kazi ya Kristo kwa ajili ya wanadamu. Linamhusu kila nafsi inayoishi duniani. Hufunua mpango wa ukombozi, na hutufikisha hadi mwisho wa wakati, likidhihirisha ushindi wa haki dhidi ya dhambi. Ni muhimu sana kwamba wote wachunguze kwa kina masomo haya, na wawe tayari kutoa jibu kwa yeyote atakayewauliza sababu ya tumaini walilo nalo. — **The Great Controversy, uk. 488, 489 (1888).**{EVsw 222:1}

Ufunguo wa Mfumo Kamili wa Kweli

Somo la Patakatifu ndio ufunguoulilofungua fumbo la kukata tamaa lililotokea mwaka 1844. Lilifungua mtazamo wa mfumo kamili wa Kweli, uliounganishwa na wa upatanifu, ukionyesha kuwa mkono wa **Mungu** uliongoza harakati kuu ya Kurudi kwa Yesu, na kufunua wajibu wa sasa kwa kuonyesha nafasi na kazi ya watu Wake. — **The Great Controversy, uk. 423 (1888).**{EVsw 222:{EVsw 222:2}

Macho Yatazame Patakatifu

Kama watu wa **Mungu**, tunapaswa kuwa wanafunzi makini wa unabii; tusipumzike hadi tuwe na uelewa wa somo la Patakatifu, kama linavyoonyeshwa katika maono ya Danieli na Yohana. Somo hili linaleta mwanga mkuu juu ya nafasi yetu ya sasa na kazi yetu, na linatupatia ushahidi usiopingika kwamba **Mungu** ametuongoza katika uzoefu wetu wa nyuma. Linaeleza kwa nini tulivunjika moyo mwaka 1844, likituonyesha kwamba Patakatifu palipotakiwa kutakaswa si dunia, kama tulivyodhani, bali ni kwamba Kristo aliingia katika sehemu ya ndani ya Patakatifu pa mbinguni, na huko anafanya kazi ya mwisho ya huduma Yake ya kikuhani, kutimiza maneno ya malaika kwa nabii Danieli: "Hata nyakati elfu mbili na mia tatu; ndipo Patakatifu patatakaswa **(Daniel 8:14).**" {EVsw 222:3}

Imani yetu kuhusu ujumbe wa malaika wa kwanza, wa pili, na wa tatu ilikuwa sahihi. Alama kuu tulizopita ni thabiti. Ingawa majeshi ya kuzimu yatajaribu kuziporomosha kutoka kwenye msingi wake, na kushangilia kuwa wamefanikiwa, bado hawakufaulu. Nguzo hizi za Kweli zimesimama imara kama milima ya milele, nazo hazitikiswi na juhudi zote za wanadamu au shetani. Tunayo mengi ya kujifunza, na tunapaswa daima kuchunguza Maandiko ili kuthibitisha kama mambo haya ni Kweli. Watu wa **Mungu** sasa wanapaswa kuelekeza macho yao kwenye Patakatifu pa mbinguni, ambako huduma ya mwisho ya Kuhani wetu Mkuu katika kazi ya hukumu inaendelea—ambako anaombea watu Wake. — **Review and Herald, November 27, 1883.**{EVsw 223:1}

Kweli Kuu Katika Mafundisho Rahisi ya Theolojia

Katika kila shule inayosimikwa, mafundisho ya theolojia yaliyo rahisi kabisa yapaswa kufundishwa. Katika mafundisho hayo, upatanisho wa Kristo unapaswa kuwa kiini kikuu, Kitovu cha Kweli. Somo la ajabu la ukombozi linapaswa kuwasilishwa kwa wanafunzi. — **Manuscript 156, 1898.**{EVsw 223:2}

Uzito wa Kweli ya Patakatifu

Wakati Kristo anapotakasa Patakatifu, waabudu walioko duniani wanapaswa kujitathmini kwa makini, na kulinganisha tabia yao na kiwango cha haki. — **Review and Herald, April 8, 1890.** {EVsw 224:1}

Mahubiri ya Mafundisho ya Patakatifu Yameidhinishwa na Roho Mtakatifu

Kwa zaidi ya nusu karne, vipengele mbalimbali vya Kweli ya sasa vimehojiwa na kupingwa. Nadharia mpya zimewasilishwa kana kwamba ni kweli, kumbe sio kweli, na Roho wa **Mungu** amefunua makosa yake. Wakati nguzo kuu za imani yetu zimewasilishwa, Roho Mtakatifu amekuwa akizishuhudia, hasa kuhusu Ukweli wa somo la Patakatifu. Mara kwa mara Roho Mtakatifu amethibitisha kwa namna ya pekee mahubiri ya mafundisho haya. Lakini leo, kama ilivyokuwa zamani, baadhi wataongozwa kuunda nadharia mpya na kukana zile Kweli ambazo Roho wa **Mungu** amezipitisha. — **Manuscript 125, 1907.**{EVsw 224:2}

Nadharia za Uongo Kuhusu Patakatifu

Katika siku zijazo, udanganyifu wa kila aina utajitokeza, na tunahitaji msingi imara wa kusimamia. Tunahitaji nguzo dhabiti kwenye jengo. Hakuna hata sehemu ndogo ya Kweli inayopaswa kuondolewa kutoka kwa kile ambacho Bwana amekiweka. Adui ataleta nadharia za uongo, kama vile mafundisho kwamba hakuna Patakatifu. Hili ni moja ya maeneo ambayo itaonekana kugeuka kutoka kwenye imani. Tutaweza kupata usalama wapi kama si katika zile Kweli ambazo Bwana ametupatia kwa kipindi cha miaka hamsini iliyopita? — **Review and Herald, May 25, 1905.**{EVsw 224:3}

Mapambano Juu ya Kweli Tofauti

Wakati umekaribia ambapo nguvu za udanganyifu za Shetani zitadhihirishwa kikamilifu. Upande mmoja kuna Kristo, ambaye amepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Upande mwingine kuna Shetani, ambaye daima amekuwa akitumia nguvu zake kuwadanganya kwa mafundisho yenye kuvutia ya kiroho (spiritual sophistries), ili kumwondoa **Mungu** katika nafasi Yake Anayostahili katika akili za wanadamu.{EVsw 224:4}

Shetani hufanya kila juhudi kuingiza mawazo ya kubuni kuhusu Patakatifu, akipotosha maonyesho ya ajabu ya **Mungu** na huduma ya Kristo kwa ajili ya wokovu wetu kuwa kitu kinachopendeza akili ya tamaa za kimwili. Anaondoa mamlaka yake katika mioyo ya waumini, na badala yake huleta nadharia za ajabu zilizobuniwa ili kufuta zile Kweli za upatanisho na kuharibu imani yetu katika Mafundisho tuliyoyaheshimu tangu ujumbe wa malaika wa tatu ulipoanza kutolewa. Kwa njia hii, Shetani hutaka kutunyang'anya imani yetu katika ujumbe uliotufanya kuwa watu wa pekee, uliotupatia utambulisho na nguvu katika kazi yetu. — **Special Testimonies, Series B, Na. 7, uk. 17 (1905).**{EVsw 225:1}

Kuwasilisha Sheria na Sabato

Ujumbe Wetu Maalum — Bwana ana ujumbe maalum kwa wajumbe Wake kuuwasilisha. Wanapaswa kuonya watu, wakiwaita kurekebisha ufa uliosababishwa na Upapa katika sheria ya **Mungu**. Sabato imefanywa kuwa jambo lisilo na maana, amri isiyo ya lazima, ambayo mamlaka ya kianadamu inaweza kuiweka pembeni. Siku takatifu ya Bwana imebadilishwa kuwa siku ya kawaida ya kazi. Wanadamu wamebomoa kumbukumbu ya **Mungu**, na kuiweka siku bandia ya pumziko badala yake. — **Manuscript 35, 1900.** {EVsw 225:2}

Ujumbe wa Mwisho kwa Dunia — Ujumbe wa mwisho wa onyo kwa dunia ni kuwaongoza wanadamu kutambua umuhimu ambao **Mungu** ameuweka juu ya sheria Yake. Kweli inapaswa kuwasilishwa kwa uwazi kiasi kwamba hakuna mvunjaji wa sheria, atakayeisikia, atakayekuwa na udhuru kwa kushindwa kutambua umuhimu wa Utii kwa amri za **Mungu**. {EVsw 225:2}

Nimeagizwa kusema: Kusanyeni kutoka katika Maandiko, ushahidi kwamba **Mungu** aliitakasa siku ya saba, na ushahidi huu usomwe mbele ya mkutano. hebu waonyesheni wale ambao hawajasikia Kweli waonyeshwe kwamba kila mtu anayepuuza "Hivi Ndivyo Asema Bwana" kwa uwazi, lazima abebe matokeo ya njia hiyo. Katika kila kizazi, Sabato imekuwa kipimo cha uaminifu kwa **Mungu**. "Ni ishara kati Yangu na wana wa Israeli milele," Anatangaza Bwana. — **Gospel Workers, uk. 148, 149 (1915).**{EVsw 226:1}

Mada ya Kufanya Maamuzi kwa Dunia Yote — Nuru kuhusu madai ya sheria ya **Mungu** lazima iwasilishwe kila mahali. Hii ni mada ya kufanya maamuzi (itakayoamua). Mada hii itaijaribu na kuipima dunia. — **Special Testimonies, Series A, No. 7, uk. 17, 18 (1874).**{EVsw 226:2}

Kujenga Katika Maeneo Mapya — Nililazimika kuacha kuandika ili kuwa na mazungumzo na Ndugu _____. Yuko katika hali ya mkanganyiko...;;; Alitaka kujua namna ya kuwasilisha Kweli anapoingia kwenye maeneo mapya, na kama Sabato inapaswa kuwasilishwa kwanza. {EVsw 226:3}

Nilimwambia kuwa mpango bora na wenye hekima zaidi ni kuanza na mada zitakazoamsha dhamiri. Aweza kuzungumza nao kuhusu utauwa wa vitendo; ibada, kujitoa wakfu na uchaji; na kuwasilisha maisha ya kujinyima, kujikana nafsi na kujitoa dhabihu kwa Yesu kama mfano wetu hadi watakapoona utofauti katika maisha yao ya kujipenda, kujifurahisha, kujiendekeza na itawafanya kutoridhika na maisha yao yasiyo ya Kikristo.{EVsw 226:4}

Kisha wasilisha unabii kwao; awaonyeshe usafi na madai ya kudumu ya Neno la **Mungu**. Hakuna herufi ndogo wala nukta ya sheria hii itakayopoteza nguvu yake, bali itabaki na madai mashiko yake juu ya kila nafsi hadi mwisho wa wakati. Wakati sheria ya **Mungu** inapokanushwa, na kubatilishwa na wanadamu (kuwa batili); wakati ulimwengu wa Kikristo unapojiunga na wa Katoliki na wa kidunia katika kuzifanya amri za **Mungu** kuwa si kitu na hazina mashiko, basi watu wa **Mungu** walioteuliwa watainuka kuitetea sheria ya Yehova.{EVsw 226:5}

Huu ndio ujanja/werevu alioutumia Paulo; hii ndiyo hekima ya nyoka; na upole wa njiwa. Tunapofika katika jamii inayofahamu imani yetu, mkakati huu wa tahadhari hauhitajiki, lakini katika kila hali, juhudi za pekee zinapaswa kufanywa kufikia mioyo kwa jitihada za kibinafsi. Epuka kuwalaumu makanisa; usiwape watu wazo kwamba kazi yako ni kubomoa, bali kujenga, na kuwasilisha ile Kweli kama ilivyo katika Yesu. Zungumza kwa kina juu ya haja ya uchaji Mungu wa kweli. — **Letter 2, 1885.**{EVsw 227:1}

Kuanza Kuwasilisha Sabato Katika Maeneo Mapya

Ujumbe wa ile Kweli ni mpya na wa kushtua kwa watu wa nchi hii [Australia]. Mafundisho ya Biblia yanapowasilishwa ni kama ufunuo mpya, na kwa kweli wanayaona maoni yanayowasilishwa kana kwamba ni ukafiri (ukana-Mungu). Katika kuwasilisha suala la Jumapili, au muungano wa kanisa na serikali, lishughulikiwe kwa uangalifu. Haitakuwa sahihi kuwasilisha misimamo mikali ambayo imeshawasilishwa na ambayo italazimu kuwasilishwa Marekani.{EVsw 227:2}

Mada hizi zinapaswa kutangulizwa kwa tahadhari. Hatujapata nafasi imara katika nchi hii. Adui wa haki yote amekuwa akifanya kazi na bado anaendelea kwa kila ujanja anaoweza kubuni ili kuzuia kazi inayopaswa kufanyika katika kuwaelimisha watu; nguvu na majeshi yake yanaongezeka. Hali za uchelewesho zimekuwa zikimpa Shetani faida, na uchelewesho huu umepoteza nafsi nyingi. Bwana hafurahishwi na kucheleweshwa kwa kazi. Kila uchelewesho hufanya kazi inayopaswa kufanywa, kuwa ngumu zaidi, kwa sababu Shetani hupata fursa ya kutangulia na kuliteka eneo hilo mahalia, na kujiandaa kwa upinzani wa nguvu.{EVsw 227:3}

Harakati za polepole za watu wetu katika kuinua bendera katika miji mikubwa si sawa na nuru tuliyopewa na **Mungu**. Mwanga mdogo umeng'aa mijini, lakini wa kutosha tu kuwafanya wachungaji wa uongo waone kuwa ni wakati wao wa kuanza kazi ya kutoa hekaya za kubuni na uongo ili kuwazuia watu wasipokee ujumbe wa Kweli.{EVsw 228:3}

Juhudi ndogo zimefanywa, lakini watu na fedha havijatolewa vya kutosha ili kazi ifanyike. Shetani amefanya kazi, na ataendelea kufanya kazi kwa ishara za uongo na maajabu ya kudanganya, na udanganyifu mkuu utakubalika mahali ambapo bendera ya Kweli ilipaswa kuinuliwa.{EVsw 228:2}

Sasa kwa kuwa watu wa **Mungu** wanaojua kweli wameshindwa kutimiza wajibu wao kulingana na nuru iliyo katika Neno la **Mungu**, ni lazima tuwe waangalifu zaidi, tusije tukawaudhi wasioamini kabla hawajasikia sababu za imani yetu kuhusu Sabato na Jumapili.....{EVsw 228:1}

Kuna haja ya kuwapa watu mafundisho kwa uvumilivu na kwa upole; elimu ya maisha yote haiwezi kufutwa haraka; hekima kubwa na juhudi za subira zinahitajika kwa wale watakaowasilisha Kweli kwa njia yoyote ile. — **Manuscript 95, 1894.**{EVsw 228:4}

Kuahirisha Kuiwasilisha

Usihisi kuwa ni wajibu wako kuanza kwa hoja kuhusu Sabato kila unapoonana na watu. Kama watu wataanzisha mada hiyo, waambie kuwa hiyo siyo mzigo wako kwa sasa. Lakini watakaposalimisha mioyo na

akili na mapenzi yao kwa **Mungu**, ndipo watakapokuwa tayari kwa unyoofu kuzingatia ushahidi kuhusu kweli hizi za majaribio. — **Letter 77, 1895.**{EVsw 228:3}

Onyo Dhidi ya Kuchelewesha Kupita Kiasi

Tahadhari inapaswa kuchukuliwa; lakini ingawa baadhi ya watendakazi wanakuwa waangalifu, na hufanya mambo polepole kwa busara, ikiwa hawatashirikiana katika kazi hiyo na wale wanaotambua umuhimu wa kuwa wakakamavu, mengi yataharibika, nafasi nyingi zitapotea, na matendo ya wazi ya uongozi wa **Mungu** hayatatambuliwa. {EVsw 228:4}

Wakati watu walio chini ya msukumo hawaletwi kuchukua uamuzi mapema iwezekanavyo, kuna hatari kwamba msukumo huo utatoweka polepole.....{EVsw 229:1}

Mara nyingi, mkutano unapofikia hatua ambapo mioyo imeandaliwa kwa ajili ya suala la Sabato, huchelewesha kwa hofu ya athari zake. Hili limefanyika, na matokeo hayajakuwa mazuri. — **Letter 31, 1892.**{EVsw 229:2}

Katika Kampeni ya Muda Mfupi

Unapokuwa na mkutano wa watu kwa muda wa wiki mbili tu, usicheleweshe kuwasilisha suala la Sabato kwa kudhania hadi kila kitu kingine kiwe kimewasilishwa, na kwamba hivyo ndivyo unavyoandaa njia. Inueni bendera — amri za **Mungu**, na imani ya Yesu. Fanya hili kuwa somo kuu. Kisha, kwa hoja zako zenye nguvu, lisisitize zaidi. Zingatia sana Ufunuo. Soma, fafanua, na sisitiza mafundisho yake.{EVsw 229:3}

Vita vyetu ni vya kushambulia. Masuala makubwa yapo mbele yetu — ndiyo, yapo juu yetu sasa. Hebu sala zetu zipae kwa **Mungu** kwamba malaika wanne wazuie pepo nne zisije zikaumiza wala kuharibu hadi onyo la mwisho litakapowasilishwa kwa dunia. Kisha na tufanye kazi kwa ulinganifu na sala zetu. Usiruhusu chochote kupunguza nguvu ya Kweli ya wakati huu. Kweli ya sasa inapaswa kuwa mzigo wetu. Ujumbe wa malaika wa tatu lazima ufanye kazi yake ya kuwatenga kutoka katika makanisa watu watakaosimama juu ya msingi wa Kweli ya milele. — **Testimonies for the Church 6:61 (1900).**{EVsw 229:4}

Ujumbe wa Uzima au Kifo

Kama watu, tuko katika hatari ya kutoa ujumbe wa malaika wa tatu kwa namna isiyoeleweka kiasi kwamba hauwaathiri watu..... Ujumbe wetu ni wa uzima au kifo, na lazima tuwasilishe kama ulivyo — nguvu kuu ya **Mungu**. Kisha Bwana ataufanya kuwa na matokeo. Lazima tuuwasilishe kwa nguvu yake yote. — **Letter 209, 1899.**{EVsw 230:2}

Ujumbe Usifungwe

Shetani ametunga hali ambayo inafanya ujumbe wa malaika wa tatu ufungwe. Lazima tujihadhari dhidi ya mipango na mbinu zake. Hakuna kupunguza nguvu ya kweli, hakuna kufifisha ujumbe wa wakati huu. Ujumbe wa malaika wa tatu lazima uimarishwe na kuthibitishwa. Sura ya kumi na nane ya Ufunuo inafunua umuhimu wa kuwasilisha kweli kwa uwazi na ujasiri... Kumekuwa na mizunguko mingi mno katika kuwasilisha ujumbe wa malaika wa tatu. Ujumbe huu haujawasilishwa kwa uwazi na uwazi unaohitajika. — **Manuscript 16, 1900.** {EVsw 230:2}

Kama Kristo Alivyowasilisha Sheria

Kristo aliwasilisha kanuni za sheria ya **Mungu** kwa njia ya moja kwa moja na yenye nguvu, akiwaonyesha wasikilizaji Wake kuwa walikuwa wameshindwa kuzitekeleza kanuni hizo. Maneno yake yalikuwa ya wazi na makusudi kiasi kwamba wasikilizaji Wake hawakupata nafasi ya kubishana au kupinga. — **The Review and Herald, September 13, 1906.**{EVsw 230:3}

Paulo Alibadilisha Mbinu Zake

Kwa watu wa Mataifa, [Paulo] aliwahubiria Kristo kama tumaini lao pekee la wokovu, lakini hakuwa na jambo mahsusi la kusema kuhusu sheria mwanzoni. Lakini baada ya mioyo yao kupashwa moto na uwasilishaji wa Kristo kama kipawa cha **Mungu** kwa dunia, na kuelewa maana ya kazi ya Mkombozi katika dhabihu yake ya gharama ili kufunua upendo wa **Mungu** kwa wanadamu, kwa unyenyekevu wa hali ya juu

aliwaonyesha upendo wa **Mungu** kwa watu wote — Wayahudi na Mataifa — kwamba waweze kuokolewa kwa kuisalimu mioyo yao Kwake. Hivyo basi, walipopata kuyeyuka na kunyenyekea, na kujitoa kwa Bwana, ndipo alipowasilisha sheria ya **Mungu** kama kipimo cha utii wao. Hii ndiyo ilikuwa mbinu yake ya kazi — kubadilisha njia kulingana na lengo la kuokoa roho. **— Special Testimonies, Series A, No. 6, uk. 55 (1895).** {EVsw 230:4}

Kwanza Mafundisho ya Msingi

Usiziweke wazi sifa hizo za ujumbe ambazo ni kushutumu mila na desturi za watu, hadi wapate fursa ya kujua kwamba sisi ni waumini katika Kristo, kwamba tunaamini katika Uungu Wake na katika kuwepo Kwake kabla. Acha ushuhuda wa Mkombozi wa ulimwengu ukaliwe juu yake. — **Testimonies for the Church 6:58 (1900).** {EVsw 231:1}

Tunaihubiri Injili

Acheni watu wa nje waelewe kuwa sisi tunahubiri Injili pamoja na sheria, nao watafurahia kweli hizi, na wengi watachukua msimamo kwa ajili ya kweli. — **Letter 1, 1889.**{EVsw 231:2}

Itamsadikisha Mtu Dhambi

Sheria na Injili, kama zilivyofunuliwa katika Neno la **Mungu**, zinapaswa kuhubiriwa kwa watu; kwa maana sheria na Injili vikichangamana, vitawahakikishia watu kuhusu dhambi. Sheria ya **Mungu**, inapokemea dhambi, huonyesha Injili, ikimfunua Yesu Kristo, ambaye ndani yake "unakaa utimilifu wote wa **Mungu** katika mwili." Utukufu wa Injili hutia nuru enzi ya Kiyahudi, na kutoa maana kwa mfumo mzima wa mifano na vivuli vya Kiyahudi. Hivyo basi, sheria na Injili vinachangamana. Katika kila mahubiri, havipaswi kutenganishwa. — **Manuscript 21, 1891.**{EVsw 231:3}

Kwa upande mmoja, watu wa dini wengi wamezitenganisha sheria na Injili; kwa upande mwingine, sisi nasi kwa kiasi fulani tumefanya hivyo hivyo kwa mtazamo mwingine. Hatukuweka wazi mbele ya watu haki ya Kristo na maana kamili ya mpango Wake mkuu wa ukombozi. Tumemwacha Kristo na upendo Wake usio na kifani, na kuleta nadharia, busara na hoja, tukihubiri mabishano tu. — **Manuscript 24, 1890.** {EVsw 231:4}

Sheria na Injili Huenda Pamoja-Sambamba

Ikiwa tunataka kuwa na roho na nguvu ya ujumbe wa malaika wa tatu, lazima tuwasilishe sheria na Injili pamoja, kwa sababu hizi huenda pamoja. — **Gospel Workers, uk. 161 (1915).**{EVsw 232:1}

Imarisheni Ujumbe Kupitia Machapisho

Siku tunazoishi ni nyakati zinazohitaji uangalifu wa kudumu, nyakati ambazo watu wa **Mungu** wanapaswa kuwa macho kutekeleza kazi kubwa ya kuwasilisha nuru kuhusu suala la Sabato... Onyo hili la mwisho kwa wakazi wa dunia ni kuonyesha watu umuhimu ambao **Mungu** ameuweka juu ya sheria Yake takatifu. Ukweli huu uwasilishwe kwa uwazi kiasi kwamba mkosaji yeyote anayesikia asishindwe kutambua umuhimu wa kutii amri ya Sabato.....{EVsw 232:2}

Kazi ipo kwa kila mmoja wetu kuhakikisha kweli rahisi za Neno la **Mungu** zinajulikana. Maneno ya Maandiko yanapaswa kuchapishwa jinsi yalivyo. Ingependeza kama sura ya kumi na tisa na sehemu kubwa ya sura ya ishirini ya kutoka, pamoja na mistari ya kumi na mbili hadi kumi na nane ya sura ya thelathini na moja, zingechapishwa kama zilivyo. Kusanyeni na kuzijaza Kweli hizi katika vijitabu vidogo na vijitabu, na mwache Neno la **Mungu** lizungumza na watu. Mahubiri yanayogusia sheria ya **Mungu** na kuwa wazi, yachapishwe katika vijitabu iwapo kuna njia ya kufanya hivyo. Kisha, wale wanaotetea sheria za Jumapili wakikutana nanyi, wapeni vijitabu hivyo mikononi mwao. Waambieni kuwa hamjadili suala la Jumapili kwa kuwa mna "Hivi Ndivyo Asemavyo Bwana" wazi kabisa kuhusu kutunza siku ya saba. —**The Review and Herald, March 26, 1908.**{EVsw 232:3}

Onyesheni Alama ya Kutofautisha kwa Wazi

Tunapaswa kuonyesha ulimwengu kanuni safi, tukufu, takatifu zitakazowatofautisha watu wa **Mungu** na watu wa dunia. Badala ya watu wa **Mungu** kufanana zaidi na wale wasiotunza Sabato ya siku ya saba, wanapaswa kuifanya Sabato kuwa ya wazi kiasi kwamba ulimwengu usishindwe kuwatambua kuwa ni Waadventista wa Sabato. —**Manuscript 162, 1903.**{EVsw 233:1}

Tumepewa Wito Kumfunua Mtu wa Dhambi (1Wathesalonike 2)

Katika wakati huu tunaouishi, Bwana amewaita watu Wake na kuwapa ujumbe wa kuufikisha. Amewaita wafunue uovu wa mtu wa dhambi aliyeifanya sheria ya Jumapili kuwa alama yake maalum, aliyedhani kubadili majira na sheria, na kutesa watu wa **Mungu** wanaoshikilia kwa uthabiti heshima ya **Mungu** kwa kuitunza Sabato ya pekee na Kweli ya uumbaji kama takatifu kwa Bwana (1Wathesalonike 2). —**Testimonies to Ministers and Gospel Workers, 118 (1903).**{EVsw 233:2}

Watu wa Pekee Wenye Ujumbe wa Kuwaangusha

Bwana amependezwa kuwapa watu Wake ujumbe wa malaika wa tatu kama ujumbe wa kujaribu mioyo ya watu duniani. Yohana aliona watu waliotengwa na dunia, wanaokataa kumwabudu mnyama au sanamu yake, bali wanashika alama ya **Mungu** kwa kuitunza Sabato Yake takatifu—siku ya saba kuwa kumbukumbu ya **Mungu** aliye hai, Muumba wa mbingu na dunia. Kuhusu hawa mtume anaandika: "Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za **Mungu** na imani ya Yesu."—**Letter 98, 1900.** {EVsw 233:3}

Alama ya Mnyama (Mark of the beast)

Wakati utakapofika ambapo utunzaji wa Jumapili utalazimishwa kisheria, na dunia itakuwa imepewa nuru kuhusu wajibu wa kuitunza Sabato ya Kweli, basi yeyote atakayeendelea kuivunja amri ya **Mungu** kwa kutii amri ***isiyo na mamlaka yoyote ya juu zaidi kuliko ya Rumi***, atakuwa anaupa heshima upapa kuliko **Mungu**. Atakuwa anatoa ibada kwa Rumi na mamlaka inayoendeleza taasisi iliyoanzishwa na Rumi. Atakuwa anamwabudu mnyama na sanamu yake. Watu wanapokataa taasisi ambayo **Mungu** ameitangaza kuwa ishara ya mamlaka Yake na kumpa heshima, na badala yake kuikubali ile iliyochaguliwa na Rumi kama ishara ya ukuu wake, basi wanakuwa wamekubali alama ya utii kwa Rumi—"alama ya mnyama." Hili halitafanyika mpaka jambo hili litakapowekwa wazi kabisa mbele ya watu, na wakaletwa kuchagua kati ya amri za **Mungu** na zile za wanadamu, ndipo wanadamu watakaoendelea kuvunja amri za **Mungu** watapokea "alama ya mnyama."—**The Great Controversy, 449 (1888).**{EVsw 233:4}

Kupokea Alama ya Mnyama ni Jambo la Wakati Ujao

Mabadiliko ya Sabato ni alama au muhuri wa mamlaka ya kanisa la Kirumi. Wale ambao, wakielewa madai ya amri ya nne, wanachagua kuitunza sabato ya uongo badala ya ile ya Kweli, wanampa heshima Yule Mwenye mamlaka pekee ya kuamuru hivyo. Alama ya mnyama ni sabato ya Kipapa, ambayo dunia imeikubali badala ya siku iliyowekwa na **Mungu**. Bado, hakuna aliyepokea alama ya mnyama sasa (Iliandikwa kabla ya 1900). Wakati wa jaribio bado haujafika. Kuna WaKristo wakweli naam, dhati katika kila kanisa, hata katika lile la Katoliki. {EVsw 234:1}

Hakuna anayehukumiwa hadi atakapopokea nuru na kuona wajibu wa kuitunza amri ya nne. Lakini siku itakapokuja ambapo amri itatolewa ya kuwalazimisha watu kuitunza sabato bandia, na sauti kuu ya malaika wa tatu itawaonya watu dhidi ya kuabudu mnyama na sanamu yake, basi mstari utawekwa wazi kati ya Kweli na uongo. Wale watakaoendelea katika uasi watapokea alama ya mnyama. {EVsw 234:2}

Kwa kasi kubwa tunakaribia kipindi hicho. Wakati makanisa ya Kipentekoste yatakapoungana na mamlaka ya serikali kuiendeleza/kuitegemeza dini ya uongo—dini waliyoipinga kwa nguvu babu zao waliopitia mateso makali—basi sabato ya Kipapa italazimishwa kwa mamlaka ya pamoja ya kanisa na serikali. Kutakuwa na uasi wa kitaifa utakaoishia tu kwenye uharibifu wa kitaifa. —**Manuscript 51, 1899.**{EVsw 235:1}

Wakati Muhuri wa Mungu Unakataliwa

Ikiwa nuru ya Kweli imewasilishwa kwako, ikikuonyesha Sabato ya amri ya nne, na kukufahamisha kwamba hakuna msingi wowote katika Neno la **Mungu** unaounga mkono utunzaji wa Jumapili, na bado wewe unashikilia sabato ya uongo, ukikataa kuitunza Sabato ambayo **Mungu** ameita "siku Yangu takatifu," basi unapokea alama ya mnyama. Je, hili linatokea lini? Linatokea pale unapotiii amri inayokuamuru kuacha kufanya kazi siku ya Jumapili na kumwabudu **Mungu**, huku **ukijua hakuna Andiko lolote** katika Biblia linaloonyesha kwamba Jumapili ni siku ya kuabudu zaidi ya siku ya kawaida ya kazi. Kwa kufanya hivyo, unakubali kupokea alama ya mnyama na kukataa muhuri wa **Mungu**. —**The Review and Herald, July 13, 1897.**{EVsw 235:2}

Matokeo ya Kupuuza Nuru

Mungu amewapa wanadamu Sabato kama ishara kati Yake na wao, kama jaribio la uaminifu wao. Wale ambao, baada ya kupata nuru kuhusu sheria ya **Mungu**, wataendelea kutotii na kuinua sheria za wanadamu juu ya sheria ya **Mungu** katika kipindi kikuu cha majaribu kilicho mbele yetu, hao watapokea alama ya mnyama. —**Letter 98, 1900**. **{EVsw 235:3}**

Kuwa na Busara Katika Kuliwasilisha Suala la Jumapili

[Hatupaswi] kuwakera wale waliokubali sabato hii bandia, taasisi ya Kipapa iliyowekwa badala ya Sabato takatifu ya **Mungu**. Kukosa kwao hoja ya mashiko kutoka katika Biblia kunawafanya wakasirike zaidi, na kutumia mbadala wa nguvu zinazotokana na nafasi waliyonayo, badala ya hoja. Mateso, kutumia nguvu kutesa watu ndizo hatua za joka. Kwa hiyo, ni muhimu sana kuwa waangalifu sana na kuepuka kuchochea migogoro. —**Letter 55, 1886. {EVsw 235:4}**

Acha Ukweli Ndio Uamue au Ukate-kate

Juhudi za Shetani dhidi ya watetezi wa Ukweli zitazidi kuwa chungu na thabiti hadi mwisho wa wakati. Kama ilivyokuwa katika siku za Kristo, ambapo wakuu wa makuhani na watawala walichochea watu dhidi Yake, vivyo hivyo leo viongozi wa dini watachochea chuki na upendeleo dhidi ya Kweli ya wakati huu. Watu watachukuliwa kufanya matendo ya vurugu, ukatili na upinzani ambayo wasingeyafanya kamwe kama wasingechochewa na uhasama wa wale wanaodai kuwa WaKristo dhidi ya Ukweli. **{EVsw 236:1}**

Na ni njia gani watetezi wa Kweli wanapaswa kufuata? Wana Neno la **Mungu** lisilobadilika, la milele, na wanapaswa kuonyesha kwamba wana Ukweli kama ulivyo katika Yesu. Maneno yao hayapaswi kuwa makali, yasiyo na upatanifu au ya kukera. Katika kuwasilisha Ukweli wanapaswa kudhihirisha upendo, unyenyekevu, na upole wa Kristo. Acha Ukweli wenyewe ndio uamue au ukate; Neno la **Mungu** ni kama upanga mkali, wenye makali kuwili, nao utajipenyeza hadi mioyoni. Wale wanaojua kuwa wana Ukweli hawapaswi, kwa kutumia maneno ya ukali au ujeuri, kumpa Shetani nafasi ya kupotosha nia yao. —**The Review and Herald, Oktober 14, 1902.{EVsw 236:2}**

Wito wa Kuuangazia Umma

Nimeonyeshwa kuwa Shetani anatupita kwa hila. Sheria ya **Mungu**, kupitia kazi ya Shetani, itatupiliwa mbali (itakanushwa). Katika nchi yetu inayojivunia uhuru, uhuru wa kidini utafikia mwisho wake. Mgogoro mkubwa utaamuliwa kupitia suala la Sabato, na jambo hili litautikisa ulimwengu mzima.**{EVsw 236:3}**

Muda wetu wa kufanya kazi ni mfupi, na **Mungu** anatuita sisi kama wachungaji na waumini kuwa tayari kila wakati. Walimu wenye busara kama nyoka na wapole kama hua lazima wajiunge katika kazi ya Bwana, ili kumsaidia Bwana dhidi ya wenye nguvu. Kuna wengi hawajui unabii unaohusiana na siku hizi, nao lazima waangaziwe. —**Letter 1, 1875.{EVsw 237:1}**

Kukabiliana na Changamoto za Kutunza Sabato

Hakuna Sababu ya Kuogopa au Kuhangaika

Mara nyingi wahudumu wetu wanapowasilisha Kweli ya Sabato inayojaribu mioyo ya watu, wengine husita kwa kuogopa kujiingiza kwenye umasikini na mashaka kwao na familia zao. Husema, "Ndiyo, naelewa unachojaribu kunionyesha kuhusu kuitunza Sabato ya siku ya saba; lakini naogopa nikitunza Sabato nitapoteza kazi yangu, na sitaweza kutunza familia yangu." Kwa hiyo, wengi huamua kuendelea kushikilia nafasi zao za kidunia na kumwasi **Mungu**. Lakini Maandiko haya **(Luka 12:1-7)** hutufundisha kuwa Bwana anajua vyema hali zetu, na uzoefu pia; Yeye anaelewa magumu na masumbufu yetu, Naye hujali wale wote wanaomfuata kwa uaminifu. Yeye Hatawahi kuruhusu watoto Wake kujaribiwa kupita uwezo wao. **{EVsw 237:2}**

Kristo aliwaambia wanafunzi Wake: "**Mathayo 6:25**, ***Luke 12:22-26 Akawaambia wanafunzi Wake, Kwa sababu hiyo nawaambia, Msisumbukie maisha yenu, mtakula nini; wala miili yenu, mtavaa nini. Kwa kuwa maisha ni zaidi ya chakula, na mwili ni zaidi ya mavazi. Watafakarini kunguru, ya kwamba hawapandi wala hawavuni; hawana ghala wala uchaga, na Mungu huwalisha. Bora ninyi mara nyingi kuliko ndege! Na yupi kwenu ambaye akijisumbua aweza kujiongeza kimo chake hata mkono mmoja? Basi, ikiwa hamwezi hata neno lililo dogo, kwa nini kujisumbua kwa ajili ya yale mengine? {EVsw 237:3}***

Kisha akayageukia maua ya kondeni: “Luke 12:27-31.

*Yatafakarini maua jinsi yameavyo; hayatendi kazi wala hayasokoti; Nami nawaambia ya kwamba hata Sulemani katika fahari yake yote hakuvikwa vizuri kama mojawapo la hayo. Basi, ikiwa Mungu huvika hivi majani ya kondeni, yaliyopo leo na kesho hutupwa kalibuni, je! Hatawatendea ninyi zaidi, enyi wa imani haba?**{EVsw 238:1}***

*Ninyi msitafute mtakavyokula wala mtakavyokunywa; wala msifanye wasiwasi, kwa maana, hayo yote ndiyo watafutayo mataifa ya duniani, lakini Baba yenu anajua ya kuwa mna haja na hayo. Bali utafuteni ufalme wa Mungu, na hayo mtazidishiwa.” **{EVsw 238:2}***

Mafundisho ya Kristo Kuhusu Kumtumikia Mungu

Kristo anafundisha somo la thamani kuhusu utumishi Wake. Yoyote yale yatakayokukuta, anasema, mtumikie **Mungu**. Licha ya magumu au mateso utakayokutana nayo, mtumainie Bwana. Hatuna sababu ya kuogopa au kuhangaika tukichukua msimamo kwa ajili ya Kweli. Kuwa na woga kwamba wewe au familia yako mtateseka, ni ishara ya kutokuamini. Mwokozi anasema, “Baba yenu anajua ya kuwa mnahitaji vitu hivi.” Tukijifunza Neno la **Mungu** kwa uadilifu na bidii, imani yetu itaongezeka. — **Manuscript 83, 1909. {EVsw 238:3}**

Wakati wa Kutoa Mkono wa Msaada

Ni wakati muhimu sana sasa kwa maeneo ambako watu wameamshwa kiroho na sasa wana shauku. Wengi wapo kwenye bonde la maamuzi. Ewe kwamba Bwana atawapa watumishi Wake hekima kusema maneno ya kuwapa ujasiri wale wanaosita, ili wakiri Kweli na kuitoa mioyo yao kikamilifu kwa **Mungu**.

Tunaomba Bwana awaguse moyo wale ambao wameona kwamba Sabato ya siku ya saba ni ya Bwana, wasikubali uongo wa adui kwamba sadaka ya kuitii ni kubwa mno. ***{EVsw 238:4}***

Ni kweli watakumbana na hasara ya kidunia, na mkono wa msaada hautakiwi kukosekana. Wengi huuliza, “Tutawezaje kuzitegemeza familia zetu? Tutapoteza kazi mara tu tutakaposema kuwa hatufanyi kazi siku ya Sabato. Je, familia zetu zitakufa njaa?” Je, tuseme nini sisi. Hatujui nini cha kusema. Umasikini na uhitaji vipo kila mahali. Watu waaminifu hawajui la kufanya. Hawawezi kuthubutu kuchukua hatua, ingawa mioyoni mwao wamehakikishiwa kuwa Sabato ya siku ya saba ndiyo siku ya Bwana. Wanajua **Mungu** aliibariki siku hiyo na kuitenga kwa ajili ya mwanadamu kama ukumbusho wa kazi ya uumbaji Wake. ***{EVsw 239:1}***

Tunaumia mioyoni tunapoona milima ya magumu wanayokutana nayo mbele, hatari ya njaa ya njaa na uhitaji kwao na kwa watoto wao ikiwakodolea macho. Mtu mmoja husema, “Nataka kuitunza Sabato, lakini pale tu nitakapomwambia mwajiri wangu, nitafukuzwa kazi.” Mamia wanasubiri kuchukua nafasi hiyo ya kazi niliyopewa. Tunapata uchungu na kusumbuliwa moyo. Tunachoweza ni kuwatia moyo wawe na imani na kuwaombea. Laiti ningekuwa na milioni moja, mara zingine mimi hufikiri ningeitumia kila dola kwa kazi hii.....***{EVsw 239:2}***

Wengi hujiunga na watenda dhambi kwa sababu ya mahusiano ya karibu na wale ambao ni vyombo vya Shetani. **Mungu** huwapa nuru, kuondoa uongo kwenye bongo zao, lakini wanakataa Neno la **Mungu** na kuamini uongo wa Shetani badala ya, “Hivi ndivyo Asema Bwana.”

> Watu hawa wanaoshabikia haya makosa, hufanya iwe vigumu sana kwa wale wanaoiona Kweli kuitii. Macho ya mwanadamu hayawezi kuona chochote ila njaa mbele ya wale wanaoishika Sabato.—Manuscript 19, 1894.
>
> . — **Manuscript 19, 1894.** ***{EVsw 239:3}***

Kumtumikia Mungu Hakusababishi Njaa

Hakuna mtu anayepaswa kuogopa kuwa kuitunza Sabato ya Kweli kutaishia kwenye njaa. [Isaya 58:11, 12; Mithali 7:2; Isaya 58:14]. Ahadi hizi zinatosha kujibu kila kisingizio cha kutokutii Sabato. Hata ikiwa hali itaonekana kuwa ni vigumu kutunza familia baada ya kuanza kuitunza amri za **Mungu**, hebu kila

mtu mwenye mashaka atambue kuwa **Mungu** ameahidi kuwahudumia wale wanaomtii. — **Manuscript 116, 1902.** *{EVsw 240:1}*

Inahitaji Ujasiri wa Maadili

Inahitaji ujasiri wa kiadili kuchukua msimamo wa kutunza amri za **Mungu**. Mtu mmoja aliyepinga Kweli alisema kuwa ni watu wasio na akili, wajinga, au wasioelimika ndio huacha makanisa na kuanza kutunza Sabato ya siku ya saba -Jumamosi. Lakini mhubiri mmoja aliyepokea Kweli alimjibu, "Kama unafikiri ni watu dhaifu wa akili wanaotii, basi jaribu mwenyewe." Inahitaji ujasiri wa maadili, uthabiti, uamuzi, uvumilivu, na maombi mengi kuchukua msimamo upande usio na wafuasi wengi, upande usiopendwa na usio mashuhuri. *{EVsw 240:2}*

Umechukua msimamo wa Kweli, hujakanyaga chini sheria ya **Mungu**. Je, Mwokozi atakuacha kweli upambane peke yako? La, kamwe. Lakini Kristo hakuwaambia wanafunzi Wake kuwa hawatakuwa na majaribu, wala hawatatoa sadaka. Alikuwa mtu wa huzuni na aliyefahamu mateso. "Mnajua neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, ya kuwa alipokuwa tajiri, kwa ajili yenu alifanywa maskini, ili kwa umasikini wake mpate kuwa matajiri." Tunamshukuru **Mungu** kuwa hata katika umasikini wako, unaweza kumwita **Mungu** Baba. — **Manuscript 37, 1894.** *{EVsw 240:3}*

Umaskini unakuja juu ya ulimwengu huu, na kutakuwa na wakati wa taabu ambao haujawahi kutokea tangu lilipoanza taifa. Kutakuwa na vita na matetesi ya vita, na nyuso za wanadamu zitabadilika rangi. Huenda ukalazimika kupata dhiki; unaweza kuwa na njaa wakati mwingine; lakini Mungu hatakuacha wewe katika mateso yako. Yeye Atajaribu imani yako. Hatupaswi kuishi ili kujifurahisha wenyewe. Tuko hapa duniani kumdhihirisha Kristo kwa ulimwengu, kumwakilisha Yeye na nguvu Zake kwa wanadamu.—Manuscript 37, 1894. {EVsw 240:4}

Wakati wa Kulitegemea Neno la Mungu

Wakiwa jangwani, **Mungu** aliwapa watu Wake mana kutoka mbinguni walipokosa chakula, ili kuwafundisha kuwa ikiwa watamtegemea Yeye, hatawaacha. Yesu alitii somo hilo. Kwa Neno la **Mungu**, msaada ulitolewa kwa Waisraeli, na kwa Neno hilo hilo ungeweza kutolewa kwa Yesu. Hakutafuta msaada kwa njia ya Shetani, bali alingoja wakati wa **Mungu**. Alithibitisha mbele ya ulimwengu kuwa ni bora kuteseka kuliko kuasi mapenzi ya **Mungu**.

"*Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha **Mungu**.*"— **The Desire of Ages, uk. 121 (1898).** *{EVsw 241:1*

"Mara nyingi mfuasi wa Kristo huletwa mahali ambapo hawezi kumtumikia Mungu na kuendeleza shughuli zake za kidunia.

Labda inaonekana kwamba utii kwa mahitaji au matakwa fulani ya wazi ya Mungu yatakatiza njia yake ya kujikimu kimaisha. Shetani angemfanya aamini kwamba lazima aache imani yake ya dhamiri. Lakini kitu pekee katika ulimwengu wetu ambacho tunaweza kutegemea, ni Neno la Mungu. "Tafuteni kwanza ufalme wa Mungu, na haki Yake; na hayo yote mtazidishiwa." Hata katika maisha haiwi kwa faida yetu kuyaacha mapenzi ya Baba yetu aliye mbinguni. Tunapojifunza nguvu ya Neno Lake Bwana, hatutafuata mapendekezo ya Shetani ili kupata chakula au kuokoa maisha yetu. Maswali yetu pekee yatakuwa, Je, Amri ya Mungu ni nini- au Neno linasemaje? na ahadi Yake ni nini? Tukijua haya, hakika tutatii moja, na kuiamini nyingine.—The Desire of Ages, 121 (1898). {EVsw 241:2}

Wito kwa Yule Aliyeko Katika Bonde la Maamuzi

Adui amekuwa akikushawishi kusubiri wakati unaofaa. Ameweka mbele yako faida utakazopata ikiwa hautatii Sabato, na hasara utazopata ukitii. Haya ni madanganyo ya Shetani. Umeamini uwongo wa Shetani kuhusu tabia ya **Mungu**. Ulifikiri ukifanikiwa kibiashara ndipo utatii Sabato. Lakini Mungu anahitaji utii

kamili. Umekuwa ukijaribu kufanya makubaliano na Mungu, lakini Shetani amekuwa akikufanya uone kwamba ni vigumu zaidi kufanya maamuzi. Mwitikio wako kwa Roho wa **Mungu** umepungua. **Mungu** amenipa ujumbe kwako na kwa watoto wako: timizeni wajibu wenu mlioacha kwa muda mrefu. "*Mpende Bwana **Mungu** wako kwa moyo wako wote.....*"*{EVsw 242:1}*

Umefikiria wakati fulani kuwa ni lazima upate mafanikio fulani katika biashara yako, ndipo ungeitii Sabato ya amri ya nne (Jumamosi). Lakini Bwana anataka kila mmoja wa raia Wake atii kikamilifu. Matakwa ya Mungu yalikuwa juu yako, na umekuwa ukifanya mjadala na Mungu. Na wakati wote Shetani amekuwa akifanya kazi moyoni mwako, ili iwe vigumu zaidi na zaidi kwako, unapoangalia jambo hilo la kuamua kuitunza Sabato. Athari ya ushawishi wa Mungu kwako imekuwa ikipungua, vivyo hivyo nguvu ya usadikisho ya Roho wa Mungu moyoni mwako. Bwana amenipa ujumbe kwa ajili yako na kwa watoto wako kubeba jukumu lako ulilolipuuzia kwa muda mrefu, kutembea katika nuru kama Yeye alivyo katika nuru. "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote." "Fanya hivi," Kristo alisema kwa wakili, "nawe utaishi." Hii ni sauti ya Mungu kwako mwenyewe leo na kwa watoto wako. Sheria ya Mungu ni njema na ya haki na yenye faida kwa wote wanaotii, nawe hakika utampa heshima Yeye unayemtii.*{EVsw 242:2}*

Akili yako inapopatana na mapenzi ya Mungu, katika kutii amri Zake, unafikiri kwamba Bwana hatakujali wewe na mambo yako ya kimwili? Ulikaribia kabisa kusadikishwa, ila hukutii. Ulidhani unapaswa kusubiri hadi njia itakaposafishwa mbele zako kabisa, ndiyo utii. Bwana amemwacha kila mwakilishi wa kianadamu awajibike binafsi kwa mwenendo wake. Madai ya Mungu yanapaswa kuwa kipaumbele chako cha kwanza kuzingatia. Utii kwa Mungu ndio wajibu wako wa kwanza. Unapaswa kuacha matokeo yote mikononi Mwake Yeye. Umekuwa ukisitasita kwa sababu sasa, umekuwa hutambui usadikisho mkali uliokuwa nao hapo awali, nawe hukukubali kujisalimisha na kuutii. Huna haja ya kutarajia usadikisho wa nguvu tena.Kazi yako sasa ni kufanyia kazi maamuzi kutoka kwa kanuni. Usitarajie kupata ule ushawishi wa kwanza, uliokuja kwako kwa nguvu.. *Utalazimika kumtii Mungu na kuchukua msimamo wako juu ya ile Kweli, iwe unahisi moyoni au la!* Kazi yako sasa ni kufanyia kazi maamuzi kutoka kwa kanuni. Lazima utii kwa msingi wa kanuni, bila kujali hisia zako wala matokeo yake. — **Letter 72, 1893.** *{EVsw 243:1}*

Ishi Kwa Nuru Yote Uliyopokea

Ishi kwa kila nuru uliyokwisha pokea. Maslahi yako ya milele yapo hatarini. Ndiyo maana nasema, "Thamini kila nuru." Piga magoti umwombe Kristo kugusa moyo wako kwa Roho Wake Mtakatifu, wala usiikatae sheria Yake. — **Manuscript 10, 1894.***{EVsw 243:2}*

Afadhali Kupoteza Kazi, Nafasi au Fursa Kuliko Yesu

Usidhani kwamba ukisimama kwa ajili ya Ukweli wa Biblia utapoteza kazi yako. Afadhali kupoteza kazi yako kuliko kumpoteza Yesu. Afadhali kushiriki katika kujinyima na kujitoa mhanga kama alivyofanya Bwana, kuliko kwenda njia yako mwenyewe ukitafuta kujikusanyia hazina za maisha haya. Huwezi kubeba chochote uendapo kaburini. Utaamka kutoka kaburini bila kitu chochote, lakini ukiwa na Yesu utakuwa na kila kitu. Yeye Ndiye yote unayohitaji ili kustahimili majaribu ya siku ya **Mungu** —Je,Yeye hatoshi kwako? — **Manuscript 20, 1894.** *{EVsw 243:3}*

Simama Imara

Watu wanaweza kuchochea upinzani kwa kiasi chochote watakavyo, lakini amri za **Mungu** bado ni amri za **Mungu tu**. Tumeamua kuzishika amri za **Mungu** ili tuishi, na kuihifadhi Sheria Yake kama mboni ya jicho letu. Watu waweza kulalamikia Sheria ya **Mungu** na kuwadharau/kuwakanyaga watu Wake wanaozishika amri Zake, lakini je, wanaweza kufanya hivyo na wakaendelea kuishi? Haiwezekani. **Mungu** ana kipimo Chake cha tabia, na ni wale wanaomtii ndio watakaoishi; wale wanaoshika Sheria Yake, ndiyo kama mboni ya jicho lake, hao ndio anaowahifadhi. — **Manuscript 5, 1891.** *{EVsw 244:1}*

Kuwapa Nafasi Washika Sabato

Miongoni mwa wale walioukubali Ukweli mahali fulani, katika majira ya baridi iliyopita, kulikuwa na kijana aliyekatisha masomo ili ashike Sabato. Alipoulizwa atafanya nini kujiendeleza kimaisha, alijibu: "**Mungu** amenipa nguvu za mwili, na nitafanya kazi ya aina yoyote ilimradi nisivunje amri Zake." Baadhi walihisi afadhali apewe kazi katika ofisi ya uchapishaji, lakini mtu mmoja akasema: "Hapana.

Atakapothibitisha kwamba yuko tayari kumtii **Mungu** kwa gharama yoyote, ndipo tutajua kuwa yeye ndiye mtu tunayemhitaji hapa. Lakini kama hana kanuni thabiti ya kufanya hivyo, basi yeye si yule mtu tunayemtaka." *{EVsw 244:2}*

Mzee--------alikuja kuniuliza kama ni vyema kumpa kijana huyo matumaini ya kuajiriwa ofisini. Nikamwambia: "**Mungu** wa mbinguni amemwekea mbele utukufu mzito wa milele unaowangojea washindi, na kama Musa, akiona thamani ya thawabu hiyo, atachukua msimamo thabiti kwa ajili ya Ukweli. Lakini haitakuwa na faida yoyote kumpa ahadi au motisha yoyote ya kidunia. Hata hivyo, wajibu wako ni kumsaidia aone kuwa anapaswa kuenenda kwa imani, nawewe usimwache apambane peke yake, kwa kuwa Shetani atamjaribu, na ni lazima umpe msaada wote kwa kadri uwezavyo." — **Manuscript 26, 1886.** *{EVsw 244:3}*

Ushirikiano wa Biashara na Wavunjaji wa Sabato

Kuna haja ya matengenezo ya utii wa Sabato miongoni mwetu tunaodai kuitunza siku takatifu ya pumziko ya **Mungu**. Wengine hujadili masuala ya biashara na kupanga mipango siku ya Sabato, na **Mungu** huona hili sawasawa tu na kufanya biashara yenyewe. *{EVsw 245:1}*

Wengine, japokuwa wanaelewa vyema ushahidi wa Biblia kuhusu Sabato ya siku ya saba, huingia ubia na watu wasioheshimu siku hiyo takatifu. Mshika Sabato hawezi kuruhusu watu wanaofanya kazi chini yake, kwa fedha au mshahara wake, kufanya kazi siku ya Sabato. Ikiwa kwa ajili ya faida ataruhusu biashara anayohusika nayo kuendelea siku ya Sabato kupitia kwa mshirika wake asiyeamini, basi anahesabiwa kuwa na hatia sawa na yule asiyeamini. Na ni wajibu wake kuvunja ushirikiano huo, hata kama atapata hasara kubwa. Watu wanaweza kudhani hawawezi kumtii **Mungu** kwa kuwa wataathirika kiuchumi, lakini kwa kweli hawawezi kumkataa **Mungu** bila madhara makubwa. Wale wasiokuwa waangalifu katika kuitunza Sabato watapata hasara kubwa. — **Review and Herald, March 18, 1884.** *{EVsw 245:2}*

Aina Moja ya Kazi kwa Wanaoshika Sabato

Hapa tunawakuta watu wa daraja bora sana wa kuwafikia. Na kwa wengi wao, haitakuwa vigumu kuitunza Sabato. Mahali fulani kuna ufugaji mwingi wa kuku. Karibu kila nyumba pembezoni mwa mji ina banda la kuku. Nyumba zimejengwa kwa kuachiana nafasi, na hakuna matuta, na mara nyingi huzungukwa na ekari kadhaa za ardhi. Aina mbalimbali za kuku hufugwa, na mayai huuzwa kwa wingi katika maeneo jirani kwani kuna soko huko-------, bidhaa hizi hupelekwa kwa mashua hadi mjini. *{EVsw 245:3}*

Ninaandika haya ili muwelewe mazingira. Katika ufugaji wa kuku, familia nyingi hupata riziki yao, na hawa hawawezi kutoa sababu kama za wengine kuwa kuitunza Sabato kungeathiri ajira zao. Wanaweza kuitunza Sabato bila hofu ya kupoteza kazi. — **Letter 113, 1902.***{EVsw 246:1}*

Kuhubiri Juu ya Kutokufa kwa Roho (Immortality of the Soul)

Chelewesha, na chukua tahadhari kutoa yale mafundisho yenye kuamsha chuki au upinzani; yasiyowapendeza watu au ya kuwakera.

Hekima kubwa inahitajika katika kuwasilisha Ukweli unaopingana moja kwa moja na maoni na desturi za watu. Mtindo wa Paulo ulikuwa wa kuanzia kwa kuzungumzia unabii kwa watu wa taifa la Kiyahudi, na akazungumza hatua kwa hatua, kisha baada ya muda kuanzisha mada ya Kristo kama Masihi wa Kweli. *{EVsw 246:1}*

Nimeonyeshwa kuwa wachungaji wetu hupita haraka sana katika mada zao na kuleta vipengele vingi vinavyokinzana na imani mapema mno katika mazungumzo yao. Kuna Kweli ambazo hazimpi mtu mshtuko mkubwa, na hizo zinapaswa kuendelea kuwa katika mawazo yao siku baada ya siku, hata wiki kabla ya kuanza kuzungumzia masuala ya Sabato na kutokufa kwa roho. Hivyo ndivyo unavyovuta imani ya watu, wakiona watu wenye hoja thabiti, na kufikiri kuwa unajua Biblia. Ukishapata imani yao, basi ndio wakati wa kuanzisha hadharani masuala ya Sabato na kutokufa kwa roho.*{EVsw 246:2}*

Lakini watu wasio na hekima huanzisha masuala haya mapema mno, na hivyo kufunga masikio ya watu, wakati wangetumia ujanja na hekima kidogo, wakati kama wangekuwa wamewapelekea watu hatua kwa hatua kupitia matukio muhimu ya unabii na kufundisha kwa njia za vitendo za Mafundisho Kristo. — **Letter 48, 1886.** *{EVsw 246:3}*

Moja ya Udanganyifu Mkubwa

Aina zote za udanganyifu sasa zinaingia ndani. Ukweli wa wazi kabisa wa Neno la **Mungu** umefunikwa na takataka za nadharia za kibinadamu. Makosa ya kufisha yanatolewa kama Ukweli ambao watu wote wanapaswa kuupokea na kuusujudia. Usahili wa utauwa wa kweli umefichwa chini ya mila na desturi za watu. *{EVsw 247:1}*

Fundisho la kutokufa kwa roho ni moja ya makosa ambayo adui anatumia kumdanganya binadamu. Makosa haya yako karibu kila mahali.....*{EVsw 247:2}*

Hili ni mmoja ya uongo uliozaliwa katika sinagogi ya adui, moja ya sumu za Babeli. "Nchi zote zimelewa na mvinyo wa hasira ya uasherati wake, na wafalme wa dunia wamefanya uasherati naye, na wafanyabiashara wa dunia wamekuwa matajiri kwa wingi wa vitu vyake vya starehe. Nami nilisikia sauti nyingine kutoka mbinguni ikisema, Tokeni kwake, watu Wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake." — **Review and Herald, March 16, 1897.** *{EVsw 247:3}*

Sisisiza Maisha Kupitia Yesu

Suala la kutokufa kwa roho linapaswa kushughulikiwa kwa makini sana, ili katika kuanzisha mada hiyo, usilipuke mjadala na mgogoro mkali utakaofunga mlango wa uchunguzi zaidi wa Ukweli.*{EVsw 247:4}*

Hekima kubwa inahitajika hata katika kutoa sababu ya tumaini tulilonalo....Je, ni Tumaini gani tunapaswa kutoa sababu yake? Tumaini la uzima wa milele kupitia Yesu Kristo.... wewe unazidi kuzingatia mafundisho maalum na nadharia, Mafundisho makuu na moyo wa asiyeamini haulainishwi. Kujaribu kumshawishi ni kujaribu kuwasha moto kwa kusugua chuma baridi.....*{EVsw 247:5}*

Tunaendelea kuhitaji hekima nyingi ya kujua wakati wa kuzungumza na wakati wa kunyamaza. Lakini daima kuna usalama kamili katika kuzungumza kuhusu tumaini la uzima wa milele. Na wakati moyo umeyeyuka na kutiishwa kwa upendo wa Yesu, basi swali litakuwa, "Bwana, nifanye nini ili nipate kuokolewa?" — **Letter 12, 1890.** *{EVsw 248:1}*

Hekima Inahitajika Katika Kuwasilisha Ukweli Mgumu Unaojaribu

Ukuaji wetu umekuwa wa polepole katika maeneo ambayo hayajafikiwa bado,, sababu ya Sabato ya siku ya saba. Kuna njia panda kali mbele ya kila roho inayokubali Ukweli.*{EVsw 248:2}*

Kuna Kweli zingine kama zile za kutokufa kwa roho na kuja kwa Kristo kwa dhahiri kwenye wingu hapa duniani kwa muda mfupi. Lakini hizi sio zenye kuleta utata kwa watu na kujaribu kama Sabato kwa watu wengi. Wengine watakubali Ukweli kwa dhati, kwa sababu ni Ukweli wa Biblia nao wanapenda kutii amri zote za **Mungu**. Vipengele hivi vinavyokinzana vya imani yetu vitazuia wengi wasitumie huduma ya **Mungu**, wasitake kuwa watu wa kipekee, tofauti na ulimwengu. Hivyo, hekima kubwa inahitajika katika namna ya kuwasilisha **Ukweli** kwa watu. Kuna malengo mahususi ya kufikia wakati wa kuanzisha kazi ya huduma ya kimishenari. Ikiwa mipango na mbinu zingekuwa tofauti, hata kama zingehitaji matumizi zaidi ya rasilimali, matokeo yangekuwa bora zaidi. — **Letter 14, 1887.** *{EVsw 248:3}*

Acha Silaha za Malumbano au Ugomvi

Baadhi ya wachungaji, wanapokutana na watu wasiokuwa waumini ambao wana chuki dhidi ya mitazamo yetu juu ya kutokufa kwa roho, huhisi shauku kubwa ya kutoa hotuba juu ya mada hiyo. Hawa wasikilizaji hawako tayari kwa ajili ya hilo, na huongeza tu chuki yao na kuibua upinzani zaidi. Hivyo, mguso wote mzuri wa moyo ambao wangepata wakati mwafaka hupotea. Wasikilizaji wanathibitisha imani yao ya kutokuamini. Mioyo ingeweza kuletwa kwa Kristo, lakini silaha za kupigana zimevaliwa. Chakula kizito kimetupwa kwao, na roho ambazo zingeweza kuletwa kwa Bwana zimeenda mbali kuliko awali.*{EVsw 248:4}*

Silaha za kupigana, roho ya mabishano, lazima ziwekwe chini. Ikiwa tunataka kuiga mfano wa Kristo, lazima tufikie watu pale walipo. — **Manuscript 104, 1898.** *{EVsw 249:1}*

Uelewa Sahihi Ni Muhimu

Uelewa sahihi wa "Kile Maandiko yasemacho" kuhusu hali ya wafu ni muhimu kwa wakati huu. Neno la **Mungu** linasema kuwa wafu hawajui chochote; chuki na upendo wao vimepotea. Lazima tubakie kwenye Neno thabiti la unabii kama mamlaka yetu. Ikiwa hatutaelewa kwa akili mahiri Mafundisho ya Biblia, tukipata nguvu kubwa za kishujaa kutoka kwa Shetani katika dunia yetu, tunaweza kudanganywa tukaita matendo hayo ni ya **Mungu**; kwa maana Neno la **Mungu** linasema kwamba, ikiwezekana, hata waliowateule

wangedanganywa. Tukikosa msingi imara katika Kweli, tutavutwa na mitego ya Shetani. Lazima tusimame imara kwenye Biblia zetu. Ikiwa Shetani ataweza kukufanya wewe uamini kwamba kuna sehemu katika Neno la **Mungu** ambazo hazivuviwa na Roho Mtakatifu, basi atakuwa tayari kukuangamiza roho yako. Jambo hili litatufanya tusiwe na na uhakika wala amani hasa pale tunapohitaji kujua **Ukweli**. — **Review and Herald, Desemba18, 1888.** *{EVsw 249:2}*

Ujumbe wa Uwakili wa Kikristo

Fundisha Kila Mwongofu—Kila nafsi iliyomgeukia **Mungu** inapaswa kupokea nuru kuhusu mahitaji ya Bwana kuhusu zaka na sadaka. Kila kitu ambacho wanadamu hufurahia wanakipata kutoka shambani Kwake **Mungu**, na Yeye anafurahia kuona warithi Wake wakifurahia vitu Vyake; lakini Yeye Ameweka mkataba maalum na wote waliomtii na kusimama chini ya bendera iliyochoviwa katika damu ya Mfalme Immanuel, ili waonyeshe utegemezi wao na uwajibikaji kwa **Mungu** kwa kurudisha sehemu fulani ya mali kwa hazina Yake kama mali Yake. Hii inapaswa kuwekezwa katika kusaidia kazi ya utume inayopaswa kufanyika ili kutimiza agizo lililotolewa na Mwana wa **Mungu** kabla hajawaacha wanafunzi Wake. — **Manuscript 123, 1898.** *{EVsw 249:3}*

Kila Mtu ni Kiungo katika Mnyororo wa Wokovu—Yeye anayekuwa mtoto wa **Mungu** anapaswa kujiangalia kama kiungo katika mnyororo ulioshushwa duniani, ili kuokoa dunia, akiwa pamoja na Kristo katika mpango Wake wa huruma, akitoka pamoja Naye kutafuta na kuokoa waliopotea. **— The Ministry of Healing, p. 105 (1905).** *{EVsw 250:1}*

Wajibu wa Mwinjilisti—Ni sehemu ya kazi yako kuwafundisha wale unaowaongoza katika Kweli, kuleta zaka katika hazina kama ishara yao ya kumtegemea **Mungu**. Wanapaswa kufundishwa kikamilifu kuhusu wajibu wao wa kurudishia Bwana mali Yake. Amri ya kulipa zaka ni wazi kabisa kiasi kwamba haipo nafasi ya visingizio vya kuepuka. Ikiwa utashindwa kuwafundisha waongofu wapya jambo hili, utakuwa umeacha sehemu muhimu ya kazi yako. —**Letter 51, 1902.***{EVsw 250:2}*

Kuongoza Kanisa Jipya— Mtendakazi anayeanzisha makundi madogo hapa na pale, kamwe hapaswi kuwaambia wale waumini wapya wa imani kwamba **Mungu** hahitaji wao wafanye kazi dhahiri kwa mpango maalumu wa ukarimu, ili kuitegemeza kazi kwa juhudi zao binafsi na kwa mali zao.... *{EVsw 250:3}*

Wote wanapaswa kufundishwa kufanya wanachoweza kwa ajili ya Bwana; Wamtolee kulingana na jinsi **Mungu** alivyowabariki. Bwana Anadai kama haki Yake sehemu ya kumi ya mapato yao 1/10 (Asilimia 10), iwe makubwa au madogo; na wale wanaoshikilia hii kibindoni, wanampora **Mungu** Mwenyewe kwa nguvu, na hawawezi kutarajia baraka za **Mungu** kuwa nao. Hata kama kanisa linajumuisha ndugu masikini wengi, somo la ukarimu wa mpangilio linapaswa kufafanuliwa kikamilifu, na mpango huo kuungwa mkono kwa moyo wote. **Mungu** ana uwezo wa kutimiza ahadi Zake. Rasilimali Zake hazina kipimo/kifani, na hutumia zote kufanikisha mapenzi Yake. Na anapoona mtu akifanya wajibu wake kwa uaminifu katika kulipa zaka, mara nyingi kwa hekima Yake huanzisha njia za kuongezeka kwake. Yeye anayefuata mipangilio ya **Mungu** kwa usahihi hata kwa kidogo anachopewa atapokea sawa na yeye anayepewa kwa wingi. — **Gospel Workers, 222, 223 (1915).***{EVsw 250:4}*

Jaribio la Ushirika wa Kimbingu—Baba yetu wa mbinguni huwapa watu vipawa na kutaka sehemu ya kurudishwa ili atujaribu kama tuko waadilifu kustahili karama ya uzima wa milele. **—Testimonies For The Church 3:408 (1875).***{EVsw 251:1}*

Jambo la Kuwasilishwa kwa Hekima na Kurudiwa Mara kwa Mara—Walimu wa Neno la **Mungu** hawapaswi kuficha sehemu yoyote ya ushauri wa **Mungu**, ili watu wasijue wajibu wao, na kisha wasielewe mapenzi ya **Mungu** kuhusu wao, na kisha wajikwae na wapotee katika uharibifu.....*{EVsw 251:2}*

Hebu usimwache mtu apuuzie kujua mafundisho ya wazi na ya Kweli kuhusu kutoa kwa uaminifu zaka. Fanya hii iwe darasa la kutoa kwa Bwana kile anachodai kuwa ni Chake; kwa maana baraka za Bwana hazitakuwa juu ya watu wanaomwibia zaka na sadaka. Mara kwa mara watu wanahitaji kuonyeshwa wajibu wao wa kuleta mali za Bwana kwa namna hii. hebu mtu anayewasilisha Kweli hii kwanza awe mwaminifu katika kuwasilisha jambo hili, na yule anayefuatilia pia shauku ya watu awasilishe kwa uwazi mahitaji ya **Mungu** kuhusu zaka, ili watu waone kuwa watendakazi wote wanafundisha Ukweli mmoja na wapo na nia moja ya kuwahimiza kutoa shauri, kwa utii kwa mahitaji yote ya **Mungu**.*{EVsw 251:3}*

Lakini watendakazi wawe na busara, kutowapa chakula kigumu wale walio watoto, wawalishe kwa maziwa safi ya Neno. Usichanganye roho na mawazo yako mwenyewe na Ukweli, wala wasifunike maagizo na

amri za **Mungu** kwa mila za watu au dhana zisizo za kweli. hebu watu wapate Ukweli kama ulivyo katika Yesu. — **Manuscript 39, 1895.***{EVsw 252:1}*

Kazi Iliyopuuzwa—Tunapaswa kutoa ujumbe wa onyo kwa dunia, lakini Je, tunafanya kazi zetu vipi? Je, ninyi ndugu mnahubiri sehemu ya Kweli inayowafurahisha watu huku sehemu nyingine za kazi zinaacha zikiwa hazijakamilika? Je, kutakuwa na ulazima wa mtu kukufuatilia wewe na kuhamasisha watu wajue wajibu wa kuleta zaka na sadaka zote kwa uaminifu katika hazina ya Bwana? Hii ni kazi ya mchungaji, lakini imepuuzwa kwa huzuni. Watu wamemwibia **Mungu**, na madhara yamejitokeza kwa sababu mchungaji hakutaka kuwachukiza ndugu zake. **Mungu** anawaita watu hawa kuwa ni mawakili wasio waaminifu." — **The Review and Herald, July 8, 1884.***{EVsw 252:2}*

Zaka ya Uaminifu, Fedha ya Kutosha—Ikiwa mali itatiririka kwa mpangilio wa **Mungu**, sehemu ya kumi ya kila ongezeko, basi kutakuwa na wingi wa rasilimali wa kuendeleza kazi Yake. — **Testimonies For The Church 5:150 (1882).***{EVsw 252:3}*

Ukusanyaji kwa Sadaka ya Mavuno kwaajili ya Utume (ingathering offering)—Kwa mpangilio wa **Mungu**, wale wanaobeba mzigo wa kazi Yake wamekuwa wakijaribu kuleta uhai katika njia za zamani za kazi, na pia kuanzisha mipango mipya na njia mpya za kuamsha hamu ya washiriki wa kanisa katika kushirikiana kuifikia dunia. Mojawapo ya mipango mipya ya kufikia wasioamini ni kampeni ya ukusanyaji wa sadaka ya mavuno kwa ajili ya utume. Katika maeneo mengi, miaka ya hivi karibuni, kazi hii imefanikiwa na kuleta baraka nyingi na kuongeza mtiririko wa mali katika hazina ya utume. Wale wasio wa imani yetu wameshuhudia maendeleo ya ujumbe wa malaika wa tatu katika nchi za watu wasiomjua Mungu (Makafiri), na huruma zao zimeamshwa, na wengine wamejitahidi kujifunza zaidi kuhusu Kweli inayobadilisha mioyo na maisha. Wanaume na wanawake wa makundi yote wamefikiwa, na Jina la **Mungu** limetukuzwa. **— Counsels on Stewardship, 190, 191.***{EVsw 252:4}*

Epuka Njia za Kidunia—Tunaona makanisa ya siku zetu yakihamasisha sherehe enye chakula kingi, ulafi, na ulevi na ngono haramu, kupitia chakula cha jioni (supper), maonyesho, vinywaji, dansi, na sherehe zinazokusudiwa kukusanya fedha kwa hazina ya kanisa. Hii ni njia iliyobuniwa na akili za kidunia kupata fedha bila kujitoa.....*{EVsw 253:1}*

Hebu na tujiweke mbali na ufisadi huu wa makanisa, starehe na sherehe ambazo zinaathiri vibaya maadili ya vijana na wazee. Hatuna haki yakuyafunika haya kwa vazi utakatitu, kwa sababu tu mali hiyo, itatumika kwa kazi za kanisa. Sadaka hizi ni zenye ulema, zenye ugonjwa, na zinabeba laana ya **Mungu**. Ni bei za roho. Mimbari inaweza kutetea sherehe, kucheza, bahati nasibu, maonyesho, na sherehe za kifahari ili kupata mali kwa madhumuni ya kanisa; lakini hatupaswi kushiriki katika mambo haya; kwa maana tukifanya hivyo, ghadhabu ya **Mungu** itakuwa juu yetu. Hatutaki kutumia tamaa ya matumbo au starehe za kidunia kumshawishi mfuasi wa Kristo kutoa mali aliyopewa na **Mungu kama wakili**. Kama hawatatoa kwa hiari, kwa upendo wa Kristo, sadaka hiyo hata hivyohaitakubalika kwa **Mungu**. **—Counsels on Stewardship, 201, 202 (1878).***{EVsw 253:2}*

Kurubuniwa kwa Mlo na vicheko na kujipatia raha na anasa—Ni Ukweli wa kusikitisha kwamba mambo matakatifu na ya milele hayana nguvu ya kufungua mioyo ya wafuasi wa Kristo, kutoa sadaka kwa hiari ili kuendeleza/kutegemeza Injili, kama vile mamilioni ya furaha na sherehe vinavyowavutia watu. Ni hali ya kusikitisha kwamba vivutio hivi vinafanikiwa wakati mambo matakatifu hayawezi kuathiri moyo kushiriki katika kazi za huruma na ukarimu.*{EVsw 254:1}*

Mpango wa Musa jangwani wa kukusanya mali ulikuwa na mafanikio makubwa. Hakukuwa na shinikizo lolote. Musa hakufanya sherehe kubwa. Hakuwaita watu kwa kuimba nyimbo za furaha na kuchangamka, kucheza, au starehe za jumla. pia hakutumia bahati nasibu au njia zozote za kidunia kupata mali ya kujenga Patakatifu/Madhabahu ya **Mungu** jangwani. **Mungu** alimuamuru Musa kuwaalika wana wa Israeli kuleta sadaka. Musa alipaswa kupokea zawadi kutoka kwa kila mtu aliyetoa kwa hiari kutoka moyoni. Sadaka hizi za hiari, zilikuja kwa wingi kiasi kwamba Musa alitangaza kuwa zilikuwa zimetosha. Walisitisha kuleta zawadi, kwa sababu walikuwa wana zaidi ya walichohitaji. —**Counsels on Stewardship, 203 (1874).***{EVsw 254:2}*

Na ni maoni gani yanatolewa kwa watu wasio wa imani? Kiwango kitakatifu cha Neno la **Mungu** kinaporomoshwa chini kwenye mavumbi. Dharau hutupiwa juu ya **Mungu** na Jina la Kikristo. Kanuni potofu zaidi zinaimarishwa na njia hii isiyo ya Kimaandiko ya kukusanya mali. Na hii ni jinsi Ibilisi anavyotaka iwe.

Watu wanarudia dhambi ya Nadabu na Abihu. Wanatumia moto wa kigeni badala ya moto mtakatifu katika huduma ya **Mungu**. Bwana hazipokei/hazikubali sadaka za aina hii.*{EVsw 254:3}*

Njia hizi zote za kuleta pesa katika hazina Yake, ni chukizo Kwake. Ni ibada potofu inayosababisha mipango hii yote. Ee ulemavu gani, Upofu na upumbavu gani ulio juu ya wengi wanaodai kuwa WaKristo! Washiriki wa kanisa wanafanya kama wakaazi wa dunia katika siku za Nuhu, wakati mawazo ya mioyo yao yalikuwa mabaya siku zote. Wote wanaomcha **Mungu** watachukia matendo kama haya kama uwakilishi potofu wa dini ya Yesu Kristo. —**Counsels on Stewardship, 205 (1896).***{EVsw 254:4}*

Uwakili wa Mwanadamu—Kuna maana ya kina zaidi ya kanuni safi ya kumpenda mwanadamu na Mungu (golden rule). Kila mtu aliyeteuliwa kuwa wakili wa neema nyingi za **Mungu** anaitwa kutoa kwa nafsi zilizo katika giza na upumbavu, kama vile yeye angekuwa katika nafasi yao, na angependa wampatie yeye. Mtume Paulo alisema, "**Warumi 1:14** *Nawiwa na Wayunani na wasio Wayunani, nawiwa na wenye hekima na wasio na hekima.*" Kwa yote uliyoyajua kuhusu upendo wa **Mungu**, kwa yote uliyopokea ya zawadi za neema Yake, zaidi ya nafsi yoyote maskini na iliyoharibiwa duniani, wewe unawiwa kwa nafsi hiyo kutoa zawadi hizi Kwake. **—Mount of Blessing, p. 193. (1896).** *{EVsw 255:1}*

Uwasilishaji wa Roho ya Unabii

Waumini Wapya Waelewe Kwa Uwazi

Kadiri mwisho unavyokaribia, na kazi ya kutoa onyo la mwisho kwa dunia inavyopanuka, ndivyo inavyokuwa muhimu zaidi kwa wale wanaoukubali Ukweli wa sasa kuelewa kwa uwazi asili na ushawishi wa Shuhuda (Testimonies), ambazo **Mungu** kwa majaliwa Yake ameziunganisha na kazi ya ujumbe wa malaika wa tatu tangu mwanzo wake. —**Testimonies For The Church 5:654 (1889).** *{EVsw 255:2}*

Mafundisho ya Mungu ya Siku hizi

Katika nyakati za kale, **Mungu** alizungumza na wanadamu kupitia vinywa vya manabii na mitume. katika siku hizi anazungumza nao kupitia shuhuda za Roho Wake. Hapakuwahi kuwepo wakati ambapo **Mungu** aliwafundisha watu Wake kwa dhati na bidii zaidi kuliko anavyowafundisha sasa wanadamu kuhusu mapenzi Yake na njia anayotaka waifuate. —**Testimonies For The Church 5:661 (1889).** *{EVsw 255:3}*

Mara Nyingi Hupuuzwa

Wachungaji mara nyingi husahau sehemu hizi muhimu za kazi—matengenezo ya afya, karama za roho, utoaji wa mpango, na matawi makubwa ya kazi ya umishenari. Chini ya juhudi zao, wengi hukumbatia nadharia ya Ukweli, lakini baadaye huonekana kuwa wengi hawatastahimili majaribu (uthibitisho) ya **Mungu**. Mchungaji anayeweka juu ya msingi majani, mbao, na mabua, haya yatachomwa na moto wa majaribu. — **The Review and Herald, 12 December 1878.** *{EVsw 256:1}*

Hazipaswi kuchukua nafasi ya Biblia

Shuhuda za Dada White hazipaswi kutangulizwa mbele za watu kuwa ni zaidi ya Neno la **Mungu**. Neno la **Mungu** ndiyo kiwango kisicho na kosa/dosari. Shuhada hazipaswi kuchukua nafasi ya Neno. Uangalifu mkubwa unapaswa kutekelezwa na waumini wote ili kuendeleza mada hizi kwa uangalifu (tahadhari), huku wakiwazia kusema tu yale yanayohitajika. Hebu wote wathibitishe misimamo yao kutoka katika Maandiko na kuthibitisha kila jambo (kunukuu) wanalodai kuwa kweli limetoka kwenye Neno la **Mungu** lililofunuliwa. — **Letter 12, 1890.** *{EVsw 256:2}*

Shuhuda Haziko Juu Zaidi Ya Biblia

Kadiri tunavyotazama ahadi za Neno la **Mungu**, ndivyo zinavyong'aa zaidi. Kadiri tunavyozitekeleza, ndivyo tunavyoelewa kwa kina zaidi. Msimamo wetu na imani yetu uko katika Biblia. Hatutaki kamwe mtu afikie hatua ya kuzileta Shuhuda mbele zaidi (kuizidi) ya Biblia. —**Manuscript 7, 1894.***{EVsw 256:3}*

Madhumuni ya Shuhuda

Neno la **Mungu** linatosha kuiangazia akili iliyozama kabisa, na yenye ukungu, nalo linaeleweka na yeyote anayetaka kulielewa. Lakini licha ya hayo, kuna baadhi wanaodai kusoma Neno la **Mungu** lakini

wanaishi kinyume na mafundisho yake yaliyo waziwazi. Hivyo, ili kuwaacha wanaume na wanawake wasibakie na udhuru, **Mungu** hutoa Shuhuda za wazi na za moja kwa moja, kuwarejesha kwenye Neno ambalo wamepuuza kulifuata. Neno la **Mungu** lina kanuni nyingi za kuunda tabia za maisha bora, na Shuhuda kwa ujumla na kibinafsi zimekusudiwa kuangazia zaidi kanuni hizi. —**Testimonies For The Church 5:663-664 (1889).** *{EVsw 256:4}*

Nuru Kubwa na Ndogo

Watu huizingatia Biblia kwa udogo sana, na Bwana ametupatia nuru ndogo ili kuwaongoza wanaume na wanawake kwenye nuru Kuu zaidi. —**The Colporteur Evangelist, 37 (1902).***{EVsw 257:1}*

Kielelezo: Uwasilishaji wa Roho ya Unabii

Mzee ____ hakuingia kwenye mgogoro na wapinzani. Alionyesha Biblia kwa uwazi kabisa, kiasi kwamba mtu yeyote aliyepingana naye ni wazi alikuwa akipingana na Neno la **Mungu**.*{EVsw 257:2}*

Ijumaa usiku na asubuhi ya Sabato alizungumza kuhusu karama za roho, hasa kuhusu Roho ya unabii. Waliokuwepo katika hotuba hizi walisema alifundisha kwa uwazi, na nguvu. **—Letter 388, 1906.** *{EVsw 257:3}*

Katika mafundisho yake, Mzee ____ alionyesha kuwa Roho ya unabii ina sehemu muhimu katika utendaji wa kuimarisha Ukweli. Alipomaliza kazi yake, aliniita ..... kuzungumza na watu. —**Letter 400, 1906.***{EVsw 257:4}*

Tumia Muda Kuupima Ushahidi

Katika maono ya mwisho niliyopewa huko Battle Creek nilioneshwa kuwa maamuzi yasiyokuwa ya busara yalichukuliwa huko ----- kuhusiana na maono kipindi cha taasisi ya kanisa. Kulikuwa na wengine huko ambao walikuwa watoto wa **Mungu**, na bado walitilia shaka maono hayo. Wengine hawakuwa na upinzani, lakini hawakuthubutu kuchukua msimamo kuhusu maoni hayo. Wengine walikuwa wanashuku (wana mashaka), na walikuwa na sababu ya kutosha kuwafanya wawe hivyo. Maono ya uongo na mazoea ya ushabiki, na matunda mabaya yaliyofuata, yalikuwa na ushawishi wa kazi huko Wisconsin kuzifanya akili ziwe na wivu kwa kila kitu kinachobeba jina la maono. Vitu hivi vyote vinapaswa kuzingatiwa, na kufanyiwa kazi kwa hekima. Hakupaswi kuwepo na jaribu au masumbufu kwa wale ambao hawajawahi kuona mtu akiwa na maono, na ambao hawana ufahamu binafsi juu ya ushawishi wa maono. Watu hao (wenye maono) hawapaswi kuzuiliwa kwa faida na manufaa ya kanisa, ikiwa mwenendo wao wa Kikristo uko sahihi, na wameonesha mwenendo mzuri wa Kikristo. *{EVsw 257:5}*

Wengine, nilioneshwa, kuwa wangeweza kupokea maono yaliyochapishwa, wakiupima mti kwa matunda yake. Wengine ni kama Tomaso mwenye mashaka; hawawezi kuamini ushuhuda uliochapishwa, wala kupokea ushahidi kupitia ushuhuda wa wengine; lakini lazima waone na wawe na ushahidi wao wenyewe. Hao hawapaswi kutengwa, lakini kwa uvumilivu kwa upendano wa ndugu unapaswa kuoneshwa kwao hadi watakapothabitika katika msimamo wao au la!Ikiwa wanapigana dhidi ya maono, ambayo hawayajui; ikiwa watabeba upinzani wao hadi kupingana na yale ambayo hawana uzoefu kwayo, na wanajisikia kuudhika wakati wale ambao wanaamini kuwa maono hayo ni ya **Mungu** wanazungumza juu yao katika mkutano, na kujifariji kwa mafundisho yanayotolewa kupitia maono, kanisa linaweza kutambua kwamba hawako sahihi. —**Testimonies For The Church 1:327-329 (1862).***{EVsw 258:1}*

Kuongozwa Katika Msimamo Usiokamilika

Nimeoneshwa kwamba, wengine, hususani kule Iowa, wamefanya maono kuwa kanuni ya kupima kila kitu, na wamechukua kusudi ambalo mume wangu na mimi hatukulifuata. Wengine hawanifahamu mimi vizuri na kazi zangu na wanashuku sana chochote kinachobeba jina la maono. Na jambo hili ni la kawaida tu na linaweza likashindwa kwa uzoefu. Kama watu hawajawa na utulivu kuhusu maono wasizidishiwe mambo mengi. Somo la kuwasaidia katika jambo hili linaweza kupatikana katika kitabu cha Shuhuda kwa kanisa gombo la 8, uk. 328,329, ambacho natumai kitasomwa na wote. Wachungaji lazima wawe na huruma kwa wengine, wakifanya tofauti, wengine waokoeni kwa hofu, mkiwanyakua toka motoni. Wachungaji wa **Mungu** wanapaswa kuwa na hekima kumpa kila mmoja sehemu ya chakula chake, na kufanya tofauti hiyo na watu tofauti kama masuala yao yanavyohitaji. Kusudi linalochukuliwa na baadhi ya watu huko ------ambao hawanifahamu mimi vizuri halijawa la uangalifu na thabiti. Wale ambao kwa kulinganisha walikuwa wageni kwa njozi wameshughulikiwa kwa hali sawa na wale waliokuwa na nuru kubwa na uzoefu kuhusu maono.

Wengine wametakiwa kuidhinisha maono wakati hawawezi kufanya hivyo kwa dhamira safi, na kwa njia hii baadhi ya roho aminifu zimeongozwa kuchukua msimamo dhidi ya maono na dhidi ya mwili wa Kristo, ambao wasingeuchukuwa kama masuala yao yangeshughulikiwa kwa busara na rehema. **—Testimonies For The Church 1:382-383 (1863).** *{EVsw 259:1}*

Kushinda upinzani

Wahubiri (wasio Waaadventista wa Sabato) wanaanza kushambulia (kupiga kelele), na dhidi ya Dada White haswa. Lakini hii inawadhuru wao wenyewe. Mimi ninaweka vitabu vya Tumaini la *Vizazi Vyote* (*Desire of Ages*), *Pambano Kuu* (*Great Controversy*), *Wazee na Manabii* (*Patriarchs and Prophets*), na (*Kristo Mwokozi Wetu*) *Christ Our Saviour* katika familia; kwa hivyo wahubiri wanaposhindana nami, nitazungumza kupitia maandiko yangu kwa watu. Ninaamini roho zitaongoka na kuifuata ile Kweli. Sasa tunawarudisha kwenye sheria na Shuhuda. *Ikiwa hawasemi sawasawa na Neno hili, bila shaka kwa hao Hapana asubuhi ISAYA 8:20.* **—Letter 217, 1899.***{EVsw 259:2}*

Kutathmini kwa matokeo au Matunda

Hebu Shuhuda zihukumiwe kwa matunda yake. Je, Roho ya mafundisho yake ni ipi? Matokeo ya ushawishi wake yamekuwa yapi? "Wote wanaotamani kufanya hivyo wanaweza kujijulisha/kujiridhisha wenyewe na matunda ya maono haya.....*{EVsw 260:1}*

"Ama **Mungu**analifundisha kanisa Lake, anakemea makosa yao na kuimarisha imani yao, ama sivyo. Kazi hii ni ya **Mungu**, au sivyo. **Mungu** hafanyi chochote kwa ushirikiano na Shetani. Kazi yangu ..... inabeba chapa ya **Mungu** au chapa ya adui. Hakuna kazi nusu nusu katika suala hilo. Shuhuda ni za Roho wa **Mungu**, au za shetani. **—Testimonies For The Church 5:671 (1889).***{EVsw 260:2}*

Mungu Anasema Kupitia Shuhuda

Lazima tufuate maelekezo yaliyotolewa kupitia roho ya unabii. Lazima tuupende na kuutii Ukweli kwa ajili ya wakati huu. Hili litatuokoa kutokana na kuukubali udanganyifu wenye nguvu. **Mungu** amesema nasi kupitia Neno Lake. Yeye Amesema nasi kupitia Shuhuda kwa Kanisa na kupitia vitabu ambavyo vimesaidia kuweka wazi wajibu wetu wa sasa na msimamo ambao tunapaswa kuwa nao sasa. **—Testimonies For The Church 8:298 (1904).***{EVsw 260:3}*

Kutoa Mafundisho ya Afya na Viwango vya Kikristo

[Tazama pia The Medical Evangelist, kurasa 513-551 na 657-665, "*Health and Health Principles*."]

Kuwasilisha Matengenezo ya Afya — Kazi yetu inapaswa kuwa ya kivitendo-maisha halisi. Tunapaswa kukumbuka kwamba mtu ana mwili vivyo hivyo roho inayohitaji kuokolewa. Kazi yetu ni zaidi ya kusimama mbele ya watu kwa ajili ya kuhubiri tu. Katika huduma yetu, tunapaswa kuwahudumia wale wenye maumivu ya kimwili tunaokutana nao. Tunapaswa kuwasilisha kanuni za matengenezo ya afya, tukiwafanya wasikilizaji wetu wahisi kuwa wao pia wanapaswa kuchukua hatua katika kudumisha afya yao.*{EVsw 260:4}*

Mwili lazima udumishwe ukiwa katika hali nzuri ya afya ili roho ipate afya pia. Hali ya mwili huathiri hali ya roho. Mtu anayependa kupata nguvu za kimwili na kiroho lazima aielimishe ladha yake ya kula kwa njia sahihi. Ni lazima awe makini asiipe roho mzigo kwa kutumia nguvu za kimwili na kiroho kupita kiasi. Kuzingatia kwa uaminifu kanuni sahihi za kula, kunywa, na kuvaa ni wajibu ambao **Mungu** amewawekea wanadamu.*{EVsw 261:1}*

Bwana anatamani tuzingatie sheria za afya na uzima. Yeye Anampatia kila mtu wajibu wa kutunza mwili wake ipasavyo ili udumishwe ukiwa na afya. — **Letter 123, 1903.***{EVsw 261:2}*

Sehemu ya Ujumbe wa Mwisho — Kanuni za matengenezo ya afya zinapatikana katika Neno la **Mungu**. Injili ya afya inapaswa kuunganishwa kwa uthabiti na karibu na huduma ya Neno. Kusudio la Bwana ni kwamba nguvu ya kuponya ya matengenezo ya afya iwe sehemu ya jitihada kubwa ya mwisho ya kuhubiri ujumbe wa Injili. — **Medical Ministry, 259.***{EVsw 261:3}*

Kama watu, tumepokea jukumu la kueneza kanuni za matengenezo ya afya. Wapo wanaodhani kuwa suala la chakula halina umuhimu wa kutosha kuingizwa katika kazi yao ya kuhubiri. Lakini hao wanakosea sana. Neno la **Mungu** linasema, "**1 Wakorintho 10:31** *Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lolote,*

*fanyeni yote kwa utukufu wa **Mungu**."* Mada ya kiasi, kwa vipengele vyake vyote, ina nafasi muhimu katika kazi ya wokovu. — **Testimonies For The Church 9:112 (1909).***{EVsw 261:4}*

Kuthibitika Kikamilifu katika Matengenezo ya Afya — Wale wanaoishi katika siku za mwisho za historia ya dunia hii wanahitaji kusimikwa/kuthibitika kabisa katika kanuni za matengenezo ya afya.....*{EVsw 262:1}*

Wanaume na wanawake walio wagonjwa wanahitaji kuwa wanamatengezo wa afya. **Mungu** atashirikiana na watoto Wake katika kuhifadhi afya zao, ikiwa watakula kwa uangalifu, wakiepuka kuwekeza mizigo isiyo ya lazima tumboni. Kwa neema Yeye Amefanya njia ya asili kuwa salama na pana kwa wote wanaotaka kuipita. Yeye Ametoa chakula kizuri na chenye afya kinachozalishwa kwenye dunia kwa ajili ya ustawi wetu.....*{EVsw 262:2}*

Wengi wameidhuru sana miili yao kwa kuacha kuzingatia sheria za uzima, na huenda wasiweze kupona kabisa kutokana na madhara ya kutosimamia vizuri; lakini hata sasa wanaweza kutubu na kubadilika-kuongoka. Mtu amejaribu kuwa mwenye hekima zaidi kuliko **Mungu**. Amejifanya yeye ndiye sheria yenyewe. **Mungu** anatuita tuzingatie mahitaji Yake, tusimwaibishe tena kwa kupunguza uwezo wa kimwili, kiakili, na kiroho. — **Letter 135, 1902.***{EVsw 262:3}*

Matengenezo ya afya ya Kivitendo — Bwana anataka wachungaji wetu, madaktari, na waumini wa kanisa kuwa waangalifu kutohimiza watu wasiojua imani yetu kubadilisha mlo ghafla, jambo linalowapa watu jaribu kabla. Tuendelee kushikilia kanuni za matengenezo ya afya, na kisha tumwache Bwana aongoze waadilifu wa moyo. Watasikia na kuamini. Bwana hataki wajumbe Wake kuwasilisha Ukweli mzuri wa maisha yenye afya kwa njia inayoweza kuleta chuki, ubaguzi ubishi au kuharibu akili za watu. Hebu tusiweke vizuizi mbele ya watu wanaotembea katika njia za giza la ujinga. Hata tukipongeza jambo zuri, ni bora tusiwe na shauku kubwa ya kupitiliza mno, ili tusitengeneze watu kupotea kwa kutoka kwenye njia. Wasilisha kanuni za afya na kiasi kwa sura nzuri na ya kuvutia zaidi.*{EVsw 262:4}*

Tusiende kwa ujuvi (bila kucheua mambo). Watendakazi wanaoingia maeneo mapya kuanzisha makanisa,wasizumguze kwa kusisitiza sana suala la chakula na kufanya mambo magumu. Wawe waangalifu wasiweke mipaka kwa haraka, maana hilo linaweza kuwa kikwazo kwa wengine. Tusisukume watu kwa nguvu, bali tuwaongoze. *{EVsw 263:1}*

Popote Ukweli unapoenezwa, elimu itolewe juu ya maandalizi ya vyakula vyenye afya-visivyokobolewa au kusindikwa (wholesome foods). **Mungu** anataka kila mahali watu wafundishwe na walimu wenye ujuzi jinsi ya kutumia kwa busara mazao wanayoyazalisha au kupatikana kwa urahisi katika sehemu yao ya nchi. Hivyo maskini na matajiri wote wanaweza kufundishwa kuishi kwa afya njema. **— Gospel Workers, 233 (1915).***{EVsw 263:2}*

Kuiweka Mbele — Kazi ya matengenezo ya afya ni njia ya Bwana ya kupunguza mateso katika ulimwengu wetu na kulitakasa kanisa Lake. Wafundishe watu kwamba wanaweza kutenda kama mkono wa kusaidia wa **Mungu** kwa kushirikiana na Mwalimu mkuu katika kurejesha afya ya kimwili na kiroho. Kazi hii ina muhuri wa mbinguni na itafungua milango kwa ajili ya kuingia kwa Kweli zingine za thamani. Kuna nafasi kwa wote kufanya kazi ambayo wataishikilia kazi hii kwa akili mahiri. *{EVsw 263:3}*

Weka mbele kazi ya matengenezo ya afya, ndio ujumbe nimeelekezwa kuubeba. Onesha kwa uwazi sana thamani yake ambayo ueneaji wake utaonesha. Kujiepusha na vyakula na vinywaji vyote vyenye madhara ni matunda ya dini ya Kweli. Yule ambaye ameongoka kabisa ataacha kila tabia mbaya inayodhuru na uchu wa kula au ulafi. Kwa kujiepusha kabisa atashinda tamaa yake ya kuendekeza anasa zinazoharibu afya. *{EVsw 263:4}*

Nimeagizwa kuwaambia wakufunzi wa matengenezo ya afya: Songa mbele. Ulimwengu unahitaji kila nukta ya ushawishi mnaoweza kuwa nao ili kurudisha nyuma wimbi la ole wa maadili. Hebu wale wanaoufundisha ujumbe wa malaika wa tatu wasimame kweli kwa viwango vyao. — **Testimonies For The Church 9:112, 113 (1909)***{EVsw 264:1}*

Kuachana Kabisa na Pombe na Sigara — Wanaume na wanawake wana tabia nyingi zinazopingana na kanuni za Biblia. Waathirika wa pombe na sigara huharibika mwili, roho, na fikra. Watu kama hawa hawapaswi kuingizwa kanisani hadi wadhihirishe kuwa wamebadilika kweli, kwamba wanahisi haja ya imani inayofanya kazi kwa upendo na kusafisha roho. Ukweli wa **Mungu** utamsafisha muumini wa kweli. mtu aliyebadilika kabisa atakataa kila tabia na tamaa zinazochafua. Kwa kuacha kabisa atashinda tamaa yake ya vitu vinavyoharibu afya. — **Letter 49, 1902.***{EVsw 264:2}*

Uongofu Siri ya Ushindi — Kitu cha kwanza na muhimu zaidi ni kuiyeyusha na kuitiisha roho kwa kumwasilisha Bwana wetu Yesu Kristo kama mbeba dhambi, Mwokozi anayesamehe dhambi, na kuifanya Injili iwe wazi kadri iwezekanavyo. ***{EVsw 264:3}***

Wakati Roho Mtakatifu anapofanya kazi kati yetu, kama alivyofanya katika mkutano wa kambi huko _____, roho zisizo tayari kwa kuja kwa Kristo husadikishwa. Wengi huja katika mikutano yetu na kubadilika hata wale ambao kwa miaka mingi hawajahudhuria katika makanisa yoyote. Ukweli sahili wa moja kwa moja huifikia mioyo yao. Unagusa tabaka zote. Wapenzi wa sigara wanatupilia mbali sanamu zao, na mnywaji wa pombe anatupa pombe yake. Hawa wasingeweza kufanya hivi kama wasingekumbatia kwa imani ahadi za **Mungu** za kusamehewa dhambi. Je, si vyema kufanya jitihada za dhati kuokoa roho hizi? — **Letter 4, 1899.** ***{EVsw 264:4}***

Anza Matengenezo Kuanzia kwenye Msingi — Kunywa pombe huhamasisha ufisadi mbaya zaidi, ulevi na huimarisha tamaa mbaya za Kishetani. Tunapotazama mambo haya na kuona matokeo mabaya ya pombe, je, hatutapigania kwa nguvu kuungana na **Mungu** katika kupambana na uovu huu mkubwa? Msingi wa pombe ni tabia mbaya za ulaji. Wanaoamini Ukweli wa sasa wanapaswa kukataa kunywa chai na kahawa, kwa sababu vinachochea tamaa ya vinywaji vyenye kusisimua zaidi. Wanapaswa kukataa kula nyama, kwa sababu pia huongeza tamaa ya pombe. Chakula chenye afya kisichokobolewa au kusindikwa, kilichopikwa kwa ladha na ustadi, kinapaswa kuwa mlo wetu sasa.***{EVsw 265:1}***

Wale wasiokuwa waongofu wa afya wanajidhalilisha kwa kutojitendea haki na kujiua wenyewe kwa kutumikia tamaa zao. Wengine wanaweza kudhani kuwa suala la mlo halina umuhimu wa kutosha kuingizwa katika dini. Lakini hao wanakosea. Neno la **Mungu** linasema, "*Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lolote, fanyeni yote kwa utukufu wa* ***Mungu*** *1 Wakorintho 10:31*." Mada ya kuwa na kiasi, na mlolongo wake, vina nafasi muhimu katika wokovu wetu. Kwa sababu ya tabia mbaya za ulaji, dunia inaendelea kuwa na maovu zaidi na zaidi na upotofu wa maadili. **— Letter 49, 1902.*{EVsw 265:2}***

Huduma Binafsi kwa Wale Wasio na Kiasi — Kazi ya umishenari si kuhubiri tu. Inajumuisha kwa pamoja jukumu binafsi kwa wale waliotumia vibaya afya zao na kujiweka katika hali isiyo na nguvu ya kudhibiti tamaa na hisia zao. Roho hizi zinapaswa kuhudumiwa sawa na wale walio katika hali nzuri zaidi. Dunia yetu imejaa wale wanaoteseka.***{EVsw 265:3}***

Mungu ameandika sheria Yake katika kila neva, misuli, nyuzi/seli, na utendaji wa mwili wa binadamu. Kuruhusu kuendekeza tamaa zisizo za asili, kama chai, kahawa, sigara, au pombe, ni kukosa kiasi, na ni vita dhidi ya sheria za uzima na afya. Kwa kutumia vitu hivi haramu, hali ya mwili inabadilika kinyume na kusudi la Muumba. Kukubali hili miongoni mwa wanadamu ni dhambi. Kula chakula ambacho hakisaidii damu iwe safi ni kinyume cha sheria za mwili wetu, na ni ukiukaji wa sheria za **Mungu**. Chanzo huleta athari. Mateso, magonjwa, na kifo ni adhabu ya dhambi hii ya kujiendekeza. — **Letter 123, 1899.*{EVsw 265:4}***

Kutafuta Furaha — Maelfu wanatafuta furaha kwa bure katika burudani za kidunia. Wanatamani kitu ambacho hawana. Wanatumia pesa zao kwa vitu visivyo chakula, na kujishughulisha kwa mambo yasiyowaridhisha. Nafsi inayohisi njaa na kiu itaendelea kuhisi njaa na kiu maadamu inaendelea kushiriki katika anasa hizi zisizoridhisha/zisizotosheleza. Laiti kama kila mmoja angeisikiliza sauti ya Yesu, *"Mtu akiona kiu, na aje Kwangu anywe!"* Wale wanaokunywa maji ya uzima hawatakuwa na kiu tena ya anasa zisizo za maana. Kristo, Chanzo cha maisha, ni chemchemi ya amani na furaha.***{EVsw 266:1}***

Mungu huwapa wanadamu vipaji na talanta mbalimbali, si kwa ajili ya kukaa bure, wala kwa ajili ya anasa au kufurahisha nafsi, bali ili wawe baraka kwa wengine kwa kuwasaidia kufanya kazi ya utume kwa bidii na kujitolea. — **The Youth's Instructor, November 6, 1902.*{EVsw 266:2}***

Maonyesho ya drama, Michezo ya Kuigiza na Sinema kwenye Kumbi za Hadhara — Shauku kuu ya Shetani ni kupotosha akili na kuwafanya watu watamani maonyesho na michezo ya uigizaji. Uzoefu na tabia ya wote wanaojihusisha na kazi hii vitakuwa sambamba na chakula kinachotolewa kwa akili zao.***{EVsw 266:3}***

Bwana ameonyesha upendo Wake kwa dunia. Hakukuwa na uongo wala uigajizaji katika kile alichofanya. Alitoa zawadi hai, yenye uwezo wa kuvumilia aibu, kupuuzwa, aibu ya dharau, na lawama. Kristo alifanya hivyo ili kuokoa wanadamu walioanguka. Wakati wanadamu walipokuwa wakitengeneza mikakati na njama za kumuua, Mwana wa **Mungu** wa Milele alikuja duniani kutupatia mfano wa kazi kuu ya wokovu wa mwanadamu. Lakini leo, wenye kiburi na wasio waaminifu wanajitahidi kupata heshima kubwa na sifa kubwa kutoka kwa watu kwa kutumia vipaji vya **Mungu** katika anasa. — **Manuscript 42, 1898.** ***{EVsw 267:1}***

Kufanya Kazi kwa Wapendao Anasa na Starehe za Dunia — Badala ya kukidhalilisha kisima cha Yakobo na kusema ni kitu kidogo tu, Kristo alitoa kitu bora mno..... Yeye Alimtolea mwanamke kitu bora kuliko alichokuwa nacho, hata maji ya uzima, furaha na matumaini ya Injili ya ufalme Wake.*{EVsw 267:2}*

Huu ni mfano wa jinsi tunavyopaswa kufanya kazi. Haina maana kwenda kwa wapendao anasa, waigizaji kwenye kumbi (theatres), washindaniao mambo ya kidunia, walevi, wacheza kamari, na kuwakashifu vikali kwa dhambi zao. Hiyo haitasaidia. Tunapaswa kuwapatia kitu bora zaidi kuliko wanachokipenda, amani ya Kristo, ipitayo fahamu zote,*{EVsw 267:3}*

Nafsi hizi maskini zimejishughulisha na mbio za kiwazimu za kufuata furaha za kidunia na utajiri wa dunia. Hawajui chochote kingine kinachovutia. Lakini michezo, maonyesho, mbio za farasi, haviwezi kuiridhisha roho. Wanadamu hawakuumbwa kuridhika kwa njia hii wala kutumia pesa kwa vitu visivyo chakula. Waonyeshe wanadamu jinsi utukufu wa mbinguni usioharibika ulivyo wa thamani isiyo na kifani, na isiyoharibika, kuliko furaha za muda mfupi na anasa za dunia hii. Jitahidi kuwashawishi kuhusu uhuru, tumaini, pumziko na amani vinavyopatikana katika Injili. "**Yohana 4:14** *walakini yeyote atakayekunywa maji yale nitakayompa Mimi hataona kiu milele*." Kristo alisema. —**Manuscript 12, 1901.***{EVsw 267:4}*

Maelekezo Kuhusu Mavazi na Starehe/Anasa—Misingi ya maisha ya Kikristo inapaswa kufafanuliwa kwa watu waliotangulia kuamini Kweli. Wanaume na wanawake waaminifu wa Kikristo wanapaswa kuwa na shauku kubwa ya kuleta roho iliyopata usadikisho kwenye uelewa sahihi wa kuhesabiwa haki katika Kristo Yesu. Iwapo mtu yeyote ameipa nafasi ya juu tamaa ya anasa au kupenda mavazi, kiasi kwamba sehemu yoyote ya akili, nafsi, au nguvu zake zinatumika kwa ajili ya kujipenda nafsi, waumini waaminifu wanapaswa kuwatunza watu hawa kama wale watakaotoa hesabu. Hawapaswi kupuuza maelekezo ya uaminifu, unyenyekevu na ya upendo ambayo ni lazima sana kwa waongofu wachanga, ili isionekane kuwa ni kazi ambayo haijafanywa kwa moyo wote. —**Manuscript 56, 1900.** *{EVsw 268:1}*

Kuwafundisha Waongofu Wapya Kuhusu Ibada ya Sanamu ya Mavazi—Moja ya mambo ambayo waongofu wapya watahitaji maelekezo juu yake ni suala la mavazi. Hebu waumini wapya wapatiwe mafunzo ya dhati kwa uaminifu. Je, wana ubatili kuhusiana na mavazi yao? Je, wanajivunia mioyo yao? Ibada ya sanamu ya mavazi ni ugonjwa wa maadili. Haipaswi kuingizwa katika maisha mapya. Katika hali nyingi, kukubali matakwa ya Injili kutahitaji mabadiliko dhahiri katika mavazi.*{EVsw 268:2}*

Hakupaswi kuwepo na uzembe katika mavazi. Kwa ajili ya Kristo, sisi tukiwa ni mashahidi, tunapaswa wa naku mwonekano mzuri zaidi. Katika huduma ya hema la kukutania, **Mungu** alibainisha kila jambo kuhusu mavazi ya wale waliohudumu mbele Yake. Hivyo tunafundishwa kuwa Yeye anajali kuhusu mavazi ya watumishi Wake. Maelekezo ya mavazi ya Haruni yalikuwa mahususi, kwani mavazi yake yalikuwa na maana ya mfano. Vivyo hivyo, mavazi ya wafuasi wa Kristo yanapaswa kuwa na maana ya mfano (symbolic). Katika kila jambo tunapaswa kuwa wawakilishi Wake. Muonekano wetu katika kila nyanja unapaswa kuonyesha unadhifu, staha, uungwana, upole, kiasi, na usafi. Lakini Neno la **Mungu** halikubali kufanya mabadiliko ya mavazi kwa sababu tu ya mtindo wa dunia—yaani kuiga dunia ili tufanane nao. Wakristo hawapaswi kujipamba kwa mavazi ya gharama au vito vya thamani.*{EVsw 268:3}*

Maneno ya Maandiko kuhusu mavazi yanapaswa kuzingatiwa kwa makini. Tunahitaji kuelewa kile Bwana wa mbingu anachokithamini hata katika mavazi ya mwili. Wote wanaotafuta neema ya Kristo kwa moyo wote watazingatia maneno haya ya thamani yaliyoongozwa na **Mungu**. Hata mtindo wa mavazi utaonyesha Ukweli wa Injili.*{EVsw 269:1}*

Wote wanaojifunza maisha ya Kristo na kutekeleza mafundisho Yake watafanana na Kristo. Mvuto wao utakuwa kama Wake. Wataonyesha uthabiti wa tabia. Wanapopita katika njia ya unyenyekevu wa utii, wakitimiza mapenzi ya **Mungu**, wataathiri watu kwa kuendeleza kazi ya **Mungu** na usafi wa kazi Yake. Katika roho hizi zilizoongoka kabisa, dunia itakuwa na ushuhuda wa nguvu ya utakaso wa Kweli juu ya tabia ya binadamu. — **Testimonies For The Church 6:96, 97 (1900).***{EVsw 269:2}*

Kulingana na Imani Yetu—Kujinyima katika mavazi ni sehemu ya wajibu wetu wa Kikristo. Kuvaa kwa unyenyekevu na kujiepusha na maonyesho ya vito na mapambo ya aina zote, kulingana na imani yetu. Je, sisi ni miongoni mwa wale wanaoona upuuzi/upumbavu wa watu wa kidunia katika kuendekeza anasa za mavazi pamoja na kupenda matumbuizo? Ikiwa ndivyo, tunapaswa kuwa wa kundi la kuepuka kila kitu kinachothibitisha roho hii inayochukua akili na mioyo ya wale wanaoishi kwa dunia tu, na wasio na mawazo au wasiwasi kuhusu maisha yajayo. **—Testimonies For The Church 3:366 (1875).***{EVsw 269:3}*

Kumfuata Kristo au Dunia—Dada mmoja aliyekuwa akikaa kwa wiki kadhaa katika taasisi yetu ya _____ alisema alihisi kukata tamaa sana kutokana na alichokiona na kusikia hapo.... Kabla ya kuamini Kweli, alikuwa akifuata mitindo ya dunia katika mavazi yake, na kuvaa vito vya dhahabu na mapambo mengine ya gharama; lakini baada ya kuamua kutii Neno la **Mungu**, alihisi mafundisho Yake yanamtaka aache kila aina ya kujipamba kupindukia. Alifundishwa kuwa Waadventista wa Sabato hawavai vito, dhahabu, fedha, wala vito vya thamani, na hawafuati mitindo ya dunia katika mavazi yao. Aliposhuhudia miongoni mwa wale wanaodai ni waumini wa imani jinsi walivyokuwa wameacha mbali kiwango cha kiasi kinachofundishwa na Biblia, alihisi kuchanganyikiwa. Je, hawakuwa na Biblia ile ile aliyokuwa akisoma, na ambayo alijaribu kuendana nayo? Je, uzoefu wake wa zamani ulikuwa ushabiki tu au kupitiliza? Je, alikuwa amekosea tafsiri ya maneno ya mtume, *"rafiki wa dunia ni uadui **Mungu**, Basi kila mtu atakaye kuwa rafiki wa dunia hujifanya kuwa adui wa Mungu- **YAKOBO 4:4**"*? ***{EVsw 270:1}***

Bi. D, mwanamke aliyehudumu katika taasisi, alikuwa akitembelea chumba cha Dada _____ siku moja,, ndipo Dada------ alipotoa mkufu wa dhahabu na mnyororo wa mapambo kutoka kwenye sanduku lake na kusema anataka kuuza vito hivi na kuweka mapato katika hazina ya Bwana. Mwenzake alisema, "Kwa nini unauza? Ningeuvaa kama ungekuwa wangu." "Kwa nini," akajibu dada _____, "nilipopokea Kweli, nilifundishwa kuwa vitu hivi vyote vinapaswa kuachwa. Hakika vinapingana na mafundisho ya Neno la **Mungu**." Na akamwonyesha msikilizaji wake maneno ya mitume, Paulo na Petro, kuhusu jambo hili, "1 Timotheo 2:9-10 *Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri, pamoja na adabu nzuri, na moyo wa kiasi; si kwa kusuka nywele, wala kwa dhahabu na lulu, wala kwa nguo za thamani bali kwa matendo mema, kama iwapasavyo wanawake wanaoukiri uchaji wa **Mungu**.*" "**1 Petro 3:3-4** *Kujipamba kwenu, kusiwe kujipamba kwa nje, yaani, kusuka nywele; na kujitia dhahabu, na kuvalia mavazi bali kuwe utu wa moyoni usioonekana, katika mapambo yasiyoharibika; yaani, roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za **Mungu**.*" ***{EVsw 270:2}***

Katika kujibu, mwanamke huyo alionyesha pete ya dhahabu iliyokuwa katika kidole chake, aliyopewa na mtu ambaye sio muumini, na kusema alidhani haikuwa kosa kuvaa mapambo kama hayo. "Sisi hatuzingatii sana hayo," alisema, "kama zamani. Watu wetu wamekuwa wakichukua tahadhari sana kuhusu suala la mavazi. Wanawake wa taasisi hii huvaa saa za dhahabu na mikufu ya dhahabu, na kuvaa kama watu wengine. Sio busara kuwa wa kipekee katika mavazi yetu; maana hatuwezi kuleta ushawishi mkubwa." ***{EVsw 271:1}***

sisi tunajiuliza, Je, hili linaendana na mafundisho ya Kristo? Je, tunapaswa kufuata Neno la **Mungu**, au mila za dunia? Dada yetu aliamua kuwa ni salama zaidi kuambatana na kiwango cha Biblia. Je, Bi. D na wengine wanaofuata njia kama hiyo watafurahia kuona matokeo ya ushawishi wao, siku ile kila mtu atakapopokea kulingana na matendo yake? ***{EVsw 271:2}***

Neno la **Mungu** liko wazi. Mafundisho Yake hayawezi kupotoshwa. Je, tutalitii, kama alivyolitoa kwetu, au tutatafuta njia ya kuporomoka kiasi gani na bado tuokolewe? Ningependa wote walioko katika taasisi zetu waipokee na kuifuata nuru ya **Mungu**, na hivyo kuwawezesha kuipeleka kwa wale ambao wanatembea gizani.***{EVsw 271:3}***

Kufuata dunia ni dhambi inayotapeli/inayofyonza roho za watu wetu, na kuingilia sana utumishi wao. Ni kazi bure kutangaza ujumbe wa onyo kwa dunia huku tunaukana/kuukataa katika maisha ya kila siku. —**The Review and Herald, Machi 28, 1882.** ***{EVsw 271:4}***

Kazi ya Moyo—Kuna wengi wanaojaribu kusahihisha maisha ya wengine kwa kushambulia tabia wanazodhani ni mbaya. Huwaendea waliokosea na kuonyesha mapungufu yao. Wanasema, "Haujavalia kama unavyopaswa." Wanajaribu kuondoa mapambo, au chochote kinachowaudhi, lakini hawatafuti kuimarisha akili zao katika Kweli. Wale wanaotaka kusahihisha wengine wanapaswa kuonyesha mvuto wa Yesu. Wanapaswa kuzungumza juu ya upendo Wake na huruma, kuwasilisha mfano Wake na kafara, kufunua Roho Wake, na hawahitaji hata kugusia suala la mavazi. Hakuna haja ya kufanya suala la mavazi kuwa msingi wa dini yako. Kuna jambo zuri zaidi la kuzungumza. Zungumzia Kristo, na moyo unapoongoka, kila kitu kisichoendana na Neno la **Mungu** kitatoweka. Ni kazi bure kuondoa majani kwenye mti ulio hai. Majani yatarudi tena. Shoka lazima liwekwe kwenye mzizi wa mti, kisha majani yataanguka, na kisha yasirudi tena.***{EVsw 272:1}***

Ili kufundisha watu thamani ya vitu vya dunia, lazima uwaelekeze kwa Chanzo Hai, na kuwafanya wanywe kutoka kwa Kristo, hadi mioyo yao ijazwe na upendo wa **Mungu**, na Kristo awe ndani yao, chemchemi ya maji yanayotiririka kuleta uzima wa milele. —**The Signs of the Times, July 1, 1889.*{EVsw 272:2}***

Safisha chemchemi, na mifereji itakuwa safi. Ikiwa moyo uko sawa, maneno yako, mavazi yako, matendo yako, yote yatakuwa sawa. —**Testimonies For The Church 1:158 (1857).***{EVsw 272:3}*

Kiasi katika Mavazi—Tunakaribia mwisho wa historia ya dunia hii. Ushuhuda wa wazi na wa moja kwa moja unahitajika sasa, kama ulivyo katika Neno la **Mungu**, kuhusu kiasi katika mavazi. Hili linapaswa kuwa mzigo jukumu letu. Lakini tumchelewa sana sasa kuanza shauku ya kujaribu suala hili. Mavazi ya watu wetu yanapaswa kuwa rahisi sana.... Hakuna mtindo sahihi nilioonyeshwa kuwa ndio sheria kamili ya kuongoza wote katika mavazi yao.....*{EVsw 272:4}*

Dada zetu wanapaswa kuvaa mavazi sahili. Wanapaswa kuvaa kwa unyenyekevu na usahili. Kofia zenu na mavazi hayahitaji mapambo ya ya lesi za ziada yaliyowekwa (trimmings). Mnapaswa kuvaa mavazi ya heshima, yasiyo ya aibu na unyenyekevu. Wanapaswa kuionyesha dunia mfano ulio hai wa maisha yenye upendo wa **Mungu** ulio ndani. Hebu dada zetu wavae kwa unyenyekevu, kama wengi wanavyofanya, wakiwa na mavazi ya nyenzo nzuri, thabiti, ya kiasi, na yanayofaa kwa zama hizi, na suala la mavazi lisijaze akili. —**Manuscript 97, 1908.***{EVsw 273:1}*

Amri/Maagizo/Sakramenti

Nguzo Mbili Kuu za Ukumbusho

Agizo la ubatizo na Meza ya Bwana ni nguzo mbili kuu za ukumbusho—moja ndani ya kanisa na nyingine nje yake. Juu ya sheria hizi, Kristo ameandika Jina la **Mungu** wa Kweli. **—Manuscript 27 1/2, 1900.***{EVsw 273:1}*

Meza ya Bwana kama Ukumbusho Endelevu

Ishara za nyumba ya Bwana ni rahisi na zinaeleweka kwa uwazi (sacraments, emblems), na Kweli zinazowakilishwa nazo zina umuhimu wa kina sana kwetu. Katika kuanzisha ibada ya huduma za ushirika mtakatifu kuchukua nafasi ya Pasaka (Meza ya Bwana), Kristo aliliachia kanisa Lake ukumbusho wa dhabihu Yake kuu kwa ajili ya mwanadamu.*{EVsw 273:2}*

"*Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu*," Alisema. Huu ulikuwa wakati wa mpito kati ya taratibu mbili na sherehe zao mbili kuu. Moja ilifungwa milele; nyingine, ambayo Kristo alikuwa ameianzisha tu, ilikuwa ichukue nafasi yake na kuendelea hadi mwisho wa wakati kama ukumbusho wa kifo Chake.*{EVsw 273:3}*

—Review and Herald, Juni 22, 1897

Kutawadhana Miguu—Ni Zaidi ya Taratibu Tu

Hatuji kufanya taratibu za Maagizo ya Bwana katika nyumba ya Bwana kama desturi tu.....*{EVsw 274:1}*

Yeye Ameanzisha ibada hii ili izungumze kila mara na hisia zetu juu ya upendo wa **Mungu** ulioonyeshwa kwa ajili yetu. Ibada hii haiwezi kurudiwa bila wazo moja kuunganika na lingine. Hivyo mnyororo wa mawazo huamsha kumbukumbu za baraka, wema, na neema kutoka kwa marafiki na ndugu ambazo zilikuwa zimesahaulika. Roho Mtakatifu, kwa nguvu Yake ya kuhuisha, huonesha ukosefu wa shukrani na upungufu wa upendo uliotokana na chimbuko ovu la uchungu. Kila kiungo cha mnyororo wa kumbukumbu huimarishwa. Roho wa **Mungu** hufanya kazi juu ya akili za wanadamu. Mapungufu ya tabia, uzembe wa wajibu, na ukosefu wa shukrani kwa **Mungu** hurejeshwa kwenye kumbukumbu, na mawazo huletwa matekani kwa Kristo. —**Review and Herald, June 7, 1898.** *{EVsw 274:2}*

Maandalizi ya Moyo

Katika siku za mwanzo za vuguvugu la marejeo, tulipokuwa wachache, tulisherehekea tafrija/sherehe hizi lilikuwa tukio lenye faida kubwa. Ijumaa kabla ya ibada hiyo, kila mshiriki wa kanisa alijitahidi kuondoa kila jambo ambalo lingesababisha utengano kati yake na ndugu zake au na **Mungu**. Mioyo ilichunguzwa kwa undani; sala za kuomba ufunuo wa Kiungu juu ya dhambi zilizofichika zilitolewa kwa bidii; kukiri kwa tamaa ya kupita kiasi katika biashara, maneno ya haraka yasiyofikiriwa, na dhambi zilizolindwa vilifanywa. Bwana alikuja karibu, na tulitiwa nguvu na kutiwa moyo sana. —**Manuscript 102, 1904.** *{EVsw 274:3}*

Kusudi la Ibada ya Huduma

Kupatana kati ya ndugu ni kazi ambayo ibada ya kuoshana miguu ilianzishwa kwa ajili yake. Kwa mfano wa Bwana wetu na Mwalimu, ibada hii ya kujinyenyekeza imefanywa kuwa agizo/sheria takatifu. Kila mara inapotekelezwa, Kristo Yupo kwa njia ya Roho Wake Mtakatifu. Ni Roho huyu Ndiye anayewaletea watu msukumo wa usadikisho moyoni.*{EVsw 275:1}*

Kristo alipoadhimisha ibada hii pamoja na wanafunzi Wake, msukumo wa moyoni unaosadikisha (ukichunguza makosa, mema na kuleta tafakari moyoni nk*) uliwagusa wote isipokuwa Yuda. Vivyo hivyo, tutaguswa katika chemichemi za mioyo yetu tunaposikia sauti ya Kristo. Vyanzo vya roho vitavunjwa, yaani kutakuwa na mwamko wa kiroho na usadikisho wa moyo kwa yale tunayoyafanya vyema au vibaya. Akili itachangamka na kuamka, ikivunja kila kizuizi kilichosababisha migawanyiko na uadui. Dhambi zilizotendwa zitaonekana kwa uwazi zaidi kuliko wakati mwingine wowote; kwa kuwa Roho Mtakatifu atazileta kwenye kumbukumbu zetu. Maneno ya Kristo, **"Yohana 13:17** Mkiyajua hayo, heri ninyi mkiyatenda." yatavikwa kwa nguvu mpya. —**Review and Herald, November 4, 1902 (*will bring conviction of heart.** *The phrase "the fountains of the soul will be broken up" means a person is experiencing a profound emotional and spiritual awakening or conviction* **).** *{EVsw 275:2}*

Kipimo cha Moyo

Ibada hii ya kutawadhana miguu ilifanywa kuwa huduma ya kidini/kiroho... Ilitolewa kama kipimo cha uaminifu kwa watoto wa **Mungu**. Waisraeli wa leo wanaposhiriki ibada ya ushirika mtakatifu, ibada hii inapaswa kuwakilisha alama za kifo cha Bwana.*{EVsw 275:3}*

Ibada hii ilitolewa kwa faida ya wanafunzi wa Kristo. Na Kristo alikusudia maana kamili ya Maneno Yake aliposema:

"Yohana 13:15, *Kwa kuwa nimewapa kielelezo; ili kama Mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo. Mkiyajua hayo, heri ninyi mkiyatenda*." Alikusudia kwa njia hii kujaribu hali ya Kweli ya moyo na akili ya wale wanaoshiriki. —**Manuscript 8, 1897.** *{EVsw 275:4}*

Kwa Wakati Wote na Katika Kila Taifa

Badala ya sherehe ya kitaifa waliyoishika Wayahudi, Kristo alianzisha huduma ya ukumbusho/kumbukizi—ibada ya kutawazana miguu na Meza Takatifu—ili ishikwe kwa wakati wote na wafuasi Wake katika kila taifa.*{EVsw 275:5}*

Ibada hii inapaswa kurudiwa daima ili watu wote waone kwamba huduma ya Kweli inahitaji huduma isiyo na ubinafsi. **—The Signs of the Times, Mei 16, 1900.** *{EVsw 276:1}*

Iwe Kumbukumbu ya Mara kwa Mara

Katika tendo hili la mwisho la Kristo la kushiriki mkate na divai pamoja na wanafunzi Wake, Yeye Alijitoa kwao kama Mkombozi wao kwa Agano Jipya, lililoandikwa na kutiwa muhuri kwamba kila anayempokea Kristo kwa imani, atapokea baraka zote za mbinguni, hapa duniani na katika maisha yajayo ya kutokufa, yaani milele.*{EVsw 276:1}*

Agano hili lilipaswa kuthibitishwa kwa damu ya Kristo Mwenyewe, ambayo dhabihu za zamani zilikuwa kivuli Chake, na hivyo kuweka kumbukumbu kwa watu Wake waliochaguliwa. Kristo alikusudia kwamba huduma hii ya ushirika mtakatifu ifanywe kumbukizi ya mara kwa mara ili kukumbusha kafara Yake kwa ajili ya msamaha wa dhambi za wote wanaomwamini na kumpokea. Ibada hii inajumuisha kila mtu, na siyo ya watu wachache tu, kama wengine wanavyofanya. Kila mmoja anapaswa kushiriki hadharani, akitangaza: "Nampokea Kristo kama Mwokozi wangu binafsi. Alitoa maisha Yake kwa ajili yangu ili niokolewe kutoka mauti." —**Review and Herald, June 22, 1897.** *{EVsw 276:2}*

Uzoefu: Kumshughulikia MchungajiAliyevutiwa

Asubuhi ya Sabato, wakati kanisa la _____ liliposhiriki ibada hizi, ndugu _____ alikuwepo. Alialikwa kushiriki katika ibada ya kuoshana miguu, lakini akasema angependa kutazama tukio hilitu. Aliuliza ikiwa kushiriki katika ibada hii ni sharti kabla ya kushiriki Meza ya Bwana, na ndugu zetu walimhakikishia kuwa sio lazima, na kwamba anakaribishwa kwenye Mezani ya Bwana. Sabato hii ilikuwa siku ya thamani sana kwa roho yake; alisema hajawahi kuwa na siku ya furaha kama hiyo maishani mwake.*{EVsw 276:3}*

Baadaye alitaka kuzungumza nami, na tukawa na mazungumzo mazuri. Mazungumzo yake yalivutia sana, na tukawa na kipindi kizuri cha maombi ya pamoja. Ninamwamini kuwa ni mtumishi wa **Mungu**. Nilimpa vitabu vyangu Pambano Kuu (The Great Controversy), Wazee na Manabii (Patriarchs and Prophets), na Njia Salama (Steps to Christ). Alionekana kufurahia sana, akasema anatamani kupata nuru yote atakayoweza ili aweze kuwajibu wapinzani wa imani yetu. Alibatizwa kabla ya kurudi nyumbani, na atarejea kuwasilisha Kweli kwa kanisa lake mwenyewe. —**Letter 23a, 1893.** *{EVsw 277:1}*

Si Ushirika wa faragha, wa Watu fulani Kujifungia

Mfano wa Kristo unakataza ubaguzi katika Meza ya Bwana. Ni kweli kwamba dhambi ya wazi humtenga mwenye hatia. Hili Roho Mtakatifu hufundisha kwa uwazi. Lakini zaidi ya hapo hakuna mtu anayepewa mamlaka ya kutoa hukumu. **Mungu** hajamwachia mwanadamu kuamua nani anayepaswa kushiriki katika ibada hizi. Maana ni nani awezaye kusoma moyo? Nani awezaye kutofautisha magugu na ngano? —**The Desire of Ages, uk. 656 (1898).** *{EVsw 277:2}*

Wanaweza kuingia miongoni mwenu watu ambao mioyo yao haijaungana na Kweli na utakatifu, lakini wanatamani kushiriki katika ibada hizi. Msiwazuie. —**Manuscript 47, 1897,** *{EVsw 277:3}*

Kwa Kicho na Uchaji Mungu

Kila jambo linalohusiana na ibada hii linapaswa kuonyesha maandalizi bora kadri iwezekanavyo. Kila Agizo na ibada ya kanisa inapaswa kuinua roho. Hazipaswi kufanywa kama vitu vya kawaida au rahisi/hafifu, au kuwekwa katika kiwango cha mambo ya kawaida... Makanisa yetu yanahitaji kufundishwa kuwa na kiwango cha juu zaidi cha kicho na uchaji kwa huduma takatifu ya **Mungu**. —**Manuscript 76, 1900.** *{EVsw 277:4}*

Ibada hii haipaswi kufanywa kwa uzembe, wala ulegevu bali kwa bidii, tukikumbuka kusudi Lake. (not to be cheap) —**Manuscript 8, 1897.** *{EVsw 278:1}*

Mkutano Uliojaa Baraka

Siku hii imekuwa kipindi cha thamani sana kwa roho yangu. Kundi hili dogo limeandikishwa kama kanisa-limepangwa, na nilikutana nao kushiriki ibada hizi. Nilihubiri kutoka **Yohana 13**, na mawazo ya thamani yalivutia akili yangu kuhusu ibada ya unyenyekevu..... Kuna mengi katika ibada hii rahisi yasiyoonekana wala kuthaminiwa. Nilibarikiwa niliposhiriki ishara za mwili uliovunjwa na damu iliyomwagika ya Mwokozi wetu mpendwa, ambaye alifanywa kuwa dhambi kwa ajili yetu ili tupate kuhesabiwa haki na **Mungu** katika Yeye. Yeye Ndiye aliyebeba dhambi zetu.*{EVsw 278:2}*

Mkutano wa leo ulikuwa tukio la adhimu kubwa kwa wote waliokuwepo. Mkutano wa ushuhuda ulikuwa bora sana. Kila jina la mtu lililotajwa mtu huyo alijibu kwa hiari yake mwenyewe. Najua kuwa Bwana Yesu alikuwa katikati yetu, na mbingu yote ilifurahia tulipofuata mfano wa Kristo. Katika nyakati kama hizi, Bwana hujifunua kwa namna ya pekee ili kulainisha na kunyenyekeza roho, kuondoa ubinafsi, kutamalaki kwa Roho Wake Mtakatifu, na kuleta upendo, neema na amani ndani ya mioyo iliyopondeka.*{EVsw 278:3}*

Mkutano ulipofungwa na tukarejea hemani mwetu, ushawishi mtamu, mwororo, laini, mtakatifu, ulitanda mioyoni mwetu. Nafsi yangu ilijaa amani tamu. —**Manuscript 14, 1895.** *{EVsw 278:4}*

SEHEMU YA 9 — KUSHIKILIA MVUTO

Kuhubiri kwa Maamuzi ya Mwisho

Kwa Mafundisho Rahisi—Si kwa Ufasaha wa Maneno

Yeye ambaye katika mahubiri yake hufanya ufasaha kuwa lengo kuu, husababisha watu kusahau Ukweli uliomo katika usemi wake wa kuvutia. Mihemko au hisia zinapopita, itabainika kuwa Neno la **Mungu** halijachukua mizizi akilini, wala wasikilizaji hawajapata uelewa wa kweli. Wanaweza kusifia ufasaha wa mhubiri, lakini hawajasogea karibu na uamuzi wa kiroho. Wanalizungumzia somo kama mchezo wa kuigiza, na mhubiri kama mwigizaji. Wanaweza kurudi kusikiliza mahubiri ya aina hiyo, lakini wataondoka bila kuguswa moyo wala kulishwa kiroho.*{EVsw 279:1}*

Sio mahubiri yenye maneno ya kupendeza bila maana tunayohitaji, bali ni mafundisho yanayosaidia watu kushika Ukweli wa uzima. —**Gospel Workers, uk. 153, 154 (1915).***{EVsw 279:2}*

Nafsi Zisizofanya Maamuzi Katika Kila Mkutano

Kuna roho katika kila kusanyiko ambazo zinasita, karibu kushawishika kuwa kwa **Mungu** kikamilifu. Uamuzi unafanywa kwa ajili ya wakati na kwa ajili ya milele; lakini mara nyingi mhubiri hana roho na nguvu ya ujumbe wa Kweli moyoni mwake, hivyo hakuna mwito wa moja kwa moja kwa wale wanaositasita katika maamuzi kwaajili ya kumchagua Mwenyezi Mungu. Matokeo yake ni kwamba mvuto haupenyi mioyo ya walioguswa; nao huondoka katika mkutano wakiwa na mwelekeo mdogo zaidi wa kumkubali Kristo kuliko walivyokuja. Huamua kusubiri wakati mwafaka zaidi—lakini kamwe hauji. —**Testimonies for the Church, 4:447 (1880).***{EVsw 279:3}*

Wengine Wanasikiliza Mahubiri ya Mwisho

Wengine huenda wanasikiliza mahubiri ya mwisho watakayowahi kusikia, na baadhi hawatapata tena nafasi ya kuwasilishwa mnyororo wa ile Kweli na kuambiwa umuhimu wake kwa mioyo yao. Fursa hiyo ya thamani/dhahabu ikipotea, imepotea milele. Kama Kristo na upendo Wake wa ukombozi vingetukuzwa pamoja na mafundisho ya Kweli, ingeweza kuwafanya kuwa tayari kumfuata Mwokozi. —**Testimonies for the Church, 4:394 (1880).***{EVsw 280:1}*

Mwito Katika Kila Hubiri

Akiwa na upako wa Roho Mtakatifu juu yake, na mzigo kwa ajili ya roho za watu, mhubiri hatawaaga wasikilizaji wake kabla ya kumtangaza Yesu Kristo, kimbilio pekee la wenye dhambi, akitoa mwito wa dhati utakaogusa mioyo yao. Ajisikie kuwa huenda hatawaona tena hadi siku ile kuu ya **Mungu**. —**Testimonies for the Church, 4:316 (1879).***{EVsw 280:2}*

Katika kila hotuba, miito ya bidii inapaswa kutolewa kwa watu kuuacha dhambi na kumgeukia Kristo. —**Testimonies for the Church, 4:396 (1880).***{EVsw 280:3}*

Mwito wa Maamuzi

Katika mikutano yetu ya makambi, juhudi za uamsho zimekuwa chache mno. Kuna kutafuta uso wa Bwana kwa kiwango kidogo sana. Ibada za uamsho zinapaswa kuendelea tangu mwanzo hadi mwisho wa mkutano. Juhudi za dhati na zenye kuazimiwa kabisa zinapaswa kufanywa ili kuwahamasisha watu. hebu watu waone kuwa uko makini kwa sababu una ujumbe wa ajabu kutoka mbinguni. Waambie kuwa Bwana anakuja kwa hukumu, na kwamba hakuna mfalme wala mtawala, mali wala ushawishi, vitakavyoweza kuzuia hukumu zitakazoanguka hivi karibuni. Mwisho wa kila mkutano unapaswa kutoa mwito wa maamuzi. —**Testimonies for the Church, 6:64, 65 (1900).***{EVsw 280:4}*

Kweli ya Sabato Itangazwe kwa Ujasiri

Ni wakati huu ambapo Sabato ya Kweli inapaswa kutangazwa kwa watu kwa kalamu na sauti. Wakati amri ya nne ya Amri Kumi na wale wanaoishika wanapopuuzwa na kudharauliwa, wale waaminifu wachache wanajua kwamba huu si wakati wa kuficha nyuso zao bali ni kuinua sheria ya Yehova kwa kufungua bendera iliyoandikwa ujumbe wa malaika wa tatu, "*Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za **Mungu**, na imani ya Yesu.*" (**Ufunuo 14:12**). *{EVsw 281:1}*

Kweli haipaswi kufichwa, haipaswi kukataliwa wala kufichwa kwa hila, bali ikiriwe kikamilifu na kutangazwa kwa ujasiri. **—Letter 3, 1890.***{EVsw 281:2}*

Mielekeo Miwili ya Kuathiri Maamuzi

Kuna misimamo miwili mikali ya kuepukwa: Wa kwanza ni kuepuka kutangaza mashauri yote ya **Mungu**, na kukimbilia roho ya watu wa uamsho wa wakati huu wa kilio, "Amani, amani; wakati hakuna amani," na kuchanganya huduma na kipengele cha kuchochea hisia bila kuleta mabadiliko ya moyo.*{EVsw 281:3}*

Ya Pili ni Kupitiliza, ni kuwa mtu wa kukaripia kila mara kwa ukali (unashusha vimbunga na mijeledi tu), na kwa njia isiyo ya Kristo, kiasi cha kuwafanya watu wahisi kuwa umeudhika. —**Letter 43, 1886.***{EVsw 281:4}*

Uwasilishaji wa Mchungaji/Mhubiri Unaweza Kuvuruga Maamuzi

Toka zamani kazi ya Ndugu _____ imeonyeshwa kwangu kwa taswira-michoro au chati. Ilionekana kana kwamba alikuwa anawapa watu chombo kilichojaa matunda mazuri sana, lakini alivyokuwa akiwapa, mtazamo wake na namna yake ya kuwasilisha ilikuwa ya kuwatisha kiasi kwamba hakuna aliyetaka kutwaa mafundisho haya. Vivyo hivyo imekuwa kwa zile Kweli za kiroho anazowasilisha. Katika uwasilishaji wake wa Kweli hizi, mara nyingine hutokea roho isiyotoka mbinguni. Husema maneno, hukemea kwa nguvu ya kushinikiza, kiasi cha kuwafanya watu wageuke mbali na Kweli nzuri alizo nazo.*{EVsw 281:5}*

Nimemuona Ndugu _____ wakati Roho ya **Mungu** ya huruma ilipokuwa juu yake. Upendo wake kwa zile Kweli ulikuwa wa dhati kabisa, na sio madai ya mdomoni tu. Alikuwa ameukuza na kuushikilia upendo huo, na bado upo moyoni mwake. Lakini ndugu yetu hana namna nzuri ya kuonyesha huruma nyororo, upole, na roho ya upendo wa Kristo. Anahitaji mafuta matakatifu yanayotiririka kutoka kwenye mifereji ya dhahabu kuingia mioyoni mwa wanadamu. Mafuta haya yaujaze moyo wake, na atakapoyapokea, Roho wa **Mungu** itakuwa juu yake. —**Manuscript 120, 1902.***{EVsw 282:1}*

Kukataa Nuru ni Jambo Zito

Wakati mtu anapopuuzia usadikisho wa Bwana moyoni mwake, na kukataa ushahidi wa Ukweli, mwanadamu analazimika kuchukua msimamo wa upinzani wa wazi na ukaidi wa makusudi. —**Manuscript 13, 1892.***{EVsw 282:2}*

Kazi ya Dhati na Bidii kwa Ajili ya Nafsi (wanadamu)

Fanya kazi kwa ajili ya wokovu wa roho kana kwamba kwa macho unaona uko mbele ya ulimwengu mzima wa mbinguni. Malaika wote wa utukufu wana nia katika kazi ya wokovu wa roho. Hatujaamka kama tunavyopaswa. Jeshi lote la malaika ni wasaidizi wetu. "**Zefania 3:17** *BWANA, **Mungu** wako, Yu katikati yako shujaa awezaye kuokoa; Atakushangilia kwa furaha kuu, Atakutuliza katika upendo Wake, Atakufurahia kwa kuimba*." Je, hatuwezi basi kufanya kazi kwa ujasiri na imani? "**Zefania 3:16 Katika siku ile Yerusalemu utaambiwa, Usiogope, Ee Sayuni; mikono yako isilegee**." Uwe na imani tu. Omba na amini, nawe utaona wokovu wa **Mungu**. —**Letter 126, 1896.***{EVsw 282:3}*

Mialiko na Wito wa Madhabahuni

Kuhimiza Nafsi Kuchukua Uamuzi

Ni kazi ya Roho Mtakatifu kuishawishi nafsi kutambua haja yake ya Kristo. Wengi hushawishika kuhusu dhambi, na huhisi haja yao ya Mwokozi anayesamehe dhambi; lakini mara nyingi hawaridhiki tu na malengo yao ya awali, na kama Ukweli hautaelekezwa kwa moyo wao kwa namna ya wazi, kama hakuna maneno yanayonenwa kwa wakati ufaao, kuwataka kufanya uamuzi kwa misingi ya ushahidi uliowasilishwa, wale walioguswa hupita tu bila kujiunganisha na Kristo. Fursa ya thamani na ya pekee hupita, nao hawajajisalimisha kwa Mwenyezi Mungu, na kisha huendelea kujitenga mbali zaidi na ile Kweli, mbali na Yesu, na kamwe hawachukui msimamo upande wa Bwana.*{EVsw 283:1}*

Sasa, mhubiri hastahili kuwasilisha Neno la **Mungu** tu kwa namna ya kuonesha dhambi kijumla, bali anapaswa kumwinua Kristo mbele ya wasikilizaji wake. Dai la Kristo juu yao linapaswa kufafanuliwa waziwazi. Watu wanapaswa kuhamasishwa kufanya uamuzi sasa hivi wa kuwa upande wa Bwana. — **Letter 29, 1890.***{EVsw 283:2}*

Kuhamasisha na Kupata Mwitikio wa Wasikilizaji

Mzee _____ amefanikiwa sana katika mfululizo huu wa mikutano. Njia yake imekuwa ni kutumia Maandiko kufafanua Maandiko; na Roho Mtakatifu ameshawishi mioyo mingi kuukubali Ukweli. Watu hawawezi kupinga

kauli iliyo wazi: ya “Hivi ndivyo Asemavyo Bwana.....” Amefundisha tu wakati wa jioni, wakati watu wamemaliza kazi zao na wanaweza kuhudhuria. Baada ya wiki chache za kazi, aliwasilisha Kweli ya Sabato, tena akiithibitisha kila kauli kwa Maandiko.*{EVsw 283:3}*

Mkutano wa kwanza wa Sabato ulifanyika ndani ya hema kubwa. Baada ya Mzee _____ kumaliza kuzungumza, kulikuwa na mkutano wa kijamii, kisha aliwaalika wote waliokuwa wameshawishika kuhusu ukweli na waliodhamiria kuchukua msimamo wa kulitii Neno la **Mungu**, wasimame. Watu hamsini waliitikia; majina yao yalichukuliwa na mkutano ukaandaliwa ili watoe ushuhuda wao. Wengi walitoa maneno bora na yenye nguvu katika kushuhudia.*{EVsw 283:4}*

Baada ya wiki kadhaa kupita, mwito mwingine ulitolewa kwa wale waliokuwa wameamua kuitii Kweli. Watu kati ya ishirini na tano na thelathini waliitikia. Wachungaji kadhaa walihudhuria mkutano huo na walitoa ushuhuda wa baraka. — **Letter 372, 1906.***{EVsw 284:1}*

Mwitikio wa Wasikilizaji Juu ya Ukweli Katika Vuguvugu la 1844

Hivi ndivyo Ukweli ulivyohubiriwa mwaka 1842, 1843 na 1844..... Hapakuwa na maneno yasiyo ya lazima yaliyotamkwa na mhubiri, bali Maandiko yaliwasilishwa kwa uwazi. Mara nyingi mwito ulitolewa kwa wale waliouamini Ukweli uliothibitishwa na Neno, wasimame, na makundi makubwa waliitikia. Maombi yaliombwa kwa ajili ya wale waliotamani msaada wa kipekee. — **Manuscript 105, 1906.***{EVsw 284:2}*

Kutambua Ishara Mpya za Usadikisho

Kwa ndugu zangu wahubiri, ningependa kusema: Kila ishara mpya ya kushawishiwa kwa neema ya **Mungu** juu ya nafsi za wasioamini ni ya kiungu. Kila kitu unachoweza kufanya ili kuwaleta watu kwenye maarifa ya Kweli, ni njia ya kuruhusu mwanga wa utukufu wa **Mungu** uangaze, kama unavyong’aa katika uso wa Yesu Kristo. Elekeza fikra kwa Yeye anayeelekeza na kutawala mambo yote. Kristo atakuwa mana na umande wa kiroho kwa hizi nafsi mpya zilizoongoka. Ndani Yake Yeye hakuna giza kabisa. Kwa Kadiri watu wenye uelewa wa kiroho wanapofanya masomo ya Biblia na watu hawa, wakiwafundisha jinsi ya kujisalimisha kwa Roho Mtakatifu ili waweze kuimarishwa kabisa katika Kweli, nguvu ya **Mungu** itadhihirika. — **Manuscript 105, 1906.***{EVsw 284:3}*

Mialiko ya Mara kwa Mara ya Hadhara

Vua kabisa sura ya kutojali, na waonyeshe watu kwamba maisha au mauti yapo katika maswali haya ya muhimu, kulingana na jinsi watakavyoyapokea au kuyakataa. Unapowasilisha Kweli zinazojaribu mioyo ya watu, uliza mara kwa mara: “Ni nani sasa aliye tayari, baada ya kusikia Maneno ya **Mungu** yanayoeleza wajibu wake, kutakasa moyo na nia yake, pamoja na mapenzi yake yote, kwa Kristo Yesu?” — **Letter 8, 1895.***{EVsw 284:4}*

Kuzungumza Binafsi na Watu Wanaouliza Maswali

Baada ya mikutano kumalizika, pawe na mazungumzo ya kibinafsi na kila mmoja aliyehudhuria. Kila mtu aulizwe jinsi atakavyopokea mambo hayo na kwenda nayo, kama atayafanya yawe yake binafsi katika mtindo wa maisha yake halisi. Kisha uchunguze na uone kama mtu huyu au yule anaonyesha shauku. Maneno matano yaliyosemwa kwa mtu binafsi yataweza kuwa na athari kubwa kuliko hotuba yote. — **Manuscript 19b, 1890.***{EVsw 285:1}*

Roho Mtakatifu Huifanya Miito Kuwa na Nguvu

Kama utamtafuta Bwana, ukiweka mbali maneno yote ya uovu na ubinafsi wote, na kuendelea kuwa na moyo wa maombi, Bwana atakukaribia. Ni nguvu ya Roho Mtakatifu inayotoa ufanisi kwa juhudi zako, mwito na kusihi kwako. Jinyenyekeze mbele za **Mungu**, ili kwa nguvu Zake uweze kuinuka hadi kiwango cha juu zaidi. — **Manuscript 20, 1905.***{EVsw 285:2}*

Upendo wa Yesu Huigusa Mioyo

Mungu na Mwanawe mpendwa lazima wawasilishwe mbele ya watu kwa utajiri wa upendo waliouonyesha kwa mwanadamu. Ili kubomoa vizuizi vya chuki na kutotubu, upendo wa Kristo lazima uwe sehemu ya kila mahubiri. Waonyeshe watu jinsi Yesu anavyowapenda, na ni uthibitisho gani aliowapa wa upendo Wake. Ni upendo gani unaweza kuulinganishwa na ule **Mungu** aliouonyesha kwa mwanadamu kupitia

kifo cha Kristo msalabani? Moyo ukijazwa na upendo wa Yesu, huo upendo unaweza kuwasilishwa kwa watu na utaathiri mioyo yao. **— Letter 48, 1886.** *{EVsw 285:3}*

Kuzisaidia Nafsi Ziongoke na Kuokolewa

Uzoefu wa Uongofu wa Kweli

Nimeonyeshwa kuwa wengi wana mawazo yaliyochanganyikana kuhusu uongofu. Mara kwa mara watu wamesikia maneno yakirudiwa kutoka mimbarini: "Imewapasa kuzaliwa mara ya pili," na "Lazima muwe na moyo mpya." Maneno haya yamewachanganya, kwa kuwa hawakuweza kuufahamu mpango wa wokovu. *{EVsw 286:1}*

Wengi wamejikuta wakiangamia kwa sababu ya mafundisho potofu ya baadhi ya wahubiri kuhusu mabadiliko yanayotokea wakati wa uongofu. Baadhi ya watu wameishi kwa huzuni kwa miaka mingi, wakingoja alama au ushahidi fulani wa pekee kuwa wamekubaliwa na **Mungu**. Ingawa wamejitenga kwa kiasi kikubwa na mambo ya kidunia, na hupendezwa na ushirika wa watu wa **Mungu**, ila bado wanaogopa kuungama kuwa ni wa Kristo kwa sababu huona kuwa ni ujuvi au kujigamba mno kusema kuwa wao ni watoto wa **Mungu**. Wanangojea mabadiliko ya kipekee ambayo wameelekezwa kuamini kwamba yanahusiana na uongofu. *{EVsw 286:2}*

Baada ya muda, baadhi yao hupokea ushahidi wa kukubalika kwao na **Mungu**, na kisha huamua kujiunga na watu Wake, na hapo ndipo huamini kuwa ndipo mwanzo wa uongofu wao. Lakini nimeonyeshwa kwamba walikuwa tayari wamekwisha kupokelewa katika familia ya **Mungu** kabla ya hapo. **Mungu** aliwakubali walipochoshwa na dhambi, walipoacha tamaa ya anasa za dunia, na kuamua kumtafuta **Mungu** kwa dhati, kwa moyo wote. Hata hivyo, kwa kutokuelewa unyofu wa mpango wa wokovu, walikosa baraka nyingi ambazo wangezipata kama tu wangeliamini tangu mwanzo kuwa **Mungu** aliwakubali. *{EVsw 286:3}*

Wengine huangukia kwenye kosa hatari zaidi. Huongozwa na hisia. Hukorogwa au kuwa na mihemko ya huruma au hisia za haraka, na hudhani kuwa hali hiyo ni ushahidi kwamba wamekubaliwa na **Mungu** na wameongoka. Lakini kanuni za maisha yao hubaki vilevile. Uthibitisho wa kazi ya Kweli ya neema moyoni hupatikana si katika hisia, bali katika maisha ya mtu. Kristo alisema: "*Mtawatambua kwa matunda yao*." *{EVsw 286:4}*

Wengi wenye dhamira safi ya kuwa WaKristo wa kweli bado wanazunguka gizani, wakingoja hisia zao ziguswe kwa nguvu. Wanatarajia nguvu fulani ya ajabu ambayo haiwezi kuzuiliwa iwashukie na kisha watekewe. Wanapuuza Ukweli kuwa muumini wa Kristo anatakiwa kuufanyia kazi wokovu wake kwa hofu na kutetemeka.*{EVsw 287:1}*

Mwenye dhambi ambaye amesadikishwa dhambi, hana budi kutubu tu; bali pia anapaswa kuchukua hatua na kuamini kwamba **Mungu** amekubali toba Yake, kama Yeye alivyoahidi: "**Waebrania 11:6** *Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye **Mungu** lazima aamini kwamba Yeye Yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao*. *{EVsw 287:2}*

Kazi ya neema moyoni si kazi ya ghafla, bali ni matokeo ya uangalizi wa kila siku na kuamini ahadi za **Mungu**. Yule atubuye kwa dhati, na anayeamini kwa moyo wote, ambaye hudumu katika imani na kutamani kwa moyo neema ya Kristo ya kufanywa upya, **Mungu** hawezi kumwacha mikono mitupu. Atampa neema, na malaika wahudumu watamsaidia anapoendelea kwa dhati na bidii katika juhudi zake za kiroho. **Manuscript 55, 1910.** *{EVsw 287:3}*

Uongofu—Sio Wote Hufanyika kwa Njia Moja

Uongofu Hauko Kwa Njia Moja Tu

Watu wote hawakuumbwa kwa namna moja, na hivyo basi, uongofu hauwezi kuwa wa namna moja kwa wote. Yesu huugusa moyo, na mwenye dhambi huzaliwa upya katika maisha mapya. Mara nyingi roho huvutwa kwa Kristo bila kuwa na mshituko mkubwa wa dhamira, bila maumivu makali ya nafsi, wala bila hofu kubwa ya kuangamizwa. Walimtazama Mwokozi aliyeinuliwa, nao wakaishi. Walitambua haja ya roho yao, wakaona kutosha kwa Mwokozi na madai Yake juu yao. Wakasikia sauti Yake ikisema, "Nifuate," nao wakaondoka na kumfuata. Uongofu huu ulikuwa wa dhati- kweli, na maisha yao ya kiroho yalikuwa dhabiti sawasawa na yale ya wale waliopitia mateso na msukosuko mkubwa wa nafsi. —**Letter 15a, 1890.** *{EVsw 287:4}*

Uongofu Hauwezi Kufungiwa Katika Mpangilio wa Kibinadamu

Wale wanaopanga kwa usahihi ni kwa namna gani ibada au kazi ya kiroho inapaswa kufanyika, na ambao ni makini mno kwa mtindo na mpangilio katika kusambaza nuru na neema wanayodhani kuwa nayo, hawa wanaonekana kutokuwa na Roho Mtakatifu kwa kiwango kikubwa…….*{EVsw 288:1}*

Ingawa hatuwezi kumwona Roho wa **Mungu**, tunajua kuwa watu waliokuwa wafu katika makosa na dhambi hufikia hali ya kusadikishwa na kuongoka kupitia kazi ya Roho huyo. Wale waliokuwa watu wasiojali, na waasi, hugeuka kuwa makini; wenye mioyo migumu hutubu dhambi zao; wasio na imani huja kuamini. Mcheza kamari, mlevi, muasherati au mtu anayehusika na ngono chafu, —vyote vinaachwa, na waliojihusisha navyo hugeuka kuwa wastahivu, wanyofu, na safi. Wale waliokuwa waasi na wakaidi hubadilika na kuwa wapole na kufanana na Kristo.Tunapoyaona haya mabadiliko ya tabia, tunajua kwamba nguvu ya kuongoa ya **Mungu** imefanya kazi ya kumbadilisha kwa ujumla. Hatukumwona Roho Mtakatifu kwa macho, lakini tumeona ushahidi wa kazi Yake katika maisha ya waliokuwa wakorofi na wenye dhambi wagumu. Kama vile upepo unavyoangusha miti mirefu kwa nguvu zake, ndivyo Roho wa **Mungu** afanyavyo kazi katika mioyo ya wanadamu, na hakuna mwanadamu yeyote mwenye kikomoduniani anayeweza kuipima au kuiwekea kazi ya **Mungu** mipaka. *{EVsw 288:2}*

Roho Mtakatifu Hutenda Kazi Kwa Njia Tofauti Kwa Watu Tofauti. Roho wa **Mungu** hujitokeza kwa njia mbalimbali kwa watu tofauti. Mmoja, anapoguswa na nguvu hii, hutetemeka mbele ya Neno la **Mungu**. kusadikishwa kwa dhamira yake hujawa na mzigo mzito kiasi kwamba kuna dhoruba ya hisia ndani ya moyo wake, na nafsi yake yote hunyenyekea chini ya nguvu ya Ukweli inayoshawishi. Pale Bwana anaposema msamaha kwa roho hiyo yenye kutubu, hujawa na shauku kuu, na upendo kwa **Mungu**, unyofu na bidii ya kweli. Na Roho ya uhai aliyoipokea haiwezi kuzuiwa. Kristo Yumo ndani yake kama kisima cha maji chemchemi ikibubujika hata uzima wa milele. Upendo wake ni wa kina na wa dhati kama vile maumivu yake yalivyokuwa makali. Roho yake ni kama chemchemi ya vilindi vikuu iliyofunguliwa, na humiminika kwa shukrani na sifa, furaha na kuimba, hadi vinubi vya mbinguni vinapigwa kwa nyimbo za furaha. Ana ujumbe, kisa cha kushuhudia, lakini si kwa mtindo wa kawaida au kwa mpangilio wa kibinadamu. Yeye ni roho iliyokombolewa kwa damu ya Yesu Kristo, na nafsi yake yote inatikisika kwa utambuzi wa wokovu wa **Mungu**. —**The Review and Herald, May 5, 1896.** *{EVsw 288:3}*

Wengine Huletwa kwa Kristo kwa Njia ya Upole au kwa namna ya taratibu na utulivu. “Upepo huvuma upendavyo, na wausikia uvumapo, lakini hujui utokako wala uendako; ndivyo alivyo kila mtu aliyezaliwa kwa Roho.” Huwezi kuuona mkono unaotenda kazi, lakini unaweza kuona matokeo yake. Nikodemo alipomwuliza Yesu **Yohana 3: 9-10**, “*Yawezaje kuwa mambo haya?” Yesu akajibu, akamwambia, Je! Wewe u mwalimu wa Israeli, na mambo haya huyafahamu*?” Yaani, mtu ambaye ni mwalimu miongoni mwa wenye hekima, aliyejiona kuwa anaweza kufahamu sayansi ya dini, na bado anajikwaa katika fundisho la uongofu! Hakutaka kukubali Kweli kwa sababu hakuweza kuelewa kila kitu kuhusu kazi ya **Mungu-operesheni ya Mungu**. Na bado alikubali Ukweli wa maumbile ingawa hakuweza kuelezea wala kuelewa kikamilifu. Kama wengine wa nyakati zote, alikuwa anaangalia mitindo na taratibu za ibada kama mambo muhimu zaidi ya dini kuliko utendaji wa kina wa Roho wa **Mungu**. —**The Review and Herald, May 5, 1896.***{EVsw 289:1}*

Uongofu Hupelekea Kutii

Uongofu wa nafsi ya mwanadamu si jambo dogo. Ni muujiza mkuu kabisa unaofanywa kwa uwezo wa Kiungu. Matokeo halisi hupatikana kwa kumwamini Kristo kama Mwokozi binafsi. Mwenye dhambi aliyesamehewa hutakaswa kwa utiifu wa sheria ya **Mungu**, na anatakaswa kwa kuitunza Sabato Yake takatifu kwa uaminifu. Tukimtumaini **Mungu**, tukiendelea kuamini, tukiwa na subira na kujitahidi kwa bidii kuu kuufanyia kazi wokovu wake kwa “hofu na kutetemeka,” tutajifunza kuwa ni **Mungu** Mwenyewe atendaye kazi ndani yetu, kutaka Kwake na kutenda kwake sawasawa na mapenzi Yake. —**Manuscript 6, 1900.** *{EVsw 289:2}*

Utakatifu ni Kwa Kutenda Ukweli

Mwanadamu hapaswi tu kulisoma Neno la **Mungu**, huku akifikiri kuwa maarifa ya juu-juu tu ya Maandiko hayo yatafanya badiliko la tabia ndani yake. Kazi hii ya kutakasa huweza kufanywa tu na Yeye aliye Njia, Kweli, na Uzima. Inawezekana mtu kushikilia mafundisho sahihi kwa uthabiti, na kuyaeleza tena na tena, hata kufikiri kuwa tayari amejaa baraka kuu ambazo mafundisho hayo yanawakilisha. Lakini hata Kweli zilizo kuu na zenye nguvu zaidi zinaweza kushikiliwa kana kwamba ni za nje tu, zikiathiri kidogo sana maisha ya kila siku. Nafsi haitatakaswa kwa Kweli ambayo haitendwi-haifanyiwi kazi. —**Letter 16, 1892.** *{EVsw 290:1}*

Mafundisho au Ushirika wa Kanisa Havichukui Nafasi ya Uongofu

Watu wote, wawe wa hadhi ya juu au ya chini, iwapo hawajaongoka, wote wanasimama kwenye jukwaa moja. Mtu anaweza kubadili kutoka dhehebu moja hadi jingine—na hili linaendelea kufanyika, na litaendelea. Wakatoliki wanaweza kutoka katika Ukatoliki na kujiunga na Uprotestanti, lakini bado wanaweza kuwa hawjui maana ya Maneno haya: "*Nami nitawapa ninyi moyo mpya.*" (Ezekieli 36:26). Kupokea mafundisho mapya, na kujiunga na kanisa, hakuleti uzima mpya kwa yeyote, hata kama kanisa hilo limejengwa juu ya msingi wa Kweli. Kujiunga na kanisa/Ushirika wa kanisa hakuchukui nafasi ya uongofu wa kweli. Kujiweka sahihi kwenye kanuni ya imani ya kanisa hakufai kitu ikiwa moyo haujabadilika kweli. ***{EVsw 290:2}***

Tunahitaji zaidi ya imani ya akili mahiri, na busara, katika Ukweli. Wayahudi wengi walithibitishwa/kusadikishwa kuwa Yesu ni Mwana wa **Mungu**, lakini walikuwa na kiburi na tamaa ya madaraka kiasi kwamba hawakutaka kujisalimisha. Waliamua kuupinga Ukweli, na waliendelea kupinga. Hawakuupokea Ukweli moyoni kama ulivyo ndani ya Yesu. Wakati Ukweli unashikiliwa kama Ukweli wa dhamiri tu (akilini tu), bila kuamsha moyo au kuufanya upokee, basi akili peke yake ndiyo huathirika. Lakini Ukweli unapopokelewa kama Ukweli wa moyo, umepita ndani ya dhamiri na kuiteka nafsi kwa kanuni zake safi. Ukweli huo huwekwa moyoni na Roho Mtakatifu, ambaye hufunua uzuri wake ndani ya akili, ili nguvu yake ya kubadili ionekane katika tabia. —**The Review and Herald, February 14, 1899.*{EVsw 291:1}***

Uongofu Ni Matokeo ya Kazi ya Pamoja

Katika kuzirejesha roho zilizopotea na zinazoangamia, si mwanadamu ndiye anayefanikisha kazi ya kuwaokoa, bali ni **Mungu** anayefanya kazi pamoja naye. **Mungu** hufanya kazi, na mwanadamu hufanya kazi. "*Maana sisi tu watenda kazi pamoja na **Mungu**.*" **(1 Wakorintho 3:9).** Lazima tufanye kazi kwa namna mbalimbali na kubuni mbinu tofauti, tukimruhusu **Mungu** kutenda kazi ndani yetu katika kuufunua Ukweli na Yeye Mwenyewe kama Mwokozi anayesamehe dhambi. —**Letter 20, 1893.** ***{EVsw 291:2}***

Kumsaidia Mwenye Dhambi Kuvuka Mstari wa Ukombozi

Uwe tayari, wakati ukufaao na wakati usikuofaa, kuwaonya vijana, na kuwasihi wenye dhambi kwa upendo uleule ambao Kristo anao kwao. Wakati kilio kinapotoka kinywani mwa mwenye dhambi, "Ee dhambi zangu, dhambi zangu, naogopa kuwa ni nzito mno kusamehewa," uwe na imani. Mtukuze Yesu juu na juu zaidi, ukisema: "*Tazama Mwana-Kondoo wa **Mungu**, aichukuaye dhambi ya ulimwengu.*" **(Yohana 1:29).** Na kilio kinaposikika: "**Mungu** uniwie radhi mimi mwenye dhambi," elekeza roho hiyo inayotetemeka kwa Mwokozi anayesamehe dhambi kama kimbilio lake. —**Manuscript 138, 1897.** ***{EVsw 291:3}***

Malaika Hushangilia

Uongofu wa roho kwa **Mungu** ni kazi kuu kabisa, kazi ya hali ya juu zaidi ambayo wanadamu wanaweza kushiriki. Katika uongofu wa roho, huruma ya **Mungu**, uvumilivu, upendo Wake usio na mipaka, utakatifu Wake, na nguvu Zake vinafunuliwa. Kila uongofu wa kweli humtukuza **Mungu** na husababisha malaika kuimba kwa furaha: "Rehema na Kweli zimekutana; haki na amani zimebusiana." —**Letter 121, 1902.** ***{EVsw 292:1}***

Kuwakusanya Wale Wenye Shauku

Wengi Wakikazia Macho Mbinguni kwa Shauku —Ulimwenguni kote, wanaume na wanawake wanakazia macho mbinguni kwa shauku. Sala, machozi na maswali huinuliwa kutoka kwa nafsi zinazotamani nuru, neema, na Roho Mtakatifu. Wengi wapo kando-kando ya ufalme, wakingoja tu wakusanywe ndani. —**The Acts of the Apostles, 109 (1911).*{EVsw 292:2}***

Nendeni Kwa Ajili ya Waliopotea — Tunapojihusisha kwa moyo wote katika kazi hii, tunaunganishwa kwa karibu na malaika; sisi ni washiriki pamoja nao na Kristo katika kazi hii. Kuna ushirika wa Kiungu, wa juu, kati ya mbingu na sisi. Tunakuwa karibu na mbingu, karibu na majeshi ya malaika, karibu na Yesu. Hivyo basi, tushiriki katika kazi hii kwa bidii zetu zote. ***{EVsw 292:3}***

Msikate tamaa katika kazi hii. **Mungu** atatusaidia. Malaika watatusaidia; kwa sababu ni kazi yao, na ni kazi wanayotaka kututia moyo kuifanya.....***{EVsw 292:4}***

Hii ni kazi ambayo ni lazima tuishike kwa dhati na bidii; na unapoona kondoo aliyepotea, mwite arejee zizini; wala usimwache hadi uone yupo salama ndani ya zizi. Hebu Mbingu na iruhusu Roho aliyekuwa

ndani ya Bwana wetu wa Kiungu atutawale. Hili ndilo tunalohitaji. Anatuambia, **Yohana 15:12** "*Mpendane, kama Mimi nilivyowapenda ninyi.*" Nendeni kwa ajili ya kuwatafuta kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli. **—Undated Manuscript 141.**

Mshikeni Kristo, na Wavuteni Watu Kwake — Kwa mkono mmoja, watenda kazi wameushika mkono wa Kristo, na kwa mkono mwingine wanawashika wenye dhambi kuwavuta kwaMwokozi. — **Review and Herald, September 10, 1903.***{EVsw 293:1}*

Muwe na imani na tumaini, na wavuteni, naam, wavuteni watu (roho) kuja katika karamu ya Injili. — **Letter 112, 1902.***{EVsw 293:2}*

Huenda Msi-pate Kuwafikia Tena — Ni wajibu wetu kwa kiasi sawa kuangalia matokeo ya baada ya mikutano ya Injili kama tunavyoangalia mafanikio ya sasa, kwa sababu wakati mwingine mnaporudi, ikiwa waliguswa na kushawishika lakini hawakuitikia ushawishi huo, huwa vigumu zaidi kuwagusa tena kuliko ilivyokuwa awali, na huenda msiweze kuwafikia tena. — **Manuscript 19b, 1890.***{EVsw 293:3}*

Kupata watu Kufanya Maamuzi Sasa Yanakuwa Magumu — Katika siku zetu, ni jambo gumu kuwaongoza wale wanaodai kuamini Kweli kuipata kwa uzoefu wa uhai wake unaotakasa na kuhuisha. Hii imewahi kushuhudiwa miaka ya nyuma, lakini mfumo wa ibada umechukua nafasi ya nguvu yake, na unyofu wake umepotea katika mizunguko ya taratibu. — **Manuscript 104, 1898.***{EVsw 293:4}*

Mfano: Kukusanya Matunda Yaliyokomaa — Katika ndoto niliyoonyeshwa Septemba 29, 1886, nilikuwa nikitembea na kundi kubwa waliokuwa wakitafuta matunda ya beri (berries)..... Siku iliendelea, lakini kazi haikufanyika sana. Hatimaye nikasema: "Ndugu zangu, ninyi mnaona hii ni safari isiyo na mafanikio. Kama hivi ndivyo mnavyofanya kazi, sistajabu kuona hamfanikiwi. Mafanikio au kushindwa kwenu kunategemea jinsi mnavyoshughulikia kazi hii. Kuna matunda hapa; kwa maana mimi nimeyapata. Wengine wenu mmekuwa mkichunguza vichaka vya chini bure; wengine mmeona matunda machache; lakini mmeacha vichaka virefu kwa sababu hamkutarajia kupata matunda humo. Mnaona kwamba matunda niliyokusanya ni makubwa na yamekomaa. Hivi karibuni matunda mengine yatakomaa, na tunaweza kupitia vichaka tena. Hivi ndivyo nilivyofundishwa kukusanya matunda. Kama mngekuwa mmechunguza karibu na gari, mngeweza kupata matunda pia.....*{EVsw 293:5}*

"Bwana ameweka vichaka hivi vyenye matunda katikati ya maeneo yaliyojaa watu, Naye Anatarajia myapate. Lakini mmekuwa mkijishughulisha sana na kula na kujifurahisha wenyewe. Hamjaja shambani kwa nia ya dhati ya kupata matunda.....*{EVsw 294:1}*

"Kwa kufanya kazi kwa njia sahihi, mtawafundisha watendakazi vijana kwamba mambo kama kula na burudani au matumbuizo siyo ya muhimu sana. Ilikuwa kazi ngumu kuleta gari la ugavi wa chakula hapa, lakini mmelipa uzito mkubwa kuliko matunda mnayopaswa kupeleka nyumbani kama matokeo ya kazi yenu. Mnapaswa kuwa na bidii, kwanza kuvuna matunda yaliyo karibu, halafu kutafuta yaliyo mbali; baada ya hapo mnaweza kurudi na kufanya kazi karibu tena, na kwa njia hiyo mtafanikiwa." **— Gospel Workers, uk. 136-139 (1886).***{EVsw 294:2}*

Kupambana na Mungu Mieleka kwa Ajili ya Nafsi (Mwanzo 32) — Ikiwa tutakuwa na shauku kama aliyokuwa nayo John Knox alipoomba mbele za **Mungu** kwa ajili ya Scotland, tunaona mafanikio. mwinjilisti huyu alilia akisema, "Nipe Scotland, Ee Bwana, au nife." Na tunaposhika kazi na kupambana na **Mungu**, tukisema, "Ni lazima nipate nafsi; sitakoma kupambana," tutagundua kuwa **Mungu** atatazama juhudi zetu na kuzikubali. — **Manuscript 14, 1887.***{EVsw 294:3}*

Usilazimishe Matokeo — Wakati kazi ya uinjilisti inapokaribia kufungwa, kuwa mwangalifu usiharakishe kuvuna matunda kabla hayajakoma, bali jitahidi kuendeleza uaminifu wa watu ikiwa inawezekana, ili wale walio katika bonde la maamuzi wapate kumwona aliye Njia, Kweli, na na Uzima wa kweli. **— Letter 7, 1885.***{EVsw 295:1}*

Mbinu za Kuthibitisha Maamuzi

Kristo Alizungumza Moja kwa Moja na Wasikilizaji Wake

Hata ule umati uliokuwa ukimfuata kwa wingi haukuwa kwa Kristo kama kundi la watu wasio na utambulisho. Alizungumza moja kwa moja na kila akili, akigusa kila moyo. Alitazama nyuso za wasikilizaji

Wake, akitambua mwangaza uliotokea usoni, mtazamo wa haraka wa kuitikia, uliodhihirisha kuwa Ukweli umefika moyoni; na ndani ya moyo Wake hisia ya furaha ilikuwa kama kinubi, ikitoa mwitikio wa furaha ya huruma. — **Education, uk. 231 (1903).*{EVsw 295:2}***

Alitazama Mabadiliko ya Uso-Yesu aliwaangalia kwa dhati na makini sana wasikilizaji Wake na mabadiliko ya nyuso zao. Nyuso zilizodhihirisha shauku na furaha zilimletea faraja kuu. Mishale ya Kweli ilipopenya mpaka moyoni, kuvunja vizuizi vya ubinafsi, na kusababisha toba hadi shukrani, Mwokozi alifurahi sana. Alipotazama umati wa wasikilizaji na kutambua nyuso alizoziona awali, uso Wake ulijawa na tabasamu na mwangaza wa furaha. Aliona ndani yao mada zenye matumaini ya Ufalme Wake. Lakini pale Ukweli ulipogusa sanamu ya ndani ya mtu, Aliona mabadiliko ya uso, mwonekano wa baridi na wa kukatisha tamaa, uliodhihirisha kuwa nuru haikukaribishwa. Wakati watu walipokataa ujumbe wa amani, moyo Wake ulijawa na uchungu mkubwa.*{EVsw 295:3}*

— The Desire of Ages, uk. 254, 255 (1898).

Hubiri kwa Lengo la Kufanya Maamuzi

Kuza bidii, unyofu na uwe chanya unapowahutubia watu. Unaweza kuwa na somo bora sana, linalohitajika na watu, lakini ni vyema kulichanganya na hali ya hewa chanya, na kushawishi kwa upole.*{EVsw 296:1}*

Wasilisha kauli iliyo wazi, Hivi ndivyo "Asema Bwana," kwa mamlaka, na mtukuze hekima ya **Mungu** iliyomo katika Neno lililoandikwa. Walete watu kwenye uamuzi; sikiliza sauti ya Biblia daima mbele yao. Waambie kuwa unasema kile unachokijua na kushuhudia kuwa ni kweli, kwa sababu **Mungu** amesema. Mahubiri yako yawe mafupi na ya moja kwa moja, na kisha wakati ufaao, toa wito wa uamuzi. Usihubiri kwa mtindo wa kidesturi tu, bali moyo wako uhuishwe na Roho wa **Mungu**, na maneno yako yasemwe kwa uthabiti wa namna ambayo wasikilizaji watajua kuwa ukweli ni halisi kwako. **— Letter 8, 1895.***{EVsw 296:2}*

Usikose Shabaha

Usiruhusu mafundisho ya Maandiko kuwasilishwa kwa namna itakayompa mtu anayefungua Neno la **Mungu** kujivuna. Kazi ya wakati huu ni kuwaelekeza wanafunzi na wahubiri katika mtazamo wa unyenyekevu na uzito, ili wasitumie muda bure katika kazi hii kubwa. Usikose kulenga shabaha. Muda ni mfupi sana kufunua yote, na umilele utahitajika kufahamu upana, kina, na urefu wa Maandiko. Kuna Kweli ambazo ni za muhimu zaidi kwa nafsi fulani kuliko nyingine. Ustadi na hekima vyahitajika katika kufundisha kwa msingi wa Maandiko. **— Manuscript 153, 1898.***{EVsw 296:3}*

Kuendelea Mbele Daima

Hatupaswi kufikiri, "Naam, tunayo Kweli yote, tunaelewa nguzo kuu za imani yetu, hivyo tunaweza kupumzika katika maarifa haya." Ukweli ni Kweli inayosonga mbele -endelevu, na tunapaswa kutembea katika nuru inayoongezeka.*{EVsw 296:1}*

Ndugu mmoja aliuliza, "Dada White, je, unadhani lazima tuielewe Kweli sisi wenyewe? Kwa nini tusikubali Kweli zilizokusanywa na wengine, na tuziamini kwa sababu wao wameshachunguza tayari, kisha nasi tuendelee mbele bila kujihangaisha kuchunguza kila kitu? Je, hawa watu waliotoa ile Kweli hapo awali hawakuvuviwa na **Mungu**?"*{EVsw 297:1}*

mimi siwezi kusema hawakuongozwa na **Mungu**, kwa kuwa Kristo huongoza katika Kweli yote; lakini inapokuja suala la uvuvio kwa maana kamili ya neno, jibu langu ni Hapana.....*{EVsw 297:2}*

Tunapaswa kuwa na imani hai mioyoni mwetu, na kutafuta maarifa mapana na nuru iliyo ya juu zaidi-endelevu, inayoongezeka. — **The Review and Herald, March 25, 1890.***{EVsw 297:3}*

Tuwape Shambulio Adui

Tunaishi katika wakati wa hatari, na tunahitaji neema itakayotufanya kuwa wamoja na hodari katika mapambano, tukitawanya majeshi ya maadui. Ndugu mpendwa, unahitaji imani zaidi, ujasiri zaidi na uamuzi thabiti katika kazi zako. Unahitaji msukumo zaidi na woga mdogo..... Vita yetu inahusisha mashambulizi-msukumo mkali (aggressiveness). Juhudi zako ni za kunyata au za upole mno; unahitaji nguvu zaidi katika

kazi zako, vinginevyo utachanganyikiwa, na kukata tamaa na matokeo yake. Kuna nyakati ambapo lazima utoe shambulio dhidi ya adui. Lazima ujifunze mbinu na njia za kuwafikia watu. Nenda moja kwa moja kwao na uwasimulie ujumbe....Hebu watu waelewe kuwa una ujumbe wa uzima, wa milele kwao ikiwa watakubali. Ikiwa kuna mada yoyote inayopaswa kuamsha roho, ni tangazo la ujumbe wa huruma ya mwisho kwa dunia inayokwisha. Lakini wakikataa ujumbe huu, kwetu watakuwa ladha ya mauti kwa mauti. Kwa hiyo ni lazima kufanya kazi kwa uadilifu na bidii, ili juhudi (kazi) zako zisionekane kuwa ni bure. Hivyo utambue hili, na kuisukuma ile Kweli kwa wengine kwa nguvu ya **Mungu**. Tumia nguvu kwa maneno yako na fanya Ukweli uonekane muhimu kwa akili zao zilizoelimika. — **Letter 8, 1895.***{EVsw 297:4}*

Kuwa na msukumo mkali katika kupeleka injili na kukabiliana na kila kitu ni Lazima (Aggressiveness is necessary)

Msukumo Mkali ni Lazima (Aggressiveness is necessary)–*Tunatakiwa kuchukua tahadhari; lakini wakati baadhi ya watendakazi wanapojihifadhi, na kujilinda na kupunguza kasi ya harakati ya injili na kutembea polepole, basi kama hawatakuwa pamoja na wale wanaoona umuhimu wa kuwa na mashambulizi au bidii kali, mengi yatapotea; fursa zitapita, na majaliwa na mwongozo wa Mungu havitaweza kutambulika au kueleweka.{EVsw 298:1}*

Wakati watu walioko chini ya usadikisho wa wazo, kuna hatari kwamba hawatafanya uamuzi mapema iwezekanavyo, kuna hatari kwamba wazo hilo litapotea polepole.....*{EVsw 298:2}*

Mara nyingi, wakati kutano lipo karibu wakati ambao moyo umeandaliwa kwa ajili ya suala la Sabato, huchelewa kufanya shauri kwa hofu ya matokeo. Hii imefanyika, na matokeo sio mazuri. **Mungu** ametupa amana ya Ukweli wa thamani; tuna ujumbe, ujumbe wa wokovu, tunaagizwa kuutoa kwa dunia, na ambao una matokeo ya milele. Nuru imetolewa kwetu ambayo inapaswa kuangaza dunia. — **Letter 31, 1892** *{EVsw 298:4}*

Nguvu za Roho kwa Ajili ya Ushindi

Zungumza na roho zilizo katika hatari, uwape fursa ya kumtazama Yesu kwenye msalabani, akikata roho ili aweze kusamehe. Zungumza na mwovu, moyo wako ukiwa umejaa upendo na upole, huruma nyororo ya Kristo. Uwe na bidii sana, lakini usikubali sauti kali au ya kelele itoke kwa yule mtu anayejaribu kuokoa roho za watu. Kwanza jinyenyekeze mwenyewe kwa **Mungu na kujitoa wakfu**. Ukimtazama Masihi, Mpatanishi wetu mbinguni, moyo wako mwenyewe na uvunjike. Kisha, ukiwa mpole na mnyenyekevu, na uliyelainishwa moyo, sasa unaweza kuwahutubia waasi wa sheria ya Mungu, kama mtu anayeelewa nguvu ya upendo wa wokovu. Ombeni pamoja na nafsi hizo, kwa imani uwaweke miguuni pa msalaba; elekeza mawazo yao na yako, na nyote mumwangalie Yesu kwa imani, Mbeba Dhambi. Waongoze kutoka katika kuangalia hali yao ya dhambi na umasikini, hadi kwa Mwokozi, na ushindi utapatikana.....*{EVsw 298:4}*

Utendaji wa Huduma ya Roho Mtakatifu ndani yetu ndiyo hitaji letu kuu. Roho ni Mungu, Naye hufanya yote na kuelekeza yote yatokanayo na **Mungu kama Wakala**. **Mungu** anataka wewe upate neema ya kiroho; kisha utakuwa na nguvu ambayo kukuijua hapo awali. Upendo, imani, na matumaini vitakuwa sehemu ya maisha yako. Hivyo, songa mbele kwa imani, ukijua kuwa Roho Mtakatifu anafuatana nawe. — **Letter 77, 1895.***{EVsw 299:1}*

Roho Mtakatifu Hutia Muhimu Ukweli

Ni Roho Mtakatifu Ndiye hugusa moyo na Ukweli ili uwe na mvuto na uvutie. Daima weka Ukweli wa vitendo mbele ya watu-Ukweli wa maisha ya uhalisia ya kila siku. — **Testimonies for the Church, 6:57 (1900).***{EVsw 299:2}*

Maamuzi Huathiriwa na Maneno na Mwenendo/hulka Yetu

Nilipoona kutaniko hilijana, nilifikiri, Maamuzi yatafanywa baada ya mkutano huu na wakati wa mkutano. Kutakuwa na baadhi watakaochukua nafasi yao milele chini ya bendera ya giza na madaraka ya maovu; na wengine watakaa chini ya bendera iliyojaa damu ya Mfalme Immanuel. Maneno yetu, hulka yetu,

haiba yetu, tabia yetu, jinsi tunavyoleta Ukweli mbele yao, vinaweza kushawishi mawazo ya watu kwa au dhidi ya Ukweli; na tunataka katika kila hotuba, iwe ya mafundisho au siyo, Kristo aonyeshwe waziwazi, kama Yohana alivyosema, "*Tazameni Mwana-Kondoo wa* ***Mungu****, aichukuaye dhambi ya ulimwengu* **Yohana 1:29**." *{EVsw 299:3}*

Kila maelezo uliyozoea kuyatoa kwa watu na wahudumu, yaliyo makali au yanayokata, kila tabia ya kulazimisha watu nafasi zenye nguvu mno walizotakiwa kukubali wakati bado hawajakuwa tayari, lazima yaachwe pembeni. Lazima kuongozwa kwa upole, Kristo asiwe sehemu ya mjadala kama kitambaa kinavyotengenezwa kwa jumla, bali awe ni uzi wa msingi na wa mwelekeo wa kitambaa (warp and woof). Kristo, Kristo, Kristo awepo kila mahali. Moyo wangu unahisi haja kubwa ya Kristo, kama ambavyo sikuwahi kuhisi hapo awali. *{EVsw 299:4}*

Hapa kuna watu wasio na elimu kuhusu Ukweli; hawajui chochote. Wamefundishwa na wachungaji kuwa hivi na hivyo ni kweli. Wakati Neno la **Mungu** linapoelezwa kwa uwazi, na wanapoona kilichoandikwa, watatenda nini? Wengine ni wachache tu watakaochukua nafasi yao kulingana na Neno hilo. Lakini nawaambia, kuwa makini jinsi mnavyolitumia Neno, kwa sababu Neno hilo ndilo litakalowapima watu na kukfanya watoe uamuzi. Acheni Neno liseme, si maneno yenu. Lakini wakati watakapofanya uamuzi wao, wewe utafanya nini? — **Manuscript 42, 1894.***{EVsw 300:1}*

Mavuno Yaliocheleweshwa

Makuhani walishawishiwa na uwezo wa kiungu wa Mwokozi. Fursa ilitolewa kwao kuujua Ukweli na kunufaika na na nuru hiyo. Kama ingekataliwa, ingewapita na kwenda zake, wala isingerudi kamwe. Nuru ilikataliwa na wengi; lakini haikutolewa na kwenda bure. Mioyo mingi iliguswa ila haikuonyesha dalili yoyote kwa wakati ule. Wakati wa maisha ya Mwokozi, kazi yake ilionekana kuwa na mwitikio mdogo tu wa makuhani na waalimu; lakini baada ya kupaa Kwake "jamii kubwa ya makuhani wakaitii ile Imani." **Matendo 6:7**." — **The Desire of Ages, uk. 266 (1898).***{EVsw 300:2}*

Ruhusu Wasikilizaji Wakukaribie

Kwa nini Kristo alienda pwani na milimani? Ili awape watu Neno la uzima. Hawakuona hilo wakati huo huo. Wengi bado hawajaamua nafasi yao wala hata hawajui, lakini mambo haya yanaathiri maisha yao; na wakati ujumbe utakapozungumzwa kwa sauti kubwa au kilio kikuu, watakuwa tayari. Hawatachukua muda mrefu; watatoka na kuchukua nafasi yao. **— Manuscript 19b, 1890.***{EVsw 300:3}*

Kukabiliana na Chuki na Upinzani

[Angalia pia kurasa 445, 446, "Chuki Iliyovunjwa."]

Chuki — Wale wanaowasilisha chachu ya Ukweli katikati ya mafunzo na mafundisho ya uongo wanapaswa kutarajia chuki. Silaha za Shetani zitafunguliwa dhidi ya wale wanaosimamia Ukweli, na wanaoibeba bendera, hawa lazima wategemee kukutana na kejeli nyingi, kukosolewa, manyanyaso na matusi magumu kuvumilia. —**The Review and Herald, October 14, 1902.***{EVsw 301:1}*

Matengenezo Huleta Chuki — Yesu na wanafunzi Wake walizungukwa na ubinafsi, ubaguzi, kiburi, chuki, ukosefu wa imani, na hasira. Watu walijaa mafundisho ya imani ya uongo, na hakukuwa na mafanikio yoyote isipokuwa kwa juhudi za pamoja, endelevu. Hata hivyo, kazi kubwa ya kuokoa roho haikuweza kusitishwa kwa sababu ya vizuizi. Ilikuwa imeandikwa kuhusu Mwana wa **Mungu** kwamba "hawapaswi kushindwa wala kuvunjika moyo." *{EVsw 301:2}*

Kazi kubwa iko mbele yetu. Kazi inayovutia na kuhusisha mbingu imetolewa kwa kanisa la Kristo. Yesu alisema: "*Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe*" **Marko 16:15**. Kazi yetu ya wakati huu inakumbwa na matatizo kama yale ambayo Yesu alikabiliana nayo, na kama yale ambayo wanamatengenezo wa zamani, na wa kila zama walipaswa kukabiliana nayo, na kuyashinda; na ni lazima tuweke mapenzi yetu kwa Bwana, na tukae imara upande wa Kristo, tukisonga mbele kwa ujasiri katika **Mungu**. —**The Review and Herald, Machi 13, 1888.***{EVsw 301:3}*

Chuki na Ubaguzi Hukataa Nuru — Kwenye moyo wa mtu kuna jambo linalopingana na Ukweli na haki.... Nguvu ya miujiza ya Kristo ilithibitisha kwamba Yeye ni Mwana wa **Mungu**. Katika miji ya Yuda, ushahidi wa

nguvu ulitolewa kuhusu Uungu na utume wa Kristo.... Lakini chuki na ubaguzi ni vigumu kuishinda, na kuishugulikia moyoni, hata kwa Yeye ambaye ni Nuru na Kweli, hakika chuki iliyokuwa imejaa ndani ya mioyo ya Wayahudi haikuwaruhusu wakubali ushahidi uliotolewa. Kwa dharau walikataa madai ya Kristo. —**Manuscript 104, 1898.***{EVsw 302:1}*

Kushikilia Ukweli ni Njia Bora Zaidi — Mara nyingi unapotafuta kuwasilisha Ukweli, upinzani utaibuka; lakini ukijaribu kuupinga kwa hoja au mabishano, utauzidisha tu, na hilo haliwezi kufaa. Shikilia upande wa Ukweli kwa ujasiri. Malaika wa **Mungu** wanakuangalia wewe, na wanajua jinsi ya kuwagusa moyo wale ambao hupinga ila wewe hubishani nao. Usijaze akili zako na mambo hasi yanayojitokeza, bali jikusanyie Kweli chanya ambazo nyote mnazishikilia, nawe uzizidishe kwa masomo mengi, bali ukazie kwa kuzisoma na uchunguzi mwingi, maombi ya dhati na bidii, na kujitoawakfu moyo wote. hebu ufanye taa yako iendelee kuwaka kwa kutoa masinzi kwenye utambi, na kuacha miale angavu ya nuru kuangaza, ili watu, wakiona matendo yako mema, wataongozwa kumtukuza Baba yako aliye mbinguni.*{EVsw 302:2}*

Kama Kristo asingekuwa ameshikilia Ukweli wakati wa majaribu jangwani, angepoteza yote aliyoyatamani kuyapata. Njia ya Kristo ndiyo njia bora ya kukabiliana na wapinzani wetu. Tunaimarisha hoja zao tunaporudia maneno yao. Daima shikilia upande wa Ukweli. Inawezekana kabisa kuwa mtu anayekupinga ndiye atakayebeba maneno yako na kuyapeleka nyumbani, na kubadilika kuwa na imani kwa Ukweli wa busara uliomfikia, naye akapata uelewa.*{EVsw 301:3}*

Mara nyingi nimesema kwa ndugu zetu: Wapinzani wenu watatengeneza taarifa za kazi yenu ambazo sio za kweli. Msirudie maneno yao, bali shikilia imani yenu kwa Ukweli unaoishi; na malaika wa **Mungu** watafungua njia mbele yenu. Tuna kazi kubwa ya kusonga mbele, na lazima tufanye kwa busara. Tusichochee hisia kali mioyoni mwetu, wala kuwaruhusu hisia za uovu kuibuka. Kristo hakufanya hivyo, na Yeye Ndiye Mfano wetu kwa kila jambo. Kwa kazi iliyo mbele yetu tunahitaji hekima ya mbinguni, iliyo takatifu, na yenye nyenyekevu, na zaidi ya ubinafsi. Tunahitaji kushika kwa nguvu, nguvu ya Mwenyezi Mungu. —**Testimonies For The Church 9:147,148 (1909).***{EVsw 302:4}*

Unapopigwa Vita, Linda Ulimi — Unapofikiwa na upinzani, utakuwa hatarini kulipiza kisasi kwa njia ya kurudisha maneno yenye mjadala mkali au jazba, isipokuwa moyo wako ulainishwe, na kujisalimisha kwa kutulia na kumtafakari Kristo, na kuwa na moyo wa kuomba, "Kristo Wewe *Uwe Mfano wangu.*" na Ukimwangalia Yesu kila wakati, ukichukua Roho Yake, ndipo utaweza kuwasilisha Ukweli kama ulivyo katika Yesu.....*{EVsw 303:1}*

Upendo lazima uwe jambo kuu na linalosheheni katika kazi zetu zote. Katika kuwakilisha wengine wasiokuwa na imani kama sisi, kila mzungumzaji lazima ajiangalie asitoe kauli kali au ya kuhukumu. Wasilisha Ukweli, hebu Ukweli, na Roho Mtakatifu wa **Mungu**, waawe ndio waonyaji na wahukumu; lakini maneno yako yasiichubue roho au kuipa jeraha.....*{EVsw 303:2}*

Usitumie neno hata moja lenye chuki au ukali. Maneno yote ya ukali unayotaka kuyasema, yatunzwe kwa ajili yako binafsi. Usimame imara kama chuma katika kanuni, mwerevu kama nyoka, lakini mpole kama hua. Ikiwa maneno yako hayatakuwa ya kumuumiza mtu yeyote, lazima uongee maneno ambayo umehakikisha hayawezi kuwa makali, ya ujeuri,, baridi, au magumu..... Kati ya watu wote duniani, wanamatengenezo wanapaswa kuwa wasio na ubinafsi, wema zaidi, waungwana, wenye staha na wenye adabu zaidi, wakijifunza njia, maneno, kazi na matendo ya Kristo. —**Letter 11, 1894.** *{EVsw 303:3}*

Roho ya Mabishano — Usichochee roho ya mabishano na migogoro. Hakuna manufaa yanayotokana na maneno ya lawama. Njia salama ya kuondoa mafundisho ya uongo ni kuhubiri Ukweli. Shikilia upande wa Kweli. Hebu Kweli za thamani za Injili ziue nguvu za maovu. Onyesha huruma nyororo na sikitiko kwa wenye makosa. Ikaribie mioyo ya watu. —**Letter 190, 1902.***{EVsw 304:1}*

Kuudhi Watu kwa Kejeli au Kuwashushua— Wakati wa hotuba yako, unapolaumu kwa dhihaka/kejeli kali kile unachotaka kukihukumu na kushushua watu, wakati mwingine unawaumiza wasikilizaji, na masikio yao hugeukia mbali wasikusikilize. Epuka maneno makali yanayoweza kuwachosha na kuwachukiza wale unaotaka kuwaokoa katika makosa; kwa maana itakuwa vigumu kuondoa hisia za upinzani zilizoibuliwa.....*{EVsw 304:2}*

Ukiondoa maneno ya magugu yenye sumu na chuki kwenye hotuba yako, ushawishi wako kwa mema utaongezeka. —**Letter 366, 1906.***{EVsw 304:3}*

Usikaribishe Ukandamizaji — Kila mtu afahamu kuwa hatupaswi kukaribisha mateso au ukandamizaji. Hatuwezi kutumia maneno makali yanayokata, na yanayoumiza. Yaondoe katika kila makala na hotuba unayotoa. Hebu Neno la **Mungu** libakie kukata, kukemea; hebu watu walio na ukomo wasionekane na kukaa katika Yesu Kristo. Hebu Roho ya Kristo ionekane. Watu wote waongozwe katika maneno yao, wasiwafanye wale wasiokuwa wa imani yetu kuwa wapinzani hatari kwetu, na kumpa Shetani fursa ya kutumia maneno yasiyopangwa kufunga njia yetu.....*{EVsw 304:4}*

sote tunahitaji upendo wa kina zaidi wa Yesu katika roho, na harara kwa udogo sana-kuudhika-udhika na jazba kwa udogo sana. Tuko katika hatari ya kufunga njia yetu wenyewe kwa kuchochea roho ya upinzani kali kwa watu walioko madarakani, kabla watu hawajaangazwa na ujumbe ambao **Mungu** anataka tuulete. **Mungu** hapendezwi tunaporuhusu kwa njia zetu wenyewe—kuzuia Ukweli usifike kwa watu. — **Manuscript 95,1894..***{EVsw 304:5}*

Upinzani Hunadi Ukweli — Shetani ni mwenye mbinu nyingi za kukwepesha Ukweli. Lakini nakuomba uamini maneno niliyosema leo. Ukweli wa mbinguni unapingana na uongo wa Shetani, na Ukweli huu utashinda..... Upinzani na kukataa husaidia tu kuonyesha Ukweli kwa njia mpya, iliyo tofauti. Kadri Ukweli unavyopingwa, ndivyo unavyong'aa zaidi. Hivyo madini ya thamani yanang'arishwa. Kila neno la uongo linalosemwa dhidi yake, kila udanganyifu wa thamani yake, huchochea watu kusoma zaidi na kuchunguza zaidi ili kujua Ukweli unaokoa. Ukweli unapewa thamani zaidi. Uzuri ulio mpya na wa thamani kubwa huonekana kwa kila mtazamo. —**Manuscript 8a, 1888.** *{EVsw 305:1}*

Waheshimu Wapinzani Wenu — Lazima tutegemee kukutana na kutokuamini na upinzani. Ukweli umelazimika kukutana na vipengele hivi. Lakini ingawa unapaswa kukutana na upinzani mkali zaidi, usiwashutumu wapinzani wako. Huenda wakafikiri kama Paulo, kwamba wanafanya utumishi wa **Mungu** vyema kabisa, na kwa watu kama hao ni lazima tuonyeshe subira, upole, na ustahimilivu.....*{EVsw 305:2}*

Bwana anataka watu Wake wafuate njia nyingine zaidi ya ile ya kushutumu maovu, ingawa hukumu ni ya haki. Yeye Anataka tufanye jambo fulani zaidi ya kuwarushia wapinzani wetu mashtaka ambayo yanawafukuza zaidi kutoka kwenye Kweli. Kazi ambayo Kristo alikuja kufanya katika ulimwengu wetu haikuwa kuweka vizuizi/utengano na daima kusisitiza juu ya watu Ukweli kwamba walikuwa wamekosea. Yule anayetarajia kuwaangazia watu waliodanganywa lazima awakaribie na kuwafanyia kazi kwa upendo. Ni lazima awe kitovu cha ushawishi mtakatifu.*{EVsw 305:3}*

Katika utetezi wa Ukweli, wapinzani wenye wachungu zaidi wanapaswa kutendewa kwa heshima na staha. Wengine hawatajibu juhudi zetu, lakini watafanya mwaliko wa injili kuwa mwepesi. Wengine—hata wale ambao tunadhania kuwa wamevuka mpaka wa rehema ya **Mungu** —watavutwa kwa Kristo. Kazi ya mwisho kabisa katika pambano hilo inaweza kuwa kuangaziwa kwa wale ambao hawajakataa nuru na ushahidi, lakini ambao wamekuwa katika giza la usiku wa manane na kwa ujinga wamefanya kazi dhidi ya Ukweli. Kwa hivyo mchukulieni kila mwanadamu kama mtu mwaminifu, asiye na hila (raia wa mbinguni mtarajiwa). Msiseme neno, msifanye tendo, litakalomthibitisha mtu yeyote katika kutokuamini. **—Testimonies For The Church 6:120-122 (1900).***{EVsw 306:1}*

Msaada Kila Wakati Katika Hali Mbaya au dharura — Kila mwalimu wa Ukweli, kila mtendakazi pamoja na **Mungu**, atapitia nyakati ngumu, ambapo imani na uvumilivu vitajaribiwa vikali. Lazima uwe tayari kwa neema ya Kristo kusonga mbele, hata kama mambo yanaonekana hayawezekani kwa vizuizi. Una msaada wa

kila wakati wa shida na dharura. Bwana anakuruhusu kukutana na vikwazo, ili umtafute Yeye ambaye Ndiye nguvu yako na utimilifu wako. Omba hekima kutoka kwa **Mungu** kwa dhati na bidii; Yeye atafungua njia mbele yako, na atakupa ushindi wa thamani ikiwa utaendelea kutembea kwa unyenyekevu mbele Zake. — **Special Testimonies, Series A, No. 7, uk. 18. (1874).***{EVsw 306:2}*

Ubatizo na Ushirika wa Kanisa

Ubatizo Ni Sharti la Uongofu

Toba, imani, na ubatizo ni hatua muhimu katika mabadiliko ya kiroho na wongofu-kugeuka kuwa mfuasi wa Kristo. **-Letter 174, 1909.***{EVsw 306:3}*

Uamuzi wa Dhahiri Kuhusu Ubatizo

Nafsi zinazohisi usadikisho wa Ukweli zinahitaji kutembelewa na kufanyiwa kazi ya kiroho kwa bidii. Wadhambi wanahitaji huduma maalum ili waongoke na kubatizwa. —**Manuscript 17, 1908.***{EVsw 306:4}*

Ishara ya Kuingia katika Ufalme wa Mungu

Kristo amefanya ubatizo kuwa ishara ya kuingia katika ufalme Wake wa kiroho. Yeye Amefanya hili kuwa sharti la uhakika na chanya ambalo wote wanapaswa kufuata wale wanaotaka kutambuliwa kuwa chini ya mamlaka ya Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Kabla mwanadamu hajapata makao katika kanisa, kabla ya kupita kizingiti cha ufalme wa kiroho wa **Mungu**, anapaswa kupokea msukumo wa Jina la **Mungu**, "Bwana Haki yetu." Yeremia 23:6.*{EVsw 307:1}*

Ubatizo ni kuukana kabisa ulimwengu. Wale wanaobatizwa katika Jina lenye sehemu tatu la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, kwenye mlango wa kuingia kabisa wa maisha yao ya Kikristo wanatangaza hadharani kwamba wameacha utumishi wa Shetani na wamekuwa washiriki wa familia ya kifalme, watoto wa **Mungu**. Mfalme wa mbinguni. Wametii amri: “Tokeni miongoni mwao, na jitengeni..... wala msiguse kitu kilicho najisi.’ Na kwao inatimia ahadi: "Mimi nitawakaribisha, Nami nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa Kwangu Wanangu wa kiume na wa kike, asema Bwana Mwenyezi." 2 Wakorintho 6:17, 18. — **Testimonies For The Church 6:91, 1900.** *{EVsw 307:2}*

Ahadi ya Utii kwa Kristo Katika Ubatizo

Wakati MKristo anapokubali tendo la kipekee la ubatizo, wanajisajili kwa kuahidi kuwa waaminifu Kwake. Nadhiri hii ni kiapo chao cha utii. Wanabatizwa kwa Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, na hivyo kuungana na mamlaka kuu za mbinguni. Wanajitolea kuukana ulimwengu na kuzingatia sheria za ufalme wa **Mungu**. Kuanzia wakati huo, wanapaswa kuishi maisha mapya. Kutoendelea kufuata desturi za watu wala mbinu za uongo, au hiana, bali kutii sheria za mbinguni na kutafuta utukufu wa **Mungu**. Iwapo watakuwa waaminifu kwa nadhiri/ahadi yao, watapewa neema na nguvu itakayowawezesha kutimiza haki zote. “**Yohana 1:12-** *Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa **Mungu**, ndio wale waliaminio Jina Lake*.” **—Letter 129, 1903.***{EVsw 307:3}*

Uongofu Mkamilifu kwa ile Kweli

Maandalizi ya ubatizo yanahitaji kufikiriwa kwa makini. Waongofu wapya katika ile Kweli wanapaswa kufundishwa kwa uaminifu Maneno ya **Mungu yaliyoagizwa kwa wazi**, "Ndivyo anavyosema Bwana." Neno la **Mungu** linapaswa kusomwa na kufafanuliwa kwa kina, kipengele kwa kipengele. *{EVsw 308:1}*

Kabla ya ubatizo, wote wanapaswa kuelewa kuwa Bwana anahitaji mapenzi yote ya mtu yasiyogawanyika. Kutenda ile Kweli ni muhimu sana. Kuzaa matunda ya maisha ni ushahidi wa hali ya moyo-hali ya moyo; mti mzuri hauwezi kuzalisha matunda mabaya. Kuna tofauti ya wazi kati ya wale wanaompenda **Mungu** na kutii amri Zake, na wale wasiompenda na kupuuza Maagizo na mafundisho Yake. Inahitajika badiliko kamili la uongofu wa moyo na maisha. —**Manuscript 56, 1900.***{EVsw 308:2}*

Inakubaliwa Wakati Nafasi Inaeleweka Kikamilifu—Jaribio la uanafunzi haliletwi kwa karibu kama linavyopaswa kuwa kwa wale wanaojitolea kwa ubatizo.... Wanapotoa ushahidi kwamba wanaelewa kikamilifu nafasi yao, wanapaswa kukubaliwa.—Testimonies to Ministers and Gospel Workers, 128 (1897).

Inapokelewa Vizuri Ikiwa Msimamo Umeeleweka Vizuri

Mtihani wa kuwa mwanafunzi usifanyike kwa namna ile inavyotakiwa kwa wale wanaojitokeza kwa ajili ya ubatizo. Wakionyesha kuwa wanaelewa kwa kina msimamo wao, wanapaswa kupokelewa. — **Testimonies to Ministers and Gospel Workers 128, 1897.***{EVsw 308:3}*

Maandalizi Kamili kwa Wanaobatizwa

Kuna uhitaji wa kujitayarisha kikamilifu zaidi kwa upande wa wale wanaotaka kubatizwa. Wanahitaji mafundisho ya uaminifu zaidi kuliko kawaida waliyopewa. Kanuni za maisha ya Kikristo zinapaswa kuwekwa wazi kwa wale ambao wamekuja hivi karibuni kwenye Kweli. Hakuna anayeweza kutegemea ukiri wao wa imani kama uthibitisho kwamba wana uhusiano unaookoa na Kristo. Hatupaswi kusema tu, "Naamini," bali kutenda Ukweli. Ni kwa kupatana na mapenzi ya **Mungu** katika maneno yetu, mwenendo wetu, tabia zetu, ndipo tunapothibitisha uhusiano wetu Naye. Wakati wowote mtu anapoacha dhambi, ambayo ni uvunjaji wa sheria, maisha yake yataletwa katika kupatana na sheria, katika utii mkamilifu. Hii ni kazi ya Roho Mtakatifu. Nuru ya Neno iliyosomwa kwa uangalifu, sauti ya dhamiri, jitihada za Roho, huzalisha ndani ya moyo upendo wa Kweli kwa Kristo, ambaye alijitoa mwenyewe dhabihu nzima ili kumkomboa mtu mzima, mwili, nafsi na roho. Na upendo unadhihirika katika utiifu. **—Testimonies For The Church 6:91-92, 1900.** *{EVsw 308:4}*

Kubatizwa kwa Watoto

Wazazi ambao watoto wao wanatamani kubatizwa wana kazi ya kufanya, katika kujichunguza na kuwapa watoto wao maagizo ya uaminifu. Ubatizo ni agizo/sakramenti takatifu na muhimu sana, na kunapaswa kuwa na ufahamu kamili wa maana yake. Inamaanisha toba kwa ajili ya dhambi, na kuingia kwa maisha mapya katika Kristo Yesu. Kusiwe na haraka isivyostahili kupokea agizo hili. Hebu wazazi na watoto wote wahesabu gharama. Katika kuridhia ubatizo wa watoto wao, wazazi wanajiapiza wenyewe kwa utakatifu kuwa wasimamizi waaminifu juu ya watoto hawa, ili kuwaongoza katika kujenga tabia zao. Wanajitolea kuwalinda kwa uangalifu wa pekee wana-kondoo hawa wa kundi, ili wasiivunjie heshima imani wanayokiri.*{EVsw 309:1}*

Mafundisho ya kidini yanapaswa kutolewa kwa watoto kutoka miaka yao ya mapema. Yanapaswa kutolewa, si kwa roho ya kushutumu, bali kwa uchangamfu, na kwa roho ya furaha. Akina mama wanatakiwa kukesha kila mara, ili watoto wasije wakapata majaribu kwa namna ya kutotambulikana kwa watoto. Wazazi wanapaswa kuwalinda watoto wao kwa mafundisho ya hekima na mazuri. Kama marafiki wazuri sana wa hawa wasio na uzoefu, wanapaswa kuwasaidia katika kazi ya kushinda, kwa maana ni kila kitu kwao kuwa washindi. Wanapaswa kuzingatia kwamba watoto wao wenyewe wapendwa ambao wanatafuta kutenda haki ni washiriki wachanga zaidi wa familia ya Bwana, na wanapaswa kuhisi shauku kubwa katika kuwasaidia kufanya mapito yaliyonyooka katika njia kuu ya utiifu ya Mfalme. Kwa kupendezwa na upendo wanapaswa kuwafundisha siku baada ya siku maana ya kuwa watoto wa **Mungu** na kuachilia mapenzi katika utiifu Kwake. Wafundishe watoto kwamba kumtii **Mungu** inahusu ndani yake kuwatii wazazi wao. Hii lazima iwe kazi ya kila siku, ya kila saa. Wazazi, angalieni, kesheni na ombeni, na wafanyeni watoto wenu kuwa waandamani wenu. *{EVsw 309:2}*

Wakati kipindi cha furaha zaidi cha maisha yao kinapofika, na wao mioyoni mwao wanampenda Yesu na kutamani kubatizwa, basi washughulikie kwa uaminifu. Kabla ya kupokea agizo hilo, waulize kama litakuwa kusudi lao la kwanza maishani kumfanyia **Mungu** kazi. Kisha waambie jinsi ya kuanza. Ni masomo ya kwanza ambayo yana maana kubwa sana. Kwa urahisi wafundishe jinsi ya kufanya huduma yao ya kwanza kwa **Mungu**. Fanya kazi iwe rahisi kueleweka kadri iwezekanavyo. Eleza maana ya kujitoa kwa Bwana, kufanya kama Neno Lake linavyoelekeza, chini ya ushauri wa wazazi WaKristo. ***{EVsw 310:1}***

Baada ya kazi ya uaminifu, ikiwa umeridhika kwamba watoto wako wanaelewa maana ya uongofu na ubatizo, na wameongoka kweli, acha wabatizwe. Lakini, narudia, kwanza kabisa jitayarisheni kutenda kama wachungaji waaminifu katika kuongoza miguu yao isiyo na uzoefu katika njia nyembamba ya utii. **Mungu** lazima afanye kazi ndani ya wazazi ili waweze kuwapa watoto wao kielelezo sahihi, katika upendo, usafi, uungwana, staha, adabu, na unyenyekevu wa Kikristo, na katika kujitoa kikamilifu kwa Kristo. Ikiwa unakubali ubatizo wa watoto wenu na kisha kuwaacha kufanya watakavyo, bila kuhisi wajibu wowote maalum wa kuweka miguu yao katika njia iliyonyooka, ninyi wenyewe mnawajibika ikiwa watapoteza imani na ujasiri na kupendezwa na "Ukweli. —**Testimonies For The Church 6:93-95, 1900.** ***{EVsw 310:2}***

Kuwaandaa Vijana kwa Ajili ya Ubatizo

Watahiniwa ambao ni watu wazima kwa mwanamume na mwanamke wanapaswa kuelewa wajibu wao vizuri zaidi kuliko vijana; lakini mchungaji wa kanisa ana wajibu wa kufanya kwa ajili ya roho hizi. Je, wana tabia na mazoea mabaya? Ni wajibu wa mchungaji kuwa na mikutano maalum pamoja nao. Wape masomo ya Biblia, zungumza na kuomba pamoja nao, na uonyeshe wazi madai ya Bwana juu yao. Wasomee mafundisho ya Biblia kuhusu kuongoka. Onyesha ni nini tunda la uongofu, uthibitisho kwamba wanampenda **Mungu**. Onyesha kwamba uongofu wa Kweli ni badiliko la moyo, la mawazo na makusudi. Tabia mbaya zinapaswa kuachwa. Dhambi za kunena maovu, wivu, uasi, zinapaswa kuondolewa. Vita lazima viazimiwe dhidi ya kila tabia mbaya ya tabia. Kisha mwenye kuamini anaweza kujichukulia kwa ufahamu ahadi hii: *"Ombeni, nanyi mtapewa." Mathayo 7:7.* **—Testimonies For The Church 6:95, 1900.** ***{EVsw 311:1}***

Mtihani wa Wataradhia wa Ubatizo

Jaribio la uanafunzi/ufuasi haliletwi kwa ukaribu kama inavyopaswa kuwa juu ya wale wanaojitoa wenyewe kwa ajili ya ubatizo. Wanapaswa kueleweka kama wanachukua tu jina la Waadventista Wasabato, au kama wanachukua msimamo wao upande wa Bwana, kutoka katika ulimwengu na kujitenga, na wasiguse kitu kilicho kichafu. Kabla ya kubatizwa kunapaswa kuwa na uchunguzi kamili kuhusu uzoefu wa watakaobatizwa. Acheni uchunguzi huu ufanywe, si kwa njia ya ubaridi na ya mbali, bali kwa fadhili, kwa upole, tukiwaelekeza waongofu wapya kwa Mwana-Kondoo wa **Mungu** aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Lete mahitaji ya injili kubebwa juu ya wanaotaka kubatizwa.***{EVsw 311:2}***

Mojawapo ya mambo ambayo wale wapya wanaokuja kwenye imani watahitaji kufundishwa ni suala la mavazi. Hebu waongofu wapya washughulikiwe kwa uaminifu. Je, wana ubatili wa mavazi? Je, wanathamini kiburi cha moyo? Ibada ya sanamu ya mavazi ni ugonjwa wa maadili. Haipaswi kuchukuliwa katika maisha mapya. Katika hali nyingi, utiifu kwa mahitaji ya injili utadai mabadiliko yaliyoamuliwa katika mavazi. ***{EVsw 312:1}***

Kusiwe na uzembe katika mavazi. Kwa ajili ya Kristo, ambaye sisi ni mashahidi Wake, tunapaswa kufanya mwonekano wetu kuwa mzuri zaidi. Katika huduma ya Patakatifu-madhabahu, **Mungu** alibainisha kila jambo kuhusu mavazi ya wale wanaohudumu mbele Zake. Hivyo tunafundishwa kwamba Yeye ana kipaumbele cha namna fulani, kuhusiana na mavazi ya wale wanaomtumikia. Maelekezo yaliyotolewa yalikuwa hususani kabisa kuhusiana na mavazi ya Haruni, kwa maana mavazi yake yalikuwa ya mfano. Kwa hiyo, mavazi ya wafuasi wa Kristo yanapaswa kuwa ya mfano. Katika mambo yote tunapaswa kuwa wawakilishi Wake Bwana. Muonekano wetu katika kila jambo unapaswa kuonyeshwa nadhifu, kiasi, staha, adabu, na usafi wa moyo. Lakini Neno la **Mungu** halitoi kibali cha kufanya mabadiliko katika mavazi kwa ajili ya mitindo tu, ili tuonekane kama ulimwengu. Wakristo hawapaswi kupamba mtu (wao wenyewe) kwa mapambo ya bei ghali au ya gharama kubwa. ***{EVsw 312:2}***

Maneno ya Maandiko kuhusu mavazi yanapaswa kuzingatiwa kwa uangalifu. Tunahitaji kuelewa kile ambacho Bwana wa mbinguni anakithamini hata katika uvaaji wa mwili. Wote walio na bidii katika kutafuta neema ya Kristo watatii Maneno ya thamani ya maagizo yaliyoongozwa na **Mungu**. Hata mtindo wa mavazi utaeleza Ukweli wa injili. ***{EVsw 312.3}***

Wote wanaosoma maisha ya **Kristo** na kutenda mafundisho Yake watakuwa kama **Kristo**. Ushawishi wao utakuwa kama Wake. Watadhihirisha busara katika tabia. Wanapotembea katika njia ya unyenyekevu ya utiifu, wakifanya mapenzi ya **Mungu**, wanatoa ushawishi unaoonyesha maendeleo ya kazi ya **Mungu** na usafi wa afya wa kazi Yake. Katika roho hizi zilizoongoka kabisa, ulimwengu unapaswa kuwa na ushuhuda wa utakatifu wa nguvu ya Ukweli juu ya tabia ya mwanadamu.***{EVsw 313:1}***

Ujuzi wa **Mungu** na wa Yesu Kristo, unaoonyeshwa katika tabia, ni kuinuliwa juu ya kila kitu kinachohesimiwa duniani au mbinguni. Ni elimu ya juu sana. Ni ufunguo unaofungua milango ya jiji la mbinguni. Ujuzi huu ni kusudi la **Mungu** kwamba wote wanaomvaa Kristo kwa ubatizo wawe nao. Na ni wajibu wa watumishi wa **Mungu** kuweka mbele ya roho hizi upendeleo wa wito wao mkuu katika Kristo Yesu. **—Testimonies For The Church 6:95-97 (1900).*{EVsw 313:2}***

Kutathmini kwa Matunda ya Maisha

Kuna jambo moja ambalo hatuna haki ya kufanya, na hilo ni kuhukumu moyo wa mtu mwenzako au kudharau nia zake. Lakini mtu anapojitokeza kuomba ushirika wa kanisa, tunapaswa kuchunguza matunda ya maisha yake, na kumwacha aajibike mwenyewe kwa nia yake. Hata hivyo, tunapaswa kuwa waangalifu sana katika kuwapokea watu kuwa washiriki wa kanisa, kwa sababu Shetani ana mbinu zake za kudanganya kwa lengo la kuingiza ndugu wa uongo ndani ya kanisa, na kisha kupitia wao anafanya kazi kwa ufanisi zaidi kuudhoofisha upendo wa **Mungu**. —**The Review and Herald, January 10, 1893.*{EVsw 313:3}***

Uendeshaji wa Huduma ya ubatizo

Wakati wowote inapowezekana, hebu ubatizo ufanyike katika ziwa safi au kijito kinachotiririka. Na hafla hiyo ipewe umuhimu wote na uzito na kuadhimisha ambako kunaweza kuletwa ndani yake. Katika huduma kama hiyo malaika wa **Mungu** huwapo kila wakati.***{EVsw 313:4}***

Yule anayesimamia ibada ya ubatizo anapaswa kutafuta kuifanya kuwa hafla ya taadhima, mvuto mtakatifu kwa watazamaji wote. Kila agizo/sakramenti ya kanisa inapaswa kuendeshwa ili kuinua mvuto wake. Hakuna kitu kinachopaswa kufanywa kuwa cha kawaida au cha ovyo ovyo, au kuwekwa kwenye ngazi na mambo ya kawaida. Makanisa yetu yanahitaji kuelimishwa kwa heshima na staha zaidi kwa utumishi mtakatifu wa **Mungu**. Wahudumu/wachungaji wanapoendesha huduma zinazohusiana na ibada ya **Mungu**, ndivyo wanavyowaelimisha na kuwazoeza watu. Matendo madogo yanayoelimisha na kufundisha na kuadibisha nafsi kwa umilele ni ya matokeo makubwa katika kuinua na kutakasa kanisa. ***{EVsw 314:1}***

Katika kila kanisa, mavazi ya ubatizo yanapaswa kutolewa kwa ajili ya waombaji. Hii haipaswi kuzingatiwa kama matumizi yasiyo ya lazima ya pesa. Ni moja ya mambo yanayotakiwa katika kutii amri hii: "Mambo yote na yatendeke kwa uzuri na kwa utaratibu." 1 Wakorintho 14:40. ***{EVsw 314:2}***

Si vizuri kwa kanisa moja kutegemea kuazima mavazi kutoka kwa lingine. Mara nyingi wakati majoho yanapohitajika, hayapatikani; muazimaji fulani wa majoho, amepuuza kuyarudisha. Kila kanisa linapaswa kutoa mahitaji yake katika Nyanja hii. Hebu pesa ipatikane kwa kusudi hili. Kanisa zima likiungana katika hili, hili halitakuwa mzigo mzito. ***{EVsw 314:3}***

should be made of substantial material, of some dark color that water will not injure, and they should be weighted at the bottom. Let them be neat, well-shaped garments, made after an approved pattern. There should be no attempt at ornamentation, no ruffling or trimming. All display, whether of trimming or ornaments, is wholly out of place. When the candidates have a sense of the meaning of the ordinance, they will have no desire for personal adornment. Yet there should be nothing shabby or unseemly, for this is an offense to God. Everything connected with this holy ordinance should reveal as perfect a preparation as possible.—Testimonies For The Church 6:97, 98 (1900).

Majoho yanapaswa kuwa na kitambaa kizuri na kikubwa, cha rangi nyeusi ambacho maji hayatadhuru, na yanapaswa kuwa na uzito chini (yasifunuke). Hebu yawe nadhifu, nguo zilizoshonwa kwamshono mzuri, naam, mshono ulioidhinishwa. Hakupaswi kuwa na majaribio ya kuweka mapambo, marinda au kuongeza vipande vya nguo. Maonyesho yote, iwe ni ni kuongezea vipande vya vitambaa au mapambo, hayafai kabisa.

Watahiniwa wanapokuwa na ufahamu wa maana ya agizo/amri hiyo, hawatakuwa na hamu ya kuipamba nafsi. Hata hivyo kusiwe na kitu kisicho nadhifu au cha hovyo ovyo au kisichofaa, kwa maana hili ni kosa kwa **Mungu**. Kila kitu kinachohusiana na agizo hili takatifu kinapaswa kudhihirisha maandalizi kamili kwa kadri iwezekanavyo. —**Testimonies For The Church 6:97, 98 (1900).***{EVsw 314:4}*

Huduma ya Ubatizo Yenye Mvuto Mkubwa

Juhudi zilizofanywa Oakland zimesababisha wokovu wa roho nyingi. Jumatatu asubuhi, Desemba 16, nilihudhuria ibada ya ubatizo katika Piedmont Baths. Wataradhia/wabatizwa thelathini na wawili waliozikwa kwa njia ya ubatizo na Bwana wao, na kufufuka katika maisha mapya. Hili ilikuwa tukio ambalo malaika wa **Mungu** walishuhudia kwa furaha..... Ibada yote ilikuwa na mvuto mkubwa. Hapakuwa na mkanganyiko, na vurugu, na mara kwa mara wimbo wa sifa uliimbwa. **—Manuscript 105, 1906.***{EVsw 315:1}*

Ubatizo wa Dharura

Mipango itatengenezwa kutekeleza ombi la mzee mmoja kwa ajili ya ubatizo. Hawezi kwenda mahali pa ibada kwa kuwa ni mdhafu, na njia pekee ya kuendesha ibada ya ubatizo ni kutumia bafu ya kuogea na kumruhusu aingie ndani ya maji. **—Letter 126, 1901.***{EVsw 315:2}*

Nguvu Mungu ya Kutulinda

Baada ya roho iliyoamini kupokea huduma takatifu ya ubatizo, inapaswa kukumbuka kuwa imejitoa kwa **Mungu**, kwa Kristo, na kwa Roho Mtakatifu.....*{EVsw 315:3}*

Wote wanaosoma maisha ya Kristo na kufuata mafundisho Yake watakuwa kama Kristo. Mvuto wao utakuwa kama Wake. Wataonyesha tabia nzuri, wakiwa wameimarishwa katika imani, na hawawezi kushindwa na Shetani kwa sababu ya ubatili au kiburi. Watanatafuta kutembea njia ya unyenyekevu na utiifu, wakifanya mapenzi ya **Mungu**. Tabia zao zikiwa na mvuto unaosaidia kuendeleza kusudi la **Mungu** na usafi wa kazi Zake.....*{EVsw 315:4}*

Katika roho hizi zilizoongoka kabisa, dunia ina ushahidi wa nguvu ya utakaso ya Ukweli kwa tabia ya binadamu. Kupitia wao, Kristo huinyesha dunia tabia na mapenzi Yake. Katika maisha ya watoto wa **Mungu** kuna furaha na baraka ya kumtumikia Bwana, na kinyume chake kinaonekana kwa wale wasiotunza amri Zake. Mstari wa mpaka unaoneka Dhahiri. Wote wanaotii amri za **Mungu** hulindwa na nguvu Zake kubwa katikati ya maovu ya waovu wa sheria Yake. Kuanzia mtu mdogo kabisa hadi mtu wa cheo kikubwa, wote hulindwa na nguvu ya **Mungu** kupitia imani kwa wokovu.—**Manuscript 56, 1900.***{EVsw 316:1}*

Kujiweka Wakfu Kwa Ajili ya Mungu

Tangu sasa muumini anapaswa kukumbuka kwamba amejitolea kwa **Mungu**, kwa Kristo, na kwa Roho Mtakatifu. Anapaswa kufanya mazingatio yote ya kidunia kuwa ya pili kwa uhusiano huu mpya. Ametangaza Hadharani kwamba hataishi tena kwa kiburi na kujifurahisha. Hatakiwi tena kuishi maisha ya kutojali, na ya uzembe. Amefanya agano na **Mungu**. Amekufa kwa ulimwengu. Anapaswa kuishi kwa ajili ya Bwana, kutumia kwa ajili Yake uwezo wake wote aliokabidhiwa, bila kupoteza kamwe utambuzi wa kwamba yeye ana sahihi ya **Mungu**, kwamba yeye ni raia wa ufalme wa Kristo, mshiriki wa asili ya mbingu. Anapaswa kukabidhi kwa **Mungu** vyote alivyo na vyote alivyo navyo, akitumia zawadi zake zote kwa utukufu wa Jina Lake. *{EVsw 316:2}*

Wajibu katika mapatano ya kiroho yaliyowekwa wakati wa ubatizo ni ya pande zote mbili. Wanadamu wanapotenda sehemu yao kwa utii wa moyo wote, wana haki ya kuomba: “Na ijulikane, Ee Bwana, ya kuwa Wewe Ndiwe **Mungu** katika Israeli; Ukweli kwamba umebatizwa katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ni hakikisho kwamba, ikiwa utadai msaada wao, nguvu hizi zitakusaidia katika kila dharura. Bwana atasikia na kujibu maombi ya wafuasi Wake wanyofu wanaovaa nira ya Kristo na kujifunza katika shule Yake upole na unyenyekevu wake. —**Testimonies For The Church 6:98, 99 (1900).***{EVsw 316:3}*

Wajibu wa Kanisa kwa Waongofu Wapya

Wanaume na wanawake WaKristo waaminifu wanapaswa kuwa na matamanio makubwa ya kuleta nafsi iliyo na hatia kwenye ujuzi sahihi wa uadilifu katika Kristo Yesu. Ikiwa kuna yeyote ambaye ameruhusu tamaa ya kujifurahisha kwa ubinafsi iwe kuu maishani mwao, waumini waaminifu wanapaswa kutazama nafsi hizi kama zile ambao lazima watoe hesabu kwa Bwana. Hawapaswi kupuuza mafundisho ya uaminifu, ya

upole na upendo ambayo ni muhimu sana kwa waongofu wachanga hivi kwamba kunaweza kuwa hakuna kazi ya moyo nusu-nusu. Uzoefu wa kwanza kabisa unapaswa kuwa sahihi.*{EVsw 317:1}*

Shetani hataki mtu yeyote aone umuhimu wa kujisalimisha kabisa kwa **Mungu**. Nafsi inaposhindwa kujisalimisha huku, dhambi haiachwi; hamu na tamaa za mwili zinataka kutawala na kuwa na ustadi; majaribu yanachanganya dhamiri, ili uongofu wa Kweli usitukie. Ikiwa wote wangekuwa na hisia ya pambano ambalo kila nafsi lazima ifanye na vyombo vya kishetani vinavyotaka kuwatega, kushawishi, na kudanganya, kungekuwa na kazi ya uaminifu na bidii zaidi kwa wale walio wachanga katika imani. *{EVsw 317:2}*

Nafsi hizi, zikiachwa zenyewe, mara nyingi hujaribiwa na hazitambui ubaya wa jaribu. Hebu wahisi kwamba ni upendeleo kwao kutafuta ushauri na kutafuta jumuiya ya wale wacha **Mungu** nao watapata nguvu.*{EVsw 317:3}*

Mazungumzo yetu na nafsi hizi yanapaswa kuwa ya tabia ya kiroho, yenye kutia moyo. Bwana huweka alama kwenye migongano/migogoro ya kila mtu mnyonge, mwenye mashaka, na anayehangaika, naye atawasaidia wote wamwitao. Wataziona mbingu zikifunguka mbele yao, na malaika wa **Mungu** wakishuka na kupanda kwenye ngazi ya inayong'aa mno, ambayo wanajaribu kupanda. **—Testimonies For The Church 6:92, 93 (1900).***{EVsw 317:4}*

Ushirika wa Kanisa

Uhusiano kati ya Kristo na kanisa Lake ni wa karibu sana na mtakatifu,—Yeye ni Bwana-arusi, kanisa ni Bibi-arusi Wake; Yeye ni kichwa, kanisa ni mwili. Muunganiko na Kristo ni kuungana na kanisa Lake. — **Education, 268 (1903).***{EVsw 318:1}*

Shetani Anajaribu Kuzuia Kujiunga na Kanisa

Ni jitihada zake [Shetani] za kuwalekeza watu wanaodai kuwa ni WaKristo mbali zaidi na mpangilio wa mbinguni; kwa hiyo huwadanganya hata watu wanaodai wa **Mungu** na kuwafanya waumini kwamba utaratibu na nidhamu ni maadui wa kiroho; kwamba usalama pekee kwao ni kila mtu afanye anavyotaka, na kutojihusisha sana na makundi ya WaKristo walioungana na kufanya kazi ya kusimika nidhamu na mshikamano. Jitihada zote za kuanzisha hili hutambulika kama hatari, vizuizi vya uhuru wa kweli, na kwa hivyo huogopwa kama ndiyo upapa. Wale watu waliodanganywa hufikiri ni jambo la kupendeza kujisifu kuhusiana na uhuru wao wa kufikiri na kutenda peke yao. Hawataki kusikiliza mtu yeyote. Hawawajibiki kwa mtu yeyote. Ilikuwa na bado ni kazi maalum ya Shetani kuwafanya watu wahisi kuwa ni mpango wa **Mungu** kusimama peke yao na kuchagua utaratibu wao peke yao, usiohusisha ndugu zao. **—Letter 32, 1892.***{EVsw 318:2}*

Umbo Lisilo na Thamani Bila Kristo

Neema ya Kristo ndiyo inayotoa uzima kwa roho. Bila Kristo, ubatizo, kama huduma nyingine yoyote, ni umbo/mfumo na desturi isiyo na maana. "asiyemwamini Mwana hataona uzima."—**The Desire of Ages, 181 (1898).***{EVsw 318:2}*

Uongofu, Sio Ubatizo Pekee

Wokovu si kubatizwa tu, si kuandikwa majina yetu kwenye vitabu vya kanisa, wala si kuhubiri ile Kweli. Wokovu ni muungano hai na Yesu Kristo, kufanywa wapya katika mioyo, kufanya kazi za Kristo kwa imani, huduma ya upendo, subira, unyenyekevu, na matumaini. Kila roho iliyoungana na Kristo itakuwa ni mmshenari hai kwa wote walioizunguka. —**Letter 55, 1886.***{EVsw 319:1}*

Onyo kwa Wainjilisti na Wachungaji

Wahudumu wetu waaminifu wanashindwa kufanya kazi yao kama Bwana anavyotaka. Hawawatengenezi watu kuwa wateule kamili katika Kristo Yesu. Hawajapata uzoefu wa mawasiliano ya karibu na **Mungu** wala maarifa ya tabia ya Kikristo; kwa hivyo wengi hubatizwa ambao hawana sifa za huduma hii takatifu, bali walioungana nafsi zao na dunia. Hawajamuona Kristo wala kumkubali kwa imani. **— The Review and Herald, February 4, 1890.***{EVsw 319:2}*

Udhaifu katika Uinjilisti Wetu

Upatikanaji wa washiriki ambao hawajafanywa upya moyoni na kufanya matengenezo maishani, ni chanzo cha udhaifu kwa kanisa. Ukweli huu mara nyingi unapuuzwa. Baadhi ya wachungaji na makanisa wanatamani sana kupata ongezeko la idadi kiasi - kwamba hawatoi ushuhuda wa uaminifu dhidi ya tabia na mazoea yasiyo ya Kikristo. Wale wanaokubali Ukweli hawafundishwi kwamba hawawezi kuwa walimwengu kwa mwenendo wakati wao ni WaKristo kwa jina tu. Hapo awali walikuwa raia wa Shetani; tangu sasa wanapaswa kuwa raia wa Kristo. Maisha lazima yashuhudie kwamba ubadilishanaji wa kiongozi umetokea (sasa ni **Mungu** anaongoza). ***{EVsw 319:3}***

Wengi wanapendelea kuukiri UKristo. Kujinyima kidogo tu au kujitoanafsi vinahitajika ili kuvaa aina ya utauwa na mtu kuandikwa jina lake kwenye kitabu cha ushirika wa kanisa. Kwa hivyo wengi hujiunga na kanisa bila kwanza kuungana na Kristo. Katika hili Shetani anashinda. Waongofu kama hao ni mawakala wake wenye ufanisi zaidi. Wao hutumika katika udanganyifu wa roho zingine. Ni nuru za uongo, zinazowarubuni wasio na tahadhari katika upotevu. Haitafaa kitu kwa watu kutafuta kuifanya njia ya MKristo kuwa pana na yenye kuwapendeza walimwengu. **Mungu** hajalainisha au kupanua njia iliyoparuza na nyembamba. Kama tunataka kuingia uzimani, lazima tufuate njia ile ile ambayo Yesu na wanafunzi Wake waliipitia- njia ya unyenyekevu, kujinyima, kuikana nafsi na kujitoa. **—Testimonies For The Church 5:172 (1882).*{EVsw 319:4}***

Lengo Letu—Washiriki Walioongoka Kweli

Wachungaji wanaofanya kazi katika miji na majiji hawapaswi kujisikia kutosheka baada ya kuwasilisha Ukweli, wala kwamba kazi yao imekamilika, mpaka wale ambao wamekubali nadharia ya Ukweli watambue kwa hakika athari ya nguvu Zake za kutakasa na wameongoka kwa **Mungu** kweli. **Mungu** angefurahi zaidi kuwa na watu sita walioongoka kikweli kwa ile Kweli kama tokeo la kazi yao kuliko kuwa na watu sitini wanaojidai wamekiri Ukweli kwa jina tu ila bado hawajaongoka kikamilifu. Wachungaji hawa wanapaswa kutenga muda mchache katika kuhubiri mahubiri na kuweka sehemu ya nguvu zao kutembelea waongofu na kusali pamoja na wale wanaopendezwa, wakiwapa mafundisho ya Bwana, ili "waweze kumleta kila mtu mkamilifu katika Kristo Yesu. ***{EVsw 320:1}***

Upendo wa **Mungu** lazima uwe unaishi ndani ya moyo wa mwalimu wa Ukweli. Moyo wake mwenyewe lazima ufurike na upendo huo mzito na wa dhati aliokuwa nao Kristo; ndipo utatoka na kuwabubujikia wengine. Wachungaji wanapaswa kufundisha kwamba wote wanaokubali Ukweli wanapaswa kuzaa matunda kwa utukufu wa **Mungu**. Wanapaswa kufundisha kwamba kujikana nafsi lazima kufanyike kila siku; kwamba mambo mengi yaliyokuwa yamekumbatiwa lazima yasalimishwe; na kwamba majukumu mengi, hata kama yanaweza kuonekana kama yasiyokubalika au kupendeza, ni lazima yatekelezwe. Maslahi ya biashara, mapenzi ya kijamii, urahisi wa maisha au maisha bwerere, heshima, sifa, - kwa ufupi, kila kitu, lazima vitiishwe chini ya madai makuu na ya juu ya Kristo. **—Testimonies For The Church 4:317 (1879).*{EVsw 320:2}***

Kumaliza Kazi Kwa Uhakika- Kwa kuhitimisha vyema

Mwinjilisti Lazima Amalize Mafundisho Yake — Mtendakazi hapaswi kuacha sehemu yoyote ya kazi bila kuitimiza kwa sababu haimpendezi kuifanya au ni ngumu, akidhani kwamba mhudumu mwingine atakuja baadaye na kuifanya. Hali hii inaleta matatizo; mtu wa pili anapoingia na kuanzisha mada ya wajibu wa **Mungu** kwa watu Wake, wengi huzidi kukata tamaa wakisema, "Mchungaji aliyetuletea Kweli hakutaja vitu hivi." Na wanakasirika kwasabu ya Neno. Wengine wanakataa mfumo wa kutoa zaka, wanageukia mbali na kuacha kutembea pamoja na wale waliokuwa waaminifu na wenye mapenzi ya dhati kwa Ukweli. Wanapopelekewa mafundisho mapya wanajibu, "Hatukufundishwa hivi," na kushindwa kusonga mbele. Ni bora sana kama mchungaji wa kwanza angefundisha kwa uaminifu na kwa kina kuhusu mambo yote muhimu hawa wongofu, hata kama watu wachache wangekuwa wameongezwa kanisani chini ya huduma yake. — **Gospel Workers, 369, 370 (1915).*{EVsw 321:1}***

Kazi Isiyopaswa Kuachwa Ifunguke — Wahudumu hawatakiwi kudhani kuwa kazi yao imeisha hadi wale waliokubali Ukweli wa imani hiyo wanapobadili maisha yao na kupokea nguvu ya utakaso wa Kweli. Neno la **Mungu**, kama upanga mkali wenye pande mbili, linapochoma mioyo na kuamsha dhamiri, watu wengi hufikiri hapo ndiyo kazi imekamilika, lakini hiyo ni mwanzo tu. Hisia nzuri moyoni zimeanzishwa, lakini isipokuwa hizi zichunguzwe kwa bidii na kwa maombi, Ibilisi atazizuia. Watendakazi hawapaswi kuridhika na kile kilichofanywa. Upanga wa **Ukweli** lazima uende ndani zaidi, na hilo litatokea kwa bidii ya kuongoza mawazo na kudumisha imani ya wale wanaojifunza **Ukweli**.***{EVsw 321:2}***

Kazi nyingi huachwa zikiwa hazijakamilika (miganda ikiwa haijafungwa pamoja), na mara nyingi huwa hazina matokeo. Baadhi ya wachungaji wanapopata watu waliokubali Ukweli, mchungaji hufikiri anapaswa kuhama haraka kwenda sehemu mpya, au kwa mara nyingine wanahamishwa bila uangalifu wa kutosha. Hii ni makosa; lazima kumaliza kazi iliyoanzishwa. Kuiacha kazi ambayo haijakamilika ni kuleta madhara zaidi kuliko manufaa. Shamba lisilojaliwa vizuri huwa na magugu yakikua kwa wingi halina matunda au matumaini. Kwa njia hii, roho nyingi zimeachwa zikiteswa na Ibilisi na kushinikizwa na wafuasi wa makanisa mengine waliokataa Ukweli, na wengi wanalazimika kuondoka mahali ambapo hawatawafikia tena. Mchungaji ni bora asianzishe kazi kama hana uwezo wa kuimaliza kwa ukamilifu na kufunga miganda vizuri ili aiweke kwenye ghala.*{EVsw 322:1}*

Isipokuwa wale wanaopokea **Kweli** wawe wameongoka kwa kina, isipokuwa kuwe na mabadiliko ya kweli katika maisha na tabia, isipokuwa nafsi imefungwa imara juu ya Mwamba wa milele, haitaweza kustahimili majaribu ya wakati wa kujaribiwa. Mara tu mhubiri anapoondoka na mvuto wa mambo mapya unapopungua, **Kweli** hupoteza mvuto wake wa kuwateka, nao hawaleti athari yoyote takatifu kuliko hapo awali.*{EVsw 322:2}*

Kazi ya **Mungu** haipaswi kufanywa kwa njia ya uzembe, ugoigoi au kwa namna isiyo ya mpangilio. Mhubiri anapoingia katika uwanja wa kazi, anapaswa kuufanyia kazi uwanja huo kwa bidii na kwa ukamilifu. Asiridhike na mafanikio ya juujuu hadi atakapoweza, kwa kazi ya dhati na bidii na baraka kutoka mbinguni, kwa kumwasilishia Bwana waongofu walio na hisia ya kweli ya uwajibikaji wao, na ambao watafanya kazi waliyoitiwa. Ikiwa amewafundisha ipasavyo wale aliokuwa akiwatunza, basi anapoondoka kwenda kwenye mashamba mengine ya kazi, kazi hiyo haitayeyuka au kuporomoka; bali itakuwa imefungwa imara kiasi cha kuwa salama na yenye kudumu. —**Gospel Workers, 367-369 (1915).***{EVsw 322:3}*

Kufanya Kazi kwa Ukamilifu — Kuna hatari kwamba wale wanaoendesha mikutano mijini wataridhika na kazi ya juu-juu tu. Hebu wahudumu na viongozi wa konferensi waamke na kufanya kazi ya kina na iliyokamilila. hebu waendelee kwa bidii na mipango mikubwa wakizingatia kwamba wakati wa mwisho unakaribia, na kwa hiyo wanapaswa kufanya kazi kwa ari na nguvu zaidi. **— The Review and Herald, January 11, 1912.***{EVsw 323:1}*

Tunapopokea mwongozo wa **Mungu**, tusipange mipango mikubwa au kuchukua maeneo zaidi ya uwezo wetu wa kuifanya kazi ipite mpaka hatua ya mwisho kwa bidii na kuendeleza matarajio ya kuanzishwa. Wakati maeneo makubwa yanapoonekana kwa watendakazi, mawazo na mtazamo wa kazi lazima vipanuke zaidi ili kuleta roho nyingi kwenye Kweli. — **Letter 34, 1886.***{EVsw 323:2}*

Kuacha Kazi Iliyokamilika Vizuri — Makanisa huchipuka na kuanguka wakati maeneo mapya yanapoanzishwa. Makanisa haya hujengwa kwa gharama kubwa za kazi na rasilimali, kisha kukosa uangalizi na kuachwa na kisha kuharibika. Hivi ndivyo mambo yanavyoendelea sasa.*{EVsw 323:3}*

Nategemea kuwa utayaangalia mambo kwa busara, na siyo kwa mihemko au misukumo ya hisia tu. Tukiwa na kazi njiani, tusitegemee au kutamani kazi za mbali. **Mungu** hataki tuache kazi tuliyoianza na kuiacha ikiwa haijakamilika kwa kuwa huwa ni tatizo zaidi kuliko pale ambapo isingekuwa imeanzishwa kabisa. Naomba uangalie mambo kwa hekima na upana na si kwa haraka au hisia. *Wachungaji wetu wahamasishwe kufunzwa na kuelimishwa kufanya kazi zao kwa bidii zaidi. Wahakikishe wanamaliza kazi zao na wasiache bila kukamilisha. Wazingatie hasa mambo waliyoanzisha, na wasihame bila kuwa na kipaumbele maalum baada ya kuondoka kanisani. Hii imekuwa ni tatizo kubwa.* **— Letter 1, 1879.***{EVsw 324:1}*

Maslahi ya Nafsi Yanapaswa Kuwa Kipaumbele — Kwa miaka nuru imekuwa ikitolewa juu ya hatua hii, ikionyesha umuhimu wa kufuatilia masilahi ambayo yamekuzwa baada ya kufikia watu, na bila kuacha mpaka wote waamue kuegemea kwenye Ukweli na wamepata uongofu unaohitajika kwa ubatizo na kuungana na washiriki wengine walio na kanisa tayari au wapande kanisa lao wenyewe. *{EVsw 324:2}*

Hakuna hali ya umuhimu wa kutosha kumwita mchungaji kutoka kwa shauku na maslahi iliyoundwa na uwasilishaji wa Ukweli. Hata magonjwa na kifo hayana matokeo kuliko wokovu wa roho ambazo Kristo alijitoa kuwa dhabihu kubwa sana kwa ajili yao. Wale ambao wanahisi umuhimu wa Ukweli, na thamani ya roho ambazo Kristo alikufa kwa ajili yao, hawataacha maslahi kati ya watu kwa kuzingatia yoyote.

Watasema: Wacha wafu wazike wafu wao. Masilahi ya nyumbani, ardhi na nyumba, hayapaswi kuwa na nguvu hata ndogo ya kuvuta mtu kutoka uwanja wa kazi.*{EVsw 324:3}*

Ikiwa wachungaji wataruhusu mambo haya ya kidunia au ya muda mfupi, kuwaondoa kwenye kazi, Jukumu pekee lao kufuata ni kuacha vyote, kutokuwa na ardhi au masilahi ya muda mfupi, ambayo yatakuwa na ushawishi wa kuwavuta kutoka kwa kazi kubwa ya siku hizi za mwisho. Nafsi moja ina thamani zaidi kuliko ulimwengu wote. Je! inakuwaje wanaume wanaodai wamejitolea kwa kazi takatifu ya kuokoa roho, waruhusu mali zao ndogo za muda, kuingilia akili na mioyo yao, na kuwazuia kutoka kwa wito wa juu ambao wanadai kuwa wameupokea kutoka kwa **Mungu** **—Testimonies For The Church 2:540, 541 (1870).** *{EVsw 324:4}*

Hasara ya Kuacha Kazi Iliyokuwa Haijakamilika — Tuna ujasiri gani, au tunaweza kupata ujasiri gani, wa kufanya Efoti (mikutano) sehemu tofauti zinazotumia nguvu zetu zote mpaka mwisho, kisha kuondoka tukiacha kazi ipotee bila mtu wa kuitunza?*{EVsw 325:1}*

Nilipofika Marekani kutoka Ulaya, sikuhamia nyumbani, bali nikaenda hotelini kula chakula, halafu nikaenda mahali fulani ambapo ilipaswa kuwepo mipango ya kumpatia mtu kazi ya kumaliza kazi. Hapo palikuwa na watu matajiri na waliokuwa na dhambi kubwa moyoni na walisadikishwa mioyo. Ilikuwa ni kazi kubwa na yenye mvuto. Watu walikuja kwenye mikutano wakiwa na macho yaliyojaa machozi; waliguswa mioyo sana; lakini hakuwepo mtu wa kufuatilia maslahi hayo; maslahi yote yaliruhusiwa kurudi nyuma. Haya sio mambo yanayompendeza **Mungu**. Aidha sisi tunazidi kuenea katika maeneo makubwa sana ama kufanya kazi nyingi kuliko uwezo wetu. **— Manuscript 19b, 1890.***{EVsw 325:2}*

{Kufanya Eneo Kuwa Gumu kwa Wengine— Wachungaji wanaofanya kazi katika miji na majiji, wasiojiweka maisha yao wakfu, wanaochochea shauku miongoni mwa watu lakini wanaacha kazi ikiwa ngumu, wanatoka na kuacha huo uwanja mgumu sana kwa wengine kuingia na kumaliza kazi ambayo walishindwa kukamilisha. Watu hawa watathibitishwa; na ikiwa hawatafanya kazi yao kwa uaminifu zaidi, baada ya kujaribiwa zaidi, watawekwa kando kama wasumbubu au waharibifu wa ardhi, walinzi wasio waaminifu.— **— Testimonies For The Church, 4:317 (1879).***{EVsw 325:3}*

Matokeo ya Kazi Isiyofanywa kwa Umakini au Shagalabagala — Maliza kazi zako kwa kina-funga miganda. Usiachie mshono wowote wa kitambaa au nguo kwa mtu mwingine kuunganisha. Usimkatishe tamaa Kristo. Jitahidi kufanikisha, na kwa nguvu za Kristo utaweza kuonesha huduma yako kwa ukamilifu.*{EVsw 325:4}*

Hakuna kinachokatisha tamaa sana katika kuendeleza Ukweli wa sasa kama kazi ya ovyo inayofanywa na baadhi ya wahudumu kwa ajili ya makanisa. Kazi ya uaminifu inahitajika. Makanisa yako tayari kufa, kwa sababu hayajaimarishwa kuwa kama Kristo. Bwana hafurahishwi na njia mbovu ambayo makanisa yanaachwa kwa sababu watu sio mawakili waaminifu wa neema ya Mungu. Hawapokei neema Yake, na kwa hivyo hawawezi kuitoa. Kazi ya uaminifu inahitajika. Makanisa yamekuwa dhaifu, na yanaugua kwa sababu ya ukosefu wa uaminifu wa wale waliowekwa kusimamia na kuangalia roho, kama wale watakaotoa hesabu. **— Manuscript 8a, 1888.***{EVsw 326:1}*

Urefu wa Efoti (mkutano wa hadhara) na Kufunga Kampeni

Urefu wa Efoti/Jitihada Usipangwe na Binadamu

Kumbuka kwamba hakuna mwanadamu aishiye anayeweza kueleza kwa usahihi kazi kamili au kuweka mipaka ya kazi ya mtu aliye katika huduma ya **Mungu**. Hakuna anayeweza kupanga ni siku au wiki ngapi mhudumu fulani anapaswa kukaa katika eneo fulani kabla ya kuhamia mahali pengine. Hali halisi za mahali ndizo zinazopaswa kuongoza kazi ya mhudumu wa **Mungu**. mtumishi kimtafuta **Mungu** kwa bidii, ataelewa kuwa kazi yake inahusu kila sehemu ya shamba la Bwana—ya karibu na ya mbali. Mtendakazi wa **Mungu** hapaswi kufungiwa ndani ya vipimo vilivyowekwa. Kazi yake ni ya kuenea popote ambapo mahitaji yanajitokeza. **Mungu** Ndiye mshirika wake katika kazi; hivyo anapaswa kutafuta hekima na ushauri kutoka kwa **Mungu** katika kila hatua, na si kutegemea ushauri wa kianadamu.*{EVsw 326:2}*

Kazi imekwamishwa sana katika maeneo mengi kwa sababu watendakazi huomba mashauri kutoka kwa wale wasiofanya kazi katika uwanja, ambao hawaoni wala kuhisi mahitaji yaliyopo, na kwa hiyo

hawawezi kuelewa hali halisi kama yule aliye mstari wa mbele kazini katika mahali fulani. —**Letter 8, 1895.** *{EVsw 327:1}*

Chunguza Hali kwa Umakini

Wakati mhudumu amepangiwa kazi fulani, hapaswi kuamini kwamba ni lazima aulize kwa mwenyekiti wa konferensi kuhusu ni siku ngapi atahudumu katika eneo fulani. Badala yake, ni lazima atafute hekima kutoka kwa Yeye aliyempa kazi hiyo—Yule ambaye ameahidi kumpa hekima na uamuzi usio na kosa, anayetoa kwa wingi bila kulaumu. Mhudumu anapaswa kufikiria kwa makini kila sehemu ya eneo alilopewa, na kwa neema anayopokea, ajue nini afanye na nini asifanye. Kuna hali mbalimbali zitakazojitokeza, ambazo, zikitazamwa kwa unyenyekevu na kwa imani huku akitafuta hekima kwa **Mungu**, zitamfanya kuwa mtendakazi mwenye busara na mafanikio. —**Letter 8, 1895.***{EVsw 327:2}*

Kazi Kamili

Kazi katika _____ inapaswa kuendelea kwa muda wote ambapo bado kuna ari ya watu. Mahali panapofaa ni lazima patengwe kwa ajili ya mikutano kuendelea kufanyika. Kazi katika _____ haipaswi kukatizwa ghafla. Kwa miaka mingi nimekuwa nikiomba kwa dhati bidii kwamba juhudi za dhati zifanywe katika mji huu, na sasa kwa kuwa kazi hiyo inaanza kufanyika, hebu tusonge mbele kwa njia iliyo sahihi. —**Letter 380, 1906.***{EVsw 327:3}*

Kampeni ya Paulo ya Muda Mrefu huko Korintho

Bwana **Mungu** wa Israeli anatamani sana kuona matunda. Anawaita watendakazi Wake kutandaza huduma yao zaidi ya wanavyofanya sasa. Mtume Paulo alisafiri kutoka mji mmoja hadi mwingine, akihubiri Ukweli kwa wale waliokuwa gizani kwa sababu ya makosa ya imani. Alifanya kazi kwa mwaka mmoja na miezi sita huko Korintho, na kudhihirisha uhalali wa Bwana kujihusisha na utume wake kwa kuanzisha kanisa lililostawi, lililojumuisha Wayahudi na watu wa Mataifa. Waongofu kutoka kwa Mataifa walikuwa wengi zaidi kuliko Wayahudi, na wengi wao waliokoka kweli-kweli—walitoka gizani wakaingia katika nuru ya Injili. **Letter—Barua 96, 1902.***{EVsw 327:4}*

Juhudi za Muda Mrefu Katika Miji Mikubwa

Katika juhudi zinazofanywa katika miji mikubwa, nusu ya matokeo hupotea kwa sababu kazi hufungwa mapema mno na kuhamia eneo jipya.....Kuharakisha kufunga kazi imekuwa chanzo cha hasara kubwa mara nyingi. —**Letter 48, 1886.***{EVsw 328:1}*

Kupima Mafanikio ya Mikutano

Mungu Ndiye Mwamuzi wa Mafanikio ya Mtendakazi

Mungu, si mwanadamu, Ndiye mwamuzi wa kazi ya mtu, Naye atampatia kila mmoja thawabu yake ya haki. Hakuna mwanadamu aliyepewa mamlaka ya kuhukumu kati ya watumishi mbalimbali wa **Mungu**. Bwana peke yake Ndiye Hakimu na mtoaji wa thawabu kwa kila kazi njema. — **The Review and Herald, December 11, 1900.***{EVsw 328:2}*

Kama Nafsi Moja Itadumu, Kazi Hiyo Ina Mafanikio

Katika maono ya usiku nilikuwa nikizungumza nawe. Nilikuwa na ujumbe wako, nami nilikuwa nikikuwasilishia. Ulikuwa na huzuni, ukijihisi kushindwa. Nikakuambia, Bwana amenituma niseme na Ndugu na Dada _____. Nilisema unahesabu kazi yako kama iliyo karibu kushindwa, lakini ikiwa nafsi moja itashikilia Kweli na kudumu hadi mwisho, kazi yako haiwezi kuitwa kazi iliyoshindwa. Ikiwa mama mmoja ameongoka kutoka kutotii hadi utii, unapaswa kufurahi. Mama huyo atakayemtafuta Bwana ataweza kuwafundisha watoto wake wamfuate. Ahadi ni kwa akina baba, mama, na watoto wao.....*{EVsw 328:3}*

Bwana hatakuhukumu kwa kiwango cha mafanikio yanayoonekana kwa macho ya kibinadamu. Niliagizwa kukuambia kuwa imani yako inapaswa kuwa hai, yenye uamsho, thabiti, na ikue daima. Ukiona kuwa wale walio na masikio hawasikii, na wale walio na akili mahiri hawataki kuelewa, baada ya wewe kufanya kadiri ya uwezo wako, songa mbele na acha matokeo mikononi mwa **Mungu**. Lakini imani yako isikate tamaa. — **Letter 8, 1895.***{EVsw 329:1}*

Usikate Tamaa kwa Matokeo Madogo

Kazi inayofanywa kwa heshima na utukufu wa **Mungu** itabeba muhuri Wake. Kristo ataidhinisha kazi ya wale wanaofanya kwa bidii kadiri ya uwezo wao. Kadiri wanavyoendelea kufanya bidii, wataongezeka katika maarifa, na ubora wa kazi yao utaimarika. — **Letter 153, 1903.***{EVsw 329:2}*

Kwa idadi, wale wanaoikataa Kweli watakuwa wengi kuliko wanaoipokea, lakini nafsi moja ina thamani kuliko dunia nzima. Hatupaswi kukata tamaa, hata kama kazi yetu haileti matokeo makubwa. — **Letter 1, 1875.***{EVsw 329:3}*

Juhudi za Pamoja, na za Kudumu Huleta Mafanikio

Juhudi za mtu mmoja mmoja, za daima, na kwa umoja huzaa mafanikio. Wale wanaotamani kufanya mema mengi duniani, lazima wawe tayari kufanya hivyo kwa njia ya **Mungu**—kwa kufanya mambo madogo. Yule anayetaka kufikia kilele cha mafanikio kwa kufanya jambo kubwa la kushangaza, hatimaye atashindwa. *{EVsw 329:4}*

Kupiga hatua thabiti katika kazi njema, kurudia kazi ya uaminifu mara kwa mara, ni ya thamani zaidi mbele za **Mungu** kuliko kufanya kazi moja kubwa tu. Wale walio waaminifu kwa majukumu yao waliyopewa na Mungu, siyo watu wa msimu, bali ni thabiti, wakisonga mbele katika ripoti nzuri au mbaya. Wanakuwa tayari kwa kila wakati, iwe wakati mgumu au siyo mgumu. — **Letter 122, 1902.***{EVsw 329:5}*

Njia Sahihi Huleta Mavuno ya Roho

Tunapofanya kazi ya **Mungu** kwa kutumia mbinu au njia sahihi na kwa bidii, mavuno ya roho yatapatikana. — **The Review and Herald, April 28, 1904.***{EVsw 330:1}*

Hatari ya Kumtukuza Mhubiri

Kusifiwa na kushangiliwa kwa mhubiri si kielelezo kuwa amehubiri kwa nguvu ya Roho Mtakatifu. Mara nyingi waongofu wapya au vijana, wasipolindwa/wasipoelekezwa, huanza kumpenda mhubiri zaidi ya Mwokozi wao. Wanaona wamebarikiwa sana kwa sababu ya huduma ya mhubiri, na wanadhani yeye ndiye mwenye vipawa na neema bora zaidi, kwamba hakuna anayeweza kufanya bora kama huyo mhubiri. Huu ni ujasiri unaowasukuma kumwabudu mwanadamu, na kumtegemea zaidi kuliko Mungu, na kwa kufanya hivi hawampendezi Mungu wala hawakui katika neema. Hili hupelekea kumtukuza mwanadamu kuliko **Mungu**, hasa akiwa kijana ambaye anaelekea kuwa mwinjilisti mwenye matumaini siku za mbeleni.*{EVsw 330:2}*

Hii ni hatari kubwa kwa mhubiri, hasa ikiwa bado ni kijana. Mhubiri wa Kristo aliyejazwa na Roho na upendo wa Bwana wake, atahakikisha kuwa tabia ya **Mungu** na ya Yesu inaakisiwa kwa uwazi na utimilifu. Atawahubiria watu ili waelewe vyema tabia ya **Mungu**, na ulimwengu umpatie utukufu. — **Gospel Workers, uk. 44-45 (1892).***{EVsw 330:3}*

Kuongolewa na Mwanadamu, Si Kristo

Miaka minne iliyopita, kulikuwa na juhudi kutoka kwa Mzee _____ mahali pa _____. Watu walikusanyika kwa wingi kusikiliza. Kama mipango sahihi ingetumika, roho nyingi zingekuja kwenye Kweli. Lakini Mzee _____ hakufanya kazi kwa njia inayofaa; lengo lake kuu lilikuwa kuvutia umati mkubwa kwa mahubiri ya kuvutia, ambayo yalitofautiana sana na mahubiri ya Yohana, mtangulizi wa Kristo. Wengi walitia sahihi agano, lakini alipoondoka ilidhihirika kuwa waliamini kwa ajili ya mtu, si kwa ajili ya Yesu Kristo.

Wengi waliotia saini walikuwa hawajaongoka, na walipoachwa pekee, waliondoka. — **Letter 79, 1893.***{EVsw 330:4}*

Kanisa la Mzee Fulani?

Ungefurahi sana kama watu walioongolewa kupitia huduma yako wangeitwa “kanisa la Mzee _____.” Ungetamani kuzinyumbulisha fikra zao kwa namna ambayo wangeongozwa na mawazo yako. Lakini **Mungu** apishilie mbali! Kwa kuwafanya wategemee akili yako, unawafanya wajitenge na Chanzo cha hekima na ufanisi wao. Tegemeo lao halipaswi kuwa ndani yako bali liwe kwa Mungu tu, kikamilifu. Ni kwa njia hiyo tu wanaweza kukua katika neema. Wakimtegemea Yeye kwa mafanikio, kwa kunufaika, kwa nguvu ya kufanya kazi pamoja na Mungu.— **Letter 39, 1902.***{EVsw 331:1}*

Mali ya Kristo—Siyo Yetu

Kumbuka daima, Ndugu _____, haijalishi kazi ya mtu ni kubwa au nzuri kiasi gani, hafai kujiona kana kwamba yeye ndiye mmiliki wa wale waliomwamini Kristo kupitia kazi yake. Hakuna mtu anayepaswa kuwafanya waongofu wajiweke chini ya udhibiti wa mhubiri. Kazi yetu ni kuwaongoza watu moja kwa moja kwa Kristo. Wao ni mali ya Kristo, na ni Wake tu. Kila mtu ana utambulisho wa kipekee usioweza kudhibitiwa na mwingine. — **Letter 193, 1903.***{EVsw 331:2}*

Mungu Apokee Utukufu wa Mafanikio

Baada ya onyo kutolewa na Kweli kufunuliwa kutoka Maandiko, roho nyingi zitashawishika. Hapo ndipo utunzaji mkubwa unahitajika. Binadamu hawezi kufanya kazi ya Roho Mtakatifu. Sisi ni vyombo tu. Mara nyingi roho ya kujitegemea huingia endapo mafanikio fulani yanapatikana. Lakini hatupaswi kujitukuza, wala kutwaa sifa. Kazi ni ya Bwana, na Jina Lake tukufu linapaswa kutukuzwa. Nafsi zetu zijifiche ndani ya Yesu. — **The Review and Herald, October 14, 1902.***{EVsw 331:3}*

Mafanikio Hufifia Kwa Kujisifu Mwenyewe

Kila mtu anayejisifu mwenyewe, huharibu mvuto wa kazi yake bora kabisa. **— Testimonies for the Church, Gombo la 4, uk. 607 (1881).***{EVsw 332:1}*

Kuwatambua Wenza katika Kazi

Kila mmoja na afanye sehemu yake kwa uaminifu, na ampe heshima mtendakazi mwenzake kwa kazi anayofanya. Usichukue sifa zote peke yako. **Mungu** ametumia vyombo vingi katika kazi Yake. Kile ulichofanya ni sehemu tu ya kazi hiyo. Wengine pia wamefanya kazi kwa bidii na uaminifu, kwa maombi na kwa akili mahiri—na wasisahaulike. "Thawabu yYake iko pamoja Naye." Siku ya hesabu ya mwisho, **Mungu** atamhukumu kila mmoja kwa haki, kulingana na kazi yake. **Mungu** ameona maisha ya wale waliopitia magumu kwa ajili ya kazi yake katika kujikana nafsi, kujitoa mhanga na kuipeleka kazi katika maeneo magumu.*{EVsw 332:2}*

Haya ni mambo ya kuzingatia. Bwana hapendezwi na watumishi Wake wanapojisifu-wanapochukua sifa za ushindi. Hebu katika uzee wetu, tuwe waadilifu, tusijichukulie sifa zisizo zetu, za mambo ambayo wengine wamefanya. Imechukua miaka mingi kukamilisha kazi hii, na makundi mengi ya watendakazi waaminifu wamechangia. — **Letter 204, 1907.***{EVsw 332:3}*

Mwenendo na Mtazamo Wetu Wamzuia Bwana Kufanya Kazi

Bwana angetenda mambo makuu kupitia watumishi Wake, lakini mioyo yao haijanyenyekea. Ikiwa Bwana angewatumia, wangejigamba na kuwadharau ndugu zao. — **The Review and Herald, July 12, 1887.** *{EVsw 333:1}*

Sababu za Kukosa Mafanikio

Katika kiburi cha hekima ya dunia na tamaa ya kidunia ya kuwa wa kwanza, ndipo sababu ya kazi ya Injili kutofaulu licha ya kuwa na rasilimali zisizo na kikomo. Mwokozi wetu alifurahi rohoni na kumshukuru

Mungu, kwa kuwa thamani ya kweli, ingawa imefichwa kwa wenye hekima na werevu, imefunuliwa kwa watoto wachanga—wale wanaotambua udhaifu wao na kutegemea msaada Wake Bwana. **— Manuscript 118, 1902.***{EVsw 333:2}*

Thawabu ya Kuongoa Roho

Thawabu kuu itatolewa kwa wale watendakazi wa Kweli, wanaojitoa kikamilifu kwa kazi hii. Hakuna furaha iliyo kuu zaidi upande huu wa mbingu kama kuongoa roho kwa Kristo. Furaha hutawala moyoni mtu anapogundua kuwa muujiza huo mkuu haukuweza kutendeka kwa uwezo wa binadamu, bali kwa Yule anayewapenda wenye dhambi waliokuwa karibu kupotea. Uwepo wa **Mungu** uko karibu na kila mtendakazi wa Kweli, akifanya mioyo kutubu. Hapo ndipo ushirika wa Kikristo huanzishwa. Mtendakazi na wale wanaofanyiwa kazi wanaguswa na upendo wa Kristo. Moyo wagusa moyo, na muungano wa nafsi kwa nafsi unakuwa kama ule wa malaika wanaohudumu mbinguni. — **Manuscript 36, 1901.***{EVsw 333:3}*

SEHEMU YA 10—KUWAIMARISHA NA KUWADUMISHA WAONGOFU WAPYA

Mbinu za Kufuatilia

Mikutano ya Pili—Hitaji la Kurudia Mafundisho

Wakati hoja za Kweli ya sasa zinapowasilishwa kwa mara ya kwanza, ni vigumu sana kuzifunga katika akili za wasikilizaji. Ingawa baadhi yao huona kiasi cha kufanya uamuzi, bado kuna haja ya kurudia njia hiyo hiyo tena, na kutoa mfululizo mwingine wa mafundisho. —**Letter 60, 1886.***{EVsw 334:1}*

Kuhakikisha Kwamba Ukweli Umepokelewa Vizuri, na uwazi

Baada ya jitihada za kwanza za mahubiri ya hadhara kufanywa katika kutoa mfululizo wa mafundisho, kuna umuhimu mkubwa zaidi wa kutoa mfululizo wa pili kuliko ule wa kwanza. Ukweli ni mpya na wa kushangaza, na watu wanahitaji tuuwasilishe tena ili wapate kuelewa hoja zake waziwazi na kupachika vipengele hivyo akilini mwao. —**Letter 48, 1886.***{EVsw 334:2}*

Umuhimu wa Kurudia Hoja za Ukweli

ikiwa hata wale waliokwisha kujua na kuthibitishwa katika Kweli wanahitaji kuweka mbele yao mafundisho haya mara kwa mara ili akili zao ziamshwe; Je, si muhimu zaidi basi, kwa wale walio wapya katika imani, kwamba wasipuuzwe? Kila jambo katika tafsiri ya Maandiko ni geni na la ajabu kwao, na wako katika hatari ya kupoteza nguvu ya Kweli au kupokea mawazo yasiyo sahihi. Mara nyingi kazi imeachwa ikiwa haijakamilika. —**Letter 60, 1886.***{EVsw 334:3}*

Mpango Makini wa Mfululizo wa Mafundisho ya Ufuatiliaji

Huenda ikawa vizuri kubadili eneo na kuhudumia makundi mapya, lakini kila mara unapofanya juhudi ya pili ya ufuatiliaji, hebu na ifanywe kwa ukamilifu kana kwamba kazi ya kwanza haijafanywa bado. Hebu kila talanta waliyo nayo watenda kazi itumiwe kwa wabadilishanaji/kuchuuza..... Hebu kila mmoja ajitahidi na kushiriki kwa nguvu katika kazi na huduma ya **Mungu**.*{EVsw 335:1}*

Kuna kazi tofauti zinazopaswa kufanywa. Nafsi ni za thamani mbele za **Mungu**; wafundishe watu na uwaelekeze namna ya kubeba wajibu wanapokubali ile Kweli. Yeye aonaye mwisho tangu mwanzo, awezaye kufanya mbegu zilizopandwa kuzaa matunda kamili, atakuwa pamoja nawe katika juhudi zako. **—Barua 48, 1886.***{EVsw 335:2}*

Mfano wa Kazi ya Ufuatiliaji Iliyofanyika kwa Ukamilifu

Mkutano wetu umemalizika. Tangu siku ya kwanza, Oktoba 21 hadi sasa (Novemba 10), hamasa haijapungua. Katika mkutano wa kwanza, hema kubwa lilikuwa limejaa, na watu walizunguka kwa wingi nje. *{EVsw 335:3}*

Nilihubiri mara sita katika siku za Sabato, Jumapili, na Jumatano mchana, kwa kutano kubwa na mara tano kwa mistari fulani kwa ndugu zetu. Tulikuwa na huduma ya kichungaji nzuri……. Neno liliwasilishwa kama upanga kwa ujasiri, kwa ushuhuda wa Roho na kwa nguvu. Hamasa iliyokuwepo ilikuwa

ya kipekee kuliko mikutano mingine ya kambi katika nchi hii. Tunamshukuru Bwana kwa fursa hii ya kuangaza nuru ya Kweli ya sasa. Kama ilivyokuwa siku za Kristo, watu walishangaa na kuvutwa. Walisema, "Hatujawahi kusikia mambo kama haya. Laiti ningeyasikia haya mapema! Sikujua kuwa mambo haya yako katika Biblia." —**Barua 27, 1897. Ninaona kazi iliyo mbele yangu, ambayo inanipasa niifanye, ni kuchunguza Maandiko, kwa njia ambayo sijafanya bado.***{EVsw 335:4}*

Hakika Neno la Mungu limekuwa kama upanga, mwepesi na mwenye nguvu. Umati wa watu umesikiliza kwa hamu kubwa, karibia saa mbili bila kuonyesha mwonekano wowote wa uchovu. Loo, ninafurahi sana, moyo wangu una shukrani nyingi. Nami ninamsifu Bwana kwa moyo, roho na sauti……{EVsw 336:1}

Wafanyakazi kadhaa wanafuatilia na kusonga mbele na shauku zilizoonyesha huko katika Stanmore. Shauku hii ya watu haijazimika, bado inaendelea. Hema kubwa limeondolewa na kupelekwa Melbourne (Australia). Hema la futi arobaini limeunganishwa katikati na hema jingine, ili liweze kuchukua watu wengi iwezekanavyo, na litatumika hapa. Nyumba ya kuwatosha watendakazi wanaohudumu imekodishwa. Chumba kimeandaliwa kwa ajili yangu, nami nikiweza, ningependa kwenda Sydney wiki hii kujiunga na watendakazi. Lazima tufanye yote tuwezayo ili kufanikisha Efoti hii. Mzee Haskell anaandika kwa furaha kuhusu kazi huko na shauku ya watu isiyoyumba.—Barua 27, 1897.{EVsw 336:2}

Kujenga juu ya Hamasa Iliyopatikana

Watendakazi wanaokuja baadaye kuendeleza kazi huenda wasiwe wanawake na wanaume wenye uwezo mkubwa kama wale walioanza kazi, lakini kama ni watu wanyenyekevu wa **Mungu**, wanaweza kuwasilisha Kweli kwa namna ambayo itagusa mioyo ambayo haikuguswa hapo awali. **Mungu** hufunua Kweli kwa nyanja mbalimbali kwa watu tofauti-tofauti, na hivyo kupitia kwa mhubiri mmoja, hoja fulani huweza kuonekana wazi zaidi. Na kwa sababu hii Mungu haruhusu mtu mmoja peke yake, kufanya kazi ya kushugulika na akili ya mwanadamu.....*{EVsw 336:3}*

Kwa hiyo, mtu asijione kuwa ni lazima afanye kazi yote peke yake. Kama kuna wengine waliobarikiwa kwa kazi hiyo, basi ashughulikie nao kwa furaha.

Mtu mmoja anaweza kufanya sehemu yake ya kazi kadiri awezavyo, na kisha Bwana atamtuma mtendakazi mwingine kufanya sehemu nyingine ya kazi ambayo mtendakazi wa kwanza hakuhisi umuhimu wa kuifanya, na wakati ilikuwa muhimu kufanywa. Kwa hivyo mtu yeyote asihisi kwamba ni wajibu wake kuianza na kuendeleza kazi ya injili mwenyewe mpaka mwisho. Ikiwa ni mapenzi ya Bwana, hebu vipawa vingine walivyonavyo watendakazi wengine vitumike ili kufanya kazi kwa ajili ya uongofu wa roho, na kisha yule mtendakazi wa kwanza, ashirikiane na wale wanaokuja baadaye kwa furaha.—Manuscript 21, 1894.

—**Manuscript 21, 1894.***{EVsw 336:4}*

Kuwafundisha Waongofu Wapya kwa Ukamilifu

Jitihada zetu hazipaswi kukoma kwa sababu mikutano ya hadhara imesitishwa kwa muda. Mradi bado kuna walio na hamu ya kujifunza, hebu tuwape fursa hiyo. Waongofu wapya wanahitaji kufundishwa na walimu waaminifu wa Neno la **Mungu** ili wakue katika maarifa na upendo wa kweli, hadi wafikie ukomavu kamili katika Kristo Yesu. Wanapaswa kuzungukwa na mazingira bora yenye ushawisi wa ukuaji wa kiroho. — **Review and Herald, February 14, 1907***{EVsw 337:1}*

Kuendeleza Vipawa vya Ndani ya Kanisa Mahalia

Fanya kazi ya mwinjilisti—mwagilia na kuendeleza mbegu iliyopandwa. Kanisa jipya likiinuliwa, lisiachwe bila msaada. Mchungaji anapaswa kukuza vipawa vya waumini ili mikutano iwe endelevu. Timotheo aliagizwa kwenda kutoka kanisa moja hadi jingine akifanya kazi hii ya kuimarisha makanisa, na kujenga makanisa kwaajili ya imani hii takatifu. Alipaswa kufanya kazi ya Mwinjilisti, na hii ni kazi muhimu zaidi hata kuliko ile ya wachungaji. Alipaswa kuhubiri Neno la Mungu, ila hakupaswa kukaa katika kanisa moja. —**Review and Herald, September 28, 1897.***{EVsw 337:2}*

Kuwatembelea Washiriki Wapya Mara kwa Mara

Kazi haipaswi kuachwa mapema. Angalieni kwamba wote wana akili katika Ukweli, wameimarika katika imani, na wanapendezwa na kila tawi la kazi, kabla ya kuwaacha na kwenda sehemu nyingine. Na kisha, kama mtume Paulo, watembeleeni mara kwa mara ili muone jinsi wanavyofanya. Loo, kazi ya ulegevu ambayo hufanywa na wengi wanaodai kwamba wameagizwa na **Mungu** kuhubiri Neno Lake, hili huwafanya Malaika kulia machozi. **—Testimonies for the Church 5:256 (1885).***{EVsw 337:3}*

Mstari kwa Mstari, Amri kwa Amri

Sio kazi ya kuhubiri tu ndiyo inayopaswa kufanywa. Tunahitaji mahubiri machache zaidi na mafundisho ya kina zaidi. Wahubiri wanapaswa kuwapa watu nafasi ya kueleza maoni yao. Ni Mafundisho ya Biblia ndiyo watu huhitaji-, mstari kwa mstari, amri kwa amri, hapa kidogo na pale kidogo.. **—Manuscript 7, 1891.***{EVsw 338:1}*

Lakini ni vigumu sana kuwasadikisha ndugu zetu wanaohudumu kwa wazo kwamba mahubiri pekee hayawezi kufanya kazi inayohitajika kwa makanisa yetu. Juhudi binafsi zinahitajika; nazo ni muhimu kwa ustawi wa kila mtu binafsi na makanisa pia.—Manuscript 7, 1891.{EVsw 338:2}

Msaada wa Kuanza Maisha Mapya

Pale ambapo hamasa imeamshwa kama ilivyo sasa,------watu wa uwezo bora wanapaswa kuchaguliwa kushiriki katika efoti, yaani mkutano wa hadhara. hebu na wajitoe kwa moyo wote katika kutembelea na kufanya masomo ya Biblia na waongofu wapya katika imani na wale wanaovutiwa, ili kuwaimarisha katika imani. Waumini wapya wanapaswa kufundishwa kwa uangalifu, ili waweze kuwa na ujuzi mahiri wa aina mbalimbali za kazi zilizotolewa kwa kanisa la Kristo. Mzigo wa kazi hii hauwezi kuachiwa mtu mmoja au wawili tu.*{EVsw 338:3}*

Mengi mema hutimizwa kwa kazi inayofanywa na kila mshiriki wa kanisa kwa kushirikiana katika kazi ya ufuatiliaji baada ya mikutano ya hema katika miji yetu. ***Wakati wa mkutano, wengi, wakiwa wamesadikishwa na Roho, wanaweza kuwa na shauku kubwa ya kuanza maisha ya Kikristo; lakini isipokuwa kuwe na uangalifu wa kila mara kwa upande wa watendakazi wanaobaki kufuatilia maslahi ya wale walioonyesha kumfuata Masihi, hisia nzuri zinazotolewa katika akili za watu hazitaweza kubainishwa. Adui, akiwa amejaa mawazo ya hila, atachukua fursa ya kila kushindwa kwa watendakazi wa Mungu, wanaoshindwa kulinda roho kama wale ambao lazima watoe hesabu kwa Bwana.*** (Bila uangalizi wa kudumu, mvuto mzuri uliopatikana utatoweka. Adui atatumia kila nafasi na hila na hoja, wanayopoteza watendakazi wa **Mungu** kuzikamata roho hizo zilizotoa maisha yao kwa Bwana.) — **Review and Herald, March 2, 1905.***{EVsw 338:4}*

Kujenga Ngome Kuzunguka Waumini Wapya

—Mara tu baada ya maamuzi kufanywa, nguvu za mamlaka ya giza hutwaa akili hizi ambazo zimesadikishwa na injili, na ambazo kwa njia fulani zimepinga kusadikishwa na Roho wa Mungu. Roho hizi zinajikuta zina ushirikina, na Shetani hufanya kazi kwenye akili hizo na kuleta upinzani mkali kwa ile Kweli na kila mtu anayeuamini Ukweli, na watu hao hufikiri wanamfanyia Mungu huduma, kama Kristo alivyotuambia, “Kila mtu awauaye ninyi atadhani anamfanyia Mungu Ibada. -Yohana 16:2.” *{EVsw 339:1}*

> Sasa tunaweza kuona msukumo wa akili zao. Nguvu hiyo iko wapi upande mwingine? Hali hii lazima ikabiliwe kwa nguvu sawa kutoka upande wa Kweli. Ungana na Roho wa Mungu aliye hai ili kutoa ulinzi kwa kujenga ngome karibu na watu wetu na karibu na vijana wetu ili kuwalinda, kuwaelimisha na kuwafunza. Hili lazima litimizwe, na lazima tuendelee moja kwa moja katika Ukweli wa Mungu kwa gharama yoyote. Sisi tunaelewa jambo fulani kuhusu hii hali, lakini kuna wengi ambao hawaelewi chochote kuhusiana na jambo hili, kwa hivyo tunahitaji kuwaongoza, kuwafundisha kwa upole na huruma nyororo, na ikiwa Roho wa Mungu Yuko pamoja nasi, tutajua nini cha kusema.—Manuscript 42, 1894.*{EVsw 339:2}*

Ufahamu wa Kusudi Kuu la Mungu

Mwanafunzi anapaswa kujifunza kulitazama Neno la **Mungu** kama jumla, na kuelewa uhusiano wa sehemu zake. Ajifunze kuhusu mada kuu—kusudi la **Mungu** tangu mwanzo, chimbuko la pambano kuu, na

kazi ya ukombozi. Aelewe asili ya kanuni mbili zinazopigana kutawala, na azitambue katika historia na unabii hadi mwisho wa yote. Aone jinsi pambano hili linavyohusiana na kila nyanja ya maisha ya binadamu, na jinsi kila tendo linavyoonyesha upande wa pambano anaouunga mkono. —**Education, uk. 190 (1903).** ***{EVsw 339:3}***

Kuwafundisha Waumini Wapya Kukabiliana na Adui

Ni sera mbaya kuwaach awatu wachache hapa na pale bila chakula na bila uangalizi, wawe lengo rahisi la mbwa mwitu au mashambulizi ya adui. Nimeonyeshwa kuwa kazi ya namna hii imetendeka sana miongoni mwetu. Maeneo yenye matumaini yameharibiwa kwa efoti za mbeleni, kuingia haraka kwenye kitui cha kufanya uinjilisti, bila kukadiria gharama na kisha kazi imeachwa nusu, na roho zenye maarifa kidogo juu ya Kweli zimesalia bila kuimarishwa na kuwasaidia waongofu wapya kusimama katika imani, na kuwafundisha kuwa wanajeshi imara, tayari kukutana na mashambulio ya adui na kumshinda kikamilifu. — **Letter 60, 1886.*{EVsw 340:1}***

Kuwajumuisha Waumini Wapya Katika Kanisa

Kuongozwa Kama Watoto

"**Mathayo 18:1-6** *Saa ile wanafunzi wakamwendea Yesu wakisema, Ni nani basi aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni? Akaita mtoto mmoja, akamweka katikati yao, akasema, Amin, nawaambia, Msipoongoka na kuwa kama vitoto, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni. Majaribu ya Dhambi. Basi, yeyote ajinyenyekeshaye mwenyewe kama mtoto huyu, huyo ndiye aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni. Na yeyote atakayempokea mtoto mmoja mfano wa huyu kwa Jina Langu, anipokea Mimi; bali atakayemkosesha mmojawapo wa wadogo hawa waniaminio, yamfaa afungiwe shingoni jiwe kubwa la kusagia, na kutoswa katika kilindi cha bahari."****{EVsw 340:2}***

Yesu aliposema "wadogo hawa" hakumaanisha watoto wachanga. Aliowakusudia katika Maneno haya ni wale "wanaoamini ndani Yangu" lakini hawajapata uzoefu kamili wa kumfuata Kristo—wale wanaohitaji kuongozwa kama watoto katika kutafuta mambo ya ufalme wa mbinguni. — **Manuscript 60, 1904.*{EVsw 341:1}***

Shauri kwa Watu Waliompokea Imani Mpya

Ninawalenga ninyi mliokuja kwenye maarifa ya Kweli kule _____. Ninyi ni wachanga katika imani, na kuna haja kubwa ya kutembea kwa unyenyekevu pamoja na **Mungu**, mkijifunza kila siku katika shule ya Kristo kwa kutafakari na kuzungumzia mafundisho Aliyowapa wanafunzi Wake. Tembeeni kwa unyenyekevu wa moyo, mkiwa hamjiamini, mkimtafuta **Mungu** wa hekima ili njia zenu zote ziambatane kwa karibu na mapenzi na njia za **Mungu**, ili kusiwe na mkanganyiko wowote.....***{EVsw 341:2}***

Tukumbuke daima kuwa ni kazi ngumu kuwaondoa watu kwenye makosa waliyopokea tangu utotoni. Tuelewe kuwa dunia si mbinguni, na tutakutana na hali za kukatisha tamaa ambazo lazima tushinde, lakini tuvumiliane kwa upole sikitiko, na huruma nyororo na wema na wale walio gizani. Kuwaleta katika nuru hakutafanikishwa kwa hoja tu, bali ni kazi ya neema ya Kristo moyoni mwenu, ikidhihirika katika tabia zenu kwa uthabiti, lakini kwa upole, usahili na unyenyekevu wa Kristo. Kwa maombi mengi fanyeni kazi kwa ajili ya roho, maana ni njia hii pekee ya kugusa mioyo. Sio kazi yenu, bali ni kazi ya Kristo aliye kando yenu, Ndiye anayegusa mioyo.....***{EVsw 341:3}***

Jitahidini kutokutofautiana ninyi kwa ninyi, bali kuwa na amani ya Kristo mioyoni mwenu. Hii ikikamilika, italeta urahisi katika kuileta pia kwenye familia zenu. Lakini kama bustani ya moyo itapuuzwa, magugu ya sumu kama kiburi, kujiona, na kujitegemea wenyewe, yatastawi kwa nguvu. Kila mmoja wetu lazima aendelee kuomba daima. ***{EVsw 342:1}***

Tabia tunazojenga zitaonekana katika maisha ya nyumbani. Ikiwa kuna maelewano mema katika familia, malaika wa **Mungu** watakuwa miongoni mwao. Ikiwa kuna uongozi wenye hekima nyumbani—upole, uvumilivu, huruma, pamoja na kanuni imara—basi baba wa familia huyo ni "kifungo cha nyumba-houseband"; huunganisha familia kwa kamba takatifu na kuiwasilisha mbele za **Mungu**, akijifunga nao juu ya madhabahu ya **Mungu**. Jinsi gani nuru kubwa hutoka katika familia kama hiyo! ***{EVsw 342:2}***

Familia inayosimamiwa ipasavyo ni hoja yenye uzito kwa ajili ya Ukweli, na kiongozi wa familia hiyo atafanya kazi hiyo hiyo katika kanisa kama afanyavyo nyumbani. Pale ambapo kuna ukali, ukatili, na ukosefu wa upendo katika familia, hakika kutakuwa na kushindwa katika mipango na uongozi wa kanisa. Umoja

nyumbani na umoja kanisani huonyesha njia ya Kristo na neema Yake zaidi kuliko mahubiri na hoja za akili..... Je! Kweli tuliyoipokea—ile ya juu zaidi—inaleta katika mioyo yetu matunda ya uvumilivu, imani, tumaini, na upendo, na hivyo kuacha athari ya wokovu juu ya akili za wanadamu, ikionyesha kuwa sisi ni matawi ya mzabibu wa Kweli kwa sababu tunazaa matunda mengi? — **Letter 6b, 1890.***{EVsw 342:3}*

Kuwa na Mizizi Ndani Yao

Sio kusudi la **Mungu** kwamba kanisa liishi kwa kutegemea maisha kutoka kwa mhubiri. Waumini wanapaswa kuwa na mizizi ndani yao wenyewe. Habari Njema za injili, ujumbe wa onyo, ujumbe wa malaika wa tatu, unapaswa kutangazwa na washiriki wa kanisa. — **Manuscript 83, 1897.***{EVsw 343:1}*

Kila mmoja anayedai kuwa MKristo anapaswa kubeba jukumu la kuhakikisha anasalia katika uhusiano sahihi na uongozi wa Neno la **Mungu**. **Mungu** humwajibisha kila mtu binafsi kwa kufuata mfano wa maisha ya Kristo na kwa kuwa na tabia iliyotakaswa na kusafishwa. — **Manuscript 63, 1907.***{EVsw 343:2}*

Wachungaji Wasichukue Nafasi ya Mungu

Wakati waongofu wapya wanapaswa kufundishwa kuomba ushauri kutoka kwa wale walio na uzoefu zaidi katika kazi hiyo, wanapaswa pia kufundishwa kutomuweka mchungaji badala ya **Mungu**. Wachungaji ni wanadamu tu, watu waliozungukwa na madhaifu. Kristo Ndiye ambaye tunapaswa kutafuta mwongozo Kwake. **— Testimonies for the Church 7:20 (1904).***{EVsw 343:3}*

Misingi ya Kuwafundishia Waumini Wapya

Wahubiri mara nyingi hupuuzia matawi haya muhimu ya kazi—matengenezo ya afya, karama za roho, utoaji wa mpango, na matawi makubwa ya kazi ya umishenari. Kwa juhudi zao, watu wengi wanaweza kuukubali Ukweli wa kiakili tu, lakini baadaye inabainika kuwa wengi hawawezi kuvumilia kujaribiwa na **Mungu**.....*{EVsw 343:4}*

Ingekuwa bora zaidi kwa kazi ya **Mungu** kama mhubiri wa Ukweli angewafundisha kikamilifu waongofu hawa kuhusu mambo haya yote muhimu, hata kama idadi ya waliopokea ubatizo chini ya uongozi wake ingekuwa ndogo.*{EVsw 343:5}*

Wachungaji lazima waweke katika mioyo ya wale wanaowahudumia umuhimu wa kubeba mizigo ya kazi ya **Mungu**. Wanapaswa kufundishwa kwamba kila idara ya kazi ya **Mungu** inahitaji msaada wao na shauku yao. Uwanja mkubwa wa kimishenariuko wazi kwa watu wote, na mada hii inapaswa kusisitizwa tena na tena.*{EVsw 344:1}*

Watu lazima waelewe kwamba si wasikilizaji wa Neno, bali watendaji wa Neno, ndio watakaopewa uzima wa milele. Hakuna mtu yeyote aliye huru dhidi ya kazi hii ya kutoa kwa ukarimu. **Mungu** anawataka wote waliopokea neema Yake kutoa, si tu kwa mali zao kwa ajili ya kazi ya **Mungu**, bali pia kujitoa nafsi zao kikamilifu kwa **Mungu ila ya kujibakiza**.....*{EVsw 344:2}*

Ukarimu si tabia ya moyo wa asili; watu lazima wafundishwe, mstari juu ya mstari, amri juu ya amri, jinsi ya kufanya kazi na jinsi ya kutoa kwa mpangilio wa **Mungu**. — **The Review and Herald, December 12, 1878.***{EVsw 344:3}*

Kukuza Mwelekeo Mpya kwa Kazi ya Mungu

Ni kiasi gani kinachotumika kwa vitu visivyo na maana, vitu vinavyoshika fikra na mapenzi—mapambo madogo yanayohitaji kusafishwa na kupangwa ili kupunguza vumbi. Muda unaotumika kupanga mapamboau sanamu hizi ungetumika kusema neno kwa wakati kwa roho fulani, akichochea kuuliza, “Nifanye nini ili niokoke?” Mambo haya madogo hutumia muda ambao unapaswa kutumika kuomba, kumtafuta Bwana, na kushika kwa imani ahadi Zake.....*{EVsw 344:3}*

Ninapoona mambo mengi yanayoweza kufanywa katika nchi kama hii niliyomo sasa, moyo wangu huwaka kwa hamu ya kuwaonyesha wale wanaodai kuwa watoto wa **Mungu** jinsi wanavyopoteza pesa nyingi kwa mavazi, samani/fanicha ya kifahari, au starehe binafsi, hata kwa safari za anasa zisizo na maana ya kiroho. Haya yote ni matumizi mabaya, ubaradhifu wa mali ya Bwana, kuitumia kwa ajili ya nafsi badala ya kuitumia katika huduma Yake. — **Letter 42a, 1893.***{EVsw 344:4}*

WaKristo Wenye Manufaa

Kazi ya mabalozi wa Kristo ni kubwa sana na ina wajibu mkubwa kuliko wengi wanavyodhani. Hawapaswi kwa namna yoyote kutosheka na mafanikio yao mpaka watakapoweza, kwa utendaji kazi wao wa dhati na mbaraka wa **Mungu**, kuwawasilisha WaKristo wanaofaa walio na utambuzi wa Kweli wa wajibu walionao na kuwa tayari kwa ajili ya kazi waliyopewa. Utendaji kazi ulio thabiti na maelekezo vitaleta mpangilio wa kazi kwa wanaume na wanawake ambao tabia zao ni imara na imani zao ni thabiti kiasi kwamba hakuna chembechembe yoyote ya ubinafsi ndani yao itakayowakwamisha wasifanye kazi, kudhoofisha imani yao, au kuwavunja moyo wasiwajibike. — **Testimonies for the Church 4:398, 399 (1880).*{EVsw 345:1}***

Kuwatunza Waumini Wapya

Wakati wanaume na wanawake wanapoikubali Kweli, hatupaswi kuwaacha na kwenda zetu bila kuwa na mzigo zaidi kwa ajili yao. Tunapaswa kuwatunza. Wanapaswa kubebwa kama mzigo juu ya roho zetu, na ni lazima tuwaangalie kama wasimamizi ambao tutatoa hesabu. tena kila unapozungumza na watu, wape kila mmoja sehemu yake ya chakula kwa wakati wake; lakini ni lazima uwe katika hali ya kuweza kuwapa chakula hiki. **— Manuscript 13, 1888.*{EVsw 345:2}***

Lisha Wana-kondoo Wangu

Bwana Yesu alimwambia Petro, ***Luka 22:32*** *"Utakapongoka, waimarishe na ndugu zako"*; na baada ya kufufuka, kabla hajapaa, alimwambia Petro: **Yohana 21: 15** "*Je, Simoni wa Yohana, wanipenda Mimi kuliko hawa*?" Akamwambia, "*Naam, Bwana; Wewe wajua kuwa nakupenda*." Yesu akamwambia, "*Lisha wana-kondoo Wangu*." ***{EVsw 346:1}***

Hili lilikuwa ni jukumu ambalo Petro alikuwa hana uzoefu nalo; lakini hangeweza kukamilika katika maisha ya Kikristo bila kujifunza kuwalisha wana-kondoo—wale walio wachanga katika imani. Letter 3, 1892 ***{EVsw 346:2}***

Jambo hili linahitaji uangalifu mkubwa, subira ya kudumu, na ustahimilivu, kuwafundisha wale wasio na maarifa kwa njia inayofaa, kufungua Maandiko na kuwaelimisha kwa ajili ya utumishi wenye kunufaisha. Hii ndiyo kazi ambayo lazima ifanyike katika kanisa leo, la sivyo watetezi wa ile Kweli watakuwa na uzoefu wa kudumaa na watawekwa wazi kwa majaribu na udanganyifu. Agizo alilopewa Petro linapaswa kuwa mwito wa kila mchungaji. Mara kwa mara sauti ya Kristo inasikika ikirudia agizo kwa wachungaji Wake wa chini: "*Lisha wana-kondoo Wangu*," "*Lisha wanakondoo wangu*." —**Letter 3, 1892.*{EVsw 345:1}***

Katika haya Maneno aliyoelekezwa Petro na Kristo, majukumu ya mhudumu wa injili ambaye anasimamia kundi la Mungu yamewekwa mbele yake.—Barua ya 3, 1892.v{EVsw 346:2}

Kulisha Kundi la Wana-kondoo wa Mungu

Ndugu zangu katika huduma ya Injili, hebu tuwalishe wana-kondoo wa **Mungu**. Hebu tulete faraja, uchangamfu na furaha mioyoni mwa watu. Hebu tugeuze macho ya ndugu na dada zetu kutoka kwa udhaifu wa tabia ya wanadamu, na watu waelekezwe kumtazama Kristo, aliye mzuri kupita wote, Mkuu kuliko elfu kumi.....***{EVsw 346:3}***

Mungu amekabidhi kwa wanadamu hazina za Kweli za thamani kubwa. Hazina hizi zinaweza kufananishwa na matunda mazuri, ambayo yanapaswa kuwasilishwa kwa watu katika vyombo safi, vitakatifu, ili wapokee matunda hayo na kuyafurahia, kwa utukufu wa **Mungu**. —**Manuscript 127, 1902.*{EVsw 346:4}***

Tembelea Kila Familia

Kama mchungaji wa kundi, [mchungaji] anapaswa kuwajali kondoo na wana-kondoo, kuwatafuta waliopotea na waliopotoka, na kuwarudisha zizini. Anapaswa kutembelea kila familia, si kwa ajili ya kustarehe tu na kufurahia kuhudumiwa kwa ukarimu na wenyeji, bali kuulizia hali ya kiroho ya kila mshiriki wa nyumba hiyo. Nafsi yake mwenyewe lazima ijazwe na upendo wa **Mungu**; kisha kwa upole na adabu anaweza kufika mioyoni mwao wote, na kufanya kazi kwa mafanikio kwa ajili ya wazazi na watoto, akihimiza, akiwaonya, na kuwatia moyo kulingana na mahitaji. —**The Signs of the Times, January 28, 1886.** ***{EVsw 346:5}***

Karibia Mioyo ya Watu

Karibia ndugu zako; watafute, wasaidie; karibia mioyo yao ukiwa umeguswa na hisia za madhaifu na mapungufu yao. Hivyo tunaweza kushinda kwa njia ambazo imani yetu ndogo haikutarajia. Watu wa familia hizi wanapaswa kupewa kazi fulani kwa ajili ya wokovu wa wengine. Upendo na imani ya pamoja vitawapa nguvu ya kimaadili kushirikiana na **Mungu**. **—Manuscript 42, 1898.***{EVsw 347:1}*

Miiba Lazima Ing'olewe

Wengi wanaodai kuwa WaKristo wamejishughulisha mno na mambo ya dunia kiasi kwamba hawana muda wa kukuza uchaji-Mungu. Hawaoni dini ya kweli kuwa ni jambo la kwanza. Mtu anaweza kuonekana amepokea ile Kweli, lakini asiposhinda tabia zisizo za Kikristo, miiba hiyo hukua na kuangamiza neema ya Roho. Miiba hiyo lazima ing'olewe na kutupwa nje, kwa kuwa mema na mabaya hayawezi kukua pamoja moyoni. Tamaa na mielekeo ya kibinadamu isiyofanywa kuwa mitakatifu lazima iondolewe kama vizuizi vya kukua kiroho. **—Letter 13, 1902.***{EVsw 347:2}*

Kukemea na Kuhimiza

Kazi ya kichungaji ni pamoja na kukemea na kuhimiza kwa uvumilivu wote na mafundisho; yaani, mhudumu anapaswa kuwasilisha Neno la **Mungu**, kuonyesha palipo na upungufu. Ikiwa kuna jambo lolote katika tabia ya wale wanaodai kumfuata Kristo, mzigo huo lazima uhisiwe na mchungaji, lakini si kwa kujifanya kuwa bwana wa urithi wa **Mungu**. Kushughulika na akili za wanadamu ni kazi nyeti kuliko zote alizowahi kupewa mtu. —**Manuscript 13, 1888.***{EVsw 347:3}*

Somo la Biblia Badala ya Mahubiri Marefu

Mara nyingi nimeonyeshwa kuwa kunapaswa kuwa na mahubiri machache kutoka kwa wahudumu wanaohudumu kama wachungaji wa maeneo, na juhudi za binafsi zichukuliwe zaidi. Watu wetu wasifikiri kuwa ni lazima kusikiliza mahubiri kila Sabato. Mara nyingi ingekuwa na faida zaidi kama mikutano ya Sabato ingekuwa ya aina ya darasa la Biblia. Kweli ya Biblia inapaswa kuwasilishwa kwa njia rahisi na ya kuvutia, ili kila mtu aweze kuielewa na kushika kanuni za wokovu. —**Letter 192, 1906.***{EVsw 348:1}*

Zaidi ya Mahubiri Yanahitajika

Mhudumu /mcungajini mtu anayehudumu. Ukijifungia tu katika mahubiri, kundi la **Mungu** litateseka; kwa maana wanahitaji juhudi za binafsi. Mahubiri yako yawe mafupi. Mahubiri marefu huwachosha watu na wewe pia. Kama wahudumu wangefanya mahubiri yao kuwa nusu ya urefu wa sasa, wangeleta manufaa zaidi na kubakiza nguvu kwa ajili ya kazi ya binafsi. Tembelea familia, sali pamoja nao, zungumza nao, chunguza Maandiko pamoja nao, nawe utawafaidisha. Wape ushahidi kuwa unajali maendeleo yao na unataka wawe WaKristo wenye afya. **—Manuscript 8a, 1888.***{EVsw 348:2}*

Kubeba Mafundisho ya Upendo wa Harufu Nzuri

Watenda kazi wa Bwana wanahitaji upendo uyeyushao wa Yesu mioyoni mwao. Hebu kila mchungaji na aishi kama mtu miongoni mwa watu. Kwa mpangilio mzuri, hebu na aende kutoka nyumba hadi nyumba, akiwa amebeba daima mafusho ya anga la mbinguni lenye harufu ya upendo. Atangulie kuhisi huzuni, matatizo na changamoto za wengine. Aingie katika furaha na mahangaiko ya wote—kwa watu wa hali ya juu na ya chini, matajiri na masikini. **—Barua 50, 1897.***{EVsw 348:3}*

Mahubiri kwa Watoto

Katika kila nafasi inayofaa, kisa cha upendo wa Yesu kisimuliwe tena kwa watoto. Katika kila mahubiri, nafasi ndogo itengewe kwa faida yao. Mtumishi wa Kristo anaweza kupata marafiki wa kudumu kutoka kwa watoto hawa wadogo. Basi asipoteze nafasi yoyote ya kuwasaidia wapate maarifa zaidi ya Kweli za Maandiko. Hili litasaidia kwa njia tunayoidharau sasa kuzuia hila za Shetani. Endapowatoto watajifunza Kweli za Neno la **Mungu** wakiwa wadogo, kuta zitajengwa dhidi ya upotovu, nao watakuwa na uwezo wa kumpinga adui kwa kusema: "Imeandikwa." **—Gospel Workers, uk. 208 (1915).***{EVsw 349:1}*

Kuwabariki Watoto kwa Mungu-Kuwatoa Wakfu kwa Mungu

Mhudumu asisahau kuwatia moyo na kuwafariji wana-kondoo wapendwa wa kundi. Kristo, aliye Mkuu wa mbinguni, alisema, **Mathayo 19:14** *"Waacheni watoto wadogo waje kwangu, wala msiwazuie; kwa maana walio mfano wa hao Ufalme wa* ***Mungu*** *ni wao."* Yesu hakuwapeleka watoto kwa marabi; wala hakuwapeleka kwa Mafarisayo; kwa maana alijua kwamba watu hawa wangewafundisha kuwakataa Rafiki yao bora. Akina mama waliowaleta watoto kwa Yesu walifanya vema. Kumbuka Andiko hili: **Mathayo 19:14** *"Waacheni watoto wadogo waje Kwangu, wala msiwazuie; kwa maana walio mfano wa hao Ufalme wa* ***Mungu*** *ni wao."* hebu wakina mama sasa, wawaongoze watoto wao kwa Kristo. Hebuwachungaji au wahudumu wa Injili na wawachukue watoto wadogo mikononi mwao, na kuwabariki kwa Jina la Yesu. Maneno ya upendo wa huruma yasemwe kwa watoto hawa; kwa maana Yesu aliwachukua wana-kondoo mikononi Mwake, na kuwabariki. **—The Review and Herald, March 24, 1896.** *{EVsw 349:2}*

Mahubiri ya Sabato kwa Wageni

Wakati watu walioelimika, wanasiasa, na wale wanaoitwa wenye heshima wanapokuwa mahali pa ibada, mchungaji hufikiri kwamba ni lazima awape chakula cha kiakili; lakini kwa kufanya hivyo hupoteza fursa ya thamani ya kufundisha masomo yale yale yaliyotolewa na Mwalimu Mkuu aliyewahi kuwapo duniani. Makanisa yote nchini mwetu yanahitaji kujifunza zaidi juu ya Kristo na Yeye aliyesulubiwa. Uzoefu wa kidini usiokuwa na msingi ndani ya Kristo na Yeye peke yake hauna faida. Watu hawa wenye akili na maarifa wanahitaji kuonyeshwa kwa uwazi na kwa maandiko mpango wa wokovu. Hebu Ukweli huu, katika usahili, unyofu na nguvu yake, uwasilishwe kwao. Kama hili halitawavuta wala kuwapa hamasa, basi kamwe hawawezi kuvutiwa na mambo ya mbinguni na ya Kiungu. *{EVsw 350:1}*

Katika kila kusanyiko, kuna roho zisizoridhika. Kila Sabato wanatamani kusikia jambo lililo wazi linaloeleza jinsi wanavyoweza kuokolewa, jinsi ya kuwa MKristo. Jambo la msingi kwao kulijua ni: Je, mwenye dhambi anawezaje kusimama mbele za **Mungu**? Hebu njia ya wokovu ielezwe kwa uwazi, kwa unyofu—kama vile unavyoweza kumweleza mtoto mdogo. Mwinue Yesu kama tumaini la pekee la mwenye dhambi. —**Manuscript 4, 1893.** *{EVsw 350:2}*

Kutelekeza Huduma kwa Ajili ya Kusoma na Kujitenga kwa kufanya utafiti wa Maandiko

Majukumu ya mchungaji mara nyingi hutupiliwa mbali kwa aibu kwa sababu mchungaji anakosa nguvu ya kutoa dhabihu kwasababu ya mwelekeo wake wa kujitenga na watu ili awe peke yake na kisha ajisomee (yale anayopenda katika theolojia nk, siku hizi pengine ajitenge na kuwa kwenye vyombo vya teknolojia nk). Mchungaji anapaswa kutembelea familia moja hadi nyingine miongoni mwa kundi lake, akifundisha, akizungumza, na kusali na kila familia, akitafuta maslahi na mema ya roho zao. Wale ambao wameonyesha nia ya kujifunza kanuni za imani yetu hawapaswi kupuuzwa, bali wafundishwe kikamilifu ile Kweli. —**Gospel Workers, uk. 337 (1915).** *{EVsw 350:1}*

Wajibu wa Walei wa Kiroho kwa Waumini Wapya

Kanisa Kuwasaidia Waumini Wapya kwa Uvumilivu

Wale wanaoingia katika imani kwa mara ya kwanza wanapaswa kushughulikiwa kwa uvumilivu, huruma nyororo na upole. Ni jukumu la washiriki wa zamani wa kanisa kutafuta njia na mbinu za kuwapatia msaada, huruma na mafundisho wale waliotoka kwa dhamira katika makanisa mengine kwa ajili ya ile Kweli, na kwa kufanya hivyo wamekatwa kutoka kwa huduma ya kichungaji waliyokuwa wakiitegemea. Kanisa lina jukumu maalum kutoka kwa **Mungu** la kuwatunza roho hizi ambazo zimeitikia mwanga wa awali walioupokea. Na ikiwa washiriki watapuuza jukumu hili, watakuwa sio waaminifu kwa agizo walilopewa na **Mungu**. — **The Review and Herald, April 28, 1896.** *{EVsw 351:1}*

Uangalizi wa Karibu na Kuwatia moyo

Tena, baada ya watu kubadilishwa na Ukweli, wanahitaji kutunzwa. Bidii ya wachungaji wengi inaonekana kushindwa mara tu kiwango fulani cha mafanikio kinapoonekana katika juhudi zao. Hawatambui kwamba hawa wapya walioongoka wanahitaji matunzo- uangalizi, msaada, na kutiwa moyo. Hawa hawapaswi kuachwa peke yao, kwani ni mawindo ya majaribu yenye nguvu zaidi ya Shetani; wanahitaji kuelimishwa kuhusu majukumu yao, kushughulikiwa kwa fadhili, kuongozwa pamoja, na kutembelewa na kuomba pamoja nao. Nafsi hizi zinahitaji chakula kilichogawanywa kwa kila mtu kwa msimu unaofaa. *{EVsw 351:2}*

Haishangazi kwamba wengine hukata tamaa, wanakawia njiani, na wameachiwa mbwa mwitu wawale. Shetani yuko katika mawindo ya wote. Anawatuma mawakala wake kukusanya nyuma kwenye safu zake roho alizopoteza. Inapaswa kuwa na akina baba na mama wengi zaidi wa kuwachukua waamini hawa wachanga katika Ukweli kwa mioyo yao, na kuwatia moyo na kuwaombea, ili imani yao isitindike wala kuwa na mkanganyiko.*{EVsw 351:3}*

Kuhubiri ni sehemu ndogo tu ya kazi inayofanyika kwa wokovu wa roho. Roho wa **Mungu** huwasadikisha wenye dhambi Ukweli, na huwaweka mikononi mwa kanisa. Wachungaji wanaweza kufanya sehemu yao, lakini hawawezi kamwe kufanya kazi ambayo kanisa linapaswa kufanya. **Mungu** analitaka kanisa Lake kuwalea wale ambao ni wachanga katika imani na uzoefu, waende kwao, sio kwa kusudi la kusengenya nao, lakini kuomba, kuzungumza nao maneno ambayo ni "kama tufaa za dhahabu katika picha za fedha.*{EVsw 352:1}*

Sisi sote tunapaswa kujifunza tabia na mienendo ili kwamba tujue jinsi ya kushughulika kwa busara na akili tofauti, ili tutumie juhudi zetu bora kuwasaidia kupata uelewa sahihi wa Neno la **Mungu** na maisha ya Kweli ya Kikristo. Tunapaswa kusoma Biblia pamoja nao, na kuwashawishi kuondoa mawazo yao mbali na mambo ya kidunia kwa masilahi yao ya milele. Ni jukumu la watoto wa **Mungu** kuwa wamishenari Kwake, kuwaelewa wale wanaohitaji msaada. Ikiwa mtu anayumbishwa na majaribu, suala lake linapaswa kuchukuliwa kwa uangalifu na kusimamiwa kwa busara; kwa maana masilahi yake ya milele yako hatarini, na maneno na matendo ya wale wanaomhudumia yanaweza kuwa wokovu wa maisha yaletao uzima, au kifo hadi mauti. **— Testimonies for the Church, 4:68-69 (1876).** *{EVsw 352:2}*

Mpango wa Kulea wa Bwana/Kiungu

Katika Kristo sote ni wa familia moja. **Mungu** ni Baba yetu, Naye anatarajia tushughulikie kwa dhati washiriki wa nyumba Yake—sio kwa muda mfupi tu bali kwa moyo wa kudumu. Kama matawi ya mzabibu wa asili, tunapata lishe kutoka chanzo kimoja, na kwa utiifu wa hiari tunakuwa na umoja na Kristo.*{EVsw 352:3}*

ikiwa mshiriki mmoja wa familia ya Kristo anadondoka majaribuni, wengine wanapaswa kumwangalia kwa huruma, wakimvuta kutoka njia ya upotovu na kumrejesha katika maisha safi na takatifu. Hili ni agizo kutoka kwa **Mungu** kwa kila mshiriki wa kanisa Lake…..... Watu wa **Mungu** wanapaswa kuwa wenye hekima na waangalifu, wakitumia kila fursa kuwaokoa ndugu zao walio dhaifu kutoka mitego ya Shetani iliyojificha.*{EVsw 353:1}*

Hii ndiyo kazi ya umishenari wa nyumbani, na inawasaidia wale wanaoifanya sawa na wale wanaosaidiwa. Huruma tunayoonyesha katika familia zetu, na maneno ya faraja tunayosema kwa ndugu zetu, hutufundisha jinsi ya kuwahudumia wale walio katika familia ya Bwana, ambao tutaishi nao milele tukidumu katika uaminifu kwa Kristo. “Uwe mwaminifu hata kufa, Nami nitakupa taji ya uzima.” Basi tunapaswa kuwa waangalifu jinsi gani, tunavyowahudumia ndugu zetu. Jifanye rafiki yao. Wakiwa maskini na wahitaji chakula na mavazi, wahudumie katika mahitaji ya kimwili na ya kiroho. Kwa kufanya hivyo utakuwa mbaraka maradufu kwao. **— Manuscript 63, 1898.***{EVsw 353:2}*

Kuwasaidia Waumini Wapya Kuwavuta Wengine kwa Kristo

Mhubiri Kuwafundisha Waumini Wapya Jinsi ya Kuwavuta Wengine

Kila mahali panatakiwa kutembelewa; makanisa yanapaswa kuinuliwa pande zote. Wale wanaoukubali Ukweli wanapaswa kupangwa katika makanisa, kisha mchungaji apite kwenda katika maeneo mengine muhimu. *{EVsw 353:3}*

Mara tu kanisa linapopangwa/kusimikwa, Hebu mchungaji awaingize washiriki kazini. Watahitaji kufundishwa jinsi ya kufanya kazi kwa mafanikio…….*{EVsw 353:4}*

Nguvu ya injili itakuja juu ya makundi yalioinuliwa, na kuwafanya wafae kwaajili ya huduma. Baadhi ya waongofu wapya watajazwa na nguvu za **Mungu,** nao wataingia kazini mara moja. Watafanya kazi kwa bidii wasiwe na muda wala nafasi ya kudhoofisha mikono ya ndugu zao kwa ukosoaji usiofaa au usio na huruma. Shauku yao moja itakuwa ni kuupeleka Ukweli katika maeneo zaidi. **— Testimonies for the Church, 7:20 (1902).** *{EVsw 354:1}*

Kutilia Mkazo Wajibu Binafsi kwa Mungu

Wajibu binafsi, na utendaji binafsi katika kuwatafuta na kuwaokoa wengine, ndilo somo kuu ambalo waongofu wapya wanapaswa kufundishwa…..*{EVsw 354:2}*

Imani ya mtu binafsi inapaswa kuonyeshwa na kufanyiwa kazi; utakatifu wa binafsi upandwe, na unyenyekevu wa Kristo uwe sehemu ya maisha yetu ya kila siku. Kazi inapaswa kuwa ya kina na ya ndani ndani ya kila mtu.*{EVsw 354:1}*

Wale wanaodai kuwa wamepokea na kuamini Kweli wanapaswa kuonyeshwa hatari ya ubinafsi, na jinsi unavyoweza kuharibu na kuharibu mioyo. Roho Mtakatifu ni lazima afanye kazi ndani ya mtu, la sivyo nguvu nyingine itachukua nafasi ya akili na maamuzi. Maarifa ya kiroho kuhusu **Mungu** na Yesu Kristo aliyemtuma, ndiyo tumaini pekee la nafsi. Kila mtu lazima afundishwe na **Mungu**, mstari kwa mstari, amri juu ya amri; lazima mwanadamu atambue jukumu lake binafsi kwa **Mungu** katika kazi ya kuwaokoa wengine kutoka mauti. **— Manuscript 25, 1899.** *{EVsw 354:3}*

Viapo cha Ubatizo—Ahadi ya Kuleta Roho

Watu wa **Mungu** wanapaswa kuwa waungwanwa, bora, wenye huruma nyororo, wenye staha na ukarimu kwa kila aina ya kazi inayoendeshwa katika shamba kubwa la mavuno. Kwa viapo vyao vya ubatizo wamejiwekea nadhiri ya kufanya juhudi za dhati, za kujikana nafsi, ili kuendeleza kazi ya kuokoa roho hata katika maeneo magumu zaidi ya kazi ya Bwana. **Mungu** ameweka juu ya kila muumini jukumu la kuwasaidia kwa bidii, wale walio dhaifu na waliodhulumiwa. — **(Australasian) Union Conference Record, June 1, 1903.** *{EVsw 354:4}*

Aliyeongoka Kweli Atafanya Kazi kwa Ajili ya Wengine

Neema ya **Mungu** ndani ya roho ya muumini mpya hukua na ni endelevu. Huongeza neema, ambayo haikupokelewa ili ifichwe chini ya pishi, bali ishirikishwe, ili wengine wanufaike. Yule aliyebadilishwa kweli atafanya kazi kuwaokoa walioko gizani. Nafsi moja iliyoongoka kweli itawafikia kwa imani ili kuwaokoa wengine zaidi. Roho hizi ni mawakala wa **Mungu**, wana na binti Zake. Ni sehemu ya kundi kubwa la **Mungu**, na kazi yao ni kurekebisha ufa uliotengenezwa na Shetani na mawakala wake katika sheria ya **Mungu** kwa kukanyaga Sabato ya Kweli na kuweka siku ya mapumziko ya uongo badala yake. — **Letter 29, 1900.** *{EVsw 355:1}*

Kwa Nini Waumini Wapya Wengine Hawakui Kiroho na kusonga mbele

Nafsi zenye unyenyekevu, wa moyo safi na waaminifu wanaweza kufanya kazi itakayoleta furaha mbinguni miongoni mwa malaika wa **Mungu**. Kazi yao katika nyumba zao, majirani, na kanisani, itakuwa ya matokeo yatakayoenea hadi umilele. Ni kwa sababu kazi hii haifanyiki ndipo waongofu wapya hukwama katika hatua za awali za kiroho- abc. Daima hubaki watoto wa kiroho, wakihitaji maziwa badala ya chakula kigumu cha Injili. — **Letter 61, 1895.** *{EVsw 355:2}*

Kudhibitishwa Katika Imani Kupitia Huduma

Wakati roho za watu zinapoongolewa, waweke katika kazi mara moja-kibarua cha kuongoa roho. kisha wanapofanya kazi kulingana na uwezo wao, watakuwa na nguvu zaidi. Ni kwa kukutana na upinzani ndipo tunathibitishwa katika imani. Nuru inapoangaza ndani ya mioyo yao, hebu wawafundishe kuieneza kwa wengine. Fundisha waongofu wapya kuwa wao ni washirika wa Kristo, wawe mashahidi Wake, na kwamba ni wajibu wao kumjulisha ulimwengu juu Yake.*{EVsw 355:3}*

Asiwepo yeyote mwenye pupa ya kuingia katika mabishano, bali waeleze watu kirahisi tu, kisa cha upendo wa Yesu. Wote wanapaswa daima kujifunza Maandiko ili kujua sababu ya imani yao, ili wakihitajika, waweze kutoa “sababu ya tumaini lililomo ndani yao kwa upole na kwa hofu.” *{EVsw 356:1}*

Dawa bora ya kiroho kwa kanisa si mahubiri marefu au kutoa hotuba, bali ni kuwapatia kazi ya kiroho. Wakipewa kazi, waliokata tamaa wangeisahau haraka, wanyonge wangekuwa na nguvu, wajinga wangekuwa na maarifa, na wote wangekuwa tayari kuwasilisha Kweli kama ilivyo ndani ya Yesu. Watampata Msaidizi asiyeweza kushindwa katika Yeye ambaye ameahidi kuwaokoa wote wamjiao. — **The Review and Herald, Juni 25, 1895.***{EVsw 356:2}*

Uhusiano Kati ya Utendaji na Ukuaji wa Kiroho

Wale ambao wanajishughulisha kwa bidii katika kazi ya uaminifu ya kuwavuta roho kwa Yesu Kristo, ndio wanaoendelea zaidi katika maisha ya kiroho na kujitolea kwa **Mungu**. Ni kwa njia ya kufanya kazi hiyo yenye shughuli nyingi ndipo maisha yao ya kiroho huimarika na kukua. Kuna hatari ya dini kupanuka kwa nje lakini kupungua kwa undani. Hili halipaswi kutokea, ikiwa badala ya mahubiri marefu, kutatolewa mafundisho ya busara kwa wale waliokuja katika imani hivi karibuni. Wafundisheni kwa kuwapa majukumu ya kufanya kazi ya kiroho, ili upendo wao wa kwanza kwa **Mungu** usife bali uongezeke kwa bidii. Wafanye wajihisi kuwa hawapaswi kubebwa wala kutegemea msaada wa daima kutoka kwa kanisa; bali wanapaswa kuwa na mizizi ndani yao wenyewe. Wanaweza kuwa wa msaada katika njia nyingi, kulingana na vipawa walivyopewa, kwa kusaidia kanisa kumkaribia **Mungu**, na pia kufanya kazi katika mazingira ya nje ya kanisa ambayo kwa njia hiyo itafanya pia kanisa linufaike. Hekima na ustawi wa kanisa unaathiri kwa kiasi kikubwa jinsi linavyoonekana mbele ya watu. Mtunga Zaburi aliomba ustawi wa kanisa kwa kusema: *"**Mungu** na atufadhiri, na kutubariki, na kutuangazia uso Wake; njia Yake ijulike duniani, Wokovu Wake katikati ya mataifa yote."* — **Zaburi 67:1-2** — **Barua 44, 1892.** *{EVsw 356:3}*

Ukuaji wa Kikristo Utaonekana

Hakuna kitu kinachonyonya maisha ya kiroho kutoka kwa roho haraka kama kujifungia ndani ya ubinafsi na kujijali mwenyewe. Wale wanaojistarehesha na kuacha kuwajali roho na miili ya wale ambao Kristo alitoa maisha Yake kwa ajili yao, hawali mkate wa uzima, wala kunywa maji kutoka kisima cha wokovu. Ni kama miti iliyokauka, isiyozaa matunda. Ni viumbe wa kiroho waliodumaa-mbilikimo tu, ambao hutumia mali yao kwa ajili ya nafsi tu; lakini kile "apandacho mtu, ndicho atakachovuna." **— The Review and Herald, January 15, 1895.** *{EVsw 357:1}*

Kanuni za Kikristo daima zitaonekana. Kwa njia elfu kanuni za ndani zitaonekana. Kristo akikaa ndani ya moyo ni kisima kisichokauka kamwe.—The Review and Herald, Januari 15, 1895.{EVsw 357:2}

Kuendeleza Uhai wa Kanisa Kupitia Huduma

Hebu mchungaji na ajitahidi kulifanya kanisa liwe hai kwa kuwafundisha washiriki wake jinsi ya kushirikiana naye katika kuwaleta wenye dhambi kwa Kristo. Huu ni uongozi mzuri sana wa kiroho-mchungaji mwema; na matokeo yake yatakuwa bora zaidi kuliko ikiwa angejaribu kufanya kazi hiyo peke yake. — **The Review and Herald, April 23, 1908.** *{EVsw 357:3}*

Kuwalinda Waumini Wapya Dhidi ya Uongo na Upotovu

Shetani Huwasumbua na Kuwavuruga Waumini Wapya

Popote ambapo kundi dogo la waumini limeanzishwa, Shetani hujitahidi kila mara kuwasumbua na kuwavuruga. Mtu anapotubu dhambi zake na kumgeukia **Mungu**, je, unadhani Shetani atamwacha? Hapana kabisa. Tunataka muangalie kwa makini msingi wa tumaini lenu. Tunataka maisha yenu na matendo yenu yashuhudie kwamba ninyi ni watoto wa **Mungu**. **— Manuscript 5, 1885.** *{EVsw 357:4}*

Pasiwepo Mawazo ya Kupotosha—

Shetani siku zote hutafuta kuwapotosha wanadamu. Yeye ndiye **mungu** wa migawanyiko yote, naye ana filosofia za kuwalaghai watu. Madhehebu mapya huibuka mara kwa mara ili kuwapotosha watu kutoka katika ile Kweli; na badala ya kulishwa mkate wa uzima, watu hupewa bakuli la hekaya za uongo ili wale. Maandiko Matakatifu hupotoshwa, na kunyang'uliwa kutoka muktadha wake wa kweli, na kunukuliwa ili kuupa uongo sura ya ukweli. Mavazi ya Kweli huibwa ili kufunika sura ya uzushi. *{EVsw 358:1}*

Paulo alipanda mbegu safi ya Injili huko Galatia. Alihubiri fundisho la haki kwa imani, na kazi yake ilizaa matunda kwa kuona kanisa la Wagalatia likimkubali Kristo. Kisha Shetani alianza kufanya kazi kupitia walimu wa uongo, akichanganya fikra za baadhi ya waumini. Majivuno ya walimu hao na madai yao ya kufanya miujiza ya kustaajabisha, yaliwafanya waumini wapya wengi kupofushwa kiroho, na wakaongozwa kwenye upotovu na makosa.....*{EVsw 358:2}*

Kwa muda fulani, Paulo alipoteza ushawishi kwa wale waliodanganywa; lakini kwa kutegemea Neno na nguvu ya **Mungu**, na kukataa tafsiri za waalimu waliopotoka, aliweza kuwaelekeza waumini kuona kuwa

walikuwa wamedanganywa, na hivyo kushinda hila za Shetani. Waongofu wapya walirudi kwenye imani, wakiwa tayari kuchukua msimamo wa kuelewa na kuitetea ile Kweli. — **Manuscript 43, 1907.***{EVsw 358:3}*

Mafundisho ya Uongo kutoka kwa Wanaodai Kuamini

Sote tutajaribiwa kwa nguvu. Watu wanaojidai kuamini Kweli watakuja kwetu na kushinikiza mafundisho ya uongo ambayo, tukiyasikiliza, yatavuruga imani yetu katika Kweli ya sasa. Ni dini ya Kweli pekee itakayoweza kustahimili mtihani wa hukumu. — **The Review and Herald, December 2, 1884.** *{EVsw 359:1}*

Juhudi za Shetani Kuwagawa Watu wa Mungu

Kristo alitabiri kwamba kuibuka kwa wadanganyifu kungelileta hatari kubwa zaidi kwa wanafunzi Wake kuliko hata mateso.*{EVsw 359:2}*

Onyo hili limerudiwa mara kadhaa. Wadanganyifu, kwa hoja zao za "kisayansi", wanapaswa kuchukuliwa kwa tahadhari zaidi kuliko hatari yoyote nyingine; kwa kuwa kuingia kwa roho hizi za udanganyifu kulimaanisha kuingia kwa makosa ya hila ambayo Shetani ameandaa kwa werevu ili kupofusha macho ya kiroho ya wale wasio na uzoefu mkubwa wa kazi ya Roho Mtakatifu, na wale wanaoridhika na maarifa finyu ya kiroho. Lengo la udanganyifu limekuwa kudhoofisha imani katika Kweli ya **Mungu** na kufanya kuwa vigumu kutofautisha kati ya Ukweli na uongo.

Masuala ya kupendeza, ya kufikirika, na ya "kisayansi" huletwa mbele ya watu kwa mvuto mkubwa kwa wale wasio na tahadhari; na isipokuwa waumini wawe macho, adui atakayejitokeza kama malaika wa nuru atawaongoza kwenye njia za uongo.....*{EVsw 359:3}*

Shetani anaweza kucheza mchezo wa maisha kwa werevu mno, akitumia hila na ujanja kuiharibu imani ya watu wa **Mungu** na kuwavunja moyo. Anafanya kazi leo kama alivyofanya mbinguni, kwa nia ya kuwagawanya watu wa **Mungu** katika hatua ya mwisho ya historia ya dunia hii. Hutafuta kuleta mafarakano, kuamsha mabishano, na kuvuruga alama za zamani za Kweli alizokabidhi **Mungu** kwa watu Wake.*{EVsw 359:4}*

Ni wakati Shetani anapojitokeza kama malaika wa nuru ndipo anaponasa roho za watu. Watu wanaodai kuwa wamefundishwa na **Mungu** watakubali mafundisho potofu, na kwa mafundisho yao watapamba upotovu huo ili kuuingiza udanganyifu wa Kishetani. Hivyo ndivyo Shetani atakavyoletwa kama malaika wa nuru, akiwa na nafasi ya kuwasilisha hekaya zake za kupendeza.*{EVsw 360:1}*

Manabii hawa wa uongo ni lazima tukabiliane nao. Watatumia nguvu kubwa kudanganya wengi kwa kuwasilisha mafundisho ya uongo kama Kweli. Maandiko mengi yatatumika vibaya ili kuonekana kama msingi au nadharia ya mafundisho hayo ya uongo. Ukweli wa thamani utachukuliwa na kutumiwa kuunga mkono na kuimarisha uongo. Manabii hawa wa uongo, wanaodai kufundishwa na **Mungu**, watatumia Maandiko mazuri yaliyopewa kwa ajili ya kupamba kweli, na kuyatumia kama vazi la haki kufunika mafundisho ya uongo na ya hatari. Hata baadhi ya wale ambao hapo awali **Mungu** watapotea kiasi cha kueneza mafundisho ya uongo kuhusu vipengele mbalimbali vya Kweli, ikiwa ni pamoja na mada ya Patakatifu (sanctuary question). — **Manuscript 11, 1906.***{EVsw 360:1}*

Kanisa Litapimwa na Kupepetwa

Daima ni vigumu kushikilia kwa uthabiti mwanzo wa imani yetu hadi mwisho, na ugumu huu huongezeka zaidi panapokuwa na mvuto wa siri wa kuleta roho tofauti, ya kupinga kazi ya **Mungu**, upande wa Shetani.*{EVsw 360:2}*

Kwa kuwa mateso hayapo, watu wengine wameingia miongoni mwetu wakionekana kama waaminifu, na UKristo wao hauna doa; lakini mateso yakitokea, hao watajitenga nasi. Katika wakati wa msukosuko, wataona hoja za kuvutia katika sababu za hila zilizowavutia mioyo yao. Shetani ameandaa mitego mbalimbali kukabiliana na aina mbalimbali za akili.*{EVsw 360:4}*

Wakati sheria ya **Mungu** itakapopuuzwa, kanisa litapimwa kwa majaribu makali, na idadi kubwa kuliko tunavyotarajia sasa itafuata roho za udanganyifu na mafundisho ya mapepo-mashetani. Badala ya kuimarishwa wakati wa dhiki, wengi wataonyesha kuwa si matawi hai ya mzabibu wa kweli; hawazai matunda, na Baba Mwenye shamba, yaani Mkulima huwakatilia mbali. — **Letter 3, 1890.** *{EVsw 361:1}*

Kushikilia kwa Uthabiti Kweli ya Biblia

MKristo anapaswa kuwa "amekita mizizi na kuimarika" katika Kweli, ili asimame imara dhidi ya vishawishi vya adui. Anahitaji kufanywa upya kila mara kwa nguvu mpya, na ashikilie kwa uthabiti Kweli ya Biblia. Hadithi na mafundisho potofu ya kila aina yataletwa ili kumwondoa muumini katika utiifu wake kwa **Mungu**, lakini ni lazima atazame juu, amwamini **Mungu**, na asimame thabiti katika Kweli.*{EVsw 361:2}*

Shikilia kwa nguvu Bwana Yesu, wala usimwachilie. Kuwa na msimamo thabiti juu ya kile unachoamini. Acha kweli za Neno la **Mungu** zikusukume kujitoa moyo, akili, nafsi, na nguvu kwa ajili ya kutenda mapenzi Yake. Shikilia kwa ujasiri Maneno ya wazi ya **Mungu**: “Bwana asema hivi.” Hoja yako ya pekee iwe: “Imeandikwa.” Hivyo ndivyo tunavyopaswa kupigania imani waliyopewa watakatifu mara moja tu. Imani hiyo haijapoteza uzito wake wa Kiungu na wa utakatifu, hata kama wapinzani wake wanaona kuwa haivutii au inawachukiza.*{EVsw 361:3}*

Wale wanaoongozwa na mawazo yao binafsi na kutembea katika njia zao watatengeneza tabia potofu-zisizo na ulinganifu. Mafundisho yasiyo na msingi na hoja za kisasa zitaletwa kwa namna ya kuvutia, ili kuwapotosha, ikiwezekana, hata wateule. Je, washiriki wa kanisa wamejenga juu ya Mwamba? Dhoruba inakuja, dhoruba itakayojaribu imani ya kila mtu, ni ya namna gani. Waumini sasa wanapaswa kuwa wamekita mizizi kwa Kristo, la sivyo watavurugwa na kupotoshwa na kila aina ya uongo. hebu imani yako na iwe imejengwa juu ya Neno la **Mungu**. Shikilia kwa nguvu ushuhuda hai wa Kweli. Kuwa na imani kwa Kristo kama Mwokozi binafsi. Yeye amekuwa na ataendelea kuwa Mwamba wetu wa Milele. Ushuhuda wa Roho wa **Mungu** ni wa Kweli. Usibadilishe imani yako kwa aina yoyote ya mafundisho, hata kama yanaonekana kuvutia, na yatakayodanganya nafsi.*{EVsw 361:4}*

Udanganyifu wa Shetani sasa unazidi kuongezeka, na wale wanaopotoka kutoka njia ya kweli watapoteza mwelekeo wao na nanga yao. Wasipokuwa na kitu cha kujishikilia, watavurugwa na kila upepo wa mafundisho ya ajabu. Shetani ameshuka na nguvu nyingi. Wengi watadanganywa na miujiza yake.....*{EVsw 362:1}*

Nawasihi kila mmoja kuwa na msimamo wazi na thabiti juu ya Kweli zile za hakika tulizozisikia, tulizozipokea, na kuzitetea. Maelezo ya Neno la **Mungu** ni wazi. Simamisha miguu yako juu ya jukwaa la Kweli ya milele. Kataa kila aina ya uongo, hata kama umejifunika kwa sura ya Ukweli. **— The Review and Herald, August 31, 1905.** *{EVsw 362:2}*

Kwenda Mbali na Misingi za Biblia

Wengi wana maarifa haba juu ya Biblia zao kiasi kwamba imani yao haijathibitika. Wanaondoa misingi ya zamani, na mafundisho ya uongo pamoja na upepo wa mafundisho huwapeperusha huku na kule. Sayansi, ambayo si ya kweli kwa jina, inadhoofisha misingi ya kanuni za Kikristo; na wale waliokuwa ndani ya imani wanazidi kwenda mbali na misingi ya Biblia, na kujitenga na **Mungu**, huku wakidai bado kuwa watoto Wake. — **Review and Herald, December 29, 1896.** *{EVsw 362:3}*

Makundi Mapya ya Wanaodai Kuamini

Kanisa linahitaji kuamka na kuelewa nguvu za siri za mawakala wa kishetani ambazo ni lazima tukabiliane nazo. Wakizivaa silaha kamili za **Mungu**, wataweza kuwashinda maadui wote, hata wale ambao bado hawajadhihirika (Waefeso 6).*{EVsw 362:4}*

Miungano ya upinzani itaongezeka kadri tunavyokaribia mwisho wa wakati. Miungano hii italeta ushawishi wa upinzani dhidi ya Ukweli, ikiunda makundi mapya ya watu wanaodai kuwa waumini lakini wakitekeleza mafundisho yao ya udanganyifu. Uasi utaongezeka. "Wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo na mafundisho ya mashetani." Wanaume na wanawake wameungana kumpinga Bwana **Mungu** wa mbinguni, na kanisa bado halijazinduka kabisa kuelewa hali halisi. Kuna haja kubwa ya maombi ya dhati zaidi, na bidii kubwa zaidi kati ya wale wanaodai kuwa waumini. — **Review and Herald, August 5, 1909.***{EVsw 363:1}*

Hatari ya Kutojua Historia Yetu ya Kale

Uzoefu wa Kweli katika mafundisho ya dini hubeba muhuri wa Yehova. Kila mtu anapaswa kuona umuhimu wa kuelewa Ukweli binafsi. Tunapaswa kuelewa mafundisho ambayo yamechunguzwa kwa bidii na kwa maombi. Nimefunuliwa kwamba miongoni mwa watu wetu kuna upungufu mkubwa wa maarifa kuhusu

kuinuka na maendeleo ya ujumbe wa malaika wa tatu. Kuna haja ya dharura ya kuchunguza vitabu vya Danieli na Ufunuo, na kuvielewa kwa undani ili tujue yaliyoandikwa.*{EVsw 363:2}*

Nimeonyeshwa kwa nguvu kwamba wengi watajitenga nasi, wakisikiliza roho zidaganyazo na mafundisho ya mashetani. Bwana anataka kila mtu (nafsi) anayejidai kuamini Ukweli awe na maarifa ya kuulewa Ukweli ni nini. Manabii wa uongo watazuka na kudanganya wengi. Kila kitu kitapimwa na kutikiswa. Je, haimpasi kila mtu kuelewa sababu za imani yetu? Badala ya kuwa na mahubiri mengi, kunapaswa kuwa na uchunguzi wa karibu wa Neno la **Mungu**, tukilifungua Andiko baada ya Andiko, na kutafuta ushahidi dhabiti unaounga mkono mafundisho ya msingi yaliyotufikisha hapa, katika msingi wa Ukweli wa milele.*{EVsw 363:3}*

Nafsi yangu hujaa huzuni kuona jinsi wengine waliokuwa na nuru na Ukweli wanavyokubali udanganyifu wa Shetani kwa haraka, wakivutwa na utakaso wa bandia. Watu wanapoiacha na misingi ambayo Bwana ameweka ili tuelewe msimamo wetu uliobainishwa katika unabii, wanapotea bila kujua wanakoelekea. — **Undated Manuscript, 148.***{EVsw 364:1}*

Makosa Yanayofundishwa kwa Kuvutia

Mafundisho ya uongo, utauwa wa bandia, imani ya bandia au feki, na mengi yanayoonekana kuwa mazuri yapo kila mahali. Walimu watajivika kama malaika wa nuru; na ikiwezekana, watawadanganya hata wateule. Vijana wanapaswa kujifunza Ukweli kwa bidii ili wasidanganywe na mtandao wa uongo ambao Shetani atatunga. Wanapaswa kuishi katika nuru ya haki ya Kristo. Wanapaswa kuwa na mizizi na msingi katika Ukweli ili waweze kuwashirikisha wengine nuru waliyoipokea. — **The Youth's Instructor, April 22, 1897.***{EVsw 364:2}*

Hatari ya Dini ya Msisimko

Hakuna usalama, wala faida, kwa watu wetu kuhudhuria mikutano maarufu ya "utakatifu"; badala yake, na tuichunguze Biblia kwa uangalifu mkubwa na maombi ya dhati na bidii, ili tuelewe msingi wa imani yetu. Hapo ndipo hatutajaribiwa kujiunga na wale ambao, ingawa wanadai mambo makuu, wanapinga sheria ya **Mungu**.*{EVsw 364:3}*

Hatupaswi kuwa na dini ya msisimko tu isiyo na mizizi katika Kweli. Mafundisho madhubuti lazima yatolewe kwa watu kuhusu sababu za imani yetu. Wanapaswa kufundishwa zaidi kuliko ilivyokuwa, kuhusu mafundisho ya Biblia, hasa mafundisho ya vitendo aliyoyatoa Yesu kwa wanafunzi Wake. Waumini wanapaswa kuhamasishwa kuhusu hitaji lao kuu la maarifa ya Biblia. Lazima kuwe na jitihada makini za kupandikiza katika akili za wote hoja madhubuti za Uukweli; kwa maana kila mmoja atajaribiwa, na wale waliopandwa mizizi na msingi katika kazi ya **Mungu** hawatasukumwa na uzushi utakaoibuka kila upande; lakini ikiwa mtu atapuuza maandalizi hayo, basi atasombwa na makosa yanayofanana na Ukweli. — **Gospel Workers, uk. 228-229 (1892).***{EVsw 364:4}*

Mkanganyiko wa Babeli na Mpinga Kristo

Ni wajibu wetu binafsi kutembea kwa unyenyekevu na **Mungu**. Hatupaswi kutafuta ujumbe wa ajabu na mpya. Hatupaswi kufikiri kwamba wateule wa **Mungu** wanaojitahidi kutembea katika nuru ni sehemu ya Babeli. Makanisa yaliyopotoka ndiyo Babeli. Babeli imekuwa ikikuza mafundisho ya sumu—mvinyo wa makosa. Mvinyo huu wa makosa unajumuisha mafundisho potofu kama vile: kutokufa kwa roho (umizimu), adhabu ya milele kwa waovu, kukanusha kuwepo kwa Kristo kabla ya kuzaliwa Kwake Bethlehemu, pamoja na kuendeleza na kutukuza siku ya kwanza ya juma juu ya siku takatifu ya **Mungu**. Makosa haya na mengine yanayofanana nayo yanawasilishwa kwa ulimwengu na makanisa mbalimbali.....*{EVsw 365:1}*

Malaika waliopotoka walio duniani wanashirikiana na watu waovu. Katika kizazi hiki, Mpinga Kristo atajitokeza kana kwamba yeye ni Kristo wa kweli, na hapo ndipo sheria ya **Mungu** itatupiliwa mbali kabisa katika mataifa ya dunia. Uasi dhidi ya sheria takatifu ya **Mungu** utakomaa kikamilifu. Lakini kiongozi wa kweli wa uasi huu ni Shetani, aliyeficha sura yake kama malaika wa nuru. Watu watadanganyika na kumtukuza Shetani hadi mahali pa **Mungu**, na hata kumfanya kuwa **Mungu** wao. — **Review and Herald, September 12, 1893.***{EVsw 365:2}*

Waumini Kuendelea Kuchunguza Maandiko

Haitoshi tu kusoma, bali Neno la **Mungu** lazima liingie ndani ya mioyo yetu na kueleweka, ili tuimarishwe katika Ukweli wenye baraka. Tukipuuza kuchunguza Maandiko binafsi ili tujue Ukweli, basi

tukipotoshwa, tutakuwa na hatia kwa kuwajibika katika hilo. Tunapaswa kuyachunguza Maandiko kwa uangalifu ili tujue kila sharti ambalo Bwana ametupa; na ikiwa tuna akili ndogo, kwa kujifunza kwa bidii Neno la **Mungu** tunaweza kuwa hodari katika Maandiko, na kuwaelezea wengine. — **Review and Herald, April 3, 1888.***{EVsw 366:1}*

Vitabu Vyetu Kama Msaada kwa Waumini Wapya

Wengi watajitenga na imani, na kusikiliza roho za udanganyifu. Wazee na Manabii (Patriarchs and Prophets) na Pambano Kuu (Great Controversy) ni vitabu vinavyofaa sana kwa wale waliokuja tu kwenye imani, ili waimarishwe katika Ukweli. Hatari zinaonyeshwa wazi zinazopaswa kuepukwa na makanisa. Wale watakaojifunza kwa makini mafundisho ya vitabu hivi wataona hatari mbele yao, na wataweza kutambua njia iliyo nyoofu iliyoandaliwa kwa ajili yao. Hawatapotea njia au kwenda njia ngeni. Watasaidia kutengeneza njia iliyo nyoofu kwa miguu yao, ili vilema na vipofu wasitolewe njiani.*{EVsw 366:2}*

Katika Tumaini la Vizazi Vyote (Desire of Ages), Wazee na Manabii (Patriarchs and Prophets), Pambano Kuu (Great Controversy), na Daniel na Ufunuo (Daniel and the Revelation), kuna mafundisho ya thamani sana. Vitabu hivi vinapaswa kuchukuliwa kuwa vya umuhimu wa kipekee, na kila jitihada ifanywe kuvifikisha kwa watu. — **Letter 229, 1903.***{EVsw 366:3}*

Busara na Maamuzi Katika Kuwashughulikia Washiriki Wapya

Matendo ya haraka na yasiyo ya busara ni matokeo ya ukosefu wa hekima, na husababisha makosa au kutenda yale yasiyo sahihi. Lakini la kusikitisha zaidi ni kuwa waongofu wapya huumizwa na hali hii, na imani yao kwa kazi ya **Mungu** hutikisika. Na tuombe kwamba wakati wa kuchukua hatua ukifika, tuwe tayari. — **Letter 16, 1907.***{EVsw 366:4}*

Kurejesha Waliopotoka

Tahadhari na Kujilinda Dhidi ya Kuanguka Kiimani (Kuasi)

Inapaswa kuwepo na uangalifu wa hali ya juu katika kuwaelimisha waongofu wapya. Hawapaswi kuachwa wakijiongoza wenyewe, na hatimaye kupotoshwa na mafundisho ya uongo, au kutembea katika njia isiyo ya Kweli. hebu walinzi wa kiroho wanapaswa kuwa waangalifu daima, wasije roho zikadanganywa na maneno laini, hotuba za kuvutia, na ujanja wa kishetani. Fundisheni kwa uaminifu yote ambayo Kristo aliamuru. Kila mtu anayempokea Kristo anapaswa kufundishwa na kuandaliwa kushiriki kwa namna fulani katika kazi kubwa inayopaswa kutendeka ulimwenguni mwetu. —**Letter 279, 1905.***{EVsw 367:1}*

Sababu za Waongofu Wapya Kupotoka

Waongofu wapya wote wanapaswa kufundishwa Ukweli huu: maarifa ya Kweli ya kudumu hupatikana tu kwa bidii na kujifunza kwa uvumilivu. Kwa kawaida, wengi wanaoongoka kwa Kweli tunayohubiri hawakuwa wanafunzi wa bidii wa Maandiko kabla ya hapo; maana katika makanisa mengi maarufu, yanayopendwa na wengi, hakuna kujifunza kwa kina Neno la **Mungu**. Watu huwaangalia wachungaji wao kuwachunguzia Maandiko na kuwaeleza maana yake.*{EVsw 367:2}*

Wengi wanakubali Ukweli pasipo kuchimba kwa undani kuelewa misingi yake. Na mara tu unapopingwa, husahau hoja na ushahidi unaounga mkono. Ingawa walivutwa kuukubali Ukweli, hawakufundishwa kwa kina kuhusu nini hasa ni Ukweli, wala hawakupelekwa hatua kwa hatua katika kumjua Kristo. Mara nyingi uchaji wao wa dini hugeuka kuwa wa kimaumbo tu, na pindi sauti zilizowaamsha mwanzoni hazisikiki tena, huingia katika hali ya mauti ya kiroho. —**Gospel Workers, uk. 368 (1915).***{EVsw 367:3}*

Namna ya Kuwashughulikia Waliopotoka au Waliorudi nyuma

Wale wanaotumwa na **Mungu** kufanya kazi maalum, hupewa jukumu la kukemea uzushi na makosa. Wanapaswa kuwa na moyo wa huruma wa Kibiblia kwa watu wote, wakilihubiri Neno kama lilivyo katika Yesu. Wengine watapinga kwa bidii na ari kubwa dhidi ya Ukweli; lakini hata hivyo, makosa yao lazima yakemewe kwa uthabiti, na matendo yao maovu yahukumiwe wazi. Hata hivyo, uvumilivu, uwenye subira na huruma nyororo vinatakiwa. "*Wahurumieni wengine walio na shaka; na wengine waokoeni kwa kuwanyanyua katika moto, na wengine wahurumieni kwa hofu, mkilichukia hata vazi lililotiwa uchafu na mwili.*" **(Yuda 22-23).** *{EVsw 368:1}*

Kanisa linaweza kulazimika kuwaondoa ushirika wale wanaokataa kukemewa. Hilo ni jambo la kuhuzunisha sana, lakini hufanyika tu pale kila njia nyingine ya kuwaokoa imekwishajaribiwa bila mafanikio. Kristo hakuwahi kufanya amani kwa njia ya maridhiano ya uongo.*{EVsw 368:2}*

Kristo hakufanya amani kamwe kwa njia yoyote kama hiyo. Mioyo ya watumishi wa Mungu itafurika kwa upendo na huruma kwa wakosaji, kama inavyowakilishwa na mfano wa kondoo aliyepotea; lakini hawatakuwa na maneno laini kwa dhambi. Huwa wanaonyesha urafiki wa kweli zaidi kwa kukemea makosa na dhambi bila upendeleo na bila unafiki. Yesu aliishi miongoni mwa kizazi chenye dhambi na kilichopotoka. Naye asingeweza kuwa na amani na ulimwengu pasipo kuuonya na kuukemea, na hilo halikuendana na mpango wa wokovu.—Barua ya 12, 1890.{EVsw 368:3}

Kushughulikia Makosa kwa Njia ya Mungu

Mungu hafurahishwi na kazi ya uvivu inayofanyika katika makanisa. Yeye Anatamani watumishi Wake wawe waaminifu katika kutoa makemeo na maonyo. Wanapaswa kuondoa uovu kwa kufuata masharti ya Neno la **Mungu** —si kwa maoni yao binafsi au mihemko/misukumo. Pasiwepo njia za ukatili zitakazotumika, wala kazi isiyofaa, ya haraka na ya kihisia. Jitihada za kulitakasa kanisa kutoka kwa uovu wa maadili lazima zifanywe kwa njia ya **Mungu**. Pasipo upendeleo, pasipo unafiki. Hakuna awezaye kulindwa kwa sababu ya upendeleo, kana kwamba dhambi zake ni ndogo zaidi. Oh, jinsi sote tunavyohitaji ubatizo wa Roho Mtakatifu! Ndipo tutafanya kazi kwa akili ya Kristo—kwa wema, huruma, na upendo—tukimpenda na kumwonyesha upendo mwenye dhambi huku tukichukia dhambi kwa chuki kamilifu. —**Manuscript 8a, 1888.***{EVsw 368:4}*

Namna Paulo Alivyorekebisha Makosa

Mizozo ndani ya mwili wa waumini si mapenzi ya **Mungu**. Hutokana na asili ya moyo wa kibinadamu. Kwa wote wanaoleta machafuko na migawanyiko, maneno ya Paulo ni ya kuzingatiwa. *"Lakini, ndugu zangu, mimi sikuweza kusema nanyi kama na watu wenye tabia ya rohoni, bali kama na watu wenye tabia ya mwilini, kama na watoto wachanga katika Kristo. Naliwanywesha maziwa sikuwalisha chakula; kwa kuwa mlikuwa hamjakiweza. Naam, hata sasa hamkiwezi."***—1 Wakorintho 3:1-2.** Paulo alikuwa akizungumza na watu waliokuwa hawajaendelea kusonga mele kiroho kulingana na fursa na nafasi waliyopewa. Walipaswa kuwa tayari kusikia Neno la **Mungu** kwa wazi, lakini bado walikuwa wachanga wa kiroho. Walikuwa kama wanafunzi ambao Kristo aliwaambia, *"Hata bado nikali Ninayo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili hivi sasa."* **Yohana 16:12.** Walisahau kuwa wanapaswa kutakaswa kutoka kwa tabia walizorithi na kujifunza kwenye uzoefu na mazingira yao, na wasidumishe sifa za kimwili. Ilikuwa vigumu kwa Paulo kuwakemea bila wengine kukasirika, ingawa walidai kuamini Ukweli. Ushuhuda wa kiroho haukuwa na manufaa kwao kwa kuwa walikuwa wamepoteza uwezo wa kupambanua mambo ya kiroho.*{EVsw 369:1}*

Wivu, mashaka mabaya, na lawama ziliwazuia wasisikie Roho Mtakatifu. Paulo alitamani kuwafundisha mambo ya kina ya Kiungu yanayohusiana na ile Kweli, lakini wasingeweza kuyavumilia. Badala yake, alichagua mafundisho mepesi—maziwa ya kiroho—ili wasije wakakwazwa. Mafundisho ya kina yalizuiwa kwa kuwa wangeitumia vibaya na kuwaeleza waongofu wapya yale yasiyowafaidi.*{EVsw 370:1}*

Utakatifu kwa **Mungu** kupitia Kristo ni hitaji kwa kila MKristo. Ikiwa kuna makosa katika kanisa, basi yashughulikiwe mara moja. Wengine huenda wakahitaji kukemewa kwa ukali—lakini hii sio kutowatendea haki. Tabibu wa Kweli wa roho hukata kwa kina ili kuhakikisha hakuna sumu itakayobaki na kulipuka baadaye. Baada ya kukemewa, huja toba na ungamo, ndipo **Mungu** hutoa msamaha na uponyaji. Yeye husamehe kila mara ungamo la kweli linapotolewa. —**Review and Herald, December 11, 1900.***{EVsw 370:2}*

Waletao Taabu katika Sayuni

Wapo watu katika makanisa yetu wanaodai kuwa waaminifu, lakini kwa Kweli ni kikwazo kwa kazi ya matengenezo. Wamekuwa kama vizuizi kwenye magurudumu ya gari la wokovu. Watu wa aina hii huwa katika majaribu ya mara kwa mara. Mashaka, wivu, na tuhuma ni zao la ubinafsi, na tabia zinaonekana kuwa

sehemu ya asili yao-zimefumwa kwenye hulka zao. Naweza kuwaita hawa "wanung'unikaji sugu wa kanisani." Mchungaji mmoja wa aina hii hufanya madhara mengi zaidi kuliko wachungaji wawili wanavyoweza kurekebisha.

Wao ni mzigo kwa kanisa na kwa wahudumu wa Kristo. Huishi katika hali ya hewa ya mashaka na tuhuma. Muda mwingi na nguvu za watumishi wa **Mungu** hutumika kusahihisha madhara yao na kurejesha umoja kanisani—jambo linalowavunja moyo na kuwanyima nguvu watenda kazi ya wokovu kwa roho zilizopotea. **Mungu** atawapa thawabu yao watu hawa wanaoleta taabu Sayuni kulingana na matendo yao. ***{EVsw 370:3}***

Wahudumu wa Kristo wanapaswa kuchukua msimamo wao wazi, na wasikubali kuzuiwa katika kazi yao na mawakala hawa wa Shetani. Kutakuwa na atu wengi wa namna hii katika kuuliza maswali, kunung'unika, na kukosoa—na hilo linaweza kuwazuia watumishi wa **Mungu** wasifanye kazi ya mwisho ya ujumbe wa wokovu duniani. Kama kanisa haliwezi kusimama dhidi ya hisia hizi za uasi kutoka kwa wanung'unikaji, wasio na utakaso, ni heri waache watu hawa waende pamoja na kanisa hilo kutumbukia huko, kuliko kupoteza nafasi ya kuwaokoa mamia ambao wangejenga makanisa bora—yenye umoja, nguvu na upendo wa Kweli. ***{EVsw 371:1}***

Njia bora kabisa kwa wachungaji na makanisa ni kuwaacha watu wa aina hii wanaotafuta makosa ya wengine, na waliopindapinda, waanguke katika uovu wao wenyewe, na kuchukua hatua mpya ya imani—kwenda baharini tena, na kutupa wavu wa Injili tena kwa ajili ya watu walioko tayari kuipokea ile Kweli kwa thamani inayostahili. Shetani hufurahi na kujiinua sana watu wa namna hii wanapokubali ile Kweli, kisha wakawa chanzo cha giza na vizuizi dhidi ya maendeleo ya kazi ya **Mungu**. Katika kipindi hiki muhimu sana cha kazi ya Injili, wachungaji hawapaswi kufungwa au kucheleweshwa kwa ajili ya watu waliowahi kuuona Ukweli lakini sasa wamegeuka kuwa watu wa lawama na upinzani. Wanapaswa kuwafunga waumini wa Kweli kwa Kristo, ambaye anaweza kuwashika imara hadi siku ya kuonekana Kwake—huku wakisonga mbele kupeleka Injili kwenye mashamba mapya ya mavuno. —**The True Missionary, February 1874.** ***{EVsw 371:2}***

Ubatizo wa Mara ya Pili-Kubatizwa Tena

Wakati Ubatizo wa Awali Hauridhishi

Kuna wengi katika siku zetu ambao, bila kujua, wamekiuka moja ya amri za sheria ya **Mungu**. Wakati fahamu zao zinaangaziwa na madai ya Amri ya Nne kuletwa kwa dhamiri zao, wanajitambua kuwa ni wenye dhambi machoni pa **Mungu**. Maandiko yasema: "Dhambi ni uasi wa sheria," **1 Yohana 3:4** na tena: "*Yeyote atakayejikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote.*" **Yakobo 2:10.** ***{EVsw 372:1}***

Mtafutaji mwaminifu wa Kweli hatatumia kutojua sheria kama kisingizio cha uvunjaji wake. Nuru ilikuwa karibu naye. Neno la **Mungu** ni wazi, na Kristo amemwagiza achunguze Maandiko. Anaiheshimu sheria ya **Mungu** kuwa takatifu, ya haki, na njema, na anatubu kwa makosa yake. Kwa imani, anadai damu ya upatanisho ya Kristo, na kushika ahadi ya msamaha. Ubatizo wake wa awali haumtoshelezi moyo tena. Sasa anajitambua kuwa ni mwenye dhambi, aliyeshitakiwa na sheria ya **Mungu**. Ameshuhudia kufa kwa dhambi upya, na anatamani tena kuzikwa pamoja na Kristo kwa ubatizo, ili apate kufufuka na kuenenda katika upya wa maisha. Njia hii iko sambamba na mfano alioutoa Paulo alipowabatiza Wayahudi waliomwamini Kristo. Tukio hilo lilirekodiwa na Roho Mtakatifu kama somo la mafundisho kwa ajili ya Kanisa. **—Sketches from the Life of Paul, uk. 133 (1883).*{EVsw 372:2}***

Ubatizo wa Pili Usifanywe Kuwa Suala la Jaribio kwa Waumini Wapya

Suala la ubatizo wa pili linapaswa kushughulikiwa kwa busara kuu. Baada ya Kweli kuhusu Sabato na mambo mengine ya msingi ya imani yetu kuwasilishwa, na roho kuonyesha ujasiri wa kimaadili kuchukua msimamo wao juu ya Ukweli, basi watakuja kuliona suala hili katika mwangaza wa Biblia ikiwa wameongoka kikamilifu. Lakini wengine wamekuwa wakilichukulia jambo hili kwa namna isiyo ya busara, na **Mungu** ametoa maonyo mara nyingi kuhusu suala hili. Wale wanaoliweka suala la ubatizo wa pili mbele, wakilipa uzito sawa na suala la Sabato, hawatoi mfano sahihi wa uelewa wa jambo hili, wala hawawakilishi mada hii kwa usahihi. nahitajika busara kuu kuunganisha Kweli zinazohusiana na Sabato kwa njia sahihi, tukiligawa Neno la Kweli sawasawa, kila mmoja akipewa chakula chake kwa wakati ufaao. ***{EVsw 372:3}***

Wale wanaoinua msalaba wa Sabato hupambana vita vikubwa dhidi ya nafsi na masilahi binafsi yanayotaka kusimama kati yao na **Mungu**. Basi, wanapochukua hatua hii kubwa, miguu yao inapopandishwa

juu ya msingi wa Kweli ya milele, wapewe muda wa kuzoea nafasi yao mpya, bila kushinikizwa kuhusu ubatizo wa pili.*{EVsw 373:1}*

Hakuna mtu anayepaswa kuwa dhamiri ya mwingine au kumlazimisha juu ya suala la ubatizo wa pili. Hili ni jambo ambalo kila mtu binafsi lazima afikie uamuzi wake mbele za **Mungu** kwa hofu, dhamiri iliyosadikishwa na unyenyekevu. Linapaswa kuwasilishwa kwa upole na upendo. Halafu kazi ya kushawishi inapaswa kuachwa mikononi mwa **Mungu**. Wape nafasi Roho Mtakatifu afanye kazi katika mioyo ya watu ili wawe na uhakika wa dhamiri kuhusu hatua hii ya juu zaidi ya kiroho. Roho ya mabishano na mvutano haipaswi kuruhusiwa kutawala juu ya suala hili. Msichukue kazi ya Bwana kutoka mikononi Mwake na kuiweka mikononi mwenu. Wale waliopokea amri za **Mungu** kwa dhamira njema, wakishughulikiwa kwa busara, watakubali Kweli yote muhimu. Lakini inahitajika hekima kushughulika na akili za watu. Baadhi watachelewa kuona na kuelewa baadhi ya Kweli zilizo karibu na Sabato, hasa suala la ubatizo wa pili. Lakini kuna mkono wa **Mungu** unaowaongoza—Roho wa **Mungu** anagusa mioyo yao, nao watajua wanachopaswa kufanya na watakifanya. *{EVsw 373:2}*

hebu wapendwa wahubiri wenye ari wasiwe na pupa kupita kiasi katika jambo hili. Watakuwa na hatari ya kumtangulia Bwana kwa kuleta majaribio ambayo **Mungu** hajawaamuru. Si kazi ya mwalimu yeyote wa Biblia kulazimisha ubatizo wa pili kwa mtu yeyote. Kazi yao ni kuweka wazi misingi mikuu ya zile Kweli za Biblia—hasa kuhusu ubatizo wa pili—na kisha kumwachia **Mungu** afanye kazi ya kushawishi akili na moyo.....*{EVsw 374:1}*

Kila nafsi ya Kweli inayokubali Sabato ya Amri ya Nne, ataelewa wajibu wake kwa wakati ufaao. Lakini hii itachukua muda kwa baadhi yao. Sio jambo la kulazimisha na kulishinikiza kwa wale waliokuja tu kwenye Kweli. Bali, jambo hili litafanya kazi kama chachu; mchakato wake utakuwa wa polepole na kimya, lakini utatimiza kazi yake—ikiwa wahubiri wetu hawatakuwa na haraka kupita kiasi na hivyo kuharibu kusudi la **Mungu**.*{EVsw 374:2}*

Wale waliolielewa jambo hili kwa muda mrefu huliona kwa wazi kabisa na hutarajia wengine walione vivyo hivyo mara moja. Hawafikirii kuwa kwa wale wapya katika imani, suala hili linaweza kuonekana kama kukanusha uzoefu wao wote wa kidini wa awali. Lakini kwa muda, wataanza kuliona kwa mtazamo tofauti. Kadri Kweli inavyoendelea kufumbuliwa akilini mwao, wataona hatua za mbele zinazopaswa kuchukuliwa; nuru mpya itang'aa katika njia yao; Roho wa **Mungu** atafanya kazi mioyoni mwao, iwapo watu hawataingilia na kujaribu kuwalazimisha kuchukua misimamo ambayo wao wanaona kuwa ni Kweli.*{EVsw 374:3}*

Na sasa, na iwe dhahiri: katika nyakati mbalimbali katika uzoefu wetu, **Mungu** amenipa Shuhuda ya tahadhari kwa ndugu zetu kuhusu namna ya kushughulikia suala la ubatizo wa pili. Ndugu yetu mpendwa _____ pamoja na wahubiri wengine kadhaa nilionyeshwa kuwa walikuwa wakifanya kosa katika uzoefu wao kwa kulifanya ubatizo wa pili kuwa swali la jaribio mbele ya watu. Hii si njia sahihi ya kulishughulikia suala hili. Ni jambo la kushughulikiwa kama fursa kuu na baraka. Na wale wote wanaobatizwa tena, ikiwa wanaelewa vyema maana yake, wataliona jambo hilo kwa namna hiyo. Wahubiri hawa wazuri walishindwa kuwasogeza wapya katika imani hatua kwa hatua, kwa tahadhari na uangalifu, na matokeo yake yakawa kwamba baadhi walijiondoa kutoka kwenye Kweli—ambapo kwa uvumilivu kidogo na namna ya upole na hekima, hali hiyo yote ya huzuni ingekuwa imeepukika. —**Letter 56, 1886.***{EVsw 375:1}*

Uongofu wa Pili na Ubatizo wa Pili kwa Waadventista Wa Sabato

Bwana anaita kwa ajili ya matengenezo ya kweli. Na mtu anapoongoka kwa dhati upya, hebu na abatizwe tena. Afanye upya agano lake na **Mungu**, Naye **Mungu** atafanya upya agano Lake pamoja naye. Uongofu mpya ni lazima miongoni mwa waumini, ili kwamba kama mashahidi wa **Mungu**, wapate kutoa ushuhuda wa mamlaka ya Kweli ambayo hutakasa nafsi. —**Letter 63, 1903.***{EVsw 375:2}*

Kujenga Majengo ya Ibada

Kumbukizi za Kweli ya Mungu — Wakati shauku inapoamshwa katika mji au jiji lolote, nia hiyo inapaswa kufuatiliwa. Mahali papaswa pafanyiwe kazi kikamili hadi nyumba ya ibada sahili isimame kama ishara, kumbukizi la Sabato ya **Mungu**, nuru katikati ya giza la kimadili. Kumbukizi hizi zapaswa kusimama mahali pengi kama mashahidi wa ile Kweli. **Mungu** katika rehema Yake ametoa majaliwa kwamba wajumbe wa injili watakwenda katika nchi zote, lugha, na watu mpaka kiwango cha Ukweli kitakapowekwa katika sehemu zote za ulimwengu unaokaliwa. **—Testimonies for the Church, 6: 100 (1900).** *{EVsw 375:3}*

Dhamana ya Kazi Imara-Uhakikisha Kazi Kuwa Imara — Popote ambapo kundi la waumini linapoanzishwa, nyumba ya ibada inapaswa kujengwa. hebu watendekazi wasiondoke mahali hapo bila kukamilisha hili.*{EVsw 376:1}*

Katika sehemu nyingi ambapo ujumbe umehubiriwa na watu wameukubali, wako katika hali ya mapungufu na wanaweza kufanya kidogo tu kupata manufaa ambayo yangeifanya kazi hiyo kuwa ya tabia ya kuonekana. Mara nyingi hii inafanya kuwa vigumu kupanua kazi. Watu wanapopendezwa na Ukweli, wanaambiwa na watumishi/wachungaji wa makanisa mengine—na maneno haya yanaungwa mkono na washiriki wa kanisa: "Watu hawa hawana kanisa, na ninyi hamna mahali pa kuabudia. Ninyi ni kikundi kidogo; maskini na wasio na elimu. Baada ya muda mfupi watumishi wataondoka, na kisha shauku ya watu itapungua. Kisha mtaacha mawazo haya yote mapya mliyopokea.*{EVsw 376:2}*

Je, tunaweza kudhani kwamba hili halitaleta majaribu makali kwa wale wanaoona sababu za imani yetu na kusadikishwa na Roho wa **Mungu** kuhusiana na Ukweli wa sasa? Inapaswa kurudiwa mara kwa mara kwamba kutoka mwanzo mdogo maslahi makubwa yanaweza kukua. Ikiwa hekima na hukumu iliyotakaswa na ujumla wa ustadi unadhihirishwa nasi katika kujenga maslahi ya ufalme wa Mkombozi wetu, tutafanya yote tuwezayo kuwahakikishia watu uthabiti wa kazi yetu. Mimbari za usahili/unyenyekevu sana zitajengwa ambapo wale wanaokubali Kweli wanaweza kupata mahali pa kumwabudu **Mungu** kulingana na maagizo ya dhamiri zao wenyewe. **—Testimonies For The Church 6:100, 101 (1900).***{EVsw 376:3}*

Kununua Majengo Mijini

Katika kila mji ambapo ile Kweli inatangazwa, makanisa yanapaswa kuanzishwa. Katika miji mikubwa, makanisa yanaweza kuhitajika katika sehemu tofauti za mji. Wakati mwingine, nyumba za mikutano zitakuwa zikiuzwa kwa bei nafuu (sale), na zinaweza kununuliwa kwa manufaa ya kazi ya **Mungu**. —**Letter 168, 1909.** *{EVsw 377:1}*

Isiwe duni kuliko makazi yetu (Kanisa lisiwe la kimasikini zaidi ya nyumba tunazoishi!) — Kumekuwa na nyakati ambapo ilibidi kumwabudu **Mungu** katika maeneo ya hali ya chini sana; lakini Bwana hakujizuia kutoa Roho Rake wala kukataa uwepo Wake kwa sababu ya hali hiyo. Ilikuwa ndicho bora wawezacho kufanya kwa wakati huo, na walipomwabudu kwa roho na Kweli, **Mungu** hakuwalaumu au kutoa uwepo Wake kwasababu ya hili. Lakini sasa **Mungu** ametubariki kwa raslimali, nasi hutumia kwa kujipendezesha na kujiinua wenyewe. Ikiwa tunamwacha Bwana nje ya mipango yetu na kumwabudu katika mahali pa chini na duni kuliko tunapojiruhusu sisi wenyewe kuishi, tukitafuta kujitukuza na kumweka **Mungu** nafasi ya pili, hakika hatutapokea baraka Zake. —**Manuscript 23, 1886.** *{EVsw 377:2}*

Iwe Sahili lakini Safi na iliyojengwa kwa Ustadi — Hatuna amri kutoka kwa **Mungu** ya kujenga jengo la fahari kama Hekalu la kale. Bali tujenge nyumba ya ibada ya hali ya kawaida (rahisi), iliyo sahili, safi na iliyojengwa kwa ustadi au iliyopangiliwa vyema.*{EVsw 377:3}*

Kisha wale walio na uwezo wa mali waonyeshe ukarimu na wenye ladha nzuri katika kujenga nyumba ya ibada kama walivyojijengea nyumba zao wenyewe na kuweka mapambo. Wasiwe wa kujitukuza kuliko kumtukuza **Mungu**. Jengo lijengwe kwa ustadi, vyema na bila ubadhirifu na lisiwe na usumbufu. Mambo ya ubinafsi yasituzuie kumtukuza **Mungu**. *Nyumba na ijengwe kwa usahili na kwa ukamilifu ili itakapowasilishwa kwa Mungu, Yeye aweze kuikubali na kuruhusu Roho Wake kutulia juu ya waabudu ambao wana jicho moja lililokita kwa utukufu Wake. Hakuna kinachopaswa kuingilia kati ya utukufu wa Mungu na sisi; hakuna mipango ya ubinafsi, hakuna njama za ubinafsi, hakuna madhumuni ya ubinafsi. Lazima kuwe na makubaliano* —**Manuscript 23, 1886.** *{EVsw 377:4}*

.—Manuscript 23, 1886.

Majengo makubwa, imara na ya Kudumu — Wengine huuliza kwa nini Ellen White hutumia maneno: "rahisi, safi, yenye nafasi na la kudumu" akizungumzia majengo. Ni kwa sababu ninataka majengo yetu yaonyeshe ukamilifu ambao **Mungu** anautarajia kutoka kwa watu Wake.*{EVsw 378:1}*

"Lakini," wengine husema, "ikiwa Bwana anakuja hivi karibuni, kwa nini mnawahimiza wajenzi wetu kuweka vifaa bora zaidi katika majengo wanayojenga?" Je, tunaweza kuthubutu kumjengea au kumtolea dhabihu Mungu ya nyumba iliyotengenezwa kwa vifaa vya bei ya chini, au kazi yenye viwango hafifu, na yenye dosari kiasi kwamba inaweza kung'olewa kutoka kwenye msingi wake inapopigwa na

upepo mkali? Je, tusingeona aibu kuweka vifaa visivyofaa katika jengo kwa ajili ya Bwana. Hakika nisingemshauri mtu yeyote kuweka vifaa visivyofaa katika nyumba ya Bwana, kwani hailipi. Sakafu za nyumba zetu zinapaswa kutengenezwa kwa mbao zilizorandwa vizuri na zinazostahimili imara kustahilimili- hewa nk. Hii itagharimu pesa kidogo zaidi, lakini mwishowe itaepusha usumbufu mwingi. Muundo wa jengo unapaswa kuwiana vizuri, imara na kuonekana vizuri. Kristo Ndiye mfano wetu katika mambo yote. Yeye Alifanya kazi ya useremala na baba yake Yusufu, na kila kitu alichotengeneza kilitengenezwa vizuri, alipima sehemu za jengo kwa uwiano sahihi na kazi yake iliweza kustahimili majaribu (hali ya hewa nk). ***{EVsw 378:2}***

Chochote unachofanya, acha kifanywe pamoja kwa kanuni zilizonyooka na nguvu na ujuzi wako, hakika unaweza kukifanya. Acha kazi yako iwe kama pateni/muundo ulioonyeshwa kwenye mlima Sinai wa Patakatifu (Sanctuary). Majengo yaliyojengwa yatajaribiwa vikali hivi karibuni.—Manuscript 127, 1901.*{EVsw 378:3}*

Washiriki Kusaidia Ujenzi — Wakati kanisa jipya linapoanzishwa, washiriki wake wanapaswa kuamka na kujenga. Waongofu wapya, chini ya uongozi wa mhubiri anayepokea ushauri wa watumishi wenzake, wafanye kazi kwa mikono yao wenyewe, wakisema, “Tunahitaji kanisa, na lazima tulijenge. Kila mmoja atafanya sehemu yake katika ujenzi wa kanisa”***{EVsw 379:1}***

Hebu Tumuonyeshe Kristo kwa kuendelea mbele. **Mungu** anawaita wale wanaodai kumfuata Yesu kufanya kazi kwa moyo mmoja na furaha katika kusudi Lake. Tutakapofanya hivyo, sauti ya shukrani itasikika: “Tazama aliyotutendea Bwana!” —**Letter 65, 1900.** ***{EVsw 379:2}***

Msaada wa Kifedha Kutoka Nje — Tunapaswa kuwa macho, kwamba kazi inapofunguliwa katika miji mikubwa, tuendelee mbele kwa hatua madhubuti. Tumechelewa sana katika kutekeleza maagizo ya kuingia miji na kujenga kumbukumbu za **Mungu**. Hatua kwa hatua, tuwaongoze watu kuingia katika mwanga kamili wa kweli. Tufanye kazi hadi kanisa litaanzishwa na nyumba ya ibada ijengwe. Nimepewa nuru kwamba watu wasiokuwa wa imani yetu watasaidia kwa kiasi kikubwa kwa mali zao, hasa katika miji mikuu ya Marekani. Msaada utatolewa na watu kama hao—**Review and Herald, September 30, 1902.** ***{EVsw 379:3}***

Aina Tofauti za Miundo (Different Architecture styles)

Makanisa yanajengwa katika maeneo mengi, lakini si lazima yawe na mtindo mmoja tu. Miundo tofauti inafaa maeneo tofauti. ***{EVsw 379:4}***

Kama vile kulivyokuwa na vito mbalimbali kwenye kifua cha kuhani mkuu, kwamba kila kito kimoja kilikuwa na mwanga tofauti wa rangi iliyoakisiwa nacho, kikiongezea uzuri wake maalumu kilipokaa na vito vingine na kuleta ukamilifu ndivyo ilivyokuwa katika kazi ya Mungu. Kila jiwe lilibeba uzito wake, na ujumbe maalumu kutoka kwa Mungu. Kulikuwa mawe mengi, ila kifuko cha kifuani cha hukumu kilikuwa kimoja. Vivyo hivyo kila mtu katika kanisa ana tabia yake ya kipekee lakini wanaunda familia moja katika Kristo. — **Letter 53, 1900.*{EVsw 379:5}***

Umuhimu wa Hewa Safi-Uingizaji Hewa Safi Uzingatiwe-Muhimu-Ventilation

Katika jumba zuri la ibada na la kifahari huko _____, mkutano wa Sabato alasiri ulijaa watu wengi. Ilikuwa siku ya joto, na hewa ilihitajika iingie toka nje na kuzunguka vyema kwenye jengo (ventilation) lakini madirisha hayakuweza kufunguliwa kwa sababu yalikuwa ya kioo maalum kisichoweza kufunguka ila yalipendeza kwa rangi za kufurahisha macho. Kutokana na hali hiyo, watu walitaabika sana, na mhubiri alipumua sumu ya hewa iliyotandaa hewani, naye aliteseka hadi akaumwa kwa wiki nzima na hakuweza kutimiza moja ya miadi yake mitatu huko New York City. Kwa nini watu wenye maarifa mengi kuhusu afya, usafi wa mazingira, na uingizaji hewa safi toka nje ya majumba, waruhusu jumba la mikutano lililojengwa vibaya namna hii kuendelea kuwapo mwaka hadi mwaka kama ghala za kufungia hewa yenye sumu?— —**W. C. White, Review and Herald, November 25, 1909.** ***EVsw 380:1}***

Muwe na Shule ya Kanisa

Watendakazi katika eneo jipya hawapaswi kujisikia huru kuacha kazi zao hadi vifaa vinavyohitajika vitolewe kwa ajili ya makanisa yaliyo chini ya uangalizi wao. Sio tu kwamba nyumba ya ibada ya unyenyekevu inapaswa kujengwa, lakini mipango yote muhimu inapaswa kufanywa kwa uanzishwaji wa shule ya kudumu ya kanisa.*EVsw 380:2}*

Jambo hili limewasilishwa kwa uwazi mbele yangu. Niliona katika sehemu mbalimbali makundi mapya ya waumini yakipandwa na nyumba za mikutano zikijengwa. Wale waamini wapya walioingia kwenye imani walikuwa wakisaidia kwa moyo na mikono ya hiari, na wale waliokuwa na mali walikuwa wakisaidia kwa mali zao. Katika orofa ya chini ya kanisa, chini ya ardhi (basement), nilionyeshwa chumba kilichoandaliwa kwa ajili ya shule ambapo watoto wangeweza kuelimishwa katika Kweli za Neno la **Mungu**. Walimu waliowekwa wakfu walichaguliwa kwenda katika maeneo haya. Idadi za wanafunzi shuleni haikuwa kubwa, lakini ulikuwa mwanzo mzuri na wenye furaha. **—Testimonies For The Church 6:108 (1900).** *EVsw 380:3}*

Songeni Mbele

Tukifungua kazi katika sehemu moja ya shamba la Bwana na kuanzisha kundi la waumini, tunaliweka wakfu katika agano na **Mungu** na kisha tunawahimiza waamini kushirikiana nasi katika kujenga nyumba ya ibada sahili. Mara tu jengo la ibada linapokamilika na kuwekwa wakfu kwa Bwana, tunaelekea sehemu nyingine ya shamba la Bwana. Neno la Bwana limekuja mbele yetu kwa uwazi na likibainishwa ni, “Songa mbele.” Na kadiri ujumbe wa onyo unavyotolewa sehemu moja, na kisha wanawake na wanaume wanainuka ili kuendeleza kazi hapo, nasi tunahamia maeneo ambayo bado hayajaguswa ya shamba la mizabibu la Bwana. **—Letter 154, 1899. {***EVsw 381:1}*

Kuendeleza Kazi Katika Maeneo Mapya (ambayo hayajafikiwa bado)

Washiriki wa Kanisa Kufundishwa Kusimama Wenyewe — Ninaposafiri kupitia Kusini mwa Konferensi, niliona mji baada ya mji ambao haukuwa umefikiwa na Injili. Kuna shida gani? Wachungaji wanazunguka-zunguka kwenye makanisa ambayo tayari yanaujua Ukweli, ilhali maelfu wanapotea bila Kristo.*EVsw 381:2}*

Kama mafundisho sahihi yangetolewa, kama mbinu sahihi zingetumika, kila mshiriki wa kanisa angefanya kazi yake kama sehemu ya mwili wa Kristo. Angefanya kazi ya kimishenari ya Kikristo. Lakini makanisa yanakufa, na wanahitaji mchungaji awahubirie.*EVsw 381:3}*

Wanapaswa kufundishwa kuleta zaka kwa uaminifu kwa **Mungu**, ili aweze kuwapa nguvu na kuwabariki. Wanapaswa kuwekwa katika hali ya utendaji, ili pumzi ya **Mungu** iwapajie. Wanapaswa kufundishwa kwamba ikiwa hawawezi kusimama wenyewe bila kuwepo kwa mchungaji, basi wanahitaji kuongoka upya, na kubatizwa upya. Wanapaswa kuzaliwa mara ya pili. — **Manuscript 150, 1901.** *EVsw 381:4}*

Nendeni Mkafanye kazi Kwa Ajili ya Roho — Badala ya kuwaweka wachungaji kazini kwa ajili ya makanisa ambayo tayari yanaijua Kweli, hebu washiriki wa makanisa wawaambie watenda kazi hawa: “Nendeni mkafanye kazi kwa ajili ya roho zinazoangamia gizani. Sisi wenyewe tutaendeleza ibada za kanisa. tutaendeleza mikutano, na, kwa kudumu ndani ya Kristo, tutadumisha maisha ya kiroho. Tutafanyia kazi roho zinazotuzunguka, na tutatuma maombi yetu, mali na karama zetu ili kuwategemeza watenda kazi katika mashamba yenye uhitaji zaidi na ukiwa. **—Testimonies For The Church 6:30 (1900).{***EVsw 382:1}*

Watenda Kazi wa Mkutano Waitwe Katika Meeneo Mapya — Kama kanuni ya jumla, watenda kazi wa makonferensi wanapaswa kutoka kwenye makanisa na kuingia kwenye maeneo mapya, wakitumia uwezo wao walioupokea kutoka kwa **Mungu** kwa makusudi ya kutafuta na kuwaokoa waliopotea. — **Letter 136, 1902.** *EVsw 382:2}*

Kazi ya Nguvu Inahitajika (aggressive work) — Wachungaji wetu wanapaswa kupanga kwa hekima kama mawakili na wasimamizi waaminifu. Hawapaswi kuona kama ni wajibu wao kuzunguka-zunguka katika makanisa yaliyokwisha kuanzishwa, bali wanapaswa kufanya kazi ya kuvunja nguvu ya Shetani kwa ukali sana (aggressive work), kwa njia ya uinjilisti wa kimkakati, wakihubiri Neno na kufanya kazi ya nyumba kwa nyumba katika maeneo ambayo bado hayajasikia Ukweli... Wataona kwamba hakuna jambo linalotia moyo zaidi kama kufanya kazi ya uinjilisti katika maeneo mapya. — **Letter 169, 1904.** *EVsw 382:3}*

Ikiwa wachungaji wangeondoka katika maeneo yaliyozoeleka, na kwenda katika maeneo mapya, washiriki wangelazimika kubeba majukumu, na uwezo wao ungeongezeka kadri wanavyoutumia. — **Letter 56, 1901.** ***EVsw 382:4}***

Nguvu za Uchungaji Zinaisha Katika Makanisa Yaliyoimarishwa — Watu wetu wamepewa nuru kuu, lakini bado sehemu kubwa ya nguvu za wachungaji wetu zinatumika katika makanisa, wakifundisha wale ambao wanapaswa kuwa walimu; kuwaangazia wale ambao wanapaswa kuwa "nuru ya ulimwengu"; kuwanyweshea wale ambao kutoka kwao kunapaswa kutiririka chemchemi za maji ya uzima; kuwaongezea utajiri wale ambao wanaweza kuwa kama migodi ya hazina ya Kweli ya kiroho; kurudia mwaliko wa Injili kwa wale ambao wanapaswa kuwa wametawanyika hadi miisho ya dunia, wakiwasilisha ujumbe wa Mbinguni kwa wengi ambao hawajapata fursa kama walizopata wao na kuzifurahia; kuwalisha wale ambao wanapaswa kuwa njiani na barabarani wakitoa mwaliko: "Njoni; kwa maana vitu vyote viko tayari sasa." Njoni kwenye karamu ya Injili; njooni kwenye chakula cha Mwana-Kondoo; kwa maana vitu vyote vimekwisha kuwa tayari. ***EVsw 382:5}***

Sasa ni wakati wa kujitahidi kwa dhati na bidii mbele za **Mungu**. Sauti zetu zinapaswa kuungana na ile ya Mwokozi katika sala ile ya ajabu:

"*Ufalme Wako uje. Mapenzi Yako yatimizwe hapa duniani kama huko mbinguni*." Hebu dunia yote ijazwe na utukufu Wake. Wengi watauliza, "Ni nani aliye wa kutosha kwa mambo haya?" Lakini jukumu hili liko juu ya kila mtu mmoja mmoja. "Sio kwamba sisi tuna uwezo wa kujitosheleza kutoka kwetu wenyewe kufikiri chochote kama kutokana na sisi wenyewe; bali uwezo wetu watoka kwa **Mungu**." **— Review and Herald, July 23, 1895.{*EVsw 383:1}***

SEHEMU YA 11—KAZI KATIKA MIJI MIKUBWA YA MAREKANI

New York

Ujumbe Uendelee— Nilipokuwa New York katika msimu wa baridi wa 1901, nilipokea nuru ya kazi katika jiji hilo kubwa. Usiku baada ya usiku kazi ambayo ndugu zetu wangeifanya ilipita mbele yangu. Huko New York ujumbe unapaswa kwenda kama taa inayowaka. **Mungu** atainua watendakazi wa kazi hii, na malaika Zake watawatangulia watu. Ingawa miji yetu mikubwa inafikia haraka hali kama ile ya ulimwengu wa kabla ya Gharika, ingawa ni kama Sodoma kwa uovu, lakini ndani yake kuna roho nyingi adilifu, ambazo, kama zinaposikiliza Ukweli wa kushangaza wa ujumbe wa marejeo, watahisi usadikisho wa Roho. New York iko tayari kufanyiwa kazi. Katika mji huo mkubwa, ujumbe wa Ukweli utatolewa kwa uweza wa **Mungu**. Bwana anawaita watendakazi. Anatoa wito kwa wale ambao wamepata uzoefu katika kazi, kuichukua na kuendelea mbele kwa hofu Yake kazi inayopaswa kufanywa New York na katika miji mingine mikubwa ya Marekani. Anahitaji pia mali zitakazotumiwa katika kazi hii. —**Testimonies For The Church 7:54, 55 (1902).{*EVsw 384:1}***

New York—Mfano wa Kazi kwa Dunia Nzima—Wale ambao wanabeba mzigo wa kazi huko Greater New York wanapaswa kupata msaada wa watendakazi bora ambao wanaweza kupatikana. Hebu kituo cha kazi ya **Mungu** kiwekwe hapa, na kila kinachofanyika kiwe ishara ya kazi ambayo Bwana anatamani kuona inafanywa ulimwenguni.**{*EVsw 384:2}***

Huko Greater New York Bwana ana roho nyingi za thamani ambazo hazijamsujudia Baali, na kuna wale ambao kwa ujinga wametembea katika njia za upotofu. Nuru ya Kweli inapaswa kuangaza Juu ya hawa, ili wapate kumwona Kristo kama Njia, Kweli, na Uzima. **{*EVsw 385:1}***

Tunapaswa kuwasilisha Ukweli katika upendo wa Kristo. Hakuna ubadhirifu au onyesho linalopaswa kuwepo katika kazi hiyo. Kazi Inapaswa kufanywa kulingana na agizo la Kristo. Inapaswa kupelekwa mbele kwa unyenyekevu, na kwa usahili wa injili. Hebu watendakazi wasitishwe na mwonekano ya nje, hata kama inatisha kiasi gani. Fundisha Neno, na Bwana kwa Roho Wake Mtakatifu atatuma usadikisho kwa wasikilizaji. —**Testimonies For The Church 7:38 (1902).{*EVsw 385:2}***

Kufanya Kazi Kwa Utaratibu wa Mungu — Njia yetu ya kufanya kazi lazima ifuate mpango wa **Mungu**. Kazi ya **Mungu** katika miji mikubwa haitakiwi kufanywa kwa mipango ya kibinadamu.....**{*EVsw 385:3}***

Katika kazi yetu tunapaswa kukumbuka jinsi Kristo alivyofanya kazi. Yeye Ndiye aliyeumba dunia. Alimuumba mwanadamu. Kisha akaja kwa mwili duniani ili kuwaonyesha watu jinsi ya kuishi maisha yasiyo na dhambi.{*EVsw 385:4*}

Ndugu fulani, Bwana amekupa nafasi ya kufanya kazi mjini New York, na huduma yako ya umishenari hapo inapaswa kuwa mfano wa jinsi kazi ya umishenari inavyopaswa kufanywa katika miji mingine. Unapaswa kuonyesha jinsi ya kupanda mbegu, na baadaye kuvuna mavuno. Wapo wengine wanaoweza kushirikiana nawe katika kazi hii kwa uelewa na huruma ya moyo mmoja.....{*EVsw 385:5*}

Kazi yako New York imeanzishwa katika mstari sahihi. Unapaswa kuifanya New York kuwa kituo cha juhudi za umishenari, ambapo kazi inaweza kuendelea kwa mafanikio. Bwana anatamani kituo hiki kiwe shule ya mafunzo kwa watendakazi, na hakuna kitu kinachopaswa kuvuruga kazi hiyo. Baada ya watu kuukubali Ukweli na kusimama imara juu yake, basi Bwana atawaandaa wapokee mafundisho kamili ya Kweli ya Biblia. Unapaswa kuwachagua wasaidizi watakaobeba kazi kwa msingi wa Ukweli, kikamilifu kwa bidii, na kwa lengo la kugeuza nafsi nzima—mwili, roho, na akili. Msingi imara unaozingatia mpango wa Injili ni lazima uwekewe msingi wa ujenzi wa kanisa. —**Letter 150, 1901.**{*EVsw 385:6*}

Mahitaji ya Umishenari wa Tiba na Elimu Katika Jiji Kubwa— Tunahitaji kituo cha afya, na usafi na shule karibu na jiji la New York, na kadri tunavyochelewa kuyapata, ndivyo itakavyokuwa vigumu zaidi.{*EVsw 386:1*}

Ingefaa sana kupata mahali pa kuishi kwa watendakazi wetu wa umishenari nje kidogo ya jiji. Ni muhimu sana kwao kuwa na maji safi, yasiyo na uchafu wowote. Kwa sababu hii, ni busara kufikiria maeneo ya vilimani. hebu pawe na ardhi kidogo ambapo matunda na mboga mboga zinazoweza kulimwa kwa ajili ya faida ya watendakazi. Pawe na kituo cha umishenari katika sehemu yenye afya, na kiunganishwe na kituo cha afya ndogo. Pia, pawe na mahali jijini ambapo matibabu rahisi yanaweza kutolewa. {*EVsw 386:2*}

Nyumba ya aina hiyo ingekuwa kimbilio la kupendeza kwa watendakazi wetu, ili wapate kuwa mbali na makelele na vurugu za jiji. Zoezi la kupanda milima huwa faida kubwa kwa wahubiri wetu, madaktari, na watendakazi wengine ambao wako katika hatari ya kutofanya mazoezi ya kutosha.{*EVsw 386:3*}

Nyumba kama hizo zipatikane karibu na miji kadhaa, na juhudi za dhati na thabiti zifanywe na watu wenye uwezo kupeleka ujumbe wa onyo katika miji hiyo. Tumegusa tu kwa juu juu baadhi ya miji. **—Medical Ministry, uk. 308 (1909).**{*EVsw 386:4*}

Msaada Bora— Kuanza kazi ya umishenari wa tiba huko New York kutakuwa jambo bora zaidi unaloweza kufanya. Nimeonyeshwa kuwa ikiwa katika kazi hiyo kutakuwepo wanaume na wanawake wenye uzoefu, watakaoonyesha mfano halisi wa huduma ya kweli ya matibabu ya umishenari, kazi hiyo itakuwa na nguvu kubwa ya kuleta mtazamo sahihi kwa watu. —**Letter 195, 1901.**{*EVsw 387:1*}

Uinjilisti wa Tiba Kwa Watu wa Mataifa Mbalimbali— Katika mji wa New York wapo wengi waliokomaa kwa ajili ya mavuno. Katika jiji hili kubwa kuna maelfu ambao hawajainama kwa Baali. Malaika alisema, “Tazama, nawapelekea habari njema ya furaha kuu, itakayokuwa kwa watu wote.” New York ni sehemu ya hao “watu wote.” Tunatamani kuona mwaka mpya ukianza na walimu wakiwa kazini katika maeneo yote ya jiji la New York. Kuna kazi ya kufanywa katika jiji hili..... Katika miji yetu mikubwa, kazi ya umishenari wa tiba ni lazima ifanyike sambamba na huduma ya Injili. Kazi hii itafungua milango kwa Ukweli kuingia. — **Manuscript 117, 1901.**{*EVsw 387:2*}

Matangazo ya Kutisha, Yanayodhuru— Muda uliopita, Mzee fulani alitoa matangazo ya kushangaza kuhusu kuangamizwa kwa New York. Niliandika mara moja kwa wale waliokuwa wakisimamia kazi pale, nikisema kuwa sio busara kuchapisha matangazo ya aina hiyo, kwani yanaweza kuleta msisimko wa kiroho usio na msingi au unaopitiliza, jambo litakalodhuru kazi ya **Mungu**. Inatosha kuwasilisha kweli ya Neno la **Mungu** kwa watu. Matangazo ya kushangaza yanadhoofisha maendeleo ya kazi yake....{*EVsw 387:3*}

Nimetuma tahadhari kwa ndugu wanaofanya kazi New York, nikiwaambia kuwa matangazo ya kuvutia ya kuogofya hayatakiwi kuchapishwa. Wakati ndugu zangu wanapokwenda mbali mno kwa kupitiliza, huathiri hata mimi, na ninalazimika kubeba aibu ya kuitwa nabii wa uongo. {*EVsw 387:4*}

Je, mnafikiri kwamba kama ningeambiwa kuwa New York itaangamizwa na mawimbi makubwa ya bahari, ningehimiza ununuzi wa ardhi umbali wa maili sitini tu kutoka jiji hilo kama eneo la kituo cha afya, na mahali pa kuendeleza kazi ya New York? **—Letter 176, 1903.**{*EVsw 388:1*}

Mipango ya Kuwafikia Wafanyabiashara— Unapaswa kuhisi jukumu la dhati la kufanya kazi New York. Wanaume walio katika biashara huko New York na miji mingine mikubwa, kwa hakika kama wapagani wa nchi za mbali, ni lazima wafikishiwe ujumbe. —**Letter 168, 1909.**{*EVsw 388:2}*

Changamoto za Majengo na Nyumba za Ibada— Nenda katika jiji la New York. Lichunguze kwa makini, na uone kama ni busara kununua ukumbi huo na ardhi ilipo. Huenda ardhi hiyo ikaweza kupangishwa kwa muda wa miaka kadhaa. Nimeelekezwa kuwa baadhi ya njia kama hizo zitahitajika katika kazi ya miji mikubwa. Ikiwa baada ya kuchunguza kwa makini mtaamua kuwa ni vyema kununua ukumbi huo, tutafanya kila tuwezalo kuchangisha fedha. Lakini ni muhimu kufanya hivyo kwa uelewa. Ombeni, ombeni, ombeni, kwa maana ikiwa inawezekana, Shetani atajaribu kufunga milango ambayo tayari imefunguliwa kwa ajili ya kuingiza Kweli. Bwana anatamani kituo cha Kweli kisimikwe katika jiji kubwa na lenye uovu la New York.....{*EVsw 388:3}*

Ninakuomba uchunguze kazi ya New York, na upange mipango ya kuanzisha kumbukumbu ya **Mungu** katika jiji hilo. Pawe kituo cha kazi ya umishenari, na kituo cha afya (sanitarium) isimikwe humo... ...Jitihada za dhati lazima zifanywe kuunganisha makanisa yetu ya New York na miji inayozunguka. Hili linawezekana, na lazima lifanyike ikiwa vita vya kimishenari New York vitafanikiwa na tusonge mbele. — **Letter 154, 1901.**{*EVsw 388:4}*

Matokeo Ya Kufanya Kazi Kwa Jinsi Inavyopasa— **Mungu** anataka kazi iendelee New York. Kunapaswa kuwa na maelfu ya wanaoshika Sabato mahali pale, na ingekuwa hivyo kama kazi hiyo ingefanywa ipasavyo. Lakini chuki huibuka. Watu hutaka kazi ifanyike kwa njia zao wenyewe, na wanakataa kukubali mipango pana ya wengine. Kwa njia hiyo fursa hupotea. New York kunapaswa kuwa na vikundi vidogo kadhaa, na watendakazi watumwe huko. Si lazima mtu awe amewekwa wakfu kama mchungaji ili aweze kumtumikia **Mungu**. Watu kama hao wafundishwe jinsi ya kufanya kazi, kisha watumwe. Watakaporudi, waeleze kazi waliyoifanya. Hebu na wamhimidi Bwana kwa baraka Zake, kisha waende tena. Watie moyo. Maneno machache ya kutia moyo yatakuwa msukumo mkubwa kwao. — **Life Sketches, uk. 385 (1915).**{*EVsw 389:1}*

Boston na New England

Miji ya New England Isiyofikiwa au Kufanyiwa Kazi— Akili yangu imekuwa na mzigo mkubwa kwa ajili ya miji mikubwa ya Mashariki ya Marekani. Mbali na jiji la New York, ambako mlifanya kazi majira ya joto yaliyopita, kuna jiji muhimu la Boston, karibu na mahali lilipo Kituo cha afya cha Melrose. Nami sijui mahali pengine penye uhitaji mkubwa zaidi wa kujengwa tena kwa kazi za kwanza kuliko Boston na Portland, Maine, ambapo ujumbe wa kwanza ulihubiriwa kwa nguvu, lakini sasa kuna kikundi kidogo tu cha watu wetu. — **Letter 4, 1910.**{*EVsw 389:2}*

Inapaswa Kufanyiwa Kazi Bila Kukawia— Ikiwa katika jiji la Boston na miji mingine ya Mashariki wewe na mkeo mtaungana katika kazi ya uinjilisti wa tiba, manufaa yenu yataongezeka, na mtapata mwanga ulio wazi wa wajibu wenu. Katika miji hii ujumbe wa malaika wa kwanza ulienda kwa nguvu kuu mnamo 1842 na 1843, na sasa wakati umefika ambapo ujumbe wa malaika wa tatu unapaswa kutangazwa kwa upana huko Mashariki. Kuna kazi kubwa kwenye Sanitarium zetu za Mashariki. Ujumbe huu utakwenda kwa nguvu kama kazi inavyokaribia mwisho wake. Portland, Maine—jiji lililo mstari wa mbele katika matengenezo ya afya na kiasi—linapaswa kufanyiwa kazi bila kuchelewa. **—Letter 20, 1910.**{*EVsw 389:3}*

Kuna miji kama Brunswick na Bangor katika Maine inayopaswa kufanyiwa kazi kwa uaminifu. Katika miji na vijiji vyote vya Mashariki, Ukweli unapaswa kung'aa kama taa iwakayo. —**Letter 28, 1910.**{*EVsw 390:1}*

Umuhimu wa Kituo cha Afya cha Karibu— Majengo na mazingira ya Melrose ni ya kiwango cha kuonyesha mfano bora wa kazi yetu ya kimishenari ya tiba, ambayo inapaswa kuendelezwa sio tu Boston, bali pia katika miji mingi ya New England ambayo bado haijafikiwa. Kituo cha Melrose ni cha aina ambayo inawezesha kuwepo kwa huduma zitakazovutia watu wasiokuwa wa imani yetu. Watu wa hali ya juu na wa kawaida watatembelea taasisi hiyo ili kufaidika na huduma za kurejesha afya.{*EVsw 390:2}*

Boston imeonyeshwa kwangu mara kwa mara kuwa ni mahali panapopaswa kufanyiwa kazi kwa uaminifu. Nuru inapaswa kung'aa katika viunga vyake na sehemu za ndani kabisa. Kituo cha afya cha Melrose ni mojawapo ya nyenzo muhimu zaidi zinazoweza kutumika kuifikia Boston kwa Ukweli. Jiji hili na viunga vyake vinapaswa kusikia ujumbe wa mwisho wa rehema kwa dunia yetu. Mikutano ya kambi inapaswa kufanyika katika maeneo mengi. Watendakazi wanapaswa kutumia kwa ubora uwezo wote waliokabidhiwa na **Mungu**. Karama za neema zitaongezeka kwa matumizi yenye hekima. Lakini kusiwepo na kujivuna au

kujitukuza. Mipango kamili isibainishwe hapo. Acheni Roho Mtakatifu awaongoze watendakazi. Wanapaswa kuendelea kumtazama Yesu daima, mwanzilishi na mkamilishaji wa imani yao. Kazi ya jiji hili kubwa na itakuwa na alama ya ufunuo wa Roho Mtakatifu, ikiwa wote watatembea kwa unyenyekevu mbele za **Mungu**.....{*EVsw 390:3}*

Tunatumaini wale wanaosimamia kazi ya New England watashirikiana na wasimamizi wa kituo cha afya cha Melrose katika kuchukua hatua za makusudi kufanya kazi inayopaswa kufanyika Boston. Watendakazi mia moja wangeweza kufanya kazi kwa mafanikio katika sehemu mbalimbali za jiji, kwa njia tofauti tofauti za huduma.....{*EVsw 391:1}*

Kazi ya uinjilisti wa tiba ni mlango ambao Ukweli utaingia kupitia kwa nyumba nyingi mijini. Katika kila jiji watapatikana wale watakaothamini Ukweli wa ujumbe wa malaika wa tatu.....{*EVsw 391:2}*

Bwana atafanya kazi kwa nguvu tunapojitahidi kutimiza wajibu wetu kwa uaminifu. Yeye Atasababisha Boston kusikia ujumbe wa Kweli ya sasa. Shirikianeni Naye katika jambo hili, ndugu yangu, dada yangu, Naye atawasaidia, atawatia nguvu, na kutia mioyo yenu kuhusika wokovu wa roho nyingi zenye thamani. —**Special Testimonies, Series B, Na. 13, uk. 12-16 (1906).** {*EVsw 391:3}*

Maelfu ya Boston Wanatamani Ukweli Rahisi— Nahisi mzigo mzito kwamba Boston inapaswa kusikia Neno la Bwana na sababu za imani yetu. Mwombeni Bwana awainue watendakazi wa kuingia katika uwanja huu. Mwombeni awaandalie watendakazi watakaopata njia ya kuwafikia watu wa Boston. Ujumbe huu lazima usikike. Kuna maelfu mjini Boston wanaotamani Ukweli rahisi kama ulivyo ndani ya Yesu. Je, ninyi mnaohubiri kwa Neno na mafundisho hamwezi kuandaa njia ya Ukweli huu kuwafikia roho hizi? —**Letter 25, 1905.**{*EVsw 391:4}*

Tukichukua Hatua kwa Imani— Ilikuwa ni katika mpango wa **Mungu** kwamba kituo cha afya cha Melrose Sanitarium kiingie mikononi mwa watu wetu, kama njia ya kuwafikia watu wa tabaka la juu. Jiji la Boston na maeneo yanayolizunguka yanapaswa kufanyiwa kazi kikamilifu. Nimeagizwa kumwambia Mzee _____ na Mzee _____ kwamba wanapaswa kushirikiana na wanaume na wanawake watakaosaidia kupaza sauti ya onyo. Kituo cha afya-sanitarium- kinapaswa kushirikishwa na msaada bora unaoweza kutoa mwelekeo wa kidini kwa taasisi hiyo.{*EVsw 392:1}*

Hebu Mzee _____ atafute msaada bora anaoweza kupata, na apige hema karibu na jiji la Boston, na ahubiri kwa watu kama Bwana atakavyompa kusema. Kusiwepo na kuchelewa kuchukua kazi hii. Mzee _____ anaweza kuimarisha juhudi hiyo kwa kufanya kazi kwa ajili ya Wayahudi. Madaktari wanaweza kusaidia sana kwa kutoa mafundisho ya afya wakati wa mikutano.....{*EVsw 392:2}*

Bwana anaita kazi ifanyike katika jiji la Boston. Mkichukua hatua kwa imani katika kazi hii, **Mungu** atawabariki sana. Hakuna haja ya maonyesho na shuguli nyingi za nje, bali fanyeni kazi kwa utulivu na bidii. Bwana atawasaidia watendakazi wake wanyenyekevu na waaminifu. Fanyeni juhudi za dhati. Semeni daima, "Sitashindwa wala kukata tamaa." **—Letter 202, 1906.**{*EVsw 392:3}*

Mungu Ataongoza katika Kuanzisha Taasisi— Usifadhaike, dada yangu. Bwana anaijua hali yako. Hakuna kinachomponyoka machoni Pake. Yeye Atasikia maombi yako; kwa kuwa Yeye ni **Mungu** asikiaye na ajibuye maombi. Weka tumaini lako Kwake, Naye atakuletea msaada, kwa njia Yake Mwenyewe. Ninashukuru sana kwa kile ninachosikia kuhusu baraka zilizofuatana na kazi huko New Bedford. Tumtumainie **Mungu**, na tuishike imani yetu kwa bidii.....{*EVsw 392:4}*

Iwapo ndugu _____ hajisikii kuwa huru kutoa mali yake ili kuanzisha kituo cha afya wakati huu, ni heri asilazimishwe. Mawazo tuyadhaniyo kuwa ni mazuri siyo daima yaliyo bora. Hebu mapenzi ya Bwana yawe yakiimarishwa-yasimikwe moyoni.{*EVsw 393:1}*

Ee, jinsi ninavyotamani kuona kazi ikiendelea kwa nguvu huko New Bedford na Fairhaven, na katika maeneo mengine mengi yenye uhitaji wa ukweli kama haya. Tunatumaini kwamba siku moja kituo cha afya cha sanitarium itaweza kuanzishwa New Bedford. Watendakazi wa uinjilisti wa tiba wanahitajika katika miji kama hiyo. Lakini, dada mpendwa, kuendesha kituo cha afya kunahitaji vipaji visivyo vya kawaida katika usimamizi Sanitarium, usafi nk. Wanaume wenye uzoefu, waliojaribiwa na kuthibitishwa, wanapaswa kuanzisha na kushika hiyo kazi hiyo.....kwamba sehemu ya watendakazi wanaojitolea kuanzisha taasisi kama hiyo wana uzoefu na sifa, haitoshi kwaajili yao wenyewe, kwa ajili ya taasisi, na kwa ajili ya kazi kwa ujumla, ni muhimu kwamba kundi kamili la wanaume na wanawake waliohitimu vizuri wapatikane kuingia katika kazi hiyo. Jicho la Bwana liko juu ya uwanja mzima, na wakati utakapofika wa taasisi kuanzishwa

katika uwanja fulani, Yeye anaweza kugeuza hapo fikra za wanaume na wanawake nao waandaliwe vyema kuingia katika taasisi hiyo{*EVsw 393:1}{EVsw 393:2}*

Kuna nyanja nyingi za kazi zinazopaswa kuendelezwa. Kuna fursa za wauguzi waliopata mafunzo bora kuingia katika familia, na kuchochea katika kaya hizo hamu ya kupokea Ukweli. Kuna haja ya haraka ya kupata wainjilisti na watendakazi wa Biblia katika miji kama Boston na New Bedford. Watendakazi kama hao watapata nafasi nyingi za kupanda mbegu njema. Kuna kazi kwa kila mtendakazi mwenye bidii, aliye makini na mnyofu. Mafundisho ya Kristo—Ukweli rahisi alioufundisha kwa mifano—unahitajiwa leo kama ilivyokuwa wakati Yeye alipokuwa duniani Mwenyewe. **—Letter 29, 1905.**{*EVsw 393:3}*

Rudia Ujumbe katika Miji ya Mashariki— Je, kuna nini kinachofanyika katika miji ya Mashariki ambako ujumbe wa kuja kwa Bwana ulitangazwa mara ya kwanza? Miji ya Magharibi imepata fursa nyingi, lakini ni nani huko Mashariki aliyekuwa na mzigo wa kurudia kazi ya kwenda tena katika maeneo ambayo katika siku za mwanzo za ujumbe yalibatizwa na Kweli ya kuja kwa Bwana? Nuru imetolewa kuwa Ukweli unapaswa urudi tena katika majimbo ya Mashariki ambako tulianza kazi yetu, na ambako tulipata uzoefu wetu wa kwanza. Tunapaswa kufanya kila juhudi kueneza maarifa ya kweli kwa wote watakaosikia, na kuna wengi watakaosikiliza. Katika miji yetu mikubwa **Mungu** anao watu waaminifu wanaopendezwa na Kweli. Kuna kazi ya bidii inayopaswa kufanywa katika majimbo ya Mashariki. Rudieni ujumbe, rudieni ujumbe, ndilo neno lililosemwa kwangu tena na tena. Waambie watu Wangu warudie ujumbe katika maeneo ambako ulihubiriwa kwa mara ya kwanza, na ambako makanisa kadhaa yalichukua msimamo kwa ajili ya Kweli, nguvu ya **Mungu** ikishuhudia ujumbe huo kwa njia ya ajabu. —**Manuscript 29, 1909.**{*EVsw 394:1}*

Miji ya Mashariki na Kusini

Ujumbe Kufikia Miji na Vitongoji Vyake — Kuna Jiji la New York, na miji yenye watu wengi iliyo karibu; kuna Philadelphia, Baltimore na Washington. Sihitaji kuitaja yote kwa majina; mnajua ilipo. Bwana anatamani ujumbe wa malaika wa tatu utangazwe kwa nguvu katika miji hii. —**Manuscript 53, 1909.**{*EVsw 394:2}*

Philadelphia: Misukosuko Yafungua Milango ya Uinjilisti — Philadelphia na maeneo mengine muhimu yapaswa kushtuliwa na kufanyiwa kazi. Wainjilisti wanapaswa kuingia maeneo yote ambako watu wameamshwa na masuala ya sheria za Jumapili na kufundishwa kwa dini katika shule za umma. Ni kwa sababu ya kupuuzwa kwa nafasi hizi za **Kiungu** na Waadventista wa Sabato kuwasilisha Ukweli, ndiko kunakobebesha moyo wangu uzito na kunifanya nisilale usiku baada ya usiku. **—Review and Herald, April 20, 1905.**{*EVsw 394:4}*

Katika Mji Mkuu wa Taifa — Nimekuwa nikiandika mengi kuhusu haja ya kuweka juhudi za dhati zaidi huko Washington, D.C.... Washington, mji mkuu wa Marekani, ni mahali hasa ambapo Ukweli huu unapaswa kung'aa na kusonga mbele. **—Letter 132, 1903.**{*EVsw 395:1}*

Mbinu za Kiasili na za Busara kwa Washington — Juhudi madhubuti za uinjilisti lazima zifanyike katika mji mkuu wa taifa.... Nimefurahi kwamba mmekumbatia kazi hii ya uinjilisti huko Washington, na kwamba kuna hamasa kubwa iliyoamshwa. Maelezo kuhusu kazi hiyo yanalingana sana na maono niliyoonyeshwa kile kitakachokuwapo mbeleni. Ninajua, kwa kuwa jambo hili limeonyeshwa kwangu, na kazi hii haipaswi kudhoofishwa kwa kuvurugwa na kuitwa kwa watendakazi sehemu nyingine.....{*EVsw 395:2}*

Kazi ya uinjilisti lazima ifanyike Washington DC, na haipaswi kukatizwa kwa wito kutoka sehemu nyingine. **Mungu** anataka kazi yake katika njia kuu ifanywe kwa njia iliyonyooka.{*EVsw 395:3}*

Mko mahali ambapo Bwana angetaka muwe. Mzee _____ na ninyi hamstahili kubebeshwa mizigo mingi. Washington imepuuzwa vya kutosha. Sasa kazi ya dhati inapaswa kufanywa pale. Bwana atatoa nguvu na neema. Watendakazi wasiruhusu chochote kuwatoa katika kazi hii kwa sababu ya mambo mengi yatakayotaka kuwatatiza na kuvuta umakini. hii ndiyo sababu nimekuwa na shauku kwamba kila kipawa cha watendakazi huko Washington kitumike ili kuendeleza kazi ya Bwana. {*EVsw 395:4}*

Ndugu _____ ametaja baadhi ya watu ambao anaona wanaweza kusaidia kazi ya Washington. Lakini kuwa waangalifu sana kuhusu nani unamwajiri kwa kazi hiyo. Kila kitu lazima kiwe juu ya viwango vya Biblia.....{*EVsw 396:1}*

Katika kazi yetu hatuambiwi twende mlimani kung'aa. Hatutakiwi kufanya maonyesho ya ajabu na ya kushangaza. Ukweli unapaswa kutangazwa katika njia kuu na njia ndogo, kwa mbinu za busara na zenye mantiki. Maisha ya kila mtendakazi, iwapo amefundishwa na Bwana Yesu Kristo, yataonyesha ubora wa maisha Yake. Kazi aliyofanya Kristo duniani ni mfano wetu; mbali na maonyesho, tunapaswa kujiepusha na maonyesho ya kisanii kama Yesu alivyojiepusha. Hisia kali siyo dini, ingawa dini ya kweli huleta mvuto wake mtakatifu, wa kuinua na kutakasa, ikiwasilisha uzima wa kiroho na wokovu. **—Letter 53, 1904.**{*EVsw 396:2*}

Mikutano ya Uinjilisti kwa Eneo la Washington DC — Kuna maeneo mengi kuzunguka Washington yanayohitaji juhudi za kimishenari. Hata ndani ya Washington kuna "ulimwengu mdogo" wa watu wasioongoka, weupe na weusi. Nani anahisi mzigo kwa ajili yao? Na pia kuna miji mingine mingi muhimu ambayo bado haijaonywa. Ninapoona kupuuzwa huku, moyo wangu huumia. Ninaomba usiku na mchana kwamba mzigo huu uwe juu ya wanaume wanaoongoza kazi. Wale walio tayari katika kazi, na wafungue njia kwa wengine wenye nia ya kutenda kazi ya uinjilisti/umishenari..... {*EVsw 396:3*}

Kuna miji muhimu karibu kabisa na Washington—jirani zetu wa karibu, kwa hakika. Ikiwa ndugu na dada zetu watafanya kazi ya uaminifu kwa kila mtu wanaokutana naye, mashamba mapya ya kazi yatafunguliwa karibu nasi. Mzigo wa kutenda kazi kwa ajili ya roho utakuja kwa wengi walioko hapa, nao watatamani kushiriki kikamilifu katika kutangaza Ukweli.{*EVsw 396:4*}

Tunaomba wale walioko Takoma Park wawe washirika wa **Mungu** katika kupeperusha bendera ya Ukweli katika maeneo ambayo bado hayajafikika. Sehemu ya michango mikubwa inayohitajika itumike kuwawezesha watendakazi katika miji iliyo karibu na Washington. Kazi ya uaminifu ya nyumba kwa nyumba ifanywe. Nafsi zinapotea nje ya safina ya wokovu. Wacha bendera ya Ukweli iinuliwe na washiriki wa kanisa katika majirani zao. Wachungaji wapige mahema yao, wahubiri kwa nguvu, kisha wahamie eneo jingine kufanya kazi ile ile. —**Letter 94a, 1909.**{*EVsw 397:1*}

Kutangaza Ujumbe Ulio Dhahiri — Nawaita waumini walioko Washington kusaidia kazi ya Bwana, kuja kumsaidia Bwana dhidi ya nguvu za giza. Kazi ya kibinafsi inahitajika katika jiji hili na vitongoji vyake. Itengenezeni njia ya Mfalme. Inueni bendera juu zaidi. Kazi ya uinjilisti inapaswa kufanywa Washington, Baltimore, na miji mingine mikubwa ya Kusini na Mashariki. Hebu Kazi ya kufundisha na kuponya na iende pamoja. Wachungaji na wamishenari wa afya wavae silaha zote za **Mungu** na waende kutangaza ujumbe wa Injili. Ujumbe wenye msimamo madhubuti unapaswa kutangazwa Washington. Tarumbeta lazima ipigwe kwa sauti ya uhakika. **—Letter 304, 1908.**{*EVsw 397:2*}

Nashville, St. Louis, New Orleans — Juhudi zote ziwezekanazo zinapaswa kufanywa kuendeleza kazi ya **Mungu**. Hivi karibuni hali zitajitokeza zitakazofanya iwe vigumu zaidi kuwasilisha Ukweli kwa wale tuliowafikia sasa. Jitihada za dhati zinapaswa kufanywa Washington, Boston, Nashville, St. Louis, New Orleans, na miji mingine mikubwa. Kazi ya kina itakamilika wanapoibuka wanaume na wanawake waaminifu, na kusimama katika nafasi zao. Kuna wito kwa mamia ya vijana wa kiume na kike, kuelimishwa kwaajili ya Huduma **—Manuscript 21, 1908.**{*EVsw 397:3*}

Nashville Kitovu — Nashville imeonyeshwa kwangu kama kitovu chenye fursa bora zaidi ya kufanya kazi ya jumla kwa watu wa kila tabaka katika Majimbo ya Kusini. Katika Nashville na maeneo ya karibu, kuna taasisi za elimu zilizoanzishwa ambazo watu wetu wanapaswa kuziheshimu. Mvuto wake umesaidia kufanya kazi nyingi za kiinjilisti kufanyika kwa mafanikio kutoka kituo hicho. **—Letter 262, 1903.**{*EVsw 398:1*}

Memphis, New Orleans, na Miji Mingine ya Kusini

Memphis na Miji ya Kusini—Bwana alinipa ujumbe kwa Ndugu _____, akimwagiza aanze kazi huko Memphis, Tennessee .... Naye alitii neno la Bwana, na ameripoti mafanikio makubwa katika kazi yake huko Memphis. {Evsw 398:2}

Memphis: Kusubiri kwa Muda Mrefu — Nimeonyeshwa kuwa katika miji kama Memphis kuna kazi kubwa ya kufanya. Muda umepita sana bila juhudi za kufaa kufanywa ili kupeleka Ukweli kwa watu wa mji huu. Kuna watu wengi huko Memphis ambao hawajasikia ujumbe wa Kweli kwa wakati huu. Wahubiri na wamishenari wa afya wanapaswa kufanya kazi kwa bidii ili kuwaleta watu kwenye maarifa ya Kweli. **—Letter 218, 1906.**{*EVsw 398:3*}

Nimeagizwa kuwaambia watu wetu katika miji yote ya Kusini, Kila kitu na kifanyike chini ya uongozi wa Bwana. Kazi inakaribia kufungwa. Tumekaribia mwisho kuliko tulipoamini kwa mara ya kwanza.—Barua ya 6, 1909.{Evsw 398:3}

New Orleans: Mlango wa Kusini — New Orleans ni mlango mkuu wa kuingia Kusini mwa nchi ya Marekani, na kazi nzuri imefanyika hapo tayari, lakini bado kuna mengi ya kufanya. Bendera ya Ukweli haijainuliwa kama inavyopaswa. Hali ya kiroho ya watu wengi ni ya chini, na kuna haja ya kazi ya bidii na ya unyenyekevu, kazi ya moyo wa mtu mmoja kwa moyo wa mtu mwingine. **—Letter 30, 1903.{Evsw 398:4}**

New Orleans, Memphis, St. Louis—Kuna kazi kubwa ya kufanywa kwenye miji hii, na tuna muda mfupi tu wa kuifanya. Kuna miji Kusini mwa Marekani—New Orleans, Memphis, St. Louis—ambayo kazi imefanywa kwa udogo tu, na kuna mingine ambayo haijaingiliwa/haijafikiwa bado. Katika sehemu hizi kiwango cha Ukweli kinapaswa kuinuliwa. Kwa nguvu na uwezo tunapaswa kupeleka Ukweli kwa watu humo.—Manuscript 56, 1904.

Uinjilisti kwa Miji ya New Orleans na Kusini—Kuna kazi kubwa ya kufanywa, na tuna muda mfupi tu wa kuifanya. Kuna miji Kusini—New Orleans, Memphis, St. Louis—ambayo kazi ndogo tu ndiyo imefanywa humo; na kuna mingine ambayo haijaingizwa. Katika sehemu hizi kiwango cha Ukweli lazima kiinuliwe. Kwa nguvu na uwezo tunapaswa kupeleka Ukweli kwa watu....{*EVsw 398:5*}

New Orleans inapaswa kufanyiwa kazi. Kwa wakati unaofaa wa mwaka juhudi za umma zinapaswa kufanywa huko. Mikutano ya kambi itafanyika katika sehemu nyingi, na kazi ya uinjilisti itafanywa baada ya mkutano wa kambi kumalizika. Hivyo miganda ya mavuno itakusanywa.{*EVsw 399:1*}

Miji Mikubwa ya Kusini: Hakuna Mji wa Kupitwa — Katika miji mikubwa ya Kusini, bado kuna kazi kubwa sana ambayo haijafanywa. Miji mingi haijaguswa hata kidogo. Katika baadhi ya miji, mikutano michache imefanywa; katika mingine, hakuna juhudi zozote zilizowahi kufanyika. Watu wengi wameachwa bila onyo. Je, **Mungu** hatatuita kuwajibika kwa kupuuza kwa namna hii kazi ambayo Ameweka mbele yetu?

Katika jiji baada ya jiji kazi haijafanywa. Kila mji mkubwa unahitaji misionari. Katika baadhi ya miji bado kuna maelfu ya watu ambao hawajasikia ujumbe wa malaika wa tatu. Na katika miji mingine hakuna hata mtu mmoja anayeielewa Sabato ya Biblia. Hakuna mji unaopaswa kupitwa. **—Letter 46, 1902.**

Atlanta, Georgia — Atlanta ni mji muhimu wa kufanya kazi. Nimeonyeshwa kuwa inapaswa kuwa kituo cha kazi ya kimishenari, na kazi ya mafunzo. Inapaswa kuwa mahali pa kupokea na kufundisha watendakazi wanaoweza kwenda sehemu mbalimbali za Kusini. **—Letter 145, 1902.**

Kwa Jumla: Uwepo wa Wenye Ukweli Katika Kila Mji — **Mungu** anatamani kuona mwangaza wa ujumbe wa mwisho wa rehema ukiangaza kutoka kila mji. Katika miji yote mikubwa na midogo, kazi ya uinjilisti wa kweli inapaswa kufanywa. Watu wa kila tabaka, kila rangi, na kila hali wanahitaji kusikia wito wa Injili. — **Review and Herald, November 17, 1904.**

Miji ya Majimbo ya Kati

Mahitaji ya Miji Mikubwa, Ikiwemo Detroit

Huko New York, Detroit, na miji mingine mingi mikubwa, kazi ndogo sana imefanyika. Miji ya Kusini, ingawa imekuwa ikiletwa mbele ya watu wetu kupitia ushuhuda wa Roho wa **Mungu**, imepuuzwa. Ingawa sitazuia mkono wa anayejitahidi kufanya kazi katika nchi za mbali, ningependa watu wetu waelewe kuwa kuna kazi ya kufanya katika eneo la nyumbani. **—Letter 43, 1903.{*EVsw 402:1*}**

Cleveland na Cincinnati

Bwana ana roho nyingi za thamani huko Cleveland, Cincinnati, na miji mingine, ambazo zinapaswa kufikiwa na kweli maalum kwa wakati huu. —**Manuscript 19a, 1890.{*EVsw 402:2*}**

Onyo Kuhusu Chicago Kutoka Kituo cha Kazi Vijijini

Kwa sasa, baadhi ya watu watalazimika kufanya kazi huko Chicago; lakini hawa wanapaswa kujiandaa kuanzisha vituo vya kazi katika maeneo ya vijijini, ambako kazi ya kuwafikia watu wa mji huo itaendeshwa. Bwana anataka watu Wake wawe macho, wakitafuta maeneo ya kawaida, yasiyo ya gharama kubwa, yawe vituo vya kazi yao. Na mara kwa mara, maeneo makubwa zaidi yatajitokeza mbele yao, ambayo watawaweza kuyapata kwa bei ya kushangaza kuwa nafuu. **—Medical Ministry, 305, 306 (1906).**{*EVsw 402:3*}**Kazi Thabiti Huko Denver**

Kama jambo hili linavyoonyeshwa mbele yangu, naona kuwa kuna haja ya kazi madhubuti kufanyika huko Denver. Zamani, mambo mengi yamekuwa kikwazo kwa ustawi wa kazi huko, na athari hiyo mbaya bado haijaondolewa kikamilifu.{*EVsw 402:4*}

Kuna kundi kubwa la watu weusi huko Denver. Na juhudi maalum zifanywe kwa ajili yao, na kwa ushirikiano kati ya waumini weupe na weusi wa kanisa. Roho ya kimishenari iwashwe mioyoni. Na kazi ya bidii ifanywe kwa ajili ya wale wasiojua Kweli. —**Letter 84, 1901.**{*EVsw 403:1*}

Miji ya Magharibi

Miji ya California

Kuna kazi ya kufanywa huko California, kazi ambayo imepuuzwa ajabu. Hebu kazi hii isicheleweshwe tena. Kama milango inafunguliwa kwa uwasilishaji wa Ukweli, hebu tuwe tayari kuingia. Kazi fulani imefanywa katika jiji kubwa la San Francisco, lakini tunapolichunguza eneo hili tunaona wazi kuwa ni mwanzo tu uliofanywa. Haraka iwezekanavyo, juhudi zilizopangwa vizuri zinapaswa kupelekwa katika sehemu tofauti za jiji hili na pia huko Oakland. Uovu wa San Francisco haujatambulikana. Kazi yetu katika jiji hili lazima ipanuke na kuongezeka. Ndani yake **Mungu** huona roho nyingi zitaokolewa. —**Testimonies For The Church 7:110 (1902).**{*EVsw 403:2*}

Je, hatupaswi kufanya yote tuwezayo kuanzisha kazi katika miji mikuu ya San Francisco na Oakland, na pia katika miji mingine yote ya California? Maelfu kwa maelfu wanaoishi katika miji iliyo karibu nasi wanahitaji msaada kwa njia mbalimbali. Wahubiri wa Injili na watambue kuwa Bwana Yesu Kristo alisema kwa wanafunzi Wake, "*Ninyi ni nuru ya ulimwengu*."—**Manuscript 79, 1900.**{*EVsw 403:3*}

Mikutano ya Makambi Katika Miji Mikubwa ya Magharibi

Mikutano ya hema iliyoandaliwa vizuri inapaswa kufanyika katika miji mikubwa, kama vile San Francisco; kwa maana si muda mrefu miji hii itapigwa na hukumu za **Mungu**. [Kumbuka: Imeandikwa mwaka 1902.] San Francisco na Oakland zinakuwa kama Sodoma na Gomora, na Bwana atazitembelea kwa ghadhabu. —**Manuscript 114, 1902.**{*EVsw 403:4*}

Kazi Itafupishwa

San Francisco imepata hukumu nzito, lakini Oakland hadi sasa imesamehewa kwa rehema. Wakati utafika ambapo kazi yetu katika maeneo haya itakatishwa/kufupishwa, kwa hiyo ni muhimu sana tufanye juhudi za dhati sasa ili kuwapelekea wakaaji wake ujumbe wa Bwana kwao. —**Manuscript 25, 1908.**{*EVsw 404:1*}

Onyo kwa Watendakazi wa San Francisco

Kazi inayoendelea huko San Francisco ni kazi njema. Lakini katika kila hatua lazima kuwe na uangalifu na sala; kwa maana mambo mengi yatatokea kuwapotosha na kuwatatiza watendakazi. Ndugu zangu, neno limepewa kwenu: "Kesheni na kuomba." Kesheni msije mkaizuia kazi ya **Mungu**, na kutoa taswira ambayo inadhuru kweli. Pambeni maungamo yenu kwa mazungumzo ya uaminifu. Leeni neema ya Roho Mtakatifu, la sivyo mtakuwa vizuizi katika kazi ya **Mungu**. Tengenezeni njia nyoofu kwa miguu yenu, ili vilema wasigeuzwe kutoka njiani. —**Manuscript 105, 1902.**{*EVsw 404:2*}

Vitongoji vya Bay City; Oakland

Nafsi yangu imejaa majuto—siwezi kueleza kwa njia nyingine—kuwa maeneo kama haya [Petaluma] yamepuuzwa. Mara chache sana mhubiri huja kuzungumza na waumini, lakini hakuna jitihada zimefanyika kuwawekea watu kweli. Kwa nini Petaluma imepuuzwa ni jambo lisiloeleweka kwangu. Iko karibu sana na San Francisco, lakini huenda ikawa mbali kama Afrika, kwa kuzingatia ukosefu wa jitihada ya kuhubiriKweli humo.{*EVsw 404:3*}

Kazi inapaswa kufanyika ndani na kandokando ya San Francisco na Oakland. Miji ya jirani inapaswa kufikiwa. Ee, naona sana haja ya wahubiri wetu kupokea roho ya mwito wa sauti kuu kabla haijawa kuchelewa kufanya kazi ya uongofu wa roho. —**Letter 113, 1902.**{*EVsw 404:4}*

Uzoefu na Mikutano ya Hadharani Katika Miji ya Mapumziko

Kwa miezi kadhaa tumekuwa tukipanga kufanya mikutano ya uwanjani karibu na St. Helena, Calistoga, na maeneo mengine ya Bonde la Napa. Ya kwanza ilifanyika Jumapili, Juni 7, katika Hot Springs Park, Calistoga. Konferensi ilitukopesha viti vya kukunjwa. Washiriki wa kanisa la Calistoga walikuwa na hamu ya kufikisha kweli kwa wale ambao hawajaisikia, na walifanya maandalizi ya kina kwa ajili ya mkutano. Tulikuwa na hakika kwamba mikutano ya wazi ingewafikia wale ambao wasingeenda kanisani. Na kweli, imethibitika hivyo.{*EVsw 405:1}*

Ingawa siku hiyo ilikuwa na joto kali, watu wengi walihudhuria. Bwana alinipa uhuru mwingi wa kuzungumza. Watu walionekana kufurahia mkutano sana, na tangazo lilitolewa kuwa mikutano itafanyika mahali pale pale siku ya Sabato na Jumapili inayofuata. Watu wetu walikusanyika mapema Jumapili asubuhi, na wakatumia siku hiyo wote pamoja uwanjani. Idadi ya waliohudhuria Jumapili ya pili ilikuwa kubwa kuliko ya kwanza. {*EVsw 405:2}*

Tunatarajia kuendelea na mikutano hii ya wazi. Ninaamini kuwa kupitia hiyo mema mengi yatafanyika. Mkutano unaofuata unatarajiwa kufanyika karibu na St. Helena, ikiwa mahali panapofaa patapatikana.{*EVsw 405:3}*

Tunatamani kufanya yote tuwezayo kuwaonya wale waliotuzunguka kuhusu kuja kwa Mwokozi kunakokaribia. Moyo wangu huvutwa kwa wale wasiojua Kweli ya wakati huu. —**The Review and Herald, July 14, 1903.**{*EVsw 405:4}*

Huko California ya Kusini

Kuna kazi ya kufanya huko Los Angeles. Katika California ya Kusini na maeneo mengine mengi kuna fursa zenye matumaini kwa kazi ya Injili kwa kushirikiana na vituo vya afya. Wahubiri wetu na wachapishaji wanapaswa kuwa eneo hilo, wakitafuta fursa ya kuwasilisha ujumbe, na kufanya mikutano kadri watakavyopata nafasi... Na waseme Neno la **Mungu** kwa uwazi na nguvu, ili wale walio na masikio ya kusikia, wapate kusikia kweli. Wahubiri wanapaswa kutafuta maeneo mbalimbali katika California ya Kusini ili kuweka Injili ya kweli ya wakati huu mbele ya wale wasioijua. —**Manuscript 105, 1902.**{*EVsw 405:5}*

Los Angeles

Nimepewa nuru maalum kuhusu tabia na ukubwa wa kazi inayopaswa kufanyika huko Los Angeles. Mara kadhaa ujumbe umetolewa kuhusu wajibu ulioko juu yetu wa kuutangaza ujumbe wa malaika wa tatu kwa nguvu katika mji huo. —**The Review and Herald, March 2, 1905.**{*EVsw 406:1}*

Redlands na Riverside

Kuna kazi muhimu ya kufanya huko Redlands na Riverside. Makanisa katika maeneo haya yanapaswa kuongezeka. Na kazi iendelee mbele. —**Letter 193, 1905.**{*EVsw 406:2}*

Ujumbe Katika Miji Mikubwa ya Magharibi

Itakuwa kosa kujenga au kununua majengo makubwa katika miji ya California ya Kusini. Wale wanaoona kana kwamba kuna faida kubwa katika kufanya hivyo hawana uelewa.{*EVsw 406:3}*

Kuna kazi kubwa ya kufanya ya kuupaza ujumbe wa Injili kwa wakati huu katika miji hii mikubwa, lakini kutengeneza majengo makubwa kwa kazi fulani inayoonekana kuwa ya ajabu imekuwa kosa. Bwana anataka watu waenende kwa unyenyekevu pamoja Naye. Ujumbe wa onyo unapaswa kupazwa katika miji mikubwa yenye uovu. —**Manuscript 30, 1903.**{*EVsw 406:4}*

SEHEMU YA 12—KUITANGAZA HABARI NJEMA KATIKA MABARA MENGINE

Kupaza Sauti ya Ujumbe Ulaya

Dunia Yote Itaangaziwa— Kwa wakati huu kunapaswa kuwa na wawakilishi wa Ukweli wa sasa katika kila mji na sehemu za mbali za dunia. Dunia yote itaangazwa kwa utukufu wa Kweli ya **Mungu**. Nuru inapaswa kuangazia nchi zote na watu wote. Na ni kutoka kwa wale ambao wameipokea nuru hiyo ndiyo iangaze.{*EVsw 407:1*}

Nchi fulani zina faida zinazoziashiria kama vituo vya elimu na zenye kuvutia. Katika mataifa yanayozungumza Kiingereza na mataifa ya Kiprotestanti ya Ulaya ni rahisi kwa kulinganisha kupata ufikiaji wa watu, na kuna faida nyingi za kuanzisha taasisi na kuendeleza kazi yetu. Katika nchi nyinginezo, kama vile India na China, watendakazi lazima wapitie kozi ndefu ya elimu kabla ya watu hao kuwaelewa, au wao kuwaelewa watu. Na katika kila hatua kuna matatizo makubwa ya kukutana katika kazi. Huko Amerika, Australia, Uingereza, na nchi zingine za Ulaya, vingi vya vizuizi hivi havipo. Marekani ina taasisi nyingi za kutoa tabia kwa kazi hiyo. Vifaa kama hivyo vinapaswa kutayarishwa kwa ajili ya Uingereza, Australia, Ujerumani, na Skandinavia, na nchi nyingine za mabara mengine kadiri kazi inavyoendelea. Katika nchi hizi Bwana anao watenda kazi hodari, watenda kazi wenye uzoefu. Haya yanaweza kuongoza katika uanzishwaji wa taasisi, mafunzo ya watendakazi, na kuendeleza kazi katika safu zake tofauti. Mwenyezi **Mungu** amepanga wawekewe nyenzo, na miundombinu na mali. Taasisi zilizoanzishwa zingetoa sifa ya kazi katika nchi hizi, na zingetoa fursa kwa ajili ya mafunzo ya watendakazi kwa mataifa ya kipagani yaliyo gizani. Kwa njia hii ufanisi wa wafanyikazi wetu wenye uzoefu ungeongezeka mara mia.....{*EVsw 407:2*}

Ninaumia kufikiria kwamba mipango kazi zaidi havitolewi kwa ajili ya kazi hiyo kote Ulaya. Nina maumivu makali ya moyo ninapofikiria kazi katika Uswisi, Ujerumani, Norway, na Uswidi. Ambapo kuna mtu mmoja au wawili wanaojitahidi kuendeleza matawi tofauti ya asili, kunapaswa kuwa na mamia kazini. **—Testimonies for the Church 6:24-26 (1900).**{*EVsw 408:1*}

Kazi Kubwa Barani Ulaya— Kuna kazi kubwa ya kufanywa barani Ulaya. Mbingu yote ina shauku si tu kwa nchi zilizo karibu zinazohitaji msaada wetu, bali pia kwa nchi zilizo mbali. Wakazi wote wa mbinguni wamo katika huduma hai, wakilitumikia ulimwengu uliodidimia. Wanajali kwa moyo wote juu ya wokovu wa wanadamu, wakaaji waliopotoka wa dunia hii. —**Manuscript 65, 1900.**{*EVsw 408:2*}

Kazi kubwa imekabidhiwa kwa wale wanaowasilisha Kweli barani Ulaya... Kuna Ufaransa na Ujerumani, pamoja na miji yao mikuu na idadi kubwa ya watu. Kuna Italia, Uhispania, na Ureno, baada ya karne nyingi za giza... zimefunguliwa kwa Neno la **Mungu**—zimefunguliwa kupokea ujumbe wa mwisho wa onyo kwa ulimwengu. Kuna Uholanzi, Austria, Rumania, Uturuki, Ugiriki, na Urusi—maskani ya mamilioni kwa mamilioni ya roho, ambazo ni za thamani machoni pa **Mungu** kama roho zetu, na ambazo hazijui lolote kuhusu zile Kweli maalum za wakati huu.....{*EVsw 408:3*}

Kazi njema tayari imefanyika katika nchi hizi. Wapo waliopokea kweli, wakiwa wametawanyika kama wabeba nuru katika karibu kila nchi... Lakini ni kazi ndogo sana iliyofanyika ikilinganishwa na kazi kubwa iliyo mbele yetu! Malaika wa **Mungu** wanagusa fikra za watu, na kuwaandaa kupokea onyo. Wamishenari wanahitajika katika mashamba ambayo bado hayajaguswa. Mashamba mapya yanaendelea kufunguka kila mara. Kweli lazima itafsiriwe kwa lugha mbalimbali ili kila taifa lipate fursa ya kufurahia mvuto wake safi na wa kuhuisha. **—Life Sketches of Ellen G. White, 304, 305 (1915).**{*EVsw 408:4*}

Mwito wa Kufanya Kazi Kuu, Imara— Muda umefika wa mengi kutimizwa huko Ulaya. Kazi kubwa, kama ambayo imefanyika Marekani, inaweza kufanywa huko Ulaya. Hebu vituo vya afya na maisha bora vianzishwe, hebu migahawa yenye kuleta afya ianzishwe. Hebu nuru ya ukweli wa sasa uangaze kutoka katika mitambo ya uchapaji. Hebu kazi ya kutafsiri vitabu vyetu isonge mbele. Nimeoneshwa kuwa katika nchi za Ulaya taa zitawashwa katika maeneo mengi. {*EVsw 409:1*}

Kuna maeneo mengi ambapo kazi ya Bwana haijaonekana inavyostahili. Msaada unahitajika nchini Italia, Ufaransa, Scotland, na katika nchi nyingine nyingi. Kazi kubwa inapaswa kufanywa katika maeneo haya. Watendakazi wanahitajika. Kuna vipawa miongoni mwa watu wa **Mungu** huko Ulaya, na Bwana anatamani vipawa hivi vitumike katika kuanzisha kote katika Uingereza na bara hili, vituo ambavyo kutoka humo nuru ya Ukweli Wake inaweza kuangaza. {*EVsw 409:2*}

Kuna kazi ya kufanywa huko Scandinavia. **Mungu** yuko tayari kufanya kazi kupitia kwa waumini wa Scandinavia kama vile kwa waumini wa Amerika. {*EVsw 409:3*}

Ndugu zangu, fungamaneni na Bwana **Mungu** wa majeshi. Mruhusu awe hofu yako, Naye umruhusu awe utisho wako. Wakati umefika wa kazi Yake kupanuliwa. Nyakati za taabu ziko mbele yetu, lakini ikiwa

tutasimama pamoja katika ushirika wa Kikristo, bila kuwa na mtu anayepambana kwa ajili ya kupata ukuu, **Mungu** atafanya kazi kwa nguvu kwa ajili yetu. **—Testimonies for the Church 8:38 (1904).** {*EVsw 409:4*}

Hitaji la Juhudi Kubwa Zaidi Ulaya— Kazi hii itahitaji jitihada kubwa zaidi kufanyika barani Ulaya kuliko Marekani kwa sababu ya umaskini wa watu. Tena, kuna wingi wa wahubiri. Tunafikiria maneno ya mtume: "Watajikusanyia walimu kwa tamaa ya kusikia maneno matamu." Mara tu ukweli unapowasilishwa mahali, wachungaji wa makanisa mbalimbali hutaharuki na mara moja hutuma wahubiri wengine kuja kufanya mikutano ya uamsho. Hapa huitwa "mikutano ya maungano." Mikutano hiyo huendelea kwa wiki kadhaa, na si chini ya wahubiri kumi huhusika; vipaji vya hali ya juu huandaliwa, na onyo na vitisho humiminwa kutoka kwa makanisa dhidi ya watu wa Sabato ya siku ya saba, ambao huchukuliwa kuwa sawa na Wamormoni, na ambao wanasemekana kuvunja makanisa na kusababisha migawanyiko.{*EVsw 410:1*}

Ni vigumu sana kuwafikia watu. Njia pekee ambayo tumeona ina mafanikio ni kwa kufanya masomo ya Biblia, na kwa njia hii shauku huanza kwa mtu mmoja, wawili au watatu; kisha hawa huwafikia wengine na kuwajaribu kuwavutia, na hivyo kazi huendelea taratibu kama ilivyokuwa Lausanne; lakini watu ishirini wameikubali kweli huko, na hiyo si faida pekee iliyopatikana, kwa kuwa vijana wanaojiandaa kuwa watendakazi wamepata mafunzo mazuri na elimu itakayowawezesha kuwa na mafanikio zaidi katika kazi ya **Mungu**. **—Letter 44, 1886.**{*EVsw 410:2*}

Kuwafikia Wafuasi wa Makanisa ya Nchi za Ulaya— Kutokana na nuru niliyopewa kuhusu watu wa sehemu hii ya nchi, na huenda ni barani Ulaya yote, kuna hatari ya kuchochea roho ya upinzani wanapowasilishiwa kweli. Kuna upungufu wa maelewano kati ya kweli ya sasa na mafundisho ya makanisa ambayo watu wengi wamezaliwa na kulelewa ndani yake; na wamejaa maonevu, na wako chini ya udhibiti mkali wa wachungaji wao kiasi kwamba mara nyingi hawathubutu hata kuja kusikiliza kweli ikihubiriwa. Swali sasa linajitokeza, Je, watu hawa wanawezaje kufikiwa? Je, kazi kuu ya ujumbe wa malaika wa tatu itafanikishwaje? Kazi hii inapaswa kufanywa kwa kiwango kikubwa kwa njia ya juhudi za mtu binafsi, kwa kuwatembelea watu majumbani mwao. **—Historical Sketches of the Foreign Missions of the Seventh-day Adventists, 149, 150 (1886).**{*EVsw 409:3*}

Mjumbe wa Kimya— "Lakini," asema mtu, "vipi kama hatuwezi kuruhusiwa kuingia nyumbani kwa watu; na tukiruhusiwa, vipi kama wanainuka dhidi ya kweli tunayowasilisha? Je, si basi tunapaswa kuacha kufanya juhudi zaidi kwa ajili yao?" Hapana kabisa. Hata wakikufungia mlango usoni, usiondoke kwa hasira, wala usikate tamaa ya kuwaokoa. Mwombe **Mungu** kwa imani akupe njia ya kuwafikia roho hizo hizo. Usiache juhudi zako, bali soma na kupanga hadi upate njia nyingine ya kuwafikia. Ikiwa huwezi kufanikiwa kwa kuwatembelea binafsi, jaribu kuwatumia "mjumbe wa kimya" wa kweli. Kuna kiburi kikubwa cha maoni ndani ya moyo wa mwanadamu kiasi kwamba machapisho yetu mara nyingi huingia mahali ambapo mhubiri hai hawezi kufika.{*EVsw 411:1*}

Nimeonyeshwa jinsi maandiko juu ya kweli ya sasa yanavyotendewa na watu wengi barani Ulaya na nchi nyingine. Mtu hupokea kijitabu au gazeti. Anasoma kidogo ndani yake, anakutana na jambo lisilokubaliana na mitazamo yake ya awali, kisha anakitupa pembeni. Lakini maneno machache aliyoyasoma hayasahauliki. Ingawa hayapendezi, hubaki akilini hadi shauku ya kusoma zaidi inapozaliwa. Tena huichukua ile karatasi; tena anakutana na kitu kisichokubaliana na mazoea na maoni aliyoshikilia kwa muda mrefu, kisha anakitupa kwa hasira. Lakini mjumbe aliyekataliwa hasemi kitu cha kuongeza upinzani au kuchochea hasira; na pale hasira yake inapopungua, na karatasi ile inalewa tena, huwasilisha ujumbe ule ule mwepesi na wa moja kwa moja, na sasa anapata vito vya thamani ndani yake. Malaika wa **Mungu** wako karibu kumgusa moyo na Neno lisilonena; na ingawa ni kwa kusita, hatimaye anakubali, na nuru hutawala moyo wake. Wale wanaobadilika kwa namna hii mara nyingi huwa waumini imara sana; na uzoefu wao huwafundisha kufanya kazi kwa uvumilivu kwa ajili ya wengine. **—Historical Sketches of the Foreign Missions of the Seventh-day Adventists, uk. 150 (1886).**{*EVsw 411:2*}

Mikutano ya Hadharani na ya Hemani— Niliombwa kusema kuhusu kufanyika kwa mikutano ndani ya hema barani Ulaya. Niliwaambia, kulingana na nuru Bwana aliyonipa, mahema yanaweza kutumika kwa faida kubwa katika maeneo fulani, na yakisimamiwa vizuri yataleta manufaa makubwa. Wakati huo sikuwa najua sababu ya kuniita kuhusu jambo hili, lakini nikagundua kuwa ni kwa sababu Ndugu _____ hapo awali alikuwa amesema vibaya kuhusu mahema kuwa bora kwa ajili ya mikutano ya ibada.{*EVsw 412:1*}

Kisha nikatoa pingamizi zangu kuhusu mikutano ya hadharani. Hiyo huwadhofisha wahubiri wetu kwa kuwa inawachosha sauti. Sauti hulazimika kupandishwa kwa nguvu isiyo ya kawaida, na huumizwa sana kwa njia hii ya kazi. Pingamizi jingine ni kuwa nidhamu na mpangilio haviwezi kudumishwa; kazi ya namna hiyo

haichochei tabia ya kujifunza kwa bidii Maandiko ili kuleta kutoka katika ghala la **Mungu** mambo mapya na ya kale. —**Letter 2, 1885.**{*EVsw 412:2}*

Mungu Atatenda kwa Nguvu— Kuna kazi kubwa ya kufanywa barani Ulaya. Huenda ikaonekana kusonga polepole na kwa ugumu mwanzoni; lakini **Mungu** atafanya kazi kwa nguvu kupitia kwenu ikiwa tu mtajitoa kikamilifu Kwake. Mara nyingi mtalazimika kutembea kwa imani, si kwa hisia. —**Historical Sketches of the Foreign Missions of the Seventh-day Adventists, uk. 128-129 (1886).** {*EVsw 412:3}*

Mpaka Miisho ya Dunia— Nuru ya Ukweli inapaswa kuangaza hadi miisho ya dunia. Nuru kubwa na kubwa zaidi inaangaza kwa uangavu wa Bwana kutoka katika uso wa Mkombozi juu ya wawakilishi Wake, ili ipate kutawanywa kupita katika giza la ulimwengu wa kishenzi. Kama watenda kazi pamoja Naye, hebu na tuombe kwa ajili ya utakaso wa Roho Wake, ili tuweze kuangaza zaidi na zaidi…...{*EVsw 413:1}*

Jitihada zetu hazipaswi kuwekewa mipaka katika maeneo machache ambapo nuru imekuwa nyingi kiasi kwamba haifurahiwi. Ujumbe wa injili unapaswa kutangazwa kwa mataifa yote na kabila na lugha na jamaa. **—Testimonies For The Church 8:40 (1904).**{*EVsw 413:2}*

Kuizunguka Dunia— **Mungu** amewawezesha watu Wake kuangaza ulimwengu. Amewakabidhi wanadamu uwezo unaowawezesha kutekeleza kazi itakayolizunguka dunia. Vituo vya afya, shule, ofisi za uchapishaji, na huduma zinazofanana nazo zinapaswa kuanzishwa katika sehemu zote za dunia.{*EVsw 413:3}*

Lakini kazi hii bado haijakamilika. Katika nchi za kigeni, miradi mingi inayohitaji rasilimali bado inapaswa kuanzishwa na kuendelezwa. Kuanzishwa kwa mikahawa ya afya, kuanzishwa kwa sanitariamu kwa ajili ya wagonjwa na wanaoteseka, ni muhimu sana Ujerumani kama ilivyo Marekani. Kila mmoja na atumie uwezo wake, akijisifia katika Bwana, na kuwabariki wengine kwa matendo mema.{*EVsw 413:4}*

Kristo anashirikiana na wale wanaojitolea kwa moyo kufanya kazi ya umishenari wa tiba. Wanaume na wanawake wanaofanya kazi bila ubinafsi kuanzisha sanitariamu na vyumba vya tiba katika nchi nyingi watapokea thawabu tele. Wale watakaotembelea taasisi hizo watapata manufaa ya mwili, akili, na roho. Waliochoka watapumzika, wagonjwa watapona, na waliolemewa na mizigo ya dhambi watapumuliwa. Katika nchi za mbali sifa na shukrani zitasikika kutoka kwa wale ambao mioyo yao imegeuka kutoka kwa dhambi kwenda kwa haki. Kwa nyimbo zao za sifa zenye shukrani, ushuhuda utatolewa utakaowavuta roho nyingine kwenye Kweli. **—Letter 121, 1902.**{*EVsw 413:5}*

Uingereza na Miji Yake

Wataonywa Vipi?

Hapa kuna miji mikubwa ya Uingereza na bara la Ulaya iliyojaa mamilioni ya wakazi ambao bado hawajasikia ujumbe wa mwisho wa onyo. Je, watu hawa wataonywa vipi? Kama watu wa **Mungu** wangeonyesha imani, **Mungu** angefanya kazi kwa namna ya ajabu ili kutimiza kazi hii. Sikiliza maneno ya Kristo: **"Mathayo 18:19**

"*Tena nawaambia, ya kwamba wawili wenu watakapopatana duniani katika jambo lo lote watakaloliomba, watafanyiwa na Baba yangu aliye mbinguni*." Ahadi ya thamani! Je, tunaamini? Matokeo ya ajabu yangedhihirika kama sala za pamoja za kundi hili zingeelekezwa kwa **Mungu** kwa imani hai! Yesu yuko tayari kupokea maombi haya na kuyaonyesha kwa Baba Yake, akisema, "Ninawajua hawa kwa majina yao. Tuma majibu kwa maombi yao; kwa maana nimeliandika jina lao kwenye viganja vya mikono Yangu." — **Historical Sketches of the Foreign Missions of the Seventh-day Adventists, uk. 152 (1886).**{*EVsw 414:1}*

Kuwasilisha Ukweli Huko London

Kanisa linahitaji bidii, na hekima ya kuiongoza bidii hiyo. Mmefanya kazi ya kuwaokoa roho kwa namna ya uvuguvugu mno. Kama mnataka kuona kazi ikifanyika London na miji ya jirani, ni lazima muwe na nguvu iliyoungana na isiyozuilika; sukumeni vita hadi langoni, na simikeni bendera kwa uthabiti, kana kwamba mnamaanisha kuwa ukweli lazima ushinde. Hofu na tahadhari mliyoonyesha imekuwa ya kutokuwa na imani; hamkutarajia matokeo makubwa.....{*EVsw 414:2}*

Kwamba mambo yanakwenda polepole Uingereza si sababu ya kazi kuu ya kimishenari pia kwenda polepole ili kukabiliana na mazoea na desturi za watu kwa hofu ya kuwashangaza. Wanahitaji kushangazwa

zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali. Kazi ya Bwana inahitaji haraka; roho zinapotea bila maarifa ya Ukweli.....{*EVsw 415:1}*

Tahadhari inapaswa kuchukuliwa; lakini ingawa baadhi ya watendakazi wanakuwa waangalifu, na hufanya mambo polepole kwa busara, ikiwa hawatashirikiana katika kazi hiyo na wale wanaotambua umuhimu wa kuwa wakakamavu, mengi yataharibika, nafasi nyingi zitapotea, na matendo ya wazi ya uongozi wa **Mungu** hayatatambuliwa. —**Letter 31, 1892.**{*EVsw 415:2}*

Kazi Kuu ya Kufanywa Uingereza

Kuna kazi kubwa ya kufanywa Uingereza. Mwangaza unaotoka London unapaswa kuangaza kwa miale angavu, tofauti hadi maeneo ya nje. **Mungu** ameigusa Uingereza, lakini ulimwengu huu unaozungumza Kiingereza umepuuzwa vya kutisha sana. Uingereza imehitaji watendakazi wengi zaidi na njia nyingi zaidi. London imeguswa kwa shida. Moyo wangu unaguswa sana huku hali katika jiji hilo kubwa inavyoonyeshwa mbele yangu. Ninaumia kufikiria kwamba mipango kazi zaidi havitolewi kwa ajili ya kazi hiyo kote Ulaya. Nina maumivu makali ya moyo ninapofikiria kazi katika Uswisi, Ujerumani, Norway, na Sweden. Ambapo kuna mtu mmoja au wawili wanaojitahidi kuendeleza matawi tofauti ya asili, kunapaswa kuwa na mamia kazini.{*EVsw 415:3}*

Katika jiji la London pekee si chini ya wanaume mia moja wanapaswa kushirikishwa. Bwana anaashiria kupuuzwa kwa kazi Yake, na kutakuwa na hesabu nzito ya kusuluhisha mara moja. **Testimonies for the Church 6:25, 26 (1900)..**{*EVsw 415:4}*

Jeshi la Watendakazi

Naona kwamba umuhimu wa kazi nchini Uingereza ni suala la maana sana kwetu hapa nyumbani. Tunazungumzia kuhusu China na nchi nyingine. Tusisahau nchi zinazozungumza Kiingereza, ambako, iwapo Kweli ingehubiriwa, wengi wangeipokea na kuifuata..{*EVsw 415:5}*

Kwa nini kazi kubwa zaidi haijafanyika Uingereza? Nini kimekuwa shida? Watendakazi hawakuweza kupata fedha. Je, hili halituonyeshi haja ya kuwa na uchumi katika kila mstari wa kazi?.....{*EVsw 416:1}*

Mtu yeyote asidhani kuwa kazi huko Uingereza inaweza kuendeshwa na mtu mmoja au wawili. Hii si njia sahihi. Ingawa lazima kuwe na wale watakaosimamia kazi, kunapaswa kuwa na jeshi la watendakazi wanaojitahidi kuwafikia tabaka mbalimbali za watu. Kazi ya nyumba kwa nyumba inapaswa kufanywa. —**The General Conference Bulletin, April 22, 1901.** {*EVsw 416:2}*

Msaada wa Kifedha Utakuja

Kuna kazi ya kufanywa London. Nimeonyeshwa kwamba kazi hii inaweza kufanyika, na kwamba msaada utatoka nje. Wale walio na fedha watatoa sehemu ya mali zao. Msione haya kuwaomba msaada wa kifedha. —**The General Conference Bulletin, April 22, 1901.**{*EVsw 416:3}*

Sehemu ya Kukutanika; Kodi Kumbi Nzuri

Kazi nchini Uingereza ingeweza kuwa mbele zaidi leo iwapo ndugu zetu, katika mwanzo wa kazi huko, wasingefanya kazi kwa njia ya bei nafuu mno. Kama wangalipanga kukodi kumbi nzuri, na kuendeleza kazi kana kwamba walikuwa na zile Kweli kuu ambazo hakika zingeshinda, wangefanikiwa zaidi. **Mungu** anataka kazi ianzishwe kwa namna ambayo mwonekano wa kwanza utakaotolewa, kwa kadri ya uwezo wake, uwe bora kabisa. —**Gospel Workers, uk. 462 (1915).**{*EVsw 416:4}*

Changamoto za Tabaka za ubaguzi wa rangi na hadhi - Caste

Ni kweli, kuna changamoto nyingi katika kuwasilisha Kweli hata katika Uingereza ya Kikristo. Moja ya changamoto kubwa ni tofauti ya hali kati ya tabaka kuu tatu, na hisia ya utabaka, ambayo ina nguvu sana katika nchi hii. Mjini, kuna wenye mitaji, wafanyabiashara, na vibarua wa kila siku; vijijini, kuna wamiliki wa ardhi, wakulima wapangaji, na vibarua wa mashambani. Hizi ni tabaka tatu kuu, zenye tofauti kubwa katika elimu, mawazo, na hali za maisha.

Ni vigumu sana kwa mtu mmoja kuhubiri kwa ufanisi kwa tabaka zote kwa wakati mmoja. Utajiri huchukuliwa kuwa ni ukuu na mamlaka; umasikini, ni sawa na utumwa. Huu sio mpango wa **Mungu** alioutaka

uwepo. **-Historical Sketches of the Foreign Missions of the Seventh-day Adventists, 164 (1886).{*EVsw 416:5}***

Tabaka za Juu Zifikiwe Kupitia Tabaka za Chini

Katika nchi ambapo sehemu kubwa ya watu wanaishi katika hali ya utumwa kwa matajiri, na tabaka za juu zimeshikwa mateka na desturi zilizopitwa na wakati, haishangazi kuwa maendeleo ya Kweli isiyopendwa ni ya polepole mwanzoni. Lakini kama ndugu watakuwa na subira, na watendakazi wawe macho na bidii, wakitumia kila nafasi inayojitokeza kueneza nuru, hakika mavuno mengi ya roho yatafikiwa katika nchi ya Uingereza. Kwa kutumia hekima na ustahimilivu, njia nyingi zitapatikana za kuwafikia watu.**{*EVsw 417:1}***

Bila shaka, daima kutakuwa na changamoto katika kuwafikia tabaka za juu. Lakini mara nyingi Kweli huwapata watu wa tabaka la juu kwa kuanzia kuwafikia wale wa kati na wa chini. **—Historical Sketches of the Foreign Missions of the Seventh-day Adventists, 166 (1886).{*EVsw 417:2}***

Kazi ya Umakini Inahitajika

Kwa sababu hujaona matokeo kama yale ya Australia, usidharau kile ambacho tayari kimepatikana katika nchi ya Uingereza. Kuna roho za thamani huko Grimsby, Ulceby, na wengine watakusanywa. Kuna watu wema huko Southampton, na yule ndugu niliyemwona kwa Ndugu____ pamoja na wale wachache walioko naye, naona ni watu wa kutegemewa.

Kwa sababu hawaoni kila jambo kama tunavyoona sisi, tunapaswa kuwa na hekima katika jinsi tunavyowatendea, tuungane nao popote inapowezekana, tusipanue tofauti baina yetu.

Ninaamini kuwa Dada_____ atakuja mbele ikiwa atasimamiwa kwa hekima. Watu kama hao hawapaswi kuachwa bila kujali, bali juhudi zinapaswa kufanywa kuwaingiza katika Kweli hii tukufu. Tunamhitaji mwanamke huyo kama mtendakazi..... Ni kazi ya neema kuwatafuta kondoo waliopotea na kufanya kila jitihada kuwaingiza kundini. Itachukua muda kuwaondolea mawazo yao ya ajabu na mitazamo isiyo sahihi, lakini lazima tuwe na subira na tusiwafukuze. **Mungu** anafanya kazi pamoja nao, na ninapotazama yaliyopita, naona kwamba tumekabiliana na hali za kukatisha tamaa kama hizi hata zaidi. — **Letter 50, 1887.{*EVsw 418:1}***

Mungu Atawajali Waaminifu Uingereza

Nikiwa na Ndugu S. H. Lane, tulienda Risely, mji mdogo umbali wa maili arobaini kutoka London. Huko, Ndugu Lane na Durland walikuwa wamefanya mikutano ya hema kwa wiki nne. Hema lilikuwa na nafasi ya watu mia tatu, na kila jioni lilijaa, na watu wengi walikuwa wamesimama nje.**{*EVsw 418:2}***

Moyo wangu ulivutwa sana kwa watu hawa, na nilipenda sana kubaki nao kwa muda mrefu zaidi. Kwa hadhira hiyo ingeweza kusemwa, "Kulikuwa na wanawake waheshimiwa si wachache." Wengi kati yao walianza kushika Sabato. Wanaume wengi walishawishika juu ya Kweli; lakini swali kwao halikuwa kama wanaweza kushika Sabato na kuwa na starehe za maisha, bali kama wanaweza kupata chakula, chakula cha kawaida, kwa ajili ya watoto wao. Baadhi ya watu waaminifu kwa dhamiri wameanza kushika Sabato. Imani ya watu kama hao itajaribiwa vikali. Lakini Je, Yeye anayewatunza kunguru hatawajali zaidi wale wanaompenda na kumcha? Jicho la **Mungu** liko juu ya watoto Wake waaminifu wa Uingereza, na Atawafungulia njia ya kutii amri Zake zote. **—Historical Sketches of the Foreign Missions of the Seventh-day Adventists, 163 (1886). {*EVsw 418:3}***

Miji ya Ulaya ya Kaskazini

Kuja Kusaidia kwa Ajili ya Bwana

Katika maono yangu ya mwisho, nilionyeshwa umuhimu wa kazi katika Ulaya ya Kaskazini. Watu wanaanza kuamka kuelekea kwenye Ukweli. Bwana amempa Mzee Matteson ushuhuda wa kugusa mioyo. Lakini kazi hii ndiyo imeanza tu. Kwa kazi ya busara na kujitolea, roho nyingi zitaletwa kwenye maarifa ya Kweli. Kunapaswa kuwa na watendakazi wengi waaminifu, wasio na ubinafsi na wanaomcha **Mungu** katika eneo hili la kimishenari, ambao watashughulika kwa bidii kwa ajili ya roho za watu, kana kwamba itawalazimu kutoa hesabu siku ya hukumu.**{*EVsw 419:1}***

Nimeonyeshwa kwamba ndugu zetu wa Sweden, Norway na Denmark hawafanyi yote ambayo wangeweza na wanapaswa kufanya kwa ajili ya watu wao. Mara tu wanapoukubali Ukweli, wanapaswa kuhisi moto wa juhudi za kimishenari ukiwaka mioyoni mwao kwa ajili ya ndugu zao walioko katika giza la upotovu. Wengi wanatazamia msaada kutoka kwa ndugu zao Wamarekani, ilhali wao hawatimizi wajibu wao wala kuhisi mzigo ambao **Mungu** anawataka wauhisi kwa ajili ya watu wa mataifa yao. Wanaweza kufanya mengi zaidi kuliko wanavyofanya sasa, ikiwa wataamua kufanya hivyo. Ndugu hawa lazima washinde ubinafsi na waamke kuelewa wajibu wao kwa **Mungu** na kwa watu wao, la sivyo watapoteza thawabu ya thamani ambayo wangeweza kuipata kwa kuwekeza vipawa vyao vya mali katika hazina ya **Mungu** na kwa juhudi binafsi zilizoongozwa kwa hekima, hivyo kuwa vyombo vya wokovu wa roho nyingi.{*EVsw 419:2}*

Vijana wanapaswa kufundishwa kuwa wamishenari kwa ajili ya mataifa yao, kufundisha Ukweli kwa wale walioko gizani. Machapisho yanapaswa kuchapishwa barani Ulaya. Lakini kwa sasa [Kumbuka: Imeandikwa mwaka 1879], kuna urahisi mwingi mno na bidii haba miongoni mwa wa Denmark, Sweden, na Norway wanaoamini Ukweli katika nchi hii, hali inayozuia uwezo wao wa kuendelea kuchangia kifedha. Kwa sababu hiyo, nawahimiza waingie katika mpango kazi, wakihisi hata shauku kubwa zaidi kwa watu wao kuliko ile ambayo ndugu zao Wamarekani wameonyesha. **Mungu** anataka ndugu hawa wajitokeze kusaidia kazi ya Bwana bila kuchelewa. **— The Advent Review Supplement, February 6, 1879.**{*EVsw 419:3}*

Tabia na Desturi Hutofautiana, Lakini Asili ya Binadamu ni ile ile

Lazima mfanye kazi hapa kama tulivyofanya kule Amerika; muanzishe vyama vya kijamii na zana nyingine za kusaidia kazi, na hata kama wakati mwingine itaonekana kama machapisho hayafanyi mengi, lazima muendelee mbele. Tulipitia uzoefu huo huo kule Amerika. Lakini tuliendelea kusambaza machapisho haya kwa makundi mbalimbali, na ilichukua muda kabla ya kuona maendeleo.{*EVsw 420:1}*

Nimeonyeshwa kuwa lazima kazi hii katika falme hizi ipate mwelekeo mpya, na lazima kuwepo nguvu kutoka kwa **Mungu** wa mbinguni kuwapa msukumo wa kufanya kazi kwa njia tofauti; na ingawa Ndugu Matteson na Olsen watasaidia katika kazi hii, nataka kuwaelekeza jambo hili sasa ili mweze kuanza kufikiri kwa namna tofauti. Kwa nini msifanye mara kumi zaidi ya mnavyofikiri mnaweza? Lakini kutokuamini kunasimama hapa hapa na kusema kuwa hamwezi kufanya jambo hili au lile. Lakini mnaweza, ndugu.{*EVsw 420:2}*

Tabia na desturi ni tofauti hapa ukilinganisha na Amerika, lakini asili ya binadamu ni ile ile, na ndugu walioupokea Ukweli mioyoni mwao wako tayari kufanya kazi ikiwa watafundishwa jinsi ya kufanya hivyo. Kwa nini ndugu zangu, sijalala zaidi ya saa tatu kwa usiku kwa sababu ya kufikiri juu ya kazi barani Ulaya, na inaonekana kama siwezi kustahimili kimwili ninapotambua mambo haya.{*EVsw 420:3}*

Nimeona kile ambacho **Mungu** Yuko tayari kuwafanyia, lakini ni kadiri ya imani yenu ndiyo **Mungu** atakavyofanya kwa ajili yenu. Hivyo basi tunataka kuamsha imani yenu, kupanua mawazo yenu, na Bwana aweke mzigo wa kazi juu ya kila mmoja wenu anayeamini Ukweli. — **Manuscript 6, 1886.**{*EVsw 421:1}*

Mipango Mipana kwa Ajili ya Copenhagen

Kama katika jiji hili tajiri na zuri [Copenhagen] hakuna chumba kinachofaa kuwasilisha Ukweli kwa watu, tunakumbuka kwamba hakukuwa na nafasi katika nyumba ya wageni kule Bethlehemu kwa ajili ya mama wa Yesu, na Mwokozi wa dunia alizaliwa katika zizi.....{*EVsw 421:2}*

Sijashawishika kabisa kwamba kumbi ndogo na zilizofichika ndizo sehemu bora kabisa zilizoweza kupatikana, au kwamba katika jiji hili kubwa lenye wakazi mia tatu na ishirini elfu 320,000, ujumbe haupaswi kutolewa kwenye chumba cha chini ya ardhi (basement) ambacho kina nafasi ya watu mia mbili tu, na hata nusu ya viti havipo, kiasi kwamba sehemu kubwa ya hadhira inalazimika kusimama. **Mungu** anapowatuma ndugu zetu kutoa msaada, wanapaswa kufanya juhudi kwa bidii, hata kama itagharimu, ili kuwaletea watu nuru. Ujumbe huu ni kwa ajili ya dunia yote; lakini kama ndugu zetu hawatakuwa na maono mapana na mipango mikubwa, hawataona mafanikio makubwa.{*EVsw 421:3}*

Ingawa tunapaswa kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya tabaka la maskini, hatupaswi kujiwekea mipaka ya kuwahudumia tu. Watu wenye nyadhifa na uwezo wanahitajika. Kadiri vipawa vya kiakili vinavyoingizwa katika kazi, mradi vipawa hivyo vimewekwa wakfu kwa **Mungu** na kutakaswa na Roho Wake, kazi itakuwa bora zaidi, na hadhi yake itaonekana mbele ya dunia. Ingawa wengi watakataa ujumbe wa onyo,

bado juhudi lazima zifanywe kuufikisha Ukweli kwa watu wa hadhi na elimu pamoja na maskini na wasiojua kusoma. — **Historical Sketches of the Foreign Missions of the Seventh-day Adventists, uk. 183-184 (1886).**{*EVsw 421:4}*

Changamoto ya Ukumbi Nchini Sweden

Katika mji wa Orebro, kama ilivyo Copenhagen, ninaamini tungeweza kupata usikivu mzuri kama ndugu zetu wangepanga kupata ukumbi unaofaa wa kuwapokea watu. Lakini hawakutarajia makubwa, kwa hiyo hawakupokea makubwa. Hatuwezi kutarajia watu waje kusikia Ukweli usio maarufu na usiopendwa kwa sasa, ikiwa mikutano imetangazwa kufanyika kwenye chumba cha chini ya ardhi (basement) au ukumbi mdogo wa watu mia moja tu. Tabia na uzito wa kazi yetu hupimwa kwa juhudi zinazofanyika kuifikisha kwa umma. Wakati juhudi hizi ni haba sana, watu hupata taswira kuwa ujumbe wetu hauna umuhimu wowote. Hivyo, kwa ukosefu wao wa imani, mara nyingine watendakazi wetu huifanya kazi kuwa ngumu zaidi. — **Historical Sketches of the Foreign Missions of the Seventh-day Adventists, uk. 200 (1886).**{*EVsw 422:1}*

Mavuno Dhahiri ya Ulaya ya Kaskazini

Nimeonyeshwa kuwa wengi katika Ulaya ya Kaskazini waliukubali Ukweli kupitia usomaji. Nafsi zao zilikuwa na njaa ya nuru na maarifa, na walipopata vipeperushi au gazeti, walionyeshwa wakiwa wanasoma. Mahitaji ya mioyo yao yalitimizwa; Roho wa **Mungu** aliigusa na kuathiri mioyo yao; macho yao yalijaa machozi, na vilio vizito vilitoka mioyoni. Waliinama wakiwa na vijikaratasi vya injili mikononi mwao, na kwa maombi ya dhati wakamsihi Bwana awaongoze na kuwasaidia kupokea nuru kana kwamba imetoka Kwake. Wengine walijitoa kwa **Mungu**. Mashaka yalitoweka; na walipoukubali Ukweli wa Sabato ya amri ya nne, walihisi kuwa kweli wamesimama juu ya Mwamba wa Milele. Watu wengi waliotapakaa kote Ulaya ya Kaskazini walionekana kuwa tayari kuikubali nuru ya Kweli. — **The Advent Review Supplement, February 6, 1879.**{*EVsw 422:2}*

Ulaya ya Kusini

Kuhubiri na Huduma Binafsi Huko Italia

Mabonde ya Piedmont yamezungumziwa (Angalia kwenye tovuti Waldensis). Kutokana na nuru niliyopewa, zipo roho za thamani katika mabonde haya yote ambazo zitapokea Kweli. Sina maarifa ya moja kwa moja juu ya maeneo haya; lakini yalionyeshwa kuwa kwa namna fulani yamehusiana na kazi ya **Mungu** ya zamani. Sasa **Mungu** ana hatua ya kusonga mbele kwa watu hawa kuichukua.{*EVsw 423:1}*

Wale wanaofanya kazi katika mabonde haya lazima wawe na shauku ya dhati kwa kazi yao, la sivyo hawatapata mafanikio. Malaika wa tatu anaonyeshwa akiruka katikati ya mbingu. Hii ni kazi inayopaswa kufanyika kwa haraka. Wanapaswa kuwa katika hali ya utayari wa kutenda, wakifanya kazi kwa akili na kwa kujitoa, na wakiwa wameandaliwa kwa neema ya **Mungu** ili kukabiliana na upinzani.{*EVsw 423:3}*

Hawatapaswa tu kuhubiri, bali pia kuhudumu. Wanapotoka kwenda kufanya kazi, wanapaswa kufanya juhudi binafsi kwa ajili ya watu, wakiwaendea watu kwa moyo wa huruma, huku wakiwafungulia Maandiko. Huenda kwa mwanzo kukawa watu wachache tu watakaopokea ile Kweli hapa na pale; lakini wale watakaoongoka Kweli wataanza kuifanya kazi kwa ajili ya wengine, na hivi karibuni, kwa juhudi zinazofaa, makundi makubwa zaidi yataanzishwa, na kazi itaendelea kwa kasi zaidi.{*EVsw 423:3}*

Kuna kazi kubwa inayosubiri kufanyika katika maeneo yote tuliyopokea taarifa zake. Katika nchi hizi zote kuna vipaji vya thamani ambavyo **Mungu** atavitumia; nasi tunapaswa kuwa macho ili kuvipata. — **Historical Sketches of the Foreign Missions of the Seventh-day Adventists, uk. 147 (1886).**{*EVsw 423:4}*

Wengi Watasimama kwa Ajili ya Kweli

Malaika anayeshirikiana na yule wa tatu ataiangaza dunia kwa utukufu Wake Bwana. Kutakuwepo na wengi, hata katika mabonde haya ya kaskazini mwa Italia, ambapo kazi inaonekana kuanza kwa ugumu mkubwa, ambao watatambua sauti ya **Mungu** ikizungumza nao kupitia Neno Lake, na, wakitoka chini ya ushawishi wa makasisi, watasimama upande wa **Mungu** na Kweli.

Eneo hili sio rahisi kufanya kazi, wala si lile ambalo huonyesha matokeo ya haraka; lakini hapa kuna watu waaminifu ambao kwa wakati wao wataitii ile Kweli. — **Historical Sketches, uk. 249 (1886).**{*EVsw 424:1}*

Huduma ya binafsi Yenye Matokeo Italia

Sio jambo la kufurahisha kila mara kwa ndugu zetu kuishi mahali ambapo watu wanahitaji msaada zaidi; lakini kazi yao ingekuwa na matokeo bora zaidi kama wangekuwa tayari kufanya hivyo. Wanapaswa kuwa karibu na watu, kuketi nao mezani, na kulala katika nyumba zao za kawaida. Watendakazi wanaweza kulazimika kupeleka familia zao katika maeneo yasiyopendeza hata kidogo; lakini wanapaswa kukumbuka kuwa Yesu hakukaa katika maeneo ya kupendeza. Yeye Alishuka duniani ili aje kuwasaidia wale waliokuwa wanahitaji msaada. **Historical Sketches, uk. 148 (1886). {*EVsw 424:2*}**

Isipokuwa watu wavutiwe, juhudi zote kwa ajili yao zitakuwa bure. Neno la **Mungu** haliwezi kueleweka kwa yule asiye makini. Wanahitaji **"Asema Bwana"** ikitamkwa moja kwa moja ili kuvuta mawazo yao. Waonyeshe kuwa maisha yao yanahukumiwa na Biblia, sio kwa maneno ya mwanadamu; kwamba wameshtakiwa mbele ya kiti cha hukumu cha haki ya milele, sio katika mahakama ya kidunia. Wakati Ukweli ulio wazi na mkali wa Biblia unapowekwa mbele yao, husimama kinyume na tamaa za muda mrefu na tabia zilizokomaa. Hukumbwa na mshtuko wa dhamiri, na hapo ndipo wanapohitaji sana ushauri wako, faraja, na maombi yako. Roho nyingi za thamani hutetereka kwa muda, na baadaye husimama upande wa upotovu, kwa sababu hawakupata msaada wa kibinafsi kwa wakati ufaao. **— Historical Sketches of the Foreign Missions of the Seventh-Day Adventists. {*EVsw 424:3*}**

Kazi ya Injili Katika Miji ya Australasia

Watu Wengi kutoka Sydney

Kuna kazi ya kufanya ulimwenguni kote, na tunapokaribia wakati wa mwisho, Bwana atagusa mioyo mingi ili ishike kazi hii. Ukitumia ushawishi wako kuwezesha kazi inayohitajika kufanywa huko Sydney, roho nyingi zitaokolewa ambazo hazijawahi kusikia Kweli. Miji lazima ifanyiwe kazi. Nguvu ya wokovu ya **Mungu** itatokea kupitia miji hiyo kama taa iwakayo. **— Letter 79, 1905.{*EVsw 425:1*}**

Fursa ya injilisti Unaofaa Sydney

Sasa kuna kazi ya dhahiri zaidi ya kufanywa Sydney na maeneo ya jirani. Vitongoji vyote viko katika hali bora zaidi kwa kazi ya injili kuliko wakati wowote uliopita, na fursa zilizopo sasa kwa kazi za umishenari wa tiba zinahitaji mipango na uzoefu zaidi katika usimamizi wa kazi... ...**{*EVsw 425:1*}**

Kutatokea matawi mengi yatakayochipuka kutoka kwa mbegu iliyopandwa sasa Sydney, na kila safu/idara ya kazi inahitaji wasimamizi wenye uzoefu ili sehemu moja iungane na nyingine, na kuleta usawa. — **Letter 63a, 1898.{*EVsw 425:3*}**

Ahadi Zaidi Katika Baadhi ya Nchi

Kazi ya umishenari wa tiba inaonekana kutoa fursa zaidi huko Australia kuliko Marekani kwa kufungua njia ya ile Kweli kufikia watu. Na watu wa Bwana sasa watii mwaliko wa mpango wa **Mungu** unaofunguka, na watambue kuwa huu ni wakati unaofaa wa kufanya kazi. **— Letter 41, 1899.{*EVsw 425:4*}**

Kila Mji na Kijiji Kusikia

Kuna maeneo mengi yanayohitaji kufanyiwa kazi. Kila mji au kijiji kando ya reli unapaswa kupokea ujumbe ambao Bwana ametupa. Hatuwezi kusimama kushangilia kwa ushindi mchache. Tunapaswa kuendeleza vita hadi malango. Bwana hajawahi kuacha kuwa na shahidi. Ukweli lazima uwasilishwe katika vitongoji mbalimbali vya Newcastle. Wakati mwingine tutalazimika kuhubiri nje ya nyumba za ibada. Nimefanya hivyo mara mbili Jumapili alasiri, na matokeo yalikuwa mazuri.....**{*EVsw 426:1*}**

Kuna Auburn, mahali pa maili nane kutoka Cooranbong, ambapo wamepata kanisa ambalo nitazungumza mara tu nitakapoweza kupata muda, ambao utakuwa Jumapili ijayo, au wiki moja kutoka Jumapili. Kama wasingetupatia kibali cha kuzungumza kanisani, tungefanyia mkutano hadharani. — **Letter 76, 1899.{*EVsw 426:2*}**

Uzoefu wa Vijijini-nje ya miji

Tunaendelea kufanya mikutano ya wazi. Hivi karibuni nimehubiri mara mbili kwa watu tisini huko Dora Creek, maili tatu kutoka Cooranbong, na pia wiki mbili zilizopita Jumapili huko Martinsville, katika kiwanja chenye nyasi, kwa watu sitini. Mbao zilizungushiwa kwa mtindo wa nusu duara, katika mfumo wa

viti. Wengine walikaa juu ya mikeka, na majani, wengine walikaa ndani ya magari yao nje ya uzio. {*EVsw 426:3*}

Hakuna njia nyingine ya kuwafikia watu hawa ila kwa kufanya mikutano ya wazi. Wengine walionekana kuwa na hamu ya Kweli. Watu wawili au watatu sasa wako karibu kutoa maamuzi, na mashamba yameiva kwa mavuno. Tusipojitoa kwa bidii kuwatembelea watu mahali walipo, tutapoteza nafasi ya uokoaji wa roho nyingi. {*EVsw 426:4*}

Hakuna nafasi kabisa ya kuingia katika makanisa madogo ya kijijini. Tumekataliwa kila nafasi ya kuzungumza na watu kwa njia hiyo. Lakini katika hekalu kuu la Bwana — anga la mbinguni likiwa paa letu, na ardhi ikiwa sakafu yetu — tunaweza kupata wasikilizaji ambao kwa njia nyingine wasingesikia. Tunahisi uzito mkubwa wa kuinua bendera ya kweli katika maeneo haya. Watu hawana mchungaji. Kanisa la nchini Cooranbong limesimama limefungwa wiki baada ya wiki, na watu hawasikii mahubiri. Tunaona kuwa kuna kazi kubwa ya kufanya katika maeneo ya mbali kwa njia ya mikutano ya wazi. Nina mialiko ya mkutano kama huo Jumapili ijayo alasiri Dora Creek. Tuna maeneo mawili sasa ya kufanya mikutano hii. — **Letter 79, 1899.**{*EVsw 427:1*}

Uzoefu wa Kuwafikia Wale Wasioingia Ukumbini

Naona kazi nyingi za kufanya. Siwezi kuona mahali pa kuachilia kazi. Nafsi zinapotea, na lazima nizisaidie. Ninanena ndani ya kanisa na nje ya kanisa. Tunapanda gari kwenda maeneo ya vijijini, na kuhubiri wazi kwa sababu ya chuki dhidi ya Kweli ni kubwa kiasi kwamba watu hawakubali sisi kunena katika nyumba yao ndogo ya ibada iliyo duni (little rough house)…….. {*EVsw 427:2*}

Jumapili tulikwenda Dora Creek, maili tatu, na tukazungumza na watu katika mikutano ya wazi-nje ya jengo. Takriban watu tisini walikuwepo, na nilikuwa na uhuru mkubwa wa kumtangaza Kristo kama Tabibu Mkuu na Mwalimu wa ajabu. Wote walisikiliza kwa makini. Kwa njia hii naweza kuwafikia watu ambao hawatakuja kamwe kwenye ukumbi au nyumba ya ibada. Tuna uimbaji mzuri. **— Letter 74, 1899.**{*EVsw 427:3*}

Kazi Kubwa Inahitajika New Zealand

Tunaona kazi kubwa ya kufanywa katika eneo hili, na tunatamani kuwa na vifaa vya kufanya kazi. Nitasema kuhusu Wellington. Ni mahali penye makanisa mengi na wahubiri wengi... Huu ni mji mkuu na kitovu kikuu cha New Zealand. Utume unapaswa kuanzishwa hapa. Kanisa, hata kama ni la kawaida kabisa, linapaswa kujengwa. — **Letter 9a, 1893.**{*EVsw 427:4*}

Miji ya Ulaya, Australia, na Maeneo ya Mbali Zaidi

> Kuna rasilimali nyingi ambazo zimefungwa na zisizotumika ila zinapaswa kuwekwa kazini kwa ajili ya miji isiyofanyiwa kazi huko Ulaya, Australia, Marekani, na maeneo ya mbali zaidi. Miji hii imetelekezwa kwa miaka mingi. Malaika wa **Mungu** wanatusubiri sisi tutoe kazi kwa ajili ya wakazi wake. Kutoka mji hadi mji, nchi hadi nchi, ujumbe wa onyo lazima utangazwe, sio kwa mavazi ya fahari ya nje, bali kwa nguvu ya Roho, kwa watu wa imani. **— Manuscript 11, 1908.**{*EVsw 428:1*}

SEHEMU YA 13—HUDUMA BINAFSI

Hitaji la Huduma binafsi-mtu mmoja mmoja

Kazi ya Umma na Kazi binafsi

Kazi ya kuhubiri hadharani ni muhimu sana, lakini ni ya thamani sawa na kazi ya nyumba kwa nyumba katika makazi ya watu. Matokeo ya kuwasilisha Ukweli mbele ya makundi makubwa huamsha roho ya kuchunguza, na ni jambo la muhimu sana kwamba shauku hii iendelezwe kwa kazi binafsi. Wale wanaotamani kuchunguza Ukweli wanahitaji kufundishwa kujifunza kwa bidii Neno la **Mungu**. Kila mmoja anahitaji msaada wa mtu atakayemsaidia kujenga juu ya msingi imara. Katika wakati huu muhimu/nyeti wa uzoefu wao wa kiroho, ni jambo la maana sana kwamba watendakazi wa Biblia walioongozwa kwa hekima wawafikie na kuwafungulia hazina ya Neno la **Mungu**. —**Gospel Workers, uk. 364 (1915).** {*EVsw 429:1*}

Kuulima Udongo

Hubiri linapotolewa, mbegu ya thamani hupandwa. Lakini ikiwa jitihada za binafsi hazifanywi kulima udongo, mbegu hiyo haioti mizizi. Moyo usipolainishwa na kutiishwa na Roho wa **Mungu**, sehemu kubwa ya mazungumzo/masomo hupotea. Angalia wale wanaoonekana kupendezwa kutanikoni, na uzungumze nao baada ya huduma. Maneno machache yanayosemwa faraghani mara nyingi yatafaa zaidi kuliko hotuba yote iliyofanywa. Uliza jinsi mada-habari zinazowasilishwa zinavyoonekana kwa wasikilizaji, ikiwa jambo hilo liko wazi akilini mwao. Kwa wema na adabu onyesha kwamba una nia ya Kweli kwao na kujali nafsi zao. —**Testimonies for the Church 6:68 (1900) (Kwa kawaida mtu anahitaji marafiki saba ili apate moyo wa kukaa kwenye imani mpya).** {*EVsw 429:2*}

Njoo Karibu na Watu

Kwa huruma ya Kikristo, mhubiri anapaswa kumwakilisha Kristo kwa mtu mmoja mmoja, akitafuta kuwachochea wapendezwe na mambo ya milele. Mioyo yao huenda ikawa migumu kama njia iliyokanyagwa sana, na inaonekana kana kwamba ni kazi bure kumtambulisha Mwokozi kwao; lakini pale wakati ambapo hoja za mantiki haziwezi kushawishi, na mabishano hayawezi kushinda, upendo wa Kristo unaodhihirishwa kwa huduma binafsi unaweza kuufunua moyo mgumu, na mbegu ya Ukweli ikaweza kutia mizizi. —**Gospel Workers, uk. 185 (1915).** {*EVsw 430:1*}

Miji Kufanyiwa Kazi, Sio Kuhubiriwa Tu

Miji haitakiwi tu kuhubiriwa, bali kufanyiwa kazi ya karibu. Ni lazima pawepo na kazi ya nyumba kwa nyumba. Baada ya onyo kutolewa, na baada ya Ukweli kuwasilishwa kutoka kwa Maandiko, nafsi nyingi zitasadikishwa. —**The Review and Herald, October 14, 1902.** {*EVsw 430:2*}

Kupunguza Mahubiri, Kuongeza Kazi Binafsi

Kama nusu ya kazi ya mahubiri ingepunguzwa na kazi ya binafsi ikaongezwa mara mbili majumbani/mitandaoni na katika makusanyiko, matokeo ya kushangaza yangeshuhudiwa.—**Manuscript 139, 1897.** {*EVsw 430:3*}

Fursa Zinapotea

Pale kazi binafsi inapopuuzwa, fursa nyingi za thamani hupotea, ambazo kama zingeboreshwa, zingesababisha maendeleo makubwa na maamuzi katika kazi ya **Mungu**. —**Gospel Workers, uk. 364 (1915).** {*EVsw 430:4*}

Nafsi Zinapotea kwa Kukosa Kazi Binafsi

Tunaweza kuzungumza maneno ya kutia moyo kwa wale tunaokutana nao. “Neno linalonenwa kwa wakati ufaao,ni litamu kama asali.” Nafsi zinapotea kwa kukosa huduma binafsi. —**Barua 151, 1903.** {*EVsw 430:5*}

Kuwa Tayari Wakati Wowote

Mchungaji anapaswa kuwa tayari “wakati ufaao na usiofaa,” akiwa na utayari wa kutumia kila fursa ili kuendeleza kazi ya **Mungu**. “Wakati ufaao” anapaswa kutumia fursa katika nyumba ya ibada, au pale watu wanapojadili mambo ya dini. “Wakati usiofaa” anapaswa kuwa tayari, iwe kando ya jiko, shambani, njiani, au sokoni, kuelekeza fikra za watu katika mambo makuu ya Biblia kwa roho yenye upole na shauku, akiwahimiza juu ya madai ya **Mungu**. Fursa nyingi sana hupotea kwa sababu watu hudhani si wakati ufaao. Lakini ni nani ajuaye athari ya wito wenye hekima kwa dhamiri? —**Gospel Workers, uk. 186-187 (1915).** {*EVsw 430:6*}

Wapende Watu Kama Kristo

Tumeitwa kuwapenda watu kama Kristo alivyowapenda; kuhisi uchungu wa nafsi hadi wenye dhambi wageuke. Wasilisha upendo wa ajabu wa Kristo, usio na mfanano. Jifiche nyuma ya kivuli cha msalaba. —**Manuscript 42, 1898.** {*EVsw 431:1*}

Huduma ya kutembea Nyumba kwa Nyumba

Kazi ya Nyumba kwa Nyumba

Ukweli haupaswi kuhubiriwa tu katika mikutano ya hadhara; kazi ya nyumba kwa nyumba inapaswa kufanyika. Hebu kazi hii isonge mbele kwa Jina la Bwana. —**The Review and Herald, August 11, 1903.** {*EVsw 431:2}*

Huduma hii ya nyumba kwa nyumba, kutafuta roho, kuwatafuta kondoo waliopotea, ndiyo kazi muhimu zaidi inayoweza kufanyika. **—Letter 137, 1898.** {*EVsw 431:3}*

Lengo la Kazi ya Nyumba kwa Nyumba

Watu wetu hufanya makosa makubwa wanapofanya mikutano ya hema na kuwapata wachache tu, kisha kufunga hema na kudhani kuwa kazi yao imekamilika. Kazi yao ndipo tu imeanza. Wamehubiri mafundisho ya imani mapya na ya ajabu kwa watu wasioyajua, na kisha kuiacha mbegu waliopanda idonolewe na kutwaliwa na ndege, au ikauke kwa kukosa unyevu…….. {*EVsw 431:4}*

Baada ya Ukweli kuwasilishwa kwa nafsi, huwa kuna marafiki, wachungaji, wahubiri, au jamaa wanaojitahidi kuondoa mbegu hiyo kwa kuipotosha. Hao ni kama ndege-wanadamu, wanaoifanya Kweli ionekane kama upotovu au makosa ya mafundisho, na hawampi mtu aliyeamini pumziko hadi waimeze mbegu hiyo kwa madai ya uongo. {*EVsw 432:1}*

Je, ni nini kifanyike? Baada ya mkutano wa hemani kwisha, anzisha utume. Tafuta watendakazi bora kabisa waandaliwe kuwa timu ya kuuza machapisho na kuwapatia wale wasioweza kununua, magazeti ya bure. Kazi ya maandalizi ni pungufu ya nusu ya kazi ya ufuatiliaji baada ya mkutano. {*EVsw 432:2}*

Baada ya watu kusikia sababu za imani yetu, kazi ya nyumba kwa nyumba ianze. Jifunze kuwafahamu watu, wasomee Maneno ya thamani ya Kristo. Mwinue Yesu aliyesulubiwa miongoni mwao, na punde wale waliosikia ujumbe wa onyo na kusadikishwa wataanza kuuliza zaidi kuhusu walichosikia. Huu ndio wakati wa kuwasilisha sababu ya imani yetu kwa upole na hofu, si hofu ya utumwa, bali hofu ya tahadhari ili usiseme bila hekima.

Wasilisha Ukweli kama ulivyo katika Yesu, kwa upole na unyenyekevu wte, kwa urahisi na kwa moyo wa dhati, ukitoa chakula kwa wakati ufaao kwa kila mtu. —**Letter 18, 1898.** {*EVsw 432:3}*

Mahubiri Hufanywa kuwa Yenye Ufanisi Kupitia Huduma Binafsi

Kwa uzoefu wa watendakazi huko _____, tunaona kuwa juhudi zinazofanywa baada ya mikutano ya makambi ni muhimu zaidi kuliko kazi iliyotangulia. Kwa miaka mingi nimeonyeshwa kuwa kazi ya nyumba kwa nyumba ndiyo kazi itakayofanya mahubiri yawe yenye matokeo ya ushindi.

Wale walioonyesha kupendezwa/kuvutiwa wasipotembelewa na watendakazi wetu, wachungaji wengine huingilia kati na kuwakanganya kwa kuyanukuu Maandiko kwa kuyanyumbulisha na kwa kupotosha. Watu hawa sio wajuzi wa Neno la **Mungu**; hudhani kuwa wachungaji wao ni wakweli, na wasio na chuki na hivyo huacha mafundisho ya Biblia waliyokuwa wameanza kuipokea. Lakini watendakazi wetu wakitembelea watu walioguswa moyo, na kuwafafanulia Neno la Kweli, wakionyesha tofauti kati ya ile Kweli na mafundisho yenye m, basi wataimarishwa. {*EVsw 432:4}*

Kama kazi hii ingefanywa kwa bidii, dhati na kukesha, kama watendakazi wangelizilinda na kuzitunza kwa bidii nafsi (roho) kama wale ambao watatoa hesabu, miganda ya mavuno makubwa yangekuwa matokeo ya mbegu iliyopandwa kwenye mikutano yetu ya makambi. {*EVsw 433:1}*

Hii kazi imefanyika pia huko _____. Sasa kuna Watunza Sabato wapya wasiopungua hamsini kwa matokeo ya huduma hii binafsi, ya kuwatafuta watu. *Shetani atafanikiwa katika kazi yake ya kuangamiza, na roho ambazo zingeweza kupatikana na kurejeshwa zitapotea.* —**Letter 18, 1898.** {*EVsw 433:2}*

Wengine Hawafikiwi kwa Huduma ya Mikutano ya hadhara au efoti

Katika miji mikubwa kuna makundi fulani ya watu wasiofikiwa kwa njia ya mikutano ya hadhara. Hawa ni lazima wafikiwe kama mchungaji anavyowatafuta kondoo waliopotea. Juhudi binafsi, za uadilifu na ya bidii ni lazima ifanyike kwa ajili yao. **—Gospel Workers, uk. 364 (1915).** {*EVsw 433:3}*

Baadhi Hawafikiwi na Juhudi za Umma—Katika miji mikubwa kuna madarasa fulani ambayo hayawezi kufikiwa na mikutano ya hadhara. Hawa ni lazima watafutwe kama mchungaji

anapowatafuta kondoo wake waliopotea. Jitihada za kibinafsi na za bidii lazima zifanywe kwa niaba yao.—Wafanyakazi wa Injili, 364 (1915).

Kwa Wale Wasioitika Wito wa Kuja Arusini

Kama hawatakuja kwenye karamu ya injili, kama wito wa Kristo unavyoalika, basi wajumbe wa **Mungu** ni lazima waendane na hali hiyo, wakifikisha ujumbe kwao kupitia kazi ya nyumba kwa nyumba, wakieneza huduma yao hadi barabarani kuu na njia panda, wakiwasilisha ujumbe wa mwisho kwa ulimwengu. **—Letter 164, 1899. {*EVsw 433:4*}**

Hata kwa Wale Wasiovutiwa

Nenda katika nyumba hata za wale ambao hawaonyeshi kuvutiwa kibinafsi. Wakati bado sauti ya rehema inamwalika mwenye dhambi, fanya kazi kwa moyo na akili na kwa bidii yote kama Paulo, **Matendo 20:31** "*Usiku na mchana, sikuacha kumwonya kila mtu kwa machozi.*" Katika siku ya hukumu, ni wangapi watatukabili na kusema, "Nimepotea! Nimepotea! Lakini wewe hukunionya au hukuniambia kabisa; hukuniomba nije kwa Yesu. Kama ningeamini kama mlivyoamini ninyi, ningeifuata kila roho iliyofungwa kwenye hukumu ndani ya uwezo wangu kwa maombi, machozi, na maonyo." **—Review and Herald, June 24, 1884. {*EVsw 434:1*}**

Peleka Neno la Mungu Mlangoni pa Kila Mtu

Vyombo vya habari na uchapaji ni njia mojawapo ya kuwafikia wengi ambao haiwezekani kuwafikia kwa juhudi ya huduma ya injili. Kazi kubwa inaweza kufanyika kwa kuwasilisha kwa watu Biblia na kuisoma kama jinsi ilivyo. Peleka Neno la **Mungu** kwenye kila mlango, yasisitize Maneno yake yaliyo wazi mbele ya dhamiri za watu wote, rudia agizo la Mwokozi: "Yachunguzeni Maandiko- Mathayo 5:37-47:." Waagize wachukue Biblia kama ilivyo, waombe nuru kutoka kwa **Mungu**, na pale nuru inapoangaza, wapokeee kwa furaha kila mwali wa thamani, na kukubali kuishi matokeo yake bila woga. **—Review and Herald, July 10, 1883. {*EVsw 434:2*}**

.

Mungu Atawaongoza kwa Wale Wanaotafuta Ukweli kwenye majumba yao

Nuru, nuru kutoka katika Neno la **Mungu**,—ndicho watu wanahitaji. Ikiwa walimu wa Neno wako tayari, Bwana atawaongoza kuwa karibu zaidi na watu. Atawaongoza hadi kwenye nyumba za wale wanaohitaji na kutamani Kweli; na watumishi wa **Mungu** wanapojihusisha na kazi ya kuwatafuta kondoo waliopotea, uwezo wao wa kiroho huamshwa na kutiwa nguvu. Wakijua kuwa wako katika mapatano na **Mungu**, hujawa na furaha na kuchangamka. Kwa uongozi wa Roho Mtakatifu, hupata uzoefu usioweza kulinganishwa kwa thamani. Nguvu zao za kiakili na maadili hufikia kilele chake; maana neema hutolewa kadri ya mahitaji. —**Review and Herald, Desemba 29, 1904. {*EVsw 434:3*}**

Kuzipata Familia kwa Huduma ya Kiroho -

Kuomba na Kujifunza Pamoja na Familia

Wakati fikra za wengi zinapoguswa na kushawishika juu ya ile Kweli, jambo hili linapaswa kufuatiliwa kwa bidii, hekima, na uvumilivu wa kweli..... Wito unatolewa kwa watu ambao watatoka wakiwa wamejazwa na Roho wa Kristo, wakifanya kazi kwa ajili ya wokovu wa roho. Mhubiri hapaswi kuishia tu mahubiri mimbari, wala asiridhike kukaa katika makazi mazuri miongoni mwa waumini. Lazima awe mlinzi wa roho. Lazima awatembelee watu majumbani mwao, na kwa juhudi binafsi ajitahidi kupandikiza Kweli katika mioyoni na dhamiri zao. Anapaswa kuomba pamoja na familia na kufanya masomo ya Biblia pamoja nao. Wakati anapowahimiza kwa busara na upole watu kutii Neno la **Mungu**, mwenendo wake wa kila siku nao unapaswa kudhihirisha usafi, wema, uungwana, upendo, heshima, na tabia njema. **{*EVsw 435:1*}**

Katika jumbe za malaika wa kwanza na wa pili, kazi hii ilifanyika kwa namna hii. Wanaume na wanawake walichochewa kuchunguza Maandiko na wakaelekeza mawazo katika kuwasilisha Ukweli kwa wengine. Ilikuwa ni kazi binafsi kwa watu na familia ndizo zilizofanikisha sana ujumbe huo na kutoa mafanikio yake ya ajabu. **—Review and Herald, January 27, 1885.** {*EVsw 435:2*}

Familia Zingine Hufikiwa Tu Majumbani Mwao

Kuna familia ambazo hazitafikiwa kamwe na Kweli ya Neno la **Mungu** isipokuwa watumishi Wake Bwana waingie majumbani mwao, na kwa huduma ya dhati na bidii iliyoongozwa na kutakaswa na Roho Mtakatifu, wavunje vizuizi. Watu wanapogundua kuwa hawa wahudumu ni wajumbe wa rehema, wahudumu wa neema, basi hufungua mioyo yao kusikia maneno yanayozungumzwa nao. {*EVsw 435:3*}

Wahudumu hao wanapoomba kwa Bwana pamoja na familia wanazozitembelea, mioyo ya washiriki huguswa kwa njia ambayo haiwezi kufikiwa na sala itolewayo katika mkutano wa hadhara. Malaika wa **Mungu** huingia katika duru ya familia pamoja nao, na akili za wasikilizaji huandaliwa kupokea Neno la **Mungu**. Ikiwa mjumbe ni mnyenyekevu, mnyofu na ana uhusiano wa hai na **Mungu**, basi Roho Mtakatifu huchukua Neno hilo na kulifunua kwa wale anaowahudumia. {*EVsw 436:1*}

Bwana anataka Kweli iletwe watu kwa karibu zaidi, na hili linaweza kufikiwa tu kwa kazi ya mtu kwa mtu binafsi. Mengi yanaeleweka kwa amri: "**Luka 14:23** *Bwana akamwambia mtumwa, Toka nje uende barabarani na mipakani-vichochoroni, ukawashurutishe kuingia ndani, nyumba yangu ipate kujaa..*"

Kuna kazi ya namna hii ambayo bado haijafanyika. Hebu watumishi wa **Mungu** wafundishe Kweli kwa familia, wawakikaribia wale wanaowahudumia. Wakitenda kwa kushirikiana na **Mungu**, Atawajalia nguvu ya kiroho. Kristo atawaongoza katika kazi yao, akiingia katika nyumba pamoja nao, na kuwapa Maneno yatakayopenya mioyo ya wasikilizaji. Roho Mtakatifu atafungua mioyo na akili kupokea nuru kutoka katika chanzo cha nuru yote. **— Review and Herald, Desember 29, 1904.** {*EVsw 436:2*}

Tafuta Njia ya Kupenyeza Kwenye Mioyo ya Watu

Kwa wote wanaoshirikiana na Kristo ningesema: Popote ambapo mnaweza kuwapata watu karibu na mahali pao pa kukota moto pale sebuleni, tumieni fursa hiyo. Chukueni Biblia, na mfunue Kweli zake kuu. Mafanikio yenu hayatategemea sana elimu na ustadi wenu, na yale mliyoyawezea maishani, bali uwezo wa kuifikia mioyo. Kwa kuwa karibu nao kijamii, na kwa ukaribu wa moyo, mtaweza kuelekeza mkondo wa fikra zao kwa haraka zaidi kuliko hotuba bora kabisa. {*EVsw 436:3*}

Kumwakilisha Kristo katika familia wakiwa sebuleni kwa mazungumzo na huku wakikota moto nyumbani, au katika mikutano midogo majumbani, mara nyingi huzaa matunda zaidi ya mahubiri ya hadhara, hata kuliko yale ya wazi au katika makanisa na kumbi.

Wote wanaofanya kazi hii binafsi wanapaswa kuepuka kufanya kazi yao kwa mazoea au kwa namna isiyo na uhai, kama vile ambavyo mhubiri wa mimbari anapaswa kuepuka hivyo. Wanapaswa kuwa watu wanaojifunza daima, wakiwa na bidii ya dhamiri kupata sifa bora zaidi, na kuwa watu waliobobea na wenye uwezo katika Maandiko. **— Gospel Workers, uk. 193 (1915).** {*EVsw 437:1*}

Wawili kwa Wawili Katika Huduma ya Binafsi

Daima wanapaswa kuwa watu wawili kwa wawili miongoni mwa ndugu wetu wanapotoka kwa ajili ya kazi ya Mungu, na kadri inavyowezekana waalike wengine zaidi ili washiriki katika kazi ya kuwatembelea watu na kuwavutia familia kwa juhudi za binafsi. **— Letter 34, 1886.** {*EVsw 437:2*}

Mchungaji na Mke Wake

Endeleeni kufuatilia roho. Tumieni hekima na ustadi mnapotembelea familia. Ombeni pamoja nao na kwa ajili yao. Pelekeni Kweli kwa moyo mwororo kabisa na upendo. Hakika matokeo mazuri yatapatikana. Ikiwa mchungaji na mke wake wanaweza kushiriki kazi hii kwa pamoja, basi wafanye hivyo. **— Letter 18, 1898.** {*EVsw 437:3*}

Huduma ya Uinjilisti kwa Njia ya Kutembelea Watu

Kufuatilia Waliovutiwa

Mchungaji anaweza kufurahia kuhubiri, kwa kuwa ni sehemu ya kupendeza ya kazi na ni rahisi zaidi; lakini hakuna mchungaji anayepaswa kupimwa kwa uwezo wake kama mnenaji mwenye umbuji. Sehemu ngumu zaidi huja baada ya kutoka kwenye mimbari/jukwaa, katika kumwagilia mbegu iliyopandwa. Masilahi yaliyoamshwa yanapaswa kufuatiliwa na kazi ya kibinafsi, - kutembelea watu majumbani, kujihusisha usomaji wa Biblia, kufundisha jinsi ya kuchunguza Maandiko, kuomba na familia na watu wanaovutiwa, kutafuta kukuza hisia zilizo kwenye mioyo na dhamiri kwa kina. **—Testimonies for the Church 5:255 (1885).** {*EVsw 437:4}*

Kujibu Maswali

Hakuna mhubiri aliye na vifaa vya kutosha kwa kazi yake ikiwa hajui namna ya kuwatembelea watu majumbani mwao na kujua mahitaji yao ya karibu. Watu wanapaswa kupewa nafasi ya kuuliza maswali kuhusu mambo yaliyowasilishwa ambayo bado hayaeleweki kwao. Nuru ya **Mungu** inapaswa kuwekwa mbele ya macho yao.

Ni mara ngapi jambo hili lilipofanyika, na mchungaji alipojibu maswali yao, nuru ikatiririka katika akili iliyokuwa gizani, na mioyo ikapata faraja pamoja katika imani ya injili! Hii ndiyo njia ya kufanya kazi ya kuangazia mioyo ya wale wanaotafuta njia ya wokovu. **— Review and Herald, April 19, 1892.** {*EVsw 438:1}*

Kufundisha Watendakazi wa Kufuatilia Watu Waliovutiwa

Wapo ambao sasa wanapaswa kufundishwa na kushirikishwa nawe katika kazi hii, ili iwapo utaitwa kwenda mahali pengine, waendelee kuwa chombo cha kuwakusanya watu na kuwashawishi. Tuombe kuhusu jambo hili. Tunapaswa kuomba, kufanya kazi, na kuamini. Bwana Ndiye ufanisi na mafanikio yetu. **— Letter 376, 1906.** {*EVsw 438:2}*

Njia Yenye Matokeo Kwa Wenye Vipaji vya Kawaida

Wanaume wenye vipaji vya kawaida wanaweza kufanikisha mengi zaidi kwa kazi ya binafsi ya nyumba kwa nyumba kuliko kuwekeza nguvu katika mikutano ya hadhara, katika maeneo yanayopendwa kwa gharama kubwa, au kujaribu kuvuta umati katika kumbi.

Mvuto binafsi ni nguvu. Kadri tunavyofanya kazi kwa karibu na watu, ndivyo mema zaidi yanavyopatikana..... Lazima umkaribie yule unayemhudumia kiasi kwamba asiishie kusikia sauti yako tu, bali ashike mkono wako, afahamu misimamo na kanuni zako, na atambue huruma yako. **— Review and Herald, Desember 8, 1885.** {*EVsw 438:3}*

Kufundisha Maisha Yenye Afya Kupitia Huduma Binafsi

Kila mwalimu wa Kweli hapaswi kudhani kwamba elimu yake imekamilika hadi atakapojifunza sheria za afya na kujua uhusiano wa tabia njema na maisha ya kiroho. Anapaswa kuwa na uwezo wa kuzungumza kwa uelewa kuhusu mambo haya na kuwapa mfano unaoendana na mafundisho yake. Kufundisha tabia sahihi ni sehemu ya kazi ya mhubiri wa injili, na mchungaji atapata fursa nyingi za kuwafundisha watu anaokutana nao. {*EVsw 439:1}*

Mchungaji anapozuru nyumba kwa nyumba, anapaswa kutafuta kuelewa mahitaji yao, akiwapa mafundisho na kanuni zinazowaletea faida ya kweli binafsi. Kwa wale wenye lishe duni, anapaswa kupendekeza vyakula vya kuongeza; na kwa wale wanaoishi kwa anasa, wakijaza meza zao kwa vyakula vya gharama kubwa na visivyo na afya, bali kuumiza mwili—keki tamu, mikate ya mafuta na viungo vikali—anapaswa kuwashauri juu ya lishe bora, yenye kuleta afya na kuchangia masalahi ya maisha ya kiroho. — **Letter 19, 1892.** {*EVsw 439:2}*

Huduma ya Wachungaji Kupitia Mafunzo ya Biblia

Hotuba Mafupi—Vipindi Vingi vya Mafunzo ya Biblia

Epukeni mahubiri marefu. Watu hawawezi kukumbuka hata nusu ya mahubiri wanayosikia. Toeni maelezo mafupi na mtenge muda mwingi kwa ajili ya mafunzo ya Biblia (Bible Readings). Huu ndio wakati wa kufanya kila hoja kuwa wazi kama alama za barabarani. — **Letter 102a, 1897.** {*EVsw 439:3}*

Kazi ya Kiroho ya Moja kwa Moja Isihamishiwe kwa Wasaidizi

Ni lazima tuchukue kila fursa kufanya kazi binafsi. Hii kazi haiwezi kuepukika, hata kama itamaanisha kupunguza idadi ya mahubiri… {*EVsw 439:4*}

Sehemu hii ya kazi ya uchungaji haipaswi kupuuzwa wala kuachwa kwa wake zenu au mtu mwingine yeyote. Ni lazima mjifunze na kujizoesha kutembelea kila familia kwa kadri iwezekanavyo. Matokeo ya kazi hii yataonyesha kuwa ndiyo kazi yenye faida zaidi ambayo mhudumu wa injili anaweza kuifanya. {*EVsw 440:1*}

Kama mchungaji atapuuzia kazi hii ya kuwatembelea watu majumbani mwao, basi yeye si mchungaji mwaminifu, na lawama ya **Mungu** iko juu yake. Kazi yake haitakuwa imekamilika hata nusu. Kama angetoa huduma binafsi, basi kazi kubwa ingefanyika na nafsi nyingi zingeokolewa kwa kukusanywa ghalani. {*EVsw 440:2*}

Mungu hatakubali udhuru wowote kwa kupuuzia sehemu hii muhimu ya huduma—yaani kufunga kazi au miganda ipasavyo, na kumfungia mjumbe wa Ukweli pamoja kundi la kondoo na kondoo mmoja na wana-kondoo wadogo wa malisho ya Bwana. Bwana Mwenyewe humfanya mhudumu kuwa chombo cha nuru kwa watu kwa njia ya juhudi zake binafsi, kwa kujitambulisha naye na watu anaowahudumia. {*EVsw 440:3*}

Wale walio dhaifu katika kundi wanahitaji kuimarishwa kwa wakati ufaao—maneno ya faraja, nguvu na uthibitisho ili waweze kuota mizizi, kudumu, na kuimarishwa katika imani. Hii ndiyo njia na namna ambayo **Mungu** ameidhinisha ili kuwafikia watu.

Nimetambua katika maeneo niliyofanya kazi kwamba kuna maeneo ambayo yamepotea kwa kazi ya **Mungu** kwa sababu wajumbe waliowapelekea Ukweli hawakuhudumu kwa sababu haikuwa kazi yenye kuvutia kwao kufanya hivyo. — **Letter 18, 1893.** {*EVsw 440:4*}

Kazi ya Mungu Haiwezi Kufanywa kwa Niaba Yako

Huduma binafsi ndiyo njia ya kuwafikia watu pale walipo. Jifunze kufahamiana na kuwasiliana nao. Kazi hii haiwezi kufanywa kwa niaba yako. Kutoa au kukopesha pesa hakutaleta matokeo haya. Mahubiri kutoka mimbari hayawezi kutosha. Kufundisha Maandiko katika familia—hii ndiyo kazi ya mhubiri wa injili, na lazima iunganishwe na kazi ya kuhubiri. Ikipuuzwa, mahubiri yatakuwa na mafanikio duni sana. {*EVsw 440:5*}

Wale wanaotafuta Ukweli wanahitaji kusikia maneno sahihi kwa wakati unaofaa, kwa kuwa Shetani huwasiliana nao kupitia majaribu yake.

Ukikutana na upinzani unapotaka kuwasaidia watu, usikate tamaa. Kama mafanikio yanakuwa madogo, usivunjike moyo. Wewe endelea kufanya kazi, uwe mwenye busara, jua wapi uzungumze na lini unyamaze. Angalia nafsi kama mtu anayepaswa kutoa hesabu kwa Bwana. Angalia hila za Shetani ili usipotoshwe. Usiruhusu ugumu wa kazi kukuvunja moyo wala kukuogopesha. Kwa imani thabiti na azimio lisilotikisika, kutana na uvipikue vikwazo hivyo. Panda mbegu kwa imani, bila kuwa na mkono wenye choyo katika kumwaga mbegu. **—Gospel Workers, uk. 188-189 (1915).** {*EVsw 441:1*}

Fundisha—Fanya Mafunzo ya Biblia

Unapenda kuhubiri, na unapaswa kupewa nafasi hiyo kila uendapo. Unaweza kufanya kazi nzuri kwenye mstari huo wa kuhubiri, lakini hiyo siyo kazi pekee na muhimu ya kufanywa—watu wanahitaji kufundishwa, kuelimishwa. Mahubiri mengi yangekuwa na manufaa makubwa zaidi kwa wasilikizaji kama yangepunguzwa kuwa nusu. {*EVsw 441:2*}

Tenga muda wa kufundisha, wa kufanya mafunzo ya Biblia. Fanya hoja na mistari ya Maandiko iwe wazi katika akili za wasikilizaji. Wape nafasi ya kuuliza maswali, na uyajibu kwa namna rahisi sana, ili akili yao ipokee Ukweli unaowasilishwa. {*EVsw 441:3*}

Fundisha kama Kristo alivyofundisha, soma mfano Wake, mbinu Zake za kufundisha. Yeye Alihubiri mahubiri machache tu, lakini kila alikokwenda, watu walikusanyika kumsikiliza maelekezo Yake (instructions). Wachungaji wanapaswa kufundishwa kufanya kazi kama kielelezo cha mbinguni. Hujafanya kazi ya kufundisha ipasavyo bado.

Watu husikiliza mahubiri mengi, moja baada ya jingine lakini hukumbuka mambo machache tu, ambayo pia hukosa nguvu kwa muda. Mambo mengine huingia na kufinya mbegu ya Ukweli. Njia ya Bwana

ndiyo bora ya kugusa akili kwa—kufundisha Ukweli kwa hoja moja baada ya nyingine, kwa ajili ya uzima wa milele. Andaa eneo la ardhi ya moyo, na upande mbegu kwa namna itakayoota na kuzaa matunda. **—Letter 29, 1890.** {*EVsw 441:4}*

Kujifunza Sanaa ya Kazi Binafsi

Wote Wawezao Kufanya Kazi ya Biblia

Wote wawezao wanapaswa kufanya kazi binafsi. Wanapotembelea nyumba kwa nyumba, wakieleza Maandiko kwa namna rahisi na wazi, **Mungu** huifanya Kweli kuwa yenye nguvu na ya kuokoa. Mwokozi huwabariki wanaofanya kazi hii. —**Letter 108, 1901.** {*EVsw 442:1}*

Kufundisha Mafundisho Makuu ya imani (doctrines) Siyo Lengo la Awali

Zipo roho nyingi zinazotamani sana nuru, hakikisho, na nguvu ambazo hazijawahi kuzipata. Zinahitaji kutafutwa na kufanyiwa kazi kwa subira na ustahimilivu. Muombe Bwana kwa maombi ya dhati. Mweleze Yesu kwa sababu unamjua Yeye kama Mwokozi wako binafsi. Acha upendo Wake unaoyeyusha moyo, ulio mwingi na neema Yake ya thamani na ajabu vitoke kupitia midomo ya mwanadamu.

Huna haja ya kuwasilisha mafundisho ya kina ya imani (doctrinal points) isipokuwa wakikuuliza. Bali chukua Neno la **Mungu**, na kwa upendo wa dhati kwa roho, waonyeshe haki ya Kristo ambaye wewe na wao lazima mwendee ili mpate kuokolewa. **—Manuscript 27, 1895**. {*EVsw 442:2}*

Kujifunza Kuvuna Mazao

Kuna haja ya elimu—kuwafunza wahudumu watakaoenda kwenye shamba la injili, sio tu kutumia mundu na kuvuna mazao, bali pia kuyayareki/kuyakusanya na kuyatunza ipasavyo. Kuvuna huku kumefanyika kila mahali, lakini matokeo yamekuwa kidogo kwa sababu hakuna kazi ya dhati na jitihada binafsi ya kukusanya ngano kutoka kwenye makapi na kuifunga katika miganda tayari kwa ghala. —**Letter 16e, 1892.** {*EVsw 442:3}*

Jifunze Kutumia Sanaa ya kuutumia Wavu wa Injili

Akili lazima iwe na utendaji makini kubuni njia bora za kuwafikia watu walio karibu nasi. Hatupaswi kuwa wabaradhaifu na kwenda mbali katika kugharimia sana kazi ya kufikia watu. Kuna watu binafsi na familia karibu nasi ambao tunapaswa kuwafikia kwa juhudi binafsi. Mara nyingi tunaacha fursa zilizopo karibu nasi ziyoyome, tukikimbilia kufanya kazi mbali isiyo na matumaini, na hatimaye kupoteza muda na rasilimali katika maeneo yote mawili. Wajibu wa sasa ni tasnia ya kujifunza jinsi ya kukusanya watu kwa wavu wa injili. —**The Review and Herald, Desember 8, 1885.** {*EVsw 443:1}*

Usahili wa Asili Katika Kuleta Roho

Kazi ya Kristo kwa kiasi kikubwa ilikuwa ya mawasiliano ya hadhira ya mtu mmoja-mmoja. Alikuwa na moyo wa kujali hata hadhira ya mtu mmoja, na mtu huyo mmoja alieneza kile alichopokea kwa akili maelfu za watu. {*EVsw 443:2}*

Waelimisheni vijana kuwasaidia vijana wenzao; na katika kufanya hivyo, kila mmoja atapata uzoefu utakaomfanya awe mhudumu aliyejitoa wakfu katika uwanja mpana zaidi. Maelfu ya mioyo inaweza kufikiwa kwa njia rahisi kabisa. Hata walio na akili mahiri sana na wanaotukuzwa kama watu wakuu na mashuhuri wa dunia wenye karama kubwa, mara nyingi hupata faraja na kuburudishwa kutoka kwa maneno rahisi sana yaliyonenwa na mtu anayempenda **Mungu**, anayezungumza juu ya upendo huo kwa urahisi kama wale watu wa dunia wanavyozungumza mambo wanayoyatafakari na kujilisha siku kwa siku. Maneno yaliyoandaliwa na kujifunzwa vizuri hayana athari kubwa, bali kazi ya Kweli na ya dhati ya mwana au binti wa **Mungu** —iwe ni kwa maneno au huduma ya mambo madogo—ikiwasilishwa kwa urahisi, inaweza kufungua milango ya mioyo iliyofungwa kwa muda mrefu. **—The Review and Herald, May 9, 1899.** {*EVsw 443:3}*

Namna ya Kuwafikia Watu—Kwa Upole na Wema

Wafikieni watu kwa namna ya upole, wema, na kwa kuwavutia na tabasamu, kwa moyo wa upendo wa Kristo…….. Hakuna lugha ya kibinadamu inayoweza kueleza thamani ya huduma ya Neno na ya Roho Mtakatifu. Hakuna maneno ya kibinadamu, yanayoweza kuelezea kikamilifu kwa akili yenye ukomo, thamani

ya kuelewa na kwa imani hai kupokea baraka inayotolewa wakati Yesu wa Nazareti anapopita. **—Letter 60, 1903. {*EVsw 444:1*}**

Umuhimu wa Kupeana Mkono

Mambo mengi hutegemea jinsi unavyowakaribisha wale unaowatembelea. Unaweza kushika mkono wa mtu kwa namna itakayomfanya akuamini mara moja, au kwa namna ya baridi itakayomfanya afikiri huna upendo au shauku naye. —**Gospel Workers, 189 (1915). {*EVsw 444:2*}**

Vijana Kwa Ajili ya Kazi ya Biblia Mijini

Vijana wanapaswa kufundishwa ili wafanye kazi katika miji. Hata kama hawataweza kuhubiri kutoka kwenye mimbari, bado wanaweza kwenda nyumba kwa nyumba na kuwaelekeza watu kwa Mwana-Kondoo wa **Mungu** aondoaye dhambi ya ulimwengu. Vumbi na taka za makosa na uongo zimeficha hazina ya Kweli; lakini watendakazi wa Bwana wanaweza kuifukua na kuifunua, ili wengi waione kwa furaha na mshangao. Kuna aina nyingi za kazi, zinazoendana na akili tofauti na vipawa mbalimbali. **—Historical Sketches of the Foreign Missions of the Seventh-day Adventists, 182 (1886). {*EVsw 444:3*}**

Chuki Kuvunjwa

Masomo ya Biblia na Kuwatembelea Watu Yatayarisha Njia kwa Kazi Kuu

Kazi hii inapaswa kuanza kimyakimya bila makelele wala matangazo kama mpiga tarumbeta. Inapaswa kuanza kwa kutoa masomo ya Biblia na hivyo kuwaelimisha watu. Mpango huu utakuwa na ufanisi mkubwa zaidi kuliko kuanza kwa mahubiri. —**Letter 89a, 1895. {*EVsw 445:1*}**

Upinzani Huepukwa Kupitia Kazi ya Binafsi

Katika huduma ya **Mungu**, lazima tukabiliane na vikwazo na matatizo. Matukio ni ya **Mungu**; na watumishi Wake lazima wakumbane na magumu na upinzani; maana haya ni njia alizochagua za kuwanidhamisha kwa upendo, na ndiyo masharti Aliyoweka kwa maendeleo ya hakika na mafanikio. Lakini nawasihi watumishi wa Bwana Yesu wakumbuke kwamba kuna kazi inayoweza kufanywa kwa utulivu, bila kusababisha upinzani mkali unaofunga mioyo dhidi ya Kweli. **—Letter 95, 1896. {*EVsw 445:2*}**

Kutembelea Nyumba kwa Nyumba Kuwezesha Maamuzi ya Hekima kwa Kazi ya Mahubiri ya hadhara au Efoti

Ninawaambia kwa Jina la Bwana kwamba kwa idadi yenu ya sasa ya watendakazi, hamko tayari kufanya kazi katika maeneo magumu ambako chuki na ubaguzi ni mkali. Ikiwa nusu ya muda unaotumika kwa mahubiri ya umma utatengwa kwa kufundisha nyumba kwa nyumba hadi watu wawaone watendakazi kuwa ni watu wanyofu kiroho na waelewe sababu za imani yao, ingekuwa bora zaidi. Baada ya kazi hiyo kufanywa, ndipo iangaliwe kama ni busara kufanya kazi ya gharama kubwa zaidi. **{*EVsw 445:3*}**

Juhudi za umma zimefanywa na zimeleta matunda mema. Baadhi wameitikia na kuipokea Kweli, lakini, lo! ni wachache sana kwa kiasi gani. Bwana anatamani Kweli iwasogelee watu kwa karibu, na kazi hii inaweza kufanyika tu kupitia kazi-binafsi. —**Letter 95, 1896. {*EVsw 445:4*}**

Busara Yahitajika Kuvunja Chuki

Nathanaeli alikuwa akiomba kujua kama kweli huyu Ndiye Kristo aliyeandikwa na Musa na manabii. Alipoendelea kuomba, mmoja wa wale waliomjia Kristo, aitwaye Filipo, alimwita akisema, "**Yohana 1:45** *Filipo akamwona Nathanaeli, akamwambia, Tumemwona Yeye aliyeandikiwa na Musa katika torati, na manabii, Yesu, mwana wa Yusufu, mtu wa Nazareti?*" Akijua jinsi chuki ambavyo ingetokea kwa haraka. Nathanaeli akasema, **Yohana 1:46** *"Nathanaeli akamwambia, Laweza neno jema kutoka Nazareti?"* Filipo akamwambia, *Njoo uone*.

Filipo alijua vema chuki kali iliyokuwa akilini mwa wengi dhidi ya Nazareti, na hakujaribu kubishana naye, kwa kuogopa kuchochea ugomvi, bali alisema kwa urahisi, "Njoo uone." **{*EVsw 446:1*}**

Hapa kuna somo kwa wahudumu wetu wote, wainjiliti/wauzaji wa vitabu na wamishenari. Unapokutana na wale ambao, kama Nathanaeli, wana chuki dhidi ya Kweli, usisitize mitazamo yako ya pekee kwa nguvu. Anza kwa kuzungumza juu ya mambo ambayo mnaweza kukubaliana. Piga magoti pamoja

nao katika maombi, na kwa imani ya unyenyekevu toeni dua zenu mbele ya kiti cha neema. Wewe na wao mtaunganishwa kwa karibu zaidi na mbingu, chuki italegea, na moyo utakuwa rahisi kufikiwa. **—Historical Sketches of the Foreign Missions of the Seventh-day Adventists, uk. 149 (1886).** {*EVsw 446:2*}

Kuwahudumia Wazee

Kuisubiri Kweli

Ni jambo la kushangaza kuona ni wazee wangapi wanaofikiwa na watendakazi ambao huhitaji kazi ndogo tu ili wakubali Kweli, pamoja na Sabato. Kwanini, Husema, "Hiki ndicho tulichokuwa tunakiombea. Tulijua kuwa Maandiko yana mengi ya kusema kuhusu mambo ambayo makasisi hawakuweza na hawawezi kutufafanulia." Hao hufanya kidogo isipokuwa hufurahia nuru na Kweli. Furaha yao inaonekana kutimia. **—Letter 18, 1898.** {*EVsw 446:3*}

Maisha Yaanza Katika Uongofu

Nimesoma hivi karibuni kisa kifuatacho: {*EVsw 447:1*}

"Mzee mmoja, wa miaka kama sabini au themanini, aliletwa kwangu, akiwa mfano wa kumbukumbu ya rehema ya **Mungu**. Nilimuuliza ana umri gani. Alinitazama kwa muda, kisha akasema kwa sauti ya kuyumba, machozi yakitiririka mashavuni mwake, 'Nina miaka miwili tu.' Nilionyesha mshangao, kisha akasema, 'Ah, hadi miaka miwili iliyopita nilikuwa ninaishi maisha ya maiti-mfu. Sijawahi kujua maana ya kuishi hadi nilipokutana na maisha yaliyofichwa pamoja na Kristo katika **Mungu**.'"—**Letter 160, 1903.** {*EVsw 447:2*}

Uzoefu na Mbinu za Ellen G. White Kama Mtendakazi Binafsi

Uzoefu wa Awali

Uhalisia wa uongofu wa Kweli ulionekana wazi sana kwangu kiasi kwamba nilihisi kutaka kuwasaidia marafiki zangu vijana kuingia kwenye nuru, na kwa kila fursa nilitumia ushawishi wangu kwa ajili ya lengo hili. {*EVsw 447:3*}

Nilipanga mikutano na marafiki zangu vijana, baadhi yao wakiwa na umri mkubwa kuliko mimi, na wachache walikuwa wameoa au kuolewa. Wengi wao walikuwa na ujinga mwingi, wanaopenda ubatili, wasiojali kuhusu mahitaji ya wengine na wapenda anasa; uzoefu wangu uliwajia kama hekaya isiyo na maana, na hawakujali ushawishi au kusihi kwangu. Lakini niliamua kuwa juhudi zangu hazitakoma hadi hawa wapendwa, ambao nilikuwa na shauku nao, wamejitoa kwa **Mungu**. Usiku kadhaa nilikesha nikiomba kwa bidii kwa ajili ya wale ambao nilikuwa nimewatafuta na kuwaleta pamoja kwa lengo la kufanya kazi na kuwaombea. {*EVsw 447:4*}

Baadhi yao walikuja kwa udadisi tu wa kusikia nilichokuwa nacho cha kusema; wengine waliniona kama mtu aliyepoteza mwelekeo kwa kuwa na bidii na kutochoka kiasi kile, hasa walipoonyesha kutokuwa na shauku kwa upande wao. Lakini katika kila mkutano wetu mdogo niliendelea kuwahimiza na kuwaombea mmoja mmoja hadi kila mmoja alipojitoa kwa Yesu, akitambua neema ya msamaha Wake Masihi. Kila mmoja alimgeukia **Mungu**. {*EVsw 447:5*}

Usiku baada ya usiku, katika ndoto zangu, nilionekana nikifanya kazi kwa ajili ya wokovu wa roho. Wakati huo, watu maalum waliwekwa akilini mwangu; hawa niliwatafuta baadaye na kuwaombea. Kila mmoja isipokuwa mmoja tu walijitoa kwa Bwana. **—Life Sketches, uk. 41-42 (1915).** {*EVsw 448:1*}

Miaka Ishirini na Mbili Baada ya Kupanda Mbegu

Baada ya mkutano [wa kambi huko Michigan] kumalizika, dada mmoja alininyoshea mkono kwa furaha, akionyesha furaha kubwa kukutana na dada White tena. Aliniuliza kama nakumbuka nilipotembelea nyumba moja ya mbao miaka ishirini na miwili iliyopita. Alitupa vitafunio na vinywaji vya kuburudishana niliwachia kitabu kidogo, kilichoitwa **Experience and Views.** {*EVsw 448:2*}

Alisema kuwa aliwaazima majirani wake kitabu hicho, na kadiri familia mpya zilivyozidi kuhamia jirani, kitabu kile kilisambazwa sana hadi kilichakaa. Alionyesha hamu kubwa ya kupata nakala nyingine. Majirani zake walipendezwa sana nacho na walitamani kumwona mwandishi wake. Alisema kwamba nilipomtembelea nilimzungumzia Yesu na uzuri wa mbinguni kwa hamasa kiasi kwamba alivutiwa na hakuwahi kusahau.Tangu wakati huo, Bwana alituma wachungaji kuwahubiria Kweli, na sasa kulikuwa na

kundi zima linaloshika Sabato. Ushawishi wa kitabu kile kidogo, sasa kikiwa kimechakaa kwa mguso wa mikono, uliendelea kimyakimya, ukifanya kazi yake ya maandalizi hadi ardhi ya mioyo ilipokuwa tayari kwa mbegu ya Kweli, kutoka sehemu moja mpaka nyingine. {*EVsw 448:3}*

Nakumbuka vizuri safari ndefu tuliyosafiri miaka ishirini na miwili iliyopita, huko Michigan. Tulikuwa njiani kuelekea mkutano huko Vergennes. Tulikuwa maili kumi na tano kutoka mahali tulipokwenda. Dereva wetu alikuwa amepita barabarani mara kwa mara na alikuwa akiifahamu vyema njia hiyo, lakini alilazimika kukubali kwamba alikuwa amepotea njia. Tulisafiri maili arobaini siku hiyo, kupitia misitu, juu ya magogo na miti iliyoanguka, ambapo hapakuwa na alama ya barabara.....{*EVsw 449:3}*

Hatukuweza kuelewa ni kwa nini tuachwe tukimangamanga katika safari hii ya kipekee jangwani. Tulifurahi sana tulipoona eneo dogo lililokuwa na kibanda cha mbao, ambapo tulimkuta dada niliyemtaja. Alitukaribisha kwa ukarimu nyumbani kwake, na akatupa viburudisho -vitafunio na vinywaji, ambavyo vilipokelewa kwa shukrani. Tulipokuwa tumepumzika, nilizungumza na familia na kuwaachia kijitabu kidogo. Alikikubali kwa furaha, na amekihifadhi hadi wakati huu.{*EVsw 449:2}*

Kwa miaka ishirini na miwili, ya kutangatanga kwetu katika safari hii kumeonekana kuwa jambo la ajabu kwetu, lakini hapa tulikutana na kundi kubwa la watu ambao sasa ni waumini katika Ukweli, na ambao wanakumbuka uzoefu wao wa kwanza kutokana na ushawishi wa kijitabu hicho kidogo. Dada ambaye alituhudumia kwa ukarimu sana, sasa, pamoja na majirani zake wengi, wanafurahia nuru ya Ukweli wa sasa.—The Signs of the Times, Oktoba 19, 1876.—The Signs of the Times, October 19, 1876. {*EVsw 449:3}*

Uzoefu Nchini Nîmes, Ufaransa

Tulipokuwa tukifanya kazi huko Nîmes, Ufaransa, tulilenga kuokoa roho. Kulikuwa na kijana aliyekuwa amekata tamaa kwa sababu ya majaribu ya Shetani na makosa ya ndugu waliokosa uelewa wa namna ya kushughulika na akili vijana. Aliacha Sabato na akaanza kufanya kazi kwenye kiwanda ili kukamilisha mafunzo ya tasnia ya kutengeneza saa. Alikuwa ni kijana mwenye kuwapa watu matumaini ya siku za mbeleni na Saa yangu ilihitaji matengenezo, na hili lilituleta pamoja, kwani nilitambulishwa kwake. {*EVsw 449:4}*

Nilipomtazama tu usoni nilijua kuwa huyu ndiye kijana ambaye Bwana alikuwa amenionyesha katika maono, mambo yote yahusuyo hii njozi yaliletwa mawazoni mwangu. {*EVsw 450:1}*

Alihudhuria mikutano alipotegemea kuwa ningehubiri, na alinikodolea macho kwa makini kipindi chote cha mahubiri yaliyotafsiriwa kwa Kifaransa na ndugu Bourdeau. Nilihisi wajibu wa kumfanyia kazi kijana huyu. Nilizungumza naye kwa saa mbili, nikamweleza hatari ya hali yake. Nilimwambia kuwa makosa ya ndugu zake si sababu ya kuhuzunisha moyo wa Kristo, ambaye alimpenda hadi akafa ili kumkomboa. {*EVsw 450:2}*

Nilimweleza historia ya maisha yake na makosa yake (yaliyokuwa ni makosa ya ujana), ambayo hayakustahili kushughulikiwa kwa ukali ule mkubwa. Kisha nikamsihi kwa machozi ageuke na amrudie Baba yake wa mbinguni, na kuacha huduma ya Shetani na dhambi, kwa kuwa alikuwa amerudi nyuma kabisa, na akawa kama mwana mpotevu na kumwambia arudi kwa Baba Yake, na kwenye huduma ya Babaye wa mbinguni. Alikuwa kwenye kazi nzuri, akijifunza sanaa yake ya kutengeza saa. Lakini ikiwa angeendelea kushika Sabato, angepoteza ajira yake..... Miezi michache tu ilikuwa imebaki amalize mafunzo yake, kisha angepata tasnia/taaluma nzuri. Lakini nilimsihi afanye uamuzi wa haraka. {*EVsw 450:3}*

Tuliomba naye kwa dhati na bidii, na nikamwambia kuwa sitamruhusu atoke nje kwa kuvuka kizingiti cha mlango, hadi aseme mbele za **Mungu** na malaika kwamba, “Kuanzia leo nitakuwa MKristo.” Lo! moyo wangu ulijaa furaha alipoitamka kauli hiyo. Hakulala usiku huo.

Alisema kuwa tangu alipotoa ahadi hiyo, alijihisi kuwa katika njia mpya. Mawazo yake yalisafishwa, makusudi nania yake ikabadilika, na jukumu alilolibeba lilionekana zito sana kiasi kwamba hakuweza kulala.

Kesho yake alimjulisha mwajiri wake kuwa hawezi kuendelea kumfanyia kazi. Hakulala vizuri kwa siku tatu, lakini alikuwa mwenye furaha, na mwenye shukrani kwa uthibitisho wa msamaha wa Bwana na upendo Wake. —**Letter 59, 1886. {*EVsw 450:4*}**

Matumizi Yenye Ufanisi ya Machapisho ya Kiroho

Kulikuwa na ndugu mmoja ambaye, pamoja na familia yake yote, tulimthamini na kumheshimu sana. Alikuwa mtu wa kujisomea, mwenye shamba kubwa lenye machungwa na limau bora kabisa, pamoja na matunda mengine. Lakini hapo mwanzo hakuchukua msimamo kamili kwa ajili ya Ukweli, na akarudi nyuma. Waliniambia kuhusu jambo hilo. Usiku mmoja katika maono, malaika wa Bwana alionekana kusimama karibu nami, akisema: “Nenda kwa Ndugu _____, mwekee vitabu vyako mbele yake, na hii itaiokoa roho yake.”

Nilimtembelea nikiwa na baadhi ya vitabu vyangu vikubwa. Nilizungumza naye kana kwamba alikuwa bado upande wetu. Nilizungumza kuhusu wajibu wake. Nikamwambia:

“Ndugu yangu, una wajibu mkubwa. Majirani zako wamekuzunguka kila upande. Unawajibika kwa kila mmoja wao. Una maarifa ya Kweli, na kama unapenda Kweli na kusimama katika unyoofu, utamwamini Kristo.” **{*EVsw 451:1*}**

Alinitazama kwa mshangao, kana kwamba alikuwa akisema, “Sidhani kama unajua kuwa nimeiacha Kweli, nimewaacha binti zangu waende kwenye dansi na shule ya Jumapili, na hatuishiki tena Sabato.” Lakini nilikuwa najua. Hata hivyo, nilizungumza naye kana kwamba bado alikuwa upande wetu. Nikamwambia:

“Sasa, tunataka kukusaidia uanze kazi ya kuwafikia majirani zako. Nataka nikukabidhi vitabu fulani.” Akasema: “Tuna maktaba ambapo tunachukua vitabu.”

Nikajibu:“Sioni vitabu vyovyote hapa. Labda unajisikia vibaya kuchukua kutoka maktaba. Nimekuja kukupa vitabu hivi ili watoto wako waweze kuvisoma, na vitakuwa nguvu kwako.”

Nilipiga magoti na kuomba pamoja naye. Tuliposimama, machozi yalikuwa yakitiririka usoni mwake, akasema:

“Nashukuru kwamba umekuja kunitembelea. Nashukuru kwa vitabu.” **{*EVsw 451:2*}**

Nilipomtembelea tena, aliniambia kuwa alikuwa amesoma sehemu ya “Wazee na Manabii” (Patriarchs and Prophets). Akasema: “Hakuna neno hata moja ambalo ningebadili. Kila aya inaongea moja kwa moja na roho.” **{*EVsw 452:1*}**

Nilimuuliza ni kipi kati ya vitabu vyangu vikubwa alichokiona kuwa muhimu zaidi. Akasema: “Ninawaazima vyotemajirani zangu, na mmiliki wa hoteli anasema “Pambano Kuu” (Great Controversy) ndicho bora zaidi. Lakini,” alisema kwa sauti iliyotetemeka, “mimi naona “Wazee na Manabii” (Patriarchs and Prophets) ndicho bora zaidi. Ndicho kilichonitoa kwenye tope lenye kunata.” **{*EVsw 452:2*}**

Kwa kifupi, alichukua msimamo thabiti kwa ajili ya Kweli. Familia yake yote iliungana naye, na wamekuwa chombo cha kuokoa familia nyingine. — **The General Conference Bulletin, April 5, 1901. {*EVsw 452:3*}**

Mazungumzo na Muumini Mpya Kuhusu Kazi ya Injili

Mwanamke mmoja wa miaka arobaini hivi aliletwa kwangu, aliyekuwa ameamua kutii Kweli huko Canterbury. Mume wake anamuunga mkono kikamilifu na hufanya kila awezalo kumpeleka kwenye mikutano. Wanamiliki nyumba yao ndogo, nzuri, ambayo tayari imelipiwa. Alikuja kwenye gari na kuzungumza nasi. Akasema kuwa watu wa Canterbury si watu wanaokwenda kanisani, lakini hema lililosimamishwa pale _____ limekuwa kama tangazo, na watu wamekuwa na hamu ya kujua linamaanisha nini. Kwa njia hii, wameanza kuhudhuria mikutano, na wengi wameonyesha kuvutiwa. Huwezi kuwavuta waingie kanisani au ukumbini, lakini katika hema watahudhuria... **{*EVsw 452:4*}**

Dada huyu aliyenizungumzia akiwa mlangoni alisema:

“Mambo haya ya Biblia ni ya thamani mno kwangu. Inashangaza kuwa hatukuwa tunaona haya awali. Biblia imejaa hazina, na nataka kutumia kila nafasi kusikia na kujifunza, ili niweze kuwasaidia wengine. Watu wa hapa Canterbury wanahitaji huduma ya namna hii. Mkisimamisha hema, watakuja.” **— Letter 89a, 1895.** {*EVsw 453:1}*

Kurasa Kutoka Katika Shajara ya 1892

Oktoba 26: Tuliahidi kumtembelea Ndugu na Dada H. Baada ya chakula cha mchana, Mchungaji Daniells, May Walling, na mimi tulienda kutimiza ahadi hiyo. Kwa sababu ya vishawishi vya adui, Dada H aliacha Kweli... Baada ya mazungumzo mafupi, tulianza maombi, na Bwana akatupa pumzi ya Roho Wake Mtakatifu. Tulihisi uwepo wa **Mungu**, na tunatumaini kuwa jitihada hii haitakuwa ya bure. {*EVsw 453:2}*

Novemba 5: Ilikuwa siku ya kupendeza, lakini nilikuwa sina nguvu kabisa. Tulihudhuria mkutano, na tukamwalika jirani yetu aende nasi. Alikubali mara moja na alionekana kuguswa sana. Alizungumza kwa uhuru tulipokuwa njiani kuelekea mkutano, lakini tuliporejea alikuwa kimya, mwenye uso wa tafakari nzito. Nilizungumza kuhusu mfano wa mtu asiye na vazi la harusi, na tulikuwa na mkutano wa kugusa moyo. Baadaye, dada huyo alimwambia mpwa wangu, May Walling, kuwa alijuta kutohudhuria mikutano yote tangu tulipofika. Aliahidi hatokosa hata mkutano mmoja tena wakati wote tutakapokuwa bado hapa. {*EVsw 453:3}*

Novemba 6: Tulikuwa tumepanga kuendesha gari la farasi milimani..... lakini nilihisi mzigo mzito moyoni kwa ajili ya Ndugu na Dada H, na sikutaka kuchelewesha kazi ya Bwana. Licha ya maelekezo duni, May Walling na mimi tulianza safari ya kuwatafuta... Hatimaye tukafika. Niliwaambia kuwa nimekuja kuzungumza nao. Tulianza saa nane na nusu, na tukazungumza hadi saa kumi na moja..... Nilijitahidi kwa uwezo wangu wote kumsaidia Dada H. Alilia karibu muda wote tuliokuwa tukizungumza. Nadhani Roho wa Bwana alimgusa. Niliomba pamoja nao kisha nikawaweka mikononi mwa **Mungu**. {*EVsw 453:4}*

Novemba 7: Nilipumzika vizuri usiku. Saa kumi na nusu wakati wa mapambazuko ya asubuhi nilianza kuandika. Saa nne asubuhi tulimtembelea Dada E. {*EVsw 454:1}*

Novemba 8: Nililala vizuri. Siku hiyo tulimpeleka Dada F ambaye anakaa na watoto wake kwa muda, tukazungumza naye kwa muda mrefu. Ni mwanamke aliyepitia taabu makubwa. {*EVsw 454:2}*

Novemba 9: Kwa mwaliko wa dhati, tulikwenda kwenye msitu mzuri, mahali ambapo wazazi na watoto wa shule ya Sabato walikuwa na karamu ya chakula. Nilizungumza kwa dakika thelathini. Wengi ambao si waumini walihudhuria. {*EVsw 454:3}*

Novemba 10: Niliandika hadi mchana, kisha tukasafiri kwenda Bourdon, kukutana na baadhi ya madada pale. Tulikuwa na kipindi cha maombi kilichobarikiwa, tukiamini ahadi ya Kristo kwamba popote wawili au watatu wanapokusanyika kwa Jina Lake, Yeye huwepo kuwabariki. Nilisoma mambo muhimu, na nikazungumza nao. Nilijitahidi sana kuzungumza kuliko ninapohubiri Sabato, kwa kuwa nilikuwa nao kwa karibu saa mbili. Tulirudi nyumbani wakati giza linaingia, lakini nilibarikiwa na Bwana na tulifurahia upendo Wake. {*EVsw 454:4}*

Novemba 11: Nahofia kwamba nimefanya kazi kupita kiasi. Tangu Sabato nimeandika kurasa themanini na sita za karatasi za barua, na pia kutembelea watu majumbani. Alasiri nilipita kwa Ndugu na Dada H na kuwaachia baadhi ya vitabu. {*EVsw 454:4}*

Novemba 21: Saa nane mchana nilimtembelea Ndugu na Dada H na kusoma baadhi ya mambo niliyokuwa nimeandika ili kusaidia kushughulikia changamoto za kiroho alizokuwa nazo Dada H. {*EVsw 455:1}*

Novemba 27: Leo nilimtembelea Dada K na binti yake. Binti huyo alikuwa amepata ajali hivi karibuni..... Tulizungumza na kuomba naye, na Bwana alijidhihirisha kwa karibu tulipomlilia ambariki mama na binti. {*EVsw 455:2}*

Kisha tulimtembelea Dada G, ambaye ni mjane..... Tulikuwa na kipindi cha maombi pamoja naye, na Roho wa Bwana alitufunika kwa upole wake. Tulizungumza na binti yake wa miaka kama kumi na sita, tukimweleza upendo wa Yesu na kumsihi amkabidhi moyo wake Mwokozi. Nilimwambia kuwa akikubali Kristo kama Mwokozi wake, atakuwa msaada wake katika kila jaribu na atampa amani na pumziko katika upendo Wake. Alionekana kuguswa na maneno yetu. Kisha tulienda tena kwa Ndugu na Dada H. — **Manuscript 21, 1892** {*EVsw 455:3}*

Maeneo Yanayopendwa na kuchukiwa na Mtumishi wa Bwana

Dora Creek, Martinsville, na makazi mengine yaliyoko msituni ambako tuliwahi kufanya kazi ni ya thamani kubwa kwangu. Natumaini kwamba jitihada za upole na huruma kubwa zitaelekezwa kwa roho zilizoko maeneo haya, na kwamba kazi ya bidii ya kuwaleta kwa Kristo itaendelea kufanywa. Mengi yamefanyika huko, na mengi zaidi yatapaswa kufanyika. **— Letter 113, 1902 {*EVsw 455:4*}**

SEHEMU YA 14 — MWALIMU WA BIBLIA

[Kumbuka: "Mwalimu wa Biblia" ni jina lililotumika rasmi kuanzia mwaka 1942 na Kamati Kuu ya Mkutano Mkuu wa Kanisa, likichukua nafasi ya jina la awali "Mtendakazi wa Biblia"—Wachapishaji.]

Kufundisha Biblia Ndilo Kusudi Kuu

Uhitaji wa Uamsho wa Kujifunza Biblia

Uamsho wa kujifunza Biblia unahitajika ulimwenguni kote. Wanadamu wasielekezwe kwenye maoni ya watu, bali kwenye Neno la **Mungu**. Hili likifanyika, kazi kuu itatendeka. **Mungu** aliposema kwamba Neno Lake halitarudi bure, alikusudia kabisa kile alichosema. Injili inapaswa kuhubiriwa kwa mataifa yote. Biblia ni lazima ifunuliwe kwa watu. Kumjua **Mungu** ndiyo elimu ya juu kabisa, na Ukweli Wake utaufunika ulimwengu kama maji yanavyoifunika bahari. —**Manuscript 139, 1898. {*EVsw 456:1*}**

Kazi ya Biblia Imewekwa na Baba wa Mbinguni

Kazi yetu imeelekezwa na Baba yetu wa mbinguni. Tunapaswa kuchukua Biblia zetu na kutoka kuiambia dunia habari ya onyo. Tunapaswa kuwa mikono ya **Mungu** ya kusaidia kuokoa roho—vyombo ambavyo upendo Wake utapita kupitia kwetu kila siku kwa waliopotea. **—Testimonies for the Church, 9:150 (1909). {*EVsw 456:2*}**

Njia Iliyotoka Mbinguni

Mpango wa kuendesha masomo ya Biblia ni wazo lililotoka mbinguni. Wapo wengi, wanaume kwa wanawake, wanaoweza kushiriki katika huduma hii ya kimishenari. Kwa njia hii, watenda kazi wa **Mungu** wanaweza kulelewa na kuwa mashujaa wa kweli wa Bwana. Kupitia njia hii, Neno la **Mungu** limewafikia maelfu; na watenda kazi huingia kwenye mawasiliano ya moja kwa moja na watu wa kila taifa na lugha. Biblia huletwa majumbani, na Kweli Zake takatifu huigusa dhamiri. Watu husihiwa wasome, wachunguze, na waamue wao wenyewe, nao watalazimika kubeba jukumu la kupokea au kukataa nuru ya Kiungu-ya Mwenyezi Mungu. **Mungu** hataruhusu kazi hii ya thamani ifanywe bure. Yeye Atatoa thawabu kwa mafanikio kila juhudi ya unyenyekevu inayofanywa kwa Jina Lake. —**Gospel Workers, 192 (1915). {*EVsw 456:3*}**

Kazi ya Biblia ni Njia ya Kina

Katika kila mji tunaouingia, msingi imara ni lazima uwekwe kwa ajili ya kazi ya kudumu. Mbinu za Bwana ndizo zinazopaswa kufuatwa. Kwa kufanya kazi ya nyumba hadi nyumba, kwa kutoa masomo ya Biblia kwa familia, mtendakazi anaweza kufikia wengi wanaoutafuta Ukweli. Kwa kufungua Maandiko, kwa maombi, kwa kutumia imani, atawafundisha watu njia za Bwana. **—Testimonies for the Church, 7:38 (1902). {*EVsw 457:1*}**

Katika Baadhi ya Maeneo Kazi ya Biblia Inazidi Mikutano ya Hadhara inayoitwa Efoti

Nilionyeshwa mahali ambapo huduma ya hema iliwahi kufanyika. Maandalizi makubwa yalifanyika na gharama ikawa kubwa. Kazi ilifanywa vya kutosha, kiasi cha kuamsha jamii nzima, na kwa namna fulani jamii iliamka; lakini ilikuwa ni kuwaonywa kuhusu makosa hatari ya wale waliokuwa wakihubiri Ukweli. Kingora cha tahadhari kilipigwa, na uongo ukarudiwa tena na tena. Hoja ya kuwazuia watu kuhudhuria ilitumika kwa mafanikio. Watendakazi walikatishwa tamaa kwa sababu watu wachache tu walihudhuria, na ni wachache sana waliokubali kutii Ukweli. **{*EVsw 457:2*}**

Nilionyeshwa tena mahali hapo. Niliwaona watendakazi wawili wa Biblia wakiwa wameketi katika familia moja. Biblia ikiwa wazi mbele yao, walimdhihirisha Yesu Kristo kama Mwokozi msamehe dhambi. Maneno yao yalitamkwa kwa uzima na nguvu. Sala ya dhati ilitolewa kwa **Mungu**, na mioyo ilitiishwa na

kuwa laini na kunyenyekeshwa na ushawishi wa Roho wa **Mungu**. Neno la **Mungu** lilipokuwa likielezwa, niliona mwanga laini kwa macho ukimulika Maandiko, nami nikasema kimyakimya, "Nendeni njiani na mipakani, mkawalazimishe waingie, ili nyumba yangu ijazwe." {*EVsw 457:3}*

Watendakazi hawa hawakuwa wenye kujivuna bali walikuwa wanyenyekevu, wenye mioyo iliyopondeka, wakitambua daima kuwa Roho Mtakatifu Ndiye nguvu yao. Chini ya ushawishi wake wa Kiungu, hali ya kutojali iliondolewa, na hamu ya kweli ikaonekana. Mwanga wa thamani ulienezwa kutoka kwa jirani hadi jirani. Madhabahu za familia zilizokuwa zimebomolewa zilijengwa tena, na wengi waligeukia Ukweli. —**Letter 95, 1896.** {*EVsw 458:1}*

Kufafanua Neno la Mungu

Mahali ulipo, na mahali watu walipo, fanya juhudi ya dhati. Neno la **Mungu** limefichwa kana kwamba li chini ya pishi/debe. Neno hilo lazima lifafanuliwe kwa wale ambao bado hawajui matakwa yake. Chunguza Maandiko pamoja na wale walioko tayari kufundishwa. Kazi hii inaweza kuanza kwa udogo, lakini wengine watajiunga ili kuiendeleza; na kadri juhudi ya dhati ikifanyika kwa imani na kumtegemea **Mungu** ili kuwaangazia watu kuhusu Kweli rahisi za Neno Lake, wale wanaosikiliza watapata maana ya ufuasi wa kweli. **—Letter 30, 1911.** {*EVsw 458:2}*

Watendakazi Binafsi na Washauri wa Hekima

Mfano Wetu Unaathiri Ushauri Wetu

Kwenye kila kipindi kigumu katika maisha ya mtu yeyote, ukijaribu kutoa ushauri au maonyo, maneno yako yatakuwa na uzito wa wem na baraka tu kadri ya mfano na roho uliyoonyesha ulivyo. Lazima uwe mwema kabla ya kutenda mema. Huwezi kuwa na ushawishi wa kuwabadilisha wengine hadi moyo wako uwe umetakaswa, umenyenyekeshwa na kufanywa laini na neema ya Kristo. Mabadiliko hayo yakitendeka ndani yako, basi itakuwa jambo la asili au kawaida kwako kuishi kwa ajili ya kuwabariki wengine, kama ilivyo kawaida kwa ua la waridi kutoa harufu nzuri au mzabibu kuwa na kishada cha matunda ya zambarau. —**Mount of Blessing, uk. 183 (1896).** {*EVsw 458:3}*

Huduma ya Binafsi Katika Kazi ya Biblia

Kuna uhitaji wa kuwakaribia watu kupitia juhudi ya binafsi. Kama muda mdogo ungetumiwa kwa mahubiri, na muda zaidi ukatolewa kwa huduma ya binafsi, matokeo makubwa yangeshuhudiwa. Maskini wanapaswa kusaidiwa, wagonjwa kutunzwa, wanaohuzunika na waliopoteza wapendwa kufarijiwa, wajinga kufundishwa, wasio na uzoefu kushauriwa. Tunapaswa kulia na wanaolia, na kufurahi na wanaofurahi. Tukisindikizwa na nguvu ya ushawishi, maombi, na upendo wa **Mungu**, kazi hii haitakuwa bure. **—The Ministry of Healing, 143-144 (1905).** {*EVsw 459:1}*

Wanawake Kama Wajumbe wa Rehema

Tunawahitaji sana wanawake waliowekwa wakfu ambao, kama wajumbe wa rehema, watawatembelea akina mama na watoto katika nyumba zao, na kuwasaidia katika kazi za kawaida za kila siku kabla ya kuanza kuwahubiria Ukweli wa wakati huu. Kwa njia hii utazipata roho kama matokeo ya huduma yako. **—The Review and Herald, Julai 12, 1906.** {*EVsw 459:2}*

Kuwafikia Watu Kupitia Kuwajali Wagonjwa

Ndugu zangu waume kwa wake, jitoleeni kwa Bwana kwa ajili ya huduma. Msipoteze fursa yoyote. Watembelee wagonjwa na watu wanaoteseka, na waonyeshe upendo wa kweli kwao. Ikiwezekana, fanyeni jambo lolote la kuwafariji na kusaidia mahitaji yao. Kupitia njia hii mnaweza kuifikia mioyo yao, na kusema neno kwa ajili ya Kristo. —**Testimonies for the Church, 9:36 (1909).** {*EVsw 459:3}*

Kuwa Rafiki kwa Familia

Wakina dada wanaweza kufanya mengi kufikia moyo wa mtu na kuufanya laini. Popote mlipo, dada zangu, fanyeni kazi kwa unyenyekevu na usahili. Mkiwa katika nyumba yenye watoto, onyesheni upendo kwao. Hebu na waone kuwa mnawapenda. Kama kuna mgonjwa, toeni msaada wa matibabu; msaidieni mama anayechoka na kuhangaika kwa wasiwasi kumtuliza mtoto wake. **—The Review and Herald, November 11, 1902.** {*EVsw 460:1}*

Watu Huokolewa Binafsi, Sio kwa Makundi

Chumvi lazima ichanganyike na chakula ili kukihifadhi, lazima ipenye ndani ya chakula; vivyo hivyo, ni kupitia mawasiliano ya karibu na ushirika wa binafsi ambapo watu hufikiwa na nguvu ya wokovu wa injili. Hawaokolewi kwa makundi, bali kama watu binafsi. Ushawishi wa binafsi ni nguvu. Lazima tukaribie wale tunaotamani kuwasaidia. **—Mount of Blessing, uk. 59 (1896). {*EVsw 460:2*}**

Uhitaji wa Wanawake Washauri- wa kawaida na wa nasaha

Kama mwanamke yeyote, haijalishi ni nani, anapokuja kwako kuomba huruma [Ujumbe kwa Mwenyekiti wa Konferensi.—Wachapishaji], Je, unapaswa kumpokea na kuanza kubadilishana barua naye kwa hisia ya kuwajibika kumsaidia? Ndugu yangu, unapaswa kubadilika katika jambo hili na kuweka mfano sahihi kwa wachungaji wenzako. Hifadhi huruma yako kwa wanafamilia wako, wanaokuhitaji zaidi na kuhitaji huruma yako. **{*EVsw 460:3*}**

Mwanamke akiwa na shida, hebu na ampelekee mwanamke mwenzake hilo tatizo. Ikiwa ana lalamiko dhidi ya mumewe, asimwendee mchungaji bali amweleze mwanamke mwingine ambaye, ikiwa ni lazima, atazungumza na wewe mchungaji bila ya kuwa na mwonekano mbaya (*appearance of evil). **{*EVsw 460:4*}**

***Yanaonekana kwamba wewe hutambui kwamba mwenendo wako katika jambo hili una ushawishi mbaya. Jihadhari katika maneno na matendo yako.—Barua ya 164, 1902.*—Letter 164, 1902. {*EVsw 461:1*}**

Kazi Kubwa Inayoungwa Mkono na Mbingu

Huduma unayoifanya [Ujumbe kwa mwanamke mwenye uzoefu mkubwa wa hadhara aliyejiunga na Waadventista wa Sabato. —Wachapishaji] ya kuwafanya dada zetu wajisikie kuwajibika binafsi kwa **Mungu** ni kazi nzuri na ya lazima. Kwa muda mrefu kazi hii imepuuzwa. Lakini inapowekwa kwa njia iliyo wazi, rahisi, na ya moja kwa moja, tunaweza kutarajia majukumu ya nyumbani yatatekelezwa kwa ufanisi na akili mahiri zaidi. Bwana angetaka tuendelee kusisitiza thamani ya nafsi ya mwanadamu kwa wale wasiofahamu thamani hiyo. **{*EVsw 461:2*}**

Tukipanga vikundi vya kawaida, vilivyo na mpangilio mzuri, na tukawafundisha kwa hekima wajibu wao kama watumishi wa Bwana, makanisa yetu yatapata uhai kwa nguvu ambayo yameikosa kwa muda mrefu. Thamani ya nafsi iliyookolewa na Kristo itathaminiwa. Kwa kawaida, dada zetu hupitia changamoto nyingi katika kulea familia zao zinazozidi kuongezeka, na huzuni zao hupuuzwa. Nimekuwa na hamu ya kuwa na wanawake watakaofundishwa kuwainua dada hawa kutoka kwenye hali ya kukata tamaa, na kuwafanya waamini kuwa wanaweza kufanya kazi kwa ajili ya Bwana. Hii huleta miale ya jua katika maisha yao wenyewe, ambayo huangaza pia katika mioyo ya wengine. **Mungu** atakubariki wewe na wale wote wanaojiunga nawe katika kazi hii kuu. —**Letter 54, 1899. {*EVsw 461:3*}**

Kuwatafuta Waliopotea

Biblia Kufikishwa Kwenye Kila Mlango — Biblia haifungwi tena. Inaweza kufikishwa mlangoni mwa kila mtu, na kweli zake zinaweza kuwekwa mbele ya dhamiri ya kila mtu. Wapo wengi ambao, kama Waberoya waungwana, wataichunguza Maandiko kila siku wao wenyewe, wakihakikisha Ukweli unapowasilishwa, ikiwa mambo hayo ni kweli. Kristo amesema: "*Yohana 5:39 Mwayachunguza maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia MIMI.*" Yesu, Mkombozi wa ulimwengu, hawaagizi wanadamu wasome tu, bali "**Wachunguze sana Maandiko**." Hii ni kazi kubwa na ya muhimu, na imetolewa kwetu; na tunapoifanya, tutapata faida ya baraka nyingi; kwa kuwa utiifu kwa amri ya Kristo hautakosa malipo. Ataweka alama maalum za kibali Chake juu ya tendo hili la uaminifu wa kufuata nuru iliyofunuliwa katika Neno Lake. **— Counsels on Sabbath School Work, uk. 84 (1889) {*EVsw 461:4*}**

Wengi Wanangojea Wakusanywe — Ulimwenguni kote, wanaume na wanawake wanatazama mbinguni kwa matumaini, kwa macho yaliyokodolewa. Sala, machozi, na maombi hutoka kwa roho zinazotamani nuru, neema, na Roho Mtakatifu. Wengi wapo ukingoni mwa ufalme, wakisubiri tu wakusanywe ndani. **— The Acts of the Apostles, uk. 109 (1911) {*EVsw 462:1*}**

Kuwatafuta Waliopotea — Kazi hii ni kazi inayopaswa kufanywa kwa bidii na kudhamiria. Kondoo waliopotea wamejaa kote maeneo mliyo. Ni jukumu lenu kuwatafuta na kuwaokoa waliopotea. Hawajui jinsi ya kujikomboa au kurejeshwa ili wapone. — **Letter 189, 1899 {*EVsw 462:2*}**

Kupata Fursa za Masomo ya Biblia — Katika kila mji unaoingia, msingi imara unapaswa kuwekwa kwa ajili ya kazi ya kudumu. Mbinu za Bwana zinapaswa kufuatwa. Kwa kufanya kazi nyumba kwa nyumba, kwa kutoa masomo ya Biblia katika familia, mtendakazi anaweza kupata njia ya kuwafikia wengi wanaotafuta Kweli. Kwa kufungua Maandiko, kwa sala, na kwa kuzoeza imani, anapaswa kuwafundisha watu njia za Bwana. **— Testimonies for the Church 7:38 (1902) {*EVsw 462:3*}**

Kuwatafuta Wenye Moyo Yenye Uaminifu — Ninapaswa kufanya kila niwezalo kuwapelekea watu wetu ujumbe kuwa Bwana anao watu waaminifu katika kila mji wetu, na kwamba lazima watafutwe. Bwana hafurahishwi na hali tuliyo nayo. Miji mingi bado haijaguswa kabisa. Wale wanaojihusisha na kazi ya kuwaonya wakazi wa miji mikubwa watapata mafunzo ya jinsi ya kuwaleta watu kwa Kristo.... Je, Watawezaje kuongoka ikiwa Ukweli haujawekwa mbele yao kwa uadilifu na bidii, mstari kwa mstari, amri juu ya amri? ... **{*EVsw 463:1*}**

Watendakazi hawapaswi kupoteza muda wao kwa kurudia rudia mahali ambapo makanisa tayari yameimarishwa katika Kweli, ilhali pande zote kuna wengi ambao hawajawahi kufafanuliwa Kweli. — **Letter 8, 1909 {*EVsw 463:2*}**

Mtendakazi Ataongozwa kwa Wenye Shauku — Nuru, nuru kutoka katika Neno la **Mungu**, —ndicho watu wanahitaji. Ikiwa walimu wa Neno wako tayari, Bwana atawaongoza kuwa karibu zaidi kimahusiano na watu. Yeye Atawaongoza hadi kwenye nyumba za wale wanaohitaji na kutamani Kweli; na watumishi wa **Mungu** wanapojihusisha na kazi ya kuwatafuta kondoo waliopotea, uwezo wao wa kiroho huamshwa na kuchochewa. **— Review and Herald, Desemba 29, 1904 {*EVsw 463:3*}**

Kwa Nguvu Zaidi ya Mara Kumi — Ikiwa nusu ya muda unaotumika sasa katika mahubiri ungetumika katika kazi ya nyumba kwa nyumba, matokeo chanya yangekuwa dhahiri. Mema mengi yangetendeka, kwa kuwa watendakazi wangeweza kuwakaribia watu. Muda unaotumika kwa utulivu kutembelea familia, kuomba, kuimba sifa za **Mungu**, na kufafanua Neno Lake, mara nyingi huleta matokeo makubwa kuliko jitihada za hadharani. Mara nyingi akili huathiriwa kwa nguvu zaidi mara kumi kwa njia ya mafundisho ya ana kwa ana kuliko kwa namna nyingine yoyote. Familia inayotembelewa kwa njia hii huzungumziwa moja kwa moja. Wanafamilia hawapo katika mkusanyiko mchanganyiko ambapo wanaweza kuyaelekeza kwa wengine yale wayasikiayo. Hawa huzungumziwa moja kwa moja, kwa dhati, ari na kwa huruma ya upendo. Wanaruhusiwa kuonyesha pingamizi zao kwa uhuru, na kila pingamizi linaweza kushughulikiwa kwa “asema Bwana.” Ikiwa kazi hii itafanyika kwa unyenyekevu, na na mioyo iliyojaa upendo wa **Mungu**, maneno haya yatatimia: “Kuingia kwa Maneno Yako huleta nuru; humpa mwenye moyo wa kawaida ufahamu.” — **Letter 95, 1896 {*EVsw 463:4*}**

Wengine Huonekana kuwa wagumu kukaribiwa — Wanaofanya kazi kwa ajili ya **Mungu** watakutana na watu wanaoonekana kuchukizwa unapowakaribia au unapojaribu kuwafikia. Wanaweza kudhani kuwa mnaamua kuingilia faragha ya imani yao na ibada yao, na hawaonyeshi uso wa neema kwa wale wanaoshirikiana na **Mungu** katika kazi. Watendakazi hawa lazima waondoe macho yao ya kimwili katika kujitazama wao binafsi, na kumtazama Yesu, wakitilia maanani kwa uangalifu maelekezo yaliyo katika Neno Lake. **— Letter 5, 1896 {*EVsw 464:1*}**

Wanawake Katika Uinjilisti

Katika Wakati Huu wa Mgogoro — Bwana anao mpango na wanawake kama aliyonayo kwa wanaume. Wanaweza kuchukua nafasi zao katika kazi Yake wakati huu wa dharura, Naye Atawatumia. Ikiwa wamejazwa na hisia ya wajibu wao, na wakifanya kazi kwa uongozi wa Roho Mtakatifu, watakuwa na ile utulivu wa ndani unaohitajika kwa wakati huu. Mwokozi atawamulikia nuru ya uso Wake wanawake hawa wanaojitoa, na atawapa nguvu inayozidi ile ya wanaume. Wanaweza kufanya kazi katika familia ambayo wanaume hawawezi kuifanya, kazi inayogusa maisha ya ndani. Wanaweza kuifikia mioyo ambayo wanaume hawawezi kufikia. Kazi yao inahitajika. — **Review and Herald, August 26, 1902 {*EVsw 464:2*}**

Wanawake Walio na Kazi Moyoni — Wanawake walioweka kazi ya **Mungu** moyoni mwao wanaweza kufanya kazi nzuri katika maeneo wanamoishi. Kristo anazungumzia wanawake waliomsaidia kuwasilisha Kweli kwa wengine, na Paulo pia anazungumzia wanawake waliomsaidia katika injili. Lakini kazi inayofanyika na wanawake walio na uwezo bado ni ndogo sana. **— Letter 31, 1894 {*EVsw 465:1*}**

Wanawake Wanaohisi Mzigo Kwa Ajili ya Roho— Nimewaza kuwa, kwa uzoefu wenu, chini ya uongozi wa **Mungu** mnaweza kutumia ushawishi wenu kuanzisha njia za kazi ambapo wanawake wanaweza kushirikiana kwa pamoja katika kazi ya Bwana. Bila shaka kunapaswa kuwa na idadi kubwa ya wanawake wanaojihusisha katika kazi ya kuwahudumia wanadamu wanaoteseka, kuwainua, kuwaelimisha jinsi ya kuamini—tu kuamini kwa usahili—katika Yesu Kristo Mwokozi wetu. Na roho zinapojitoa kwa Yesu, wakifanya kujitoa kuwe na ukamilifu, wataelewa mafundisho.... {*EVsw 465:2}*

Ninasikitika kwa kuwa dada zetu huko Marekani ambao hawafanyi kazi ambayo wangeweza kuifanya kwa ajili ya Bwana Yesu. Wakiwa ndani ya Kristo, wangepokea ujasiri, nguvu, na imani kwa kazi hiyo. Wanawake wengi wanapenda kuongea. Mbona basi wasizungumze maneno ya Kristo kwa nafsi zinazopotea? Kadiri tunavyokaribia zaidi kwa Kristo, ndivyo moyo unavyojifunza hali ya kutisha ya roho zisizomjua **Mungu**, na ambazo hazihisi aibu wanayomletea Kristo aliyewanunua kwa gharama. {*EVsw 465:3}*

Wakati wanawake waamini watakapohisi mzigo wa roho, na mzigo wa dhambi zisizo zao wenyewe, watafanya kazi kama Kristo alivyofanya. Hawataona kuwa kuna sadaka yoyote kubwa mno ya kutolewa ili kuwaleta roho kwa Kristo. Na kila mmoja anayependa roho kwa namna hiyo, amezaliwa na **Mungu**; Yuko tayari kufuata nyayo Zake, na maneno yao na sauti yao zitakuwa vipawa vilivyotolewa kwa ajili ya huduma ya Bwana; lishe ile ile kutoka kwa Shina kuu kwa nafsi yao itaendelea kutiririka katika njia tofauti tofauti za upendo kwa roho zilizokauka na kunyauka. {*EVsw 465:4}*

Katika kazi hii kuna elimu endelevu. Tamaa ya kuwa baraka humpeleka mtendakazi kugundua udhaifu na upungufu wake. Hii humpeleka kwa **Mungu** kwa maombi, na Bwana Yesu huwapa nuru na Roho Wake Mtakatifu, nao huelewa kuwa ni Kristo anayevunja na kuyeyusha mioyo migumu. —**Letter 133, 1898** {*EVsw 466:1}*

Wanahitajika Katika Matawi Mbalimbali ya Kazi — Katika matawi mbalimbali ya kazi ya **Mungu**, kuna uwanja mpana ambao dada zetu wanaweza kuitumikia kazi ya Bwana. Njia nyingi za kazi ya kimishenari zimepuuzwa. Katika makanisa mbalimbali, kuna kazi nyingi ambazo mara nyingi huelezwa kama zisizofanyika au kufanywa kwa kiwango cha chini, lakini kwa msaada wa kina mama, kama wangefunzwa ipasavyo, zingefanyika vizuri. Kupitia njia mbalimbali za kazi ya kimishenari ya nyumbani wanaweza kuwafikia tabaka watu ambao wahubiri wetu hawawafikii. Miongoni mwa wanawake waungwana na bora waliothubutu kuamua kuufuata Ukweli wa wakati huu wapo waliokuwa na busara, upeo, na uwezo mzuri, na wanaweza kuwa watendakazi wenye mafanikio. Kazi ya wanawake wa Kikristo kama hao inahitajika. — **Review and Herald, Desember 10, 1914** {*EVsw 466:2}*

Sehemu ya Wanawake Katika Uinjilisti — Katika kazi mbalimbali za nyumbani za kimishenari, mwanamke mnyenyekevu, mwungwana, anayejistahi na mwenye maarifa anaweza kutumia uwezo wake kwa kiwango cha juu kabisa. Ni nani anayeweza kuwa na upendo wa kina kwa nafsi za wanaume na wanawake ambao Kristo amekufa kwa ajili yao kama wale wanaoshiriki neema Yake? Ni nani anayeweza kuonyesha ileKweli na mfano wa Kristo vizuri zaidi kuliko wanawake wa Kikristo wanaoishi wenyewe ile Kweli? — **Review and Herald, Desember 10, 1914** {*EVsw 466:3}*

Kama Mshauri, Rafiki na Mtendakazi Mwenza — Mwanamke, akitumia vyema na kwa busara muda na uwezo wake wa vitivyo vyote, akimtegemea **Mungu** kwa hekima na nguvu, anaweza kusimama sawasawa na mumewe kama mshauri, rafiki, na mtendakazi mwenza, na bado asipoteze utu wake wa kike, staha, uungwana au unyenyekevu wake. Anaweza kuinua tabia yake mwenyewe, na kadiri anavyoifanya, ndivyo anavyoinua na kuboresha tabia za familia yake, na kueneza ushawishi mkubwa, bila hata mwenyewe kugundua, kwa watu waliomzunguka. Kwa nini wanawake wasikuze akili zao? Kwa nini wasitimize kusudi la **Mungu** katika maisha yao? Kwa nini wasielewe uwezo wao wenyewe, na wakijua kuwa uwezo huo umetoka kwa **Mungu**, basi wajitahidi kuutumia kikamilifu kwa ajili ya kuwafanyia wengine mema, kusukuma mbele kazi ya matengenezo, na Kweli na wema halisi duniani? Shetani anajua kuwa wanawake wana nguvu kubwa ya ushawishi kwa mema au kwa maovu; kwa hiyo huwajaribu kuwavuta kujiunga na kazi yake. **— Good Health, June 1880** {*EVsw 467:1}*

Nguvu ya Maisha Yanayoambatana na Kweli — Wa ajabu ni utume wa wake, mama, na wanawake wachanga wanaofanya kazi. Ikiwa watataka, wanaweza kuwa na ushawishi mkubwa wa mema kwa wote waliowazunguka. Kwa unyenyekevu katika mavazi yenye staha na mwenendo ulio wa tahadhari, wanaweza kuwa mashahidi wa Kweli kwa njia ya maisha yao ya unyenyekevu na usahili. Wanaweza kuangaza nuru yao mbele ya watu wote, hadi wengine waone matendo yao mema na kumtukuza Baba yao aliye mbinguni. Mwanamke aliyeongoka kweli atakuwa na ushawishi mkubwa wa kubadilisha maisha kwa mema. Akiwa ameunganishwa na mumewe, anaweza kumsaidia katika kazi yake, na kuwa chanzo cha kutia moyo na

baraka kwake. Wakati mapenzi na njia yake vinapoletwa chini ya Roho wa **Mungu**, hakuna kikomo kwa mema yatakayofanyika. **— Manuscript 91, 1908 {*EVsw 467:2*}**

Wabeba Mizigo kwa Ajili ya Yesu — Dada zetu, vijana, watu wa makamo, na hata waliozeeka, wanaweza kushiriki katika kazi ya mwisho ya wakati huu; na wanapofanya kazi hii kadiri nafasi inavyopatikana, watapata uzoefu wenye thamani kubwa sana kwao wenyewe. Kwa kujisahau nafsi, watakua katika neema. Kwa kuufundisha akili katika mwelekeo huu, watajifunza jinsi ya kubeba mizigo kwa ajili ya Yesu. **— Review and Herald, January 2, 1879 {*EVsw 468:1*}**

Wale Wafanyao Kazi Nyumbani — Wale wanaowaajiri wanaume au wanawake kusaidia katika kazi za nyumbani wanapaswa kuwapa mshahara wa haki. Na wanapaswa pia kuwathamini kwa haki. Wasiwaache wafikiri kuwa uaminifu wao katika kazi hautambuliwi au kuthaminiwa. Kazi yao ni muhimu kama kazi ya wale wanaotoa masomo ya Biblia, na wanapaswa kupokea maneno ya kuthaminiwa. Mara nyingi wanatamani huruma na moyo wa kuonewa huruma, na hili halipaswi kunyimwa kwao, kwa kuwa wanastahili. **{*EVsw 468:2*}**

Wale wanaopika na kufanya kazi nyingine za nyumbani wanahusika sawasawa na huduma ya **Mungu** kama wale walio katika kazi ya Biblia. Na wao wanahitaji zaidi huruma na faraja; kwa kuwa katika kazi za kiroho kuna kitu kinachopandisha moyo, kuutia nguvu, na kufariji. Na kumbuka, sote ni watumishi. Yule anayefanya kazi za nyumbani si mdogo machoni pa Bwana kuliko yule anayetoa masomo ya Biblia. — **Manuscript 128, 1905 {*EVsw 468:3*}**

Wanaume na Wanawake Walioitwa kwa Kazi ya Kufundisha Biblia

Kuunganisha Vipawa kwa Ajili ya Kazi ya Maamuzi

Wakati kazi kuu na ya uamuzi inapaswa kufanyika, **Mungu** huchagua wanaume na wanawake kutekeleza kazi hiyo, na kazi hiyo itapungukiwa sana iwapo vipawa vya jinsia zote mbili havitaunganishwa. — **Letter 77, 1898. {*EVsw 469:1*}**

Wanawake kama kwa wanaume wanaweza kushiriki katika kazi ya kuuficha Ukweli ambapo unaweza kufanikiwa na kudhihirishwa. **—Testimonies For The Church 9:128 (1909). {*EVsw 469:2*}**

Baadhi ya Wanawake Kuasiliwa kwa Kazi ya Biblia

Kuna wanawake walio na kipawa maalum cha kazi ya kutoa mafundisho ya Biblia, na wamefanikiwa sana katika kuwasilisha Neno la **Mungu** kwa urahisi kwa wengine. Wanakuwa baraka kubwa katika kuwafikia kina mama na mabinti zao. Hii ni kazi takatifu, na wale wanaoshiriki wanapaswa kutiwa moyo. — **Letter 108, 1910. {*EVsw 469:3*}**

Wanawake Wasio wazungu, weusi nk Walioitwa kwa Kazi

Hivi karibuni, mahitaji ya eneo hili yamenielemea sana kiasi cha kuninyima usingizi, nimelala masaa chache sana. Kazi ya umishenari tiba inapaswa kufanyika miongoni mwa watu hawa [weusi], ambao wanapaswa kufundishwa uuguzi, upishi, na kazi zingine muhimu. Kuna baadhi yao wanaopaswa kufundishwa kuwa walimu, watendaji wa kazi ya Biblia, na wasambazaji wa machapisho. — **Letter 221, 1904. {*EVsw 469:4*}**

Wanaume Wasio wazungu, au Weusi Wafundishwe

Wanaume weusi wanapaswa kufundishwa na kuelimishwa kikamilifu ili waweze kutoa mafundisho ya Biblia na kufanya mikutano ya hema miongoni mwa watu wao. Kuna wengi wenye uwezo ambao wanapaswa kuandaliwa kwa ajili ya kazi hii. —**Testimonies For The Church 9:207 (1909). {*EVsw 469:5*}**

Mafundisho ya Biblia Kutolewa na Wanaume Wenye Ufahamu wa Kiroho

Mioyo imeguswa, na nafsi zimeongoka, wakati mmekuwa mkihubiri kweli kuu za Biblia—Kweli za neema ya Kristo. Sasa ni muhimu kuungana nanyi katika kazi hii wanaume wenye ufahamu wa kiroho, ambao watashirikiana nanyi na wakati wa mchana kutoa mafundisho ya Biblia kwa waongofu wapya, wakiwaeleza jinsi ya kujisalimisha kwa Roho Mtakatifu, ili wapate kuthibitishwa na kuimarishwa katika Kweli. Wanahitaji mafundisho binafsi ya moja kwa moja katika masuala mengi. **— Letter 376, 1906. {*EVsw 470:1*}**

Kuwafundisha Wanaume na Wanawake Kazi ya Biblia

Mzee na Bi. Haskell walikuwa wakitoa mafundisho ya Biblia kila asubuhi, na mchana na wale waliokuwa katika mafunzo walikuwa wakitembelea nyumba kwa nyumba. Ziara hizi za kimishenari na uuzaji wa vitabu na machapisho vilifungua njia ya kufanya mafundisho ya Biblia. Takribani wanaume na wanawake arobaini walihudhuria masomo ya asubuhi, na wengi wao walijihusisha na kazi ya mchana. — **Review and Herald, November 29, 1906. {*EVsw 470:2*}**

Mtembeleaji watu Kwaajili ya Injili

Walimu wa Biblia na Watandaaji

Kuna wale wenye uzoefu fulani ambao, katika kila jitihada wanayofanya kwa makanisa yaliyokufa pamoja na maeneo mapya, wanapaswa kuchagua vijana au watu waliokomaa kuwasaidia katika kazi hiyo. Kwa njia hii, watapata maarifa kwa kushiriki katika juhudi za kibinafsi, na makumi ya wasaidizi wataandaliwa kuwa walimu wa Biblia, wauzaji vitabu vya injili, wasambazaji wa vitabu, Wake wanaozuru watu ili kushiriki injili nao na watandaaji wa familia. **— Letter 34, 1886. {*EVsw 470:3*}**

Vijana Walioitwa kama Watandaaji wa Injili

Kuna njia nyingi ambazo vijana wanaweza kujihusisha kwa ufanisi. Makundi yanapaswa kuundwa na kufundishwa kikamilifu kufanya kazi kama wauguzi, watu wanaozuru kwaajili ya injili=watandaaji wa injili, walimu wa Biblia, wasambazaji wa vitabu, wahubiri, na wainjilisti wa umishenari wa tiba. **—Counsels to Parents, Teachers, and Students, 546 (1913). {*EVsw 471:1*}**

Wanawake Kutembelea Watu

Wanawake wanaweza kufanya kazi nzuri kwa **Mungu** endapo watajifunza kwanza somo la thamani la unyenyekevu katika shule ya Kristo. Wataweza kuwasaidia wanadamu kwa kuwaeleza utoshelevu wa Yesu... **{*EVsw 471:2*}**

Wengi wanaoamniwa na kazi ya kawaida kwa ajili ya Bwana hujihisi kutotosheka, wakifikiri wanapaswa kuwa walimu na viongozi. Wanataka kuacha huduma yao ya unyenyekevu, ambayo ni muhimu sana kwaajili ya majukumu kazi kubwa zaidi. Wale waliowekwa kwa kazi ya kutembelea wengine huanza kufikiri kwamba yeyote anaweza kufanya kazi hiyo—kwamba yeyote anaweza kusema maneno ya faraja na matumaini, huruma na kuwaongoza watu katika njia ya kuelewa Maandiko kwa njia tulivu na unyenyekevu ili watu wa. Lakini ni kazi inayohitaji neema nyingi, uvumilivu mwingi, na hazina ya kila mara ya hekima... ….**{*EVsw 471:3*}**

Hakuna kazi yoyote inayofanywa kwa ajili ya Bwana inayopaswa kuchukuliwa kuwa ya chini au isiyo na thamani... Ikiwa inafanywa kwa furaha, kwa unyenyekevu, na kwa unyenyekevu wa Kristo, italeta matokeo utukufu kwa **Mungu**. **— Letter 88, 1895. {*EVsw 471:4*}**

Wanawake Katika Huduma ya Umma

Ufanisi wa Kazi ya Wanawake

Wanawake wanaweza kuwa vyombo vya haki, wakitoa huduma takatifu. Mariamu ndiye aliyekuwa wa kwanza kuhubiri kuhusu Yesu aliyefufuka..... Kama kungekuwa na wanawake ishirini badala ya mmoja, waliotenga kazi hii takatifu kuwa huduma yao ya thamani, tungeshuhudia wengi zaidi wakiongoka kwa Kweli. Ushawishi wa upole, uliotakaswa na usafi wa wanawake wa Kikristo unahitajika sana katika kazi kuu ya kuhubiri Kweli. — **Review and Herald, January 2, 1879. {*EVsw 471:5*}**

Mume na Mke Katika Kazi ya Pamoja

Kuna wanawake wanaopaswa kufanya kazi katika huduma ya injili. Kwa hali nyingi wanaweza kufanya kazi bora kuliko wachungaji wanaopuuzia kuwatembelea kondoo wa **Mungu**. — **Manuscript 43a, 1898. {*EVsw 472:1*}**

Hekima Inahitajika Katika Kuchagua Walimu wa Injili

Wanapaswa kuchaguliwa kwa kazi hii wanaume wenye hekima na waliojiwekwa wakfu, ambao wanaweza kufanya kazi nzuri katika kuzfikia roho. Wanawake pia wanapaswa kuchaguliwa ambao wanaweza kuwasilisha Kweli kwa njia iliyo wazi, yenye akili mahiri na yenye kueleweka. Tunahitaji watendakazi wanaotambua haja ya kazi ya kina ya neema moyoni; na watu wa namna hiyo wanapaswa kutiwa moyo kushiriki katika kazi ya kimishenari. Kwa muda mrefu kumekuwepo na uhitaji wa watendakazi wa aina hii. Tunapaswa kuomba kwa bidii: "Bwana, tusaidie kusaidiana sisi kwa sisi." Nafsi-ubinafsi unapaswa kufa pamoja na Kristo, na lazima tubatizwe kwa Roho Mtakatifu wa **Mungu**. Ndipo matendo yetu, roho yetu, na namna ya kazi yetu itaonyesha wazi kuwa Roho wa **Mungu** Ndiye anayetuongoza. {*EVsw 472:2}*

Tunahitaji wanaume na wanawake kama watendakazi, wanaoelewa sababu ya imani yetu, wanaotambua kazi iliyopo ya kuwasilisha Kweli, na ambao hawatasema chochote kinachoweza kudhoofisha imani ya mtu yeyote katika Neno la **Mungu** au kuharibu ushirika wa waumini wa imani moja. **— Letter 54, 1909. {***EVsw 472:3}*

Mwalimu wa Biblia Kuhutubia Mkutano

Kila wiki inaeleza kisa chake; roho moja au mbili hupokea Kweli, na mabadiliko ya ajabu katika sura zao na tabia zao huonekana waziwazi na majirani, kiasi kwamba maisha yao huwashawishi wengine wapokee Kweli; na sasa wanachunguza Maandiko kwa bidii…….. {*EVsw 472:4}*

Dada R na Dada W wanafanya kazi kwa mafanikio sawa na wahubiri; na katika baadhi ya mikutano ambapo wahubiri wote wameitwa sehemu nyingine, Dada W huchukua Biblia na kuhubiri mbele ya mkutano. — **Letter 169, 1900. {***EVsw 473:1}*

Dada Kuwahubiria Umati

Tunaamini kikamilifu katika mpangilio wa kanisa (church organization, lakini si kwa jambo lolote linaloweka njia ya lazima ya jinsi tunavyopaswa kufanya kazi; kwa kuwa akili zote hazifikiwi kwa njia moja……. {*EVsw 473:2}*

Kila mtu ana taa yake mwenyewe ya kuendelea kuangaza…... Mwanga mwingi zaidi huangaza kutoka katika taa moja tu kwa ajili ya mtembea njia anayetangatanga, kuliko mwanga wa gwaride la maandamano ya mwangaza mkubwa wenye maonyesho na heshima. Ee, hivi ni kazi kubwa inayoweza kufanyika kama sisi tutajinyumbulisha kupita kiwango chetu! {*EVsw 473:3}*

Fundisha jambo hili, dada yangu. Una njia nyingi zilizo wazi mbele yako. Hubiria umati kila unapoweza; tumia kila nafasi uliyo nayo ili kueneza chachu ndani ya unga. Kila mwanamume na mwanamke ana kazi ya kufanya kwa ajili ya Bwana-Mwalimu. Kujitolea kibinafsi na kutakaswa kwa **Mungu** kutaleta matokeo makubwa kwa njia rahisi kuliko onyesho lolote la ajabu. — **Review and Herald, May 9, 1899. {***EVsw 473:4}*

Darasa la Biblia Kwenye Kambi Linaloendeshwa na Wanawake

Mikutano yetu ya kambi inapaswa kuendeshwa kwa namna ambayo itakuwa shule kwa ajili ya kuelimisha watendakazi. Tunahitaji kuelewa vizuri zaidi kuhusu mgawanyo wa kazi, na kufundisha wote jinsi ya kushughulikia kila sehemu ya kazi kwa mafanikio……. Hebu Mahubiri mafupi yatolewe, kisha madarasa ya Biblia yaandaliwe. Mzungumzaji ahakikishe kuwa Kweli imejikita akilini mwa wasikilizaji. Wanawake werevu, ikiwa wameongoka kweli, wanaweza kushiriki katika kazi hii ya kuendesha madarasa ya Biblia. Kuna uwanja mpana wa huduma kwa wanawake kama ilivyo kwa wanaume. — **Letter 84, 1910. {***EVsw 473:5}*

Mafunzo na Usuli

Thamani ya Watendakazi Waliofunzwa Vizuri

Mungu anawaita watendakazi, lakini anataka wale walio tayari kujinyenyekeza kwa mapenzi Yake na kufundisha Kweli kama ilivyo katika Yesu. Mtendakazi mmoja aliyeelimishwa na kufunzwa vizuri, na ambaye anatawaliwa na Roho wa Kristo, atafanya kazi zaidi ya watendakazi kumi walio na upungufu wa maarifa na dhaifu katika imani. Mmoja anayefanya kazi kwa mshikamano na ushauri wa **Mungu**, na kwa umoja na ndugu zake, atakuwa na ufanisi mkubwa kuliko kumi ambao hawatambui haja ya kumtegemea **Mungu** na kutenda kwa mpango wa kazi uliopangwa kwa jumla. —**The Review and Herald, May 29, 1888. {***EVsw 474:1}*

Watendakazi wa Biblia Kutoka Shule Zetu

Katika kila shule aliyoiinua **Mungu**, kutakuwa na haja kubwa ya mafundisho ya Biblia kama ambavyo haijawahi kutokea. Wanafunzi wetu wanafaa kufundishwa ili kuwa watendakazi wa Biblia, na walimu wa Biblia wanaweza kufanya kazi ya ajabu ikiwa wao wenyewe watajifunza kutoka kwa Mwalimu Mkuu. {*EVsw 474:2}*

Neno la **Mungu** ndilo falsafa ya Kweli, sayansi ya Kweli. Maoni ya kibinadamu na mahubiri ya msismko yana faida ndogo sana. Wale waliotiwa nguvu na Neno la **Mungu** wanaweza kulifundisha kwa njia rahisi kama vile Kristo alivyolifundisha. Mengi yanategemea kufungua Maandiko kwa wale walioko gizani, hivyo hatupaswi kutumia hata neno moja gumu kueleweka. {*EVsw 474:3}*

Watendakazi wanahitajika ambao watawakaribia wale wasioamini, na wasingoje mpaka watu wasioamini wawakaribie wao. Wanapaswa kuwatafuta kondoo waliopotea, kufanya kazi ya binafsi, na kutoa mafundisho wazi, bainishi na ya kueleweka. {*EVsw 474:4}*

Malengo ya shule zetu yanapaswa kuwa kutoa mafundisho bora kwa ajili ya kazi ya Biblia. Mikutano yetu inapaswa kuhakikisha kwamba shule zinafundishwa na walimu waliokomaa katika Biblia na walio na uzoefu wa kiroho wa kina. Vipawa bora kabisa vya kazi ya uchungaji vinapaswa kuletwa shuleni. —**Manuscript 139, 1898.** {*EVsw 475:1}*

Elimu Pana Inayojumuisha Kazi ya Biblia

Bwana anapenda shule zetu ziwe sehemu ya mafunzo ya kazi kwaajili ya wanawake—mapishi, kazi za nyumbani, ushonaji nguo, uhasibu, usomaji sahihi na matamshi. Wanawake waandaliwe kushika nafasi yoyote yenye pengo—wasimamizi, walimu wa shule ya Sabato, watendakazi wa Biblia. Wawe tayari kufundisha shule za kutwa kwa watoto. **—Letter 3, 1898.** {*EVsw 475:2}*

Watendakazi Wenye Uzoefu, Si Watoto (Wavulana na Wasichana)

Kazi ya huduma ya kiroho haiwezi kuwa chini ya wavulana wanaoaminiwa, wala kazi ya kutoa mafundisho ya Biblia isiwe chini ya wasichana wasio na uzoefu, hata kama wako tayari kutoa huduma na kubeba nafasi za uwajibikaji. Bila kuwa na uzoefu wa kiroho, elimu ya kina na mafunzo sahihi, hawatawakilisha kazi yetu kwa usahihi. *Lazima wathibitishwe ili kuona kama watastahimili mtihani; na isipokuwa kama kutakuwa na kanuni thabiti na ya dhamiri iliyoandaliwa kuwa yote ambayo Mungu angependa wawe, hawatawakilisha kwa usahihi kusudi la kazi yetu kwa wakati huu.*{*EVsw 475:3}*

Lazima dada zetu walio kwenye kazi utume wawe na uzoefu wa kina, waliojifunza kutoka kwa watu wenye uzoefu waliotangulia na wanaojua namna na tabia ya kufanya kazi. Kazi ya umishenari daima hukumbwa na changamoto ya kuaibishwa kila mara kwa kukosa watendakazi wa aina sahihi inayohitajika, wenye akili inayofaa na uchaji Mungu wa Kweli ambao utawakilisha imani yetu kwa usahihi. —**Christian Education, uk. 45-46 (1894).** {*EVsw 475:4}*

Kazi Inahitaji Akili Mahiri

Vijana hawapaswi kuanza kufundisha Maandiko na kutoa mafundisho ya unabii bila kuwa na maarifa ya Kweli ya Biblia. Ikiwa wamepungukiwa na elimu ya msingi, hivyo watashindwa kufanya yale ambayo wangeweza kufanya wakiwa na elimu bora. Kutojua hakumuongezei mtu unyenyekevu wala uaminifu wa kiroho. Kweli za Neno la **Mungu** zinaeleweka na kuthaminiwa vyema zaidi na MKristo mwenye akili timamu. Kristo anatukuzwa zaidi na wale wanaomtumikia kwa akili. Lengo kuu la elimu ni kutumia uwezo wetu kwa njia itakayoonyesha dini ya Biblia na kumtukuza **Mungu**. **—Testimonies for the Church, 3:160 (1872).** {*EVsw 476:1}*

Watendakazi Waliofunzwa kwa Kina

Malaika wa tatu anaonyeshwa akiruka katikati ya mbingu, akiashiria kuwa ujumbe unapaswa kuenea ulimwenguni kote duniani, kwa mapana na marefu. Huu ni ujumbe mzito kuliko yote kuwahi kutolewa kwa wanadamu. Wote wanaojiunga na kazi hii lazima kwanza watambue haja ya elimu na mafunzo ya kina-

kamili, kwa ajili ya mafanikio ya baadaye na kuwa watu wenye kunufaisha. Lazima kuwe na mipango ya kuboresha kundi hilo linalokusudia kuingia katika tawi lolote la kazi. —**The Review and Herald, June 21, 1887** {*EVsw 476:2}*

Mwalimu Lazima Ajue Kanuni Halisi za Kweli

Hakikisha unazijua kanuni halisi za ile Kweli; na kisha utakapo kutana na wapinzani, haitakuwa kwa nguvu zako mwenyewe, bali malaika wa **Mungu** atasimama kando yako, kusaidia kujibu kila swali. Kila siku jifunike kwa Yesu, na maneno na mfano wako vitakuwa na mvuto na matokeo makubwa kwa ajili ya wokovu. **—Gospel Workers, uk. 105 (1915).** {*EVsw 476:3}*

Wito kwa Walimu Zaidi wa Biblia Walioelimika

Napenda kuanzisha mfuko wa kuwalipa wanawake wacha **Mungu** wanaofanya kazi bora katika kutoa mafundisho ya Biblia. Pia nasisitiza kuwa tunapaswa kuelimisha watendakazi zaidi kwa ajili ya huduma hii ya kufundisha Biblia. **—Letter 83, 1899.** {*EVsw 477:1}*

Sifa za Mwalimu wa Biblia

Ubora wa Wanawake Katika Kazi ya Mungu

Wanawake wa kanuni imara na tabia thabiti wanahitajika, wanawake wanaoamini kwamba tunaishi katika siku za mwisho na kwamba tunao ujumbe wa mzito wa mwisho, kuonya kwa dunia. Wanatambua kuwa wameitwa kueneza nuru ya mbinguni waliopewa. Hakuna litakalowazuia kutimiza kazi yao. Wana imani na uthabiti wa kufanya kazi kwa ajili ya wakati huu na wa milele. Wanamcha **Mungu** na hawawezi kushawishiwa kutoka kwenye njia kwa pesa wala tamaa za maisha. Sabato ya amri ya nne wanaishika kwa utakatifu kwa sababu **Mungu** ameifanya takatifu. Hawa ndio wanaoiwakilisha imani yetu kwa usahihi, na maneno yao yatakuwa kama “tofaha za dhahabu katika vyombo vya fedha.” Dada zangu, **Mungu** anawaita mfanye kazi katika shamba Lake, mkisaidia kuvuna miganda ya nafaka. **—The Review and Herald, Desember 19, 1878.** {*EVsw 477:2}*

Nguvu Changamfu na Isiyo Lemavu

Ili kazi ya **Mungu iende mbele katika matawi yake yote, Mungu anatoa wito kwa** nguvu za ujana, bidii, ari na ujasiri. **Mungu** amewachagua vijana kusaidia kuendeleza kazi Yake, kupanga na kufikiria kwa akili wazi, umakini na kutenda kwa ujasiri kunahitaji nguvu mpya zisizolemazwa. Vijana wa kiume na wa kike wanakaribishwa kumtolea **Mungu** nguvu za ujana wao, ili kupitia utumiaji wa nguvu zao, mawazo makini na hatua kali waweze kumletea utukufu Mungu na wokovu wa wanadamu wenzao. —**Counsels to Parents, Teachers, and Students, uk. 535 (1913).** {*EVsw 478:1}*

Kuna uhitaji wa vijana wa kiume na wa kike ambao hawatayumbishwa na hali, wanaotembea na **Mungu**, wenye maombi mengi, wanaojitahidi sana kukusanya nuru yote wanayoweza. —**Counsels to Parents, Teachers, and Students, 537 (1913).** {*EVsw 478:2}*

Wote wanaofanya kazi kwa ajili ya **Mungu** wanapaswa kuwa na sifa za Martha na Mariamu zilizochangamana pamoja-- utayari wa kuhudumu na upendo wa dhati wa ile Kweli. Nafsi/Ubinafsi na uchoyo ni lazima viondolewe machoni. **Mungu** anawaita wanawake wafanyao kazi kwa dhati na bidii, wafanya kazi walio na busara, wachangamfu, wapole, wenye moyo laini, wacheshi, wenye moyo wa kirafiki na waaminifu kwa kanuni. Anawaita wanawake wavumilivu ambao watachukua akili zao kutoka kwa nafsi na urahisi wao binafsi, na kuziweka kwa Kristo, wakisema maneno ya Ukweli, wakiomba pamoja na watu ambao wanaweza kupata ufikiaji, wakijitahidi kufanya kazi kwaajili ya uongofu wa roho. **—Testimonies For The Church 6:118 (1900).** {*EVsw 478:3}*

Wanawake Wenye Uwezo wa Kufanya Maamuzi Sahihi

Kuna wanawake wakuu au maarufu ambao wamekuwa na ujasiri wa kimaadili wa kuamua kuunga mkono Ukweli kutokana na uzito wa Ushahidi. Wamekubali Ukweli kwa dhamiri zao. Wana busara, utambuzi,

na uwezo mzuri, na watakuwa ni watendakazi wenye mafanikio kwa Bwana wao. Wanawake wa Kikristo wanahitajika. **—The Review and Herald, December 19, 1878.** {*EVsw 478:4}*

Nguvu ya Tabia na Nguvu ya Mvuto

Baadhi ya wanaoshiriki katika huduma ya umishenari ni dhaifu, hawana hisia zozote, hawana nishati, hawana ujasiri, na wanavunjika moyo kirahisi. Wanakosa msukumo. Hawana sifa chanya za tabia zinazowapa uwezo wa kufanya jambo fulani—hawana roho na nishati inayotia joto matamanio yao au inayowasha moto wa usongo. Wale ambao wangejitwalia mafanikio, ni lazima wawe na ujasiri na matumaini. Hawa wanapaswa kustawisha sio tu sifa tulivu zisizoonekana au zisizo na sauti, bali pia sifa za utendaji hai. Ingawa wanapaswa kutoa jibu laini ambalo hugeuza hasira, lakini ni lazima pia wawe na ujasiri wenye ushujaa unaosaidia kuupinga uovu. Wakiwa tayari na upendo unaostahimili mambo yote, wanahitaji msukumo wa tabia ambao utafanya mvuto wao kuwa na nguvu chanya. **—The Ministry of Healing, uk. 497-498 (1905).** {*EVsw 479:1}*

Uwezo wa Kuchambua Kwa Kina

Kama umeitwa kuwa mwalimu katika kazi yoyote ya **Mungu**, unaitwa pia kuwa mwanafunzi katika shule ya Kristo. Ukikubali jukumu takatifu la kufundisha wengine, basi una jukumu la kuchambua kwa kina kila somo unalotaka kufundisha. **—Counsels on Sabbath School Work, uk. 31 (1892).** {*EVsw 479:2}*

Ujasiri, Nguvu, Bidii, msukumo na Uvumilivu

Maisha ya Kikristo ni zaidi ya ambavyo wengi wanavyoyafikiria kuwa. Hayajumuishi tu uungwana, subira, upole, na wema. Hakika neema hizi ni za muhimu sana; lakini pia kuna haja ya kuwa na ujasiri, moyo mkuu, nguvu, msukumo, na uvumilivu. Njia ambayo Kristo anaiwekea alama, ni njia nyembamba, yenye kujikana nafsi. Kuingia kwenye njia hiyo na kusonga mbele katika magumu na kukatishwa tamaa kunahitaji watu ambao wana zaidi ya tabia ya unyonge au watu dhaifu-dhaifu. {*EVsw 479:3}*

Wengine hawana uimara wa tabia. Mipango na madhumuni yao haina umbo, uendelevu na uthabiti. Utendaji wao halisi ulio na manufaa kwa ulimwengu ni mdogo sana. Tunapaswa kupata ushindi kutoka kwenye udhaifu huu wa kutokuwa na maamuzi, na uzembe. Katika tabia ya Kikristo ya kweli kuna hali ya ujasiri ya kufanya tusiweze kushindwa ambayo haiwezi kufinyangwa au kutawaliwa na mazingira magumu au mabaya. Ni lazima tuwe na uti wa mgongo wa maadili, uadilifu ambao hauwezi kubembelezwa, kusifiwa kwa kupakwa mafuta kwa chupa ya mgongo, kuhongwa, au kujikunja au kushtuka kwa vitisho. —**The Ministry of Healing, uk. 497-498 (1905).** {*EVsw 480:1}*

Uangalifu, Usahihi, kuwa macho wakati wote na Uharaka

Kusudi la kazi ya **Mungu** inahitaji watu wenye kuona mambo kwa haraka, au papo hapo na kutenda kwa wakati kwa nguvu. Ukingojea kupima kila tatizo, na kusawazisha kila jambo unalokutana nalo, hakika hautafanya kazi kubwa. Utakuwa na vizuizi na changamoto kila mahali, na lazima uchukue uamuzi wa kushinda, au mambo yatakushinda. **—Testimonies for the Church, Juzuu 3:497 (1875).** {*EVsw 480:2}*

Mpangilio, Mfumo na Kasi Katika Kazi Zote

meftly.—The Youth's Instructor, January 28, 1897.

Chumba chako kinaweza kuwa na mapambo madogo madogo mengi yaliyowekwa kwa ajili ya kuvutia macho; lakini iwapo jicho lako litakuwa limekita kwa utukufu wa **Mungu** pekee, itakuwa busara kuzipaki kwenye sanduku hizi sanamu na kuziweka mbali (vitu vingi vya mapambo vyumbani na sebuleni). Katika kushugulika nazo, kuzifuta vumbi, na kuzirudisha tena mahali pake, muda mwingi wa thamani hupotea—muda ambao ungetumika kufanya kazi yenye manufaa, ambayo ni lazima ifanywe. Lakini ikiwa mapambo (trinkets) haya hayawezi kuwekwa mbali, basi kuna somo jingine la kujifunza: kuwa mwepesi katika kazi. Usishike kila pambo kwa uzembe kana kwamba hutaki kuliachilia mkononi mwako. Ni wajibu wa wale walio na mwendo wa polepole kubadilika katika jambo hili. Bwana amesema, "*Fanyeni kazi kwa bidii, si walegevu; mkiwa na juhudi katika roho zenu; mkimtumikia Bwana.*" **Warumi 12:11** {*EVsw 480:3}*

Katika maandalizi ya chakula, fanya mahesabu yako kwa hekima, ukijipa muda wote ambao kwa uzoefu unajua utatosha kupika chakula kikamilifu na kukiweka mezani kwa wakati unaofaa. Lakini ni heri

kuwa tayari dakika tano kabla ya muda kuliko kuchelewa kwa dakika tano. Katika kuosha vyombo pia, kazi inaweza kufanywa kwa haraka, lakini kwa uangalifu na kwa usafi wa kutosha. Tabia za uvivu na kuchelewachelewa hufanya kazi ndogo ionekane kuwa nzito mno. Lakini ikiwa utataka, unaweza kushinda tabia hizi za kukawia na kuzungu-kazunguka,. Matumizi ya nguvu ya mapenzi (nguvu ya nia) yatafanya mikono yako kuwa ya haraka na yenye ustadi. **—The Youth's Instructor, January 28, 1897 {*EVsw 480:4*}**

Mbinu za Kazi ya Biblia

Masomo Rahisi, Yenye Uhai ya Biblia

Lazima tuinuke na kushirikiana na Kristo... Tii agizo la injili; enenda barabarani na vichochoroni. Tembelea maeneo mengi kadri iwezekanavyo. Fanya masomo ya Biblia yaliyo rahisi na yenye uhai, yatakayokuwa na mvuto sahihi kwa akili za watu. — **Manuscript 53, 1910. {*EVsw 481:1*}**

Ujumbe wa Kuzindua Watu Kusoma Biblia

Ujumbe wa kujaribu mioyo kwa wakati huu unapaswa kutangazwa kwa uwazi na uthabiti kiasi cha kuwazindua wasikilizaji na kuwafanya watamani kujifunza Maandiko. — **Testimonies for the Church 9:109 (1909). {*EVsw 481:2*}**

Fundisha Kuiendea Biblia kwa Roho ya Kujifunza

Mwanafunzi wa Biblia anapaswa kufundishwa kuikaribia/kuiendea kwa roho ya kujifunza. Tusitafute ndani yake ushahidi wa kuunga mkono maoni yetu binafsi, bali tujifunze ili tujue kile ambacho **Mungu** amesema. — **Education, uk. 189 (1903). {*EVsw 481:3*}**

Kila Somo la Biblia Lisiwe Bila Mpango Mahususi

Kila mwalimu anapaswa kuhakikisha kuwa kazi yake inalenga kupata matokeo mahususi. Kabla ya kuanza kufundisha somo lolote, anapaswa kuwa na mpango maalum akilini, na ajue hasa analotaka kufanikisha. Asiridhike hadi mwanafunzi aelewe kanuni inayohusika, aitambue kama Kweli, na aweze kuieleza kwa ufasaha. — **Education, uk. 233-234 (1903). {*EVsw 481:4*}**

Urahisi wa Maneno

Usijitahidi kutumia maneno magumu ili uonekane kuwa na elimu kubwa. Kadiri unavyoongea kwa urahisi, ndivyo maneno yako yatakavyoeleweka vizuri zaidi. — **Testimonies for the Church 6:383 (1900). {*EVsw 482:1*}**

Maelezo Rahisi Yafaa Kuliko Mabishano

Ingawa mabishano yana nafasi yake, mengi zaidi yanaweza kufanikishwa kwa maelezo rahisi ya Neno la **Mungu**. Mafundisho ya Kristo yalielezewa kwa namna ambayo hata wasiojua kusoma waliweza kuelewa kwa urahisi. Yesu hakutumia maneno marefu na magumu, bali lugha rahisi iliyofaa akili za watu wa kawaida. Hakuzama sana kwenye somo kuliko uwezo wa wasikilizaji Wake kufuatilia. **— Gospel Workers, uk. 169 (1915). {*EVsw 482:2*}**

Hoja Chache Zatosha

Sio sera yenye hekima kusema kila kitu kuhusu jambo fulani. Mara nyingi hoja chache zinatosha kwa madhumuni ya kuwashawishi au kuwanyamazisha wapinzani. **— Gospel Workers, uk. 376 (1915). {*EVsw 482:3*}**

Wasilisha Kweli kwa Mtindo Rahisi

Katika kizazi hiki ambacho hekaya za kuburudisha zinaelea juu juu na kuvutia akili, Ukweli, unaowasilishwa kwa njia rahisi, ukithibitishwa na ushahidi thabiti mchache, ni bora kuliko kuwasilisha mlolongo mrefu wa hoja unaochosha watu. Kwani mara nyingi pingamizi hazionekani waziwazi katika akili nyingi pale ambapo hizo pingamizi na ushahidi havijaletwa mbele ya watu. Kwa wengi kauli na mafundisho ya Biblia yatolewayo huenda mbali zaidi kuliko hoja ndefu. Watu wengi huchukulia mafundisho na kufikisha injili kwa wepesi sana, wakijua kuwa mambo hayo yapo tu hapo siku zote tu.**Ushahidi hausaidii kesi au hoja**

katika akili za watu kama hao -(Hivyo uwe na hekima, usilete yasiyohitajika kwa wakati huo, na sema kweli tu nk!). — **Testimonies for the Church 3:36 (1872). {*EVsw 482:4*}**

Mstari kwa Mstari

Hebu Kweli iwasilishwe kama ilivyo katika Yesu, mstari kwa mstari, amri juu ya amri, hapa kidogo na pale kidogo. — **Testimonies for the Church 9:240 (1909). {*EVsw 483:1*}**

Nguvu ya Huruma ya Kikristo

Maneno ya fadhili yaliyotamkwa kwa unyenyekevu, na usahili, matendo madogo ya wema yaliyoonyeshwa kwa dhati, yatafukuza mawingu ya majaribu na mashaka juu ya roho. Onyesho la moyo wa huruma wa Kikristo, uliotolewa kwa unyofu, na usahili vina uwezo wa kufungua milango ya mioyo inayohitaji mguso mwororo wa Roho wa Kristo. **— Testimonies for the Church 9:30 (1909). {*EVsw 483:2*}**

Tafuta kufikia Mioyo ya Watu

Popote unapopata nafasi ya kuingia kwenye sebule ya familia wakiwa wanakota moto au kufanya jambo fulani pamoja, boresha fursa hiyo vyema. Chukua Biblia yako na ufungue zile Kweli zake kuu mbele yao. Mafanikio yako hayatategemea sana elimu au vipawa vyako, au mafanikio bali uwezo wako wa kufikia moyo. Kwa kuwa wa rafiki wa karibu na watu, unaweza kuelekeza fikra zao kwa urahisi zaidi kuliko kwa hotuba bora kabisa. — **Gospel Workers, uk. 193 (1915). {*EVsw 483:3*}**

Kufundisha na Kuziishi Kanuni

Haya mafundisho hayapaswi kufundishwa kama nadharia kavu. Wale wanaoleta Kweli kwa wengine wanapaswa kwanza kuishi kwa kanuni zake. Ni kwa kuakisi tabia ya **Mungu tu** kupitia uadilifu, heshima, na kujikana nafsi, ndipo wanaweza kuwavuta wengine. — **Education, uk. 41 (1903). {*EVsw 483:4*}**

Ushawishi wa Msalaba kwa Uinjilisti

Msalaba wa Kalvari unapaswa kuinuliwa juu zaidi ya pale watu walipo, ili uvute fikra zao na kuongoza akili zao kukita hapo. Watendakazi wa injili watatuma miale ya nuru kwa dunia, wakilitangaza Neno kama mawakala hai wa nuru. — **Mount of Blessing, uk. 70 (1896). {*EVsw 483:5*}**

Jibu Maswali

Kazi bora unayoweza kufanya ni kufundisha, kulea na kuelimisha. Kila unapopata nafasi, kaa na familia, waruhusu kuuliza maswali, kisha yajibu kwa uvumilivu na unyenyekevu. Endelea na kazi hii sambamba na huduma zako za hadharani. Hubiri kidogo, na fundisha zaidi kwa kufanya masomo ya Biblia na kusali na familia na vikundi vidogo. — **Gospel Workers, uk. 193 (1915). {*EVsw 484:1*}**

Huduma binafsi ya Biblia kwa Uvumilivu na Umakini

Wahudumu wengi hushindwa kwa sababu hawakaribii wale wanaohitaji msaada zaidi. Akiwa na Biblia mkononi, mwinjilisti anapaswa kwa upole, uungwana na heshima kutambua pingamizi zilizoko mioyoni mwa wanaoanza kuuliza, “Je, Ukweli ni nini?” Waongoze kwa tahadhari na huruma, kama walimu kwa wanafunzi. Wengi hulazimika kujifunza upya nadharia mpya baada ya kushikilia kwa muda mrefu mafundisho potofu. Wanapogundua wamekuwa wakikosea kuhusu Biblia, hujawa na mashaka na mashambulizi ya kiroho. Wanahitaji huruma ya hali ya juu, na msaada wa busara, wanapaswa kufundishwa kwa makini, kuombewa, na kufuatiliwa kwa upendo. — **Gospel Workers, uk. 190-191 (1915). {*EVsw 484:2*}**

Panapo Chuki au Upinzani

Yesu alivuta mioyo ya wasikilizaji Wake kwa kuonyesha upendo Wake, kisha, polepole, kadri walivyoweza kustahimili, aliwafunulia zile Kweli kuu za ufalme wa **Mungu**. Nasi lazima tujifunze kurekebisha kazi yetu na hali ya watu—kuwafikia pale walipo. Ingawa mada za sheria ya **Mungu** ni muhimu kuwasilishwa, tusisahau kwamba upendo—upendo wa Kristo—ndio nguvu pekee inayoweza kulainisha moyo na kumwelekeza mtu kwenye utii. **{*EVsw 483:3*}**

Kweli zote za Maandiko zinaelekeza kwa Kristo; zikieleweka kwa usahihi, zote huongoza Kwake. Hebu Kristo awasilishwe kama Mwanzo na Mwisho wa mpango wa wokovu. Wasilisha masomo yale yatakayoimarisha imani ya watu na ujasiri kwa **Mungu** na Neno Lake, na waongoze kujifunza wao wenyewe. Na Watakapozidi kuendelea hatua kwa hatua katika kujifunza Biblia, wataweza kuelewa vizuri zaidi uzuri na mshikamano wa Kweli zake na thamani yake. — **Review and Herald, June 13, 1912. {*EVsw 485:1*}**

Wasilisha Kweli Zenye Kujaribu Mioyo Baada ya Watu Kuongoka

Usihisi kuwa ni wajibu wako kuanza mabishano kuhusu Sabato mara unapokutana na watu. Ikiwa watu wataanzisha mada hiyo, waambie kuwa hiyo siyo mzigo wako kwa sasa. Lakini wakisalimisha kwa **Mungu** mioyo yao, nia, akili na mapenzi yao, ndipo watakuwa tayari kupokea ushahidi wa Kweli hizi za kujaribu mioyo. **— Letter 77, 1895. {*EVsw 485:2*}**

Ujumbe Zaidi ya Mabishano

Kauli zilizopangwa, mada zenye mabishano tu, hazileti matokeo ya kudumu. Upendo wa **Mungu** ulio ndani ya mioyo ya wahudumu utatambulika na wale wanaohudumiwa. Nafsi zinahitaji maji ya uhai. Msiwe visima visivyo na maji. Mkionyesha upendo wa Kristo, mnaweza kuwaongoza watu wenye njaa na kiu kwa Yesu, Naye atawapa mkate wa uzima na maji ya wokovu. **— Letter 77, 1895. {*EVsw 485:3*}**

Simulia Uzoefu Wako Katika Uongofu (Kuongoka)

Amsha kila nguvu yako ya kiroho. Waambie wale unaowatembelea kuwa mwisho wa mambo yote umekaribia. Bwana Yesu Kristo atafungua mioyo yao na kuweka alama za kudumu akilini mwao. Jitahidi kuwaamsha watu kutoka usingizi wa kiroho na ulegevu wa kutotambua. Waambie jinsi ulivyompata Yesu, na jinsi ulivyobarikiwa tangu upate uzoefu wa maisha katika huduma Yake. Waambie baraka unazopata unapokaa miguuni pa Yesu na kujifunza kutoka kwa Neno Lake. Waambie furaha na shangwe iliyo katika maisha ya Kikristo. Maneno yako ya jotojoto na motisha yatawathibitishia kuwa umepata lulu ya thamani kuu. Hebu maneno yako yenye matumaini na uchangamfu yaonyeshe kuwa kweli umeipata njia iliyo kuu. Huu ndio uinjilisti wa kweli, na ukitekelezwa, wengi wataamka kana kwamba kutoka usingizini au ndotoni. — **Testimonies for the Church 9:38 (1909). {*EVsw 485:4*}**

Maombi kwa Ajili ya Roho Ndiyo Siri ya Mafanikio ya Yule anayeleta watu kwa Bwana

•

Zamani, walikuwapo watu waliolenga nafsi moja moja kwa bidii, na kisha walikita akili zao wakiomba, “Bwana, nisaidie kuiokoa nafsi hii.” Lakini sasa hali kama hizo ni nadra. Ni wangapi wanaotambua hatari ya wenye dhambi? Ni wangapi wanaompeleka mtu anayejulikana kuwa katika hatari mbele za **Mungu** katika sala, wakiomba kwa bidii mtu huyo aokolewe? **— Gospel Workers, uk. 65. {*EVsw 486:1*}**

Masomo Kutoka kwa Mwalimu Mkuu

Kuwasilisha Neno kwa Njia ya Kristo — Ikiwa unawasilisha Neno kwa njia ya Kristo, wasikilizaji wako wataguswa kwa kina kwa Kweli unazofundisha. Watashawishika kwamba hili ndilo Neno la **Mungu** aliye hai. **— Testimonies for the Church, 9: 143 (1909). {*EVsw 486:2*}**

Upendo wa Subira na Kujali Waliopotea — Bwana Alifundisha watu kwa upendo wa subira. Hekima Yake ya kina na ya kuchunguza mioyo ilitambua mahitaji ya kila nafsi kati ya wasikilizaji Wake; Naye Alipowaona wakikataa ujumbe wa amani na upendo aliokuja kuwapatia, moyo Wake ulihisi maumivu ya huzuni hadi vilindi Vyake. — **Gospel Workers, uk. 49 (1915). {*EVsw 486:3*}**

Upole na Unyenyekevu — Hakukuwa na chembe hata moja ya ubaguzi wala sera za ukali, ubaridi au uchoyo katika mwenendo Wake. Mkombozi wa ulimwengu alikuwa na asili kuu zaidi ya ya malaika, lakini pamoja na ukuu Wake wa Kiungu kulikuwepo upole na unyenyekevu vilivyowavuta watu wote Kwake. — **Mount of Blessing, uk. 29, 30 (1896). {*EVsw 487:1*}**

Tumaini Linachochea Shauku/matamanio na Imani — Kwa kila mwanadamu aliona uwezekano usio na mwisho. Aliwaona watu vile ambavyo wangeweza kuwa—wamebadilishwa na neema Yake—katika "uzuri wa Bwana **Mungu** wetu." Aliwaangalia kwa tumaini, na kwa kufanya hivyo aliwatia moyo kuwa na tumaini. Alichochea kumtegemea, na hivyo aliwatia moyo kuwa na imani. Kwa kuonyesha mfano wa kweli wa mwanadamu ndani Yake Mwenyewe, aliwasha ndani yao tamanio na imani ya kufikia kiwango hicho. Mbele za uso Wake, roho zilizodharauliwa na kuanguka zilitambua kuwa bado ni watu, na walitamani kujithibitisha kuwa wanastahili heshima Yake. Katika mioyo mingi iliyokuwa kana kwamba imekufa kwa mambo matakatifu, uliamka msukumo mpya. Kwa wengi waliokata tamaa, mlango wa maisha mapya ulifunguliwa. — **Education, uk. 80 (1903). {*EVsw 487:2*}**

Bidii. Udhati na Nguvu ya Kushawishi — Wakati wanaume na wanawake waliposikiliza Kweli zilizotoka midomoni Mwake, zilikuwa tofauti sana na mila na mafundisho ya marabi-dogma, na tumaini likazuka mioyoni mwao. Katika mafundisho Yake kulikuwapo bidii ya dhati iliyosababisha Maneno Yake kuingia mioyoni kwa nguvu ya kushawishi. — **Gospel Workers, uk. 188 (1915). {*EVsw 487:3*}**

Kutoa Uzima na Furaha — Alipopita katika miji na vijiji, Alikuwa kama mkondo wa uzima, akieneza maisha na furaha. — **The Ministry of Healing, uk. 20 (1905). {*EVsw 487:4*}**

Tunaweza kuwa watu wenye furaha. **Mungu** hataki nyuso zenye huzuni hapa duniani; Bwana hataki mtu yeyote kuwa mwenye huzuni au giza; Yeye Anataka tuinue nyuso zetu Kwake, na kumruhusu atumwagie mwangaza wa Jua la Haki. — **Manuscript 42, 1894. {*EVsw 488:1*}**

Kristo Alifundisha Kwa Mamlaka — Ingawa mafundisho Yake yalikuwa rahisi, alinena kama Mwenye mamlaka. Sifa hii iliweka mafundisho Yake kando na yale ya wote wengine. Marabi walifundisha kwa mashaka na kusitasita, kana kwamba Maandiko yanaweza kufasiriwa kwa namna moja au kinyume chake kabisa. Wasikilizaji walizidi kupotea katika mkanganyiko. Lakini Yesu alifundisha Maandiko kama yenye mamlaka isiyotiliwa shaka. Haijalishi mada ilikuwa ipi, aliiwasilisha kwa nguvu kana kwamba maneno Yake hayawezi kupingwa. — **The Desire of Ages, uk. 253 (1898). {*EVsw 488:2*}**

Shauku ya Kuwaokoa Wenye Dhambi — Shauku ile ile ya kumwokoa mwenye dhambi iliyojulikana katika maisha ya Mwokozi, inaonekana pia katika maisha ya mfuasi Wake wa kweli. — **Testimonies for the Church, 7: 10 (1902). {*EVsw 488:3*}**

Nguvu Inayovuta — Utii wa haraka na usio na masharti wa watu hawa, bila ahadi ya malipo, ni wa kushangaza; lakini Maneno ya Kristo yalikuwa mwaliko uliokuwa na nguvu ya kuvuta kama ilivyo sumaku. — **Gospel Workers, uk. 24 (1915). {*EVsw 488:4*}**

Matokeo ya Kazi ya Biblia

Malaika Karibu na Mtendakazi — Mtendakazi anapojitahidi kuwapa wengine nuru aliyopokea kutoka kwa **Mungu**, Bwana humwongezea nuru zaidi na zaidi; na anapofanya kazi yake kwa bidii, akiwa na nia ya kumpa **Mungu** utukufu, anatambua thamani ya roho. Anapozuru nyumba kwa nyumba, akifungua Maandiko kwa wale ambao uelewa wao umefunikwa na giza, malaika wa **Mungu** watakuwa karibu naye ili kugusa mioyo ya wale wenye kiu ya maji ya uzima. — **Review and Herald, October 6, 1896. {*EVsw 488:5*}**

Bwana Hufanya Kazi Pamoja na Walimu wa Biblia — Hebu Sababu thabiti za imani yetu na zielezwe kwa kutumia Neno la **Mungu**, na Ukweli katika nguvu yake ya kutakasa uliyeyushe njia hadi mioyoni na akilini mwa wale walioko chini ya msukumo. Pale wasaidizi wanapotoa mafundisho ya Biblia majumbani mwa watu, Bwana hufanya kazi mioyoni mwao kwa uhakika sawa na vile ilivyo katika huduma za hadharani. — **Letter 160, 1901. {*EVsw 489:1*}**

Miujiza Kupitia Neno — Daima kutakuwa na mapambano ya kufikia mioyo ya wasio na maarifa na waovu. Lakini Je, kila mmoja wetu anajitahidi kwa bidii na uaminifu wa kibinafsi kama tunavyopaswa? Je, hatujitengi mno na roho maskini ziliokufa katika dhambi na makosa na kuonyesha hatuna shauku? Je, hatuwezi sisi sote kujivika bidii ya dhati ya Kristo, na kufanya zaidi? **{*EVsw 489:2*}**

Nina hofu kwamba hatuna ile imani inayohitajika. Je, hatupaswi kujitia nguvu dhidi ya kuvunjika moyo na majaribu? **Mungu** ni Mwenye rehema, na pamoja na Ukweli unaoshangilia, utakaso, na kuinua maisha, tunaweza kufanya kazi bora na thabiti kwa **Mungu**. Maombi na imani vitafanya mambo ya ajabu. Neno lazima liwe silaha yetu ya vita. Miujiza inaweza kufanywa kupitia Neno; maana linafaa kwa kila jambo. **— Letter 75, 1896. {*EVsw 489:3*}**

Thamani ya Roho — Roho inayojitoa kwa Kristo ni ya thamani zaidi machoni Pake kuliko dunia nzima. — **The Desire of Ages, uk. 480 (1898). {*EVsw 489:4}***

Kama nafsi moja tu ndiyo ingekubali Injili ya neema Yake, Kristo angelichagua maisha ya taabu na unyenyekevu, na kufa kifo cha aibu kwa ajili tu ya kuokoa hiyo nafsi moja. — **The Ministry of Healing, uk. 135 (1905). {*EVsw 489:5}***

Hebu Kazi Hii Iendelee Mbele — Wengi watasikia ujumbe lakini watakataa kuutii; hata hivyo, onyo lazima litolewe kwa wote kwa sauti iliyo wazi na dhahiri. Ukweli haupaswi tu kuwasilishwa katika mikutano ya hadhara; kazi ya nyumba kwa nyumba inapaswa kufanyika. Na kazi hii iendelee mbele kwa Jina la Bwana. Wanaojishughulisha nayo wana malaika wa mbinguni kama wenzao. Watapinga mashambulizi ya adui dhidi ya wale wanaoshirikiana na **Mungu**. — **Letter 140, 1903. {*EVsw 490:1}***

Ujasiri katika Kuamini Ahadi za Mungu — Mbegu njema huenda ikakaa kwa muda bila kuonekana katika moyo wa baridi, wa ubinafsi, na wa kidunia, bila kutoa dalili kuwa imeota; lakini baadaye, Roho wa **Mungu** anapovuvia nafsi hiyo, mbegu iliyojificha huota, na hatimaye huzaa matunda kwa utukufu wa **Mungu**. Katika kazi yetu ya maisha hatujui ni kazi ipi itafaulu—hii au ile. Hili si jambo la sisi kuliamua. Tunapaswa kufanya kazi yetu na kuyaacha matokeo mikononi mwa **Mungu**. **Mhubiri 11:6** "*Asubuhi panda mbegu zako, Wala jioni usizuie mkono wako*." **{*EVsw 490:2}***

Agano kuu la **Mungu** linatangaza katika **Mwanzo 8:22**

"Kadiri itakavyodumu nchi majira ya kupanda na kuvuna, ya baridi na joto, ya masika na kiangazi, usiku na mchana, hayatakoma." Kwa kujiamini katika ahadi hii, mkulima hulima na kupanda. Sisi pia, kwa kazi ya kiroho, tunapaswa kufanya kazi kwa kujiamini, tukiamini ahadi Yake: "**Isaiah 55:11** *ndivyo litakavyokuwa neno langu, litokalo katika kinywa changu; halitanirudia bure, bali litatimiza mapenzi yangu, nalo litafanikiwa katika mambo yale niliyolituma*." "**Zaburi 126:6** *Ingawa mtu anakwenda zake akilia, Azichukuapo mbegu za kupanda. Hakika atarudi kwa kelele za furaha, Aichukuapo miganda yake*." — **Christ's Object Lessons, uk. 65 (1900). {*EVsw 490:3}***

Mshahara wa Kutosha kwa Watendakazi Wanawake

Kulipwa Sawasawa na Waume Zao

Iwapo inawezekana, mhubiri na mkewe waende pamoja katika huduma. Mara nyingi mke anaweza kufanya kazi bega kwa bega na mumewe, akitimiza kazi bora na ya thamani kuu. Anaweza kutembelea nyumba za watu na kuwasaidia wanawake katika familia hizo kwa namna ambayo mumewe hawezi kufanya... **{*EVsw 491:1}***

Chagueni wanawake ambao watashiriki kazi hii kwa moyo wa bidii. Bwana atawatumia wanawake wenye akili mahiri katika kazi ya kufundisha. Na mtu yeyote asione kuwa wanawake hawa, ambao wanaelewa Neno la **Mungu** na wana uwezo wa kufundisha, hawastahili malipo au fidia kwa kazi yao. Wanapaswa kulipwa kwa hakika kama vile waume zao walipwavyo. Kuna kazi kubwa sana kwa wanawake katika kazi ya Kweli ya wakati huu. Kupitia hekima ya kike na matumizi ya busara ya maarifa ya Kweli ya Biblia, wanaweza kuondoa vikwazo ambavyo ndugu zetu wanaume hawawezi kuviondoa. Tunahitaji wanawake waaminifu kufanya kazi pamoja na waume zao, na tunapaswa kuwatia moyo wale wanaotamani kushiriki katika njia hii ya kazi ya kimishenari. **— Letter 142, 1909 {*EVsw 491:2}***

Kujitolea Kusichukuliwe Kama Jambo la Wanawake Pekee

Kuna kazi kubwa ya kufanywa duniani, na kila kipawa kinapaswa kutumiwa kwa kuzingatia kanuni za haki. Iwapo mwanamke ameteuliwa na Bwana kufanya kazi fulani, basi kazi yake inapaswa kuthaminiwa kulingana na thamani yake. Kila mtendakazi anapaswa kulipwa haki yake. **{*EVsw 491:3}***

Huenda ikadhaniwa kuwa ni jambo jema kuruhusu watu kutumia vipawa vyao na kufanya kazi kwa bidii katika huduma ya **Mungu** bila kulipwa chochote kutoka hazina ya kanisa. Lakini hili linaonyesha ubaguzi, na kuwanyima watendakazi hawa malipo yao halali. **Mungu** hataidhinisha mpango wa namna hiyo. Wale walioanzisha mpango huo huenda walidhani wanamtumikia **Mungu** kwa kutolipa watendakazi waaminifu wanaomcha **Mungu** na wanaopenda roho za watu. Lakini kutakuwa na kutoa hesabu kwa Bwana siku ile ya mwisho ya hukumu, na wale wanaofikiri kuhusu ubahili huu katika au dili la ubaguzi na ujanja au hila,

watapata aibu ubinafsi/uchoyo wao. **Mungu** huyaona mambo haya kwa mwanga tofauti kabisa na mwanadamu wenye ukomo. {*EVsw 491:4}*

Wale wanaofanya kazi kwa dhati na bidii na bila ubinafsi—iwe ni wanaume au wanawake—huwaletea Bwana mavuno; na roho zinazobadilishwa kupitia kazi yao zitaleta zaka zao kwenye hazina ya **Mungu**. Lakini kunapohitajika kujinyima kwa sababu ya ukosefu wa fedha, basi isiwe wanawake wachache tu ndio wanaofanya kazi kwa bidii nao ndio wajinyime na kujitolea kufanya kazi bila malipo. Wote wanapaswa kushiriki katika kujinyima. **Mungu** ametangaza: **Isaya 61:8** *Nauchukia wivi na uovu*. **— Manuscript 47, 1898** {*EVsw 492:1}*

Kustahili Kulipwa Kutokana na Zaka

Zaka inapaswa kuelekezwa kwa wale wanaofanya kazi ya Neno na Mafundisho, wawe wanaume au wanawake. **— Manuscript 149, 1899** {*EVsw 492:2}*

Hatua Itakayowazuia Wanawake Watendakazi

Haki haijatendeka kwa baadhi ya wanawake wanaofanya kazi kwa bidii kama waume zao tu, na ambao **Mungu** amewatambua kuwa muhimu katika kazi ya huduma. Mpango wa kuwalipa wanaume wanaofanya kazi na kutowalipa wake zao ambao wanashiriki kazi hiyo hiyo, sio mpango wa Bwana, na ukiendelezwa katika Konferensi zetu, unaweza kuwakatisha tamaa dada zetu wasijiandae kwa kazi wanayopaswa kuifanya. **Mungu** ni **Mungu** wa haki, na ikiwa wahubiri wanalipwa kwa kazi yao, wake zao wanaojitolea vivyo hivyo wanapaswa kulipwa kando na mishahara ya waume zao, hata kama wao wenyewe hawajaomba kulipwa. {*EVsw 492:3}*

Waadventista wa Sabato hawapaswi kwa namna yoyote kuidharau kazi ya wanawake. Ikiwa mwanamke amemkabidhi kazi ya nyumbani kawke msaidizi mwaminifu na mwenye busara, na kuwaacha watoto wake katika uangalizi mzuri, ili aingie katika kazi ya Bwana, basi Koferensi inapaswa kuwa na hekima ya kutambua kuwa huyo mama anastahili kulipwa. — **Gospel Workers, uk. 452-453 (1915)** {*EVsw 492:4}*

Mungu Ameshatoa Uamuzi Katika Suala Hili

Ikiwa wanawake wanafanya kazi ambayo si ya kupendeza kwa wengine wanaohubiri na kufundisha, na ikiwa matunda ya kazi yao yanaonyesha kuwa wanafanya kazi ambayo kwa muda mrefu imesahauliwa, Je, kazi hiyo haipaswi kutambuliwa kuwa ina matokeo ya thamani sawa na kazi ya wahubiri waliowekwa wakfu? Je, mtendakazi hastahili malipo yake? {*EVsw 493:1}*

Swali hili sio la wanadamu kuliamua. Bwana tayari ameliamua. Ninyi mnapaswa kutenda haki kwa wanawake wanaofanya kazi ya injili, kazi ambayo inaonyesha kuwa ni muhimu katika kupeleka Ukweli wa Biblia kwenye familia. Kazi yao ni ile kazi ambayo ni lazima kufanyika, na inapaswa kuungwa mkono kwa kuwatia watu moyo. Kwa hali nyingi, mwanamke anaweza kuwafundisha dada zake mambo ambayo mwanamume hawezi. Kazi ya Bwana ingepata hasara kubwa sana kama wanawake hawangehusika katika huduma hii. Mara kwa mara Bwana amenionyesha kuwa walimu wanawake ni wa lazima kama walivyo wanaume katika kazi waliyoitiwa. — **Manuscript 142, 1903** {*EVsw 493:2}*

Tahadhari kwa Mwalimu wa Biblia

Kazi ya binafsi Inachosha Zaidi

Wanawake, kama vile wanaume, wanahitajika katika kazi hii. Wale wanawake wanaojitoa kwa huduma ya Bwana, wanaofanya kazi ya kuokoa roho kwa kwenda nyumba hadi nyumba—kazi ambayo ni ya kuchosha kama sio zaidi ya ile kusimama mbele ya kusanyiko na kuhubiri—wanapaswa kulipwa kwa kazi yao. **— Manuscript 149, 1899** {*EVsw 493:3}*

Epukeni Uchovu Kupita Kiasi

Kuna hatari kwamba wanawake walioungan ishwa na kazi hii watahitajika kufanya kazi kupita kiasi bila muda wa kupumzika. Mzigo wa namna hiyo haustahili kuwekwa juu ya watendakazi. Baadhi hawataathirika, lakini wengine, hasa wale waaminifu na wenye dhamiri kali, watachoka sana na kuathiri afya. Vipindi vya mapumziko ni vya lazima kwa wote, hasa wanawake. **— Letter 61, 1896** {*EVsw 494:1}*

Sisi ni Viumbe Tunaokufa

Ndugu _____, natumaini utakuwa mwangalifu sana juu ya afya ya Dada _____. Usimruhusu afanye kazi nyingi sana kwa hali ya kuchosha akili na mishipa ya fahamu. Utajua ninachomaanisha. Anapaswa kuelewa kuwa sisi ni wanadamu tunaokufa, na ikiwa hatutajali afya zetu, tunaweza kuzipoteza. **— Letter 44, 1900** {*EVsw 494:2}*

Wakati wa Kutenda kwa Uhuru

Kuna mazingira yanayofaa kwa mwanamke kutenda kwa haraka na kwa uhuru, akifanya uamuzi kwa uthabiti katika njia anayojua kuwa ni ya Bwana. Mke anapaswa kusimama upande wa mumewe kama yule aliye sawa naye, akishiriki majukumu yote ya maisha, huku akimheshimu mume wake ambaye amemchagua kuwa mwenzi wake wa maisha. — **Manuscript 17, 1891** {*EVsw 494:3}*

Epukeni Kuwasifia Wanaume na Kuwa na Mahusiano ya Karibu Yasiyofaa

Ninaumizwa ninapoona wanaume wakisifiwa, kudekeshwa na kubembelezwa. **Mungu** amenifunulia kuwa baadhi ya wanaume wanaopokea umakini huu hawastahili hata kulitaja Jina la **Mungu** kwa midomo yao; lakini wanatukuzwa kama malaika mbele ya macho ya wanadamu wanaokufa, wanaotazama tu muonekano wa nje. Dada zangu, kamwe msibembeleze au kujikomba kwa wanaume waliodhoofika na wenye makosa—iwe ni vijana au wazee, waliooa au wasiooa. Wewe hujui udhaifu wao, na hujui kama sifa na umakini huu unaowapa wa kupita kiasi unaweza kuwa sababu ya maangamizi yao. Ninashangazwa na upofu na ukosefu wa hekima ambao wengine huonyesha kuhusu ukaribu huu usiofaa..... {*EVsw 494:4}*

Wanaume waliooa wanaopokea umakini, sifa, kutongozwa na kubembelezwa na wanawake, na kushikwashikwa wanapaswa kufahamu kuwa upendo na huruma ya aina hii haina stahiki yoyote kuipokea-(ni uovu). {*EVsw 495:1}*

Nasisitiza tena juu yenu hitaji la usafi katika kila wazo, kila neno, na kila tendo. Kila mmoja wetu anawajibika binafsi mbele za **Mungu**, kazi ya kipekee ambayo hakuna mtu mwingine anayeweza kuifanya kwa ajili yetu: ni kufanya dunia hii kuwa mahali bora kwa mafundisho, jitihada za binafsi, na kwa mfano wa maisha yetu. Ingawa tunapaswa kuwa wakarimu na wa kijamii (sociable), lengo lisiwe maburudisho tu, bali kuokoa roho, si kwa ajili ya starehe tu. **— The Review and Herald, November 10, 1885** {*EVsw 495:2}*

SEHEMU YA 15—UINJILISTI KWA NJIA YA WIMBO

Huduma ya Wimbo

Chombo cha Kuokoa Roho — Sauti ya nyimbo inayomiminwa kutoka kwenye mioyo mingi kwa uwazi, ikitamka maneno kwa ufasaha, na kueleweka ni moja ya njia ambazo **Mungu** hutumia kuongoa roho. **— Testimonies for the Church, 5:493 (1889).** {*EVsw 496.1}*

Nguvu ya Wimbo — Kama vile Waisraeli walivyotumia nyimbo takatifu kuwapa moyo na kuwachangamsha walipokuwa wakisafiri jangwani, vivyo hivyo **Mungu** anawaamuru watoto Wake leo wafurahie maisha yao ya hija ya hapa duniani, au safari ya hapa duniani kwa nyimbo. Hakuna njia nyingi bora za kuweka Neno Lake moyoni kuliko kulirudia kwa wimbo. Wimbo wa namna hii unao uwezo wa ajabu. Wimbo unaweza kulainisha tabia ngumu, yenye ujeuri na isiyostrabika; huamsha fikra na huruma; huleta mshikamano katika matendo; na hufukuza huzuni na hofu zinazovunja ujasiri na kudhoofisha jitihada. {*EVsw 496.2}*

Ni mojawapo ya njia zenye ufanisi mkubwa wa kupenyeza Ukweli wa kiroho moyoni. Mara nyingi, kwa mtu aliyelemewa na majaribu na kukata tamaa, hukumbuka Maneno ya **Mungu**—mzigo wa zamani wa wimbo wa utotoni—na majaribu hupoteza nguvu zake, maisha yanapata maana mpya na kusudi jipya, na ujasiri na furaha huenea kwa wengine. —**Education, uk. 167, 168 (1903).** {*EVsw 496.3}*

Mahubiri Endelevu — Maneno haya [wimbo wa Musa] yalirudiwa mbele ya Israeli wote, na yakawa wimbo uliokuwa ukiimbwa mara kwa mara kwa sauti ya juu. Hii ilikuwa hekima ya Musa: kuwasilisha Ukweli kwa wimbo, ili kwa njia ya sauti za nyimbo Ukweli huo uingie akilini mwa taifa lote, vijana kwa wazee. Watoto walipaswa kujifunza wimbo huu kwani ulikuwa muhimu; kwa kuwa ungewasemea, kuwatia moyo, kuwaonya, kuwazuia, kuwakemea na kuwahimiza. Ulikuwa ni mahubiri yanayoendelea. **—Manuscript 71, 1897.** {*EVsw 496.4}*

Mvuto Unaofika Mbali — Huduma ya wimbo iliwekwa kuwa sehemu ya ibada ya kawaida, na Daudi akaandika Zaburi, si tu kwa ajili ya matumizi ya makuhani katika huduma ya Patakatifu, bali pia kuimbwa na watu walipokuwa wakisafiri kuelekea madhabahu kuu ya taifa kwenye sikukuu za kila mwaka. Athari ya ibada hii ilikuwa ya kina na ilichangia taifa kuachana na ibada ya sanamu. Watu wa mataifa jirani, walipoona mafanikio ya Israeli, waliwaza mema kuhusu **Mungu** wa Israeli, aliyewatendea watu Wake mambo makuu. — **Patriarchs and Prophets, uk. 711 (1890).** {*EVsw 497.1*}

Kuvutia Kweli — Usiku mmoja akili yangu ilisumbuka sana nikitafakari jinsi ya kuwafikia watu katika miji mikubwa kwa ujumbe wa ile Kweli. Tulijua kwamba iwapo tu wangepata kusikia ujumbe huu, baadhi yao wangekubali Ukweli na kuwashirikisha wengine. {*EVsw 497.2*}

Wachungaji huonya makutano yao na kusema kuwa mafundisho haya ni ya hatari, na kwamba wakisikia watahadaaika na Mafundisho ya imani yaliyo mageni kabisa. Ubaguzi huu ungeondolewa tu kama watu wangesikia kwa masikio yao. Tulikuwa tunaombea jambo hili, tukiamini kuwa Bwana atafungua njia kwa ujumbe huu wa onyo na mafundisho kuwafikia watu katika siku hizi za mwisho. {*EVsw 497.3*}

Katika ndoto usiku, nilijikuta kwenye kikao cha ushauri ambapo mambo haya yalijadiliwa. Mtu mmoja mwenye wadhifa- heshima kubwa na umakini alisema, “Mnawaombea Bwana awainue wanaume na wanawake wenye vipaji wajiunge na kazi. Mnayo vipaji miongoni mwenu ambavyo havithaminiwi.” Mapendekezo kadhaa yenye busara yalitolewa, kisha akasema, “Nawashauri kuhusu kipawa cha uimbaji ambacho kinapaswa kuendelezwa/kukuzwa; kwa kuwa sauti ya mwanadamu katika wimbo ni kipawa kutoka kwa **Mungu** kilichotolewa kama dhamana kwa ajili ya utukufu Wake. Adui wa haki huweka thamani kubwa kwa kipawa hiki kwa huduma Yake. Na kile kilichopewa na **Mungu** kama baraka kwa nafsi, kinapotumiwa vibaya, humtumikia Shetani. Kipawa hiki cha sauti ni baraka ikiwa kitatakaswa kwa ajili ya kazi ya Bwana. _____ ana kipaji, lakini hakithaminiwi. Nafasi yake inapaswa kuzingatiwa na kipawa chake kitawavutia watu, nao watasikia ujumbe wa Kweli.” **—Letter 62, 1893.** {*EVsw 497.4*}

Muunganiko na Mungu — Lazima kuwe na muunganiko wa kweli na **Mungu** katika maombi, na pia katika nyimbo za sifa na shukrani. **—Letter 96, 1898.** {*EVsw 498.1*}

Kumpinga Adui — Kristo alipokuwa mtoto kama hawa watoto, alijaribiwa kutenda dhambi, lakini hakujisalimisha kwa majaribu. Alipokuwa mtu mzima, alijaribiwa pia, lakini nyimbo alizofundishwa na mama yake zilikumbuka akilini mwake, Naye akainua sauti yake ili kuimba. Na kabla ya rafiki Zake kutambua, walikuwa wanaimba pamoja Naye. **Mungu** anataka tutumie kila njia ambayo Mbingu imetoa ili kupinga majaribu ya adui. **—Manuscript 65, 1901.** {*EVsw 498.2*}

Kuleta Furaha ya Mbinguni — Saa za asubuhi mapema mara nyingi zilimkuta katika mahali pa faragha, akitafakari, akichunguza Maandiko, au katika maombi. Alipaza sauti Yake kwa kuimba, akiukaribisha mwanga wa asubuhi. Alizichangamsha saa zake za kazi kwa nyimbo za shukrani na kuileta furaha ya mbinguni kwa wale waliochoshwa na suluba na kuvunjika moyo. —**The Ministry of Healing, uk. 52 (1905).** {*EVsw 498.3*}

Wimbo wa Sifa — Mara nyingi Kristo alieleza furaha ya moyo Wake kwa kuimba Zaburi na nyimbo za mbinguni. Mara nyingi wakazi wa Nazareti walisikia sauti Yake ikipaa kwa sifa na shukrani kwa **Mungu**. Alikuwa akiwasiliana na mbingu kwa njia ya wimbo; na rafiki zake walipolalamika kwa uchovu wa kazi, walitiwa moyo na melodi tamu kutoka midomoni Mwake. Sifa Zake zilifukuza malaika waovu, na kama uvumba, zikajaza mahali hapo na harufu nzuri. Akili za wasikilizaji Wake zilielekezwa mbali na ugeni wa dunia hii hadi nyumbani mbinguni. **—The Desire of Ages, uk. 73-74.** {*EVsw 499.1*}

Silaha Dhidi ya Kukatishwa Tamaa—Kama kungekuwa na kumsifu zaidi Bwana, na maneno machache ya kukatisha tamaa, ushindi mwingi zaidi ungepatikana. **—Letter 53, 1896.** {*EVsw 499.2*}

Hebu sifa na shukrani zionyeshwe kwa nyimbo. Tunapojaribiwa, badala ya kutoa matamko ya kuelezea hisia zetu, hebu kwa imani tuinue wimbo wa shukrani kwa **Mungu**. {*EVsw 499.3*}

Wimbo ni silaha ambayo tunaweza kutumia kila wakati dhidi ya kukata tamaa. Tunapofungua hivyo moyo kwa nuru ya jua ya uwepo wa Mwokozi, tutakuwa na afya na baraka Zake. **—The Ministry of Healing, 254 (1905).** {*EVsw 499.4*}

Kuhifadhi Uzoefu wa Kikristo — Asubuhi na jioni, jiunge na watoto wako katika ibada ya **Mungu** kwa pamoja, mkisoma **Neno** Lake na kuimba sifa Zake. Wafundishe kurudia sheria ya **Mungu**. Kuhusu amri,

Waisraeli waliagizwa: **“Kumbukumbu la Torati 6:7** *"Nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo.”* Kwa kuzingatia agizo hilo, Musa aliwaelekeza Waisraeli kuyaweka Mafungu ya sheria ya Mungu katika ala za muziki. Watoto wakubwa walipiga vyombo vya muziki, nao wadogo wakatembea kwa mpangilio, wakiimba pamoja nyimbo za amri za **Mungu kwa pamoja**. Miaka ilipopita, waliendelea kuyakumbuka Maneno ya sheria waliyojifunza utotoni. {*EVsw 499.5}*

Ikiwa ilikuwa muhimu kwa Musa kuweka amri katika nyimbo takatifu ili watoto wajifunze kuziimba aya kwa aya walipokuwa wakisafiri jangwani, basi ni muhimu kiasi gani kwetu leo hii kuwafundisha watoto wetu **Neno** la **Mungu**! Na tujitokeze kwa bidii kwa ajili ya Bwana, tukiwafundisha watoto wetu kuzishika amri za **Mungu** kwa ukamilifu. Na tufanye kila tuwezalo kuujaza muziki mtakatifu katika nyumba zetu, ili **Mungu** apate kuingia na kutawala. **—The Review and Herald, September 8, 1904. {***EVsw 500.1}*

Mbingu Yote Inaitikia Mwangi Furaha—

Ni lazima tukumbuke furaha kuu iliyodhihirishwa na Mchungaji katika kuwapata waliopotea. Anawaita jirani zake: "*Furahini pamoja Nami*; kwa maana nimempata kondoo Wangu aliyepotea." Na mbingu yote inarudia noti ya furaha. Baba Mwenyewe hufurahi juu ya aliyeokolewa kwa kuimba. Ni shangwe takatifu iliyoje inayoonyeshwa katika mfano huu! Furaha hiyo ni fursa yako kushirikisha wengine. —**Testimonies For The Church 6:125 (1900) {***EVsw 500.2}*

Muziki Katika Uinjilisti

Kugusa Moyo kwa Ukweli wa Kiroho — Wimbo ni mojawapo ya njia zenye ufanisi mkubwa wa kugusa moyo na kuingiza Ukweli wa kiroho moyoni. Mara nyingi kwa maneno ya wimbo mtakatifu, chemchemi za toba na imani hufunguliwa. —**The Review and Herald, Juni 6, 1912. {***EVsw 500.3}*

Vyombo vya Muziki — Kipawa cha uimbaji kiletwe katika kazi. Matumizi ya vyombo vya muziki hayapaswi kuonekana kuwa na tatizo lolote. Vilitumika katika ibada za zamani. Waabudu walimsifu **Mungu** kwa kinubi na matoazi, na muziki unapaswa kuwa na nafasi yake katika ibada zetu. Itaongeza mvuto. **—Letter 132, 1898. {***EVsw 500.4}*

Huduma ya Wimbo Sio Tamasha — Nilionyeshwa kuwa kama Ndugu _____ atazingatia mashauri ya ndugu zake, na aache tabia ya kujitahidi kupita kiasi kuwakusanya watu wengi, atakuwa na ushawishi mkubwa zaidi kwa wema, na kazi yake italeta matokeo bora zaidi. Anapaswa kuondoa kutoka kwenye mikutano yake kila kitu kinachoonyesha maigizo ya kisanii au tamasha la jumba la maonyesho-theatrical display; kwa kuwa maonyesho ya nje hayaongezi nguvu kwa ujumbe anaoleta. Wakati Bwana atakapoweza kushirikiana naye, kazi yake haitahitaji kufanyika kwa gharama kubwa kama ilivyo. Hatahitaji kutumia kiasi kikubwa kwa matangazo ya mikutano yake. Hatahitaji kutegemea sana ratiba ya muziki-music program. Sehemu hii ya huduma zake inafanywa kwa namna inayofanana na tamasha la ukumbi wa michezo (theatre concert), kuliko ibada ya nyimbo katika mkutano wa kidini. **—Letter 49, 1902. {***EVsw 501.1}*

Shauku ya Neno — Mioyo ya wengi ulimwenguni, na pia ya washiriki wa kanisa, inahisi njaa ya mkate wa uzima na kiu ya maji ya wokovu. Wanaweza kuvutiwa na ibada ya nyimbo, lakini hawana matamanio ya hizo nyimbo au hata maombi. Wanatamani kufahamu Maandiko. "Neno la **Mungu** linasema nini kwangu mimi?" Roho Mtakatifu anafanya kazi juu ya akili na mioyo yao, akiwavuta kwa mkate wa uzima. Wanaona kila kitu kinachowazunguka kinabadilika. Hisia za kibinadamu, maoni ya watu kuhusu dini au mambo ya kiroho yanabadilika. Wanakuja kusikiliza Neno jinsi lilivyoandikwa. **—Manuscript 11, 1899. {***EVsw 501.2}*

Mada ya Kila Wimbo — Sayansi ya wokovu iwe mzigo wa kila mahubiri, hebu na iwe mada ya kila wimbo. Hebu na itolewe katika kila dua. **—Manuscript 107, 1898. {***EVsw 502.1}*

Epuka Mhemuko wa Hisia — Wengine huenda upande wa pili, wakisisitiza hisia za kidini kwa mihemko, na wakati wa hafla maalum huonyesha bidii ya juu kupita kiasi. Dini yao huonekana kuwa kama kichocheo tu badala ya imani ya kudumu kwa Kristo. {*EVsw 502.2}*

Watumishi wa kweli wa **Mungu** wanatambua thamani ya kazi ya ndani ya Roho Mtakatifu katika mioyo ya wanadamu. Wanaridhika na unyenyekevu katika huduma za kidini. Badala ya kuzipa uzito nyimbo maarufu, wanazingatia sana kujifunza Neno, na kutoa sifa kwa **Mungu** kwa moyo kwa moyo wao wote. Zaidi ya mapambo ya nje, wanathamini mapambo ya ndani, yaani, kito cha roho ya upole na utulivu. Vinywani mwao hamna hila. **—Manuscript 21, 1891. {***EVsw 502.3}*

Huduma ya Wimbo Majumbani — Wanafunzi, tokeni na kwenda barabarani na kwenye vichochoro. Jaribuni kuwafikia watu wa hali ya juu na ya chini. Ingieni katika nyumba za matajiri na maskini, na mkipata nafasi, waulizeni, "Je, mtapenda tuwaimbie? Tutafurahi kufanya ibada ya wimbo pamoja nanyi." Kisha, mioyo itakapoguswa, njia inaweza kufunguliwa kwa ajili ya kutoa maneno machache ya maombi kwa ajili ya baraka ya **Mungu**. Sio wengi watakaokataa. **—The Review and Herald, August 27, 1903**. {*EVsw 502.4}*

Katika Huduma ya Nyumba kwa Nyumba — Jifunze kuimba nyimbo rahisi kabisa. Hizi zitakusaidia katika kazi ya nyumba kwa nyumba, na mioyo itaguswa kwa mvuto wa Roho Mtakatifu……. Tunajifunza katika Neno kuwa kuna furaha miongoni mwa malaika kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye, na kwamba Bwana mwenyewe anafurahi juu ya kanisa Lake kwa nyimbo. **—The Review and Herald, November 11, 1902.** {*EVsw 502.5}*

Kutoa wito kwaajili Maamuzi kwa Njia ya Wimbo — Katika ndoto zangu usiku uliopita nilikuwa nikizungumza na kundi la vijana. Niliwaomba waimbe wimbo "Almost Persuaded-karibu nishawishike na injili." Baadhi ya waliokuwapo waliguswa sana. Nilijua kuwa walikuwa karibu kushawishika, lakini kama hawangechukua hatua madhubuti za kukusudia ya kumrudia Kristo, msukumo wa hatia yao ungefifia. Mlifanya baadhi ya ungamo, nami nikauliza, "Je, hamtakubali, kuanzia sasa, kusimama upande wa Bwana?" Kama Mkimpokea Yesu, Yeye atawapokea ninyi. **—Letter 137, 1904.** {*EVsw 503.1}*

Uzoefu wa Huduma ya Wimbo Ndani ya Gari la Abiria — Siku ya Sabato tulikuwa na ibada ya wimbo. Ndugu Lawrence, ambaye ni mwanamuziki, aliongoza uimbaji. Abiria wote katika gari walifurahia huduma hiyo sana, wengi wao wakiimba nasi. {*EVsw 503.2}*

Siku ya Jumapili tulifanya tena ibada ya wimbo, kisha Mzee Corliss akatoa hotuba fupi, akitumia maneno haya kama somo: "Tazameni, ni pendo la namna gani Baba alilotupa, kwamba tuitwe watoto wa **Mungu**." Abiria walisikiliza kwa makini na walifurahia ujumbe huo. {*EVsw 503.3}*

Siku ya Jumatatu tuliimba tena, na wote tulionekana kuwa karibu zaidi kwa kila mmoja. —**Letter 135, 1905.** {*EVsw 503.4}*

Muziki Katika Dunia Mpya — Wale wote wanaojitolea kwa **Mungu**, bila kujali chochote kingine, kuwa na kufanya yote apendayo **Mungu**, wataona Mfalme katika uzuri Wake. Watautazama uzuri Wake wa ajabu, na kwa kugusa vinubi vyao vya dhahabu, wataijaza mbingu yote na muziki mtamu na nyimbo kwa ajili ya Mwanakondoo. {*EVsw 503.5}*

Ninafurahi kusikia vyombo vya muziki mlivyo navyo hapa. **Mungu** anataka tuwe navyo. Anataka tumtukuze kwa moyo, nafsi na sauti, tukilitukuza Jina Lake mbele za dunia. —**The Review and Herald, June 15, 1905.** {*EVsw 503.6}*

Mwinjilisti wa Mwimbaji

Kujiandaa kwa Huduma ya Uimbaji — Lazima kuwe na hamasa kubwa zaidi katika kukuza/kuendeleza kipawa cha sauti kuliko ilivyo sasa. Wanafunzi waliopata kujifunza kuimba nyimbo tamu za injili kwa sauti ya kupendeza (melodi) na inayosikika kwa uwazi, wanaweza kutenda wema mwingi kama waimbaji wa injili. Watapata fursa nyingi za kutumia kipawa walichopewa na **Mungu**, wakipeleka melodi na mwanga wa furaha katika maeneo mengi ya upweke yaliyofunikwa na giza la dhambi, huzuni na mateso, wakiimba kwa wale wasiopata nafasi ya kuhudhuria ibada kanisani mara kwa mara. — **The Review and Herald, August 27, 1903.** {*EVsw 504.1}*

Nguvu ya Kuvuta Roho kwa Kristo — Kuna huruma kuu na nyororo na mvuto katika sauti ya mwanadamu, na iwapo mwanafunzi atafanya juhudi ya dhati, atajenga mazoea ya kuzungumza na kuimba ambayo yatakuwa kwake nguvu ya kuwaleta watu kwa Kristo. **— Manuscript 22, 1886.** {*EVsw 504.2}*

Kubeba Ujumbe Maalum kwa Njia ya Wimbo — Wapo wale waliopokea kipawa maalum cha kuimba, na zipo nyakati ambapo ujumbe maalum hubebwa kwa uimbaji wa mtu mmoja au kikundi cha watu. Lakini sio vyema kuacha uimbaji ufanywe na wachache tu. Uwezo wa kuimba ni talanta ya ushawishi, ambayo **Mungu** anatamani kila mmoja wetu aikuze na kuitumia kwa utukufu wa Jina Lake (watu wengi wakiimba ni bora kuliko mmoja tu etc_. — **Testimonies for the Church 7:115, 116 (1902).** {*EVsw 504.3}*

Matamshi ya Wazi na Uelewa wa Maneno — Hakuna maneno yanayoweza kueleza baraka ya kweli ya ibada halisi. Wanadamu wanapoimba kwa Roho na kwa kuelewa, malaika wa mbinguni huungana nao katika wimbo wa shukrani. Yeye aliyetupatia vipawa vyote vinavyotuwezesha kushirikiana na **Mungu**, anatarajia watumishi

Wake wakuze sauti zao, ili waweze kuzungumza na kuimba kwa namna ambayo wote wanaweza kuelewa. Sio uimbaji wa sauti ya juu unaohitajika, bali ni matamshi ya wazi, ya usahihi, na yenye kueleweka. Wote na watumie muda kukuza sauti zao, ili sifa za **Mungu** ziimbwe kwa sauti nyororo na iliyo wazi, si kwa ukali na miungurumo inayokera masikio. Uwezo wa kuimba ni zawadi kutoka kwa **Mungu**; hebu uwezo huo na utumike kwa utukufu Wake. — **Testimonies for the Church 9:143, 144 (1909). {*EVsw 504.4*}**

Vipengele vya Muziki Wenye Athari — Muziki unaweza kuwa nguvu kuu kwa wema; lakini hatulitumii ipasavyo tawi hili la ibada. Mara nyingi uimbaji hufanyika kwa msukumo wa ghafla au kujaza nafasi fulani, na wakati mwingine waimbaji huachwa wajihangaikie wenyewe, na hivyo muziki hupoteza athari yake sahihi kwa akili za waliopo. Muziki unapaswa kuwa na uzuri, huruma, na nguvu. Hebu inueni sauti zenu katika nyimbo za sifa na ibada. Ikiwezekana, tumieni pia vyombo vya muziki kwa ustadi, na ruhusuni harmoni tukufu ipae kwa **Mungu** kama sadaka inayokubalika. **{*EVsw 505.1*}**

Lakini mara nyingine ni vigumu zaidi kuwaongoza na kuwanidhamisha waimbaji na kuwafanya wafanye kazi kwa mpangilio, kuliko kuboresha mazoea ya kuomba na kuhubiri. Wengi wanataka kufanya mambo kwa mtindo wao wenyewe; hawapendi kushauriana, na huwa na uvumilivu mdogo chini ya uongozi. Wakati mpango uliokomaa vyema unahitajika katika kazi ya **Mungu**. Hekima ya kawaida ni zawadi ya thamani katika ibada ya Bwana (commonsense). — **Gospel Workers, 325 (1892). {*EVsw 505.2*}**

Kiongozi wa Nyimbo za Mbinguni — Nimeonyeshwa utaratibu wa mbinguni, uliokamilika, na nimevutiwa sana niliposikia muziki mkamilifu huko. Nilipotoka katika maono, uimbaji wa hapa duniani ulionekana kuwa mkali na usio na mpangilio. Nimewaona makundi ya malaika, wakiwa wamesimama katika umbo la mraba, kila mmoja akiwa na kinubi cha dhahabu... Kuna malaika mmoja anayeongoza kila mara, huanza kwa kugusa kinubi chake na kutoa sauti ya kwanza, kisha wote huungana katika muziki mzuri wa mbinguni. Huwezi kuuelezea. Ni melodi ya mbinguni, ya Kiungu, huku uso wa kila mmoja uking'aa kwa sura ya Yesu, ukiangaza kwa utukufu usioweza kuelezeka. — **Testimonies for the Church 1:146 (1857). {*EVsw 505.3*}**

Programu nzuri iliyotengenezwa ya Nyimbo — Mchungaji au mhubiri asichague nyimbo za kuimbwa kabla hajathibitisha kuwa zinajulikana kwa waimbaji. Mtu sahihi anapaswa kuteuliwa kuongoza kipengele hiki cha ibada, na awe na jukumu la kuhakikisha kuwa nyimbo zilizochaguliwa zinaweza kuimbwa kwa roho na kwa kuelewa. **{*EVsw 506.1*}**

Uimbaji ni sehemu ya ibada kwa **Mungu**, lakini iwapo utafanyika kwa namna isiyo ya mpangilio yaani hovyo ovyo tu, basi hautaleta heshima kwa Ukweli, wala kwa **Mungu**. Lazima kuwe mfumo fulani na mpangilio na nidhamu katika kipengele hiki kama ilivyo kwa kazi nyingine yoyote ya Bwana. Panga kikundi cha waimbaji bora, ambao sauti zao zinaweza kuliongoza kusanyiko, kisha wote wanaotaka kuimba, waungane nao. Waimbaji wanapaswa kujitahidi kuimba kwa harmoni; watoe muda kwa mazoezi, ili watumie kipawa hiki kwa utukufu wa **Mungu**. **{*EVsw 506.2*}**

Lakini uimbaji usiruhusiwe kuvuruga mawazo ya ibada. Kama mojawapo ya vipengele vitahitaji kuachwa, basi ni heri kuacha uimbaji. — **The Review and Herald, July 24, 1883. {*EVsw 506.3*}**

Mvuto wa Sauti ya Mwanadamu — Sauti ya mwanadamu inayomwimbia **Mungu** kutoka moyoni iliojaa shukrani na furaha, humfurahisha zaidi **Mungu** kuliko muziki wa vyombo vyote vilivyowahi kutengenezwa na mikono ya binadamu. **— Letter 2c, 1892. {*EVsw 506.4*}**

Tahadhari — Nilipelekwa katika baadhi ya mazoezi yenu ya uimbaji, na nikalazimishwa kusoma hisia zilizokuwa katika kundi hilo, wewe ukiwa kiongozi wake. Kulikuwapo na wivu wa kijinga, husuda, mashaka mabaya, na maneno ya kashfa..... Huduma ya moyo ndiyo **Mungu** anayoitaka; taratibu na ibada za midomo ni kama upatu unaogonga-gonga tu, na shaba iliayo bila maana. Uimbaji wenu ni kwa maonyesho tu, si kwa kusifu **Mungu** kwa Roho na uelewa. Hali ya moyo huonyesha ubora wa dini ya mtu anayedai kuwa wa Mwenyezi Mungu- Kiungu. **— Letter 1a, 1890. {*EVsw 507.1*}**

Msisitizo Katika Uimbaji wa Kusanyiko

Kwaya na Uimbaji wa Kusanyiko — Katika mikutano inayofanyika, na wateuliwe watu wachache kushiriki katika huduma ya uimbaji. Na uimbaji uambatane na vyombo vya muziki vinavyopigwa kwa ustadi. Hatupaswi kupinga matumizi ya muziki wa ala katika kazi yetu. Kipengele hiki cha ibada kinapaswa kuendeshwa kwa makini, kwani ni sifa kwa **Mungu** katika wimbo. **{*EVsw 507.2*}**

Uimbaji usifanywe kila wakati na wachache tu. Kadiri iwezekanavyo, kusanyiko zima na lishiriki. — **Testimonies for the Church 9:144 (1909). {*EVsw 507.3*}**

Huduma ya Uimbaji — Uimbaji usifanywe na watu wachache tu. Wote waliopo wahimizwe kushiriki katika huduma ya nyimbo. — **Letter** 157, 1902. **{*EVsw 507.4*}**

Kufikia Upatanifu wa Kwaya ya Mbinguni — Muziki ni sehemu ya ibada ya **Mungu** katika viwanja vya mbinguni. Tunapaswa kujitahidi, katika nyimbo zetu za sifa, kufikia kadiri iwezekanavyo harmoni ya kwaya za mbinguni. Mara nyingi nimeumia kusikia sauti zisizo na mafunzo, zilizopandishwa hadi kilele cha juu, zikipiga kelele kama mayowe, kwa maneno matakatifu yanayohimiza sifa. Sauti hizo kali, zinazopasua masikio, hazifai kwa ibada ya **Mungu** iliyo ya heshima na furaha. Natamani kufumba masikio yangu au kukimbia kutoka mahali hapo, nami hufurahia sana zoezi hilo la kuumiza linapomalizika. **{*EVsw 507.5*}**

Wale wanaoufanya uimbaji kuwa sehemu ya ibada takatifu wanapaswa kuchagua nyimbo zenye muziki unaofaa kwa tukio hilo, si nyimbo za huzuni za mazishi, bali zile za furaha ila zenye kicho. Sauti inaweza na inapaswa kupunguzwa, kulainishwa, kusalimishwa na kutulizwa. — **The Signs of the Times, Juni 22, 1882. {*EVsw 508.1*}**

Kwa Moyo na Kwa Uelewa — Nikaonyeshwa kuwa wote wanapaswa kuimba kwa Roho na kwa kuelewa pia. **Mungu** hapendezwi na sauti zisizo na mpangilio na zisizoeleweka. Kilicho sahihi huupendeza zaidi moyo Wake kuliko kisichofaa. Na kadiri watu wa **Mungu** wanavyoweza kufikia uimbaji ulio sahihi na wa harmoni, ndivyo **Mungu** hutukuzwa zaidi, kanisa hunufaika, na wasioamini huvutwa kwa njia nzuri. — **Testimonies for the Church 1:146 (1857). {*EVsw 508.2*}**

Pasipo Roho na Uelewa — Wengi wanaimba nyimbo nzuri katika mikutano, nyimbo za kile watakachofanya au wanachonuia kufanya; lakini baadhi hawafanyi hayo mambo; hawaimbi kwa Roho na kwa kuelewa pia. Vivyo hivyo na katika usomaji wa Neno la **Mungu**, baadhi hawapati faida, kwa kuwa hawaliingizi somo hili ndani ya maisha yao, hawalitekelezi. **— The Review and Herald, September 27, 1892. {*EVsw 508.3*}**

Viongozi wa Muziki

Wale Wenye Mioyo Iliyojitolea Kazi Hii

Katika jitihada zao za kuwafikia watu, wajumbe wa Bwana hawapaswi kufuata njia za kidunia. Katika mikutano inayoandaliwa, hebu wasitegemee waimbaji wa kidunia au maonesho ya kisanii ili kuvutia watu. Je, wale wasio na hamu yoyote ya Neno la **Mungu**, ambao hawajawahi kulisoma kwa nia ya dhati ili kulielewa, wanaweza kuimba kwa roho na kwa ufahamu kweli? Je, mioyo yao inaweza kuambatana na maneno ya wimbo mtakatifu? Je, kwaya ya mbinguni itawezaje kuungana na muziki ambao ni wa kiibada tu kwa nje bila uhai wa kiroho? (umbo la ibada tu, lenye urasmi) **— Testimonies for the Church, 9:143 (1909) {*EVsw 508.4*}**

Kuimba Kwa Upole na Unyenyekevu

Mungu anawezaje kutukuzwa iwapo mnaitegemea kwaya ya kidunia inayoimba kwa ajili ya malipo? Ndugu yangu, ukiona mambo haya kwa mwanga wa kweli, utaongoza mikutano yako kwa kuimba kwa upole na unyenyekevu, na kuwaalika wote walioko mkutanoni kuungana katika wimbo. Hata kama baadhi ya waliopo hawana sauti zenye mvuto kama wengine, maadamu uimbaji ni wa namna ambayo malaika wa mbinguni wanaweza kuungana nao, basi mvuto wa kipekee huachwa mioyoni—mvuto ambao hawezi kutolewa na nyimbo kutoka midomo isiyotakaswa. — **Barua 190, 1902 {*EVsw 509.1*}**

Waimbaji wa Kidunia

Epukeni kuwaajiri waimbaji wa kidunia ikiwa hilo linawezekana. Kusanyeni waimbaji watakaoimba kwa roho na kwa ufahamu pia. Maonyesho ya ziada mnayoyafanya mara nyingine huleta gharama zisizo za lazima, ambazo ndugu hawapaswi kuletewa kama mzigo. Zaidi ya hayo, baada ya muda wale wasioamini hawatakuwa tayari tena kuchangia fedha kwa ajili ya kugharamia mambo hayo. — **Letter 51, 1902 {*EVsw 509.2*}**

Kukubali Msaada wa Muziki Unapotolewa

Katika mikutano inayoandaliwa, uimbaji usipuuzwe. **Mungu** anaweza kutukuzwa kupitia sehemu hii ya ibada. Na wanapoonekana waimbaji walio tayari kujitolea, basi huduma yao ipokelewe. Hata hivyo, fedha zisihusishwe kama njia ya kuwaajiri waimbaji. Mara nyingi, uimbaji wa nyimbo rahisi za imani na kusanyiko lote huwa na mvuto wa kipekee unaochangamsha watu na ambao hata kwaya yenye ujuzi mkubwa huenda isiuwe nao. — **Letter 49, 1902 {*EVsw 509.3}***

Muziki Unaomkera Mungu

Maonyesho ya nje siyo dini, wala siyo utakaso. Hakuna kitu kinachomkera **Mungu** zaidi kama uchezeshaji wa ala za muziki kwa namna ya maonyesho, ilhali washiriki wa huduma hiyo hawajatakaswa, wala hawaimbi kwa moyo kwa ajili ya Bwana. Sadaka yenye harufu tamu na inayopendeza mbele za **Mungu** ni moyo ulionyenyekea kwa kujikana nafsi, kwa kubeba msalaba na kumfuata Yesu. **{*EVsw 510.1}***

Hatuna muda wa kupoteza tukitafuta vitu vinavyopendeza tu hisia za mwili. Tunahitaji kujichunguza kwa undani wa moyo. Kwa machozi na maungamo ya kweli, hebu tujitahidi kumkaribia **Mungu**, Naye atatukaribia. — **Review and Herald, November 14, 1899 {*EVsw 510.2}***

Mungu Hutukuzwa

Mungu hutukuzwa kupitia nyimbo za sifa zitokazo kwa moyo safi uliojaa upendo na kujitoa wakfu kwa ibada Kwake. — **Testimonies for the Church, 1: 509 (1867) {*EVsw 510.3}***

Tahadhari za Wakati Muafaka

Sifa za Muziki Mzuri

Maboresho makubwa yanaweza kufanyika katika uimbaji. Wengine hudhani kwamba kadiri wanavyoimba kwa sauti kubwa ndivyo wanavyotoa muziki zaidi; lakini kelele si muziki. Uimbaji mzuri unapaswa kufanana na wimbo wa ndege—uliotulia na wenye mvuto wa kimelodi. **{*EVsw 510.4}***

Katika baadhi ya makanisa yetu, nimesikia solo ambazo hazifai kabisa kwa ibada katika nyumba ya Bwana. Midundo mirefu inayovutwa sana na sauti zisizo za kawaida kama zile za waimbaji wa opera, sio za kupendeza kwa malaika. Malaika hufurahia nyimbo rahisi za sifa zinazoimbwa kwa sauti ya kawaida. Nyimbo ambazo kila neno linaimbwa kwa uwazi, kwa lafudhi ya kimuziki, ndizo nyimbo ambazo malaika wanazojiunga kuimbia nasi. Hujiunga nasi katika kiitikio cha nyimbo hizo endapo zinaimbwa kwa moyo, kwa roho na kwa ufahamu. **—Manuscript 91, 1903. {*EVsw 510.5}***

Uwiano Unaofaa wa Muda Unaotolewa kwa Uimbaji

Maboresho yanaweza kufanyika katika namna tunavyoendesha mikutano ya kambi, ili kwamba wote wanaohudhuria wapate huduma ya moja kwa moja zaidi. Kuna mikutano ya kijamii inayofanyika chini ya hema kubwa ambapo wote hukusanyika kwa ibada; lakini kwa kuwa ni mikutano mikubwa sana, ni wachache tu wanaopata nafasi ya kushiriki, na wengi huzungumza kwa sauti ya chini kiasi kwamba ni wachache wanaoweza kuwasikia…….. Katika hali nyingine, muda mwingi ulitumiwa katika kuimba. Kulikuwa na wimbo mrefu kabla ya sala, wimbo mrefu baada ya sala, na nyimbo nyingi katikati ya ibada. Hivyo, muda wa thamani ulitumiwa vibaya, na hata haikupatikana nusu ya faida ambayo ingeweza kupatikana kama vipindi hivi vya thamani vingesimamiwa vizuri. —**The Review and Herald, November 27, 1883. {*EVsw 511.1}***

Sherehe na Maonyesho ya Juu

Mienendo ya nje na sherehe siyo Ufalme wa **Mungu**. Sherehe huwa nyingi na za kupindukia pale ambapo kanuni hai za Ufalme wa **Mungu** hupotezwa. Lakini siyo mionekano ya kidini anayoitaka Kristo. Yeye Anatamani kupokea kutoka katika shamba Lake la mizabibu matunda ya utakatifu na kutokuwa na ubinafsi, matendo ya wema, rehema, na Kweli. **{*EVsw 511.2}***

Nguo za kifahari, uimbaji mzuri wa kitaaluma, na ala za muziki kanisani haviwavutii malaika wa mbinguni. Mambo haya ni kama matawi ya mtini usiozaa matunda, wenye majani tu ya kuonekana. Kristo anatafuta matunda—kanuni za wema, huruma, na upendo. Hizi ndizo kanuni za mbinguni, na zinapodhihirishwa katika maisha ya wanadamu, twaweza kujua kuwa Kristo ameumbika ndani yetu, tumaini la utukufu. Kusanyiko linaweza kuwa masikini zaidi katika nchi, pasipo muziki wala mapambo ya nje, lakini kama lina kanuni hizi, washiriki wake wanaweza kuimba, kwa kuwa furaha ya Kristo imo mioyoni mwao, na

hiyo wanaweza kuitoa kama harufu nzuri ya manukato ya sadaka kwa **Mungu**. —**Manuscript 123, 1899.** {*EVsw 511.3}*

Muziki Unaokubalika na Mungu

Vitu vya ziada vilivyoingizwa katika ibada huko _____ ni lazima vikemewe kwa nguvu... Muziki hupendeza kwa **Mungu** pale tu moyo unapokuwa umetakaswa na kufanywa laini na takatifu kupitia vipaji hivyo. Lakini wengi wanaofurahia muziki hawajui lolote kuhusu kuimba nyimbo za moyo kwa Bwana. Mioyo yao imekwenda "baada ya sanamu zao." —**Letter 198, 1899.** {*EVsw 512.1}*

Matumizi Mabaya ya Muziki

Wakati WaKristo wa kweli watafikia kiwango cha juu ambacho wanaweza kufikia, unyofu wa Kristo utaonekana katika kila sehemu ya ibada yao. Mienendo ya nje, sherehe, maumbo ya ibada yasiyofaa na ustadi wa kimuziki si nguvu ya kanisa. Lakini mambo haya yamechukua nafasi ambayo **Mungu** anapaswa kuwa nayo, kama ilivyokuwa kwa Wayahudi katika ibada zao. {*EVsw 512.2}*

Bwana amenifunulia kuwa moyo unapotakaswa na washiriki wa kanisa kuwa washiriki wa asili ya **Kiungu**, basi nguvu fulani hutoka kwa kanisa linaloamini ile Kweli, ambayo hutoa uimbaji wa moyoni. Wanaume na wanawake hawatategemea ala za muziki, bali nguvu na neema ya **Mungu**, ambayo huleta furaha kamili. Kuna kazi ya kufanyika ya kuondoa taka zilizoletwa ndani ya kanisa... {*EVsw 512.3}* Ujumbe huu hauhusu tu kanisa la _____, bali pia kila kanisa lingine lililofuata mfano huo. —**Manuscript 157, 1899.** {*EVsw 512.4}*

SEHEMU YA 16—UINJILISTI WA TIBA

Njia ya Kuangilia

Kufungua Milango kwa Uinjilisti

Hakuna jambo linalofungua milango kwa ajili ya Ukweli kama kazi ya uinjilisti wa umishenari wa tiba. Kazi hii huifikia mioyo na akili za watu, na huwa njia ya kuwaongoa wengi kuipokea Kweli. {*EVsw 513.1}*

Mwinjilisti aliyejiandaa kuwahudumia wenye magonjwa ya mwili hupewa nafasi adhimu zaidi ya kuwahudumia wenye magonjwa ya dhambi. Mwinjilisti wa namna hii anapaswa kuwa na mamlaka ya kubatiza wale wanaoongoka na kutamani ubatizo... Kazi ya umishenari wa tiba ni mkono wa kuume wa injili, kufungua milango ya kutangaza ujumbe... {*EVsw 513.2}*

Milango ambayo ilifungwa kwa yule anayehubiri tu injili hufunguliwa kwa mishenari wa afya mwenye maarifa. **Mungu** huwafikia watu kwa njia ya kupunguza mateso ya mwili. —**Manuscript 58, 1901.** {*EVsw 513.3}*

Njia Kuu ya Kuingilia

Naweza kuona katika uongozi wa Bwana kwamba kazi ya umishenari wa tiba inapaswa kuwa ndio daraja kuu la kuingia ambapo roho inayoumwa itaweza kufikiwa. —**Counsels on Health, 535 (1893).** {*EVsw 513.4}*

Huondoa Chuki na ubaguzi

Kazi ya kimishenari ya kitabibu ni kazi ya mwanzo ya injili, mlango ambao kupitia kwake kweli ya wakati huu hupenya katika nyumba nyingi..... Onyesho la kanuni za matengenezo ya afya litafanya mengi katika kuondoa upendeleo dhidi ya kazi yetu ya uinjilisti. Tabibu Mkuu, Mwanzilishi wa kazi ya umishenari wa tiba, atawabariki wote wanaojitahidi kutoa Kweli ya wakati huu kwa njia hiyo. —**Counsels on Health, 497 (1902).** {*EVsw 513.5*}

Hufungua njia kuingia ndani ya Mioyo

Fanya kazi ya kimishenari ya tiba. Ndipo utapata njia na nafasi ya kuingia mioyoni mwa watu. Njia itatayarishwa kwa ajili ya kutangaza Kweli kwa kudhamiria zaidi. Utagundua kwamba kwa kuwapunguzia mateso ya kimwili unapata nafasi ya kuwahudumia mahitaji ya kiroho... {*EVsw 514.1*}

Muunganiko wa kazi ya Kristo ya huruma kwa mwili pamoja na kazi yake ya huruma kwa roho ndio tafsiri ya Kweli ya Injili ya Kristo. **—An Appeal for the Medical Missionary College, uk. 14, 15 (1902).** {*EVsw 514.2*}

Mahubiri ya Matengenezo

Nimejulishwa na Kiongozi wangu kwamba sio tu waumini wa Kweli wanapaswa kuishi kulingana na kanuni za matengenezo ya afya, bali pia wafundishe kwa bidii wengine; kwa kuwa matengenezo haya yatakuwa chombo cha kuwafikishia wasioamini Ukweli. Wataanza kufikiri kwamba ikiwa tuna mawazo mazuri kiasi hiki kuhusu afya na kiasi, basi hakika kuna jambo la thamani katika imani yetu ya kidini linalostahili kuchunguzwa. Tukidhoofika na kurudi nyuma katika matengenezo ya afya, tutapoteza ushawishi wetu mkubwa mbele ya ulimwengu. {*EVsw 514.3*}

Masomo yanayotolewa katika mikutano yetu mikubwa yanapaswa kuwa yenye asili ya matengenezo. Vipawa vyote vinavyopatikana vinapaswa kutumika kuwasilisha ujumbe huu kwa watu. {*EVsw 514.4*}

Wengi wamechoshwa na kuchukizwa na ibada kavu isiyo na uhai inayoonekana katika ulimwengu wote wa Kikristo (dry formulas). Wengine wamekuwa wapagani kwa sababu hawaoni uchaji wa Kweli kwa **Mungu** miongoni mwa wanaodai kuwa WaKristo. Kazi nzuri inaweza kufanyika kuandaa njia ya kufikisha Ukweli ikiwa ushuhuda thabiti utatolewa juu ya kazi ya afya na kiasi... {*EVsw 514.5*}

Kufundisha kanuni za Kweli za afya na kiasi si jambo la kupuuzwa kana kwamba halina umuhimu; kwa kuwa karibu kila familia inahitaji mafundisho kuhusu jambo hili. Karibu kila mtu anahitaji dhamiri yake iamshwe ili awe mtendaji wa Neno la **Mungu**, aishi kwa kujinyima, Kujikana nafsi na ajiepushe na tamaa zisizo halali za chakula-uchu wa chakula usiofaa na ulafi. Unapowafundisha watu kuhusu hekima ya kanuni za matengenezo ya afya, unafanya kazi kubwa ya kuandaa njia ya kufikisha Ukweli wa wakati huu. Kiongozi wangu alisema, “Fundisha, Elimisha, Elimisha.” Akili lazima itaangaziwe, kwa maana ufahamu wa watu umetiwa giza. Shetani hupata nafasi ya kuifikia nafsi kwa njia ya tamaa zilizopotoka ili kuiharibu na kuiangamiza. —**Letter 1, 1875.** {*EVsw 515.1*}

Kuunganishwa Imara na Huduma ya Neno

Kanuni za matengenezo ya afya zinapatikana katika Neno la **Mungu**. Injili ya afya inapaswa kuunganishwa kwa uimara na huduma ya Neno. Ni mpango wa Bwana kwamba athari ya urejeshwaji wa afya, uponyaji na matengenezo ya afya iwe sehemu ya juhudi kuu ya mwisho ya kuitangaza injili. —**Medical Ministry, uk. 259 (1899).** {*EVsw 515.2*}

Katika Maeneo Mengi

Kama njia ya kushinda chuki na ubaguzi na kufikia akili za watu, kazi ya umishenari wa tiba lazima ifanyike, si katika sehemu moja au mbili tu, bali katika maeneo mengi ambayo bado Ukweli haujatangazwa. Tunapaswa kufanya kazi kama wamishenari wa injili ya afya, kuponya roho zenye ugonjwa wa dhambi, tukiwaambia watu walioumia kwa dhambi ujumbe wa wokovu. Kazi hii itavunja chuki kwa namna ambayo hakuna kitu kingine kinavyoweza. —**Testimonies for the Church, 9: 211 (1909).** {*EVsw 515.3*}

Muhimu kwa Maendeleo ya Kazi ya Mungu

Huduma ya umishenari ya afya ni mkono wa kulia wa injili. Ni muhimu kwa maendeleo ya kazi ya **Mungu**. Kupitia kazi hii, wanawake na wanaume wanaelekezwa kuona umuhimu wa mazoea sahihi na nidhamu ya kuishi, na nguvu ya kuokoa ya Ukweli huwekwa wazi na kujulikana. Kila mji unapaswa kuingiliwa na watenda

kazi waliofunzwa kwa huduma ya umishenari wa tiba. Kama mkono wa kulia wa ujumbe wa malaika wa tatu, njia za **Mungu** za kutibu magonjwa zitafungua milango ya kuingiza Ukweli wa wakati huu. —**Testimonies, 7: 59 (1902). {*EVsw 515.4*}**

Hufungua Milango

Kila mahali kuna wagonjwa, na wale wanaokwenda kufanya kazi kwa niaba ya Kristo wanapaswa kuwa wanamatengenezo wa afya wa kweli, waliotayari kuwapa wagonjwa tiba rahisi zitakazowapunguzia maumivu, na kisha kuwaombea. Kwa kufanya hivyo, watafungua mlango wa kuingiza Ukweli. Kufanya kazi hii kutaleta matokeo mema. —**Medical Ministry, uk. 320 (1911). {*EVsw 516.1*}**

Kusudi la Kweli la Uinjilisti wa Tiba

Huleta Mavuno Yenye Thamani

Kazi ya umishenari wa tiba hutoa nafasi ya kuendeleza kazi ya uinjilisti kwa mafanikio. Ni katika kuunganisha juhudi hizi ndipo tunaweza kutarajia kuvuna matunda ya thamani kwa Bwana. —**Review and Herald, September 7, 1905. {*EVsw 516.2*}**

Kufariji, Kuponya, na Kusaidia

Yesu aliwatafuta watu mahali walipo, na aliwawekea mbele Ukweli mkuu kuhusu ufalme Wake. Alipokuwa akipita kutoka mahali hadi mahali, aliwabariki na kuwafariji walioumia, na akawaponya wagonjwa. Hii ndiyo kazi yetu. **Mungu** anataka tuwasaidie wahitaji na kuwapa unafuu katika uhitaji wao. —**Letter 54, 1898. {*EVsw 516.3*}**

Mfano Katika Isaya 58

Sura ya hamsini na nane ya kitabu cha Isaya ina ujumbe wa wakati huu kwa watu wa **Mungu**. Hapa tunaona jinsi kazi ya umishenari wa tiba na huduma ya injili vinavyopaswa kufungamanishwa pamoja katika kupeleka ujumbe kwa dunia. Kwa wale wanaoshika Sabato ya Bwana, limewekwa jukumu la kufanya kazi ya rehema, ukarimu na fadhili. Kazi ya umishenari wa tiba inapaswa kufungamanishwa na ujumbe huu na kutiwa muhuri wa **Mungu**. **—Manuscript 22, 1901. {*EVsw 516.4*}**

Mioyo Hulainishwa

Ulimwengu unahitaji tiba ya kuondoa sumu ya dhambi. Wakati mmishenari wa tiba anapofanya kazi kwa busara na akili mahiri kupunguza mateso na kuokoa maisha, mioyo huwekwa tayari kupokea kwa kulainishwa. Wale wanaosaidiwa hujaa shukrani. **{*EVsw 517.1*}**

Pale mmishenari wa tiba anaposhughulika na mwili, **Mungu** anafanya kazi juu ya moyo. Maneno ya faraja yanayosemwa huwa kama mafuta laini ya uponyaji, yakileta tumaini na imani. Mara nyingi mtoa huduma mwenye ujuzi hupata nafasi ya kumweleza mgonjwa kazi ya Kristo alipokuwa duniani. Mwambie mtu anayepata mateso habari za upendo wa **Mungu**. **—Manuscript 58, 1901. {*EVsw 517.2*}**

Kurejesha Imani kwa Mungu na Binadamu

Wengi wamepoteza ufahamu wa mambo ya milele, wamepoteza mfano wa **Mungu**, na hata hawajui kama wana nafsi za kuokolewa. Hawana imani kwa **Mungu** wala ujasiri kwa wanadamu. Wanapoona mtu asiye na tamaa ya sifa za kidunia wala malipo, akiingia katika nyumba zao zilizojaa mateso, akiwahudumia wagonjwa, kuwalisha wenye njaa, kuwavisha walio uchi, na kwa upole kuwaelekeza kwa Mwenyezi Mungu, ambaye ni mtoa huduma ni mjumbe Wake tu—wanapoona haya, mioyo yao huguswa. Shukrani hububujika kama chemichemi. Imani huamshwa kwa jotojoto. Wanatambua kuwa **Mungu** anawajali, na wanakuwa tayari kusikiliza Neno Lake linapofunguliwa. **{*EVsw 517.3*}**

Watoto wa **Mungu** wanapojitoa kwa kazi hii, wengi wataushika mkono wa Kristo unaonyoshwa kuwaokoa. Watashawishika kuacha njia zao mbaya na za uovu. Baadhi yao watamwamini kwa Kristo, watainuliwa hadi nafasi za juu za utumishi, na kuaminiwa kwa majukumu ya kuwaokoa wengine. Kwa kuwa wamepitia shida hizo, wanajua mahitaji ya wale wanaowatumikia kwa uzoefu. Wanajua namna ya kuwasaidia; wanajua njia bora ya kuwaokoa waliopotea. Mioyo yao imejaa na kuamshwa kwa shukrani kwa baraka walizopokea; wamejawa na upendo, na nguvu zao zimeimarishwa ili kuwainua wengine ambao hawawezi kuinuka pasipo msaada. **—Review and Herald, August 3, 1905. {*EVsw 517.4*}**

Sayansi ya Kweli ya Huduma ya Tiba

Masomo ya upasuaji na sayansi nyingine ya tiba yanapewa umakini na nafasi kubwa ulimwenguni, lakini sayansi ya Kweli ya huduma ya umishenari wa matibabu, inayoendeshwa kama Kristo alivyoifanya, ni jambo geni kwa makanisa ya madhehebu mbalimbali na kwa ulimwengu. Lakini kazi hii itapata nafasi yake sahihi mara wale wanaoitwa kuwa watu wa nuru kubwa— Waadventista wa Sabato—watakapozinduka kutambua wajibu wao na kuboresha fursa zao. {*EVsw 518.1*}

Vijana wa kiume na wa kike lazima wafundishwe ili wajitayarishe kuwa madaktari na wauguzi wa umishenari wa tiba. Lakini kabla ya watendakazi hawa kupelekwa katika uwanja wa kazi, lazima waonyeshe ushahidi wa kuwa na roho ya utumishi, kwamba wanapumua hewa ya huduma ya umishenari wa tiba, na kwamba wako tayari kwa kazi ya uinjilisti. {*EVsw 518.2*}

Wanafunzi wanapaswa kuandaliwa kwa ajili ya kazi ya utume wa mwanzo (pioneer missionary work). Wamisheni wa afya wanaopelekwa nchi za kigeni wanapaswa kwanza kupata mafunzo ya kina. Hao ni mabalozi wa Kristo, na wanapaswa kumtumikia kwa ujuzi wote walionao, huku wakiomba kwa bidii kwamba Tabibu Mkuu awaonee huruma na kuokoa kwa uwezo Wake wa miujiza. —**Manuscript 33, 1901.** {*EVsw 518.3*}

Huduma ya Kweli ya Umishenari wa Tiba

Funzo tunalopaswa kujifunza ni: Je, ni nini huduma ya Kweli ya umishenari wa tiba katika mstari wa injili kwa vitendo? Hebu tuweke mbele ya watu kila mahali masharti ya uzima wa milele, kama yalivyoandikwa katika Neno la **Mungu**. Wale wanaotii Neno hili, wakimcha **Mungu** na kumpa Mungu heshima anayostahili, wataonyesha katika utendaji wao kwamba wanaelewa maana ya huduma ya Kweli ya umishenari wa tiba. Nafsi inapaswa kunyenyekezwa, na sio kutukuzwa... Ni jambo lenye matokeo makubwaa kwamba wale wote wanaodai kuelewa kazi ya huduma ya umishenari wa tiba katika injili, wafundishe kanuni za ile Kweli. — **Manuscript 126, 1905.** {*EVsw 519.1*}

Uhusiano na Huduma ya Injili

Hufanya Uinjilisti Kufanikiwa Maradufu Zaidi

Baadhi ya watu wanashindwa kabisa kutambua umuhimu wa wamishenari kuwa pia wamishenari wa tiba. Mhubiri wa injili atakuwa na mafanikio maradufu katika kazi yake iwapo ataelewa jinsi ya kutibu magonjwa..... Mhubiri wa injili ambaye pia ni mtaalamu wa afya, ambaye anaweza kutibu magonjwa ya mwili, ni mtendakazi mwenye ufanisi zaidi kuliko yule asiyeweza kufanya hivyo. Kazi yake kama mhubiri wa injili huwa imekamilika zaidi. **—Medical Ministry, 245 (1901)** {*EVsw 519.2*}

Isitenganishwe Kamwe

Huduma ya umishenari wa tiba haipaswi kutenganishwa hata kidogo na huduma ya injili. Bwana ameagiza kwamba hizi kazi mbili ziunganishwe kwa karibu kama mkono na mwili. Bila muunganiko huu, sehemu yoyote kati ya hizi mbili haiwezi kuwa kamili. Huduma ya umishenari wa tiba ni taswira ya injili kwa vitendo-(upendo kwa vitendo). — **Testimonies For The Church 6:240, 241 (1900).** {*EVsw 519.3*}

Mipango ya Bwana kwa Ajili ya Kazi Iliyounganishwa

Haja ya ulimwengu leo haiwezi kutimizwa kikamilifu na wahudumu wa **Mungu** waliopewa mwito kuhubiri injili ya milele kwa kila kiumbe. Ingawa ni vyema, kadiri inavyowezekana, kwa watendakazi wa injili kujifunza jinsi ya kuhudumia mahitaji ya mwili pamoja na yale ya roho—kwa kufuata mfano wa Kristo—lakini hawawezi kutumia muda na nguvu zao zote kuwasaidia wale wanaohitaji msaada. Bwana ameagiza kwamba pamoja na wale wanaohubiri Neno, waunganishwe watendakazi wa huduma ya umishenari wa tiba—madaktari na wauguzi WaKristo waliopata mafunzo maalum ya kuponya magonjwa na kuongoa roho. — **Counsels to Parents, Teachers, and Students, 468 (1913)** {*EVsw 519.4*}

Wamishenari wa Tiba ni Wainjilisti

Madaktari wakumbuke kuwa mara nyingi watahitajika kutekeleza wajibu wa mchungaji. Wamishenari wa tiba huangukia katika kundi la wainjilisti. Watendakazi hawa wanapaswa kwenda wawili wawili, ili waweze kuomba na kushauriana pamoja. Kamwe wasitumwe peke yao. Bwana Yesu Kristo

aliwatuma wanafunzi Wake wawili wawili katika miji yote ya Israeli. Aliwapa agizo: "**Luka 10:9** *waponyeni wagonjwa waliomo, waambieni, Ufalme wa Mungu umewakaribia.*" {*EVsw 520.1}*

Tunaelekezwa katika Neno la **Mungu** kwamba mwinjilisti ni mwalimu. Apaswa pia kuwa mmishenari wa tiba. Lakini si wote wamepewa kazi ile ile. "Alitoa wengine kuwa mitume, wengine manabii, wengine wainjilisti, wengine wachungaji na waalimu; kwa ajili ya kuwakamilisha watakatifu, kwa kazi ya huduma, kwa kuujenga mwili wa Kristo….." {*EVsw 520.2}*

Wale wanaofanya kazi kama wachungaji/wahubiri katika konferensi zetu wanapaswa kufahamu pia kazi ya kuwahudumia wagonjwa. Hakuna mhubiri anayepaswa kujivunia ujinga katika mambo ambayo anapaswa kuwa na hekima. Huduma ya umishenari wa tiba huunganisha mtu na wanadamu wenzake na pia na **Mungu**. Maonyesho ya huruma na kuaminiana hayatakiwi kuzuiwa kwa muda au umbali. **—Medical Ministry, 249, 250 (1901).** {*EVsw 520.3}*

Kutofautiana Miongoni mwa Wahubiri

Kuna watendakazi WaKristo wengi ulimwenguni ambao bado hawajasikia Kweli kuu na za ajabu tulizopewa. Hawa wanafanya kazi nzuri kulingana na mwanga waliopokea, na wengi wao wamepiga hatua kubwa zaidi katika kazi ya vitendo kuliko wale waliopata mwanga mkubwa na fursa nyingi. {*EVsw 521.1}*

Kutokujali ambako kumekuwapo miongoni mwa wahubiri wetu kuhusu matengenezo ya afya na huduma ya umishenari wa tiba ni jambo la kushangaza. Baadhi ya watu wasiokiri kuwa WaKristo wanaheshimu mambo haya zaidi kuliko baadhi ya watu wetu, na isipokuwa tutachukua hatua, hakika watatutangulia na kwenda mbele yetu. **—Testimonies to Ministers and Gospel Workers, 416, 417 (1898)** {*EVsw 521.2}*

Mwenyekiti wa Konferensi Aitambue

Tunawaomba sasa wale watakaochaguliwa kuwa wenyeviti wa koferensi zetu za kanisa waanze kazi kwa njia sahihi katika maeneo ambayo bado hakuna kazi yoyote. Watambue kazi ya umishenari wa tiba kama mkono wa msaada wa **Mungu**. Kama wakala Wake aliyeagizwa, kazi hii inapaswa kupewa nafasi na kutiwa moyo. Wamishenari wa tiba wanapaswa kupewa moyo sawa na mwinjilisti yeyote aliyeidhinishwa. Ombeni pamoja na watendakazi hawa. Wapeni ushauri wanapouhitaji. Msivunje bidii wala nguvu zao. Hakikisheni kwa kujitolea kwenu binafsi kuweka kiwango cha juu mbele yao. Watendakazi wanahitajika sana katika shamba la Bwana, na hakuna neno la kukatisha tamaa linalopaswa kusemwa kwa wale wanaojitoa wakfu kwa kazi hii. **—Medical Ministry, 240, 241 (1901).** {*EVsw 521.3}*

Katibu wa Idara ya Huduma ya umishenari wa Tiba wa Konferensi

Huduma ya umishenari wa tiba inapaswa kuunganishwa kwa karibu na kazi ya kuhubiri. Watu wanaopaswa kuteuliwa kwa kazi hii ni wale waliothibitishwa kuwa waaminifu, waadilifu katika kanuni. Katika kila konferensi, mtu mmoja anapaswa kuwekwa wakfu kusimamia kazi hii. Awe mtu mwenye ushahidi wa dhamiri safi, mnyoofu katika kushughulika na watu wa dunia na wale wa imani yetu. Asiwe mwenye tamaa wala ubinafsi. **—Letter 139, 1898.** {*EVsw 521.4}*

Tahadhari Dhidi ya Kazi Huru Isiyounganishwa

Kadiri kazi ya huduma ya umishenari wa tiba inavyopanuka, kutakuwa na majaribu ya kuifanya isitegemee konferensi zetu. Lakini nimeonyeshwa kuwa mpango huu si sahihi. Mifumo mbalimbali ya kazi yetu ni sehemu za kazi moja kuu. Zote zina kiini kimoja... {*EVsw 522.1}*

Katika kazi ya injili, Bwana hutumia vyombo mbalimbali, na hakuna chochote kinachopaswa kutenganisha vyombo hivi. Kamwe sanitarium au taasisi ya afya isianzishwe kama mpango wa kujitegemea nje ya kanisa. Madaktari wetu wanapaswa kuungana na kazi ya wahubiri wa injili. Kupitia kazi zao, roho zitaongolewa, na jina la **Mungu** litukuzwe….. {*EVsw 522.2}*

Mungu hakupanga kazi ya umishenari wa tiba kuchukua nafasi ya ujumbe wa malaika wa tatu. Mkono usiwe mwili. Ujumbe wa malaika wa tatu ni ujumbe wa injili kwa siku hizi za mwisho, na kamwe usitiwe kivuli kwa maslahi mengine na kufanya kuonekana siyo wa maana au jambo la msingi. Endapo katika taasisi

zetu jambo lolote litapewa nafasi ya juu kuliko ujumbe wa malaika wa tatu, basi injili haitakuwa tena nguvu kuu inayoongoza. **—Testimonies For The Church 6:235-241 (1900). {*EVsw 522.3*}**

Huduma ya Umishenari wa tiba Isichukue Nafasi ya Uinjilisti

Huduma ya umishenari wa tiba haipaswi kuchukua nafasi ya huduma ya Neno. Haitakiwi kutumia fedha ambazo zinapaswa kusaidia kazi ya Bwana katika maeneo ya nje ya nchi. Fedha yoyote iliyopo hazinani ni ya Bwana, na haipaswi kutumika kwa wingi katika ujenzi wa majengo nchini Marekani. Misaada ya watu haipaswi kuelekezwa kwenye kazi zisizoonyesha matokeo. Kweli inapaswa kutangazwa, ili njia ya Bwana iandaliwe. Baragumu haipaswi kutoa sauti isiyoeleweka, sauti yake yapaswa kuwa bainishi..... **{*EVsw 523.1*}**

Huduma ya umishenari wa tiba lazima iache nafasi kwa huduma ya Neno. Dharau haipaswi kuonyeshwa kamwe dhidi ya kutangazwa kwa Neno la **Mungu**. Ujumbe wa malaika wa tatu usizimishwe kabisa na kufa. —**Manuscript 177, 1899. {*EVsw 523.2*}**

Kazi ya Mwisho ya Huduma

Ningependa kuwaambia kuwa hivi karibuni hakutakuwa na kazi yoyote ya huduma ya injili isipokuwa kazi ya huduma ya umishenari wa tiba. Kazi ya mhubiri ni kuhudumu. Wahubiri wetu wanapaswa kufanya kazi kwa mpango wa injili wa kuhudumu..... **{*EVsw 523.3*}**

Hamtaweza kuwa wahudumu wa mpangilio wa injili hadi mthibitishe kuwa na moyo wa kushiriki katika huduma ya umishenari wa tiba, injili ya uponyaji, baraka na kuimarisha... **{*EVsw 523.4*}**

Ni kwa sababu ya maagizo niliyopokea kutoka kwa Bwana ndipo nina ujasiri wa kusimama miongoni mwenu na kusema kama ninavyosema, licha ya jinsi mnavyotazama huduma ya umishenari wa tiba. Ningependa kusema kuwa huduma ya umishenari wa tiba ni kazi ya **Mungu**. Bwana anataka kila mhudumu wake kujiunga na mstari wa kazi hii. Shikeni kazi Yake ya umishenari wa tiba, nanyi mtapata njia ya kuwafikia watu. Mioyo yao itaguswa mnapowahudumia katika mahitaji yao. Mnapopunguza mateso yao, mtapata fursa ya kuwaeleza juu ya upendo wa Yesu. **—Counsels on Health, 533 (1901) {*EVsw 523.5*}**

Usahili wa Mbinu

Kristo Ametuonyesha Jinsi ya Kuwasaidia Wanadamu — Soma simulizi la jinsi Mwokozi alivyolisha umati kwa mikate mitano na samaki wawili.... Utoaji huu wa muujiza na rehema kwa mahitaji ya kimwili ya muda mfupi, ulisaidia kufunga katika akili za watu maneno ya neema ya Kweli aliyokuwa amesema.... **{*EVsw 524.1*}**

Katika muujiza huu, Kristo ameonyesha jinsi huduma ya umishenari wa tiba inavyopaswa kuunganishwa na huduma ya Neno. Wanafunzi Wake wanapaswa kuchukua mkate wa uzima na maji ya wokovu na kuwapatia wale walio na kiu ya msaada wa kiroho. Na kadiri kunavyokuwa na uhitaji, wawalishe wenye njaa na kuwavika wasio na mavazi. Kwa kufanya hivi wanamtumikia Bwana kwa huduma mbili. Uzuri na manufaa ya kazi tunayofanya kwa ajili ya **Mungu** yapo katika uwiano, maelewano, na ufanisi wake katika kuendana na kila upande. **— Manuscript 5, 1901. {*EVsw 524.2*}**

Kuwa Karibu na Binadamu Wanao Teseka — Kristo ametupatia mfano, ili tupate kufuata nyayo Zake. Daima alikaribia wale walio na uhitaji mkubwa zaidi, waliokata tamaa zaidi, na, waolivutwa na huruma Yake, na hawa walimkaribia Yeye. Anaihakikishia kila nafsi inayoteseka, yenye dhambi na uhitaji, kwamba hatapungukiwa na hitaji la Daktari Mkuu wa kumpa msaada wa kiroho. Sisi tunasimama mbali mno na binadamu wanaoteseka. Hebu na tumkaribie Kristo, ili nafsi zetu zijazwe na neema Yake, pamoja na tamanio la kuwashirikisha wengine neema hii. **— Letter 17, 1903. {*EVsw 524.3*}**

Kwa Njia za Kivitendo — Tunapaswa kukumbuka kwamba kazi ya kuwafikia roho haiwezi kufungwa katika mbinu moja tu. Huduma ya umishenari wa injili kwa njia ya afya inapaswa kuendelezwa, si kwa kufuata mpangilio wa mtu mmoja, bali kwa njia za Kristo. Kila kitu kinachofanyika, kiwe na mguso wa alama ya Roho Mtakatifu. Hebu tufanye kazi kama Kristo alivyofanya, kwa njia zile zile za kivitendo. Hapo ndipo tutakapokuwa salama. **{*EVsw 524.4*}**

Agizo la **Mungu** halina haja ya marekebisho. Njia ya Kristo ya kuwasilisha Kweli haiwezi kuboreshwa. Mtendakazi anayejitahidi kuleta mbinu za kuwavutia watu wa kidunia, akidhani kuwa hivyo ataondoa

pingamizi wanazohisi kuhusu kuchukua msalaba, hupunguza ushawishi wake. Dumisha usahili wa utauwa. **— Letter 123, 1903.** {*EVsw 525.1}*

Kuandaliwa Kutoa Matibabu Rahisi — Hebu Wahubiri wetu waliopata uzoefu wa kuhubiri Neno wajifunze pia kutoa matibabu rahisi, kisha waende kufanya kazi kama wamishenari wa tiba wanaohubiri injili. Watendakazi—wamishenari wa injili ya afya—wanahitajika sana sasa. — **Manuscript 141, 1903.** {*EVsw 525.2}*

Kufundisha Kanuni za Maisha ya Afya — Watendakazi wa injili wanapaswa pia kuwa na uwezo wa kutoa mafundisho juu ya kanuni za maisha ya afya. Magonjwa yapo kila mahali, na mengi kati yao yangeweza kuzuilika kwa kuzingatia sheria za afya. Watu wanahitaji kuona uhusiano wa kanuni za afya na ustawi wao, kwa maisha haya na yale yajayo. Wanahitaji kuamshwa kuhusu wajibu wao kwa makazi ya mwanadamu aliyotayarishiwa na Muumbaji kuwa makao Yake, na ambayo anatamani wawe mawakili waaminifu (mwili ni makazi Mungu ametupa). {*EVsw 525.3}*

Maelfu wanahitaji na wangepokea kwa furaha mafundisho kuhusu njia rahisi za kuwatibu wagonjwa—mbinu ambazo zinachukua nafasi ya matumizi ya dawa zenye sumu (poisonous drugs). Kuna haja kubwa ya mafundisho kuhusu matengenezo ya lishe. Mazoea mabaya ya kula na matumizi ya vyakula visivyo na afya ndiyo kwa kiasi kikubwa chanzo cha kutokuwa na kiasi, ulevi, uhalifu, uharibifu, na taabu zinazolaani dunia. {*EVsw 525.4}*

Katika kufundisha kanuni za afya, weka mbele lengo kuu la matengenezo—kwamba kusudi lake ni kupata maendeleo ya juu kabisa ya mwili, akili, na roho. Onesha kwamba sheria za asili, ambazo ni sheria za **Mungu**, zimetungwa kwa ajili ya faida yetu; kwamba utii kwa sheria hizo huleta furaha katika maisha haya, na hutusaidia kujiandaa kwa ajili ya maisha yajayo. {*EVsw 526.1}*

Watie moyo watu kujifunza ule muundo wa ajabu wa mwili wa mwanadamu, na sheria zinazouongoza. Wale watakaotambua ushahidi wa upendo wa **Mungu**, wanaoelewa kitu kuhusu hekima na wema wa sheria Zake, na matokeo ya utii, watatazama majukumu yao kwa mtazamo tofauti kabisa. Badala ya kuona utii kwa sheria za afya kama jambo la kujinyima, kujikana nafsi, wataona kama ilivyo kweli, kuwa ni baraka isiyo na kifani. {*EVsw 526.2}*

Kila mtendakazi wa injili anapaswa kuhisi kwamba kufundisha kanuni za maisha ya afya ni sehemu ya kazi aliyopewa. Kazi hii inahitajika sana, na dunia iko wazi kuipokea. **— Counsels on Health, uk. 389, 390 (1914).** {*EVsw 526.3}*

Kufundisha Mapishi ya Afya — Shule za mapishi zinapaswa kuanzishwa, na mafundisho ya nyumba kwa nyumba yatolewe kuhusu sanaa ya kupika chakula bora kisichokobolewa au kusindikwa, na kisicho na nyama. Wazee na vijana wajifunze jinsi ya kupika kwa usahili zaidi. Popote ambapo Kweli inawasilishwa, watu wafundishwe jinsi ya kuandaa chakula kwa njia rahisi, lakini kinachovutia na chenye ladha nzuri. Waonyeshe kwamba lishe yenye virutubisho inaweza kupatikana bila kutumia vyakula vya nyama. {*EVsw 526.4}*

Wafundishe watu kwamba ni bora kujua jinsi ya kubaki na afya kuliko kujua jinsi ya kutibu ugonjwa. Madaktari wetu wanapaswa kuwa waalimu wenye hekima, wakiwaonya wote dhidi ya kuendekeza ulafi au uchu wa chakula kupita kiasi, na kuwaonyesha kwamba kujiepusha na vitu ambavyo **Mungu** amekataza ndiyo njia pekee ya kuepuka uharibifu wa mwili na akili. — **Testimonies for the Church 9:161 (1909).** {*EVsw 526.5}*

Umuhimu wa Shule za Mapishi — Shule za mapishi zinapaswa kuanzishwa katika maeneo mengi. Kazi hii inaweza kuanza kwa unyenyekevu, lakini wapishi wenye maarifa wanapojitahidi kuwaelimisha wengine, Bwana atawapa ujuzi na ufahamu. Neno la Bwana ni: “Msiwazuie; kwa maana nitajifunua kwao kama Mwalimu wao.”

Bwana atashirikiana na wale wanaotekeleza mipango Yake, akiwaelimisha watu jinsi ya kuleta matengenezo katika lishe yao kwa maandalizi ya vyakula vya afya visivyo na gharama kubwa. Hivyo maskini watahamasishwa kuufuata ushauri wa matengenezo ya afya; watawezeshwa kuwa na bidii ya kazi, tasnia, na kujitegemeza kwa kazi zao. {*EVsw 527.1}*

Nimeonyeshwa kuwa wanaume na wanawake wenye uwezo wanafundishwa na **Mungu** jinsi ya kuandaa chakula bora kisichosindikwa wala kukobolewa na kitamu kwa njia inayokubalika. Wengi wao ni vijana, lakini wapo pia walio wa umri mkubwa. Nimeagizwa kuhamasisha uendeshaji wa shule za mapishi

katika maeneo yote ambako huduma ya afya inafanyika. Kila kichocheo cha kuwavuta watu kuelekea matengenezo lazima kiwekwe mbele yao. Wapewe mwangaza mwingi kadiri iwezekanavyo. Wafundishe kufanya kila maboresho wanayoweza katika maandalizi ya chakula, na wahamasishwe kuwashirikisha wengine yale wanayojifunza. **— Testimonies for the Church 7:113 (1902).** {*EVsw 527.2*}

Kufundisha Mapishi Nyumba kwa Nyumba — Wengine wanapaswa kufanya kazi nyumba kwa nyumba, wakitoa mafundisho juu ya sanaa ya kupika chakula bora. Wengi, wengi wataokolewa kutoka katika uharibifu wa kimwili, kiakili, na kimaadili kwa njia ya ushawishi wa matengenezo ya afya. Kanuni hizi zitajieleza zenyewe kwa wale wanaotafuta nuru; na hao watasonga mbele na kuikubali Kweli kamili kwa wakati huu. — **The Review and Herald, Juni 6, 1912.** {*EVsw 527.3*}

Elimisha, Elimisha, Elimisha — Lazima tuelimishe, tuelimishe, tuelimishe kwa upole, kwa njia nzuri na kwa uelewa. Tunapaswa kuihubiri Kweli, kuiombea Kweli, na kuishi Kweli, tukiileta, pamoja na athari zake za neema na kuponya, karibu na wale wasioweza kuijua. Wagonjwa wanapokaribiana na Mtoaji wa Uhai, akili na miili yao itafanywa upya. Lakini ili hili litokee, ni lazima wajifunze kujinyima, kujikana nafsi na kuwa na kiasi katika mambo yote. Hivyo tu ndivyo watakavyookolewa kutoka kwa mauti ya mwili na ya roho, na kurejeshwa katika afya. {*EVsw 528.1*}

Wakati mashine ya mwanadamu (mwili) inapofanya kazi kwa ulinganifu na mipango ya uhai ya **Mungu**, kama inavyofunuliwa kupitia injili, ugonjwa hushindwa na afya huibuka kwa haraka. Wanadamu wanaposhirikiana na Mtoaji wa Uhai, aliyetoa maisha Yake kwa ajili yao, mawazo ya furaha hujaza akili. Mwili, akili, na roho hutakaswa. Wanadamu hujifunza kutoka kwa Mwalimu Mkuu, na kila kitu wanachotazama huwainua na kuimarisha mawazo. Mapenzi yao huvutwa kwa furaha na shukrani kwa Muumbaji. Maisha ya mtu anayefanywa upya kwa mfano wa Kristo ni kama mwangaza uangazao gizani. **— Medical Ministry, 262, 263 (1905).** {*EVsw 528.2*}

Mtazamo Mpana wa Huduma — Kuna sayansi katika kushughulika na wale wanaoonekana kuwa dhaifu zaidi. Ikiwa tunataka kuwafundisha wengine, ni lazima sisi wenyewe tujifunze kwanza kutoka kwa Kristo. Tunahitaji mtazamo mpana, ili tuweze kufanya kazi ya Kweli ya kimishenari....{*EVsw 528.3*}

Lazima tuwe na busara tunaposhughulika na wale wanaoonekana kutojua na waliopotea. Kwa jitihada za kudumu kwa niaba yao, lazima tuwasaidie kuwa wa wenye kunufaisha katika kazi ya Bwana. Waitikia kwa haraka upendo wenye uvumilivu na huruma. {*EVsw 529.1*}

Tunapaswa kushirikiana na Bwana Yesu katika kuwarejesha wale wasio na ufanisi, wasiojali, wabaradhifu na waliopotoka wawe na akili mahiri na usafi wa moyo. Kazi hii ni ya umuhimu sawa na huduma ya injili. — **Medical Ministry, 208, 209 (1905).** {*EVsw 529.2*}

Ujumbe wa Kiasi na Kupinga Tumbaku

Mwanadamu Ameuza Akili Yake

Shetani anauteka ulimwengu kupitia matumizi ya vileo na tumbaku, chai zenye Kafein na kahawa. Akili ambayo **Mungu** ameitoa ili ibaki safi na angavu, inapotoshwa kwa matumizi ya vitu vyenye kulevya (narcotics). Ubongo umepoteza uwezo wake wa kutambua lililo sahihi. Adui huuteka ufahamu. Mwanadamu huuza mantiki yake kwa kitu kinachomfanya kuwa mwendawazimu. Hana tena hisia za kutambua lililo jema. Hata hivyo, laana ya pombe imehalalishwa, na inaleta uharibifu mkubwa kupitia mikono ya wale wanaopenda kujishughulisha na kile ambacho si tu kinaharibu mhusika, bali pia familia yake nzima. {*EVsw 529.3*}

Laana ya unywaji wa pombe inaonyeshwa wazi katika mauaji ya kutisha yanayotokea. Ulevi umeenea kwa kiwango kikubwa. Haiwezekani kuelezea kwa ukamilifu jinsi akili ya mwanadamu inavyopotoka kwa matumizi ya vilevi au dawa zenye vilevi (intoxicating drugs). —**Manuscript 11, 1899.** {*EVsw 529.4*}

Jukumu Muhimu

Miaka mingi iliyopita tuliona kwamba kueneza kanuni za afya na kiasi ni mojawapo ya wajibu wetu muhimu sana. Ndivyo inavyopaswa kuwa hata leo. **—Medical Ministry, uk. 266 (1907).** {*EVsw 529.5*}

Njia za Kuwasilisha Ujumbe wa Kiasi

Somo la kiasi linapaswa kufundishwa kwa msisitizo na uwazi. Waonyesheni watu jinsi kuishi kwa kufuata kanuni za afya ni baraka kwao. Waonyesheni kusudi la **Mungu** juu ya mwanamume na mwanamke—kile alichowakusudia wawe. Waonyesheni dhabihu kuu iliyotolewa kwa ajili ya kuinua na kuinua hadhi ya jamii ya wanadamu. Ukiwa na Biblia mkononi, wasilisheni matakwa ya **Mungu**. Waambieni kuwa anatarajia watumie akili na miili yao kwa njia itakayomtukuza Yeye. Waonyesheni jinsi adui anavyotaka kuwaburuza wanadamu kwa kwa kuwaongoza katika tamaa ya chakula.**{*EVsw 530.1*}**

Kwa uwazi, kwa uaminifu, na kwa bidii, waambieni jinsi maelfu ya wanaume na wanawake wanavyotumia mali ya **Mungu** kujiharibu wenyewe na kuifanya dunia hii kuwa kuzimu. Mamilioni ya pesa hutumika kwa vitu vinavyowafanya watu kuwa wazimu. Wasilisheni jambo hili kwa uwazi kiasi kwamba nguvu yake haiwezi kufichika. Halafu waambieni juu ya Mwokozi, aliyekuja duniani kuwaokoa wanadamu kutoka katika mazoea yote ya dhambi. “Kwa maana jinsi hii **Mungu** aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.” **{*EVsw 530.2*}**

Waombe waliohudhuria mikutano washirikiane nanyi katika kazi hii mnayoifanya. Waonyesheni jinsi mazoea mabaya yanavyozaa miili iliyoharibika, akili zilizodhoofika, na maisha ya mateso na uharibifu yasiyoweza kuelezwa kwa kalamu. Matumizi ya pombe yamewanyang’anya maelfu akili zao na busara. Lakini hata hivyo, biashara ya pombe imehalalishwa. Waambieni kuwa wana mbingu ya kurithi na kuzimu ya kuepuka. Waombe wasaini ahadi ya kiasi. Amri ya **“MIMI NIKO”** iwe mamlaka yenu. Andikeni ahadi hizo, na ziwe tayari kisha mzitoe mwishoni mwa mkutano. **{*EVsw 530.3*}**

Mtu mmoja asijaribu kuifanya kazi hii peke yake. Wengine waungane naye katika jitihada hii. Hebu watu wasimame na kuja mbele wakiwa na ujumbe kutoka mbinguni, wakiwa wamejazwa na nguvu ya Roho Mtakatifu. Na wavute kwa nguvu zao zote, kwa maneno yaliyojaa mvuto wa Roho. Hebu waombe wasikilizaji wao washiriki katika kazi ya kuonya miji. Waonyesheni wanaume na wanawake uovu wa kutumia fedha kwa anasa zinazoangamiza afya ya mwili, akili, na roho. **{*EVsw 531.1*}**

Ufalme wa Kristo hauanzishwi kwa tamasha la nje wala kwa uungwaji mkono wa kidunia, bali kwa kupandikizwa kwa asili ya Kristo ndani ya ubinadamu kwa kazi ya Roho Mtakatifu. “Wote waliompokea, Yeye aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa **Mungu**; ndio wale waliaminio jina lake, waliozaliwa, si kwa damu, wala kwa mapenzi ya mwili, wala kwa mapenzi ya mtu, bali kwa **Mungu**.” Hii ndiyo nguvu pekee inayoweza kuinua ubinadamu. Na chombo cha kianadamu cha kazi hii ni kufundisha na kuhubiri Neno la **Mungu**. **—Manuscript 42, 1905. {*EVsw 531.2*}**

Uzoefu wa Kuwasaidia Wavutaji Tumbaku

Nchini Australia nilikutana na mwanaume mmoja aliyekuwa anaonekana kuwa mbali na aina zote za ulevi, isipokuwa tabia moja—alitumia tumbaku. Alikuja kusikiliza mahubiri yetu hemani, na usiku mmoja baada ya kurudi nyumbani, kama alivyotuambia baadaye, alipambana na tabia ya uvutaji tumbaku, na akapata ushindi. Baadhi ya jamaa zake walikuwa wamemwahidi kumpa paundi hamsini ikiwa angetupa tumbaku, lakini alikataa. Alisema, “Lakini mlipowasilisha kanuni za kiasi mbele yetu jinsi mlivyofanya, sikuweza kupinga. Mlitupatia mfano wa kujikana nafsi wa Yule aliyetoa maisha Yake kwa ajili yetu. Simfahamu sasa, lakini natamani kumjua. Sijawahi kusali katika nyumba yangu. Nimetupa tumbaku yangu, lakini sijaenda mbali zaidi ya hapo.” **{*EVsw 531.3*}**

Tulisali naye, na baada ya kuondoka tulimwandikia na baadaye tukamtembelea tena. Hatimaye, alifika hatua ya kujitoa kwa **Mungu**, na sasa amekuwa nguzo kuu ya kanisa katika eneo analoishi. Anajitahidi kwa moyo wake wote kuwaongoza jamaa zake katika kuijua Kweli. **—The General Conference Bulletin, April 23, 1901. {*EVsw 532.1*}**

Ushindi Kupitia Imani

Katika kazi hii, tabaka zote zitafikiwa. Roho Mtakatifu anapofanya kazi kati yetu, roho ambazo hazikuwa tayari kwa ujio wa Kristo husadikishwa. Wengi huja kwenye mikutano yetu na kubadilishwa, hata wale ambao kwa miaka hawakuwahi kuhudhuria ibada katika kanisa lolote. Usahili na unyofu wa Ukweli huvigusa mioyo yao. Wapenda tumbaku huacha sanamu yao, na walevi huacha pombe. Hawawezi kufanya hivyo bila kushika ahadi za **Mungu** za kusamehe dhambi zao kwa imani. Ukweli kama ulivyo katika Neno huja mbele ya walio juu na walio chini, matajiri na maskini, na wale wanaoupokea ujumbe huu wanakuwa washiriki nasi na wa **Mungu**, na huinuka kuwa jeshi lenye nguvu la kufanya kazi kwa ushirikiano. Hii ndiyo kazi yetu. —**Manuscript 3, 1899. {*EVsw 532.2*}**

Kutoka Mji hadi Mji, Kijiji hadi Kijiji

Kwa watu wote, matajiri na maskini, walio huru na walio kifungoni, Kristo, Mjumbe wa Agano, aliwaletea habari njema za wokovu. Jinsi gani watu walimiminika kumfuata! Walitoka mbali na karibu kwa ajili ya kuponywa, naye aliwaponya wote. Sifa Zake kama Mponyaji Mkuu zilienea kote Palestina, kutoka Yerusalemu hadi Shamu. Wagonjwa walikuja katika maeneo ambayo walidhani angepita ili wamwite awasaidie, naye aliwaponya maradhi yao. Hata matajiri walikuja, wakiwa na shauku ya kusikiliza maneno Yake na kupata mguso wa mkono Wake. Hivyo, alienda kutoka mji hadi mji, kijiji hadi kijiji, akihubiri injili na kuponya wagonjwa—Mfalme wa utukufu akiwa amevaa mwonekano wa unyenyekevu wa kibinadamu. — **The Review and Herald, July 23, 1914** {*EVsw 532.3}*

Wito wa Mungu Leo

Mungu anatoa wito, si kwa wachungaji tu, bali pia kwa madaktari, wauguzi, wauzaji wa vitabu vya kiroho, waalimu wa Biblia, na waumini wengine walio wakfu, wenye vipawa mbalimbali, wanaolijua Neno la **Mungu** na walioonja nguvu ya neema Yake, kutazama mahitaji ya miji ambayo bado haijaonywa. Wakati unakwenda kwa kasi, na kuna kazi nyingi ya kufanyika. Kila chombo kinapaswa kuwekwa kazini ili fursa zilizopo zitumiwe kwa hekima. **— The Acts of the Apostles, uk. 158, 159 (1913)** {*EVsw 533.1}*

Mlango wa Kuingilia Nyumba za Mjini

Huduma ya umishenari wa tiba ni mlango ambao Ukweli utaingia kupitia kwake katika nyumba nyingi mijini. Kila mji una watu watakaothamini Ukweli wa ujumbe wa malaika wa tatu. — **Counsels on Health, uk. 556 (1906)** {*EVsw 533.2}*

Kila Juhudi ya Mjini

Kanuni za matengenezo ya afya zinapaswa kufundishwa kama sehemu ya kazi mijini. Sauti ya ujumbe wa malaika wa tatu inapaswa kusikika kwa nguvu. Mafundisho ya matengenezo ya afya yaingizwe katika kila juhudi/efoti ya kupeleka nuru ya Ukweli kwa watu. Hebu wachaguliwe watendakazi walio na uwezo wa kufundisha Ukweli kwa hekima kwa namna rahisi na wazi. — **Medical Ministry, uk. 304 (1910)** {*EVsw 533.3}*

Tumechelewa Sana Katika Kazi Hii

Tumechelewa sana kufanya kazi ambayo ilipaswa kufanyika katika miji hii iliyopuuzwa kwa muda mrefu. Sasa kazi hii itakuwa ngumu zaidi kuliko ilivyokuwa miaka michache iliyopita. Lakini tukianza kazi kwa Jina la Bwana, vizuizi vitavunjika na ushindi wa hakika utapatikana kwetu. {*EVsw 533.4}*

Katika kazi hii, madaktari na wahubiri wa injili wanahitajika. Lazima tupeleke dua zetu kwa Bwana na kufanya bidii yote kwa nguvu tulizonazo kufungua njia katika miji mikubwa kwa ubora. Kama tungalifuata mpango wa Bwana tangu mwanzo, taa nyingi zingekuwa zinang'aa mahali ambapo sasa zinazimika. — **Medical Ministry, uk. 301, 302 (1909)** {*EVsw 534.1}*

Ujumbe wa Afya na Kiasi kwa Watu Wote

Kuna kazi kubwa ya kufanywa ya kupeleka kanuni za matengenezo ya afya kwa watu. Mikutano ya hadhara inapaswa kufanyika ili kuanzisha somo hili, na shule zianzishwe kwa ajili ya wale walio na shauku wapate kufundishwa zaidi kuhusu vyakula vya afya na jinsi ya kuandaa lishe bora, yenye ladha, isiyohusisha nyama, chai yenye kafein wala kahawa... {*EVsw 534.2}*

Sisitizeni somo la kiasi kwa nguvu zote chini ya upako wa Roho Mtakatifu. Onyesheni hitaji la kujiepusha kabisa na vileo vyote. Onyesheni madhara makubwa ya tumbaku na pombe kwa mwili wa binadamu. Elezeni mbinu zenu za matibabu. Hotuba zenu ziwe zenye kuleta nuru kwa wasikilizaji wenu. Mungu ana rehema kwa wasio haki. Huduma hii itakuwa fursa ya kufafanua matengenezo ya kweli ya afya. — **Letter 343, 1904** {*EVsw 534.3}*

Sanitarium Karibu na Miji Mikuu

Bwana amenionyesha kuwa kunapaswa kuwa na sanitoriumu karibu na miji mingi muhimu... Pawepo na maeneo yanayofaa ambapo tunaweza kupeleka wagonjwa na wanaoteseka walioko mijini, wasiojua chochote kuhusu watu wetu wala Kweli ya Biblia. Kila jitihada ifanywe kuwaonyesha wagonjwa kuwa maradhi yanaweza kuponywa kwa njia za Busara zisizotegemea dawa hatarishi na zenye madhara. Hebu wagonjwa waondolewe kwenye mazingira yenye madhara na kupelekwa katika vituo vyetu vya afya ambapo wanaweza kuhudumiwa na wauguzi na madaktari WaKristo, na hivyo wapate kujua Neno la **Mungu**. **— Letter 63, 1905 {*EVsw 534.4*}**

Kuweka Misingi ya Ujumbe

Ni mapenzi ya Bwana kuwa juhudi mpya zifanywe mahali pengi, na vituo vidogo vianzishwe. Kazi ya kufungua njia kwa ajili ya kuendeleza Kweli inapaswa kufanyika, kazi ambayo pia itaimarisha imani ya nafsi…..**{*EVsw 535.1*}**

Kuna maeneo mengi ya kazi, na hatupaswi kupanga kuanzisha vituo vikubwa tu katika maeneo machache yaliyopewa upendeleo. Bwana amenielekeza kuwa tusijenge vituo vikubwa vingi hapa, kwa kuwa kila uwanja unapaswa kuwa na vifaa vya kurahisisha mafanikio ya kazi. Kwa sababu hii, taasisi chache kubwa zisiruhusiwe kutumia rasilimali zote. Katika miji mikubwa na midogo, hata kwenye makazi yaliyo nje ya miji, pawe na vituo vidogo ambapo walinzi waaminifu watasimama na kufanya kazi kwa ajili ya roho za watu. Popote mmishenari anapokwenda, juhudi zake zifuatiwe na kuanzishwa kwa kituo kidogo kitakachoharakisha maendeleo ya kazi. Watumishi wa **Mungu** wakifanya kazi kwa uaminifu, uongozi wa **Mungu** utafungua njia ya kuanzishwa kwa vituo hivi mahali pengi-sanitarium. **{*EVsw 535.2*}**

Katika njia kuu na vichochoroni, juhudi zinapaswa kufanyika. Hatufanyi kazi hii kwa mpango bora unaowezekana. Tunapaswa kupanga kugawa na kugawanya vikosi vyetu vya kazi ili tuweze kufikia mashamba mapya. **— Letter 30, 1911 {*EVsw 535.3*}**

Miji Katika Nchi Nyingi

Huduma ya umishenari wa tiba ni mkono wa kulia wa injili. Ni ya lazima kwa maendeleo ya kazi ya **Mungu**. Kupitia huduma hii, watu wataelekezwa kutambua umuhimu wa kuishi kwa maadili na mazoea bora ya afya, na uwezo wa kuokoa wa Kweli utafunuliwa. Kila mji unapaswa kufikiwa na watendakazi waliopata mafunzo ya kazi hii ya matibabu ya kimishenari. Kama mkono wa kulia wa ujumbe wa malaika wa tatu, mbinu za **Mungu** za kutibu maradhi zitafungua milango kwa ajili ya kuingia kwa Ukweli wa sasa. Machapisho ya afya yanapaswa kusambazwa katika mataifa mengi. Madaktari wetu walioko Ulaya na nchi nyingine wanapaswa kuamka na kutambua umuhimu wa kuwa na machapisho ya afya yaliyoandikwa na watu walioko kwenye maeneo hayo, watu wanaoweza kuwafikia watu kwa mafundisho muhimu yanayohitajika zaidi. — **Testimonies for the Church 7:59 (1902) {*EVsw 536.1*}**

Kusudi la Kuanzishwa kwa Taasisi

Zimeanzishwa kwa Ajili ya Kueneza ujumbe wa Injili-Kuhubiri injili ni zaidi ya vile wengi wanavyofikiri. Ni kazi pana na ya kufikia mbali. Vituo vyetu vya afya (sanitariamu) vimeonyeshwa kwangu kuwa ni vyombo vyenye ufanisi mkubwa kwa ajili ya kueneza ujumbe wa injili. —**Manuscript 5, 1908 {*EVsw 536.2*}**

Kuleta Afya ya Roho-Wengine huvutwa na upande mmoja wa injili, na wengine na upande mwingine. Bwana wetu ametufundisha kufanya kazi kwa namna itakayowafikia watu wa kila tabaka. Ujumbe huu lazima uwafikie watu wote duniani. Vituo vyetu vya afya, yaani sanitarium zinapaswa kusaidia katika kuwaleta watu katika idadi ya watu wa **Mungu**. Hatupaswi kuanzisha taasisi chache kubwa mno, kwa maana itakuwa vigumu kuwapatia wagonjwa ujumbe utakaowaletea nafsi zao afya. Vituo vya sanitarium vidogo vidogo vinapaswa kuanzishwa sehemu mbalimbali. **—Medical Ministry, uk. 327 (1905) {*EVsw 536.3*}**

Kuifanya Injili Ivutie-Wale wanaofanya kazi katika sanitarium zetu wanapaswa kuwa waalimu-waelimishaji. Kupitia maneno ya mazuri na matendo ya fadhili, wanapaswa kuifanya injili ivutie. Kama wafuasi wa Kristo, wanapaswa kuacha picha bora ya dini yao na kuamsha mawazo bora. Wengine wataathiriwa kwa uzima na kwa milele kutokana na mvuto wao. **{*EVsw 537.1*}**

Katika kazi ya kuwasaidia wengine, tunapata ushindi wa thamani sana. Tunapaswa kujitolea kwa bidii bila kuchoka, kwa uaminifu wa kweli, kwa kujinyima, kujikana nafsi na kwa uvumilivu, ili kuwasaidia wale wanaohitaji maendeleo. Maneno ya fadhili na ya kutia moyo yanaweza kufanya maajabu. Wapo wengi

ambao, iwapo juhudi thabiti na zenye furaha zitaelekezwa kwao pasipo lawama wala kulaumu, wataonyesha kuwa wanaweza kubadilika. Kadri tunavyokoma kuwakosoa wengine, ndivyo mvuto wetu wa kuwafanya mema unavyoongezeka. Kwa watu wengi, maonyo ya mara kwa mara na yenye msisitizo hufanya madhara zaidi kuliko faida. Hebu wema wa Kristo uwatawale wote. **—Medical Ministry, uk. 208-209 (1905) {*EVsw 537.2}***

Lengo Kuu-Kule kugeuzwa kwa roho ndilo lengo kuu la kuanzishwa kwa taasisi zetu za tiba. Wagonjwa na walioteseka wanapokuja vituo vyetu vya afya, wanawekwa karibu na wahudumu wa injili. Lo!, ni fursa ya thamani jinsi gani ya kupanda mbegu ya Kweli! **—Letter 213, 1902 {*EVsw 537.3}***

Uwasilishaji wa Ujumbe kwa Hekima

Hebu hali ya kiroho ya taasisi hizi iwe ya namna ambayo wanaume na wanawake wanaokuja kupata tiba ya miili yo pia watambue kuwa nafsi zao pia zinahitaji uponyaji.... **{*EVsw 537.4}***

Mazungumzo rahisi na ya dhati yanaweza kufanyika sebuleni, yakiwaelekeza wagonjwa kwa tumaini lao pekee la wokovu wa nafsi. Mikutano ya aina hii iwe mifupi na yenye maana, nayo italeta baraka kwa wasikilizaji. Neno la Yule aliyeumba dunia kwa siku sita, na katika ya saba "akapumzika na kufarijika," lifikishwe kwa ufanisi kwa akili za wagonjwa.... **{*EVsw 538.1}***

Machapisho yenye Ukweli wa thamani wa injili yawepo kwenye vyumba vya wagonjwa au sehemu ambapo wanaweza kuyaona kwa urahisi. Kila sanitariamu inapaswa kuwa na maktaba yenye vitabu vinavyobeba nuru ya injili. Mipango ya busara iwekwe ili wagonjwa wapate kila mara nafasi ya kusoma Maandiko yenye nuru ya Kweli ya sasa.... **{*EVsw 538.2}***

Hebu Sanitarium zetu na ziwe kama nyumba zenye huduma kwa nafsi zilizojeruhiwa kwa dhambi. Na jambo hili litawezekana ikiwa watendakazi wake wana uhusiano wa moja kwa moja na Mponyaji Mkuu. **—Manuscript 5, 1908 {*EVsw 538.3}***

Watendakazi Wanaoweza Kutoa Msaada wa Kiroho

Katika sanitarium zetu—kuliko mahali pengine popote duniani—tunahitaji madaktari waliogeuzwa kweli kweli na watendakazi wenye hekima—wanaume na wanawake ambao hawatawasukumia wagonjwa mawazo yao binafsi, bali watawasilisha Kweli za Neno la **Mungu** kwa namna ya kuleta faraja, matumaini, na baraka kwao. Hii ndiyo kazi ambayo vituo vyetu vya Sanitarium vimeanzishwa kufanya—kuiwakilisha kwa usahihi Kweli ya Neno la **Mungu** na kuwaelekeza wanawake kwa wanaume kwa Kristo. **{*EVsw 538.4}***

Ibada za kila siku ziwe fupi lakini za mafundisho kwa tabia. Wasilisha Biblia na Muumbaji Wake—**Mungu** wa mbingu na dunia, pamoja na Kristo Mwanawe, zawadi kuu ya Mungu kwa dunia. Waambie wagonjwa jinsi Mwokozi alivyokuja hapa duniani kuonyesha upendo wa **Mungu** kwa wanadamu. Weka wazi dhabihu Yake kuu ya kuja hapa kuishi na kufa. Waeleze kwamba kupitia imani kwa Kristo, kila mwanadamu mwenye dhambi anaweza kuwa mshiriki wa asili ya Kiungu na kushirikiana na **Mungu** katika kazi ya wokovu. —**Medical Ministry, uk. 208 (1909) {*EVsw 538.5}***

Kuondoa Chuki na Ubaguzi

Mafundisho yanayowasilishwa kwa wagonjwa hayapaswi kuwa kama sheria ambazo lazima watii. Ilisemwa: “Kila kinachoweza kufanywa kifanywe ili kuwaelekeza wagonjwa na walioteseka katika njia ya kweli na haki. Huduma ya umishenari wa tiba ni njia moja ya kufanya hivi. Hatujui kiasi gani cha chuki na ubaguzi huondolewa watu wanapokutana na wahudumu wa kweli wa umishenari wa tiba. Madaktari na wauguzi wanapojitahidi kufanya kwa ajili ya wanaoteseka yale ambayo Kristo mwenyewe alifanya, Kweli ya wakati huu hupenya akilini na mioyoni.” **{*EVsw 539.1}***

Vipindi vya ibada jioni katika vituo vyetu vya afya viendeshwe kwa namna itakayowapa nafasi wagonjwa kuuliza maswali. **—Letter 213, 1902 {*EVsw 539.2}***

Masuala ya Mafundisho ya Imani

Sebule ya sanitarium, mahali ambapo kuna kundi la watu tofauti tofauti, si mahali pa kuzungumzia mafundisho ya imani. Wacha maisha yetu yenye uthabiti yaamshe hamu ya watu kujua sababu za imani yetu. Kisha waalikeni wale wanaouliza wahudhurie ibada za Sabato. **—Manuscript 53, 1899 {*EVsw 539.3}***

Kujizuia kwa Hekima

Mna kazi muhimu ya kufanya katika sanitariamu. Msijaribu kuonyesha kwamba mna hamu sana ya kuwafanya wagonjwa waelewe na kukubali imani yetu. Ni kawaida kwa mtu kuwa na juhudi kali, lakini mara nyingine kujizuia kwa busara ni muhimu. Wakati mwingine Maneno ambayo yanaweza kuonekana yanafaa, yanaweza kufanya madhara makubwa na kufunga mlango wa injili. {*EVsw 539.4}*

Onyesheni upendo wa huruma nyororo na subira ya hekima. Iwapo mna nafasi ya kusema jambo kali la kushawishi, ni bora wakati mwingine kuacha. Msitoe kila ushahidi mnaoujua wenye nguvu kila mara, kwa kuwa hii inaweza kuzua shaka kuwa mnalenga tu kuwaongoza watu kwenye imani ya Waadventista wa Sabato. {*EVsw 540.1}*

Neno rahisi la **Mungu** lina nguvu kubwa ya kushawishi. Wacha Neno lenyewe lizungumze na lifanye kazi yake. Hebu kuwe na kiasi katika jitihada za kiinjilisti kwa kujizuia kwa hekima. Msilazimishe kuwasilisha vipengele vya kupima imani. Subirini hadi maswali yaulizwe. hebu mfano wenu ufundishe. Maneno na matendo yaonyeshe kuwa mnaamini mafundisho ya Kristo aliye hai. —**Letter 308, 1906** {*EVsw 540.2}*

Njia ya Busara ya Kuwafikia Wengine

Kweli ya **Mungu** iliyo hai inapaswa kujulikana katika taasisi zetu za tiba. Hii haimaanishi kuwa kila mtendakazi au daktari aanzishe mazungumzo ya imani na kila mgonjwa. Hiyo sio njia sahihi ya kufanya kazi. Wauguzi na watendakazi hawapaswi kwena kwa wagonjwa na kuwaambia moja kwa moja, “Sisi tunaamini ujumbe wa malaika wa tatu,” isipokuwa wagonjwa wenyewe waonyeshe nia ya kusikia, wakiwa wamelainishwa mioyoni mwao na hoja au chuki imeondolewa moyoni mwao. {*EVsw 540.3}*

Tenda kwa namna itakayofanya wagonjwa waone kuwa Wasabato ni watu wenye akili timamu au busara (common sense). Wafanye wahisi kuwa taasisi ni mahali pa utulivu, pa kupumzika. Kweli ya Biblia iwasilishwe, lakini mambo maalumu ya mafundisho yasitangazwe mbele ya wagonjwa wote. Wakiuliza maswali, wapeni sababu za imani yenu. Kwa njia hii, nuru itang’aa. {*EVsw 540.4}*

Wagonjwa wanaweza kualikwa kuhudhuria ibada zetu, na huko wataisikia Kweli bila kulazimishwa. Watakapotoka sanitariamu na wasikie watu wakisema, “Sitaki kwenda huko nikafanywe kuwa Msabato,” wao watajibu kwamba watendakazi wa sanitariamu hawalazimishi mtu yeyote kupokea ile Kweli. {*EVsw 541.1}*

Haitawezekana kuwazuia wagonjwa kuulizia kuhusu imani yetu. Wapo wanaohisi njaa na kiu ya Kweli, na hao wataipata. Ndiyo maana tunataka taasisi zetu zianze kazi mara moja. —**Manuscript 111, 1899** {*EVsw 541.2}*

Ushuhuda wa Maisha Thabiti ya Kikristo

Kweli hizi takatifu, zikiaminiwa na kufuatwa, hazipaswi kuwasilishwa kwa nguvu wala shuruti, bali katika roho ya Bwana. Roho Mtakatifu atayafikia mawazo ya ya waungwana na watu bora na nafsi zilizo tayari. Katika vituo vyetu vya sanitarium zote, lazima kuwepo na wanaume wanaoelewa mafundisho ya ile Kweli na wanaoweza kuyaeleza kwa kalamu na kwa sauti. Wataletwa karibu na watu wa akili mahiri, na wanapaswa kuwaelekeza kwa upole kama ambavyo wangemsihi mwana wao wa pekee. Linapaswa kuwa lengo letu, ni agizo la Bwana kuwa tusikabidhi nyadhifa muhimu za amana kwa watu ambao hawajaiva kiroho, au wenye uzoefu unaotosheleza au ambao hawana uelewa wa kina wa Kweli ya Biblia. {*EVsw 541.3}*

Wengi hudhani kuwa mwonekano, mtindo na maonyesho ya nje ya maigizo yana nafasi kubwa ya kuwafikia watu wa tabaka la juu. Lakini hili ni kosa. Watu wa aina hii wanaweza kutambua na kutathmini mambo hayo kwa urahisi. Ingawa mwonekano wa nje una nafasi, ndiyo katika kutoa athari akilini mwa watu, ni lazima uwe wa Kiungu. Hebu na ionekane wazi kuwa wale wanaofanya kazi hii wameunganika na **Mungu** na mbingu. Tusihenyeke kutafuta sifa au kutambuliwa na watu wa dunia ili kazi yetu ipate heshima, sifa na ushawishi katika siku hizi za mwisho. Mwendelezo wa maisha ya uaminifu ni wa thamani kuu. Imani yetu, mavazi yetu, na mwenendo wetu vinapaswa kuakisi tabia ya ujumbe wetu—ambao ni ujumbe mzito kuliko yote kuwahi kutolewa kwa dunia. {*EVsw 541.4}*

Kazi yetu ni kuwaleta watu waamini katika kweli—kwa mahubiri na kwa mfano wa maisha. Kwa kuishi maisha ya utauwa, kweli inapaswa kuonekana ikitendeka. Thamani ya imani yetu itaonekana kwa

matunda yake. Bwana anaweza na atagusa mioyo ya watu kupitia bidii na juhudi zetu za kweli. Mavazi yetu, mwenendo wetu, mazungumzo yetu, na kina cha uzoefu wetu wa kiroho, vyote vinafaa kuonyesha kwamba kanuni kuu za kweli tunayohubiri ni halisi kwetu. Kwa njia hii, kweli itakuwa na mvuto wa jumla na kugusa akili. Kweli ya Biblia ndiyo iwe mamlaka kwa dhamiri, chanzo cha upendo, na uhai wa roho. — **Letter 121, 1900** {*EVsw 542.1}*

Si Maneno Bali Matendo

Kuhusu kujulisha watu imani yetu, tusijitahidi kwa makusudi kuificha, wala tusitumie njia zisizo na busara kuifanya ijulikane kwa nguvu. Watu watakuja kwenye sanitarium wakiwa katika hali nzuri ya kupokea Kweli. Wakija wakakuuliza kuhusu imani yetu, ni vizuri kuwaeleza kwa uwazi na kwa maneno rahisi kile tunachoamini. Utauwa wa ndani huleta nguvu inayodhihirika katika mwenendo wa muumini wa kweli, na kumpa ushawishi wa upande wa haki na ulio sahihi. {*EVsw 542.2}*

Lakini katika jambo hili tunapaswa Kutenda kwa hekima. Wapo watu wenye dhamiri njema, wanaoamini kuwa ni wajibu wao kuzungumza kwa uhuru juu ya vipengele vya imani ambavyo kuna utofauti wa maoni, kwa namna ambayo huwafanya wanaozungumza nao kuwa wakali au wapinzani. Juhudi moja isiyokuwa ya wakati unaofaa au yenye ukosefu wa busara inaweza kufunga masikio ya mtu ambaye angeweza kusikiliza kwa uvumilivu, lakini sasa atawashawishi wengine kuwa na mtazamo mbaya. Hivyo mizizi ya uchungu huchipuka, na wengi hunajisika. Kupitia kutokosa busara kwa mtu mmoja, masikio na mioyo ya wengi inaweza kufungwa dhidi ya ile Kweli. {*EVsw 542.3}*

Ni jambo la kujulikana kuwa waumini wenye ushupavu wa madhehebu (zealous religionists) mbalimbali wamekuza na kuonyesha uwazi mdogo na busara kwa viwango vyao kwa wale wanaotofautiana nao kidini. Watu wa kundi hili huwatarajia Wasabato wa siku ya Saba wawe na roho hiyo hiyo ya kutovumiliana, na hivyo hujiandaa kujilinda au kujihami mapema dhidi ya kila kitu kitakachohusisha mtazamo wa kipekee. {*EVsw 543.1}*

Katika nyakati zilizopita, baadhi ya watu katika sanitarium wamehisikuwa ni wajibu wao kuzungumzia suala la Sabato kila mahali, na walikuwa wakilisukuma kwa wagonjwa kwa bidii na msisitizo. Kwao, malaika wa **Mungu** wangewaambia: “Si maneno bali matendo.” Maisha ya kila siku huzungumza zaidi kuliko maneno mengi. Uchangamfu wa kudumu, wema wa huruma nyororo, ukarimu wa Kikristo, subira na upendo vinayeyusha upinzani na kufungua mioyo kupokea Kweli. Watu wachache wanaelewa nguvu ya mvuto huu wa thamani. — **Manuscript 53, 1899** {*EVsw 543.2}*

Daktari Aliyejitakasa na Mhudumu wa Umishenari

Madaktari na Wauguzi Wa Kikristo

Bwana amepanga kuwa madaktari na wauguzi WaKristo wafanye kazi kwa kushirikiana na wale wanaohubiri Neno. Huduma ya umishenari wa tiba ni sehemu ya huduma ya injili. — **Medical Ministry, uk. 240 (1908)** {*EVsw 543.3}*

Mfano ni Luka

Katika kazi yetu leo, huduma ya Neno na huduma ya umishenari wa tiba vinapaswa kuunganishwa. {*EVsw 543.4}*

Luka aliitwa “daktari mpendwa.” Paulo aliposikia kuhusu ujuzi wake kama daktari, alimtafuta kwa kuwa aliona kuwa **Mungu** alimpa kazi maalum. Alimhusisha na kazi yake ya huduma. Baada ya muda alimwacha Filipi, ambako Luka aliendelea kufanya kazi kwa miaka kadhaa, akihudumu kwa huduma mbili kama daktari na mhubiri wa injili. Alikuwa kweli mmishenari wa tiba. Alifanya kazi yake kwa bidii, na kisha kumwomba Bwana kwa ajili ya uponyaji wa wagonjwa. Ujuzi wake wa tiba ulifungua njia kwa ujumbe wa injili kuingia mioyoni mwa watu, na kumpa nafasi ya kuwahubiria watu hata wapagani. {*EVsw 544.1}*

Ni mpango wa **Mungu** tufanye kazi kama mitume walivyofanya. Tukiunganishwa na Mponyaji wa Kiungu, tunaweza kufanya mema makubwa duniani. Injili ndiyo tiba pekee ya dhambi. Kama mashahidi wa Kristo, tunapaswa kutoa ushuhuda juu ya nguvu yake. Tunapaswa kuwaleta walio wagonjwa kwa Mwokozi. Neema Yake ya kubadilisha na uwezo Wake wa kufanya miujiza vitawavuta wengi kwenye Kweli. Nguvu yake ya uponyaji ikiunganishwa na injili italeta mafanikio katika hali ngumu za dharura. Roho Mtakatifu atafanya kazi mioyoni, na tutaona wokovu wa **Mungu**. Kwa namna ya kipekee, uponyaji wa wagonjwa ni kazi yetu. {*EVsw 544.2}*

Ahadi ya Kristo ya kuwa nasi haijabadilika kwa sababu ya muda kupita. Yeye Yuko nasi leo kama alivyokuwa na mitume, na atakuwa nasi "hata mwisho wa dunia." Kristo alipanga kwamba watu wafuate kazi ya injili kwa mfululizo, wakipata mamlaka yao kutoka Kwake, Mwalimu Mkuu. — **Letter 134, 1903** {*EVsw 544.3}*

Mihadhara ya Umma na Madaktari

Yeyote aliye daktari na mwalimu wa dini atapata kazi ya kufanya itakayowaletea watu wokovu. Mafundisho ya dini yenye kutegemezwa na msingi wa "asema Bwana" yatakuwa na mvuto wa wokovu. Daktari anaweza kujieleza kwa namna ambayo ataalikwa kuzungumza katika mikutano mbalimbali naye atapokelewa. Kama mwalimu, daktari anaweza kufuatilia fursa zake, kwa kuwa Neno la **Mungu** linapaswa kwenda kwa uhuru. — **Letter 4, 1910** {*EVsw 544.4}*

Fursa Maalum za Wauguzi wa Umishenari

Kila mahali Kweli inapowasilishwa, juhudi za makusudi zinapaswa kufanywa tangu mwanzo kuhubiri injili kwa maskini na kuponya wagonjwa. Kazi hii ikifanywa kwa uaminifu itaongeza kwenye kanisa roho nyingi ndani ya kanisa ambazo zitakuwa tayari kuokolewa. {*EVsw 545.1}*

Wale wanaofanya kazi ya nyumba kwa nyumba watapata fursa nyingi za huduma. Wanapaswa kuwaombea wagonjwa, na kufanya kila wawezalo kuwapunguzia mateso. Wanapaswa kufanya kazi miongoni mwa wanyonge, maskini, na waliokandamizwa. Tuwaombee na kuomba nao wale wasio na nguvu ya kiroho, nia ya kushinda tamaa ya chakula au tamaa zingine za mwili zilizowaharibu. Bidii ya dhati na ya kudumu inahitajika kwa wokovu wa wale ambao mioyo yao imeguswa na kuamshwa. Wengi wanaweza kufikiwa tu kwa matendo ya wema usio na ubinafsi. Mahitaji yao ya kimwili lazima yatatuliwe kwanza. Watakaposhuhudia ushahidi wa upendo wetu usio wa ubinafsi, itakuwa rahisi kwao kuamini upendo wa Kristo. {*EVsw 545.2}*

Wauguzi wa kimishenari ndiyo walio na sifa bora zaidi kwa kazi hii; lakini wengine wanapaswa kuungana nao. Ingawa wengine hawajafundishwa rasmi kazi ya uuguzi, wanaweza kujifunza kutoka kwa wenzao mbinu bora za kazi ya huduma. — **Testimonies for the Church, Juzuu ya 6, uk. 83-84 (1900)** {*EVsw 545.3}*

Kuwafikia Watu wa Tabaka la Juu

Madaktari wenye ujuzi wa kitaaluma uko juu zaidi kuliko watendakazi wa kawaida wanapaswa kushirikishwa katika kazi ya **Mungu** mijini. Hebu watafute kuwafikia watu wa tabaka la juu. {*EVsw 545.4}*

Wamishenari wa tiba wanaofanya kazi katika huduma ya injili wanafanya kazi ya kiwango sawa cha juu kama wahubiri wa injili. Kazi hii ya tiba ikijumuishwa na kazi ya huduma ya kichungaji, haipaswi kulengwa tu kwa maskini. Tabaka la juu limekuwa likipitwa kwa njia ya kushangaza. Katika jamii ya watu wenye uwezo wa juu, kuna wengi watakaoitikia ile Kweli kwa sababu ni thabiti na endelevu na ina mhuri wa tabia ya juu ya injili. Si wachache kati ya watu wenye vipawa wataingia kwa juhudi katika kazi hii. Kwa kutumia vipawa vyao walivyopewa na **Mungu**, watakuwa wazalishaji, na sio watumiaji tu. {*EVsw 546.1}*

Daktari mwaminifu na mhubiri wanashiriki kazi ile ile. Wanapaswa kushirikiana kwa maelewano kamili. Washauriane kwa pamoja. Kwa umoja wao watatoa ushuhuda kuwa **Mungu** alimtuma Mwana Wake wa pekee ili kuwaokoa wote watakaomwamini kama Mwokozi wao binafsi. — **Manuscript 79, 1900** {*EVsw 546.2}*

Huduma ya Kiroho ya Daktari

Kazi ya wamishenari wa tiba wa Kweli ni kazi ya kiroho kwa kiasi kikubwa. Inahusisha maombi na kuweka mikono juu ya wagonjwa. Kwa hiyo, wanapaswa kutengwa kwa kazi yao kwa namna ya heshima kama ile ya wahubiri wa injili. Wale wanaochaguliwa kuwa madaktari wamishenari, wawekwe wakfu kwa kazi hiyo. Hii itawasaidia kupinga vishawishi vya kuondoka katika kazi ya sanitarium ili kufanya kazi binafsi (private practice). Hakuna nia ya ubinafsi inayopaswa kumvuta mtenda kazi kutoka kwenye kituo chake cha ulinzi na wajibu. Tunaishi katika wakati wa majukumu mazito; wakati ambao kazi ya kujitoa wakfu inapaswa kufanywa. Basi tumtafute Bwana kwa bidii na kwa uelewa. — **Manuscript 5, 1908.** {*EVsw 546.3}*

Huduma Yetu ya Uinjilisti wa Ngazi Tatu

Mungu hufanya kazi kwa kutumia vyombo au visababishi vya pili. Hutumia huduma ya injili, kazi ya umishenari wa tiba, na machapisho yenye Kweli ya wakati huu ili kugusa mioyo. Vyote hufanyika kwa ufanisi kwa njia ya imani. Wakati watu husikia au kusoma Kweli, Roho Mtakatifu huipeleka moyoni mwa wale wanaosikia na kusoma kwa shauku ya dhati ya kujua lililo sahihi. Huduma ya injili, kazi ya kimishenari ya tiba, na machapisho yetu ni vyombo vya **Mungu**. Kimoja hakipaswi kuwa juu ya kingine. **— Letter 54, 1903.** {*EVsw 547.1}*

Ongeza Neno "Tiba"

Huduma ya injili haipaswi kupungua katika ufanisi, bali inapaswa kuongezeka hadi kiwe wakala mkuu wa kuleta nuru duniani. Kila juhudi iwekwe kuhakikisha kuwa watendakazi zaidi wanatumwa kwenye shamba la kazi. Hakuna ushawishi wowote unaopaswa kuelekezwa kuwazuia vijana kujiandaa kwa kazi ya umishenari wa huduma ya injili. Kwa hili tunaweza kuambatanisha neno "tiba"; kwa kuwa ni muhimu kwa mhudumu wa injili kuwa na maarifa kuhusu magonjwa na sababu zake. Anapaswa kujua namna ya kuwasaidia wagonjwa, na pia aweze kuwafundisha watu jinsi ya kutunza "nyumba" tunamoishi—yaani miili yetu. Hili ni sehemu ya injili. **— Letter 123, 1900.** {*EVsw 547.2}*

Kazi Yetu ya Kipekee Kama ile ya Muller

Mungu hamwelekezi sasa mtu yeyote katika kazi ile ile aliyomwelekeza Muller wa Bristol, Uingereza. Muller alifanya kazi tukufu. Lakini **Mungu** amewapa watu Wake kazi ya namna tofauti. Amewapa ujumbe kwa ajili ya ulimwengu mzima. Wanapaswa kuingia eneo baada ya eneo na kufanya vita kali dhidi ya dhambi zinazoharibu roho. — **Letter 33, 1900.** {*EVsw 547.3}*

Kazi Yenye Msawaziko/Balansi—Kwa Maskini na Matajiri

Hivi karibuni [mwaka 1899], kumekuwa na hamasa kubwa ya kuwasaidia maskini na watu wanaobaguliwa au waliotengwa; kazi kubwa imeanzishwa ya kuinua waliodhalilika, walioanguka na kudidimia. Hii ni kazi njema. Daima tunapaswa kuwa na roho ya Kristo, na tufanye kazi ile ile aliyoifanya kwa ajili ya wanadamu waliokuwa wakiteseka. Bwana anao mpango-kazi kwa ajili ya watu wanaobaguliwa na kutengwa. Hakuna shaka kwamba ni wajibu wa baadhi ya watu kufanya kazi miongoni mwao na kujaribu kuwaokoa roho zinazopotea. Kazi hii ina nafasi yake sambamba na kutangazwa kwa ujumbe wa malaika wa tatu na kupokelewa kwa Kweli ya Biblia. Lakini kuna hatari ya kuwabebesha watu wote kazi hii kwa uzito mwingi kwa sababu ya nguvu na msisimko unaotumika. Kuna hatari ya kuwaongoza watu waweze kuelekeza nguvu zao zote katika kazi hii, ilhali **Mungu** amewaita kwa kazi nyingine. {*EVsw 548.1}*

Swali kuu la wajibu wetu kwa wanadamu ni jambo zito, na neema nyingi za **Mungu** zinahitajika katika kufanya maamuzi ya namna ya kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa. Sio wote walioitwa kuanza kazi yao kwa kufanya kazi miongoni mwa tabaka la chini kabisa. **Mungu** hawahitaji watendakazi wake kupata elimu na mafunzo ili wajitoe kikamilifu tu kwa makundi haya. {*EVsw 548.2}*

Utendaji wa **Mungu** hujionyesha kwa namna itakayoweka msingi wa kuaminika kuwa kazi hii ni ya Kiungu, na kwamba misingi madhubuti ndiyo inayouongoza. Lakini nimepokea maelekezo kutoka kwa **Mungu** kuwa kuna hatari ya kupanga kazi kwa ajili ya waliotengwa kwa namna itakayozalisha harakati za ghafla zisizo na mpangilio. Harakati hizo hazitaleta matokeo ya kweli yenye manufaa. Kutakuwa na tabaka la watu litakalohimizwa kufanya kazi ya namna ambayo haitaimarisha kazi yote kwa ujumla kwa njia ya ushirikiano wa pamoja. {*EVsw 548.3}*

Mwito kuwaalika watu kwa injili ni kwa matajiri na maskini, wakuu na wanyonge, na tunapaswa kubuni mbinu za kupeleka Kweli mahali mapya na kwa kila tabaka la watu. Bwana anatuita, "Nendeni kwenye njia kuu na vichochoroni, kawalazimisheni kuingia ili nyumba Yangu ijae." Anasema, "Anzeni na njia kuu; zifanyeni kazi kwa bidii; andaa kikundi cha watu ambao kwa umoja wenu wanaweza kutoka kwenda kufanya kazi ile ile aliyoifanya Kristo—kutafuta na kuokoa waliopotea." {*EVsw 549.1}*

Yesu aliihubiri injili kwa maskini, lakini hakujifunga kwa kundi hilo pekee. Alifanya kazi kwa wote waliokuwa tayari kusikia Neno Lake—si tu watoza ushuru na waliotengwa, bali pia kwa watu walioelimika kama Mafarisayo matajiri, wakuu wa Kiyahudi, maakida wa Kirumi, na wakuu wa dola ya Roma. Hii ndiyo kazi niliyoona daima kuwa inapaswa kufanyika. Hatupaswi kutumia kila nguvu ya misuli ya kiroho kufanya kazi kwa tabaka la chini kabisa tu na kulifanya kuwa jambo kuu. Kuna roho nyingine zinazohitaji Kweli,

ambazo zinabeba majukumu makubwa, na zikitakaswa zitatumika kwa bidii na kutumika kwa ajili ya wale watu wa juu na wa chini pia. {*EVsw 549.2*}

Kazi kwa ajili ya maskini haina mwisho. Haiwezi kuisha kamwe, na lazima itazamwe kama sehemu ya kazi kuu kwa ujumla. Kutoa kipaumbele cha kwanza kwa kazi hii, ilhali kuna maeneo mengi ya shamba la Bwana bado hayajaguswa, ni kuanza mahali pabaya. Kama mkono wa kuume ulivyo kwa mwili, ndivyo kazi ya umishenari wa tiba ilivyo kwa ujumbe wa malaika wa tatu. Lakini mkono wa kuume usiwe mwili wote. Kazi ya kuwatafuta waliotengwa ni muhimu, lakini isiwe mzigo mkubwa unaozidi mingine yote katika utume wetu. **—Medical Ministry, 311, 312 (1899).** {*EVsw 549.3*}

Kazi Iliyopangwa Kwa Uwiano

Kazi ya umishenari wa tiba haipaswi kuwa kubwa kupita kiasi na kukosa uwiano. Lazima iwe kazi iliyopangwa sambamba na kazi nyingine. — Letter 38, 1899. {*EVsw 550.1*}

Afya ya Watendakazi

Wale wanaojitolea kwa moyo wao wote katika kazi ya umishenari wa tiba, wanaofanya kazi bila kuchoka, katikati ya hatari, mateso, kukesha mara kwa mara, uchovu na maumivu, wako katika hatari ya kusahau kuwa wanapaswa kuwa walinzi waaminifu wa nguvu zao za kimwili na kiakili. Hawapaswi kuruhusu miili yao kuchoka kupita kiasi. Lakini kwa kuwa wamejawa na bidii na ari, mara nyingine hufanya maamuzi bila ushauri, na hivyo kujibebesha mizigo mizito. Wasipobadili, mwenendo huu, watendakazi hawa, watapata matokeo ya maradhi na hatimaye kuvunjika nguvu kabisa. {*EVsw 550.2*}

Wakati watendakazi wa **Mungu** wanapaswa kujawa na shauku bora na azimio la kufuata mfano wa Kristo, Tabibu Mkuu wa Kiungu, hawapaswi kubebeshwa majukumu mengi kupita uwezo wao kwa siku moja. Wakifanya hivyo, watalazimika kuacha kazi mapema, wakiwa wamevunjika kabisa kwa sababu ya mzigo mzito uliowalemaza. Ndugu yangu, ni sahihi kwako kutumia kwa busara fursa ulizopewa na **Mungu** kwa juhudi za kuokoa wenye shida, wanaoteseka na roho zilizopotea. Lakini usitoe kafara afya yako. {*EVsw 550.3*}

Tumepokea mwito wa juu kuliko maslahi ya kawaida ya ubinafsi, kama mbingu ilivyo juu kuliko dunia. Lakini wazo hili halipaswi kuwafanya watumishi waaminifu wa **Mungu** wanaofanya kazi kwa bidii kubeba kila mzigo wawezao bila misimu ya kupumzika. {*EVsw 550.4*}

Ingekuwa jambo tukufu kiasi gani kama wote wanaoshiriki katika kutekeleza mpango huu wa ajabu wa **Mungu** wa wokovu wa roho, wangekuwa wachapa kazi halisi na siyo waota ndoto tu wanaorandaranda. Tungefanikiwa zaidi kama kila mmoja angesema:

"**Mungu** ananiwajibisha mimi kuwa macho, na kuacha juhudi zangu zizungumze upendeleo wa ile Kweli ninayoikiri kuamini! Mimi ni mtenda kazi hai na halisi, siyo mtu wa kuishi kwenye ndoto za kufikirika tu." — **Medical Ministry, 292, 293 (1904).** {*EVsw 550.5*}

SEHEMU YA 17—KUFANYA KAZI KWA MAKUNDI YOTE

Kufikia Tabaka Zote

Hubiri Kweli kwa Tabaka Zote

Mwito wa injili ni kwa matajiri na maskini, wakuu na wanyonge, na ni lazima tutafute mbinu za kufikisha Ukweli katika maeneo mapya na kwa watu wa kila tabaka. —**Medical Ministry, 312 (1899).** {*EVsw 552.1*}

Wape Nafasi ya Kuelewa

Asije mtu yeyote akadhani kuwa maskini na watu wasioenda shule ni wa kupuuzwa. Njia sahihi za huduma hazipaswi kuwatenga hawa kwa namna yoyote ile. Mojawapo ya uthibitisho wa Umasihi wa Kristo ilikuwa ni kuwa maskini walihubiriwa injili. Tunapaswa kujifunza na kujitahidi kuwapa watu wa kila tabaka

fursa ya kuelewa Kweli maalum ya wakati huu. —**The Review and Herald, November 25, 1890.** {*EVsw 552.2}*

Ujumbe wa Wokovu kwa Kila Roho

Wengi wana kiu ya ndani ya moyo—kiu ya hitaji ambalo mali wala starehe za dunia haziwezi kuituliza; lakini hawajui namna ya kupokea kile wanachokitamani. {*EVsw 552.3}*

Injili ya Kristo, tangu mwanzo hadi mwisho, ni injili ya neema iokoayo. Ni dhana kuu na ya kipekee. Itakuwa msaada kwa wahitaji, nuru kwa macho yaliyo kipofu kwa Kweli, na mwongozo kwa roho zinazotafuta msingi wa Kweli. Wokovu kamili na wa milele uko ndani ya uwezo wa kila nafsi kufikia. Kristo anangojea na kutamani kutamka msamaha na kutoa neema bure. Anatazama na kungojea, akisema kama alivyomwambia yule kipofu karibu na lango la Yeriko: "Je, *wataka nikutendee nini*?" Nitaondoa dhambi zako; nitakuosha kwa damu Yangu. {*EVsw 552.4}*

Katika njia zote za maisha, kuna roho za kuokolewa. Vipofu wanapapasa gizani. Wapeni nuru, na **Mungu** atawabariki kama watendakazi Wake. **—Letter 60, 1903.** {*EVsw 553.1}*

Mipango kwa Tabaka la Juu Itafikia Wote

Panua mawazo yenu hadi kufikia ukubwa wa kazi hii. Mipango yenu finyu, mawazo yenu yenye mipaka, hayapaswi kuwa sehemu ya mbinu zenu. Lazima kuwe na matengenezo katika jambo hili, na kutakuwa na njia zaidi za kusaidia kazi ifikie hadhi ya juu inayostahili. Kutakuwa na watu wenye mali ambao wataona kwa sehemu tabia ya kazi hii, hata kama hawatakuwa na ujasiri wa kubeba msalaba na aibu ya Kweli isiyo maarufu na isiyopendwa. Kwanza jaribuni kufikia tabaka la juu ikiwezekana, lakini msipuuze tabaka la chini. {*EVsw 553.2}*

Mara nyingi mipango na juhudi zimeelekezwa zaidi kwa tabaka la chini tu, kwamba peke yao ndiyo wanaweza kufikiwa. Lakini mbinu zinaweza kubuniwa ili kuwafikia watu wa tabaka la juu ambao pia wanahitaji nuru ya Kweli kama ilivyo tabaka la chini. Hawa wanaiona Kweli, lakini ni kama wamefungwa katika utumwa wa umasikini, na wanaona njaa mbele yao endapo watakubali Kweli. Pangeni kuwafikia watu wa tabaka bora-au lenye uwezo zaidi, nanyi hamtashindwa kuwafikia wa tabaka la chini. —**Letter 14, 1887.** {*EVsw 553.3}*

Vipawa na Mvuto Vilivyobadilishwa

Watumishi wa **Mungu** hawapaswi kutumia muda wao wote kwa wale waliomtumikia Shetani maisha yao yote hadi kuharibika kabisa kwa ufisadi. Lakini wale waliotupwa na kutengwa watakapokuja, nao watakuja kama walivyokuja kwa Kristo, tusiwakataze kuja. Lakini **Mungu** anawaita watendakazi kuwafikia watu wa tabaka la juu, ambao wakigeuzwa, wanaweza kuwahudumia wa tabaka lao. Yeye Anataka kuona vipawa na ushawishi vilivyogeuzwa vikihusishwa na kazi Yake. Mungu anatenda kazi juu ya wanaume na wanawake wenye talanta na ushawishi, akiwaunganisha na wale ambao wanatoa ujumbe wa mwisho wa rehema kwa dunia—**Manuscript 6, 1902.** {*EVsw 553.4}*

Njia za Paulo Zilifikia Mataifa na Watu Wote

Katika safari zake, Paulo alichanganya huduma ya nyumbani na ya nje, katika nchi za kigeni. Mara zingine alikuwa akihubiri kwa Wayahudi mahali pao pa ibada; mara nyingine kwa Mataifa mbele ya mahekalu yao na hata mbele ya miungu yao. Paulo hakuwahubiria Wayahudi Masihi wa kuharibu Agano la Kale, bali Masihi aliyekuja kutukuza na kukuza uchumi wa Israeli kulingana na ile Kweli (Jewish Economy-Uchumi wa Kiyahudi wa Kibiblia ulikuwa mfumo wa theokrasia uliozingatia mwenendo wa kimaadili, kanuni za Kiungu, na uwajibikaji wa kijamii, ukisisitiza kazi ya uaminifu, kuwatunza maskini (tzedakah), mishahara ya haki, na usimamizi wa utajiri kama baraka ya Mwenyezi Mungu, huku ukikataza riba (riba) miongoni mwa Waisraeli na kuamuru msamaha wa deni na upangaji upya wa ardhi (Yubile) ili kuzuia umaskini wa kudumu na kudumisha usawa, yote haya yalikuwa chini ya sheria ya Mungu badala ya kanuni za kidunia, ikilenga jamii yenye haki.utajiri wa kiroho nk Jewish economy). {*EVsw 554.1}*

Wanafunzi waliolieneza Neno kwa upana walikuwa tayari kwa mahojiano ya aina yoyote na waliobaki nyumbani. UKristo ulipata ushindi wa wazi, na Wayahudi waliogeuka kuwa Wakristo, walichukua msimamo wa juu kuwa UKristo na wokovu ni kwa mataifa yote, lugha zote, na watu wote wa duniani. —**Letter 17, 1900.** {*EVsw 554.2}*

Kuwafikia Wenye Mali na Ushawishi

Wapeni Wito Viongozi wa Biashara na Serikali

Wito wa kubebwa katika “njia kuu” unapaswa kutangazwa kwa wote walio na nafasi za kazi muhimu duniani—walimu na viongozi wa watu. Wale wanaobeba majukumu mazito katika maisha ya umma—madaktari na walimu, mawakili na majaji, maafisa wa serikali na wafanyabiashara—wanapaswa kupewa ujumbe ulio wazi na usio na mushkeli. **—Testimonies For The Church 6:78 (1900) {*EVsw 554.3}***

Watafutwe Wenye Ushawishi

Wale wa tabaka za juu katika jamii wanapaswa kutafutwa kwa upendo wa kipekee na kwa heshima ya kindugu. Wanaume walioko katika maisha ya biashara, walioko katika nafasi za juu za amana, watu wenye vipaji vya uvumbuzi na maarifa ya kisayansi, watu wa akili mahiri/genius na vitivo vya ubunifu, walimu wa injili ambao hawajawahi kuujua Ukweli wa wakati huu—hawa wawe wa kwanza kusikia wito wa injili. **—Christ’s Object Lessons, 230 (1900). {*EVsw 555.1}***

Tunazungumza na kuandika sana kuhusu maskini waliopuuzwa; Je, hatupaswi kutoa umakini wetu kwa matajiri waliopuuzwa? Wengi huwaona watu wa kundi hili kama wanadamu wasio na tumaini, na hufanya juhudi kidogo sana kufungua macho yao, na kuwaonyesha njia. Ingawa matajiri wamepofushwa na kughafilishwa na nguvu za Shetani, wamesahaulika kwa sababu ya kuonekana wamejaa fahari au hawahitaji chochote, katika makadirio yasiyokuwa kweli ya wainjilisti, kundi hili la matajiri limepoteza umilele. Maelfu ya watu matajiri wamekufa bila kuonywa kwa sababu walihukumiwa kwa sura ya nje na kupitwa kana kwamba watu wasio na tumaini. Lakini japokuwa wanaonekana kama watu wasioguswa, nimeonyeshwa kuwa wengi wao wameelemewa na mizigo ya roho. Maelfu ya matajiri wanakufa kwa njaa ya chakula cha kiroho. Wengi walioko katika maisha ya hadhi wanatambua kuwa wanahitaji kitu ambacho hawana. Ni wachache tu miongoni mwao huenda makanisani, kwasababu wanafikir hawapati faida yoyote. Mafundisho wayasikiayo hayagusi roho. Je, hatutafanya juhudi za binafsi kwa ajili yao? —**Testimonies For The Church 6:78 (1900). {*EVsw 555.2}***

Watendakazi Wenye Akili Mahiri Ili Kuwafikia Wa Daraja la Juu

Hakujakuwa na juhudi za kutosha kufikia tabaka la juu. Japokuwa tunapaswa kuihubiri injili kwa maskini, pia tunapaswa kuiwasilisha kwa nutu kuvutia zaidi kwa wale wenye vipawa na uwezo. Tufanye juhudi zilizo bora zaidi, zilizojaa hekima na kumcha **Mungu** kuliko tulivyowahi kufanya, ili kuwavuta kwenye ile Kweli. **{*EVsw 555.3}***

Lakini ili hili lifanikishwe, watendakazi wote lazima wajiweke katika kiwango cha juu cha maarifa na akili mahiri. Hawawezi kufanya kazi hii huku wakididimia na mawazo ya kawaida na wakihisi kwamba haijalishi namna wanavyofanya kazi au wanavyosema kwa tabaka lolote, kwa sababu wanafanya kazi kwa maskini na wasio na elimu. Lazima wajikite katika ubora kwa kujinoa kiakili wawe na silaha za maarifa ili kuwasilisha Kweli kwa uelewa na akili mahiri na kuwafikia watu wa daraja la juu. Akili zao lazima zipande juu, na kuonyesha nguvu na uwazi... **{*EVsw 556.1}***

Sababu moja iliyofanya juhudi za kuwafikia wa tabaka la juu zisiwepo ni ukosefu wa imani ya Kweli na ujasiri ndani ya **Mungu**. **—Manuscript 14, 1887. {*EVsw 556.2}***

Kwa Ndoano Iliyowekwa Chambo Inayofaa

Wenye akili, waliostaarabika, wameachwa sana-wamepitwa. Ndoano haijawekewa chambo kwa ajili ya kundi hili, na mbinu na njia za kuwafikia kwa ile Kweli hazijabuniwa kwa maombi ili waweze kuhekimishwa kwa wokovu. Kwa kawaida, matajiri, walio katika mitindo ya kifahari, wenye majivuno, tayari wanajua kutokana na uzoefu kuwa furaha haiji kwa kiasi cha pesa walicho nacho, au kwa nyumba nzuri na fanicha za kifahari na picha za ukutani. Wanataka kitu wasichokuwa nacho. Lakini watu hawa huvutiwa na wenzao wa daraja lao, na ni vigumu kuwapafikia walipo; na kwa sababu hiyo wengi huangamia katika dhambi zao, ingawa wanatamani kitu kitakachowaletea pumziko la moyo, utulivu na amani ya kweli. Wanamhitaji Yesu, nuru ya haki. **{*EVsw 556.3}***

Kuna namna ya huduma inayoendelea kwa njia ya kawaida ambayo inaacha watu wengi wa kundi hili bila kufikiwa..... **{*EVsw 556.4}***

Matajiri wanaoachwa bila juhudi ya kuwaokoa hujifungia zaidi ndani ya mawazo yao wenyewe. Mwelekeo wao wa kufikiri na ushirika wao unapoteza kabisa wazo la milele kwenye fikra zao. Wanaendelea kukua kwa majivuno zaidi, ubinafsi, uchoyo, ugumu wa moyo na wasioguswa. Wanashuku kwamba kila mtu anazitaka pesa zao, ilhali maskini huwaonea kijicho matajiri, ambao wanahitaji kusikitikiwa zaidi kuliko kuonewa wivu. Waleteni wote hawa chini ya nguvu ya Kweli inayookoa, na kazi ya kuujenga Ufalme wa **Mungu** itasonga mbele kwa mafanikio makubwa zaidi. **—Manuscript 66, 1894. {*EVsw 556.5*}**

Kuvutwa na Kweli ya Maandiko

Watu walioko katika nafasi za juu za heshima duniani watavutwa na wasilisho lililo wazi, lisilo na ujanja, la Kweli ya Maandiko. **—Letter 111, 1904. {*EVsw 557.1*}**

Epukeni Mabishano Makali

Watu wakuu, wenye nyadhifa kubwa, wenye elimu, wanaweza kufikiwa zaidi kwa unyenyekevu na usahili wa maisha ya utauwa kuliko kwa mabishano makali ya hoja wanayomwagiwa. Taswira nzuri hutolewa pale dini inapokuwa hai, ambayo itatoa uzima na maendeleo. Mbegu ya ile Kweli inapopata makazi moyoni kupitia kazi ya Roho wa Kristo, mpokeaji hutambua uovu wa tamaa za kibinadamu, majivuno, ubatili na ujinga. Mambo haya yote lazima yasafishwe katika hekalu la roho, na neema ya **Mungu** iwe kanuni ya kudumu. Ndipo kanuni zote za Kweli zitachanua katika bustani ya **Mungu** —unyenyekevu, upole, subira, na upendo. —**Letter 6b, 1890. {*EVsw 557.2*}**

Wasilisha Kweli kwa Mafumbo na Mifano

Kweli inapaswa kuwasilishwa kwa namna mbalimbali. Baadhi ya walio juu katika jamii za juu wataielewa Kweli ikiwa itawasilishwa kwa mafumbo na mifano. **—Medical Ministry, uk. 318 (1905). {*EVsw 557.3*}**

Kuvutwa na Urahisi/Usahili wa Injili

Hata watu wakuu huvutwa zaidi na unyofu na usahili wa injili kuliko kwa juhudi yoyote inayofanywa kwa nguvu ya kibinadamu. Tunamhitaji zaidi **Mungu** na nafsi zetu kwa udogo sana. **Mungu** atafanya kazi kupitia chombo dhaifu kabisa cha kibinadamu kwa ambaye amejazwa na Roho Wake. **—Letter 72, 1899. {*EVsw 557.4*}**

Vipawa vya Akili na Mali

Tunapaswa kufanya kazi maalum kwa wale walio katika nafasi za juu za uaminifu-amana. Bwana anawaita wale ambao Amewakabidhi mali Yake, kutumia vipawa vyao vya akili na vya mali kwa ajili ya kazi Yake. Wengine watahamasishwa na Roho Mtakatifu kuwekeza mali ya Bwana kwa namna itakayoendeleza kazi Yake. Wataitimiza nia Yake kwa kusaidia kuanzisha vituo vya mvuto katika miji yetu mikubwa. Watendakazi wetu wanapaswa kuwasilisha mbele ya watu hawa maelezo ya wazi kuhusu mahitaji yetu. Wajulishe kile tunachohitaji ili kuwasaidia maskini na wahitaji na kuimarisha kazi hii kwa msingi thabiti. — **Medical Ministry, uk. 329 (1900). {*EVsw 558.1*}**

Fanya Kazi kwa Ajili ya Watu Kama Kornelio

Katika kisa cha Kornelio tunapaswa kujifunza somo ambalo litatusaidia sana tukilielewa. **Mungu** wa mbinguni hupeleka wajumbe Wake duniani ili kusababisha mfululizo wa matukio ambayo yangemwunganisha Petro na Kornelio, ili Kornelio aweze kujifunza Kweli. Kupitia huduma ya malaika, Petro analetwa kushirikiana na roho zinazotafuta, ambazo zilikuwa tayari kabisa kusikia Ukweli na kupokea nuru mpya... **{*EVsw 558.2*}**

Kuongoka kwa Kornelio na nyumba yake ulikuwa ni mavuno ya kwanza tu ya mavuno makubwa kutoka kwa watu wa mataifa- yatakayovunwa. Kupitia nyumba hiyo kazi kubwa ya neema ilienea katika jiji la kipagani. **—Letter 17, 1900. {*EVsw 558.3*}**

Kunahitajika kuamka miongoni mwa watu wa **Mungu**, ili kazi Yake iendelee kwa nguvu. Tunahitaji ubatizo wa Roho Mtakatifu. Tunahitaji kuelewa kuwa **Mungu** ataongeza kwenye safu ya watu Wake wanaume wenye uwezo na ushawishi, ambao watashiriki kazi ya kutoa onyo kwa ulimwengu. Sio watu wote duniani ni waasi, wasiojali sheria au waovu. **Mungu** ana maelfu ambao hawajapiga goti kwa Baali. Kuna watu wacha

Mungu katika makanisa yaliyoanguka. Ikiwa haingekuwa hivyo, tusingepewa ujumbe huu wa kusema, "Umeanguka, umeanguka Babeli ule mkuu... Tokeni kwake, enyi watu Wangu." {*EVsw 558.4}*

Injili inapaswa kutangazwa mijini mwetu. Watu wa elimu kubwa na ushawishi wanapaswa kusikia ujumbe huu. Sio watu weupe tu, bali hata watu weusi wenye uwezo wanapaswa kuikubali imani. Hao watafanya kazi kwa ajili ya watu wao wenyewe, nao wanapaswa kusaidiwa katika kufanya kazi ambayo Bwana anatamani ifanywe. {*EVsw 559.1}*

Maombi zaidi, tabia ya kufanana na Kristo zaidi, na utiifu zaidi kwa mapenzi ya **Mungu** vinapaswa kuletwa katika kazi ya **Mungu**. Maonesho ya nje, matumizi makubwa ya fedha hayatafanya kazi hiyo. Wengi wanapumua kwa shida wakihitaji pumzi ya uzima kutoka mbinguni. Watatambua injili iwapo italetwa kwao kwa njia ambayo **Mungu** ameikusudia. {*EVsw 559.2}*

Katika dunia yenye shughuli nyingi, iliyojaa kelele za biashara na ugomvi wa soko katika bei za bidhaa miongoni mwa mataifa, ambamo watu wanapambana kwa uchoyo kujipatia faida binafsi, Kristo alikuja; na juu ya kelele zote, sauti Yake, kama tarumbeta ya **Mungu**, ilisikika:

"**Mathayo 16:26** "*Kwani atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote, na kupata hasara ya nafsi yake? Au mtu atatoa nini badala ya nafsi yake*?" {*EVsw 559.3}*

Kristo anawaelekeza watu kwenye ulimwengu bora ambao wameusahau katika mahesabu yao, na Anatangaza kwamba mji pekee utakaodumu ni ule ambao mjenzi na mtengenezaji Wake ni **Mungu**. Anawaonesha kizingiti cha mbingu, kimejaa utukufu wa **Mungu** aliye hai, na anawahakikishia kwamba hazina za mbinguni ni kwa wale wanaoshinda. Yeye Anawaita kujitahidi kwa matamanio makuu ya takatifu kupata urithi usiokufa. Anawahimiza kuweka hazina zao karibu na kiti cha enzi cha **Mungu**. Ndipo, badala ya kujitaabisha karibu kupita mipaka ya uwezo wa mawnadamu kwa ajili ya kupata mali za dunia, watafanya kazi kwa nguvu zote za mwili na akili kwa ajili ya Kristo. Kwa kutumia vipawa vyao vya mali ili kuwaleta watu kwa Kristo, watakuwa wakifanya kazi ya muhimu zaidi kuliko kazi nyingine yoyote duniani. {*EVsw 559.4}*

Miongoni mwa matajiri wa dunia, wapo watakaopokea ujumbe wa onyo:

"**1 Timoteo 6:17-19** "*Walio matajiri wa ulimwengu wa sasa uwaagize wasijivune, wala wasiutumainie utajiri usio yakini, bali wamtumaini* ***Mungu*** *atupaye vitu vyote kwa wingi ili tuvitumie kwa furaha. Watende mema, wawe matajiri kwa kutenda mema, wawe tayari kutoa mali zao, washirikiane na wengine kwa moyo; huku wakijiwekea akiba iwe msingi mzuri kwa wakati ujao, ili wapate uzima ulio kweli kweli.*" —**Letter 51, 1902. {***EVsw 560.1}*

Wafalme na Wakuu Wanapaswa Kusikia

Nuru inapaswa kufikishwa mbele ya wafalme na watu wakuu wa dunia, hata kama wataipokea kwa namna ileile ambayo Farao alipokea ushuhuda wa watumishi wa Bwana, na kuuliza, **Kutoka 5: 2** "*Bwana ni nani, hata niisikilize sauti Yake*?" {*EVsw 560.2}*

Wafalme, magavana, na watu wakuu watasikia habari zenu kupitia ripoti za wale walio na uhasama nanyi, na imani yenu pamoja na tabia zenu zitatafrisiwa vibaya mbele yao. Lakini wale wanaosingiziwa uongo watapewa fursa ya kujitetea mbele ya washtaki wao, kutoa majibu wenyewe. Watakuwa na nafasi ya kuleta nuru mbele ya wale wanaoitwa watu wakuu wa dunia, na kama mmejifunza Biblia, mkiwa tayari kujibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu kwa upole na kwa hofu ya Mungu, adui zenu hawataweza kupinga hekima yenu. **—The Review and Herald, April 26, 1892. {***EVsw 560.3}*

Kuwaonya Viongozi wa Nchi

Watawala wa mataifa wanapaswa kukanyaga miguu yao juu ya msingi wa Kweli ya milele. Hawapaswi kuachwa, na kuruhusiwa kwa sababu ya ujinga, kujenga nyumba zao juu ya mchanga. Watu hawa hawapaswi kuabudiwa kama miungu. Waowanawajibika kwa **Mungu** kwa mwenendo wao. Watapaswa kujibu kwa **Mungu** ikiwa watakuwa harufu ya mauti iendayo mauti kwa wale walioko chini ya mamlaka yao. **— Letter 187, 1903. {***EVsw 561.1}*

Hatari za Mafanikio

Katika historia ya wanadamu tunajifunza jinsi ustawi (mafanikio) ulivyo hatari. Sio wale waliopoteza mali na vitu vyao ndio walio katika hatari kubwa, bali wale waliopata utajiri na kuwekwa katika nafasi ya juu. Hawa wanahitaji huduma ya uangalifu na ya dhati na bidii. Dhiki huweza kutufanya tunyenyekee, lakini ustawi huinua hadi kiburi. {*EVsw 561.2}*

Maombi huombwa sana kwa ajili ya watu wanaopatwa na mateso, jambo ambalo ni sahihi; lakini maombi yenye bidii zaidi yanapaswa kuombwa kwa ajili ya wale walioko katika hali ya ustawi-mafanikio. Hawa ndio walio katika hatari kubwa ya kupoteza nafsi.

Katika bonde la kuaibishwa na kudhiliwa tunaweza kutembea kwa usalama, tukiwa tunamcha **Mungu** na kumtumainia. Lakini kwenye kilele cha juu sana, pale ambapo tunapewa sifa na watu, ambapo hekima na ukuu wetu vinatukuzwa, tunahitaji nguvu ya pekee, mkono maalumu wa kututunza. {*EVsw 561.3}*

Hivi ndivyo tunavyopaswa kuwaona wale wasio wa imani yetu. Watu wanaotukuzwa na kusifiwa wanahitaji msaada mkubwa zaidi katika unyenyekevu na usahili wa Kristo kuliko wanavyopata. Wanahitaji maombi ya dhati, ya kudumu, ili waweze kuokolewa na maangamizi. —**Letter 72, 1899**. {*EVsw 561.4}*

Wahudumu wa Madhehebu Mengine

Kuwakaribia Wachungaji wa Madhehebu Mengine

Wachungaji wetu wanapaswa kujitahidi kuwa karibu na wachungaji wa madhehebu mengine. Wawaombee na waombe pamoja na watu hawa, ambao Kristo anawaombea mbele za Baba. Wana jukumu zito sana. Kama wajumbe wa Kristo, tunapaswa kuonyesha shauku ya dhati na ya kina na ya kweli kwa wachungaji hawa wa kundi. **—Testimonies for the Church, Gombo la 6: 78 (1900).** {*EVsw 562.1}*

Umuhimu wa Kuwafikia Wachungaji Wengine

Kazi yenye busara na thabiti inapaswa kufanywa kwa wachungaji ambao si wa imani yetu. Wapo waumini wengi ambao wanadanganywa kwa sababu ya kutojua, kwa mafundisho ya wahudumu wa makanisa mengine. Hebu watendakazi waaminifu, wenye kumcha **Mungu**, na walioficha maisha yao ndani ya Kristo, waombe na kufanya kazi kwa ajili ya wachungaji waaminifu ambao wamefundishwa kupotosha Neno la Uzima. {*EVsw 562.2}*

Wahudumu wetu waamue kwa moyo wao wote kufanya kazi ya kuwafikia wahudumu wa madhehebu mengine. Hawapaswi kuingia katika mabishano nao, bali, wakiwa na Biblia mikononi mwao, wawahimize wajifunze Neno. Tukifanya hivi, kuna wahudumu wengi wanaohubiri makosa leo, ambao watahubiri Kweli ya wakati huu. **—Letter 72, 1899.** {*EVsw 562.3}*

Kwa Nini Wasipuuzwe?

Tumepoteza mengi kwa kufuata mipango finyu kiasi kwamba tabaka la watu wenye elimu na maarifa ya juu au akili mahiri hawakufikiwa. Mara nyingi kazi yetu imefanywa kwa namna inayowafanya wasioamini waione kuwa ni jambo la hatima ndogo tu—kama tawi dogo la dini lililojitenga, lenye msingi na usongo wa kidini li, lisilostahili hata kutazamwa (offshoot enthusiastic). Tumepoteza mengi kwa kukosa mbinu za busara za kufanya kazi. Kila jitihada inapaswa kufanywa ili kuipa kazi tabia, hadhi na heshima. {*EVsw 562.4}*

Inahitaji hekima nyingi kuweza kuwafikia wachungaji na watu wenye ushawishi. Lakini kwa nini wamepuuzwa kwa muda mrefu na watu wetu? Watu hawa wanawajibika mbele za **Mungu** kulingana na vipawa walivyopewa. Yule aliyepewa mengi, atahitajika kutoa hesabu ya mengi. Je, hatupaswi kuwa na tafakari ya kina na kuomba kwa bidii ili kupata hekima ya kuwafikia watu wa tabaka hili? Je, hatupaswi kutumia hekima na busara ili kuzipata roho hizi, ambazo zikipata uongofu wa kweli, zitakuwa vyombo vilivyopambwa mikononi mwa **Mungu** kwa ajili ya kuwaongoa wengine? ... Tukiweza kuzifikia roho hizi ambazo **Mungu** amewakabidhi vipawa vikubwa, basi kupitia wao, ushawishi wetu utaenea zaidi, na kuwa nguvu ya mbali kwa mema. {*EVsw 562.5}*

Mungu anao mpango wa kazi ambayo bado watendakazi hawajauelewa kikamilifu. Wachungaji na wenye hekima wa dunia watajaribiwa kwa nuru ya Kweli ya sasa. Ujumbe wa malaika wa tatu unapaswa kuwekwa mbele yao kwa busara, ukiwa katika hadhi yake ya kweli. Lazima kuwe na kutafuta kwa dhati na bidii uso wa **Mungu**, na kujifunza kwa kina; maana nguvu za akili zitahitajiwa kikamilifu kushugulishwa katika kuweka mipango ya kuiinua kazi ya **Mungu** juu katika kiwango cha heshima. Hapo ndipo kazi hii

inapaswa kuwa daima, lakini mawazo finyu yenye mipaka ya wanadamu na mipango yao midogo imeifanya ishuke chini na itembee kwa ufinyu. —**Review and Herald, November 25, 1890. {*EVsw 563.1*}**

Siyo Wote Watakaopokea Kweli

Baada ya juhudi za dhati kufanyika ili kuipeleka Kweli kwa wale ambao **Mungu** amewakabidhi majukumu makubwa, hebu msiwe na moyo wa kukata tamaa ikiwa wataikataa Kweli. Hii ilitokea pia katika siku za Kristo. Hakikisheni kuwa mnaendeleza hadhi ya kazi kwa mipango iliyo bora na maisha ya utauwa na maneno yenye uchaMungu. Msifikiri kuwa mmekinyanyua juu mno kiwango cha kazi. **—Letter 12, 1887. {*EVsw 563.2*}**

Kuzungumza Katika Makanisa Mengine

Huenda mkapewa nafasi ya kuzungumza katika makanisa ya madhehebu mengine. Mnapoboresha nafasi hizo, kumbukeni Maneno ya Mwokozi: **Mathayo 10:16** "*Basi iweni na busara kama nyoka, na kuwa watu wapole kama hua.*" Msichochee chuki ya adui kwa kutoa hotuba za laana au shutuma. Kwa kufanya hivyo mtawafungia watu njia ya kuupokea Ukweli. Ujumbe wa Kweli usio na madoa unapaswa kutolewa. Lakini jihadharini na kuibua upinzani. Kuna roho nyingi za kuokolewa. Zuieni maneno ya ukali. Katika maneno na matendo yenu iweni na hekima kwa ajili ya wokovu, mkimwakilisha Kristo kwa wote mnaokutana nao. Wote waone kuwa miguu yenu imevalishwa kwa maandalizi ya Injili ya amani na mapenzi kwa wanadamu. Matokeo ya ajabu yataonekana tukifanya kazi tukiwa tumejazwa na Roho wa Kristo. Msaada utapatikana pale tunapohitaji, ikiwa tutaisogeza mbele kazi kwa haki, rehema, na upendo. Ukweli utashinda, na kubeba ushindi. **—Manuscript 6, 1902. {*EVsw 563.3*}**

Kufanya Kazi kwa Tabaka la Watu wa Kati

Kundi Linaloweza Kufikiwa Kwa Urahisi

Kuna kundi lingine linaloweza kufikiwa kwa urahisi zaidi. Wengi wao wana stahiki kuliko matajiri, kwa kuwa si wote walio matajiri wamepata mali zao kwa uadilifu wa kweli. Wapo wale ambao kamwe hawatakubali kukiuka kanuni au uaminifu ili kupata mali yoyote. Hiki ndicho kikundi ambacho, ikiwa Kweli ingeletwa kwao kwa hekima, wangeipokea na kuwa watendakazi waaminifu pamoja na **Mungu**. Mtendakazi wa **Mungu**, kwa hekima atakayopewa, atafanya kazi kwa namna ya kuwaunganisha watu hawa katika Kristo Yesu. **—Manuscript 66, 1894. {*EVsw 564.1*}**

Tunawezaje Kuwafikia?

Na tunawezaje kuwafikia watu wa kawaida? Kristo alijaribu kufanya kazi na viongozi wa juu kabisa wa taifa. Lakini hawakumpokea, kwa sababu aliwaambia Ukweli. Walikuwa na mawazo yaliyoinuliwa ya kufikiria ucha Mungu wao. Hawakuwa tayari kufundishwa. Walidhani kazi yao ni kuwafundisha wengine, si wao kufundishwa. Lakini kuhusu maskini, Maandiko yanasema, "Watu wa kawaida walimsikiliza kwa furaha." **Zaburi 68:10-11** "*Ee **Mungu**, kwa wema Wako uliwaruzuku walioonewa, "Bwana analitoa Neno Lake; Wanawake watangazao habari ni jeshi kubwa.*"—**Manuscript 125, 1897. {*EVsw 564.2*}**

Kristo Aliwafikia kwa Njia ya Akili Zao

Tunaweza kufanya mengi kwa muda mfupi ikiwa tutafanya kazi kama Kristo alivyoifanya. Tunapaswa kutafakari kwa faida kuhusu mtindo Wake wa kufundisha. Alijitahidi kuwafikia watu wa kawaida. Mtindo Wake ulikuwa wazi, rahisi, na uliojumuisha wote na kueleweka. Alichukua mifano kutoka katika mazingira yaliyowazunguka wasikilizaji Wake, yale waliyofahamu. Kwa kutumia mambo ya asili alifafanua Kweli za milele, na kwa njia hiyo akaunganisha mbingu na dunia. **—Manuscript 24, 1903. {*EVsw 565.1*}**

Jifunze Unyofu wa Kristo

Mwokozi alikuja "kuhubiri Injili kwa maskini." Katika mafundisho Yake alitumia Maneno rahisi sana na alama na vielelezo vilivyo wazi kabisa. Na imeandikwa kwamba "Watu wa kawaida walimsikiliza kwa furaha." Wale wanaotafuta kufanya kazi Yake katika wakati huu wanahitaji kuelewa kwa undani zaidi mafundisho Aliyoyatoa. **—The Ministry of Healing, 443 (1905). {*EVsw 565.2*}**

Watu wa Bwana Wengi Ni Watu wa Kawaida

Watu wa Bwana kwa sehemu kubwa ni maskini wa dunia hii, watu wa kawaida. Si wengi walio na hekima, wala si wengi wenye nguvu, au wenye cheo wanaoitwa. **Mungu** “amewachagua maskini wa dunia hii.” “Maskini wanahubiriwa Injili na wanasikia.” Matajiri wanaitwa, kwa namna fulani; wanakaribishwa, lakini hawakubali mwaliko. Lakini katika miji hii ya uovu, Bwana anao wengi walio wanyenyekevu na wanaomtegemea na kumwamini. **—Manuscript 17, 1898. {*EVsw 565.3*}**

Ikiwa Nuru ya Mungu Itatunzwa

Hakuna tabaka mbele za **Mungu**. Yeye hapuuzi mtu kwa misingi ya hadhi au jamii. Kila roho ina thamani mbele Zake. Kufanya kazi kwa ajili ya wokovu wa roho ni ajira yenye heshima kuu. Haijalishi kazi yetu ni ya namna gani, au tunafanya kazi miongoni mwa tabaka lipi, la juu au la chini. Kwa **Mungu**, tofauti hizi hazibadilishi thamani ya kweli ya kazi hiyo. Roho ya unyofu, ya dhati, yenye kutubu, hata kama ni jinga, ni ya thamani machoni pa Bwana. **Mungu** huweka muhuri Wake juu ya watu, si kwa kuwahukumu kwa cheo chao, au kwa utajiri wao, wala kwa umahiri wa akili zao kuu, bali kwa kuungana kwao na Kristo. Asiyekwenda shule, aliyepuuzwa, aliyetengwa au hata mtumwa, kama amefanya kadiri ya nafasi na fursa alizopewa, na ameithamini nuru aliyopewa na **Mungu**, basi ametimiza yote anayohitajika kutimiza. Dunia inaweza kumwita mjinga, lakini **Mungu** humwita mwenye hekima na mwema, na jina lake huandikwa katika vitabu vya mbinguni na linaonekana hapo. **Mungu** atamwezesha kumtukuza, si tu mbinguni, bali pia hapa duniani. **—Gospel Workers, ukurasa 332 (1915). {*EVsw 566.1*}**

Kufanyakazi kwa Ajili ya Binadamu Aliyeanguka

Binadamu Aliyeanguka Ndiyo Uwanja Wetu wa Kazi

Wako wengi walio wavivu, wavutaji wa tumbaku, na wanywaji wa pombe. Lakini Ukweli lazima uwafikie. Umefanya mambo ya ajabu mahali hapa [Australia], na bado utaendelea kufanya mambo makuu. Imani yetu kwa Bwana Yesu Kristo na katika Kweli ya wakati huu haipaswi kubaki tu kwa wale waliompokea Kristo. Kristo alikufa kuokoa ulimwengu, nasi tunapaswa kufanya kazi kwa bidii na ari zaidi katika kutimiza wajibu wetu. Tuwatazame binadamu walioanguka kama uwanja wetu wa kazi. **Mungu** anawajali... Asikosekane hata mtu mmoja katika giza. **—Letter 76, 1899. {*EVsw 566.2*}**

Wengine Matajiri Waliopotoka Wataokolewa

Miji yetu mikubwa inaendelea kwa kasi kufikia hali iliyokuwepo kabla ya Gharika, ambapo " **Mwanzo 6:5**

“*BWANA akaona ya kuwa maovu ya mwanadamu ni makubwa duniani na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya tu sikuzote*." Dhambi zinazomvunjia heshima **Mungu** zinafanywa na watu wanaoishi katika nyumba za kifahari; lakini baadhi ya watu hawa, wakihudumiwa na ujumbe wa mwisho wa wenye kujaribu, wataguswa na kuongolewa. **{*EVsw 567.1*}**

Kutoka katika hazina isiyoisha ya neema, **Mungu** anaweza kuwajalia wote wanaomjia. Anapolitazama binadamu aliyeanguka na aliyepotoka, anatangaza kuwa Roho Mtakatifu atamwagwa juu ya wote. Wengi ambao hawajawahi kusikia zile Kweli maalum kwa wakati huu watahisi msukumo wa Roho wanaposikia ujumbe wa umuhimu na wa ajabu... **{*EVsw 567.2*}**

Mungu atainua watendakazi ambao watashika nafasi za pekee za ushawishi, watakaobeba Ukweli hata kwenye maeneo yasiyo na matumaini. Watu watasema, “Ndiyo,” mahali walipokuwa wakisema, “La.” Baadhi waliokuwa maadui hapo awali watakuwa wasaidizi wa thamani, wakisukuma mbele kazi kwa mali na ushawishi wao. —**Review and Herald, September 30, 1902. {*EVsw 567.3*}**

Kufanya Kazi kwa Ajili ya Waliopotoka

Hakuna jambo litakalotoa hadhi kwa kazi ya kuwasilisha ukweli kama kusaidia watu pale mahali walipo, kazi kama ile ya Msamaria mwema. Kazi inayofanywa ipasavyo ya kuwaokoa wenye dhambi maskini waliopitwa na makanisa, itakuwa kama daraja la kuingilia ambayo itafanikisha kupenya kwa Ukweli. Mfumo tofauti wa mambo unahitaji kuanzishwa miongoni mwetu kama watu wa **Mungu**, na katika kufanya kazi ya aina hii, mazingira tofauti kabisa yatakuzwa katika nafsi za watendakazi, kwa kuwa Roho Mtakatifu huwasiliana na wote wanaofanya kazi ya **Mungu**; na wale wanaoendeshwa na Roho Mtakatifu watakuwa nguvu ya wema katika kuinua, kuimarisha, na kuwaokoa wale walio karibu kupotea. —**Manuscript 14a, 1897. {*EVsw 567.4*}**

Kuzuia Watu Wasifike Hatua ya Kutelekezwa Kabisa

Tuitumie mali yetu na vipawa vyetu vya ushawishi kutangaza ukweli ambao utazuia watu kufikia hali ya kutelekezwa kabisa. Tukishika kazi ambayo Bwana ametupa, Ukweli utawafikia wengi wa tabaka hili kwa njia mbalimbali. Lakini tusipuuze kazi zile ambazo Bwana ametuagiza tuzisimamie na kusonga mbele. Tabaka zote zinapaswa kufikiwa. {*EVsw 568.1*}

Ikiwa wale wanaofanya kazi kwa ajili ya waliotelekezwa na waliopotoka watafanya kazi kwa kumcha Bwana, wakijitahidi kuwasaidia wale wanaowahudumia kuelewa Ukweli ni nini, basi wengi wa waliotengwa watatambulika kuwa watoto wa **Mungu**. **—Letter 143, 1904.** {*EVsw 568.2*}

Uchaguzi wa Watendakazi kwa Ajili ya Waliotengwa

Tahadhari kubwa inapaswa kuchukuliwa katika kufanya kazi kwa ajili ya waliotengwa na jamii. Vijana wa kiume wala wa kike hawapaswi kutumwa katika maeneo ya chini kabisa ya miji yetu. Macho na masikio yao vijana yaepushwe na maovu. Vijana wanaweza kufanya mengi kwa ajili ya Bwana. Wakiomba, wakikesha, na kumtumaini **Mungu**, wataweza kufanya kazi bora mbalimbali chini ya uongozi wa watumishi wenye uzoefu. **—Medical Ministry, uk. 312 (1901).** {*EVsw 568.3*}

Mgeni Miongoni Mwetu

Kuwafikia Watu wa Kila Taifa, Tabaka, na Dini

Kristo hakutambua tofauti za kitaifa, cheo, hadhi au dini. Mafarisayo na waandishi walitaka karama za mbinguni zibaki kuwa faida ya kitaifa na ya eneo lao tu, wakitaka kuwanyima watu wengine wa familia ya **Mungu**. Lakini Kristo alikuja kubomoa kila ukuta wa utengano. Alikuja kuonesha kuwa neema na upendo Wake havina mipaka—ni kama hewa, mwanga na mvua vinavyonyeshea dunia. **—The Ministry of Healing, uk. 25 (1905).** {*EVsw 568.4*}

Wageni Katika Nchi ya Kigeni

Katika mitaa mikuu na pembezoni mwa vijiji kuna familia na watu binafsi—labda wageni walioko nchi ya kigeni—wasio na uhusiano wowote na makanisa, na ambao katika upweke wao huhisi kana kwamba **Mungu** amewasahau. Hawaelewi wafanye nini ili waokolewe. Wengi wao wamemezwa na kuzama na dhambi. Wengine wapo katika taabu, wakikandamizwa na mateso, umasikini, kukosa imani, na kukata tamaa. Wameathirika na maradhi ya kila namna ya mwili na roho. Wanatamani kupata faraja kwa mateso yao, na Shetani anawajaribu watafute raha na starehe hizo katika tamaa na anasa zinazowaangamiza na kuwaua. Anawapa “matunda ya Sodoma,” ambayo huishia kuwa majivu midomoni mwao. Wanatumia fedha kwa kile kisicho chakula, na juhudi kazi zao kwa kisichotosheleza moyo. **—Christ’s Object Lessons, uk. 232-233 (1900).** {*EVsw 569.1*}

Madhumuni ya Mungu kwa Ajili ya Wageni wa Nchini Mwetu

Wakati mipango inaendelea kufanywa kwa ajili ya kuwafikia watu wa mataifa mbalimbali katika nchi za mbali, kazi kubwa inahitajika kufanyika kwa niaba ya wageni waliokuja kuishi kwenye nchi yetu. Nafsi zilizoko China si za thamani zaidi kuliko zile zilizo karibu na milango yetu. Watu wa **Mungu** wanapaswa kufanya kazi kwa uaminifu katika nchi za mbali, kama **Mungu** atakavyofungua njia na majaliwa Yake, lakini pia wana wajibu kwa wageni wa mataifa mbalimbali walioko mijini, vijijini na mikoa ya jirani. {*EVsw 569.2*}

Ni jambo jema kwamba viongozi sasa wanapanga kwa hekima kutangaza ujumbe wa malaika wa tatu kwa mamia ya maelfu ya wageni walioko Marekani. **Mungu** anataka watumishi wake watimize wajibu wao kikamilifu kwa mamilioni wasioambiwa lolote kuhusu onyo, walioko katika miji, hasa kwa wale waliokuja kutoka mataifa mengine. Wengi wao hawa wageni, wapo hapa kwa mipango ya **Mungu**, wapate fursa ya kusikia ukweli wa wakati huu. {*EVsw 569.3*}

Faida kubwa zingeipata kazi ya **Mungu** katika maeneo ya mbali iwapo juhudi za kweli zingefanywa kwa niaba ya wageni walioko hapa nchini. Miongoni mwa hawa wanawake na wanaume wapo wale ambao wakikubali Ukweli, wataweza kufundishwa haraka na kuwa watendakazi kwa watu wao, hapa nchini na hata katika nchi walizotoka. Wageni wengi wanaweza kurudi kwa jamaa na majirani zao kwa tumaini la kuwasaidia waongoke katika ile Kweli. Wanaweza kuwatafuta jamaa, ndugu na majirani na kuwasilisha kwao maarifa ya ujumbe wa malaika wa tatu. **—Review and Herald, October 29, 1914.** {*EVsw 570.1*}

Njia ya Kupanua Kazi kwa Mataifa Yote

Mungu angefurahi kuona kazi kubwa ikifanyika zaidi na watu Wake katika kuwasilisha Ukweli wa wakati huu kwa wageni walioko Amerika kuliko ilivyokuwa hapo awali..... kama nilivyoshuhudia hapo awali kwamba, kama tungekuwa wepesi kutambua majaliwa na mipango ya **Mungu**, tungeona katika fursa zinazozidi kuongezeka za kuwafikia wageni wengi walioko Amerika kama njia iliyowekwa na **Mungu** ya kueneza haraka ujumbe wa malaika wa tatu kwa mataifa yote duniani. Kwa majaliwa Yake ya kipekee, **Mungu** amewaelekeza watu hawa kwenye milango yetu, kana kwamba amewasukuma mikononi mwetu, ili wapate kujifunza Ukweli na kuhitimu kufanya kazi ambayo sisi hatuwezi kuifanya ya kuwapelekea watu wa lugha nyingine nuru ya Kweli. {*EVsw 570.2*}

Kuna kazi kubwa mbele yetu. Dunia inapaswa kuonywa. Ukweli unapaswa kutafsiriwa kwa lugha nyingi, ili mataifa yote yapate kufurahia ushawishi wake safi na wa uzima. Kazi hii inahitaji kutumia vipawa vyote ambavyo **Mungu** ametukabidhi—kalamu, mashine ya uchapaji, vyombo vya habari (simu, magazeti, media, runinga), pochi, sauti, mali, na mapenzi ya nafsi yaliyotakaswa. Kristo ametufanya mabalozi wa kutangaza wokovu Wake kwa wana wa wanadamu; na tukivaa haki ya Kristo na kujazwa na furaha ya Roho Wake anayeishi ndani yetu, hatutaweza kuwa na amani moyoni, tukikaa kimya. —**Review and Herald, October 29, 1914.** {*EVsw 570.3*}

Wale Walioko Kwenye Kivuli cha Milango Yetu

Ujumbe lazima ufikishwe kwa maelfu ya wageni wanaoishi katika miji hii ya ndani ya nchi... {*EVsw 571.1*}

Ni nani anahisi mzigo mzito wa kuhakikisha ujumbe unatolewa katika jiji kuu la New York na miji mingine mingi ambayo bado haijafikiwa? Sio fedha zote zinazokusanywa zinapaswa kupelekwa nje na mbali ya Marekani, huku hapa ndani ya nchi kukiwa na fursa za wazi za Bwana za kuwasilisha Ukweli kwa mamilioni ambao hawajawahi kuusikia kwenye maeneo ya nyumbani. Kati ya mamilioni haya wako wawakilishi wa mataifa mengi, wengi wao wakiwa tayari kupokea ujumbe.

Bado kuna kazi kubwa ya kufanyika chini ya kivuli cha milango yetu—katika miji ya California, New York, na majimbo mengine mengi..... {*EVsw 571.2*}

Amkeni, amkeni, ndugu zangu na dada zangu, ingieni katika mashamba ya Marekani ambayo bado hayajafanyiwa kazi. Baada ya kutoa kitu kwa ajili ya mashamba ya mataifa ya nje ya kigeni, msidhani kwamba wajibu wenu umekwisha. Kuna kazi ya kufanywa katika nchi za mbali za kigeni, lakini pia kuna kazi ya muhimu sawa ya kufanywa ndani ya Amerika. Katika miji ya Marekani kuna watu wa karibu kila lugha. Hawa wanahitaji mwangaza ambao **Mungu** ameutoa kwa kanisa Lake. **—Testimonies for the Church 8:34-36 (1904).** {*EVsw 571.3*}

Tunafurahia kwamba juhudi zilizofanywa na waanzilishi/mapayonia wa kwanza miongoni mwa mataifa ya kigeni nchini Marekani na Kanada zimezaa mavuno tele ya roho. **—Review and Herald, October 29, 1914.** {*EVsw 571.4*}

Miji Mikuu kama Kituo cha Kazi ya Nchi za Kigeni

Tulielekea kwa gari kuona utume wa Sweden ulioanzishwa hivi karibuni katika Mtaa wa Oak [Chicago]. Pale tuliangalia jengo ambalo ndugu zetu wa Sweden, wakiongozwa na Mzee -----, wamenunua hivi karibuni kama makao makuu ya kazi yao huko Chicago. Jengo linaonekana vizuri. Katika ghorofa ya chini huko ardhini, kuna mkahawa wa chakula cha mimea ulio na vifaa vyote (Vegeterian restaurant). Katika ghorofa ya kwanza kuna ukumbi mzuri wa mikutano, wenye viti vya kutosha kwa kundi la watu wapatao mia na hamsini, na ghorofa mbili za juu zimepangishwa kwa wapangaji. Nilifurahi sana kuona ushahidi huu wa maendeleo ya kazi ya Kiswidi huko Chicago. {*EVsw 572.1*}

Kuna kazi kubwa ya kufanywa kwa watu wa mataifa yote walioko miji mikubwa ya Marekani Kaskazini, na vituo vya kukusanyikia kama hivi vinaweza kuwa msaada mkubwa katika kuvuta umakini wa watu na kuwaandaa watendakazi. Katika kila jiji kubwa la Marekani kuna watu wa mataifa mbalimbali, ambao lazima wasikie ujumbe wa wakati huu. Ninatazamia kwa shauku kuona ushahidi kuwa njia za kazi ambazo Bwana ameainisha zinatiwa alama na kufuatwa kwa moyo wa kujitolea, bila ubinafsi. Kazi kama ile inayofanyika Chicago kwa ajili ya Waswidi inapaswa kufanyika katika maeneo mengi. **—Review and Herald, February 9, 1905.** {*EVsw 572.2*}

Njia za Hekima na Zenye Umakini Zinapaswa Kutumika

Kuna mtu mmoja aliyekuwa akifanya kazi kule -----, ... nasi tulimsaidia kufanya naye kazi kwa bidii, tukijitahidi kumsaidia ashike kazi, si kama mpiganaji, mwenye kubishana na kupinga, kuleta hoja, kama ilivyokuwa desturi yake, akiwakimbiza watu mbali na Ukweli badala ya kuwavuta ndani yake. Aliona kuwa sisi tunafundisha Ukweli si kwa kelele au hasira; hatukuwashushia watu shutuma kama mvua ya mawe... {*EVsw 572.3}*

Ndugu huyu... alisema alikuwa amepokea mwanga mwingi, na angefanya kazi kwa namna tofauti kabisa na hapo awali. Watu wa _____ ni watu wa kusisimka kwa haraka. Wanaweza kutumia nguvu zote ghafla, na kwa msisimko mkubwa husema, "Je, hili ni kweli? Utafanya nini basi? Utashika Sabato? Sema Ndiyo au Hapana!" Wana makali kama wembe, ... hukata masikio ya watu, ... na hapo ndipo jambo linapokwisha kuhusu kuwageuza watu hao kuwa waumini wa ile Kweli. {*EVsw 573.1}*

Sasa tunapaswa kufanya kazi na watu hawa ambao kwa kweli ni wenye akili mahiri, kama tulivyofanya na wengine mmoja baada ya mwingine katika nyakati za mwanzo za kazi ya Waadventista wa Sabato; tukiwatenga kutoka kwa mwenendo na desturi zao zisizotakaswa; tukizungumza nao juu ya Yesu, upendo Wake mkuu, unyenyekevu Wake, kujikana Kwake. Mawe haya rafu tukiyaleta inapowezekana kwenye karakana ya **Mungu** ili yakatwe na kusawazishwa, na pembe zake zote zinazoparuza ziondolewe, na yang'arishwe chini ya mkono wa Mwenyezi Mungu hadi wafanyike kuwa mawe ya thamani katika hekalu la **Mungu**, wakiwa ni mawe hai yanayotoa nuru. Kwa njia hii watakua na kufanyika sehemu ya kuta za hekalu takatifu kwa ajili ya **Mungu**. —**Letter 44, 1886. {***EVsw 573.2}*

Machapisho kwa Kila Lugha

Lengo la juhudi zetu ni kufikisha ujumbe wa onyo kwa mataifa yote... Kutoka mji hadi mji, na nchi hadi nchi, watu wanapaswa kubeba machapisho yaliyo na ahadi ya kuja kwa Mwokozi hivi karibuni. Machapisho haya yanapaswa kutafsiriwa kwa kila lugha; kwa kuwa injili ni lazima ihubiriwe kwa ulimwengu wote. **—Review and Herald, February 9, 1905. {***EVsw 573.3}*

Kuwafikia Wakatoliki

Kujihadhari na Njia Tunazotumia

Tunapoingia mahali fulani, hatupaswi kujenga vizuizi visivyo vya lazima kati yetu na madhehebu mengine, hasa Wakatoliki, kwa njia ambayo watafikiri sisi ni maadui zao wa dhahiri. Hatupaswi kuamsha chuki mioyoni mwao pasipo sababu kwa kuwashambulia moja kwa moja... Kutokana na yale ambayo **Mungu** amenionyesha, idadi kubwa ya watu wataokolewa kutoka miongoni mwa Wakatoliki. — **Manuscript 14, 1887 {***EVsw 573.4}*

Kazi ya Uangalifu

Ndugu, fanyeni kazi kwa tahadhari, msishambulie ubaguzi au chuki za watu kwa ukali kupita kiasi. Hakuna haja ya kwenda kinyume kwa makusudi ili kushambulia madhehebu mengine; jambo hilo huleta tu roho ya upinzani na kufunga masikio na mioyo ya watu wasisikie kweli. Tuna kazi yetu ya kufanya— nayo sio kubomoa bali kujenga. Tumeitwa kurekebisha ufa uliofanyika katika sheria ya **Mungu-Isaya 58**. Kazi iliyo ya heshima na bora zaidi ni ile ya kujenga, kuwasilisha Ukweli kwa nguvu na mamlaka yake, na kuuacha Ukweli ukate njia yake kupitia ubaguzi na chuki na kufunua makosa kwa kuyalinganisha na ile Kweli. {*EVsw 574.1}*

Kuna hatari kwamba wachungaji wetu watasema mambo mengi kupita kiasi dhidi ya Wakatoliki, na kwa kufanya hivyo kuamsha chuki kali kutoka kwa kanisa hilo. Wapo wengi katika imani ya Kikatoliki wanaoangalia kwa matumaini kwa watu wetu; lakini mamlaka ya makasisi juu ya waumini wake ni makubwa, na kama ataweza kuwahamasisha watu kuwa na ubaguzi kwa hoja za kuwazuia kwa kuwaambia wakae mbali, ili wasisikilize Ukweli utakaposemwa dhidi ya makanisa yaliyoanguka, hakika atafanya hivyo. Lakini sisi, kama watenda kazi pamoja na **Mungu**, sisi tumetunukiwa silaha za vita ambazo sio za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome na kuangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo 2 Wakor 10:3-5 **—Letter 39, 1887 {***EVsw 574.2}*

Kuepuka Maneno ya Kukera ambayo siyo mema

Wale wanaoandika kwa ajili ya machapisho yetu wasitoe kauli zenye ukali, yasiyo na fadhili au vidokezo vya kuudhi ambavyo hakika vitadhuru kazi yetu, na kufunga njia ya kufikia watu wa kila tabaka kama tunavyopaswa, Wakatoliki wakiwemo. Kazi yetu ni kusema Ukweli kwa upendo, bila kuchanganya na

Ukweli huo mambo yasiyo matakatifu yatokayo katika asili ya moyo wa kibinadamu, au kusema mambo yaliyo na roho ile ile waliyo nayo maadui zetu.

Mashambulizi yote makali yatatuletea madhara mara dufu wakati nguvu zitakapokuwa mikononi mwa wale wanaoweza kuitumia kutudhuru. Mara kwa mara ujumbe huu umenifikia: tusiandike neno moja, wala hata kuchapa sentensi moja ya mashambulizi ya binafsi, isipokuwa iwe ni lazima kwa ajili ya kutetea Ukweli, ambayo inaweza kuchochea chuki dhidi yetu na kuamsha hasira kali ya maadui wetu... {*EVsw 574.3}*

Ni kweli kwamba tumeamriwa "**Isaya 58:1** *Piga kelele, usiache, Paza sauti yako kama tarumbeta; Uwahubiri watu Wangu kosa lao, Na nyumba ya Yakobo dhambi zao*." Ujumbe huu lazima utolewe, na japo inapaswa tufanye hivyo, lakini tunapaswa kuwa waangalifu tusitumie ujumbe huo kuwatupia shutuma au kuwalaumu wale wasio na mwanga tulio nao. Tusiendelee kwa makusudi kutoa mashambulizi dhidi ya Wakatoliki. Miongoni mwa Wakatoliki wapo watu wengi waaminifu kwa dhamiri zao, wanaotembea katika mwanga wote waliopewa, na **Mungu** atafanya kazi kwa niaba yao. Wale waliopata fursa na nafasi nyingi, lakini wakashindwa kuboresha vipawa vyao vya kimwili, kiakili, na kimaadili kwa utukufu wa **Mungu**, bali wakaishi kwa ajili ya kujipendeza nafsi zao wenyewe na wamekataa kubeba majuku yao, wako katika hatari kubwa zaidi, na hukumu kali zaidi mbele za **Mungu**, kuliko wale walio na makosa ya mafundisho ya imani lakini ambao wanajaribu kuishi kwa kuwafanyia mema wengine. Usihukumu wengine; usiwalaumu. — **Testimonies For The Church 9:241-244 (1909).** {*EVsw 575.1}*

Kuwafungia Mlango kwa Maneno Makali Nyusoni mwao

Hubiri Ukweli, lakini zuia maneno yenye roho ya ukali; kwa kuwa maneno ya namna hiyo hayawezi kusaidia wala kuangaza yeyote. 'The Echo' ni gazeti ambalo linapaswa kusambazwa sana. Usifanye lolote litakaloharibu uuzaji na usambazaji wake. Hakuna sababu yoyote inayofanya gazeti hilo kuwa kama nuru ing'aayo mahali pa giza.

Kwa ajili ya Kristo, tafadhali zingatia maonyo yaliyotolewa kuhusu kutoa kauli kali dhidi ya Wakatoliki. Wakatoliki wengi husoma *Echo*, na miongoni mwao wapo watu (roho) waaminifu watakaolikubali ile Kweli. Lakini ipo hatari ya kuwafungia mlango usoni mwao wakati wanakaribia kuingia kwenye ile Kweli. Wekeni ushuhuda wa kuchangamsha, shukrani na faraja zaidi katika Echo. Msizuie njia yake ya kwenda ulimwenguni kote kwa kuifanya kuwa chombo cha maneno makali na magumu. Shetani hufurahia pale neno moja la uchungu linapopatikana kwenye kurasa zake. — **Counsels to Editors, uk. 45 (1896)** {*EVsw 575.2}*

Kufichua Uongo kwa Kuwasilisha Kweli

Ujumbe wa wazi uliodharimiwa unapaswa kutangazwa. Lakini kuhusu kazi hii, nimeagizwa kuwaambia watu wetu: jihadharini. Mnapotoa ujumbe huu, msifanye mashambulizi ya binafsi dhidi ya makanisa mengine, hata Kanisa Katoliki. Malaika wa **Mungu** huwaona walioko katika madhehebu mbalimbali, ambao wanaweza kufikiwa tu kwa tahadhari kubwa. Kwa hiyo, hebu tuwe waangalifu na maneno yetu. Hebu wachungaji wetu wasiongozwe na misukumo-mihemuko yao ya kibinadamu katika kulaani na kufichua "siri za uovu." Katika masuala haya, kunyamaza ni hekima. Wengi wamepotoshwa. Sema Kweli kwa sauti/toni za upendo. Mtukuzeni Yesu Kristo. Dumu katika Ukweli uliothibithishwa wazi na Biblia. Usipotoke kutoka njia aliyochora i **Mungu watu wapite,** kwa lengo la kumpiga mtu kwa maneno. Hilo linaweza kudhuru zaidi kuliko kusaidia. Linaweza kuzima msukumo wa usadikisho katika nafsi nyingi. Acha Neno la **Mungu**, ambalo ni Kweli, litoe kisa cha makosa na kutofautiana kwa maneno yao na Maandiko. {*EVsw 576.1}*

Watu hawawezi kutarajiwa kuona mara moja faida ya Kweli dhidi ya uongo waliouzoea na kuuthamini. Njia bora ya kufichua udanganyifu wa makosa ni kwa kuwasilisha ushahidi wa Kweli. Hili ndilo karipio kubwa zaidi kwa uongo. Ondoa giza linalowafunika watu kwa kuangaza nuru ya Jua la haki - Kristo. — **Manuscript 6, 1902** {*EVsw 576.2}*

Tunaweza Tukawa na Mengi ya Kusema/Kunyamaza

Kuna haja ya kujifunza kwa kina zaidi Neno la **Mungu**; hasa vitabu vya Danieli na Ufunuo vinapaswa kupewa umakini zaidi kuliko wakati mwingine wowote katika historia ya kazi yetu. Tunaweza tukaongea kidogo zaidi kuhusu nguvu mistari fulani ya utalawa wa Kirumi na Upapa, lakini tunapaswa kuelekeza umakini wa watu kwenye yale yaliyosemwa na manabii na mitume waliovuviwa na Roho wa **Mungu**. Roho Mtakatifu ameweka mambo haya kwa namna ambayo, katika kutoa unabii na matukio yanayoonyeshwa, wakala wa kibinadamu anapaswa kufichwa ili asionekane, ila awe ndani ya Kristo, na **Mungu** wa mbinguni pamoja na sheria Yake kutukuzwa. **— Counsels to Editors, uk. 45-46 (1896)** {*EVsw 577.1}*

Kweli ya Picha Huwagusa Wakatoliki

Mzee S ameweza kuamsha shauku kubwa kupitia mikutano yake. Watu wa tabaka zote wanakuja kusikiliza na kuona michoro ya picha kubwa za wanyama wa Ufunuo. Wakatoliki wengi huja kumsikiliza. Mahubiri yake mengi hutumia Maneno ya Biblia. Anatumia Maneno yake mwenyewe kwa kiasi kidogo sana kwa kadri inavyowezekana. Hivyo, wasikilizaji wakipinga yale asemayo, basi wanapinga Neno la **Mungu**. — **Letter 352, 1906 {*EVsw 577.2*}**

Hakuna anayepaswa kuhisi kwamba Wakatoliki hawawezi kufikiwa. — **Manuscript 14, 1887 {*EVsw 577.3*}**

Mavuno Makubwa Miongoni Mwa Wayahudi

Wayahudi Kuhesabiwa na Israeli wa Mungu — Katika siku zetu hizi, tunaona watu wa Mataifa wakianza kushangilia pamoja na Wayahudi. Kuna Wayahudi waliogeuzwa mioyo ambao sasa wanafanya kazi katika —— na katika miji mbalimbali kwa ajili ya watu wao. Wayahudi wanaingia katika Jeshi la wafuasi waliochaguliwa wa **Mungu**, na wanahesabiwa kuwa miongoni mwa Israeli wa **Mungu** katika siku hizi za mwisho. Hivyo basi, baadhi ya Wayahudi wataunganishwa tena na watu wa **Mungu**, na baraka za Bwana zitakuwa juu yao kwa wingi ikiwa wataingia katika hali ya furaha iliyowakilishwa katika Maandiko: "Na tena anena, Furahini Mataifa, pamoja na watu Wake." **—Manuscript 95, 1906 {*EVsw 577.4*}**

Wengi Watakuja Katika Nuru — Kuna kazi kubwa inayopaswa kufanywa ulimwenguni. Bwana ametangaza kuwa watu wa Mataifa watakusanywa, na si wao tu bali pia Wayahudi. Miongoni mwa Wayahudi wapo wengi watakaogeuka, na kupitia kwao tutaona wokovu wa **Mungu** ukienea kama taa iwakayo (watamwamini Masihi). Wayahudi wako kila mahali, na kwao nuru ya Kweli ya sasa inapaswa kufikishwa. Kuna wengi miongoni mwao ambao watapokea nuru, na watatangaza kutokubadilika kwa sheria ya **Mungu** kwa nguvu ya ajabu. Bwana **Mungu** atafanya kazi. Atatenda mambo ya ajabu kwa haki. — **Manuscript 87, 1907 {*EVsw 578.1*}**

Wayahudi Katika Mataifa Mbalimbali — Imenishangaza kuona kuwa ni wachache sana wanaojihisi kuwa na mzigo wa kufanya kazi kwa ajili ya Wayahudi waliotawanyika katika nchi nyingi. Kristo atakuwa pamoja nanyi mnapojitahidi kuimarisha uwezo wenu wa kutambua mambo ili muweze kumtazama kwa dhahiri Mwana-Kondoo wa **Mungu** aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Vipawa vya Wayahudi vilivyolala vinapaswa kuamshwa. Maandiko ya Agano la Kale, yakichanganywa na ya Agano Jipya, yatakuwa kwao kama mapambazuko ya uumbaji mpya, au kama ufufuo wa roho. Kumbukumbu zitafufuliwa wakati Kristo atakapotambuliwa katika kurasa za Agano la Kale. Nafsi kutoka kwa taifa la Wayahudi zitaokolewa, wakati milango ya Agano Jipya itakapofunguliwa kwa funguo ya Agano la Kale. Kristo atatambuliwa kuwa Mwokozi wa ulimwengu, kwa kuwa itaonekana jinsi gani Agano Jipya linavyofafanua Agano la Kale kwa wazi. Wengi wa Wayahudi kwa imani watampokea Kristo kama Mkombozi wao. — **Letter 47, 1903 {*EVsw 578.2*}**

Wayahudi Walioongoka Katika Kazi ya Mwisho — Kutakuwa na wengi kutoka kwa Wayahudi watakaoongoka, na waongofu hawa watachangia katika kuandaa njia ya Bwana, na kusawazisha katika jangwa njia kuu kwa ajili ya **Mungu** wetu. Wayahudi waliogeuka wana nafasi muhimu ya kutekeleza katika maandalizi makubwa ya siku zijazo kwa ajili ya kumpokea Kristo, Mkuu wetu. Taifa litazaliwa kwa siku moja. Jinsi gani? Kwa watu waliowekwa na **Mungu** kugeukia kweli. Itaonekana: "Kwanza jani, kisha suke, halafu ngano kamili katika suke." Unabii wa Maandiko utatimia. — **Manuscript 75, 1905 {*EVsw 579.1*}**

Uinjilisti Kwa Watoto

Watoto Wako Tayari Kusikia na Kupokea — Katika watoto walioletwa karibu Naye, Yesu aliona ndani yao, wanaume na wanawake ambao wangekuja kuwa warithi wa neema Yake na raia wa ufalme Wake, na baadhi yao wangekuwa wafia imani kwa ajili Yake. Alijua kwamba watoto hawa wangemsikiliza na kumkubali Yeye kama Mkombozi wao kwa utayari zaidi kuliko ambavyo wangekuwa watu wazima, ambao wengi wao wangelikuja kuwa wenye hekima ya kilimwengu na wenye mioyo migumu. Katika kufundisha, alishuka chini hata kuwa sawa na wao kwa hadhi. Yeye, Mkuu na enzi ya mbinguni, alijibu maswali yao na kurahisisha masomo Yake muhimu ili kukidhi ufahamu wao wa kitoto. Alipanda akilini mwao mbegu za ile Kweli, ili baada ya miaka mingi zije kuchipuka na kuzaa matunda ya uzima wa milele. **{*EVsw 579.2*}**

Yesu alipowaambia wanafunzi wasiwazuie watoto kuja Kwake, alikuwa akizungumza na wafuasi Wake katika vizazi na zama zote—kwa maofisa wa kanisa, wachungaji, wasaidizi, na WaKristo wote. Yesu anawavuta watoto Kwake, Naye atuamuru leo, “Waacheni watoto wadogo waje Kwangu, wala msiwazuie”; ni kana kwamba anamaanisha kwamba, Watakuja Kwangu tu, ikiwa ninyi hamtawazuia. **{*EVsw 580.1*}**

Usiiruhusu tabia yako isiyo kama ya Kristo imwakilishe Yesu visivyo. Usiwaweke watoto wadogo mbali Naye Bwana kwa ubaridi na ukali wako (hasira, ukatili au manyanyaso). Kamwe usiwape sababu ya kuhisi kwamba mbinguni hapatakuwa mahali pazuri kwao ikiwa wewe ungekuwa huko. Usizungumzie dini kama kitu 20 ambacho watoto hawawezi kukielewa (mambo ya kiroho), au kutenda kana kwamba wao hawatarajiwi kumkubali Kristo katika utoto wao. Usiwafanye wawaze visivyo kwamba dini ya Kristo ni dini ya huzuni, na ya kwamba katika kuja kwao kwa Mwokozi ni lazima wayaache mambo yote ambayo huyafanya maisha kuwa ya furaha. {*EVsw 580.2}*

Kadiri Roho Mtakatifu anavyogusa mioyoni mwa watoto, unga mkono kazi ya Roho kwa kushirikiana na kazi Yake. Wafundishe kwamba Mwokozi anawaita, kwamba hakuna kitu kinachoweza kumpa furaha kubwa Bwana kuliko wao kujitoa Kwake katika miaka ile wanayoongezeka kwa kimo na kupendeza (kuchanua, yaani miaka yao ya ujanani). {*EVsw 580.3}*

Mwokozi, kwa huruma nyororo isiyokuwa na kikomo, anajali sana roho ambazo amezinunua kwa damu Yake. Wao ndio madai ya upendo Wake. Huwatazama watoto kwa shauku isiyotamkika. Moyo Wake huvutiwa, si tu na wale watoto waliolelewa na kufunzwa vyema na wanaovutia bali pia na wale ambao, kwa kurithi na kwa kupuuzwa wana sifa za tabia zinazochukiza. **—The Ministry of Healing, 42-44 (1905).** {*EVsw 580.4}*

Mawazo ya Awali Yanaathiri Maisha ya Baadaye — Mafundisho yanayotolewa kwa watoto na vijana huacha mguso mkubwa moyoni unaoathiri maisha yao kuliko watu wazima wanavyotambua. Nilipokuwa mtoto, mhubiri mmoja aliyekuja katika katika nyumba yetu, Portland, Maine alisoma sura ya Matendo kuhusu kuokolewa kwa Petro, wakati malaika wa Bwana alipochukua mawindo kutoka kwa adui aliyedhamiria kumwua (Petro alipotolewa kutoka gerezani na malaika wa **Mungu)**. Sura hiyo ilisomwa kwa taratibu na kwa hisia nzito, na ilitoa mguso sana akilini mwangu kama mtoto, kiasi kwamba bado naikumbuka hadi leo. {*EVsw 580.5}*

Kutoka kwa nuru niliyopewa na **Mungu**, najua kuwa kama watu, hatujaboresha ipasavyo fursa ya kuwaelimisha na kuwafundisha vijana. Tunapaswa kuwafundisha jinsi ya kusoma na kuelewa Maandiko. Mahali popote penye taasisi ya chuo cha Biblia kwa ajili ya wachungaji na watu, tunapaswa pia kuanzisha darasa kwa ajili ya vijana. Majina yao yaandikwe kwenye usajili. Kila mtu ahisi umuhimu wa kuwafundisha vijana kuelewa Maandiko. *Acha kazi ichukuliwe katika usahili wa Ukweli wenyewe. Ongoza akili za vijana kutoka Ukweli hadi Ukweli hatua kwa hatua, juu zaidi na zaidi, ukiwaonyesha jinsi Maandiko yanavyotafsiri Maandiko, Fungu moja likiwa ufunguo wa mafungu mengine vingine.* Hivyo basi, Maandiko yenyewe yatakuwa chanzo cha nguvu ya kuelimisha, yakishika mawazo yao katika utii kwa Kristo. — **Letter 27a, 1892** {*EVsw 581.1}*

Mikutano Maalum ya Watoto Katika Uinjilisti -efoti za watoto— Malaika wa tatu anaruka katikati ya mbingu akiwa na bendera yenye maandishi: "Amri za **Mungu** na imani ya Yesu." Kila mahali ambako hema la injili linapigwa, juhudi kubwa za dhati zifanywe tangu mwanzo kuhubiri injili kwa maskini na kuponya wagonjwa. Kazi ya kuwapa vipofu wa kiroho kuona imeongeza roho nyingi katika idadi yetu, wale ambao wataokolewa. {*EVsw 581.2}*

Mikutano ya watoto isifanywe tu kwa ajili ya elimu na kuwatumbuiza watoto kwa burudani, bali ili waongoke. Na jambo hili litatokea. Tukimwamini **Mungu** kwa kweli, ndipo tutaweza kuwaelekeza kwa Mwana-Kondoo wa **Mungu** aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Wote wanaohudhuria mikutano yetu mikubwa wanapaswa kufanyiwa kazi—watu wa juu na wa chini, matajiri na maskini, wanapaswa kufikiwa na aina hii ya kazi. — **Manuscript 6, 1900** {*EVsw 582.1}*

Upendo Humvuta Mtoto Kwa Kristo — Kwa namna unavyoshughulika na watoto, unaweza kwa neema ya Kristo kuunda tabia zao kwa ajili ya uzima wa milele, au kwa mwenendo usiofaa ukawapa mfano wa tabia ya kishetani. Unapoongoza usitende kwa msukumo au jazba. Acha mamlaka na upendo viambatane. Kuza, palilia na stawisha yote yaliyo mema na ya kupendeza, na waelekeze wapende yaliyo ya juu kwa kumdhihirisha Kristo kwao. Unapowanyima vitu vinavyowaumiza, waonyeshe kwamba pia kuwa unawapenda na unataka kuwawezesha kuwa na furaha. Kadri wanavyokuwa wakorofi na wasiopendeza, ndivyo unavyopaswa kujitahidi zaidi kuwaonyesha upendo wako kwao. Mtoto anapoamini kwamba unataka kumfanya yeye awe na furaha, upendo utavunja kila kizuizi. Hii ndiyo kanuni ya Mkombozi kwa wanadamu; na ni lazima kanuni hiyo iletwe kanisani. — **Letter 23a, 1893** {*EVsw 582.2}*

Jitihada Zilizopangiliwa Vizuri kwa Ajili ya Watoto — Shauku hapa Australia katika mkutano wetu wa kambi ulikuwa na mvuto wa kipekee zaidi kuliko tulivyowahi kuona popote Marekani au katika nchi nyingine. Pale baada tu ya zile sikukuu-Krismas na mwaka mpya, katikati ya burudani nyingi za kuvutia, tulikuwa na watu wapatao 1200 hemani siku za kazi, yaani Jtatu mpaka Ijumaa—watu dhati na wenye akili mahiri. Watoto wengi kutoka kwa wasio wa imani yetu walihudhuria. Jumapili iliyopita pekee, walikuwepo watoto wapatao 400 kwenye mkutano wa watoto. Mikutano hiyo iliongozwa na dada _____, ambaye aliwapanga watoto katika madarasa yenye walimu walioteuliwa, aliowafundisha na kuwasaidia katika kazi hiyo. Mbinu za ufundishaji wa chekechea zilifuatwa kwa kadri iwezekanavyo... {*EVsw 582.3}*

Fedha zilizotumika kwa magari ya injili (Gospel Wagons) zingefaa zaidi kama zingewekezwa katika kazi ya kudumu. Ingawa magari ya injili yatafanya mema kiasi, ila niliona kuwa kutakuwa na kukatishwa tamaa kwa matokeo ya mwisho. Kwa kulinganisha upande mwingine, nilionyeshwa kazi tofauti—hema zilikuwa zikihamishwa sehemu mbalimbali katika nyakati za misimu mbalimbali ya mwaka. Mikutano ya kambi ilikuwa ikifanyika katika maeneo mengi, ikiongozwa na watu wa **Mungu** wenye uwezo, wacha Mungu na wasaidizi wanaofaa. Mikutano ya watoto iliendelea, pia mikutano ya uamsho ili kuwavuta watu kuchukua msimamo kwa ajili ya ile Kweli... {*EVsw 583.1}*

Katika mkutano huu wa kambi, kazi iliyopaswa kufanyika imefanyika. Mikutano ya watoto, yaani shule ya Biblia ya chekechea, imefanya kazi nzuri. Masomo yaliyotolewa yamerudiwa na watoto nyumbani, na akina mama walionesha shauku kwa kuwaandaa watoto wao vizuri kwa shule. Wengi ni watoto wa wazazi wasio wa imani yetu. Mbegu za Kweli za Biblia zimeota katika ardhi ya mioyo yao. Sio zoezi rahisi, lakini inaleta matunda mema. Athar za mguso wa moyo, zimeonekana mioyoni mwa watoto na wazazi. Wema wa mikutano hii utafichuliwa katika siku kuu ya **Mungu**. Hili ni shamba kubwa la kulimwa. Acha kazi hii iendelee mbele. Talanta zitatumika wapi vyema zaidi? Watenda kazi hawa wanapanda kwa ajili ya mavuno..... Wanaume, wanawake na watoto wana hamu ya kujua wafanye nini ili warithi uzima wa milele. **— Letter 2, 1899 {*EVsw 583.2}***

Masomo ya Asili — Mikutano ya watoto ilifanyika mara mbili kwa siku. Baada ya somo la asubuhi, katika siku nzuri, walimu na watoto walitembea umbali mrefu, na wakati wa kutembea, kwenye kingo za mto au katika nyasi za uwanja, walifanya mapumziko mafupi na kufundishwa somo kutoka katika uumbaji-maumbile. Ilionekana kwamba katika siku ambazo watoto walitembea kwenye majani, walikuwa watulivu na wenye nidhamu katika kambi. Mahudhurio ya watoto kwenye kambi yalikuwa 30 asubuh, wakati watoto wanaoishi kambini tu ndiyo walikuwepo. Alasiri, watoto kutoka shule za jirani walihudhuria, na kufika idadi ya 50-60. — **Manuscript 27, 1895 {*EVsw 584.1}***

Kuwafikia Wazazi Kupitia Watoto — Mikutano yetu ya kambi ni mojawapo ya njia muhimu sana katika kazi yetu. Katika kila mkutano wa kambi, kazi maalum ifanywe kwa ajili ya watoto. Watendakazi wanaofaa wafundishe daima watoto. Ombeni baraka ya Bwana juu ya mbegu inayopandwa, na ushawishi wa Roho wa **Mungu** utawagusa hata watoto wadogo. Kupitia watoto, wazazi wengi watafikiwa. — **Manuscript 52, 1900 {*EVsw 584.2}***

Wale Walio Katika Vituo vya Utalii

Kwanini Yesu Alichagua Kapernaumu

Wakati wa huduma Yake hapa duniani, Mwokozi alitumia fursa zilizopatikana kando ya njia kuu za usafiri mwingi. Kapernaumu ndiko Yesu alikokaa mara kwa mara katika safari Zake za huku na kule, na mji huu ukajulikana kuwa “mji Wake mwenyewe.” Mahali hapa palikuwa panafaa sana kuwa kitovu cha kazi ya Mwokozi. Kwa kuwa palikuwa kwenye njia kuu kutoka Dameski hadi Yerusalemu na Misri, na pia kuelekea Bahari ya Mediterania, palikuwa mahali pa mzunguko mkubwa wa wasafiri. Watu kutoka mataifa mbalimbali walikuwa wakipita hapa au kupumzika katika safari zao wakienda na kurudi. Hapa Yesu aliweza kukutana na mataifa yote na tabaka zote—matajiri, wakuu na watu wa heshima, pamoja na maskini na wanyenyekevu; na mafundisho Yake yangesambazwa hadi katika nchi nyingine na katika familia nyingi. Hili lingeamsha uchunguzi wa unabii; watu wangeelekeza fikra zao kwa Mwokozi, na ujumbe Wake ungetangazwa kwa ulimwengu. **—Testimonies For The Church 9:121 (1909). {*EVsw 584.3}***

Kuwavutia Umati

Katika vituo maarufu vya afya na maeneo yenye trafiki za vituo vinavyovutia watalii ambayo huwajaa maelfu ya watu wanaotafuta afya na starehe, wachungaji na wauzaji vitabu wenye uwezo wa kupata umakini wa kadamnasi za watu wanapaswa kuwekwa ili kuwafikia watu hawa. Watendakazi hawa

wangalie uwezekano wa kuwasilisha ujumbe wa wakati huu, na wafanye mikutano kadri wanavyopata nafasi. Wajitahidi kuwa wepesi katika kutumia kila nafasi kuongea na watu. Wakiwa wameandamana na nguvu ya Roho Mtakatifu, na wawafikie watu kwa ujumbe alioubeba Yohana Mbatizaji: "*Tubuni, kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia.*" **(Mathayo 3:2).** Neno la **Mungu** liwasilishwe kwa uwazi na kwa nguvu, ili wale wenye masikio ya kusikia wasikie Kweli. Kwa njia hii, injili ya Kweli ya wakati huu itawekwa njiani mwa wale wasioijua, na wengi wataikubali na kuibeba hadi katika makazi yao katika maeneo mbalimbali duniani. **—Testimonies For The Church 9:122 (1909). {*EVsw 585.1*}**

Mikutano ya Hema katika Vituo vya Watalii na mapumziko (resorts)

Mikutano ya hema ni lazima ifanyike katika vituo vikubwa vya utalii, kadri ambavyo Konferensi ya _____ itaweza kufanya kazi hiyo kwa kutumia watenda kazi walio nao. Kama kuna wakat ikulikuwa na haja ya kuamka na kutambua umuhimu wa kufanya kazi katika maeneo haya, basi ni sasa. **—Letter 138, 1902. {*EVsw 585.2*}**

Mahali Watu Hupita-Wakienda na Kurudi

Kazi maalum ni lazima ifanyike mahali ambapo watu huja na kuondoka daima. Kristo alifanya kazi nyingi huko Kapernaumu kwa sababu palikuwa mahali pa wasafiri wengi kupita na kukaa kwa muda. **—Review and Herald, July 12, 1906. {*EVsw 585.3*}**

Watenda Kazi kwa Ajili ya Vituo vya Watalii

Ni vigumu kupata vijana wa kiume na wa kike waliobobea wanaoweza kuingia mijini na kufanya huduma yenye matokeo yenye ufanisi. Katika vituo vya utalii, ambako watu wengi huja kwa ajili ya afya na starehe, tunahitaji sana vijana walio imara katika Kweli ya ujumbe wa malaika wa tatu, ili wazunguke miongoni mwa watu, na kuwahudumia, wakisema Neno la wakati kwa huyu, na kutoa faraja kwa yule mwingine. —**Review and Herald, July 12, 1906. {*EVsw 586.1*}**

Mikutano ya Mitaani

Kuwafikia Wengine Kupitia Mikutano ya Hadharani-nje ya jengo

Miji inahitaji kazi zaidi. Kuna maeneo ambapo watu wanaweza kufikiwa vyema kupitia mikutano ya nje ya majengo. Wapo wengi wanaoweza kufanya aina hii ya kazi, lakini ni lazima wavae silaha zote za haki. Tumekuwa waoga mno katika kazi yetu (delicate kama mayai); lakini bado vinahitajika viwango, maadili na na akili zenye busara. **—An Appeal for Missions, 15, (1898). {*EVsw 586.2*}**

Changamoto za Umati Unaosogea

Mikutano hii ya nje ya jengo yaweza kufanyika mara kwa mara, na wakati mwingine ni njia bora ya kuwafikia watu kwa mikutano ya wazi; lakini kuifanya hii mikutano kuwa mtindo wa kawaida wa kazi hakutazaa matokeo yanayotarajiwa kwa sasa. Mtendakazi hawezi kuthibitisha kikamilifu huduma yake. Hotuba ya bahati au ujumbe wa ghafla unaweza kuchochea fikra ambazo, kwa msaada wa mvuto mingine, huweza kuzaa usadikisho na toba; lakini visa kama hivi ni vichache sana. **—Gospel Workers, 339, 340 (1892). {*EVsw 586.3*}**

Katika mikutano ya nje haiwezekani kukamilisha kazi ya kufunga miganda kwa kuwasilisha watu wahesabiwe wakamilifu katika Kristo Yesu. Wakati mwingine matokeo makubwa huweza kupatikana kwa njia hii ya kazi. Lakini kama kawaida, ni bora zaidi kuwafikia watu kwa njia nyingine. **—Letter 2, 1885. {*EVsw 587.1*}**

Kumwasilisha Kristo katika familia, kando ya jiko la moto sebuleni, na katika mikusanyiko midogo ndani ya nyumba za watu binafsi, mara nyingi huzaa matunda zaidi ya mahubiri ya hadharani, nje ya jengo, au hata kuliko yale yanayotolewa katika kumbi au makanisa. **—Gospel Workers, 193 (1915). {*EVsw 587.2*}**

Mikutano ya Hadharani Kuhusu Kiasi

Lazima tufanye kazi katika pembe za giza za dunia hii.... Nimesimama mara nyingi katika hewa ya wazi kuzungumza na makundi ya watu waliokusanyika kunisikiliza. Nimewaona wanawake wakiwa na watoto mikononi mwao wakisimama kwa saa nzima wakinisikiliza. Kulikuwa na wanaume na wanawake wakinizunguka. Nimewauliza, "Ni wangapi kati yenu mna imani ya uelewa ndani ya Yesu Kristo? Ni wangapi

ni WaKristo? Wale mlio Wakristo, inueni mikono yenu." Hakuna hata mmoja aliyeinua mkono. Je, hawakumhitaji Kristo? Je, hawakuhitaji kujua Maarifa ya Kweli? Je, hawakuhitaji kujifunza kiasi? Bila shaka walihitaji (pengine waliogopa kunyosha mikono mbele za watu, kwenye mkutano wa hadhara). {*EVsw 587.3*}

Mungu anatamani tuwe mahali ambapo tunaweza kuwaonya watu. Yeye Anatamani tuingie kwenye suala la kiasi. Kwa tabia zenye makosa katika kula na kunywa, watu wanajiharibia uwezo wao wa kufikiri na kuelewa-akili mahiri. Hatuhitaji kuchukua shoka na kuvunja baa au vilabu vyao vya pombe. Tuna silaha iliyo bora zaidi—Neno la **Mungu** aliye hai. Hili litapenya kupitia kivuli cha kishetani ambacho Shetani anajaribu kuweka juu ya njia yao. **Mungu** ni Mwenye uwezo na nguvu. Ataongea na mioyo yao. Tumeona Yeye akifanya hivyo. Tumeona roho zikiletwa kwenye ile Kweli. **—General Conference Bulletin, Aprili 23, 1901.** {*EVsw 587.4*}

SEHEMU YA 18—KUKABILIANA NA SAYANSI YA UONGO, USHIRIKINA, ITIKADI POTOVU, NA JUMUIYA ZA SIRI

(Kupe-Parasite)

(Fake science, cults, isms, and secret societies)

Shetani Anapata Nafasi Kupitia Mafundisho ya Uongo

Uongo Unapata Uhai Kutoka kwa Kweli—Shetani ametenda kazi kwa nguvu za udanganyifu, akiingiza wingi wa makosa yanayoficha ile Kweli. Uongo au makosa haviwezi kusimama peke yake, na ungepotea au kufa haraka kama usingejifunga kama bakteria/kupe juu ya mti wa Kweli. Uongo hupata uhai kutoka kwa Kweli ya **Mungu**. Mapokeo ya wanadamu, kama vijidudu vinavyoambukiza magonjwa vinavyoelea hewani (germs), hujishikiza kwenye Kweli ya **Mungu**, na wanadamu huyachukulia kama sehemu ya ile Kweli. Kupitia Mafundisho ya imani ya uongo (false doctrines), Shetani hupata nafasi ya kupenyeza mguu wake na kuziteka akili za watu, akiwaongoza kushikilia nadharia zisizo na msingi wowote wa ile Kweli/Biblia. Watu kwa ujasiri hufundisha mapokeo ya wanadamu kama ndiyo Mafundisho ya Mungu; na kadri mapokeo haya yanavyorithiwa zama hadi zama, hupata nguvu juu ya akili za watu. Lakini umri au miaka mingi haigeuzi kosa kuwa Kweli, wala uzito wake wa mzigo wa miaka mingi hauufanyi mche wa ile Kweli kuwa kupe. Mti wa Kweli huzaa matunda Yake halisi, yakionyesha asili na tabia yake ya Kweli. Vivyo hivyo, kupe wa uongo huzaa matunda yake, na huonyesha wazi kuwa tabia yake ni tofauti na mche/mmea wa asili ya mbinguni (**Cult**-ni Ibada ya kundi dogo lenye imani kali na zisizo za kawaida, mara nyingi hujikita katika kiongozi mwenye haiba kali na misukumo isiyo na msingi wa Biblia au maadili ya mwanadamu wa kawaida. Kiongozi hudai kujitolea sana na wakati mwingine hutumia udanganyifu, tofauti na dini kuu na tamaduni maarufu zinazoendeshwa na wafuasi waaminifu kwa mambo ya kawaida ya ibada. Kwa ufupi, ni kundi lenye mawazo yasiyo ya kawaida, kiongozi anadhibiti watu kupita kiasi na kuwa mungu wa kikundi, na wafuasi wake hawana mashaka na, hufuata kila kitu asemacho, hivyo wanaweza kuburuzwa tu na kumtumikia kiongozi kwa kila anachosema hata akiwaambia wanywe sumu au wajiue, mara nyingi hutengwa na jamii na wao wenyewe hupenda kujitenga kwa vile wako kinyume na serikali na jamii, mfano mzuri ni wa Mackenzie mkikuyu wa Shakahola aliyewaambia watu wasile kabisa au kunywa kwa siku 40, na watu zaidi ya 70 walikufa mwaka 2023 au Jim Jones wa Marekani aliyewaambia watu wanywe sumu na alikoroga hii sumu na kuua watu 900. Kwa kawaida watu wapweke, wasio na marafiki, au wasiojua kupata ushauri wa hekima hujiunga na kundi la cult, mpaka wanakuwa wameenda mbali sana na uhusiano kwenye kambi hiyo ya cult na wanashindwa kurudi nyuma kwa vile wanapewa tishio la kuuawa au familia zao kuchukuliwa nk). {*EVsw 589.1*}

Ni kupitia nadharia na mapokeo ya uongo ambapo Shetani hupata mamlaka ya kuziteka akili za wanadamu. Tunaweza kuona jinsi anavyotawala kwa kuangalia hali ya kutokuwa watu waaminifu duniani. Hata makanisa yanayodai kuwa ya Kikristo yamegeuka kutoka kwa sheria ya Yehova na kuweka viwango vya uongo. Shetani ameweka mkono wake katika yote haya; kwa kuwaelekeza watu kwenye viwango vya uongo, huharibu tabia ya mwanadamu, na huwafanya wamkiri yeye ndiye wa juu kupita nafsi yoyote. Anatenda kinyume na sheria takatifu ya **Mungu** na anakana mamlaka ya **Mungu**. Ni katika kiti chake cha enzi ndipo kazi zote za uovu hupata mwanzo na msaada wake (sapoti yake). **—The Review and Herald, October 22, 1895.** {*EVsw 589.2*}

Njia Tofauti za Ukweli na Uongo/makosa—Malaika wa Shetani wana hekima ya kutenda maovu, na wataunda kile ambacho baadhi ya watu watakidai kuwa ni nuru ya juu, na watakitangaza kuwa ni mpya na ya ajabu; lakini ingawa ujumbe huo unaweza kuwa na sehemu fulani ya ile Kweli, utakuwa umechanganywa na ubunifu wa kibinadamu, na kufundisha mapokeo ya wanadamu kama Mafundisho ya imani ya Biblia. Ikiwa

kuna wakati wowote ambapo tunapaswa kuomba na kukesha kwa bidii, ni sasa. Mambo mengi yanayoonekana kuwa mazuri yatahitaji kuchunguzwa kwa maombi mazito, kwa kuwa ni mbinu za hila za adui ili kuzipotosha roho kwa njia ambayo imekaribiana sana na ile ya Kweli kiasi kwamba haitaweza kutofautishwa kirahisi. Lakini jicho la imani linaweza kutambua pale njia inapopotoka, japo kwa udogo na hila, kutoka kwenye njia sahihi. Mwanzoni inaweza kuonekana kuwa sahihi kabisa, lakini baadaye inaonekana kugeuka kabisa kutoka kwenye njia ya utakatifu na ya kuelekea mbinguni. Ndugu zangu, nawaonya kutengeneza njia zilizonyoka kwenye miguu yenu, ili wale wasio na nguvu kama viwete wasipotee. **—Manuscript 111. {*EVsw 590.1*}**

Uzushi Unaowasilishwa Kama Mafundisho ya Biblia—Wakati umefika ambapo hatuwezi kutegemea Mafundisho ya imani tunayosikia isipokuwa tuone kama yanapatana na Neno la **Mungu**. Kuna uzushi wa hatari utakaowasilishwa kama mafundisho ya Biblia; nasi tunapaswa kuifahamu Biblia vyema ili tuweze kukabiliana nao. Imani ya kila mtu itajaribiwa, na kila mmoja atatahiniwa na kupitia jaribu la uchunguzi na ukosoaji wa karibu. **—The Review and Herald, May 3, 1887. {*EVsw 590.2*}**

Shetani Hupotosha Maandiko kwa Kunukuu Isivyo—Wote wanapaswa kuwa na uelewa wa Neno la **Mungu**; kwa sababu Shetani hupotosha na kunukuu Maandiko vibaya, na watu hufuata mfano wake kwa kuwasilisha sehemu ya Neno la **Mungu** kwa wale wanaotaka kuwapotosha kwenye njia za uongo, huku wakificha sehemu ambayo ingewaharibia mpango wao. Kila mtu ana haki ya kufahamu wazi “Hivi Ndivyo Asemavyo Bwana” .... **{*EVsw 591.1*}**

Kuna wachungaji wa uongo watakaosema na kufanya mambo ya kupotosha. Watoto wanapaswa kufundishwa ili wajue Neno la **Mungu**, na waweze kutambua pale Maandiko yanaposomwa kwamba ni nusu ipi imeachwa na nusu ipi imesomwa, kwa lengo la kuleta dhana potofu, yaani uongo. **—Manuscript 153, 1899. {*EVsw 591.2*}**

Upotoshaji Unaotokana na Viongozi wa Kidini—Wakiwa na Biblia wazi mbele yao, na wakidai kuheshimu mafundisho yake, viongozi wengi wa kidini wa wakati huu wanaharibu imani ya watu katika Biblia kama Neno la **Mungu**. Wamejishughulisha na kulikatakata Neno la Mungu na kuweka maoni yao juu ya kauli zilizo wazi kabisa za Biblia. Mikononi mwao, Neno la **Mungu** linapoteza nguvu yake ya kubadilisha maisha. Hii ndiyo sababu ya kuenea kwa ukafiri na uovu kuendelea kusheheni. **{*EVsw 591.3*}**

Wakati Shetani anapohafifisha imani ya watu katika Biblia, huwaelekeza watu kwenye vyanzo vingine vya nuru na nguvu. Hivyo hujipenyeza mwenyewe na kudokeza ajenda zake. Wale wanaoachana na Mafundisho wazi ya Maandiko na nguvu ya Roho Mtakatifu wanakaribisha udhibiti wa mapepo. Ukosoaji, dhana na ubashiri kuhusu Maandiko umefungua mlango kwa Ushetani na Itikadi za Kifalsafa za Umizimu na Theosofi—mifumo ya kisasa ya ushirikina wa kale—ili kupata nafasi hata ndani ya makanisa yanayodai kwamba ni ya Bwana wetu Yesu Kristo (*Soma Harakati iliyoanzishwa mwaka 1875 kama Jumuiya ya Theosophiki na Helena Blavatsky na Henry Steel Olcott (1832–1907, Umizimu ni mawasiliano na watu waliokufa kupitia wachawi nk). **{*EVsw 591.4*}**

Pamoja na kuhubiri injili, kuna mawakala yanayofanya kazi kama vyombo vya pepo wa uongo. Watu wengi hujaribu kushugulika na hizi roho kwa udadisi tu, lakini wanapoona ushahidi wa nguvu isiyo ya kibinadamu, wanakuwa wameshavutwa zaidi hadi wanakuwa chini ya udhibiti wa mapenzi yaliyo na nguvu kuliko yao. Hawawezi kujinasua kutoka kwenye nguvu hizo za ajabu za mapepo. **{*EVsw 592.1*}**

Ngome za roho zao huvunjwa. Hawana kinga dhidi ya dhambi. Mara baada ya vizuizi vya Ukweli wa Neno la **Mungu** na Roho Wake kukataliwa, hakuna mwanadamu ajuaye ni kina kipi cha uovu na uharibifu ambacho mwanadamu anaweza kushuka. Dhambi za siri au tamaa kuu za mwili na mapepo huweza kumtawala na kumfunga kama yule mtu aliyekuwa amepagawa kule Kapernaumu. Hata hivyo hali yake haijakosa tumaini kabisa (japo mtu anaweza kuwa amejipeleka, na akadidimia kwa mapepo huko, bado Bwana anaweza kumsaidia atoke kwa mtawala mkatili). —**The Desire of Ages, uk. 258 (1898). {*EVsw 592.2*}**

Uongo na Makosa, Madanganyo na Ushetani Katika Huduma Iliyopotoka, Ushupavu—**Mungu** anawaita watu Wake kuwa WaKristo kwa mawazo, kwa maneno, na kwa matendo. Luther alisema kuwa dini huwa hatarini zaidi inapokuwa mikononi mwa wachungaji, makasisi na wahudumu-Viongozi wa makanisa ya Kikristo (reverend men). Naweza kusema kuwa wengi wanaoshughulika na Ile Kweli hawajatakaswa kwa hiyo Kweli. Hawana ile imani ifanyayo kazi kwa upendo na kuitakasa roho. Wamezoea kushugulika na mambo matakatifu, na kwa sababu hiyo, wengi hushika Neno la **Mungu** kwa kutojali, na bila kicho (wamemzoea Mungu). Hawakutembea katika nuru bali wamefunga macho yao kwa nuru. **{*EVsw 592.3*}**

Hizi ni zama za kukataliwa kwa neema ya **Mungu** aliyoikusudia kuwapa watu Wake, ili katika hatari za siku za mwisho watu wasishindwe na uovu unaotawala na kuungana na ukatili na chuki ya dunia dhidi ya watu wa **Mungu** waliosalia. Chini ya joho la UKristo na utakatifu, uovu wa wazi na kutomcha Mungu kutatawala kwa kiwango kikubwa na kuendelea hadi Kristo atakapokuja kutukuzwa kwa wote wanaoamini. Hata katika nyua za hekalu, matukio yatafanyika ambayo watu wachache watayagundua. Watu wa **Mungu** watajaribiwa na kupimwa, ili Yeye apate kutambua "kati ya yule amtumikaye **Mungu** na yule asiyemtumikia." **—Manuscript 15, 1886. {*EVsw 592.4*}**

Migogoro Kati ya Sayansi ya Uongo na Dini—Nimeonywa kwamba kuanzia sasa tutakuwa katika mapambano ya kudumu. Sayansi, kama iitwayo hivyo, na dini zitawekwa kinyume ya kila kimojawapo, sababu wanadamu wenye upeo finyu hawawezi kufahamu uwezo na ukuu wa **Mungu**. Maneno haya ya Maandiko Matakatifu yaliwasilishwa kwangu: "Miongoni mwenu wenyewe watatokea watu watakaosema mambo ya kupotosha ili kuwavuta wanafunzi wawafuate." Hili litadhihirika hakika miongoni mwa watu wa **Mungu**, na kutakuwa na wale ambao hawawezi kutambua zile Kweli ya ajabu na muhimu kwa wakati huu, Kweli ambazo ni za muhimu kwa ulinzi, usalama na wokovu wao wenyewe, wakati mambo yasiyo na maana yatakuzwa na nguvu ya Shetani hadi kuonekana ya umuhimu mkubwa kupita kitu kingine chochote. {*EVsw 593.1*}

Uoni wa kimaadili wa watu hawa una ugonjwa; hawajihisi kuhitaji upako wa mbinguni wa Roho Mtakatifu ili waweze kutambua mambo ya kiroho. Wanafikiri kuwa ni werevu mno kufanya kosa. Watu wasio na uzoefu wa kila siku katika mambo ya **Mungu** hawatafanya maamuzi yenye busara wanapopewa majukumu matakatifu; ndipo watakosea kutofautisha nuru, na giza na kusema kuwa ni giza ni nuru, na kuwa nuru ni giza, wakichanganya mapepo/udanganyifu na Ukweli, wakiona mapepo/udanganyifu kuwa ufunuo, na ufunuo wa Kweli kuwa ndoto, wakisema dunia ni atomi, na atomi ndiyo dunia. Watangukia katika uongo na udanganyifu wa Shetani uliofichwa kama mitego ya kuvizia na kufungwafungwa miguu ya wale wanaojiona kuwa wanaweza kutembea katika hekima yao ya kibinadamu bila neema maalum ya Kristo. Yesu anataka mwanadamu aone, si watu kama miti inayotembea, bali aone vitu vyote kwa wazi. Ipo tiba moja pekee kwa nafsi yenye dhambi ni ile ya mbinguni, na isipokubaliwa, wanadamu watakubali udanganyifu mmoja baada ya mwingine mpaka fahamu zao zipotoshwe. **—Manuscript 16, 1890. {*EVsw 593.2*}**

Miujiza Siyo Kipimo cha Ukweli

Shetani Atafanya Miujiza—Wengi wanaokataa ujumbe ambao Bwana anawatumia wanatafuta vigingi vya kuweka mashaka yao, wakitafuta visingizio vya kukataa nuru ya mbinguni. Mbele ya ushahidi wa wazi wanasema kama Wayahudi, "Tuonyeshe muujiza nasi tutaamini. Kama hawa wajumbe wana ile Kweli, kwa nini basi hawaponyi wagonjwa?" ... {*EVsw 594.1*}

Laiti macho yao yangefunguliwa, wangeona malaika waovu wakishangilia karibu nao na wakifurahia uwezo wao wa kuwadanganya. Siku iko karibu ambapo Shetani atajibu ombi la watu hawa wenye mashaka kwa kuleta miujiza mingi ili kuthibitisha imani ya wale wote wanaotafuta ushahidi wa aina hiyo kwa kuwaleta miujiza. Jinsi hali itakavyokuwa mbaya kwa wale wanaofumba macho yao kwa nuru wa Kweli na kutaka miujiza kuwathibitishia uongo! **—Letter 4, 1889. {*EVsw 594.2*}**

Uponyaji wa Miujiza na Ushupavu—Vituo vyetu vya afya vya sanitarium vimekusudiwa kuwafikia kundi la watu ambao njia nyingine haziwezi kuwafikia. "Mbona au kwanini," wengine huuliza, " kwanini maombi hayatumiki kwa ajili ya uponyaji wa miujiza kwa wagonjwa badala ya kujenga sanitariamu nyingi?" Kama hilo lingefanyika, ushetani mkubwa ungejitokeza miongoni mwetu. Wale wenye kujiamini kupita kiasi wangejitokeza kama wale wa _____ waliokuwa na mengi ya kusema kuhusu mwili mtakatifu. Hawa walipelekwa mbali na udanganyifu wa kiroho. Katika Mkutano Mkuu wa 1901 walikemewa kwa ujumbe niliopewa na Bwana kwa ajili yao. Kama tungefuata mipango ambayo wengine wangependa tufuate, makundi yangetokea yakileta maonyesho ya kiroho yatakayochanganya imani ya wengi.... {*EVsw 594.3*}

Makosa yataingia, na mafundisho ya ajabu na mageni yataenezwa. Baadhi watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo na mafundisho ya mashetani. Tangu kuanzishwa kwa sanitariamu ya kwanza, mambo haya yalianza kujitokeza. Yalikuwa kama yale yaliyotokea baada ya kukatishwa tamaa kwa watu, kwa Yesu kutokurudi mwaka wa 1844 kushindwa. Kulionekana wimbi kubwa la ushetani likidai kuwa ni ushuhuda wa Roho Mtakatifu. Nilipewa ujumbe wa kukemea kazi hii ovu. **—Letter 79, 1905. {*EVsw 595.1*}**

Utakaso wa Uongo na Utakatifu wa Bandia

Jihadharini na Mafundisho wewe"Amini Tu"—

Tutakutana na mafundisho ya uongo ya kila aina, na isipokuwa tuwe na ufahamu wa yale Kristo aliyoyasema na kufuata maagizo Yake, tutaangushwa na kupotoshwa. Miongoni mwa mafundisho haya hatari sana ni ule wa utakaso wa uongo. Wapo wale wanaodai kuwa watakatifu, lakini wanavunja amri za **Mungu**. Dai lao ni kwamba hawatendi dhambi si la kweli, na halipaswi kukubaliwa. {*EVsw 595.2*}

Pia kuna mafundisho mengine yatakayoletwa yakisema kwamba, "Jambo la kufanya ni kuamini tu kwa Kristo—kuamini kuwa ametusamehe dhambi zetu, na kwamba baada ya kusamehewa, haiwezekani tena sisi kutenda dhambi." Hili ni mtego wa Shetani. Ni kweli tunapaswa kumwamini Kristo; Yeye Ndiye tumaini letu pekee la wokovu. Lakini pia ni Kweli kwamba tunapaswa kuitenda kazi ya wokovu wetu binafsi kwa hofu na kutetemeka kila siku kwa imani, si kwa majivuno, bali kwa hofu na kutetemeka. Tunapaswa kutumia kila uwezo tulio nao katika huduma kwa **Mungu**, na baada ya kufanya yote tuwezayo, bado tunapaswa kujiona kuwa watumishi wasiofaa.

Nguvu ya Kiungu itaungana na jitihada zetu, na tunaposhikamana na **Mungu** kwa mkono wa imani, Kristo atatupatia hekima na haki Yake. Hivyo basi, kwa neema Yake, tutawezeshwa kujenga juu ya msingi ulio thabiti. —**Manuscript 27, 1886.** {*EVsw 595.3*}

Kukiri Utakatifu kwa Maneno matupu tu

Wale wanaotaka kumfuata Kristo lazima wasimikwe katika msingi wa kanuni za Kweli. Wa msimamo wa uongo wa yafahamu kwa undani mafundisho ya Biblia kuhusu imani na utakaso kupitia ile Kweli. Wanapaswa kuwa thabiti na kusimikwa katika haya maarifa kiasi cha kutoyumbishwa na fundisho la utakatifu, bali maisha yao yaweze kuonyesha utendaji hai wa matokeo ya kweli ya kanuni hii ya mbinguni kwa vitendo. Watu wa **Mungu** lazima wawe na uwezo wa kutofautisha kati ya halisi na bandia. {*EVsw 596.1*}

Kuna wale wanaodai kuwa watakatifu, wakisema kuwa wao ni wa Bwana kikamilifu, na wanadai kuwa na haki ya kudai ahadi za **Mungu**, ilhali hawatii amri Zake. {*EVsw 596.2*}

Ni Kweli kwamba kuna wengi ambao hawajawahi kupata nuru ya Kweli ya sasa, ambao kwa neema ya Kristo waliyopewa, wanatii sheria kulingana na wanavyoielewa. Wale wanaoishi kwa Nuru ndogo waliyopokea sio miongoni mwa wale ambao mtume Yohana aliwalaani. Maneno yake yanawahusu wale wanaojivunia kuamini katika Yesu, wanaodai kuwa watakatifu, lakini wanapuuza masharti ya sheria ya **Mungu**. Wakiwa wanazungumzia upendo wa Yesu, upendo wao si wa kina kiasi cha kuwaleta kwenye utii. Matunda ya maisha yao yanaonyesha asili ya mti, na kuthibitisha kuwa imani yao si ya kweli. Hata hivyo, kundi hili, licha ya kutostahili chochote, wanadai baraka zote za **Mungu** kwa ujasiri. Japo hawatoi chochote, lakini wanadai kila kitu. Hufunga masikio yao dhidi ya Kweli, hukataa kusikia maneno ya wazi ya "Asema Bwana," lakini kwa kudai utakatifu wanadanganya wengi, wakiwapotosha kwa imani yao ya bandia isiyo na msingi. —**Gospel Workers, uk. 226, 227 (1892).** {*EVsw 596.3*}

Mafundisho ya Uongo—Haijalishi Unachoamini

Wapo watu wengi ambao dini yao ni ya kinadharia tu. Kwao, hisia ya furaha ni sawa na kuwa na utauwa. Husema, "Njoo kwa Yesu, wewe umwamini tu. Haijalishi wewe unaamini nini mradi tu uwe mkweli katika imani yako." Hawajishughulishi kumfanya mwenye dhambi kuelewa asili ya kweli ya dhambi. {*EVsw 597.1*}

Shetani anafurahia pale kila mvunjaji wa sheria ya **Mungu** anapodai kuwa mtakatifu. Hilo ndilo analofanya yeye mwenyewe. Anatosheka anapoona watu wakiegemeza imani yao kwenye mafundisho ya bandia na shauku ya kidini; kwa sababu anaweza kuwatumia kwa faida kubwa katika kupoteza roho. Wapo wengi wanaodai kuwa wamepata utakaso, lakini kwa kweli wanamsaidia Shetani katika kazi yake. Huzungumza sana juu ya hisia; husema kuwa wanampenda **Mungu**. Lakini **Mungu** hatambui upendo wao, kwa sababu ni udanganyifu wa adui. **Mungu** amewapa watu hawa nuru, lakini wamekataa kuikubali. Kwa baba wa uongo, hawa watu watapokea malipo ya kutotii. —**The Review and Herald, June 26, 1900.** {*EVsw 597.2*}

Upotovu Mwingine—Kufuta Sheria za Mungu

Kristo aliwaonya wafuasi Wake, "Jihadharini na manabii wa uongo, wanaokuja kwenu kwa mavazi ya kondoo, lakini kwa ndani ni mbwa mwitu wakali." Yeye Anatuhimiza tusidanganywe wakati wachungaji wa uongo wanapokuja na mafundisho yao. Watu hawa hutuambia kuwa amri za **Mungu** zilifutwa alipokufa Kristo. Je, tuwaamini watu hawa wanaodai kuwa ni watakatifu au wamewekwa wakfu, lakini wanakataa kumtii **Mungu**?

Husema kuwa Bwana amewaambia kwamba hawapaswi kutii Amri Kumi; lakini je, Bwana amewaambia hivyo kweli? La, **Mungu** hawezi kusema uongo. {*EVsw 597.3*}

Shetani, baba wa uongo, alimdanganya Adamu kwa njia hiyo hiyo, akimwambia kuwa hahitaji kumtii **Mungu**, na kwamba hatakufa kama atavunja sheria. Lakini Adamu akaanguka, na kwa dhambi yake akafungua milango ya maafa duniani. Tena, Shetani alimwambia Kaini kwamba hahitaji kufuata agizo la wazi la **Mungu** la kutoa sadaka ya mwana-kondoo aliyechinjwa. Kaini alitii sauti ya mdanganyaji; na kwa sababu **Mungu** hakukubali sadaka yake bali alikubali sadaka ya Abeli, Kaini alighadhibika na kuinuka na kumuua ndugu yake. {*EVsw 598.1*}

Tunapaswa kujua wenyewe ni sauti ipi tunaisikia—sauti ya **Mungu** aliye hai au sauti ya mwasi mkuu. {*EVsw 598.2*}

Wakati kivuli kilikutana na halisi katika kifo cha Kristo, kutoa dhabihu za kafara kulikoma. Sheria ya kaida iliondolewa (ceremonial law). Lakini kwa kusulubiwa kwa Yesu, sheria ya Amri Kumi ilithibitishwa. Injili haijafuta sheria, wala kupunguza madai yake kwa kiwango chochote kidogo cha herufi au nukta - Mathayo 5:18. Injili bado inadai utakatifu katika kila sehemu ya sheria. Sheria ni mwangwi wa sauti ya **Mungu** Mwenyewe, ikitoa mwaliko kwa kila nafsi: Panda juu zaidi. Uwe mtakatifu, mtakatifu zaidi. **—The Review and Herald, June 26, 1900.** {*EVsw 598.3*}

Tahadhari ya Wakati

Sisi kama watu tumepotoka kwa upande mwingine. Tunakubali madai ya sheria ya **Mungu**, na tunawafundisha watu wajibu wa kutoa utii. Tunaamini katika kutoa kila kitu, lakini hatuoni kwamba tunapaswa kupokea pamoja na kutoa. Tunakosa ile imani inayofanya roho kukaa ndani ya Kristo. Tunadai kidogo, ilhali tungeweza kudai mengi; kwa maana hakuna kikomo kwa ahadi za **Mungu**. {*EVsw 598.4*}

Kwa sababu ya ukosefu wa imani, wengi wanaojitahidi kutii amri za **Mungu** wana amani ndogo na furaha ya kweli; hawawakilishi kwa usahihi utakaso unaotokana na utii kwa ile Kweli kwa Neno la **Mungu**. Hawajaweka nanga yao ndani ya Kristo. Wengi wanahisi pengo katika uzoefu wa maisha yao ya kiroho; wanatamani kitu ambacho hawajakipata; na hivyo, baadhi yao hujikuta wakihudhuria mikutano ya "utakatifu," na huvutiwa na mafundisho ya wale wanaovunja sheria ya **Mungu**. {*EVsw 599.1*}

Ni wajibu wetu kuhubiri imani, kuwasilisha upendo wa Kristo pamoja na madai ya sheria; kwa maana hakuna mojawapo linaloweza kueleweka ipasavyo pasipo lingine. Katika kila hubiri, upendo wa **Mungu** ulioonekana katika Kristo, tumaini pekee la mwenye dhambi, unapaswa kufafanuliwa mpaka watu wapate kuelewa nguvu na uzuri wake. Ikiwa hili litafanyika ipasavyo, haitasemwa tena juu ya watu hawa kwamba, wanafundisha na kuhubiri sheria lakini hawaamini katika toba, imani, na uongofu. Tunataka masomo haya yachanganywe kama vile **Mungu** alivyochanganya. Kisha Ukweli utaonyeshwa kwa ukamilifu wake, si kama nadharia tu, bali kama nguvu inayobadilisha tabia. Ukweli utafundishwa kwa ushahidi wa Roho na kwa uwezo. Kisha wale waliokubali mafundisho ya Biblia hawatabaki na njaa ya kiroho; watahisi mvuto wa uhai wa Roho Mtakatifu. **—Gospel Workers, uk. 227, 228 (1892).** {*EVsw 599.2*}

Nadharia za Kipagani-Pantheismu na Umizimu-

Hatari ya Sayansi ya Uongo na Nadharia za Kudanganya

Katika jimbo la New Hampshire kulikuwapo na watu waliokuwa wakieneza mawazo ya uongo kuhusu **Mungu**. Nimeonyeshwa kuwa watu hawa walikuwa wakilitangua Neno yaani ile Kweli kwa mitazamo ya mapokeo yao (Marko 7:13), baadhi ya mawazo hayo yakiendeleza maisha ya uasherati kwa jina la uhuru wa mapenzi (free-lovism*). Nikaonyeshwa kwamba watu hawa walikuwa roho zinazoshawishi wakiwasilisha kwa nadharia za kubuni kuhusu **Mungu**…..("Upendo huru" (au harakati ya Mapenzi Huru) inarejelea harakati ya kijamii ya karne ya 19 inayotetea mahusiano ya kimapenzi bila kufuata sheria za serikali au sheria za ndoa, au za Biblia kuhusu taaasisi ya ndoa, ikikuza uhuru binafsi katika mapenzi na ngono. Ndoa ikawa utumwa na wakaunga mkono uhuru wa wanawake wakisukuma ukombozi kutoka kwa kanuni zote za za jadi zinazohusu ngono.) {*EVsw 600.1*}

Miongoni mwa mafundisho yao ya uongo, walidai kuwa wale waliotakaswa hawawezi tena kutenda dhambi, na walikuwa wakiyawasilisha mafundisho haya kana kwamba ni chakula cha injili. Nadharia hizi za uongo, zenye ushawishi wenye udanganyifu mzito, zilikuwa zikiwadhuru wao wenyewe na pia wengine. Walikuwa wakipata mamlaka ya umizimu juu ya wale waliokuwa hawawezi kutambua ubaya uliofichwa

katika nadharia hizi zilizovikwa kwa uzuri kwa udanganyifu. Maovu makubwa yalikuwa tayari yamekwishatokea. Fundisho la imani kwamba wote ni watakatifu lilipelekea watu kuamini kuwa mapenzi ya wale waliotakaswa hayakuwa hatarini kuwaongoza kwenye upotefu. Matokeo yake yakawa kutimizwa kwa tamaa mbaya za mioyo ambayo, ingawa walidai imetakaswa, ilikuwa mbali na usafi wa fikra na matendo. {*EVsw 600.2*}

Hili ni mojawapo tu ya matukio ambayo niliitwa kuyakemea, ambapo watu walikuwa wanawasilisha mafundisho kuhusu **Mungu** asiye na umbo wala nafsi, anayesambaa kwenye maumbile/asili , na fundisho la "mwili mtakatifu, holy flesh" yalikuwa yakienezwa (Pantheismu ni neno la Kigiriki -Pan ikimaanisha kila kitu na theos-mungu. Pantheismu ni falsafa au nadharia inayosema kwamba mungu ni siyo nafsi, ila ni sawa na ulimwengu, ikimaanisha kuwa ulimwengu wenyewe na kila kitu ndiyo mungu na huyu mungu yuko katika kila kitu, hai na kisicho hai. Kuanzia mwamba hadi mwanadamu, ni dhihirisho la mungu huyu, anayemzunguka kila kiumbe na kila kitu. Inamkataa Muumba Mmoja na ikipata uungu ndani ya asili na uwepo. Inachanganya falsafa na mambo ya kiroho, yenye mizizi katika mila za kale za Mashariki (kama vile Brahman ya Uhindu) na mawazo ya Kigiriki, yaliyopendwa sana ila Magharibi utambulisho wake ulikuja na Baruch Spinoza utambulisho wa 'mungu ni Asili' katika karne ya saba. Mawazo muhimu ya hii falsafa ni pamoja na umoja wa uwepo wa yote, heshima kwa ulimwengu wa asili, na kutokuwa na mtazamo wa Mungu mmoja kwamba "kila kitu, yaani vyote ni mungu" *(This is only one of the instances in which I was called upon to rebuke those who were presenting the doctrine of an impersonal god diffused through nature, and the doctrine of holy flesh.)). {*EVsw 600.3*}

(

Katika siku za usoni, Kweli itapotoshwa na mafundisho bandia ya wanadamu. Nadharia za udanganyifu zitawasilishwa kuwa ndiyo mafundisho salama. Sayansi ya uongo ni mojawapo ya mawakala ambazo Shetani alitumia hata katika nyua ya mbinguni, na anatumia hadi leo... {*EVsw 600.4*}

Nawasihi wote wanaofanya kazi kwa ajili ya **Mungu** waepuke kuchukua bandia kwa mahali pa kile kilicho halisi na kweli. Tuna Biblia nzima iliyojaa Kweli zenye thamani kuu. Hatuna haja ya kubuni dhana au msisimko wa uongo. Katika chetezo cha dhahabu cha Kweli kama ilivyowasilishwa na mafundisho ya Kristo, tunacho kile ambacho kina na kubadili mioyo. Wasilisha katika usahili na unyenyekevu wa Kristo, zile Kweli ambazo alikuja kuzitangaza duniani, na nguvu ya ujumbe wako utaweza kufanya uhisiwe wenyewe. Usilete nadharia au majaribio yasiyo na msingi katika Maandiko. Tuna majaribio mazito na makubwa ya kuwasilisha. "Imeandikwa" ndilo jaribio ambalo lazima lifikishwe nyumbani kwa kila mtu. **— Review and Herald, Januari 21, 1904.** {*EVsw 600.5*}

Nadharia ya Uongo—Mungu Ni Kiini Kinachoenea Katika Maumbile

Tayari mafundisho ya umizimu yanaingia miongoni mwa watu wetu, na yatadhoofisha imani ya wale watakaoyasikiliza. Nadharia kwamba **Mungu** ni kiini kinachoenea kila mahali katika maumbile ni mojawapo ya nyenzo za hila za Shetani. Inamwakilisha **Mungu** kwa njia ya kupotosha na ni fedheha kwa ukuu na utukufu Wake. {*EVsw 601.1*}

Nadharia ya ya kipagani ya Pantheismu haina msingi wowote katika Neno la **Mungu**. Nuru ya Kweli ya **Mungu** inaonesha kuwa nadharia hizi ni mawakala ya kuangamiza nafsi. Giza ndilo mazingira yao; tamaa ya mwili kama ya ngono ndiyo uwanja wao wa kazi. Yanapendeleza moyo wa asili, na kumpa mtu leseni ya kufuata tamaa zake. Matokeo yake ni kujitenga na **Mungu**. {*EVsw 601.2*}

Kuna nguvu moja tu inayoweza kuvunja minyororo ya uovu kutoka kwa moyo wa mwanadamu, nayo ni nguvu ya **Mungu** katika Kristo Yesu. Ni kupitia Yule Aliyesulubiwa tu ndiyo kuna utakaso kutoka kwa dhambi. Neema ya Kristo peke yake ndiyo inayoweza kutuwezesha kushinda na kutiisha mielekeo ya asili yetu ya anguko. Hii nguvu ya mafundisho ya nadharia ya umizimu kuhusu **Mungu** huyafanya haya yote kuwa batili. Ikiwa **Mungu** ni kiini kilichoenea katika maumbile yote, basi inamaanisha kwamba **Mungu** Yumo ndani ya kila mtu; na kwa hiyo, ili mtu awe mtakatifu, inatosha aendelee tu kukuza nguvu alizo nazo ndani yake tayari. {*EVsw 601.3*}

Mafundisho haya au nadharia hizi zikifuatiwa hadi mwisho wake wa mantiki, yanafagilia mbali kabisa mpango mzima wa UKristo na neema yake. Yanaondoa haja ya Upatanisho, na kumfanya mwanadamu kuwa mwokozi wake mwenyewe. Nadharia hizi kuhusu **Mungu** hulitangua Neno Mungu na kulifanya kwa mapokeo ya mwanadamu, na wale watu wanaoyakubali wako katika hatari kubwa ya hatimaye kuongozwa katika kuanza kuangalia Biblia nzima kuwa riwaya tu. Huenda wakaona kuwa wema ni bora kuliko uovu, lakini

wanapomwondoa **Mungu** katika kiti Chake cha enzi, wanaegemeza tumaini lao katika nguvu ya kianadamu, bila **Mungu**, haina maana. Mapenzi ya mwanadamu peke yake bila msaada, hayana nguvu ya kweli kufanya upinzani na kushinda uovu. Ulinzi wa nafsi umevunjwa. Mwanadamu hana kinga dhidi ya dhambi. Mara tu Neno la **Mungu** na Roho Wake wanapokataliwa, hakuna anayeweza kujua ni kina cha urefu gani mtu anaweza kuangukia. {*EVsw 601.4*}

Wale watakaoendelea kushikilia nadharia hizi za umizimu hakika wataharibu uzoefu wao wa Kikristo, na kukata uhusiano wao na **Mungu**, na hata kupoteza uzima wa milele. {*EVsw 602.1*}

Ubunifu huu wenye udanganyifu kuhusu **Mungu** na maumbile, yanayofurika katika ulimwengu kwa mashaka na upagani, umevuviwa na yule adui aliyeanguka kutoka mbinguni. Yeye ni mwanafunzi mahiri wa Biblia, anayejua Ukweli ambao ni muhimu kwa watu a kuupokea, na anafanya kila juhudi kutoa akili zao kutoka kwenye Kweli hizo zilizokusudiwa kuwaandaa wanadamu kwa yale yatakayoujia ulimwengu. {*EVsw 602.2*}

Nimeona matokeo ya mitazamo hii ya kufikirika kuhusu **Mungu**, katika kuasi, umizimu, na mapenzi huria (free-lovism). Mwelekeo wa mapenzi huria ulioenezwa na mafundisho haya ulikuwa umefichwa kiasi kwamba mwanzoni ilikuwa vigumu kueleza kwa hakika tabia yake. Hadi pale Bwana aliponionesha, sikujua niite hali hii kwa jina gani, lakini niliagizwa niite "upendo wa kiroho usio mtakatifu." — **Testimonies for the Church, 8:291, 292 (1904).** {*EVsw 602.2*}

Aina Mbalimbali za Umizimu

Umizimu Huu U Karibu Kuchukua Dunia Mateka

Umizimu uko karibu kuiteka dunia yote. Wengi hudhani kuwa umizimu unainuliwa juu na ujanja na udanganyifu wa wanadamu, lakini hiyo si kweli. Kuna nguvu isiyo ya mwanadamu, ya kishetani inayofanya kazi kwa namna mbalimbali, na ni wachache wanaojua yale yatakayodhihirika kupitia umizimu huu katika siku zijazo. Misingi ya mafanikio ya umizimuimewekwa tayari kupitia madai yaliyotolewa kutoka kwa mimbari mbalimbali katika nchi yetu. Wachungaji wametangaza kama mafundisho ya Biblia ya uongo ambayo kwa hakika yametoka kwa mdanganyaji mkuu (Shetani). {*EVsw 602.4*}

Fundisho la kuwa na ufahamu baada ya kifo, na la kuwa roho za wafu huwasiliana na atu walio hai, halina msingi wowote wa Kimaandiko. Lakini mafundisho haya yamekuwa yakisisitizwa kwamba ndiyo Kweli. Kupitia mafundisho haya ya uongo, njia imeandaliwa kwa ajili ya pepo wachafu kujifanya kuwa ni roho za mashetani kuwadanganya watu kwa kuwawakilishakama wafu. Mawakala wa Shetani hujifanya kuwa ni watu waliokufa na kwa njia hiyo huziteka nafsi za watu. Shetani ana dini yake, ana sinagogi na waabudu wake waaminifu. Ili kuongeza idadi ya waumini wake, hutumia kila aina ya udanganyifu. **—Undated Manuscript 66.** {*EVsw 603.1*}

Udanganyifu Unaolenga Watu Waliofiwa

Kutukuzwa kwa wafu limekuwa jambo la kawaida karibu katika kila mfumo wa dini za kipagani, pamoja na imani ya kuwa na ‘mawasiliano na wafu’. Miungu ya kipagani iliaminika kuwa ina uwezo wa kuwasiliana mapenzi yao kwa wanadamu wanapoafutwa kwa ushauri. Hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa watabiri maarufu huko Ugiriki na Roma. {*EVsw 603.2*}

Imani ya kuwasiliana na wafu bado inaendelezwa hata katika nchi zinazodai kuwa za Kikristo. Chini ya jina la umizimu, utendaji wa kuwasiliana na nafsi zinazodai kuwa roho za watu waliokufa, umeenea sana. Mbinu hii imeundwa ili kuwinda watu wenye sikitiko na majonzi baada ya kuzika wapendwa wao kaburini, kwa huruma na matumaini bandia. — **The Signs of the Times, June 23, 1890.** {*EVsw 603.2*}

Kuweka Msingi wa Roho za Mizimu

Shetani hujifanya yaani aweza kuigiza, na mara nyingine huja katika umbo la kijana mrembo au kivuli kizuri chenye mvuto. Hufanya uponyaji, na huabudiwa na watu wanaokufa waliodanganyika humwabudu kana kwamba yeye ndiye mfadhili na mkombozi wa jamii ya binadamu…... Maelfu ya watu huzungumza na kupokea maagizo kutoka kwa “mungu -pepo” huyu, na hufuata mafundisho yake. Dunia, ambayo hudhani kuwa inanufaika na mafundisho kama frenolojia na sumaku ya wanyama, haijawahi kuwa katika hali ya upotovu kama sasa. Shetani hutumia mambo haya kuharibu maadili na wema na kuweka msingi wa umizimu (*Phrenolojia -Phrenolojia ilikuwa sayansi bandia maarufu ya karne ya 19 ikidai kwamba matuta na maumbo kwenye fuvu la mtu yalionyesha tabia, utu, na uwezo wake wa akili, kulingana na wazo kwamba

maeneo maalum ya ubongo (viungo) yanadhibiti sifa zilizopo au zilizopungua, na kuunda fuvu. Aliyekuja na nadharia hii ni Franz Joseph Gall.

Animal magnetism au mesmerism, au sumaku ya wanyama ilikuwa nadharia ya uponyaji ya karne ya 18 na Franz Mesmer, akipendekeza majimaji yasiyoonekana ulimwenguni kote, ndani ya viumbe hai wote ambapo ungeweza kubadilishwa (kwa sumaku kupitishwa kwa mkono) ili kutibu magonjwa kwa kurejesha usawa, na kusababisha hali ya akili kuchukuliwa msukule au kuvutwa hii ndiyo imezaa tiba ya saikolojia leo, inayoitwa hypnosis, ingawa tiba hii ilikanushwa rasmi kwa kukosa uthibitisho, inahusisha pia uasherati wa namna fulani).

— Testimonies for the Church, Gombo la 1, uk. 296-297 (1862). {*EVsw 604.1*}

Maonyesho ya Kushtua Yataongezeka

Wafuasi wa umizimu wanaongezeka kwa idadi. Watakuja kwa wale wanaoshikilia Kweli kama Shetani alivyomjia Kristo, wakiwajaribu wafanye ishara na miujiza ili kuthibitisha kuwa wao ndio watu waliopendelewa na **Mungu** na wanao Ukweli..... Ulinzi pekee kwa watu wa **Mungu** ni kuwa na maarifa ya kina ya Biblia na kuelewa kwa umahiri sababu za imani yetu kuhusu kulala kwa wafu. {*EVsw 604.2*}

Shetani ni adui mwerevu sana. Na si jambo gumu kwa malaika waovu kuigiza ni watakatifu au waovu waliokufa, na kujionesha mbele za macho ya kibinadamu. Maonyesho haya yataongezeka, na matukio ya kushtua zaidi yatajitokeza kadri tunavyokaribia mwisho wa wakati. **— Review and Herald, April 1, 1875.** {*EVsw 604.3*}

Wahubiri Hupamba Mafundisho Haya

Wahubiri waliovuviwa na Shetani wanaweza kupamba kwa ustadi kiumbe huyu wa kutisha, wakaficha uharibifu wake na kuufanya aonekane mzuri kwa wengi. Lakini chanzo chake ni moja kwa moja kutoka kwa fahari ya shetani, na wale wote wanaohusiana nacho Shetani hudai kuwa ni mateka wake, kwa kuwa wameingia katika maeneo yaliyokatazwa, na wamepoteza ulinzi wa Muumba wao. **— Review and Herald, May 13, 1862.** {*EVsw 604.4*}

Umizimu na Madhehebu ya Uongo Hupotosha Akili (Spiritism and Cultism debase minds)

Maelfu, nilioneshwa, wamepotoshwa kupitia falsafa ya frenolojia na sumaku ya wanyama na wamesukumwa katika kutokuamini. Mara akili inapokubali kupitia mkondo huu, ni vigumu sana kuitoa na huishia kuthibitiwa na pepo (angalia 604.1). {*EVsw 605.1*}

"Udanganyifu wa bure" hujaza akili za wanadamu. Hufikiri kuwa na uwezo wa kufanya mambo makuu, kiasi kwamba hawatambui tena hitaji la nguvu ya juu. Kanuni na imani yao ni "kulingana na mapokeo ya wanadamu, kulingana na mafundisho ya dunia, na siyo ya Kristo." Yesu hakuwafundisha wanadamu falsafa hii. Hakuna kitu cha namna hii kinachopatikana katika mafundisho Yaje. Hakuzielekeza akili za mwanadamu anayekufa awaze kuhusu uwezo wao binafsi. Daima alikuwa akiwaelekeza kwa **Mungu**, Muumba wa ulimwengu na sayari zote, kama chanzo cha nguvu na hekima... {*EVsw 605.2*}

Walimu wa umizimu huja kwa njia ya kupendeza, wakiloga watu ili kuwadanganya. Na ikiwa utasikiliza hekaya zao, utatekwa na adui wa haki kwa uongo wake, na hakika utapoteza thawabu yako. Mara tu mvuto huu wa kudanganya wa baba wa uongo Shetani unapokushinda, unakuwa umelishwa sumu, na ushwaishi wa hiyo sumu unagushi na kuharibu imani yako katika Kristo kuwa ni Mwana wa **Mungu**, na utaacha kutegemea sifa na uweza wa damu Yake Masihi. Wale waliodanganyika na falsafa hii hulogwa hata kukosa thawabu yao ya kweli, kwa madanganyo ya Shetani hujiamini katika haki na sifa zao wenyewe, hujinyenyekeza kwa hiari, huwa yao tayari hata kujitoa dhabihu kwa hiar, na hujishusha chini kimaadili, lakini pia huamini upuuzi wa hali ya juu (nonsense), wakipokea mawazo yanayoshtua kwa kukosa hekima kabisa, kupitia wale wanaoamini kuwa ni wafu wao waliokufa-aidha ndugu au marafiki. Shetani amefunga macho yao na kupotosha uamuzi wao kiasi kwamba hawaoni uovu wa kile wanachokifanya; na hufuata maagizo ambayo wanadhani yametoka kwa wapendwa wao waliokufa—ambao wao wanadhani ni malaika wa hali ya juu huko mbinguni (ila ni mapepo). **— Testimonies for the Church, 1: 297-298 (1862).** {*EVsw 605.3*}

Sayansi ya Kikristo, Madhehebu ya Mashariki ya mbali, na Vikundi vya Uponyaji

(Christian Science, Oriental and Healing Cults)

Kuna wengi wanaokwepa kwa hofu wazo la kwenda kwa wapiga ramli, wabashiri au waongeaji na mapepo, lakini huvutiwa na maonyesho ya kuvutia ya umizimu kama vile harakati ya Emmanuel. Wengine hupelekwa mbali na mafundisho ya Sayansi ya Kikristo (Christian Science), Mysticism of Theosophy, na dini nyingine za Mashariki ya mbali zenye mafumbo (Theosofi ni filosofia mpya ya kidni, ni aina ya uchawi wa magharibi hufundisha kuhusu Mungu na ulimwengu kulingana na ufahamu wa kifumbo. 2. Mafundisho ya harakati hii yalianzia Marekani mwaka wa 1875 na kufuata nadharia za Kibuddha na Kibramani hasa za mageuzi ya imani ya miungu na kuzaliwa upya baada ya kufa mahali fulani kama mtu bora zaidi (reincarnation). Ilianzishwa hasa na Mrusi aitwaye Helena Blavatsky na kwa kiasi kikubwa kulingana na maandishi yake, inatokana sana na falsafa za zamani za Ulaya kama vile Neoplatonism na dini za Kihindi kama vile Uhindu na Ubuddha. Ingawa wafuasi wengi wanasisitiza kwamba Theosofi si dini, imeainishwa kwa njia mbalimbali na wasomi wa kidini kama uchawi wa Magharibi. . {*EVsw 606.1*}

Karibu kila mitume wa kila aina ya umizimu hudai kuwa na uwezo wa kuponya wagonjwa. Hudai kuwa uwezo wao unatokana na umeme (electricity), sumaku ya wanyama (animal magnetism), tiba zenye huruma (sympathetic remedies), au nguvu fiche zilizomo katika akili ya mwanadamu. Na sio wachache, hata katika enzi hii ya Kikristo, huwakimbilia waganga hawa badala ya kutegemea nguvu ya **Mungu** aliye hai au ujuzi wa madaktari wa Kikristo stadi, yaani Matabibu Wakrito waliobobea. {*EVsw 606.2*}

Mama anapoketi karibu na kitanda cha mwanawe mgonjwa, akilia kwa uchungu: “Sijui kilichobakia cha kufanya sasa! Je, hakuna daktari mwenye uwezo wa kurejesha afya ya mwanangu?” Anaambiwa habari za uponyaji wa kushangaza unaofanywa na mpiga ramli anayebashiri ya mbeleni (pyschic) au mganga wa umizimu anayetumia sumaku, naye huamua kumkabidhi mtoto wake mikononi mwao—kwa hakika, anamweka mikononi mwa Shetani, hakika ni kana kwamba Shetani alikuwa amesimama hapo pembeni yake. Na mara nyingi, maisha ya baadaye ya mtoto huyo hutawaliwa na nguvu ya kishetani, ambayo huonekana kuwa vigumu mno kuivunja. **— Review and Herald, January 15, 1914.** {*EVsw 606.3*}

Faida Zidanganyazo

Wale wanaojitoa kwa uchawi wa Shetani wanaweza kujisifia kuwa wamenufaika sana, lakini je, hii inathibitisha kuwa njia yao ni ya hekima au salama? Inakuwaje basi kama maisha yataongezwa?, inakuwaje wakipata faida au mali ya muda kitambo?—je, hiyo faida ya muda kitambo itawafaidi mwishoni wakiwa waakati wamekataa kutii mapenzi ya **Mungu**? Faida yoyote ya bandia itageuka kuwa hasara isiyorekebishika. Hatuwezi, pasipo madhara, kubomoa hata kizuizi kimoja ambacho **Mungu** amekisimamisha ili kuwalinda watu Wake dhidi ya nguvu za Shetani. — **Review and Herald, January 15, 1914.** {*EVsw 606.4*}

Hatari ya Kuwategemea Waganga wa Kishirikina

Kuna hatari kubwa katika kuacha hata kwa kiwango kidogo cha maagizo ya Bwana. Tunapokengeuka kutoka njia ya wazi ya wajibu, kuna mlolongo wa matukio utakaoanza kujitokeza ambao huonekana kama nguvu ya ajabu inayoendelea kututongoza mbali zaidi na njia ya haki. Ukaribu usio wa lazima na wale wasiomheshimu **Mungu** unaweza kutudanganya kabla hatujatambua. Hofu ya kuwakera au kutowafurahisha rafiki wa kidunia itatuzuia kuwa na moyo wa shukrani kwa **Mungu au kutoa ushuhuda hadharani au** kukiri utegemezi wetu Kwake... {*EVsw 607.1*}

Malaika wa **Mungu** watawalinda watu Wake ilimradi wamo katika njia ya wajibu, lakini hakuna ahadi ya uhakika kuhusu ulinzi kwa wale wanaoamua kwa hiari kujitosa katika maeneo ya Shetani. Wakala wa mdanganyaji mkuu atasema na kufanya kila kitu ili afikie lengo lake. Haijalishi umuhimu wake hata pale anapojitambulisha kama nafsi inayoshugulika mambo ya kiroho katika shuguli ya mpiga ramli, “daktari wa umeme,” au “mganga wa sumaku.” Kwa hila na ujanja hujipatia ujasiri na imani ya watu wasio na tahadhari (kujiita spiritualist, haina mambo ya kiroho ya Mungu wa mbinguni, wakala wa Shetani na mapepo na Shetani mwenyewe ni roho). Hudai kuwa anaweza kusoma historia ya maisha ya mtu na kuelewa matatizo yote ya wale wanaomjia. Akiwa amejificha kama malaika wa nuru, wakati moyo wake umejaa giza la shimo la kuzimu, huonesha kujali sana kwa wanawake wanaokuja kutafuta ushauri wake. Huwaambia kuwa matatizo yao yote yanatokana na ndoa isiyo ya furaha. Na ingawa hili linaweza kuwa la kweli, mshauri huyu haifanyi hali ya kesi hiyo kuwa bora. Huwaambia kuwa wanahitaji upendo na huruma. Kwa kujifanya kuwa anawajali sana, huwaloga- na kwa uchawi wake—huwavutia kama nyoka anavyomvutia ndege anayetetemeka anayejikuta tu anavutwa kama kwa sumaku kumfuata nyoka bila hiari yake. Punde hujikuta akiwa katika mamlaka yake kabisa, na matokeo ni dhambi, aibu, na maangamizi. — **Review and Herald, June 27, 1882.** {*EVsw 607.2*}

Kibali cha kufanya uovu wa kutisha, Kukata Tamaa na Maangamizi

(Vilest licence, Despair, and Ruin)

Ujumbe wa pepo kwa Sauli, ingawa ulikuwa wa shutuma dhidi ya dhambi na unabii wa kisasi, haukulenga kumletea matengenezo, bali ulimsukuma kwenye kukata tamaa na maangamizi. Hata hivyo, mara nyingi zaidi, Shetani hupata mafanikio zaidi kwa kuwajaribu watu kwa mtego wa kuwapa sifa za kinafiki, hujikomba kwao kwa kutia chumvi sifa hadi huwaangamiza. Mafundisho ya miungu ya kipagani ya zamani yaliendeleza uovu wa kutisha na kuchukiza. Amri za **Mungu** zilizokemea dhambi na kuhimiza haki ziliwekwa kando; Kweli ilidharauiwa, na uchafu haukuruhusiwa tu, bali ulishuritishwa kufanywa. Umizimu wa kisasa unatangaza kuwa hakuna kifo, hakuna dhambi, hakuna hukumu, hakuna kisasi; kwamba "wanadamu hawakuanguka bali ni nusu-miungu"; kwamba tamaa ya mwili ndiyo sheria ya juu zaidi; na kwamba mwanadamu anawajibika kwake mwenyewe tu. Vizuizi ambavyo **Mungu** ameweka kulinda ile Kweli, usafi wa moyo, na heshima vinavunjwa, na wengi hujikuta wakijitosa katika dhambi. Je, mafundisho kama haya hayapendekezi asili inayoshabihiana kabisa na ibada ya pepo? **— The Signs of the Times, June 30, 1890. {*EVsw 608.1*}**

Sauti za Mafumbo, Wapiga Ramli na Watabirio

(Mystic voices, mediums, clairvoyant, and fortune tellers)

Sauti za mafumbo zenye nguvu zisizo za kawaida, zilizozungumza huko Ekroni na Endori bado zinaendelea kuwapotosha wanadamu kwa uongo wao (Soma Samweli 28). Mkuu wa giza ametokea kwa mtindo mwingine wa kujivika sura mpya. Vyanzo vya uchawi na upagani wa zamani vinafanana na vyombo vya umizimu vya leo—wapiga ramli, wachawi, watu wenye maono na wabashiri wanaotabiri mambo yajayo. Mafumbo ya ibada za kipagani yamebadilishwa na vyama vya siri na mikutano ya umizimu ya kisasa inayohusisha wachawi (secret societies and seances)—maajabu na mambo yasiyofahamika ya wachawi wa ulimwengu wa leo. Na mafunuo yao yanapokelewa kwa shauku na maelfu ambao wanakataa nuru kutoka kwa Neno au Roho wa **Mungu**. Wanaadamu wa leo wanadharau na kuwang'onga wachawi wa kale, ilhali mdanganyifu mkuu anashangilia wanapodanganywa na kujisalimisha chini ya sura tofauti za uchawi, na Shetani--- (Secret societies) -Vyama vya siri ni mashirika yanayoficha shughuli zao, uanachama, au utendaji kazi wa ndani, kwa kutumia kufundwa kwa siri, mila, alama, na kupeana mikono, kuanzia vikundi vya kihistoria kama vile Knights Templar, Freemasons, na Illuminati hadi udugu wa kisasa, mara nyingi huchochea hekaya na njama lakini pia hutoa ushawishi mzito kwenye siasa za nchi kupitia viongozi wa nchi na utamaduni kupitia mitandao ya binafsi na maarifa yaliyoshirikiwa. Malengo yao hutofautiana lakini mara nyingi huhusisha udugu, maarifa yaliyoshirikiwa ya siri, ushawishi wa kisiasa, au ukuaji wa kiroho katika kuabudu nguvu za giza, huku usiri ukitumika kuunda upekee na uaminifu wa kujaribu. Kundi mashuhuri la vyama vya siri ni lile la Freemasons). **{*EVsw 608.2*}**

Wakala hawa wa Shetani hudai kuponya magonjwa. Hudai kuwa nguvu yao hutoka kwa umeme, sumaku, au "tiba za huruma," lakini kwa kweli ni njia tu za mkondo wa umeme wa Shetani. Kwa njia hii adui huwatupia uchawi na kuwaloga wanadamu ili wafungwe kimwili na kiroho. **— The Signs of the Times, March 24, 1887. {*EVsw 609.1*}**

Njia Iendayo Jehanamu

Falsafa ya kiburi na ubatili hutumika kuelezea njia iendayo jehanamu kuwa ni salama. Kwa mawazo yaliyoinuliwa na sauti zenye mvuto wa muziki, huonyesha njia pana kuwa ni njia ya furaha na utukufu. Matamanio ya ukuu huonyeshwa kwa roho zilizopofushwa kana kwamba ni uhuru na furaha isiyowahi kufikiriwa kama pale mapendekezo aliyopewa Hawa, katika Bustani ya Edeni. Watu waliotembea njia pana iendayo upotevuni husifiwa, na baada ya kufa hupewa hadhi ya juu katika ulimwengu mwa milele. Shetani, akiwa amejivika joho la kung'aa kama malaika aliyeinuliwa, alimjaribu Mkombozi wa dunia bila mafanikio. Lakini anapokuja kwa mwanadamu kama malaika wa nuru, huwa anapata mafanikio zaidi. Huficha makusudi yake ya kutisha, na huwapumbaza kwa mafanikio wale wasioweka nanga yao katika Kweli thabiti ya milele. — **The Review and Herald, April 1, 1875. {*EVsw 609.2*}**

Nguvu ya Maombi Katika Kukabiliana na Shetani

Maombi ya imani ni nguvu kuu ya MKristo, na hakika hushinda dhidi ya Shetani. Ndiyo maana Shetani hutoa wazo kwetu kwamba sisi hatuhitaji kuomba. Jina la Yesu, Wakili na Mpatanishi wetu, adui analichukia; na tunapomwendea kwa dhati na bidii kuomba msaada, majeshi yake huingiwa wasiwasi na tahadhari kama ile ya king'ora. Kusudi lake hufanikiwa vizuri/Inamfaidia sana Shetani tukipuuza mazoea ya mamba, kwani

maajabu yake ya uongo hupokelewa kirahisi zaidi. — **Testimonies for the Church 1:296 (1862).** {*EVsw 609.3*}

Ushupavu wa Dini au Usongo unaopitiliza, unaokosa busara na Itikadi Kali

Kughushi Karama za Kiroho

Makosa mengi yaliibuka, na ingawa nilikuwa bado mtoto mdogo, Bwana alinileta kutoka sehemu moja hadi nyingine kukemea wale waliokuwa wakishikilia mafundisho ya uongo. Kulikuwepo hatari ya watu kuingia katika ushupavu wa kiroho wenye usongo wa kupitiliza, nami niliagizwa kwa Jina la Bwana kuwapa onyo kutoka mbinguni. {*EVsw 610.1*}

Lazima tutakutana tena na mafundisho haya ya uongo. Kutakuwa na watu watakaodai kuwa na maono. **Mungu** akikupa ushahidi wazi kuwa maono ni kutoka Kwake Yeye, basi unaweza kuyakubali; lakini usiyakubali kwa ushahidi mwingine wowote, kwa kuwa watu watapotoshwa sana, ndani na nje ya nchi. Bwana anataka watu Wake kutenda kama wanaume na wanawake wenye utambuzi, na busara. {*EVsw 610.2*}

Katika siku zijazo, udanganyifu wa kila aina utatokea, nasi tunataka miguu yetu isimikwe kwenye msingi imara. Tunataka nguzo imara kwa ajili ya jengo la imani. Hakuna hata mhimili mmoja wa jengo, yaani mafundisho makuu ya imani, utakaondolewa kutoka kwa kile ambacho Bwana amekianzisha.... Tutapata wapi usalama isipokuwa katika zile Kweli ambazo Bwana amekuwa akitupa kwa miaka hamsini iliyopita sasa—The Review and Herald, Mei 25, 1905. — **The Review and Herald, May 25, 1905.** {*EVsw 610.3*}

Kama Nyoka Aliyemdanganya Hawa

Nadharia za uongo, zinaporudiwa mara kwa mara, huonekana kuvutia kama tunda la mti uliopigwa marufuku katika Bustani ya Edeni. Tunda hilo lilikuwa la kuvutia/kupendeza, na zuri kwa cha kula. Kupitia mafundisho ya uongo, roho nyingi tayari zimepotezwa/zimeharibiwa. — **Manuscript 37, 1906.** {*EVsw 610.4*}

Waliokumbwa na Ujinga wa Dini na Msimamo Mkali

Kama vile macho ya mwili yanavyoweza kulemaa hadi kufikia kutofanya kazi, na kutomnufaisha mtu, ndivyo pia uwezo wa kiroho wa kutambua mema na mabaya unavyoweza kupotoka kwa watu wenye ushupavu wa misimamo mikali ya kidini, kiasi kwamba wanakosa busara. Uelewa wa kiroho huwa umepotoka kiasi kwamba roho ya Kweli haiwezi kutofautishwa na roho ya uongo. Busara nzuri ya maamuzi uharibiwa, hivi kwamba roho wa kweli na haki haiwezi kutofautisha roho ya akosa na ushabiki (fanatism) {*EVsw 610.5*}

Kuna ugonjwa wa vitivyo vya kiroho pale mwanamume au mwanamke anapokuwa na mawazo ya kufikirika na kuona vitu ambavyo havipo. Yupo kama mlevi aliyelewa kwa udanganyifu wa kinywaji kikali sana. Kuna msukumo wa kiroho, lakini sio kutoka kwa **Mungu**. Vitivo vya akili hupotoka. Hebu kila roho (mtu) imtegemee **Mungu** na ipate uzoefu ulio wa afya njema na uzima. — **Manuscript 41, 1900.** {*EVsw 611.1*}

Katika Moto au Majini

Kuna kundi la watu ambao kila wakati huwa tayari kubadilisha njia yao na kwenda kushugulikia jambo lolote jipya na la ajabu; hutaka kufuatilia mambo ya ajabu, mageni na yasiyoeleweka, lakini **Mungu** anatamani sote tusonge mbele kwa utulivu na busara, tukichagua maneno yetu kwa hekima, kwa kuambatana na Ukweli thabiti wa wakati huu. Ukweli unapaswa kuwasilishwa kwa akili kwa namna isiyojaa hisia za mihemko au misukumu, ingawa unapaswa kubeba uzito na adhima ya Kiungu unaoendana na tabia yake. Tunapaswa kujihadhari dhidi ya kuwatia moyo wale walio na misimamo mikali, isiyo na busara na iliyopitiliza, ambao daima wako ama “motoni” au “majini.” {*EVsw 611.2*}

Nawasihi muondoe kila kauli ya kupitiliza usongo au mipaka katika mafundisho yenu, kila kitu ambacho akili zisizotulia au watu wasio na uzoefu wataweza kukitumia kuanzisha mienendo ya ajabu na inayofanya akili ithibitiwe kama mwendawazimu au mnyama wa mwituni na wala sio mwanadamu tena. Ni muhimu kujifunza tahadhari katika kila kauli, la sivyo mtaanzisha kwa watu mwelekeo mbaya, na kuleta vurugu itakayohitaji kazi ngumu na ya huzuni kuirekebisha na kurudi kwenye mpangiliio tena—na hivyo mtabadilisha nguvu ya watendakazi kutoka katika njia ambazo **Mungu** hakukusudia waingie. Udhihirisho mmoja wa ushabiki wenye usongo uliopitiliza, na usio na busara wa kiimani miongoni mwetu utafunga milango mingi dhidi ya kanuni za hekima na thabiti za ile Kweli. — **Manuscript 82, 1894.** {*EVsw 611.3*}

Kweli Takatifu Inapoabishwa kwa Msisimko

Tunapaswa kuwa watu wa kutafakari na utulivu, na kufikiri juu ya zile Kweli za ufunuo. Msisimko hautoi mazingira bora kwa ukuaji katika neema, usafi wa moyo wa kweli, na utakaso wa Roho. {*EVsw 612.1*}

Mungu anataka tujihusishe na Kweli takatifu. Hii pekee ndiyo inayoweza kumshawishi mpingaji. Kazi yetu lazima ifanyike kwa utulivu na busara, na kazi ya Mungu lazima isonge mbele……. {*EVsw 612.1*}

Mungu anawaita watu Wake kutembea kwa kiasi na kwa maisha ya uendelevu katika utakatifu. Wapate kuwa waangalifu sana ili wasiwe wakipotosha na kuyakosea heshima mafundisho matakatifu ya ile Kweli kwa maonyesho ya ajabu, vurugu, na msisimko wa sauti ya makelele na mkanganyiko. Kwa njia hiyo watu wasioamini hufikiri kwamba Wasabato ni kundi la mashabiki, watu wenye usongo uliopilitiza kwa kukosa busara. Hali hii huleta chuki na ubaguzi ambao huwazuia watu kupokea ujumbe wa wakati huu. Wakati waumini wanaposema Kweli kama ilivyo katika Yesu, huonyesha utulivu wa mbinguni/Kiungu na wenye busara, sio dhoruba ya machafuko. **— Manuscript 76a, 1901. {*EVsw 612.3*}**

Walimu wa Uongo Hupotosha Unabii

Katika siku zetu kama ilivyokuwa katika siku za Kristo, kuna hatari ya watu kusoma na kutafsiri vibaya Maandiko. Kama Wayahudi wangesoma Maandiko kwa moyo wa dhati, bidii na sala, utafutaji Maandiko wao ungewaletea maarifa ya Kweli ya wakati, na siyo wakati tu, bali pia namna ya kuja kwa Kristo. Wasingelichanganya kuja kwa pili kwa utukufu na kuja kwa kwanza kwa Kristo-kwa kuzaliwa Bethlehemu. Walikuwa na ushuhuda wa Danieli, Walikuwa na ushuhuda wa Isaya, na manabii wengine; walikuwa na mafundisho ya Musa; na hapa Kristo Mwenyewe alikuwa katikati yao, lakini bado walikuwa wakitafuta ndani ya Maandiko ushahidi wa kuja Kwake Masihi. Walikuwa wakimfanyia Kristo yale mambo ambayo tayari yalikuwa yametabiriwa kuwa wangemfanyia. Walikuwa na upofu mkali, kiasi cha kutofahamu walichokuwa wakifanya. {*EVsw 612.4*}

Na wengi leo hii wanafanya vivyo hivyo (1897), kwa sababu hawajapata uzoefu katika Zinazojaribu za malaika wa kwanza, wa pili, na wa tatu. Kuna wale ambao wanachunguza Maandiko ili wapate ushahidi wa kwamba Jumbe hizi tatu bado zinakuja siku za usoni-mbeleni na siyo sasa. Wanakusanya pamoja ukweli unaohusu ujumbe huu, lakini wanafeli kuuweka katika mahali pake sahihi katika historia ya unabii. Kwa hiyo watu wa namna hiyo wako katika hatari ya kupotosha wengine kuhusu nafasi ulipo ujumbe huu. Hawaoni wala kuelewa wakati wa mwisho, au namna ya kuona nafasi ya ujumbe huu. Siku ya **Mungu** inakuja kwa kunyemelea taratibu kwa siri, lakini wale wanaodhaniwa kuwa werevu na wakuu wanabwebweja midomo kama wapumbavu kuhusu "elimu ya juu." Hawajui dalili za kuja kwa Kristo, wala mwisho wa dunia. — **Manuscript 136, 1897. {*EVsw 613.1*}**

Upotoshaji wa Nafsi za Uungu (Utatu, Mungu Baba, Mungu Mwana na Roho Mtakatifu)

Acha watu Wajue Msimamo Wetu

Sera yetu ni hii: Tusifanye vipengele vya imani yetu vinaoonekana kwa hakika kupingana vikali na desturi na kaida za watu kuwa ndivyo muhimu sana au kuwa kama mlima, mpaka Bwana awape upendeleo ambao ni haki ya kila mwanadamu, kujua kwamba sisi ni waumini katika Kristo, kwamba tunaamini katika Uungu wa Kristo na kuwepo Kwake kabla ya kuzaliwa hapa duniani (Yesu ni Mungu, na alikuwepo milele zote nyuma, na milele zote mbele). — **Testimonies to Ministers and Gospel Workers, uk. 253 (1895). {*EVsw 613.2*}**

Tutakutana na Mafundisho ya Uongo

Tena na tena tutaitwa kukabiliana na ushawishi wa watu wanaojifunza sayansi za asili ya kishetani, ambazo Shetani anazitumia kumfanya **Mungu** na Kristo kuonekana kuwa si nafsi au si kitu. Baba na Mwana kila mmoja ana nafsi. Kristo alitangaza, “Mimi na Baba tu Umoja.” Ilikuwa ni Mwana wa **Mungu Ndiye** aliyekuja duniani kwa umbo la kibinadamu. Akiweka kando mavazi Yake ya Mkuu wa utukufu na taji Kifalme, aliuvisha Uungu Wake kwa ubinadamu, ili ubinadamu, kwa dhabihu Yake isiyo na kifani, waweze kuwa washiriki wa asili ya Uungu na kuepuka uharibifu wa tamaa za dunia. **— Testimonies for the Church 9:68 (1909). {*EVsw 613.3*}**

Kweli Chanya/Halisi Dhidi ya Mawazo ya Umizimu

Nimeelekezwa niseme kwamba maoni ya wale wanaotafuta maarifa ya kisayansi ya juu hayapaswi kuamiwa au kutumainiwa. Mifano kama ifuatayo imewasilishwa:

“Baba ni kama nuru isiyoonekana; Mwana ni nuru iliyo katika umbo; Roho ni nuru inayomiminwa katika eneo kubwa.”

“Baba ni kama umande, mvuke usioonekana; Mwana ni kama umande ulio katika umbo la zuri la kupendeza; Roho ni kama umande ulioshuka kwenye kiti cha uzima.” Wasilisho jingine ni: “Baba ni kama mvuke usioonekana; Mwana ni kama wingu jeusi zito linalotembea kwa ugoigoi; Roho ni kama mvua iliyoshuka na kufanya kazi kwa nguvu ya kuburudisha.” {*EVsw 614.1*}

Mifano hii yote ya kiroho iliyowasilishwa ni bure kabisa-sifuri. Haina ukamilifu, sio ya kweli. Inapunguza na kupotosha ukuu wa **Mungu** ambaye hakuna mfano wa kidunia unaoweza kulinganishwa Naye. **Mungu** hawezi kufananishwa na vitu vilivyo mikononi Mwake. Hivyo vitu ni vya kidunia, vikiwa chini ya laana ya **Mungu** kwa sababu ya dhambi za mwanadamu. Baba hawezi kufafanuliwa kupitia vitu vya dunia. Baba ni utimilifu wote wa Uungu katika mwili, Naye haonekani kwa macho ya mwanadamu anayekufa. {*EVsw 614.2*}

Mwana ni onyesho la utimilifu wote wa Uungu unaodhihirishwa. Neno la **Mungu** linamtangaza kuwa “mfano kamili wa nafsi ya **Mungu**.” “**Yohana 3:16** *Kwa maana jinsi hii **Mungu** aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele*.” Hapa tunaonyeshwa haiba na nafsi ya Baba. {*EVsw 614.3*}

Mfariji ambaye Kristo aliahidi kumtuma baada ya kupaa mbinguni ni Roho katika utimilifu wote wa Uungu, akidhihirisha nguvu ya neema ya Kiungu kwa wote wanaompokea na kumwamini Kristo kama Mwokozi binafsi. Kuna nafsi tatu zilizo hai za Utatu wa mbinguni; kwa Jina la hizi Mamlaka tatu kuu—Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu—wale wanaompokea Kristo kwa imani iliyo hai hubatizwa, na Mamlaka hizi tatu hushirikiana na raia wa mbinguni wanaomtii **Mungu** katika juhudi zao za kuishi maisha mapya ndani ya Kristo. **— Special Testimonies, Series B, Na. 7, uk. 62-63 (1905).** {*EVsw 615.1*}

Mwana wa Mungu Aliyekuwepo Kabla, Asiye na Mwanzo Wala Mwisho

Kristo ni Mwana wa **Mungu** aliyekuwepo kabla ya mwanzo wa mambo yote, milele zote, asiye na chanzo wala mwanzilishi..... Katika kuzungumza juu ya uwepo Wake kabla ya kuzaliwa duniani, Kristo huturudisha katika enzi zisizo na tarehe, yaani milele zote huko nyuma. Anatuhakikishia (Kristo) kwamba hakukuwa na wakati wowote ambapo Yeye (Kristo) hakuwa katika ushirika wa karibu na **Mungu** wa milele. Yeye (Kristo) ambaye sauti Yake Wayahudi walikuwa wameisikiliza (kwa miaka maelfu), alikuwa ameishi na **Mungu** kama nafsi iliyoishi pamoja Naye (Mungu Baba). **— The Signs of the Times, Agosti 29, 1900.** {*EVsw 615.2*}

Yeye alikuwa sawa na **Mungu**, asiye na mwisho, na Mwenye uwezo wote.... Yeye ni Mwana wa milele, |Asiye na mwanzo, Amekuwepo Mwenyewe, bila Kuumbwa (self existent) . **— Manuscript 101, 1897.** {*EVsw 615.3*}

Tangu Milele

Ingawa Neno la **Mungu** linazungumzia juu ya ubinadamu wa Kristo alipokuwa duniani, pia linasisitiza Uwepo Wake kabla ya kuumbwa Uumbaji wa chochote. Neno alikuwepo kama **Mungu**, naam, Mwana wa **Mungu Milele**, katika umoja na ushirika kamili na Baba. Tangu milele alikuwa Mpatanishi wa agano, Yule ambaye katika Yeye mataifa yote ya dunia—Wote Wayahudi na watu wa Mataifa—kama wakimkubali, wangepata baraka. “Naye Neno alikuwako kwa **Mungu**, Naye Neno alikuwa **Mungu**.” Kabla ya kuumbwa kwa wanadamu au malaika, Neno alikuwa pamoja na **Mungu**, Naye alikuwa **Mungu**. **— The Review and Herald, Aprili 5, 1906.** {*EVsw 615.4*}

Kristo aliwaonyesha kwamba, ingawa katika maisha Yake ya kianadamu walidhania kuwa hayakufikia miaka hamsini, uhai Wake wa Uungu hauwezi kupimwa kwa hesabu za kibinadamu. Uwepo wa Kristo kabla ya kuutwaa/kuvikwa mwili hauwezi kupimwa kwa namba au idadi ya miaka. — **The Signs of the Times, Mei 3, 1899.** {*EVsw 616.1*}

Uzima wa Asili, Usioazimwa, Usionakiliwa Kutoka kwa Mwingine, au Usiotoka kwenye chanzo cha Kingine chochote

Yesu alisema, “Mimi Ndimi ufufuo, na uzima.” Katika Kristo kuna uzima wa asili, usioazimwa, usiotegemea chanzo Kutoka nafsi au kitu chochote kingine. “Yeye aliye na Mwana anao uzima.” Uungu wa Kristo ndio uhakika wa muumini wa uzima wa milele. **— The Desire of Ages, uk. 530 (1898).** {*EVsw 616.2*}

Pamoja na Baba Kule Sinai

Walipofika (Israeli) Sinai, Alitumia fursa hiyo kuwakumbusha upya matakwa Yake. Kristo na Baba, wakiwa wamesimama pamoja juu ya mlima, kwa utukufu na uzito wa hali ya juu, walitangaza Amri Kumi. **— Historical Sketches, uk. 231 (1866).** {*EVsw 616.3*}

Mamlaka za Milele Za Wakuu na za Utatu

Mamlaka za milele za Wakuu wa mbinguni—**Mungu**, Kristo, na Roho Mtakatifu—waliwapa [wanafunzi] nguvu zaidi ya zile mwanadamu anayekuwa anayekufa huwa nazo... na wangesonga mbele nao katika kazi hiyo, wakiusadikisha ulimwengu juu ya dhambi. — **Manuscript 145, 1901.** {*EVsw 616.4*}

Uwepo wa Nafsi Halisi wa Roho Mtakatifu

Tunapaswa kufahamu kuwa Roho Mtakatifu, ambaye ni nafsi sawa kama **Mungu** alivyo nafsi, anatembea miongoni mwetu hapa. **— Manuscript 66, 1899** (Hotuba kwa wanafunzi wa Shule ya Avondale). {*EVsw 616.5*}

Roho ni nafsi kwa kuwa hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa **Mungu**; **Warumi 8:16.** Wakati ushuhuda huu unapokuwa unabebwa, hubeba ushahidi wake wenyewe. Wakati huo tunaamini na tuna uhakika kwamba sisi ni watoto wa **Mungu**.... {*EVsw 616.6*}

Roho Mtakatifu ana nafsi, la sivyo hangeweza kushuhudia kwa roho zetu na pamoja nazo kwamba sisi ni watoto wa **Mungu**. Pia ni lazima awe nafsi ya Kiungu, la sivyo hangeweza kuchunguza mambo ya **Mungu** yaliyo sirini mwa Mungu. “Kwa maana ni nani miongoni mwa wanadamu anayeweza kujua mambo ya mwanadamu isipokuwa roho ya mwanadamu iliyo ndani yake? Vivyo hivyo, mambo ya **Mungu** hakuna mtu anayejua isipokuwa Roho wa Mungu.” **— Manuscript 20, 1906.** {*EVsw 617.1*}

Nguvu ya Mungu Katika Nafsi ya Tatu

Mkuu wa nguvu ya uovu anaweza kuzuiwa tu kwa nguvu ya **Mungu** katika nafsi ya tatu ya Uungu, yaani, Roho Mtakatifu. **— Special Testimonies, Series A, Na. 10, uk. 37 (1897).** {*EVsw 617.2*}

Kushirikiana na Mamlaka Tatu Kuu za Mbinguni

Tunapaswa kushirikiana na mamlaka tatu kuu zaidi zilizo mbinguni—Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu—na nguvu hizi zitafanya kazi kupitia sisi, kutufanya watendakazi pamoja na **Mungu**. **— Special Testimonies, Series B, Na. 7, uk. 51 (1905).** {*EVsw 617.3*}

Jumuiya za Siri-Vyama vya Siri

Hatari za Jumuiya za Siri

Amri ya Bwana isemayo, “*Msifungiwe nira na wasioamini*,” hairejeli tu ndoa kati ya WaKristo na watu wasio wa **Mungu**, bali pia ni kwa mikataba yote ambayo wahusika wanakuwa na uhusiano wa karibu na wa ndani, na ambayo inahitaji umoja wa roho na matendo.... {*EVsw 617.4*}

Bwana anasema kupitia nabii Isaya: “**Isaya 8:9-13** *Fanyeni ghasia, enyi kabila za watu, Nanyi mtavunjwa vipande vipande; Tegeni masikio, ninyi nyote wa nchi zilizo mbali; Jikazeni viuno, nanyi mtavunjwa vipande vipande; Jikazeni viuno, nanyi mtavunjwa vipande vipande. Fanyeni shauri pamoja, nalo litabatilika; Semeni neno, lakini halitasimama; Kwa maana* ***Mungu*** *Yu pamoja nasi. Maana BWANA aliniambia hivi, kwa mkono hodari, akanifundisha nisiende katika njia ya watu hawa, akisema, Msiseme, Ni fitina, katika habari za mambo yote ambayo watu hawa watasema, Ni fitina; msihofu kwa hofu yao, wala msiogope. BWANA wa majeshi Ndiye mtakayemtakasa; na awe Yeye hofu yenu, na awe Yeye utisho wenu.*” {*EVsw 617.5*}

Kuna baadhi ya watu wanaouliza kama ni sahihi kwa WaKristo kuwa wanachama wa FreeMasons na vyama vingine vya siri. Hebu wote hawa wazingatie mafundisho haya ya Biblia yaliyotajwa yaliyonukuliwa

hapo juu. Ikiwa sisi ni WaKristo kweli basi lazima tuwe WaKristo kila mahali, tukizingatia na kutilia umakini ushauri uliotolewa ili tufanye kuwa WaKristo kulingana na kiwango cha Neno la **Mungu**.... {*EVsw 618.1}*

Tulipokubali Kristo kuwa Mkombozi wetu, tulikubali pia sharti la kuwa watendakazi pamoja na **Mungu**. Tulifanya agano Naye kuwa kuwa Wake Bwana kikamilifu; kama watunza waaminifu wa neema ya Kristo, tufanye kazi kwa ajili ya kujenga ufalme Wake duniani. Kila mfuasi wa Kristo ameahidi kuweka roho, akili, na mwili yake kwa Yeye aliyetulipia fidia ya nafsi zetu. Tulijiandaa kuwa askari, kuingia katika huduma hai, kuvumilia majaribu, aibu, kashfa, kupigania vita vya imani, tukimfuata Kapteni wa wokovu wetu. {*EVsw 618.2}*

Katika muunganiko wako na vyama vya kidunia, je, unadumisha agano lako na **Mungu**? Je, uhusiano huo unalenga kukuleta wewe na wengine karibu na **Mungu**, au unapindisha shauku ya moyo wako na umakini wako kwa Mungu ? Je, unaimarisha muungano wako na mawakala wa mbinguni/Kiungu au unageuzia mawazo yako kuelekea kwa wanadamu badala ya **Mungu**? {*EVsw 618.3}*

Je, unamheshimu, unamtumikia na kumtukuza **Mungu**, au unamkosea heshima na kumtenda dhambi? Je, wewe unakusanya na Kristo, au unatawanya? Je, Mawazo yote, mipango, na matamanio, yaliyotolewa wakfu kwa ajili ya makundi haya, yamenunuliwa kwa damu ya thamani ya Kristo; lakini Je, wewe unamfanyia Mungu huduma unapoungana na watu wakana-Mungu na makafiri, watu wanaomtukana **Mungu**, wanywa pombe, walevi na watu waliojitoa kwa tumbaku? {*EVsw 618.4}*

Ingawa huenda katika vyama hivi kuna vitu vingi vinavyoonekana kuwa vizuri, pia kuna mengi yaliyochanganyima humo ambayo ambayo hutangua mema yote na kufanya makundi haya kuwa hatari kwa maslahi ya nafsi.... {*EVsw 619.1}*

Nawauliza nyinyi mnaoona raha mkiwa katika makundi haya, mnaopenda kukusanyika kwa ajili ya vicheko, ubunifu wa mizaha inayoonyesha werevu, raha, kula vyakula vingi na sherehe, Je, mnachukua Yesu pamoja nanyi mnapokwenda huko? Je, mnatafuta kuokoa nafsi za wenzenu? Je, hiyo ndiyo lengo la uhusiano wenu nao? Je, washirika wenu wanaona na kuhisi kuwa ndani yenu kuna roho hai ya Kristo katika maisha yenu? Je, ni dhahiri kuwa wewe ni shahidi wa Kristo, mtu wa watu wa pekee, mnaotamani mema? Je, ni inaonekana dhahiri kwamba maisha yako yanaongozwa kanuni za mafundisho ya Mungu , **"Luka 10:27** *Akajibu akasema, Mpende Bwana* ***Mungu*** *wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako*?" .... {*EVsw 619.2}*

Wale wasioweza kutofautisha kati ya yule anayemtumika **Mungu** na mtu asiye mtumishi Wake, huenda wakalogwa au kuvutwa na makundi haya yasiyo na uhusiano na **Mungu**, lakini hakuna MKristo wa kweli anayeweza kustawi au kufanikiwa katika mazingira hayo. Hewa ya mbinguni itoayo nguvu haipo hapo. Roho ya mtu huyo ni kavu, na anahisi hana unyonge kwa kutokuwa na Roho Mtakatifu kama vile milima ya Gilboa ilivyo mikavu bila umande na mvua. {*EVsw 619.3}*

Wakati mwingine mfuasi wa Kristo analazimishwa kutokana na hali fulani kushuhudia matukio ya starehe zisizo takatifu, lakini kwa moyo wa huzuni. Lugha inayotumika huko si lugha ya Kanani, na mtoto wa **Mungu** hatatafuta kamwe kuwa kwenye ushirika wa aina hiyo. Anapoingia mahali pasipo hiari yake mahali kama hapa, hebu na amwegemee **Mungu**, na Bwana atamlinda. Lakini hapaswi kamwe kuupoteza msimamo wake kwa kutoa dhabihu kanuni zake, haijalishi anatahiniwa kwa majaribu magumu kiasi gani. {*EVsw 619.4}*

Kristo hatamwongoza mfuasi Wake kuchukua kiapoambacho kitamwunganisha na watu ambao hawana uhusiano na **Mungu**, wasiokuwa chini ya ushawishi wa Roho Mtakatifu. Kigezo pekee sahihi cha tabia ni sheria takatifu ya **Mungu**, na haiwezekani kabisa kwa mtu yeyote anayefuata sheria hiyo ya Mungu kama kanuni ya maisha yake, kuuungana kwa ujasiri na ushirika wa kidugu wa dhati na watu wanaoigeuza Kweli ya **Mungu** kuwa uongo, na kuchukulia mamlaka ya **Mungu kama jambo lisilokuwepo au lisilo na maana**. {*EVsw 620.1}*

Kuna korongo kubwa linalosimama kati ya mtu wa dunia na yule anayemtumika **Mungu** kwa unyofu. Kuhusu masuala makubwa-- **Mungu**, ukweli, na uzima wa milele, mawazo, huruma na hisia zao hazina maelewano. Kundi moja linaandaliwa kukomaa kama ngano kwa ajili ya ghala la **Mungu**, lingine kama magugu ya sumu kwa moto wa maangamizi. Je, kuna uwezekano wa umoja wa madhumuni au matendo kati yao? **"Yakobo 4:4** *Enyi wazinzi, hamjui ya kwamba kuwa rafiki wa dunia ni kuwa adui wa* ***Mungu****? Basi kila atakaye kuwa rafiki wa dunia hujifanya kuwa adui wa* ***Mungu***? **"Luka 16:13** *Hakuna mtumishi awezaye kutumikia mabwana wawili; kwa maana, ama atamchukia huyu na kumpenda huyu, ama atashikamana na*

huyu na kumdharau huyu. Hamwezi kumtumikia ***Mungu*** *na mali.”* **—Should Christians Be Members of Secret Societies? pp. 3-10. (1892). {*EVsw 620.2*}**

Kutengana Kwa Hali Dhahiri

Jioni nilikutana na ndugu _____ na kumwambia nina kitu kutoka kwa Bwana kwa ajili yake. Akaniambia, “Mbona usiniambie sasa?” Nilikuwa dhaifu, lakini alikaa _____, maili kumi kutoka jengo la shule ambalo lingekuwa nyumba yangu. Nilisimama na kumsomea kurasa hamsini za barua, kwa kurejelea kuhusu ofisi na watendakazi wa ofisi na nilibainisha watendakazi fulani waliokuwa wakifanya kazi ofisini (rejelea inahusu mawasiliano ambayo yapo hapa chini). {*EVsw 620.3*}

Nilikazia ... kwa uwazi na maneno wazi kuhusu kazi yake ya zamani na hasara iliyotokea kwa ofisi. Uhusiano wake na Free Masonry ulikuwa umemeza muda wake na kumfanya awe butu kabisa katika uelewa wake wa kiroho. Mawazo yake, nia yake, akili yake vilikuwa kwenye mwili huu, katika uhusiano huu wa chama cha free mason; na palikuwa na watu wasio na Mungu humo, wale wasio na dini yoyote, watu wa pombe, na kila aina ya kundi la mamb tofauti. Alikuwa amejifunga na mashirika haya ya siri. Kuna kitu kimoja tu ambacho angeweza kufanya, nacho ni kuachana nao na kuwa upande wa Bwana; kwa maana hawezi kumtumikia **Mungu** na mali-mammon. {*EVsw 621.1*}

Alisema, “Ninakubali ushuhuda huu; nitatii maelekezo yake.” —**Manuscript 17, 1892.** {*EVsw 621.2*}

Ndugu _____ alikuwa katika hatarini, kama mtu aliyeelekea kupoteza balansi na kuangukia korongo. Nilijua ni kazi nzuri jinsi gani kushughulikia akili za binadamu, na nilishukuru wakati ilipokuwa salama kwangu kuwasilisha kwake hatari yake. Bwana wa mbinguni anatuambia tuogope kuhukumu wenzetu; sisi sote tuko kama watu wenye ukomo, na wenye makosa, na tunapaswa kujishuku wenyewe tunapaswa kuogopa kumkosea **Mungu** kwa kujeruhi roho za watoto Wake. Wao ni ununuzi wa Mwana wa **Mungu**, wanenunuliwa kwa damu Yake ya thamani, na hawapaswi kushutumiwa au kunyanyaswa kwa neno au tendo, kwa maana Bwana atawasimama kwaajili yao, ili kuwalinda-kuwatetea. {*EVsw 621.3*}

Jumatano nilivutwa kuzungumza juu ya kanuni ambazo tunapaswa kutumia katika kushughulikia akili na nia na kuziongoza kwa njia sahihi. Wengi duniani wana mapenzi kwa vitu ambavyo vinaweza kuwa vizuri tu, lakini mawazo yao huridhika na mambo hayo tu, na hawatafuta mema zaidi na ya juu ambayo Kristo anatamani kuwapa. Sasa hatupaswi kutufuta kwa uchokozi au ujeuri kwa kuwanyima au kuchukua vitu wanavyothamini. Waonyeshe uzuri na thamani ya ukweli. Wafunulie waone Kristo na uzuri Wake, ndipo watageuka upande mwingine na kuachana na kila kitu kitakachowavuta mbali Naye Bwana. **—Letter 23a, 1893.** {*EVsw 621.4*}

Ujumbe wa Pongezi

Nashukuru sana Baba yetu mkarimu wa mbinguni kwa kuwa amekupa nguvu kupitia neema Yake ili ujing’atue kutoka kwenye mikono ya chama cha Free Masons Lodge na kila kinachohusiana na shirika hilo. Haikuwa salama kwako kuhusika na chama hichi cha siri. Wale waliosimama chini ya bendera yenye damu ya Mfalme Immanuel hawawezi kuungana na Free Masons wala mashirika mengine ya siri. Muhuri wa **Mungu** aliye hai hauwezi kuwekwa kwa mtu yeyote anayehifadhi uhusiano huo baada ya nuru ya Ukweli kuangaza njia yake. Kristo hana mgawanyiko, na WaKristo hawawezi kutumikia **Mungu** na mali. Bwana anasema, “**2 Wakorintho 6:17-18** Kwa hiyo, Tokeni kati yao, Mkatengwe nao, asema Bwana, Msiguse kitu kilicho kichafu, Nami nitawakaribisha. Nitakuwa Baba kwenu, Nanyi mtakuwa Kwangu Wanangu wa kiume na wa kike, asema Bwana Mwenyezi.” —**Letter 21, 1893.** {*EVsw 622.1*}

Udanganyifu Kupitia Jumuiya za Siri

Ulimwengu ni ukumbi wa maonesho (theatre); wahusika, wakazi wake, wanajiandaa kuigiza sehemu zao katika drama kuu ya mwisho. Miongoni mwa umati mkubwa wa wanadamu hakuna umoja, isipokuwa pale watu wanapoungana pamoja ili kutimiliza makusudi yao ya ubinafsi-uchoyo. **Mungu** anaangalia. Makusudi Yake kuhusu raia Wake waasi yatatimizwa. Ulimwengu haujawekwa mikononi mwa wanadamu, ingawa Mungu anaruhusu vipengele vya mkanganyiko na kuchanganyikiwa kutawala kwa msimu. Nguvu kutoka chini inafanya kazi kuleta matukio makuu ya mwisho kwenye drama hii - Shetani akija kama Kristo, na kufanya kazi kwa udanganyifu wote wa udhalimu ndani ya wale ambao wanajifunga pamoja katika mashirika ya siri. Wale ambao wanaosalimu amri kwa mapenzi makali kwa ajili ya shirikisho wanatekeleza mipango ya adui. Sababu itafuatiliwa na matokeo. {*EVsw 622.2*}

Uovu karibu unafikia kikomo chake. Fujo na mkanganyiko umeujaza ulimwengu, na hofu ya kutisha kuu hivi karibuni itakuja juu ya wanadamu. Mwisho umekaribia sana. Sisi ambao tunaujua Ukweli tunapaswa kujiandaa kwa ajili ya kile kitakachoupasukia ulimwengu hivi karibuni kama mshangao mkubwa. — **Testimonies For The Church 8:27-28 (1904).** {*EVsw 623.1*}

Kupinga kwa ukali na Mafundisho ya Uongo

Kukabiliana na Udanganyifu wenye hila kwa Ukweli

Nimeelekezwa kusema nanyi kwamba sio jambo bora kuendelea kujadili maoni ya ngeni za upotoshaji na nadharia za ajabu na nadharia za kupotosha ambazo kwa miaka mingi zimekuwa zikiingia miongoni mwetu. {*EVsw 623.2*}

Si vyema kuhubiri kuhusu pantheismu (imani ya upagani kwamba Mungu sio nafsi na yumo ndani ya kila kitu) au kusoma nukuu kutoka kwa waandishi wanaoendeleza hoja hiyo na makosa ya kijanja na ya udanganyifu yanayoambatana nayo. Kauli hizi zitafanya mengi zaidi kuelimisha akili kuliko maelezo au nadharia zote ambazo wachungaji na walimu wetu wanaweza kutoa kuhusu mambo haya. {*EVsw 623.3*}

Unapojaribu kushugulika na hizi mada, utaongonzwa kurudia udanganyifu wa Shetani, na hivyo kumsaidia kueneza nadharia zake potovu kwa watu. Badala yake, amua kutokurudia kamwe makosa au uongo kamwe, bali kufundisha Ukweli daima. Jaza mioyo na akili za watu kwa Ukweli wa kipekee, ulio mzito na mtakatifu wa wakati huu. {*EVsw 623.4*}

Kazia ukweli wa sasa, ujio wa pili wa Kristo. Bwana anakuja upesi sana. Tuna muda mchache tu kuwasilisha Ukweli wa wakati huu—Ukweli ambao utaongoa roho. Ukweli huu unapaswa kuwasilishwa kwa usahili na unyenyekevu mkubwa, kama Kristo alivyouwasilisha, ili watu waelewe Ukweli ni nini. Ukweli utaondoa mawingu ya udanganyifu. {*EVsw 624.1*}

Wape watu Ukweli wa sasa. Zungumza Ukweli. Jaza akili zao na Ukweli. Jenga ngome za ukweli. Usilete nadharia za Shetani kwa akili ambazo hazipaswi hata kuzikia habari hizi. Wanachohitaji watu si maonyesho ya ujanja wa kutongoza watu wa Shetani, bali uwasilishaji wa Ukweli ulio katika Yesu. Kumbuka kuwa Shetani anaweza kutumikiwa vyema kwa uongo wake kurudia. Kadiri tunavyojiepusha kushugulika masuala haya ya upotoshaji na kuchukiza, ndivyo akili na kanuni zetu zitakavyobaki safi na wazi zaidi, na akili zetu hazitachafuliwa zaidi na kanuni zetu…….. {*EVsw 624.2*}

Pia, nimeonyeshwa kuwa hatupaswi kujihusisha na migogoro kuhusu nadharia hizi za umizimu zinazopotosha, kwa kuwa malumbano kama hayo itawachanganya watu tu. Mambo haya hayapaswi kuletwa katika. Ikiwa wachungaji wetu wanachukua muda wao kujifunza nadharia hizi za uongo na makosa, wengine wataondoka kutoka kwenye imani kwa kusikiliza roho zidanganyazo na mafundisho ya Shetani-mapepo. Hatupaswi kufanya kazi ya kuzikanusha Sio kazi ya mhubiri wa Injili kueneza kuzizungumzia nadharia za Shetani. {*EVsw 624.3*}

Inua Ukweli, utukuze Ukweli, na kusema, “Imeandikwa.” — **Letter 175, 1904.** {*EVsw 624.4*}

Uongo Lazima Uondolewe Barakoa Kwa Ustadi

Mtume Paulo alitufundisha kwamba “*wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo na mafundisho ya mashetani*. **1 Timothy 4:1**” Hili ni jambo tunalopaswa kulitarajia. Jaribu letu kubwa zaidi litatokana na wale waliokuwa watetezi wa Ukweli ila wanaugeuka na kuielekea dunia, na na kuukanyaga kwa chuki na kuudhihaki. {*EVsw 624.5*}

Mungu anayo kazi kwa watumishi Wake waaminifu. Mashambulizi ya adui yanapaswa kukabiliwa kwa Ukweli wa Neno la **Mungu**. Uongo unapaswa kufichuliwa; tabia yake halisi ionekane wazi, na nuru ya sheria ya Yehova ing'ae katika giza la maadili ya dunia hii. Tunapaswa kuwasilisha madai ya Neno Lake. Hatutakosa hatia kama tutapuuza wajibu huu adhimu. Ijapokuwa tunasimama ili kuulinda Ukweli, tukijitetea nafsi wetu wenyewe na kutimua vumbi jingi la shida bila sababu ya maana, kwa vile tu tumeita kubeba na kubeba aibu au mateso au kusingiziwa na kuwakilishwa vibaya. Hebu tusijihurumie, bali tuwe na wivu mkubwa kwa sheria ya Yeye Aliye Juu Zaidi. {*EVsw 625.1*}

Mtume asema, “2 Timotheo 4:3-4 *Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti*; *nao watajiepusha wasisikie yaliyo Kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo*.” Kila upande tunawaona watu

wakivutwa kwa urahisi na fikra za uongo wa kufikirika kwa wale wanaokanusha Neno la Mungu; lakini Ukweli unapowekwa mbele yao, hujaa hasira na kukosa subira. Lakini ushauri wa Paulo kwa mtumishi wa **Mungu** ni: “2 Timotheo 4:5 “*Bali wewe, uwe na kiasi katika mambo yote, vumilia mabaya, fanya kazi ya mhubiri wa Injili, timiliza huduma yako.*”... {*EVsw 625.2}*

Tunapaswa kuyathamini kwa uangalifu sana maneno ya **Mungu** wetu ili tusije tukayachafua kwa kuyaweka pamoja na uongo wa watu waliacha imani. Tunapaswa kuipinga roho na ushawishi wao kwa silaha ileile aliyotumia Bwana wetu aliposhambuliwa na mfalme wa giza—“Imeandikwa.” Tujifunze kulitumia Neno la **Mungu** kwa ustadi. Maagizo ni: **“2 Timotheo 2:15**

*Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na **Mungu**, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali Neno la Kweli.*” Lazima kuwe na kazi ya bidii, maombi ya dhati, na imani, ili kukabiliana na hila na udanganyifu wa walimu wa uongo, washawishi/watongozaji; kwa maana “*katika siku za mwisho, kutakuwa na nyakati za hatari.*” — **The Review and Herald, January 10, 1888. {*EVsw 625.3}***

Wenye Moyo dhati Huokolewa Kutoka Kwa Udanganyifu

Mbinu tunayoweza kutumia kumshinda yule mwovu ni ile ile iliyotumiwa na Yesu kushinda, - nguvu ya Neno. **Mungu** hatawali akili zetu bila ukubali wetu; bali kama tunatamani kujua na kufanya mapenzi Yake, ahadi zake ni zetu: "Mtaifahamu Kweli, nayo hiyo Kweli itawaweka huru." "Mtu akipenda kuyatenda mapenzi Yake, atajua habari ya yale mafunzo." **Yohana 8:32; 7:17**. Kupitia imani juu ya ahadi hizi, kila mtu anaweza kuokolewa kutoka katika mitego ya makosa na uongo na kutawaliwa na dhambi. {*EVsw 626.1}*

Kila mtu yupo huru kuchagua mamlaka ya kumtawala. Hakuna mtu ambaye ameanguka chini sana, hakuna ambaye ni mwovu sana kiasi cha kutoweza kupata ukombozi katika Kristo. Yule aliyepagawa, badala ya kutoa ombi, aliweza kutamka maneno ya Shetani tu; lakini bado kusihi kwa moyo wake ambako hakukutamkwa kulisikiwa. Hakuna kilio cha moyoni kinachotoka kwa mhitaji ambacho hakitasikiwa, hata kama anashindwa kutamka kwa maneno, kilio chake hakitaacha kusikiwa. Wale watakaoridhia kuingia katika mahusiano ya agano na **Mungu** wa mbinguni hawajaachwa katika nguvu za Shetani au katika udhaifu wao wa asili. Wanaalikwa na Mwokozi akisema, "Na Azishike nguvu Zangu, Afanye amani Nami; Naam, afanye amani Nami." Isaya 27:5. Roho wa giza watapambanavita kwa ajili ya mtu aliyepata kuwa chini ya miliki yao, lakini malaika wa **Mungu** watampigania mtu huyo kwa nguvu za kushinda. — **The Desire of Ages, uk. 258, 259 (1898). {*EVsw 626.2}***

Wale Wenye Udadisi Wanakiri Hatufahamu

Barua zimekuja zikihusu mambo ambayo **Mungu** hajatupa nuru juu yake, nasi tuna furaha kusema kwa waulizaji hawa: HATUJUI. Shauku kuu katika kila moyo inapaswa kuwa kumjua **Mungu** na kufanya kile Achotaka Yeye. Heri wale wanaosikia Neno la **Mungu** na kulishika... {*EVsw 626.3}*

Wale wanaopenda sana kudadidi mambo ili kujua mambo ambayo hayajafunuliwa katika Maandiko, mara nyingi ni wale wanafunzi wa juu juu tu kuhusiana na yale mambo yanayohusu maisha ya kila siku na utendaji wake. ……Tunapaswa kuufunulia ulimwengu kile ambacho **Mungu** ameona kuwa ni muhimu atufunuliwe. Hatufanyi mapenzi ya Baba yetu wa mbinguni tunapobashiri mambo ambayo Yeye ameamua kuyaficha kutoka kwetu. Ni fursa ya kila mtu kuwafunulia wengine kwamba ana moyo wa shukrani kwa zile Kweli za MUNGU za thamani, kwamba anathamini hazina ya uzima wa milele, kwa kuwa tayari kutoa kila dhabihu ili kupata thawabu ya uzima wa milele. — **Manuscript 104, 1898. {*EVsw 627.1}***

SEHEMU YA 19—MTENDAKAZI NA SIFA ZAKE

Roho ya Huduma

Kuhenyeka kwa Ajili ya Roho

Pale mchungaji aendapo kumtafuta kondoo aliyepotea, asiwe na nia ya juu juu tu, bali awe na shauku ya dhati na maumivu ya moyoni kwa ajili ya roho. Hili linahitaji uchunguzi wa kina wa moyo, na maombi ya dhati kwa **Mungu**, ili tumjue Yeye na nguvu ya neema Yake, “ili katika vizazi vijavyo aweze kuonyesha wingi wa neema Yake kwa fadhili Zake kwetu katika Kristo Yesu.” **—Letter 8, 1895. {*EVsw 628.1}***

Huruma kwa Wasiookoka

Lakini ni wachache mno kiasi gani kati yetu wanaoona wokovu wa wakosefu kwa nuru ambayo mbingu huitazama—kama mpango ulioanzishwa tangu milele katika akili ya **Mungu**! Ni wachache kiasi gani, walio moyo kwa moyo na Mkombozi katika kazi hii ya mwisho yenye uzito. Ni nadra kupata hata sehemu ya kumi ya watu wakiwa na huruma ambayo inapaswa kuwapo kwa ajili ya roho ambazo bado hazijaokolewa-1/10. Kuna wengi wa kuonywa, lakini ni wachache wanaohisi huruma na uchungu wa **Mungu** kwa kiwango cha kuwa tayari kuwa kitu au kutokuwa chochote ili tu waone nafsi zikipatikana kwa Kristo! **—Gospel Workers, uk. 116 (1915).** {*EVsw 628.2*}

Kujitoa wakfu, Upendo, na Kujikana Nafsi

Mtumishi wa **Mungu** anapaswa kutumia akili na maadili ya hali ya juu, kwa kadiri alivyojaliwa na asili, malezi, na neema ya **Mungu**; lakini mafanikio yake yatalingana na kiwango cha kujitoa na kujikana nafsi katika huduma Yake, zaidi ya vipawa vya asili au vya kujifunza... Neema ya **Mungu** ndiyo msingi mkuu wa nguvu ya wokovu; bila hiyo, juhudi zote za kibinadamu ni bure. **—Counsels to Parents, Teachers, and Students, uk. 537, 538 (1913).** {*EVsw 628.3*}

Upendo na Huruma/Sikitiko

Bwana anataka watu wajisahau wenyewe na wajikane nafsi zao katika jitihada za kuwaokoa wengine. Maisha yetu ni hasara zaidi ya kushindwa ikiwa tutapita duniani pasipo kuacha alama za upendo na huruma. **Mungu** hatafanya kazi na mtu mkali, mkaidi, asiye na upendo. Mtu wa namna hiyo huvuruga mfano ambao Kristo anataka watendakazi Wake wauonyeshe kwa ulimwengu.

Watendakazi wa **Mungu**, katika kila aina ya huduma wanayofanya, wanapaswa kuleta katika kazi zao wema, ukarimu, na upendo wa Kristo. {*EVsw 629.1*}

Mungu anawaita watoaji nuru, watakaoujaza ulimwengu kwa mwanga, amani, na furaha itokayo kwa Kristo. Yeye Atatumia watu wanyenyekevu, wanaotambua udhaifu wao, wasiodhani kazi ya **Mungu** inawategemea wao. Watu wa namna hiyo watakumbuka maadili ya maneno na matendo wanayodaiwa na **Mungu**. Wataonyesha kwamba Kristo anakaa mioyoni mwao, akiisafisha nafsi yote. **—Letter 197, 1902.** {*EVsw 629.2*}

Unyenyekevu wa Watoto

Na tufanye kazi kwa uwezo wote tuliojaliwa, tukitafuta kuifanya ile Kweli ya wakati huu kuwa wazi kwa wale wasioielewa. Baraka ya Bwana itakuwa juu ya kila nafsi atakayejishughulisha kwa uelewa katika kazi Yake... {*EVsw 629.3*}

Hebu na tukuze na tujifunze unyenyekevu wa watoto wadogo. Biblia Takatifu, Kitabu cha **Mungu**, ndicho Mwalimu wetu. Kwa wote watakaotembea kwa unyenyekevu na **Mungu**, Yeye Atawapa Roho Wake Mtakatifu na tawahudumia kupitia malaika watakatifu kuacha athari sahihi katika akili za wanadamu. **—Manuscript 77, 1909.** {*EVsw 629.4*}

Kufanya Bila Kusifiwa

Tunapaswa kufanya kazi yetu kwa uaminifu na uadilifu, hata kama hakuna mtu duniani wa kusema, “Umefanya vizuri au vyema.” Maisha yetu yanapaswa kuwa kama vile **Mungu** anavyotaka yawe—wema katika maneno, matendo ya fadhili na ya kufikiria wengine, na kuonyesha unyenyekevu, usafi, na upendo. Hivyo ndivyo tunavyomwakilisha Kristo kwa ulimwengu... {*EVsw 630.1*}

Wale wanaotaabika, walio mstari wa mbele katika kazi kuu ya wokovu wa roho, ndio ambao **Mungu** atawaheshimu. **—Barua 120, 1898.** {*EVsw 630.2*}

Hatari ya Kusifiwa kwa kutia chumvi au kujikomba kwa watu

Mtazame Kristo. Usimwangalie kwa msisitizo mchungaji fulani wa injili, ukianza kuiga mfano wake na matendo yake; kwa kifupi, usiwe kivuli chake. Mtu yeyote asikuvishe sura yake... {*EVsw 630.3*}

Usimsifu mtu yeyote; usimfagilie mtu yeyote; na usiruhusu mtu yeyote kukusifu au kukufagilia. Shetani atafanya vya kutosha katika jambo hili. Poteza mtazamo wa chombo (mtu anayetumiwa na Mungu), na tafakari juu ya Yesu. Msifu Bwana. Mpe **Mungu** utukufu. Imbeni nyimbo za sifa moyoni mwenu kwa **Mungu**.

Zungumzeni juu ya Kweli. Zungumzeni juu ya tumaini la Kikristo, mbingu ya Kikristo. **—Manuscript 8a, 1888.** {*EVsw 630.4*}

Hisia Zisijeruhiwewe Kirahisi

Hatupaswi kuruhusu hisia zetu kujeruhiwa kwa urahisi. Tunapaswa kuishi ili tuokoe roho za watu na siyo kuzilinda hisia, hadhi au jina letu. Tunapovutiwa na wokovu wa roho za watu, tutaacha kuweka moyoni mwetu tofauti ndogo-ndogo ambazo mara nyingi hutokea katika mahusiano yetu na watu wengine. Haijalishi kile ambacho wengine wanaweza kufikiria kutuhusu au kutufanyia,hakika hakipaswi kuuvuruga umoja wetu na Kristo, ushirika wa Roho.**—The Ministry of Healing, uk. 485 (1905).** {*EVsw 630.5*}

Roho ya Furaha na Shangwe

Tunapokuwa na hakikisho lililo wazi na angavu la wokovu wetu binafsi, tutaonekana kuwa watu wa furaha na shangwe, ambayo inampendeza kila mfuasi wa Yesu Kristo. Uwepo wa upendo wa **Mungu** ulioleta upole na unyenyekevu katika maisha ya vitendo utaacha athari katika akili za watu ambayo itakuwa harufu ya uzima iendayo uzimani. Lakini roho ya ukali na shutuma, ikidhihirishwa, itawageuza wengi kutoka katika Kweli na kuwa upande wa jeshi la adui. Ni jambo la kutisha! Kushugulika kwa uvumilivu na watu waliojaribiwa kunahitaji vita dhidi ya nafsi. **—Letter 1a, 1894.** {*EVsw 630.6*}

Upole na Unyenyekevu wa Moyo

Thamani ya kazi yetu haiko katika kufanya kelele kubwa duniani, wala kuwa na usongo na juhudi katika nguvu zetu binafsi. Thamani ya kazi yetu inatokana na kushukiwa kwa Roho Mtakatifu. Ina msingi wa kuamini **Mungu**, jambo linaloleta sifa takatifu katika akili, ili tuweze kuvumilia kwa subira mioyoni mwetu. Tunapaswa kuomba daima kwa **Mungu** atuongeze nguvu, kutufanya kuwa hodari katika nguvu Yake, kuwasha ndani ya mioyo yetu moto wa upendo wa Kiungu. Kusudi la kazi ya **Mungu** huendelezwa kwa mafanikio zaidi na wale walio wapole na wanyenyekevu wa moyo. **—Manuscript 38, 1895.** {*EVsw 631.1*}

Ni Kazi ya Mungu, Siyo Yetu

Hili ndilo jambo tunalotakiwa kulielewa: kwamba hii si kazi yetu, bali ni kazi ya **Mungu**, nasi ni vyombo tu mikononi Mwake ili kuitimiza. Tunahitaji kumtafuta Bwana kwa moyo wote, Naye Mwenyezi Mungu atatufanyia kazi. **—The Review and Herald, May 10, 1887.** {*EVsw 631.2*}

Sadaka au kujitoa Dhabihu Kila Hatua

Tunakaribia mwisho wa historia ya dunia hii, na kila idara ya kazi ya **Mungu** inapaswa kufanywa kwa kujitolea zaidi kuwa dhabihu kuliko ilivyowahi kufanyika. Kazi ya siku hizi za mwisho ni kazi ya kimishenari. Kweli ya sasa, kuanzia herufi ya kwanza hadi ya mwisho ya alfabeti yake, ndiyo juhudi ya kimishenari. Kazi inayopaswa kufanywa inahitaji kujikana nafsi katika kila hatua ya maendeleo. Watendakazi wanapaswa kutoka katika majaribu, wakiwa wametakaswa na kusafishwa, kama dhahabu iliyochomwa kwenye moto. **—The Review and Herald, November 18, 1902.** {*EVsw 631.3*}

Kufundisha na Kuyaishi Mafundisho Makuu ya imani (Doctrines)

Watumishi wa **Mungu** wanapaswa kuwa waangalifu sana kuhusu Mafundisho wanayofundisha, mfano wanaoutoa, na ushawishi wanaouacha kwa wale wanaoshirikiana nao. Mtume mkuu aliliomba kanisa na **Mungu** kushuhudia Ukweli na unyofu wa imani yake. **"1 Wathesalonike 2:10** *Ninyi ni mashahidi, na* ***Mungu*** *pia, jinsi tulivyokaa kwenu ninyi mnaoamini, kwa utakatifu, na kwa haki, bila kulaumiwa.*" **—The Review and Herald, Desemba 11, 1900.** {*EVsw 632.1*}

Kujiepusha na Shughuli Zinazokoroga-koroga

Sisi ni watendakazi pamoja na **Mungu**. Wale walioko katika huduma Yake wanapaswa kujitenga na shughuli za kibiashara zitakazowafunga-funga tabia yao isifanane na Kristo na hivyo kuwa ya hovyo ovyo. Wale wavuvi aliowaita Mwokozi waliziacha nyavu zao mara moja. Wale wanaojitoa kwa huduma ya injili hawapaswi kujihusisha na biashara zitakazoharibu maisha yao au kudumaza maendeleo yao ya kiroho katika kazi waliyoitiwa na Bwana. **—Letter 53, 1905.** {*EVsw 632.2*}

Kutokuwa dhati au kukosa Unyofu, ni Hatari ya Mauti

Hapapaswi kuwapo udanganyifu wowote wala njia ya inayopindapinda katika maisha ya mtendakazi. Ingawa kosa linaloshikiliwa kwa unyofu ni hatari kwa yeyote, kutokuwa mkweli au dhati katika Kweli ni hatari ya mauti. **—The Medical Missionary, January, 1891.** {*EVsw 632.3*}

Roho ya Ukali Humkana Kristo

Mtu anaweza kuzungumza kwa ufasaha kuhusu mafundisho, na anaweza kuonyesha imani kubwa katika nadharia, lakini je, ana upole na upendo wa Kikristo? Kama anaonyesha roho ya ukali na ya hukumu, basi anamkana Kristo. Kama mtu sio mpole, mwenye huruma nyororo, mwenye fadhila, mwenye uvumilivu, yeye si kama Yesu; anajidanganya mwenyewe. Roho yoyote iliyo kinyume na upendo, unyenyekevu, upole, na huruma nyororo ya Kristo, inamkana Yeye, haijalishi mtu huyo anadai nini. **—The Review and Herald, February 9, 1892.** {*EVsw 632.4*}

Zungumzeni Imani na Matumaini

Na tuwe waangalifu na maneno yetu. Tuseme maneno ya imani, nasi tutakuwa na imani. Kamwe tusikubali wazo la kukatishwa tamaa katika kazi ya **Mungu**. Kamwe tusitamke neno la shaka. Maneno hayo ni kama mbegu inayopandwa katika mioyo ya mzungumzaji na wasikilizaji, ambayo itazaa mavuno ya kukatisha tamaa na kutokuamini. **—Letter 77, 1895.** {*EVsw 633.1*}

Kukosoa Watendakazi Wenzetu Kunavunja Moyo

Ni haki au fursa yetu kusema maneno yatakayotia moyo wale tunaoambatana nao katika kazi; si haki yetu kusema maneno yatakayowavunja moyo. Si busara kujilinganisha na watendakazi wengine, tukiangazia mapungufu yao na kupinga mbinu zao za kazi. Haitakuwa jambo la ajabu kwa wale walio chini ya mizigo mizito na majaribu mengi, kufanya makosa mara kwa mara…... {*EVsw 633.2*}

Hebu na tujifunze mema yanayofanywa na ndugu zetu, nasi tuzungumze kuhusu hayo. —**Letter 204, 1907.** {*EVsw 633.3*}

Wivu na Shaka Husababisha Utengano

Hakuna kitu kinachorudisha nyuma na kulemaza kazi katika sehemu mbalimbali kama wivu, mashaka, na mawazo ya uovu dhidi ya wengine. Mambo haya yanaonyesha kuwa kutokuwepo kwa umoja miongoni mwa watendakazi wa **Mungu**. Ubinafsi ndio chanzo cha maovu yote. **—Letter 113a, 1897.** {*EVsw 633.4*}

Kudhuru Wenzetu kwa Njia Isiyorekebishika

Mtu yeyote asitawale au kuwa mkali anaposhughulika na watendakazi wa **Mungu**. Wale wanaopenda kulaumu wengine wakumbuke kuwa wao pia wamewahi kufanya makosa makubwa na ya kutisha kama yale wanayoyalaumu kwa wengine. Hebu na wainame mbele za **Mungu** kwa toba, wakimwomba msamaha kwa maneno makali waliyoyasema na roho isiyo na tahadhari waliyoionyesha. Kumbuka kuwa **Mungu** anasikia kila neno unalosema, na kwa kipimo unachotumia kuwahukumu wengine, nawe utahukumiwa…... {*EVsw 633.5*}

Je, hatupaswi kutatua matatizo yaliyopo kwa jitihada za kuponya waliojeruhiwa, badala ya kuwakatilia mbali viungo vyao, na kuwaacha vilema milele, huduma yao ikiwa imelemaa, ilhali wangeweza kurejeshwa katika hali bora? **—Manuscript 143, 1902.** {*EVsw 634.1*}

Kuwakosoa Wengine Hudhoofisha Kazi Yetu

Mipango na mbinu za watendakazi wa **Mungu** zinapaswa kutakaswa kabisa dhidi ya mbinu na sera za kidunia. Kazi yao inapaswa kufanywa kwa unyofu wa Kikristo. Kumbuka kwamba anayejifanya mkosoaji hujidhofisha mwenyewe kwa kiasi kikubwa. **Mungu** hajampa mtu yeyote, mwanamume au mwanamke, kazi ya kukosoa kazi ya wengine. —**The Review and Herald, September 2, 1902.** {*EVsw 634.2*}

Jaribu Maalum la Shetani

Ikiwa mtu anatamani kuwekwa mahali ambapo Mungu anaweza kumtumia, basi asiwakosoe wengine kwa kuonyesha udhaifu wao. Hili ni jaribu maalum la Shetani, analotumia kuzuia kazi ya **Mungu**. **—Manuscript 152, 1898.** {*EVsw 634.3*}

Kujitosheleza Kunabomoa Kazi

Tunahitaji watu watakaoimarisha na kuijenga kazi, sio kuivunja na kujaribu kuharibu kazi ambayo wengine wanajitahidi kuifanya. Tunahitaji wanaume na wanawake ambao **Mungu** anaweza kuwafanya kazi nao, ambao ardhi ya mioyo yao imelimwa na kuvunjwa. {*EVsw 634.4}*

Hatuhitaji watendakazi ambao lazima wasaidie na kubebwa na wale walioko katika imani kwa muda mrefu, wanaojiona kuwa wakamilifu. Kwa watu wa namna hiyo tutasema, "Kaeni huko huko mlipo." Tumeshughulika vya kutosha na aina hiyo ya watendakazi. Tunahitaji watendakazi ambao sio wabinafsi, wasio na kujitosheleza wenyewe. **—Manuscript 173, 1898.** {*EVsw 634.5}*

Kufanya Maendeleo ya Ujumbe kuwa magumu (complicating work)

Sifa za adui wa **Mungu** na wanadamu mara nyingi hujitokeza katika roho na mtazamo wa watu kwa wao kwa wao. Hujeruhi wengine kwa sababu hawashiriki asili ya Kiungu; na hivyo huvuruga ukamilifu wa tabia zao wenyewe. Wanaleta matatizo kwao wenyewe, na kufanya kazi kuwa ngumu na yenye taabu, kwa sababu wanachukulia roho yao na mapungufu yao ya tabia kuwa ni fadhila za thamani, ambazo wanapaswa kuzishikilia na kuziendeleza..... {*EVsw 635.1}*

Watu hufanya kazi ya kuendeleza Kweli kuwa ngumu mara kumi zaidi kuliko ilivyo, kwa kujaribu kuchukua kazi ya **Mungu** mikononi mwao na kuiacha mikononi mwa **Mungu**. Hufikiri lazima wawe wakibuni jambo kila mara ili kuwafanya watu wafanye kile wanachodhani watu hao wanapaswa kufanya. Muda unaotumika kwa njia hiyo hutumika kufanya kazi kuwa ngumu zaidi; kwa sababu Mkuu Mkuu wa kazi ameondolewa katika utunzaji wa urithi Wake. Watu huchukua jukumu la kurekebisha tabia mbovu za wengine, na huishia kuzifanya kuwa mbaya zaidi. Ingekuwa bora zaidi kuwaacha **Mungu** afanye kazi Yake; kwa kuwa hawamwoni mtu yeyote kuwa na uwezo wa kuumba upya tabia. **—General Conference Bulletin, February 25, 1895.** {*EVsw 635.2}*

Kuchongwa na Kusuguliwa Katika Huduma

Wale walio na dosari katika tabia, mwenendo, mazoea, na matendo, wanapaswa kukubali ushauri na maonyo. Dunia hii ni karakana ya **Mungu**, na kila jiwe litakalotumika katika hekalu la mbinguni, ni lazima lichongwe na kusuguliwa na kung'arishwa (polish), hadi liwe jiwe la thamani lililojaribiwa, linalofaa kwa nafasi yake katika jengo la Bwana kama tofali. Lakini tukikataa kufundishwa na kufinyangwa, tutakuwa kama mawe yasiyoweza kuchongwa na kusuguliwa, ambayo mwisho wake yatatupwa pembeni kwani hayana faida au manufaa. **—The Youth's Instructor, August 31, 1893.** {*EVsw 635.3}*

Neema utamaduni/kuelimishwa **na Ukarimu**

Mfano Mkuu Wetu — Kristo aliishi maisha yanayoendana kikamilifu na mafundisho Yake ya Kiungu. Bidii Yake haikumpelekea kuwa na hasira au mihemko. Alionesha uthabiti bila ukaidi au kuchukiza watu, ukarimu bila udhaifu, huruma nyoror na hisia za upendo bila kuwa na hisia nyepesi zisizo na msingi. Alikuwa mtu wa kijamii sana-urafiki na kuchangamana na watu (social); lakini alimiliki heshima ya ndani iliyozuia mazoea ya kupita kiasi. Unyenyekevu Wake haukupelekea kuwa mlaghai au mkali. Hakufuata namna ya dunia hii; lakini hakuwa mpuuzi kwa mahitaji ya wale wadogo miongoni mwa wanadamu. Alikuwa macho kwa mahitaji ya wote. — **Manuscript 132, 1902.** {*EVsw 636.1}*

Mfano Ulio Kamili — Tangu utotoni hadi utu uzima, Kristo aliishi maisha yaliyo mfano kamili wa unyenyekevu, bidii ya kazi na tasnia, na utii. Daima alifikiria na kujali wengine, daima alijikana nafsi. Alikuja akiwa na muhuri wa mbinguni, si kutumikiwa bali kutumika... {*EVsw 636.2}*

Maisha yasiyo ya ubinafsi ya Kristo ni kielelezo kwa wote. Tabia Yake ni mfano wa tabia tunazoweza kuunda tukifuata nyayo Zake. — **Manuscript 108, 1903.** {*EVsw 636.3}*

Heshima/hadhi, Adabu, na Ustaarabu — Hakikisha unalinda heshima ya kazi hii kwa maisha yaliyo nadhifu na mazungumzo ya Kiungu. Usiogope kuinua kiwango. Familia zinazoshiriki katika kazi ya kimishenari zinapaswa kufikia mioyo ya watu. Roho ya Yesu inapaswa kujaza nafsi ya mtendakazi; ni maneno ya huruma nyororo na upole, uonyeshaji wa upendo usio na ubinafsi kwa roho za watu, vinavyobomoa kuta za kiburi na ubinafsi, na kuwaonesha wasioamini kwamba tunao upendo wa Kristo; ndipo Kweli itaingia moyoni. Hii ndiyo kazi yetu, na ni utimilifu wa mpango wa **Mungu**. Lazima tuondoe ujeuri, mambo ya hovyo ovyo (kuwa rafu) na ukorofi. Tunapaswa kuenzi adabu, ustaarabu/uungwana, na heshima ya Kikristo. Jiepushe na kuwa mkali au mkweli kupita kiasi kwamba usijali hisia za watu, bali unajisemea lolote na kukosoa au kuzungumza kila kinachokuja kichwani (blunt). Usichukulie tabia hizo kuwa ni fadhila; kwa

maana **Mungu** hazioni hivyo. Jitahidi kuepuka kumkosea yeyote bila sababu. — **The Review and Herald, November 25, 1890.** {*EVsw 636.4}*

Kristo Mfano Wetu wa Maadili na miiko mizuri ya uungwana katika jamii (etiquette) — Ustaarabu wa Kweli wa fikra na mienendo hujifunzwa vyema zaidi katika shule ya Mwalimu wa Kiungu kuliko kwa kufuata tu sheria zilizowekwa. Upendo Wake unapojaza moyo huipa tabia ule ukamilifu wa umbo unaofanana na Wake Mwenyewe. Mafunzo haya huleta heshima ya asili ya mbinguni na hisia ya busara. Hutoa tabia tamu na mwenendo wa upole na uungwana ambao hauwezi kufikiwa na mapambo ya juujuu ya jamii za kisasa ambayo ni feki (Etiquette mfano-salimia na mkono wa kulia, ngoja uambiwe ingia ndani, ukimwona mzee anabeba kuni msaidie). **— Education, uk. 241 (1903).** {*EVsw 637.1}*

Adabu na Uungwana wa Kweli: Huruma na Ukarimu Mpana — Wengi wanaosisitiza sana adabu na miiko ya uungwana katika jamii huonyesha heshima ndogo kwa chochote kisichokidhi viwango vyao vya bandia hata kikiwa kizuri. Hii ni elimu ya uongo. Huchochea kiburi cha ukosoaji, ufinyu wa akili na upendeleo wa kibinafsi. {*EVsw 637.2}*

Kiini cha adabu ya kweli ni kuwajali wengine. Elimu ya kweli na ya kudumu ni ile inayopanua huruma na kuhimiza ukarimu wa wote. — **Education, uk. 241 (1903).** {*EVsw 637.3}*

Mguso laini na Wema — Nyote wawili mnahitaji kuwa na mguso wa upole na uungwana zaidi-genle touch. Maneno yenu yanapaswa kutuliza, sio kuumiza au kukasirisha. Hebu mioyo yenu ijazwe na upendo kwa roho. Kwa moyo wa huruma ya kina, fanyeni kazi kwa ajili ya wale walio karibu nanyi. Ukiona mtu anafanya kosa, mkaribie kwa njia aliyoweka Kristo katika Neno Lake, uzungumze naye kwa upole wa Kristo. Ombeni pamoja naye, mkiamini kuwa Mwokozi atawaonyesha njia ya kutoka katika shida hiyo. {*EVsw 637.4}*

Wahudumu wanahitaji neema nyingi ya **Mungu** ili kutimiza kazi yao kwa kukubalika. Mchungajii akiona waumini wa kanisa wanapingana, na asimamishe hali hiyo na kuleta uelewano, kazi yake itakuwa imepotea. Hebu asitoe ushauri mkali au amri. Sio lazima. Kazi hiyo sio tu imepotea, bali ina madhara zaidi... {*EVsw 638.1}*

Bwana anawaita kutenda kazi kwa ushawishi wa kuinua wengine. Pokeeni Kweli za Neno la **Mungu** mioyoni mwenu. Ni kwa njia hiyo tu mtaweza kuwa na nia ya **Mungu**. Jiwekeni chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu. Kisha mtakuwa na nguvu zaidi kwa ajili ya mema... {*EVsw 638.2}*

Mahali popote upendo wa Yesu utakapokuwa, kutakuwa na amani na raha. Pale ambapo upendo huu unathaminiwa, ni kama kijito cha maji katikati ya jangwa, kikibadilisha ardhi yenye ukame kuwa rutuba. — **Manuscript 105, 1902.** {*EVsw 638.3}*

Busara na Hekima Hugusa Mioyo — Busara na hekima huongeza mafanikio ya mtendakazi mara mia. Yule anenaye maneno sahihi kwa wakati sahihi, na kuonyesha roho sahihi, atakuwa na nguvu ya kuyeyusha moyo wa yule anayesaidiwa. — **Gospel Workers, uk. 119 (1915).** {*EVsw 638.4}*

Ukarimu kwa Tunaotofautiana kwa Mafundisho — Wale wanaotofautiana nasi kwa imani na mafundisho wanapaswa kutendewa kwa wema. Ni mali ya Kristo, na tutakutana nao katika siku ile kuu ya hesabu ya mwisho. Tutapaswa kutazamana uso kwa uso katika hukumu, na kuona kumbukumbu ya mawazo yetu, maneno na matendo yetu, si kama sisi tulivyoyaona sisi kwa mtazamo wetu, bali kama yalivyokuwa katika Ukweli. **Mungu** ametuwekea wajibu wa kupendana sisi kwa sisi kama Kristo alivyotupenda. — **The Youth's Instructor, Desemba 9, 1897.** {*EVsw 638.5}*

Bila Hisia binafsi na Ubinafsi-Uchoyo — Watu lazima wafanye kazi kulingana na sheria na mpango wa **Mungu** ikiwa wanataka kufanikiwa. **Mungu** atakubali tu juhudi zinazofanywa kwa hiari na kwa moyo mnyenyekevu, bila hisia binafsi wala ubinafsi. **— Letter 66, 1887.** {*EVsw 638.6}*

Vaa Viatu vya Injili — Ndugu yangu, nina tamanio kubwa kwamba uwe mtu anayeufuata moyo wa **Mungu**. Lazima ubadilishe maisha yako. Una Kweli yenye thamani ya kipekee ya kuiwasilisha, lakini unapaswa kuvaa viatu vya injili—miguu yako lazima "ivae maandalizi ya injili ya amani." Namna yako ya kuwahutubia au kuzungumza watu sio ile ambayo daima inapendeza kwa **Mungu**. Unahitaji kuhisi nguvu ya uongofu wa **Mungu** juu ya roho yako kila siku. Una nguvu nyingi za kimwili na nishati, lakini unahitaji neema nyingi ya Kristo, ili isemwe juu yako kama ilivyosemwa juu Yake, "Upole Wako umenifanya kuwa mkuu." Roho Mtakatifu anapoutawala moyo wako na kudhibiti hisia zako kali, utakuwa mwenye kufanana zaidi na Kristo. **— Letter 164, 1902.** {*EVsw 639.1}*

Utakatifu wa Kazi ya Mungu— Kushughulikia mambo matakatifu kama vile ni mambo ya kawaida ni kosa mbele za **Mungu**; kwa maana kile ambacho **Mungu** amekiweka wakfu kwa ajili ya huduma Yake ya kuupa dunia nuru ni kitakatifu. Wale walio na uhusiano wowote na kazi ya **Mungu** hawapaswi kutembea kwa hekima yao ya kibinadamu, bali katika hekima ya **Mungu**, vinginevyo watakuwa katika hatari ya kulinganisha vitu vitakatifu na vya kawaida, na kwa kufanya hivyo watakuwa wamejitenga na **Mungu**. — **The Review and Herald, September 8, 1896. {*EVsw 639.2*}**

Kujua Wajibu Mtakatifu — Vijana wa kiume wanaibuka kushiriki katika kazi ya **Mungu**, lakini baadhi yao hawana hata chembe ya ufahamu kuhusu utakatifu na uzito wa kazi hiyo... Wananena upuuzi mtupu (nosense), na kucheza na wasichana wadogo, ilhali (huku) karibu kila siku wakisikia Kweli za zilizo kuu na zenye kugusa moyo. — **Testimonies for the Church 3:473 (1875). {*EVsw 639.3*}**

Siyo Waigizaji Bali Walimu wa Neno — Ninaona kwamba lazima kuwe na matengenezo makubwa katika huduma ya injili kabla haijawa jinsi **Mungu** anavyotaka. Wahubiri katika mimbari hawana ruhusa ya kujifanya kama waigizaji kwenye kumbi za maonyesho ya drama, wakichukua misimamo na maonyesho ya sura yanayolenga kuleta hisia. Hawako katika mimbari takatifu kama waigizaji, bali kama walimu wa Kweli za **Mungu**. Kuna pia wahubiri wanaopitiliza kwa kuzungumza kwa unafiki ambao, wanapojaribu kumhubiri Kristo, hupiga kelele helo helo, na kupiga miguu chini, kuruka juu chini, na kupiga mimbari kana kwamba mazoezi hayo ya mwili yana faida yoyote. Matendo hayo hayaongezi uzito kwa Kweli inahohubiriwa, bali huwachukiza watu wa akili timamu na walioko juu kimaadili. Ni wajibu wa mtu anayejitoa kwa huduma kuacha ukorofi, kukosa uungwana na tabia za kishenzi nje ya mimbari angalau (boistereous). **{*EVsw 640.1*}**

Harakati zisizo na mpangilio, na za kiajabu-ajabu na za kishenzi hazivumiliki hata katika maisha ya kawaida; sembuse katika kazi takatifu ya huduma ya injili. Mchungaji anapaswa kukuza neema, adabu, uungwana, na ustaarabu wa mwenendo. Hebu na aenende kwa heshima tulivu inayolingana na wito wake wa juu. Adhima, mamlaka ya Kiungu iliyochanganyika na unyenyekevu, viwe sifa za mwenendo wa mwalimu wa kweli za **Mungu**. **{*EVsw 640.2*}**

Wachungaji hawapaswi kuzoea kusimulia visa au hadithi katika mimbari (anectodes); huchafua uzito na adhama ya Kweli inayotolewa. Simulizi za visa au matukio yanayosababisha kicheko au mawazo mepesi kwa wasikilizaji yanapaswa kukemewa vikali. Ukweli unapaswa kuwasilishwa kwa lugha safi na ya kuvalishwa hadhi; na mifano itumiwayo iwe ya aina hiyo hiyo ya tabia. **{*EVsw 640.3*}**

Kama huduma ya injili ingekuwa ilivyo na inavyopaswa kuwa, walimu wa Kweli za Kristo wangekuwa wakifanya kazi kwa ushirikiano na malaika; wangekuwa washirika wa Mwalimu wao Mkuu. Kuna maombi machache sana kati ya wahubiri wa Kristo, na kujitukuza kupita kiasi. Kuna maombi machache sana ya Kweli, ya kutoka rohoni wa kulia machozi kwa kuomba kati ya Patakatifu na madhabahu Yoeli 2:17 "*Uwaachilie watu Wako, Ee Bwana, wala usiutoe urithi wako upate aibu, hata mataifa watawale juu yao, kwani kusema kati ya watu, Yuko wapi Mungu wao.*" Wahubiri wengi wanahubiri mafundisho ya imani marefu sana (doctrines) bila hata cheche ya moto wa kiroho wala upendo wa **Mungu**. Kuna ishara nyingi za mikono na simulizi za kuchekesha katika mimbari, na maneno machache sana kuhusu upendo na huruma ya Yesu Kristo. **{*EVsw 640.4*}**

Haifai tu kuhubiria watu; tunapaswa kuwaombea na kuomba pamoja nao; tusijitenge nao baridi, bali tuingie kwa huruma karibu na roho tunazotaka kuziokoa, tuwatembelee na kuzungumza nao. Mhubiri anayefanya kazi nje ya mimbari kwa namna inayofaa atafanikiwa mara kumi zaidi ya yule anayejifungia tu katika mimbari. — **The Review and Herald, August 8, 1878. {*EVsw 641.1*}**

Epuka Mizaha na Utani wa Kipuuzi

Roho ya Mizaha na Utani wa Kipuuzi—Roho hii ya mizaha na utani wa kipuuzi, ya wepesi na mambo ya kijinga, ni kikwazo kwa wenye dhambi, na ni kikwazo kikubwa zaidi kwa wale wanaoendekeza mielekeo ya mioyo yao isiyotakaswa. Ukweli kwamba wengine wameiruhusu tabia hii kujijenga na kuimarika hadi mzaha ukawa ni wa asili kama pumzi yao, haupunguzi madhara yake. Iwapo mtu anaweza kuonyesha neno moja la mzaha alilolisema Bwana wetu, au hali yoyote ya wepesi iliyojitokeza katika tabia Yake, ndipo aweze kuhisi kuwa wepesi na mizaha vinaweza kusameheka kwake. Lakini roho hii si ya Kikristo; kwa kuwa MKristo ni kuwa kama Kristo. Yesu ni kielelezo kamili, nasi lazima tufuate mfano Wake. MKristo ni kiumbe wa hali ya juu kabisa—mwakilishi wa Kristo. **{*EVsw 641.2*}**

Wengine ambao wamezoea mizaha na maneno mepesi ya kuchekesha, wanaweza kuonekana wakiwa na wadhifa wanapokuwa madhabahuni. Wanaweza kubadilika ghafla na kuingia kwenye mawazo ya mambo

makubwa ya kiroho, na wakaweza kuwasilisha mbele ya wasikilizaji wao Kweli zilizo kuu kabisa kuwahi kupewa wanadamu; lakini huenda wenzao waliovutiwa na kuungana nao katika mizaha ya kizembe, wasiwe na uwezo wa kubadilika kwa wepesi hivyo. Wanajihisi kuwa na hatia, akili zao zinavurugika, na hawako tayari kwa tafakari ya mambo ya mbinguni wala kuhubiri juu ya Kristo aliyesulubiwa. {*EVsw 641.3}*

Tamaa ya kusema maneno ya kuchekesha ili kuvuta kicheko, hata wakati masuala ya kazi ya Bwana yanajadiliwa—iwe ni katika mkutano wa kamati, mkutano wa bodi, au mkutano mwingine wa kiutendaji—sio ya Kristo. Ucheshi huu usio wa wakati wake unaharibu maadili. **Mungu** hatukuzwi tunapogeuza kila jambo kuwa la mzaha siku moja, halafu kesho yake tunakata tamaa, tukiwa hatuna mwanga wowote kutoka kwa Kristo, tukiwa tayari kulaumu na kunung'unika. **Mungu** hupendezwa watu Wake wanapoonyesha uimara, nguvu, na uthabiti wa tabia, na wanapokuwa na roho ya uchangamfu, furaha, na matumaini. {*EVsw 642.1}*

Iwapo akili imelengwa kwenye mambo ya mbinguni, maongezi pia yatafuata mkondo huo. Moyo utajaa furaha ya matumaini ya Kikristo, na ahadi kuu sana na za thamani sana zilizotolewa kwa ajili ya kututia moyo; na furaha yetu mbele ya rehema na wema wa **Mungu** haina haja ya kuzuiliwa—ni furaha ambayo hakuna mtu anayeweza kuitwaa kutoka kwetu. — **The Review and Herald, June 10, 1884.** {*EVsw 642.2}*

Wahudumu Wenye Mizaha

Kuna mtu mmoja katika konferensi yenu (sijui jina lake) ambaye hastahili kuwa sehemu ya huduma ya konferenze kama mhudumu, kwa sababu athari yake kwa wale wanaotafuta Ukweli si nzuri. Alinionyeshwa na maneno haya yakasemwa:

"Kazi ya **Mungu** haina haja ya wahudumu wenye mizaha wasioongoka. Roho ya mtu huyu haiendani hata kidogo na kazi ya heshima na wakfu tunayoshughulika nayo." Ukweli tunaodai kuamini hautaki watu wa mizaha wawasilishe mada. Mtu mmoja mwenye roho ya mchezo na wepesi anaweza kuambukiza makanisa kwa roho hiyo ya kijinga ambayo watu kumi wema watakuwa hawaa uwezo wa kuiondoa. {*EVsw 642.3}*

Nguvu ya **Mungu** inayobadilisha lazima ishuke juu ya mioyo ya wachungaji, kama sivyo, basi ni heri watafute kazi nyingine. Iwapo mabalozi wa Kristo wataelewa uzito wa kuwasilisha Kweli kwa watu, watakuwa watu wa heshima, wenye kufikiri kwa makini, wenye kiasi,wakishirikiana na **Mungu** katika kazi. Wakiwa na hisia ya kweli ya agizo alilowapa Kristo wanafunzi Wake, watafungua Neno la **Mungu** kwa kicho na kumsikiliza Bwana kwa maagizo, wakiomba hekima kutoka mbinguni, ili, wanaposimama kati ya walio hai na waliokufa, watambue kuwa watatoa hesabu mbele za Mungu kwa kazi itokayo mikononi mwao. {*EVsw 643.1}*

Mchungaji asiye na Yesu atafanya nini? Bila shaka hakuna. Na iwapo ni mtu wa mzaha na utani, basi hayuko tayari kutekeleza wajibu aliopewa na Bwana. Kristo alisema:

"*Maana pasipo Mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote*." **Yohana 15:15**

Maneno ya dhihaka yanayotoka kinywani mwake, hadithi zinazosimuliwa ili kuchekesha watu, maneno ya yasiyo na umakini na adabu kwa ajili ya kuchekesha tu— haya yanahukumiwa na Neno la **Mungu**, na hayana nafasi kabisa katika madhabahu takatifu…….. {*EVsw 643.2}*

Isipokuwa wahudumu wawe watu walioongoka na kutakaswa, makanisa yataugua na yatakuwa yanachungulia kaburi. Ni nguvu ya **Mungu** pekee inayoweza kuubadilisha mioyo ya wanadamu na kuijaza upendo wa Kristo. Ni nguvu ya **Mungu** pekee inayoweza kudhibiti tamaa na nia, kutakasa hisia, mapenzi na matamanio. Wote wanaohudumu ni lazima wanyenyekeze mioyo yao yenye kiburi, wawasilishe mapenzi yao kwa mapenzi ya **Mungu**, na wayafiche maisha yao pamoja na Kristo katika **Mungu**. {*EVsw 643.3}*

Lengo la huduma ni nini? Je, ni kuchanganya vichekesho na mambo ya dini/kiroho? Jukwaa la michezo ndilo pahali pa maonyesho ya namna hiyo (kumbi za drama). Iwapo Kristo amefanyika ndani ya moyo, iwapo Kweli pamoja na nguvu yake ya utakaso imeingia katika Patakatifu pa ndani la nafsi, hutakuwa na wahudumu wa mizaha—wala hutakuwa na watu wagumu, wenye hasira, wanaoudhika haraka na wenye mikunjo ya uso, wa kuzifundisha roho zilizo kifoni masomo yenye thamani kutoka kwa Kristo. **— Letter 15, 1890** {*EVsw 644.1}*

Kutembea kwa Tahadhari Maadili (Efe 5:15)

Ujasiri wenye ubaridi ambao umezoeleka, ishara za maigizo, wepesi wote wa kijinga na mizaha yote ni mambo ambayo mtu anayevikwa nira ya Kristo lazima ayaone kuwa "hayafai"—ni machukizo mbele za **Mungu** na ni kumkanusha Kristo. Hali hiyo huifanya akili isiyo imara kwa fikra nzito na kazi ya kina. Huwafanya watu kuwa wasiofaa, wa juujuu, na wagonjwa kiroho. {*EVsw 644.2}*

Hebu kila mhudumu na awe mtu wa utulivu. Anapojifunza maisha ya Kristo ataona umuhimu wa kutembea kwa tahadhari na kukesha. Lakini anaweza kuwa mwenye furaha, na mchangamfu wa Kweli, na wa matumaini, iwapo ataunganishwa na Jua la Haki—akionyesha sifa za Yeye aliyemwita kutoka gizani kuingia katika nuru Yake ya ajabu. Mazungumzo yake yatakuwa safi, yakiwa yameachana kabisa na maneno ya kihuni au misemo ya mtaani. — **Manuscript 8a, 1888** {*EVsw 644.3}*

Kutumika Kazini

Kujitolea kwa Kazi Yake - Kristo alijitosa kikamilifu katika kazi aliyokuja kuitimiza. Upendo Wake kwa kazi ya kuokoa wanadamu waliopotea ulionekana kila mara. —**Manuscript 132, 1902.** {*EVsw 644.4}*

Moyo wa Mtendakazi Kwenye Huduma- Chukulia kazi hii kama kazi ya Bwana, ukiifanya kwa makini na kwa uvumilivu. Hii ndiyo huduma ya kweli, ambayo Bwana atairidhia. Fanya kazi ukiwa na ufahamu wazi wa wajibu uliokuegemea, ukijua kwamba malaika wa **Mungu** wapo, kuweka muhuri wa mbinguni juu ya uaminifu, na kulaani kutoamini au kukosa uaminifu kwa namna yoyote. {*EVsw 644.5}*

Kwa kushika kazi hiyo kwa ujasiri na kuiingiza mioyo yetu kikamilifu, kazi hiyo huwa ya raha na starehe na huleta mafanikio. Hivyo **Mungu** hutukuzwa…{*EVsw 645.1}*

Unapofanya kazi yako kwa uaminifu, akili yako itakuwa kama akili ya Kristo. Kwa maombi na dua, tafuta baraka iliyohidiwa. Mwombe **Mungu** akupe ufahamu wa kweli kuhusu kazi inayopaswa kutekelezwa. Usikubali kuvutwa mbali au kuzuiliwa na ushawishi wowote wa unaopinga. Fanya sehemu yako kwa uaminifu katika kuleta baraka kwa wanadamu wenzako. Msifu **Mungu** kwa fursa ya kushirikiana Naye katika kazi Yake. Unapoiweka mioyo yenu yote katika kazi, mtapata ushirika wa Kweli na watendakazi wenzenu. Mtamwona Kristo ndani ya ndugu zenu..... {*EVsw 645.2}*

Kazi yoyote huwa ya kuchosha iwapo moyo haupo ndani yake. Wakati ni wa thamani sana, hakika ni kama dhahabu. Kuna kazi ya kufanya, na tunapaswa kuiingiza mioyo yetu yote katika kuitekeleza. Majukumu ambayo **Mungu** hutuwekea mbele yetu yapaswa kufanywa siyo kwa namna baridi na ya kuchosha na kujilazimisha kwa kuwa yabidi tu tuyafanye, bali kama huduma ya upendo. Leta nguvu zako kuu na huruma zako katika kazi yako. Na utagundua kuwa Kristo Yumo humo. Uwepo Wake utaifanya kazi kuwa nyepesi, na moyo wako utajawa na furaha. Utaifanya kazi katika maelewano na **Mungu**, kwa uaminifu, upendo, na utiifu. {*EVsw 645.3}*

Lazima tuwe WaKristo walio dhati/wanyofu, waaminifu kwa kazi zilizowekwa mikononi mwetu, tukimtazama daima Yesu, Mwanzilishi na Mkamilishaji wa imani yetu. Thawabu yetu haitegemei mafanikio ya nje yanayoonekana, bali hutegemea roho ambayo kazi imefanywa kwayo... {*EVsw 645.4}*

Nguvu zote za nafsi nzima lazima zitumike katika huduma isiyo ya ubinafsi. Kila kipawa kinapaswa kutumika. Boresha siku zijazo zaidi ya zile zilizopita. Wekeza vipawa vyako kwa ajili ya huduma, maana Kristo ana njaa ya roho. **—Manuscript 20, 1905**. {*EVsw 646.1}*

Bidii na Umakinifu - Bwana hapendezwi na kazi Yake kufanywa kwa uzembe au kwa njia hafifu na hovyo ovyo, kana kwamba ni mzigo wa kuchosha. Hatuna muda wa kupoteza kwa vitendo vya uvivu na kusitasita. Shauku tunayopaswa kuwa nayo kwa kila tunachofanya itafanya kazi yetu iwe yenye kuvutia na ya kufundisha. **—Letter 147a, 1897.** {*EVsw 646.2}*

Bidii ya Kudumu na Umakini wa Kazi - Pale ambapo kuna ukosefu wa bidii ya kudumu na umakini katika mambo ya kawaida ya maisha, hali hiyo hiyo hujitokeza katika mambo ya kiroho. **—Testimonies for the Church 2:498 (1870).** {*EVsw 646.3}*

Kudanganywa na Shetani - Baada ya kuonyeshwa kuhusu tabia yako ya kupenda kuenenda polepole na kutenda mambo kwa wastani huku ukipoteza fursa nyingi za kuboresha, nakisha unapoteza muda, hamasa, na kuchukua mambo kwa urahisi kiasi kwamba Shetani hukushinda tena na tena. Hii kazi unayoifanya, siyo ya kawaida miongoni mwa watu walio mbali na **Mungu**, wale wanaohitaji juhudi za dhati kwa ajili yao... {*EVsw 646.4}*

Kama hakuna matokeo ya kazi yako kwa muda wote uliokuwepo kwenye maeneo ya chini huko bondeni, basi huenda wewe sio mtu anayefaa kwa uwanja huo wa shamba la Bwana... {*EVsw 646.5*}

Je, umepanga kufanya mikutano hii kuwa yenye kuvutia kadri iwezekanavyo? Natumaini mzigo wa kazi uko moyoni mwako. Je, umekaa kwenye hema hapo kwenye eneo la kazi au umekuwa ukirudi nyumbani kila siku na kubeba mizigo isiyo sehemu ya kazi ya injili? Kazi hii katika huduma ya **Mungu**, kukabiliana na giza la maadili, inahitaji kujinyima, kujikana nafsi, kuhenyeka, juhudi za kudumu, na imani ya Kweli. Wengi hujidanganya kwamba wangeweza kufanya mambo makubwa kama wangepata fursa, lakini kila wakati kwao kuna kitu kilichowazuia; majaliwa ya **Mungu** yamewazunguka wasiweze kufanya walichotamani. Hatutarajii fursa kubwa kukutana nasi njiani, bali kwa vitendo vya haraka na vya nguvu lazima tuitumie kila fursa, kuunda nafasi na kushinda changamoto. {*EVsw 646.6*}

Unahitaji nguvu hai kutoka mbinguni. Katika kazi yetu, hatupaswi tu kupiga chuma wakati kikiwa na moto, bali kufanya chuma hicho kuwa moto kwa kukipiga. Mwendo wa taratibu, mlegevu, na ugoigoi hautatufanikisha katika kazi hii. Tunapaswa kuwa tayari wakati wote iwe ni katika msimu au nje ya msimu. Huu ni wakati wa dharura wa kazi. Kwa kusitasita na kuchelewa, tanapoteza nafasi nyingi nzuri... {*EVsw 647.1*}

Kinachokuzuia sana kutimiza wajibu wako ni kutokuwa na msimamo, udhaifu wa nia, na kutofanya maamuzi. Hebu **Mungu** na akusaidie kuvaa silaha zako za vita mwilini na kufanya kazi ya Bwana wako. —**Letter 13, 1886.** {*EVsw 647.2*}

Uaminifu—Bidii—Utii kwa Uongozi

Masuala ya Maslahi ya ufalme wa Kristo yanadai bidii na uaminifu kwa kiwango kikubwa zaidi, kama ambavyo mambo ya kiroho na ya milele ni ya thamani zaidi kuliko yale ya muda mfupi. Hakutakiwi kuwe na kazi dhaifu, wala hatua za kutembea polepole kama konokono kwa maana hali hiyo huweka hatarini roho zetu sisi wenyewe na roho za wengine... {*EVsw 647.3*}

Je, ni jenerali gani atakubali kuongoza jeshi wakati maafisa wake wanakataa kutii hadi wajiridhishe kwamba amri yake ina mantiki? Tabia kama hiyo hupelekea hasara kwa jeshi zima. Inawavunja moyo wanajeshi, na huwafanya waanze kujiuliza: “Je, hakuna njia bora zaidi?” Lakini hata kama kuna njia bora, bado amri lazima itekelezwe, au kushindwa na maangamizi hutokea. Muda mdogo wa kuchelewa, na faida iliyokuwa ipatikane inapotea. {*EVsw 647.4*}

Kila askari mzuri hutoa utii wa papo hapo na usiotetereka kwa kiongozi wake. Mapenzi ya kiongozi huwa ndiyo mapenzi ya askari. Wakati mwingine askari hushangazwa na amri aliyopokea, lakini hastahili kusimama kuuliza sababu ya amri hiyo. Hata amri ya kiongozi ikigongana na matakwa ya askari, hastahili kusitasita wala kulalamika akisema, “Sioni mantiki ya mipango hii.” Haipaswi kutoa visingizio na kuacha kazi ikiwa haijakamilika. Askari wa namna hiyo haatafikia viwango vya kushiriki katika vita vya dunia, sembuse kukubaliwa katika jeshi la Kristo. Kristo anapotoa amri, askari wake wanapaswa kutii bila kusita. Wanapaswa kuwa askari waaminifu, la sivyo Yeye Hataweza kuwapokea. Huru wa kuchagua hutolewa kwa kila mtu, lakini baada ya mtu kujiandikisha, anapaswa kuwa thabiti kama chuma, iwe ni kufa au kupona. —**Manuscript 7½, 1900.** {*EVsw 648.1*}

Nidhamu ya Akili na Mpangilio wa Kazi

Wale wanaofundisha Neno hawapaswi kukwepa nidhamu ya akili. Kila mtendakazi, au kundi la watendakazi, wanapaswa kwa bidii kuweka sheria na kanuni zitakazosaidia kuunda mazoea sahihi ya fikra na matendo. Mafunzo ya aina hiyo sio kwa vijana tu bali pia kwa wazee, ili huduma yao iwe haina makosa, na mahubiri yao yawe wazi, sahihi, na ya kushawishi. {*EVsw 648.2*}

Akili nyingine ni kama duka linalouza vitu vidogo vidogo vingi vya kale na vitu vya ajabu vinavyoleta udadisi mawazoni mwa watu, ambavyo huwa ni vingi na vimezagaa katika duka lote (curiosity shop). Ukweli ulio katika vipande vipande umekusanywa na kuwekwa humo, lakini hawajui namna ya kuwasilisha katika mtiririko wa kueleweka. Thamani ya mawazo haya imo katika uhusiano wake na mawazo mengine. Kila wazo na kauli vinapaswa kuunganishwa kama vile viungo vya mnyororo. Mhubiri anapotoa wingi wa mawazo ovyo mbele ya watu bila mwelekeo, kazi yake inakuwa ya bure na hivyo kupotea; maana wachache sana wataweza kuyaweka sawa. —**Review and Herald, April 6, 1886.** {*EVsw 648.3*}

Utendaji wa Kimuundo Huharakisha Mafanikio

Wapo vijana wa kiume na wa kike ambao hawana mpangilio katika kazi zao. Ingawa daima wako na shughuli nyingi, hawana matokeo ya maana. Wana mawazo yasiyo sahihi kuhusu kazi, na hudhani wanafanya kazi kwa bidii, lakini kama wangetumia mpangilio, na kutumia akili zao kwa kile walichopaswa kukifanya, wangeweza kutimiza mengi kwa muda mfupi. Kwa kucheleweshe mambo yasiyo ya msingi, hujikuta wamechanganyikiwa, na wenye haraka wanapotakiwa kutekeleza mambo muhimu zaidi. Wanaendelea tu "kufanya", na kudhani wanafanya kazi kwa bidii; lakini kuna matokeo machache ya kuonyesha watu. —**Youth's Instructor, August 31, 1893. {*EVsw 649.1*}**

Mpangilio na Muda Sahihi Huokoa Wakati

tunapaswa kuwa na watu ambao wataanza kazi kwa njia sahihi, waishikilie, na kuisukuma kwa nguvu. Kila kitu kinapaswa kufanywa kwa mpango uliofanyiwa tafakari na kuiva vyema, na kwa utaratibu. **Mungu** ameweka kazi Takatifu mikononi mwa wanadamu, na anataka ifanywe kwa makini. Mpangilio katika kila jambo ni muhimu. Usichelewe kwenye miadi. Katika kila ofisi au idara, muda usipotezwe kwa mazungumzo yasiyo ya lazima. Kazi ya **Mungu** inahitaji mambo ambayo mara nyingi haipati kwa sababu watu hawajifunzi kutoka kwa **Mungu** wa hekima. Wanaweka mambo mengi kupita kiasi katika maisha yao, wanaahirisha hadi kesho kile kinachohitaji kutekelezwa leo, na muda mwingi hupotezwa kwa maumivu wakijaribu kurekebisha walichopoteza... **{*EVsw 649.2*}**

Wengine wanapaswa kuacha njia za kufanya kazi polepole zinazotawala, na kujifunza kufanya mambo kwa haraka. Kasi ni muhimu kama vile bidii ilivyo. Kama tunataka kufanya kazi kama apendavyo **Mungu**, ni lazima tuifanye kwa haraka, lakini bila kukosa uangalifu. **—Manuscript 24, 1887. {*EVsw 650.1*}**

Kupanga Ratiba ya Kazi ya Kila Siku

Watu ambao hawajazoea nidhamu ya kazi na matumizi sahihi ya muda wanapaswa kuwa na sheria za kuwasaidia kuwa na ratiba na kasi katika kazi. George Washington, Rais wa Marekani wa kwanza, aliweza kufanya kazi nyingi za shuguli na biashara kwa sababu alikuwa makini katika kuweka utaratibu na mpangilio. Kila karatasi ilikuwa na tarehe na nafasi yake, na hakuna muda uliopotea kwa kutafuta kilichopotea. —**Gospel Workers, 277, 278 (1880). {*EVsw 650.2*}**

Kuhamasisha Jambo litokee katika Mpango wa Kazi

Mhubiri anapowekwa kwenye sehemu fulani ya shamba la Bwana, kazi yake anapewa kama mtendakazi mwaminifu kushirikiana na **Mungu katika shamba la Bwana**. Hapaswi kungojea kuambiwa kila kipengele cha kufanya amri kwa wanadamu bali kupanga kazi yake kwa hekima pale anapohitajika. Mwenyezi Mungu amekupa wewe nguvu za akili ili uzitumie. Mahitaji ya waumini na wasioamini yanapaswa kuchunguzwa kwa makini, na kazi yako inabidi ikidhi mahitaji yao. Unapaswa kumwuliza **Mungu**, na sio kwa mwanadamu anayeishi, nini cha kufanya na siyo mwanadamu. Wewe ni mtumishi wa **Mungu** aliye hai, si mtumwa wa mtu yeyote. Huwezi kufanya kazi ya **Mungu** kwa hekima ukiwa kivuli cha mawazo na maagizo ya mtu mwingine. Wewe upo chini ya **Mungu**. **—Letter 8, 1895. {*EVsw 650.3*}**

Kufanya mambo kwa wakati Huzuia Mkanganyiko

Miongoni mwa watendakazi kuna ukosefu wa ustadi, mkanganyiko, kutokuelewana, na kuchelewa. Mambo hayafanywi kwa wakati. Matokeo yake, matatizo na changamoto hutokea ambazo ni vigumu kuzitatua kwa sababu ya ukosefu wa ushirikiano wa pamoja. Hali hii, isipopata tiba, itaonekana na kuumiza zaidi siku za usoni kuliko zamani, kwa kuwa kazi itazidi kukua na uhitaji wa uelewano kamili utafanyika mkubwa zaidi. Tabia ya kukosa kushughulikia jambo maalum kwa wakati uliopangwa huongeza mara tatu ugumu wa kulitekeleza baadaye kwa usahihi bila kuacha kitu kikiwa hakijakamilika. **—Manuscript 24, 1887. {*EVsw 650.4*}**

Kuamka kwa Wakati wa Kawaida

Vijana wengine hawapendi utaratibu na nidhamu. Hawaheshimu kanuni za nyumbani kwa kuamka kwa saa iliyoamriwa. Hukaa kitandani wakijigaragaza masaa kadhaa baada ya mapambazuko, wakati ambapo kila mtu anapaswa kuwa ameamka. Huwasha taa za usiku, wakitegemea mwanga wa bandia kuchukua nafasi ya mwanga wa asili uliotolewa na **Mungu** kwa wakati unaofaa. Kwa kufanya hivyo, si tu kwamba wanapoteza fursa za thamani bali pia huongeza gharama za ziada. Lakini mara nyingi husema, "Siwezi kumaliza kazi yangu; nina kazi ya kufanya; siwezi kulala mapema." Kwa hiyo, wanalala usingizi mzito wakati wanapaswa

kuwa wameamka pamoja na asili na ndege wa asubuhi. Tabia hizi nzuri za utaratibu huvunjika; na dakika zinazopotezwa asubuhi huvuruga siku nzima. {*EVsw 651.1}*

Mungu wetu ni **Mungu** wa utaratibu, Naye anataka watoto Wake wajifunze kujileta wenyewe kwenye mpangilio na chini ya nidhamu Yake. Je, haitakuwa bora, basi, kuvunja tabia ya kugeuza usiku kuwa mchana, na saa safi za asubuhi kuwa usiku? —**The Youth's Instructor, January 28, 1897**. {*EVsw 651.2}*

Faida za Kufanya Mambo kwa Wakati Mwafaka

Kupanga kwa wakati mwafaka kunaweza kuimarisha Ukweli. Ushindi mwingi hupotezwa kwa kuchelewa. Patakuwepo na hali za dharura katika kazi hii. Hatua ya haraka na thabiti kwa wakati mwafaka italeta ushindi mkuu, ilhali kuchelewa na kupuuza huleta kushindwa kubwa na aibu kwa **Mungu**. **—Testimonies for the Church 3:498 (1875).** {*EVsw 651.3}*

Thamani ya Kutumia Daftari la Kumbukumbu

Kama vijana wangejifunza kuwa na mazoea ya utaratibu na mpangilio, wangeboresha afya yao, hali zao za moyo, kumbukumbu, hulka na tabia. {*EVsw 652.1}*

Ni wajibu wa kila mmoja kufuata kanuni madhubuti za maisha yao. Hii ni kwa ajili ya faida yao binafsi, kimwili na kimaadili.

Unapoamka asubuhi, tafakari, kadiri uwezavyo, kuhusu kazi utakayohitaji kutekeleza siku hiyo. Ikiwezekana, kuwa na daftari dogo la kuandika mambo yanayopaswa kufanyika, na jipangie muda wa kuyakamilisha. **—The Youth's Instructor, January 28, 1897.** {*EVsw 652.2}*

Kazi ya Mungu Haipewi Muda Maalumu

Mfumo wa saa nane haupati nafasi katika mpango wa mhudumu wa **Mungu**. Lazima awe tayari kwa huduma saa yoyote ile. **—Gospel Workers, 451 (1915).** {*EVsw 652.3}*

Kazi ya Yesu Jioni

Mchana kutwa Alikuwa akihudumia waliomjia; jioni Alihudumia wale ambao walikuja Kwake na jioni, aliwapa umakini wale ambao walikuwa wakifanya kazi ili kupata riziki kwa familia zao. **—The Ministry of Healing, 18 (1905).** {*EVsw 652.4}*

Kazi ya Bidii Husaidia Kujibu Maombi

Ingawa tunapaswa kuomba baraka ya **Mungu**, tunapaswa kuendeleza maombi yetu kwa kazi ya bidii, makini, na yenye shauku. **—Manuscript 25, 1895.** {*EVsw 652.5}*

Tusitegemee Miujiza

Kwa kawaida Mungu hafanyi miujiza kila mara ili kuendeleza Kweli Yake. Kama mkulima anasahau kulima ardhi baada ya kupanda mbegu, **Mungu** hafanyi muujiza kuzuia matokeo ya uzembe huo. Katika mavuno, atakuta shamba lake tupu. **Mungu** hufanya kazi kwa kufuata kanuni kuu alizoweka mbele ya wanadamu, na ni sehemu yetu kutengeneza mipango ya hekima ambayo imeiva vizuri, na kuendesha njia zitakazofanikisha matokeo anayokusudia. {*EVsw 652.6}*

Wale wasiofanya juhudi yoyote iliyodhamiriwa, bali wanangoja Roho Mtakatifu awasukume kwa lazima, wataangamia gizani. Tunawauliza wale wanaongojea muujiza, Je, mmejaribu njia zipi ambazo **Mungu** amewawekea? Tunawauliza wale wanaotarajia kazi isiyo ya kawaida ifanyike yaani ya miujiza, wanaosema tu, "Amini, amini," Je, mmeyatii maagizo ya **Mungu** yaliyo wazi?

Bwana amesema, "Usifanye hivi," na, "Fanya hivi." {*EVsw 653.1}*

Hebu kila mtu na ajifunze mfano wa talanta, na kutambua kwamba **Mungu** amempa kila mtu kazi—kila mtu amepewa vipawa vyake, ili kwa kutumia uwezo wake, aweze kuongeza ufanisi wake. Hupaswi kukaa tu, bila kufanya lolote katika kazi ya **Mungu**. **—Review and Herald, September 28, 1897.** {*EVsw 653.2}*

Msiwe Wazembe-Wavivu

Fanyeni kazi kwa ajili ya wale wanaopoteza maisha yao bure, wakitimiza nusu tu ya kile wangeweza kwa ajili ya Bwana. Jitahidini kuwahamasisha kuhusu wajibu wao. Ombeaneni na himizaneni, tena kwa bidii kadiri mnavyoona siku ile ikikaribia. Ndugu na ndugu, waambiane, "Njoo, mwezangu katika kazi, tuitimize kwa bidii yote kazi yetu; kwa maana usiku unakuja ambapo hakuna awezaye kufanya kazi." {*EVsw 653.3}*

Mtu anayependa kuongea akumbuke kuwa kuna wakati ambapo hana haki ya kuzungumza. Wapo wanaopoteza muda kwa kusimama bila kazi. Hebu Sauti ya mlinzi mwaminifu isikike, "Msiwe wazembe katika biashara; muwe wenye bidii rohoni; mkimtumikia Bwana."

Una kazi ya kufanya kwa ajili ya Bwana? Je, unajenga nyumba ambayo kazi Yake inaweza kuendelezwa? Funga mdomo wako. Usifanye wengine wavivu kwa kuwavutia kusikiliza mazungumzo yako. Wakati wa wengi hupotea mtu anapotumia ulimi wake badala ya zana zake za kazi. **—Manuscript 42, 1901.** {*EVsw 653.4}*

Wahudumu Wasijihusishe na Mambo ya Kidunia

Nataka kusema kwa Ndugu _____ na _____ kwamba kazi yao kubwa iko kwa watu wasiomjua Bwana. Wale wanaofanikiwa kufundisha ile Kweli ya Biblia wanapaswa kusimama mbele ya wale ambao hawajasikia ujumbe wa wakati huu. Lakini ndugu hawa niliowataja, ambao majina yao nimeyataja, wana kazi ya kufanya katika mkutano wa hema, ambayo hufanywa mijini ila wako hatarini kujiondolea sifa ya kufanya kazi waliyopewa na **Mungu**. Mzee ____ hakika_ atapoteza dira bila shaka ikiwa hataacha kujihusisha na kazi ambayo **Mungu** hamwombi afanye, kazi ambayo inahitaji kushughulika na mambo ya biashara. Kwa kujihusisha na kazi ya kidunia siyo hatakuwa anatimiza wito aliokabidhiwa na **Mungu**. Kutangaza ujumbe wa injili ndicho chanzo chake cha nuru na uhai wake. **—Manuscript 105, 1902.** {*EVsw 654.1}*

Kwa Lengo Moja—Jicho limekita kwa Utukufu wa Mungu

Ni kibarua cha kawaida ya Shetani kuzuia kazi ya **Mungu**, na kufanya kazi kwa ajili ya maangamizi ya binadamu. Mara nyingi wakati kazi inakuwa na mvuto mkubwa mahali fulani, Shetani hufanya ionekane kwa mtendakazi kuwa kuna jambo dogo nyumbani linalohitaji kuhudumiwa haraka. Kwa kuwa jicho la mtendakazi halijakazwa kwa utukufu wa **Mungu** pekee, huacha kazi isiyokamilika na kukimbilia nyumbani. Huenda akakawia kwa siku au hata wiki, na kazi aliyokuwa ameianza huharibika na kuchanganyikiwa. Kazi hiyo huwa haikamiliki tena, mshono hadi mshono wa kitambaa cha kazi unapotea unaachwa kuendelezwa mpaka mtu anaacha kazi. Hili humfurahisha adui. Naye Shetani, anapoona kuwa amefanikiwa kumfanya mtu aweke mambo ya kidunia kuwa ya kwanza, humtengenezea matatizo ya nyumbani, ili kumhangaisha zaidi na kumchanganya kabisa na kumtoa kabisa kwenye kazi... {*EVsw 654.2}*

Wakati roho zinachukua uamuzi kwa au dhidi ya Kweli, nawasihi, msijiruhusu kuvutwa mbali na uwanja wa kazi. Usiiache kazi kwa adui, hata kama kuna mtu mmoja amekufa nyumbani mwako. Kristo alisema, "Nifuate; waache wafu wawazike wafu wao." Laiti ungeweza kuona umuhimu wa kazi hii kama ulivyoonyeshwa kwangu, ganzi iliyoko juu ya wengi ingewatetemesha, na kungekuwa na kufufuka kutoka kwa wafu na uzima mpya ndani ya Yesu Kristo… {*EVsw 655.1}*

Tukisimama imara kama watendakazi wa **Mungu** tukisema, "Bwana ametupa ujumbe, hatuwezi kuwa walinzi waaminifu tukiacha nafasi yetu; tutaendeleza kazi hii kwa gharama yoyote," basi tutakuta kwamba malaika wa **Mungu** watatumikia familia zetu nyumbani, na kumwambia adui, "Simama huko mbali."— **Historical Sketches, uk. 127-128 (1886).** {*EVsw 655.2}*

Kujikita Katika Kazi Kuu-Jukumu lenye kipaumbele

Wokovu wa Nafsi Wapotea kwa Sababu ya Kugawanyika kwa Juhudi—Baadhi ya wachungaji wamejishughulisha na kazi ya kuandika wakati wa kipindi cha mwamko wa kidini, lakini mara nyingi maandiko yao hayakuwa na uhusiano wowote maalum na kazi iliyokuwa mbele yao. Hii ni kosa la dhahiri linalotoa ilani kwa kimulimuli; kwa kuwa nyakati kama hizo ni wajibu wa mchungaji kutumia nguvu zake zote kusukuma mbele kazi ya **Mungu**. Akili yake inapaswa kuwa wazi, na kuzingatia lengo moja la kuwaokoa watu. Iwapo mawazo yake yataelekezwa kwenye masuala mengine, wengi huenda wakapotea, ambao wangeweza kuokolewa kwa mafundisho ya wakati mwafaka. —**Testimonies for the Church 4:265 (1876).** {*EVsw 655.3}*

Hasara Inayotokana na Juhudi Zilizogawanyika—Kosa lako limekuwa hili: Mara tu unapoanza kampeni ya injili yaani Efoti, wewe huanza kuandika sana. Sasa, kama sehemu yako ya kazi ni kuandika, kama **Mungu**

amekuambia kama alivyomwambia Yohana, “Andika mambo haya,” basi jitolee kikamilifu kwa kazi hiyo, na usijaribu kufanya zaidi. Lakini kama unapaswa kutoa mahubiri, akili yako haina nguvu ya kutosha kuhimili mzigo wa kuhubiri, kutembelea na kuandika kwa wakati mmoja. Unapaswa kupumzisha akili yako kwa kiasi kikubwa unapojitosa kuwasilisha Kweli mpya na zenye kuchokoza kwa watu, ambazo kupokelewa kwake kunahitaji mtu kuchukua msalaba. Unahitaji kuchagua mada kwa uangalifu, kuyafanya mahubiri yako kuwa mafupi, na kufafanua wazi mambo muhimu ya mafundisho…..... {*EVsw 656.1*}

Ili kufanikisha kazi hii ni lazima ufanye jambo moja kwa wakati mmoja, ukilenga nguvu zako zote kwenye kazi hiyo. Uamuzi wako katika jambo hili umekuwa na dosari. Unapoanza mfululizo wa mahubiri, yafanye hayo kuwa kazi yako kuu. Usiandike barua au makala kwa magazeti, kwa kuwa hii hugawanya nguvu zako. Wazee _____ na _____ walisahihishwa kuhusu jambo hili. Bwana alinionyesha kuwa kazi muhimu ya kuwasilisha Ukweli ilikuwa ikiharibika mikononi mwao; si nusu ya nguvu waliiweka katika kazi yao kwa sababu walitumia muda mwingi kuandika barua. Kutembelea watu ndicho kiini cha huduma hii, yaani kazi muhimu; lakini muda wa ndugu hawa ulikuwa ukitumika karibu muda wote wakiandika, hali iliyowachosha, kuwanyima muda, na kuzuia kazi ya sasa badala ya kuisaidia. Watu waliporwa/walinyimwa maelezo wazi na yenye kusadikisha ya Maandiko, na sehemu ya ibada ya kazi ilipuuzwa... ... {*EVsw 656.2*}

Sababu ilikuwa hii: Walipotoka mimbari walitumia muda mwingi kuandika, wakijitetea kuwa walikuwa na kazi nyingi na kuchoka hivyo hawakuwa tayari kutembelea watu nyumba kwa nyumba. Matokeo yake walipokuwa mimbarini walikuwa wamechoka kiakili; hawakuwa tayari kufanya kazi ambayo **Mungu** angeweza kuiweka muhuri Wake. Hawakufanya jambo lolote kuwa wazi. Hata walipojihamasisha hadi kufikia kiwango cha juu cha msisimko, wakahubiri kwa sauti kubwa wakidhania mahubiri yao yalikuwa na nguvu. Waligusa hapa na pale, wakileta wingi wa mambo waliodhani ni ushahidi wenye kushawishi, lakini kwa kweli waliufunika Ukweli kwa wingi wa habari, kiasi kwamba hoja kuu haikueleweka. Kila walichowasilisha kilichanganya. Masomo mengi yaliletwa kwa mahubiri moja, kiasi kwamba hakuna hata hoja iliyothibitishwa wazi kwa wale wasioufahamu ukweli, walizungumza hili na lile, kila kitu walichokileta kilikuwa na modeli yaani kilibuniwa na kuwasilisha na kutolewa mfano bainishi na kanuni zake... Wakati Mada moja, hoja chache zilizofafanuliwa kwa uwazi na kufanywa wazi, zingekuwa na thamani zaidi kwa msikilizaji kuliko wingi wa maelezo unayoyaita ushahidi. **—Letter 47, 1886.** ... {*EVsw 657.1*}

Afya na Kanuni za Afya

Wainjilisti Hujaribiwa Kupuuzia Afya—Shetani anafanya kazi ili kuharibu. Hujitahidi kuelekeza mawazo ya wale wanaompenda **Mungu** na wanaohubiri injili kuwa wasiojali afya yao ya kimwili, ilhali afya hii ina uhusiano mkubwa sana na kiwango cha jumla cha maadili na wema. Wachungaji hutumia muda mwingi sana katika kuhubiri, na hatimaye huchoka kabisa…….. Ni kuwasilisha mahubiri marefu sana yanayochosha. Nusu ya chakula cha kiinjili kinachotolewa kingekuwa na athari ya faida kubwa zaidi. **—Letter 91, 1898.** {*EVsw 657.2*}

Kujikamua koo Katika kuzungumza kwa Jinsi ya Kuchosha katika Huduma ya Uinjilisti (strain on you) - Uchovu—Mikutano yako ya Jumapili usiku hukuletea uchovu mkubwa kwa sababu unalichosha sana koo lako, kwa kuwa huwa unajihamasisha hadi kiwango cha juu sana na kujiletea msongo. Kisha baada ya hapo hufuata hali ya kushuka kwa hisia, na hivyo ushirika wako na kanisa hauleti amani na haki... {*EVsw 658.1*}

Juhudi kubwa unazofanya katika maandalizi ya mikutano hazifanikishi kazi inayohitajika zaidi. Unaweza kusifiwa na kuinuliwa na watu, lakini hiyo sio ishara kuwa kazi yako ina mvuto sahihi. {*EVsw 658.2*}

Asema Bwana: “Ni lazima ujiepushe na hali ya kujihamasisha mno unapojitayarisha kuzungumza na watu.” **—Letter 51, 1902.** {*EVsw 658.3*}

Kuwa na Kiasi Katika Kazi ya Mungu —Watumishi wa Kristo hawapaswi kuipuuzia afya yao. Mtu asifanye kazi hadi kuchoka kupita kiasi kiasi cha kuharibu uwezo wa kufanya kazi baadaye. Usijaribu kusongamanisha kazi ya siku mbili katika siku moja. Mwishowe, wale wanaofanya kazi kwa uangalifu na kwa busara watakuwa wametimiza mengi tu kama wale waliotumia nguvu zao zote za kimwili na kiakili kiasi kwamba hawakubakiwa tena hifadhi ya nguvu za kutumia wakati wa dharura. **—Gospel Workers, uk. 244 (1915).** {*EVsw 658.4*}

Fanya Kazi kwa Akili—Kila mtendakazi anapaswa kufanya kazi kwa busara, kwa lengo moja tu, lile la utukufu wa **Mungu**. Anatakiwa kuzingatia sana kutotumia vibaya uwezo wake aliowekewa na **Mungu**. {*EVsw 658.5*}

Bwana angependa wewe, ndugu yangu, ufanye matengenezo katika njia yako ya kazi, ili uwe na akili iliyosawazika, tabia iliyonyooka kwa uwiano, na nguvu za kiroho za kushauri kwa hekima. Wanaume waliobobea katika maarifa ya Kweli ni wachache mno kiasi kwamba huwezi kujitoa dhabihu kwa kazi hadi kuanguka. Karibu kila wakati unalemea uwezo wako wa mwili na akili, kwa sababu unajiruhusu kuhisi mambo kwa uzito sana. Una mawazo yenye nguvu na unajitahidi sana katika mahubiri yako, jambo ambalo hufanya akili kukosa mapumziko, sauti hubakia kwenye kiwango cha juu, na sio tu wewe unachoka, bali pia watu wanaudhiwa na kusumbuliwa, hivyo kupunguza usikivu wao. Baada ya kushinikizwa kwa muda mrefu, mwili huchoka hakika matokeo huja baada ya kusumbua mwili wako, kwa sababu hujui jinsi ya kujipumzisha na kushuka chini taratibu baada ya hiyo mihemko uliyoipitia iliyokuweka juu kihisia. Kushuka kwa nguvu na hata sonona, hufuatilia hali ya msukumo wa juu wa hisia. {*EVsw 658.6*}

Usiruhusu kazi zako kuwa nzito isivyohitajika. Unajichosha katika kuandika kama ilivyo katika kuhubiri. **Mungu** hahitaji jambo hilo. Fuata kikamilifu sheria za afya, nawe utakuwa mpya na tayari kufanya kazi nzuri kwa ajili ya Bwana, ukiwa umeburudishwa; utakuwa na mana mpya ya kuwapa kondoo walioko katika malisho ya Kristo. **—Letter 39, 1887.** {*EVsw 659.1*}

Acha Nafasi kwa Mapumziko ya Lazima—Baadhi ya wahubiri wetu huhisi kuwa ni lazima kila siku wafanye kazi fulani ambayo wanaweza kuripoti kwenye konferensi. Na kwa sababu ya jitihada za kulazimisha hili, juhudi zao mara nyingi huwa dhaifu na zisizo na ufanisi. Wanapaswa kuwa na vipindi vya mapumziko, vipindi vya kuachana kabisa na kazi inayochosha. Lakini mapumziko haya hayawezi kuchukua nafasi ya mazoezi ya kila siku ya mwili. **—Gospel Workers, uk. 240 (1915).** {*EVsw 659.2*}

Kujiandaa kwa Majukumu ya Baadaye—Mhubiri anapokuwa amelemewa na mzigo mzito wa majukumu na wasiwasi, na kuchoka kimwili na kiakili, anapaswa kujitenga kidogo na apumzike kwa muda, si kwa ajili ya kujiridhisha binafsi, bali ili aweze kujiandaa vyema kwa kazi za baadaye. Tunaye adui makini, aliye makini kila mara hufuatilia hatua zetu, tayari kutumia kila udhaifu kama faida ya kufanya majaribu yake yawe na athari. Akili inapochoka kupita kiasi na mwili ukiwa dhaifu, huyasukuma majaribu yake makali zaidi kwa roho. Hebu mtumishi wa Bwana anapaswa kuilinda kwa uangalifu nguvu yake, na anapochoka kwa kazi, ajitenge kwa muda na apate ushirika wa karibu na Yesu. **—Gospel Workers, uk. 245 (1915).** {*EVsw 659.3*}

Epuka Mzigo wa Kufanya Kazi Kupita Kiasi—Nasikia habari za watendakazi ambao afya zao zinadhoofika kwa sababu ya mzigo mzito wanaoubeba. Jambo hili halipaswi kuwepo. **Mungu** anataka tukumbuke kuwa sisi ni wanadamu tunaokufa. Hatupasi kukumbatia kazi nyingi kupita kiasi kiasi kwamba tupate kuchosha kimwili na kiakili. Tunahitaji watendakazi wengi zaidi, ili baadhi ya mizigo iondolewe kwa wale ambao kwa sasa wamelemewa sana. **—The Review and Herald, April 28, 1904.** {*EVsw 660.1*}

Wakati wa Kupumzika, Mazoezi, na Majukumu ya Familia—Iwapo mhubiri, wakati wa mapumziko yake, atajihusisha na kazi katika bustani, shamba la matunda au shamba lake, je, anapaswa kukata sehemu ya mshahara wake kwa ajili ya muda huo? Bila shaka hapana, si zaidi ya pale anapofanya kazi zaidi ya muda katika huduma ya uchungaji. Wahubiri wengine hutumia saa nyingi kwa mapumziko ya dhahiri wakiwa wamestarehe kabisa, na ni jambo jema kwamba wapumzike watakapopata nafasi; kwa kuwa mwili usingeweza kuhimili mzigo mzito iwapo hakutakuwa na muda wa kupumzika. Kuna saa za siku zinazoleta mzigo mkubwa wa kazi, ambao mhubiri halipwi mshahara wa ziada kwa ajili yake, na kama atachagua kuchanja kuni au kufanya kazi ya bustani kwa saa kadhaa, hiyo ni haki yake kama vile ilivyo kuhubiri. Mhubiri hawezi kuwa anahubiri na kutembelea watu kila wakati, kwa kuwa kazi hii inachosha. {*EVsw 660.2*}

Nuru niliyoonyeshwa ni kwamba kama wahubiri wetu wangefanya kazi ya mikono zaidi, wangepata baraka nyingi kiafya. Baada ya siku ya kazi ya kuhubiri, kutembelea na kujifunza, mhubiri anapaswa kuwa na muda wa kushughulikia mahitaji yake mwenyewe. Kama ana mshahara mdogo, anaweza kutafuta njia ya kuongeza kipato chake. Wenye akili finyu huenda wakaona jambo la kulaumu katika hili, lakini Bwana anasifu mtazamo wa namna hiyo. {*EVsw 660.3*}

Nimeonyeshwa kuwa wakati mwingine wale walio katika huduma hulazimika kufanya kazi usiku na mchana na kuishi kwa lishe duni. Wakati wa dharura, kila misuli na neva hutumika kwa nguvu nyingi. Kama watu hawa wangeweza kujitenga na kupumzika kwa muda, wakifanya kazi za mikono, hiyo ingekuwa faraja kubwa. Kwa njia hiyo watu wangeweza kuokolewa ambao wamepotea hadi kaburini. Ni jambo la lazima kwa afya ya mwili na uwazi wa akili kufanya kazi fulani ya mikono kila siku. Hili husaidia damu kutoka kwenye ubongo na kusambaa sehemu nyingine za mwili. **—Letter 168, 1899.** {*EVsw 661.1*}

Uboreshaji Endelevu

Wahubiri Wenye Umri Mkubwa Wana Wajibu wa Kuendelea Kukua—Wahubiri wetu waliotimiza umri wa miaka arobaini au hamsini hawapaswi kuhisi kuwa kazi yao si yenye matokeo kama hapo awali. Watu wa umri na uzoefu huo ndio wanaohitajika sana kwa juhudi zenye nguvu na mwelekeo sahihi. Kanisa haliwezi kuwakosa watu wa namna hiyo, hakika wanahitajika. Wasiwe wakizungumza juu ya udhaifu wa mwili na akili, wala kujihisi kuwa wakati wao wa manufaa umeisha. {*EVsw 661.2}*

Wengi wao wamepitia msongo mkubwa wa kiakili bila kupatiwa nafuu kwa njia ya mazoezi ya mwili. Matokeo yake ni kudhoofika kwa uwezo wao na kuanza kuogopa majukumu. Wanachohitaji ni kazi hai zaidi. Hali hii haikuwapitia wazee tu, bali hata vijana wameangukia katika hali hiyo hiyo, na kuwa dhaifu kiakili. Wana mfululizo wa mahubiri waliouzoea; lakini wakijaribu kutoka nje ya mipaka ya hayo, hupoteza mwelekeo. {*EVsw 661.3}*

Mchungaji wa zamani, aliyezururа kwa farasi na kutumia muda mwingi kuwatembelea kondoo wake, alikuwa na afya bora zaidi na furaha, licha ya mashaka na tabu zake, kuliko wahubiri wa leo, ambao hujiepusha na kazi yoyote ya mwili na kujifungia kwenye vitabu. {*EVsw 662.1}*

Wahubiri wenye umri mkubwa na uzoefu wanapaswa kuhisi kuwa ni wajibu wao, kama watendakazi walioajiriwa na **Mungu**, kuendelea mbele, wakikua kila siku, wakiboresha kazi yao kwa ufanisi zaidi, na daima wakikusanya maarifa mapya ya kuwaeleza watu. Kila jitihada ya kufundisha injili inapaswa kuwa bora zaidi kuliko ile iliyopita. Kila mwaka wanapaswa kukuza uchaji-Mungu, utauwa wa kina zaidi, roho ya upole zaidi, hali ya kiroho zaidi, na maarifa ya kina zaidi ya kweli ya Biblia. Kadri wanavyozidi kuwa na umri na uzoefu, ndivyo wanapaswa kuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kugusa mioyo ya watu na kusogelea watu kwa ufanisi zaidi, kwa kuwa na maarifa kamili zaidi ya watu. **—Testimonies for the Church 4:269, 270 (1876).** {*EVsw 662.2}*

Shida za Kifedha —Wahubiri na walimu wanapobeba mzigo wa wajibu wa kifedha na kuingia mimbari au darasani wakiwa wamechoka kiakili na neva zao kuchoka, ni nini kingine kinachoweza kutarajiwa zaidi ya kwamba watatumia “moto wa kigeni” badala ya “moto mtakatifu” uliowashwa na **Mungu**? Juhudi hizo zilizokosa uhai huwavunja moyo wasikilizaji na kumuumiza mhubiri. Kwani hajapata muda wa kumtafuta Bwana, wala muda wa kuomba kwa imani kupakwa mafuta ya Roho Mtakatifu. **—Testimonies for the Church 7:250, 251 (1902).** {*EVsw 662.3}*

Epuka Mikutano Mirefu ya Kamati Usiku—Mhubiri hawezi kubaki katika hali bora ya kiroho akiwa anaitwa mara kwa mara kushughulikia matatizo madogo katika makanisa. Hiyo sio kazi yake aliyopewa na **Mungu**. **Mungu** anataka kila kipawa cha wajumbe Wake walioteuliwa kitumike kwa ajili ya kazi ya injili. Akili zao hazipaswi kuchoka kwa mikutano mirefu ya usiku; kwa kuwa **Mungu** anataka uwezo wao wote wa kiakili utumike katika kutangaza injili kama ilivyo katika Yesu Kristo. {*EVsw 662.4}*

Mhubiri anapolemewa, mara nyingi huwa na haraka kiasi kwamba hana muda hata wa kujitafakari na kujichunguza mwenyewe kama bado yumo katika imani. Hana muda wa kutafakari wala kuomba. Kristo katika huduma Yake aliunganisha maombi na kazi. Usiku baada ya usiku Aliutumia katika maombi. Wachungaji lazima wamtafute **Mungu** kwa ajili ya Roho Mtakatifu, ili waweze kuwasilisha Ukweli kwa usahihi. **—Manuscript 127, 1902.** {*EVsw 663.1}*

Msimamo Imara—Wito kwa Mwinjilisti Maarufu

Imeonyeshwa wazi kwangu kwamba watu wa **Mungu** wanapaswa kusimama imara dhidi ya ulaji wa nyama au samaki (kile kichotoka kwa mimea). Je, **Mungu** angeweza kutoa kwa muda wa miaka thelathini ujumbe kwa watu Wake kwamba, kama wanatamani kuwa na damu safi na akili iliyo wazi, ni lazima waache kutumia nyama, kama asingetaka wautii ujumbe huo? Kwa kula nyama, hulka ya mnyama huimarishwa na hulka ya kiroho hudhoofishwa. Watu kama wewe, ambao wamepewa kazi iliyo ya kusudi na ya maana zaidi kuwahi kuaminiwa kwa wanadamu, wanapaswa kuwa waangalifu sana kuhusu kile wanachokula. {*EVsw 663.2}*

Kumbuka kwamba unapokula nyama au samaki, unakula nafaka na mboga kwa njia ya mnyororo wa pili-(chakula mtumba au second hand yaani, kwa njia ya mnyama aliyekula majani); kwa kuwa mnyama hupokea virutubisho kutoka kwenye chakula cha mbogamboga au mimea na hivyo, anapochinjwa na kuliwa huachilia mwilini mwake vitu lishe ambayo binadamu hula kutoka kwa huyo mnyama. Uhai uliokuwepo katika nafaka na mboga huingia kwenye mwili wa mnyama na kuwa sehemu ya maisha yake, halafu binadamu hula mnyama huyo. Kwa nini basi tukubali kula chakula kwa njia ya pili au mtumba wa chakula? {*EVsw 663.3}*

Hapo mwanzo, matunda yalitangazwa na **Mungu** kuwa “yanakufaa kwa chakula.” Ruhusa ya kula nyama ilikuja kama matokeo ya anguko la mwanadamu. Hadi baada ya Gharika ndipo mwanadamu aliruhusiwa kula nyama ya wanyama. Kwa nini basi sasa tuendelee kula nyama? Watu wachache wanaokula nyama wanajua ni kwa kiasi gani imejaa magonjwa. Nyama au samaki, haikuwa chakula bora kamwe, na sasa imejaa laana ya magonjwa. {*EVsw 663.4*}

Uharibifu wa Maumbile ya Kibinadamu—Wazo la kuua wanyama kwa ajili ya kuliwa ni jambo la kutisha. Kama hisia ya asili ya mwanadamu haingekuwa imepotoshwa kwa kujitindikia na kuendekeza tamaa au uchu wa chakula, wanadamu wasingewaza hata kula nyama ya wanyama. {*EVsw 664.1*}

Tumepewa kazi ya kuendeleza matengenezo ya afya. Bwana anatamani watu Wake wawe na umoja katika jambo hili. Kama unavyojua, hatutaacha nafasi ambayo kwa miaka thelathini na tano iliyopita Bwana ametutaka tusimame ndani yake. Jihadhari usije ukaweka nafsi yako katika upinzani dhidi ya kazi ya matengenezo ya afya. Kazi hii itasonga mbele, kwa kuwa hiyo ni njia ya Bwana ya kupunguza mateso ulimwenguni na ya kuwatakasa watu Wake. {*EVsw 664.2*}

Uwe mwangalifu na mtazamo unaouchukua, usije ukawa chanzo cha mgawanyiko. Ndugu yangu, hata kama wewe mwenyewe bado hujaleta baraka za kufuata kanuni za matengenezo ya afya katika maisha yako na familia yako, usiwadhuru wengine kwa kupinga nuru ambayo **Mungu** ameitoa kuhusu jambo hili. {*EVsw 664.3*}

Ingawa hatuufanyi ulaji wa nyama kuwa kipimo cha ushirika, wala hatulazimishi mtu yeyote kuacha matumizi yake, bado ni wajibu wetu kuomba kwamba mhubiri yeyote wa konferensi asifanye mzaha au kupinga ujumbe wa matengenezo ya afya kuhusu jambo hili. Kama, licha ya nuru ya **Mungu** kuhusu athari ya ulaji wa nyama katika mwili, utaendelea kula nyama, ni lazima ubebe matokeo yake. Lakini usichukue nafasi mbele ya watu ambayo itawafanya waamini kwamba si muhimu kutoa wito wa matengenezo kuhusu ulaji wa nyama, kwa sababu Bwana mwenyewe anatoa wito wa matengenezo. Bwana ametupa sisi kazi ya kutangaza ujumbe wa matengenezo ya afya, na kama huwezi kusonga mbele pamoja na wale wanaoutangaza ujumbe huu, huna budi kutokufanya upinzani kuwa wa wazi. Unapopinga juhudi za ndugu zako wanaofundisha matengenezo ya afya, uko nje ya utaratibu, ukifanya kazi upande usio sahihi. —**Letter 48, 1902.** {*EVsw 664.4*}

Sauti ya Mtendakazi wa Injili

Mhubiri Msemaji wa Mungu

Mtu anayekubali kuwa msemaji wa **Mungu** anapaswa kuchukulia kwa uzito mkubwa wajibu wake wa kuwasilisha Ukweli kwa neema na akili yote iwezekanayo, ili Ukweli huo usipoteze uzito au mvuto wake mbele ya watu. Wale wanaochukulia kwa wepesi kusema kwa matamshi yasiyo sahihi wanamdharau **Mungu**. **—Manuscript 107, 1898.** {*EVsw 665.1*}

Kwa Sauti Iliyo Wazi na Kamili

Uwezo wa kusema kwa uwazi na kwa sauti iliyo kamili ni wa thamani kuu katika aina yoyote ya kazi. Sifa hii ni ya lazima kwa wale wanaotamani kuwa wachungaji, wahubiri, wainjilisti, walimu wa Biblia, au wauzaji wa vitabu vya kiroho. Wale wanaojipanga kuingia katika huduma hizi wanapaswa kufundishwa kutumia sauti yao kwa njia ambayo itafanya Ukweli uingie kwa athari njema moyoni mwa msikilizaji na kuwe na maamuzi yaliyodhamiriwa. Ukweli hautakiwi kuharibiwa kwa kuwasilishwa kwa matamshi yaliyo na upungufu. **—Testimonies for the Church 6:380 (1900).** {*EVsw 665.2*}

Kuzungumza kwa Wazi na kwa Hisia

Watenda kazi wote, wawe wanaoongea mimbarini au wanatoa mafundisho ya Biblia, wafundishwe kusema kwa namna iliyo wazi na yenye maelezo yenye hisia. **—Letter 200, 1903.** {*EVsw 665.3*}

Msomaji wa Biblia Awe na Sauti Nyororo na ya Kuvutia

Yule anayesoma Biblia mbele ya kusanyiko au katika familia anapaswa kuwa na uwezo wa kusoma kwa sauti laini na yenye mdundo wa kuvutia wa muziki ambayo itawavutia wasikilizaji (soft and musical). **—Testimonies for the Church 6:381 (1900).** {*EVsw 666.1*}

Kushawishi na Kuvutia kwa Sauti

Sayansi ya kusoma kwa usahihi na kwa msisitizo unaofaa ni ya thamani kuu. Haijalishi umejifunza kiasi gani katika mistari mingine, ikiwa umepuuzia kukuza kipawa chako cha kuboresha sauti na namna ya kuzungumza kwa uwazi, akili mahiri na kueleweka, basi mafunzo au elimu yako yote haitakuwa ya faida kubwa. Kwa kuwa bila kuwa na utamaduni bora wa sauti, huwezi kuwasiliana kwa utayari na kwa kueweleweka kwa uwazi, kuhusu yale ambayo umejifunza. {*EVsw 666.2}*

Kujifunza kuwasilisha maarifa kwa njia inayoshawishi na kugusa mioyo ni faida yenye thamani ya pekee kwa wale wanaotaka kuwa watenda kazi katika kazi ya **Mungu**. Kadiri maneno ya Ukweli yanavyotamkwa kwa hisia, kadri unavyoweza kujieleza vyema kwa sauti na mwili na mifano, ndivyo utakavyogusa moyo zaidi moyo wasikilizaji. Uwasilishaji ufaao wa Ukweli wa Bwana unastahili jitihada zetu kuu kabisa. Wanafunzi wanaojiandaa kwa ajili ya kazi ya Bwana na wajifunze kwa bidii kusema kwa usahihi na kwa msisitizo, ili wanapozungumza kuhusu Ukweli, iwe faraghani au hadharani, waweze kuuwasilisha kwa njia inayolingana na asili yake ya mbinguni. **—Manuscript 131, 1902. {*EVsw 666.3}***

Sauti ya Mzungumzaji Huathiri Maamuzi

Baadhi ya watu huharibu athari takatifu waliyokuwa wameweka kwa watu kwa kupandisha sauti kupita kiasi, kwa kupiga kelele na kupaza sauti sana. Ukweli unapotamkwa kwa namna hiyo hupoteza upole, utamu, nguvu, na uzito wake. Lakini ikiwa sauti itarekebishwa vizuri, ikawa ya uzito wa Kiungu, na kusihi moyo wa msikilizaji kwa hisia ya huruma na upendo na ikiwa itatamkwa kwa namna ya kusikitisha, italeta athari nzuri zaidi. Hivi ndivyo Kristo alivyofundisha wanafunzi Wake—alizungumza kwa kuweka uzito/adhima na sauti ya huruma. *Kelele na kupaza sauti hakubebi ujumbe bora; bali huleta hisia zisizopendeza na kuharibu sauti ya mzungumzaji (halooing tone-angalia mtandaoni- inafanana kama sauti ya mbwa anayeomboleza kidogo), ***Haiwapi watu maoni yoyote yaliyotukuka kuhusu Ukweli, na haina mvuto kwao. Inasababisha tu hisia zisizopendeza kwa watu wanaokusikia, na huchakaza viungo vya sauti vya mzungumzaji.** Toni za sauti zina nguvu kubwa ya kugusa na kuathiri mioyo ya wasikilizaji. **—Testimonies for the Church 2:615 (1871). {*EVsw 666.4}***

Matumizi Sahihi ya Sauti

Tahadhari na mafunzo yanapaswa kutolewa kwa viungo vya sauti. Huzidi kuwa imara kwa matumizi sahihi lakini hudhoofika kwa matumizi mabaya. Viung hivi vikitumiwa kupita kiasi, kama vile kuhubiri kwa muda mrefu, huathiri si tu viungo vya sauti bali pia mfumo wa neva. Ala hiyo nyeti ya nyuzi elfu kwenye koo lako ambayo ni kama kinubi, hupoteza ladha, na badala ya kutoa melodi tamu, hutoa sauti kama ya ugomvi na kukera. {*EVsw 667.1}*

Ni muhimu kwa kila mhubiri kuifundisha sauti yake ili ibaki katika hali ya afya, na ili aweze kusema Maneno ya uzima kwa watu. Ni muhimu kila mtu awe na akili na ufanisi katika kutumia sauti yake aliyopewa na Mwenyezi Mungu inavyopaswa na kuitumia sauti vyema, Sio lazima kuzungumza kwa sauti kubwa au ya juu mno (kumbuka siku hizi tuna vipaza sauti, sio kama siku zile), kwani jambo hilo huleta madhara kwa msemaji. Kuzungumza haraka-haraka hupunguza athari ya ujumbe, kwa sababu maneno hayafahamiki kwa uwazi kama yangetamkwa kwa utulivu na kwa kukusudia, hebu ampe msikilizaji muda kutambua ni nini kinazungumziwa katika kila neno. {*EVsw 667.2}*

Sauti ya binadamu ni zawadi ya thamani kutoka kwa **Mungu**; ni nguvu kwa ajili ya mema. Bwana anataka watumishi Wake waendelee kuikuza sauti yao kwa mwelekeo wa sauti yenye hisia za faraja, sikitiko, huzuni na uzuri wa melodi, ili sauti hiyo iweze kuwasiliana na mioyo ya watu inapofika masikioni mwao na kuwagusa moyo. {*EVsw 667.3}*

Bwana anamtaka mwakilishi Wake wa kianadamu asisonge kwa msukumo katika kunena, bali asonge kwa utulivu, kwa kuzungumza polepole, na kisha amruhusu Roho Mtakatifu afanye ile Kweli iwe na ufanisi. Msifikirie kamwe kwamba katika kujishughulisha kwa shauku au mihemko mingi katika uwasilishaji wa injili, kwamba mtakapozungumza kwa msukumo, na mkizitaabisha hisia zenu kwa kuinua sauti yenu kwa ufunguo wa sauti ya juu usio wa kawaida, ndiyo mtaweza kutoa ushahidi wa nguvu kuu ya Mungu juu yenu... Sio kwa msisimko wa mihemko au kwa kuacha hisia zichukue usukani, bali kwa utulivu na chini ya mwongozo wa Roho Mtakatifu. {*EVsw 668.1}*

Ushawishi wako unapaswa kuwa mkubwa, na nguvu zako za usemi zinapaswa kuwa chini ya udhibiti wa hekima aliyokupa Bwana. Unapovikaza viungo vyako vya sauti au kuzungumza, unapoteza kuitawala sauti yako ili iwe na mabadiliko ambayo husaidia mkazo au shauku ya watu kukusikiliza. Tabia ya kuzungumza haraka inapaswa uishinde kabisa. Mungu anadai kwa wanadamu huduma yote ambayo mwanadamu anaweza kutoa. Vipaji vyote vilivyokabidhiwa kwa wakala wa kianadamu, hivi vinapaswa kuthaminiwa na kutumiwa kama zawadi ya thamani kutoka mbinguni. Watendakazi katika shamba la mavuno ni mawakala walioteuliwa na Mungu, njia ambazo Yeye anaweza kuwasilisha nuru kutoka mbinguni. Matumizi yasiyojali jambo hili na yasiyo na mpangilio ya nguvu yoyote wanadamu waliyopewa na Mungu hupunguza ufanisi wao kiasi kwamba katika dharura, wakati wema mkubwa zaidi unaweza kutimizwa, wao wanakuwa katika hali dhaifu sana, wagonjwa na vilema kiasi kwamba wanaweza kutimiza kidogo tu katika kueneza injili.— Ushuhuda Maalum, Mfululizo A, 7:9-11. (1874) (*Modulatio of voice-Ubadilishaji wa sauti, iwe tofauti na ya kimakusudi -sauti ya juu au chini, toni, ukubwa pale inakuwa nzito au laini, na kasi, hufanya mawasiliano kuwa ya kuvutia zaidi, hufafanua maana, huwasilisha hisia, na hujenga muunganisho kwa kuzuia watu wasichoke na kusisitiza mambo muhimu, na kubadilisha uwasilishaji sambamba kuwa usemi wenye nguvu kwa ajili ya kuhifadhi ubora wa hadhira na athari katika usemi na uimbaji).{*EVsw 668.2}*

—Special Testimonies, Series A, No. 7, pp. 9-11 (1874). {*EVsw 668.2}*

Umuhimu wa Mafunzo ya Sauti kwa Wachungaji

Walimu wa shule zetu hawapaswi kuvumilia wanafunzi wenye mitindo mibaya ya kusoma, matamshi yasiyo sahihi au mkazo usiofaa kwa kutumia sehemu ya mwili isivyopaswa (uncorrect gestures, mikono, miguu, kichwa, macho nk). Ufanisi wa usemi na sauti unapaswa kusisitizwa kwa kila mwanafunzi. Kwa sababu ya uzembe na mafunzo duni, mazoea na hulka mbaya huweza kujengeka, ambazo ni kikwazo kikubwa kwa mhubiri mwenye kipawa kingine kizuri. Mwanafunzi asisitizwe kwamba ana uwezo, kwa neema na jitihada, wa kujijenga kuwa mtu bora. Vipawa vya akili na mwili alivyopewa na **Mungu** vinaweza, kwa bidii na juhudi, kukuzwa na kuboreshwa ili kuwa nguvu kwa ajili ya kuwabariki wanadamu. —**Manuscript 22, 1886. {*EVsw 668.3}***

Kufundisha Sauti

Kufundisha sauti ni jambo muhimu katika mafunzo ya kimwili, kwani husaidia kupanua na kuimarisha mapafu na kuzuia magonjwa. Ili kuhakikisha kwamba unazungumza au kusoma kwa usahihi, hakikisha misuli ya tumbo inahusika kwa upumuaji kikamilifu, na viungo vya kupumua havijazuiliwa. Hebu msukumo wa sauti uwe kwa misuli ya tumbo, sio ya koo. Hii husaidia kuzuia uchovu na magonjwa ya koo na mapafu. Toa umuhimu kwa kutamka wazi, sauti laini na yenye mpangilio mzuri unaotawalika inavyofaa (angalia modulation 668.3), na usizungumze kwa kasi kupita kiasi. **—Education, 199 (1903). {*EVsw 669.1}***

Zungumza kwa Maelfu kwa urahisi Kama kwa Watu Kumi tu

Zungumza kwa kuruhusu sehemu za juu za viungo vya sauti kutumika, maneno yatoke kwenye sehemu za juu za viungo vya sauti, usivisumbue viungo na kuvikera kwa kuvikwaruza hiyo huathiri afya na ufanisi wa sauti. Vuta pumzi kamili na usukume sauti ukiachia misuli ya tumbo kufanya hiyo kazi na siyo koo. Hebu mapafu yawe ni njia tu ya sauti kupita, ila sio vyanzo vya nguvu ya kuzungumza. ***Ukiruhusu maneno yako yatoke kutoka ndani kabisa kwenye misuli ya tumbo, ukifanya mazoezi ya misuli ya tumbo, unaweza kuzungumza na maelfu kwa urahisi kama unavyoweza*** kuzungumza na watu kumi. **—Testimonies for the Church 2:616 (1871). {*EVsw 669.2}***

.

Zingatia Upumuaji Sahihi (deep breathing, jifunze zaidi kwa kuona mifano ya watu au video)

Hebu wachungaji wasimame wima, wazungumze kwa utulivu, uthabiti, na kwa uwazi, wakichukua pumzi kamili kwa kila sentensi, na kutoa maneno kwa kutumia misuli ya tumbo. Kwa kufuata kanuni hii rahisi na kuheshimu sheria nyingine za afya kwa umakini, wanaweza kuendelea kuwa na afya na ufanisi na kunufaisha watu au kunufaika kwa muda mrefu maishani zaidi kuliko watu wa taaluma zingine. Kifua kitapanuka zaidi, na sauti haitapotea kirahisi hata kwa huduma ya mara kwa mara. Badala ya kuwa na magonjwa kwenye njia

ya upumuaji, wahudumu wanaweza, kuwa waangalifu, na kushinda tabia zote zinazochochea magonjwa ya mapafu, kama vile kifua kikuu (consumption),— **—Testimonies for the Church 4:404 (1880). {*EVsw 670.1*}**

Zungumza Kwa Utulivu na Kwa tarabibu

Nilipokuwa binti nilikuwa naongea kwa sauti kubwa mno. Bwana alinifunulia kuwa siwezi kuwa na athari stahiki kwa watu kwa kuongea kwa sauti ya juu isiyo ya kawaida. Ndipo Kristo akaonyeshwa kwangu, na namna Yake ya kuongea; kulikuwa na sauti tamu ya melodi katika sauti Yake. Alizungumza kwa utulivu na kwa taratibu, na Maneno Yake yalipenya mioyoni mwao na wakaweza kuelewa yote kabla ya sentensi inayofuata. Baadhi huamini kuwa lazima wazungumze haraka na kwa sauti ya juu la sivyo watapoteza "msukumo" wa kiroho. Lakini ikiwa huo ndio uvivio, basi ni bora upotee—na ukipoea mapema iwezekanavyo, ndio itakuwa vyema zaidi. **—Manuscript 19b, 1890. {*EVsw 670.2*}**

Mwonekano Binafsi wa Mwinjilisti

Haiba na Hulka ya Mwinjilisti

Kutokana na nuru niliyopewa, huduma ya injili/kichungaji ni ofisi takatifu na ya heshima kuu, na wale wanaoikubali wanapaswa kuwa na Kristo mioyoni mwao, wakionesha shauku ya dhati ya kumwakilisha kwa heshima mbele za watu—katika matendo yao, mavazi yao, usemi wao, na hata namna yao ya kuongea. **{*EVsw 670.3*}**

Maneno yetu, matendo yetu, hulka yetu, mwenendo wetu, na mavazi yetu—kila kipengele cha utu wetu—vinapaswa kuwa mahubiri hai. Sio kwa maneno pekee tunapaswa kuwahubiria watu, bali kila kitu kinachotuhusu kinapaswa kuwa hubiri/somo la maadili kwao. **—Testimonies for the Church 2:615, 618 (1871). {*EVsw 671.1*}**

Roho Zinapotea kwa Sababu ya Uzembe

Mchungaji ambaye ni mzembe katika mavazi yake huumiza mioyo ya wale walio na ladha nzuri na wenye hisia nyeti zilizosafishwa kwa ladha. Wale ambao wana kasoro katika jambo hili wanapaswa kujirekebisha na kuwa waangalifu na wenye busara zaidi. Watu wengine wamepotea milele, na itakuja kujulikana kwamba sababu ya kutokuwa nadhifu katika mwonekano wa kwanza ya mhubiri kulichangia. Watu hawakuweza kuhusianisha kabisa mwonekano wake wa kwanza na ujumbe wa zile Kweli alizoziwasilisha. Mavazi yake yalikuwa dhidi yake; na ujumbe wa ndani uliambatana na taswira ya kwamba wale watu aliowawakilisha (waamini etc) walikuwa wazembe, wasiojali kuhusu mwonekano, uvaaji au nguo zao na hivyo wasikilizaji wake hawakutaka kuwa na uhusiano na watu wa kundi kama hilo. **—Testimonies for the Church 2:613 (1871). {*EVsw 671.2*}**

Ladha, Rangi, na Jinsi Vazi livyomkaa Kwenye umbo la mtu (Linavyofiti)

Baadhi ya wahudumu wa mambo matakatifu huvaa mavazi yao kwa njia ambayo, kwa kiasi fulani, huharibu mvuto ya kazi yao ya kufikisha injili. Kuna ukosefu wa ladha katika uteuzi wa rangi au unadhifu na jinsi vazi linavyokaa kwenye umbo la mtu. Je, ni taswira gani inayoletwa na mtindo kama huo wa mavazi? Ni kwamba kazi wanayoifanya haionekani kuwa takatifu au ya heshima kuliko kazi ya kawaida kama kulima shambani. Kwa mfano huo, mhubiri huyashusha mambo matakatifu hadi kiwango cha mambo ya kawaida. **—Testimonies for the Church 2:614 (1871). {*EVsw 671.3*}**

Uchaguzi wa Rangi

Nguo za rangi nyeusi au za rangi ya giza ni za kupendeza zaidi kwa mhubiri anapokuwa mimbari, na huacha taswira bora zaidi kwa watu kuliko kuchanganya rangi mbili au tatu katika mavazi yao (dark brown, dark grey, dark green-mchungaji asivae suti ya njano, orange, pink au rangi kama hizo, hata mwanamke asivae rangi za kung'aa sana kwenye kuhubiri, pengine na rangi ya mtu inaweza ikawa bora kitambaa kikiwa kinang'aa kidogo nk). **—Testimonies for the Church 2:610 (1871). {*EVsw 672.1*}**

Heshima Katika Mavazi na Tabia

Katika mavazi na mwenendo wetu, tunapaswa kuonyesha maadili, tabia, viwango na hadhi (propriety). Kamwe tusiruhusu kuwa na mwonekano wa hovyo ovyo au wa uchakavu katika mavazi yetu au kazi yetu. **—Letter 49, 1902. {*EVsw 672.2*}**

Tabia ya Mtendakazi Mwanamke Inahukumiwa Kwa Mavazi

Tabia ya mtu inahukumiwa kwa mtindo wake wa mavazi. Ladha iliyosafishwa, akili iliyokuzwa au kufunzwa, huonekana katika uteuzi wa mavazi rahisi lakini yanayofaa. Unyenyekevu safi katika mavazi, ukichanganywa na tabia ya uungwana na staha katika mwenendo, utamweka binti mbali katika anga ya heshima kwa yale yaliyo matakatifu jambo hili litakuwa ngao dhidi ya hatari na majaribu mengi. **—Education, 248 (1903). {*EVsw 672.3*}**

Wasioamini Wanathamini Unyenyekevu wa Mavazi

Wengine huvaa kama watu wa dunia ili kupata ushawishi kwa watu wasioamini, lakini haya ni makosa makubwa. Ikiwa wanataka kuwa na ushawishi wa Kweli na unaookoa, na waishi imani yao, hebu waonyeshe imani yao kwa matendo ya haki, na wafanye tofauti kati ya MKristo na mtu wa dunia kuwa wazi. Maneno yao, mavazi yao, na matendo yao yapaze sauti kwa ajili ya **Mungu**. Hapo ndipo ushawishi mtakatifu utatanda juu ya wote walio karibu nao, na hata watu wasioamini watatambua kuwa wamekuwa na Yesu. Kama mtu anataka kuwa na ushawishi kwa ajili ya Ukweli, basi na aishi kile anachokiri, na kwa njia hiyo amwige Mfano wa unyenyekevu**. —Testimonies for the Church 4:633, 634 (1881). {*EVsw 672.4*}**

Kiburi Katika Mavazi Huwa Kikwazo kwa Wasioamini

Wapo wengi waliothibitishwa juu ya Ukweli, lakini waliamua kuukataa kwa sababu ya kiburi na mapenzi ya dunia yaliyoonyeshwa na dada zetu. Mafundisho yaliyohubiriwa yalionekana wazi na yenye upatanifu, na wasikilizaji walihisi kuwa msalaba mzito ulipaswa kubebwa ili kuukubali Ukweli. Lakini walipoona baadhi ya dada zetu wakionyesha fahari kwa kujionyesha kupita kiasi katika mavazi yao, walisema, “Hawa watu huvaa kama sisi. Hawawezi kuamini kile wanachokiri; kwa kweli, na hivyo hufikiria kuwa lazima wamepotoshwa-wamedanganywa tu. Kama wangekuwa wanaamini Kweli kuwa Kristo anakuja hivi karibuni, na hatima ya kila nafsi iko karibu kuamuliwa kwa uzima wa milele au mauti, wasingeweza kutumia muda na fedha kwa ajili ya kufuata fasheni/mitindo ya sasa ya mavazi.” Ni madada wangapi kweli, waliodai kuamini injili, waliokuwa wanaelewa kuwa mavazi yao yalikuwa yalikuwa mahubiri na kwamba yalikuwa yakihubiri nini! **{*EVsw 672.5*}**

Maneno yetu, matendo yetu, na mavazi yetu ni wahubiri hai kila siku—wanakusanya pamoja na Kristo au wanatawanya. Hili sio jambo dogo la kupitwa hivi hivi kwa mizaha. Mada ya mavazi inahitaji tafakari makini na sala nyingi. Wengi wasioamini wamehisi kuwa si sawa kujifunga katika utumwa wa mitindo ya dunia; lakini wanapoona wale wanaodai kuwa watauwa wa kweli wakivaa kama watu wa dunia, wakifurahia marafiki wa kidunia, wenye mizaha husema: “Hakuna kosa katika mwenendo kama huo.” **—Testimonies for the Church 4:641 (1881). {*EVsw 673.1*}**

Mavazi Rahisi/sahili Hayatawaumbua Maskini Katika

Mavazi yetu yanapaswa kuwa rahisi na ya kawaida, ili tunawapotembelea watu maskini, wasijisikie vibaya kwa aibu wanapolinganisha mwonekano wao na wetu. **—Gospel Workers, 189 (1915). {*EVsw 673.2*}**

Mavazi Yanayolingana na Wito wa Takatifu

Uangalifu katika mavazi ni jambo la muhimu. Mchungaji anapaswa kuvaa kwa namna inayolingana na heshima/hadhi ya wito wake. Baadhi ya wachungaji/wahudumu wameshindwa katika jambo hili. Katika baadhi ya matukio, si tu kwamba kumekuwepo ukosefu wa ladha na mpangilio katika mavazi, bali pia mavazi yamekuwa yasiyo nadhifu au machafu na yasiyopendeza. **{*EVsw 673.3*}**

Mungu wa mbinguni, ambaye mkono Wake huendesha dunia, anayetupa uhai na kutushibisha/kututegemeza wa afya, huheshimiwa au hudharauliwa kwa namna mavazi ya wale wanaohudumu kwa heshima Yake yanavyokuwa. **—Gospel Workers, 173 (1915). {*EVsw 674.1*}**

Mke wa Mwinjilisti

Kuwajibika kwa Talanta Zake

Wajibu mkubwa unamkabili mke wa mhudumu, ambao hawezi wala hastahili kuupuuza kwa wepesi. **Mungu** atadai talanta aliyopewa, ikiwa imezalisha faida na riba. Anapaswa kufanya kazi kwa dhati, bidii, kwa uaminifu, na kwa kushirikiana kwa moyo mmoja na mume wake katika kuokoa roho. Asiwe mtu wa kushinikiza matakwa yake binafsi, wala kuonyesha kutopendezwa au kutokuwa na shauku na kazi ya mume wake, wala kuendelea kufikiria hali ya kutamani kurudi nyumbani au hali ya kutoridhika, au kutokuwa na muunganiko na huduma, watu au mumewe (homesick). Anapaswa kuyashinda mazoea ya hisia zote za asili kama hizi. Anapaswa kuwa na lengo maalum katika maisha, ambalo analitekeleza kwa uaminifu usiotetereka. Je, ikuwaje basi ikiwa lengo hili linapingana na hisia, ladha yake ya asili na starehe zake? Vitu hivyo vya asili vinapaswa kutolewa dhabihu kwa furaha na utayari ili kutenda mema na kuokoa roho. {*EVsw 674.2*}

Wake wa wahudumu wanapaswa kuishi maisha ya kujitoa wakfu na maombi. Lakini baadhi yao wangependa dini isiyo na misalaba, isiyo na kujinyima au jitihada kwa upande wao. Badala ya kusimama kama waungwana na kwa ubora kwa niaba yao, wakimtegemea **Mungu** kwa nguvu, na kuchukua wajibu wao binafsi, mara nyingi wamekuwa tegemezi kwa wengine, wakiuiba uhai wao wa kiroho kutoka kwa watu. Laiti wangemtegemea **Mungu** kwa ujasiri, kwa imani kama ya mtoto, na wakamwekea Yesu mapenzi yao, wakipata uhai wao kutoka kwa Kristo, mzabibu wa uzima—ni mema kiasi gani wangeweza kufanya! Wangeweza kuwa msaada mkubwa kwa wengine kwa kiasi gani, na nguzo kwa waume zao, na hata mwishowe thawabu yao kuwa kubwa mno! — **Testimonies for the Church 1:452, 453 (1864).** {*EVsw 674.3*}

Kusafiri na Mume kwa Ajili ya Uinjilisti

Ikiwa mke wa mhudumu atamsindikiza mumewe katika safari za huduma, lengo lake lisiwe ni kwa ajili ya raha au kupata kutumikiwa na wengine, bali awe amesafiri ili kushiriki naye katika kazi. Awe na nia ya pamoja ya kufanya mema.

Anapaswa kuwa tayari kumsindikiza mumewe, ikiwa majukumu ya nyumbani hayazuii, na kumsaidia katika jitihada za kuokoa roho. Kwa upole na unyenyekevu, lakini akiwa na ujasiri wa Kiungu wa kujitegemeza, anapaswa kuwa na ushawishi mkuu kwa watu waliomzunguka. Hebu na shiriki kazi, achukue msalaba wake, na aendelee kuwa chombo cha baraka katika mikutano, katika ibada za familia, na katika mazungumzo ya kawaida nyumbani pale sebuleni, watu wanapokota moto. Watu wanatarajia haya, na wana haki ya kutarajia. Kama matarajio haya hayatatimizwa, ushawishi wa mume wake huathirika vibaya kwa zaidi ya nusu. {*EVsw 675.1*}

Mke wa mchungaji anaweza kufanya mengi ikiwa atataka. Akiwa na roho ya kujinyima na upendo kwa roho, anaweza kushirikiana na mume wake kufanya kazi ya thamani sawa. Mwanamke anayefanya kazi katika huduma ya ile Kweli anaweza kufikia mioyo ambayo mhudumu hawezi, hasa miongoni mwa wanawake wenzake. **— Testimonies for the Church 1:452 (1864).** {*EVsw 675.2*}

Mavazi ya Wake wa Wachungaji

Haswa wake wa wahudumu wetu wanapaswa kuwa waangalifu sana kutoenda kinyume na mafundisho ya Biblia kuhusu mavazi. Wengi huyadharau maagizo haya ya Maandiko wakiyahesabu kuwa ya zamani mno (old fashioned), lakini Yeye aliyewapa wanafunzi wake maagizo hayo alijua hatari ya mapenzi ya anasa za mavazi katika kizazi chetu, na akatupa onyo. Je, tutalisikia onyo hilo na kuwa wenye hekima? Anasa katika mavazi inaongezeka kila siku. Mwisho bado haujafika. Mitindo hubadilika daima, na dada zetu hufuata mkondo huo bila kujali gharama wala muda. Fedha nyingi zinapotezwa kwenye mavazi, ambazo zingepaswa kurudishwa kwa **Mungu**, aliye mtoaji. — **Testimonies for the Church 4:630, 631 (1881).** {*EVsw 675.3*}

Mfano wa Dini ya Nyumbani

Mke wa mhudumu aliye na watoto na akumbuke kwamba nyumbani mwake kuna uwanja wa kimisheniri ambamo anatakiwa kufanyakazi kwa bidii isiyoisha na kwa juhudi zisizopungua, akijua kuwa matokeo ya kazi yake yatadumu milele. Je, roho za watoto wake hazina thamani sawa na roho za watu wa mataifa na wapagani? Basi na awatunze kwa upendo. Mama huyu amepewa jukumu la kuonyesha kwa ulimwengu nguvu na uzuri wa dini ya nyumbani. Anapaswa kuongozwa na kanuni, si hisia, na afanye kazi yake kwa kujua kuwa **Mungu** ndiye msaidizi wake. Asiruhusu chochote kumtenganisha na wajibu wake. {*EVsw 676.1*}

Ushawishi wa mama aliye na uhusiano wa karibu na Kristo hauna kifani. Huduma yake ya upendo huwafanya watu wajisikie kama wako Betheli (nyumba ya Mungu). Kristo hutenda kazi pamoja naye,

akigeuza maji ya kawaida ya maisha kuwa divai ya mbinguni. Watoto wake watakua na kuwa baraka na heshima kwake hapa duniani na katika uzima ujao. — **Gospel Workers, 206 (1915).** {*EVsw 676.2}*

Kazi Muhimu ya Nyumbani

Iwapo wanaume waliooa wataingia kwenye huduma, huku wake zao wakibaki nyumbani kulea watoto, basi wake na mama hao wanafanya kazi iliyo kubwa na muhimu sawa na ile ya waume zao, na baba wa familia. Wakati mmoja yuko katika eneo la utume, mwingine ni mmishenari wa nyumbani, ambaye mara nyingi huzidi kwa mbali katika majukumu, masumbufu, wasiwasi na mizigo anayobeba kuliko yule aliye uwanjani. Kazi ya mama ni kazi adhimu na takatifu na muhimu sana—kuunda akili na tabia za watoto wake, kuwalea wawe watu wa faida hapa duniani na kuwaandaa kwa ajili ya uzima wa milele. {*EVsw 676.3}*

Mume aliye uwanja wa umishenari anaweza kupata sifa kutoka kwa wanadamu, wakati yule anayefanya kazi ya nyumbani hapati sifa yoyote ya kidunia kwa kazi yake; lakini kama anafanya kazi kwa ajili ya faida ya familia yake, akijitahidi kuunda tabia zao kwa mfano wa Kiungu, malaika mwandishi huandika jina lake kama mmoja wa wamishenari wakuu ulimwenguni. {*EVsw 677.1}*

Mke wa mhudumu anaweza kuwa msaada mkubwa kwa mumewe katika kuupunguzia mzigo, ikiwa atahifadhi moyo wake katika upendo wa **Mungu**. Anaweza kuwafundisha watoto Neno la **Mungu**, akaendesha shughuli za nyumbani kwa hekima na uchumi. Akiwa ameungana na mumewe, anaweza kuwafundisha watoto tabia ya kuwa waangalifu katika matumizi ya busara kuhusiana na fedha na vitu, na kuwafundisha kujizuia. — **Gospel Workers, 203 (1915).** {*EVsw 677.2}*

Roho ya Kulalamika ni Mzigo Mzito/mfu

Dada hawa wameunganishwa kwa karibu sana na kazi ya **Mungu**, ikiwa **Mungu** amewaita waume zao kuihubiri Kweli ya sasa. Watumishi hawa, ikiwa kweli wameitwa na **Mungu**, watasikia uzito wa kweli hiyo. Wamesimama kati ya walio hai na wafu, na lazima walinde roho kama wale ambao watatoa hesabu. Wito wao ni wa wakfu sana, na wake zao wanaweza kuwa baraka kubwa au laana kubwa kwao. Wanaweza kuwafariji wanapovunjika moyo, kuwafariji wanapohuzunika, na kuwahimiza kumtazama **Mungu** kwa imani wanapolegea. Au wanaweza kufuata mkondo wa tofauti, kuona upande wa giza, kudhani kuwa maisha yao ni magumu, kukosa imani kwa **Mungu**, kuongea masumbufu yao na hali ya kutoamini kwa waume zao, kuendekeza roho ya kulalamika na kunung'unika, na kuwa mzigo mzito hata laana kwa waume zao... {*EVsw 677.3}*

Mke asiyetakaswa kwa neema ya Kristo ni laana kubwa kwa mhudumu yeyote. Watumishi wa **Mungu** ambao wamejikuta katika hali hii ya kusikitisha ya kuwa na ushawishi wa kuua matumaini nyumbani, wanapaswa kuongeza maombi yao, kuwa waangalifu mara mbili, kuchukua msimamo thabiti, na wasiruhusu giza hilo kuwashinda. Wanapaswa kushikamana kwa karibu zaidi na **Mungu**, kuwa thabiti na wenye maamuzi, kuiongoza vyema nyumba yao, na kuishi kwa namna ambayo wataweza kupata kibali cha **Mungu** na ulinzi wa malaika. Lakini wakikubali kushinikizwa na tamaa za wenzi wasio wakfu, hasira ya **Mungu** huelekezwa juu ya nyumba hiyo. Sanduku la Agano la **Mungu** haliwezi kukaa katika nyumba hiyo kwa sababu wanahimiza na kuunga mkono maovu ya wake hao kwa mtazamo wao. **— Testimonies for the Church 1:138, 139 (1856).** {*EVsw 677.4}*

Kutunza Viwango vya Juu vya Maadili

Kutelekezwa kwa Kanuni Kunatambulisha Majira ya Sasa

Kila mahali yanaonekana mabaki ya ubinadamu baada ya uharibifu , madhabahu za familia zilizovunjika, nyumba zilizoharibika. Kuna hali ya ajabu ya kutelekezwa kwa kanuni, kiwango cha maadili kimeshushwa, na dunia inazidi kufanana na Sodoma kwa kasi. Matendo yaliyoleta hukumu ya **Mungu** juu ya ulimwengu wa kabla ya gharika, na yaliyosababisha Sodoma kuchomwa kwa moto, yanaongezeka kwa kasi. Tuko karibu kufikia mwisho, wakati dunia itatakaswa kwa moto. **—Gospel Workers, uk. 125, 126 (1915).** {*EVsw 678.1}*

Wahudumu Lengo Maalum la Shetani-Shabaha ya adui

Majaribu maalum ya Shetani yanalengwa kwa wahudumu. Anajua kuwa wahudumu ni wanadamu tu, hawana neema wala utakatifu wao wenyewe; kuwa hazina ya injili imewekwa katika vyombo vya udongo, ambavyo ni uwezo wa **Mungu** tu unaweza kuvifanya kuwa vyombo vya heshima. Anajua kuwa **Mungu** amewaweka wakfu wahudumu kuwa njia yenye nguvu ya wokovu wa roho, na wanaweza kufanikiwa katika

kazi yao mpaka wanaporuhusu Baba wa milele kutawala maisha yao. Kwa hiyo, Shetani hutumia ujanja wake wote kuwaongoza katika dhambi, akijua kuwa cheo chao hufanya dhambi yao kuwa ya kuchukiza zaidi; maana kwa kutenda dhambi, wao hujifanya wahudumu wa uovu. **—Gospel Workers, uk. 124 (1915). {*EVsw 678.2*}**

Kuwa na Msawaziko Kati ya Heshima na Ushirikiano -kubalansi

Somo la usafi, hekima, maadili, viwango na uungwana katika mwenendo ni jambo ambalo hatupaswi kulipuuzia. Tunapaswa kujilinda dhidi ya dhambi za kizazi hiki kilichopotoka. Hebu Mabalozi wa Kristo wasishuke hadi kwenye mazungumzo ya mzaha, au kuwa wa karibu mno na wanawake, walioolewa au wasioolewa. Hebu wajifunze kukaa mahali pao panapofaa kwa hadhi inayopendeza; lakini wakati huo huo wawe wakarimu, wenye moyo wa urafiki (sociable), wema, na waungwana kwa wote. Wajiepushe na kila kilicho cha kawaida au cha mazoea ya karibu kwa mwonekano wa uovu na kutojali. Hii ni ardhi iliyokatazwa, isiyo salama kuweka mguu. Kila neno, kila tendo, linapaswa kuelekezwa juu, kusafisha, kutakasa na kuinua tabia. Kuna dhambi katika kutojali mambo haya. **—Gospel Workers, uk. 125 (1915). {*EVsw 679.1*}**

Kemea Wanawake Kujikomba kwako na kujipendekza

Wakati mwingine utasifiwa na wanaume wanaojikomba kwako, watakusifu kwa kutia chumvi, au kupita kiasi, wakikudanganya, lakini wanawake ndiyo ambao mara nyingi watakusifu na kujikomba kwako. Haswa unapowasilisha Ukweli katika maeneo mapya, utakutana na watu watakaofanya haya kwa hila, yaani watajipendekeza au kujikomba kwako na kukusifu-sifu kwa kutia chumvi. Kama mtumishi wa Kristo, usifurahie upendeleo wa namna hii; uepuke kama vile unavyomkwepa nyoka mwenye sumu. Mkemee mwanamke anayekusifu kwa werevu wako, akishika mkono wako kwa muda mrefu kadiri awezavyo. Usiwe na mengi ya kusema na watu wa namna hii; wao ni mawakala wa Shetani, na hutekeleza mipango yake kwa kuweka mitego ya kuvutia kama uchawi il kukupotosha kutoka njia ya utakatifu. Mwanamke yeyote MKristo mwenye busara atakuwa na staha na uungwana; atafahamu hila za Shetani, na hatakuwa mtendakazi mwenza wa Shetani. {*EVsw 679.2*}

Usijipatie sifa ya kuwa mchungaji anayebainishwa kuwa anapendwa sana na wanawake. Jiepushe na wale ambao kwa hila zao hata kwa udogo tu, wanaweza kudhoofisha lengo lako la kufanya yaliyo sahihi, au kuleta doa kwenye dhamiri yako safi. Usiwape wakati wako au ujasiri wako; maana watakuacha ukiwa umetengwa na nguvu yako ya kiroho. Usifanye jambo lolote miongoni mwa watu usiowajua, ndani ya treni, nyumbani, au mitaani, ambalo linaweza kuwa na mwonekano wa uovu hata ukiwa midogo. **—The Review and Herald, July 8, 1884. {*EVsw 680.1*}**

Epuka Kila Dalili ya Uovu

Mtu anayedai kufundisha Ukweli lakini hupenda sana kuwa karibu na wanawake vijana au mabinti au hata wanawake walioolewa, akigusa au kushika miili yao kwa mazoea yanayotiliwa mashaka, au kuzungumza nao kwa mazoea yasiyo na adabu—muogope mtu huyo; kanuni safi za Ukweli hazijaingia moyoni mwake. Hao sio watendakazi pamoja na Yesu; hawamo ndani ya Kristo, na Kristo haishi ndani yao. Wanahitaji uongofu wa kweli kabla **Mungu** hajakubali kazi yao. Ukweli wa asili ya mbinguni hauwezi kumshusha mpokeaji, hauwezi kumpeleka kwenye mazoea yasiyo ya heshima; badala yake, humtakasa muumini, huboresha ladha yake, humuinua na kumtukuza-kumboresha, na humleta katika ushirika wa karibu na Yesu. Huweka moyoni amri ya Paulo ya kujiepusha hata na mwonekano au sura yoyote ya uovu, ili mema yake yasisingiziwe kuwa uovu... {*EVsw 680.2*}

Watu wanaofanya kazi ya **Mungu** na ambao Kristo anaishi mioyoni mwao hawatashusha kiwango cha maadili, bali daima watatafuta kukitukuza. Hawatafurahia kusifiwa-sifiwa kwa hila, au kutongozwa na wanawake, kudekeshwa, na kufanywa vipenzi (pets) au kufanyiwa urafiki wa kimahaba nao. Vijana na hata wale waliokwisha kuoa waseme, “weka Mikono yako mbali! (hands off) Sitatoa nafasi yoyote kwa mema yangu kusemwa mabaya.” Jina langu jema ni mtaji wenye thamani kubwa kuliko dhahabu au fedha. Hebu nilihifadhi jina hilo ili lisichafuliwe. Na kama watu watalivunjia heshima, haitakuwa kwa sababu mimi niliwapa nafasi kufanya hivyo, bali kwa sababu ya kama ile iliyompata Kristo, kwamba watu walichukia usafi na utakatifu wa tabia ya Kristo; maana ilikuwa ni kemeo la daima kwao. {*EVsw 680.2*}

Ningependa kugusa moyo wa kila mtendakazi katika kazi ya **Mungu** kuwa na maisha ya sala ya daima na bidii. Hawawezi kuwa magotini daima, ila wanaweza kuinua mioyo yao kwa **Mungu** kila wakati. Hivyo ndivyo Henoko alivyotembea na **Mungu**. **—The Review and Herald, November 10, 1885. {*EVsw 681.1*}**

Kujikinga kiroho— "Kuweka Uzio Katika Nafsi"

Kutakuwa na wanawake watakaokuwa wajaribu wa watu, na watafanya kila juhudi kuvutia na kuvuta usikivu wa wanaume kwao. Kwanza, watatafuta huruma yao, kisha mapenzi yao, na hatimaye kuwashawishi wanaume wavunje sheria ya **Mungu**. Wale waliodhalilisha akili na mapenzi yao kwa kuyaelekeza mahali ambapo Neno la **Mungu** limepiga marufuku, hawatasita kumdhalilisha **Mungu** kwa namna mbalimbali za ibada ya sanamu. **Mungu** atawaacha waende kwa tamaa zao chafu. Ni lazima kulinda mawazo; kuiwekea nafsi uzio wa maagizo ya Neno la **Mungu**; na kuwa waangalifu sana katika kila wazo, neno, na tendo, ili tusikumbwe na kusalitiwa kutenda dhambi. **—The Review and Herald, May 17, 1887. {*EVsw 681.2*}**

Kulinda Vizuizi vya Maadili

Adui wetu mkuu ana mawakala wake wanaowinda daima fursa na nafasi ya kuharibu roho, kama vile simba awindavyo mawindo yake.... Kinga moja ikiondolewa katika dhamiri, kwa kuendekeza mazoea mabaya, au kupuuzia wajibu wa juu kwa muda mfupi, kunaweza kuwa mwanzo wa safari ya udanganyifu inayokufanya uingie katika jeshi la wale wanaomhudumia Shetani, huku ukiendelea kudai kumpenda **Mungu** na kazi Yake. Wazo moja la kutojali, au hatua moja ya upotovu, inaweza kugeuza kabisa mkondo wa maisha yako, kuelekea njia isiyo sahihi. Na huenda usijue kilichosababisha maanguko yako hadi itakapotamkwa kwako siku ya hukumu, "Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu." **Mathayo 7:23 —Testimonies for the Church, Gombo la 5, uk. 397, 398 (1885). {*EVsw 681.3*}**

Kuongolewa na Wahudumu Ambao Hawajaongoka

Mtu anaweza kusikia na kukiri Ukweli wote, na bado asiwe na uchaji wa **Mungu** wa Kweli au dini ya kweli ya uzoefu binafsi. Anaweza kufafanua njia ya wokovu kwa wengine, naye mwenyewe akakataliwa. Ukweli ni mtakatifu na wenye nguvu, na hupeleleza makusudi na nia za moyo. Umuhimu na mamlaka ya Ukweli katika mpango mkuu wa wokovu unatokana na Asili Yake ya Kiungu, Yeye Ndiye Mwanzilishi na kwamba vyombo visivyo vitakatifu vinavyoutangaza Ukweli, haviwezi kuufanya kuwa batili au usiofaa. **{*EVsw 682.1*}**

"Mwanamume mmoja aliyeendelea mwovu na bado alikuwa akitenda uovu aliuliza, 'Kwa nini roho zinageukia Ukweli kupitia ushawishi wangu?'" Nikamjibu, "Kristo daima huzivuta roho Kwake, na Humulika nuru katika njia yao. Mtafutaji wa wokovu haruhusiwi kusoma tabia ya anayemfundisha. Akiwa dhati katika kumkaribia **Mungu** kwa imani mwenyewe,a kisha akaaziungama dhambi zake, atakubalika." **—Letter 12, 1890 {*EVsw 682.2*}**

Kipindi cha Mafunzo ya Huduma

Vijana Waingie Katika Safu za Mbele (internship)

Kuna vijana waaminifu wanaojiandaa kuingia kazini, ili kuimarisha ngome za mbele. Wakitembea kwa unyenyekevu na **Mungu**, Yeye Atazungumza nao na kuwafundisha. Kwao ningependa kusema, Fanya kazi pale ulipo, fanya kila uwezalo kueneza Ukweli uliodhahiri kuwa wa thamani kwako. Dumisha unyenyekevu, na kisha, panapotokea nafasi ya kujazwa, utasikia maneno haya: Rafiki, panda juu zaidi. Unaweza kusita kusonga mbele, lakini songa kwa kumwamini **Mungu**, ukileta katika kazi Yake uzoefu mpya, wa dhati, na moyo uliojaa uaminifu na imani ifanyayo kazi kwa upendo na kuitakasa nafsi. Unapopatwa na kiu ya maji ya uzima, muombe Kristo, naye atakupa kunywa maji ya uzima bure. Yeye atakuwa kwako kisima cha maji, yakibubujika hata uzima wa milele. —**Letter 9, 1899 {*EVsw 682.3*}**

Mwanzo Sahihi Hufanikisha Huduma

Faida ya vijana wanaohisi kuitwa na **Mungu** kuhubiri inategemea sana namna watu wanavyoanza kazi yao. Wale wanaochaguliwa na **Mungu** kwa ajili ya huduma watatoa uthibitisho wa wito wao wa juu, na kwa kila njia watajitahidi kuwa watenda kazi hodari. **—The Acts of the Apostles, uk. 353 (1911) {*EVsw 683.1*}**

Kuanza Kazi Wakiwa Pamoja na Wahudumu Wakongwe

Katika maandalizi ya kazi ya huduma, vijana wanapaswa kuambatana na wahudumu wakongwe. Wale waliopata uzoefu katika huduma hai wanapaswa kuwachukua vijana wasiokuwa na uzoefu kwenye shamba la mavuno, wakiwafundisha jinsi ya kufanya kazi kwa mafanikio kwa ajili ya wokovu wa roho. Kwa upole na kwa upendo, hawa wakongwe wanapaswa kuwasaidia vijana kujiandaa kwa kazi ambayo Bwana atawaita kuifanya. Na vijana walio katika mafunzo wanapaswa kuheshimu ushauri wa waalimu wao,

wakikumbuka kujitolea kwao kazi na kukumbuka kwamba miaka ya kazi yao imewapa hekima... {*EVsw 683.2*}

Watendakazi wakongwe na wawe waalimu, wakijishikilia chini ya nidhamu ya **Mungu**. Hebu vijana waone kuwa ni fursa ya pekee kujifunza kutoka kwa wakongwe, na wabebe kila mzigo kadiri umri, ujana na uzoefu wao unavyoruhusu. Hivyo ndivyo Eliya alivyowafundisha vijana wa Israeli katika shule za manabii; na leo vijana wanapaswa kupata mafunzo sawa. Haiwezekani kushauri kila jambo maalum la kufanya, lakini wanapaswa kufundishwa kwa uaminifu na kuonyeshwa kumtegemea Yeye aliye mwanzilishi na mkamilishaji wa imani yetu na watendakazi wakongwe. **—Gospel Workers, uk. 101, 102 (1915)** {*EVsw 683.3*}

Kufanya Kazi Pamoja, Lakini Wasinakili Tabia za Wakongwe

Wanaoanza bila uzoefu hawapaswi kutumwa peke yao. Wapaswa kusimama karibu na wahudumu wazoefu, ambao wanaweza kuwafundisha. Lakini wahudumu wakongwe wawambie wazi: "haupaswi kuiga ishara zangu, wala toni yasauti yangu, hata watu wasijue kama ni mimi au wewe unayezungumza. Wewe simama na silaha zako mwenyewe, kwa awamu na tabia yako binafsi, iliyotakaswa na **Mungu**." Haupaswi kuchukua awamu yangu ya tabia yangu, wala ishara zangu, wala sauti yangu,wala maneno yangu. {*EVsw 684.1*}

Nimeonyeshwa jambo hili mara nyingi—karibu mara ishirini katika maisha yangu. Nimekuwa nikijaribu kuwaambia ndugu, lakini uovu wa tatizo bado halijarekebishwa. Wakati mtu asiye na uzoefu anasimama karibu yako wewe mhubiri mkongwe, hebu asifikirie kila jambo kama unavyofikiria, au kuliona kama unavyoliona; kiasi kwamba pale utaamua kuacha ile Kweli, naye asiseme: "Basi nami naacha." Waachwe wapate usawaziko wa tabia kutoka kwa **Mungu** wa mbinguni; si kutoka kwa mawazo yako, au mtindo wako wa kufanya mambo, kisha ukawa na ushawishi uliofinyangwa na kuganda-waache waelekezwe kwenye Biblia kama kielelezo chao. Uzito wa jambo hili umeonyeshwa kwangu mara nyingi kiasi kwamba najihisi kuwa na mzigo mzito juu yake. —**Manuscript 19b, 1890** {*EVsw 684.2*}

Wasikandamizwe wala Kukatishwa Tamaa

Mungu hakuwahi kupanga kwamba mawazo na mipango ya mtu mmoja ichukuliwe kuwa ndiyo ya mwisho. Anasema: "Ninyi ni watendakazi pamoja na **Mungu**." Hebu mtu asijaribu kuwakandamiza wengine au kuwakata tamaa. Hebu asiwavalishie mavazi yake ya vita ndugu zake, maana hawajazijaribu... Wachungaji wasinase tabia ya kuiga ishara za mtu yeyote, tabia, mazoea, mwenendo, kuzungumza kwake mtazamo, au sauti yake. Wasifanywe kuwa vivuli vya mtu mwingine katika mawazo, hisia, au mipango. Ikiwa **Mungu** amekufanya kuwa mchungaji wa kundi, basi amekupa stahiki/sifa zinazostahili kazi hiyo. — **Manuscript 104, 1898.** {*EVsw 685.1*}

Vijana Walioitwa Katika Huduma ya Mstari wa Mbele

Wanaume wenye nywele za mvi wanapaswa kutembea kwa tahadhari na hekima na kuwapa vijana wanaojitahidi kukua kila fursa ya kuja mbele. Wazee wasione kuwa ni kutoheshimiwa na vijana, ambao lazima watumie vipawa vyao, na kushika nafasi zao binafsi, na kuwa watu wanaoaminika, na wanaowajibika kusonga mbele. Wale wazee wanapaswa kuwahimiza vijana kuendeleza vipawa vyao. {*EVsw 685.2*}

Tunahitaji watu watakaochukua kazi kana kwamba wanamaanisha kweli. Vijana lazima wapewe fursa ya kukua. **—Letter 97, 1896.** {*EVsw 685.3*}

Wapate Kutambuliwa

Kristo alikubali kushuka chini ili wanafunzi Wake waende mbele ya makundi makubwa ya watu ili kuwajengea stahiki na heshima, kwamba wengi wangetambua katika matendo yao kuwa walifanya kazi kama vile Kristo alivyofanya. Matendo yale yale ya rehema yaliyofanywa na Bwana wetu yatafungua mlango kwa wanafunzi wake. **—Letter 252, 1906.** {*EVsw 685.4*}

Vijana Katika Shule ya Nidhamu

Hebu tuwatendee kwa heshima vijana wa familia ya Bwana. Vijana wanaoanza huduma wanaweza kufanya makosa mengi, lakini hata wachungaji wakongwe hawako huru dhidi ya makosa, ijapokuwa wamekuwa wakifanya kazi kwa miaka mingi. Bwana Mwenyewe atawashughulikia vijana hawa, wakati mwingine akiwaadhibu na kuwaruhusu wapate maumivu kwa makosa yao, lakini kamwe hatawaacha. Yeye Atawapa nafasi ya kuwa washiriki wa familia ya kifalme—watoto wa Mfalme wa mbinguni. **—Manuscript 127, 1902.** {*EVsw 685.5*}

Vijana Wanaoitwa Katika Shamba la Mavuno

Bwana anawaita vijana kuingia katika shamba la mavuno na kufanya kazi kwa bidii kama watenda kazi wa mavuno. Anawaita kufanya kazi kwa ajili Yake, si kufanya kazi kati ya makanisa yaliyokwisha kusimikwa, bali waungane na watendakazi wenye uzoefu katika kazi kubwa ya mavuno. Hebu vijana wenye uwezo waende na kutendea kazi vipawa vyao. Na wakienda, hebu wategemee uongozi wa Bwana... {*EVsw 686.1*}

Hii ndiyo kazi ambayo vijana wanapaswa kuhamasishwa kuifanya, si kuhubiria hadhira isiyohitaji huduma yao isiyokomaa, hadhira ambayo inatambua hali hiyo, na haihisi mvuto wa Roho. Bwana hajawapa vijana kazi ya kuwa kati ya makanisa. Wajibu wao wa kwanza ni kujifunza somo katika nyanja mbalimbali kutoka kwa Mwalimu Mkuu... {*EVsw 686.2*}

Kristo aliwaambia wanafunzi Wake nini? “Mtu akinitumikia, na anifuate.” Hii ndiyo kanuni iliyotolewa katika Neno la **Mungu**. Kwa kujifunza maisha ya Kristo, hebu watendakazi wajifunze jinsi alivyokuwa akiishi na kufanya kazi. Na kila siku wajaribu kuishi maisha ya Kristo, wakitafuta kujua njia ya Bwana. **—Manuscript 75, 1900.** {*EVsw 686.3*}

Baada ya Majaribio ya Mwaka Mmoja

Kwa wale wanaoitwa katika kazi ya huduma, Bwana atawapa maarifa, ustadi na ufahamu. Lakini kama baada ya kufanya kazi ya uinjilisti kwa muda wa miezi kumi na miwili katika mavuno na mtu hana matunda ya kuonyesha kwa kazi yake, kama watu aliowahudumia hawajanufaika, kama hajainua kiwango cha ile Kweli katika maeneo mapya, na hakuna nafsi iliyogeuzwa kwa juhudi zake—mtu huyo anapaswa kunyenyekea mbele za **Mungu**, na kujihoji kama kweli hakukosea wito wake. Mshahara wa Konferensi unapaswa kutolewa kwa wale wanaoonyesha matunda ya kazi yao. Kazi ya mtu anayemkiri **Mungu** kama chanzo chake cha nguvu, mwenye uelewa wa Ukweli wa thamani ya roho, na moyo uliojaa upendo wa Kristo, itakuwa na matunda. —**Manuscript 26, 1905.** {*EVsw 686.4*}

Mwito na Uhamisho wa Mtendakazi wa Uinjilisti

Kusonga Mbele kwa Ajili ya Watu Wasioonywa

Mara nyingi wakazi wa miji aliyohudumu Kristo walitamani abaki na kuendelea kufanya kazi miongoni mwao. Lakini aliwaambia kwamba Yeye hana budi kwenda katika miji mingine ambayo bado haijasikia Kweli aliyoletwa kuihubiri. Alipokwisha kuwapa watu wa mahali pamoja ujumbe wa Kweli, aliwaacha wajenge juu ya msingi alioweka, Naye akaendelea katika miji mingine. Njia hizi za kazi ndizo zinazopaswa kufuatwa leo na wale walioachiwa kazi Yake. Tunapaswa kuhama kutoka eneo moja hadi jingine tukibeba ujumbe wa wokovu. Mara tu ujumbe wa kweli unapohubiriwa katika sehemu moja, tunapaswa kwenda kuwaonya wengine. **—Manuscript 71, 1903.** {*EVsw 687.1*}

Kuhama Pale Wingu Linapoondoka

Usiwe na msukosuko wala usikate tamaa ; vaa silaha ya vita kwa utayari mwilini mwako, imarisha nafsi yako kwa **Mungu**, nawe utaweza kushinda kwa ujasiri. Ndani ya **Mungu** ndipo nguvu na ufanisi wetu.... Wingu likiondoka, na **Mungu** akaonyesha wajibu wako wa kufungua kazi katika eneo jingine, unaweza kuhama kwa ufahamu. Lakini usiache kazi katika uwanja ambapo kazi nyingi imekwishafanywa na bado kuna kazi zaidi ya kufanywa. **—Letter 77, 1895.** {*EVsw 687.2*}

Sauti ya Wajibu

Sauti ya wajibu ni sauti ya **Mungu**—miongozo ya ndani kutoka mbinguni. **—Counsels on Health, uk. 562 (1896).** {*EVsw 688.1*}

Kujua Kama Mungu Anaongoza

Hatupaswi kuweka jukumu la wajibu wetu juu ya wengine, tukisubiri watuambie cha kufanya. Hatupaswi kutegemea ushauri wa wanadamu. Bwana atatufundisha wajibu wetu kama ambavyo angefundisha wengine. Tukimwendea Yeye kwa imani, Atatufunulia mafumbo na kutuambia siri Zake binafsi.... Wale wanaoazimia kutofanya lolote litakalomchukiza **Mungu**, watakapowasilisha jambo lao mbele zake kwa sala, watajua wazi hatua ya kuchukua. Nao watapokea sio hekima tu, bali pia nguvu. **—The Desire of Ages, uk. 668 (1898).** {*EVsw 688.2}*

Watendakazi Wenye Hisia za Wajibu

Katika kila hatua ya kusonga mbele ambayo **Mungu** ametuelekeza kupiga, kila hatua ya ushindi kwa watu Wake, kumekuwa na vyombo vya Shetani miongoni mwetu nyuma yetu-watu waliokuwa tayari kutoa mashaka, kutia moyo wa kukata tamaa, na kuweka vizuizi mbele yetu ili kudhoofisha imani na ujasiri wetu. Tumelazimika kusimama kama mashujaa wa vita, tukiwa tayari kupigana na kusonga mbele katikati ya upinzani. Hii imefanya kazi yetu kuwa mara kumi ngumu zaidi kuliko ingekuwa. Tumelazimika kusimama imara kama mwamba, bila kujisalimisha kwa adui.... {*EVsw 688.3}*

Wapo wengine... ambao hawaonekani kuwa na nanga. Watu wa namna hii wameharibu kazi ya Kweli kwa kiasi kikubwa. Wapo pia ambao hawaonekani kuwa na msimamo wa kudumu, hawawezi kusimama imara wakati **Mungu** anaita wapiganaji waaminifu kuwa katika nafasi zao.... Wengine hawana kabisa wazo la kujitosa kwa jambo lolote au kudiriki kujitoa dhabihu mwenyewe. Lakini mtu fulani hana budi kufanya hivyo; mtu fulani lazima ajitokeze na kubeba hatari ya kujitosa na kuthubutu kwa ajili ya kazi hii. **—Testimonies for the Church, Juzuu ya 3, uk. 315-316 (1873).** {*EVsw 688.4}*

Wainjilisti Wakamilishe Juhudi Zao (efoti zao)

Sina taarifa za kina kuhusu hali ya Mzee -----, isipokuwa kwamba amekuwa akitumika na **Mungu** kwa kazi Yake huko Los Angeles, na amekuwa akibarikiwa sana. Zaidi ya watu mia moja wamesimama kwa ajili ya Kweli kutokana na juhudi zake. Mwishoni mwa mfululizo wa mikutano yake ya hemani, alifikiria kuhamia uwanja mwingine, lakini alipokea ombi lililosainiwa na watu wengi wa jiji hilo likimtaka aendelee na mikutano hiyo. Bwana amempa Ndugu ----- roho ya kuendana na mambo na kuyaratibu kulingana na mazingira, pamoja na amembariki kwa hekima ya kupanga na kutekeleza kazi yake, na amemfanikisha katika kuandaa vijitabu vidogo, matangazo, na chati ambazo zimeamsha shauku ya watu. {*EVsw 689.1}*

Napendekeza kwamba Ndugu ----- aendelee kufanya kazi mahali ambapo ujumbe wake unaonekana kutekeleza matokeo mema na makubwa. Wale wanaohudhuria mikutano yake wametoa msaada wa fedha kwa hiari yao ambayo imeendeleza kazi hiyo.... {*EVsw 689.2}*

Kwa sasa, na hebu na abaki Los Angeles, California, kwa kuwa Bwana anamfanikisha kwa namna ya pekee kuwafikia watu. Hebu na apige tarumbeta ya ujumbe wenye sauti iliyo dhahiri, akiwaamsha wale ambao hawajawahi kusikia ile Kweli. Bwana na amtie moyo aendelee kubaki Los Angeles hadi washiriki wa kanisa waamshwe na kujifunga silaha za kiroho viunoni mwao, wakionyesha kuwa nao pia wana mzigo wa kupeleka ujumbe.... {*EVsw 689.3}*

Asikubali mtu yeyote, kwa maneno au kwa mfano, kumvuta Mzee ----- kutoka kwenye kazi aliyopewa na **Mungu**. Wote na washirikiane naye katika juhudi za kuendeleza kazi hiyo kwa mistari iliyo wazi. **—Letter 75, 1905.** {*EVsw 689.4}*

Kanuni za Mwongozo wa Kumwita Mwinjilisti

Kuhusu iwapo ni sawa kwa Mzee ----- kuondoka Los Angeles na kwenda kufanya kazi kwa muda katika mji wa Kaskazini, niseme kwamba mara nyingine ni lazima tumwaachie mtu mwenyewe ajiamulie mambo haya. Kuna uhamishaji mwingi wa watu wanaofanya kazi njema—kazi ambayo Bwana amesema inapaswa kufanywa. Wakati mwingine, mtu anapokuwa akifanikiwa katika kazi yake na watu wanaonyesha shauku kubwa, swali la kumhamisha halipaswi kabisa kumjia, maana humtia mkanganyiko. Ikiwa Bwana anachochea watu wa Los Angeles kwa nguvu kupitia mikutano ya hemani, basi hakuna jambo linalopaswa kuingilia kati kazi hiyo.... Hebu mtu asimvute mtu yeyote Ndugu ----- kutoka mahali ambapo kuna maslahi makubwa na fursa ya kipekee ya kuwasilisha Kweli. Hii ni fursa ya Los Angeles. **—Letter 193, 1905.** {*EVsw 689.5}*

Watendakazi Kuumizwa kwa Kuhamishwa Bila Sababu

Ninaamini si vyema kuwatoa watendakazi kutoka sehemu moja ya shamba la mizabibu ambapo wanafanya kazi nzuri, na kuwapeleka sehemu nyingine ya kuanza upya. Nafikiri jambo hili huwapa mawazo kwamba wao ni watu wa umuhimu mkubwa kuliko walivyo kweli, na huwadhuru kiroho. Nawashauri kuwa waangalifu sana kuhusu kubadilisha watendakazi pasipo na sababu ya msingi. —**Letter 179, 1900.** {*EVsw 690.1*}

Kuhama Mapema Kunavyowaathiri Waongofu

Nilijua kwamba Ndugu na Dada ----- hawakuwa huru dhidi ya mapungufu, lakini walikuwa wakijitahidi kumjua na kumtendea Bwana mapenzi Yake, na walikuwa na vipawa vya kuwafikia watu wa hadhi ya juu, na kwamba kupitia kazi yao wengi wangeweza kuvutiwa na kweli. Nilijua pia kwamba kuhamishwa kwao kungeinyima sehemu hiyo muhimu ya kazi iliyokuwa inahitajika sana, na pia kwamba uhamisho huo ungewagharimu sana kibinafsi, kwa kuwa walikuwa wameanza tu kustawi katika makazi yao mapya. Sikuona uhuru wa kutumia ushawishi wangu ili kuwahamisha. {*EVsw 690.2*}

Uhamisho wao chini ya hali hizo ungesababisha mtazamo mbaya katika fikra za wale waliokuwa wamekubali imani mpya kupitia juhudi zao. Zaidi ya hayo, kama ni kweli walikuwa na tabia zisizofaa, hali hiyo isingebadilishwa kwa kuwapeleka sehemu nyingine, maana wangekwenda na tabia na mbinu hizo hizo zisizofaa. **—Letter 48, 1907.** {*EVsw 690.3*}

Kuwahamisha Watu Mapema Sana—Njama ya Shetani

Kama mtumishi angekataa kabisa kusikiliza taarifa zilizopotoshwa na zisizo kamili kutoka kwa watu fulani, na badala yake kutoa ushauri kulingana na kanuni za Biblia na kusema kama Nehemia, “Nafanya kazi kubwa, siwezi kushuka,” basi kanisa hilo lingekuwa katika hali bora zaidi.

Huu mwenendo wa kuwaondoa watumishi kutoka kwenye mashamba yao ya kazi umetokea tena na tena katika maendeleo ya kazi hii. Hii ni hila ya adui mkuu wa roho ili kuzuia kazi ya **Mungu**. Wakati roho ziko karibu kuchukua uamuzi kwa ajili ya Kweli, huachwa wazi kwa ushawishi usiofaa, na mara chache sana msukumo huo mkubwa huweza kurudiwa. Shetani kila mara hutafuta njia ya kumvuta mhubiri kutoka kwenye uwanja wa kazi katika kipindi hicho nyeti, ili matokeo ya kazi yake yapotee. **—Manuscript 1, 1878.** {*EVsw 691.1*}

SEHEMU YA 20 — UJUMBE WA USHINDI

Wakati Sauti Kuu Inapopiga

Kweli Itashinda Karibu — Mwisho umekaribia, ukitujia kwa siri, kama mwizi, bila kuonekana, kama ujio usio na kelele wa mwizi usiku. Hebu Bwana atujalie tusilale tena kama wengine, bali tukeshe na kuwa na kiasi. Kweli hivi karibuni itashinda kwa utukufu, na wote wanaochagua sasa kuwa watenda kazi pamoja na **Mungu** watashinda Pamoja nayo. Muda ni mfupi; usiku waja upesi ambapo hapana mtu awezaye kufanya kazi. **—Testimonies For The Church 9:135 (1909).** {EVsw 692:1}

Kuongoka Kama Siku ya Pentekoste — Wakati unakuja ambapo watu wengi wataongoka siku moja kama ilivyokuwa katika siku ya Pentekoste, baada ya wanafunzi kupokea Roho Mtakatifu. **—The Review and Herald, June 29, 1905.** {EVsw 692:2}

Maelfu Bado Wataingia Katika Nuru — Wengi wamepuuza mwito wa injili; wamejaribiwa na kutahiniwa, lakini vizingiti vikubwa kama milima, vimeonekana mbele yao vikizuia mbele yao. Kwa imani, uvumilivu, na ujasiri, wengi watazidi vizingiti hivi na kutembea kuelekea nuru ya utukufu. {EvVw 692:3}

Bila hata wao kujua, vizuizi vimesimikwa katika njia nyembamba na ngumu; mawe ya kuangusha yamewekwa njiani; yote haya yatabiringishwa na kuondolewa. Vizingiti vya usalama binafsi ambavyo wachungaji wa uongo wameviweka kuzunguka makundi yao vitaanguka kuwa haina maana; maelfu watajitokeza kwenye nuru na kufanya kazi ya kueneza nuru hiyo. Akili za mbinguni zitaungana na watendakazi wa dunia. Kwa kuhamasishwa hivi, kanisa litainuka na kuangaza, likitumia nguvu zake zote zilizo takatifu katika mapambano; kwa hivyo mpango wa **Mungu** utafanikiwa; vito vilivyopotea vitarejeshwa. {EVsw 692:4}

Manabii waliona kazi hii kubwa kutoka mbali, wakaudaka msukumo wa wakati, na kuandika maelezo ya ajabu ya mambo ambayo bado hayajatokea. **—The Review and Herald, July 23, 1895.**{EVsw 693:1}

Wengi Waliorudi nyuma kiroho, Watarudi tena — Wakati dhoruba ya mateso itakapovunja Kweli juu yetu, kondoo wa kweli watawasikia sauti ya mchungaji wa kweli. Jitihada za kujitolea zitafanywa kuokoa waliopotea, na wengi waliotengana na kundi watarudi kumfuata mchungaji mkuu. Watu wa **Mungu** wataungana, wakimkabili adui kwa mshikamano.... Upendo wa Kristo, upendo wa ndugu zetu, utathibitisha ulimwenguni kuwa tumekuwa na Yesu na tumemejifunza kuhusu Yeye. Ndipo ujumbe wa malaika wa tatu utaongezeka hadi kuwa Kilio Kikuu (loud cry), na dunia nzima itajazwa na utukufu wa Bwana. **—Testimonies For The Church 6:401 (1900).**{EVsw 693:2}

Ushawishi wa Vyombo vya Habari kama Vile Nyumba ya Uchapaji, media nk — **Mungu** atatenda mambo makubwa kwetu hivi karibuni, kama tutaabudu kwa unyenyekevu na imani mbele Zake.... Zaidi ya watu elfu moja wataongoka kwa siku moja, wengi wao ambao watagundua kwamba usadikisho wao na kupokea imani vilikuja kwa kusoma machapisho yetu. **—The Review and Herald, November 10, 1885.**{EVsw 692:3}

Nguvu ya 1844 Itajirudia — Nguvu ambayo iliwachochea watu kwa nguvu kubwa katika harakati ya mwaka 1844 itaonekana tena. Ujumbe wa malaika wa tatu utaenda, si kwa sauti ya chini ya kunong'ona, bali kwa kilio kikuu. **—Testimonies For The Church 5:252 (1885).**{EVsw 693:4}

Sauti Kuu — Wakati wa sauti kuu, kanisa, likisaidiwa na ushawishi wa **Mungu** mkuu wake aliye juu, litaeneza maarifa ya wokovu kwa wingi kiasi kwamba nuru itafikia kila jiji na mji. Dunia itasheheni na maarifa ya wokovu. Roho mtakatifu wa **Mungu** atakuwa amesababisha mafanikio makubwa kwa mashirika yenye shughuli nyingi, hata nuru ya Kweli ya sasa itaonekana ikimetameta kila mahali. **—The Review and Herald, October 13, 1904.**{EVsw 694:1}

Sababu ya Kucheleweshwa

Kucheleweshwa Kwa Rehema — Usiku mrefu wa giza ni changamoto, lakini asubuhi imechelewa kwa sababu za rehema, kwa maana kama Bwana angekuja, wengi wangekutwa hawako tayari. Kutokuwa na hamu kwa **Mungu** kuwa watu Wake wafe, ndilo sababu ya kucheleweshwa kwa muda mrefu**. —Testimonies For The Church 2:194 (186).**{EVsw 694:2}

Kazi Ingeweza Kumalizika — Kama watu wa **Mungu** wangefuata magoli/mpango wa **Mungu** katika kutoa ujumbe wa rehema duniani, Kristo angekuja hapa duniani hivi karibuni, na watakatifu wangeongozwa kuelekea mji wa **Mungu kwa makaribisho makubwa**.—**Testimonies For The Church 6:450 (1900).**{EVsw 694:3}

Watu wa Mungu Wangekuwa Katika Kanaani Mbinguni — Najua kama watu wa **Mungu** wangehifadhi uhusiano wa kweli na **Mungu**, na wangezizuia amri Zake, wangekuwa leo katika Kanaani ya mbinguni. **—The General Conference Bulletin, March 30, 1903.**{EVsw 694:4}

Shetani Amejua siri na hivyo amejipatia faida kutoka kwa wanadamu (steal on a march) — Kama kila mlinzi katika kuta za Sayuni angepiga tarumbeta kwa sauti fulani, dunia ingeweza kupata ujumbe wa onyo hivi karibuni. Lakini kazi iko nyuma kwa miaka mingi. Wakati watu walilala, Shetani aliwapita na mbele kwa hila ili ajinufaishe (aliwaovateki wanadamu katika kipindi fulani)**. —Testimonies For The Church 9:29 (1909).**{EVsw 694:5}

Hakuna Kushindwa kwa Ahadi za Mungu — Malaika wa **Mungu** katika ujumbe wao kwa watu wanasema wakati ni mfupi sana, hivi ndivyo imewakilishwa kwangu mara nyingi. Ni kweli kuwa wakati umeendelea zaidi kuliko tulivyotarajia mwanzoni mwa ujumbe huu. Mwokozi wetu hakutokea haraka kama tulivyohitaji. Lakini Je, Neno la Bwana limefeli? Kamwe! Inapaswa kukumbukwa kuwa ahadi na vitisho vya **Mungu** ni vya masharti.{EVsw 695:1}

Mungu aliwakabidhi watu Wake kazi ya kufanikisha hapa duniani. Ujumbe wa malaika wa tatu ulikuwa Kutolewe, akili za waumini zielekezwe katika hema la Patatifu pa mbinguni, ambako Kristo aliingia kufanya dhabihu kwa watu Wake. Matengenezo ya Sabato yalipaswa kusonga mbele. Mvunjiko wa sheria ya **Mungu** kulipaswa kurekebishwa -Mpasuko wa sheria ya Mungu. Ujumbe ulipaswa kutangazwa kwa sauti kuu, ili wakazi wote wa dunia wapokee onyo. Watu wa **Mungu** walipaswa kusafisha nafsi zao kwa kuutii Ukweli na kujiandaa kusimama wasio na dosari mbele Zake wakati wa kuja Kwake.{EVsw 695:2}

Kama wanamarejeo 'Waadventista', baada ya kukata tamaa kubwa mwaka 1844, wangehifadhi imani yao na kuendelea kwa mshikamano katika mpango, na kufunguliwa kwa majaliwa ya **Mungu**, wakipokea ujumbe wa malaika wa tatu na kwa nguvu ya Roho Mtakatifu kuta ngaza kwa ulimwengu, wangeona wokovu wa **Mungu**, Bwana angekuwa na nguvu na juhudi zao, kazi ingekamilika, na Kristo angekuja hivi karibuni kuwapokea watu Wake kwa thawabu. Lakini wakati wa shaka na kutokuwa na uhakika baada ya kukata tamaa, wengi wa waumini wa Marejeo walipoteza imani yao..... Hivyo kazi ilizuiliwa, na dunia ikaachwa gizani. Kama kikundi kizima cha Wanamarejeo kingeungana juu ya amri za **Mungu** na imani ya Yesu, historia yetu ingekuwa tofauti sana kwa kiasi gani!{EVsw 695:3}

Haikuwa mapenzi ya **Mungu** kucheleweshe kuja kwa Kristo kwa namna hii. **Mungu** hakukusudia watu wake, Israeli, wapite miaka arobaini jangwani. Yeye Aliahidi kuwaongoza moja kwa moja katika nchi ya Kanaani, na kuwaweka kuwa watu watakatifu, wenye afya, na wenye furaha. Lakini wale waliotangazwa kwanza, hawakuingia kwa sababu ya ukosefu wa imani. Mioyo yao ilijaa malalamiko, kuasi, na chuki, na hakuweza kutimiza Agano Lake nao.{EVsw 696:1}

Kwa miaka arobaini, ukosefu wa imani, kulalamika, na uasi viliwazuia Israeli wa kale kuingia nchi ya Kanaani. Makosa yale yale yamechelewesha kuingia kwa Israeli wa kisasa katika Kanaani ya mbinguni. Katika hali zote mbili, ahadi za **Mungu** hazikuwa na makosa. Ni ukosefu wa imani, ulimwengu, kutokujitoa wakfu, na ugomvi kati ya watu wa **Mungu** waliodai kuishi kwaajili Yake, vilituweka katika dunia hii ya dhambi na huzuni kwa miaka mingi. **—Manuscript 4, 1883.**{EVsw 696:2}

Usimwekee Mungu Lawama — Tunaweza kuhitaji kubaki hapa duniani kwa sababu ya kutotii, kwa miaka mingine mingi kama watoto wa Israeli; lakini kwa ajili ya Kristo, watu Wake wasizidishe dhambi kwa kumlaumu **Mungu** kwa matokeo ya maamuzi yao mabaya. **—Letter 184, 1901.**{EVsw 696:3}

Tunaweza Kuharakisha Siku Ya Kuja kwa Bwana — Kwa kutoa injili kwa dunia, tunaweza kuharakisha kurudi kwa Bwana wetu. **—The Desire of Ages, 633 (1898).** {EVsw 696:4}

Ni fursa na haki ya kila MKristo si tu kutegemea ujio wa Kristo, bali hata pia kuharakisha kuja Kwake Bwana Yesu Kristo. Kama wote wangezaa matunda kwa utukufu Wake, dunia nzima ingepambwa haraka na mbegu ya injili. Haraka mavuno ya mwisho yangeiva/yangekomaa shambani, na Kristo angekuja kukusanya nafaka yenye thamani. **—Testimonies For The Church 8:22, 23 (1904).**{EVsw 696:5}

Wakati Ujumbe Utakapokamilika — Kuja Kwake [Bwana] hakutachelewa baada ya ujumbe kufika kwa mataifa yote, lugha zote, na watu wote. Je, sisi tunaodai kuwa wasomi wa unabii tutaweza kusahau kuwa uvumilivu wa **Mungu** kwa waovu ni sehemu ya mpango mpana na wenye rehema anaotumia kumfikia mwanadamu kwa wokovu? **—The Review and Herald, Juni 18, 1901.**{EVsw 697:1}

Nguvu ya kuimaliza kazi

Kwa Nini Wengi Wamefeli/wameshindwa Katika Kuongoa Nafsi

Wengi huwasilisha mafundisho na nadharia za imani yetu; lakini uwasilishaji wao ni kama chumvi isiyo na ladha; kwa kuwa Roho Mtakatifu hafanyi kazi kupitia huduma yao isiyo na imani. Hawajafungua mioyo yao kupokea neema ya Kristo; hawaujui utendaji wa Roho; ni kama unga usioumuka kwa vile hauna hamira, kwa kuwa hakuna kanuni ya maisha katika kazi yao yote, nao hushindwa kuwaleta watu kwa Kristo. Hawatumii sifa na haki ya Kristo; ni kama vazi ambalo hawajawahi kulivaa, utimilifu ambao haujafahamika kwao, kisima ambacho hawajawahi kukigusa.{EVsw 697:2}

— The Review and Herald, Novemba 29, 1892.

Uhitaji wa Bidii ya Kuwaathiri Wasioamini

Tunahitaji kuwa dhati na bidii zaidi katika kazi ya Kristo. Ujumbe wa Kweli wenye uzito unapaswa kutolewa kwa nguvu ya kusisimua ambayo itawaathiri wasioamini kuwa **Mungu** anafanya kazi pamoja na juhudi zetu, kwamba Yeye Aliye Juu Ndiye chanzo chetu hai cha nguvu. **— The Signs of the Times, Desemba 9, 1886.**{EVsw 697:3}

Wakati tunapoileta mioyo yetu katika umoja na Kristo, na maisha yetu kuwa sawia na kazi Yake, Roho aliyewashukia wanafunzi siku ya Pentekoste atatushukia nasi pia.{EVsw 697:4}

— The Review and Herald, Juni 30, 1903.

Kwa Ari ya Mitume

Ari kwa ajili ya utukufu wa **Mungu** iliwasukuma wanafunzi kushuhudia Ukweli kwa nguvu kuu. Je, ari hii haipaswi kuwasha mioyo yetu na kututia tamaa ya kuusimulia ujumbe wa upendo wa ukombozi, wa Kristo na Yeye aliyesulubiwa? Je, nguvu ya **Mungu** haipaswi kudhihirishwa kwa nguvu zaidi leo kuliko hata wakati wa mitume? **— The Signs of the Times, February 17, 1914.**{EVsw 698:1}

Chanzo cha Nguvu Yao

Baada ya kupaa kwa Kristo, wanafunzi walikusanyika pamoja mahali pamoja kwa ajili ya kuomba kwa unyenyekevu. Baada ya siku kumi za kuchunguza mioyo na kujichunguza, njia ilifunguliwa kwa ajili ya Roho Mtakatifu kuingia ndani ya hekalu za roho zilizotakaswa na kutengwa kwa ajili ya **Mungu**. Kila moyo ulijazwa na Roho, kana kwamba **Mungu** alitaka kuwaonyesha watu Wake kwamba ni upendeleo na haki Yake kuwabariki kwa baraka za juu kabisa za mbinguni..... Upanga wa Roho ulimeremeta kushoto na kulia. Ukiwa umeongezewa makali mapya kwa nguvu, ukapenya hata kugawanya nafsi na roho, viungo na mafuta ya mifupa. Ibada ya sanamu iliyokuwa imechanganyika na ibada ya watu iliangushwa chini. Maeneo mapya yaliongezwa katika ufalme wa **Mungu**. Mahali palipokuwa tasa na ukiwa zikasikika sifa Zake. **— The Review and Herald, June 10, 1902.**{EVsw 698:2}

Walihisi Mzigo wa Nafsi

Kumbuka kuwa, ilikuwa baada ya wanafunzi kuingia katika umoja kamili, walipoacha kushindania vyeo vya juu, ndipo Roho alipoimiminwa. Walikuwa wa moyo mmoja. Tofauti zote ziliwekwa kando. Na ushuhuda uliotolewa juu yao baada ya Roho kutolewa ulikuwa huu-tafakari: “Wale watu wengi waliomwamini Bwana walikuwa wa moyo mmoja na roho moja.” Roho wa Yeye aliyekufa ili wenye dhambi wapate kuishi, aliwachochea waumini wote.{EVsw 698:3}

Wanafunzi hawakuomba baraka kwa ajili yao wenyewe. Walilemewa na mzigo wa nafsi. Injili ilipaswa kufikishwa hadi miisho ya dunia, nao walidai ule upako wa nguvu za Roho Mtakatifu ambao Kristo alikuwa ameahidi. Ndipo Roho Mtakatifu alipotolewa, na maelfu waliongoka kwa siku moja. **— The Signs of the Times, February 17, 1914.**{EVsw 699:1}

Kanisa Lililoamshwa

Tunapojitoa kikamilifu kwa kazi ya Kristo kwa moyo wote, **Mungu** atatambua jambo hilo kwa kumimina Roho Wake bila kipimo; lakini hili halitatendeka wakati sehemu kubwa ya kanisa haifanyi kazi pamoja na **Mungu**.{EVsw 699:2}

— The Review and Herald, Julay 21, 1896.

Dunia Itaangazwa

Niliona miale ya nuru iliyokuwa ikienda kwa kasi, iking’aa kutoka mijini na vijijini, kutoka sehemu za juu na za chini za dunia. Watu walitii Neno la Mungu, na matokeo yake kulikuwa na kumbukumbu kwa ajili Yake katika kila mji na kijiji. Ukweli Wake ulitangazwa ulimwenguni kote. **— Testimonies for the Church 9:28, 29 (1909).**{EVsw 699:3}

Mamia kwa maelfu walionekana wakitembelea familia, na kuwafungulia Neno la **Mungu**. Mioyo ilisadikishwa na nguvu ya Roho Mtakatifu, na roho ya uongofu wa Kweli ikaonekana. Kila upande milango ilifunguliwa kwa ajili ya kutangazwa kwa Ukweli. Dunia yote ilionekana kung’aa kwa ushawishi wa mbinguni. **— Testimonies for the Church 9:126 (1909).**{EVsw 699:4}

Kupitia Vyombo Vinyenyekevu

Kadiri wakati unavyowadia ambapo ujumbe wa malaika wa tatu utapewa kwa nguvu kuu, Bwana atafanya kazi kupitia vyombo vya unyenyekevu, akiongoza akili za wale wanaojitenga kwa ajili ya huduma Yake. Watenda kazi hawatatunikiwa stahiki kwa mafunzo ya taasisi za elimu bali kwa upako wa Roho Wake badala ya mafunzo kutoka kwenye majengo ya taasisi. Watu wa imani na maombi watalazimika kutoka kwa ari takatifu, wakitangaza Maneno ambayo **Mungu** anawapa. Dhambi za Babeli zitawekwa wazi. Matokeo ya kutisha ya kulazimisha sheria za kanisa kupitia mamlaka ya serikali, kuenea kwa Umizimu wa Kishetani, na maendeleo ya kasi ya mamlaka ya Kipapa—yote yatafichuliwa-barakoa itaondolewa. Kwa maonyo haya yenye

uzito, watu wataamshwa. Maelfu kwa maelfu watasikiliza ambao hawajawahi kusikia maneno kama hayo. — **The Great Controversy, 606 (1888).**{EVsw 699:5}

Umati Utajiunga na Jeshi la Bwana

Wengi..... wataonekana wakikimbia huku na huko, wakisukumwa na Roho wa **Mungu** kupeleka nuru kwa wengine. Ukweli, Neno la **Mungu**, ni kama moto ndani ya mifupa yao, ukiwajaza tamaa kali ya kuwaangazia wale walioketi gizani. Wengi, hata miongoni mwa watu wasioenda shule, sasa wanatangaza Maneno ya Bwana. Watoto wanasukumwa na Roho kwenda kutangaza ujumbe kutoka mbinguni. Roho anamiminwa juu ya wote watakaoitikia mwito Wake, na kwa kuweka kando vyombo na mikakati ya mwanadamu, kanuni zake za kufunga kazi isiende mbele, na mbinu za tahadhari, kisha watatangaza Ukweli kwa nguvu ya Roho. Umati mkubwa utapokea imani na kujiunga na jeshi la Bwana. — **The Review and Herald, Julay 23, 1895.**{EVsw 700:1}

Maelfu ya Sauti Zitasikika Zikitoa Onyo

Watumishi wa **Mungu**, nyuso zao zikiwa zenye mwangaza na kung'aa kwa utakaso mtakatifu, watakimbia kutoka sehemu moja hadi nyingine wakitangaza ujumbe kutoka mbinguni. Kwa maelfu ya sauti, kote duniani, onyo litatolewa. Miujiza itatendwa, wagonjwa wataponywa, na ishara na maajabu yatafuatana na waumini. Shetani pia atafanya kazi kwa maajabu ya uongo, hata kushusha moto kutoka mbinguni mbele ya watu.{EVsw 700:1}

Kwa njia hii wakaaji wa dunia watalazimika kuchukua msimamo wao. Ujumbe hautaenezwa sana kwa hoja za kiakili au mabishano, bali kwa msukumo wa kina wa Roho wa **Mungu**. Hoja zimekwisha wasilishwa. Mbegu imeshapandwa, na sasa itamea na kuzaa matunda. Machapisho yanayogawiwa na wamishenari yamekuwa na ushawishi, lakini wengi ambao akili zao ziliguswa walizuiliwa wasielewe kikamilifu Ukweli au kutii. Sasa miale ya mwanga inaingia kila mahali, Ukweli unaonekana kwa uwazi, na watoto wa **Mungu** waaminifu wanakata minyororo iliyowashikilia. Uhusiano wa kifamilia, wa kidini, hauwezi tena kuwazuia. Ukweli ni wa thamani zaidi kuliko vyote. Pamoja na kuwa maadui wameunganika dhidi ya Ukweli, idadi kubwa watasimama upande wa Bwana. — **The Great Controversy, 612 (1888).**{EVsw 701:1}

Ushuhudiaji wa Roho Mtakatifu

Kushuka kwa Roho Mtakatifu juu ya kanisa huangaliwa kama jambo la siku za usoni; lakini ni Upendeleo na fursa ya kanisa kuupokea sasa. Mtafute Roho Mtakatifute, uombe kwa ajili Yake, na uamini kuwa utapewa. Ni lazima tuwe nao, na Mbingu inausubiri kuutoa. — **The Review and Herald, March 19, 1895.**{EVsw 701:2}

Mvua ya Mwisho-Mvua ya Masika

Waumini... na waombe kwa imani baraka iliyoahidiwa, Nayo itakuja. Kumiminwa kwa Roho katika siku za mitume ilikuwa mvua ya awali-vuli, na matokeo yake yalikuwa ya utukufu. Lakini mvua ya mwisho/masika itakuwa itasheheni zaidi.{EVsw 701:3}

— The Signs of the Times, February 17, 1914.

Fursa ya Saa ya Sasa

Kazi ya Leo

Ujumbe wa malaika wa tatu unazidi kupanuka na kuwa mwito wa sauti kuu-kilio kikuu, na hupaswi kujihisi huru kuacha wajibu wa sasa huku ukiendekeza mawazo ya kwamba wakati fulani ujao utapokea baraka kuu, wakati hakuna juhudi yoyote kutoka kwako, na bado uamsho wa ajabu utatokea.... Leo hii ni lazima chombo chako kisafishwe, kiwe tayari kupokea umande wa mbinguni, tayari kwa mvua ya masika; kwa kuwa mvua ya masika itakuja, na baraka za **Mungu** zitaujaza kila moyo uliosafishwa kutoka kila najisi. Kazi yetu leo ni kujitoa kwa Kristo ili tuweze kufaa kwa ajili ya nyakati za kuburudishwa zitokazo mbele za Bwana—tukifaa kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu.....{EVsw 701:4}

Badala ya kuishi kwa matarajio ya msimu wa msisimko maalum, ni busara kutumia fursa za sasa kwa hekima, tukitenda yale yanayopaswa kufanywa ili nafsi ziokolewe. Badala ya kutumia nguvu za akili katika

kutafakari kuhusu nyakati na majira ambayo **Mungu** ameyaweka katika mamlaka Yake na kuyaficha kwa wanadamu, ni lazima tujitoe chini ya uthibiti wa Roho Mtakatifu, tutimize wajibu wa sasa, tukiwapa watu mkate wa uzima usiochanganywa na maoni ya kibinadamu, kwa nafsi zinazohitaji sana Ukweli. **—The Review and Herald, Machi 22, 1892.**{EVsw 702:1}

Fursa za Kipekee,Ambazo Hatujawahi Kuzipata

Katika siku hizi za usafiri wa kasi (na tovuti), fursa za kukutana na wanaume na wanawake wa kila tabaka na mataifa mengi ni kubwa zaidi kuliko ilivyokuwa siku za Israeli. Njia kuu za usafiri zimeongezeka mara elfu nyingi. **Mungu** ameandaa njia kwa namna ya ajabu. Chombo cha uchapishaji, pamoja na vifaa vyake vingi, Viko mikononi mwetu. Biblia na machapisho katika lugha mbalimbali, yakieleza Ukweli wa wakati huu, yapo tayari na yanaweza kuenezwa kwa haraka kila sehemu ya dunia. {EVsw 702:2}

Ni lazima tuitoe onyo la mwisho la **Mungu** kwa wanadamu, na bidii yetu ya kujifunza Biblia na ari na juhudi yetu ya kueneza nuru kwa dhati inapaswa kuwa kubwa kiasi gani! **-The Review and Herald, January 25, 1906.**{EVsw 702:3}

Mungu Anatoa Fursa Hizi

Pambano kubwa lipo mbele yetu. Ni lazima sasa, kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, tutangaze Kweli kuu za siku hizi za mwisho. Haitachukua muda mrefu kabla kila mmoja kusikia onyo hilo na kufanya uamuzi wake. Ndipo mwisho utakapokuja.... **Mungu** Ndiye Mtendaji Mkuu, na kwa mpango Wake wa Kiungu Hutayarisha njia ili kazi Yake itimie. Yeye hutoa fursa, hufungua njia za ushawishi na njia za utendaji. Ikiwa watu Wake watakuwa waangalifu kuona dalili za majaliwa na mpango Wake, na wawe tayari kushirikiana Naye, hakika wataona kazi kuu ikitimia. **—Testimonies for the Church, 6:24 (1900).**{EVsw 703:1}

Mgogoro wa Kitaifa Waleta Mwamko wa Kidini

Leo hii, watu na mataifa wanajaribiwa na chombo kinachopima mkononi mwa Yule asiyeweza kukosea (kinapima maanguko).....{EVsw 703:2}

Ishara za nyakati zinaonyesha wazi kuwa tunasimama kwenye ukingo wa matukio makuu na ya kusisimua. Kila kitu duniani kiko katika msisimko. Machoni petu unabii wa Mwokozi kuhusu matukio yatakayotangulia kurudi Kwake unatimia: “Nanyi mtasikia habari za vita na uvumi wa vita.... Taifa litainuka juu ya taifa, na ufalme juu ya ufalme; na kutakuwa na njaa, na tauni, na matetemeko ya ardhi pahali na mahali.”{EVsw 703:3}

Wakati wa sasa ni wa kuvutia mno kwa wote walio hai. Watawala na wanasiasa, watu walioko kwenye nafasi za mamlaka na uaminifu, wanaume na wanawake wenye fikra makini wa kila tabaka, wameelekeza macho yao kwenye matukio yanayotukia. Wanafuatilia uhusiano baina ya mataifa, wanatazama msisimko unaotawala kila kipengele cha dunia, na wanatambua kuwa jambo kubwa na la mwisho liko karibu kutokea—kwamba dunia iko kwenye ukingo wa mgogoro mkuu. **—Prophets and Kings, 536, 537 (1916).**{EVsw 703:4}

Wajibu Wetu Katika Kipindi Hiki cha Pumziko

Malaika sasa wanazuia pepo za migogoro-vita, hadi dunia iwe imeonywa juu ya hukumu yake ijayo; lakini dhoruba inakusanyika, iko tayari kulipuka duniani, na **Mungu** atakapowaamuru malaika Wake waachilie pepo hizo, kutakuwa na hali ya mapambano ambayo hakuna kalamu inayoweza kuieleza.....{EVsw 704:1}

Mungu ametupatia kwa neema kipindi cha pumziko. Kila nguvu tuliyoazimwa kutoka mbinguni ni lazima itumike katika kufanya kazi aliyoitwika juu yetu kwa ajili ya waliopotea kwa kutojua.....{EVsw 704:2}

Watu wa **Mungu** wanapaswa kufanya maombezi makubwa Kwake kwa ajili ya msaada sasa. Na ni lazima watumie nguvu zao zote katika juhudi za kueneza ile Kweli wakati huu wa pumziko.....{EVsw 704:3}

Kila siku tumekuwa tukikutana na wanaume na wanawake walioko karibu na hukumu. Kila siku inaweza kuwa ndiyo siku ya mwisho kwa nafsi fulani. Kila siku mtu anaweza kuwa amefanya uamuzi utakaoamua hatima yake ya milele. **—The Review and Herald, Novemba 23, 1905.**{EVsw 704:5}

Umuhimu wa Mgogoro

Hatujafahamu ipasavyo mapambano makubwa yanayoendelea kati ya majeshi yasiyoonekana, vita kati ya malaika waaminifu na waasi. Kila mwanadamu anapiganiwa na malaika wa mema na waovu. Hii sio vita ya kuigiza. Huu sio michezo ya kuigiza kuhusu vita; bali ni mapambano ya kweli. Tunakabiliana na maadui wenye nguvu, na inatupasa sisi kuamua nani atashinda. Nguvu yetu lazima itokane pale mitume wa kwanza walipotafuta msaada. **—The Signs of the Times, Februari 17, 1914.** {EVsw 704:5}

Upagani Wafufuliwa; Mtu wa Dhambi Afichuliwa—Tunapokaribia mwisho wa wakati, kutakuwa na gwaride la nje litakalokuwa kubwa zaidi na zaidi, la nguvu za kipagani; miungu ya kipagani itaonyesha nguvu zao za ishara, na itajionyesha mbele ya miji ya ulimwengu; na hakika hali hii imeshaanza tayari kutimia. Bwana wetu Yesu alimwonyesha Yohana katika kitabu cha Ufunuo, kwa picha mbalimbali, tabia za uovu na nguvu ya ushawishi za kuwavuta wale ambao wamejulikana kwa kuwatesa watu wa Mungu. Wanadamu wote wanahitaji hekima kwa kuwa waangalifu ili kutafuta fumbo/siri ya uovu ambayo kwa kiasi kikubwa inajitokeza katika kuhitimisha historia ya dunia hii.....**{EVsw 705:1}**

Katika wakati huu tunaoishi, Bwana amewaita watu Wake na amewapa ujumbe wa kubeba. Yeye Amewaita kufichua uovu wa mtu wa dhambi ambaye ameifanya sheria ya kuabudu Jumapili kuwa nguvu ya kipekee, ambaye amefikiria kubadilisha nyakati, majira na sheria, na kuwakandamiza watu wa Mungu wanaosimama imara na kumheshimu Yeye kwa kuitunza ile Sabato ambayo ndiyo ya Kweli peke yake, uumbaji wa Sabato, takatifu kwa Bwana.—Shuhuda kwa Wachungaji na Watendakazi wa Injili, 117, 118.**{EVsw 705:2}**

Wajumbe wa Mungu Wasio na Hofu—Wakati huu, ambao ndio wakati wa mwisho wa mambo yote ya dunia unakaribia kwa kasi, Shetani anafanya juhudi kubwa na hata kutapatapa ili kuunasa ulimwengu. Adui anabuni mipango mingi ya kutawala akili, na kugeuza umakini wa wanadamu kutoka kwenye zile Kweli muhimu za wokovu.....**{EVsw705:3}**

Uovu unafikia kilele ambacho hakijawahi kufikiwa hapo awali, na bado wachungaji na wahudumu wengi wa injili wanapaza sauti wakisema, “Amani na usalama.” Lakini wajumbe waaminifu wa Mungu wanapaswa kuendelea mbele na kazi yao. Wakiwa wamevaa silaha za vita za mbinguni, wanapaswa kusonga mbele kwa uthabiti, na bila woga na kwa ushindi, bila kuacha vita vyao hadi kila roho iliyo karibu nao itakapopokea ujumbe wa Kweli kwa wakati huu.—The Acts of the Apostles, 219, 220 (1911).**{EVsw 705:4}**

Kilele cha Haraka na Ushindi

Injili Iliitikisa Dunia Enzi za Mitume

Kwa kushirikiana na Roho Mtakatifu, mitume walifanya kazi iliyoitikisa dunia. Injili ilipelekwa kwa kila taifa ndani ya kizazi kimoja tu. {EVsw 706:1}

Matokeo ya huduma ya mitume wa Kristo walioteuliwa yalikuwa ya utukufu.... {EVsw 706:2}

Hawakufanikisha kwa nguvu zao wenyewe utume, bali kwa nguvu ya **Mungu** aliye hai. Kazi yao haikuwa rahisi. Mwanzo wa kazi ya kanisa la Kikristo ulizingirwa na mateso na huzuni kali. Kazi yao ilikuwa ya kukabiliana na shida, kashfa, na mateso; lakini hawakuhesabu maisha yao kuwa na thamani kwao wenyewe, bali walifurahia kuitwa kuteseka kwa ajili ya Kristo. Kutokuwa na maamuzi thabiti, kutokuwa na dhamira, na udhaifu wa kusudi, havikuwa na nafasi katika kazi yao. Walikuwa tayari kutoa na kujitoa na kitu kilitolewa na hata maisha yao. Dhamira ya wajibu uliowakabili iliwatakatisha na kuimarisha uzoefu wao; na neema ya mbinguni ilionekana wazi katika ushindi walioupata kwa ajili ya Kristo. Kwa nguvu ya Uweza, **Mungu** alifanya kazi kupitia kwao kuifanya injili kushinda. **—The Acts of the Apostles, 593-595 (1911).** **{EVsw 706:3}**

Anga la Wateule wa Mungu — Miongoni mwa wakaaji wa dunia, waliotawanyika katika kila nchi, wapo wale ambao hawajaipigia magoti sanamu ya Baali. Kama vile nyota za mbinguni zinazojitokeza tu wakati wa usiku, waaminifu hawa wataangaza watakapojitokeza wakati giza likiwa limeifunika dunia, na giza kuu limewafunika watu. Katika Afrika ya kipagani, katika nchi za Kikatoliki za Ulaya na Amerika ya Kusini, huko China, India, visiwani, na katika kila pembe yenye giza duniani, **Mungu** ana akiba ya kundi la nyota—wateule Wake—watakaong'aa katikati ya giza, wakidhihirisha kwa uwazi mbele ya dunia iliyoasi nguvu ya ibadilishayo maisha kupitia utii kwa sheria Yake. Hata sasa, wanaendelea kujitokeza katika kila taifa, kwa kila lugha na kwa kila jamaa; na wakati wa uasi mkuu kabisa, ambapo Shetani atakuwa amefanya juhudi yake ya mwisho kuwalazimisha "wote, wadogo kwa wakubwa, matajiri kwa maskini, walio huru kwa watumwa," wapokee, kwa tishio la kifo, alama ya utii kwa siku ya mapumziko ya uongo—waaminifu hawa, "wasiokuwa na doa, wasiokuwa na hatia, wana wa **Mungu**, wasioweza kushitakiwa," watang'aa kama "mianga katika ulimwengu." Kadiri usiku unavyokuwa na giza totoro, ndivyo watakavyoangaza kwa mwangaza mkuu zaidi. **—Prophets and Kings, 188, 189 (1916).** {EVsw 706:4}

Kanisa la Ushindi

Kazi itafungwa hivi karibuni. Wale washiriki washindi, waliokuwa waaminifu ndani ya kanisa la mapambano, watakuwa kanisa la ushindi. **—Letter 32, 1892.{EVsw 707:1}**

Na bado Jenerali wetu, ambaye hajawahi kukosea, anatuita: "Songeni mbele; ingieni maeneo mapya; peperusheni bendera katika kila nchi. '**Isaya 60:1** *Ondoka, uangaze; kwa kuwa nuru yako imekuja, Na utukufu wa BWANA umekuzukia*....." (Aluta Continua) **{EVsw 707:2}**

Neno letu la kaulimbiu ni, Mbele, mbele milele! Malaika wa mbinguni watatangulia mbele yetu ili kuandaa njia. Mzigo wetu kwa maeneo ya ng'ambo hauwezi kuwekwa chini, hadi dunia nzima iangazwe na utukufu wa Bwana. —Gospel Workers, 470 (1915).

Wakati umefika ambapo kupitia kwa wajumbe wa **Mungu**, gombo linafunuliwa kwa ulimwengu. Ukweli wa ujumbe wa malaika wa kwanza, wa pili, na wa tatu ni lazima uwafikie kila taifa, jamaa, lugha, na watu; ni lazima uangaze giza la kila bara, na kufikia visiwa vya bahari. Hapapaswi kuwa na uchelewesho katika kazi hii. {EVsw 707:3}

Kauli yetu iwe: "Mbele, daima mbele! (Aluta Continua)" Malaika wa mbinguni watatutangulia kututayarishia njia. Jukumu letu kwa ajili ya maeneo ya mbali hauwezi kuwekwa chini hadi dunia yote iangazwe kwa utukufu wa Bwana. **—Gospel Workers, 470 (1915).** {EVsw 707:4}

ALUTA CONTINUA MSOMAJI-tuombeane katika mapambano haya!

Wakati wa Fursa ya Sasa

Kazi ya Leo — Ujumbe wa malaika wa tatu unazidi kupanuka na kufika katika kilele cha mwito wa sauti kuu, na hupaswi kujihisi kuwa na uhuru wa kuacha wajibu wa sasa kwa matumaini kwamba wakati fulani ujao utapokea baraka kuu, kana kwamba bila jitihada yoyote kwa upande wako, uamsho wa ajabu utatokea....

Leo ni wakati wako wa kutakaswa, ili uwe tayari kupokea umande wa mbinguni, tayari kwa mvua ya masika; kwa kuwa mvua ya masika itakuja, na baraka ya **Mungu** itajaza kila nafsi iliyotakaswa na kila najisi. Ni kazi yetu leo kuikabidhi mioyo yetu kwa **Kristo**, ili tuweze kuandaliwa kwa ajili ya wakati wa kuburudishwa kutoka katika uwepo wa Bwana—kuwekwa tayari kwa ajili ya ubatizo wa Roho Mtakatifu....

Badala ya kuishi kwa matarajio ya msimu maalumu wa msisimko wa kiroho, ni busara kwetu kutumia fursa zilizopo sasa kwa hekima, tukifanya kile kinachopaswa kufanywa ili roho zipate kuokolewa. Badala ya kuchosha akili zetu kwa kubashiri nyakati na majira ambayo Bwana ameweka katika mamlaka Yake mwenyewe na kuzuia kuyafichua kwa wanadamu, tunapaswa kujiweka chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu, tukitimiza wajibu wa sasa, na kuwapa watu waliopotea chakula cha uzima—kisicho na mchanganyiko wa maoni ya kibinadamu—kwani wanazimia kwa kukosa **Ukweli**. **—The Review and Herald, March 22, 1892.**

Fursa za Kipekee Zisizokuwa na Kawaida

Katika siku hizi za usafiri wa haraka, fursa za kukutana na wanaume na wanawake wa tabaka mbalimbali na wa mataifa mengi ni kubwa zaidi kuliko ilivyokuwa katika siku za Israeli. Njia kuu za usafiri zimeongezeka mara elfu moja. **Mungu** ameutayarisha njia kwa namna ya ajabu. Chombo cha uchapishaji, kikiwa na nyenzo zake nyingi, kiko mikononi mwetu. Biblia na machapisho kwa lugha nyingi, yanayoeleza **Ukweli** wa wakati huu, yapo karibu nasi, na yanaweza kusambazwa kwa haraka kila kona ya dunia.

Sisi tumekabidhiwa kazi ya kutoa onyo la mwisho la **Mungu** kwa wanadamu—na ni kwa kiwango gani tunapaswa kuwa na bidii katika kujifunza Biblia, na ari katika kueneza nuru hii! —**The Review and Herald, January 25, 1906.**

Mungu Hutoa Fursa Hizi — Kuna shida kubwa inayokaribia sana mbele yetu. Sasa ni wakati wa kutangaza kwa nguvu ya Roho Mtakatifu **Ukweli** mkuu wa siku hizi za mwisho. Haitachukua muda mrefu kabla kila mtu kusikia onyo hilo na kufanya uamuzi wake. Kisha mwisho utakuja… **Mungu** ndiye Mtendaji Mkuu wa kazi yote, na kwa mipango Yake ya Kiungu Huandaa njia ya kutimiza kazi Yake. Yeye hutoa fursa, Hufungua njia za ushawishi, na mikondo ya utendaji. Ikiwa watu Wake watakuwa waangalifu kutambua ishara za uongozi Wake na kusimama tayari kushirikiana Naye, wataona kazi kubwa ikifanyika. — **Testimonies For The Church 6:24 (1900).**

Mgogoro wa Kitaifa Wazaa Mwamko wa Kidini —

Leo hii, wanadamu pamoja na mataifa wanapimwa kwa kipimo kisicho na makosa, kilichomo mikononi mwa Yeye asiyeweza kukosea...

Leo dalili za nyakati zinatufahamisha kuwa tumesimama katika kizingiti cha matukio makubwa na ya kutisha. Kila jambo duniani limeingiwa na msukosuko. Mbele ya macho yetu unabii wa Mwokozi unatimilika kuhusu matukio yatakayoutokea kabla ya kuja Kwake: "***Mathayo 24:6-7*** *Nanyi mtasikia habari za vita na matetesi ya vita; angalieni, msitishwe; maana hayo hayana budi kutukia; lakini ule mwisho bado. Kwa maana taifa litaondoka kupigana na taifa, na ufalme kupigana na ufalme; kutakuwa na njaa, na matetemeko ya nchi mahali mahali."*

Wakati uliopo ni wa shauku kuu kwa kila aliye hai. Watawala na viongozi wa serikali, watu waliowekwa katika nafasi za uaminifu na mamlaka, pamoja na wanaume na wanawake wenye kufikiri kutoka kila tabaka, wanaelekeza macho yao kwa matukio yanayoendelea kutokea mbele yetu. Wanachunguza kwa makini mahusiano yaliyopo kati ya mataifa. Wanaona jinsi hali ya taharuki inavyotawala kila jambo la kidunia, nao wanatambua kuwa jambo kuu na la kuamua linakaribia kutokea—kwamba dunia iko ukingoni mwa pambano kubwa.

Biblia na Biblia peke yake, ndicho kitabu kinachotoa nuru sahihi kuhusu haya. Ndani yake yamefunuliwa matukio makuu ya mwisho katika historia ya dunia yetu-matukio ambayo tayari vivuli vyake vinaonekana mbele yetu, na sauti ya kuja Kwake inatikisa dunia, na mioyo ya wanadamu inazimia kwa hofu. **—Prophets and Kings, 536, 537 (1916).**

Wajibu Wetu Katika Kipindi cha Mapumziko— Malaika sasa wanazuia pepo za mashindano na mafarakano, hadi dunia iwe imeonywa kuhusu hukumu inayokuja; lakini dhoruba kubwa inajikusanya, iko tayari kulipuka juu ya dunia, na wakati **Mungu** atakapowaamuru malaika ake waachilie pepo hizo, patakuwa na hali ya mashaka na ugomvi isiyoweza kufafanuliwa kwa kalamu ya mwanadamu....

Mungu kwa rehema Zake ametupatia kipindi kifupi cha mapumziko. Kila uwezo tulioazimwa kutoka mbinguni unapaswa kutumika kutekeleza kazi ambayo Bwana ametukabidhi kwa ajili ya wale wanaoangamia katika ujinga....

Watu wa **Mungu** wanapaswa kumwomba kwa bidii kuu msaada Wake sasa. Na wanapaswa kuweka nguvu zao zote katika juhudi za kuitangaza **Kweli** wakati huu wa rehema uliopewa....

Kila siku tumekuwa tukiishi na watu ambao wako njiani kuelekea hukumu. Kila siku inaweza kuwa ndiyo siku ya maamuzi ya mwisho kwa nafsi fulani. Kila siku kuna mtu anayefanya uamuzi utakaotawala hatima yake ya milele. —**The Review and Herald, November 23, 1905**

Umuhimu wa Mapambano— Hatufahamu ipasavyo lile pambano kubwa linaloendelea kati ya majeshi yasiyoonekana, yaani, vita kati ya malaika waaminifu na wale waasi. Juu ya kila mtu, malaika wema na waovu hupigana vita. Hili si pambano la kubuni wala si mchezo wa kivita tunaoshiriki. Tunakabiliana na maadui wenye nguvu kuu, na ni juu yetu kuamua ni upande upi utakaoshinda. Tunapaswa kutafuta nguvu zetu pale ambapo wanafunzi wa kwanza walizipata. **—The Signs of the Times, February 17, 1914.**

Upagani Kufufuka; Mtu wa Dhambi Kufunuliwa

Tunapokaribia mwisho wa wakati, kutakuwa na maonyesho ya wazi ya nguvu ya upagani; miungu ya kipagani itajionyesha kwa ishara zake, na itajitokeza wazi mbele ya miji ya dunia; na maelezo haya tayari yameanza kutimia. Kwa picha mbalimbali, Bwana Yesu alimfunulia Yohana tabia ya uovu na mvuto wa udanganyifu wa wale waliotambulika kwa mateso waliyowaletea watu wa **Mungu**. Kila mtu anahitaji hekima kuchunguza kwa makini fumbo la uovu linalojitokeza sana katika hitimisho la historia ya dunia....

Katika wakati huu ambao tunaishi, Bwana amewaita watu Wake na kuwapa ujumbe wa kupeleka. Amewaita kufunua uovu wa mtu wa dhambi, ambaye ameifanya sheria ya Jumapili kuwa alama yake kuu, ambaye amedhani kubadili majira na sheria, na kuwatesa watu wa **Mungu** wanaosimama imara kumheshimu kwa kuitunza Sabato ya kweli—Sabato ya uumbaji—kama takatifu kwa Bwana**. —Testimonies to Ministers and Gospel Workers, 117, 118.**

Wajumbe Jasiri wa Mungu

Wakati huu wa sasa, ambapo mwisho wa mambo yote ya duniani unakaribia kwa haraka, Shetani anajitahidi sana kuunasa ulimwengu. Anapanga mikakati mingi ya kuwashughulisha watu na kuwapotosha kutoka kwenye kweli za wokovu....

Uovu umefikia kiwango ambacho hakijawahi kushuhudiwa kabla, na bado wahubiri wengi wa injili wanalalamika, “Amani na usalama.” Lakini wajumbe wa kweli wa **Mungu** wanapaswa kuendelea mbele bila kuyumbishwa katika kazi yao. Wakiwa wamevalia silaha kamili za mbinguni, ni lazima waendelee mbele kwa ujasiri na ushindi, bila kuacha mapambano yao hadi kila roho waliyo nayo karibu ipokee ujumbe wa kweli wa wakati huu**. —The Acts of the Apostles, 219, 220 (1911).**

Kilele cha Ushindi wa Kasi

Injili Iliyowahi Kuitikisa Ulimwengu—Kwa ushirikiano wa Roho Mtakatifu, mitume walifanya kazi iliyoitikisa ulimwengu. Kwa kila taifa injili ilipelekwa katika kizazi kimoja.

Matokeo yaliyoambatana na huduma ya mitume wateule wa Kristo yalikuwa matukufu....

Mitume hawakutimiza utume wao kwa nguvu zao wenyewe, bali kwa nguvu ya Mungu aliye hai. Kazi yao haikuwa rahisi. Kazi za ufunguzi za kanisa la Kikristo ziliambatana na ugumu na huzuni kali. Katika kazi yao wanafunzi walikumbana na umaskini, kejeli, na mateso kila mara; lakini hawakujihesabia maisha yao kuwa ya thamani kwao wenyewe na walifurahi kwamba waliitwa kuteseka kwa ajili ya Kristo. Kutokuwa na azimio, kutokuwa na uamuzi, udhaifu wa kusudi, haukupata nafasi katika juhudi zao. Walikuwa tayari kutumia na kutumiwa. Ufahamu wa jukumu lililokuwa juu yao ulitakasa na kutajirisha uzoefu wao; na neema ya mbinguni ilifunuliwa katika ushindi walioupata kwa ajili ya Kristo. Kwa uweza wa uweza wote Mungu alifanya kazi kupitia wao ili kuifanya injili ishinde.—Matendo ya Mitume, 593-595 (1911).

Anga la Wateule—Miongoni mwa wakazi wa dunia, waliotawanyika katika kila nchi, kuna wale ambao hawajapiga magoti kwa Baali. Kama nyota za mbinguni, zinazoonekana usiku tu, waaminifu hawa

watang'aa giza litakapofunika dunia na giza kuu litakapowafunika watu. Katika Afrika ya kipagani, katika nchi za Kikatoliki za Ulaya na Amerika Kusini, nchini China, India, katika visiwa vya bahari, na katika pembe zote za giza za dunia, Mungu ana anga la wateule ambalo bado litang'aa katikati ya giza, likifichua waziwazi kwa ulimwengu ulioasi nguvu inayobadilisha ya utii kwa sheria Yake. Hata sasa wanaonekana katika kila taifa, kati ya kila lugha na watu; na katika saa ya uasi mkubwa zaidi, wakati juhudi kuu ya Shetani inafanywa kusababisha "wote, wadogo kwa wakubwa, matajiri kwa maskini, walio huru na watumwa," kupokea, chini ya adhabu ya kifo, ishara ya utii kwa siku ya mapumziko ya uongo, waaminifu hawa, "wasio na lawama na wasio na madhara, wana wa Mungu, bila kukemewa," "watang'aa kama mianga duniani." Kadiri usiku unavyozidi kuwa mweusi, ndivyo watakavyong'aa kwa uzuri zaidi. — Manabii na Wafalme, 188, 189 (1916).

Kanisa Lenye ushindi—Kazi itafungwa hivi karibuni. Washiriki wa kanisa la mpiganaji ambao wamethibitisha kuwa waaminifu watakuwa kanisa la ushindi.—Barua ya 32, 1892.

Na bado Jenerali wetu, ambaye hafanyi makosa, anatuambia, "Songa mbele; ingia katika eneo jipya; inua bendera katika kila nchi. 'Ondoka, uangaze; kwa kuwa nuru yako imekuja, na utukufu wa Bwana umekuzukia.'"

Wakati umefika ambapo kupitia wajumbe wa Mungu Gombo linakunjuliwa kwa ulimwengu. Ukweli uliomo katika jumbe za malaika wa kwanza, wa pili, na wa tatu lazima uende kwa kila taifa, jamaa, lugha, na watu; lazima uangaze giza la kila bara, na kuenea hadi visiwa vya bahari. Haipaswi kuwa na ucheleweshe katika kazi hii.

Neno letu la kaulimbiu ni, Mbele, mbele milele! Malaika wa mbinguni watatangulia mbele yetu ili kuandaa njia. Mzigo wetu kwa maeneo ya ng'ambo hauwezi kuwekwa chini, hadi dunia nzima iangazwe na utukufu wa Bwana.—Wafanyakazi wa Injili, 470 (1915).